

Roho ya Paka

1

ILIKUWA ghafla, kama pigo la kisu ambalo lilipenya mwilini na kuujeruhi moyo wa Inspekta Kombora. Kati ya yote aliyoyatarajia jioni ya leo, simu kama hiyo, ya maafa, haikuwamo kabisa akilini mwake. Kwa jumla, ilikuwa kama iliyopigwa muda huu kwa ajili ya kumsimanga au kumdhihaki.

Muda mfupi uliopita alikuwa akiitazama kwa furaha kubwa chati yake ya taarifa za wizi, ujambazi na mauaji nchini. Ingawa tabasamu ni kitu ambacho huutembelea uso wa Kombora kwa nadra sana, lakini leo liliutawala uso huo kwa muda mrefu wakati akiitazama chati hiyo. Furaha iliyotokana na jinsi idadi ya vitendo hivyo ilivyokuwa ikishuka kwa kasi. Ukiacha udokozi mdogomdogo, wizi wa kuaminiana na ule wa kalamu vinginevyo rekodi hiyo ilikuwa ikielekea kwenye sifuri. Wakati wowote Tanzania ingeweza kujitangaza duniani kama taifa pekee ambalo limeushinda kabisa ujambazi.

Kombora alikuwa mtu wa kwanza aliyestahili kuifurahia hali hiyo kwani alikuwa mstari wa mbele kati ya wale wachache ambao huumiza vichwa vyao na kukesha usiku na mchana pindi linapotokea tukio lolote ambalo hutishia usalama wa taifa hili. Hivyo, alichekelea huku akimpongeza kimoyomoyo Waziri wa Mambo ya Ndani, Augustine Mrema, ambaye alisimamia kwa dhati ulinzi wa sungusungu ambao uliwajumuisha raia wenyewe kujilinda usiku. Kombora aliamini kabisa kuwa hilo lilichangia sana kupunguza wizi, uvunjaji wa majumba na mauaji ambayo yalifikia kiwango cha kukatisha tamaa.

Hata hivyo, tabasamu la Kombora lilitoweka. Lile wazo lililokuwa likimpekecha ubongo mara kwa mara lilipomjia tena, wazo la kwamba, kama imefikia hatua ya raia wenyewe kukesha nje wakijilinda, vyombo ambavyo vina jukumu hilo vinafanya nini? Havitoshi? Haviwezi? Havifai? Haviaminiki? Na kama jibu limo katika moja ya maswali hayo kuna umuhimu gani wa kuwa na vyombo hivyo na kuvitengea mamilioni ya pesa kila mwaka?

Akiwa askari mwaminifu, anayeipenda na kuiamini kazi yake Kombora alijisikia haya. Angefurahi zaidi kama idadi hiyo ya matukio ya kijambazi ingekuwa inashuka kutokana na uwezo wa polisi au usalama. Angefurahi zaidi kama raia wote wangelala usingizi wao kwa amani kama ilivyokuwa miaka michache iliyopita. Pamoja na hayo, aliendelea kuifurahia hali ya usalama. Alijiona kama kwamba wanausalama wako mapumzikoni au chuoni wakiandaa mkakati ambao utawafanya warudipo kazini watimize jukumu lao kwa uhakika zaidi.

Ni wakati alipotoka mbele ya jedwali hilo na kuketi juu ya kiti chake pindi ilipolia simu hii na kuupasua moyo wake kwa habari za mauaji. “Unasema unaitwa nani vile?” Kombora aliuliza kwa ukali kidogo.

“Sajini Brashi, mzee. Wa kituo Kikuu… Ni kweli hunifahamu. Lakini mimi nakufahamu…”

Kombora alimkatiza tena, safari hii kwa ukali zaidi, “Kwa nini unipigie mimi? Huna mkuu wako wa kazi? Sikiliza, Sajini. Kama hadi leo hujafahamu taratibu za kazi yako nadhani njoo zako hapa tukupe barua ili urudi tena chuoni.”

“Sivyo, mzee,” upande wa pili ulijibu, kiasi sauti yake ikiwa na hofu. “Naufahamu wajibu wangu. Lakini kuna jambo katika mauaji haya, ambalo nadhani ungependa kuliona kabla ya mtu mwingine yeyote.”

“Jambo lipi hilo?”

“Labda nikuombe uje mara moja. Ni mwendo wa dakika tano tu, mzee…”

***

PONGWE Hotel ni moja kati ya yale mamia ya hoteli za kitalii ambazo ziliibuka kama uyoga huku na huko nchini, mara baada ya kutangaza ule uhuru wa kiuchumi. Hii ipo katika Mtaa wa Livingstone, Kariakoo. Ina ghorofa sita, vyumba mia na ishirini vya kulala, vyote vikiwa vinajitegemea kwa bafu, choo na mashine ya kurekebisha hewa.

Kwa nje hoteli hii inaonekana kama hoteli nyingine nyingi za mji huu, kana kwamba wajenzi wake walikusudia kumfanya mpitanjia asivutiwe kabisa na majengo, rangi wala mandhari yake. Lakini ndani, hali ilikuwa tofauti kabisa. Utaalamu na utajiri vilijumuishwa kiasi cha kumfanya Kombora, ambaye hapati nafasi ya kutembelea hoteli mara kwa mara, atikise kichwa chake.

Zilimchukua dakika tisa, badala ya tano, kutoka ofisini kwake hadi hapa, hali ambayo ilisababishwa na msongamano wa magari na ubovu wa barabara. Alimkuta Brashi, kijana mwembamba, mrefu, mwenye nywele nyingi aliyevalia kiraia, akimsubiri mlangoni.

“Hadi sasa, zaidi ya mhudumu wa chumba hicho na meneja wa hoteli, hamna mtu mwingine anayejua kilichotokea,” Brashi alimweleza Inspekta akimwongoza ndani. “Ni katika ghorofa ya tano, chumba namba 108.”

Walipita mapokezi ambapo mhudumu wa kike alikuwa akiwakaribisha wageni wanne kwa maneno na tabasamu lililotosha kabisa kuwashawishi wakae hotelini hapo kwa miaka. Kutoka hapo waliingia chumba cha vinywaji. Huko nusu ya viti vyote tayari ilimezwa na wateja walioonekana wachangamfu zaidi kutokana na bia nyingi zilizokuwa wazi mbele yao. Wawili kati ya wateja hao waligeuza nyuso zao kuwatazama Brashi na

Inspekta Kombora, waliokuwa katika mavazi yao ya kawaida. Watumiaji hao waliwapuuza mara moja kwa kuwachukulia kama wanywaji wenzao. Brashi alimwongoza Kombora kuifuata ngazi ya kupandia juu.

Mbele ya chumba walichokihitaji walimkuta meneja akinong'ona na mzee mmoja mwenye tumbo nene na uso wa mtoto mdogo ambaye, kwa kumtazama tu, Kombora alifahamu kuwa ni Mchaga. Nyuso zao zilijawa na wasiwasi.

"Karibu mzee," Meneja aliwakaribisha. "Huyu hapa ni bwana Mmari, ndiye tajiri wa hoteli hii. Nilikuwa nikimfahamisha mkasa uliotukuta."

Walishikana mikono. Kisha, wote wakaingia katika chumba hicho ambacho kwa mtazamo wa kawaida kilikuwa kama kawaida. Shuka zilitandikwa vizuri kitandani. Juu ya kitanda hicho alilala kifudifudi msichana mwembamba, mweupe, ambaye huhitaji kumtazama usoni ili ujue kuwa ni mzuri. Alivaa nguo zake zote; gauni jepesi, refu japo lilifunua paja moja na kuonekana kutokana na kulala vibaya. Mikono yake laini ilijaa bangili na pete ya dhahabu. Shingoni pia alikuwa na mkufu wa dhahabu ambao ulioana na nywele zake ambazo pia zilibeba rangi ya dhahabu. Kwa kila hali alikuwa msichana mzuri wa kileo.

Angeweza kuwa amelala… angeweza kuwa amejipumzisha. Kombora alimtazama Brashi kama anayetaka ufafanuzi wa hayo.

"Amekufa mzee," Brashi alijibu swali hilo ambalo alilisoma katika macho ya kombora. "Amekufa kifo cha kikatili kupita kiasi."

Kombora hakuelewa. Alimwonyesha hivyo Brashi katika macho yake.

"Labda nikuonyeshe, mzee," alisema akimsogelea marehemu. "Nikuonyeshe jeraha mzee?" Kombora alipotikisa kichwa kukubali, Brashi alichukua kitambaa cha meza ndogo kando ya kitanda hicho na kukifunga katika mkono wake wa kushoto. Kisha, akautia mkono wake tumboni mwa marehemu na kumgeuza taratibu huku akiyafumba macho yake na kusema taratibu, "Jiandae kwa mshituko."

Kwanza Kombora hakuelewa. Ilikuwa kama anaota ndoto ya ajabuajabu inayotisha kuliko vitisho vyote. Kisha, akadhani kuwa haoti, bali anatazama sinema ya kuogofya kupita kiasi. Alipotanabahi kuwa hayuko pichani wala ndotoni alihisi alishikwa na kichefuchefu. Hakuhitaji kutapika kwani bwana Mmari alikuwa akitapika badala yake huku akitokwa na sauti ya kilio cha ghafla.

Ilikuwa picha ya kutisha, picha isiyoelezeka wala kutazamika. Yeyote aliyefanya kitendo hiki hakuwa binadamu wa kawaida isipokuwa mnyama. Vinginevyo, hangewezaje kuthubutu? Angewezaje kufikiria hilo?

Bila kujua atendalo, Kombora alijikuta akimshika Sajini Brashi mkono kwa vidole vyake vikubwa na kumbana huku akimuuliza kwa sauti ndogo, "Mimi nahusika vipi na maiti hiyo Sajin? Kitu gani hapo ambacho uliona kitapendeza sana niskikiona?"

Brashi alijaribu kujitoa katika mkono wa kombora. Ilikuwa kama kujaribu kujikwatua toka katika pingu. Badala yake ndiyo kwanza vidole hivyo vilizidi kudidimia katika ngozi yake. Japo maumivu yalikuwa makali, lakini hayakumzuia kushangazwa na nguvu za mzee huyu. "Anakula nini?" alijiuliza akimtazama usoni.

"Kitu gani ulichodhani kitanipendeza hapa?" Kombora aliuliza tena.

"Unaniumiza Inspekta."

Ndiyo kwanza Kombora akafahamu kuwa alikuwa amemshika Brashi mkono. Akamwachia na kuiona damu ambayo ilianza kutoka katika michubuko iliyosababishwa na vidole vyake. Angeweza kumwomba radhi, lakini hakufanya hivyo. Rohoni mwake, aliona adhabu hiyo ndogo inatosha kabisa kumfunza adabu sajini huyu kwa kosa lake la kuivuruga amani na starehe aliyokuwa nayo moyoni kwa siku chache zilizopita bila misukosuko ya kutisha.

Kumwita hili atazame maiti hii iliyokuwa katika taswira ya kutisha kupita kiasi, maiti ambayo haitamtoka akilini wala katika ndoto zake, kwa muda mrefu bila sababu ya maana, aliona ni ufedhuli wa hali ya juu. Alimkazia Brashi macho akifikiria adhabu ipi ya pili ambayo ingemfaa zaidi.

Brashi hawezi kuwa mbumbumbu kiasi hicho. Hawezi kuwa mtu pekee nchini na duniani ambaye hafahamu kuwa Kombora alikuwa akiongoza idara maalumu na pekee ambayo hushughulikia yale masuala mazito na yanayotishia usalama wa serikali na taifa, si masuala madogomadogo, ya kawaida ambayo yangeweza kushughulikiwa na polisi wa kawaida.

Kana kwamba anayasoma mawazo yake, Sajini Brashi alisema, “Samahani sana Inspekta, nilidhani wewe na Joram Kiango mna aina fulani ya uhusiano. Sijui namna yoyote ya kumpata Joram, ndipo nikaona nikuarifu wewe kabla ya kulipeleka suala hili kwa wakuu wangu ambako linaweza likatangazwa ovyo au kupuuzwa. Kama nimekosea, Inspekta, naomba radhi…”

“Sijakuelewa Joram anahusika vipi na huyu marehemu?” Kombora aliuliza, moyoni akitetemeka kidogo kwa jibu atakalopata.

“ Yawezekana huyu marehemu ni Nuru, yule mwenzi na mpenzi wake Joram Kiango. Kama ndiye…”

“Hukuona mzee?” Brashi alikatiza mawazo yake. “Hukuona? Basi nitalazimika kumfunua tena marehemu.”

“Kuona nini?”

Kombora alijaribu kumzuia, lakini alichelewa. Tayari alikwishamgeuza maiti chali. Kombora alilazimika kulitazama tena jeraha hilo.

Bado lilikuwa halitazamiki. Utalitazamaje jeraha ambalo lilikuwa zaidi ya jeraha? Pale ambapo palitakiwa kuwa na uso wa msichana huyo, toka sikio hadi sikio, na paji la uso hadi kidevu, badala yake palikuwa na shimo la kutisha lililokuwa limekula nyama zote na kuacha mifupa mitupu. Pale yalipostahili kuwepo macho, pua, midomo na ulimi sasa yalikuwa mashimo ambayo yaliacha wekundu wa nyama na damu uonekane kiasi cha kutisha zaidi ya fuvu lolote la binadamu.

Safari hii, akitazama kwa makini zaidi, Kombora aliweza kubuni kilichokula nyama hiyo. Kama si biological weapon ya kisasa zaidi ambayo inatoa wadudu wadogo na wengi sana ambao wanashambulia nyama ya binadamu kwa dakika kadhaa kabla ya kufa, basi ni aina kali sana ya asidi ambayo ilimchoma binti huyo uso mzima na kuacha mifupa mitupu.

“Unaona mzee?” Brashi alimzindua.

“Nini?”

“Tazama hapa,” alielekeza mkono wake pale ambapo palistahili kuwa kinywa, ambapo sasa palikuwa na meno yaliyotokeza kana kwamba yanalia au yanacheka. Kombora aliinama na kuchungulia. Ndipo alipoweza kukiona kipande cha karatasi kilichokuwa kimelazwa humo kinywani. Kilikuwa na maandishi. Kombora aliinama na kuyasoma.

“TUNAMTAKA JORAM KIANGO”

Kombora aliyasoma kwa mara ya pili kabla hajaupata ujumbe huo. Alipoupata aliingiza mkono wake mfukoni na kutoa kitambaa. Akakizungushia katika vidole vyake na kuvididimiza humo kinywani hadi alipofikia hicho kipande cha karatasi. Alikichukua na kukizungushia katika kitambaa hicho na kisha kukitia mfukoni mwake.

Baada ya hapo alimgeukia Brashi na kumwambia, “Sikia sajini, umefanya kazi nzuri. Wanamtaka Joram Kiango. Tutampa ujumbe wao.” Alimkazia macho kabla hajaendelea, “Sasa unaweza ukaendelea na taratibu zako zote, kama kawaida. Tafadhali nitaomba unipe taarifa kamili ya upelelezi wenu juu ya mauaji haya mara mtakapokuwa tayari. Sawa?”

Brashi alitikisa kichwa.

“Na unajua sajini? Sikio la mtu yeyote nje ya chumba hiki lisisikie kuwa mauaji haya ni salamu tu kwa Joram Kiango. Nataka iwe siri, tafadhali.”

“Bila shaka Inspekta.”

“Ngoja nikuonyeshe,” alisema akiinama tena kitandani na kumshika maiti.

***

HADITHI ilikuwa fupi na nyepesi. Kwa jina aliitwa Sofia Ali, mzaliwa wa huko Dodoma, wilayani Mpwapwa. Alikuja Dar es Salaam kama ilivyowatokea wasichana wenzake wengi wa hirimu yake. Amemaliza shule darasa la saba hana kazi wala mchumba. Jirani, mke wa bwana fulani huko Dodoma mjini anatokea na kumshahuri wafuatane naye mjini kumtunzia nyumba. Mshahara? Mia tano kwa mwezi. Chakula bure, malazi bure, nguo alizochoka nazo mama mwajiri bure, Akatae? Kama wengi wengine Sofia alijikuta yuko mjini.

Maji ya bomba ya mara kwa mara, chai ya maziwa kila asubuhi, chakula chenye viungo vyote; pamoja na ile dokoadokoa ya vipodozi vya mama ilifichua kiumbe mrembo aliyejificha katika umbo lile lililochakaa la Sofia Ali.

Badala yake, miaka miwili baadaye, aliyesimama mbele ya mama mwajiri alikuwa Sofia mwingine kabisa, Sofia aliyewiva, Sofia aliyejaza, Sofia ambaye alimfadhaisha baba mwenyenyumba na kumtisha mama. Matokeo yake Jumapili moja alipewa tiketi ya kurudi Mpwapwa. Kufanya nini? Kazi basi.

Hakurudi Mpwapwa. Akafuate nini? Jembe na mpini wake? Amwachie nani starehe za sinema na muziki ambazo ndio kwanza alikuwa ameanza kuzionjaonja? Rafiki yake aliyekuwa akiishi Tambuka Reli, ambaye alikuwa ameanza kujitegemea baada ya kupitia mkondo huohuo, alimpokea.

Chumba chao chenye upana wa futi tano kilibeba kitanda chao cha futi tatu na majukumu yote ya jiko, ghala; na mengineyo. Ungewatembelea mchana wakati wa joto, huku moshi ukiwaadhibu, usingekosa kuwahurumia. Lakini waone jioni, wakati tayari wameoga, wamevaa na kujitengeneza usingekosa kujiuliza kwa nini hawajatokea wachumba wakawaoa.

Mwaka mmoja baadaye, Sofia alikuwa Sofia hasa. Hata shoga zake walianza kumchukia kwa wivu. Hakujali, kwani alikuwa na marafiki wengi wa kiume kuliko wa kike. Na ni hao ambao aliwahitaji. Wakati huo hata jina alianza kulibadili. Badala ya Sofia sasa alijiita Soffy. Na alipenda sana baba yake aitwe Ally badala ya Ali. Hata lugha yake ilianza kubadilika. Katika kila sentensi alijikuta akiweka walau neno moja la Kiingereza. Hakujua kilipotokea hicho Kiingereza chake Lakini alikuwa na hakika nacho.

Sofia alifanya kosa. Mimba iliingia bila taarifa wala hiyari. Bwana hakumjua wala hakuhitaji mtoto. Alimeza vidonge mimba ikafa. Miezi miwili baadaye mimba ya pili ilimkamata. Hii haikusikia vidonge. Miezi mitatu, minne, mitano! Kila mtu alianza kumshuku. Elfu tatu zilimaliza kazi. Daktari mmoja asiye na huruma, alifanya kazi hiyo na kutupa mtoto anakokujua. Sofia aliponea chupuchupu. Baada ya miezi mitatu ya maumivu, afya yake ilimrudia. Mji wa Dodoma akauona nuksi. Huyoo, akaingia Dar es Salaam.

Dar ilimlaki juujuu. Rafiki yake mmoja wa Kinondoni, akijua kuwa umbo la Sofia lingemwongezea riziki, alimkaribisha kwake na kumwonyesha mji. Madisko ya Lang’ata na Ushirika yaliwakoma. Madansi ya DDC na Friend’s Corner yaliwatambua. Mabaa ya Sky Way na Kilimanjaro, yaliwaheshimu. Mabwana walikuwa tele, wa kila kabila na kila rangi. Sofia hakujua kumkataa mtu. Ni yeye aliyeanzisha msemo wa “… Ni pochi yako tu.”

Jioni ya leo alikuwa katika Hoteli ya Sky Way, ndipo alipomwona yule kijana mrefu, mnene, ambaye alikuwa akinunua vinywaji kwa fujo kuliko mtu mwingine yeyote hotelini hapo. Na mifuko yake bado ilionekana kuwa imetuna. Wasichana wengi waliokuwa wakimzengeazengea walipewa bia na kufukuzwa toka mezani pake. Sofia hakuwa mtu wa kuomba bia. Yeye huitwa au kufuatwa. Alimtupia jicho moja tu kijana huyo na kuona tayari ameimeza ndoano yake. Hakukosea kwani dakika mbili baadaye alianza kuletewa bia, oda ya kijana huyo. Na dakika kumi baadaye tayari waliketi pamoja, na kuanza kushikanashikana.

“Unasemaje?

“Pochi yako tu, darling.”

“Kiasi gani?”

“Hata wewe? Nilidhani umesoma, brother.”

Maongezi yao yaliishia katika kimojawapo cha vyumba vya hotelini. Baada ya nusu saa ya vilio na vicheko vya uongo na kweli Sofia alipokea “pochi” yake. Wakati akijiandaa kuondoka kijana huyo alimshika mkono na kumwambia, “Unajua Soffy, ni tamaa tu iliyonifanya niamue kuanguka nawe. Kwa kweli, nina rafiki yangu mpenzi, mwenye kitita cha pesa, kuliko hiki changu ambaye amenituma hapa Sky Way kumtafutia mwanamke mzuri. Kweli, hata hizi pesa nilizokuwa nikizinywa ni zake, kama hujachoka nikupeleke.”

“Kuchoka!” Sofia alicheka. “Nani aliwahi kuchoka kupokea pochi? Kama una wivu, I can understand, kama huna nipeleke.”

Kisha, Sofia alishituka na kusita kidogo wazo jipya lilipomjia. “Huyo, rafiki yako, What is his name?” aliuliza.

“Jina simfahamu.”

“Why! Ni binadamu kweli?”

“Sema, maana mambo ya siku hizi you can’t understand. Mimi sijachoka kiasi cha kumvulia underware yangu mnyama.”

Kijana huyo alicheka. “Unadhani mimi ni crazy kiasi hicho? Huyo ni mtu mwenye hadhi na heshima zake. Naamini hujapata kukutana na mtu mzito kama huyo.”

Bado Sofia alisitasita kidogo. “Jina humjui. Wewe mwenyewe unaitwa nani, honey?”

“Niite Ram Shog.”

“Na huyo friend wako yuko wapi?”

Alipomalizia kuvaa, Ram alimshika mkono Sofia na kumwambia, “Twende nikupeleke. Amepata chumba katika Hoteli ya Pongwe.”

***

Kiti cha Kombora kilikuwa kama chenye moto. Hakikukalika, mara aliinuka mara aliketi kana kwamba alikalia kaa ambalo lilikuwa likimchoma. Mkononi alikumbatia redio call yake kwa utulivu kama roho yake. Aliitazama na kuitingisha kama yai ambalo hakuwa na hakika kama ni zima au bovu.. Hata hivyo, alikuwa na kila hakika kuwa haikuwa mbovu. Ni ile ya upande wa pili ambayo alihitaji kuitilia shaka.

Muda mfupi tu uliopita alikuwa akiwasiliana na Koplo Shoka toka Lang’ata. Mara mawasiliano hayo yakakatika. Hakujua kama ilitokana na ubovu wa chombo hicho au Shoka alikata ghafla maongezi kuepuka mtu ambaye angeweza kuyasikia. Alichokuwa ameambulia ni “…Afande … tumempata…” na kisha “ amefika…” kisha chombo kikazimwa. Juhudi zote za Kombora kumpigia tena hazikuzaa matunda.

Wazo la kufanya uchunguzi kwa makini hapo Lang’ata lilimjia Kombora kutokana na uzoefu wake juu ya tabia za muuaji. Mara kwa mara katika kesi nyingi za mauaji hutokea muuaji akapenda kutembelea eneo na hata nyumba yalimotokea mauaji hayo.

Mara nyingine hutokea muuaji akadiriki hata kuhudhuria mazishi ya mtu aliyemuua. Kitu ambacho Kombora alikuwa haelewi ni sababu ipi ambayo hufanya wauaji hao wafanye hivyo. Hakujua kuwa walikuwa katika upelelezi wa kuelewa polisi wamefikia wapi katika uchunguzi wao, ama ni yaleyale waliyosema wahenga kuwa “damu nzito…” kwani mara kadhaa wauaji wengi wamepatikana kutokana na makosa hayo. Ni hilo tu ambalo lilimfanya amwamuru Shoka kuendelea na uchunguzi wake hapa Lang’ata ingawa siku mbili zilizopita hazikuwa na mafanikio.

Hivyo basi, redio yake ilipopata uhai na sauti ya Shoka ilipojitokeza na kusema “Tumempata” alijisikia kulia kwa furaha. Mara ukimya huu ukazuka. Dakika saba sasa zilikuwa zimepita. Aliendelea kuisubiri redio ya Shoka ipate uhai, aendelee kumwarifu alichogundua.

Dakika nane.

Dakika tisa.

Mara Kombora akaruka kama aliyeguswa na waya wa umeme. Akapiga ngumi kwa nguvu juu ya meza. Ameanza kuwa mzee? alijiuliza kwa hasira akiutia mkono katika fungati la meza yake na kuutoa ukiwa umeshikilia bastola yake kubwa ambayo aliitia mfukoni mwake.

Akatoka nje ya ofisi yake na kuchungulia ofisi ya msaidizi wake. Hakuwepo. Chumba cha pili alimpata askari mmoja ambaye alimtumia kuwakusanya askari wote waliokuwa ofisini wakati huo. Ukiwa usiku wa saa tano kasoro kituo kilikuwa na askari wanne tu. Wengine walikuwa katika shughuli nyinginezo au mapumzikoni. Kombora aliwachukua askari wawili na kumwamuru mmojawao aendeshe gari kasi iwezekanavyo kuelekea Lang’ata.

Gari lilikuwa likiruka, nusura lipae, lakini Kombora alizidi kumhimiza kijana huyo akanyage mafuta. Mara mbili askari mmoja alijaribu kumdadisi Kombora Lang’ata kulikoni lakini hakupata jibu lolote. Si kwamba Inspekta hakupenda kuzungumza, la! Isipokuwa hakuiamini sauti yake.

Hisia za hatari zilikuwa zikichemka akilini mwake na kumjaza hofu kila alipoyakumbuka maneno ya Shoka “…tumempata…” na kisha maongezi kukatika. Ni hili la mwisho lililomtisha zaidi. Amefika! Bila shaka ni Kakakuona. Amefika wapi? Alikuwa amefika katika ukumbi au alimfumania Shoka akiipiga redio hiyo? Kama ni hivyo kipi kinachofuata? Kombora alimwamini Shoka. Lakini pia aliamini kuwa Kakakuona yu kiumbe hatari zaidi ya simba aliyejeruhiwa. Ni hilo lililomtoa kasi ofisini.

Wakati wanafika mbele ya lango la ukumbi huo walisikia muziki ukikatika ghafla na kimya kikubwa kuzuka ndani ya ukumbi.Kombora aliruka nje ya gari na kumwambia askari mmoja alinde lango, asiingie wala kutoka mtu yeyote. Askari wa pili aliamriwa kufuatana naye.

“Kakakuona,” Kombora aliwanong’oneza. “Inawezekana yumo humu ndani. Picha zake mnazo. Mkimwona, kama hana silaha, msisite kumuua kwanza, maswali tutamuuliza baadaye. Okey?”

Ndani aliwakuta watu wakizungumza kwa sauti ya hofu na minong’ono. Umati mkubwa ulikuwa ukipambana kuingia choo cha wanaume ambako kila aliyetoka huko alikuwa kimya, aliyeduwaa kama aliyeona mzimu.

“Kuna nini?” Kombora alimuuliza mtu mmoja.

“Mtu amepigwa risasi.”

“A-me-kufa?” Kombora aliuliza akijaribu kuficha mshituko uliomkumba ghafla.

“Ataponaje? Unajua risasi mzee?” Kijana huyo alimjibu.

Ilimchukua Kombora na msaidizi wake dakika tatu nzima kuweza kupenya umati huo kuyafikia maiti. Hakuwa na haja ya kuyatazama kwa makini kabla ya kumtambua Shoka ambaye alilala kifudifudi kama anayechungulia kitu katika shimo la choo huku damu ikiendelea kutiririka na kufanya bwawa dogo jekundu liendelee kupanuka.

Kombora aliyasaga meno yake kwa hasira. Kisha alimwamuru mgambo ambaye alikuwa mbele ya mlango huo wa choo, akijaribu kuwazuia watu, kuufunga mlango wa choo hicho na kuulinda. Akarudi mlangoni ambako alitoa amri mpya. Watu wote watoke ukumbini humo, lakini si kabla ya kukaguliwa kila mmoja, tangu mifuko hadi vitambulisho.

Polisi wa Kituo cha Magomeni ambako tayari walikuwa wamepigiwa simu walipewa amri hiyo pia na kusaidiwa kuitekeleza. Wasichana, watoto na watu ambao hawakuwa na haja ya kushukiwa walitoka kwa urahisi. Watu wenye vitambulisho halali na shughuli zinazofahamika pia waliachiwa bila tabu. Lakini kuna wale ambao hata wao wenyewe hawazifahamu kazi zao, wale wenye zaidi ya kitambulisho kimoja, wao walitokwa jasho kwa maswali.

Baadhi yao walijikuta wakitupwa katika magari ya polisi na kupelekwa kituoni ambako waliendelea kuchunguzwa.

Muda wote huo Inspekta Kombora alikuwa nje ya ukumbi, kaegemea gari lake, mkono mfukoni ukiipapasapapasa bastola yake. Macho yake yalikuwa makini yakiuangalia kila uso na kila sura. Hakuiona dalili yoyote ya Kakakuona. Wala hakuwa na matumaini makubwa ya kuiona. Alivyomfahamu, kama mauaji hayo alikuwa kayatenda yeye, kwa vyovyote muda huo alikuwa maili kadhaa nje ya eneo hilo.

Hata hivyo, yawezekana akawa hakuyafanya yeye. Mtu aliyeyafanya anaweza akazubaa humo ukumbini, au akawa ameshirikiana na mtu ambaye atazubaa. Hilo ndilo lililomfanya asisitize uchunguzi wa makini kwa kila mtu.

Baada ya muda alimwita mgambo mwingine aliyekuwa akilinda magari na kumuuliza taratibu, “Ulikuwepo muda wote au ulitoka?”

“Nilikuwepo mzee.”

Unaweza kukumbuka ni magari mangapi yameondoka dakika kumi kabla ya tukio hili.”

“Kama sikosei, ni magari matano tu mzee.”

“Jaribu kukumbuka taratibu, unieleze magari hayo ni ya aina gani, yaliwachukua kina nani na yaliwapeleka wapi?”

Mgambo huyo alikuwa na kumbukumbu kali ambayo ilimfurahisha sana Kombora. Aliweza hata kukumbuka namba za magari matatu kati ya hayo, mawili ya kwanza yakiwa ya wenye disko hilohilo lililokuwa likipigwa hayakumvutia Kombora. Gari la tatu ambalo lililokuwa na wavulana wawili na wasichana wao pia halikumsisimua. Magari mawili ya mwisho ndiyo yalimfanya amtazame mgambo huyo kwa makini zaidi huku akitoa daftari lake dogo.

“Datsun nyekundu! Unasema ilikuwa na shombe wawili tu! Ambao walifika wakakaa dakika tano na kuondoka?”

“Ndiyo, mzee.”

“Namba yake…”

“TZA 42112”

Kombora aliinakili na kuuliza “Ilielekea wapi?”

“Sikumbuki vizuri nadhani ilielekea mjini.”

“Na hii nyingine unasema ni TZB 414, sio?”

“Ndiyo.”

“Toyota Corolla?”

“Ndiyo.”

“Ilikuwa na mtu mmoja tu! Ulimwangalia vizuri?”

“Sikupata nafasi ya kumwona vizuri. Lakini kwa harakaharaka nilimwona kama afisa hivi. Hata mavazi yake yalikuwa ya bei. Alitembea taratibu sana mkono mmoja mfukoni na kuingia katika gari lake. Nilitegemea atanipa walao asante kwa kumlindia gari lake, lakini hata kuniaga hakuniaga. Nadhani hiyo ndiyo sababu iliyonifanya niitazame gari yake na kuiweka namba akilini.”

Kombora alimsikiliza kwa makini na kunukuu hili na lile. Wakati akitaka kumtupia swali lingine, aliitwa mlangoni haraka. Mtu mmoja alikuwa amekamatwa na bastola. Alijaribu kuificha katika mapaja yake lakini mikono ya askari hao, ambayo imeelimika, ikaifikia.

Akapelekwa katika chumba cha ofisi ambamo aliendelea kuhojiwa huku Kombora akiifungua bastola hiyo na kuangalia risasi. Ilikuwa na risasi sita. Haikuwahi kufyatuliwa. Kibali cha kuwa na silaha? Hakuwa nacho. Kazi anayoifanya? Hakuijua. Kwa nini alikuja kwenye starehe na silaha? Hakujua. Kwa mtazamo wa harakaharaka, Kombora hakumwona kama mtu wake. Hivyo, aliamuru apelekwe kituoni pamoja na watuhumiwa wengine.

Hadi anahojiwa mtu wa mwisho ilikuwa yakaribia saa tisa alfajiri. Ndipo Kombora aliporudi ofisini baada ya kuhakikisha maiti yanapelekwa Muhimbili na familia yake kuarifiwa.

Ofisini Kombora aliinua simu na kumpigia Mkuu wa Usalama Barabarani, Mkoa wa Dar es Salaam. Bosi huyo, akiwa na usingizi mzito, alikoroma kwa hasira katika chombo cha simu “Nani?”

Lakini aliposikia jina na sauti ya Inspekta Kombora usingizi ulimtoka mara moja, akakiacha kitanda na kuuliza kwa upole, “Nikusaidie nini, mzee?”

“Samahani kwa kukusumbua,” Kombora alimwambia. “Ni suala ambalo haliwezi kulala. Naomba uwaambie vijana wako ambao wako zamu wanitafutie habari za magari haya mawili. TZB 414 na Datsun TZA 42112. Ikiwezekana waambie wayafuatilie kuona sasa hivi yako wapi. Waonye wasiwaulize wenyewe swali lolote ambalo linaweza kuwafanya washukiwe. Sawa?”

“Sawa.”

“Naweza kuyapata maelezo haya ofisini hapa kesho kabla ya saa moja asubuhi?”

“Tutajitahidi… nadhani tutapata.”

Kombora akaizima simu na kumtazama kijana wake mmoja ambaye alikuwa ameingia chumbani humo na kusimama kama aliyeitwa.

“Enhe?” Kombora akamtupia.

“Nimepokea simu kwa niaba yako mzee, baada ya kuona una simu nyingine. Imetokea Central ambako wanasema wamearifiwa na wavuvi juu ya maiti ya msichana mcheza disko ambayo wameiokota ufukweni. Wanasema amenajisiwa na kulawitiwa…”

“Kwa nini waniarifu mimi?” Kombora alimkatiza kwa ukali kidogo.

“Sura”

“Sura?”

“Wameniambia kwamba nikikwambia sura yake…”

“Inatosha!” Kombora alimwambia akiinua mkono wake kuuegemeza kwenye kichwa chake. Kwa mara ya kwanza katika maisha yake alihisi uzee ukianza kumshinda nguvu.

AKIWA mgeni katika hoteli hiyo, Sofia alivutiwa mara tu baada ya kushuka toka katika teksi iliyowaleta. Ram akamwongoza hadi mapokezi ambako aliomba ufunguo wa chumba namba 108. Walipanda ngazi hadi ghorofani ambako walifungua na kuingia hadi chumbani.

“Itabidi umsubiri,” Ram alimwambia Sofia ambaye alikwishajitupa juu ya kitanda na kujilaza. Usingizi wa pombe ukamchukua.

Hakuamka tena hadi majuzi, meneja wa hoteli alipojaribu kumwamsha na, hatimaye, Sajini Brashi alipomgeuza na kukutana na uso ule ambao aliokutana nao.

GARI lilimteremsha Joram Kiango mtaa wa pili. Kama ilivyo Dar es Salaam nzima, pamoja na kwamba sasa ilikuwa usiku wa manane, bado mitaa yote ilikuwa na watu waliokuwa na shughuli zao. Wako walioketi kwa makundi wakinywa pombe mbele za nyumba mbalimbali ambazo zimetokea kuichukulia biashara hiyo kama kitegauchumi muhimu.

Wengine walikuwa wakiuza chipsi, chai, au kahawa katika magenge. Baadhi walikuwa wamekaa tu kuepuka joto na mbu waliokuwa wakiwasubiri vyumbani mwao. Hivyo, ilikuwa rahisi kwa Joram kujipenyeza hapa na pale hadi alipoupata uchochoro uliomfikisha nyuma ya nyumba yake.

Alisikiliza kwa makini hadi alipohakikisha kuwa nyumba ilikuwa tupu kama alivyoiacha kisha, kama mwizi alifungua mlango taratibu na kujipenyeza ndani. Kama mwizi, vilevile hakuthubutu kuwasha taa. Badala yake alitumia tochi yake ndogo kufanya uangalifu mkubwa kuepuka asiguse kiti kilichotegwa bomu. Alilifikia kochi. Akaketi na kuanza kusubiri.

Kusubiri, ikiwa kazi ngumu kuliko zote kwa Joram Kiango, kulianza kumkinaisha dakika tano tu baadaye. Hata hivyo, alijua hiyo ilikuwa silaha yake pekee ambayo ingemfanya akabiliane na adui ana kwa ana. Maadui hao wakiwa wanaamini kuwa wamemlazimisha kuketi juu ya kiti chenye bomu, alikuwa na hakika kuwa baada ya muda wangependa kujua matokeo ya kikao hicho. Hivyo, wangetuma watu au mtu kuangalia. Ni mtu huyo ambaye Joram alikusudia amfikishe mbele ya bosi wao na mbele ya Nuru ambaye wamemteka nyara, apende asipende.

Subira ilikuwa dawa pekee.

Nuru pia alikuwa akivuta subira. Walikuwa wametua mahali fulani katika pwani ya Zanzibar kitambo. Lakini yeye aliendelea kujifanya hana fahamu adui zake hao walipokuwa wakiufunga vizuri mtumbwi wao na kisha kujitenga kando ambapo walipanga mambo yao kwa sauti za mnong’ono. Baada ya muda walimrudia Nuru, mmojawao akimtikisa.

“Bado amezirai?” mwenzie alijiuliza kwa mshangao.

“Asidanganye huyu,” yule ambaye alikuwa amemshika mkono alisema.

“Dawa yake ndogo sana.”

Aliupeleka mkono wake mfukoni na kutoa kibiriti, akawasha njiti moja na kukichoma kidole cha Nuru. Maumivu yalikuwa makali kupita kiasi. Lakini Nuru alijikaza kisabuni, bila kutikisika wala kufumbua macho.

“Au amekufa?” mwenzie aliuliza tena. “Angalia usimtie jeraha. Bosi hatafurahi. Angependa sana kumpata akiwa kamili. Mpe Konyagi kidogo itamzindua.”

Kiberiti kikazimwa na Konyagi kutolewa kutoka katika mfuko wa koti la mmojawao. Nuru aliponyweshwa fundo la pili alijitia kupiga chafya huku akifumbua macho.

“Ni… ni…niko wapi?” alijitia kuuliza.

Adui zake wakaangua kicheko.

“Uko wapi?” Chongo alimdhihaki. “Uko kisiwani. Uko katika kisiwa cha karafuu. Uko likizo ndogo.” Kisha, akazungumza kwa sauti ya amri. “Ni hivi. Tuko Zanzibar kwa ajili ya mapumziko kidogo. Tunataka kukuburudisha kwa wiki moja hivi kabla ya kurejea Dar. Mimi na rafiki yangu hapa tumeafikiana kuwa wewe ni msichana mzuri.”

“Na mtamu,” mwenzie alidakia.

“Ndio, mtamu tosha,” aliendelea. “Hatuna shaka kuwa tutakuwa kama wewe. Tumeafikiana, itakuwa mmoja anaburudika mmoja anashuhudia, ni mchezo mzuri… tunaamini utapenda.”

Nuru alihisi akiingiwa na hofu kubwa zaidi. Atafanya nini na watu hawa wenye wazimu? Alijiuliza. Apige kelele? La! Ni aibu kwake. Vilevile, kabla sauti yake haijafika popote risasi zingekuwa tayari zimeifumua kichwa chake. Hawakuwa watu wenye hata chembe ya simile.

Alichohitaji ni subira. “Tunaye rafiki yetu mmoja anayeishi hapahapa,” yule mwenye chongo aliendelea kueleza. “Tutakufungua kamba za miguu na kukufunga za mikono kwa namna ambayo itakuruhusu kutembea kwa urahisi zaidi. Mimi nitakuwa nyuma yako, ndugu yangu. Lazima utembee kama kawaida kana kwamba tupo pamoja. Sawa?”

Nuru alitikisa kichwa.

“Sina mchezo! Sina mchezo kabisa!” Chongo aliendelea kubweka. “Unaiona hii?” aliitoa bastola yake na kumwonyesha Nuru. “Unaona kuwa ina kiwambo cha kupotezea sauti! Kwa taarifa yako, mara tu utakapojitia unaanza umalaya wako mimi nitabonyeza. Kwangu ni rahisi sana. Unaonaje?” alisema akilenga bastola hiyo kwenye uso wa ajabuajabu wa mwenzie na kuifyatua.

Nuru hakuyaamini macho yake. Alimtazama adui huyo anavyotapatapa na hatimaye kuanguka chini kama gunia, huku tundu kubwa lililojitokeza hapo usoni likivuja damu nyingi.

Nuru alipomtazama tena mwenye chongo alimwona akitabasamu. Kwa sauti inayotabasamu vilevile alimsikia akijigamba, “Unadhani ningekubali kuchangia mtoto mzuri kama wewe na dude hilo? Usiwe na shaka mpenzi, ni mimi na wewe tu.”

Baada ya maneno hayo alianza kufanya kazi harakaharaka. Alimzoa Nuru na kumbwaga chini. Kisha akamzoa mwenzie huyo ambaye alikuwa akipapatika na kumbwaga ndani ya mtumbwi. Akautia mkono wake mfukoni na kuutoa ukiwa na kititita cha pesa na kukididimiza mfukoni mwake. Kisha, akaufungua mtumbwi na kuuelekeza baharini. Akautega usukani vizuri na kuufunga kwa kamba halafu aliwasha mashine, mtumbwi huo uliondoka kasi kuelekea baharini. Akamrudia Nuru na kumfungua kamba za mikononi na miguuni.

‘Sasa!’ Nuru aliwaza na kujiandaa kupambana. Hata hivyo, alisita. Hakuona kama ulikuwa usiku wake, kwa jumla ulikuwa usiku wa adui yake. Wangeweza kufanya chochote walichotaka. Hata ukimya na uhaba wa anga lao, mvuvi mmoja katika pwani yote hiyo ilikuwa dalili ya ushindi wa maadui. Ni hilo lililomfanya Nuru asite, azidishe unyonge na ulegevu, pindi kamba zikifungwa upya ubavuni mwake.

“Twende zetu,” Chongo alisema baada ya kuhakikisha ubora wa kazi yake. “Kama nilivyosema, kumbuka hila ndogo tu ni mauti yako.”

Wakaondoka, Nuru mbele, Chongo nyuma. Ulikuwa sawasawa na msafara wa malaika wa shetani.

Saa kumi na mbili kamili ilimkuta Kombora akiwa tayari ofisini mwake. Alikuwa amejiiba kwa dakika arobaini tu kwenda nyumbani kwake ambako alioga na kubadili mavazi. Akajaribu kunywa kifungua kinywa ambacho kilikataa kushuka, akaishia kunywa kahawa kikombe kimoja na kuipooza kwa glasi ya maji ya kunywa.

Ofisini alikuta majalada kadhaa yakiwa juu ya meza yake. Moja ilikuwa taarifa ya magari aliyoyahitaji, ambalo lilifika nusu saa iliyopita. Nyingine ilikuwa taarifa ya uchunguzi mbalimbali la watu waliokuwa wamekamatwa pale Lang'ata. Jalada la tatu lilikuwa la taarifa ya kifo cha Doll.

Shingo upande, Kombora alianza na jalada hilo la mwisho, mara tu alipolifunua macho yake yalikutana na ile picha ya kusikitisha ambayo hakutaka hata kuiona. Picha ya marehemu, msichana mzuri, ambaye alilala juu ya mchanga, ufukoni, uchi kama alivyozaliwa, mavazi yake yakiwa yametupwa kando. Umbo lake lilikuwa zuri, la kuvutia toka miguuni hadi shingoni, usoni kulikuwa hakutazamiki. Sura yake ilikuwa imeharibiwa kinyama kama wale marehemu waliotangulia. Kombora alifunika huku akisaga meno yake kwa hasira kisha akayasoma maelezo yalioambatana na picha hiyo.

Ilikuwa kama ilivyotarajiwa maiti aliokotwa na wavuvi mnamo saa sita na robo usiku akiwa kama alivyo pichani. Taarifa ya madaktari ilithibitisha kuwa aliuawa kwa aina ileile ya sumu iliyowaua waliotangulia, sumu ambayo hadi sasa wanamaabara walikuwa hawajapata kuifahamu. Taarifa hiyo ilieleza jina la marehemu, wazazi wake, marafiki zake na kwamba jioni hiyo alionekana katika ukumbi wa Lang'ata muda mfupi kabla ya kifo chake.

Kombora aliliweka kando jalada hilo na kutwaa lile lenye maelezo ya watu walioshukiwa usiku huo. Alifunua harakaharaka akitafuta maelezo ambayo yangemfanya ayape uzito mkubwa zaidi. Kama alivyotarajia, hakuona kuwa kati ya hao kuna yeyote ambaye angeweza kuwa mtu wake.

Yule aliyekamatwa na bastola alitambulika baadaye kama jambazi mkubwa ambaye alikuwa akitafutwa muda mrefu kwa kosa la mauaji ya tajiri mmoja wa Kihindi huko Mwanza. Watu wawili waliokuwa na vitambulisho vya bandia walifahamika kama matapeli wenye tabia ya kughushi hundi za bandia. Mmoja hakuwa na akili timamu. Alikuwa kavaa vizuri anazungumza kama kawaida. Hata hivyo, iliwachukua polisi saa nzima kugundua kuwa wanazungumza na punguani.

Inspekta Kombora aliandika maelezo mafupi ya jalada hilo. Aliagiza wasio na hatia waachiwe mara moja. Kisha, akalitupa kando na kuvuta jalada la mwisho ambalo ndilo hasa alilolihitaji, taarifa ya mienendo ya magari mawili ambayo aliyatilia shaka. Maelezo yalikuwa mafupi, lakini yakiwa wazi kabisa.

Datsun TZA 42112 ni mali ya Swaleh Akbar, Mwarabu mwenye damu mchanganyiko, mama mswahili wa Rufiji, aliondoka nchini zaidi ya miaka kumi iliyopita na kuhamia Oman ambako amerudi juzi na malori matatu, basi kubwa la abiria na gari hilo dogo la kutembelea.

Akiwa na umri wa miaka ishirini na mitatu tu, Swaleh ni mtundu na mtumiaji kupita kiasi. Kila jioni gari lake huwa liko njiani, katika majumba ya starehe. Katika usiku mmoja gari lake linaweza kuonekana katika majumba kumi ya starehe. Si mnywaji sana, lakini anapenda sana kunywa katika makundi huku akinunua bia kama maji.

Baada ya kupokea amri ya kulisaka gari hilo askari wa barabarani walilipata mnamo saa kumi kasoro, likitokea Buguruni. Lilikuwa likielekea Kariakoo. Ghafla waliliona likibadili njia na kuelekea Keko. Sasa hivi gari hilo liko mbele ya nyumba moja mbovumbovu, hukohuko Keko. Askari mmoja wa Kombora ameichukua kazi hiyo toka mabegani mwa polisi wa Usalama Barabarani. Analitazama gari hilo toka mbali, akiisubiri amri ya Kombora.

Kombora aliwaza kwa muda, kisha, akaichukua kalamu yake na kuandika juu ya karatasi hiyo, "Watu wawili zaidi waende huko. Watumie njia yoyote kuingia humo ndani, kuona wanafanya nini na kama ni watu wetu waletwe mara moja."

Taarifa ya pili ilikuwa fupi zaidi, lakini Kombora aliisoma kwa makini zaidi. Si kwa ajili ya hisia ambazo zilikuwa zikichemka katika roho yake tu, bali kwa kuwa aliona taarifa nyingine zote hazikumpa hali aliyotarajia.

Gari dogo aina ya Toyota Corolla TZB No. 414 lilionekana katika Barabara ya Ocean likitembea taratibu. Lilipofika mbele ya Hoteli ya New Africa, lilipaki na dereva wake kuingia hotelini ambamo alionekana kuchukua ufunguo mapokezi na kupanda lift hadi ndani ambako yaelekea amelala.

Gari hili ni mali ya kampuni moja ya ukodishaji magari iitwayo Shabir Safaris Limited ya Morogoro. Kwa mujibu wa mwenye kampuni hiyo, Shabir Datoo, gari hilo lilikodishwa wiki mbili zilizopita kwa Mmarekani mweusi mmoja na mkewe, hati ya usafiri namba… iliyotolewa mjini Miami miaka minne iliyopita chini ya jina la Morrice Juakali.

Huyu ni mtu wetu! Kombora aliwaza akiisoma tena taarifa hiyo. Alitafuna ncha ya kalamu yake kwa muda kabla hajainama na kuandika katika jalada hilo.

“Ongezeni ulinzi nyuma na mbele ya hoteli. Kila mmoja awe na silaha na awe na picha halisi ya mtu wetu akilini. Kila hadhari ichukuliwe kumfanya mtu huyu asishuku anachunguzwa. Na mara tu atakapoonekana akitoka nitaarifiwe mara moja.”

Baada ya hayo Kombora alijaribu kutulia kwa kuagiza aletewe kahawa huku akivuta jalada la Kakakuona na kuanza kulipekua tena. Japo alilisoma mara kadhaa swali lilelile lilikuwa wazi, bila majibu yoyote, rohoni na akilini mwake; Kakakuona anahitaji nini kwa Joram Kiango? Kwa mara nyingine aliamua kuliweka swali hilo kando na kuendelea kusubiri kukamatwa kwa Kakakuona.

Alipoikumbuka kahawa yake tayari ilikuwa imepoa tena.

‘Mchezo umeanza kuwa mtamu,’ Kakakuona aliwaza akichungulia dirishani katika tundu dogo aliloliunda kwa kutoboa pazia la dirisha. Akiwa mtu mwenye uwezo wa kumnusa polisi hata awe wapi, hakuwa kipofu wa kushindwa kuwatambua watu walioiinamia injini ya teksi aina ya BMW, iliyoegeshwa mbele ya hoteli hiyo, kando ya gari lake, kuwa ni polisi.

Mtu wa tatu alikuwa ameongezeka, polisi pia. Chumba chake kikiwa upande mzuri, ghorofa ya tano katika hoteli hii, alikuwa na nafasi nzuri sana ya kuwatazama.

Tangu usiku alipokuwa akirejea toka ufukoni, ambako alimshughulikia kikamilifu yule msichana na kumwacha maiti baada ya kuiharibu sura yake, Kakakuona alihisi kuwa anafuatwa. Hakuwa na hakika.

Hivyo, alifanya hila za kupita hapa na pale, kupinda kona hii na ile, kupunguza na kuongeza kasi n.k. Wakati alipoamini kuwa amelipoteza gari hilo aligeuza njia na kuja New Africa. Alipokuwa akivikusanyakusanya vifaa vyake na kuvitia katika briefcase ndipo alipoliona gari hili likizimika katikati ya barabara na watu wawili kushuka. Walilivuta hadi kando ya gari lake na kulifunua boneti. Kisha, wakafunga hiki na kufungua kile. Hawakuinua uso kumtazama, lakini Kakakuona alijua kabisa kuwa wako pale kwa ajili yake. Alitulia katika gari kwa dakika kadhaa akivuta sigara huku mkono wake ukiipapasa bastola yake, Alipoona hawamjii alifahamu kuwa askari hao hawakuwa na amri ya kumkamata. Hivyo, aliingia chumbani ambako, alioga akaweka vifaa vyake sawa na kisha akazima taa na kujilaza kitandani.

Nusu saa baadaye aliamka na kuwachungulia. Mtu mmoja alikuwa ndani ya gari wa pili akiendelea kuhangaika na injini ‘Watasubiri sana’ aliwaza akijilaza tena na kujaribu kuwaondoa akilini.

Hata hivyo, akili yake haikumruhusu kustarehe. Hisia za hofu, kitu ambacho kwa kawaida hakimo kabisa katika damu yake, zilikuwa zikimnyemelea. Alijihisi akijilaumu na kujutia uamuzi wake wa kwenda Lang’ata na kumfuata yule msichana ambaye aliamini kwa namna moja au nyingine amekuwa chanzo cha polisi kumnusa mapema namna hiyo.

Pamoja na ukweli kuwa hakuwa hata na chembe ya hofu ya kukamatwa na polisi hao, bado hakuona kama ilimstahili kushukiwa mapema hivyo, jambo ambalo lingemfanya aanze upya maisha ya kujifichaficha hata kabla ya kwenda kuyazoa yale mamilioni ambayo yanamsubiri pindi atakapomfikisha Joram Kiango au mzoga wake mbele ya wadhamini wake.

‘Hawana lolote la haja wanalofahamu juu yangu,’ aliwaza. ‘Wangekuwa nalo wangekuwa wamekwishanipigia hodi. Nitalala zangu kwa amani. Kesho mchana nitamshughulikia Joram na kisha kumfuata Chongo popote alipojichimbia.’

Sasa ilikuwa saa mbili asubuhi. Gari lile lilikuwa likiendelea kuchokonolewa. Mara liliwaka. Wale watu wawili wa mwanzo walitabasamu. Baadaye walionekana wakimlipa yule mtu wa tatu na kisha kuondoka zao. Yule mtu wa tatu alitazama huku na huko, kisha, akavuka barabara na kuanza kutembea taratibu kando ya Benki ya City Drive hadi alipotokomea, miongoni mwa watu wengine.

Kakakuona hakuwa mtu wa kuingia katika mtego mdogo kama huo. Alijua fika kuwa kuondoka kwa watu hao ni kubadili zamu tu. 'Wako wengine sehemu nyingine, ambao wananichunguza kwa makini. Acha waendelee kupoteza muda wao,' aliwaza akiingia bafuni ambako alioga, akabadili nguo na kisha kupakia vitu vyake vyote muhimu katika briefcase yake maalumu. Kisha, akawaita wahudumu wa vyumba na kuagiza kifungua kinywa na gazeti la Daily News. Alikunywa chai yake kwa utulivu huku akilipekuapekua gazeti hilo.

Mara macho yake yakavutwa habari fupi iliyopachikwa kando katika ukurasa wa nne. Ilieleza juu ya mtumbwi wa mashine ambao uliokotwa baharini na wavuvi wa Zanzibar, ukiwa na maiti ya mtu mwenye jeraha la risasi. Habari hiyo iliendelea kueleza kuwa marehemu huyo alikutwa na bastola mfukoni mwake, jambo ambalo lilifanya iaminike kuwa alijiua mwenyewe.

Maelezo juu ya umbile na mavazi ya hayati huyo, yalimfanya Kakakuona amtambue mara moja. 'Chuchu' alinong'ona. 'Chongo amemuua. Sasa bado zamu yake.'

Alitazama saa yake, tatu kasoro. Akainuka, akauchukua mkoba wake na kutoka nje ya hoteli. Baadaye akamtupia macho msichana wa mapokezi ambaye alikuwa akimchekea kana kwamba yuko katika mashindano ya kutabasamu. Akalifuata gari lake na kuingia.

Alhaji Salum Banduka ni mmoja kati ya watu wanaojiheshimu na wanaoheshimika sana mjini Zanzibar. Tangu alipohamia hapa toka Bara, aliondokea kuwa mtu ambaye kila mtu alipenda kumtolea mfano.

Tazama aliingia hapa hana kitu zaidi ya mtaji wake wa shilingi elfu ishirini, kanzu moja, suruali ya pili na makubazi miguuni. Tripu nane za Bara na Pemba zilimfanya aache biashara ya chakula na kuanza kwenda zake Uarabuni. Leo hii tayari anayo maduka matatu, daladala nne na hoteli kubwa ya kitalii!

Tazama! Pamoja na utajiri wote huu hata sala moja haimpiti. Tayari amehiji Makka mara tatu na anatarajia kwenda tena mwaka huu. Wala hana kiburi. Kila siku huwa yupo katika magenge ya vijana na wazee akisimulia jinsi shilingi elfu ishirini zilizomfanya awe tajiri.

"Hawakukosea wazee waliposema, "Akili ni mali…" Banduka alipenda sana kuitumia methali hiyo mwisho wa maelezo yake, kwa sauti ya kicheko."

Huyo alikuwa Banduka wanayemjua wao; mtu mfupi, mnene, mwenye tumbo la kutosha na kovu lililomeza nusu ya shavu lake la kushoto, mtu ambaye alitulia na wake zake wawili, mmoja akiwa na damu ya Kiarabu wa pili ya Kimvita.

Kama wangefahamu kuwa Banduka huyuhuyu ndiye yule aliyevuma sana huko Bara zaidi ya miaka kumi iliyopita kwa ushiriki wake katika wizi, ujambazi na mauaji, kamwe wasingempa hadhi msikitini wala heshima mtaani.

Kama wangejua kuwa kuja kwake visiwani ilikuwa ni kujificha baada ya kushiriki katika kazi nzito ambayo iliacha familia nzima ya Mhindi mmoja mahututi hali wao wakiondoka na milioni saba kamwe visiwa hivi vya amani na utulivu visingempokea.

Banduka alikuwa na bahati ya mtende. Siku hiyo kazi yake ilikuwa ndogo tu, kukaa chonjo, bastola mkononi, akilinda mtu yeyote ambaye angetokea kuitibua kazi yao katika nyumba hiyo. Kazi ilikwisha kwa amani. Yeye, ambaye hakujitokeza mbele ya uso wa Mhindi, akapewa jukumu la kulinda furushi hilo la fedha ili ikipoa wagawane.

Kama muujiza, usiku huohuo wenzake wote walikamatwa. Yeye akatoroka na jahazi la makasia hadi hapa ambapo alijichimbia. Kwa kuwa haukupatikana ushahidi wa kutosha wenzake walichukua miaka saba, saba. Hakuna aliyemtaja.

Ndipo alipolivua jina lake la Bandua na kujiita Banduka. Akauvua ujambazi pia katika fikra zake na kuapa kuwa kamwe asingejihusisha nao tena kwa namna yoyote.

Lakini kiapo chake hicho hakikudumu muda mrefu. Mara tu alipoanza kuipanua miradi yake alijitokeza askari kanzu mmoja ambaye jioni moja alijipenyeza hadi katika chumba chake cha sala. Banduka alishtukia mtu kasimama mbele yake akitabasamu kifedhuli.

"We' nani?" alifoka.

“Usitake kunifahamu. Suala ni kwamba mimi nakufahamu wewe. Unaitwa Alhaji Banduka. Mimi najua kuwa wewe ni Bandua, mwizi, muuaji na tapeli mkubwa ambaye unasubiriwa Bara kwa hamu kubwa sana. Kataa…”

Banduka aliduwaa. Hakutarajia kuwa kisiwani hapa kulikuwa na binadamu yeyote anayehifahamu rekodi yake.

“Usishangae,” askari huyo alimzindua “Wewe una pesa, mimi ninayo siri yako. Leta pesa nikufichie siri. Vinginevyo, kesho hutakuwa huru.”

Baada ya ubishi mrefu, Banduka akijaribu kukanusha, aligundua kuwa kidudumtu huyo alikuwa na ushahidi tosha dhidi yake.

“Unataka kiasi gani?” alimuuliza.

“Milioni tatu tu.”

“Milioni tatu!” Banduka alifoka. “Una wazimu!”

“Labda. Lakini ni milioni tatu au roho yako. Mimi pia nimechoka kukesha usiku na mchana nikiwalinda wenye pesa zao. Nataka kupumzika kama wewe.”

Baada ya ubishi mwingine mfupi Banduka aliafiki. “Njoo kesho kuchukua.”

Kauli hiyo ilimfanya askari huyo aangue kicheko. “Nina akilia bwana Banduka. Mara tu nikiondoka utaanza kubuni mbinu za kuniangamiza. Pesa hizo nazitaka leo. Sasa hivi. Nimeingia humu kwa siri bila ya mtu yeyote kuniona ili tumalizane kabisa. Nikitoka kila mtu ajue lake.”

Kipande hicho cha habari kilimsaidia sana Banduka. Alikuwa amechoka kusumbuka. Alikuwa ameishiwa na hamu ya kufungwa na kuwakimbiakimbia polisi. Alivuta droo yake ndogo kama anayetaka kuchukua ufunguo. Alipoutoa mkono wake ulikuwa umeshikilia kisu chake kirefu ambacho dakika hiyohiyo kilipotelea katika kifua cha askari huyo, ambaye hakuwahi kupiga hata kelele. Alianguka hali katokwa macho kwa mshangao na maumivu.

Banduka aliifanya kazi ya kufuta damu na kumzika marehemu kwa siri sana. Kisha, akatulia kusikiliza kama kuna mtu yeyote ambaye angemuunganisha yeye na “kutoweka” kwa askari mgeni aliyetokea Bara. Wala.

Ikafuata miaka ya starehe, amani na utulivu. Banduka akaweka kiapo kingine cha kutojihusisha tena na aina yoyote ile ya ujambazi, kiapo ambacho leo hiihii alikikumbuka na kuanza kukitilia shaka kama kweli atatimiza.

Alfajiri hii aliamka mapema, kama ilivyokuwa kawaida yake ili aende zake msikitini. Alipoitazama saa yake aligundua kuwa alikuwa ameamka nusu saa kabla ya muda wa sala. Akiwa chumbani peke yake, baada ya mkewe mkubwa kwenda zake Bara, aliamua kuamka na kuoga. Akajaza maji baridi katika beseni la kuogea na kuyapoza kwa maji moto kidogo. Wakati akivua taulo alilojifunga kiunoni ili ajitumbukize alihisi mlango wa bafuni ukifunguka na umbo la mtu kujipenyeza.

“Nani?” alifoka kwa mshangao.

“Taratibu, aisee. Mie wako. Tuseme umenisahau?”

Banduka alimtazama mtu huyo aliyeingia kama kivuli. Roho ikamlipuka. Miaka zaidi ya kumi iliyowatenganisha katu isingemfanya amsahau Chongo, mmoja kati ya watu ambao Banduka hakupenda kabisa kuwatia machoni. Hisia za hatari zilimwingia. Aliduwaa kwa muda kabla hajauliza kwa sauti ya unyonge, japo ilijaa hasira, “Umeingiaje humu?”

“Nimeingiaje? Mimi na wewe! Usiniambie kuwa umekuwa bwege kiasi hicho Banduka. Jumba lako hili halina kufuli hata moja. Kila nilipokuwa nikija hapa Zanzibar kutumia, nilikuwa naitembelea nyumba yako kuichunguza. Nilishangaa unavyoishi kama ndege ukijifanya mswahilina. Nasikia hata Makka umekwenda. Si umekwenda tu kuutia nuksi mji ule takatifu? Wewe ni wa kwenda Maka!”

Hofu ilianza kumtoka Banduka. Akijua kila dakika anayokaa na mshenzi huyo ilikuwa ikihatarisha usalama wake, alimwambia kwa ukali kidogo, “Sijui umefuata nini hapa. Sina hamu ya kuisikiliza sauti yako mbovu wala kuitazama sura yako nzuri. Inatosha. Sasa ondoka niendelee na sala zangu.”

“Sala!” Chongo alicheka. “Sala! Ha! Ha! Wadanganye binadamu usimdanyanye Mungu. Sala zako hazitoki nje ya chumba hiki, Banduka,” alisema na kuongeza, “Unajua Banduka nakudai pesa nyingi, mamilioni. Nafahamu kuwa ulitusaliti ukituacha tuozee gerezani hali wewe unatumia pesa zetu. Lakini hakuna anayekulaumu. Hakuna mwenye shida kati yetu. Kwa upande wangu mimi sihitaji utajiri. Nahitaji pesa kidogo za kula. Lakini kwako sihitaji pesa. Nahitaji hifadhi kwa siku mbili tatu tu. Niko na mpenzi wangu.”

“Siwezi kukupa hifadhi. Katafute pengine.”

2

“Usinilazimishe kukulazimisha,” Chongo alifoka. “Mbona huna shukrani, mtu wewe? Ombi dogo kama hilo likushinde wakati unanenepa tumbo kwa mamilioni yangu?” alimaliza kwa kicheko chake cha kikohozi.

Banduka alipoona kuwa hana uwezo wa kumkana alijitia kuafiki huku akibuni mbinu zaidi ambazo aliamini zingemfanya Chongo ajute milele kumtibulia maisha yake ya amani ambayo amekuwa akiishi miaka nenda rudi.

“Nitakuhifadhi,” alimwambia, “lakini kwa masharti kwamba hutatoka nje ya nyumba hii mchana, na utakapokamatwa usithubutu kunitaja kwamba tunafahamiana. Upo?”

Chongo alipochelewa kujibu aliongeza, “Usijidanganye kuwa ushahidi ulionao utakusaidia chochote. Nina marafiki wakubwa hapa. Ukikorofisha ukamatwe elewa kuwa utakufa na ushahidi wako hata kabla hujafika mbele ya mahakama.”

Hilo lilimchekesha Chongo. Baada ya kicheko chake alisema, “Kabla sijafa mimi elewa kuwa wewe utakuwa na risasi sita kichwani mwako. Hilo nakuomba ulitie maanani. Hila yoyote itakuletea balaa. Unaiona hii?” kwa wepesi wa ajabu, bastola yake ilitolewa na kuzungushwa angani, akairusha mara mbili na kuidaka huku ikizunguka. Kisha, aliipunga kumwelekea Banduka

“Unaona?” alimuuliza. “Sina mchezo, sitaki mzaha. Na kuanzia sasa hivi ni mimi nitakayetoa amri zote katika nyumba hii hadi nitakapoondoka. Tumeelewana?”

Muda mfupi baadaye, kwa amri ya Chongo, Nuru ambaye alikuwa amelazwa nje ya mlango kwa nyuma, aliingizwa humo akiwa amebebwa na Alhaji Banduka. Nuru akiwa taabani kwa uchovu. Alijifanya mgonjwa zaidi kiasi kwamba hata alipoongea kuomba maji iliwachukua dakika mbili kumwelewa. Alipatiwa maji. Kisha, Banduka aliamriwa kuleta chakula. Ulipatikana wali mkavu kwa kahawa. Nuru alifunguliwa mkono mmoja na kutakiwa ale. Kwa jinsi alivyokuwa na njaa aliusikia wali huo kama biriani ya kuku.

“Unaweza kwenda kulala,” Banduka aliambiwa. “Nitakuhitaji kesho saa mbili. Kumbuka ukijitia akili utajuta kuzaliwa. Nenda.”

Banduka akatoka.

Chongo akaufunga mlango nyuma yake na kuutia ufunguo. Kisha akamgeukia Nuru na kusema, “Mpenzi… tupo peke yetu kama nani na nani vile?… Adamu na Hawa,” akajijibu mwenyewe. “Wapi ilikuwa vile?… Bustani ya Edeni… au sio?…”

Nuru hakujua kama ilimpasa kulia ama kucheka kwa kipande hicho cha habari. Kufanya mapenzi na dude hilo, rohoni mwake ilikuwa ni aibu na tusi lisilostahimilika. Kwa mara nyingine akafanya uamuzi kuwa ni maiti yake tu ambayo ingelala na chongo. Yeye hapana.

“Unasemaje mpenzi?” Chongo alikuwa akiendelea. “Si unajua kuwa roho yako iko mikononi mwangu? Basi uweke pia mwili wako miguuni mwangu. Ukifanya kazi nzuri naweza kukuachia roho yako. Tuna muda wa saa tatu za kusubiri. Nataka tutumie kwa kujiburudisha. Baada ya hapo nitapiga simu moja Dar es Salaam. Majibu yakiwa mazuri utatoka chumba hiki ukiwa na sura nyingine kabisa, yakiwa mabaya utatoka kama ulivyo, pengine na mtoto wetu tumboni mwako. Upo?”

Nuru alimtumbulia macho, hasira zikichemka rohoni mwake.

“Sema,” Chongo alisema akimsogelea na kumminya titi. Nuru alitazama kwa makini zaidi.

Kabla hajaliwasha, alichunguza kila kitu kwa makini. Hakuona kasoro yoyote. Akaliwasha na kuliondoa kufuata Mtaa wa Samora. Macho yake yalikuwa makini. Alisimamisha gari hilo mbele ya duka moja na kuingia. Hakuona gari lolote. Alipotupa macho mbele aliona gari moja dogo jeupe likisimama, magari manne mbele yake. Alipomfikia dereva wa gari hilo, alimtazama kiujanjajanja katika kioo chake cha ndani. Akatabasamu na kumpita huku yeye pia akijitia hamwoni.

Aliendesha gari moja kwa moja hadi Mtaa wa Lumumba. Mbele ya Jengo la Ushirika. Hapo alishuka na kukiendea kikundi cha watu ambacho kilikuwa kikisubiri lifti. Yeyote aliyekuwa akimfuata Kakakuona aliamini kuwa hakuwahi kuipanda lifti hiyo kwani mara tu alipofika lifti ilifika, naye akawa mtu wa mwisho kuingia.

Alipanda hadi ghorofa ya mwisho kisha akashuka nayo hadi mwisho wa lifti hiyo ambako ni ghorofa moja zaidi chini ya ardhi. Huko aliacha lifti na kufanya haraka kuifuata ngazi ambayo inatokea upande wa pili wa jengo hilo. Huko alitembea hadi mtaa wa pili ambapo alikodi teksi iliyomfikisha Kariakoo ambako alishuka na kukodi teksi nyingine iliyompeleka Ilala.

Akaingia ofisi ya ndege za kukodi, AirTanzania, na kuomba usafiri wa haraka kwenda Zanzibar. Akitumia pesa nyingi na hati zake za bandia dakika ishirini baadaye alikuwa akielekea juu ya anga ya Zanzibar.

Ulikuwa usiku mrefu mno kwa Joram Kiango, usiku unaochosha na kukinaisha kupita kiasi. Kwa mtu wa vitendo kama yeye, ilikuwa kama adhabu kukesha wima, ndani ya chumba chako, kando ya kitanda chako, ukisubiri jambo ambalo halitokei.

Kucha aliyatega macho yake yakipasua kiza kuchunguza chochote ambacho kingekuwa kigeni chumbani humo. Kadhalika, masikio yake yalikuwa makini, tayari kunasa mchakacho wowote ambao angeusikia. Lakini hadi kulipopambazuka hakusikia wala kuona chochote, jambo ambalo lilimfanya ajikute akipandwa na hasira kali zaidi dhidi ya yeyote aliyekuwa akimtendea kitendo hicho, hasira ambazo kiasi zilimfanya ajione mpumbavu kwa uamuzi wake wa kuwasubiri adui hao.

Ilikuwepo haja gani ya kupoteza usiku mzima akiwa ameketi akiwasubiri badala ya kuwa mitaani akipambana nao? ‘Haiwezekani kuwa kitendo chake cha kukesha hapo bila ya kushughulika ndicho hasa walichokihitaji ili waendelee na unyama wao mitaani? Wamenifanya mpumbavu!’ aliwaza kwa uchungu na hasira. Na kwa hasira hizo alitabasamu.

Hata hivyo, hakujilaumu sana. Alijua kama siyo leo, kesho wangekuja kuhakikisha mauti yake. Na alikusudia wamkute akiwa anajua adui yake ni nani na anakusudia nini. Hivyo, asubuhi hiyo aliamua kuitumia kwa uchunguzi.

Kulipopambazuka kikamilifu, Joram akaingia bafuni kuoga. Kisha, akaliendea kabati la nguo na kutafuta moja kati ya mavazi yake ambayo humfanya asitambulike kwa urahisi wala kumtazama kwa makini. Leo alivaa kanzu nyeupe, kijikoti cheusi juu, ndala miguuni, kofia pana kichwani na miwani myeusi.

Akachukua fimbo yake ya kutembelea na kutoka nje akitumia mlango wa nyuma. Baada ya kupenya hapa na pale, aliifikia barabara kuu ambako alikodi gari lililomfikisha mjini. Huko alitafuta hoteli na kujipatia kifungua kinywa. Kutoka hapo alikwenda Mtaa wa Mkwepu kwenye duka moja ambalo wanaruhusu wapita njia kupiga simu kwa malipo. Alimwomba Mhindimwenye simu hiyo aitumie nusu saa huku akimpa shilingi elfu tano.

“Napiga hapahapa mjini zikiisha, nitaongeza,” alimwambia.

Huku akiwa na mshangao, mwenye duka huyo alipokea harakaharaka na kumpisha Joram kiti.

Polisi ni watu wanaojua sana kufumba midomo. Kujaribu kunyofoa ukweli toka katika mikono ya polisi ni kazi ngumu kama kujaribu kung’oa ulimi wa jabali. Lakini si kwa mtu kama Joram Kiango. Hadhi yake katika masuala ya mapambano ilimpatia marafiki wengi katika jeshi hilo. Aidha, alikuwa na marafiki zake wawili, watatu ambao humuuzia siri na habari mbalimbali anazohitaji, kama vile ambavyo yeye huwapa ‘tip’ wanapofuatilia masuala fulanifulani anayoyafahamu.

Akiwa na hakika kuwa mauaji ya wasichana wote wawili yalikwishagundulika na polisi, simu yake ya kwanza aliielekeza Idara ya Upelelezi ya kituo kikuu. Alikuwa na bahati ya kumpata mtu wake.

Baada ya maongezi mafupi ya mafumbo-mafumbo, Joram aliweka simu chini. Habari alizopata licha ya kuwa hazikumnufaisha sana bado zilimwongezea hasira. Mpelelezi huyo alikiri kuwa bado kuna jambo la ‘moto sana’.

Anachofahamu ni kwamba, raia watatu na askari kanzu mmoja wamekwishauawa. Ni hilo lililomsikitisha Joram Kiango. Watu zaidi wameendelea kufa wakati yeye ameketi juu ya kochi akisubiri adui ajilete. Aibu iliyoje!

Maswali yake yaliyofuata hayakupata majibu zaidi. Hivyo, Joram akakata na kupiga kwenye simu ya Kombora. “Namtaka Shoka,” aliomba.

“Hayupo”

“Yuko wapi?”

“Amehama.”

Moyo wa Joram ulidunda kwa nguvu. Hakuwa mgeni wa msamiati huo. Askari anapotamka moja kwa moja kuwa askari fulani amehama, huwa haina maana nyingine zaidi ya kufa. Yawezekana ni yeye aliyekufa kwa ajili yake? Joram alijikaza na kutaja jina la pili.

“Hayupo,” mtu wake wa tatu pia hakuwepo.

Wakati Joram akiwa ameduwaa, mtu aliyekuwa upande wa pili wa simu alimshangaza alipomwambia, “Au nikupe Inspekta Kombora mwenyewe Joram?”

“Ndi…yo… hapana. Labda hahitaji kuniona. Pengine wewe unaweza kunisaidia…”

“Najua Inspekta hana muda wa kukuona. Wala asingependa kukushirikisha. Hata hivyo, mimi nitakuibia siri. Suala hili ni zito na gumu. Watu wanaendelea kuteketea kwa ajili yako, wakati uko gizani. Mwiba hutokea ulikoingilia. Tunaweza kuonana wapi nikudokolee hicho tulichonacho?”

“Tukutane New Africa…”

“Hapana.”

“Embassy.”

“Haifa?”

“Wewe unadhani wapi panafaa?” Joram alimuuliza.

“Hapohapo ulipo. Dakika tano baadaye. Uko wapi?”

Joram akaeleza.

Kama walivyo vijana wote wa Inspekta Kombora, kijana huyu ambaye alimtokea Joram Kiango dakika saba baadaye, alikuwa mkakamavu, mtulivu na mstaarabu kiasi kwamba haikuwa rahisi kumshuku kuwa ni kachero. Lakini si kwa Joram. Alitambua mara tu alipoingia katika mgahawa huo, gazeti mkononi na kuketi kama wateja wengine, akimsubiri mhudumu ambaye aliagizwa kuleta soda. Joram aliiacha meza yake na kuhamia meza aliyoketi bwana huyo.

“Ningeomba kuwa mwenyeji wako,” alimnong’oneza.

Mgeni huyo alimtazama Joram kwa mshangao kidogo, mshangao ambao uligeuka kuwa tabasamu baada ya kumtambua, licha ya mavazi yake bandia.

“Vizuri. Nadhani tunaweza kuzungumza hapahapa. Au?”

“Siyo pabaya.”

“Kwanza, ningeomba unielewe kuwa kwa kuzungumza nawe navunja amri zote za kazi yangu. Jambo ambalo natarajia kuzungumza ni siri kubwa sana ambayo haikutakiwa kuyafikia masikio ya raia yeyote yule. Mzee Kombora ataninyonga kwa mkono wake kama atasikia kuwa nimekudokezea. Natumaini unanielewa.”

“Vizuri sana,” Joram alimjibu.

“Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, sioni umuhimu wa kutokukuhusisha. Hakuna asiyefahamu mchango wako katika kupambana na udhalimu hapa nchini na kote duniani. Zaidi, sioni kwa nini watu wasio na hatia waendelee kuuawa kinyama wakati wewe umestarehe. Sidhani kama wewe u mvivu kiasi hicho. Natumaini tutakuwa bega kwa bega kupambana naye. Sawa.”

Joram aliona kama anayepotezewa muda kwa maelezo yasiyo ya msingi. Alichohitaji ilikuwa ni kitu kidogo sana. Kuelewa makachero wanaelewa nini juu ya adui huyo, ili aanze harakati. Kulala ndani kulikuwa kumemchosha.

“Unaonaje ukikata mahubiri na kunieleza kile ulichopanga kunieleza. Huoni kama tunapoteza muda?” alimuuliza.

“Yote ambayo naweza kukueleza yako katika gazeti hili. Ambacho hakimo ni kwamba sasa hivi Kakakuona yuko Zanzibar.”

“Kakakuona?”

“Inaonekana humfahamu,” kachero huyo alieleza. “Huyo ndiye mbaya wako. Anaweza kuwa ni mtu hatari zaidi ya kifaru aliyejeruhiwa. Anaua huku ametulia kama anakunywa maji baridi. Kifo chake ni muhimu kitokee kabla hajatuathiri,” alimaliza akiinuka huku akiliacha gazeti lake mezani.

“Wazulu wa kale hawakuwa na neno ‘asante’ katika msamiati wao, wala samahani, mimi na wewe tunaishi katika dunia na kucheza na kifo. Hatuna tofauti yoyote na Wazulu hao. Hivyo, sina la kusema…” Joram alimwambia kachero huyo huku akijaribu kumpa mkono ambao ulipuuzwa.

“Hunijui, sikujui. Sawa?”

“Sawa,” alijibu akitabasamu. Kisha, akalichukua gazeti hilo na kuhamia hoteli nyingine ambako nako pia alichukua meza ya kando, isiyo na mtu. Baada ya kupata kinywaji chake alitoa nakala sita za kopi za maandishi yaliyoonekana kama yaliyotoka kwenye faili.

Alizisoma kwa makini. Dakika mbili baadaye alizichanachana huku akiwa tayari amezichora akilini.

‘Kakakuona!’ aliwaza kwa hasira. ‘Anamtaka nini? Ameibuka kutoka wapi? Nani anamtumia? Kwa nini? Kwa nini? Kwa nini?’ alifoka kimoyomoyo.

Maswali yalikuwa mengi na marefu. Majibu yalihitaji muda. Kuwasiliana na wenzake wa nje. Kuwasiliana na benki, kujadiliana na nyumba za wageni, kufuata nyayo zake zinakotokea, kuwalipa maajenti wa nje, wenye kompyuta ambazo zinaweka kumbukumbu za vitendo vya watu kama hao n.k. Yote hayo yalihitaji muda, kitu ambacho Joram hakuona kama kilikuwepo. Kilichohitajika ni kumuua Kakakuona kwanza, na kuuliza maswali baadaye.

Baada ya kuwaza hayo, alifanya haraka kwenda Air Tanzania ambako walimvunja moyo kwa kutokuwa na ndege ambayo ingeondoka muda huo isipokuwa “Saa kumi na mbili za jioni.”

Shingo upande, akageuza njia na kuifuata Sea Express.

Boti ambayo ingeondoka mapema zaidi ilikuwa ni ya saa tisa mchana, saa nne baadaye. Joram alikata tiketi yake. Kisha, akatafuta simu ambapo alipiga moja Zanzibar na ya pili Nairobi. Zote hazikuwa na majibu ya mara moja. Akaahidi kupiga tena usiku huo.

Muda wa kusubiri Joram aliuona mrefu kupita kiasi. Kila dakika iliyopita ilizidi kumtia wasiwasi. Mara kwa mara akilini ilimjia picha ya Nuru akiwa na uso kama ulioteketezwa kinyama kama nyuso alizoziona katika picha alizotumiwa, jambo ambalo lilizidi kumtia hasira na kumfanya atamani kuruka, apae hadi Zanzibar, mbele ya Kakakuona.

“Ndege yake inatua mzee.”

Kombora aliarifiwa katika simu, kutoka Uwanja wa Ndege Zanzibar.

“Vizuri,” alijibu.

“Anashuka. Abiria ni mmoja tu. Amebeba mkoba. Mavazi yake ni kama uliyoyaeleza. Haonekani kama mtu mwenye wasiwasi wowote. Sasa hivi amefika meza ya Uhamiaji. Tumkamate?”

“Nimesema msimsogelee hadi nitakapotoa amri nyingine. Ni mtu hatari kuliko mnavyoweza kufikiria nyie,” Kombora alifoka. Kisha akaongeza “Endelea kuniarifu kila tukio na wekeni makachero wengi waangalie kila hatua yake. Angalieni asifahamu kuwa anafuatwa. Sawa?”

“Sawa”

Baada ya muda, “Amekodi teksi. Anaelekea mjini. Magari yetu mawili ya teksi yanamfuata kwa uangalifu.” Na baadaye “Inaelekea kama anafahamu kuwa anafuatwa. Lakini yaelekea hajali.”

Dakika kumi baadaye Kombora aliarifiwa ghafla, “Ameshuka mzee! Amechoropoka ghafla sehemu za Darajani. Haonekani alipo. Yaelekea amejichanganya katikati ya watu na kuingia mitaa ya Mji Mkongwe. Tufanyeje?”

“Asipotee.” Kombora alinguruma “Makachero wote wafanye kazi ya kumtafuta ili awe chini ya miwani yenu kila dakika. Nataka kujua anafanya nini, anakutana na nani, na kadhalika, na bado naonya asisogelewe wala kushtuliwa. Sawa?”

“Sawa, Afande.”

“HUWEZI kulala na mwanamke aliyefungwa kamba mikononi na miguuni, ukafaidi, huwezi ukatamba mbele ya marafiki zako kuwa mwanamke yule nimefanya naye mapenzi, wakati alikuwa kafungwa mikono na miguu, ambapo hakukukumbatia, hakukubusu wala hakukufurahia. Ni aibu. Ni kitendo cha kihanithi.”

Nuru aliyasema hayo kwa sauti aliyoifanya dhaifu kuliko ilivyokuwa, macho yake yakimtazama Chongo kwa ulegevu huku akiruhusu tabasamu dogo kuutembelea uso huo.

Ilimgharimu kila kitu kuyatamka maneno hayo. Tangu kiumbe huyo alipoonyesha dalili za kumtaka mapenzi roho ilipasuka na akili kufadhaika. Alijisikia kulia, alijisika kucheka na alijisikia kutapika. Yote hayo hakuyafanya. Badala yake alijikaza kisabuni na kuyatamka hayo kwa nia ya kumlaghai Chongo.

Chongo hakuwa mpumbavu kwa namna ambavyo Nuru alimkadiria. Kama jibu kwa maelezo ya Nuru alikitoa kitu kile ambacho alikusudia kuwa tabasamu usoni mwake. Kisha, alimwambia, “Una hila kama kinyonga, mpenzi. Ningeweza kukukomoa zaidi kwa kunifikiria bwege kiasi hicho. Bahati mbaya muda wa kuketi chumbani humu ni mrefu mno. Siwezi kuvumilia kukuachia. Ila tu nakuomba wakati nikifanya vitu vyangu usiote kabisa kunivamia. Nitakufungua miguu. Na nitakuwa na bastola mkono mmoja.”

“Na mikono?”

“Siwezi kukufungua.”

“Nitakukumbatia vipi? Au unaniogopa? Mwanamke mmoja tu katika chumba kilichofungwa, huku una bastola mkononi! Nilidhani wewe ni mwanaume..!”

Sauti hiyo yenye dhihaka ilimwingia Chongo. Akiwa mtu ambaye hana asili ya kukubali kudharauliwa, alimwambia Nuru, “Vizuri. Nitakufungua mikono na miguu. Lakini nakuonya. Kama nia yako ni kujaribu ushangingi, kwangu sina lawama. Nitakuharibu bila kujalI kuwa nitakuuza kwa mamilioni. Upo?”

Kitu kimoja Chongo hakuelewa. Hakuelewa kuwa Nuru alikuwa ameamua kitambo kuwa alikuwa tayari kuacha maiti yake ilale na Chongo, siyo yeye! Hivyo, alitulia pindi Chongo alipokuwa akizikata kamba za miguuni na mikononi. Akatulia pia wakati nguo zake zikipambuliwa moja baada ya nyingine na kuwekwa kando ya kitanda.

Na alizidi kutulia alipolazwa chali juu ya kitanda hicho, miguu yake ikipelekwa mmoja huku mwingine kule. Kisha, bila ya kuitua bastola iliyokuwa imara mkononi mwake, Chongo akaanza kufungua vifungo vya suruali yake.

Ni kitendo hicho ambacho Nuru alikuwa akikisubiri. Aliifyatua miguu yake kama mshale, akailenga shingo ya Chongo!

Lilikuwa pigo zuri. Lakini Nuru naye alikuwa gizani. Hakuwa na habari kuwa Chongo alikitarajia kitendo hicho. Hivyo, teke hilo zuri lilipepea angani na kuikosakosa shingo hiyo iliyokusudiwa kwa nusu inchi. Wakati huohuo, Chongo aliachia ngumi nzito ambayo pia ilimkuta Nuru ameviringika kutoka kitandani na kusimama, akiwa tayari kwa lolote.

Tayari kufa.

Tayari kuua.

Ilikuwa dhahiri kuwa Chongo hakupenda kutumia bastola. Aliididimiza mfukoni na kumsogelea Nuru huku akiyumba kwa mbinu. Nuru alimsubiri. Ngumi mbili za Chongo zilimkosa Nuru, kitendo ambacho kilikuwa kosa kubwa katika maisha yake, kwani wakati huohuo vipigo vya Nuru vilimnyeshea kama mvua kiasi cha kumfanya aanguke kitandani. Nuru alipojaribu kumfuata kitandani hapo alisita baada ya kuona Chongo akiichomoa bastola yake na kumwelekezea huku akinguruma “Naua!”

Mauaji yalikuwa wazi katika macho yake. Huku uso wake ukitetemeka kwa hasira na maumivu, aliilenga vizuri bastola yake. Kwa sauti nzito akasema, “Malaya mkubwa nimejaribu kukuhurumia hadi dakika hii bado unanionyesha ushangingi. Sasa sina budi kukuondoa duniani.”

Kwa mara ya kwanza maishani Nuru alijikuta hana la kufanya. Kana kwamba mwili mzima umeshikwa na ganzi alijikuta katulia kimya akiisubiri risasi!

Baada ya kuuacha uwanja wa ndege huku akiwa na hakika kuwa anafuatwa, Kakakuona alimwamuru dereva wa gari alilokodi kumshusha katika kundi la watu eneo la Darajani. Alipiga chenga mbili tatu za mwili na kuingia sokoni. Kutoka hapo akapenya hadi mbele ya duka mashuhuri la vitabu, ambako alijinunulia gazeti la Heko na kisha kuingia katika mgahawa mdogo ulioelekeana na duka hilo.

Akiwa katika mji huo mkongwe wenye vichochoro vingi, alikuwa na hakika kuwa amewapiga chenga ya mwili makachero waliokuwa wanamwandama. Hata hivyo, alijua hiyo ni chenga ya muda mfupi tu. Mji wa Zanzibar ulivyo mdogo, na mkongwe kiasi kwamba karibu raia wote wanafahamiana alijua baada ya saa chache atakuwa tena machoni mwao, akichunguzwa kwa kila kitendo chake. Hivyo alitaka atumie muda huo mfupi wa Uhuru kukamilisha suala la kumuua Chongo na kumtia Nuru mikononi mwake. Mengine yangefuata baadaye.

Hofu ya kukamatwa kabla ya kutimiza azma yake haikuwa na nguvu akilini mwake. Alikuwa na hakika kuwa japo polisi walikuwa wanamshuku bado hawakuwa na ushahidi wowote wa haja ambao ungemfanya asimamishwe kizimbani kwa kosa la mauaji. Na ni hilo peke yake lililowafanya wasite kumvamia wakati walipopata mwanya.

Kwa utulivu alifikiria wapi ambapo mtu kama Chongo angeweza kujichimbia. Suala la kwamba angeweza kwenda hotelini alilitupia mbali. Akiwa na “mateka” ambaye ni msichana mzuri na maarufu kama Nuru kwenda hoteli yoyote ingekuwa sawa na kwenda Central Police. Lazima atakuwa amejificha katika majumba ya majambazi wengine, ambao ni haba sana Zanzibar. Kakakuona akiwa mtu ambaye alikuwa nje ya nchi kwa muda mrefu, hakumjua jambazi hata mmoja.

Baada ya kuwaza sana alimkumbuka Alhaji Banduka. Akakumbuka kuwa aliwahi kusikia maongezi juu ya mzee huyo ambaye aliamua kubadili maisha yake kabisa na kuondokea kuwa mmoja kati ya matajiri wakubwa mjini hapo. Aliyeogelea hafi maji. Aliwaza. Banduka atamsaidia walao kwa kumwelekeza wapi aanzie kumtafuta Chongo. Alikuwa hafahamu Banduka anakaa upande gani wa kisiwa hicho.

Lakini hilo halikumsumbua. Alikuwa na hakika kuwa kama angeuliza mtu yeyote angeweza kumsaidia.

Akiwa na wazo hilo kichwani, aliuacha mgahawa huo na kujichomeka ndani zaidi ya Mji Mkongwe. Ikamshangaza zaidi kuona hoteli za kitalii zilizokuwa zikifunguliwa katika majumba hayo makuukuu. Alichagua hoteli moja ndogondogo ambamo alijipatia chumba na kulipia. Alichofanya chumbani humo ilikuwa kuyabadili mavazi yake ili aweze kuwachanganya polisi walau kidogo.

Macho yake akayafunika kwa miwani myeusi na kuweka kofia kichwani. Kisha, akazikagua silaha zake. Akatoa bastola yake ndogo na kuifutika katika mfuko wa suruali. Dakika kumi baadaye alikuwa tena mitaani, briefcase mkononi, akiuliza iliko nyumba ya Banduka.

Baada ya kuwauliza watu wawili watatu, mtoto mdogo aliamua kumpeleka. Walipenya vitongoji hivyo vya kihistoria hadi walipotokea mbele ya hoteli ya kitalii iitwayo Africa House. Kutoka hapo mtoto huyo alimwelekeza uchochoro unaoteremka ufukoni ambao ungemfikisha mbele ya nyumba aliyoihitaji, ambayo aliiona meta mia tatu toka hapo walipokuwa. Kakakuona alimshukuru kijana huyo na kuondoka.

Akiwa mbele ya nyumba hiyo alisikia sauti za minong'ono. Lakini mara tu alipogonga mlango alishangaa kusikia akijibiwa kwa ukimya wa ghafla. Akagonga tena. Kimya. Alipogonga kwa mara ya tatu alisikia sauti ya kiume ikiitika toka katika chumba kimojawapo, "Nani?"

"Mimi."

"Wewe nani?"

Kakakuona alipochelewa kujibu alisikia hatua za mtu zikiujia mlango. Ukafunguliwa kidogo na uso wa mwanamume wa makamo kuchungulia nje.

"Nikusaidie nini?" aliulizwa.

Kakakuona hakuwahi kuhusiana sana na Banduka enzi za ujambazi. Hivyo, alikuwa hamfahamu, japo aliwahi kumwona mara mbili, tatu katika vikao vya matumizi na kuonyeshwa kwa mbali kuwa "Yule ni wetu kabisa."

Sura hiyo haikumkaa sana akilini. Lakini hakuhitaji kutambulishwa kufahamu huyu hapa mwenyeji wake. Hata hivyo, alisita baada ya kumwona mwenyeji huyu akiwa katika hali ambayo hakuitarajia. Macho yake yalijaa wasiwasi, uso wake uliloa jasho, sauti yake ilikuwa ya mashakamashaka na kwa mbali alikuwa akitetemeka. Macho makali ya Kakakuona yaliona kitu kingine zaidi katika mkono wa Banduka, damu.

Damu mbichi! Ikilowesha kiwiko cha mkono huo na kusahaulika katika juhudi za kufutwa.

"Unataka nini?" Banduka aliuliza tena akitaka kufunga mlango.

"Nina shughuli ndani."

"Naomba unikaribishe ndani. Mimi mgeni wako," alisema akiuzuia mlango huo kwa mguu

"Mimi sikufahamu"

"Mimi nakufahamu. Kwani wewe si Banduka?"

Banduka alionekana kaduwaa. "Pamoja na hayo" akamwambia,

"Sina nafasi ya kupokea mgeni yeyote leo. Labda uje jioni naweza kukusikiliza."

Kakakuona aliusukuma mlango huo na kuingia ndani. Kitendo ambacho kilimfanya Banduka apepesuke na kutaka kuanguka. Wakati anajiweka vizuri Kakakuona alikuwa akiufunga mlango kwa utulivu kabisa nyuma yake. "Kuna nini humu ndani?" alimuuliza Banduka ambaye alitokwa na macho ya hasira na mshangao.

Kakakuona aliyatupa macho yake huko na huko ukumbini hapo na kuona dalili nyingi za mshughuliko usio wa kawaida. Kochi moja lilikuwa limevutwa upande, kiatu kimoja cha kiume kilikuwa juu ya kochi hilo na glasi iliyovunjika ilikuwa haijazolewa toka juu ya meza ilipovunjikia. Akapiga hatua mbili tatu kukiendea chumba ambacho aliona macho ya mwenyeji wake yakielekezwa mara kwa mara. Banduka alimfuata na kujaribu kumzuia, lakini alisukumwa kando na kupepesuka kama kishada, jambo ambalo lilimfanya apandwe na hasira na kuingiza mkono wake katika mfuko wa suruali ambamo aliificha bastola yake yenye kiwambo cha kupotezea sauti ili amwadhibu mgeni huyu "mkaidi". Lakini hakujua

kiasi gani ameondokea kuwa mzito. Hata kabla mkono huo haujatoka mfukoni alijikuta tayari yumo ndani ya kabali ngumu ya Kakakuona huku mkono huo ukinyongwa hadi bastola ilipopokonywa. Aligugumia kwa maumivu na kutapatapa, nusura pumzi imwishie kama asingeachiwa na kuanguka chini kama mzigo.

"Tatizo lako wewe huelewi kama u steki tupu," alimsikia mgeni huyo akimwambia. "Huna uwezalo kufanya. Unaiona bastola yangu hii? Dude la uhakika. Sio hili toi lako unalochezea. Kwa hii naweza kufumua bichwa lako kwa urahisi kama kuvunja yai. Upo?"

Banduka, kinywa wazi, akitetemeka, hakuwa na la kujibu zaidi ya kutokwa na jicho la hofu; macho kayakodoa kuitazama bastola hiyo ambayo ilimlenga paji la uso.

"Nadhani unanielewa," Kakakuona alimwambia. "Sasa niambie kuna nini nyumba hii."

Alipochelewa kujibu Kakakuona alimwinua na kumshurutisha kutangulia katika chumba hicho alichokuwa akikiendea.

Banduka alifungua mlango na kusita mlangoni. Macho ya Kakakuona yalimpita hadi chumbani humo. Kinyume na matarajio yake alikiona chumba kikiwa kitupu ingawa kulikuwa na dalili zote za vurumai. Alimtazama Banduka kwa namna ya kudai maelezo. Macho yake yalimsaliti tena. Yalikuwa yakilitazama kabati kubwa la ukutani kiwiziwizi kwa namna ya wasiwasi. Kakakuona aliliendea kabati hilo na kulifungua.

Kama asingekuwa mzoefu wa masuala hayo angeweza kushtuka sana kwa kukabiliana ghafla na maiti ambayo ilisimama ndani ya kabati hilo, damu ikiendelea kumvuja toka katika jeraha la risasi ya kifo. Jicho pekee la marehemu huyo lilikuwa wazi, kama linalomtazama Kakakuona kwa namna ya kuomba radhi.

Kakakuona alimgeukia Banduka na kumwona jinsi alivyokuwa akitetemeka mwili mzima kama mgonjwa wa homa. Kwa kumtoa wasiwasi Kakakuona alimwambia, "Kama ni wewe uliyemuua mtu huyu umekuwa rafiki yangu. Kwa kweli nilikuja hapa kwa kazi moja tu ya kumtia risasi ya kifua. Umenitangulia."

Kiasi Banduka alipata ahueni.

"Ni wewe uliyemuua?" Kakakuona aliuliza ghafla.

Huku akikerwa na mgeni huyo alivyotamka neno "kuua" kwa urahisi kama "kula" au "kunywa Banduka alitikisa kichwa kukubali.

"Alifuatana na mwanamke?"

"Ndiyo…"

"Mwanamke huyo ni mpenzi wangu. Mshenzi huyu alifanya kumtorosha tu. Ningemuua kwa tabu kuliko ulivyomuua wewe."

Alisita kidogo akiitazama maiti ya Chongo ndani ya kabati hilo na kumrudia Banduka. "Ebu nieleze kila kitu. Toka mwanzo hadi mwisho," aliamuru. "Nadhani ukiketi tutazungumza kwa urahisi zaidi."

Banduka alijibweteka juu ya kochi. Kwa suti hafifu, alimweleza jinsi alivyoingiliwa na marehemu huyo alfajiri hiyo akiwa amefuatana na "mateka" ambaye ni mwanamke mzuri. Ili kuifanya habari yake ikubalike zaidi Banduka alilaghai kwa kueleza kuwa marehemu alitishia maisha yake kwa kumwelekezea bastola na kudai pesa.

"Kama si mwanamke huyo kupiga teke bastola hiyo na mie kuidaka sasa hivi tungekuwa marehemu badala yake. Sikukusudia kumuua." Banduka aliongeza. "Ilikuwa katika kumtishia kwani alikuwa akiendelea kunifuata, ndipo nilipolenga na kusikia ikifyatuka."

“Usijali. Alistahili kufa,” Kakakuona alisema na kuuliza, “Yu wapi Nuru?”

“Nuru! Nuru yupi?”Banduka alishangaa.

“Yule msichana… mpenzi wangu. Yuko wapi sasa hivi?”

Banduka alielekeza mkono wake mlango wa bafu na kusema, “Anaoga, ili kuondoa uchovu. Yaelekea amepata shida nyingi sana…” Kisha, alisita na kujiuliza huyu mgeni ni nani na ana uhusianao gani na mkasa huu wa ajabu ambao hakujua umemfikisha wapi na kuishia wapi?” alimuuliza.

“Wewe ni nani?”

Kakakuona alitabasamu na kumwambia, “Usijali kunifahamu.” Na kisha, aliongeza “Nadhani ameoga kwa muda mrefu. Mgongee mwambie mpenzi wake anamsubiri hapa nje. Una hakika hana silaha?”

Banduka aliduwaa, “Silaha…mpenzi wako…”

“Usijali. Mgongee.”

‘Una hakika hana silaha?’ Hilo lilitosha kabisa kumdhihirisha Nuru kuwa kifo cha Chongo kwake kilikuwa sawa na kuruka jivu na kukanyaga moto. Hakuwa na shaka tena kuwa kijana huyu mtanashati, ambaye amekuwa akimsikiliza na kumchungulia katika tundu la ufunguo, hakuwa rafiki bali adui yake mkubwa; adui ambaye bila ya shaka yoyote ndiye aliyekuwa akimtumia Chongo na marehemu wenzake wote.

Hofu, ambayo ilimtinga saa mbili zilizopita alipokata tamaa kabisa ya kuendelea kuishi mara Chongo alipomlenga bastola tayari kabisa kuifyatua, ambayo ilianza kumtoka, ilimrudia tena. Akiwa hana la kufanya Nuru alikuwa akiisubiri risasi hiyo wakati jambo ambalo hakulitarajia lilipotokea.

Picha iliyokuwa katika ukuta mmoja wa chumba hicho iliteleza ghafla na kuanguka. Papohapo bastola ambayo ilikuwa na kiwambo cha kupotezea sauti ilichungulia na kufyatuka. Risasi mbili zilimpata Chongo kifuani na kumfanya aanguke chini ambapo alitapatapa kwa muda kabla ya kukata roho.

Nuru alipotazama ilipotokea risasi hiyo aliuona uso wa Banduka ukichungulia na sauti yake kumfikia ikisema, “Usiogope, nakuja.” Baada ya muda alisikia funguo zikichomekwa katika kitasa cha mlango. Harakaharaka, Nuru aliinama na kuiokota bastola ya Chongo akaifutika katika vazi lake la ndani. Banduka alipofungua mlango na kuingia chumbani humo huku akitetemeka alimkuta Nuru kaketi juu ya kochi akimtazama marehemu.

“Nimeua. Sikutegemea kuua…” aliropoka. Kisha, kana kwamba ndio kwanza anamwona Nuru alifoka, “Msichana, huu nani wewe?? Nilikuwa nikichungulia unavopigana. Sijaona mtu akipigana kama wewe.”

“Ni hadithi ndefu, isiyo na kichwa wala miguu,” Nuru alimwambia “Nadhani kwa wakati huu ningekushauri tuwapigie simu polisi ili waje wamwondoe huyo,” alisema akielekeza mguu wake kwa marehemu.

Polisi? La! La! La! Siwezi kuwashirikisha.”

“Lakini umeua katika kujihami. Amekuvamia na angeweza kuniua mimi na wewe pia… Mimi nitakuwa shahidi,” Nuru alijaribu kumwelimisha.

“Na wakati huo nitakuwa mahabusu wanangu wakifa njaa na biashara zangu kuharibika. Polisi hapana” Alisita kidogo akiwaza. Kisha akaongeza. “Labda nikuombe unisaidie tuufiche huu mzigo ndani ya kabati, wakati nafikiria la kufanya. Baada ya hapo unaweza kwenda zako.”

Waliifanya kazi hiyo kwa tabu kuliko Nuru alivyotarajia. Kuua ni jambo moja, kubeba maiti ni jambo lingine. Kwa Nuru ilikuwa kazi ya kutisha na ilimtia kichefuchefu. Alijikaza kisabuni na kustarehe pale tu ambapo maiti hiyo ilifungiwa kikamilifu ndani ya kabati hilo.

Baada ya kazi hiyo ndiyo kwanza Nuru alijitazama na kuona alivyokuwa mchakavu. Nguo hizo chafu pia zilikuwa zimetatuka ovyo hapa na pale. Kwa jumla, nguo zilimfanya awe nusu uchi. Alimtazama Banduka kwa aibu na kumwomba msaada wa kuazimwa nguo za mkewe ili aondoke akiwa katika hali nzuri kiasi.

Bila kusita Banduka alimletea gauni moja zuri, jozi ya viatu na khanga mbili. Nuru alimshukuru na kuingia bafuni ambako alivua na kuufariji mwili wake kwa maji baridi.

Ni wakati alipomaliza kuvaa aliposikia hodi na hatimaye, kuchunguliwa na mtu huyo ambaye alikuwa akizungumza kwa kujiamini; mtu ambaye alionekana hatari zaidi.

Afanye nini? Alijiuliza. Apige kelele? Hilo alilipuuza mara moja. Yeye si msichana wa kufanya hilo. Zaidi, udadisi ulikuwa umeipiku hofu katika moyo wake. Alijisikia hamu ya kufahamu ni kina nani wanaofanya mambo haya yasiyoeleweka na kiini chake. Kujificha bafuni kusingemsaidia. Aliipapasa tena bastola yake na kuhakikisha kuwa imefichika vilivyo. Kisha, alijitazama katika kioo na kurekebisha nywele zake. Baada ya hapo alifungua mlango wa bafu na kutoka taratibu.

Picha za Nuru ambazo Kakakuona alikuwa nazo zilimdhihirishia kuwa binti huyo ni “kipande kizuri cha kazi ya sanaa ambayo mungu aliifanya kikamilifu.” Hayo aliwahi kuyasema kimoyomoyo. Hata hivyo, hakujua kuwa msichana huyu alikuwa mzuri kiasi hiki. Alimwangalia kwa mshangao tangu alipoufungua mlango na kutoka taratibu kana kwamba anafanya majaribio ya kupigwa picha za sinema. Alimtumbulia macho pia wakati alipowasogelea na kuwasalimu kwa sauti dhaifu, ambayo Kakakuona aliiona tamu. Kisha, alijikusanya na kuukumbuka wajibu wake.

“Pole sana, darling,” alimwambia.

Nuru alimtumbulia macho yake mazuri, huku akiliweka vizuri gauni lake la kuazima, ambalo alihisi linampwaya japo lilimkaa kana kwamba mshonaji alimfikiria yeye.

“Pole kwa misukosuko yote iliyokukumba. Maadamu nimefika hakuna lingine litakalotokea,” aliendelea.

Nuru hakumjibu. Hakuwa na la kumjibu, jambo ambalo lilimfanya Kakakuona ahisi kuwa anamwogopa Banduka. Hivyo, alimwomba akatayarishe chakula ili azungumze faragha na mpenzi wake.

Walipobaki peke yao, Nuru alimuuliza, “Wewe ni mmoja wao?”

“Ndiyo na hapana.”

“Una maana gani?”

“Nina maana hiyohiyo. Ndiyo, mimi ni mmojawao na hapana; mimi si mmojawao.”

Alipoona Nuru hajamwelewa aliongeza baada ya kutoa tabasamu pana, “Maana yangu ni kwamba, mimi ndiye niliyewatuma wakulete. Amri ya kufa au kuishi kwako iko mikononi mwangu. Niliwalipa vizuri sana ili wafanye kazi ndogo sana ya kukuchukua na kukuleta kwangu. Kwa bahati mbaya wamekuwa kundi kubwa la wapumbavu watupu. Wote sasa ni marehemu. Mmoja anaoza humo ndani ya kabati. Sio?”

Nuru hakumjibu.

“Wamekufa wote. Wanaume wanne. Wewe huko hai. Umetulia huna wasiwasi wowote. Ndio kwanza unatoka zako kuoga. Sivyo?”

Nuru alipochelewa kujibu Kakakuona aliongeza, “Sijui una kitu gani. Sielewi umetumia hila gani kuwaangamiza watu wote wale. Ila ninachokuarifu ni kitu kimoja. Naitwa Kakakuona. Mimi na kifo hatutofautiani sana. Nikisema kufa, lazima utakufa. Upo?”

Nuru aliamua kutomjibu.

“Napenda uelewe hivyo. Wala usidhani kuwa najipendekeza kwako. Ngoja nikuonyeshe.”

Aliinama na kuichukua briefcase yake. Akaifungua na kuipekua hadi mkono ulipotoka ukiwa umeshikilia picha ya yule msichana aliyeharibiwa uso.

“Unaona?” alisema akimkabidhi Nuru. “Unaona? Hiyo ni kazi yangu.”

Ilikuwa haitazamika mara mbili. Nuru alimrudishia upesiupesi huku akijisikia kutapika.

“Hiyo ni kazi yangu,” Kakakuona alirudia akicheka. “Nafurahi kuwa umeipenda picha hiyo. Unaonaje hapo utakapojikuta na sura kama hiyo? Utafika mbele ya yule hawara yako, Joram Kiango? Si atakufa kwa uchungu?”

Kutajwa kwa jina la Joram kuliisisimua damu ya Nuru. Alijikuta akirudiwa na maswali ambayo yamekuwa yakimsumbua sana juu ya usalama wake. Alitamani amuulize mtu huyo kama wamemkamata au la. Kwa jumla, alikuwa na maswali mengi ya kumuuliza. Lakini aliamua kutumia silaha ya ukimya na utulivu ili kupambana na mtu huyo ambaye alikuwa akijaribu kupandikiza hofu katika moyo wake, mchezo ambao Nuru hakuwa mgeni nao.

“Nasikia Joram ni shujaa na ana roho ngumu. Nasikia hakutokwa hata na chozi moja baba yake alipofariki. Hivyo, bila shaka hatashtushwa na kifo chako. Lakini atakapokuona uko hai, ukiwa na sura kama hii, hatalia kweli?”

Kana kwamba anajijibu mwenyewe aliongeza harakaharaka, “ Lakini haitatokea, labda kama utakuwa mbishi. Jitahidi akija mwenyeji wetu tuwe kama mtu na mpenzi wake. Baada ya kula tutaondoka zetu kwenda Dar es Salaam, mkono kwa mkono hadikwenye chombo. Tutakaa mkono kwa mkono hadi tuendako. Ukijitia kujua umeumia. Iwe mbele ya watu, iwe mimi na wewe, upo?”

Penye wengi hapakosi mengi. Katika mkusanyiko wa wasafiri waliokuwa wakiisubiri Sea Express bandarini Dar es Salaam, ili iwapeleke Zanzibar kulikuwa na pilikapilika nyingi ambazo hazikuwa na msingi wowote. Kwa mfano, pamoja na ukweli kwamba kila msafiri alikuwa na tiketi yake mkononi, yenye namba ya kiti chake, bado kuna wale waliojifanya kuwa wana haraka zaidi ya wengine. Hawa walikuwa wakikimbia huku na huko, mizigo mikononi, na kisha hukaa katika ukingo wa kivuko tayari kuivamia meli hiyo ambayo ndio kwanza ilikuwa inatia nanga.

Milango ilipofunguliwa na abiria watokao Zanzibar kuanza kushuka taratibu abiria hawa “wenye haraka” walikuwa kikwazo kwa jinsi walivyosababisha msongamano mkubwa mlangoni hapo. Watumishi wa Bandari walifanya kazi ya ziada kuwadhibiti abiria hao ili wenzao washuke kwa utaratibu.

Kati ya abiria hao wenye haraka alikuwamo Joram Kiango. Pengine yeye alikuwa na haraka zaidi ya watu wote katika msafara huo. Lakini, kama kawaida yake haraka au shauku yake ya safari hiyo ilikuwa siri yake binafsi. Usoni alionekana mtulivu, ambaye isingekuwa rahisi kufahamu kama anasafiri, amekuja kupokea mgeni, au anasindikiza.

Aliketi juu ya kiti cha mbao, ambacho wasafiri wengi walikiacha na kusimama wima na mizigo yao. Akiwa katika mavazi yake yaliyomfanya awe mtu asiyetazamika sana, yaani kanzu ya kawaida, kijikoti juu ya kanzu hiyo, kilemba kichwani na ndevu za bandia huku kijimfuko kidogo kikiwa miguuni pake, hakuna aliyejisumbua naye.

Lakini yeye alikuwa akijisumbua na kila mtu. Macho yake yenye uzoefu yalimpitia karibu kila mtu katika umati huo. Watu wawili katika umati huo walimsumbua. Ingawa walikuwa wageni kwake, lakini macho yao na tazama yao ilimfanya Joram aone kuwa si wasafiri wa kawaida. Neno “kachero” lilikuwa wazi katika tazama yao, zungumza yao na simama yao.

Joram alihisi kuwa hawa pia wako safarini kwenda Zanzibar kumfuatilia Kakakuona, jambo ambalo halikumpendeza kwani alitamani sana ngoma hiyo aicheze peke yake. Hata hivyo, alitulia kimya, akiendelea kutazama kwa makini zaidi, aone nani mwingine yumo katika msafara huo.

Kwa uzoefu wake wa upelelezi hiyo haikuwa kazi kubwa kwake. Alifuatilia tazama ya makachero hao wawili. Kila walipoelekeza macho yao kwa hila, yeye pia aliyaelekeza huko kwa mbinu, akichunguza ishara zote.

Haukupita muda mrefu kabla Joram hajakipata hicho alichokusudia. Macho ya makachero hao yalikosea kulitazama gari moja, aina ya Toyota Land Cruiser, lililokuwa limepaki nje kidogo yabandari, ndani yake mkiwa na watu watatu. Joram Kiango alimtambua mmoja kati yao mara moja. Alikuwa Inspekta Kombora.

'Kombora pia anakwenda Zanzibar!' Joram alijiuliza kwa mshangao. Ndio kwanza akahisi kuwa Kakakuona ni mtu hatari sana. Awali ya hapo alimchukulia kama mtu kichaa tu, ambaye anaua watu wanyonge na kumteka mtu asiye na hatia, kama Nuru, kwa sababu zake anazozijua yeye mwenyewe, ambazo Joram Kiango hakuona kama angepata muda wa kuzifahamu kwani alichokusudia, mara tu baada ya kukutana na kichaa huyo ana kwa ana, ilikuwa kumuua kwanza, kumuuliza maswali baadaye.

Akaamua kumpuuza Kombora na makachero wake wote na kuendelea kuwasubiri abiria waliokuwa wakiendelea kushuka kutoka katika chombo hicho waishe ili awe miongoni mwa watu wa kwanza kuingia.

Kama kawaida ya abiria wa meli, ile haraka yao ya kupanda waanzapo safari, haitofautiani sana na ile ya kushuka wanapofika mwisho wa safari. Hivyo, pilikapilika zilikuwa nyingi. Joram alitulia akiwatazama abiria hao, hali fikra zake zikiwa nje kabisa ya eneo hilo. Hakuwatilia maanani watu mbalimbali waliopita mbele yake, mizigo yao mikononi.

Lakini haukupita muda kabla hajashuka abiria mmoja aliyemfanya agutuke ghafla kama aliyenaswa na waya wa umeme. Kama si mzoefu katika masuala ya upelelezi angeweza kuinuka na kumkimbilia abiria huyo. Angeweza kumkumbatia na kumbusu. Lakini si yeye. Pamoja na kushtuka kwake, pamoja na kutoyaamini macho yake, alitulia kwa utulivu kana kwamba abiria huyo ni miongoni mwa abiria wa kawaida machoni mwake; kana kwamba hamfahamu na wala hajapata kumwona maishani mwake.

Abiria huyo alikuwa msichana mzuri kupita kiasi, mwenye umbo zuri kupindukia, alilolificha katika baibui alilojitanda juu ya mavazi yake. Mkono mmoja wa abiria huyo ulikuwa umeshika briefcase ya kiume hali mkono wa pili umeshikana na ule wa kijana mmoja ambaye alionekana kama mpenzi wake. Mkono wa pili wa kijana huyo wa kiume ulikuwa ndani ya mfuko wake wa koti.

Abiria huyo wa kike hakuwa mwingine zaidi ya Nuru.

Wala Joram hakuhitaji kuambiwa kwamba mtu huyo aliyeandamana naye alikuwa mtu baki zaidi ya Kakakuona.

Kwa mtazamo wa kawaida, mtu yeyote angepata hisia kuwa abiria hao walikuwa wapenzi wawili ambao ndio kwanza wameoana, hivyo, wanatoka zao Zanzibar kusheherekea ndoa yao. Lakini kwa mtazamo wa mtu kama Joram alifahamu fika kuwa uhusiano wa kimapenzi baina ya viumbe hao wawili ulikuwa sawa na ule wa kondoo na mbwa mwitu. Joram aliona wazi kuwa Nuru alikuwa ametekwa nyara na mtu huyo. Aliona wazi vilevile kuwa mkono wa mtu huyo uliofutikwa mfukoni ulikuwa umeshikilia bastola iliyomlenga Nuru kikamilifu na asingesita kuifyatua iwapo lolote lingetokea.

Adui huyo alikuwa akitembea kwa mwendo wa kujiamini kwa kiwango kilichomshangaza Joram. Hakutarajia muuaji mwoga, kiasi cha kuua watoto wa kike wasio na hatia, angeweza kuwa na moyo sugu kiasi hicho.

Macho ya Joram yaligongana na ya Nuru. Mavazi bandia aliyoyavaa hayakuwa kipingamizi cha kumfanya Nuru asimtambue mara moja. Joram alihisi kitu kama faraja ikichepuka ghafla katika macho yake mazuri.

Hata hivyo, akili yake ilikuwa nzuri vilevile kwa kiwango ambacho kilimfanya Joram Kiango azidi kumheshimu. Zaidi ya kumtupia jicho hilo moja la kawaida kama ilivyokuwa kwa watu wengine, Nuru aliendelea na safari yake kama kawaida.

Pamoja na uduni wa mavazi yake, Joram alikuwa kamili kikazi. Isingemchukua sekunde moja kuifikia bastola yake na kuufumua ubongo wa Kakakuona. Hali kadhalika, maungo yake yalikuwa yakichemka kwa hamu ya kumfanyia mazoezi ya judo mpuuzi huyo.

Hata hivyo, kwa kuchelea kuyanadi maisha ya Nuru, hasa baada ya kukumbwa na misukosuko yote ile isiyokadirika, Joram aliamua kuacha mchezo huo uendelee kidogo.

Jambo lingine lililomfanya Joram aahirishe kumchukulia hatua muuaji huyo ni ile heshima au hadhi mpya ambayo alijikuta akimpatia muuaji huyo kutokana na kitendo chake hicho cha aina yake. Halikuwa jambo la kawaida muuaji ambaye anafahamu fika kuwa anawindwa zaidi ya kifaru mwenye kichaa, kujitokeza hadharani, mchana kweupe, akiwa na mateka ambaye ni mwanamke hatari zaidi ya nyoka aina ya swila. Hivyo, Joram alijikuta akiamua kujionea kitu kinachomtia ujeuri huo.

Kisha, akamkumbuka Kombora na makachero wake. Ndio kwanza akafahamu kuwa hawakuwa safarini, bali walikuja kwa ajili ya kumlaki mwuaji huyo kwa matumaini ya kumkamata.

Akageuka kuwatazama makachero hao. 'Polisi ni polisi, avae magwanda asivae,' Joram aliwaza alipoona hali ya makachero hao. Japo walijitahidi kujikaza, kana kwamba hakuna kinachoendelea, lakini hakushindwa kusoma ramani ya misukosuko katika nyuso zao.

Kila mara mikono yao ilichopoka na kupelekwa mifukoni, kuzipapasa bastola zao; miguu yao ikichezacheza kwa namna ya ukosefu wa utulivu mioyoni mwao. Mara kwa mara waliyatupa macho yao katika gari alilokuwemo Kombora kwa namna ya watu wanaosubiri amri ili wafanye jambo, amri ambayo Joram hakuona kama Kombora alikuwa tayari kuitoa kwa jinsi alivyopigwa butwaa ingawa alijifanya mtulivu; akivuta sigara yake, gazeti mkono wa pili.

Wakati huo Kakakuona na Nuru walikuwa wakimaliza ngazi na kuanza kutoka nje ya banda. Kakakuona aligeuka kumtazama mmoja kati ya makachero wa Kombora kwa namna ya kumwambia, "Nimekutambua."

Joram alihisi kuona tabasamu la kebehi katika macho hayo.

Kama kuna siku ambayo Inspekta Kombora aliwahi kuhisi akili yake imeduwaa, huku fikra zake zikiwa zimedumaa, ni hii. Mwili mzima ulimlegea, mikono ikamtetemeka kwa kitu ambacho asingeweza kukipambanua kati ya hasira na aibu. Sigara ambayo aliiwasha kitambo iliendelea kuteketea mdomoni mwake.

"Mzee… anakwenda zake… Tufanye nini mzee?" mmoja kati ya wasaidizi wake, aliyekuwa kiti cha nyuma cha gari hilo alimuuliza Kombora akigeuka kumtazama, ingawa macho yake yalidhihirisha kuwa alikuwa hamwoni.

Akili yake bado ilikuwa imepaa au kuzama katika lindi refu la mshangao na kutoyaamini macho yake.

3

Zaidi ya saa moja iliyopita alipokea habari toka Zanzibar kuwa Kakakuona ambaye alitoweka ghafla, aliibuka toka katika mitaa ya mji huo akiwa amefuatana na msichana ambaye alionekana kama Nuru. Kombora aliwakumbusha waendelee kumchunguza bila kumshtua. Lakini dakika tano baadaye, alipoambiwa kuwa Kakakuona alikuwa akija Dar es Salaam kwa Sea Express na kwamba Nuru alionekana kama ambaye yuko chini ya ulinzi, aliongoza kikosi cha vijana wake wazuri, sita, ambao walikuwa tayari; wakisubiri amri yake.

Kombora alisita kuitoa amri baada ya kuona kile ambacho hakutarajia kukiona katika macho ya Kakakuona. Kitu kisichoelezeka kwa jinsi kilivyofungwa pamoja katika fungati la ukatili, dharau, unyama na dhihaka ya hali ya juu.

Kombora alishangaa alipoona kuwa Kakakuona alijua fika kuwa amezingirwa na makachero wengi, ambao walikuwa tayari kumuua mara tu wapewapo ishara, lakini bado alipita kwa kujiamini. Dharau yote hiyo ya Kakakuona ilitokana na ukweli kuwa asingekufa kabla hajamuua Nuru, jambo ambalo alifahamu kuwa yeyote duniani asingelifanya kwa urahisi.

Kwa ajili ya unyama wa mtu huyo, kwa jinsi ambavyo alikuwa anaendelea kuteketeza maisha ya watu wasio na hatia, Kombora angekuwa tayari kutoa amri avamiwe na kuuawa bila kujali ambacho kingemtokea msichana huyo.

Ndiyo, angefanya hivyo, iwapo tu msichana huyo asingekuwa Nuru.

Nuru ni mmoja kati ya wasichana wachache wenye nafasi ya pekee katika moyo Kombora. Ingawa hakupata kumwambia hivyo waziwazi, lakini aliheshimu sana mchango wake katika harakati za yule mpenzi wake Joram Kiango.

Kombora asingeweza kusahau jinsi msichana huyo alivyobadilika kutoka katika umbile laini la kike na kuwa jabali la chuma tangu aliposhirikishwa katika ule mpango wa kinyama wa kuwaua viongozi wa nchi huru za Kiafrika mjini Arusha, mkasa ambao tayari umehifadhiwa katika kitabu kinachoitwa Salamu Toka Kuzimu ambao kwa jinsi unavyotisha hata baadhi ya watu wanauchukulia kama riwaya ya kubuni.

Baada ya hapo ndipo Nuru alipoamua kuudhihirisha uanamapinduzi wake katika visa na mikasa kadha wa kadha ambavyo pia vimetolewa vitabu vinavyoitwa Tutarudi na roho zetu? Malaika wa Shetani na vinginevyo.

Kazi ya Nuru katika mikasa hiyo ilikuwa kubwa kiasi kwamba bila ya yeye pengine Joram Kiango asingekuwapo duniani leo hii.

Kombora hakuona kama inayumkinika kutoa amri msichana kama huyo afe kwa ajili ya kumwogopa Kakakuona na unyama wake. Akaendelea kuduwaa.

“Mzee… wanaondoka,” msaidizi wake aliendelea kumkumbushia.

Wakati huo Kakakuona alikuwa akimaliza kuingia katika gari la kukodi, aina ya Datsun, baada ya kumtanguliza Nuru kukaa na dereva mbele, yeye, nyuma. Dereva akiwa haelewi lolote alitia gari moto na kuondoka taratibu.

Wakati gari hilo likiondoka, kijikaratasi cheupe kilidondoka toka dirisha la nyuma. Mmoja kati ya makachero wa Kombora alikiokota. Baada ya kusoma alikileta kwa Kombora huku akiwa na dalili za mshtuko mkubwa. Alimkuta Kombora akiongea katika Redio call kuwaarifu watu wake waliokuwa nje ya eneo hilo walifuate gari hilo kwa hila. Aliwapa namba za gari na rangi yake.

Kisha, aliitupa sigara yake ambayo ilikuwa imekwisha na kujiwashia nyingine.

“Ni nini?” alimuuliza askari huyo huku akipokea kipande cha karatasi.

“Ujumbe.”

“Ujumbe gani?”

Ulikuwa ujumbe mfupi ambao uliandikwa kwa peni ya wino mweusi;

Fanyeni upumbavu wa aina yoyote ile mtashangaa kuiokota maiti ya msichana huyu barabarani ikiwa na sura ya wale waliotangulia. Na sipendi kufuatwafuatwa.

Kakakuona.

Kombora aliisoma kwa mara ya pili. Kisha, akaitumbukiza katika mfuko wa koti, hasira zikichemka kichwani mwake, kutokana na dhihaka hiyo ya Kakakuona. Kombora alijikuta akizungumza peke yake kwa minong'ono, "It's too much. Kama anajua anafuatwa ya nini kuendelea kujificha?"

Kwa sauti alikoroma, "Ok, twendeni."

"Wapi?"

"Mfuateni," aliamuru. "Usijali kama atafahamu kuwa anafuatwa au la," alimwambia dereva. "Anaonekana kama anayetaka tumfuate."

Magari mengine matatu ya polisi, yenye namba za kiraia, ambayo yaliegeshwa katika eneo hilo yalianza kuondoka moja baada ya jingine, kwa maelekezo ya Kombora kupitia Walkie talkie yake magari mawili kati ya hayo yalilipita gari la Kakakuona, ambalo lilikuwa likienda kwa mwendo wa wastani, na kulitangulia. Mbele ya safari gari moja lilichepuka kama vile halina habari na msafara huo, la pili likiendelea taratibu.

Gari la Kakakuona liliifuata Barabara ya Sokoine na lilipoifikia Barabara ya Morogoro likaifuata, jambo ambalo lilifanya gari la makachero wa Kombora lililotangulia lipitilize hadi katika mzunguko wa Mnara wa Saa ambapo lilipinda na kuingia samora hadi walipopishana na Kombora, ambaye aliwaashiria kurudi ofisini kazi yao ilichukuliwa na teksi moja yenye namba za TX ambayo ilionekana kama imechukua abiria watatu.

Kichwa cha Kombora kiliendelea kusumbuliwa na hali ya kucheza na mtu kama Kakakuona. Alijihisi kuwa yeye na askari wake wote wako katika duru wakicheza ngoma wasiyoifahamu, ngoma ambayo mpigaji hakuwa mwingine zaidi ya Kakakuona mwenyewe. Jambo hilo lilizidisha hisia za hatari kichwani mwa Kombora.

Ingekuwa rahisi sana. Kati ya magari yake yaliyotangulia, moja lingeweza kusababisha ajali ya ghafla kwa lile lililomchukua Kakakuona, papohapo, yeye na askari wake kuivamia ili kumuua Kakakuona na kujaribu kumwokoa Nuru. Ni moja kati ya mambo ambayo yamekwishafanywa sana. Hata hivyo, ilikuwa kama kamari ambayo Kombora hakuwa tayari kuicheza. Hivyo, ikabidi aendelee kustahimili, akiruhusu magari yake yaendelee kumsindikiza Kakakuona kama shujaa anayepelekwa Ikulu kuchukua wadhifa wa nchi.

Kwa Joram Kiango ilikuwa kazi rahisi kuliko alivyotarajia. Mara tu alipomwona Inspekta Kombora akishindwa kuchukua hatua dhidi ya Kakakuona, badala yake akianzisha msafara wa kumfuata, yeye pia alifanya hima kuliendea mojawapo ya magari mengi yaliyokuwa yakisubiri abiria nje ya stesheni.

Alichagua gari jipya, aina ya Suzuki, lenye namba za Posta, ambalo ingawa dereva alidai kuwa yuko kazini, lakini Joram hakuchelewa kugundua kuwa alikuwa akisubiri abiria yeyote ambaye angemkodi ili ampatie chochote cha kutia mfukoni.

"Una petroli ya kutosha?" alimuuliza.

"Kwani unakwenda mbali mzee?"

"Itategemea," Joram alijibu akizunguka upande wa pili ambako alifungua mlango na kuingia ndani. "Ifuate ile. Ifuate taratibu wasijue kuwa wanafuatwa."

Dereva huyo alionyesha wasiwasi kidogo. "Gari ile, mzee! Kwa nini tuifuate? Unajua…" alisita kidogo. Lakini alipoona kitita cha shilingi elfu tano kikiwekwa juu ya mapaja yake alionekana kubadilika kidogo.

“Wakienda mbali zaidi nitakuongeza,” Joram alisisitiza, huku akimhimiza kuondoa gari.

“Tatizo ni kwamba ile gari naijua brother,” alisema akiondoka shingo upande. “Ile ni gari ya wenyewe ile. Inatumiwa na manjagu, pamoja na kuwa na namba za kiraia. Naogopa wasije wakaniletea matatizo wakijua kuwa wanafuatwa.”

“Usijali, hawatafahamu.”

Akili ya Kakakuona ikiwa juu ya magari ya Kombora ambayo alikwishayakariri namba zake vizuri sana kichwani, hakujishughulisha na gari dogo la Posta ambalo lilionekana kwa mbali sana miongoni mwa magari mengine.

Aidha, Kombora vilevile fikra na hisia zake zote zikiwa katika gari la mbele yake, ambalo lilimchukua muuaji hatari kama Kakakuona, hangeweza kulitazama gari hilo la Posta lililokuwa nyuma yao. Hali kadhalika, ikiwa tabia ya polisi ni kufuata badala ya kufuatwa, kusaka badala ya kusakwa, wazo la kugeuka nyuma mara kwa mara halikumjia akilini kabisa. Tabia hii ilifanya kazi ya Joram na dereva wake iwe nyepesi kama ilivyokuwa.

Ulikuwa ni msafara usio na kona nyingi wala mizunguko mingi. Ilielekea kama Kakakuona alikuwa hana haja ya barabara nyingine zaidi ya ile ya Morogoro, Hata hivyo, walipofika Mtaa wa Jamhuri, gari hilo lilionekana likipinda kulia kuufuata mtaa huo. Gari la Kombora likafanya hivyohivyo. Joram pia akamwamuru dereva wake kuwafuata.

Njia hiyo ilikuwa na msongamano mkubwa wa magari hivyo, safari yao ilikuwa ya taratibu, jambo ambalo lilimtia hofu Kombora kuwa Kakakuona angeweza kuitumia fursa hiyo kuchepuka ghafla mahala ambapo asingekuwa mwepesi wa kuona alipoelekea.

Lakini Kakakuona hakuonekana kama mwenye haraka ya kufanya hivyo. Aliendelea na safari yake taratibu kama ambaye alikuwa na nia njema sana ya kumwongoza Kombora na msafara wake hadi alipoufikia uchochoro ambao unachepuka na kuunga mtaa huo hadi Mtaa wa Kisutu ambapo alionekana akisogea kulia na kuliingiza gari katika ukumbi wa jengo moja jipya, ambalo liliacha eneo zuri la kupaki magari chini yake kwa meta kama kumi ndani yake.

Kombora alilitazama gari hilo likipaki kwa utulivu. Alitumia dakika mbili tatu za kuduwaa, akijiuliza afanye lipi, kwa makini. Jengo hilo lenye ghorofa nne lilikuwa moja kati ya majengo mapya yaliyokuwa yakiibuka huko na huko jijini Dar es Salaam.

Vibao vya kampuni na biashara mbalimbali vilionekena katika kuta mbalimbali za jengo hili chini ya kibao kilichoandikwa Sunrise Modern Club. Kibao hiki kilimeza karibu robo ya ghorofa zima ya chini. Maandishi yake yalikuwa juu ya kioo kikubwa, kwa rangi mbalimbali ambazo usiku ziliwaka kwa namna ya kuchezacheza katika hali ya kuvutia macho. Kombora aliwahi kupita hapa mara nyingi usiku na kuvutiwa, kama watu wengine, lakini hakuwahi kuingia ndani. Kumwona Kakakuona akipaki hapo aliyakumbuka mauaji ambayo amekuwa akiyafanya katika hoteli na kumbi za starehe kama yale ya Lang’ata; akajikuta akipatwa na hisia za hatari kuliko awali.

“Liwalo na liwe,’ aliwaza. “Tunamfuata hukohuko ndani,” aliamuru, “Angalieni. La msingi ni kuyaokoa maisha ya Nuru. Hivyo, risasi za kwanza, kama itabidi, ziwe za kumvunja mabega, ili asiweze kuitumia mikono yake. Aliye kulia, alenge mkono wa …”

Kombora alilazimika kuyakatisha maongezi yake alipomwona Kakakuona akishuka huku akifuatiwa na Nuru ambaye alikumbatiwa kiuno kama wapenzi wa damu.

Walishuka harakaharaka na kuingia ndani ya jengo hilo.

Kombora, akiwaongoza askari wake wawili, pia alishuka na kumfuata. Alipolifikia gari lililokuwa likitumiwa na Kakakuona nusura atokwe na ukelele wa mshtuko, mshangao na hasira, alipomtazama dereva.

Alikuwa amelalia usukani wake akitapatapa; tundu kubwa la risasi likiwa limekifumua kichwa chake kisogoni, na kuruhusu damu nzito iliyochanganyika na ubongo iendelee kumwagika kama uji mwekundu unaomwagika toka katika birika.

“Haraka… ndani,” Kombora alinguruma akiitoa bastola yake na kutangulia ndani ya jengo hilo. Mlango uliwaongoza katika korido nyembamba iliyowafikisha katika chumba cha mapokezi, ambacho kilikuwa na makochi manne makubwa yaliyokuwa matupu. Makochi hayo yalikielekea chumba cha kioo ambamo hamkuwa na mtu. Kombora alitazama huku na huko kama anayeomba msaada. Aliiona lifti, na upande wa pili aliiona ngazi iendayo juu.

“Mmoja atumie lifti, mwingine apande kwa ngazi. Upesi. Kama nilivyosema, mkimwona msizungumze naye. Acheni risasi zizungumze. Ok?”

Wakati yule aliyeamriwa kwenda kwa miguu alipoanza kupanda ngazi harakaharaka na yule wa lifi akiita kwa kubonyeza tufe, Kombora aliitoa walkie talkie yake na kuwaamuru makachero wengine kuja mara moja. Kisha, akasogea kaunta bila kujua alihitaji nini. Kama awali alijisikia kupiga kelele, safari hii akijisikia kuzimia kwa kile ambacho alikiona chini ya meza hiyo ya kaunta.

Mzoga wa mtu ulikuwa umelala kifudifudi katika dimbwi la damu nyingi ambayo ilikuwa ikiendelea kujaa sakafuni. Dalili yoyote ya uhai haikuwamo katika umbile hilo ambalo sare alizovaa msichana huyo zilionyesha kuwa alikuwa mhudumu wa mapokezi.

Akili ya Kombora ilidumaa kwa kitambo cha robo dakika. Watu wawili, wasio na hatia, kuuawa huku yeye anashuhudia…! Aliwaza kwa uchungu. Alishindwa kuendelea kuwaza. Badala yake alikurupuka mbio kuiendea ngazi ambayo aliipanda kwa kuruka ngazi tatu tatu, bastola ikiwa imemtangulia.

Kwa Nuru ilikuwa kama mtu anayeshuhudia mchezo wa sinema ya kusisimua ambao yeye mwenyewe ndiye mtazamaji, wakati huohuo mwigizaji. Naam, ilikuwa kama ndoto tu; tangu alipojikuta akihama kutoka katika mikono ya yule muuaji Chongo na kuangukia katika milki ya Kakakuona. Kama kondoo, aliafiki kila alichoelekezwa. Aliafiki kuushika mkono wa muuaji huyo huku akitabasamu.

Kadhalika, aliafiki kupita kote huku akijua kabisa kuwa kila hatua anayopiga na muuaji huyo inamsogeza karibu zaidi na mauti yake mwenyewe.

Hata hivyo, ile kiu yake ya kufahamu kwa undani zaidi kiini cha mauaji haya ilikuwa sababu nyingine iliyomfanya aendelee na ukondoo huo. Aidha, ile bastola yake, ambayo aliificha vyema alipokuwa akioga bafuni ilimpa moyo na kumpa matumaini ya kupata fursa nzuri ambayo ingemwezesha kuyaokoa maisha yake mara mambo yatakapovuka kina.

Matumaini hayo yaliongezeka maradufu mara aliposhuka bandarini na kumwona Joram Kiango akimsubiri, bila ya Kakakuona kumtambua. Nuru alizidi kupata moyo.

Ilikuwa mara yake ya kwanza kumtia Joram Kiango machoni. Ile hofu yake kuwa tayari wauaji hawa wamempata ikatokomea. Ingawa hawakuongea wala kupeana ishara yoyote, lakini bado kule kumwona akiwa hai na kuyaona macho yake yaking’ara kama ilivyo kawaida yake kulimwongezea ari na kumpa matumaini makubwa ya ushindi.

Hivyo, hakuwa na hofu kubwa sana pindi walipochukua gari na kuondoka huku domo la bastola ya Kakakuona, iliyofichwa mfukoni, likiendelea kumtekenya ubavuni. Wala hakubabaika Kakakuona alipouandika ule ujumbe wa kejeli kwa Kombora, ambao ulikusudiwa kumwongezea hofu.

Lakini, mara tu baada ya gari kusimama hapa na Kakakuona kufanya kile kitendo ambacho Nuru hakukitarajia, alijikuta akiingiwa na hofu kubwa iliyochanganyika na hasira.

Ndiyo, Nuru ameshuhudia mara nyingi watu wakiuawa. Kamwe hakuwa mgeni kwa hilo. Lakini kuuawa kwa kijana huyu wa Kipemba, asiye na hatia, ambaye aliwaendesha bila hofu wala hisia zozote za hatari, kuliufanya moyo wake ukose baadhi ya mapigo yake, hasa pale alipoona kijana wa watu akianguka ghafla juu ya usukani kama mbuzi.

KAKAKUONA alitenda kitendo hicho kwa wepesi wa ajabu. Sekunde ya kwanza alitulia akiupima mwendo wa gari la Kombora lililokuwa nyuma yao. Sekunde ya pili tayari alikuwa ameua na kuirejesha bastola yake mfukoni, huku akimwamuru Nuru kutoka nje ya gari haraka.

Mshangao, kutotarajia na wepesi huo wa ajabu ulimfanya Nuru aduwae kwa hofu; kama mtazamaji asiye na uwezo wa kufanya lolote. Jambo hilo lilimuumiza sana rohoni. Kama angejua kinachokaribia kutokea angemuua Kakakuona kwanza, yeye binafsi kufa baadaye, badala ya kushuhudia kijana huyo asiye na hatia akiuawa mbele yake, kwa ajili yake.

“Fanya mzaha, kifo kitakachofuata kitakuwa chako,” Kakakuona alimwonya wakati wakiingia ndani ya jengo hilo, akiwa mtulivu.

Tabasamu laini lilitanda usoni mwake kama mtu aliyeua mbu tu. Akiwa na tabasamu hilohilo, huku kashikilia kiuno cha Nuru, alimsogelea msichana wa mapokezi. Nuru alihisi nia yake huku tayari akiwa amechelewa sana kwa nusu sekunde nzima. Wakati huo risasi ilikuwa imekwishapenya katika paji la uso mzuri wa msichana huyo.

Kwa wepesi uleule aliupenyeza mkono wake ndani ya vazi lake la ndani na kuishika bastola yake. Lakini hakuwahi kuitoa. Kitako cha bastola iliyomuua msichana huyo tayari kilikuwa kimepigwa upande mmoja wa kichwa chake na kumfanya arukwe na fahamu na kupepesuka. Aliongezwa kipigo cha pili ambacho kilimmaliza kabisa. Kama ndoto, alihisi akididimia katika shimo lenye kiza na kina kirefu kisicho na mwisho.

Wakati hayo yakimtokea Nuru, kikosi cha makachero wasiopungua kumi, wakiongozwa na Inspekta Kombora walikuwa tayari wamelivamia jengo hilo, wakichungulia kila uchochoro na kuchunguza kila chumba. Wenzi wao, vijana sita machachari, walikuwa nje ya jengo wakichungulia kila kona na kila uchochoro. Wote walikuwa makini, silaha zao mikononi, tayari kwa lolote.

Inspekta Kombora alikuwa makini zaidi ya wote. Akiwa na hasira ambayo iliimeza kabisa hofu ya kifo dhidi ya muuaji huyu, aliwaongoza askari katika kila chumba, akiamuru kupekuliwa kila kabati. Kila jokofu na kila sanduku; kuchungulia kila choo na kufunua kila kitanda na kadhalika.

Bastola yake ikiwa wazi mkononi, mikunjo ya hasira tele usoni, iliwafanya wapangaji wa jengo hilo kushindwa kumwuliza lolote. Badala yake waliduwaa, wakimtazama, kama ambavyo hawakuyaamini macho yao.

Baada ya dakika kumi za kuepuka hapa na pale, Kombora na kikosi chake kizima walijikuta wamerudi tena katika ukumbi wa disko wa Sunrise huku wakitazamana kwa namna ya kukata tamaa; kila mmoja akitokwa na jasho jingi lililotokana na mbio walizozipiga katika jengo hilo.

“Haiwezekani,” Kombora alinong’ona kama anayezungumza peke yake. “Nilimwona kwa macho yangu mwenyewe akiingia katika jengo hili. Na ameua watu wawili, wasio na hatia, mbele ya macho yangu katika jengo hilihili. Haiwezekani kuwa ametoweka.”

“Kwani kuna nini mzee?” aliyeuliza ni mzee wa makamo aliyekuwa nyuma ya kaunta, ambayo alimezwa na kila aina ya pombe ipatikanayo katika sayari hii, katika karne hii. Mzee huyu pamoja na wateja wake watatu, Mhindi na waswahili wawili, ambao alikuwa akiwahudumia, walishikwa na bumbuazi walipoliona kundi la watu wenye silaha, likiuvamia ukumbi huo na kuanza kuchungulia kila mahali huku nyuso zao zikionyesha wazi kuwa walikuwa tayari kwa lolote, tayari kuua, tayari kufa.

“Kuna nini?” mmoja wao aliuliza.

Alijibiwa kwa swali la harakaharaka, “Yuko wapi?”

“Nani?”

Kombora alihisi kama anayezungumza na ukuta. Alimwacha huyo na kujishughulisha kikamilifu katika msako huu wa aina yake, ambao hakumbuki lini amewahi kuufanya tena. Baada ya kukata tamaa ndipo aliporudi chumbani humu na kujumuika na askari wake. Alimtazama mhudumu huyo wa baa na kugundua kuwa alikuwa hajui lolote, wala hakumwona mtu yeyote akiingia au kutoka.

Hivyo alimpuuza na kuwatazama wasaidizi wake, akisubiri mawaidha yao. Alipowaona kimya alizungumza tena kwa sauti dhaifu, “Haiwezekani kuwa ametoweka, lazima yumo humu ndani. Chumba gani ambacho hatujakikagua?”

“Nadhani hakuna chumba tulichokiacha mzee,” mmojawao alimjibu. “Kama yumo katika jengo hili tungekuwa tumempata…” Alisitasita maneno yake aliposhuhudia macho maangavu ya Kombora yakimtazama kwa ukali.

“Yumo humu…” alifoka. “Yuko humuhumu. Lazima apatikane leo hiihii. Ikibidi kila tofali la jengo hili lifunuliwe hadi apatikane. Mnanielewa?”

Kimya kilichofuata, baada ya kauli hiyo nzito ya Kombora, kilifuatiwa na mshindo mkubwa wa ajabu ambao ulisikika ghafla na kumeza anga nzima. Ulikuwa mshindo wa aina yake ambao Kombora hakupata kamwe kuusikia maishani mwake, mshindo ambao ulilifanya jengo hilo zima litikisike kama ambalo lilikaribia kubomoka. Mshindo ambao ulidumu kwa nusu dakika tu, nusu iliyofuata, kila kitu kilikuwa shwari kana kwamba hakuna kilichotokea.

Kombora na vijana wake walitazamana kwa mshangao.

“Ni nini hicho?” mmojawao aliuliza kwa mshangao.

Wenzake wote walimtumbulia macho.

Joram alipoliona gari hilo likipaki katika mtaa huo wa Kisutu, alimshauri dereva wake kupitiliza kana kwamba hana shughuli nao. Alimwelekeza dereva huyo kufuata barabara ya umoja wa wanawake, upande wa pili wa mtaa huo, ambapo alishuka na kumruhusu dereva huyo kuondoka.

Kijana huyo hakuamini, shilingi elfu tano kwa kazi ndogo kiasi hicho! Alionekana kama aliyetaka kumwambia hivyo Joram. Lakini Joram hakuonekana kama yuko tayari kwa maongezi zaidi. Alikwishashuka garini na kuliacha hatua kadhaa huku macho yake yakitazama jengo refu lenye maandishi makubwa: Kangaroo Enterprises Ltd, ambalo alihisi lilielekeana na Sunrise Club ambapo Kakakuoa alishukia.

Nia ya Joram ilikuwa kutafuta upenyo au uwezekano ambao ungemwezesha kuifikia klabu ile kwa njia ya mkato badala ya kufuata njia aliyojia.

Uwezekano ulikuwa mdogo. Jengo hilo lenye ghorofa nne lilikuwa limeungana na majengo mengine kwa ukuta mkubwa wenye chupa zilizobandikwa juu. Magari ya watumishi, wateja wa ofisi hiyo walikuwa nje badala ya ndani ambako Joram angeweza kutumia hila kuingia.

Wakati Joram akiendelea kutafakari afanye nini, hakuyaamini macho yake alipomwona mtu aliyekuwa akitoka nje ya jengo akiwa ameshikilia briefcase mkononi. Ingawa macho yake alikuwa ameyafunika kwa miwani, Joramasingeshindwa kumtambua maramoja. Alikuwa Kakakuona. Alikuwa akitembea kwa mwendo wa harakaharaka kuliendea moja ya magari yaliyopaki hapo ambalo alilifungua na kuingia. Kisha, kama aliyekumbuka jambo,Kakakuona alitoka nje ya gari hilo na kuufunga mlango. Akaanza kurudi ndani harakaharaka kama alivyokuja.

Joram Kiango hakuweza kuamini bahati yake. Ilikuwa kama mungu kamleta kwake moja kwa moja. Alikuwa na nafasi nzuri ya kumtia risasi ya kisogo. Lakini kwakuwa alimhitaji alimfuata, rohoni akijua kuwa wakati wa kukijaribu kile ambacho alikuwa akijikumbushia huko kisiwani umewadia.

Ni wakati huohuo anga lilimezwa na mlio mkubwa wa ghafla ulioitetemesha ardhi. Joram alipepesuka na kujikuta akiliegemea gari la Kakakuona. Alifanya harakaharaka kujiweka sawa ili asimpoteze muuaji huyo.

Hakumwona.

Kakakuona alikuwa ametoweka mbele yake kama muujiza. Pale ambapo alikuwa hatua kumi tu aliposimama Kakakuona, palikuwa patupu bila dalili yoyote ya binadamu wala uhai. Joram alitazama huku na huko na kuambulia macho ya mshangao ya wapiti njia ambao waliduwaa, baadhi wakitetemeka kwa tukio hilo ambalo hawakuweza kulitafsiri.

“Ni kitu gani?” mpita njia mmoja aliuliza, akimtazama mwenzie ambaye kapu alilokuwa amelibeba lilikuwa limedondoka chini.

“Tetemeko la ardhi…”

“Wala!” alidakia, “Tetemeko gani lenye mlio wa kutisha kama huu.”

Walitazamana. Wakatazama huku na huko kisha wakaachana. Kila mmoja alishika njia yake.

“Kuna nini jamani?” Fidels Sembera, mfanyakazi wa Shirika la Maktaba ya Taifa ambayo iko katika barabara hiyo, nyumba kadhaa toka aliposimama Joram, alifoka.

“Nani anayejua?” mtu mmoja alimjibu. “Au ndio mwisho wa dunia?”

Kicheko.

“Nini tena hicho?” Muhidini Michuzi, mwandishi wa habari wa Daily News alimwuliza Wilson Kaigarula ambaye waliketi meza moja wakijadili jambo.

“Mwangwi.”

“Mwangi, toka wapi!”

“Labda mvuayataka kunyesha!”

“Mvua kweupe hivi!. Hata hivyo mvua za Dar es Salaam tangu lini zikaanza kunguruma?”

“Kwahiyo?”

Kisha, “Achana nayo. Tulikuwa tukisema nini vile?”

Mhindi, dereva wa daladala ambaye alikuwa akipinda kona kuiacha Umoja wa wanawake aingie Maktaba, alijikuta akisimamisha gari ghafla na kushuka chini huku akitetemeka. Aliamini kuwa amegongana au kagongwa. Alipoona gari likiwa halina dosari, huku kila mtu kaduwaa akauliza, “Nini hiko nalia?”

Hakupata jibu.

Jibu alikuwa nalo mtu mmoja tu, Joram Kiango. Ni yeye aliyeona na kujua kilichotokea. Kakakuona alikuwa ameuawa! Mlio uliosikika ni silaha ya aina yake, ambayo tangu ilipogundulika iliaminika kuwa ilikuwa imekwisha tumiwa mara mbili tu. Mara ya kwanza ilitumika nchini Urusi, kwa amri ya Stalin. Ilitumiwa kumwondoa duniani mjerumani mmoja ambaye alijipenyeza hadi katika jeshi la Urusi , miaka nenda miaka rudi akiiba siri mbalimbali ambazo alikusudia kuzipeleka kwao. Wakati huohuo Urusi na Ujerumani ikiwa katika vita, Stalin aliamuru bunduki hiyo itumike juu yake ikiwa pia kama sehemu za majaribio kwa silaha hiyo. Matokeo yake yaliwasisimua sana warusi.

Lakini matokeo hayo yaliwavutia pia Wamarekani ambao walifanya jitihada zote hadi baada ya miaka kumi wakawa wameiba mbinu za kuitengeneza. Na walijikuta wakilazimika kuitumia miaka saba baadaye.

Kijana mmoja aliibuka kusikojulikana na kutangaza kuwa aliwahi kufanya mapenzi ya kimwili na mke wa Rais wa Marekani ambaye alikuwa madarakani wakati huo. Alidai kuwa anamtaka Rais huyo ajiuzulu, vinginevyo angezitoa hadharani picha za video alizopiga akifanya mapenzi na mama huyo. Siku chache baada ya madai hayo, kijana huyo alipokuwa akitoka nje ya nyumba yake, alisikia akiitwa na watu waliokuwa ndani ya gari lililosimama mbele ya nyumba hiyo. Wakati akilisogelea ulisikika mlio kama huu. Ukawa mwisho wake na mwisho wa madai yake.

Silaha hii, ambayo wenyewe huiita 'kifutio' ilikuwa kali kiasi kwamba mara unapopokea kipigo chake unasambaratika katika vipande vidogovidogo zaidi ya milioni mbili.Matokeo yake ni kwamba hakionekani kipande cha mfupa, nyama wala tone la damu. Unakuwa umefutika katika uso wa dunia kana kwamba hukuwai kuwepo.

Ni silaha hiyo iliyotumiwa kwa Kakakuona, mbele ya macho ya Joram Kiango. Sekunde moja alikuwa hai mbele ya macho yake, sekunde iliyofuata haikuwepo hata dalili yake.

Joram alilitazama jengo hilo kwa makini. Hakuona mtu wala kitu. Yeyote Yule aliyeifyatua bunduki hiyo alitumia mfadhahiko uliowakumba. Joram pia aliamua kuitumia fursa hiyo. Alitumia funguo zake Malaya, akalifungua gari la Kakakuona na kuichukua ile briefcase yake aliyokuwa nayo mkononi. Akaurudishia mlango na kuondoka taratibu.

Akiwa na shahuku kubwa ya kufahamu chochote ambacho angeweza kufahamu juu ya hayati Kakakuona, Joram Kiango hakwenda mbali. Aliivuka barabara hiyo ya UWT na kuingia katika moja ya majengo ya SIDO ambayo baadhi yamepangishwa kwa watu wanayoyatumia kama ofisi.

"Naomba kwenda haja," alimweleza mtu wa kwanza ambaye alimkuta mbele ya ofisi mojawapo, msichana mtanashati ambaye alimchekea na kisha kumwelekeza kwa mkono.

Joram aliufuata mkono huo na kujikuta katika choo ambacho bila shaka hakikuwa na mwangalizi kwa jinsi kilivyokuwa kichafu. Hata hivyo, alijifungia kwa komeo, kisha akajibanza nyuma ya mlango huo na kuanza kuishughulikia ile briefcase ya Kakakuona. Kwa mtu wa kawaida, briefcase hizi zinafunguliwa kwa namna maalumu, ingemchukua miaka kuifungua. Lakini si kwa Joram Kiango. Yeye alikuwa na mbinu zake ambazo alizitumia kucheza na namba hizo. Dakika mbili baadaye tayari ilikuwa wazi ikimchekea.

Kati ya yote aliyoyategemea katika mfuko huo, kamwe hakutegemea kukuta mabunda mengi ya pesa za kigeni kiasi hicho. Kwa hesabu ya harakaharaka zilikuwa paundi za kiingereza laki moja. Zaidi ya pesa hizo ilikuwemo hati ya kusafiria yenye jina la Bruno Malapaka ambaye alielezewa kuwa raia wa Naijeria ambaye alikuwa ni mfanyabiashara. Picha ilikuwa ya Kakakuona. Chini ya vitu hivyo kulikuwa na bastola.

Joram alivitazama vitu hivyo kwa mshangao. Kwa kiasi fulani, mategemeo yake katika kuuchukua mfuko huo yalididimia. Alitegemea kupata maelezo ya kutosha ambayo yangemwezesha kufahamu mengi juu ya Kakakuona; aliajiriwa na nani, mwajiri yuko wapi, kwa nini anafanya mauaji hayo, na mengine mengi. Badala yake alichoambulia ni hati ya usafiri ambayo bila shaka yoyote ni ya bandia, bastola ambayo hakuihitaji sana na pesa ambazo bila ya Nuru kupatikana mapema, akiwa hai, kamwe zisingeweza kumfariji.

Kulifikiria kwake jina la Nuru kulimrejeshea hasira na hofu aliyokuwanayo juu ya usalama wake. Hisia zilimfanya ashuku kuwa waliomuua Kakakuona ni watu haohao waliotumwa kumkamata Nuru. Hisia zilionyesha kuwa mara baada ya Kakakuona kumfikisha Nuru mikononi mwao hawakuuona tena umuhimu wake. Hivyo, walichofanya ilikuwa kumlipa malipo waliomwahidi na kisha kumshawishi aondoke mara moja. Wakati akiondoka ndipo walipoamua kumfuta duniani kwa matumaini kuwa hakuna ambaye angeona wala kuelewa kilichotokea, jambo ambalo lingewafanya polisi waendelee kumsaka Kakakuona ambaye hayuko tena duniani hali wao wakiwa wametulia zao raha mustarehe.

Kuwa kwao na silaha hatari kama hiyo, ambayo ni wachache tu waliowahi kuisikia na uwezo wao kiuchumi, ni miongoni mwa mambo yaliyomfanya Joram azidi kuamini kuwa hawa hawakuwa watu wa kawaida. Licha ya kujizatiti kwao kwa kiwango hicho bado walikuwa wakatili kupindukia. Kitendo chao cha kumwua mtumishi wao, Kakakuona, kikatili kiasi kile, na kupuuza mamilioni ya pesa walizompa kulimfanya Joram aamini kuwa walikuwepo kwa kazi moja tu, kuua.

Hali hiyo ilimfanya ataabike sana moyoni kila alipowaza kuwa Nuru yuko mikononi mwao, mikononi mwa viumbe wasihofahamika, katili kuliko shetani mwenyewe.

'Lazima atoke mikononi mwao… mapema iwezekanavyo…' Joram aliwaza huku akiyasaga meno yake kwa hasira. Hata hivyo, alijirudi mara moja na kujaribu kuituliza hasira yake alipojikumbusha, kwa mara nyingine, kuwa dhamira kubwa ya watu hao, kwa kila aina ya ukatili wanaoufanya, ilikuwa kumtia uchungu na hasira, ili ashindwe kufikiri kikamilifu, jambo ambalo litamfanya akurupuke na kuangukia katika mikono yao kama kinda la ndege.

'Lazima nitulie… nipange kila kitu kwa tuo…' alijinong'oneza moyoni.

Akiwa ameituliza akili yake alijiuliza anafahamu nini juu ya maadui hao. Hakuna! Aliwaza kwa uchungu muda wote alikuwa akihangaika na Kakakuona ambaye sasa ni marehemu. Hivyo, alikuwa hajui chochote zaidi ya ukweli kuwa anapambana na watu wenye nguvu zote: kiuchumi, kiulinzi na kiukatili.

Chanzo pekee cha kufahamu juu ya watu hao ni katika jengo hilo la kampuni ya Kangaroo ambamo silaha iliyomwua Kakakuona ilitokea. Alijua kuwa jumba hilo au chumba katika jumba hilo kilihusika, kwa namna moja au nyingine, na mkasa huu. Ni hapo ambapo angeanzia. Hata hivyo, Joram alifahamu fika asingekurupuka na kwenda huko kwani ingekuwa sawa na kujitumbukiza wakati moto anauona, hakuwa na shaka kuwa maadui hao wanamsubiri kwa hamu.

Kwamba angehitajika kushughulika mara moja ili kumtoa Nuru katika mikono yao, hilo halikumsumbua tena. Alikuwa na uhakika kuwa Nuru alikuwa akitumiwa kama chambo cha kumfanya aharakishe kuwaendea, jambo ambalo lilimtia moyo kuwa wasingemdhuru kabla hajatokea.

'Nitatokea… nikiwa tayari…' aliwaza.

Wazo lake lilikatizwa kwa mlango kusukumwa kwa nguvu nyuma yake. Kitendo hicho kilifuatiwa na sauti nzito ya kiume iliyoita toka njeikiuliza, "vipi braza, bado tu?"

Ndio kwanza Joram akakumbuka kuwa alikuwa chooni. Akaitazama saa yake na kugundua kuwa alikuwa ametumia zaidi ya robo saa, akiwa amejifungia katika choo hicho cha watu. Sasa aliweza hata kusikia harufu kali ya mchanganyiko wa kinyesi na mkojo chooni humo.

Akahakikisha kuwa ameifunga briefcase hiyo kama ilivyokuwa na kutoka nje ya choo huku akijitia kufunga vifungo vya suruali yake. "samahani ndugu yangu." Alimwambia kijana wa kiume aliyekuwa amenyoa panki, ambaye alikuwa kasimama nje ya choo hicho katika hali ya kubanwa sana na haja ndogo. "Tumbo lilikuwa likinisumbua sana," alimlaghai.

"Shauri ya bia za Mtikila." Kijana huyo alimjibu akiingia na kujifungia.

Joram aliduwaa hapo nje kwa muda. Kisha, akajiwashia sigara na kuipachika mdomoni. Kwa mwendo wa utulivu, alivuta hatua moja baada ya nyingine akielekea katika hoteli ya Mawenzi ambako alipanga achukue chumba na kuziifadhi zile pesa. Mengine yangefuata baadaye.

Wakati Joram Kiango alipokuwa ameduwaa chooni, Inspekta Kombora alikuwa pia ameduwaa robo kilomita toka hapo. Yeye aliduwaa akiwa ameliegemea gari lake kwa mgongo, katika hali ya kukata tamaa.

Hakutaka kuamini kuwa Kakakuona alimponyoka katikati kabisa ya mtego wake kama samaki katika mdomo wa mamba. Hakupenda kuamini ingawa hali iliashiria hivyo. Upekuzi wa hali ya juu kupita kiasi tayari ulikuwa umefanyika katika jengo zima.

Tayari Kombora alikuwa na malalamiko ya baadhi ya wapangaji hao, mmoja akidai kuwa alilazimishwa kutoka bafuni akiwa uchi,mwingine akidai kuwa kapigwa ngwara bila sababu; watatu wakilalamika kusukumwa na kusachiwa bila maelezo. Halikadhalika, kulikuwa na malalamiko ya kuvunjwa kwa kabati moja ambalo funguo wake ulichelewa kupatikana, kubomolewa kwa tundu la ndege, kuharibiwa kwa mafriji matatu na friza moja; kuchanwa kwa mazulia na mapazia yasiyo na idadi, n.k. yote hayo Kombora alijua yangeletwa kwake kwa maandishi. Hakujali.

Ambacho alijali, ambacho kilimtisha ni kule kutopatikana kwa dalili yoyote ya Kakakuona. Alikuwa ametoweka! Nuru akiwa mikononi mwake! Ni hilo lililomfanya Kombora aduwae, Na kwa mara ya kwanza maishani mwake alijikuta akiwa hajui la kufanya kwa dakika kadhaa.

Alipotanabai kuwa karibu vijana wake wote walikuwa wamerejea na kumzunguka kwa namna ya kusubiri maelekezo zaidi ndipo alipojiinua toka kwenye gari na kupiga hatua mbili tatu za taratibu, huku akiwaza. Mara akagundua kuwa hakujua awaze lipi zaidi. Ndipo ikamjia akilini kuwa alihitaji kupata muda wa kutuliza akili yake ili aweze kuwaza kwa makini zaidi.

"Wanne wabaki hapa na kulilinda jengo hili kwa uangalifu mkubwa kila dakika, kila upande wa nyumba uwe katika macho yenu; mpo?" alisema.

“Tupo.” Msaidizi wake wa karibu alijibu

“Vizuri. Nitarudi ofisini kwa muda. Baadaye nitaleta maelekezo mapya. Bado naamini mshenzi huyu yupo humuhumu ndani. Na sitamruhusu aiachie nyumba hii akiwa hai, alisema akigeuka kuliendea gari lake.

“Hayumo mzee, kama angekuwemo hata kama angekuwa amejigeuza sisimizi tungempata. Naamini hayo…” kachero kijana aliyeyasema hayo alilazimika kusita ghafla huku akiulaani ulimi wake baada ya kuona Kombora akimgeukia na kumtupia jicho kali, ambalo lilipenya uso wake na kuunyanyasa moyo wake kiasi cha kumfanya atetemeke miguu, jicho ambalo kamwe hatalisahau.

Kombora alipanda gari na kumwamuru dereva kuelekea ofisini. Lakini kabla dereva hajalitia moto wazo jipya lilimjia. Akashuka garini na kumwita tena sajini Kangua, msaidizi wake wa karibu “Nadhani tunahaja ya kutupia macho majumba ya jirani kabla ya kuendelea na ulinzi wa nyumba hizi. Unasemaje?”

“Wazo zuri afande,” Kanguru alimjibu “Kwasababu kama angekuwa humu ndani kwa vyovyote angekuwa amepatikana.”

Walifuatana kuiendea nyumba iliyokuwa kushoto mwa jengo hilo. Lilikuwa duka kubwa, la Mhindi mmoja aliyenenepa kupita kiasi. Mhindi huyo, ambaye bila shaka yoyote alikuwa anafahamu kuwa kwa jirani kuna jambo, alijizoazoa kwa tabu na kumfuata Kombora kaunta.

“Ndio bana kuba, iko taka nini?”

Kombora alimvuta nje ya wateja na watumishi wake, ambao walitega masikio yao kwa makini ili wasikie kinachoendelea. “Tungependa kuikagua nyumba yako hii.”

“Iko kosa gani? Mimi niko fanya biashara lali bana kuba. Bana Rema iko jua ivo. Iko toa michango mingi. Iko lipa kodi pato. Iko…” alisema huku akitetemeka.

Kombora angeweza kumwacha aropoke hadi mwisho wa maelezo yake, akiwa na hakika kuwa wafanyabiashara hawa hawakosi madhambi. Lakini kwa kuwa hakuwa na nafasi hiyo alimkatiza kwa kumwambia kwa upole, “Hatuna haja na wewe wala biashara zako. Tunataka tuone kama kuna uwezekano wowote wa mtu kupenya toka jengo hilo la jirani yako kupitia hapa kwako.”

“Hakuna mitu pita hapa,” alijitetea

“Tunajua. Lakini tunataka kuwa na hakika,” Kombora alisema akianza kuingia ndani. Mhindi huyo alimzuia kwa kono lake zito lililolowa jasho.

“Hapana taka… Ngoja mimi iko piga simu kwa waziri Rema ulizia yeye. Iko subiri.”

Kauli yake ilipandisha hasira za Kombora. Aliutoa mkono huo kifuani pake kwa pigo moja la kiganjakwa mkono wake wa kushoto. “Sikia,” baadae alifoka huku kamkazia macho makali mhindi huyo, “Ukiendelea kunipotezea muda wangu nitaruhusu vijana wangu ishirini waingie humu na kuipekua nyumba hii. Na nakuhakikishia baada ya dakika ishirini tu utakuwa mahabusu kwa makosa yasiyo na idadi.”

Ukali wa Kombora ulifikisha ujumbe katika kichwa cha Mhindi huyo. Kwa unyonge, huku akijitia kutabasamu, alimpisha Kombora na kumfuata taratibu huku akisema, “Mimi iko mitu mema iko penda saidia…”

Kombora hakumsikiliza alimwita hadi uwani akifuatiwa na msaidizi wake. Huko walikutana na ukuta mnene, mrefu ambao ulikingwa na vipande vya chupa. Kombora hakuona uwezekano wa mtu kuupanda ukuta huo katika muda mfupi kama ule. Akageuka kumtazama msaidizi wake ambaye macho yake yalionekana kuwa na wazo hilohilo.

“Kwa mtu kama Kakakuona ukuta huu unapandika. Lakini apande yeye, ampandishe na mateka wake kwa nguvu, huku akiwa na bastola mkononi sio rahisi.”

Hata hivyo, Kombora na msaidizi wake, bastola zikiwatangulia, walianza ziara ya chumba hadi chumba. Mhindi huyo ambaye tayari alikuwa ameamuru kufunga duka alikuwa akiwafuata nyuma huku akitetemeka na kulalamika kwa maneno mengi ambayo Kombora aliyapuuza.

Karibu kila chumba kilikuwa na vitu mbalimbali vya thamani kubwa kama mashine za kupozea hewa, TV, deki za video, mazulia, nguo na vitu mbalimbali. Kwa jinsi Mhindi huyo alivyokuwa akitetemeka Kombora alijua fika kuwa kama angehoji mengi juu ya vitu hivyo angegundua kuwa nyingi zilikuwa mali za magendo au hazikulipiwa ushuru bandarini, au zimelipiwa nusu n.k. hata hivyo hakuwa na muda huo hadi alipofikia chumba ambacho Mhindi alitetemeka hadi kutokwa na machozi wakati Kombora akimshurutisha kukifungua.

“Iko kupa pesa milioni, sawa?” alibembeleza.

Kombora alimshika ukosi wa shati na kumsukasuka kwa hasira hadi funguo zikamtoka mkononi. Sajin kangua alizidaka na kuufungua mlango huo. Huku bastola ikimtangulia alitangulia kuingia, Kombora akimfuatia, na kumvuta mhindi huyo ambaye baada ya kuona hana hila alijikaza kisabuni na kuendea sefu la chuma lililokuwa katika kona moja ya chumba hicho. Alilifungua na kutoa mabunda ya pesa za kigeni na kumkabidhi Kombora.

“One hundred thousand dollars. Please…”

Kombora alizichukua fedha hizo na kuzikabidhi kwa msaidizi, “Yaani hata benki ya fedha za kigeni unayo katika chumba hikihiki, sio?” alimwuliza “Very well. Suala lako litamalizwa na polisi,” aliongeza akizungumza katika redio call yake na kuombwa aunganishwe na kituo kikuu cha polisi. Kilipopatikana aliwataka kuja kumchukua mtu wao mara moja.

Alipomgeukia Mhindi huyo nusura amhurumie kwa jinsi alivyolowa jasho na mkojo ambao ulikuwa ukimtoka kama mtoto hali mwenyewe hana habari. Kombora alimtazama kwa dharau na kumwacha mikononi mwa kachero wake mmoja kuwasubiri polisi. Kisha, akaongoza kutoka akiifuata nyumba ya upande wa kulia.

Nyumba hiyo haikuwasumbua. Lilikuwa jengo la ofisi ya idara moja ya serikali moja ambayo wafanyakazi wake wote tayari walikuwa wameondoka na kumwacha mlinzi ambaye hakuwa na funguo. Baada ya kutazama Kombora aliona mara moja kuwa Kakakuona hakuwa katika jengo hilo pia. Kuta zilikuwa ndefu, imara, ambazo pia zilipambwa kwa vipande vya chupa.

“Turudi ofisini,” aliamuru kwa sauti ya unyonge.

Nyumba hiyo haikuwasumbua. Lilikuwa jengo la ofisi ya Idara moja ya serikali ambayo wafanyakazi wake wote tayari walikuwa wameondoka na kumwacha mlinzi ambaye hakuwa na funguo. Baada ya kutazama Kombora aliona maramoja kuwa Kakakuona hakuwa ndani ya jengo hilo pia. Kuta zilikuwa ndefu, imara ambazo pia zilipambwa kwa vipande vya chupa.

“Turudi ofisini,” aliamuru kwa sauti ya unyonge.

Wakati wakipanda magari yao walipishana na polisi wengi wenye magwanda ambao walikuwa wakimburura Yule Mhindi mwenye duka huku tayari alikuwa ametiwa pingu “Tutawaandikieni ushahidi mdogo tulionao dhidi yake.” Kombora alimwambia kiongozi wao ambaye alikuwa amesimama kwa ukakamavu mbele yake baada ya kupiga saluti ambayo Kombora aliipuuza.

Msafara wa Kombora ulitanguliwa na gari lake. Waliuacha mtaa huo na kuingia barabara ya umoja wa wanawake. Walipopinda kushoto na kuelekea hatua kadhaa Kombora alitupa macho kulia na kuliona jengo ambalo kwake limekuwa kama fumbo la aina yake, fumbo lililomtia aibu na hasira kubwa kwa kushindwa kulifumbua.

Jengo hilo lilionekana nyuma ya jengo jingine la ghorofa mbili lililobeba maandishi yaliyosomeka Kangaroo Enterprises. Kampuni hiyo ilikuwa sambamba mgongo kwa mgongo na Sunrise Modern Club. Hisia zilimfanya Kombora ashuku kuwa inawezekana kabisa Kakakuona alitorokea katika jengo hilo. Akaamuru gari lisimamishwe mara moja. Huku akimwashiria Kanguru kumfuata, alishuka na kuliendea lango la kampuni hiyo.

Mlango ulifunguliwa hata kabla hawajaugusa. Aliyeufungua alikuwa askari aliyevaa magwanda ya mgambo ambayo ilionyesha ni moja ya kazi yake kuwafungulia wageni wote mlango waingiapo na watokapo.

Ilikuwa moja ya zile ofisi nyingi ambazo unaweza kudhidharau kwa nje lakini ndani ukaziogopa. Ndio kwanza Kombora na msaidizi wake wakagundua kuwa walikuwa wamechakaa kwa jasho baada ya kujikuta katika chumba hicho cha mapokezi, chenye vioo kila upande ambavyo viliwafanya wajitazame. Chumba kilikuwa na hewa safi ambayo ilikuwa ikitokea katika vipozea hewa. Mbele yao, nyuma ya meza ya mapokezi kulikuwa na wasichana wazuri watatu. Kushoto kwao kulikuwa na msichana mwingine, nyuma ya ukuta wa kioo, ambaye alikuwa akiendelea kuwachekea huku akisema kwa mara nyingine, “Karibuni kwenye viti.”

Kombora alianza kujiona mpumbavu kwa uamuzi wake wa kuingia humo. Kati yao hakuna aliyeonekana kuwa na wasiwasi wowote juu ya lolote ambalo lilitokea nje ya ofisi hiyo.

Kakakuona hakuwa amepita hapo. Alishawishika kuketi kwenye makochi ya kuvutia chumbani humo, kutokana na uchovu aliokuwa nao.

“Kangaroo Enterprises shughuli zenu hasa ni zipi?” Alimwuliza msichana huyo ambaye alianza kupoteza tabasamu lake kutokana na jinsi alivyomwona mgeni wake.

Kabla ya kujibu msichana huyo aliinama na kuinuka huku mkono wake ukiwa umeshikilia kijitabu chenye kurasa zaidi ya ishirini zilizochapwa kwa rangi mbalimbali ndani na nje. Juu ya kijitabu hicho lilitajwa jina la kampuni hiyo na nenoCatalogue chini yake. Kombora alikipokea na kukididimiza mfukoni mwake. Msichana huyo alipoona hana walau nia ya kukitupia macho alisema kwa sauti ya kibiashara “Tuna fanya mambo mengi, tunajenga viwanda, tunasafirisha watalii, tunaagiza na kuingiza mali nje ya nchi, tuna maduka ya kubadili fedha n.k. Hii ni ofisi kuu hapa nchini. Ni tawi la kampuni ya Kangaroo yenye makao yake makuu nchini Marekani na matawi katika nchi mbalimbali za dunia” msichana huyo alieleza kwa ufasaha. Alipoona maelezo yake hayaelekei kumvutia. Kombora aliongeza harakaharaka.

“Sijui nikusaidie nini mzee wangu?”

“Naweza kumwona bosi wako?” lilikuwa jibu la Kombora

“Bosi huwa hapatikani kwa urahisi, labda ueleze shida yako ili tumwulize kama anahitaji kukuona..”

“Shida yangu ni kumwona yeye!” Kombora alijibu kwa sauti nzito iliyoonyesha madaraka. Alipomwona msichana huyo kaduwaa aligeuka na kuufuata mlango ulioandikwa Mkurugenzi Mkuu.

Akifuatana na msaidizi wake, walipanda ngazi ambazo ziliwachukua hadi ghorofa ya kwanza ambapo walijikuta ndani ya ofisi nyingine iliyojaa watu ambao pia walikuwa katika mishughuliko mingi. Alikuwepo msichana mwingine wa mapokezi. Kwa mshangao wa kombora msichana huyo aliwaelekeza kwa adabu katika chumba kilichoandikwa Mkurugenzi Mtendaji. Nje ya ofisi hiyo kulikuwa na chumba cha kusubiria chenye makochi bora zaidi, ambayo yaliizunguka meza ndogo iliyojaa makabrasha ya kujisomea. Kombora hakuketi. Aligonga mara moja mlango wa mkurugenzi na kisha kuusukuma. Ulifunguka na kumruhusu kuwa ndani ya chumba kipana nadhifu, ambacho kilinukia kila dalili ya pesa. Zulia lililotandikwa hapo sakafuni lingetosha kujenga madarasa matatu ya shule ya msingi, meza kubwa iliyokuwemo ingeweza kuwafanya ombaomba kuwa matajiri kwa miaka mitatu. Viti vilivoizunguka meza hiyo vingewafanya watoto wa mitaani wanane wasahau kuwa hawana wazazi.

Lakini vitu hivyo havikumvuta Kombora kama alivyovutwa na mtu aliyeketi nyuma ya meza hiyo pana akiwatazama. Kombora alitegemea kumkuta Mkurugenzi wa kampuni iliyonona kama hiyokuwa mtu aliyenona, mtu ambaye hakuhitaji kujitambulisha ili umtambue.

Badala yake aliyeketi nyuma ya meza hiyo alikuwa mtu wa kutisha au kutatanisha. Haikuwa rahisi kujua kama alikuwa mzungu au mwafrika kutokana na kovu kubwa jeusi ambalo lilikula nusu ya uso wake, kuharibu jicho lake moja na kuchoma robo tatu ya nywele zake kiasi cha kumfanya awe katikati ya mataifa hayo mawili.

“Yes. Sir what can l do for you?” mwenyeji huyo alimwambia Kombora ambaye tayari alikuwa ameketi mbele ya kimojawapo ya viti hivyo.

Kabla hajajibu Kombora alitia mkono mfukoni mwake na kutoa moja ya kadi zake, ambazo humfanya awe na cheo kidogo kuliko kile cheo chake kamili, kile ambacho ni siri yake yeye pamoja na mkuu wa nchi. Meneja huyo alipokea kwa mkono wake wa kushoto, jambo lililomfanya Kombora aamue kuutazama mkono wa kulia na kugundua kuwa ulikuwa wa bandia ambao ulitengenezwa kwa mbao au plastiki kwa ufundi kiasi cha kufanana na ule wa kawaida.

"Vita… vita sio mchezo. Vita vya Angola ndiyo ilinifanya hivi," alisema ghafla kana kwamba alikuwa akiyafuata macho na mawazo ya Kombora. " Kwa hiyo wewe ndiyo Inspekta Kombora? Tumekuwa tukizisikia jitihada zako. Hongera sana."

Kombora hakujua ni jitihada zipi hizo, na huyo bwana alizifahamu vipi, "Sijui na wewe mwenzangu unaitwa nani?" aliuliza badala yake.

"Naitwa Paul Powel. Ni mkurugenzi mwendeshaji wa kampuni hii. Sina budi kushukuru sana kutembelewa na mtu mzito kama wewe."

Kombora alihisi kitu kama kebehi katika sauti yake. Naam, aliweza hata kuiona waziwazi katika jicho lake moja ambalo lilikuwa likimcheka ingawa mdomo wake ulikuwa hauna tabasamu lolote.

"Vizuri." Alimjibu kwa utulivu. "Shida yetu ilikuwa ndogo sana. Kuna mtu wa hatari ambaye ametoroka jengo la jirani yenu upande wa pili wa mtaa. Tulichohitaji ni kukagua jengo zima ili tuwe na hakika kuwa hayuko humu ndani."

Powel alicheka. "Jengo hili haliingiliki hovyo. Tuna biashara ya mamilioni hapa, hivyo tumelijenga kwa usalama wa hali ya juu. Mtu atakayeingia hapa itambidi kupitia mlangoni peke yake…"

"Hilo tunaelewa. Lakini kiutaratibu lazima tuhakikishe kwa macho yetu wenyewe, kwa usalama wenu…" Kombora alilazimika kusita ghafla alipoona pazia lililokuwa nyuma ya Powel likifunuka

taratibu na Powel mwingine kuingia ghafla kama kivuli na kuketi kwenye kiti kilichomuelekea Kombora.

Kombora alimfikiria kama Powel mwingine, kwa jinsi walivyofanana kimaumbile na kimavazi.Yeye pia alikuwa ameungua uso na sehemu mbalimbali za mikono yake. Yeye pia alikuwa na jicho moja, ingawaje lake lililoungua lilikuwa wazi nyuma ya kovu kana kwamba linaona. Badala ya mkono wa bandia yeye alikuwa na mguu mmoja wa mbao. Hilo Kombora aliligundua wakati alipoukunja kwa mikono yake yote miwili pindi akiketi chini, vinginevyo isingekuwa rahisi kugundua.

Powel aliyaona macho ya Kombora yakitembelea uso huu hadi ule kana kwamba yanadai maelezo. Kwa sauti ilelile inayocheka Powel alisema, "Watu wengi wanasema tumefanana. Wengine wanadhani tu mapacha. Lakini wanakosea sana. Hatujafanana hata kidogo. Ukishatuzoea, utagundua kuwa huyu mwenzangu ni mrefu kuliko mimi, mnene kuliko mimi." Alipoona maelezo hayo hayajamridhisha Kombora aliongeza, " kinachotufanya tufikiriwe ndugu ni haya masahibu yaliyotukuta, siku moja, saa moja, kwa bomu moja. Ilikuwa tufe pamoja, kwa bahati mungu alitunusuru pamoja. Tungeweza kuwa ombaomba barabarani, lakini mungu ametusaidia vilevile na kutuwezesha kuwa wafanyabiashara wakubwa duniani…"

"Hujaniambia mwenzako anaitwa nani," Kombora alimkatiza

"Oh kweli anaitwa Philip Benjamin. Yeye ni Mkurugenzi wa Fedha" alimgeukia mwenzake huyo na kumwambia, "Philip, huyu hapa ni Inspekta Kombora bila shaka umepata kumsikia"

Philip alitikisa kichwa kukubali.

Powel aliendelea "Inspekta Kombora anadhani kuna mwizi ambaye amejificha katika jengo hili. Unadhani inawezekana Philip?"

Badala ya kujibu Philip aliangua kicheko.

“Unaona Inspekta? Unapoteza muda wako bure.”

4

Kombora alianza kupandwa na hasira juu ya watu hawa. Aliona wazi kuwa ama walikuwa punguani wa akili kama ilivyokuwa kwa baadhi ya viungo vyao, ama walikuwa wakimdhihaki. Akaamua kucheza mchezo waliotaka wao. Aliinuka akawashukuru na kutoka nje huku akihisi kila jicho linaloona, la kila mmoja kati yao, likiwa limemganda mgongoni huku linamcheka.

Alipanda gari na kuamuru liondoke. Baada ya kupinda kona moja alisimamisha gari na kumwamuru kachero mmoja arejee na kutafuta uwezekano wa kuilinda ofisi hiyo kwa makini bila ya yeye mwenyewe kuonekana.

11

Ilikaribia saa kumi na mbili Kombora aliporejea ofisini kwake kama mgonjwa aliyeruhusiwa kutoka hospitali baada ya kukata tamaa ya kuendelea kuishi. Alijibweteka juu ya kiti chake na kujiinamia kwa muda, mikono yake yote miwili ikiwa imekilea kichwa chake.

‘Msichana mzuri, asiye na hatia yuko mikononi mwa muuaji wa hatari, aliwaza kwa uchungu, mbele ya macho yangu mwenyewe jambazi huyohuyo ameua watu wawili wasio na hatia… Na ametoweka…mbele ya macho yangu mwenyewe. Mimi … ambaye najiita mkuu wa kikosi hiki…’ alishindwa kuendelea kufikiri. Hasira zilikuwa zimefura katika kichwa chake kiasi cha kufanya ubongo wake ukitishia kuchemka. ‘Lazima nitunze kichwa changu,’ alinong’ona kimoyomoyo huku akiiitoa mikono yake kichwani na kuipeleka mezani ambako ilirudi na faili ambalo hakulihitaji. Alilitupa mezani hapo na kuiingiza mikono mfukoni ambamo alitoka na kile kijitabu cha maelezo ya kampuni ya Kangaroo. Alikipekuapekua kwa dakika chache kabla hajainua simu na kumpigia mmoja wa wasaidizi wake, ambaye alifika mbele yake mara moja na kupiga saluti ambayo haikujibiwa.

“Fanya kila unaloweza nipate taarifa za kampuni hiyo kabla ya saa mbili,” alimwamuru akimwonyesha kijitabu hicho. “Nataka kujua imeanzishwa lini na wapi, hapa nchini imeingia lini, nani hasa mwenye kampuni hiyo, shughuli zake hasa ni zipi na kila unachoweza kupata. Zaidi, jitahidi nipate kila ambalo linaweza kupatikana juu ya wakurugenzi wake wawili walioko hapa, Paul Powel na Philip Benjamin. Tumia watu wote unaoweza kuwapata. Upo?

“Nipo afande.”

“Haya! Bado unasubiri nini zaidi?”

Amri ya pili ambayo Kombora aliitoa na kumtaka Sajin Kangura mwenyewe kuhakikisha inatekelezwa mara moja ni ile ya kupata ramani ya majengo ya Sunrise Modern Club na Kangaroo Enterprises katika muda wa saa mbili.

“Ni zaidi ya saa mbili sasa, afande. Ofisi ya Ardhi na jiji zitakuwa zimefungwa…”

“Zinaweza kufunguliwa. Kama wanaohusika hawapatikani mtafute waziri wao azifungue. Na kama hana funguo mwambie azivunje.”

“Ndiyo, afande.”

Kombora alipobaki peke yake alijaribu tena kukisoma kijitabu cha maelezo ya kampuni ya Kangaroo. Maelezo yalikuwa mengi, marefu yaliyowekwa katika mpangilio ambao ungemfanya msomaji yeyote ahisi kuwa kampuni hiyo ilikuwa moja ya makampuni makubwa sana duniani. Yalitaja matawi yake katikasehemu mbalimbali za dunia. Hata hivyo, ilimshangaza Kombora kuona kuwa anuani za matawi hayo hazikutajwa wala makao makuu, ambayo yalidaiwa kuwa yako New York, Marekani. Hali kadhalika, zaidi ya Powel na Philip, kijitabu hicho hakikuwa na jina jingine la Mkurugenzi yeyote.

Hayo yaliyoongeza mashaka ya Kombora juu ya kampuni hiyo, mashaka ambayo yalianza tangu alipowatia machoni wakurugenzi hao wawili, ambao pamoja na kutojiweza kwao hawakuonekana kuwa na lugha ya biashara hata chembe. Kwa ujumla, Kombora hakuwaona kama wafanyabiashara. ‘Kama wanafanya biashara, lazima biashara hizo zitakuwa haramu,’ aliwaza. ‘Si biashara walizoziorodhesha hapa.’

Kombora alijua ambacho angefanya kesho. Alijua kuwa angehitajika kuwataka msaada polisi wa kimataifa, Interpol, toka nchi zote ambazo Kangaroo ilizitaja kuwa ina matawi yake na kumwomba juu ya uhalali wa makampuni hayo, biashara halisi wanazozifanya na taarifa kamili za wakurugenzi wake.

Hilo lilikuwa la kesho. La leo ambalo lilikuwa likimsumbua Kombora na ambalo lisingesubiri kesho lilikuwa la kumtoa Nuru mikononi mwa Kakakuona, akiwa hai. Alitazama saa yake na kuona ikikaribia moja na nusu usiku; lakini hajapata bado jibu toka kwa watu aliowataarifu kupata taarifa za Kangaroo, jengo lao na lile la Sunrise. ‘Wako wapi hawa’ alinung’una akiinua uso wake kutazama mlangoni.

Juu ya meza yake Kombora alishukuru kuona kuwa mtu mmoja alimwekea chupa ya chai au kahawa na mayai matatu ya kuchemsha. Ndio kwanza akahisi kuwa alikuwa na njaa kali. Akavunja yai moja na kulitafuna. Yai la pili vilevile alilila kavukavu. La tatu ndilo aliloshusha kwa chai nzito ya maziwa toka katika chupa. Baadaye, aliinuka na kuukamilisha mlo wake kwa glasi mbili za maji toka katika friji yake ndogo ya ofisini. Wakati akirudi mezani simu ililia. Kombora aliinyakua na kuidaka masikioni mwake.

“Afande, Kabweka hapa.”

“Najua, uko wapi?”

“Napiga toka bandarini, nilikuwa katika kuhakikisha kama kweli hawa Kangaroo wanaingiza vitu toka nje.”

“Enhe!”

“Ni waingizaji maarufu wa vitu vya nje, Mzee, nimeona mizigo yao mingi ambayo haijatolewa. Nimeambiwa pia kuwa safari hii wamekodi meli mbili. Moja inatarajiwa kuanza kushusha mali zao wakati wowote. Ya pili haijapata nafasi ya kuingia bandarini, imetia nanga nje kidogo ya pwani.”

Hazikuwa habari nzuri sana kwa Kombora. “Ni hayo tu uliyoyapata?” Kombora aliuliza akitaka kuthibitisha kama hakukuwa na habari nzuri zaidi.

“Ndiyo mzee, lakini…”

“Lakini nini?”

“Kuna jambo moja ambalo limenitatanisha.”

“Lipi?”

“Hawa wakurugenzi wake. Idara yetu inayoshughulikia taarifa za wageni haina lolote kabisa juu ya Philip na Powel. Hakuna kinachofahamika zaidi ya kuwa ni raia wa Urusi ambao walikwenda Angola kuwasaidia wazalendo dhidi ya Wareno, wakati walipokuwa wakipigania uhuru wao. Taarifa

hizo hazionyeshi maisha yao huko Urusi, waliondoka lini na walikuwa wakipigana kikosi kipi. Zinaonyesha kuwa MPLA tayari wameulizwa juu ya watu hawa na wakashindwa kutoa majibu. Wanasema kwa kuwa watu wengi vitani hupenda kutumia majina ya bandia huenda watu hao walishiriki. Urusi nako, kikosi chao cha KGBkimesema hakina majina hayo katika kumbukumbu zao."

Kombora alimsikiliza kwa makini, "Kwa hiyo, unawafikiriaje watu hawa, Kabweka?" Kombora alimwambia.

"Nahisi kuna kitu wanaficha na kuna kitu zaidi wanafanya. Inawezekana hawa ni wanachama wa kikundi cha Mafia ambao wanajishughulisha na biashara haramu za dawa za kulevya au nyara za serikali," alieleza na kuongeza kwa sauti ya kujiamini. "Inawezekana mzee, hawa ni maadui wa Joram Kiango."

"Ahsante kwa mchango wako. Endelea na usikose kuniarifu kila utakapopata kitu kipya," Kombora alisema akiitua simu chini.

Papo hapo ikaita tena. Safari hii aliyepiga alikuwa Sajin Kangura. Alikuwa akipiga toka Halmashauri ya jiji. Alimwarifu Kombora habari ambazo zilimsisimua zaidi. "Inashangaza, afande. Si wizara ya Ardhi wala jiji ambao wana nakala ya ramani ya majengo hayo yote mawili."

"Kwanini?"

"Haieleweki. Jiji wanadai kuwa wana hakika walikuwa na nakala za majengo hayo lakini hawazioni. Hata hivyo, mmoja wa maafisa wa jiji ananieleza kuwa jengo la Sunrise lilikuwa dogo la ghorofa moja lakini liliibuka ghafla na kupanuliwa hata kabla ya kukamilisha taratibu za ujenzi. Kuwa waliingia katika mgogoro na mwenye jengo hilo ambapo baadae ulitatuliwa na akaruhusiwa kundelea."

"Hamkuweza kumpata mwenye jengo hili awapeni ramani hiyo?" Kombora alimwuliza.

"Yeye pia yalimkuta makubwa," Kombora aliambiwa "Inadaiwa kuwa huu mwaka wa tatu tangu alipotoweka"

"Katoweka!"

"Ndiyo, afande. Tumeambiwa kuwa bwana huyo, Fabian Kalila, ambaye alikuwa maarufu kwa ujenzi mara tu baada ya kukamilisha jengo hilo la Sunrise aliaga siku moja kuwa anakwenda Kigamboni kukagua uwanja mpya ambao ulihitajiwa kujengwa nyumba ya pili. Bwana huyo alifika hadi Ferry ambapo alionekana akizungumza na watu anaofahamiana naye.Watu waliomwona kwa mara ya mwisho walidai alipanda na kwenda ng'ambo. Lakini huko ng'ambo hakuna aliyemwona, yametolewa matangazo magazetini na maredioni lakini hazijafika taarifa zozote juu yake, wala maiti yake."

"Naam, iko namna," Kombora aliropoka kwa namna ya mtu anayezungumza peke yake.

Kangura alikuwa akiendelea, "pamoja na hayo, afande, tumefanya upekuzi mkubwa katika makabrasha yake yote, tumeweza kuona karibu nakala za majengo yote aliyowahi kushughulikia isipokuwa hili la Sunrise na Kangaroo. Hatukuweza kupata hata zile za majaribio."

"Ni yeye aliyeshughulikia jengo lile pia?"

"Ndio, afande"

Kombora hakujua afanye nini zaidi. Alichanganyikiwa kupita kiasi. Kwa ujumla, hakujua kama anakwenda mbele au anarudi nyuma katika suala hilo. Alitua simu chini bila kusema neno lolote zaidi.

Mtu mwingine aliyekuwa jengo Fulani mtaa fulani, wa jijini hapo, baada ya kuyasikiliza maongezi hayo ya Kombora na wasaidizi wake aliitua simu yake chini taratibu. Kisha, akakichunguza chombo chake cha kunasia sauti kuona kama kilikuwa kinafanya kazi vizuri.

“Not so bad” alitamka, akitabasamu. Aliitoa kanda hiyo na kuitia mfukoni mwake. Akategesha upya chombo chake na kisha kuondoka zake toka chumbani humo, tabasamu likiwa bado usoni mwake.

Mtaa wa tatu toka hapa mtu mwingine alikuwa akitabasamu. Lakini hili lilikuwa tabasamu lake la kwanza kwa siku hiyo, na pengine kwa wiki hiyo. Mtu huyo aliitwa Joram Kiango.

Kama ungemtazama harakaharaka alivyoketi juu ya kochi, ndani ya chumba alichokodi katika hoteli hii ya Mawenzi usingemfikiria kabisa kuwa alikuwa na tatizo kubwa la kutisha ambalo lingetosha kabisa kumtia kichaa. Badala yake ungemwona kijana mtanashati, aliyevaa suti yake nyeusi iliyomkubali vilivyo; akiwa ameketi juu ya kochi pana glasi ya wiski ikiwa mbele yake, sigara mkono mmoja na simu mkono wa pili.

Hali hii ilimrejea joram baada ya kujiaminisha tena na tena kuwa alihitaji kutuliza kichwa chake ili kupambana kikamilifu na janga hilo. ‘wewe ni Joram Kiango’ nafsi yake ilimwambia, ‘Endelea kuwa Joram Kiango vinginevyo Nuru utampoteza na maisha yako yatapotea.’

Hakujali sana juu ya maisha yake lakini alipomkumbuka Nuru na ukatili wa watu wanaomshikilia, alituliza akili yake na kuwa Joram Kiango. Na kwa mshangao wake alikuta akili yake ikichemka kwa ukamilifu kama betri zilizochajiwa upya.

Aliwakumbuka marafiki zake wote, wa nje na ndani. Namba zao za simu teleksi na faksi ziliibuka kama chemichemi akilini mwake. Akiwa na pesa za kutosha haikumchukua muda kukifanya chumba hicho kidogo kigeuke ofisi kubwa ya mawasiliano ambayo yalitoka huku na huko.

Simu yake ya kwanza ilimwendea rafiki yake mmoja anayemiliki kampuni yake binafsi jijini. Huyu akiwa ni mtu ambaye kila kitu kwake ni biashara, alikuwa anafahamu kila mtu na kila kampuni jijini Dar es Salaam. Hivyo, Joram alipomwuliza anafahamu nini juu ya Kangaroo Enterprises rafiki yake aliangua kicheko.

“Vipi? Sioni kama jina hilo linachekesha,” Jorama alimsaliti.

“Sio jina braza, ni pesa” Sauti ilijibu toka upande wa pili.

“Pesa?”

“Pesa hazina macho,” alieleza na kuongeza “pesa, kwa kweli mara nyingine inapotea njia.”

“Sijakuelewa?” Joram alimkumbusha.

“Kwani hujawaona wakurugenzi wa kampuni hiyo?”

“Wakurugenzi gani?”

“Powel na Philip.”

“Wanakasoro gani?”

“Swali sio wana kasoro gani , ila kasoro gani hawana” kicheko “Wale mabwana ukiwaona utafikiri pacha. Wenyewe wanadai hawana undugu wowote. Ukiwaona utadhani ndio kwanza wanaibuka toka kaburini; utafikiri waliwekwa katika pipa wakachemshwa na kisha kutolewa kabla ya kukata roho. Mmoja ni nusu kipofu asiye na mkono wa pili, mwingine nadhani kiziwi na hana mkono mmoja. Kwakweli mabwana wale ni watu wa kuchekesha sana.”

“Sioni wamewezaje kupata pesa,” Joram alichochea.

Baada ya maswali mengi alibaini kuwa kampuni ya Kangaroo Enterprises ni mpya inayoongozwa na watu wasiojiweza, Paul powel na Philip Benjamin. Pamoja na kwamba kampuni hiyo ilidai inajishughulisha na mambo mengi, lakini taarifa alizozipata ni kuwa kazi kubwa ambayo kampuni hiyo imekwishafanya ni uingizaji wa pickup, bidhaa toka nje na kuzisambaza kwa wauzaji mbalimbali wa jumla jijini. Bidhaa yao kubwa, Joram aliarifiwa, ni vipodozi vya aina kwa aina, hasa kwa kina mama.

Alifahamishwa kuwa kampuni hiyo ilijenga maghara yake kando ya barabara ya Nelson Mandela katika eneo la Tabata.

Joram alimshukuru rafiki huyo na kumtaka amwarifu kila atakachokipata juu ya wakurugenzi hao wawili.

Rafiki yake mwingine alikuwa miongoni mwa vijana wa Inspekta Kombora. Kila alipopata wasaa aliwatoroka wenzake na kumdokeza Joram juu ya kila tukio. Alimfahamisha jinsi ambavyo Inspekta Kombora alikuwa taabani baada ya watu wawili wasio na hatia kuuawa mbele yake na Nuru kutoweka mbele ya macho yake. Aidha, alimfahamisha juu ya harakati zote ambazo zilifanyika kulikagua jengo hilo na majengo yote ya jirani bila mafanikio yoyote.

“Sasa hivi ukimwona mzee Kombora utadhani ana umri wa miaka mia moja, kwa jinsi alivyozeeka ghafla,” Rafiki huyo alidokeza katika maongezi hayo.

Baada ya Joram kuuliza kwa makini ukubwa wa jengo la Sunrise Modern Club, Kangaroo Enterprises zilivyojengwa ndani na nje, sehemu ambayo Kakakuona alimwua dereva wa taksi na alipomwua msichana wa mapokezi, na mengine mengi, alipatiwa majibu yote aliyoyahitaji kwa kiwango cha kuridhisha. Maelezo hayo yalifuatwa na onyo, “Joram kama unakusudia kufuata nyayo za Kakakuona, lazima ujihadhari sana. Huyu sio mtu wa kawaida. Mambo aliyoyafanya hapa ambayo nimeyaona kwa macho yangu sio mambo ya kawaida. Labda tunayoona katika filamu baada ya watu wa studio kuweka utaalamu wao. Huyu si binadamu ningekushauri ufikirie mara mbili.”

Ni hilo ambalo lilimfanya Joram atabasamu kwa mara ya kwanza siku hiyo. Yalimchekesha mengi. Moja likiwa lile la kujua kuwa nje ya maadui, ni yeye peke yake ambaye alifahamu kuwa Kakakuona hayuko duniani tena. Jingine alipoona rafiki yake huyo asivyomwelewa kikamilifu kwa kumtahadharisha kumfuata Kakakuona. Laiti angejua kuwa alikuwa tayari kumfata hadi kuzimu, na kuhakikisha akirejea na Nuru, akiwa hai au salama! Hata hivyo, Joram alimshukuru rafiki huyo na kumtaka aendelee kuwa macho.

Joram alipata msaada mkubwa zaidi toka kwa rafiki yake mmoja wa kampuni ya simu. Huyu, alimwezesha kupata moja kwa moja mawasiliano yote ya simu yaliyokuwa yakiendelea katika ofisi ya Kombora kwa kuiunganisha na laini moja ya hoteli ambayo Joram aliikodi kwa bei mbaya.

Mawasiliano hayo yalimpunguzia Joram kazi kwa kiasi kikubwa. Hakuhitaji tena kujishughulisha na uraia wa watu hao kwa wakati huo kutokana maongezi baina ya Kombora na msaidizi wake. Hakuwa na haja tena ya kutafuta ramani ya majengo hayo wala ujenzi wake kutokana na taarifa hizohizo. Hali kadhalika, asingepoteza muda wa kutafuta habari za kampuni hiyo huko nje kwani tayari ilionyesha kuwa taarifa zao sio za kweli. Zaidi, Joram hakuwa na wasiwasi juu ya Nuru kuhamishwa toka jengo hilo kwa kujua kuwa vijana wa Kombora walikuwa wakilinda doria na kumtaarifu juu ya kila tukio lililotendeka, taarifa ambazo yeye pia alikuwa akizipata.

Kitu ambacho kwa sasa kilisumbua sana akili ya Joram Kiango kilikuwa kushindwa kuoanisha maelezo juu ya maumbile ya wakurugenzi hao wa Kangaroo na mkasa huu mzima. Kama kweli ni watu wasiojiweza,wenye biashara zao halali, vipi wajihusishe na ujasusi huo wa kimachomacho? Watakuwa wanajiamini nini?

Kitendo chao cha kumteketeza Kakakuona hata kabla hajakamilisha jukumu alilopewa pia lilimtatiza. Kama wangemwua Kakakuona na kisha kumwachia Nuru angeweza kuelewa. Ingekuwa ishara ya kukubali kushindwa. Lakini kumwua Kakakuona, na kuendelea kumshikilia Nuru kwa vyovyote vile ni dalili ya kutangaza shari zaidi, shari ambayo kwa maumbile yao yalivyo, wasingeweza kuitekeleza bila msaada wa mtu mwingine mwenye uwezo na akili timamu zaidi ya Kakakuona.

Joram alihitaji kumfahamu mtu huyo kwa gharama yoyote ile kwani ni yeye tu aliyekuwa kipingamizi baina yake na Nuru. Vinginevyo, angeweza kwenda zake, mchana kweupe, na kumpokonya Nuru toka mikononi mwao.

Simu ililia. Akaipokea na kuisikiliza, kisha akaitua, haikuwa na kitu cha muhimu.

Teksi ikapata uhai. Taarifa ilitoka katika tawi moja wapo la NBC mjini hapo, ilimtajia namba ya akaunti ya Kangaroo Enterprises na kitita cha pesa kilichokuwemo. Kwa kampuni kama hiyo, bilioni moja na nusu si ela nyingi. Kilichomsisimua Joram ni habari kuwa pesa hizo ziliingia toka katika akaunti moja ya mjini New York, Marekani.

Joram aliitazama saa yake. Ilikuwa saa kumi kasoro. Aliandika ujumbe harakaharaka na kuutuma kwa faksi kwenda kwa rafiki yake mmoja mwenye kampuni ya upelelezi wa kujitegemea mjini humo, akimtaka kuichunguza akaunti hiyo kuona ina pesa kiasi gani na nani anamiliki. Ujumbe ulichukua nusu dakika kufika na baadaye kupata jibu ambalo lilimfahamisha kuwa anashughulikiwa.

Nusu saa baadaye alipata majibu ya maswali yake. Benki hiyo haikuwa na akaunti yoyote yenye jina la Kangaroo wala namba zilizotajwa si za benki hiyo.

'Haya.' Joram aliwaza baada ya kuisoma faksi hiyo, ambayo pia iliandikwa kwa mkono, kazi ndio kwanza inaanza! Hata hivyo, hilo alikumsumbua sana Joram. Kitendo cha kuficha ukweli wa pesa zao ni jambo la kawaida kwa wafanyabiashara kote duniani. Alipoitazama tena saa yake aligutuka kugundua kuwa imetimia saa tatu za usiku akiwa ameketi kwenye kochi hilohilo. Akiwa si mtu wa kuketi alifurahi kuona usiku umeingia. Kwake giza ni mali, giza ni uhai; hali ambayo alihitaji sana.

Akavuta kabati na kutoa vifaa vyake vyote muhimu alivyokuwa ameviandaa kwa safari yake ya Zanzibar; bastola moja, visu viwili, funguo zake Malaya, bomu moja la mkono alilolitengeneza mwenyewe na vikorokoro vingine vingi. Vyote alivifutika katika mifuko ya siri baada ya hapo alichukua kitita cha pesa na kukifutika mifukoni. Kabla ya kutoka alitegesha chombo cha kupokelea simu ambazo angepigiwa. Wakati akikamilisha kufanya hivyo, simu iliyomwunga na redio call ya Kombora ilipata uhai. Joram akainua chombo cha kusikilizia na kulitegesha sikio lake.

"Ni mimi afande koplo Shomari. Bado nilikuwa nikilinda ofisi ya Kangaroo ninamashaka kuna kitu wanafanya mzee…"

"Kitu gani?"

"Ni sanduku kubwa ambalo linatosha kupakia watu watatu wazima. Sioni kwanini mzigo huo usafirishwe saa hizi…"

"Nisubiri nakuja." Sauti ya Kombora ilisikika. "Usiache mzigo huo ukupotee machoni. Kadhalika, usiruhusu wajue kuwa unawatazama."

"Sawa, afande…"

Jibu hilo la mwisho halikumfikia Joram. Alikuwa tayari amekwisha funga mlango na kukimbia hadi nje ambako alimwomba dereva wa teksi bubu moja, aina ya Toyota Corolla, aliyekuwa amepaki nje ya hotel hiyo, amwazime gari. Ili mtu huyo asiwe na shaka Joram alimkabidhi laki tano. "Nikirudisha gari salama laki mbili zako, laki tatu utanirejeshea," alimwambia baada ya kumwelekeza namba ya chumba chake na kumtajia jina lake la bandia.

Dakika tano baadaye gari hilo likawa limepaki jengo moja toka ilipo ofisi ya Kangaroo, boneti ikiwa imefunguliwa huku dereva wake akihangaika, mara achungulie ndani ya injini mara aingie ndani na kujaribu kuwasha, mara ajitie kulisukuma. Lakini wakati wote huo macho yake yalikuwa yakiangalia kwa umakini kila kinachoendelea katika ofisi hiyo.

Utulivu wake na jinsi alivyokuwa akiitazama saa yake mara kwa mara vilimfanya Joram aanze kuhisi kuwa chochote kilichomo ndani ya sanduku hilo hakikuwa na thamani yoyote kama alivyotarajia. Hakuamini kama Nuru alikuwa ndani ya sanduku hilo. Badala yake alihisi kuwa zilikuwa zinafanyika njama za kuwaita polisi nje ya eneo hilo ili aweze kuhamishwa kwa utulivu zaidi.

Wakati Joram alipokuwa akiwaza hayo, aliona gari ya Inspekta Kombora likifika katika eneo hilo. Lilikuwa Rangerover lenye namba za kiraia. Lilijipitisha katika eneo hilo kama ambalo halina shughuli yoyote na jengo hilo, kwa mwendo wa taratibu na kutokomea mitaani.

Kana kwamba dereva wa pickup yenye 'mzigo' alikuwa akisubiri ishara hiyo, aliingia ndani ya gari lake na kulitia moto. Alifuata barabara ya UWT na baadaye kuingia ya Morogoro. Dakika mbili baadaye Joram aliona gari ya Kombora, likiwa na watu wawili zaidi, waliovaa sare za polisi wakilifuata gari hilo.

Joram alisita kabla ya kuamua kulifuata gari hilo au la. Lakini, shingo upande alilifanya gari lake Lionekane kama limepona, akaliwasha na kuyafuata magari ambayo yalikuwa yakitokomea mbele yake.

Saa hizo, magari yakiwa yamepungua barabarani, haikumchukua muda kuyapata magari hayo. Aliacha magari mawili, moja likiwa daladala yamtenganishe na Kombora ambalo lilikuwa nyuma ya ile pickup. Waliipata kariakoo wakaivuka jangwani na kuingia magomeni ambapo pia waliinuka hadi Manzese.

Wakati wakikaribia kiwanda cha urafiki, Joram alimwona Inspekta Kombora akilipita gari hilo na kisha kulisimamisha kwa mkono. Liliposimama yeye na wenzake wawili, bastola zikiwa wazi mikononi, walishuka na kumfuata dereva wa pickup hiyo.

“Una nini ndani ya sanduku…? Joram alimsikia Kombora akiuliza alipokuwa akiwapita taratibu.

Asingeweza kusimama hapo. Hivyo, aliwapita kama hatua mia moja na kisha kulisimamisha gari lake kando ya barabara. Huku akijifanya anakagua matairi ya gari, macho yake yalikuwa makini yakitazama kinachoendelea baina ya Inspekta Kombora na dereva wa pick up. Alimwona dereva akishuka na kuzunguka nyuma ya gari. Alihangaika kama anayetaka kulifungua sanduku hilo. Kisha, jambo la ajabu lilitokea. Joram alimwona Inspekta Kombora akipaa angani na kisha kuanguka chini kama mzoga. Alipojaribu kuinuka alipokea kipigo kingine ambacho kilimfanya apepesuke na kurudi chini huku bastola yake ikifyatuka na askari wengine walikuwa wakigalagala chini, mmoja kashikilia mbavu zake, wa pili shingo ikiwa haifanyi kazi.

Tukio hili lilifanyika kwa muda mfupi sana kiasi kwamba ilimchukua Joram Kiango nusu dakika kuelewa kinachotokea. Baada ya hapo alikuwa ameliacha gari lake na kutimka mbio kuelekea eneo la tukio. Alikimbia kwa kunyata kama chui. Alimfikia dereva huyo ghafla na kuachia teke ambalo lilitua tumboni barabara. Dereva huyo alipepesuka na kutokwa na macho ya mshangao. Hata hivyo, Joram aliporusha teke la pili lilidakwa na mguu wake kuanza kupindwa. Alitumia mguu wake wa pili kuruka tiktak ambayo ilimpata barabara dereva huyo usoni na kumfanya aanguke na kumwachia Joram ambaye aliviringika! Waliinuka kwa pamoja na kuanza kunyatiana kwa mwendo wa chui walio mawindoni. Macho yao yalitazamana. Hayakuwa macho ya kawaida. Kila mmoja aliona kitu katika macho ya mwenzie, kitu kisichoelezeka, kinachoonyesha waziwazi wao ni nani katika dunia hiyo.

Joram alihisi kupata kuyaona mahali fulani macho hayo. Macho ambayo yana dalili zote za tamaa ya kuwa kiu ya mauaji. Wapi aliyaona macho haya? Alijiuliza wakati akinyata kutafuta fursa nzuri ya kummaliza adui yake, huku akijua fika adui huyo pia anatafuta nafasi ya kumwua.

Wakati huo kikundi cha wapita njia kilikwisha wazingira, kila mmoja akiwa mdomo wazi kwa mshangao na kutoelewa kinachotukia. Dereva huyo alitazama huko na huko kisha akatia mkono wake mfukoni na kuutoa ukiwa umeshikilia tufe ambalo alilipiga chini kwa nguvu. Papo hapo ulitokea moshi mzito unaowasha zaidi ya bomu la machozi. Joram alilazimika kufumba macho huku akiruka upesi kutoka eneo hilo, kitendo ambacho kilimwokoa na pigo la judo ambalo lingemmaliza. Akiwa ameyafumba macho yake yaliyojaa machozi, huku watu wengi wakilia na kukimbia ovyo, hakuwa na uwezo wa kufanya lolote kuizuia pick up hiyo kuondoka kwa mwendo wa kasi.

‘Ninja’ aliwaza kwa mshangao. ‘Ninja Tanzania!’

Fahamu zilipomrudia Kombora alijikuta kaketi juu ya sakafu hali kaegamia ukuta, wasaidizi wake wawili wamelala chali; kila mmoja akiwa amekilaza kichwa chake juu ya paja lake moja. Walilala kwa utulivu, kila mmoja akiwa amekiacha kinywa wazi na kutokwa na macho nje. Haikimchukua Kombora muda kuelewa kuwa wote wawili walikuwa maiti. Alipatwa na mshituko mkubwa na kukurupuka wima huku akitazama huko na huko.

Ndio kwanza akagundua kuwa alikuwa katika chumba kisichokuwa cha kawaida, chumba kipana chenye kuta za chuma kisicho na mlango wala dirisha. Hewa chumbani humo ilikuwa nzito iliyojaa harufu ya kifo au maiti. Kombora alitazama huko na huko, akitafuta uwezekano wa kutoka katika chumba hicho. Hakuuona. Kwa kila hali, kilionekana chumba madhubuti kilichojengwa chini ya ardhi maalumu kwa ajili ya kumfanyia binadamu unyama.

Akayarudisha macho yake kuwatazama wasaidizi wake ambao sasa walikuwa marehemu. Kila dalili ilionyesha kuwa walikufa baada ya mateso makubwa ya kinyama. Mmoja alikuwa kavunjika shingo, jambo ambalo lilimfanya alale kama mzoga wa mbuzi. Na wa pili alikuwa na jeraha kubwa kifuani, ambalo lilionyesha kitu kigumu kilipenya humo na kuzifumua figo zake.

Kombora aliitazama saa yake. Dakika arobaini tu zilikuwa zimepita toka alipotoka ofisini kwake kufuata wito wa Koplo Shomari, ambaye sasa ni marehemu, ikimwarifu juu ya sanduku lililokuwa likisafirishwa toka ofisi Ya Kangaroo. Tayari watu wawili ni marehemu hali yeye akiwa hai kwa

fadhila au kebehi ya wauaji hawa. ‘Kwanini hawakumwua yeye pia? ’ kwa nini?’ alifoka kimoyomoyo akitembea huku na huko chumbani humo kwa uchungu. Hasira zilianza kumpanda zikamfanya asahau hofu aliyonayo juu ya maisha yake na kujikuta akijenga chuki kwa yeyote Yule aliyekuwa akimtendea haya. Alitamani ampate papo hapo, amchanechane kwa mikono yake na kuacha viungo vyake vikiliwa na fisi.

Hasira zilikuwa zikimcheka kichwani mwa Kombora, hasa zikisababishwa na unyama wa binadamu huyu ambaye hakuwa na shaka ni Kakakuona mwenyewe; bali jinsi alivyoufanya unyama wake mbele ya macho yake, hadharani, kana kwamba Kombora hakuwa lolote wala chochote mbele yake. Yeye, ambaye historia ya Tanzania na dunia kwa ujumla haitamsahau kwa mengi aliyoyatenda kuifanya serikali iendelee kuwepo na amani izidi kutawala nchini! Yeye ambaye jina lake tu lilikuwa sumu kali kwa yeyote aliyekuwa na ndoto za kuidhuru Tanzania!

Kamwe asingejisamehe kwa tukio hili la leo ambalo lilimfanya atoke ofisini bila kuaga, na kujikuta akisindikiza mzigo ambao hakujua ni wa nini. Asingejisamehe kuruhusu dereva wa pick up hiyo atoke nje na kuwazubaisha kwa maelezo marefu ya kebehi na mara ageuke kama chui ambaye alipaa angani na kuanza kuwachalaza kwa kong fu, judo na kareti kwa namna ambayo Kombora na umri wake wote katika ukachero hakupata kuiona.

Ilikuwa kama hadithi ambazo hutokea katika michezo ya sinema. Dakika moja walikuwa wima wakizungumza naye, dakika ya pili walikuwa wakigalagala chini kwa maumivu yasiyosemeka. Kwa mbali, kama ndoto, Kombora alihisi kumwona mtu mwingine akipambana kwa kiwango kama kilekile, kana kwamba hayati Bruce Lee amefufuka na anafanya vitu vyake. Lakini tukio au ndoto hiyo ilitoweka ghafla kwa mlio wa kutisha uliofuatwa na moshi mzito unaowasha, ambao ulimfanya Kombora aishiwe nguvu kabisa. Hakuwa na la kufanya wakati alipobebwana kutupiwa nyuma ya gari kama mzoga.

Wala hakuwa na neno alipohisi akinukishwa kitu fulani ambacho kilimfanya apoteze kabisa nusu ya fahamu alizobaki nazo. Na zilipomrudia ndipo alijikuta kaegemea ukutani. Maiti za vijana wake zikiwa zimelazwa juu ya mapaja yake kwa namna ya kumdhihaki.

‘Nitalipa kisasi’ kosa moja wamefanya kuniacha hai. Kwa vyovyote watalijutia.’

Wakati akiwaza hayo, alikuwa akitembea huko na huko kukikagua chumba hicho. Alikuwa na hakika kuwa kina mlango na dirisha, vinginevyo wao wasingeingizwa chumbani humu. Alikagua kwa makini kila sentimita ya chumba hicho. Haikumchukua muda kugundua sehemu aliyotaka. Nusu ya ukuta huo ulikuwa pande zito la chuma ambalo lilionekana kama mlango. Hata hivyo ilikuwa dhahiri kuwa lango hilo lilifunguliwa kwa umeme, toka nje ya chumba hicho.

‘Watafungua tu na watanikuta tayari nikiwasubiri.’ Kombora aliwaza akiupeleka mkono wake kuitafuta bastola kama alivyotegemea ilikuwa tayari imetoweka. ‘No problem, nitawasubiri na kupambana nao hata kwa meno.’

Mara taa ya umeme iliyokuwa inawaka chumbani humo ilizimwa, likafuata giza nene la kutisha. Kisha, ziliwashwa taa nyingi zaidi zenye Nuru kali kuliko giza lililokuwemo. Nuru hiyo ikafuatwa na joto kali ambalo dakika moja baadae lilimfanya Inspekta Kombora aanze kutapatapa huku tayari ameloa jasho.

“Karibu sana Inspekta Kombora’ sauti nzito ambayo haijulikani inapotokea, ilitamka ghafla kwa kiingereza. “Karibu kwetu. Karibu katika chumba cha mauti. Hajawahi binadamu yeyote kuingia humo akiwa hai na kutoka hai”

Sauti ikafuatiwa na kicheko ambacho binadamu yeyote asingekiita kicheko kwa jinsi kilivyokuwa hakina hisia zozote za binadamu.

Haikuwa sauti ngeni kwa Kombora. Wala Kombora hakuhitaji kufikiri sana ili kukumbuka alipata kuisikia wapi. Ilikuwa sauti ya mmoja kati ya wale wakurugenzi wawili wa Kangaroo, Paul na Philip.

“Nilijua kitambo kuwa mna kasoro fulani akilini mwenu” Kombora alifoka bila kujua kama anasikika au la. ‘Kama mlivyo na kasoro katika miili yenu.’ Alitamani kuongeza kwa hasira lakini hakufanya hivyo. Badala yake alisema “Kwahiyo mtindo wenu ndio huu, wa uoga na kujificha nyuma ya ukuta ndipo muweze kumkabili binadamu? Ni hili ambalo pia mmelifanya kwa msichana wa watu asiye na hatia.”

Kicheko kingine kibaya kilifuata. Kikafuatwa na sauti ileile ikisema, “Hatujifichi Inspekta, hatuna haraka ya kuonana nawe, kwa ujumla hatukuhitaji sana. Orodha yetu ilikuwa na watu wawili tu katika Tanzania. Wewe umejilazimisha na kuwa wa tatu. Hivyo, bado mmoja, Yule kijana mtukutu ambaye nyie mnamwita Joram Kiango. Baada ya muda mfupi tutakuwa naye hapa. Na hapo ndipo tutaanza kufanya vitu vyetu ambavyo mtavishuhudia kwa macho yenu wenyewe.”

“Mnataka kufanya nini?” Kombora hakustahimili kuuliza. Kicheko kingine cha kebehi kikafuata.

“Usiwe na haraka Inspekta. Uko hapa utajionea mwenyewe. Kwanza, lazima ujihesabu kama mtu mwenye bahati kuwa hai hadi sasa hivi. Ungeweza kuwa marehemu kama hao kuku wenzako waliolala hapo. Kwa bahati, bado tunakuhitaji. Tunahitaji uwe shahidi, uone kwa macho yako mwenyewe kile ambacho kitatokea nchi yako. Baada ya hapo utakufa kwa amani utapumzika kuzimu hali ukiwa na picha halisi akilini mwako, picha ya kupendeza ambayo kamwe haitafutika akilini mwako.”

Kombora hakuweza kumsikia vizuri. Joto kali lilimzidi kimo na kumfanya aanze kutapatapa kama samaki anayekaangwa akiwa hai. Aliruka huko na huko akiyavua magwanda yake, mishipa ya fahamu ikikaribia kupasuka, macho yake yalipoteza nuru na kizunguzungu kumshika ghafla. Polepole alijikuta akiteleza na kuanguka sakafuni, kando ya maiti ya vijana wale.

“Twende huku, ukamwone hawara yako mwingine aliyekuja kukusalimu,” Nuru aliamrishwa akiinuliwa toka sakafuni alipojibweteka na kusukumwa kama mzigo.

Mikono iliyomwinua toka sakafuni hapo ilikuwa mikakamavu yenye nguvu kama chuma. Hakuwa na hali ya kupingana nayo ingawa moyo wake ulimtaka sana kufanya hivyo. Mwili wake haukuwa na uwezo wala akili yake hakuiona kama ilifanya kazi kwa kiwango chake. Kwa ujumla alijiona kama kondoo au zezeta lililokuwa tayari kufuata amri yoyote ambayo alipewa na viumbe hawa wawili, amri yoyote ile; hata kama ingekuwa kujitumbukiza mwenyewe katika shimo ambalo lingempeleka moja kwa moja hadi kuzimu.

Kitu kimoja Nuru alikuwa na hakika nacho. Ukondoo au uzezeta haukumjia hivihivi kutokana na ukatili usioelezeka ambao aliushuhudia kwa macho yake mwenyewe ukifanywa na Kakakuona mbele yake, la hasha! Aliamini kabisa kuwa uzezeta huu ulitokana na sindano alizokuwa akichomwa mara kwa mara zilimfanya apoteze fahamu na zilipomrejea akajikuta mzembe akilini na mwilini kiasi cha hata kuwa mvivu na kukumbuka yote yaliyomtokea.

Kwa namna ya ndoto tu, alikumbuka yaliyomtukia kisiwani mara moja tu Joram alipoondoka. Alikumbuka jitihada zake ambazo zilisababisha vifo vya watu wawili kati ya wale waliokuja kumkamata, lakini waliobaki wakafanikiwa kumteka nyara. Alikumbuka alivyopelekwa Zanzibar na chongo kumwua mwenzie na kisha yeye mwenyewe kuuwawa. Alikumbuka pia kuwa mwenyenyumba Banduka, alivyouawa na kufichwa na Kakakuona ambaye alimrejesha Dar Es Salaam kwa mtutu wa bastola huku watu waliosafiri nao wakiwa hawana habari. Na alikumbuka alivyofika forodhani na kumwona Joram Kiango akiwa katika mavazi bandia yaliyomfanya asifahamike na yeyote zaidi yake.

Matukio ya kutisha zaidi, ambayo Nuru aliyakumbuka kama mabaya zaidi ni yale ya kuuawa kwa dereva wa teksi na msichana wa mapokezi, hadharani, mbele yake bila ya yeye kuwa na uwezo wa kufanya lolote. Mkono wake ambao aliutia haraka katikati ya miguu yake ili kuichukua bastola yake mbayo alikuwa ameificha mahali hapo, haukuweza kutoka na silaha hiyo kama alivyokusudia kwani ni wakati huohuo alipopigwa kitako cha bastola kilichomfanya azirai na kupokonywa bastola hiyo.

Na alipozinduka ndipo akajikuta katika chumba hiki, ambacho kwa kila hali, kilionekana kuwa kilichojengwa chini ya ardhi, maalum kwaajili ya kufanyia maasi au maovu. Na baada ya hapo ndipo alipoanza kudungwa sindano zilizomlewesha na kumpumbaza hata akawa hajiwezi, hajitambui. Kila dawa hizo zilipoisha nguvu alidungwa tena, jambo ambalo lilimfanya awe taabani daima.

Wakati akiwa taabani, kama ndoto vilevile, Nuru aliwaona watu wawili wenye maumbo ya ajabu wakimjia na kumtazama kwa muda mrefu. Mara mbili tatu watu hao walimvua nguo na kumchezea matiti na sehemu zake za siri kwa vidole vyao vikavu. Mara moja mmoja wao alijaribu kumnajisi, lakini Nuru alihisi kuwa alishindwa kwani hakuuhisi uume wake mwilini mwake. Hata hivyo waliendelea kumchezea wakifurahia kila kitendo chao.

Nuru alihisi kupata kuwaona watu hawa, lakini hakumbuki wapi. Watu wasiojiweza, wasio na viungo kamili, wanaoonekana kama walipata kutupwa katika tanuru la moto na kisha kutolewa kabla hawajateketea kabisa; aliwaona wapi? Mara kwa mara aliituma akili yake nzito kumfahamisha, lakini nayo haikuwa na jibu. Hivyo, alijikuta akiamua kuamini kuwa hakuna mahala popote ambapo aliwaona isipokuwa usingizini, katika moja ya zile ndoto zake mbaya ambazo humtokea binadamu mara chache katika maisha yake; ndoto za viumbe wa ajabuajabu wanaotisha ambao humwandama mtu usingizini na kumfanya aamke huku akitweta, jasho likiwa limemjaa mwilini tepetepe.

Kitu kikubwa kilichoisumbua zaidi akili iliyodumaa ya Nuru ni dawa hizo alizokuwa akilazimishwa kutumia. Baada ya kudungwa mara tatu alihisi mwili wake ukizitamani na kutaka apewe mara kwa mara. Ni jitihada kubwa sana zilizomfanya asitamke kwa sauti, kuomba tena au kuzidishiwa

Hili lilimtisha sana kwani alijua fika kuwa anachotumia ni kitu hatari kwa maisha ya binadamu. Kama haikuwa Cocaine basi ilikuwa Heroine au Mandrax. Hakuwa mtaalamu sana katika masuala ya madawa ya kulevya, lakini hicho kidogo alichofahamu kilimfanya aelewe kuwa alikuwa katika hatari kubwa wa kuwa teja wa dawa hizo, jambo ambalo lingemfanya apoteze akili, afya na hata uhai wake.

"Nimekwambia inuka, nenda kule ukamwone hawara yako mwingine," sauti ilimwamrisha tena Nuru akizidi kusukumwa kwenda mbele. Msemaji alikuwa akizungumza kiingereza.

Macho ya Nuru yalikuwa mazito kufunguka. Lakini alitumia akili yake kufikiri sauti hiyo. Haikuwa sauti ya Kakakuona. Ilikuwa sauti ya mtu mwingine. Hata lafudhi yake haikuwa ya Kiafrika. Nuru alihisi kuwa msemaji alikuwa Mjapan au Mchina. Akajilazimisha kufungua macho yake. Kwa taabu, aliweza kumwona mtu huyo. Alikuwa mrefu mwenye kifua cha simba ingawa alitembea kwa kunyata kama chui aliye mawindoni.

Nuru hakujisumbua kuwaza uwezo wa kupambana naye. Hali haikumruhusu. Hivyo, aliruhusu kusagwa kikondoo hadi katika chumba kingine ambacho kilifunguka baada ya mtu huyo kubonyeza tufe la umeme na sehemu ya ukuta huo kumeguka. Alisukumwa chumbani humo na kujikuta ameangukia mwili wa mtu mnene, wa makamo ambaye Nuru alimtambua mara moja.

'Inspekta Kombora.' Alinong'ona. Sauti haikutoka. Kando ya Inspekta huyo ambaye alilala nusu uchi, baada ya kuitupa suruali na shati yake huku na huko kupunguza joto kali ambalo lilimfanya azirai, Nuru aliona miili ya watu wawili ambao hakuhitaji kuambiwa kuwa wamekufa.

Hakushituka. Wala hakushangaa. Alikwisha vuka kiwango hicho.

Kwa Joram Kiango, ulikuwa usiku mfupi kuliko matarajio yake. Angependa sana uwe mrefu zaidi. Usimame, kama Biblia inavyodai jua lilisimama wakati Waisrael wakiwateketeza wapalestina ili waweze kushinda vita vile ambavyo viliwawezesha kuichukua nchi ya Ahadi. Lakini Joram hakuwa na bahati hiyo. Alipoitazama saa yake ilimwambia kuwa ilikwishatimia kumi na robo za usiku. Alihitaji saa sita zaidi ya kiza ili aweze kukamilisha awamu ya pili ya kazi yake.

Awamu ya kwanza alihisi kuwa ameitimiza. Ilikuwa kumtia adui jeraha la moyo ili naye apate uchungu na kuanza kutapatapa, kama ambavyo adui huyo aliamini Joram anatapatapa, kwa kuteketeza watu wasio na hatia, kumteka Nuru na hatimaye Inspekta Kombora.

"jeraha" ambalo litausononesha moyo wa adui huyo ni pale alipoamua kuteketeza maghala yake yote ambayo yalikuwa na mali ya mamilioni ya pesa za kigeni. Joram alihakikisha kila kitu kinateketea na kuwa jivu kwa moto aliouanzisha.

Hatua ya kutenda kitendo hicho, ambacho kilikuwa kinyume na desturi yake, Joram aliichukua ghafla mara baada ya tukio la saa chache zilizopita Barabara ya Morogoro.

Akiwa taabani kwa maumivu ya Moshi ule, ambao ulipenya hata kooni na kukwaruza, Joram alifanya haraka kukimbilia nyumba za jirani ambako aliomba maji na kunawa. Wakati akiondoka eneo hilo, alisikia kishindo cha watu waliozolewa na kutupwa katika pick up, na kisha kusikia ikiondoka kasi. Hakuwa na uwezo wa kufanya lolote.

Baada ya kunawa na macho yake kurudia hali ya kawaida alilirudia gari lake huku akipishana na watu waliokuwa wakitapatapa, baadhi yao wakipiga mayowe kwa maumivu na taharuki. Alilitia moto gari lake na kuifuata njia hiyohiyo ya Morogoro hadi alipofika ubungo ambako alipinda kushoto na kufuata barabara ya Mandela. Haikumchukua zaidi ya dakika kumi kabla hajaona kibao ambacho kiliashiria kuwa ameyafikia maghala ya kiwanda hicho.

Alisimamisha gari lake toka hatua kadhaa toka kibao hicho. Kisha, akavuka barabara kuyafuata majengo hayo ambayo toka hapo alipokuwa aliyaona kuwa yalikuwa makubwa kuliko alivyotegemea, alipoyafikia, kama alivyotegemea, alikutana na ukuta mkubwa uliyoyazunguka. Mbele ya ukuta huo kulikuwa na lango kubwa la chuma ambalo lililindwa na watu wawili waliovaa mavazi ya Jeshi la Mgambo. Joram alisita kwa muda akiwatazama.

Tangu alipoipata safari hii, hata kabla hajaamua kuifuata pick up ambayo iliwatorosha Kombora na wasaidizi wake, Joram alijua kuwa ingekuwa safari ya hatari. Alikuwa na kila hakika kuwa viumbe wale, kwa mujibu wa maelezo aliyoyapokea toka pande zote, hawakuwa watu wa kawaida na hivyo hawakuwa wakifanya biashara za kawaida. Hivyo, dhamiri yake kuu ilikuwa kuikagua biashara hiyo ili aelewe kabla ya kuwakabili viumbe wenyewe.

Hali kadhalika, alikuwa na mashaka kuwa mabohari hayo yalitumiwa kuficha maovu yao mengi, ambayo yaliwafanya wajiamini na kufanya maovu yao kwa dharau, bila hofu wala wasiwasi wowote. Kwa ujumla, licha ya biashara haramu kama dawa za kulevya au nyara za serikali, Joram alitegemea maghala hayo kuwa maficho ya kikosi cha mauaji ambayo yalikuwa yakiendelea nchini. Na alijiandaa kwa hilo.

Ambacho hakujiandaa nacho ni kukutana na ninja. Kamwe hakutarajia kuwa watu hao, ambao pamoja na ukatili wao walionekana wapuuzi, wangefikia hatua ya kumleta ninja nchini, ili waweze kufanikisha adhma yao.

Sio kwamba Joram alimwogopa ninja. Kinyume na watu wengi yeye alifahamu kuwa ninja ni binadamu kama binadamu wengine. Kilichowapa umaarufu, licha ya ukatili wao, ni upya wa taaluma yao machoni mwa watu kiasi cha watu kuondokea kudhani kuwa ninja ni zaidi ya kuwa binadamu wa kawaida.

Joram hakuwa ninja, lakini taaluma ya uninja iliiva kichwani mwake sawa na ninja yeyote yule. Alichokosa ni Master ambaye angeweza kumtangaza U-ninja kwa kumpa baraka ambazo angeambatana nazo maishani.

Lakini hilo halikumsumbua hata chembe. Kwa kiwango chake, baada ya visa na mikasa yote iliyomkumba wakati akiishi nchini Marekani, hakuhitaji mwalimu ambaye angemtangaza rasmi kwani hakuwa katika kikundi chochote wala ukoo wowote ambao ulihitaji kumkubali au kumkataa.

Joram aliipata taaluma ya u-ninja kwa gharama ya sehemu kubwa ya jasho na damu yake, nusura imgharimu roho yake. Alianza kwa kujiunga na vyuo vidogovidogo vya kareti na judo, ambavyo wakati huo vilienea sana nchini Marekani. Jitihada zake kubwa zilifanya apendwe na walimu wake ambao baada ya kumfundisha kila walichojua walipendekeza vyuo vingine hadi alipojikuta katika chuo kile ambacho kilikuwa kikifundishwa na hayati Bruce Lee mwenyewe.

Joram alikuwa mtoto mweusi pekee katika darasa hilo. Lakini jitihada zake na uwezo wake wa kuzingatia kila alichofundishwa kilimfanya awe kipenzi cha hayati huyo, jambo lililomfanya achukiwe na wanafunzi wenzake wote shuleni hapo.

Kifo cha kutatanisha cha hayati Bruce Lee kilipotokea, Joram alihisi kama aliyepotelewa na baba au kaka yake wa damu. Alikosa raha kwa siku kadhaa. Baada ya msiba alijaribu kutafuta chuo kingine ambacho kingemfaa, lakini alijikuta akipoteza muda wake bure kutokana na jinsi mbavyo alijiona amevuka kiwango cha mafunzo mengi yaliyotolewa kitaaluma na kivitendo. Hivyo, mafunzo mengi kwake ilikuwa kujikumbushia tu.

Hali hiyo ilimwongezea uadui hata miongoni mwa walimu. Wako walimu wa Kichina na Kijapan ambao waliamini kuwa taaluma hiyo ni maalumu kwa ajili yao tu. Hivyo, hawakuona haki ya mgeni kuifahamu kama wao au zaidi ya wao. Na wamarekani hawakuona haja ya mtu mweusi kutamba mbele yao. Hivyo, kila ilipotokea nafasi, Joram alijikuta akiingia katika ugomvi ambao hakuujua chanzo chake. Lakini aliibuka mshindi katika kila tukio. Baadaye walianza kumshambulia katika vikundi. Bado mara kwa mara Joram alivisambaratisha au kutoroka bila matarajio yao.

Lakini ilitokea jioni ya siku moja, akiwa katika viwanja vya mazoezi peke yake, Joram alijiwa na mtu aliyevaa mavazi meusi kiasi cha kufunika mwili mzima isipokuwa macho tu. Alikuwa akitembea harakaharaka lakini kwa kunyata kama kivuli. Joram hakuitaji kuambiwa kuwa alitembelewa na ninja. Alikwisha soma habari zao katika vitabu vingi, ingawa hakupata kukutana ana kwa ana.

“Joram Kiango?” mgeni huyo alimwuliza.

“Kama ndiye?” Joram alimjibu kwa swali jingine.

Mgeni huyo alimtazama toka miguuni hadi utosini. Akaonyesha kuridhika na alichokiona, “Nimekuwa nikizisikia sifa zako. Nimekuja nione kama ninachokisikia ni kweli. Uko tayari?”

Joram hakuwai kukataa kupambana na mtu yeyote, hasa anapoonyesha shahuku ya kumjaribu kama huyo. Alimkubalia na kujiandaa. Adui yake alimtazama kisha akaanza kunyata huku na huku, kabla hajapata fursa ya kuachia pigo ambalo lilikingwa na Joram kirahisi. Pigo hilo lilikuwa kama la kumzindua tu kwani wakati huohuo alifyatuliwa miguu kwa namna ambayo hakuitegemea na kujikuta akiviringika. Mara tu alipoinuka alifyatuliwa tena. Wakati huohuo akiwa amekwisha jiandaa alianguka hali akiachia teke ambalo lilimpata adui yake tumboni na kumfanya apepesuke. Aliviringika toka sakafuni hapo na kumfuata adui yake ambaye aliruka na kudaka miti ya mazoezi ambayo aliitumia kukimbia kwa mikono kama nyani. Wakati Joram akiwa ameduwaa kwa hilo adui huyo alichupa hewani kama chui na kutua juu ya kifua chake.

Kilichofuata ni kitu ambacho Joram hatokisahau hadi leo. Vipigo vilimnyeshea kama mvua. Hakupata fursa kujitetea kwani alipouinua mkono wake ulikuwa hauna kazi, hauna nguvu. Walimwokota hapo, dakika ishirini baadaye, walimpeleka hospitali moja kwa moja, ambako alipimwa na kugundulika kuwa alivunjika mkono, mbavu tatu na kuteguka mguu.

Alikaa hospitali mwezi mmoja. Aliporuhusiwa kutoka, hata kabla ya POP halijaondolewa alianza mazoezi. Na mara lilipoondolewa, wiki tatu baadaye, alikuwa safarini toka mjini Washington kuelekea mjini Carfornia ambako alisikia kuna mwalimu wa kichina aliyekuwa akitoa mafunzo ya U-ninja kwa "wateule" wachache aliodhani kuwa wanafaa. Joram aliondoka bila kuwaaga wazazi wake ambao walipinga hatua yake ya kujihusisha na mambo hayo.

Ilimchukua wiki nzima kugundua kilipojificha. Chuo hicho kilikuwa katika moja ya misitu mikubwa iliyokuwa haijaanza kutumika ya mtengenezaji mmoja mashuhuri wa filamu katika mji wa Hollywood. Chuo hicho kilikuwa kinaongozwa na mzee mmoja mfupi, mnene mwenye upara uliomeza robo tatu ya kichwa chake. Mzee huyo alimtazama Joram kwa macho yaliyojaa chuki na dharau dakika mbili nzima kabla ya kumjibu kwa swali, "alikuambia nani kuwa nafundisha taaluma hiyo? Na hata kama, nitamfundishaje panya mchezo wa paka?"

Joram alitumia hekima yake kubembeleza na kusihi hadi alipoona mwalimu huyo akianza kumsikiliza kwa makini "Unadhani unafahamu nini juu ya taaluma hii?" mwalimu huyo aliuliza.

"Sifahamu chochote"

"Kwa hiyo, unifahi, sifundishi watu mbumbumbu."

Joram alipozidi kumbembeleza mzee huyo alipiga makofi. Mara miti iliyokuwa imeenea eneo hilo ikapata uhai. Zaidi ya vijana sita, ambao Joram hakujua kuwa walijificha juu ya matawi hayo wakimtazama, waliruka na kutua chini wakiwa wamemweka kati. Joram alimfahamu mmoja wao. Alikuwa Yule ambaye majuzi tu alimfanya alazwe hospitali kwa mara ya kwanza maishani mwake.

"Niondoleeni mbele yangu hii takataka" mwalimu huyo aliamrisha.

Mara vijana hao wakageuka mbogo. Kwa pamoja walimvamia joram na kuanza kumshambulia. Akijua kuwa huu ulikuwa mtihani mbele ya mkufunzi huyo Joram alichachamaa na kupigana kwa nguvu zake zote na moyo wake wote. Dakika mbili baadaye watatu kati ya hao walikuwa wakigaragara chini, hawajitambui. Joram mweyewe akiwa taabani, lakini hakukubali kushindwa. Muda si mrefu aliwatupa wawili wengine na kujikuta amebakiwa ana kwa ana na yule mkuu. Wote walitweta kama majogoo yanayoogopana baada ya Joram kuikwepa kila hila iliyofanywa na kijana huyo.

"Inatosha." Mkufunzi huyo alisimamisha pambano, uso wake ukionyesha kufurahishwa sana na alichokiona "Pumzikeni, kesho tutaangalia ambacho tunaweza kufanya kwa mgeni wetu huyo machachari."

Joram aliliona jicho la chuki likimtazama toka kwa kijana huyo.

Kesho yake, bila ya mwalimu huyo kujua chuki baina yao bado alimkabidhi Joram kwa kijana huyo ili ampe zoezi kabla hajaanza kumfundisha mwenyewe.

Kijana huyo ambaye baadaye Joram alifahamu kuwa anaitwa Adrian, mchina aliyechanganyika na Mmarekani, aliondokea kuwa mwalimu, hasa kwa Joram. Kutwa nzima ambayo alimchukua porini alimtesa kwa kumpa adhabu za kutisha, huku akitamba kwa kumwonyesha Joram ujuzi wake katika hila ambazo wengi hudhani ni mazingaombwe, mbinu za kuruka ambazo wengi hudhani ni miujiza, kuparamia miti ambako baadhi wanafikiri ni uwezo utokanao na mitishamba, kuzua moshi ambako hata Joram alidhani ni uchawi n.k.

Yote hayo Adrian aliyafanya kwa kujisifu, kwa nia ya kumwonyesha Joram kuwa hajui kitu. Lakini hakujua kiasi gani Joram alikuwa akiyafuatilia yote hayo na kuyachora katika ubongo wake.

Jioni moja Master alitangaza mwenyewe kuwa angeanza kumfundisha Joram. Usiku huohuo Adrian alimnong'oneza Joram, "Hii sio taaluma ya nyani weusi. Kesho alfajiri ondoka urudi kwenu. Ukiendelea kukaa hapa mpaka jioni nitakuua."

Joram alimpuuza lakini kilichotokea mchana huo kilimfanya aamini kuwa Adrian hakuwa na mzaha. Mwalimu alikuwa amekwenda nje ya kambi na kuwataka waendelee na mazoezi. Adrian alimwita Joram na kumtaka amfuate ili amwonyeshe kitu ambacho hakupata kukiona huko nyuma. Walipofika katikati ya kichaka, Adrian ghafla aligeuka mbogo na kuanza kumshambulia Joram. Mapigo yake yote yaliashiria kuua. Kwa bahati mbaya hakujua Joram amejizatiti kiasi gani. Baada ya dakika arobaini za mapambano, Joram alikuwa amelowa jasho na damu, mkono wake mmoja ukiwa haujiwezi. Lakini Adrian alikuwa chini, chali, nusu maiti.

Joram alijikongoja na kumburuza hadi kambini ambako alikutana na macho makali ya Master akimsubiri kwa ukali.

“Wewe ni mnyama. Huyu ni mwanangu, mwanangu wa pekee. Tazama ulivyomfanya! Sasa nakuamuru uondoke mara moja katika kambi yangu. Ukiendelea kukaa, dakika moja zaidi nitakuua kwa mikono yangu mwenyewe.”

Joram hakuwa na hili wala lile zaidi ya kuondoka.

Naam, Joram hakuwa mgeni wa maninja. Hata hivyo, kitendo cha ninja huyo kumdhihaki na kuondoka na mtu mkubwa kamaa Inspekta Kombora mbele ya macho yake, kilimwongezea hasira na kumpa ari ya kuteketeza bidhaa hizo bila huruma.

Wale walinzi wawili waliovaa mavazi ya mgambo hawakumpa shida. Alichofanya ilikuwa ni kuwanyemelea hadi mita nne nyuma yao, kisha akachupa hewani na kutua huku wote wawili wakiwa chini yake. Kabla hawajafahamu kinachotokea alikwishawagonganisha vichwa mara kadhaa hata wakapoteza fahamu. Baada ya hapo aliwafunga kamba za mikono na miguu, akawatia matambara mdomoni ili watakapozinduka, wasiweze kupiga kelele na kisha akawavuta na kuwalaza katika kibanda chao cha ulinzi.

Kwa kutumia funguo zake malaya aliufungua mlango wa geti na kisha kushughulika na makufuli ya kuingilia ghalani. Ilimgharimu dakika kumi, ambazo Joram aliona kama miaka kumi hadi makufuli yalipokubali. Alipigwa na butwaa kwa wingi wa mali zilizokuwemo humo ndani. Jengo zima lilifurika kwa makatuni yaliyopangwa vizuri hadi kufikia kabati. Joram alishusha baadhi ya makatuni na kutazama majina yake, Glamorous Perfume, Glamorous Cream, Glamorous toilet soap, Glamorous powder, n.k.

Joram alikumbuka kuona matangazo ya bidhaa hizo katika magazeti na televisheni. Aidha, alipata kusikia yakitangazwa pia katika redio. Akiwa mtu ambaye hajishughulishi na vipodozi, hakuyatilia maanani matangazo hayo.

Hata hivyo, alikuwa na uhakika kuwa hazijaanza kuuzwa nchini kwakuwa tangazo moja lilikuwa likitangaza tarehe ambayo bidhaa hiyo ingeanza kusambazwa kote nchini. Hakutegemea kama bidhaa inayoingia nchini kwa majaribio, ambayo ilitajwa wazi kuwa ingeanza kutumika duniani kwa mara ya kwanza, ingeweza kuletwa kwa wingi kiasi hicho.

‘Bahati yao mbaya, itabidi walete mali mpya,’ aliwaza wakati akipanda juu ya masanduku hayo na kuchokonoa umeme. Kuanzisha moto ukiwa mchezo mdogo kwake, haikumchukua nusu saa kuona nyaya za umeme alizozitegesha zikianza kusafirisha moto ambao utakapokutana mlipuko usingekuwa wa kawaida.

Alifanya hivyo katika jengo la pili pia. Kisha, akatoka nje na kuwaburuza walinzi wale wawili hadi barabarani ambako aliwafungua kamba na kuwaacha wakiwa wameduwaa. Akapanda gari lake na kulitia moto, akilielekeza mjini.

Kabla hajafika popote mlipuko wa kwanza ulitokea. Ulifuatiwa na moto mkubwa ambao ulifanya usiku ugeuke mchana. Mlipuko wa pili ulimkuta keshafika mjini.

Ukubwa wa mlipuko na ukali wa moto toka katika maghala hayo ulimshitua karibu kila mtu katika maeneo ya Tabata, Buguruni, Ubungo na kwingineko. Watu wengi waliamka na kuutazama kwa hofu, huku vibaka wakifukuzana kwenda katika eneo hilo kwa matumaini ya kujipatia chochote. Hakuna kilichopatikana. Hata zima moto ambao walifika katika eneo hilo, nusu saa baadaye, waliduwaa wakiutolea macho moto huo jinsi ulivyokuwa unatafuna na kuteketeza kila kitu katika majengo hayo. Hakuna aliyethubutu kuusogelea.

Taarifa za kuungua kwa maghala ya Kangaroo iliwafikia wakurugenzi wa kampuni hiyo, Paul na Philip, dakika arobaini baadaye. Walikurupuka toka katika ofisi yao, ambayo kwa juu yalikuwa makazi yao na kujikongoja kulielekea gari lao.

“Number One!” mmoja aliita. Alipoita mara ya pili kile kilichoonekana kama kivuli, ambacho kilisimama katika kivuli cha mchongoma ulioizunguka ofisi hiyo, kilipata uhai na kuwaendea kwa mwendo wa kunyata.

“Tulikuajiri kwa kazi moja tu” Philip alisema kwa sauti yake ya mkwaruzo. “Kumpata Joram Kiango na kumleta kwetu akiwa hai, wewe umekaa hapa kivulini wakati yeye anatufanyia madhara ghalani. Twende tuone ni kiasi gani cha madhara alichotufanyia”

Number One hakuwajibu. Hakuwa mtu wa maneno mengi isipokuwa vitendo. Zaidi, alikuwa na mashaka kuwa waajiri wake hawa walikuwa na dosari katika vichwa vyao kama ilivyokuwa katika miili yao. Hakupata kuwaelewa hata mara moja. Hata hivyo, alilazimika kuwatii kwa kuwa tu alihitaji pesa zao ambazo aliziona kama za bure kwa wepesi wa kazi waliyomtajia.

5

Si kawaida ya ninja kukodiwa kwa kazi ya aina hii. Lakini dunia ilikuwa imebadilika kitambo. Akiwa ametulia hotelini kwake mjiniCalifornia, asubuhi hiyo alifuatwa na ajenti wake ambaye alimwambia kuwa kuna kazi ya kufanya nje ya nchi.

“Wapi?”

“Afrika”

“Nchi gani?”

“Tanzania”

Hakujua Tanzania. Kwa ujumla nchi za Afrika alizozifahamu ni Naijeria na Cameroon kwa ajili ya mpira; Uganda kwa ajili ya vituko vya Idd Amin, Kenya kwaajili ya utalii na Afrika Kusini kwa ajili ya Mandela Tanzania haikuwemo kabisa katika ramani ya kichwani.

Lakini baada ya kukutana na watu hao waliomuhitaji, ambao nusura wamfanye aangue kicheko kwa maumbile yao, alijikuta akiijua Tanzania. Ilikuwa baada ya kutajiwa jina la mtu ambaye alitakiwa wamkamate, Joram Kiango, alikuwa hajamsahau. Hakuwa na uwezo wa kusahau kipigo ambacho “nyani” huyo anayejiita Joram Kiango alimpa, kipigo cha kwanza katika maisha yake. Hivyo, aliafiki mara moja.

Kumkamata Joram lilikuwa jukumu la pili la kwanza lilikuwa kumfuta duniani “nyani” mwingine anayeitwa Kakakuona, kwa kosa la kushindwa kumpata Joram na kuhatarisha harakati zao kwa kufanya mauaji kwa fujo, kimachomacho. Jukumu hilo alilitekeleza kwa urahisi sana, hasa baada ya kuandaliwa silaha safi ya aina yake, ambayo alikuwa akiisikia tu katika simulizi za kihistoria. Kidole chake cha shahada kilipoifyatua bunduki hiyo na kumfanya binadamu, ambaye alikuwa kando ya barabara, atoweke kama tufe la barafu, lililoyeyuka ghafla, alijisikia kama mungu.

Baada ya kazi hiyo ndipo alipotakiwa kumnasa Inspekta Kombora ambaye waajiri wake walidai kuwa anajitia “kimbelembele” ambacho kinawea kuwaharibia mipango yao kabla hawajampata Joram. Haikuwa kazi kubwa kumtia mikononi. Wakiwa na hakika kuwa makachero wake wanaichunguza nyumba hiyo kwa uficho, na wakiyasikiliza maongezi yake baina yake na vijana wake, ingawa walitegemea mfasiri kuwafahamisha kwa kiingereza, iliwagharimu kutumia hila za kizamani, ya kupakia sanduku katika pick up na mara wakamsikia akimwambia kachero wake kuwa anakuja.

Tatizo pekee katika kumnasa Kombora ni pale alipotokea mtu ambaye hakujulikana na kuanza kupambana naye. Number one hakumtegemea. Na zaidi alishangazwa na uwezo wake wa kupigana ambao ulimfanya ashindwe kuamini kuwa anapambana na binadamu wa kawaida kwani hakuna

binadamu wa kawaida ambaye alipata kumpa shida kama huyu. Wingi wa watu ambao walianza kujazana na ufupi wa muda aliokuwa nao, vilimfanya Number one atumie njia ya uoga, ya kupiga lile bomu la moshi unaowasha, na kuitumia fursa hiyo kuwachukua mateka wake na kuwarejesha mjini.

Ni wakati alipokuwa akiendesha pick up hiyo kurudi mjini, ndipo ilipomjia akilini kuwa aliyekuwa akipambana naye hakuwa mwingine ila ni Joram Kiango. Miaka mingi waliyotengana ilimfanya aanze kumsahau lakini asingeusahau upiganaji wake usio kifani. Alijilaumu kuruhusu, kwa mara nyingine, aponyoke toka mikononi mwake kama samaki aliyepenya toka kinywani mwa mamba. 'mwanaharamu yule, ama zake ama zangu,' aliwaza akiwageukia Philip na Paul ambao walikuwa wakiendelea kusema kitu ambacho hakuwa amekisikia.

"Tunasema twende huko ghalani tukaone madhara yaliyosababishwa." Paul alisema akiingia nyuma ya benzi lao na kufuatiwa na Philip. Number one ambaye jina lake lingine la bandia katika hati ya usafiri lilikuwa Newton Kelly, aliingia mbele na kulitia moto gari.

Ingawa alikuwa na siku tatu tu tangu alipoingia Dar es Salaam, lakini ramani alizopewa na jinsi alivyoutumia muda huo mfupi kulivinjari jiji tayari alikwishakuwa mwenyeji. Hakuhitaji kuelekezwa, wala hakusubiri kuamriwa afuate njia ipi. Badala yake alikanyaga petrol na kuacha gari liteleze kuifuata UWT na baadaye, Maktaba, hadi Samora ambako aliichukua uhuru na kuambaa nayo hadi Buguruni. Alipofika Mandela alipinda kulia na kuelekea Tabata.

Toka hapo macho yao yalivutwa na moto mkubwa ambao uliufanya usiku huo uonekane mchana. Philip na Paul hawakuyaamini macho yao walipoona kuwa moto huo ulikuwa ukiiteketeza hazina yao yote, hazina ambayo pia ilikuwa ndoto yao pekee ambayo waliiweka akilini kwa miaka zaidi ya sita na kuigharamia kwa kila senti waliyokua nayo. Waliutazama moto huo kwa huzuni, hisia zao zikionyesha ni miili yao inayoteketea katika majengo hayo, badala ya mafuta ya kujipaka na vipodozi. Mmoja wao alitokwa na sauti ya kilio bila machozi, hali mwingine alitokwa na machozi bila kilio.

Number one aliwatazama kwa mshangao jinsi walivyobadilika. Alitamani kucheka lakini hakuthubutu. Alitamani kuwahurumia, lakini hakujisikia. Hakuona vipi tukio kama hilo, kwa wafanyakazi wakubwa kama wao, liwe kama mwisho wa dunia. "Kwani hamna bima?" aliwauliza. Hakuna aliyemjibu. Badala yake Philip alimgeukia na kumkazia macho. Baada ya muda, kama anayezungumza peke yake, alisema, "Najua hii ni kazi ya Joram Kiango. Mwanaharamu, kwa mara nyingine ametutia kilema. Kwa bahati mbaya safari hii ametutia kilema cha moyo badala ya mwili. Unasemaje Paul?"

Paul aliendelea kulia.

Philip akamrudia Number one, "Kelly" kwa mara ya kwanza alimwita kwa jina lake, kinyume na maafikiano yao.

"Tumekuhaidi ngapi kwa kutuletea Joram Kiango?"

Number one hakukumbuka. Tangu alipojua kuwa mtu wake ni Joram kiango alijikuta amesahau malipo ya kazi hiyo na kuifanya yake binafsi, kwa nia ya kulipa kisasi.

"Ngapi?" Philip alirudia. "Okey pengine hamna haja ya kutaja. Ninachosema ni hiki. Tunamtaka Joram Kiango usiku huu huu; awe hai au amekufa. Tutakulipa mara kumi ya chochote tulichokuhaidi. Upo?"

Number one alikubali kwa kichwa.

"Usiku wa leo." Philip alisisitiza. Kabla ya kesho tutakuambia wapi amejificha. Unasemaje Paul?

Joram Kiango pia alikuwa ameapa kuwa usiku huohuo angemaliza "unyama huu wa kipuuzi." Mara tu alipohakikisha moto aliouanzisha umepamba moto, alifika mjini na kuliegesha gari lake mbele ya kiwanda cha printpak. Kisha, akatembea kwa mguu kurudi hotelini kwake ambako alikisikiliza chombo chake cha kupokelea ujumbe wa simu zake.

Akafahamu kuwa Inspekta Kombora alikuwa hajarudi na kwamba vijana wake walikuwa wakitapatapa kwa “kutoweka” huko kwa afande wao. Aidha, mtu wake wa kampuni ya simu alimwarifu kuwa bado ilikuwa vigumu kunasa maongezi ya ofisi ya Kangaroo kutokana na mitambo iliyotengwa kuepusha jambo hilo. Habari alizotegemea toka nje juu ya wakurugenzi wa Kangaroo zilikuwa bado hazijapatikana. Akakitegesha tena chombo hicho na kusimama.

Uchovu aliokuwa nao haukuwa na kifani; alitamani kuingia bafuni aoge. Alikitamani kitanda chake, lakini hakuweza kufanya lolote kati ya hayo kila alipokuwa akiitazama saa yake ilikuwa ikimkera kuona mapambazuko yakikaribia. Hivyo, alijinyoosha, akachunguza vifaa vyake vyote vilikuwa kamili katika mifuko yake ya siri. Kisha, akakifunga chumba chake na kutoka.

Hakuhitaji gari, alipenya vinjia vya uchochoroni na akiiendea ofisi ya Kangaroo. Nyumba mbili kabla ya kuifikia ofisi hiyo, alitafuta uchochoro na kujificha, macho yake yakiwa kazini kulitazama jengo hilo kwa makini.

Matumaini ya Joram yalikuwa kwamba taarifa za kuungua kwa maghala yao zitakapowafikia wakurugenzi hao wasingesita kutoka kwenda kutazama uharibifu uliotokea. Fursa hiyo alihitaji ili aingie katika jengo hilo na kumtoa Nuru kabla hajawashughulikia wendawazimu hao.

Kama alivyotegemea, haikupita robo saa kabla hajaona benzi likitoka eneo hilo kwa mwendo wa kasi kuifuata UWT. Aliwapa dakika tano kisha aliiendea ofisi na kushughulikia geti ambalo halikumchukua dakika mbili. Alilifunga nyuma yake na kuliendea lango akipenya katika kivuli cha michongoma.

Joram alikuwa na taarifa zote jinsi jengo hilo linavyolindwa kwa umeme. Alifahamu fika kuwa kwa kugusa mlango au dirisha ovyo angekuwa amejichongea kwa kutoa ishara ambayo ingeweza kuwafikia wakurugenzi hao huko huko waliko na hata kituo cha polisi. Hali kadhalika, alijua kuwa ndani ya jengo hilo kuna milango ya siri ambayo isingeweza kufunguka bila ya kujua hila ambazo hutumiwa. Ni hayo ambayo yalimfanya Joram ahitaji ramani za jengo hilo au mhandisi aliyelishughulikia. Lakini baada ya kusikia kilichomtokea mhandisi huyo, na kunasa maongezi ya kikosi cha Kombora juu ya ramani ya jengo hilo, hakuona kama alikuwa na muda wa kutosha zaidi ya kufanya kile ambacho waingereza ukiita short in the dark, kujituma kazini.

Kwa mujibu wa taarifa za kikosi cha Kombora, na kile alichokiona mwenyewe Kakakuona alipojituma kupitia jengo la Sunrise na kutokea Kangaroo, Joram alikuwa na uhakika kuwa nyuma au chini ya meza kulikuwa na njia ya siri ambayo ama ilifunguka kwa kubonyeza tufe lililofichwa ukutani au kwa chombo maalumu cha mkononi. Joram hakupenda kupitia njia hiyo kwa kuhofia kupotezewa muda na makachero wa Kombora ambao pia wangeweza kumharibia mambo. Hali kadhalika, alijua jicho la adui linatazama upande huo baada ya Kakakuona kukorofisha. Hivyo, aliamua kutumia mlango wa mbele.

Akiwa amejiandaa kwa vifaa vya umeme, Joram alitafuta hadi alipopata nyaya za umeme. Alizifuata hadi zinapoungana na zile za ndani. Akashughulika nazo kwa dakika kadhaa na kufanikisha kutegesha chombo chake maalumu ambacho kina nguvu ya kuvuruga mpangilio wote wa vifaa vya umeme katika jengo kiasi cha mitambo iliyotegeshwa kushindwa kufanya kazi. Baada ya hapo alitumia funguo zake malaya kufungua ofisi hiyo na kuingia. Alihofia kuwasha taa za umeme ambazo zilikuwa zimezimwa. Akatumia tochi yake ndogo yenye ukubwa wa kalamu kumulika hapa na pale hadi alipoipata ofisi ya wakurugenzi. Alihangaika na makasha mbalimbali na kupekua nyaraka hizi na zile hadi alipoona kuwa alikuwa akiupoteza bure muda wake. Akageuka ukutani na kumulika hapa na pale, akipapasa hapa na kutomasa pale hadi alipata kitu alichokuwa akikihitaji. Picha moja ukutani hapo ilikuwa imficha tufe moja lenye namba toka 0 hadi 9. Joram alicheza na namba hizo kwa dakika kama kumi. Wakati akikaribia kukata tamaa, kama ndoto, aliona nusu ya ukuta huo ikimeguka na kumruhusu kuingia katika chumba kipana, cha siri. Hicho ndicho chumba alichokihitaji.

“wewe malaya, inuka hapo ulipo, kuja hapa,” sauti yenye mkwaruzo , iliyojaa chuki na hasira ilimwashiria Nuru.

Ilikuwa sauti Philip, Paul akiwa nyuma yake. Ndio kwanza walikuwa wamerejea toka kushuhudia hasara kubwa waliyoipata. Wakiwa wamejawa na hasira, akili yao ilikuwa najambo moja tu akilini, kuua, hawakuweza kushuku chochote walipoingia katika jengo lao hilo; kupita katika ofisi ya siri hadi katika chumba cha mateso.

Nuru alijikongoja kuinuka toka sakafuni alipolala, kando ya Kombora. Akawaendea na kusimama mbele yao akitetemeka. Hasira zilimjaa moyoni, lakini macho yake yalijaa upole yakiomba kitu ambacho akili yake haikumruhusu kutamka. Kilio chake kilikuwa wazi machoni mwa Philip na Paul. Pamoja na hasira zilizowajaa rohoni, walitazamana, wakacheka.

“Unataka chakula chako sio?” Philip alimkebehi, “Leo hutapata chakula chako, mama. Tunakutaka uwe mzima na akili zako zote ili ufe huku unaona. Usikie kila ladha ya kifo hadi roho yako itakapokutoka. Upo mpenzi?”

“Na nitakuambia jambo jingine la kupendeza,” Paul aliongeza. “Kabla hujafa utashuhudia kifo cha hawara yako Joram Kiango. Wakati wowote kuanzia sasa ataletwa hapa akiwa hai au maiti. Tutapenda umpatie busu la mwisho kabla hamjaagana na kuanza safari yenu ya mwisho ya kwenda motoni.”

Inspekta Kombora aliyasikia yote hayo hali kalala chali juu ya sakafu. Alikuwa akilaani kila dakika ambayo ilikuwa ikimfanya aendelee kuwa shahidi wa unyama huo bila uwezo wa kufanya lolote. Aliiona bastola moja iliyoshikwa kizembe katika mkono mmoja wa Paul. Angeweza kabisa kuipokonya bastola hiyo kirahisi na kisha kuvifumua vichwa vyao wote wawili kabla hawajajua kinachowatokea. Kilichomzuia kufanya hivyo ni hali aliyokuwa nayo. Sindano waliyomchoma mara tu alipozinduka baada ya lile joto la kutisha ilimlegeza kila kiungo na kumlegeza akili. Alijiona kama dubwana ambalo lingeweza kuambiwa “lala vizuri tukuchinje” likalala bila kipingamizi. Pamoja na ukweli kwamba alijaribu kupambana na hali hiyo, bado alijua fika kuwa anajidanganya. Hakuwa na hali.

Hilo Kombora alilifahamu tangu alipoona miili ya vijana wake ikiburuzwa kama mizoga ya mbwa na kutumbukizwa ndani ya shimo chumbani humo. Shimo hilo, mara tu lilipofunuliwa liliruhusu harufu mbaya isiyostahimilika ambayo iliashiria kuwepo kwa maiti nyingine nyingi zilizoachwa kuozea humo. Alijaribu kuinuka awatetee vijana wake. Hakuweza. Alipojaribu kufoka sauti haikutoka. Alichoambulia ni kutoa macho tu, kama kondoo.

“Unajua kwanini mnakufa leo?” Philip aliendelea kumsimanga Nuru, “Mnakufa kwaajili ya roho zenu mbaya. Mnakufa kwaajili ya tamaa yenu ya fisi. Mnakufa kwakua nyie sio watu, ni mijibwa tu isiyostahili kuishi.”

“Inatosha Philip, inatosha sana. Huna haja tena ya kuendelea kumnyanyasa msichana huyo asiye na hatia yoyote,” Sauti kubwa, iliyowazi na inayojiamini ilisikika ghafla chumbani humo na kuwafanya Philip na Paul watazamane kwa hofu kubwa.

Ilikuwa sauti ambayo kamwe Nuru asingeweza kuisahau, sauti ya mtu aliyempenda zaidi ya alivyojipenda mwenyewe. Sauti ya Joram Kiango. Ilimfanya Nuru ahisi akipata nguvu mpya.

Mara sehemu ya ukuta chumbani humo ikamenyeka. Umbo refu, lililokakamaa; la Joram Kiango likaingia taratibu, hatua moja baada ya nyingine. Akiwa amevaa suti yake nyeusi, iliyochafuka kwa mavumbi machoni mwa Nuru alionekana mchovu kupita kiasi, lakini macho yake yalikuwa maangavu yakitoa nuru ambayo Nuru asingeweza kuisahau kila aionapo; Nuru ya ushindi. Mkononi alikuwa na bastola ambayo ilimwelekea Philip, lakini hakuijali sana. Alimwendea taratibu na kusimama mbele yake. Akamtazama kwa muda mrefu. Kisha alikizungusha kichwa chake na kumpokonya bastola hiyo ambayo aliitumbukiza katika moja ya mifuko yake. “wewe, umeingiaje humu ndani?” Philip alifoka baada ya kupigwa na butwaa muda mrefu.

“Wewe ni Joram kiango?” Paul naye alipata sauti yake.

“Naam, nadhani mlikuwa mkinitarajia kwa muda mrefu. Sioni kwanini mshangae kuniona,” Joram aliwajibu kwa kebehi huku akiwatazama.

Macho yao yalijaa chuki, hasira na kisasi kwa kiwango ambacho Joram hakupata kukiona. Hata hivyo, ilikuwa dhahiri kuwa hawakuwa na uwezo wa kufanya lolote, hasa baada ya ngao yao kubwa, ambayo ilitokana na mitambo yao ya umeme waliyoiamini kubomolewa. Walitazamana. Kisha, wakatazama huko na huko kama wanaotarajia msaada. Mmoja wao alifyonza na kutema mate.

Joram aliwapuuza akamwendea Nuru na kumkumbatia. Alichokiona katika macho yake kilimtisha. Hakuwa Nuru aliyemfahamu, Nuru ambaye siku zote alikuwa sharp kwa maneno na vitendo. Nuru huyu macho yake yalionekana kana kwamba yuko maili elfu moja nje ya chumba hicho. Ingawa alimtambua Joram lakini alionekana kama amemwona katika ndoto, si katika dunia halisi. Hata mwili wake, Joram alipomkubatia ilikuwa kama aliyekumbatia zombie au maiti yanayotembea.

Hali hiyo iliamsha upya hasira za Joram “Mmemtendea haya msichana huyu?” alimwuliza kwa sauti ndogo ambayo, kwa anayeifahamu ilikuwa kali, yenye hasira zake siku zote. Mmemfanya nini mpenzi wangu? Vizuri. Muda si mrefu baadaye mtajuta kuzaliwa. Nilitegemea niwafikishe katika vyombo vya sheria, lakini sioni kama kuna haja ya kufanya hivyo. Nitawaadhibu mimi mwenyewe, kwa njia ninazofahamu mimi.”

Alimwendea inspekta Kombora na kumtazama machoni. Hali yake haikutofautiana sana na ya Nuru. Kombora aliduwaa, akamtazama Joram bila kuonyesha dalili zozote za kuelewa kama amekuja kummaliza au kumwokoa.

Joram hakuhitaji kuambiwa kuwa walikuwa wamepewa kiasi kikubwa cha dawa za kulevya,Sedative Hyprotics, kama Mandrax na mengineyo ambayo yaliwapumbaza miili na akili. Baada ya kuitazama hali yao kwa muda, Joram alijikuta akibuni njia ya kuweza kuwachangamsha walao kwa muda. Miongoni mwa vitu vyake vya siri ambavyo hutembea navyo siku zote ni pamoja na vidonge vya kuongeza nguvu, kuhamasisha mwili na kutoa maumivu, vichocheo ambavyo ni mchanganyiko wa Cocaine, Amphetamine, Heroine na mengineyo. Ingawa matumizi ya dawa hizo pia hayaruhusiwi bila ushauri wa daktari, Joram, kwa nadra sana alizitumia kila ilipobidi; na mara nyingi zilimsaidia. Alitoa vidonge viwiliviwili kati ya hivyo na kuwapa Nuru na Kombora.

“Samahani, mkitoka hapa mtakwenda Muhimbili, watarekebisha afya zenu.” Aliwaeleza wakati akiwashawishi kumeza.

Philip na Paul walijaribu kutumia fursa hiyo kutoroka. Walinyata kuiendea sehemu ya kubonyeza tufe ili wafungue lango na kutoka. Hawakujua jinsi Joram alivyo mwepesi. Aliwaona bila kugeuza kichwa chake. Na kabla hawajabonyeza tufe hilo, alikwisha ruka na kuwachota teke moja ambalo liliwapeleka chini wote wawili, kama magunia.

“Bado nina shughuli na nyinyi,” aliwaambia akiwaburuza katikati ya chumba.

Alipowarejea Nuru na Kombora walionekana wakianza kuchamgamka. Dakika moja baadaye Nuru alitamka kile ambacho roho yake ilitamani kukitamka muda mrefu “Joram!”

Alisogea na kumkumbatia tena, machozi yakianza kumtiririka.

Joram alimbusu na kumfuta machozi huku akisema, “Wewe ni msichana mkubwa Nuru. Unafahamu kabisa kuwa huu sio muda wa kutokwa na machozi. Bado tuna kazi ya kufanya.”

Pamoja na kuanza kuchangamka, Inspekta Kombora alionekana mnyonge sana. Alijitahidi kukwepa macho ya Joram, kila alipomtazama. Joram akiwa mtu anayemfahamu fika mzee huyo, alijua kuwa alikuwa akikionea aibu kitendo chake cha kupatikana kirahisi na maadui hao kuruhusu vijana wake wauwawe mbele yake na kuaibishwa mbele ya Joram na Nuru. Joram alimpa maneno ya mzaha ambayo yalimfanya asahau aibu hiyo, aamke na kuanza kuwachunguza maadui hao. “Viumbe duni na dhaifu hawa wamewezaje kufanya unyama wote huu” Kombora aliuliza na kumtazama Joram kwa mshangao.

“pesa.”

“pesa?”

“Wanapesa nyingi sijapata kuona. Katika ofisi yao nimepata akaunti yao ya siri ambayo ina pesa inayotosha kulisha jeshi letu zima kwa miaka miwili.”

Alimsimulia Kombora uchunguzi alioufanya katika chumba hicho ambao ulimfanya atetemeke baada ya kugundua kuwa walikuwa wakipambana na watu ambao wanaweza kuiharibu Tanzania na kuiweka katika msiba usiomithilika hapa duniani.

“Sijapata kuona binadamu wenye mioyo ya kinyama kama hawa, Inspekta Kombora. Wangeifanya Tanzania liwe taifa la kusikitisha, lenye machozi na majonzi yasiyo na mwisho kwa miaka nenda rudi. Mbinu waliyobuni, ambayo haijapata kutumiwa na mtu yeyote duniani, kwa kiwango kikubwa, ilikuwa imekwishafanikiwa. Hasira na chuki waliyonayo dhidi yangu pengine ndiyo iliyowaharibia. Walitaka wahakikishe wanashuhudia kifo au maiti yangu kabla hawajaanza rasmi harakati zao za kishetani,” Joram alieleza na kumwuliza Kombora, “Inspekta si unawakumbuka wale marehemu ambao mlipata maiti zao na kukuta nyuso zao zikiwa zimeliwa nyama na kubakia mafuvu?”

Kombora aliitikia kwa kichwa.

“Basi yale yalikuwa majaribio tu. Ama yalifanywa kimachomacho mno ili kufikisha ujumbe kwangu. Hali ya marehemu wale ndio ingewatokea watanzania wengi, wake kwa waume, katika sura na miili yao. Lakini ingetokea taratibu, hatua kwa hatua, baada ya miezi mitatu au minne ya matumizi ya perfume, mafuta, sabuni, poda na vipodozi vingine mbalimbali ambavyo viumbe hawa wameingiza nchini.” Joram alisita kidogo na kutazama jinsi taarifa hiyo ilivyopokelewa na Kombora kwa hasira iliyochanganyika na hofu.

“Vipodozi hivyo ambavyo wamevipa jina Glamour ni sumu kali sana ambayo imefanyiwa utafiti wa miaka mingi, kwa gharama kubwa, hadi ilipoonekana ipo tayari ndipo imewekwa katika mafuta, perfume, cream, sabuni n.k ambazo zina harufu nzuri sana tofauti kabisa na matokeo ambayo yatafuata baada ya miaka mitatu, yasiyo na dawa, ikizingatiwa kuwa tayari sumu hiyo itakuwa imeenea mwilini na hakuna daktari ambaye amejiandaa.”

Kwa Kombora ilikuwa kama ambaye tayari ameshuhudia maafa hayo, kama ambaye tayari anauona msululu wa watu waliokata tamaa mbele ya madaktari walioduwaa, huku vilio vikisikika toka katika kila nyumba na kila mtaa. Aidha, aliona majeneza mengi yakipelekwa katika viwanja vya makaburi ambayo tayari vilikuwa vimefurika.

Kombora aliweza hata kuhisi harufu iliyotapakaa katika kila nyumba harufu ya uozo, harufu ya nyama, sura na miili ya wasichana wazuri ambao wanaoza taratibu huku wakiwa hai, hadi pale wanapokata tamaa na kusalimu amri ya kifo. Kana kwamba anayasoma mawazo yake, Joram kiango aliongeza ghafla, “Naamini mpango wao haukufanikiwa. Maghala yao mawili ambayo yalikuwa yamefurika mali zikisubiri zianze kutawanywa kote nchini, baada ya matangazo mengi katika vyombo vya habari, nimeyateketeza kwa moto. Kila kitu kimegeuka jivu, mizigo yao ambayo ipo bandarini, ambayo nashuku pia ina bidhaa za aina hii, kama nilivyoona katika hati zao za siri, pia haitawafikia wananchi. Itateketezwa kabla vibaka hawajaiba hata kopo moja.”

Kombora alishusha pumzi kabla hajasema, “Mambo yote umenieleza, Joram, kama ilivyokawaida yako umenitafunia na umeacha nimeze tu. Hata hivyo, kuna mawili hujaniambia. La kwanza hujaniambia adui yangu mkubwa zaidi ni nani, Kakakuona yuko wapi. Usiniambie kuwa amekuponyoka kwasababu ningependa kushuhudia kifo chake kwa macho yangu, kama si kumwua kwa mkono wangu.”

“Kakakuona tayari amekufa,” Joram alimjibu.

“Amekufa! Amekufa lini?

“Ni hadithi ndefu Inspekta. Tutaizungumza baadaye. Kuhusu swali lako la pili, nadhani unataka nikwambie hawa viumbe ni kina nani na wanahusika vipi na mkasa huu wa kutisha. Au sio Nuru?” alisita akimtazama Nuru na Inspekta Kombora kwa zamu, kisha akaendelea, “Hiyo ni hadithi nyingine ndefu, ningeshauri tutoke katika chumba hiki cha mauti twende katika ofisi ya kifahari ya wakurugenzi hawa ambamo tutaketi na kuzungumza kwa utulivu kabla hatujawakabidhi watu hawa kwa vijana wako ambao watajua la kuwafanya.”

“Kuwakabidhi?” Kombora alifoka ghafla. “Niwakabidhi kwa mtu mwingine watu kama hawa! Sikiliza Joram, mwanangu. Naweza kuwa mtu ninayeheshimika sana kisheria. Naweza pia kuwa mtu aliyeajiriwa kwa kuhakikisha sheria zinafuatwa. Lakini sio kwa suala la mashetani kama haya. Hawa, niliapa nitawauwa kwa mikono yangu,na ni hilo nitakalolifanya.” Aliwatazama Nuru na Joram kwa zamu. kisha, akauelekeza mkono wake kwenye shimo ambalo lilikuwa likiendelea kutoa harufu mbaya za maiti.

“Mnaliona shimo lile? Watu hawa wamelitumia shimo lile kuangamiza watu wengi wasio na hatia. Shimo lilelile litakuwa kaburi lao. Na nitawazika ili waisheherekee kila kila dakika ya safari yao kuelekea kuzimu.” Baada ya kusema hayo, bila kutaka ushauri wa Joram wala Nuru, alimwendea Philip na kumpiga teke moja ambalo lilimfanya aanguke kando ya shimo hilo, damu zikimvuja puani na mdomoni. Teke la pili, ambalo bila shaka liliuvunja mguu wake mzima, lilimfanya aviringike na kutumbukia shimoni humo kuungana na maiti nyingine.

Paul alianza kutetemeka hata kabla ya Kombora hajamfikia. Kwa jicho lake kali, ambalo lilijaa kisasi, alimtazama Joram kwa muda mrefu hadi Kombora alipompiga ngumi iliyomfanya ateme meno mawili na kuvunjika pua. Huku bado akimtazama Joram, badala ya Kombora aliyekuwa akimwadhibu, aliangukia shimoni kama mzoga. Kwa msaada wa Joram, Kombora aliitoa miili ya vijana wake wawili. Kisha, wakafunga mlango wa shimo hilo ambao ulifanya ionekane kama sakafu ya kawaida.

“Msijali” kombora aliwaambia, akiwatazama Jorama na Nuru. “Kwa hili nipo tayari kujieleza hata mbele ya mungu.”

Nuru na Joram walitazamana kisha, kwa sauti ndogo Nuru akamwambia, “Tuondokeni katika chumba hiki. Ni chumba cha mauti, hakitufai.”

Joram aliendea tufe la ukutani na kulibonyeza. Ukuta ukafunguka na kuwaruhusu kuingia katika ofisi safi ya wakurugenzi hao ambao walikuwa wakitapatapa chini ya ardhi kwa kukosa hewa safi. Wakaufunga nyuma, Joram akiwa amemshika Nuru mkono, aliwaongoza hadi juu ya viti ambako waliketi.

Ndio kwanza wakafahamu kuwa kulikuwa kumepambazuka. Nuru toka nje kupitia katika vioo, ambavyo viliruhusu kuona nje hali mtu wa nje hawezi kuona ndani, iliwawezesha kuona kundi dogo la polisi wenye silaha wakiwa wamelizingira jengo hilo. Kiongozi wao, akiwa na kipaza sauti mkononi, alikuwa akizungumza kitu fulani mara kwa mara kabla hawajalivamia. Kundi kubwa la raia walionekana wakiwa wamesimama nyuma ya askari hao wakitazama kwa macho yanayouliza, kulikoni!

Joram aliwapuuza watu hao wa nje. Akainuka na kuiendea ofisi ya mkurugenzi mtendaji na kuketi juu ya kiti chake cha starehe. “Kisasi ni kitu cha ajabu sana” Joram alianza kuamini.

“Nuru” alimwita akimtazama. “Unaweza kuamini kuwa hawa watu wawili ni binadamu pekee walionusurika katika jengo ambalo lilikuwa na ile mitambo iliyokuwa ikiendesha satelaiti ya ajabu ya Afrika Kusini ambayo ilikuwa isababishe ile mioto ya ajabu ajabu katika nchi za mstari wa mbele?”

“Philip na Paul walikuwa miongoni mwa mainjinia waliokuwa wakiiongoza mitambo hiyo. Ni wao pekee walionusurika kufa, baada ya moto tuliouanzisha kuteketeza kila mtu na kila kitu,” aliogeza.

Hakuna mtu ambaye angeweza kulisahau tukio hilo. Kombora asingesahau jinsi yeye, na kila Mtanzania, alivyokuwa roho mkononi, akisubiri maafa ambayo yaliandaliwa na serikali ya kidhalimu iliyokuwa ikiongoza nchi wakati huo. Nuru asingeweza kusahau yaliyomkuta. Asingesahau alivyoonja kifo baada ya mateso na kudhalilishwa kusiko na kifani. Ingawa yeye na Joram walitoka kama washindi na mashujaa wa Afrika na dunia nzima, bado tukio hilo ambalo limeandikwa vitabuni kwa lugha mbalimbali kama Tutarudi na Roho Zetu? Na Zero Hour bado kila anapolikumbuka, Nuru hujisikia kichefuchefu.

“Kwa nini hukuniambia kabla Joram?” aliuliza taratibu. “Nisingeacha wabakie hai humo shimoni.”

“Hawako hai.” Kombora alijibu. “Wamekufa taratibu, kifo ambacho kinawastahili kabisa.”

Joram aliendelea, “Ilivyotokea ni kwamba, baada ya wale jamaa kupona majeraha yao walijaribu kujihusisha tena na mipango ileile. Na kwakuwa jambo lile lilikuwa la siri sana likiwa limetengewa mamilioni ya pesa ambazo wao walikuwa miongoni mwa walioruhusiwa kuzitumia benki, walichofanya ilikuwa kuhamisha pesa hizo na kuziweka Marekani kwa majina yao. Wakati huo harakati za ukombozi nchini humo zilizidi kupamba moto, na hatimaye Mandela kuchukua urahisi baada ya kutoka kifungoni. Hasira zao juu ya mtu mweusi zilizidi. Na walizielekeza hasira hizo kwangu kwa kudhani kuwa nimesaidia kuwafanya washindwe na Watanzania wote kwa kuamini kuwa wamechangia kuwezesha ubaguzi utokomezwe, hivyo, wakabuni njia mbalimbali hadi walipopata msaada wa wanasayansi ambao walifanikisha jaribio la kutengeneza sumu ambayo ilikuwa almanusura iangamize Tanzania.”

“Nadhani wameona kuwa Tanzania bado si nchi ya kuchezea,” Kombora alisema.

“Nadhani,” Joram alisema akijiuliza mangapi zaidi amweleze Kombora. Katika uchunguzi wake alipata namba za akaunti za watu hao ambazo alikuwa tayari kumpa Kombora. Pia alipata nyaraka nyingi za siri ambazo angempa ili zimsaidie kukamilisha kazi yake.

Lakini katika uchunguzi huohuo aligundua uficho wa siri katika ofisi hiyo, ambao ulikuwa na mamilioni ya pesa taslimu za nje na za kigeni. Hilo asingemwambia Kombora kwani alipangakuzihamisha usiku utakapoingia. Aidha, kwa kumuhurumia mzee huyo alivyochoka hakupenda kumsimulia muda huo juu ya kiumbe wa hatari kuliko Kakakuona, mwenye taaluma kamili ya ninja, ambaye yuko mahali fulani, akisubiri. Joram aliamua kuwa hilo pia liwe siri yake hadi atakapolishughulikia.

Akiwa na hakika kuwa Kombora na jeshi lake hata wapekue jengo hilo mara ngapi wasingeweza kuzifikia pesa hizo aliinuka na kumshika Nuru mkono. “Nadhani huyu msichana amechoka. Anahitaji kupumzika. Kila kitu unachohitaji kiko humu. Kwa hiyo, nadhani utaturuhusu twende zetu.” Alipiga hatua mbili tatu kuuendea mlango, kisha akamgeukia Kombora na kumwuliza, “Kwa jinsi watu walivyojaa huko nje, unaonaje, nani aanze kutoka. Wewe au mimi na Nuru?”

Mamia ya watu walioduwaa nje ya jengo hilo walishangaa kuona mlango ukifunguka taratibu na kumruhusu kijana mmoja mkakamavu na msichana kuanza kuondoka. Mvulana akiwa katika suti yake nyeusi, isipokuwa kwa vumbi kidogo, katika mavazi yake alionekana mtanashati kama ambaye anatoka katika jumba la starehe kinyume na watu waliokuwa nje walivyoamini. Lakini msichana alikuwa taabani, kachakaa mwili na mavazi kama aliyetoroka kuzimu. Alitembea kwa kujikongoja huku akipata msaada wa mkono wa mvulana uliomshika kiuno.

Sura za vijana hawa zilikuwa maarufu nchini kama zilivyomashuhuri kote duniani. Haukupita muda kabla ya watu waliokuwa hapo nje hawajaanza kunong'ona, "Ni joram Kiango!"

"Ndiyo. Na Nuru"

Polisi ambao walianza kuziweka silaha zao sawa kuwaelekea, walipowafahamu walizirudisha makwapani na kusimama kwa utulivu. Mmoja wao saluti ilimtoka, na Joram akapokea kwa kutabasamu kidogo. Kabla askari hao hawajajua wafanye nini na Joram, bosi wao, Inspekta Kombora, alitokea, na askari wote wakamkimbilia.

Yeye pia alikuwa taabani kama Nuru. Nguo zake zilichakaa na kuchafuka, mwili wake ulijaa marejaha, macho yake yalilegea kana kwamba alikuwa amekesha akinywa pombe kali. Akiushikilia ukuta alitembea taratibu na kuzipuuza saluti ambazo zilielekewa kwake.

"Pole sana mzee."

"Nipelekeni ofisini… hapana nyumbani," alisema kwa udhaifu

"Tukupeleke hospitali afande?"

"Nimesema nyumbani."

Dereva mmoja alimsogezea gari. Kabla hajalipanda alitoa maelekezo kwa askari hao, akiwataka wahakikishe jengo hilo linalindwa kwa makini usiku na mchana hadi atakapokuwa tayari kukamilisha suala hilo ambalo alidai limekwisha!

Joram alitumia fursa hiyo kuutoroka umati wa watu. Alimfuata mtu mmoja aliyekuwa ameketi ndani ya gari lake, Toyota Saloon, na kumwomba lifti. Mtu huyo, kwa furaha, aliwafungulia milango na kuwakaribisha ndani. Joram akamwingiza mgonjwa wake kisha yeye akaingia na kumtaka awapeleke hotel ya Mawenzi.

"Nina bahati sana leo" msamaria alisema.

"Bahati gani?" Joram alimwuliza

"Kukutana ana kwa ana na wewe. Ni jambo ambalo sikulitegemea kabisa. Nimekuwa nikikusoma katika vitabu na magazeti tu. Hivi huko ndani kulikuwa na nini?"

"Ngoja gazeti la kesho utaelewa, ni hadithi ndefu sana"

"Hivi haya wanayoyaandika juu yako ni ya kweli? Sio kwamba waandishi wanatia chumvi sana ili magazeti na vitabu vyao vinunuliwe?"

Joram, akiwa hana hamu na magazeti, alijikuta akimwambia, "Hayo unayoyasikia yazidishe mara nne, utoe nane na kuongeza mbili ndipo utapata ukweli wenyewe"

Akiwa amechanganyikiwa, dereva huyo aliendesha gari bila maongezi zaidi mpaka alipowafikisha mbele ya hoteli yao.

Joram alimshukuru kwa ukarimu wake, akamzoa Nuru ambaye alianza kulala na kumwingiza hotelini. Watu waliokuwa mapokezi walitokwa na macho ya mshangao, hasa kutokana na hali ya Nuru, lakini Joram hakuwapa nafasi ya maswali. Badala yake alichukua ufunguo wake na kwenda chumbani kwake, akiwa bado amemshikilia Nuru kiuno. Hakuhitaji funguo huo, chumba kilikuwa wazi, kinyume na alivyokiacha. Jicho lake moja

chumbani humo lilimfanya afahamu kuwa alikuwa ametembelewa. Ingawa karibu kila kitu kilikuwa kama alivyokiacha, lakini bado dalili zilimwonyesha kuwa kila kitu kilikuwa kimekaguliwa na kuvurugwa kwa uangalifu mkubwa.

Joram akamtua Nuru kwenye kitanda na kumlaza taratibu. Alipovuta mto ili amweke vizuri, aligutuka kuona mto huo ulikuwa umetumiwa kuficha maiti ya paka mnene, aliyenawiri, ambayo yalilazwa kitandani hapo. Kando ya mzoga huo, Joram aliona maandishi mekundu yalioandikwa juu ya shuka kwa lugha ya kiingereza 'you're next' yakimaanisha kuwa ni yeye Joram atakayefuatia.

Alipomgeukia Nuru kuona kama naye pia alikuwa ameuona mzoga huo, alifurahi kumwona tayari kalala kwa utulivu, akikoroma taratibu. Akainama na kumchunguza paka huyo kwa makini zaidi. Akabaini kuwa aliuawa kwa kunyongwa kwa kwa mkono muda mfupi uliopita kwani alikuwa bado ana joto. Lakini Joram alipozidi kumchunguza aligundua kuwa bado alikuwa akipumua taratibu. Badala ya kumtupa dirishani kama alivyokusudia, Joram alimwinua polepole na kumweka nje ya chumba, upande wa mapumziko.

Baada ya kuduwaa kwa mara ya pili, Joram alimnusisha paka huyo dawa ya kulevya, jambo ambalo lilimfanya mnyama huyo mdogo apige chafya na dakika chache baadaye ainuke na kujikongoja taratibu kuelekea nje.

Joram hakuhitaji kuambiwa paka huyo ameletwa na nani chumbani humo. Adrian!… Ni yeye pia aliyekipekua chumba chake ambamo dalili zilimwonyesha Joram kuwa alikaa muda mrefu akimsubiri.

Kitendo cha kupata uhai kwa paka huyo, ambaye Joram alijua fika aliwekwa hapa kwa njia ya kumtisha huku adui huyo akiamini kuwa ni mzoga, kilimdhihirishia Joram kuwa mapambano bado yalikuwa yanaendelea. Hata hivyo, ilimtia matumaini makubwa ya kuibuka mshindi akizingatia uhai wa paka huyo ulivyorejea baada ya muuaji kuamini kuwa ametimiza kazi yake.

Akifahamu fika jinsi roho ya Adrian ilivyolemaa kwa chuki na fikra zake zilivyomezwa na kiasi Joram alijua kuwa alikuwa na wajibu mkubwa kumteketeza kiumbe huyo kabla hajafanya madhara zaidi. "Ni yeye, au mimi!" aliwaza akiondoka kurudi kitandani ambako Nuru alilala kwa utulivu.

Joram alimtazama msichana huyu alivyolala na mavazi yake yote. Aliitazama sura yake nzuri na umbo lake la kuvutia lilivyopendeza katika mavazi hayo yaliyochakaa na kuchafuka.

Pamoja na hasira zake, Adrian alichukua wasaa wa kujilaumu kimoyomoyo. Kwa kiasi kikubwa alihisi alishiriki kuwaangusha waajiri wake ambao alikwisha amua kuwa wana aina fulani ya kichaa. Kitendo chake cha kupenya toka katika eneo hilo la ofisi hadi katika hoteli ya Joram Kiango ili akammalize hukohuko, badala ya kumsubiri, kama wenyeji wake walivyomwelekeza, kwa kila hali kimechangia kumfanya awe hai hadi sasa na awaokoe mateka wake.

Jambo hili, limezifanya jitihada zake zote, za kupenya katika uchochoro wa hoteli hiyo, hadi nyuma ambako alitumia kamba kupanda hadi juu na kisha kwa kutumia tundu la moshi kujipenyeza hadi ndani ziwe za bure.

Chumbani mwa Joram, Adrian alipekua kila sehemu bila kujua anatafuta nini. Hakupata chochote. Hata hivyo, ili asiondoke bila zawadi yoyote, ndipo alipochukua mkufu wa dhahabu uliokuwa kama umesahauliwa katika begi mojawapo.

Adrian alijua ingemchukua muda Joram kugundua upotevu huo, lakini kwake ingekuwa fahari kubaki na kumbukumbu ya kumfuta duniani.

Ni wakati alipokuwa akitoka nje ya chumba hicho alipokutana na paka yule ambaye alipita akinusa huko na huko. Adrian hakuchelewa kumdaka na kumminya koo kwa vidole viwili hadi paka alipokata roho, kisha akamlaza juu ya kitanda cha Joram kama salamu ambazo alijua zitamsisimua zaidi ya kupotea kwa mkufu mdogo wa dhahabu.

Adrian akaamua kurudi kwa waajiri wake. Akiwa nje ya jengo hilo la Paul na Philip, alimwona inspekta Kombora, pamoja na uchovu wake mwingi, akitoa maelekezo juu ya ulinzi wa jengo hilo. Akiwa na hakika kuwa mambo yalikuwa yamewaendea kombo waajiri wake, Adrian alitazama kwa makini jengo hilo huku rohoni akijua wazi kuwa japo jeshi zima la polisi liletwe kulinda usiku huo lazima angeingia katika jengo hilo na kuchukua kila kilicho chake.

Hakukuwa na mtu yeyote, duniani na mbinguni, ambaye angemzuia.

Kwa miji yote mikubwa ilivyo kote duniani, jiji la Dar es Salaam pia halijui usiku. Mara tu jua linapozama na kiza kutanda, wako baadhiya watu ambao huona kana kwamba ndio kwanza kumepambazuka. Hivyo, wakati wenzao wakijiandaa kulala wenzao hujiandaa kutoka tayari kwa shughuli zao mbalimbali, baadhi wakiwa wafanyakazi wa zamu za usiku, baadhi watumiaji tu wa pesa zao, hali wengine wakiwa waviziaji tu, wezi na Malaya wa bandarini.

Usiku wa leo Joram alikuwa mmoja wao. aliporejea toka muhimbili akiwa na aina mbalimbali za dawa ambazo alielekezwa jinsi ya kumpa Nuru, alimwamsha na kumshurutisha kuzinywa.

Kama alivyokuwa ameambiwa na daktari yule, mara tu baada ya kuzinywa, Nuru alichukuliwa tena na usingizi, usingizi mzito ambao ungempumzisha kwa saa ishirini na nne wakati dawa zikifanya kazi.

Baada ya kuhakikisha Nuru amelala kwa utulivu, ndipo Joram pia alipolala kando yake na usingizi mnono, usio na ndoto, kumchukua. Alizinduka saa moja usiku. Akafanya haraka kuoga, kisha kuvaa suti yake.

Baada ya hapo aliichukua bastola yake, bomu moja la mkono, kisu na silaha zake nyingine akazitokomeza katika mifuko yake ya siri. Alipojitazama katika kioo na kuridhika kuwa hata askari mdadisi kiasi gani asingemshuku kuwa anakwenda vitani badala ya kwenda kufanya matumizi, ndipo alipombusu Nuru, akamfunika vizuri na kisha kuondoka baada ya kuufunga mlango vyema nyuma yake.

Hakuwa na haraka. Alipita katika chumba cha maakuli ambako aliagiza ugali kwa kuku wa kuokwa. Wakati akisubiri chakula hicho alijipongeza kwa bia mbili za stella. Chakula chake kilipofika alikula kwa utulivu, huku akiteremsha kwa kopo la tatu la stella. Alipomaliza aliwasha sigara na kuivuta taratibu huku kopo la nne lilkikoza moshi. Saa yake ilipomwashiria kuwa imetimia nne kasorobo za usiku ndipo alipolipa bili yake na kuingia mitaani.

Kwa mwendo ule ule wa taratibu, alivuta hatua moja baada ya nyingine kuziendea ofisi za Kangaroo. Alijua fika kuwa watakuwepo na silaha zao mikononi. Hata hivyo, akiwa amedhamiria kuingia alikwishajiandaa kwa njia moja au nyingine ambayo ingemwezesha kuingia. Hivyo, hilo hakulitilia wasiwasi. Ambalo lilimtia wasiwasi na kumwongezea shahuku ya kufika aendako ni Adrian. Alikuwa na hakika kuwa Adrian, alivo kichwa maji, lazima pia angebuni kuingia katika jengo hilo. Na ni hilo lililomfanya awahi. Alitaka awe wa kwanza kufika katika jengo hilo ili amsubiri na kumpokea. Alijua fika kuwa mkutano wao wa ana kwa ana ulikuwa na maana moja tu, ya kumwacha mmoja hai, mwingine maiti. Joram alikuwa na uhakika kuwa huyo maiti asingekuwa yeye.

Wakati akikaribia ofisi hiyo, Joram aliichomoa tai yake nyeupe na kuisokomeza mfukoni. Kuondolewa kwa tai hiyo, kulimfanya abadilike ghafla na kuwa kama kivuli au sehemu ya kiza. Aliubadili pia mwendo wake na kuanza kunyata kwa uangalifu, toka ukuta hadi ukuta; kichaka hadi kichaka. Wapita njia waliomtazama kwa macho ya udadisi aliwapumbaza kwa kujifanya ama anajisaidia haja ndogo au anafunga kamba za viatu vyake, ama amelewa na hivyo, anakwenda bila mpangilio wowote.

Alipofika mbele ya Kangaroo, kama ivyotegemea, alimwona askari mmoja mwenye silaha na magwanda akiwa amesimama kuuegemea ukuta, bunduki yake kaishika mkono mmoja, wa pili ukiwa mfukoni. Joram alimtazama kwa makini. Akashangazwa na utulivu wa askari huyo. Alipotupa macho kutazama huko na huko hakumwona askari mwingine.

Akaitazama saa yake ambayo ilimuashiria saa nne na dakika kumi. Alihitaji kuwa katika jengo hilo mapema. Hivyo, alipoona askari huyo hatoki hapo aliposimama, aliamua kumfuata. Aliiwasha sigara yake na kuipachika mdomoni, akakohoa, kisha akaanza kumsogelea. Alitegemea kuambiwa simama au kupewa amri yoyote ile. Haikutoka. Joram alizidi kumsogelea hadi alipomfikia na kumsalimu. Hakuitikia.

“Hujambo, brother?” Joram alisalimu tena.

Bado hakuitikiwa, jambo ambalo aliona halikuwa la kawaida. Alimtazama askari huyo kwa makini zaidi na kubaini kuwa alikuwa hatingishiki, haoni wala hasikii. Alipojaribu kumtikisa aliporomoka na silaha yake na kuanguka sakafuni.

Ndio kwanza Joram akabaini kuwa alikuwa anaongea na maiti. Akainama na kumshika kifuani ambako alimkuta kapoa kitambo. Kiasi Joram alitahayari. Alitegemea ukatili. Lakini hakutegemea ukatili wa kiasi hicho. Kwa ujumla, aliondokea kuamini kuwa kipindi cha mauaji ya kinyama kilikuwa kimepita, wazo ambalo sasa alilijutia.

Hakuhitaji kuambiwa kuwa mauaji hayo yamefanywa na nani. Wala hakuiona haja ya kujiuliza kwanini yamefanyika. Adrian alikuwa amemtangulia. Akamwua askari huyo, bila shaka kwa hila, ili asiwe kipingamizi cha kumfanya ashindwe kuingia ndani. Hivyo, ama alikuwa ndani ama ametoka.

Wakati akiyafikiri hayo Joram Kiango tayari alikuwa ameusimamisha mzoga huo wa askari kama alivyoukuta na kuirejesha bunduki mkononi mwake na kuanza kunyata akielekea mlangoni. Kando ya mlango huo, kwenye kibanda kidogo cha mapokezi, Joram aliikuta maiti ya askari wa pili. Huyu alikuwa ameketishwa juu ya kiti na kuiinamia meza, bunduki mkononi. Joram hakuitaji kumgusa kujua kuwa amekufa.

Aidha, hakuwa na haja ya kumshika shingo ili kubaini kuwa lilikuwa limevunjwa kwa pigo kali la judo. Alichofanya ni kukimbilia ndani, ambako aliukuta mlango ukiwa wazi, kama unaomsubiri. Harakaharaka bastola yake ikiwa mkononi, alinyata toka chumba hadi chumba. Akitumia tochi yake yenye ukubwa wa kalamu, alichungulia kila kona, kila uvungu wa meza, kila kabati, kila uvungu wa friji, bila mafanikio. Kila dalili ilimwonyesha kuwa Adrian amekuja na kuondoka.

Joram akaziacha ofisi za kawaida na kuzifuata zile za siri ambako waliwazika hai Paul na Philip. Huko pia Adrian alikuwa amemtangulia na alichokifanya hakikustahili kutazamwa. Mateka hao wawili ambao yeye na Kombora waliamua kuwafungia hai, Adrian alikuwa amewachoropoa toka shimoni humo na kuwachinja kama kuku, mmoja baada ya mwingine. Miili yao, aliitupa juu ya sakafu na kuwafanya walale wakiwa wamekumbatiana ndani ya dimbwi la damu yao wenyewe.

Joram alikiacha chumba hicho na kukimbilia kile ambacho kilihifadhi mamilioni ya pesa za kigeni. Alisogeza sefu ambalo liliwekwa kwa geresha na kulifikia lile la siri ambalo liliunganishwa na ukuta kwa hila. Alipojaribu kulifungua alishangaa kulikuta likiwa wazi. Pale ambapo palikuwa na vitita vya noti za ndani na nje sasa hapakuwa na kitu chochote. Hapana, palikuwa na kitu fulani, kitu kidogo, cheusi. Joram aliisogeza tochi yake na kutazama. Kama macho yake yalichelewa kumwashiria yanatazama nini, pua yake haikuchelea kufanya hivyo. Kitu hicho kilikuwa kinyesi. Baada ya kuchukua pesa hizo, kwa kuonyesha dharau, Adrian, akijua mtu yeyote angetamani kuzipata pesa hizo ndipo alipoamua kufanya hivyo.

Mara ya kwanza maishani mwake hasira hizo zilimfanya atetemeke mwili mzima. “Mshenzi” aliropoka kwa mara ya pili. “Haendi popote! Kamwe haondoki nje ya nchi hii akiwa hai,” alinguruma akigeuka kuanza kutoka nje ya chumba hicho taratibu kwa mwendo wa sismba aliyejeruhiwa mwili na roho.

MWISHO

Ben R. Mtobwa
NAJISKIA
KUUA
TENA

Simulizi : Najisikia Kuua Tena

1

POLISI…kikosi cha kumi na mbili…Inspekta Kombora anaongea. Nani mwenzangu?"

Kwa muda kukawa kimya. Kombora alisikiliza kupumua kwa dalili ya hofu katika chombo cha simu kutoka upande wa pili. "Nani mwenzangu?" akaongeza nguvu kidogo.

"Ni Kombora mwenyewe anayeongea?" iliuliza sauti hiyo yenye wasiwasi kutoka upande wa pili.

"Ni mimi, nani mwenzangu?"

"Ndiye! Mkuu wa kituo hicho sio?"

"Ndiye, tu…"

"Sikiliza Inspekta," sauti ilidakia na kunong'ona harakaharaka, "Nina tatizo zito sana. Sijui kama utaweza kunisaidia."

“Nadhani tunaweza. Tutajie tatizo lako na jina lako ili tujadiliane.”

“Jina sitaji,” iliongeza sauti hiyo, “Na tatizo lenyewe ni zito sana, siyo mzaha. Najisikia kuua mtu Inspekta. Najisikia kuua. Na ni lazima niue. Waweza kunisaidia Inspekta?”
“Kuua!” Kombora aliropoka. Katika matatizo yote, hilo kamwe hakulitegemea. Ni rahisi mtu kupiga simu polisi na kusema “mtu anataka kuniua.” Ni rahisi pia mtu kudai “nilimwona fulani akiua” lakini “nataka kuua” lilikuwa jipya kwa Inspekta Kombora.

Angeweza kulichukulia suala hilo kwa mzaha; kwamba ni chizi au mlevi mmoja ambaye ameamua kuwasisimua polisi lakini uchizi au ulevi haukuwemo kabisa katika sauti hiyo. Ilikuwa sauti dhaifu iliyojua kipi inasema. Kwa muda Kombora aliduwaa akiwa hajua lipi amjibu mtu huyo.

“Upo Inspekta?” ilihoji sauti.

“Nipo ndugu yangu,” Kombora alijibu kwa unyonge.

“Mbona kimya? Huna msaada wowote?”

“Ninao. Sikia rafiki yangu, njoo zako hapa mara moja ili tukae na kulijadili tatizo. Naamini tutakusaidia.”

“Hilo sifanyi Inspekta. Nikija huna uwezalo kufanya zaidi ya kunitia ndani, na mimi nauhitaji uhuru wangu. Kama huna msaada mwingine…”

“Ninao. Ni hivi, u nani jina lako?…Uko wapi?…Na unayetaka kumuua ni nani…Kwa nini?…Haloo!…Haloo!…”

Haikumchukua muda Kombora kung’amua kuwa alikuwa akizungumza katika simu iliyokatwa. Kwa muda aliendel;ea kuduwaa, simu mkononi, macho kayakodoa kutazama ukuta uliokuwa mbele yake, akiwaza mengi. Kisha alitua simu na kuinuka. Mara akakumbuka kuwa hakujua anakotaka kwenda. Akaketi na kutikisa kichwa kwa wingi wa mawazo mazito yaliyomjaa ghafla.

KITENGE alizinduka kutoka usingizini kwa kugutuka kidogo. Hakujua kilichomwamsha ghafla hivyo. Akatazama huku na huko kama anayejaribu kutafuta kitu hicho kilichomfanya auache usingizi wake ambao haukuwa na ndoto yoyote.

Mara mlango ukagongwa tena, ndipo alipokumbuka kuwa kilichomwamsha ni mlio wa mlngo huo. Kwa dalili za uchovu aliinuka kutoka kitandani na kuvuta taulo iliyokuwa juu ya kiti, akaitanda kiunoni, kisha aliuendea mlango na kuufungua.

Mlango huu ulimfikisha ukumbini ambapo alipita kuuendea mlango mkubwa, macho yake yakiipitia saa ya ukutani ambayo ilidai kuwa ni saa kumi na mbili kasoro dakika nne, jambo ambalo lilimshangaza mno, kuona ugeni wa alfajiri kama hiyo.

Alifungua mlango; aliyesimama hapo nje alikuwa ni mwanamke ambaye Kitenge, baada ya kumtazama kwa muda, alimkumbuka. Alikuwa ni Machozi Rashidi. Mwanamke ambaye alipokuwa msichana waliishi jirani na Kitenge wakihusiana kwa njia mbalimbali katika harakati za maisha baina ya wasichana na wavulana.

Kitenge hakujua kama ilimpasa kumkaribisha au la. Kwa kila hali huyu hakuwa yule Machozi ambaye Kitenge alimfahamu wakati ule. Huyu, wakati ulikuwa umemwathiri sana na kumtenga mno na Kitenge kiasi cha kumfanya aionee aibu kila dakika ambayo aliendelea kusimama naye hapo mlangoni.

Hakuwa mwanamke wa haja hata kidogo. Kama aliwahi kuwa mzuri, Kitenge hakuiona dalili yoyote ya uzuri iliyosalia katika sura hiyo. Sasa ilikuwa sura kavu, yenye mikwaruzo mingi, macho mekundu kwa athari ya kitu kama gongo au bangi, nywele nyekundu, kavu zenye dalili zote za kutoonja aina yoyote ya mafuta. na mwili mzima ulikuwa na mikwaruzo juu ya ngozi hiyo kavu na ilikuwa dhahiri kuwa mwanamke huyu aliishi kwenye mazingira yasiyofaa. Ngozi hiyo ilifunikwa na mavazi hafifu ambayo pamoja na kuwa dhaifu yalikuwa yamechanika hapa na pale.

“Haunikaribishi Boni?” aliuliza mwanamke huyo. Sauti yake pia ilikuwa tishio jingine, haikuwa ya mwanamke hata kidogo, wala haikumfaa mwanamume. Boni lilikuwa jina la utotoni la Kitenge ambalo sasa lilikuwa limetoweka kabisa baada ya majina mengine kuibuka, majina ambayo yalifungamana na hadhi yake mpya. Kwani sasa Boni alikuwa mwandishi maarufu wa vitabu.

Ghafla jina hilo likamkumbusha uhusiano wa kimapenzi aliokuwanao awali na kiumbe huyu.

“Ingia,” alimwambia.

Mwanamke huyo aliingia ndani na kufuata moja ya makochi sita yaliyopangwa kistaarabu katika ukumbi huo. Alitazama kila upande akihusudu hiki na kuvutiwa na kile. Kisha akamtupia Kitenge macho yake mabaya. “Hongera,” akakoroma kwa sauti hiyo ya kuchukiza.

“Kwa?”

“Vitabu vyako. Hukujua kuwa hata sisi washamba ambao hatukusoma tungeweza kuviona? Ulidhani kuwa tusingeona hata picha nyuma ya vitabu hivyo? Ama hujui kuwa hata redioni vinaongelewa? Pamoja na hayo, ningependa kukujulisha kuwa ingawa sikusoma sana, naweza kuelewa waandishi wanasema nini katika magazeti yao. Karibu wote wanakusifu. Hongera tena Boni.”

Kitenge hakujua kwamba ilimpasa kufurahi au kuchukia kwa sifa hizo. Kusifiwa halikuwa jambo geni kwake. Tangu alipotoa kitabu chake cha kwanza, MACHOZI YA DAMU, kupata sifa lilikuwa jambo la kawaida. Kitabu cha pili, KIFO USONI, kilimzidishia sifa kemkem, cha tatu na ambacho ni kama cha mwisho katika vitabu vilivyokwishatolewa; ALIKUFA ANACHEKA, kilifanya sifa zitapakae pembe zote kiasi cha kumtia katika mashaka ya kukosa nafasi ya kufikiria vitabu vingine.

Kila alikopita aliandamwa na ‘hongera’, yeyote aliyemfahamu alimtupia tabasamu. Waandishi wa habari walimtaka picha na mahojiano mara kwa mara. Katika baa moja aliwahi kuona maandishi yanayosema ‘Kondokondo Kitenge zaidi…’ na kadhalika. Hata katika basi ilikuwa ni jambo la kawaida kukuta kikundi cha watu kikizijadili sifa zake.

Naam, kusifiwa kwake sasa lilikuwa jambo la kawaida. Lakini sifa hizi za alfajiri, kutoka kwa mama huyu ‘aliyechoka’ kwa sauti yake ambayo licha ya kuchakaa, ilidhihirisha kitu kama kebehi, unafiki au uadui katika sifa hizo, zilimfanya ghafla ahisi jambo lisilo la kawaida katika nafsi yake. Wasiwasi ukamwingia rohoni. Wasiwasi ambao nafsi yake ilipokonywa na hasira, akajikaza kisabuni kumtazama mama huyo huku akisema, “ Nadhani hukuja asubuhi yote hii kwa ajili ya kunisifu. Niwie radhi, kama huna zaidi, nenda zako ili nijiandae kwenda zangu kazini.” Machozi akacheka. Kicheko chake kilikuwa kitu kingine cha kutisha, na kilikuwa mbali kabisa na kicheko cha mwanamke, na karibu zaidi na kile cha shetani.

“Nilitegemea hutasema hayo,” alisema. “Najua umekuwa mtu mkubwa na tajiri sasa. Umetoa nakala elfu ngapi hadi sasa? Haikosi una akiba ya milioni benki. Mungu akujalie,” akacheka tena. Bila kusubiri jibu la Kitenge, aliongeza, “Ndiyo nimekuja kukusifu, kwani hukumbuki kuwa mimi ni mpenzi wako? Hukumbuki kuwa uliniahidi kuwa bila mimi usingeishi? Kwamba lazima tungeoana tu. Hukumbuki?”

Kitenge aliduwaa, hakujua mwanamke huyu anaelekea wapi katika maongezi hayo. Hivyo akaamua kunyamaza akimtazama.

Baada ya kicheko kingine Machozi aliongeza, “Nimekuja mpenzi, nimekuja kukukumbusha ahadi hiyo, kama umesahau. Nyumba yako hii nimeitafuta mwaka mzima, leo ndiyo nimeipata. Nimefika nyumbani, kwa hiyo wewe nenda zako kazini utanikuta mkeo nimekuandalia kila kitu. Au ulianza kusahau mapenzi yetu hadi ukaoa mke mwingine?”

Bado Kitenge aliamini Machozi alikuwa akimkebehi, hakuwa amesema alilokusudia. Hata hivyo tayari alianza kupandwa na hasira, huku akiificha hasira hiyo katika sauti yake alisema, “Sikia Machozi, mimi sina muda wa kupoteza. Kama umechanganyikiwa nenda mahala ukazungumze yote unayotaka kuzungumza. Hapa sipo kabisa. Sasa inuka utoke zako.”

“Kweli mpenzi tuseme umesahau ahadi zako zote?”

“Toka…”

"…. umesahau barua zako tamu…"

"…uende zako haraka!"

"….zenye kila neno la mapenzi na ahadi za kuishi pamoja?"

"Nasema toka!"

"Pamoja na jinsi nilivyokupenda nikajitoa kwako mwili na roho? Umesahau kweli mara hii? Siamini!"

Ana wazimu mwanamke huyu? Kitenge alijiuliza. Mapenzi!
Mapenzi gani hayo ambayo hakumbuki? Kwa kadri ya kumbukumbu zake, neno 'nakupenda' wakati huo lilikuwa moja ya michezo ya kawaida mongoni mwa watoto. Angeweza kumwambia yeyote wakati wowote 'wewe ni wangu wa heri na shari,' kadhalika angeweza kusikiliza jibu lolote la msichana yeyote na kumwamini.

Halikuwa jambo la ajabu mtu kumwambia mtu 'nikila sishibi kwa ajili yako' au 'usiku silali'. Karibu kila mvulana alikuwa na faili kubwa la barua za mapenzi. Barua hizo zilikuwa zikiandikwa kwa ufundi au kunakiliwa kutoka vitabuni huku zikiwa zimenakshiwa kwa maua ya kuvutia pamoja na kupambwa kwa harufu ya poda. Machozi alikuwa na akili gani hadi leo hii kuendelea kuamini mambo kama hayo?

Mchezo wa mapenzi, vichakani na hata nyumbani ni jambo lililokuwa la kawaida pia. Ingawa Kitenge hakuwa mpenzi sana wa mchezo huo, lakini Machozi alikuwa mmoja tu katika orodha ndefu ya wasichana aliowahi kufanya nao mapenzi.

Yalitokea, yakatoweka. Yeye Kitenge baada ya kufaulu darasa la saba, akiwa mtoto pekee aliyetoka katika kijiji hicho cha Mayange, wilayani Kasulu, alijibidiisha zaidi katika masomo yake. Kila aliporudi likizo wasichana wote walimlaki kwa furaha na kuridhia lolote alilotaka; Machozi akiwa mmojawao.

Alipohitimu kidato cha sita na kupata kazi hapa Dar es Salaam, alikata mguu kijijini hapo. Hakuwa na muda wa kutosha kumfikisha huko mara kwa mara kutokana na shida ya usafiri. Huu ulikuwa mwaka wake wa sita tangu alipofika huko kwa mara ya mwisho. Likizo ya mwaka huu alikuwa akijiandaa au kutarajia kuwa angeenda. Katika mapya na mageni yote aliyotarajia kuyakuta huko nyumbani, hili hakulitarajia kabisa.

"Unatoka katika nyumba hii au hutoki?" aliuliza ghafla.

Machozi hakumjibu haraka. Alitazama huku na huko kisha akasema, "Nikisema sitoki nadhani utaniitia mgambo. Vizuri sana. Sasa nitasema dhamira ya safari yangu hii; ilikuwa ni kukupa hongera, ndiyo, lakini si hongera ya mafanikio ya kuandika kwako vitabu. Ni hongera kwa kufanikiwa kwako kuniharibia maisha yangu. Kwa kunidanganya hata nikadanganyika na kuamini kuwa ulikuwa wanipenda kumbe la. Haukuishia hapo, ukanijaza mimba na kisha ukaikana. Hongera sana Boni."

Ndipo Kitenge alipokumbuka kuwa aliwahi kupata barua moja kutoka kwa baba au mmoja wa wadogo zake ambaye alidai kuwa amemtia mimba msichana mmoja. Ati aende akamuoe! Wakati huo, Kitenge alikuwa ndiyo kwanza anaanza kazi. Wazo la kuoa, na hasa kumuoa mtu kama huyo, lilikuwa nje ya ratiba yake a maisha. Hivyo suala hilo alilipuuza. Hakumbuki kuwa aliwahi kujibu barua hiyo. Kumbe ilikuwa kweli? Yaweza kuwa kweli? Alijiuliza.

"Nikikuruhusu kusema utaanza kuikana mimba hiyo. Waweza hata kudai kuwa hukuwahi kufanya nami mapenzi japo ni wewe uliyeniharibia ubikira. Napenda kukufahamisha kuwa mwanao alikuwa msichana. Nilimtupa katika mapipa ya takataka za hospitali ya Maweni. Kama walimwokota akiwa hai au maiti, sijui. Sikujali. Najua na wewe hujali wala usingejali." Machozi akanyamaza akimtazama Kitenge kuona hadithi yake ilimwingia vyema.

Alipomwona akitoa macho ya mshangao aliongeza: "Usiseme unasikitika, najua una moyo wa jiwe kama mimi. Ingawa mimi sikuzaliwa na moyo huo, nimeupata ukubwani kwa haki kabisa ingawa nikiiambia hivyo jamii haitanielewa."

Akasita kidogo na kuendelea, “Ninachotaka kueleza ni taabu niliyoipitia baada ya kumtupa mtoto huyo. Njaa ilinifanya niangukie mikononi mwa mwanamume mwingine. Huyu, tangu awali nilijua ananilaghai, lakini sikuwa na njia ya kumzuia asinitie mimba nyingine. Alipogundua nina mimba aliniepuka, ikabidi niteseke sana kutunza mimba hiyo bila mafanikio. Mwisho, niliamua kumeza dawa za kuitoa. Ilitoka kwa taabu, nami niliponea chupuchupu. Nilipopata nafuu zawadi yangu ilikuwa kifungo cha miaka mitatu.

“Majuzi tu ndiyo nimetoka jela. Maisha yangu yamekuwa mpira usio na thamani. Unaochezwa na kila mwanaume atakaye. Nadhalilishwa, naonewa na kufanywa kiumbe duni asiye na haki ya kuwa hai. Yote hayo ni kwa ajili yako Boni. Ni wewe uliyenivuta katika mkondo huu ukahakikisha siwezi kutoka.”

“Mimi!” Kitenge aliropoka akiwa hajui la kufanya.

“Wewe!” Machozi alijibu. Sauti yake haikuwa ya kebehi tena, wala haikujali kuweka furaha ya kinafiki. Ilikuwa wazi ikitangaza kulipiza kisasi na uadui.

“Wewe!” aliongeza, “Na nilichokuja kukuambia si kukuomba unioe au unipe pesa za kutumia, la. Nimekuja kukuambia kuwa nakuchukia. Ninakuchukia kama ninavyomchukia shetani. Sasa hivi, mimi ni kama maiti ambaye hajaanza kunuka tu. Sina mbele wala nyuma. Lakini kabla sijaoza nitahakikisha na wewe unalipa gharama za madhambi yako. Lazima twende wote ahera Mungu akatuamulie nani mwenye haki. Nitakuua Boni. Tena kwa mkono wangu huu!” Aliutikisa mkono huo huku akiinuka na kuanza kutoka.

Mlangoni aligeuka na kuanza kumtazama Kitenge. “Kwa heri,” alisema, Tutakapoonana tena, ujue ndiyo mwisho wa uhai wako.” Akatoka na kutoweka.
Kitenge alibaki akiduwaa juu ya kiti chake. Aliyemzindua ni mama mwenye nyumba, kikongwe ambaye huwa hapitwi na neno lolote humo au nyumba za jirani. Alibisha hodi na kusimama mlangoni.

“Baba, mwanamke huyo ni nani?” aliuliza.

“Simfahamu. Nadhani ni mwendawazimu,” Kitenge alilaghai akiinuka na kuelekea bafuni.
“Anasema anakufahamu…. jihadhari baba,” sauti ya Bi mkubwa huyo ilimfuata.

Hakujishughulisha kumjibu.

ASUBUHI hiyo, Kitenge alikuwa mtu wa kwanza kuwasili ofisini. Milango yote ilikuwa imefungwa. Akatumia funguo zake za akiba kufungua na kuingia hadi katika ofisi yake. Alikuwa na maandishi yaliyochorwa kisanii kabisa, juu ya kipande cha ubao kilichowekwa juu ya meza yake yaliyosema, KONDOKONDO KITENGE, MANAGING DIRECTOR-BLACK POWER PUBLISHERS. Zamani maandishi haya yalikuwa yakimvutia sana na aliyatazama mara kwa mara. Si sasa ambapo aliweza kushinda ofisini humo macho yake yalitazama na kuona kila kitu isipokuwa maandishi hayo.

Hii ilikuwa ofisi yake. Ofisi ya kampuni ambayo alikuwa ameianzisha miaka miwili iliyopita, kushughulikia vitabu vyake na vya wandishi wengine ambavyo vilionekana vyafaa. Wazo la kuanzisha kampuni hii lilikuwa limemjia baada ya kuona alivyowatajirisha wachapishaji wake wa awali, huku yeye akimegewa kidogo kutoka katika faida hiyo kubwa, wakati huohuo wakichelewesha uchapishaji wa vitabu vyake bila sababu ya kuridhisha.

Kitabu chake cha kwanza ambacho alikiandika akiwa shuleni kilikuwa kimesubiri miaka minne ndipo kikatolewa. Cha pili kiliwahi sana, miaka miwili! Tangu alipoanzisha kampuni hii mambo yalianza kumwendea vyema, ingawa yapo matatizo kadhaa yaliyomkwamisha hapa na pale. Alifurahi kupambana nayo mwenyewe badala ya mtu mwingine kumpigania.

Tatizo kubwa ambalo lilimtisha ni lile la kuona kama aliyeelekea kuishiwa na ule uwezo wake wa uandishi. Tangu alipobeba mzigo huo wa Ukurugenzi Utendaji, mtiririko wa mawazo yake ulipungua kasi. Na alipojikongoja hadi kumaliza kitabu washauri wake walidai kuwa hakifai kutolewa. Kwamba kingemvunjia hadhi yake. Ati mambo mengi yalikuwa marudio ya vitabu vya waandishi wengine, hasa wa magharibi.

Jambo hilo lilimtia hofu sana, kuona akielekea katika hatari ya kuishia vitabu vitatu tu ilhali alidhamiria kutoa vitabu vingi kama kina James Hadley Chase, Shabani Robert, Ngugi wa Thiong’o na wengi wengine. Aibu ilioje! Mara kadhaa alijiuliza kama alitumia busara kuamua kuwa mchapishaji badala ya kuacha wachapishaji wake waendelee kushughulikia miswada yake, yeye akishughulikia mawazo mapya.

Akiwaza hayo Kitenge alikuwa ameketi juu ya kiti chake, hafahamu wala hajaamua lipi aanze katika shughuli nyingi alizoacha jana. Kulikuwa na mengi ya kufanya. Kuna ule muswada wa kusoma, miswada miwili ya kusahihisha lugha, mmoja wa kumrudishia mtunzi afanye marekebisho, madai ya fedha katika maduka ya vitabu, kuwasukuma wachapaji waliokwamisha vitabu viwili vya hadithi za watoto na kadhalika. Mengi. Hakujua lipi aanze kushughulikia na lipi liahirishwe tena.

Mara, mawazo yake yakaikumbuka tena ziara ya alfajiri ya yule mwanamke, Machozi. Ana nini? Wazimu au upungufu wa akili? Madai yake yana ukweli kiasi gani? Na hata kama yana ukweli wowote, si yamhitaji mtu mwendawazimu sana kuyafuatilia madai ya aina hiyo! Ati ulinitia mimba miaka mingapi iliyopita, kwa hiyo tangu leo mimi mkeo! Ati nitakuua kwa kuwa ni wewe uliyeniharibia maisha yangu!

Wazimu ulioje! Kitenge akaangua kicheko. Hakujua kama alikuwa akimcheka Machozi alivyochakaa au madai yake yasiyokubalika.

KAMA kawaida Rusia alikuwa katika moja ya mavazi yake ya thamani zaidi ya mshahara wake, nywele kazitia mafuta au madawa yaliyozifanya zifanane na za Kizungu, kama si chotara. Ni sura yake tu ambayo Kitenge aliona hairidhishi. Hakumbuki kwa nini alimwajiri mtu mwenye sura kama hiyo kuwa karani wake mahususi. Kilichomshangaza ni wale watu wakubwa ambao huja mara kwa mara na magari yao kumchukua msichana huyu kwa chakula cha mchana.

Hakujua nini wanaona cha haja katika sura hii. Hawaioni kasoro yoyote? Wakati mwingine alijiona pengine ni yeye mwenye kasoro. Kwani hajawahi kumpenda msichana yeyote kwa dhati. Wote aliotembea nao, na anaotamani kutembea nao, huwatoa kasoro kemkem. Jambo ambalo limemfanya hadi leo hii kutokuwa na mke.

“Naona unaendelea kucheka, vipi? Au tayari umepata hadithi mpya kichwani? Najua wewe huridhishwi na chochote zaidi ya hadithi,” Rusia aliendelea.

Mara wazo likamwingia Kitenge; kweli! Tukio la leo asubuhi baina yake na Machozi ni hadithi nzuri sana! Hadithi ya mapenzi! Mapenzi ambayo yatageuka kuwa chuki. Hata jina la riwaya sasa lilielea kichwani mwake. Ataiita MAPENZI HUCHUJA. Naam, itakuwa hadithi nzuri. Mwisho? Akajiuliza. Uweje mwisho wake? Machozi alipendekeza mauaji, yeye ataangalia mwisho wa kuridhisha. Akacheka tena.

Safari hii kicheko kilimtia Rusia mashaka. “Mwenzangu! Nadhani tumwite daktari. Tangu nilipoingia husemi lolote, hufanyi lolote zaidi ya kucheka. Sema tumwite kama unaona mambo si ya kawaida,” alisisitiza bila mzaha wowote.

“Usiwe juha we mwanamke,” Kitenge alimjibu akiukunja uso wake. “Siku nikianza wazimu itakuwa ni kwa hasira si furaha. Na katika ofisi hii hatatoka mtu. Nitavunjavunja kila kitu na kila mtu, huyo daktari atakayenisogelea ataadhirika.”

Wote wakacheka.

“Basi tuombe Mungu isitokee.”

“Wala haitokei. Hata shetani ni mwoga, anaangalia wapi aelekeze pepo wake mchafu.”

Baada ya maongezi hayo walizama katika shughuli zao. Kitenge alikuwa hajafanya lolote mhudumu alipomtaka radhi ili afagie. Akaamua kutoka nje kabisa. Ofisi yao ambayo ilikuwa katika Mtaa wa Samora, haikuwa mbali sana na Hoteli ya Salamander. Kitenge alivuka huku akiendelea kuitayarisha hadithi yake mpya kichwani. Akataka kuiandika mara moja, lakini roho nyingine ikamzuia na kumshauri aitafiti vyema na kuipamba kabla hajaitia katika maandishi.
Aliporejea ofisini, Rusia alimtambulisha kwa mgeni ambaye hakuwa mgeni sana machoni mwa Kitenge.
“Bwana Bazile Ramadhani, mwenye ule muswada ambao bado tunautafuta. Nimemwambia aje kesho, lakini mwenyewe anadai anataka kuzungumza na wewe.”

Kitenge akaukumbuka muswada huo, ulikuwa mmoja kati ya ile miswada ambayo huwezi kuitilia maanani. Ulikusudiwa kuwa hadithi ya upelelezi, lakini ilivyoandikwa si hadithi ya upelelezi, isipokuwa mtiririko wa mauaji ya kikatili yanayotokea bila sababu za kuridhisha. Muswada huo ulimfanya Kitenge kumfikiria mwandishi kama mtu mwenye hasira dhidi ya ulimwengu wote, mtu atakayefurahi sana endapo lolote lingetukia kuharibvu dunia na vyote vilivyomo.

Ni kama mtu ambaye alidhani au kuamini maisha yanamwonea na binadamu wote wanamchukia, hivyo akaondokea kumchukia kila mtu ikiwa ni pamoja na yeye mwenyewe. Kwa kuwa hana silaha wala uwezo wa kuiangamiza dunia, ndipo akaandika kitabu hicho ambacho binadamu wanateketezwa ovyo na mhusika wake mkuu kujiua mwishoni. Sababu ya vifo vyao haionekani, sababu ya kujiua kwake haikutajwa. Nje ya hayo, muswada huo uliandikwa kwa mtindo usioleweka na lugha isiyotamanika. Kitenge hakumbuki alivyofaulu kuusoma mpaka mwisho.

Kitenge akamgeukia mwandishi huyo na kumtazama. Naam, uso wake ulidhihirisha yote, macho yake yalisema kila kitu. Ni mtu aliyetaabika akakata tamaa. Tazama uso ulivyojikunja! Tazama macho yanavyotangaza uadui! Tazama tabasamu lake lilivyoficha chuki! Kitenge akajikuta akimwogopa.

“Ndivyo, bwana Ramadhani,” alisema kwa jitihada. “Muswada wako kama alivyokwambia dada huyu, haujafikia kiwango. Unahitaji marekebisho mengi. Kwa kuwa hapa tunayo miswada mingi mno si rahisi kufahamu wapi uliwekwa. Pengine tumeutuma kwa wasomaji wa nje. Mpe muda aendelee kuutafuta.”

“Sina muda zaidi bwana Kitenge,” sauti yake ilikuwa na hasira kama macho yake. “Hujui taabu kiasi gani nilipata hata kuukamilisha. Bado huo ni wa nne, yote imo mikononi mwa wachapishaji. Na jibu ni hilohilo, ‘ngoja.’ Tafadhali leo hii nitoke na muswada wangu. Jana nilipiga simu nikiwaambia niukute, leo mnasema kesho. Nisipoupata leo kwa kweli utajilaumu Kitenge.”

Kitenge na Rusia wakatazamana. “Ya nini maneno yote hayo?” alihoji Kitenge baada ya kucheka kidogo. “Unadhani tuna haja gani ya kukaa na muswada wa aina ile? Mara tu utakapopatikana utapewa.”

“Nitapewa?” Ramadahani alidakia akiinuka, Kitenge akashangaa kuona alivyo mrefu mwenye mwili mkubwa. Fedha au chakula zaidi kingeweza kumfanya awe pande la mwanamume zaidi ya alivyokuwa.

“Nitapewa!” alinguruma tena. “Wadhani sifahamu kitu gani kinatokea? Usijidanganye bwana Kitenge, nafahamu vizuri sana kuwa muswada huo umeubadili jina na kufanya umeutunga wewe. Najua kuwa sasa hivi, uko KIUTA ambako unachapwa.”

“Nini?” Kitenge aliuliza kwa mshangao akimgeukia Rusia. Wakaangua kicheko.

“Chekeni, ndiyo. Lakini kaeni mkijua kuwa hicho ni kicheko chenu cha mwisho pamoja. Nisipoupata muswada wangu kesho nitahakikisha mmoja wenu anachekea kuzimu, naapa!” Akamgeukia Rusia na kuongeza, “Nakupa hadi saa nane niwe nimeupata, vinginevyo mtajilaumu.” Akageuka na kuanza kuondoka.

Kitenge akamwahi kumshika mkono, “Ngoja bwana Rama,” alimweleza, “Hivi unafahamu usemalo?”

“Nafahamu.”

“Kwamba nimeubadili muswada wako uonekane kuwa nimeutunga mimi?”

“Ndiyo.”

“Ni nani huyo aliyekupa wazo la kipumbavu kama hilo?”

Ramadhani hakujibu. Si kwamba hakutaka kujibu bali hakuwa na jibu halisi. Alijua na kuamini kuwa Kitenge aliubadili muswada huo. Alikuwa na hakika, hakika ambayo ilimtatanisha yeye binafsi kila alipojiuliza ni wapi alikoipata. Anachokumbuka vyema ni kitu kama maongezi ambayo aliyasikia baina ya watu wawili wafanyao kazi KIUTA wakisema wameletewa muswada wa mtu anayeitwa Bazile Ramadhani watayarishe na kubadili jina la mtunzi kuwa Kitenge.

Watu hao walisema kuwa muswada huo utamtajirisha sana Kitenge. Kwamba kama wangekuwa wao, wangeamua kuua kuliko kuacha Kitenge asifike na kujitajirisha kwa jasho lao. Ramadhani hakumbuki pia kama aliwajibu chochote watu hao, anachokumbuka vyema ni nadhiri aliyoweka

ya kujiua au kumuua Kitenge endapo muswada huo usingepatikana. Hilo alilidhamiria akizingatia taabu alizokwishazipata katika harakati zake za uandishi wa vitabu.

Kama utunzi huwaletea watu wengine faraja, yeye ulimzalia simanzi. Kama wengine huwapa utajiri, kwake ulimfanya fukara zaidi. Alikuwa ameanza kutunga tangu akiwa shuleni, muda wake wote wa mapumziko aliutumia kuandika. Senti zake zote za matumizi ziliishia kununua kalamu, karatasi na stempu za kusafirishia. Akawa hana rafiki.

Wenzake wote walimdharau wakimwita mwendawazimu. La kusikitisha zaidi ni jinsi miswada yake ilivyorudishwa na wachapishaji wakidai 'haieleweki' wala hana 'fununu' juu ya mtunzi. Hakukata tamaa. Alipokuwa sekondari vitabu vilianza kutoa 'picha' ya kutamanika. Wachapishaji walianza kumtia moyo kwa kumwelekeza hapa na pale. Halafu miswada ikaanza kupotea. Kila alipotuma haukurudi. Barua za madai hazikusaidia. Ofisi za wachapishaji wengine hata hazikujulikana kama kweli zipo, alizitafuta bila mafanikio. Miswada mingi ikatoweka!

Huu aliompa Kitenge ulikuwa wa nne kati ya zile zilizokuwa mikononi mwa wachapishaji. Aliupenda na kuuthamini kuliko yote. Hakudiriki kuutuma kwa posta, bali aliupeleka kwa mkono baada ya kuitafuta ofisi hii kwa siku kadhaa. Matumaini yalikuwa yamezidi baada ya kumwona Kitenge, mtunzi mashuhuri, akitabasamu baada ya kusoma sehemu kadhaa siku ile alipouleta. Leo aambiwe hauonekani, wakati ana uhakika uko mitamboni! La asingevumilia, lazima huu uwe ama mwanzo wa faraja zake ama mwisho wa mateso yake!

"Nani alinipa wazo hilo?" alijibu Kitenge kwa swali jingine. "Sina haja ya kumtaja," akalaghai. "Ninalokutaka uelewe ni kuwa njama zako ziko hadharni. Ukiendelea nazo utapoteza bure maisha yako. Saa nane nitarudi hapa. Tafadhali nikute muswada wangu, vinginevyo, kichwa chako halali yangu."

Akatoka na kuufunga mlango kwa nguvu.

Rusia akajaribu kucheka kicheko ambacho alikikatiza ghafla baada ya kuhisi kuwa hakikuwa na ladha yoyote ya kicheko. Kadhalika macho ya Kitenge ambayo yalimtazama kwa namna ambayo hakupata kuiona huko mbeleni, ilikuwa sababu nyingine iliyomkatisha kicheko hicho.

"Usijali bosi, ana wazimu…"

"Labda," Kitenge alidakia, "Suala ni watu wangapi wenye wazimu watakaonisumbua asubuhi ya leo? Nisipoangalia wataniambukiza wazimu wao." Alipoona Rusia akipanua mdomo kuuliza swali, aliongeza harakaharaka, "Hatuhitaji watu wenye wazimu katika ofisi hii. Jitahidi kutafuta muswada wake umpatie. Usisahau kumwonya asilete kazi yake nyingine hapa."

Baada ya maneno hayo alitoka nje.

HUKO nje Kitenge hakujua aende wapi. Moyo haukumpa kwenda kokote. Kurudi ofisini roho ilikataa vilevile. Kwa muda aliduwaa hapo nje ya ofisi yake akitazama pande zote. Mara, akajikuta akiifuata miguu ambayo ilianza safari bila idhini yake. Ilimwongoza hadi Coffee Bar, chini ya Telephone House.

Hapo aliwakuta baadhi ya rafiki zake ambao walimkaribisha kwa kahawa ambayo aliinywa japo hakushiriki katika maongezi. Baada ya kitambo, alijikuta kabaki peke yake. Miguu ikamchukua tena hadi British Library ambamo alishika kitabu hiki na kile na kukodolea macho maandishi, lakini akiwa haoni chochote.

Mawazo yake yalikuwa yakitatanishwa na siku kama ya leo kwake. Wazimu? Alikuwa akijiuliza. Ramadhani pia ana wazimu? Na vipi kisa chake, si kinatosha kuwa hadithi nzuri? Hadithi ya mtunzi aliyechanganyikiwa, ambaye baada ya kushindwa kuitumia vyema kalamu yake anatumia ulimi wake kwa vitisho. Naam, ni hdithi nzuri. Ataiunganisha na tukio la Machozi. Atawafanya wote wahusika wakuu. Mwisho wa hadithi? Swali hilo alilipuuza tena. Atapata mwisho wa kuridhisha baada ya hadithi kuanza.

Mara akasikia furaha ikimjia tele moyoni. Pengine alicheka kwa nguvu, kwani aliwaona watu kadhaa waliokuwa wakisoma kimya wakiinua macho kumtazama. Akatua mezani kitabu alichokuwa nacho mkononi na kutoka nje.

Akaifuata tena Barabara ya Samora hadi alipoifikia sanamu ya askari. Hapo alielekea baharini akiiendea hoteli ya New Africa. Hotelini hapo alipata kiti katika meza iliyokuwa imekaliwa na Wazungu watatu, mmoja akiwa mwanamke. Akaagiza bia nne aina ya Safari, akiwakaribisha wale Wazungu. Walipokataa alizinywa zote moja baada ya nyingine. Baada ya hizo aliagiza whisky. Jinsi alivyokunywa harakaharaka, haukupita muda akawa hajiwezi.

Mmoja kati ya Wazungu hao akamwinamia na kumnong'oneza: "Excuse me sir, i think you have taken too much. Can't you switch off and go back home?"
Kitenge alimkosa kofi hafifu huku akisema, "Go to hell."

Wazungu hao wakaondoka na kuhamia meza nyingine. Aliendelea kunywa. Kisha usingizi ukamchukua, akainamia meza na kujilaza kwa starehe.

Alipoinuka alijikongoja kuendea teksi. Dereva akamsaidia kuingia baada ya kuuliza anakoishi. Kitenge aliitazama kwa taabu saa yake ambayo ilisema ni saa mbili za usiku kasoro dakika kadhaa. "Magomeni Mapipa Mtaa wa Kiyumba namba kumi na mbili," alijibu kilevi huku akilala tena.

Kilichomzindua tena ni dereva ambaye alimsukasuka kumwamsha. Walikuwa wamewasili. Akajikongoja kuingia ndani, nusura amgonge mama mwenye nyumba ambaye alikuwa kasimama mlangoni akimtazama kwa mshangao kwani alikuwa hajawahi kumwona Kitenge akilewa kiasi hicho. Kitenge alifungua mlango kwa shida, alipoingia hadi chumbani hakujishughulisha kuwasha taa wala kuvua viatu. Alijibwaga kitandani na kuanza kukoroma.

Ilikuwa usiku wa manane alipokurupuka ghafla kwa maumivu makali ambayo yalipenya kifuani mwake. Mkono wenye nguvu ulimkandamiza asiweze kuinuka kutoka kitandani hapo. Mkono wa pili ulimziba mdomo hata akashindwa kutoa sauti. Pigo la pili lilipenya hadi moyoni, Kitenge akahisi maumivu yakipungua na badala yake akimezwa na usingizi mzito wenye kiza cha kutisha. Usingizi ambao ulimfanya asisikie chochote kisu kilipopenya kwa mara ya tatu katika kifua chake.

"SEMA kama mwanamume, sajini Abdala!" InspeKta Kombora alifoka, macho kayatoa. "Zungumza lugha ya kiaskari; amekufa au ameuawa?"

"Ameuawa afande,"Abdalla alisema akitua faili lililokuwa kwapani mwake. "Taarifa kamili ya kifo na mauaji yake utaipata katika faili hilo."

Kombora alipokea faili na kulitupia jicho la haraka haraka. Kisha alitazama saa yake ambayo mshale wa dakika ulikuwa juu ya kumi na mbili, wa saa ukiwa juu ya nane. Ghafla, aliinua uso wake na kumtazama sajini Abdala. Macho yake yalitulia kwa muda juu ya uso huo wenye macho maangavu, yakateleza hadi juu ya kifua chake kipana na kiwiliwili kirefu ambacho kilitoa picha ya ukakamavu.

Ingawa alimtazama kijana huyo ni macho tu yalikuwa yakimwona. Kifikra alikuwa mbali akifikiria kifo hiki na kujaribu kulinganisha na simu ile aliyoipokea jana kutoka kwa mtu asiyejulikana. Mtu ambaye alidai anajisikia kuua mtu. Sauti hiyo ikiwa haina chembe yoyote ya mzaha ilikuwa imemfanya Kombora ashinde kutwa nzima ya jana akiwa na hofu ya kupokea habari mbaya.

Usiku ulipoingia hofu hiyo ilimzidi, kwani mara nyingi ni usiku ambapo waovu hutenda maovu yao. Hakupata usingizi kikamilifu, kila dakika alitegemea simu ambayo ingemfahamisha maafa. Hivyo kulipopambazuka bila habari hiyo kumfikia, alianza kufarijika akidhani kuwa pengine aliipa uzito usiostahili ile sauti; yawezekana ni mlevi au mpungufu wa akili na hata mtu mzima kabisa ambaye alikuwa na muda wa kuchezea akaamua kuutumia kwa kuwasisimua polisi, lakini mawazo hayo yalimtoka Kombora mara alipopokea simu ya kumjulisha kifo hicho alipokuwa akijiandaa kuja kazini.

"Nani aliyeuawa?" alinguruma katika chombo cha simu.

"Kitenge."

"Kitenge! Tuna vitenge madukani sajini?"

"Kondokondo Kitenge afande. Yule mtunzi mashuhuri wa hadithi za ujambazi na upelelezi."

“Alaa!”

Alifahamishwa kwa ufupi maafa hayo yalivyotokea. Ndipo akaharakisha kuja ofisini ambako alikabidhiwa faili la mkasa huo ambalo bado alikuwa kaduwaa nalo kabla hajaanza kulisoma.

“Ungelisoma haraka mzee,” sajini Abdalla alimzindua, “Kuna mengi ambayo hayajaanza kutekelezwa, yanayoisubiri idhini yako. Kwa maoni yangu, muuaji hayuko mbali, tutamtia mikononi mara moja.”

Kombora akayateremsha macho yake mezani na kuanza kupekua faili hilo. Hakujishughulisha kuipokea saluti ya Abdala, alipokuwa akiondoka. Badala yake, kama kwa kumtupia aliongeza, “Usiende mbali. Nitakuona mara baada ya hii,” alisema.

Aliisoma kwa makini. Hakukuwa na mengi zaidi ya aliyokwisha simuliwa. Marehemu alikuwa ameuawa kwa kisu baina ya saa nne na saa nane usiku. Maiti yake ilikutwa chali juu ya kitanda. Kwa mujibu wa daktari, marehemu alikuwa amelewa sana kabla ya kufa, hivyo hakufanya vurugu yoyote kabla ya kukata roho.

Ripoti ya wataalamu wa vidole inadai haimo alama yoyote ya vidole zaidi ya zile za marehemu mwenyewe. Jambo ambalo linaonyesha kuwa muuaji au wauaji walivaa glovu maalumu kwenye mikono yao kabla ya kugusa kitu chochote humo ndani. Silaha iliyotumiwa haikuonekana. Taarifa iliongeza kwamba, aliyearifu polisi ni mmoja wa wapangaji ambaye aliarifiwa na bi kizee mwenye nyumba aliyeigundua maiti alfajiri.

Kilichomsisimua Kombora katika ripoti hiyo ni madai ya bi kizee huyo kwa makachero kwamba anamfahamu muuaji, ati ni mwanamke ambaye alidai kwa sauti na kuapa kuwa angemuua Kitenge. Hilo Kombora hakulitegemea.

Kwanza hakutegemea ufumbuzi uje kwa urahisi namna hiyo; pili hakudhani kuwa muuaji angetukia kuwa mwanamke. Sauti iliyompigia simu ilikuwa ya kiume. Aliamini kuwa ni mwenye sauti hiyo ambaye alielekea kuwa muuaji. Hivyo aliinua simu yake na kumtaka opereta amwitie sajini Abdala.

“Afande.”

“Sajini. Unaonaje kesi hii, waweza kuyaamini maneno ya huyu mama?”

“Hadi dakika tano zilizopita nilikuwa nikiyaamini afande…”

“Sikia Abdala,” Kombora akamkatiza kwa ukali, “Hatuna muda wala nafasi ya kuzungumza kwa mafumbo. Katika ripoti yako mwenyewe unadai kuwa silaha ya mauaji haikupatikana. Hilo peke yake linatosha kukufahamisha kuwa muuaji bado ana nia au uwezo wa kufanya unyama mwingine kwa silaha ileile au nyingine, wakati wowote. Hatutaki jambo hili litokee. Sasa, haya mambo ya kuamini ripoti yako mwenyewe dakika tano zilizopita yanaingiaje katika swali langu?”
Sajini Abdala, akiwa mtu anayemfahamu vyema ofisa wake, hasa katika masuala ya aina hii, kuwa hapendi mzaha wala maneno mengi, alitabasamu kwa uficho, kisha akamjibu mara moja.

“Nilichotaka kusema ni hivi afande, taarifa hiyo ya mama mwenye nyumba alinipa mimi mwenyewe asubuhi ya leo. Alikuwa na hakika na kile anachosema. Nikaelekea kumwamini, hasa baada ya kusema kuwa mama huyo anayeshukiwa anayo kila dalili ya ulevi wa gongo na bangi. Mlevi wa vitu hivyo anaweza kufanya lolote afande, hasa anapoondokea kuamini kuwa ni wewe uliyemfanya yeye aishie kuwa mlevi hali wewe unainuka kimaisha.”

“Sawa,” Kombora alijibu. “Na baada ya dakika hizo tano?”

“Baada ya dakika tano, siyo kwamba simwamini kabisa, ila nimechanganyikiwa tu. Nilikuwa nikipiga simu katika ofisi ya marehemu kuwafahamisha maafa haya. Katibu wake mahsusi akaropoka kuwa, alitegemea jambo hilo. Nilipomuuliza kwa vipi, akaniambia kuwa anamfahamu hata muuaji kwa jina na sura. Nilipomuuliza kama mtu huyo ni mwanamke, alikanusha na kudai kuwa ni mwanamume, mtunzi wa vitabu. Kwamba mtu huyo alifika ofisini hapo na kuahidi kumuua Kitenge. Unaona ilivyo vigumu mzee? Wauaji wawili, marehemu mmoja! Kila shahidi ana imani na ushahidi wake.”

“Kweli inatatiza,” lilikuwa jibu la Kombora baada ya kuwaza sana. Kisha akaongeza, “Nitapenda kuonana na hawa mashahidi mara moja. Andaa gari twende kwanza huko nyumbani kwake halafu tutamwona huyo karani wake ofisini.”

“Timamu afande.”

Dakika chache baadaye walikuwa ndani ya Land Rover wakielekea Magomeni Mapipa. Walipoufikia Mtaa wa Kiyungi hawakuhangaika kuipata nyumba waliyoihitaji. Nje kulikuwa na watu wengi waliozungumza hili na lile.

Kombora na Abdala waliupenya umati huo kwa urahisi, kwani watu wenyewe walijitenga kuwapisha. Ndani walikuta umati mwingine ambao ulimzunguka mama mwenye nyumba aliyekuwa akiendelea kueleza kwa sauti yenye shauku kubwa. Kombora aliwataka radhi majirani hao na kumchukua mama katika chumba cha marehemu.

“Sijisikii kabisa kuingia chumba hiki baba, kinatisha,” alisema bibi huyo huku akiingia.

“Usijali mama. Hamna litakalotokea,” Kombora alijibu bila kumtazama. Macho yake yalikuwa yakitazama kila upande. Kama ilivyosema taarifa, haikuonekana dalili yoyote ya kuashiria mauaji katika chumba hicho. Kila kitu kilikuwa katika hali inayostahili. Ni shuka moja tu yenye damu iliyosaliti siri hiyo. Shuka nyingine bila shaka zilikuwa zimechukuliwa na polisi kwa uchunguzi zaidi. Kisha Kombora aliyarejesha macho yake kumtazama kizee ambaye alikuwa akisema.

“Wamekuja hapa wenzako baba. Wanauliza mengi ambayo hayana maana. Muuaji najua ni yule mwanamke tu. Sauti yake inaonyesha wazi alikuwa akisema kweli. Kama angekuwa mwingine, lazima angeiba kitu chochote humu ndani. Yule hakuwa na nia ya chochote bali kumuua tu.”

“Kweli mama,” alijibu Kombora. “Unaweza kumfahamu iwapo utamwona tena?”

“Bila shaka. Hata wewe baba, ukimwona japo hujawahi kumwona utamjua tu. Ana sura ya kutisha sana.”

“Unadhani tunaweza kumpata wapi bibi?” aliongeza Abdala.

“Mjukuu wangu, usiniambie hujui wanakopatikana walevi wa gongo. Darisalama hii ni kubwa, ndiyo, lakini nyie mnajua wapi na wapi mnaweza kumpata mwanamke yule.”

Kombora alitabasamu kwa haya kidogo kabla hajajibu, “Kweli mama, tutampata hivi karibuni. Unasema ulisikia marehemu akimwita Machozi sio?”

“Ndiyo baba, nitafurahi mkimkamata. Aweza kuua tena yule.”

“Tutamkamata bibi.”

Yakafuata maswali mengine ya kawaida. Ilimshangaza Kombora kuona bibi huyo alivyokuwa hodari wa kujibu maswali ambayo yangeweza kuwatatanisha wasomi na vijana. Walipotosheka walimshukuru na kumuaga. Wakatia moto gari na kurudi mjini.

OFISI ya BLACK POWER PUBLISHERS ilikuwa kimya kupindukia Kombora na Abdala walipoingia. Waliwakuta vijana wawili wa kiume wameinamia meza zao, na msichana ambaye mikono yake ililalia mashine ya chapa. Kombora aliyaona machozi yakimlengalenga msichana huyo pindi alipoinua uso kumtazama.
“Karibuni,” mmoja kati ya vijana wale alitamka polepole.

“Asante,” maofisa hao walijibu wakijiketisha juu ya viti vilivyokuwa wazi.

Yalifuata maongezi mafupi, Kombora akihoji juu ya hili na kutaka kujua juu ya lile. Mengi yalimsaidia ingawa ni machache yaliyopata nafasi katika daftari lake. Mengi yalikuwa yaleyale ambayo alikwishaambiwa kabla. Aliporidhika, alimgeukia msichana huyo ambaye alikuwa akijibu kwa nadra sana na kumwita, "Tafadhali bibie. Bibi Rusia kwa jina sio?"

"Ndiyo."

"Nadhani ni wewe mwenye ufunguo juu ya suala hili. Nina maana kuwa, ni ushahidi wako ambao utatuwezesha kumtia mkononi huyu muuaji mapema zaidi. Unasema una uhakika kuwa huyu kijana anayeitwa Bazile Ramadhani ndiye aliyemuua bwana Kitenge?"

"Naamini hakuna mwingine," alijibu bila kuwatazama.

"Kwa nini?"

"Mwenyewe alisema hivyo. Zaidi ya kusema anaonyesha kuwa ni mtu katili. Aliporudi mara ya pili nilipomjulisha kuwa muswada wake bado ulikuwa haujapatikana alitoa macho na kukimbilia katika chumba cha marehemu. Kama angemkuta naamini angemuua papohapo. Kwa bahati nzuri hakuwepo. Hata hivyo…" akasita na kufuta machozi yaliyomtoka ghafla.

"Pole dada," alitamka Abdala.

"Ulikuwa unahusu nini huo muswada wake?" Kombora alihoji.

"Mauaji tu, yaelekea ni mtu anayependa sana mauaji?"

"Na unafikiri umekwenda wapi?"

"Muswada huo sio? Kwa kweli hata mimi nashangaa. Iko hapa miswada iliyoletwa miaka miwili iliyopita. Huo wake hatujakaa nao miezi minne, hauonekani. Kama ungekuwa wa kuvutia, tungesema mwenzetu mmoja kauchukua nyumbani kwake akausome. Kila aliyejaribu kuusoma alikata tamaa."

Kombora akamshukuru na kuongeza, "Waweza kutusaidia vipi kumpata mtu huyu, Rusia?"

"Sidhani kama…"

"Huna barua yake yoyote yenye anuani yake?"
"Zipo nyingi. Alikuwa akiandika kila mara. Barua nyingine hata tulichoka kuzisoma. Nakumbuka iko moja ambayo aliiambatanisha na picha yake. Eti iwekwe nyuma ya kitabu."

"Itafute tafadhali."

Baada ya upekuzi mfupi katika majalada, Rusia alimkabidhi Inspekta Kombora barua tatu, moja ikiwa na picha. Kombora aliitazama picha hiyo kwa makini.

Akiwa mtu mzoefu wa kusoma picha za wahalifu alimwona Bazile vilivyo: kijana mwenye ndevu changa, umri baina ya miaka ishirini na mbili hadi ishirini na sita, sura yenye busara ingawa ilibeba macho yaliyokuwa yakitangaza mengi na hayakuwa na ladha ya maisha wala uangavu wowote, na ni kama ambayo yalikuwa yakinong'oneza kwa huzuni: "nimeonewa jamani."

“Ndiyo, huyu anaweza kuwa muuaji,” aliwaza Kombora, huku akimpa Abdala picha hiyo. Akafunua barua kusoma anuani. Ilikuwa rahisi kuliko alivyotarajia. Anuani zote zilitaja sanduku la kazini pale TEGRY. Kiwanda cha kutengenezea vifaa vya plastiki.

“Tunashukuru sana dada,”Kombora aliaga ghafla akiinuka. “Nadhani sasa tuondoke tukawahi shughuli nyingine.”

“Asante mzee,” alijibu msichana huyo akiinuka kuwatazama kikamilifu kwa mara ya kwanza. Macho yake hayakuchelewa sana juu ya umbo la makamo la Inspekta Kombora, ambalo nywele zilianza kumezwa na mvi, uso ukiingiliwa na mikunjo. Lakini macho hayo yalikawia katika umbo lenye kiasi kikubwa cha ujana la Sajini Abdala. Sura ikiwa nzuri na umbo la mwanamichezo, Sajini Abdala alipendeza vyema katika magwanda yake ya kipolisi machoni mwa Rusia.

“Karibuni tena.”

“Asante bibie,” Abdala alijibu.

Walipofika katika ofisi yao walianza maongezi yenye lengo la majadiliano. Kila mmoja alitaka wazo la mwenziwe.

“Nadhani mwenye nafasi nzuri ya kuua ni huyu mwanamke Inspekta. Yeye ndiye aliyefika nyumbani kwa marehemu. Pia bado anaongozwa na nguvu za bangi na gongo. Simwamini mtu yeyote anayetumia vileo hivyo.”

“Kwa hiyo?”

“ Kwa hiyo, napendekeza uturuhusu tumsake huyu mama. Tukiwatuma vijana huko katika mageto ya Luhanga, Buguruni, Kigamboni, Kawe, Tandale na kote nadhani atapatikana tu. Sidhani kama yuko nje ya jiji hili mara hii.”

Kombora hakujibu mara moja. Yeye alimshakia zaidi huyu mtunzi, Bazile. Sauti katika simu ile haikuwa ya kike. Wala hakuona kama mwanamke huyu mlevi wa gongo angekuwa na haja ya kumwandaa na kumpigia simu polisi kama hadithi ile ya Simu ya Kifo.

Hata hivyo, bado aliona umuhimu wa kuwapata wote wawili mapema iwezekanavyo. Yawezekana kuwa mtunzi yule hahusiki. Yawezekana vilevile kuwa yeyote kati yao hahusiki! Aliwaza ghafla kwa hofu. Jambo ambalo litaongeza uzito katika jukumu hili.

2

KOMBORA hakujibu mara moja. Yeye alimshakia zaidi huyu mtunzi, Bazile. Sauti katika simu ile haikuwa ya kike. Wala hakuona kama mwanamke huyu mlevi wa gongo angekuwa na haja ya kumwandaa na kumpigia simu polisi kama hadithi ile ya Simu ya Kifo.

Hata hivyo, bado aliona umuhimu wa kuwapata wote wawili mapema iwezekanavyo. Yawezekana kuwa mtunzi yule hahusiki. Yawezekana vilevile kuwa yeyote kati yao hahusiki! Aliwaza ghafla kwa hofu. Jambo ambalo litaongeza uzito katika jukumu hili.

Kwa kawaida kesi hii isingemjia yeye Kombora au kikosi chake moja kwa moja. Ingekuwa kesi ya kushughulikiwa na vituo vya kawaida vya polisi. Kikosi hiki cha kumi na mbili kilikuwa chini ya idara maalumu inayoshughulikia masuala makubwa ya mauaji katika jiji hili. Kesi ambayo ilielekea kuwashinda polisi wa kawaida au yenye masuala yanayokanganya au hujuma za kiuchumi na kisiasa ndiyo iliyokuwa ikiletwa hapa.

Hii haikuwa kubwa kiasi hicho. Lakini alikuwa ameipokea na kuiomba toka majuzi alipopata simu ile inayodai mauaji. Alihisi muuaji huyo anamhitaji yeye. Ndipo akawaarifu polisi kumletea kesi yoyote ya mauaji ambayo ingetokea katika saa ishirini na nne.

Hata hivyo, hakuwa amemgusia yeyote juu ya simu ile. Wala hakuwa tayari kumgusia Sajini Abdala suala hilo. Hivyo alimwambia kwa sauti ya amri akisema, "Vizuri sajini. Nawahitaji haraka hawa wawili. Machozi na huyu Bazile. Nafahamu wajua lipi utafanya ili wapatikane kabla ya kesho."

"Bila shaka afande."

ULIKUWA ni usiku mbaya mno kwa walevi wa pombe haramu, hasa wanawake. Kote kulikofahamika au kushukiwa kuwa maskani ya walevi hao kulizingirwa na vijana wa polisi na JKT wenye kiu kubwa ya kuupima ujana wao. Wengi walikamatwa na kusukwasukwa kwa makofi na mabuti ya vijana wa polisi. Waliochukuliwa moja kwa moja walichukuliwa, walionusurika walinusurika. Mamia waliyosalia walichujwa hata wakasalia kina Machozi arobaini. Ni hao waliofikishwa kituo cha polisi. Huko pia walichekechwa hadi waliposalia watatu waliofanana kwa sura na tabia. Ni katika watatu hao alipopatikana Machozi aliyetakiwa.

"Wewe unasema umekamatwa Luhanga sio?"

"Ndiyo."

"Ulikuwa ukifanya nini?"

"Kwani vijana wako walikwambia nini bwana askari? Nilikuwa nikinywa na kustarehe. Sina jambo lingine la kufanya."

"Hujui kwamba gongo ni haramu kidini na kisheria?"

"Mangapi ni haramu na yanafanywa? Siachi gongo kwa taarifa yako! Bia haitengenezwi kwa ajili yangu wala watu wa aina yangu!"
Sajini Abdala akamkazia macho. Pamoja na uzoefu wake wa kutazamana na wahalifu wa kila aina, lakini macho ya huyu yalimtisha. Yalikuwa ya kila hali ya ulevi na wazimu. Yalitangaza waziwazi kuwa 'lolote laweza kutokea'. Baada ya misukosuko yote ya vijana wa polisi ambayo iliacha ushahidi wa jeraha dogo katika mdomo wa mama huyo na ngeu katika paji lake la uso, macho hayo hayakuonyesha athari yoyote. Yalikuwa imara yakimtazama sajini huyo na askari wote kwa dharau, kebehi na kutojali.

"Unamfahamu Kondokondo Kitenge?" Abdala alifoka ghafla.

"Mara ngapi nikwambie kwamba namfahamu?" Machozi alirudisha.

"Ni nani wako?"

"Mara ngapi nikwambie kwamba ni baba watoto wangu?"

Ni majibu hayo aliyokuwa kayatoa tangu aanze kuhojiwa suala hilo. Kilichomshangaza Abdala ni jinsi mama huyo alivyozungumza kwa uhakika kama aliyeamini anachokizungumza.

"Sikia wewe mwanamke," alinguruma Abdala. "Uko hapa si kwa mzaha ila ni suala gumu mno kwako. Hivyo nataka uache majibu ya kilevi. Unijibu kikamilifu. Sawa? Kwa taarifa yako, Kondokondo Kitenge amekufa. Ameuawa usiku wa jana!" Abdala alisita akiutazama uso wa Machozi kuona vipi ujumbe huo ungemwingia.

Kama alitarajia kuona mshangao au hofu katika uso huo, lolote kati ya hayo halikutokea. Machozi alikuwa vilevile kama mama aliyearifiwa kifo cha panya au kifaranga. “Umesema kweli askari?” Alihoji polepole. “Amekufa kweli?”

“Amekufa. Ameuawa usiku wa jana. Waweza kutuambia ni nani kamuua?”

Ndipo kitu cha kutisha kikatokea katika uso wa Machozi. Tabasamu. Lilikuwa la kutisha kuliko tabasamu lolte la mwanadamu. Abdala alililinganisha na lile la sokwe alilowahi kuliona katika hifadhi za wanyama. Baada ya tabasamu hilo Machozi aliropoka kwa sauti ya juu.

“Amekufa sio! Ameuawa….sikupata kupokea habari njema kuliko hiyo katika maisha yangu bwana polisi. .. ndiyo, namjua aliyemuua. Ni mimi mwenyewe. Nimemuua kwa mkono huu!” Akaupunga mkono wake wa kulia angani.

Sajini Abdala akaduwaa. Akawageukia wenzake ambao walikuwa katika mshangao pia. Hakuna aliyetarajia jibu rahisi kama hilo. Hivyo, badala ya kulikubali kama walivyotaka, wakajikuta wakilitilia shaka.

“Nadhani dada yangu hujui unalosema. Huna habari kuwa suala hili linaweza kukufanya ule kitanzi?” alisema askari mmoja.

“Najua! Na nitaingia kitanzini kwa furaha maadamu nimemuua!”

“Ulimuua lini?”

“Jana usiku.”

“Saa ngapi?”

“Sikumbuki vizuri, sijawahi kuwa na saa.”

“Ulitumia silaha gani?”

“Kisu!”

Askari wakatazamana tena. Kisha walibadili mtindo na kuanza kumuuliza mfululizo. Walishangaa kukuta mama huyo akisimama imara akiendelea kudai: “Nimemuua… Nimemuua.”

Taarifa hiyo ilipopelekwa kwa Inspekta Kombora nusura imtie wazimu. Alimsikiliza Sajini Abdala kwa makini kisha akakuna kichwa huku kainamia meza. Kisha alikuna macho akitazama dari. Aliporudisha macho hayo mbele yake yalikuwa yamejaa maswali.

“Unadhani anasema ukweli sajini?”

“Nani, mwanamke huyo sio? Hilo ndilo tatizo lenyewe afande. Ni vigumu kukataa au kukubali kuwa anasema ukweli. Mwenyewe kang’ang’ania hivyo.”

“Achana na maneno ya mlevi,” alidai Kombora. “Kinachotakiwa ni ukweli. Waruhusu vijana maalumu kwa shughuli za aina hiyo wafanye kazi yao hadi watakapohakikisha kuwa kama hasemi, anautapika ukweli huo. Sawa?”

“Sawa, afande.”

Kilichomfanya Kombora achanganyikiwe ni hiyo taarifa nyingine aliyoipata kwa sajini aliyepewa jukumu la kumpata Bazile Ramadhani, mtunzi ambaye Kombora alimshuku zaidi katika mauaji haya. Sajini huyo alirejesha majibu kwa 'radio call' ambayo yalimtisha Kombora.

Kwamba alipoenda Barabara ya Pugu kwenye kiwanda cha TEGRY ambako Bazile alikuwa akifanya kazi, aliarifiwa na wakubwa wake kuwa alikuwa hajafika kazini hapo siku mbili nzima. Baada ya kuhangaika sana, walimpata msichana mmoja ambaye alisemekana kuwa alikuwa rafiki wa Bazile.

Ni huyo aliyewaongoza hadi Kigamboni ambako Bazile alipanga chumba. Huko pia walikuta chumba kitupu. Jirani zake walidai kuwa 'ametoweka ' tangu majuzi. Hakuna aliyefahamu alikoenda. Hakuna aliyeagwa.

Ni hilo lililomtia Kombora mashaka zaidi. Aweza kuwa popote. Aweza kuua tena wakati wowote. Hivyo, alimwamuru sajini huyo kuendelea na upelelezi juu ya tabia na mwenendo wa mtu huyo.
Maongezi hayo Kombora aliyasikiza moja kwa moja katika 'radio call' hiyo.

"Bi nani sijui mwenzangu."

"Mimi sio? Naitwa Ashura."

"Ndiyo, bi Ashura. Waweza kutusaidiaje ili kumpata mapema huyu rafiki yako? Aweza kuwa kaenda wapi?"

"Kwanza ningeomba nisieleweke moja kwa moja mimi ni mpenzi wake Bazile, bwana askari. Niwie radhi kwa hilo lakini ndio ukweli wenyewe. Niliondokea kumpenda lakini hapendeki. Hana muda wa mapenzi. Na hata maongezi hajui. Ukitaka kumsikia akizungumza lazima uongelee vitabu. Mimi mambo ya vitabu siyajui. Hivyo nilikuwa kama najilazimisha kwake tu. Mara kwa mara muwapo pamoja utamkuta kakusahau kabisa yuko maili elfu moja katika dunia ya peke yake. Hivyo kuhusu swali lako siwezi kulijibu. Hakuwahi kuniamini katika masuala yoyote ya maisha yake isipokuwa ya vitabu tu."

"Ahsante sana. sasa dada Ashura, unadhani Bazile aweza kuua mtu?" kicheko laini cha msichana yule kikamfikia Kombora.

"Kuua! Bazile! Siamini. Kwa kuwa anaandika vitabu vya mauaji siyo? Kwa kweli sijapata kuona mtu mwoga au mstaarabu kama yeye. Hajapata kumtukana mtu, hajapata kumpiga mtu kofi, ataanzaje kuua? Ebu bwana askari, kweli mnamtafuta kwa nini? Eti mnamshuku kaua mtu?
"Kuua au kuuawa. Hajaonekana siku mbili. Unadhani habari hiyo ni njema? Chumbani kwake kila kitu kimo, isipokuwa yeye tu."

"Kweli kabisa!"

Baba mwenye nyumba naye alikuwa na yake.

"Kuua siyo? Japo ni mtulivu, mimi nadhani anaweza kabisa. Mtoto hakai nje na wenzake kuongea. Kutwa nzima chumbani. Ukimuuliza nini anafanya atadai anasoma. Ukichungulia utamwona kainamia meza anaandika. Hachoki kuandika. Nadhani alikuwa na aina fulani ya wazimu. Yaweza kumtuma kufanya lolote."

Hayo ndiyo yaliyokisumbua kichwa cha Kombora. Kafa mtu mmoja. Washukiwa wawili ambao hawafahamiani wala kuishi pamoja. Mmoja anadai kuwa kaua, wa pili haonekani aliko. Angewezaje kulipeleka mbele suala hilo likiwa katika utatanishi mzito kama huo?

La muhimu lilikua kupatikana huyo Bazile. Akiwa katika milki ya polisi, Kombora angeweza kufarijika zaidi na kufahamu namna ya kutatua msongamano huo. Hakujua vipi na lini Bazile angeingia mkononi.

Simu ikalia. Kombora akainyakua na kuiweka sikioni akinguruma. "Inspekta Kombora hapa."

“Kombora! Rafiki yangu Kombora siyo?”

Haikuwa sauti ngeni masikioni mwa Kombora. Ilikuwa ileile ambayo alihitaji kumpata mwenyewe. Naam, sauti ileile ambayo sasa, Kombora hakuitarajia, akishuku mwenyewe tayari yu ahera. Hakujua kama ilimpasa kuisikiliza au la. Hakujua ajibu nini zaidi.

Maadamu chombo cha kusikilizia bado kilikuwa sikioni, aliendelea kumsikiliza.

“Mbona kimya rafiki yangu Inspekta? Upo? Sikia ndugu yangu najisikia kuua mtu mwingine. Waweza kunisaidia?”

“Wewe! Ni wewe Bazile Ramadhani?” aliuliza Kombora kiasi akitetemeka.

“Umelipataje jina langu mapema hivyo Inspekta? Kumbe u hodari kiasi hicho? Ndiyo ni mimi. Kwa heri Inspekta.”

“Sikiliza….” Tayari simu ilikatwa.

Kombora aliduwaa nusu dakika. Katika nusu nyingine alikuwa alikuwa akimngurumia opereta kuchunguza ilikotoka simu hiyo.

Jibu halikumfariji. Simu ilipigwa kutoka katika vibanda vya simu vilivyoko huko Forodhani. Simu ya wazi ambayo mtu yeyote wakati wowote anaweza kupiga.

Hata hivyo hakusita kutuma makachero hao. Hakutokea yeyote aliyekuwa tayari kueleza sura na umbile la mtu au watu walomtangulia kutumia simu. Pamoja na watu wote waliokuwa hapo kuonyeshwa picha ya Bazile, jibu la haja halikupatikana.

IWAPO Kombora alikuwa akisubiri habari za kifo kimoja, basi alikosea sana. Usiku huo walikufa watu wawili. Wa kwanza alikuwa Fambo Wamangi.

Kama ilivyo kawaida ya kifo, kilimtokea bila kutarajia. Kutwa nzima alikuwa ameshinda katika ofisi yake alikuwa akiendelea na shughl zake za kila siku. Alikuwa meneja-masilahi katika kampuni ya Enterprise.

Kampuni hii ilishughulikia biashara za aina zote na mataifa mbalimbali. Wote waliomwona siku hiyo walishangazwa na jinsi alivyokuwa mchangamfu na mcheshi zaidi ya kawaida yake.

Baada ya kazi, alirejea nyumbani kwake ambapo alicheza na wanawe, akacheka na mkewe na kutaniana sana na jirani zake. Saa mbili za usiku alitoka na mmoja wa jirani hao kwenda baa ya jirani ambapo walipata chupa mbili mbili zilizomfanya Wamangi azidi kuchangamka. Kisha walirejea nyumbani. Wamangi akakiendea kitanda ambako alikuwa ‘mtundu’ kama siku zile za ujana wao, jambo ambalo lilimfurahisha sana mama watoto wake. Usingizi uliwakuta katika hali hiyo ukawachukua na kuwahamisha hadi katika milki nyingine, ya ndoto na starehe.

“Nilipoamka nilijikuta bafuni,” yalikuwa maelezo ya mama huyo kesho yake. “Nilikuwa nimefungwa kamba mkononi na kitambaa mdomoni. Nikajitahidi hata kamba hizo zikafunguka. Nikarejea chumbani ambako niliyoyakuta yalikuwa hayatazamiki. Mume wangu mpenzi alikuwa kalala chali kitandani, uchi kama alivyolala usiku wa jana, mwili wake mzima ukiwa umelowa damu nzito ambayo ilikuwa ikiendelea kutiririka kutoka katika jeraha baya mno la kisu au sime lililokuwa wazi kifuani. Sikuweza kutazama mara mbili. Sikuweza kupiga kelele. Nadhani nilianguka na kuzirai kwani nilipopata fahamu tena nyumba nzima ilijaa watu, askari na jirani ambao walikuwa wakinihudumia.”

Kifo hicho ni katika Mtaa wa India, jengo la Abdulkar lenye ghorofa nne. Marehemu alikuwa akiishi katika ghorofa hiyo ya nne pamoja na jirani ambao ni familia mbili za Kiafrika na tano za Kihindi. Ni mmoja kati ya jirani hao aliyeipigia simu polisi alfajiri baada ya kusikia watoto watatu wa marehemu wakilia kwa nguvu bila msaada wowote wa wazazi wao. Alipochungulia na kuwaona wazazi katika hali hiyo, alidhani wote walikuwa wamekufa, hivyo aliiambia polisi, “Bana na bibi ake yote kafa.”

Kifo cha pili kilikuwa kimetokea kilomita kadha wa kadhaa nje ya wilaya hii ya Ilala. Hicho kilitokea huko Kinondoni Mkwajuni. Marehemu kama bwana Jugeni Kawamba, kama Wamangi kutwa nzima ilikuwa ya kawaida kwake.

Kwa muda wa miezi kadhaa, Kawamba hakuwa na kazi. Hivi alikuwa kamrejesha mama watoto wake pamoja na wanawe wote kwao katika vijiji vya Wilaya ya Mbulu mkoani Arusha, ili aweze kuyakabili maisha pindi akiendelea na msako wa kutafuta kazi.

Akiwa mtu aliyepitia madaraka makubwa, yenye marupurupu ya kutosha, maisha ya kuishiwa yalimtatiza mno. Ingawa hakuwa kaishiwa kiasi cha kukosa pesa ya matumizi, lakini kule kuona akiba yake ya benki ikielekea kumezwa kabisa bila matumaini ya kuongeza chochote juu ya akiba hiyo siku za usoni kulimtia hofu.

Hivyo alikata makundi ya urafiki wa matumizi na kuwa mtu wa kutulia nyumbani akijisomea.

Usiku huo usingizi ulimtoka kabisa. Japo alijituliza kitandani macho kayafunga na kujaribu kubembeleza usingizi, haukukubali kabisa. Mawazo yalikuwa yakimrejesha kuitazama hali yake kiuchumi inakoelekea. Haikuridhisha. Mara akaanza kuijutia safari yake ya majuzi aliposafiri kwa ndege kwenda na kurudi Zanzibar ambako aliitwa kwenda kufanya mahojiano ya ijara. Labda asingesafiri kwa ndege, meli ingetosha! Aliwaza. Mara alihisi kuinamiwa na dude refu jeusi na alipojaribu kufumbua macho yalizibwa kwa mkono wenye nguvu kama chuma. Juhudi zake zote za kuutoa mkono huo hazikufua dafu. Alipojaribu kurusha teke lilidakwa kwa mkono mwingine. Dakka hiyohiyo jisu kali lilipenya kifuani kwake kwa maumivu makali. Hakuwahi kupiga kelele, kwani mkono uliokuwa usoni ulihamia mdomoni kuuziba. Pigo la pili lilimmaliza. La tatu hakulisikia kabisa.

Akiwa mtu anayeishi peke yake katika nyumba hiyo ambayo hata alikuwa hajamaliza mkopo wake aliopewa na THB, ilichukua muda kabla maiti yake haijagunduliwa. Ni kijana muuza magazeti ambaye aliigundua. Kijana huyo akiwa na mkataba wa kumletea magazeti kila siku, asubuhi hiyo pia alimfikia.

Akashangaa kuona mlango ukiwa wazi alfajiri yote hiyo jambo ambalo halikuwa la kawaida katika nyumba hiyo. Hivyo aliamua kuchungulia. Mlango wa chumbani pia ulikuwa wazi.

Macho yalipofika chumbani humo yalivutwa na damu kavu ambayo ilitapakaa sakafuni, kitandani akiwa kalala mzee Kawamba, jeraha kubwa likicheka kifuani mwake. Akitetemeka, kijana huyo aliwaita jirani ambao walijua la kufanya.

“HAIWEZEKANI. Hawezi kuvumiliwa zaidi. Lazima yeye au maiti yake ipatikane katika muda wa saa ishirini na nne zijazo.
“Unasikia Sajini Abdala?” alifoka Inspekta Kombora, macho kayatoa kwa ukali na hasira.

Mbele yake kulikuwa na majalada lukuki. Jalada la Machozi ambalo lilikusanya habari zake zote na kutokuacha mwanya wowote unaomuunga na kifo cha Kitenge japo mwenyewe aliendelea kudai hivyo licha ya mateso ili aseme ukweli.

Jalada la marehemu Wamangi na Kawamba lilionyesha mienendo yao ya kutwa nzima pamoja na shughuli zao za nyuma. Hayo pamoja na maandishi mengine, yalifurika mbele ya Kombora yakimdai atulie na kuyasoma. Hakujisikia kusoma chochote.

Hakujisikia kutulia. Alitamani apate uwezo wa kupaa, aruke hadi mbele ya Bazile popote alipo ammiminie risasi zote zilizokuwepo katika bastola yake. Ni hilo tu alilohitaji.

“Lazima afe,” akaongeza.

“Ni kweli afande. Ni mtu hatari mno kuendelea kuishi nje ya kuta za magereza. Tatizo ni jinsi alivyoondokea kuwa hodari mno pamoja na mitego yote ya polisi usiku na mchana, bado anawakwepa na kutimiza nia yake,” alijibu Sajini Abdala aliyekuwa kaketi mbele ya Kombora.

“Mimi pia hilo linanishangaza,” Kombora alimuunga mkono.
“Nilivyoichunguza historia yake ya nyuma inaonyesha kuwa aliwahi kupitia JKT. Pengine ni hilo linalompa uwezo wa kutushinda ujanja. Bila hivyo, ningeweza kupendekeza kuwa anasaidiwa na mtu au watu.”

“Kweli mzee, kwa mfano alivyoua siku ya leo. Ameweza kuua hapa mjini kisha akasafiri hadi Kinondoni ambako ameua tena. Utadhani kuna mtu anayemsaidia kwa usafiri.”

“Aweza kuwa anatumia mabasi ya abiria. Akiwa kakificha kisu chake vyema, kondakta na abiria wanamwona kama mtu wa kawaida tu. Nimejaribu kutazama uwezekano wa mtu yeyote kumsaidia sikuona. Yeye ni kichaa aliyepata kichaa hicho baada ya utunzi kuiathiri akili yake na vitabu vyake visivyoeleweka kudharauliwa na watoaji. Amepata wazimu. Nani atakayemsaidia mwendawazimu kama huyo? Angeweza kusaidiwa na mwehu mwenzake Machozi, lakini katika uchunguzi inaonyesha kuwa hawafahamiani kabisa. Na bado Machozi tunaye ndani. Hapana sajini, tusisumbue vichwa vyetu kutafuta mambo yasiyo ya muhimu. La muhimu ni kumpata huyu Bazilw kwanza. Endapo baada ya kupatikana kwake vifo vitaendelea, ndipo tutaanza msako mpya.”

“Ndiyo afande.”

“Na kuhusu picha yake, peleka katika magazeti yote. Tangaza kuwa yeye ni mtu hatari ambaye anatakiwa hai au maiti mapema mno. Yeyote atakayemwona aiarifu polisi mara moja. Sawa?”

“Lakini afande…” Abdala akasita tena kidogo kabla ya kuendelea. “Suala hili naona unalipa uzito mno. Ni rahisi sana kutoa maelekezo yasiyoridhisha endapo utakuwa katika hali uliyonayo siku hizi. Tangu kisa hiki kilipoanza sijakuona ukivuta; jana nzima hukunywa hata chai; leo pia naona huna wazo la kutia chochote. Licha ya hayo, uso wako umegeuka kabisa utadhani mtu anayefuata katika orodha ya vifo hivi ni wewe. Kwa nini afande? Huoni kuwa ni hatari kwako? Nadhani hii ni kesi ya kawaida kama nyingine nyingi ambazo tumezitatua kwa njia ya kawaida. Isikutishe sana…”

“Isinitishe!” Kombora alifoka. Kisha alijirudi na kujaribu kutabasamu, lakini tabasamu halikutokea. Akamtazama Abdala kwa huzuni huku akiwaza: Huyu hajui. Hafahamu kuwa napata simu za muuaji kila kabla ya mauaji hayo. Naweza kustarehe vipi, mimi kama kiongozi wa polisi, hali muuaji ananikebehi kwa siku kabla ya kumwaga damu isiyo na hatia?

“Hapana sajini,” akajibu. “Kama ni mzaha tutaufanya baada ya kumtia Bazile katika mikono yetu. Kwa sasa jambo muhimu ni kumpata tu. Sawa?”

“Bila shaka atapatikana afande.”

“Sawa.”

“…ATAPATIKANA afande….sawa…” Brown Kwame akafunga chombo chake na kumgeukia mwenzake aliyeketi upande wa pili wa meza. Wakaangua kicheko.

“Umeona Chenja?” alimuuliza mwenzake. “Hakuna lolote watakalozungumza hapo kituoni kwao ambalo linapita bila kulisikia. Nafahamu kila mpango wao kabla hawajaanza kuutekeleza. Kwa hiyo, kaa ukijua kuwa hakula chochote wala lolote litakalotukwamisha. Moto tuliouwasha umeshashika mbuga nzima. Hawawezi kuuzima. Acha waendelee kujua adui yao ni yule bwana mdogo Bazile. Napenda waendelee kuamini hivyo. Watakapogutuka itakuwa ‘too late’ kwao. Sisi tutakuwa tumemaliza kazi yetu.”

“Kwa kweli watu hawa ni wazembe kuliko nilivyotegemea,” Chenja alisema. Kama ilivyo kawaida yake, alisema huku akipapasa tumbo lake ambalo lilichomoza nje ya kifua chake. “Hadi sasa wanaamini kuwa adui yao ni Bazile?”
“Na bado nitawafanya wazidi kuamini hivyo,” Kwame alijibu kwa majivuno. “Huu ni mpango wa kimataifa bwana Chenja. Mbinu zilizotumika ni za kitaalamu ambazo mtu yeyote mwenye akili za kawaida lazima ahadaike tu. Leo nitawaonyesha adui yao. Bazile atawatembelea. Nataka kumfurahisha zaidi rafiki yangu Kombora.”

“Angalia usi-over do.”

“Hakuna litakalotokea. Bado kifo kimoja tu, baada ya hapo amri iko mikononi mwetu, nchi miguuni mwetu. Utaona bwana Chenja. Subiri kidogo tu.”

“Sawa, sasa nadhani niende zangu. Ni hatari kukawia hapa.”

“Hakuna mahala penye usalama kama hapa. Mtu yeyote anayevuka geti hapa ndani namwona vizuri. Silaha zilizotegwa katika chumba hiki zimepangwa kwa namna ambayo mtu kwa kawaida haoni na zaweza kumteketeza wakati wowote nitakapo. Zaidi ya hayo, vyumba vya jirani wapo walinzi waliohitimu kuua na kuadhibu endapo nitatoa amri hiyo. Licha ya yote hayo, ulikoingia wewe watu wanadhani uko maliwatoni. Hakuna anayejua siri ya mlango huo. Hatufanyi mzaha hata kidogo bwana Chenja. Tumedhamiria. Na kwa kuwa tuko ukingoni hatuna lolote la kuhofia. Hata hivyo bora uende zako.”

“Kwaheri.”

Kwame alibonyeza dude fulani, sakafu ya chini ya meza ikafunuka na kuachia mwanya wenye ngazi inayoingia ardhini. Chenja aliaga tena na kisha kuifuata ngazi hiyo. Alitokea katika nyumba moja upande wa pili wa mtaa. Nyumba hiyo siku zote ikiwa haina watu wengi, isipokuwa wachache ambao walijua wanachokifanya, ilikuwa rahisi kwa Chenja kutoka nje ya mlango huo ulioandikwa GUEST LAVATORY bila kuonekana na kuingia katika gari lake ambalo lilimrejesha kazini kwake.

Kwame aliendelea kutulia juu ya meza yake akitabasamu. Kila kitu kilikuwa kikimwendea kama ilivyokusudiwa. Furaha ilioje!

Machoni mwa serikali na mbele ya kila mtu, Brown Kwame alikuwa yuleyule, mtu mfupi, mnene, kidevu kilichofunikwa na ndevu nyingi zilizozunguka uso mpana wenye macho maangavu, mtu ambaye siku zote alionekana mtanashati kwa suti za nje na viatu ambavyo vilitengenezwa kwa matakwa yake binafsi katika viwanda mashuhuri.

Mtu huyu kikazi alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni mashuhuri iliyoitwa Snow Fund ambayo ilishughulikia mambo mengi yakiwa pamoja na huduma za usafiri kwa watalii, uuzaji wa vinyago nchi za nje, uwakala wa uingizaji na usafirishaji wa bidhaa na kadhalika. Ofisi hii ilikuwa ikifanya kazi vyema na wafanyakazi wake walikuwa wakiridhika kabisa kimshahara.

Ni hiyo picha ya nje iliyokuwa wazi machoni mwa wengi. Hata wafanyakazi wote wa matawini na hapa makao makuu walikuwa na picha hiyohiyo. Kwame alipenda iendelee kuwa katika hali hiyo. Hakupenda upande wa pili uonekane, hadi hapo baadaye kidogo.

Katika upande huu wa pili, Kwame hakuwa Kwame, bali alikuwa
Joe Kileo, mwakilishi wa kampuni moja kubwa ya kijasusi kutoka nchi za Magharibi. Kampuni ambayo ilikuwa ikiendesha shughuli nyingi za hatari katika nchi kubwa na ndogo kuhujumu tawala na uchumi ili zielekee upande wautakao kwa manufaa yao na nchi zao.

Shirika hilo la ujasusi, licha ya kumlipa Kwame fedha nyingi za kigeni, ndilo lililompa mtaji mnene ambao aliutumia kufungua kampuni hii. Haja yao haikuwa faida wala huduma kwa jamii, bali ilikuwa kupata fursa nzuri ambayo iliwawezesha kukutana na watu wao waliojifanya watalii kuingiza silaha, dawa hatari na vitu vingine ambavyo vilikusudiwa kutumiwa siku za usoni.

Tayari walikuwa wamefanya mengi maovu. Bado walikusudia kufanya mengi. Wakiwa katika kuyaandaa hayo ambayo walikusudia kuyafanya ‘pigo la mwisho’, ndipo Kwame alipomwona kijana yule Bazile Ramadhani akimjia ofisini kwa mwendo wa haya haya na miswada mitatu mikononi, akiomba msaada wa kusaidiwa kuchapishiwa vitabu.

Kwame akajitia huruma, akampa ushauri wa kuwaona wachapishaji. Kijana huyo akamweleza jinsi alivyokata tamaa kwa wachapishaji hao. Kwame akazidi kumhurumia. Kumbe Joe Kileo, kama alivyojulikana kwa washiriki wake, alikuwa amepata. Alifurahia sana kimo cha kijana huyu, hasa urefu wake ulivyosadifu na kupatana na matakwa yake.

Njama alizokuwa ameinjika zilikuwa kwenye hatari ya kuvuja-sasa eti Muumba kamwonyesha njia. Hivyo aliwaamuru makachero wake ambao walimfuata Bazile kwa siri hadi kwake ambako walitekeleza jukumu walilopewa la kufanya waamini kwamba kaibiwa muswada kwa kumlaza kwa dawa zao za kitaalamu na kuanza maongezi hayo yaliyomfanya aamini. Kisha waliingia ofisi ya Kitenge usiku na kuiba muswada huo; ndipo yakafuata yote ambayo yalikuwa yakiendelea kutukia. Yote ambayo yalikuwa yakizungusha kichwa au ubongo wa Inspekta Kombora na wenzake wote kwa namna alivyokusudia kabisa Kwame.

Jambo lingine la kutia moyo ambalo lilizuka bila kutarajiwa katika wakati unaostahili ni lile la kujitokeza yule mwanamke malaya, Machozi na madai yake ya ‘kumuua’ Kitenge. Hayo Kwame alikuwa ameyasikiliza katika chombo chake kilichonasa kila maongezi yanayofanyika katika ofisi ya Kombora.

Kwanza yalimshangaza kisha yakamfanya acheke kwa furaha. Ilikuwa nyongeza nyingine juu ya mtafaruku uliokuwa umepangwa kumsumbua Kombora na polisi wote wasiweze kupata walao wazo ambalo lingewaelekeza kulikokuwa na ukweli.

Lingine ni jinsi Kitenge alivyolewa usiku ule hata wasipate haja ya kutumia dawa zao za kulevya. Bahati ilioje. Polisi wangeendelea kumsaka muuaji wa bandia katika sehemu ambazo hayupo hali yeye Kwame na kikosi chake wakiwacheka na kuendelea na harakati zao pasi ya aina yoyote ya hofu.

Kwame alitabasamu tena, alijipongeza kwa jinsi mambo yalivyokuwa yakimwendea kwa utaratibu na bahati kubwa. Kisha aliitazama saa yake ya mkono, akainuka na kumpitia katibu wake ambaye alikuwa kainamia mashine ya chapa akichapa barua.

“Natoka kidogo,” alisema na kuendelea na safari yake bila kusubiri jibu. Je, alielekea Kituo cha Polisi namba kumi na mbili.

Kituoni aliomba kumwona Kombora. Alimkuta akiwa kachakaa uso kwa mikunjo ya hasira na mshughuliko. Nusura Kwame acheke au kumpa pole. Lakini alijifanya hajui lolote linalotokea. Badala yake alimsalimu Kombora kirafiki na kujikaribisha juu ya kiti kilichomwelekea.

Hawakuwa wageni kwa kila mmoja, ingawa kazi zao zilikuwa zikiwanyima fursa ya kufahamiana zaidi. Mara mbili, tatu wamekutana katika baa au tafrija fulani, mara kadhaa wameonana kikazi Kwame akileta malalamiko au matakwa fulani fulani ya kampuni yake.

Kwa Kombora, Kwame alikuwa mtu wa kuheshimiwa, ambaye ‘amebahatika’ kupata wadhifa mnono wenye nafasi zote za kutumia. Wadhifa ambao ulimruhusu kusafiri kokote kule nje ya nchi bila hofu ya wanawe kulala njaa. Kinyume na yeye ambaye kazi yake ilikuwa kulinda masilahi ya nchi na watu wengine usiku na mchana sehemu za hatari ambazo dakika yoyote waweza kupoteza maisha. Kazi ambayo malipo hayakuwa ya kuridhisha sana kulingana na uzito wa jukumu.

Hata hivyo, Kombora aliipenda sana kazi yake. Aliona furaha mno kuona matajiri wa matajiri na maskini maisha yao yakiwa mikononi mwake na kuutegemea msaada wake. Ilikuwa tamu zaidi ya utajiri kuona baba mzima mwenye umri zaidi ya baba yake akikulilia ili umwokoe kutokana na ‘mtu’ au ‘jambazi’ ambalo linakusudia kumuua. Wadhifa ulioje!

“Ndiyo bwana Kwame, unaendeleaje huko Snow Fund?”
“Vizuri tu.”

Kwame alipoona Kombora akimtazama kwa macho yanayomuuliza shida yake aliongeza, “Nilichofuata ni kukueleza juu ya lile suala lililonileta majuzi.”

“Suala la?”

“Wizi wa shilingi elfu moja.”

“Alaa!” Kombora akakumbuka. Lilikuwa moja kati ya masuala madogo ambayo kwa kawaida hayashughulikiwi na ofisi hii. Zaidi ilimshangaza kuona Kwame na ukurugenzi wake aking’oka toka ofisini na kuja kutoa ripoti juu ya wizi mdogo kama huo. Kwa nini asipige walao simu? Alikuwa amejiuliza siku hiyo.

Hakujua kuwa ni siku hiyo ndiyo Kwame alipoleta chombo chake kidogo chenye ukubwa wa gololi na kukipachika kwa hila sehemu fulani kwenye meza ya Kombora. Chombo ambacho kilikuwa kikinasa na kupeperusha maongezi yote yaliyokuwa yakifanyika katika ofisi hii.

“Kwa kweli ndugu Kwame, suala lako bado…”

“Ndiyo, ndiyo Inspekta,” Kwame alikatiza. “Nilichofuata ni kukuomba ufute kesi hiyo. Nilikosea kuileta mbele yako. Ulikuwa wizi mdogo mno. Kuufanya ufahamike itakuwa kuwatangazia wafanyakazi wote wenye nia ya wizi kuthubutu kufanya hivyo. Watakuwa wameona kuwa Snow Fund si imara kama wanavyodhani.”

“Siyo vibaya ndugu Kwame. Hata hivyo endapo tutampata mwizi hatutasita kumfungulia mashtaka.”

“Vizuri,” Kwame alijibu akiinuka. “Kwa heri Inspekta.”

“Karibu tena bwana Kwame.”

Nje ya kituo kicheko kingine kilimtoka Kwame. Hata hivyo, hakukiruhusu kitoke nje. Alichekea tumboni.

USIKU huo, kama mwingine wowote, tangu mauaji yalipoanza kutokea, jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake lilifurika askari polisi na JKT ambao walikuwa makini wakilinda doria. Kila mlinzi alikuwa na picha ya Bazile akilini na rohoni. Picha ambayo ilikuwa imetangazwa na kusambazwa kote kwa juhudi kubwa. Walevi, wachawi, wazinzi na wote wenye maradhi ya kutembea usiku walitaabika sana usiku huo.

Kila mmoja alihojiwa na kutazamwa sana akilinganishwa na picha ya Bazile. Wale ambao waliondokea kufanana naye walao kidogo walitaabika zaidi kwa maswali ya mdomo na vitendo. Baadhi waliendelea na safari zao baada ya kupitia vituo vya polisi.

Mtu aliyehitajika hakuonekana. Polisi mmoja alikuwa kajibanza kwenye uchochoro wa Mtaa wa Nkurumah. Hakuwa usingizini wala hakusikia kusinzia. Hata hivyo, alitahamaki akipatwa na kitu kama kizunguzungu au usingizi wa ghafla. Alipojaribu kupambana na hali hiyo alisikia kishindo kutoka kwa nyuma yake. Pindi akigeuka alikutana na pigo la judo ambalo lilitua shingoni mwake na kumlainisha. Akaanguka chali, silaha ikimtoka mkononi na kudakwa na jitu lenye mavazi meusi. Jitu hilo lilimwinua na kumsogezea askari huyo uso wake likisema:

“Natumaini wanifahamu.”

Askari huyo hakujua ajibu nini. Uso huo haukuwa mwingine zaidi ya ule wa Bazile Ramadhani. Uso wa mtu katili ambaye alikuwa tayari kuua wakati wowote. Huku akitetemeka, askari huyo alijaribu kujitetea, lakini aliambulia pigo jingine ambalo lilizidi kumlegeza viungo.

“Naona wanifahamu,” liliongeza jitu hilo likiutia mkono wake mfukoni na kuuchomoa ukiwa umeshikilia jisu refu ambalo licha ya kiza kilichotanda katika uchochoro huo, lilimeremeta. “Hiki ni kisu kilichowaua wote. Kingeweza kukuua wewe pia endapo kingehitaji. Hata hivyo nitakuacha hai, nakuhitaji. Nataka upeleke salamu kwa rafiki yang mpendwa Mkwaju Kombora.”

Polisi huyo hakuwahi kusikia yote. Alikuwa hajifai kwa kutetemeka, kutetemeka ambako kulikoma na nafsi yake kuchukuliwa na mshtuko mkubwa pindi kisu hicho kilipopita ghafla kifuani na kuacha jeraha kubwa kwa alama ya msalaba. Maumivu hayo makali pamoja na mshtuko vilimfanya aruke na kuanguka sakafuni ambako alitulia kwa dakika nzima kama anayesikiliza ili afahamu kama yungali duniani au tayari kawasili kuzimu. Akiwa katika hali hiyo alisikia kwa dhiki kubwa sauti ya jitu hilo iliyosikika ikicheka na kisha kusema, “Mpe Kombora salamu tafadhali.”

Fahamu zilipomrudia vyema, askari huyo alijikuta yu peke yake, damu zikimvuja na kuiharibu sare yake. Silaha yake ilikuwa imetupwa hatua chache kando yake. Akajitahidi kuinuka na kuiokota silaha hiyo. Kisha alikumbuka kupuliza kipenga ambacho kiliwaleta askari wote karibu na alipokuwa. Baada ya kuona mkasa huo, askari walijitoma mbio huku na huko wakisaka na kusakanya kila pande ya eneo hilo. Hawakuona chochote.

Wakati huohuo, Inspekta alikuwa akiamshwa kutoka katika usimgizi ambao ulikuwa ndiyo kwanza anaupata baada ya saa sita za kufanya doria jijini na baadaye kuduwaa chali kitandani akifikiri kwa nguvu. Simu ilikuwa imemfuata nyumbani baada ya kupigwa kituoni baada ya kuunganishwa.

“Kombora hapa, nani mwenzangu?”

“Inspekta Kombora? Ni mimi rafiki yako kipenzi…”

Kombora asingeweza kuisahau sauti hii. Ilikuwa ya yuleyule adui yake mkubwa katika orodha ya maadui zake wote walioko hai. Hakupenda kuisikia sauti hii. Lakini bado pia alipenda kuisikia ili ajue lipi mwendawazimu huyu alikusudia kutenda.

"…wako. Nimeona nikufahamishe mwenyewe kuwa nimekutumia salamu za upendo kwa mkono kwa mmoja wa askari zako. Utafurahi sana kumwona Inspekta. Anavutia kwa rangi nyekundu na kidani cha aina yake alichovaa kifuani."

Kombora hakuwa na hamu ya kuendelea kusikiliza sauti hiyo. Sauti ambayo sasa ilikuwa ikisikika masikioni mwake kama mwito wa mauti yenyewe utokao kuzimu moja kwa moja. Hata hivyo, aliendelea kusikiliza. Haja haikuwa kumsikia bali kuwapa fursa makachero wake ili waifuate simu. Alikwishatoa siri ya simu baina yake na muuaji huyo na kuweka wataalamu tayari kujua simu inatoka wapi na kuwaashiria vijana ambao waliandaliwa kutoa ishara kwa askari wa doria katika eneo hilo ambao waliruhusiwa kuua chochote watakachokikuta kikipiga simu hiyo. Uzoefu wake kikazi ulimfanya Kombora ajue kwamba vijana hao walikuwa kazini wakisikiliza simu hiyo a kutimiza wajibu wao.
"Inspekta?"

"Nipo."

"Mbona kimya rafiki yangu?"

"Hujajibu chochote."

"Juu ya nini?"

"Salamu zangu. Zaidi ya salamu ni kwamba najisikia kuua mtu mwingine. Unasemaje?"

"Unataka nisemeje? Nikupigie magoti kukusihi usiue? Niwezalo kusema ni ukae ukijua kuwa nitakutia mbaroni. Na utajuta kuzaliwa. Pamoja na hayo, bado nakushauri kuwa ujitokeze mwenyewe. Upo uwezekano wa kukusamehe," Kombora alimaliza huku akijiuliza kama hajavuka kiwango kiasi cha kumtoa mtu huyo kwenye simu mapema kabla watu wake hawajamfikia.

"Inspekta! Mbona maelezo mengi mno?"

"Siyo mengi, ningeweza kueleza mengi zaidi…"

"Inspekta. Uko peke yako kwenye simu?" alidakia mtu huyo.

"Ndiyo. Nitakuwa na nani tena?"

"Uongo. Unajaribu kupata nilipo kwa simu. Hongera kwa juhudi zako na pole kwa kazi yako isiyo na matunda."

"Sivyo…sikia…" ilikuwa kazi bure. Kicheko kilisikika upande wa pili kikifuatwa na kukatwa simu. Kilichobaki katika masikio ya Kombora ni kicheko ambacho kilitisha na kuchukiza mfano wa kicheko cha mauti yenyewe.

HABARI mbaya husafiri haraka sana kuliko habari njema. Hii ya mauaji ilienea haraka mara mbili zaidi ya kawaida. Licha ya picha ile ambayo ilitokea magazetini na maandishi ya waandishi ambayo yalieleza kwa ufupi chini ya vichwa vya habari: "MUUAJI HATARI AZUKA JIJINI" na la Kiingereza lililodai "THE MURDERER STILL AT LARGE", bado kuna mengi yaliyosemwa baina ya mtu na mtu mitaani. Huyu alisema hivi na yule akaongezea lake ikawa habari pana ya kutisha kuliko ilivyokuwa.

Kama watu wengine, Joram Kiango akiwa mkazi wa jijini Dar es Salaam, alipokea habari hiyo kwa njia zote. Aliwasikiliza wambeya wa mitaani, akayasoma magazeti yote na kisha kuulizia vizuri kwa miongoni mwa rafiki zake walioko katika Jeshi la Polisi. Baada ya kuipata kikamilifu na kuona jinsi polisi walivyokuwa wakitapatapa katika hali ya kukata tamaa, alitabasamu.

Kwa Joram, tabasamu hili halikuwa la furaha ya kusikia watu wasio na hatia wanateketea pasi sababu, hasha. Kwake, tabasamu hili huwa dalili ya shauku. Shauku kubwa ambayo humjia na kumteka kikamilifu kila litokeapo tukio la kutisha na kusikitisha kama hili ambalo huhitaji mtu shujaa kulitatua. Moja kwa moja Joram hujihisi kama mtu huyo na kujitupa katika duru la mapambano kwa mbinu zake ambazo humfanya aponee chupuchupu, huku katatua au kuweka hadharani siri za hatari ambazo polisi huwa wamefikia hatua ya kukata tamaa.

Hakuna asiyemjua Joram Kiango. Ni yule kijana mrefu, mwenye maungo yenye nguvu na sura nzuri ambaye wakati wote huwa mchangamfu. Yule kijana mwenye ofisi yake inayoitwa Private Investigator ambayo hushughulikia upelelezi wa aina mbalimbali toka kwa wateja ambao huwa kampuni au mashirika yenye haja ya kujua jambo fulani, watu binafsi wanaohitaji kutatuliwa hili na lile na yeye anapojisikia haja au njaa ya kusaidia polisi katika shughuli zao za kila siku.

Kijana huyu mwenye umri usiozidi miaka ishirini na sita ni juzi tu aliporejea kutoka Marekani ambako alikuwa akiishi na wazazi wake wanaoishi huko. Ni huko ambako Joram alipata moyo wa kishujaa baada ya kukua miongoni mwa watoto weusi na kuona walivyokuwa wakinyanyaswa na wenzao weupe.

Ingawa alipata elimu nzuri lakini mara baada ya elimu hiyo alijiunga na vikundi vya wahuni weusi waliokuwa wakisumbua sana Jeshi la Polisi. Waliiba na kupigana wakiharibu na kusumbua katika maduka na benki. Baada ya hapo Joram alijiunga na CID na kufanya kazi nzuri, lakini ghafla akaacha kazi baada ya kujiona kakamilika kimwili, kifikra na kimtazamo.

Ndipo akaja Dar es Salaam ambako alifanya mengi, yaliyoipendeza polisi kabla hajapatiwa kibali cha kufungua ofisi hii.
Machache kati ya aliyoyafanya yaliwavuta waandishi hata wakayaandikia vitabu na kuviita DIMBWI LA DAMU na LAZIMA UFE…

Alitabasamu tena akalitupa gazeti na kumtazama Neema Idd katibu wake ambaye pia alikuwa akimtazama.

“Unajua Neema…”

“Usiniambie. Najua kila kitu. Macho yako yanaonyesha kuwa unataka kujiingiza katika mambo haya. Sijui umelogwa mwenzangu. Labda hukusikia juu ya yule polisi aliyepewa salamu za kumpa Kombora?” Neema alimaliza.

“Yule bwege? Mtu una bunduki mkononi kama siyo uzembe ni nini hata mtu mwenye kisu akuchanje kifuani?” Joram alijibu akicheka.

“Siyo kuchanjwa Joram! Amejeruhiwa vibaya sana.”

“Pamoja na hayo,” kisha sauti ya Joram ikabadilika na mzaha ukatoweka kabisa. “Jambo linalonishangaza katika suala hili ni huyu mwandishi Bazile! Imekuwaje akawa hodari ghafla kiasi hiki?

Vipi awe mjanja wa kuepuka mitego yote ya polisi, shujaa kiasi cha kumkabili polisi mwenye silaha na kumpa salamu za jeraha kifuani na wakati huohuo akimdhihaki mkuu wa polisi kwa simu za kashfa mara kwa mara? Hamu yangu ni kujua alivyopata uwezo huo kwanza, kisha nitajua namna ya kumtia mikononi.”

“Yaani umeshaanza kazi?”

“Bila shaka. Sina haki ya kustarehe hali mtu yuko hai na ameahidi kumwaga damu nyingine zisizo na hatia. La, Joram Kiango si mvivu kiasi hicho mama.”

Neema hakuwa na la zaidi. Kwa kadri anavyomfahamu, Joram kamwe hatastarehe tena, tayari kazama kichwa na miguu katika dimbwi la mkasa huo. Kumshauri kusingesaidia. Hata hivyo alimwambia neno lilelile ambalo amemwambia mara nyingi:

“Angalia Joram. Jihadhari.”

“Hakuna anayemfahamu Joram Kiango zaidi yako Neema. Ninayo nafasi nzuri ya kumtia muuaji mkononi kwani kama ujuavyo, adui huyo kajizatiti kukabiliana na jeshi la polisi, hana habari ya mtu mmoja anayejiita Joram. Huoni kama hiyo ni nafasi nzuri ya kumfumania?” alimalizia akiwasha sigara na kuanza kuivuta kwa utulivu.

Katika utulivu huo, alikuwa akipambana vikali na tamaa ambayo ilikuwa ikimshawishi ainuke na kuanza uchunguzi juu ya mkasa huo. Tamaa ambayo aliishinda nguvu baada ya kujikumbusha tena na tena kuwa alikuwa hajajiandaa kikamilifu kuweza kusimama kiume dhidi ya muuaji au mauaji mazito kama hayo, mauaji ambayo sasa yalikuwa yamewashinda polisi kuyakabili.

Kujitumbukiza kiholela ingekuwa sawa na kumwalika muuaji ampe yeye Joram salamu ambazo safari hii zingeelekezwa si kwa Kombora bali ahera. Naye Joram hakuwa tayari kwenda huko mapema kiasi hiki.

Hivyo alijituliza akiwaza yapi ameyafahamu tayari dhidi ya muuaji huyo, mangapi polisi imefanya katika juhudi zao za kumtia mbaroni, kiasi gani wamefanikiwa na vipi wamefeli. Kadhalika alihitaji kujua mangapi yanafahamika juu ya marehemu, mangapi hayafahamiki na yapi yalistahili kufahamika.

Baada ya kuyafahamu hayo, yeye kama Joram Kiango angekuwa tayari kufuata njia zake ambazo zingemfikisha hadi kisogoni au usoni pa muuaji huyo. Joram, angependa zaidi kukutana naye uso kwa uso, aupime na kuushuhudia kwa macho yake ujabali wa mtu huyo aliyeondokea kuwa jitu kwa muda mfupi tu.

Akiwa na uhakika na mbinu zake, pamoja na matumaini juu ya njia atakazopitia ambazo ni kinyume na zile za polisi, alijisikia furaha kana kwamba tayari kamtia adui huyo mikononi mwa sheria. Akaitupa sigara yake katika kasha la taka na kutoka nje akipiga mluzi.

3

BAADA ya kuyafahamu hayo, yeye kama Joram Kiango angekuwa tayari kufuata njia zake ambazo zingemfikisha hadi kisogoni au usoni pa muuaji huyo. Joram, angependa zaidi kukutana naye uso kwa uso, aupime na kuushuhudia kwa macho yake ujabali wa mtu huyo aliyeondokea kuwa jitu kwa muda mfupi tu.

Akiwa na uhakika na mbinu zake, pamoja na matumaini juu ya njia atakazopitia ambazo ni kinyume na zile za polisi, alijisikia furaha kana kwamba tayari kamtia adui huyo mikononi mwa sheria. Akaitupa sigara yake katika kasha la taka na kutoka nje akipiga mluzi.

BAADA ya kuwaona tena rafiki zake ambao humuuzia habari za siri kutoka polisi na kupata anuani za marehemu wato, alirudisha gari lake nyumbani kwake Ilala na kuanza kutumia ‘Dala Dala’ kwenda hapa na pale.

Safari yake ya kwanza iliishia Mapipa ambako alionana na mama aliyekuwa amempangisha marehemu Kitenge. Alizungumza naye mengi ambayo alidhani au kuamini kuwa polisi wasingekumbuka au kujishughulisha kuuliza. “mwenendo wa marehemu siku chache kabla ya kifo…” “Wageni au rafiki zake wa karibuni.” “Tabia na maongezi yao….’ Na kadhalika. Pia, alihoji sana juu ya Yule mwanamke ambaye alidai au kutishia kumuua marehemu. Majibu aliyoyapata aliona kama hayakuwa na msaada mkubwa. Bibi huyu alikuwa kama mtu aliyechanganyikiwa sana baada ya kuwa na kila hakika kuwa aliyemuua Kitenge ni Yule ‘malaya’ kisha vifo vya aina na vya kutisha mno vikaendelea kutokea.

“Yawezekana kuwa muuaji wa kitenge ni Yule mama. Huyu mwingine pengine anaitumia nafasi hiyo ili kutimiza dhamira yake tu,” Joram alimshauri.

“Yawezekana baba. Haya mambo kwa kweli yanatisha, yaweza hata kunitia wazimu kwa jinsi ninavyoyafikiria na kuwajibika kujibu maswali magumu kutwa kucha. Nadhani utaniwia radhi nipumzike baba.”

“Bila shaka bibi,” aliitikia Joram akiinuka na kumshukuru mama huyo. Kutoka hapo alienda mtaa wa india ambako alikutana na mke wa marehemu Wamangi. Jorah alimkuta mjane kajiinamia huku mkononi kashika gazeti ambalo baada ya Joram kulitupia macho alifahamu kuwa lilikuwa na habari za mauaji hayo. Baada ya kumsalimu na kumpa pole mama huyo, Joram aliwataka radhi jirani wawili ambao waliketi kando ya mama huyo, wakimfariji kwa kuwepo kwao pale. Watu hao wakaondoka na kumwacha Joram na mama huyo ambaye alianza kutokwa na machozi.

“Usilie mama,” Joram alimfariji, macho yake yakilikagua umbo la mama huyo na kuona kuwa umri wake wa kati ya miaka thelathini na arobaini ulikuwa haujauathiri sana uzuri ambao ni dhahiri uliwahi kuwepo katika umbo hilo nene lenye ngozi laini nyekundu.

Macho ya mama huyo yalikuwa malegevu, pengine yaliashiria ulegevu wa moyo, pengine ulegevu wa mapenzi. Joram akiwa mzoefu wa mitazamo hiyo hakubabaika bali alianza kumtupia maswali kwa sauti yake nzuri.

“Nadhani polisi wamekuuliza mara nyingi swali hili mama, lakini naomba si majibu bali maoni yako juu ya mtu ambaye anaweza kuwa kamuua mumeo. Yaani kufuatana na taarifa juu ya kifo hiki inaonyesha muuaji ni mtu ambaye ama anaifahamu sana nyumba hii, ama alidhamiria kwa hali na mali kumuua mumeo. Vinginevyo, asingepanda ngazi zote hizi na kuthubutu kuua hali na wewe umo kitandani. Unadhani ni nani mama?”
“Muuaji? Na huyu hapa aliyetajwa gazetini? Baba unauliza swali gani hilo? Kama unahaja ya msaada ni kumsaka huyu mtu ili apatikane haraka,” mama huyo alijibu kwa udhaifu.
“Nina maana,” Joram alitamka baada ya kumpa mama huyo moja ya tabasamu zake ambazo humsaidia mbele ya wanawake kupata akitakacho, “….nilikuwa na maana kuwa mtu huyo Bazile anaweza kuwa anafahamiana na mumeo au kuifahamu nyumba hii kiasi cha kufanya yote yale bila vikwazo? Yaani, kama nia yake ni kuua tu, kwa nini asivizie walevi huko manzese na buguruni? Kwa nini afanye kila njia kumuua mumeo?”

“Hata mimi nashangaa,” mjane alijibu. “Nadhani hiyo ndiyo kazi yenu kama wapelelezi.”

“Ni kweli,” Joram alijibu akitabasamu tena, “Lakini tunahitaji msaada wako pia mama. Kwa mfano, juu ya kifo kilichotokea, wewe na mumeo mlilala kitandani kama kawaida siyo?”

“Ndiyo.”

“Ulipoamka ukajikuta bafuni, ukiwa umefungwa kamba mikononi na miguuni, mumeo akiwa kachinjwa…” Joram alilazimika kusita mama lipoangua kilio. “Unadhani yawezekana katika usingizi wako wa kawaida mtu akufunge kamba na kukubeba hadi bafuni hali hujaamka tu?”

“Nimesema mara nyingi kwa polisi kuwa mtu huyo alitumia uchawi. Nashangaa walivyonicheka. Haijawahi kunitokea kamwe nikalala usingizi wa aina hiyo. Wala sifahamu mangapi mtu huyo alinitendea baada na kabla ya hapo.” Akaangua kilio tena kwa sauti ndogo.

“Una hakika kuwa haukuwa usingizi wa kawaida?”

“Kila hakika. Unajua mume wangu alikuwa ndiyo bado karejea toka Zanzibar ambako aliishi huko kwa miezi miwili na zaidi kwa shughuli za kikazi. Sidhani kama nina hakika ya kusema haya, lakini sina budi kukuambia kuwa kila arejeapo toka safari za mbali tulikuwa tukirejewa na ujana wetu. Tulilala na kukesha huku tumekumbatiana , kila mmoja kiwa hataki kumwacha mwenziwe.
Fikiria basi, katika hali kama hiyo, nani mwenye uwezo wa kututenganisha bila uwezo wa mazingaombwe? Zaidi nashangaa kwa nini hamtaki kuamini kuwa uchawi ulitumika. Wangapi wameibiwa kwa njia hiyo?”

Joram aliendelea kuhoji madhumuni ya safari hiyo ya Zanzibar ilikuwa lini , hali ya mume baada ya kutoka huko na mengi mengine. Majibu akiyopata yalikuwa ya kawaida kiasi cha kumfanya ashindwe kuona kama alikuwa akiendelea mbele au nyuma katika upelelezi wake. Hata hivyo alinukuu mengi katika daftari lake kisha akamshukuru mama huyo na kuaga.

Baada ya hapo Joram alipanda basi ambalo lilimfikisha katika kituo cha mabasi cha Mkwajuni, Kinondoni. Akasoma namba ya mtaa na nyumba ya marehemu Jugeni Kawamba. Joram hakuwa na matumaini mengi ya kumkuta mtu katika nyumba hiyo, hasa baada ya kuarifiwa kuwa marehemu alikuwa akiishi peke yake. Lakini alifurahi kukuta watu watatu jamii ya marehemu,wakiwa wamehamia hapo kulinda nyumba.

Walimkaribisha kwa huzuni huku macho yao yakimuuliza ni nani na anahitaji nini. Kama kawaida yake alijieleza kwa hila kisha kuanza kuwatupia maswali ambayo walibabaika kuyajibu.

Alipoona msaada wao ni mdogo kwa jinsi ambavyo hawakuwa wakiishi na marehemu, aliinuka na kuaga. Kabla hajainua mguu kuondoka macho yake yalidakwa na ganda la tiketi ya ndege ya ATC iliyokuwa imeanguka chini ya meza. Akainama kuiokota.

Alipoisoma ilimsisimua zaidi. Ilikuwa ya kutoka Zanzibar, ikiwa na tarehe ileile aliyoitaja mjane wa marehemu Wamangi mume wake alipotoka Zanzibar.

“Kumradhi marehemu alikwenda kufanya nini Zanzibar?” aliwahoji akimtazama mmojawao , mwanamume mwenye ndevu nyingi kinyume cha wenzake japo walionekana wana umri mkubwa zaidi yake.

“Alikuwa wapi? Zanzibar? Kijana huyo alimhoji Joram badala ya kumjibu.

“Kufanya nini?” mwingine aliongeza.

Joram akagundua kuwa hakukuwa na habari zozote za karibuni kuhusu marehemu ndugu yao. Akaondoka zake polepole baada ya kuwashukuru kwa mara nyingine. Nje ya nyumba alilihifadhi ganda hilo mfukoni huku akiingia katika teksi iliyosimama mbele yake ghafla.

“Airport,” alisema bila kumtazama dereva. Alikuwa akitazama saa yake ambayo ilidai ni saa tisa kasoro dakika kadhaa. “Tafadhali tupitie hapo Mapipa Mtaa wa Kiyungi,” aliongeza.

“Bila tafadhali,” dereva alisema huku akiigeuza gari yake kiufundi na kutia mwendo kufuata Barabara ya Morocco. Walipowasili nyumbani kwa marehemu Kitenge ,Joram alifanya haraka kuingia ndani ambako alipokewa na bi kizee kwa mshangao.

“Kumradhi mama, nimerudi tena baada ya kupata swali moja la muhimu. Nilitaka kufahamu kama marehemu aliwahi kufanya safari yoyote ya Zanzibar hivi karibuni. Kwa ndege au meli.”

“Siwezi kufahamu baba. Watu hapa mjini wanaweza kufanya lolote bila mtu wa chumba cha pili kufahamu. Na kama ni safari ya ndege si anaweza kwenda na kurudi bila watu kujua? Nasikia ni safari ya dakika kumi tu. Pengine …”

“Ahsante mama,” Joram alimshukuru akiondoka harakaharaka.

“Tafadhali endesha gari kama mwanamume,”alimweleza dereva. “Kama hujiamini acha niendeshe mwenyewe.”

Dereva alitabasamu na kumwambia, “ Utachoka mwenyewe.”

Naam, Joram alikubali kuwa wapo vijana wanaojua kukimbiza gari.

Baada ya dakika chache tu gari ilikuwa tayari imewasili uwanja wa ndege wa Dar es Salaam.
“Nisubiri, tafadhari “ alisema akimpa mqalipo yake. Kisha akaenda katika chumba cha kuhudumia wasafiri ambako alikuta watu wengi wakihudumiwa. Akaingia upande wa watumishi na kujieleza vizuri kwa mhudumu mmoja wa kike ambaye alionekana kuvutiwa na tabasamu la Joram pamoja na sura yake zaidi ya maombi yake. Hata hivyo baada ya muda mfupi tayari alikuwa kamkabidhi Joram orodha kamili ya abiria wote waliosafiri katika ndege aliyoitaka Joram, siku hiyohiyo tarehe 17 Machi 1984 saa ya kuondoka Zanzibar ikiwa kumi na moja kamili za jioni .”Niliwahudumia mimi,” alisema kwa furaha.

Safari hiyo ilikuwa imefanyika katika ndege ndogo aina ya Twin Otter. Abiria walikuwa watano: majina ya wasafiri yalikuwa kama ifuatavyo:
J. Kawamba-S.L.P 71701 Dar es Salaam

B. Kwame-S.L.P 6142 Dar es Salaam
F. Wamangi-S.L.P 4700 Dar es Salaam
D. Kombo-S.L.P 41421Dar es Salaam
K.Key- S.L.P 1600010 Dar es Salaam

Joram Kiango aliyanukuu majina hayo na kumshukuru msichana huyo. Baada ya kumtupia maneno mawili matatu ya ahadi za kukutana katika madisko ambazo alijua zisingetekelezwa na upande wowote, aliondoka harakaharaka.

Kichwani alikuwa na mawazo mengi. Hakuwa na uhakika kama anachofanya ni kitu cha maana chenye manufaa katika upelelezi wake. Hata hivyo damu ilikuwa ikimsisimka kwa kushuku jambo katika safari au orodha hiyo. Tangu alipogundua majina ya marehemu wawili waliokufa usiku mmoja yakiwa katika orodha ya safari moja, alijikuta akihisi kuwa lipo jambo fulani katika safari ambalo laweza kuwa kisa au mkasa wa vifo vyao.

Lakini alikuwa akirudiwa na mashaka kwa kuona majina mawili tu. Jina la Bazile ambaye alikuwa mshukiwa wa kwanza katika mauaji yaliyokuwa yakiendelea lilikuwa halimo. Pia jina la Kitenge – marehemu wa kwanza – lilikuwa halimo. Yawezekana kuwa alikuwa anaupoteza bure muda wake? Alijiuliza alipokuwa akijikumbusha msorokoto uliokuwa katika kesi au mauaji hayo: Kwanza yule mwanamke anayedai kwamba alimuua Kitenge, pili, Bazile Ramadhani anayeaminika kuwa muuaji na anaendelea kupigia simu polisi kuwa ataua tena. Aidha, yote hayo yalishangaza. Yakoje mambo haya?

Joram akaamua kutosumbua kichwa chake hadi atakapopata nafasi ya kufahamu na ikiwezekana kujadiliana na abiria waliosalia ambao angeweza kuwapata.

Nje ya jengo la huduma za wasafiri, Joram aliingia katika kibanda cha simu na kujipatia kitabu cha orodha za masanduku ya posta.
Akakipekua haraka haraka kutafuta anuani za abiria wale watatu ambao alikuwa hawafahamu. Anuani ya K. Key haikumsumbua sana. Mara moja aligundua kuwa haikuwepo katika orodha ya namba za masanduku. Ilikuwa imekosewa au imebuniwa. Kwa nini? Hakuwa na muda wa kujibu. Akaamua kutafuta anuani nyingine. Ya D. Kombo ilikuwa ya kazini kwake Kamata, na B. Kwame ilisemwa Snow Fund.

Mara moja Kiango akalikumbuka jina pamoja na kukumbuka ilipo ofisi yake. Akatoka kibandani hima na kukimbilia kituo cha teksi.
Gari lililomleta kwanza lilikuwa limeondoka kitambo. Akavamia jingine na akamwamuru dereva aichukue mbio iwezekanavyo kumfikisha mjini. Dereva hakuwa mbaya, ingawa Joram hakuridhika naye.

Saa kumi na moja kamili walikuwa mbele ya kituo cha mabasi ya Kamata. Joram akamtaka radhi dereva, akateremka na kuingia ofisini. Karani mwanamume akamtazama kwa makini.

“Tafadhali, nataka kumwona ndugu D. Komba,” Joram alisema.

“Komba? Dismas Komba?” alihoji kijana huyo. “Leo siku ya ngapi sijui hajafika kazini. Watu wengi mno wanamtafuta. Hatujui kwa nini haonekani. Pengine kapata kazi nyingine, pengine amerusha mali za watu huko mitaani na kutoweka.”

“Yaani hamna taarifa yoyote juu yake,” Joram alifoka kwa mshangao na hofu ambayo ilianza kumpanda.

“Hatuna taarifa…”

“Mnajua wapi anakoishi?”

“Hakuna anayejua…”

“Hakuna! Ofisi hii nzima hakuna anayejua?” Joram alifoka ghafla.

Sauti yake ilikuwa kali yenye amri ikamfanya kijana huyo kuinua uso kutoka katika majalada yaliyokuwa mbele na kumtazama Joram kwa makini zaidi. Ndiyo kwanza akayaona macho yake yalivyodhamiria na paji la uso lilivyokunjamana. Kwa muda kijana huyo aliduwaa. Joram, alipoona hivyo akamtia moyo kwa kucheka kidogo, kisha akaongeza kwa sauti laini kiasi.

“Sikia kaka, tuna shida kubwa ya kumpata haraka. Huwezi kufahamu mtu yeyote anayeweza kutuelekeza kwake?”

“Wewe ni CID?” alihoji kijana huyo.

“La, ni mgeni wake tu.”

Kijana huyo alionekana kutokuliamini jibu la Joram. Hata hivyo, alitoka ili kuwaona wenzake ambao wangeweza kumpa habari hizo. Aliporejea alikuwa na kipande cha karatasi chenye anuani ya Komba ambayo alidai anaishi Kigamboni hatua kadhaa kutoka Kivukoni. Joram alimshukuru na kutoka akiitazama saa yake ambayo ilisema dakika chache mbele ya saa kumi na moja.
“Kigamboni,” alimweleza dereva wake.

Walipita Barabara ya Nkurumah na kuifuata hadi mnara wa saa ambapo walifuata Mtaa wa Railway hadi Sokoine Drive. Msongamano wa magari ulivyokuwa mkubwa ilibidi gari liende polepole, kwa mwendo ambao ulimchukiza sana Joram Kiango.

Lakini baada ya muda alitabasamu alipoona ofisi ya makao makuu ya Snow Fund ikiwa wazi mbele yake. Mara moja akamwamuru dereva kusimamisha gari kando, akateremka na kufuata mlango wa ofisi hiyo.

“Kumradhi kwa kuchelewa kwangu,” alimwambia askari mgambo aliyesimama mlkangoni tayari kumzuia. “Nina miadi ya kuonana na bwana Kwame.”

“Saa hizi?” alihoji mgambo huyo. “Tulikuwa tukifunga. Tumechelewa kidogo…”

“Unazidi kucheleweshа. Atakufukuza kazi kwa kuniweka hapa muda mrefu,” Joram alitishia.

Mgambo huyo akatabasamu kidogo kuficha hofu iliyomwingia,
“Pita hapa,” akaelekeza. “Uende moja kwa moja hadi mlango ule utamwona katibu wake umweleze shida yako. Sijui kama atakuruhusu. Wafanyakazi wote wamekwishatoka.”

Joram alimwacha akiendelea kusema. Alipofika chumba hicho aligonga na kufungua mlango. Macho ya msichana mwenye dalili zote za uanamji yakampokea kwa mshangao. “Unataka nini saa hizi?” aliuliza alipomwona Joram akijiweka vizuri kitini.

“Samahani mpenzi,” alisema akiachia moja ya zile tabasamu zake. “Nina ahadi ya kuonana na Bwana Kwame.”

“Hana miadi ya kuonana na mtu yeyote leo. Isitoshe saa zimekwisha,” msichana alimjibu.
“Ni kweli dada yangu. Lakini mwambie kuwa kuna mgeni wake anayetaka kuzungumza naye jambo muhimu.”

“Jambo gani?”

“Mwambie ni juu ya safari yake ya Zanzibar majuzi.”

“Imefanya nini?”

Joram akachoka na upuuzi wa katibu huyo. “Sikia sister, kama huwezi kumwambia leta simu nizungumze naye mwenyewe,” alisema huku tayari amevamia mkono wa simu. Binti huyo akaupokonya mkono na kubonyeza kidude kilichomuunga na bosi wake.

“Jina lako nani?” akamuuliza Joram.

“Wananiita Kalulu bin Kalulumanga.”

“Nani?”
Joram akarudia jina hilo la bandia. Baada ya maswali mengi kiasi aliruhusiwa kwenda. Ikamshangaza Joram kuona ilivyokuwa safari ndefu kumfikia ‘bosi’ huyo. Ilimlazimu kupita vyumba vidogovidogo zaidi ya vitatu ambavyo havikuwa na chochote zaidi ya taa za umeme ambazo zilitoa nuru kali sana. Mjenzi wa aina gani huyu asiye na wazo lolote la kiuchumi kiasi cha kujenga hivi?” alijiuliza Joram. Alipofikia mlango wa Kwame aliukuta ukiwa wazi.

Macho makali yaliyofunikwa na miwani mieusi yalimlaki. Macho ya Kwame ambaye alikuwa kaketi nyuma ya meza pana iliyozingirwa na viti kadha wa kadha, mfano wa chumba cha mikutano.

Kwame alikuwa kavaa suti ya kijivu ambayo ilimkubali vyema na kuoana na umbo lake refu, nene lenye nguvu. Ofisi nzima ilikuwa katika hali ya kuvutia, mapambo ya aina mbalimbali, vinyago vya aina aina na vitu vingine ambavyo Joram hakuweza kuvifahamu vikiwa vimepangwa vyema kabisa, macho ya Joram yalitambaa kwa muda juu ya vitu hivyo kama ambaye hakusikia Kwame akiuliza kwa mara ya pili;

“Unataka nini kijana?”

“Ofisi hii nzuri sana bwana Kwame,” lilikuwa jibu la Joram.
“Nadhani hukuja hapa kuisifu ofisi yangu. Sema unachotaka kisha uende zako. Nina shida za muhimu ambazo zimeniweka hapa hadi saa hizi.”

“Usijali. Mimi pia sina muda wa kuchezea,” Joram alimjibu.
“Nimekuja kwa nia njema kwako. Nadhani unafahamu mauaji ambayo yanaendelea kutokea?”

Mauaji gani? Haya ya huyu mtu mwehu ambaye anaendelea kuua ovyo? Hiyo ni kazi ya polisi. Wewe ni nani hadi unifuate kuyajadili? Nami nahusika vipi?”

Jorah hakujishughulisha na kuyajibu maswali ya Kwame. Badala yake aliongeza swali lingine, “Unamfahamu kijana huyo muuaji mzee?”

“Kumfahamu vipi?” Kwame alihoji akimchunguza Joram kwa makini zaidi. “Namfahamu kupitia magazetini, toka alipojitokeza kuwa muuaji,” akaongeza.

“Hujamwona ana kwa ana kabla ya hapo? Huku Zanzibar…”

“Sijamwona kabisa. Wala sitaki kumwona,” alidakia. “Suala la Zanzibar linahusika vipi na mjadala huu?”

“Ndiyo. Umegusa dhamira kubwa Kwame. Nimekuja hapa kukutahadharisha maisha yako yapo mashakani. Muuaji huyu anaua watu wote mliosafiri katika ndege moja tarehe 17 Machi kutoka Zanzibar. Wawili wameshakufa. Bado wewe na wenzako wawili.”

“Upuuzi ulioje? Nani aliyekwambia hayo?”

“Nani aniambie? Nimefanya uchunguzi na kuona. Dakika yoyote muuaji anaweza kukufikia wewe au yeyote kati yenu. Ushirikiano wako ni muhimu mno bwana Kwame. Ni…”

“We ni nani?” Kwame alikatiza tena.

“Kwa jina ni Kalulu, kama nilivyokwambia. Swali lako halina maana kwa sasa tunachotaka ni maelezo yoyote uliyonayo juu ya safari hiyo, yepi yaliyotokea ambayo yangeweza kuleta kitu kama hiki. Vilevile naomba uniambie yukoje msafiri mwenzenu aliyejiita K. Key.”

Joram aliona tahayari katika macho ya Kwame mara alipolitaja jina hilo. Hapana alikosea. Lilikuwepo tabasamu usoni mwake! Tabasamu la dharau au kebehi! Nyuma ya tabasamu hilo macho ya nafsi ya Joram yalisoma kitu kingine kabisa. Kitu ambacho ni kinyume na tabasamu.

“Sikia kijana,” alisema Kwame baadaye. “Sina muda wa kupoteza hapa. Wala sina jibu lolote la kumpa C.I.D au wewe, kwani nikiwa safarini sijishughulishi na jambo lolote la mtu yeyote zaidi ya shughuli zangu. Zaidi, siamini kama una lolote la ukweli katika maongezi yako. Yaelekea wewe kama si punguani wa akili u mhuni mwenye nia nyingine nje ya madai yako. Kwa hiyo. Kabla sijakuitia polisi, inuka uondoke zako haraka. Na angalia usirudi hapa tena.”

“Joram akacheka, “Yaelekea unajua mengi bwana Kwame,” akamwambia. “Shukrani kwa kunionyesha hali hiyo. Nakwenda na nitarudi nikiwa na jambo ambalo litakusisimua zaidi.” Akainuka.

“Na kama madai yako ni ya kweli, huoni kuwa unakitafuta kifo kwa miguu yako mwenyewe? Ungali kijana sana bwana mdogo. Kifo chako hakiwezi kunifurahisha hata kidogo.”

Lilikuwa kama onyo la kidugu. Lakini masikioni mwa Joram akiyatazama macho ya Kwame ambayo yalikuwa na udugu, lilikuwa tishio kali ambalo lilikusudiwa kumfanya aache harakati zake zote. Jambo ambalo lilimfanya Joram atabasamu tena kwa namna ya kumweleza Kwame:
“Nimekuelewa,” lakini hakusema hilo.

“Nakushukuru tena ndugu Kwame, tutaonana…” akageuka na kuvuta hatua kuelekea mlangoni.”

“So this is Joram Kiango” Kwame alinon’gona akitazama picha tatu ambazo zilifotolewa na mashine yake maalumu pindi Joram alipoondoka. Ilikuwa baada ya kulinganisha picha hizo na zile kadhaa za Joram ambazo hutokea gazetini, zilizohifadhiwa katika mafaili yenye habari zake na watu wengine ambao Kwame aliona haja ya kuhifadhi harakati zao.

Alizitazama picha hizo kwa makini, akihusudu uangavu wa macho ya Joram ambao ulidhihirisha busara na ubishi. Kadhalika alivutiwa na umbo lake refu lililokaa kiriadha, Joram Kiango! Akanong’ona tena akizidi kutabasamu. “Well…” akasita akiukunja ghafla uso wake.

ALIKUWA amelikumbuka lile pendekezo la mmoja wa wanakamati wenzake ambaye alitaka Joram auawe au kufanyiwa njama za kumfungisha jela kwa muda pindi harakati zao zikiendelea.

Kwamba angeweza kuingilia kati na kuharibu mipango yao yote kwa ukatili zaidi ya polisi. Lakini yeye Kwame alilidharau pendekezo hilo kwani kwa kadri alivyomfahamu Joram alimwona kama kijana mtundu tu, play boy, ambaye huingilia harakati za kitoto na kufanikiwa kuziharibu; si hizi ambazo zilikuwa zikifanywa na wasomi waliokubuhu katika fani ya ujasusi huku hatua zote na za ziada zikiwa zimechukuliwa kuweka siri.
“Hivyo, ilimshangaza sana kuona Joram amemfikia na kuuliza maswali ambayo yalimdhihirishia kuwa alikuwa hajapata picha yoyote dhidi ya mipango yao. Kuja kwake hadi mbele yake ilikuwa kubahatisha tu kama wasemavyo Waingereza ‘a shoot in the dark’.

Hata hivyo, Joram hakuwa mtu wa kuruhusiwa zake vivi hivi. Aweza kuwa hajui lolote lakini pengine ameona kitu katikka mambo nya Kwame. Hastahili kupewa mwanya wa kufikiri lolote. Akainua mkono wake na kubonyeza kidude fulani kilichowekwa kwa siri nyuma ya meza yake. Mara sauti ikasikika ikitokea katika kijisanduku kilichokuwa mezani kikisema:
“Number two here. On duty sir,”

‘Vizuri,” Kwame alimjibu. “Umemwona mtu aliyetoka humu ndani sasa hivi?”

“Nimemwona mzee.”

“Ni mtu hatari. Nataka afuatwe na kuangaliwa kila anachokusudia kufanya. Asiruhusiwe kuongea na watu hatari ambao orodha yao unayo. Sawa?”

“Bila shaka mzee.”

“Huenda nikayahitaji maisha yake wakati wowote baada ya uchunguzi wangu. Nitapenda kazi ifanyike vizuri sana. Afe kwa ajali ya gari, kizunguzungu au maradhi yoyote ambayo hayatamshangaza yeyote. Sawa?”

“Bila shaka, mzee.”

“Well.”

NJE ya nyumba hiyo, Joram alisita mlangoni akijaribu kuyaunga maandishi yote aliyoyasoma katika sura ya Kwame ili aupate kikamilifu ujumbe uliokuwemo. Haikuwa rahisi.

Mambo yote yalikuwa nusu nusu kiasi cha kutokupata ujumbe kamili. Alichoweza kufanya ni kupata hisia tu. Hisia ambazo zilimfanya amshuku Kwame kwa jambo moja au lingine.

Alimshuku hasa kwa hotuba zake ambazo zilidhamiria kumtisha., Kwa nini atishwe? Na ilikuwa vipi hata maongezi yake na Kwame yawe kwa maana ya uadui badala ya urafiki? Lazima lilikuwepo jambo. Na lazima afahamu ni lipi jambo hilo.

Wazo au mawazo hayo yakamtia shauku hata akajikuta kajawa na hamu kubwa ya kuendelea na upelelezi wake. Kwa hatua ndefu ndefu akaliacha eneo la ofisi hiyo na kuliendea gari aliloacha likimsubiri. Rohoni akihisi kama anayetoka makaburini au kuzimu na kurejea katika dunia hai.

“Twende zetu brother,” Joram alimweleza dereva ambaye alikuwa kainamia usukani akifikiri au kusinzia.

“Kwa nini? Tunaenda Kigamboni?”

“Kweli! Nilikuwa naanza kusahau,” alijibu akitia gari moto kuiondoa polepole. Msongamano wa magari uliwafanya wapoteze dakika kadhaa kabla ya kupata mwanya wa kurejea barabarani.

Walipoupata na kuanza kuifuata Sokoine Drive, Joram bila kujua kisa cha hofu yake, alijikuta akitazama kila pande kuhakikisha kama halikuwepo gari lolote linalowafuata. Baada ya kusoma kitu kile kisichoelezeka katika macho ya Kwame hakutaka ifahamike na yeyote wapi anakoelekea. Hakuona kama ilikuwepo gari yoyote inayowafuata katika msafara uliokuwa nyuma yao.

Hata hivyo, alimshauri dereva kuiacha Sokoine Drive na kuifuata Samora Avenue akipitia Barabara ya Makunganya. Ni hapo alipoona gari moja iliyokuwa mbele yao ikisita kidogo. Kisha iliendelea na safari. Ilikuwa Datsun yenye namba ambazo Joram hakuweza kuzisoma kikamilifu.

Akiwa katika barabara hiyo ya Samora mbele ya jengo la Kitega Uchumi, Joram aliona gari ile ya Datsun ikitokea mbele yao kasi na kuwapita baada ya dereva kumtupia Joram jicho la haraka haraka. Ndipo Joram alipopatwa na hakika ya kufuatwa huko.

Akamwamuru dereva kusimama, akamlipa na kumtaka aondoke.

“Kwa nini ndugu? Si tunaenda Kigamboni?” alihoji dereva huyo kwa mshangao.

“Nimebadili mawazo. Nitaenda siku nyingine.”

“Pamoja na hayo ndugu, itakuaje nikuache ovyo namna hii? Si bora nikufikishe nyumbani kabisa.”

“Usijali.”

Baada ya kufanikiwa kumwondoa dereva huyo, Joram aliingia katika jengo hilo na kupanda kwa lifti hadi ghorofa ya tano ambapo aliacha lifti na kusimama kando ya dirisha akichungulia chini. Haikumchukua muda kabla hajaiona ile Datsun ileile ikirudi polepole na dereva wake kutoka nje na kutazama huku na huko.

Ilikuwa dhahiri kuwa alimwona Joram alipoachana na ile teksi. Ilikuwa dhahiri pia kuwa mtu au watu hao walimhitaji Joram binafsi, si dereva wa gari ile.

Baada ya kupata hakika hiyo, Joram aliteremka chini na kutoka njeya jumba hilo kwa mwendo wa kawaida, kama ambaye hakujua kuwa kuna mtu anayemsubiri. Joram alipita kando ya gari hiyo bila kuitazama na kuanza kurudi katikati ya jiji. Mara tu alipoipita, Dutsun ilitiwa moto na kuendelea na safari kama gari yoyote isio na shughuli na Joram. Lakini jambo hilo halikumpumbaza Joram hata kidogo. Badala yake ilikuwa ushahidi mwingine ambao ulimtia hakika kuwa anapambana na timu kubwa inayojua wajibu wao. Kwani kuondoka kwa dereva huyo kulimaanisha kuwa huko aendako Joram alikuweko mtu au watu ambao wangeendelea na jukumu la kumfuata.

Hayo yalimfanya Joram acheke rohoni. Kadhalika damu ilimchemka na akili yake kuchangamka. Alihisi kuwa tayari ameingia katika mapambano. Ingawa alikuwa hajawafahamu adui zake, bado alifarijika kwa kuona adui hao tayari wameujua uwezo wake ndipo wakachukua hatua hizo za kumfuatafuata wajue lipi anafanya. Lipi zaidi angehitaji zaidi ya hilo kupata hakika kuwa alikuwa amegundua jambo fulani katika upelelezi wake dhidi ya vifo vya kina Kitenge? Sasa alichohitaji Joram kilikuwa kitu kimoja tu; kumjua adui huyo. Baada ya kumfahamu, isingemchukua muda kufahamu kiini cha mauaji hayo yote.

Kwa Joram Kiango kumjua mtu anayemfuata halikuwa tatizo. Alichofanya ni kuendelea kutembea polepole huku akiwa na hakika kuwa anafuatwa. Alipofikia sanamu ya askari, alipanda kufuata Barabara ya Maktaba.

Alisita kidogo mbele ya maktaba ya Wafaransa akitazama picha zilizowekwa ukutani, kisha aliendelea. Akapinda kona kuifuata Barabara ya Jamhuri. Baada ya kuifuata kidogo, aliacha barabara na kufuata uchocho mdogo wenye giza.

Hapo alijificha akichungulia barabarani. Haikuchukua muda kabla hajamwona mtu mrefu mwenye dalili zote za tabia ya kutumia nguvu akifika hapo na kutazamatazama. Mtu huyo alisita, kisha akajitoma kuufuata uchochoro huo. Alitembea kwa tahadhari na uangalifu.

“Unanitafuta mimi ndugu?” Sauti ya Joram ilimgutusha mtu huyo. Kabla hajajua afanye nini alipokea pigo la judo ambalo lilimtua vyema shingoni. Akalalamika na kuanza kuanguka. Lakini Joram alimdaka na kumweka chini kistaarabu huku akimzindua kwa ngumi ya uso. Mtu huyo alijaribu kujitetea lakini pigo lingine la Joramu usoni mwake lilimlegeza kabisa. Akakoroma kwa maumivu huku akiruhusu damu kumtoka kinywani na puani.

“Hiyo ni kukufahamisha kuwa sipendi kufuatwafuatwa,” Joram alimweleza kwa kebehi. “Sasa nataka uniambie mara moja nani amekutumeni kunifuata?” jitu hilo liliguna tu. Joram akalizawadia pigo lingine ambalo lilifanya lilalamike na kusema kwa udhaifu.

“Utaniua bure. Mimi simjui mkubwa wangu. Napewa amri na mtu mmoja anayeitwa Kauzibe bin Kaubandike. Nasikia naye pia si mkubwa wala hatumjui mkubwa wetu.”

“Mnapewa amri gani?” Joram alizidi kusaili.

“Amri ya kufanya lolote, hata kuua ikibidi. Tunachojali ni pesa ambazo ni nyingi.”

“Leo pia kawapeni amri ya kunifuata?”

“Ndiyo.”

“Saa ngapi?”

“Muda mfupi uliopita. Ilikuwa amri ya haraka sana.”

“Ilisemaje amri hiyo?”

“Tulipewa picha zako. Tukaambiwa usivuke kwenda Kigamboni.ukilazimisha kufanya hivyo tukuue. Hivyo endapo ungelazimisha ukiwa ndani ya gari ile ajali ingetukia. Na ingekuwa muujiza kama ungepona.”

“Mko wangapi?”

“Tuko wengi sana, lakini hatufahamiani. Sasa hivi watafika hapa endapo nitachelewa.’

Joram alijua huo ni ukweli ambao pia ulikusudiwa kuwa tishio kwake. Akaikagua mifuko ya mateka wake na kupata bastola ambayo aliipachika mfukoni mwake na vitambulisho vya uongo ambavyo alivichana.

“Unasikia wewe,” alifoka baadaye. “Mwambie yeyote huyo unayemwita bosi wako kuwa sipendi mzaha wa kufuatwa. Ningeweza kumwonyesha kuwa sipendi tabia hiyo kwa kukufanya wewe maiti, aiokote kesho, maadamu wewe mtumwa nimekusamehe. Mwambie akithubutu tena kufanya hivyo atapata salamu za Joram Kiango.”

Jina hilo lilimfanya yule mtu agutuke na kutoa macho ya mshangao na kutokuamini. “Nani… Joram…” Joram hakumjibu, aliondoka zake polepole lakini kwa hadhari zaidi.

Dakika kadhaa baadaye, hakuwa Joram Kiango yuleyule tena. Alikuwa mtu mwingine aliyebadilika kimavazi kiasi cha kuweza kumchanganya mtu yeyote. Sasa alivaa suti yake nyeusi, tai nyeusi, shati jeusi na kofia nyeusi. Kitu pekee cheupe mwilini mwake kilikuwa ni kitambaa cheupe alichofunga shingoni.

Kitambaa ambacho kukiondoa hapo kungemfanya aonekane kivuli au sehemu ya kiza ambacho kilitanda kwa silaha zake ambazo ni pamoja na bastola, visu, nyembe, tochi yenye ukubwa wa kalamu na dawa ambazo humsaidia katika shughuli zake.

Akiwa karidhika na hali yake, aliyaacha makazi yake, sehemu za Ilala na kukiendea kituo cha basi ambapo alijiunga na watu waliokuwa wakisubiri usafiri wa kwenda mjini kufunga siku kwa starehe za dansi, sinema na vinywaji.

Hayo yalikuwa yakitokea dakika arobaini na tano tu baada ya Joram kumwacha mahututi yule jambazi aliyekuwa akimnyemelea katika vichochoro vya Mtaa wa Jamhuri. Alikuwa amesafiri harakaharaka, akisaidiwa na usiku ambao ulianza kutawala na kumficha asionwe na gaidi mwingine na kuweza kusumbuliwa pindi akienda kwake.

Alipofika nyumbani alipiga simu ya haraka kwa katibu wake kumjulisha hali ilivyo, kisha hima akaanza kubadili mavazi na baadaye kujitokeza mitaani akiwa kama alivyo. Sura ikionyesha utulivu, mavazi yakitangaza starehe hali rohoni kabeba furushi la mashaka na taharuki kwa kufikiria jukumu lililokuwa mbele yake.

Hofu yake haikuwa juu ya maisha yake, ingawa kwa mujibu wa taarifa ya yule jambazi aliyepambana naye dakika chache zilizopita, alifahamu kuwa anaelekea eneo la hatari sana. Hasa, hofu yake ilikuwa juu ya maisha au usalama wa mtu aliyekuwa akimfuata; Dismas Komba. Aliamini kwamba yupo mashakani. Moyo ulimshawishi kufanya haraka sana ili kujaribu kumtoa katika hatari hiyo.

Lilitokea basi lielekealo Posta, Joram alikuwa mtu wa kwanza kulidandia. Na lilipowasili aliwatangulia wote kuteremka. Akafanya haraka kuchukua teksi ambayo ilimfikisha Ferry ambako alijiunga na wavuvi pamoja na watu wengine waliokuwa wakinunua samaki. Alijitia mteja wa kawaida lakini macho yake yalikuwa kazini yakisoma sura za watu kuangalia kama alikuwepo yeyote kati ya maadui ambao walipewa jukumu la kutokumruhusu kufika Kigamboni. Aliporidhika na nyuso hizo alimshawishi mvuvi mmoja, kijana ambaye alikubali kumvusha hadi upande wa pili kwa shilingi hamsini akitumia ngalawa yake.

Joram alimsaidia kijana huyo kwa kupiga kasia kwa namna ambayo ilimchekesha sana kijana huyo kwa jinsi asivyofahamu kazi hiyo. “Acha tu mzee,” alisema kijana huyo. Kisha alibadili sauti katika kicheko chake na kukifanya kiwe cha kitu kama dharau ama mshangao. Kicheko hicho kilifuatwa na swali lililodai, “Yaonyesha u tajiri sana mzee?”

“Kwa nini? Alihoji Joram.

“Watu wenye fedha ndogo kama mimi si rahisi kukodi mtumbwi. Pantoni iko pale na inachukua watu bure kwa haraka na usalama zaidi.”

Ikawa zamu ya Joram kucheka. Kijana huyu hakujua kuwa alikuwa ameepuka pantoni hiyo kwa hadhari akijua kuwa kama kuna ulinzi wowote dhidi yake, haikuwepo sehemu nzuri zaidi ya hapo kivukoni. Hivyo, alikuwa akiepuka kuonekana na jicho ambalo halikustahili kumwona hasa kwa wakati huo. Lakini alimjibu kijana huyo kwa kumlaghai, “Siku nyingi mno sijasafiri katika chombo kidogo kama hiki. Hizo shilingi hamsini nilizokupa ni kati ya mia nilizozipata katika bahati nasibu. Hazikuwa katika bajeti.”

“Kwa nini basi usingekuja mchana? Saa mbili u nusu za usiku! Utafaidi nini?”

“Safari ya usiku naipenda zaidi.”

Walipowasili upande wa pili nje kabisa na kituo cha kawaida, Joram alimshukuru kijana huyu na kisha kuanza safari ya kuingia Kigamboni. Akiyafuata maelekezo ya yule mtumishi wa Kamata alifikia nyumba ambayo alidhani ingekuwa ya Komba. Lakini mara baada ya kuuliza kwa mtoto aliyeketi nje ya nyumba hiyo aligundua kwamba aliikosea.

“Ni ile pale. Si yule Komba wa Kamata?”

“Ndiye.”

“Ile pale.”

Joram alipoanza kuondoka ili aiendee, mtoto huyo alimzuia kwa kusema, “Unakwenda pale mzee? Hapafikiki siku hizi. Hasa usiku kama huu!”

“Kwa nini?”

“Pana miujiza sana. Mambo ya ajabu yanatokea katika nyumba ile. Nadhani kuna jinsi au majini.”

“Kwani vipi bwana mdogo?”

“Mengi yanatukia pale. Wapangaji wote wamehama. Amebaki Dismas peke yake. Inasemekana kwamba anajifungi achumbani usiku na mchana. Bila shaka kati ya kesho na keshokutwa atakuwa chizi.”

Joram akajikuta akizidiwa na hamu ya kuyaelewa maongezi hayo. “Kijana, nieleze vizuri nikuelewe. Unataka kusema kwamba kuna mambo ya ajabu ajabu yanatokea katika nyumba ile? Kama yapi? Nieleze hatua kwa hatua.”
“Ni habari ngumu kueleweka. Watu wanadai kuwa kabeba jini kutoka Unguja alikokwenda hivi karibuni. Tangu alipotoka huko mambo yake hayaeleweki. Siku ya kwanza aliporudi, alikuwa katika hali ya kawaida. Usiku huo alisikika akilia na kunyamaza ghafla. Jirani aliyeamka na kumwendea alirudi mbio akilia ati kapigwa kama jiwe tumboni na mtu asiyeonekana. Asubuhi waliomwona Dismas walidai kuwa alikuwa kachubuka usoni na damu ikiwa imekaukia puani. Yasemekana alitoka ili aende mjini, akaingia katika pantoni na kuvuka ng’ambo, lakini aliporudi alirudi nalo huku akitetemeka.

“Ni hapo alipoanza tabia ya kujifungia ndani. Yasemekana pia kuwa wapangaji hao waliohama walikuwa wamelala ndani lakini walipoamka alfajiri walijikuta wamelala nje, uchi wa mnyama, hali vitu vyao humo ndani vikiwa vimetapanywa ovyo ovyo. Hata sisi watoto ambao tumekuwa

tukicheza mbele ya nyumba hiyo tumeacha baada ya mwenzetu mmoja usiku wa juzi kutoweka ghafla na kuokotwa baada ya muda mrefu kalala ufukoni. Alipoulizwa kilichomfanya alale huko na vipi alienda huko hakuwa na jibu zaidi ya kushangaa tu."

"Ni hadithi nzuri," Joram alimjibu akitabasamu.

"Siyo hadithi. Yametokea na yanaendelea kutokea…"

Joram hakuwa na nafasi ya kumsikiliza zaidi. Mawazo yake tayari yalikuwa kazini yakiifikiria taarifa hiyo. Macho yake pia yalikuwa yakipambana na kiza kujaribu kutazama eneo la nyumba hiyo ambayo kiasi ilijitenga na nyumba nyingine kutokana na utaratibu usioridhisha wa mjenzi au mpimaji. Nyumba hiyo ilizungukwa na kichaka kikubwa cha miti au maua yasiyo katika utaratibu mzuri.

Kwa mtu kama Joram ilikuwa ni rahisi kuhisi kichaka hicho kingeweza kuwa hifadhi nzuri ya mtu au watu waliodhamiria kumtendea Dismas Komba jambo fulani, si kama walivyodhani watu wengine kuwa ni majini yaliyofanya yote hayo. Joram alimshuku pia kuwa kile kitendo cha watoto na majirani kilidhamiriwa kuwaweka watu wote mbali ya eneo hilo ili wapate nafasi nzuri ya kuendelea na harakati zao. Harakati ambazo zilikusudiwa kupoteza maisha ya Komba. Kwa nini?

Hakuwa na nafasi ya kujijibu maswali hayo. Damu ilikuwa ikimchemka na moyo kumwenda mbio huku nafsi ikimshawishi kufanya haraka kabla halijatukia lolote baya zaidi kwa Komba.

Hata hivyo, baada ya kumshukuru mtoto huyo kwa sauti ambayo haikuonyesha kuwa kaamini lolote kati ya hayo, aliondoka zake polepole akielekea upande mwingine. Mikono yake ilikuwa shingoni kuondoa kile kitambaa cheupe. Mara akawa kama kivuli. Ili kupima kama alikuwa katika hali ya kuridhisha alipiga hatua mbili nje ya barabara na kusimama.

Watu wengi walipita bila ya kumwona. Mara alitokea mzee, kafutana na binti mwenye umri wa mjukuu wake. Walikuwa wakizungumza mambo ambayo yalimshangaza Joram kupita kiasi. Walipomkaribia zaidi walisimama na kuendelea na maongezi yao.

Nusura atokwe na kicheko kwa kusikiliza utongozaji huo wa kizamani mno. Lakini alijikuta akishindwa kustahimili kuondoka pindi maongezi hayo yalipopamba moto na kubadilika kuwa mahaba kwa mtindo ambao Joram hakutarajia kuwa binti mdogo kama huyo angediriki kumtendea babu wa kiasi hicho.

Aliondoka kwa kunyata akiifuata nyumba ya Dismas Komba. Alipoikaribia alitafuta nafasi nzuri katika kichaka cha maua na kuketi chini akisubiri.

Alisubiri sana. Kusubiri ikiwa miongoni mwa shughuli zake hakukinai kuketi hapo, akivumilia mirija ya mbu huku macho yake ambayo yalikwishazoea giza yakiwa wazi kutazama lolote. Nia yake ilikuwa ifike saa saba au nane ya usiku ndipo aendelee na safari yake hadi katika nyumba ambamo alikusudia kuonana na Komba. Kwenda papara baada ya kusikia 'hadithi' ya yule kijana juu ya nyumba hiyo isingetofautiana na nondo aendavyo katika moto kwa tamaa ya mwanga.

Joram alipoitazama tena saa yake na kuona ikikaribia saa sita za usiku, alianza kujiandaa kuisogelea nyumba hiyo. Nia yake ikiwa ashughulikie dirisha moja au mlango na kuingia ndani ambako angehitaji kupata hakika kama sehemu ya kiza ikichezacheza hatua kadhaa mbele yake. Baada ya kutazama kwa makini aliona dalili za kiumbe hai, kikitembea polepole kuiendea nyumba hiyohiyo. Alikuwa mtu! Kavaa mavazi mieusi kama yake. Macho ya Joram yaliongeza juhudi kutazama kama mtu huyo alikuwa peke yake. Hakuona dalili ya mtu mwingine. Ndipo Joram alipouinua mguu mmoja baada ya mwingine kwa hadhari na utulivu kama kivuli akimfuata.

Mtu huyo alipoufikia mlango hakuchelewa sana kuushughulikia, ukafunguka polepole naye akaingia huku akiufunga. Joram alimpa dakika mbili, tatu kisha akausogelea mlango na kuujaribu. Haukuwa umefungwa. Akaufungua na kunyata ndani huku masikio yake yakiwa wazi, mkono wake ukiipapasa bastola yake.

Humo ndani kulikuwa na kiza ambacho kilitisha mno. Nuru hafifu sana ilionekana kwa shida kutoka chumba kimoja. Joram alikifuata chumba hicho na kutega sikio lake katika tundu la ufunguo akisikiliza. Haikuwepo haja ya kusikiliza kwa makini kiasi hicho.

Sauti ya mtu au watu wanaogombana kidhaifu ilimfikia kwa urahisi. Mmoja alikuwa akisema, “Wapi? Usiposema nitakuua…” Mwingine alilalamika tu.

“Nitakuua kweli,” ilidai tena sauti hiyo nzito zaidi. Ikafuatwa na malalamiko ya maumivu makali.

Joram hakustahimili zaidi. Akaufungua mlango kimyakimya kwa haraka zaidi na kujitoma ndani. Aliingia wakati mzuri sana wa kuwa shahidi aliyeshuhudia jisu kali na refu likiingia katika kifua cha mtu aliyelala juu ya sakafu.

Pigo la pili Joram alilizuia kwa kumpiga muuaji huyo judo ya shingo. Hakuwa amelipiga vizuri pigo hilo, kwani badala ya mtu huyo kuzirai kama alivyotarajia Joram, alishangaa kumwona akiinuka na kumtazama Joram kwa macho makali yenye mshangao. Joram akaachia pigo jingine. Hili lilimwingia mtu huyo, lakini halikumtosheleza. Alichofanya ni kupepesuka kidogo tu na kuinuka tena akimjia Joram huku kajiandaa tayari. Joram akaona kuwa alikuwa kakukutana na mtu hatari kwa judo.

Akajiandaa vyema zaidi. Mt huyo alimjia Joram, mikono yake iliyotapakaa damu ikiwa imetangulia. Joram alimwepuka nsa kurusha kung fu ambayo ilikwepwa na kufuatwa na karate ambayo ilimkubali Joram ubavuni. Kabla hajakaa vyema pigo la pili lilimtua shingoni.

Joram alitamani kuuzamisha mkono wake mfukoni ili apate bastola yake, lakini alihisi hiyo ni dalili ya woga na bado alifurahia nafasi hiyo ya kuupima uwezo wake kijudo. Hata hivyo alijutia uamuzi wake huo baada ya dakika kadhaa za mapambano na kujikuta katupwa chali, mikono ya jitu hilo ikitambaa kooni ili kumkaba. Joram alijitahidi kurusha mateke na mikono, haikusaidia.

Mikono ya mtu huyo ilikwishapata koromeo lake na sasa ilianza kumkaba kwa nguvu kana kwamba ni vidole vya chuma. Macho yakaanza kumtoka Joram kwa hofu. Lakini macho hayo yalibadilika na kutazama kwa faraja pindi alipoona yule mtu aliye sakafuni akijikongoja kuinuka na kuchomoa jisu kutoka kifuani mwake na kukididimiza mgongoni mwa adui aliyemkalia kifuani.
Lilikuwa pigo dhifu mno lakini lilimfanya mtu huyo kumsahau Joram na kugeuka nyuma. Joram aliitumia nafasi hiyo kuachia pigo zito la mwisho. Pigo ambalo lilitimiza wajibu wake. Muuaji akaanguka sakafuni. Joram akamwahi kwa kumtia kamba za miguuni na mikononi haraka haraka. Kisha akamwinamia na kumtazama vizuri.

“Mama.”

Sauti hiyo ilimzindua Joram. Akamwacha muuaji huyo aliyelala kama mzoga na kumsogelea mtu huyo aliyekuwa akijaribu kuinuka ili ainue tena jisu na kummaliza adui yake. Joram hakuwa na haja ya kuambiwa kuwa mtu huyo ni Dismas Komba!

“Asante kwa kuokoa maisha yangu Bwana Dismas,” alimweleza haraka haraka. “Unadhani kwa nini walitaka kukuua?” aliuliza.

“Wamekwishaniua…Nakufa…” Komba aliendelea kulalamika.

“Wewe sio mmojawao?”

“Mimi ni adui yao mkubwa.”

“Wewe ni nani?”

“Huwezi kunifahamu. Kwa jina ni Joram Kiango.”

“Joram! Nakujua sana…” Komba alisema kwa juhudi kubwa. “Joram! Walinitesa sana…Laiti wangeniua…nilikuwa sina hali siku zote. Nikienda huku nakutana nao. Nikikaa hapa usiku wanafika na kuniadhibu kwa vitisho na mateso. Wameniua…” akaanza tena kulalamika.

4

SAUTI hiyo ilimzindua Joram. Akamwacha muuaji huyo aliyelala kama mzoga na kumsogelea mtu huyo aliyekuwa akijaribu kuinuka ili ainue tena jisu na kummaliza adui yake. Joram hakuwa na haja ya kuambiwa kuwa mtu huyo ni Dismas Komba!

"Asante kwa kuokoa maisha yangu Bwana Dismas," alimweleza haraka haraka. "Unadhani kwa nini walitaka kukuua?" aliuliza.

"Wamekwishaniua…Nakufa…" Komba aliendelea kulalamika.

"Wewe sio mmojawao?"

"Mimi ni adui yao mkubwa."

"Wewe ni nani?"

"Huwezi kunifahamu. Kwa jina ni Joram Kiango."

"Joram! Nakujua sana…" Komba alisema kwa juhudi kubwa. "Joram! Walinitesa sana…Laiti wangeniua…nilikuwa sina hali siku zote. Nikienda huku nakutana nao. Nikikaa hapa usiku wanafika na kuniadhibu kwa vitisho na mateso. Wameniua…" akaanza tena kulalamika.

Ingawa nuru ilikuwa hafifu, ikitoka katika mshumaa uliowekwa kwenye kona moja ya chumba, lakini ilitosha Joram kuona katika macho yake Dismas Komba kuwa uhai ulikuwa ukimtoka harakaharaka. Hakuwa na muda wa kuishi zaidi.

"Sema haraka," Joram alimhimiza. "Dismas kwa nini walitaka kukuua?"
"Wameniua tayari… nakufa…"

"Kitu gani wanadai kutoka kwako?"

"Wa…wame…wa…" Komba akaishiwa na uwezo wa kuzungumza. Alichofanya ni kuinua mkono kwa udhaifu akiuelekeza katika pembe moja ya chumba. Joram aliufuata mkono huo na kuona unaelekea debe lililokuwa hapo. Akaliendea na kuchungulia.

Alilakiwa na harufu kali ya kinyesi cha haja kubwa na ndogo ambacho kilikuwepo ndani ya debe hilo. Akarudisha macho ya kutoelewa kwa Komba. Akaona kakazana kuelekeza kidole papohapo, akajitahidi kutamka neno ambalo halikutamkika. Joram akahisi kuwa lazima kama kuna chochote alikuwa kaficha haikuwepo nafasi ambayo isingeweza kufikiriwa zaidi ya hapo. Hivyo akazidi kupekuapekua kando ya debe.

Akaliinua. Chini yake akakuta bahasha iliyofurika karatasi. Akaitwaa na kumgeukia Komba. Alimwona akitabasamu kisha kuanguka kwa nyuma. Mara akaanza kutapatapa kwa maumivu pindi roho ikimtoka. Joram alikimbia na kujaribu kumshika, haikusaidia. Tayari, Komba alilala kwa utulivu katika usingizi usio na mwisho.

Joram hakuona lipi zaidi angeweza kulifanya kuokoa maisha ya mtu huyo. Akaiendea swichi ya taa ya umeme na kuiwasha, haikuwaka. Hivyo akaichomoa tochi yake yenye ukubwa wa kalamu na kuiwasha. Nuru ilitoka kumwezesha kusoma neno moja tu ambalo liliandikwa juu ya bahasha hiyo USIFUNGUE.

Joram hakumtii yeyote aliyeandika neno hilo, akaifungua na kutoa karatasi ndefu ambayo iliandikwa kwa mashine ya aina yake kwa lugha ya Kiingereza, maneno ambayo tafsiri yake ilisema:

…NI DHAHIRI KUWA NJAMA ZETU ZA KUCHANGIA HALI NGUMU YA KIUCHUMIAMBAYO ILIKUWA IKIIKABILI NCHI HII HAZIKULETA MATUNDA TULIYOYAHITAJI, YAANI KUWAFANYA WANANCHI WAENDE KINYUME NA UTARATIBU WAO NA KULETA GHASIA AMBAYO TUNGEINGILIA KATI NA KULETA UTAWALA WETU. NI WAZI KABISA KUWA WAMEWAELEWA VIONGOZI WAO NA WAKO NAO BEGA KWA BEGA KUJENGA UPYA UCHUMI WAO. BAADA YA MUDA MFUPI, NJAMA ZETU ZA KUCHANGIA HALI HII NGUMU ZITAJULIKANA.

NA HAPO WANANCHI WATAKAPOAMKA NA KUPATA MOYO MPYA AMBAO SI KWAMBA UTAWAFANYA WASHINDE VITA VYA KIUCHUMI TU BALI WATAENDELEA KUIAMINI NA KUITEGEMEA KABISA SIASA YA UJAMAA NA KUJITEGEMEA. HAPO NDOTO ZETU ZA KUUWEKA UTAWALA MIKONONI MWETU KATIKA NCHI HII ZITAKUWA ZIMEKWISHA.

NAAMINI INAFAHAMIKA WAZI KUWA, NCHI HII NI KAMA NURU AMBAYO AFRIKA NZIMA INAIFUATA. UKOMBOZI WA NCHI ZOTE ZA KUSINI AMBAZO ZILIKUWA HAZIJAPATA UHURU WAKE NA ZINAZOENDELEA KUUPATA UMETOKANA NA MSIMAMO WA NCHI HII.

BAYA ZAIDI NI UHURU WA KIUCHUMI AMBAO NCHI HII INAONGOZA MAPAMBANO. MARA ITAKAPOJIIMARISHA KIUCHUMI NCHI YA SIASA YA UJAMAA, NCHI ZOTE ZITAONA NURU NA KUIFUATA HILO LITALETA MUUNGANO WA AFRIKA. HATUTAKI MAMBO HAYO YATOKEE LEO WALA KESHO. INASIKITISHA KUWA PAMOJA NA HALI KUWA NGUMU YANAELEKEA KUTOKEA.

KWA HIYO UAMUZI ULIOFIKIWA NA TWAA, WADHAMINI WETU NI KUUCHUKUA UTAWALA HUU KIMABAVU. YATAFANYIKA MAPINDUZI YA SILAHA. HATUJALI KUMWAGIKA DAMU WALA MAAFA, MAADAMU TUMESHINDA. WATU TULIOWAANDAA HUKO JESHINI, KATIKA BARAZA LA MAWAZIRI, NDANI YA CHAMA, KATIKA MASHIRIKA YA UMMA NA VYUO VIKUU WATASAIDIA KUULAGHAI UMMA ILI UTUUNGE MKONO. VILEVILE WANANCHI WATAPAKWA MAFUTA KWA MGONGO WA CHUPA KWA KULETEWA VITU ADIMU KAMA SUKARI, SABUNI, MAFUTA, NGUO NA KADHALIKA. WATAAMBIWA KUWA HAYO NI MATUNDA YA UTAWALA MPYA.

WATAFURAHI. BAADA YA HAPO MAMBO YATABADILIKA. UBEPARI UTARUDI MTINDO MMOJA. HATAKUWEPO YEYOTE MWENYE AMRI YA KUUPINGA UTAWALA WETU.

MPAKA SASA MASHARTI BADO NI YALEYALE ; KUWAPA WADHAMINI KISIWA KIMOJA ILI WAFANYE KAMA KITUO CHAO CHA UTAFITI WA SILAHA. WANANCHI WOTE WATAHAMISHIWA HADI KISIWA KINGINE ILI KUWARUHUSU KUANZA BIASHARA ZOZOTE ZA KIUCHUMI BILA MASHARTI, KUWASHUKURU KUTEUA AU KUPENDEKEZA VIONGOZI WANAOWATAKA NA MENGINE YATAKAYOJITOKEZA.

KWA SASA BADO VIONGOZI NI WALEWALE AMBAO WALITAJWA KATIKA KIKAO KILICHOPITA;

TOP KOLOTO – RAIS WA NCHI
MOTO MATATA – MAKAMU WA RAIS
BOMBO MTORO – WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE
CHEMA CHITIME – WAZIRI WA HABARI
JOE KILEO – WAZIRI WA ULINZI.

WALIOSALIA WATATEULIWA KUTOKA KATIKA ORODHA YA WANACHAMA WETU WALIOKO KATIKA NAFASI KUBWA SERIKALINI.

Taarifa hii ni ya mwisho itakayofanyika kwa siri kubwa kiasi hiki. Wakati wowote katika wiki mbili zijazo mambo yatapamba moto. Watu wetu wataarifiwa kwa dharura ili kuanza mambo. Ndipo maji yatakatwa kwa siku kadhaa kuwalegeza wananchi, vyombo vya habari vitatoa habari za ajabuajabu zenye nia ya kuwachukiza wananchi dhidi ya Serikali yao, kisha siku hiyo umeme utakatika ghafla na mapambano kuanza. Itakuwa rahisi sana. Wachache watatiwa pingu, wachache watauawa na kutakapopambazuka utawala utakuwa mpya.
Joram alimaliza kuisoma karatasi hiyo huku akitetemeka kidogo. Haikuwa na mzaha hata chembe ingawa aliamini kuwa iliandikwa na watu wenye wazimu na tamaa ya madaraka ya uroho wa utajiri wa haraka haraka. Kama alivyokuwa amehisi kitambo, zilikuwepo njama kubwa zaidi ya ile iliyofikiriwa na polisi ya mwandishi aliyechanganyikiwa –Bazile – kupata kichaa na kuanza kuua ovyo. Mauaji hayo yalipangwa tu, yakitumia jina

la Bazile ili yaendelee kufanyika kwa siri bila wahusika kuhisi lolote. Na kiini cha mauaji pengine kilikuwa hiki cha kuficha siri hii ambayo kwa namna moja au nyingine iliondokea kuifikia mikono ya watu wasiohusika.

Mara Joram akagutuka na kumsogelea yule adui aliyekuwa akipambana naye muda mfupi uliopita. Alikuwa amekumbuka kuwa sura yake haikuwa ngeni machoni mwake. Akainama na kummulika usoni kwa kurunzi lake. Naam, sura ilikuwa ile ile ambayo si yeye tu bali karibu kila mtu aliifahamu na kuiogopa. Sura ya mtu yuleyule ambaye alikuwa akihitajiwa sana na polisi. Yule mtunzi wa vitabu vya mauaji na ambaye aliondoka kuwa muuaji mkubwa; Bazile Ramadhani.

Ugunduzi huu ungeweza kuwafurahisha polisi, kwani mtu hatari sana alikuwa amenaswa. Lakini kwa Joram Kiango, kunaswa kwa Bazile hakungeweza kumpa furaha hata chembe: Taarifa ya njama za mapinduzi ilikuwa mfukoni ikimkodolea macho. Hakuona vipi Bazile aliweza kuingia katika kikundi hicho na vile aliondokea kuwa hodari kwa mauaji.

Kwa kweli alikuwa haamini kuwa muuaji ni Bazile. Na kama alikuwa huyo, kulingana na madai au ushahidi wa polisi hasa kwa kifo cha Kitenge yule mtoaji vitabu, basi Joram aliamini ni kifo hicho tu ambacho angeweza kukifanya. Vifo vingine alihisi kuwa ziko njama za mtu au watu wengine. Lakini leo kashuhudia mwenyewe, na anaye mkononi Bazile huyohuyo, muuaji, anaweza vipi kuendelea kukanusha? Akazidi kumtazama vizuri.

Akaingiza mikono yake mifukoni na kutoa silaha za kijasusi ambazo hutumiwa na majasusi wa hali ya juu sana. Vitu kama vikopo vyenye sumu za kulevya, vidonge viwezavyo kuua kwa muda mfupi sana, bastola ndogo, kitambulisho na kadhalika. Vyote hivyo Joram alivitia mfukoni mwake. Kisha akarudisha macho yake juu ya uso wa Bazile kwa mshangao.

Macho yake yalikuwa wazi yakimtazama kwa ujeuri na kutokujali. Hayakuwa macho ambayo Joram alimtegemea mwandishi huyo kuwa nayo. Akaupeleka mkono wake kuupapasa uso huo. Mara Joram akaangua kicheko. Alipoutoa tena mkono wake ulikuwa umeshikilia ngozi ya uso wa Bazile ambao uling'oka kwa taabu. Uliobaki badala ya uso huo ulikuwa uso mweupe wa mtu mwenye sura mbaya. Uso wa jasusi lenye moyo wa mnyama ambalo bila
shaka lilikuwa limekodiwa kufanya mauaji hayo.

"Kill me" lilimwamuru Joram jitu hilo.

"Who are you?" Joram alimuuliza.

"Just kill me."

Joram akaokota tambara chafu na kulididimiza katika domo la jitu hilo ili lisiendelee kusema. Kisha akahakikisha kamba alizotumia kulifunga jitu hilo zilitosha. Akaongeza nyingine na kutoa kila kifaa mwilini mwa jitu hilo. Aliporidhika, alitoka chumbani na kuufunga mlango vizuri akiwa na hakika kuwa jasusi huyo asingepata mwanya wowote wa kutoroka.

Saa yake ilidai ni zaidi ya saa nane za usiku. Bado alikuwa na saa nne ili aendelee na harakati zake za kumaliza upelelezi huo.
Akaamua kusubiri papohapo akimlinda mateka wake. Alitumia funguo zake 'malaya' kuingia chumba cha pili ambako alikuta kitanda kizuri kikimsubiri. Akajilaza. Usingizi haukumjia. Akijua kwamba chumba cha pili kina muuaji hatari na maiti ya mtu, mawazo hayakuweza kutulia.

Zaidi, alishindwa kulala kwa jinsi fikara zilivyokuwa zikimpita kichwani juu ya barua hiyo ya siri aliyokuwa nayo. Alifahamu kagundua siri kubwa. Lakini bado alifahamu kuwa hajagundua lolote dhidi ya watu hao wanaokusudia kuichukua nchi. Ilikuwa wazo kuwa majina hayo yalikuwa bandia tu. Hakuwa na muda wa kujisumbua kumtesa mateka wake mzungu ili amwambie.

Kwani, kwa kadri anavyowafahamu majasusi hao, hawawezi kutamka lolote. Hata hivyo, Joram alijua lipo ambalo angefanya kesho ili kuweza kupata walao njia ambayo ingemwezesha kuwafahamu watu hao waliochoshwa na amani. Kiasi pia alijiuliza juu ya Bazile. Kama muuaji alikuwa akiutumia uso wake, yeye mwenyewe yuko wapi? Pengine naye kauawa na kuzikwa kwa siri?

Mapambazuko! Joram aliyasubiri kwa hamu kubwa mapambazuko ili apate majibu ya maswali hayo na mengi mengine.

KULIPOPAMBAZUKA, Joram aliwachungulia maiti na mateka na kuona wako katika hali ile ile ya usiku. Akawafungia tena na kuamua kuwaacha katika hali hiyo. “Maadam nyumba inaogopwa kuwa ina mkosi au majini, wanaweza kuendelea kukaa humu walau kwa saa sita bila kuonekana,” alijisemea akihifadhi vizuri vifaa vyake vyote alivyopata katika nyumba hiyo. Akakiendea kivuko ambako alikuwa miongoni kwa abiria wa kwanza. Upande wa pili alitembea kwa mguu hadi kituoni ambako alipanda basi lililompeleka uwanja wa ndege.

Wafanyakazi walikuwa ndio bado wanawasili na mabasi yao. Joram alitazama hadi alipomwona yule binti aliyempa orodha ya wasafiri wa ndege aliyoihitaji jana. Binti huyo alimtazama kwa macho ya kufahamiana na tabasamu.

“Mbona mapema hivyo?” alihoji.

“Kuna kitu nilisahau kuuliza jana,” Joram alihoji na kuongeza,
“Tafadhali jaribu kukumbuka kama uliona tukio lolote la ajabu au ambalo halikuwa na kawaida siku ile?”

“Ipi?”

“Ile waliposafiri watu hawa,” akamwonyesha orodha ya majina yao.
Msichana huyo alijaribu kuwaza sana. mara akakumbuka jambo.

“Nakumbuka yuko mzee mmoja kati yao ambaye alitujia katoa macho pima na kudai kuwa begi lake limeibwa, mikononi alikuwa na begi lingine aina ileile ya suitcase. Tulipomuuliza hiyo kapata wapi alisema ameikuta badala yake. Tukamwelekeza kwenda chumba ambacho begi hilo lingeweza kufunguliwa ili ijulikane nani mwenyewe. Alienda huko. Aliporudi huko alikuwa akicheka na kutuambia kuwa begi lilikuwa lake isipokuwa lilikwaruzwa kidogo ndipo akalisahau.”

“Unamfahamu mtu huyo?”

“Sana. huwa anasafiri mara kwa mara. Jina lake ni Kwame. Nasikia ana kampuni yake binafsi.”

Joram hakuweza kujizuia kuonyesha furaha aliyoipata baada ya kusikia hayo. Tayari alikuwa na shilingi mia mbili mfukoni akimpa binti huyo huku akisema, “Umenisaidia sana mpenzi.”

“Sioni nimekusaidia vipi.”

“Utaona baadaye,” Joram alisema akiondoka kuendea teksi zilizosimama kando yao zikiwasubiri abiria.

Hisia zake za awali juu ya kuhusika kwa Kwame kwa njia fulani katika njama hizi sasa zilikuwa zimethibitika. Kupotelewa na mfuko, Joram alifahamu ni jambo lililotokea. Pengine marehemu Komba aliuchukua mfuko huo kwa kukosea, pengine alikusudia. Kwame bada ya kugundua hayo, akijua kuwa kuna siri kubwa ambayo hakupenda ijulikane, alichanganyikiwa na kuwapigia kelele wahudumu.

Lakini baada ya kufikiri zaidi ndipo alibuni uongo kwa kudai kuwa mfuko ni wake kwa matumaini ya kumfahamu mwenye mfuko huo kwa kusoma hati ambazo zingekuwepo ndani ya mfuko huo.

Ni njia hiyo iliyomwezesha kumpata marehemu Komba. Pengine, hata kuchelewa kumuua kulitokana na hofu yao ya kutojua iliko barua ile ya siri. Naye Komba yaelekea alikuwa mgumu wa kuitoa kwa kufahamu kuwa mara waipatapo, wasingesita kummaliza.
Wakati wakiwaza hayo, Joram alikuwa ndani ya gari akielekea mjini. Teksi ilimfikisha nyumbani kwake ambako alioga vizuri, akavaa mavazi yaliyomstahili na kuweka mifukoni vitu alivyovihitaji, kisha alitoka kwenda ofisini.

Neema alimlaki na maswali mengi. Joram alijibu machache tu akimwahidi kuwa baada ya saa chache atajibu yote. Kisha, aliandika kadi moja ya ‘express’ na kumwomba Neema aipeleke Posta. Aliporudi, Joram alimpa maelekezo mengine ambayo yalimfanya Neema atoe macho kwa shauku na tamaa akijua kuwa mambo yameanza.

Joram aliitazama saa yake, kisha akajistarehesha juu ya meza akisoma gazeti la Daily News ambalo lilikuwa na habari za kuchekesha chini ya kichwa cha habari: BAZILE MUUAJI HATARI YU HAI BADO

Joram aliisoma habari iliyofuata kama hadithi kisha akalitupa juu ya meza na kuendelea kusubiri, sigara zikiungua mdomoni mwake moja baada ya nyingine.

Kwame, kwa mara ya kwanza tangu alipoanza harakati zake alijikuta katika hali ya wasiwasi na mashaka makubwa. Kwa mbali, moyoni mwake, hofu ilikuwa iitishia kuutawala hasa kwa hisia zilizokuwa zikimnong'oneza kuwa mambo yameanza kumwendea mrama. Rohoni alipata wazo lililomshawishi kutoroka nchini mara moja, aende kokote duniani ambapo angeishi kwa starehe akitumia utajiri wake mkubwa. Wazo hilo alilipinga kwa kujikumbusha mara kadhaa kuwa hiyo dalili ya uoga wa kike.
Mashaka hayo yalikuwa yamemnyima usingizi usiku kucha tangu alipoarifiwa kuwa Joram Kiango alikuwa ametoweka baada ya kumshambulia mmoja kati ya watu aliowaamini waliokabidhiwa jukumu la kumlinda. Ingawa alikuwa na uhakikia kuwa Joram bado alikuwa hajui lolote la haja, lakini alimshakia sana hasa kwa kujua kuwa, iwapo angefika Kigamboni na kumsikia Komba angeweza kugundua mengi ya hatari. Kwa hofu hiyo, baada ya Joram kutoweka, ndipo akaamua Komba auawe mara moja bila kujali tena kupatikana kwa zile nyaraka za siri ambazo Komba alizipata kwa ajali na kuzing'ang'ania kama roho yake.
Mtu aliyetumwa kuua, Kaburu Vosgan Bon alikuwa mtu mwenye hakika na kazi yake. Kwame hakuwa na shaka naye, hasa kwa kukumbuka alivyokwisha fanya mauaji yote kwa ukamilifu chini ya kivuli cha yule kijana mtunzi, Bazile Ramadhani, kiasi cha polisi na taifa zimakuendelea kuamini kuwa muuaji si mwingine zaidi ya kijana huyo.
Hata hivyo, hofu ilianza kumshika baada ya kuona mapambazuko yakifika kabla ya kupewa taarifa juu ya kazi hiyo.Pengine alifanya makosa kuondoa makachero wote waliokuwa wakimlinda Kombaili Bon afanye kazi yake vyema? Yawezekana Bon amekwama kwa njia moja au nyingine? Hata hivyo, alifarijik kidogo baada ya kukumbuka kuwa pantone hufungwa saa fulani za usiku hadi alfajiri ya siku ya pili, hivyo yangewezekana baada ya kuua, Bon ameshin dwa kuvuka na angetokea kama kawaida kesho yake. Yawezekana? Bon ni mtu wa kushindwa kupata ngalawa au hata kuogelea hata alale mahala penye hatari kiasi hicho?
Ni hayo yalimtia Kwame mashaka, ingawa alipotoka asubuhi na kwenda kzini kwake alikuwa katika hali ya kawaida. Aliwasalimu wafanyakazi wengine na kumpita katibu wake mahsusi hadi ofisini mwake ambamo aliketi juu ya kiti akijiuliza lipi afanye katika hali kama hiyo. Kabla hajajua la kufanya katibu wake alimjia akiwa na barua mkononi yenye bahasha iliyobandikwa kijikaratasi cha 'express' yaani haraka. Aliipokea kwa mashaka na kuitazama kwa makini kabla hajagundua kuwa bahasha hiyo ni ile ile ambayo ilikuwa imehifadhi nyaraka za siri alizokuwa akizitafuta sana kutoka kwa Komba.
"Umeipata wapi hii?" alihoji hafla alipoikumbuka bahasha hiyo.
"Imeletwa na mtu wa posta asubuhi hii hii."
"Vizuri unaweza kwenda."
Binti huyo malipoondoka Kwame aliifungua haraka haraka na kutoa kadi ambayo iliyavuta macho yake kwa hofu kubwa .ilikuwa imeandikwa: Bwana Kwame, nadhani bado una ndoto za kuendelea na mipango yako michafu ya kuleta maafa katika nchi hii. Kama bado unayo, nakushauri uiache tangu dakika hii. Nimekwisha kufahamu wewe pamoja na wenzako wote. Ninachokushauri ni nyie wenyewe kujitoa serikalini na kuomba radhi. Iwapo itafika saa sita kabla hamjafanya hivyo nitachukua hatua mabzo zitakuonyesha kuwa sina mzaha hata chembe.
Kwame alisoma mara kadhaa kabla hajayaamini macho.Alipojikuta akiwajibika kuyaamini, alijisikia akitetemeka ghafla. Hakuwa na uwezo wa kueendelea kukanusha kuwa tayari siri imemfikia mtu hatari kama Joram. Hakujua ilitokea vipi hadi siri hiyo akaipata. Wala hakuwa na nafasi ya kujua hayo kwa sasa. Alichotaka sasa ni kupata ufumbuzi kabla ya saa sita, awe amemfanya Joram marehemu, siri irudi katika milki ya siri na harakati ziendelee kama zilivyopangwa.
Hilo halikuwa jukumu rahisi.
Hivyo aliinua simu na kuwapigia washirika wake ili kuwatane hapo ofisini haraka iwezekanavyo. Simu ya pili iliwaamuru wasaidizi wake wa idara ya mauaji wahakikishe kabla ya saa sita za mchanawawe wamempata Joram Kiango na kumuua. Alisistiza kuwa kazi hiyo lazima ifanyike haraka, mahala popote na kwa njia yoyote.
Baada ya simu hizo, alitulia kwa muda akiwaza wa uchungu uwezekeano wa kufa kwa Jorm bila ya kuwepo kwa muuaji aliyekubuhu-Bon, ambaye hadi sasa hakujulikana aliko. Yaweza kuwa amekamatwa na kuuawa na Joram? Alijiuliza. Pengine…
Mlango wake wa siri sakafuni ukatoa alama ya kudai kufunguliwa. Akabonyeza kidude ambacho kiliufungua. Mtu mmoja akapanda ngazi na kuingia chumbani. Wakasalimiana kimya kimya. Baada ya muda walifuata watu wengine kwa njia hiyo hiyo. Nyuso zao zilionyesha wasiwasi, hivyo walisalimiana bila uchangamfu wowote, huku kila mmoja akiketi juu ya kimojawapo ya viti vilivyomzunguka Kwame. Walipokamilika Kwame alimtahadharisha katibu wake kuwa asingependa kusumbuliwa na mtu yeyote. Kisha akawatazama wageni wake kwa macho yaliyoonyesha kuchanganyikiwa, hajui wapi aanzie kueleza.
"Nadhani tulikubaliana kuwa tusikutane tena katika hali kama hii hadi mambo yatakapoonyesha kuwa nchi iko mikononi mwetu," mmoja kati ya wageni hao alisema alipoona Kwame ameduwaa. Kwa hali hiyo nadhani Bwana Kwame angetueleza haraka kisa cha mwito huu ili tuondoke hapa." Wenzake wakatikisa vichwa kumuunga mkono.
"Ni juu ya waraka huu," Kwame alisema akiwapa ile kadi. Waliisoma na kisha kutazamana kwa hofu kubwa.
"Nilisema zamani kuwa singewezekana…" mmoja alisema ghafla.
"Hata mimi," alidakia mwingine.
"Kwa hiyo?" mwingine akaropoka.
"Tusubiri kitanzi," jibu lilitolewa.
Yakafuata mengi. Kila mmoja akisema hili na lile. Hawa wakifokeana, huyu akilalamika, yule akjilaumu na kadhalika. Kisha Kwame alifanikiwa kuwanyamazisha kwa kusema, "Jamani, tusiwe kama watoto. Nimekuiteni ili tupate jawabu la pamoja. Joram ni mtu mmoja tu, kijana mdogo sana, ambaye hwei kushinda kundi hili pamoja na jeshi letu la siri lililojengeka. Kisha kafanya ujinga wa kutuarifu kwanza na kutupa muda wa kutosha. Bado tuna saa mbili. Zinatosha kabisa kumpata Joram na kumweka kaburini.

"Labda humfahamu Joram, bwana Kwame," alidakia mwingine..
"Mimi namjua vizuri sana. ni kijana mdogo lakini anajua anachokifanya. Tusijidanganye…"
Kwame akamkatiza kwa hasira. "Uoga siyo dawa," aliongeza," sisi ni wanaume. Tunajua kabisa tusingeweza kutegemea utajiri mkubwa na vyeo vinono bila kutaabika kidogo. Bsuala la Joram ni tatizo dogo tu kati ya mengi yawezayo kutokea. Nilichotaka kupendekeza ni kuharakisha mambo yetu. Leo hii tukamilishe mipango, usiku mapinduzi yatokee, kesho sisi tulio hapa tuwe baraza lipya la mawaziri. Mnasemaje?"

“Joram jee?” alihoji mtu.
“Suala lake niachieni mimi. Hadi saa sita atakuwa safarini akielekea walikohamia babu zake. La muhimu ni sisi wenyewe. Tukubaliane moja. Tukitoka hapa kila mmoja akafanye jukumu lake haraka. Mnasemaje jamani? Angalieni hii ni nafasi yetu ya pekee ya kula nchi.”
Kabla hajajibiwa simu kutoka kwa katibu wake ilimfikia Kwame. Alii9nua chombo cha kusikilizia na kuunguruma ndani yake, “Nimesem sitaki usumbufu. Una nini kichwani wewe msichana?”
“Kumradhi mzee. Kuna mtu mwenye haja kubwa kukuona. Anasema jina lake ni Von.”
“Nani? Von! Mwambie aingie mara moja.”
Macho yake yalielekea mlangoni kumsubiri mgeni huyo. Aliingia taratibu bila haraka yoyote mikono mifukoni, macho yake yakimtazma kila mgeni kabla hayajamrudia Kwame ambaye kama wenzake wote alikuwa katika hali ya mshangao na mashaka mashaka. Mashaka ambayo yalitokana hasa na mgeni huyo kuwa katika sura ya Bazile Ramadhani, mtu ambaye alisadikiwa kuwa yu muuaji na aliyekuwa akitafutwa sana na kila mtu.
“Bon!” Kwame alifoka kwa Kiingereza. “Unawezaje kutebea hadharani mchana huu katika sura hiyo?”
“Usijali, siyo rahisi kujulikana.”
Sauti yake ilizidi kumtia Kwame mashaka. “Bon?” aliuliza tena.
“Ni wewe Bon! Ulikuwa wapi muda wote huu?”
Akajibiwa kwa tabasamu. Mikono ikatolewa mfukoni na kuelekea mdomoni ikiwa na sigara. Ilikuwa mikono ya mtu mweusi.
“Wewe sio Bon!” Kwame alifoka ghafla.
“Ndiyo.”
“Wewe ni nani?”
“Unataka kujua mimi ni nani? Ni rafiki yako mpenzi.
“Labda nitoe dude hili usoni unione vizuri.” Dude lilipotolewa kiufundi uso uliotulia mbele yao ukitabasamu ulikuwa wa Joram Kiango.
“Joram!” wote waliropoka kwa hofu na mshangao.
“Ndiye,” aliwajibu kwa dhihaka.
“Joram,” Kwame alifoka tena. Very well. Umejileta mwenyewe. Hutatoka humu ukiwa hai.”
Joram hakuonyesha kushtushwa na vitisho vya Kwame. Aliendelea kuivuta sigara yake, huku akiwatazama kwa makini. Nadhani tufahamiane vizuri ndugu zangu. Sipendi sana tabia ya kutumia majina ya bandia. Nani kati yenu anayejiita Top Koloto?” aliwahoji.
Alimuona mmoja akigutuka na wawili kumtazama mwezi wao jambo ambalo lilimfanya Joram amfahamu mara moja.
“Na Moto Matata?”
Wakazidi kugutuka. Joram akaangua kicheko. “Sikieni waheshimiwa,” akasema. “Hasa mheshimiwa Joe Kileo ambaye naamini u kiongozi wa kikundi hiki,” alikuwa akimtazama Kwame.
“Najua hii ni jumuia ya watu wenye njaa kali ya utajiri na kiu kubwa ya vyeo. Najua nyote hamtosheki na mlichonacho na kamwe hamtatosheka na lolote mtakalopata. Wengi wenu mmebahatika kuwemo katika madaraka makubwa, lakini hii ndiyo zwadi ya kwanza toka kwenu kwa nchi na wananchi; kupanga njama ambazo zimedhamiria kuleta umwagaji wa damu na kisha nchi iangukie mikononi mwenu. Iwe kama shamba lenu, wananchi wote wakiwa watumwa badala ya watu huru katika nchi huru. Waheshimiwa,” alipunguza hasira kutoka katika hali ya hasira na na kuwa ya huruma zaidi.
“Hamwoni aibu kwa uchafu wa vitendo vyenu?”
Hutuba yake ilikuwa imewafanya wote waduwae.walipopata nafasi ya kujikumbuka baada ya kuulizwa swali hilo, walitazamana kwa kutojua la kujibu. Kisha Kwame akafoka ghafla.
“Tusibabaishwe. Tusibabaishwe na kijana huyu mwenye hila kama knyonga.” Akainuka na kusogea mbele hatua moja akiendelea kusema, “Dakika chache kabla hajaingia hapa tulikuwa tukijadili kifo chake. Hatujabadili utaratibu huo. Atakuwa marehemu muda mfupi ujao.” Akageuza sauti kuwa amri. “Haya wote nendeni mkaendelee na mopango, huyu niachieni mimi.”
Umati ukaanza kuinuka. Joram akagutuka kidogo. Kama kawaida yake kujileta kwake haikuwa moja kati ya njia zake za kuwadhihaki adui zake tu. La hasha, nia ilikuwa ni kupata hakika juu ya kuhusika kwa Kwame ktika mpango ule wa mapinduzi – jambo ambalo tayari alikuwa amelipata – pamoja na kutaka kuwafahamu wote wengine ambao walikuwemo katika njama hizo. Kwani baada ya kutuma warakaule aliamini Kwame asingesita kuita wenzi wakeili wajadiliane kabla haujawadia muda aliotishia. Na ndipo akaingia ofisini huko mapema zaidi ili awafumanie kama alivyowafumania. Hakuwa amekuja mikono mitupu. Silaha zake muhimu zote zilikuwa tayari katika sehemu zake za siri. Zaidi kamera yake ndogo ya siri ilikuwa ikiendelea kupiga picha za umati huo hali kinasa sauti kkiendelea kunasa yote yaliyokuwa yakisemwa. Hivyo, ushujaa wa Kwame kiasi ulimtisha. Alihitaji muda zaidi ilia pate ushahidi zaidi kisha aondoke na kupata msaada wa polisi kuwanasa. Maadamu hakuwa tayri kwa hilo, aliona heri abadili mbinu na kuwaambia.
“Bado. Msiondoke kabla. Hamjafahamu kwa nini niko hapa na nije peke yangu badala ya kuongozana na polisi ambao wangewatieni pingu kesho muwe vizimbani na kesho kutwa mahabusu mkisubiri kitanzi.”
“Hatuna muda wa kukusikia…” Kwame alizidi kufoka. “Umejileta mbele ya mauti na hutatoka kwa miguu yako mwenyewe. Haya wote ondokeni mkaendelee na mipango yetu. Fanyeni haraka.”
“Msiondoke,” Joram akaamuru. “Angalieni, huyu anataka kuwaponza. Nilikuwa na nia njema kwenu nyote, nikizingatia kuwa nyote mna hadhi serikalini kiasi kuwa endapo mambo haya yatajulikana itakuwa aibu mno kwenu.” Alipoona wametulia kumsikiliza, aliongeza, “Kwa hali hiyo, nia ya kuja kwangu ilikuwa kuwashaurini kwa amani muache ndoto hizo. Na endapo mmedhamiria, mimi nipeni chochote ili nikae kimya. Milioni moja zinanitosha. Najua mnazo, au siyo Kwame?

Kwame alianza kubadilika, uso ukichukiza na macho kutisha, “Una wazimu,” alinguruma. “Huna utakachopata zaidi ya zawadi ya kifo. Nazifahamu sana hila zako za kitoto. Kwangu umekwama bwana mdogo.”
Joram akatabasamu, “Kwa hiyo uko tayari niipeleke siri polisi? Yuko mtu ambaye nimempa jukumu la kupeleka mambo haya polizi na kumtaka awaambie waje hapa mara moja endapo dakika kumi zaidi zitapita kabla sijamfikia hapo anaponisubiri.”
Kwa mshangao, Joram alimwona Kwame akiangua kicheko. “Polisi? Watafanya nini? Najua huo ni uongo lakini hata wakija hawatagundu lolote. Watakachofanya ni kuizoa maiti yako. Pindi watakaposubiri kesho kupata ushahidi, nchi itakuwa mikononi mwetu.” Kwame akawageukia wenzake. “Hamjaondoka tu? Tafadhalini ondokeni na mkatimize wajibu wenu bila hofu.”
Hayo Joram hakuyategemea. Lakini hakuduwaa kuwaza. “Hakuna atakayeondoka,” alifoka ghafla. Walipomtazama walijikuta wakitazamana na bastola yake ambayo aliishika kishujaa, “Wote mtaketi chini na kuwasubiri polisi.”
Wenzi wa Kwame waliduwaa, hata hivyo walipata moyo walipotazama na kuona naye kashika bastola iliyokuwa ikimwelekea Joram huku akicheka na kusema, “Kinda anapoamua kucheza na chatu asitegemee fadhila. Haya nendeni mmoja mmoja, huyu niachieni mimi.”
“Atakayethubutu kuondoka, risasi yangu halali yake,” Joram alionya.
“Msiogope vitisho vyake,” Kwame aliongeza. “Kama mnavyomfahamu, yeye ni mtundu tu, lakini yu mwoga mno wa kuua. Nendeni.”
“Aondoke mtu…” Joram alifoka tena. Lakini sauti yake ilikatizwa na king’ora chenye sauti kali ambacho kililia ghafla mezani mwa Kwame. Kikafuatwa na sauti ya watu waliokuwa wakisema haraka.

“Inspekta Kombora hapa. Kikosi cha kumi na mbili…”
… “Kombora? Sikieni, kuna mauaji yanafanyika katika ofisi ya Snow Fund. Nendeni haraka mtawapata wauaji.”
“Wapi? Snow… haya… tunaondoka mara moja…”
Wote wakazidi kuchanganyikiwa. Joram aliwatazama kwa kebehi. Lakini, alipomgeukia Kwame, aliambulia kuona akibonyeza kidude fulani na chumba kumezwa na giza Ghafla. Mlio wa bastola ukasikika. Joram alijtupa sakafuni na kutambaa kutoka alipokuwa. Mra akasikia harufu ya aina fulani ya marashi ikimfikia ghafla. Papo hapo usingizi mzito ukammeza na kumteka. Kama ndoto, alisikia ubishi mkali ukiendelea kwa sauti za wasiwasi, huyu akisema hili na huyu lile.
“Tumuue.”
“Nasema hapana. Mwacheni alale. Anajitia kujua. Hivyo atafurahi sana atakapoamka baada ya saa ishirini nan ne na kuona bendera mpya ikipepea.”
“Tumuue…”
“Nasema hapana.”
Kisha alisikia hodi kwa mbali. “Hodi… fungua…” huku mikono inayotetemeka ikijatribu kumbeba na kushindwa. “Polisi… funguia…” ikaendelea kusikika. Joram hakusikia lolote zaidi.

Bazile Ramadhani aliibuka kutoka katika kitu kama ndoto au usingizi mzito ambao ulikuwa umemmeza kwa muda mrefu ambao hakuweza kukadiria. Usingizi ambao ulikuwa umemwanza kwa namna isiyoelezeka tangu usiku wa siku ile ambayo alimwendea Kitenge ofisini kwake kumpa maneno ya hasira kwa ajili ya muswada wake alioupenda kuliko yote. Kumpa yale maneno makali ambayo hata hakumbuki wapi alipata uwezo wa kuyaropoka.
Alipofika nyumbani aliendelea na shughuli zake kama kawaida. Usiku alipanda kitandani na kujilaza. Usingizi uliomchukua ulikuwa na tofauti kubwa na ule aliouzoea. Ulikuwa mzito mno. Ndoto zake zikiwa kama jinamizi. Mara, alihisi kubebwa na kupakiwa kama gunia. Mara, alihisi akilazwa juu ya meza kubwa huku uso wake ukipimwa na jitu lenye madevu. Mara, alihisi kusikia watu wakipanga au kujadili kifo na mazishi yake na mengi mengine ya kutisha.
Hakuwa na uwezop wa kuamka wala kufumbua macho isipokuwa leo baada ya kuhisi na kisha kuona mtu akimdunga sindano. Alijikuta akiwa katika chumba ambacho hakupata kukiona maishani.
“Ni.. nini? Niko wapi?” alihoji kidhaifu.
Mtu aliyekuwa akimhudumia alimtazama kwa macho makali na kumwamuru ainuke, “Pita hapa uende huko,” aliambiwa.
“Wapi?” Bazile alihoji kwa udhaifu huku akijikongoja kuinuka.
“Fanya haraka!” alifokewa.
“Kama kondoo aliinuka na kufuata mlango alikoelekezwa. Baada ya kupita milango na vyumba kadhaa, aliamriwa kusimama.
“Geuka huku.”
Alipogeuka alikutana na risasi ya bastola isiyo na mlio ambayo ilimfanya ausahau udhaifu wake na kupaa juu. Alipotua chini tena alikuwa chali, damu nzito zikimvuja huku akiwa tena kamezwa na na aina nyingine ya usingizi ambao haukuwa na ndoto wala hisia.

“Fungua,” Kombora alifoka tena. “Polisi hapa,” aliongeza akiitazama saa yake. Dakika tatu zilikuwa zimepita tangu alipowasili hapo na kuwakuta askari wa doria wakiendelea kuugonga mlango wa ofisi ya Kwame
“Mnadhani kuna nini kinachofanyika humo ndani?” aliwahijo.
“Hatujui mzee. Hatusikii chochote.”
“Msichana anayekaa hapa mmemkuta?”
“Hatukumkuta.”
“Okay, tutavunja mlango. Nitaita kwa mara ya mwisho… FUNGUA!” akafoka.
“Mara mlango ukafunguka polepole. Kwame alitokeza akitetemeka mwili mzima isipokuwa macho yake tu. Kombora hakuyaona kuwa na dalili yoyote ya hofu. Aliwatazama kwa mshangao na shukrani.
“Karibu,” aliwaambia akiwapisha mlangoni.
Walipoingia macho yao yalidakwa na mizoga ya binadamu wawili waliolala juu ya sakafu. Mmoja akiwa kalala chali bastola mkononi. Wa pili ambaye ilikuwa dhahiri alikuwa marehemu alikuwa chali, sura yake ikitazama angani. Kombora na wasaidizi wake sita walimtazama marehemu huyo mara moja na kisha kutazamana.

5

“Fungua,” Kombora alifoka tena. “Polisi hapa,” aliongeza akiitazama saa yake. Dakika tatu zilikuwa zimepita tangu alipowasili hapo na kuwakuta askari wa doria wakiendelea kuugonga mlango wa ofisi ya Kwame
“Mnadhani kuna nini kinachofanyika humo ndani?” aliwahijo.
“Hatujui mzee. Hatusikii chochote.”
“Msichana anayekaa hapa mmemkuta?”

“Hatukumkuta.”
“Okay, tutavunja mlango. Nitaita kwa mara ya mwisho… FUNGUA!” akafoka.
“Mara mlango ukafunguka polepole. Kwame alitokeza akitetemeka mwili mzima isipokuwa macho yake tu. Kombora hakuyaona kuwa na dalili yoyote ya hofu. Aliwatazama kwa mshangao na shukrani.
“Karibu,” aliwaambia akiwapisha mlangoni.
Walipoingia macho yao yalidakwa na mizoga ya binadamu wawili waliolala juu ya sakafu. Mmoja akiwa kalala chali bastola mkononi. Wa pili ambaye ilikuwa dhahiri alikuwa marehemu alikuwa chali, sura yake ikitazama angani. Kombora na wasaidizi wake sita walimtazama marehemu huyo mara moja na kisha kutazamana.

“Bazile Ramadhani!” mmoja wao akajaliwa kutamka.
“Ni Bazile siyo? Ule muuaji anayeua ovyo? Basi Mola asifiwe kwa kufa kwake. Angeweza kuniua au kumuua huyo kijana hapo,” alitamka Kwame kwa namna ya furaha.
“Kombora alimtazama kijana huyo na kumwona akipumua polepole. Akainama na kumgeuza uso. Mara alijikuta kashtuka akiwageukia wenzake kwa macho ya kutokuamini.
“Kati yenu hakuna anayemfahamu mtu huyu?” aliwahoji.
Watu hao walimtazama mtu huyo na kumrudushia Kombora macho ya mshangao. “Huyu si Joram Kiango mzee?” mmoja wao alijibu.
“Joram Kiango!” Kwame alifoka tena. “Yule kijna wa C.I.D? La haula! Angeweza kufa mbele ya macho yangu kama asingeweza kutumia vyema bastola yake.”
“Joram sio C.I.D,” Kwame aliambiwa. “ Ni kijana mwenye ofisi yake ya upelelezi, ambaye amefanya mengi kulisaidia taifa.” Kombora alisita, kisha akamgeukia Kwame, “Ndiyo ndugu Kwame. Nadhani waweza kutufunua macho na kutueleza kinachotokea katika ofisi hii.”
Kwame akiwa katika hali ile ile ya kuchanganyikiwa ingawa macho yake yakiwa maangavukinyume cha hali yake, alisema kwa sauti ya utulivu, “Sidhani kama kuna mengi ya kueleza bwana inspekta. Nilikuwa nikiendelea na shughuli zangu kama kawaida, dakika chache tu zilizopita, mara akatokea bwana huyo mmnayemwita Joram na kuingia huku mbio. Kabla sijamuuliza lolote marehemu huyo naye akaingia. Wakavaana na kupigana kwa muda. Joram alipoelekea kuzidiwa aliitoa bastola na kuifyatua. Muda mfupi nanyi mnaingia.” Alipoona Kombora hajaridhika aliongeza, “Ni hayo tu bwana Kombora.”
“Hayo tu? Hujasema lolote juu ya simu. Umepiga baada au kabla? Kombora alihoji.
“Simu! Simu ipi?”
“Simu iliyotuleta hapa.”
“Siifahamu simu hiyo. Yaani mmepata simu? Basi bila shaka hyo ni katibu wangu. Nadhani aliona pindi wakiingia ndipo akakupigia.
“Yuko wapi?”
“Sijamwona tangu alipoanza haya. Nadhani mara tu baada ya simu hiyo kukufikia amekimbia. Nakuambia bwana ilikuwa hali ya kutisha kweli. Nilichanganyikiwa…”

Kombora akamkatiza kwa kuuliza, “ Wakati wote wa mapambano wewe hukuweza kufanya lolote? Umeshindwa walao kuinua simu kama alivyofanya karani wako?”
Haikuwa hali ya kawaida inspekta. Nakuambia nilichanganyikiwa…”
Huonekani kama mtu uliyechanganyiokiwa kiasi hicho! Kombora aliwaza, nusura ayatamke. Wala hakuona kama Kwame alikuwa mtu mwenye asili ya kushtushwa na jambo lolote kiasi cha kushindwa kujua la kufanya. Hata hivyo, hayo hayakuwa na nafasikubwa katika fikra za Kombora. Alikufa na mengi kichwani.
Sana alilitazama suala la mauaji hatimaye kifo cha muuaji na kuhisi tamati yake haimridhishi kama alivyotegemea. Hakuna alichopenda zaidi ya kifo cha Bazile. Na angependa zaidi kama fursa ya kukifumua chake kwa risasi angekuwa kaipata yeye. Lakini bado angeridhika zaidi kama tukio hilo lingetukia kwa namna nyingine. Namna iliyoridhisha zaidi.
Jana tu alikuwa kaanza kupata mawazo mapya juu ya mauaji hayo. Ilikuwa baada ya kuufuata ushauri wa msaidizi wake na kuikusanya pamoja akili yake katika kulishughulikia suala hilo. Alikuwa amemfikiria Bazile Ramadhani kama alivyo: kijana mwandishi chipukizi asiye na mengi ya ajabu, vipi aondokee kuwa hodari wa kuua kiasi cha kumkabili askari mwenye silaha na kumjeruhi? Zaidi, vipia askari huyo baada ya kuhojiwa sana bado anang’ang’ania kuwa alipoteza fahamu zake pindi akifanyiwa ukatili? Ingawa askari huyo alithibitisha kuwa mtu huyo alikuwa Bazile, bado Kombora alisisitiza hata alama za vidole zikachukuliwa kutoka katia uso huo ili zilinganishwe na alama nyingine. Lakini matokeo yalikuwa ya kutatanisha zaidi. Hazikupatikana alama zozote katika sehemu zote ambazo askari huyo alistahili kuwa ameguswa na Bazile. Yaelekea zilifutwa kwa uangalifu na alikuwa kavaa glovu. Hilo lilimshangaza Kombora. Kwa nini afiche alama hizo naye alikuwa akijitangaza mara kwa mara kwa simu? Mara Kombora akawa na mawazo mapya juu ya mauaji hayo. Alihisi kuwa kuna jambo zaidi ya wazimu wa mwandishi huyu. Vinginevyo, Kombora hakuona vipi kijana huyo angeendelea kutaabisha jiji huku akiepuka kila kikwazo ambacho polisi walijaribu kumwekea.
Hayo yalikuwa mawazo tu. Lakini yaligeuka kuwa mashaka. Mashaka ambayo yalijiimarisha kichwani mwake hata akiziruhusu fikra zake kutambaa huku na huko akitafuta uwezekano wa Bazile kushirikiana na watu wengine. Kwa nini? Ni ipi sababu ya mauaji hayo? Kuna uhusiano gani baina ya marehemu wote? Mara akapata wazo ambalo lilimshtua sana. yawezekana lipo jambazi au majambazi ambayo yalikuwa yakiitumia sura ya kivuli cha Bazile? Alijiuliza.
Yawezekana kabisa katika dunia hii iliyopiga hatua ndefu katika ndefu katika sayansi na teknolojia, lolote lawez kufanyika. Bazile aweza kuwa kofia tu ambayo imefunika mengi.
Mengi? Yepi? Kombora akajiuliza kwa hofu. Mara moja akamwita msaidizi wake na kumtaka achukue jukumu la haraka kujaribu kupata habari, mienendo, vitendo na uhusiano baina ya marehemu wote. Alisisitiza kuwa kazi hiyo ni muhimu na ipewe umuhimu zaidi ya lile jukumu la kumsaka Bazile.
Pindi Kombora akiwa ofisini kuisubiri taarifa hiyo ndipo ikamfikia simu hii ambayo ilimwita hadi hapa na kumkuta Bazile akiwa marehemu. Ni Bazile yuleyule. Si sura ya bandia wala mtu mwingine zaidi yake. Na inasemekana kafa pindi akikusudia kuua tena. Kumuua Joram Kiango. Joram ambaye mchango wake ni mkubwa mno katika harakati za kijambazi. Yawezekana kuwa Joram pia alikuwa akimsaka muuaji huyu? Na yawezekana huu ukawa mwisho wa kisa hiki cha kikatili? Hakutakuwepo na kusimama mahakamani kumsikia Bazile akikiri au kukanusha mauaji haya.?
Kombora angeweza kuwaza mengi zaidi. Lakini hakuiona sababu yoyote ya kuendelea kuusumbua ubongo wake pindi Joram alikuwa hai. Baada ya sindano moja tu ya daktari atazinduka na kutoa maelezo kamili.
“Well!”
“Well?” Kwame alihoji.
Kombora akagundua kuwa alikuwa ameropoka. Akamtazama Kwame kwa macho yenye maswali mengi lakini hakuuliza chochote.

Na awaze apendavyo! Kwame alijinong'oneza kimoyomoyo. Awaze anavyotaka. Asingeweza kuutengua ushahidi aliouandaa hata kama ni askari mwenye shahada ngapi.
Hadithi nzuri ilioje. Hadithi isiyopingika kabisa…. Kwame aliendelea kuwaza. Bazile Ramadhani, mwandishi, kapata wazimu. Kamuua mchapishaji wake. Damu ikampanda kichwani, akachemka kuua ovyo. Mara kupambana na Joram Kiango. Ramadhani kazidiwa na kuuawa na Joram. Polisi wenyewe ni mashahidi. Wamemkuta muuaji anakufa. Nani aikatae hadithi. Na ataikataa kwa misingi ipi pindi hakuna anayejua ukweli?

Ukweli ulikuwa siri yake Kwame na wachache ambao hawawezi kufunua midomo yao na kuitoa. Hakuna mwingine anayefahamu kuwa muuaji si Bazile ila hilo kundi lake ambalo dakika chache tu limetoweka na kumwachia yeye, Kwame fursa ya kutia risasi katika mwili wa Bazile. Wala hakuna atakayefahamu kuwa mauaji ya Kitenge, mchapishaji, yalipangwa ili kuwapotezea askari lengo la kuwafanya polisi wazidi kuamini kuwa muuaji ni Bazile Ramadhani. Na kwamba Fambo Wamangi na Jugeni Kawamba walikuwa wameuawa bila hatia yoyote. Kosa lao kubwa ilikuwa kusafiri katika ndege moja na Kwame alipotoka visiwani kukamilisha mipango ya kuuza kisiwa. Ilionekana kuwa wao wangeweza kuwa daraja la kuwafanya wapelelezi kumfikia Kwame au walao kushuku jambo endapo kifo cha Dismas Komba kingetukia.
Ni Komba tu aliyetakwa. Na ni yeye aliyekuwa na hatia ingawa yeye pia alipata hatia hiyo kwa ajali. Akiwa uwanja wa ndege baada ya kutua kutoka Zanzibar, alikosea na kuchukua suitcase ya Kwame badala ya yake. Alipofika nyumbani aliifungua na kukutana na kile ambacho macho yake hayakutakiwa kuona. Kabla hajajua la kufanya kwa siri hiyo, wafuasi walishapeleleza anakoishi na kumwandama kwa hadhari huku wakimtesa kwa mbinu aina aina ili arejeshe bahashahiyo yenye siri. Naye akijua mara tu aitoapo watamuua ndipo akaing'ang'ania kwa udi na uvumba. Jambo ambalo halikuyaokoa maisha yake, kwani Bon alikuwa ametimiza wajibu wake.
Nani atayajua yote hayo? Kwame alijiuliza kwa kiburi. Zaidi, nani atayajua katika muda mfupi uliosalia?
Huyu askari mkuu hapa haonekani mjinga, lakini hana nafasi ya kuunga vipande vyote vya matukio na kupata pande zima la kisa na ushahidi wake wakati unaofaa. Joram? Joram yuko usingizini na ataendelea kulala hadi kesho. Atakapoamka kujua hakutamsaidia yeye wala mtu yeyote, itakuwa….
Kwame alilazimika kusita alipomsikia Kombora akitoa amri ambayo hakuitegemea.
"Unasemaje inspekta? Apelekwe Muhimbili? Ya nini kusumbuka. Nimekwisha mpigia daktari wa kampuni yangu aje mara moja kumpa huduma ya kwanza," Kwame alisema.
"Daktari wako?" Kombora akauliza akitazama, "Umempigia lini simu hiyo?"
Muda mfupi kabla yenu."
"Nadhani ulisema kuwa hujapiga simu yoyote."
"Nilipiga. Atafika wakati wowote, kama una msaada wa haja bwana inspekta nadhani msaada huo ungekuwa kuiondoa maiti hii mbele yangu. Ofisi hii si jumba la maiti. Suala la Joram niachie mimi. Ameyaokoa maisha yangu. Ningeweza kufa."
"Joram hatatibiwa hapa," sauti kali ya kike ilitamka ghafla. Wote wakageuka kumtazama msemaji. Alikuwa msichana mwenye umo na sura nzuri ambaye aliingia ghafla baada ya kubishana sana na askari wa mlangoni.
Kombora alimfahamu kwa sura na jina. "Neema!" akaita.
"Ni mimi inspekta. Ni mimi niliyekupigia simu kama nilivyoelekezwa na Joram," akaongeza akiinama kumgusa Joram ambaye alilala kwa utulivu mkubwa. "Inspekta, Joram hawezi kutibiwa hapa. Tena ningeomba apelekwe Muhimbili mapema iwezekanavyo."
"Kwa nini? Daktari wangui…" Kwame alijaribu kusema. Alikatizwa na Kombora ambaye alifoka kwa Kiingereza.
"Shut up!" akawageukia wasaidizi wake na kuwaamuru wamchukue Joram mara moja.

Fahamu zilipomrejea, Joram alifumbua macho polepole na kuyafumba mara moja kwa kushindwa kustahimilinuru ambayo aliona kali mno. Alipoyafumbua tena, alifaulu kutazama pande zote. Kitu cha kwanza alichokiona ilikuwa kofia ya kipolisi, ilikuwa juu ya kichwa cha mtu mwenye mavazi ya kipolisi aliyesimama kando akimtazama. Huyo alikuwa mmoja kati ya polisi wane waliokuwa chumbani humo silaha mikononi. Kisha, Joram aliweza kuwaona daktari na nesi ambao walikuwa wakimhudumia.
Baada ya kutazama sana aligundua kuwa alikuwa katika chumba maalumu katika hospitali ya Muhimbili. Joram akiwa mtu asiye na mazoea ya kufika hospitali kwa miaka, hilo lilimshangaza sana.
"Nini kinatokea? Niko hapa kwa nini?" akauliza.
"Pole sana bwana Kiango," daktari alimjibu. "Pumzika kidogo umsubiri inspekta Kombora ambaye yuko nje akisubiri kuzungumza nawe. Kabla hajafika huruhusiwi kuzungumza lolote."
"Kwa nini?" Joram alihoji. Lakini mara akarudiwa na matukio yote ya muda mfupi uliopita. Akakumbuka kuwa alikuwa mbele ya umati wa wauaji wenye dhamira ya kumwaga damu na kupoteza uhuru wa wananchi usiku wa leo. Akakumbuka pia kuwa katika juhudi zake za kuwazuia ndipo alinusa harufu ambayo bila shaka ilitoka katika mitambo ya Kwame, ikamtia usingizi. Baada ya hapo, hakusikia lolote isipokuwa hisia tu, kama ndoto alisikia majadiliano ya haraka haraka kwa sauti za hofu baina ya watu hao waliochanganyikiwa. Yaliyofuata hakuyafahamu.
"Ndiyo!" akafoka ghafla akiitazam saa yake na kuona ikikaribia saa nane mchana. "Yuko wapi Kombora?" akawageukia askari, "Mwiteni haraka."
Haikuwepo haja ya kumwita. Wakatri huo huo, Kombora aliingia. Baada ya kupokea saluti kutoka kwa askari hao akawataka wasubiri nje. Daktari na msaidizi wake pia waliombwa kutoka.
"Ndiyo bwana Joram. Kwanza nikupe pole kwa yote yaliyokupata. Kisha nitakuomba unifafanulie kwa niaba ya jeshi zima la polisi kitu gani kinachotokea," alisema akiketi kitandani.
"Kitu kinachotokea? Nadhani sijakuelewa vizuri inspekta," Joram alimjibu. Alipoona upinzani katika macho ya Kombora aliongeza haraka, "Sivyo. Nina maana kuwa nitapenda kufahamu yepi unafahamu na yepi yamenifanya niwe hapa Muhimbili chini ya ulinzi mkali wa polisi badala ya kuwa mahala fulani huko ahera au peponi. Ilikuaje hata ukafaulu kuniokoa.
"Yametokea mengi zaidi ya kukuokoa Joram," Kombora alisema akitoa sigara na kumpa Joram moja. "Mengi mno. Nikianza mwanzo ni kwamba nilipokea simu kutoka kwa msichana wako, kama alivyodai yeye, kuwa mtu anauawa katika ofisi ya Kwame. Nikaenda mara moja na kukuta wewe umezirai na bastola ambayo imemuua yule mtu tuliyekuwa tukimsaka kama kunguni, Bazile Ramadhani."

Bazile amekufa! Umemwona!…" Joram alihoji kwa mshangao.
"Ndiyo. Kwani hukumuua wewe?"
"Mimi!"
Kombora akatikisa kichwa na kuendelea, "Hilo ni lingine katika mengi ya kutatanisha katika mkasa huu. Lingine ni matokeo yaliyotokea pindi tukikuleta hapa. Ulikuwa kwenye gari aina ya Landrover iliyokuwa ikiendeshwa na askari wangu. Msichana wako alikuwa katika hiyo gari pia.

Gari hiyo ilipokuwa imalize barabara ya Morogoro iingie mtaa wa Umoja wa Mataifa iligongwa makusudi kabisa na gari nyingine aina ya Landrover. Wewe kwa kuwa ulikuwa umelazwa kwenye kiti hukudhurika. Dereva wangu ameumia kidogo. Lakini msichana wako…."
"Neema! Tafadhali Inspekta! Usiniambie kuwa Neema amekufa!" Joram alidakia.
"Hakufa, ila…"
"Ila?"
"Ametoweka."
"metoweka? Sijakuelewa Inspekta."
"Kwa kweli ni tukio la kutatanisha. Mimi nimefika katika eneo la dakika nne tu baada. Nimekuta watu wakishughulika. Nikaambiwa kuwa teksi moja imejitolea kumchukua Neema na dereva wa gari iliyogonga ambaye hakuumia sana. kwamba imewaleta hapa hospitali. Lakini tumeshakagua hospitali nzima bila dalili yoyote ya Neema wala huyo dereva.
"Jambo la kutisha zaidi ni barua hii fupi ambayo imeokotwa katika chumba hiki pindi ukitibiwa. Imeandikwa jina lako."
Joram akaipokea na kuifunua. Iliandikwa kwa mashine, wino mwekundu ikisema;

Mpendwa Joram,
Nakuonya usifunue mdomo kwa yeyote kusema lolote. Vinginevyo kesho utaamka hapo kitandani na maiti ya mpenzi wako.
Rafikio Joe Kileo.

Baada ya kuisoma Joram alimgeukia Kombora. Ingawa alijitahidi kuficha mshtuko alioupata kwa habari hiyo, hakufanikiwa kumfanya Inspekta Kombora asihisi mteremo katika sauti yake aliposema, "Endelea mzee."
"Nadhani sina zaidi," Kombora alimjibu. "Labda naweza kusema kuwa nina mashaka na mtu anayeitwa Kwame. Vitendo na maneno yake vinaonyesha kuwa anajua mengi kuhusu mkasa huu. Kifo cha Bazile bado kinatatanisha. Barua hiyo kwako inaongeza uzito katika mashaka yangu.kwa ajili hiyo, nimewapa wapelelezi kadhaa kazi ya kuchunguza mienendo ya Kwame na kuniletea taarifa mara kwa mara. Inashangaza ripoti zote zinaposema yuko katika hali ya kawaida na anaendelea n shughuli zake kama kawaida baada ya kutoka mara moja kwenda Salamander ambapo amepata kahawa na kuzungumza na watu wachache juu ya 'mkasa' katika ofisi yake. Sasa hivi inasemekana yuko ofisini mwake kama kawaida ingawa katibu wake hajapatikana."
Hayo yalizidi kumfumbua Joram macho. Akaipata picha kamili ya yote yaliyokuwa yametukia. Akaelewa kuwa baada ya jaribio la Kwame la kumuua kwa gari kukwama, aliona hatari ya Joram kueleza polisi ukweli na ndipo akamteka Neema na kuleta waraka huu ili kumtisha asiendelee na mipango yake hatari.
"Hivyo ndugu Joram," Kombora alikuwa akiendelea kueleza, "Kadri n inavyokufahamu, natumaini hutakuwa tayari kutii waraka huo ambao unakusudia kuwaweka mapenzi mbele ya jambo la hatari kama hili. Utakkuwa mwanamume kama ulivyo na kueleza kwangu yote unayofahamu ili tushirikiane kuyaokoa maisha ya mpenzi wako pamoja na…"
"Neema si mpenzi wangu," Joram alitamani kufoka hivyo, lakini alijizzuia. Ingemchukua muda mrefu mno kumfanya Kombora na watu wengine waelewe kuwa uhusiano wake na Neema ulikuwa wa kikazi tu. Muda ambao hakuwa nao kabisa. Kwa sasa, alifikiria jinsi Kwame alivyokuwa akiendelea na mipango yake bila hofu yoyote akiamini kuwa iwapo majasusi wake walifaulu kuleta barua hiyo kwa siri wasingeshindwa kumuua. Bila shaka walidharau wakijua kuwa muda waliokuwa nao ungetosha kuwawezesha kutawala nchi. Aliwaza pia kuwa huenda wameacha vifaa vyao ambavyo sasa vinapeperusha kila neno linalotamkwa chumbani humu hadi masikioni mwa Kwame kama alivyowafanyia polisi. Hivyo, Joram alimkatiza Kombora kwa kumjibu akisema , "siwezi kutishwa na kijibarua kama hicho Inspekta. Wewe wanifahamu vyema. Kwa bahati mbaya sifahamu lolote kinyume cha ukweli ulivyo."
"Ukweli upi?" Kombora alihoji kwa mshangao. "Unataka kusema kuwa ni wewe uliyemuua Bazile?"
"Oh, Yes," Joram alidakia.
"Hatukufahamu kama muuaji Jopram."
"Kwa hiyo tangu leo mmenifahamu kuwa sishindi kutumia bastola yangu kwa muuaji kama yule. Kama unataka kunitia kizimbani kwa kosa hili niambie."
Kombora akaonekana kuchanganyikiwa, "Acha uoga Joram. Mapenzi…"
"Tafadhali Inspekta. Suala la mapenzi yangu na Neema halikuhusu," alijitia mkali.
Wakati huo mikono ya Joram ilitambaa polepole mwilini mwake akipapasa alikoficha silaha zake za siri, kamera ndogo pamoja na kanda ya kunasia sauti. Akatabasamu kwa furaha kuona vitu hivyo pamoja na misukosuko yote, vilikuwa salama katika mifuko yake ya siri.
Akavitoa na kumpa Kombora huku akimfanyia ishara ya kutokusema lolote. Kombora alivitazama kwa mshangao, lakini akavifahamu mara moja na kuvidaka kwa furaha.
"Kwa hivyo bwana Kombora maadamu nimepata nafuu naomba uniruhusu nijipumzishe. Kama maswali nitayajibu kesho. Siwezi kuihama nchi usiku mmoja."
Kombora , akiwa kamwelewa Joram, alijitia kubisha kidogo.
"Mpenzi wako?"
"Suala lake niachie mwenyewe. Kesho nitampata."
"Sikujua kuwa u mwoga hivyo Joram. Lakini sina budi kukwambia kwamba tuna mashaka. Polisi itafanya kila njia kupata ukweli. Nawe utahesabiwa kuwa mwenye hatia kwa kuficha habari."
"Kesho Inspekta, tafadhali," Joram alijibu akiinuka na kutoka. Ndiyo kwanza akagundua alivyodhoofika. Mwendo wake ulikuwa wa kujikongoja hadi nje ya chumba ambapo alisimama kwa muda akikusnya nguvu.

"Umesikia?" Kwame alitabasamu, macho yake ambayo dakika chache nyuma yalimtazama mwezi wake kwa hasira ya kutisha kidoo yalikuwa yameisahau hasira hiyo, ingawa yaliendelea kutoa nuru ya kuogofya. "Umesikia mwenyewe Joram akikiri kuwa amemuua Bazile. Hawezi kuwa mjinga na kukubali kumpoteza msichana mzuri kama yule kwa ajili ya mabadiliko tu ya serikali. Atakachoofanya ni kuwazungusha hadi kesho. Na kesho hiyo…"
"Simwamini hata chembe kijana yule. Ana akili za ajabuajabu," mwezi wake alikanusha. "Aweza kuwa sasa hivi anabuni jambo lingine la kututia mikononi."
Kwame akaukunja uso wake, "Uoga wa aina hiyo siupendi kabisa bwana Matata," alifoka. "Kama huniamini wala kuwaamini wataalamu, matajiri na watu mashuhuri walioandaa mipango yote hii, tamka mara moja ili tukuondoe katika mipango yetu. Na nafikiri sina haja ya kukumbusha adhabu ya mtu anayevunja kiapo cha hatari kama hiki."

“Siyo hivyo bwana Kileo. Ila…”
“Ila nini?” alifoka tena. Kisha akaishusha sauti yake akisema, “Joram yumo mikononi mwetu. I kwa kuwa tunaye msichana wake, bali pia makachero kadhaa wako nyuma yake. Wakati wowote watakapoarifu kuwa anaelekea kwenda kinyume cha matakwa yangu atakula risasi. Kumwachia hadi sasa ni pamoja na hamu yangu ya kutaka kuona hayo machachari yake hapo kesho wakati tutakapokuwa Ikulu, nchi itakapokuwa chini ya miguu yetu.”
Kimya kifupi kikafuata.
“Kwa hiyo, bwana Matata, sikuiona kabisa sababu yaw ewe kurejea hapa kwa ajili ya kule kusita tu ati Joram amenusurika katika ajali ya gari. Nakupa amri ya mwisho kuondoka hapa. Na nakuomba tusionane tena hadi kesho tutakapokutana Ikulukuapishwa kama baraza lipya la mawaziri na baadaye katika ukumbi wa Karimjee au Kilimanjaro Hoteli kwa tafrija maalumu. Sawa?”
“Sawa bwana…”

MOTO Matata alipowasili katika jengo la wizara yake, alilisahau mara moja jina hilo na kuendelea katika jina lake halisi na hadhi yake katika wizara hii. Kama mtu mkubwa, alitumia lifti maalumu ambayo ilimfikisha ghorofa ya nane ilikokuwa ofisi yake.

Akautumia mlango wa pili kuingia ofisini mwake ambamo alijibwatika juu ya kiti na kuitazama saa yake. Ilisema saa nane na dakika ishirini. Saa kadha wa kadha zilisalia kabla ya kutokea jambo ambalo lingebadili historia ya nchi.

Matata alihofia sana muda huo wa kusubiri. Hakuwa na hakika kama anastahili kuendelea na mipango yake au atoroke nchini mara moja kama roho ilivyokuwa ikimshawishi. “Utajiri hauji kwa starehe”… alijikumbusha kwa taabu maneno ya Kwame.

Kuyakumbuka huko kukamtia moyo hata kicheko kikamtoka na akasahau ndoto mbaya zilizomwandama usiku wa jana akijiona yuko kitanzini huku umati wa watu ukimcheka na kumsimanga.

“Ndoto au woga tu,” aliwaza. “Kesho ni siku nyingine. Nitakuwa mtu mwingine; tajiri na mwenye matumaini na nafasi ya kuwa tajiri na tajiri tena..”

Simu iliyomuunga na katibu wake ikakoroma ghafla. Akaiinua na kulitaja jina lake.

“Umerudi mzee?”

“Ndiyo Salome, lakini sijisikii vizuri, hivyo sitapenda kusumbuliwa kwa matatizo madogo madogo.”

“Nimeelewa mzee, ila kuna huyu kijana hapa. Anadai kuwa ni lazima akuone kwa hali yoyote. Anasema mnafahamiana na kwamba ana hakika utafurahi kumwona.”

“Amekutajia jina lake?”

“Ndiyo. Anajiita Joram Kiango.”

“Nani?” Bwana mkubwa alinguruma katika simu kiasi cha kuyaumiza masikio ya katibu wake. Hakujua afanye nini. Hakujua kama alistahili kumwona au la. Akabaki kaduwaa na simu mkononi hana uwezo wa kumjibu Salome ambaye aliendelea kuongea upande wa pili.

Joram alimkuta katika hali hiyo.

“Nadhani nitasamehewa kwa kuingia kabla ya kibali chako mzee,” Joram alisema kwa sauti yake tulivu akijiweka kitini bila kusubiri kukaribishwa. Nimeona nikutembelee mapema ili nishirikiane nawe kujadili maisha yako ya baadaye. Unasemaje mzee?”

Jibu halikusikika hivyo Joram aliendelea, “Kitendo chako na wachache wenye nyadhifa kadha wa kadha serikalini, ambao mmethubutu kula njama dhidi ya taifa lenu, taifa changa, ambalo linakutegemeeni ninyi kuliokoa, ni kitendo cha aibu kubwa mno. Ni kitendo ambacho hakistahili kuyafikia masikio ya taifa hili ambalo lilikutegemea sana hata likakupa wadhifa muhimu kama huu.

Hivyo nilichofuata hapa ni kukushauri tuondoke pamoja hadi Ikulu kwa mtukufu Rais ambako utakiri madhambi yako yote na kumwachia jukumu la kuamua.

"Usijidanganye kuwa ndoto yenu yaweza kuwa kweli," Joram aliendelea. "Orodha yenu, picha zenu, maongezi yenu ya asubuhi ya leo na njama zenu zote sasa hivi ziko mikononi mwa wanaohusika. Kuchelewa kujitoa kutakufanya uaibike zaidi. La muhimu ni kwenda mwenyewe mbele ya Baba wa Taifa ambako utatubu na kukiri yote bila kusahau kuwa unahusika kwa kila hali katika mauaji ya watu wengi wasio na hatia."

Bwana mkubwa huyo alishindwa kujibu lolote, walao kumtazama Joram usoni. Baada ya muda mrefu alinong'ona kwa sauti ya aibu akisema, "Siwezi. Siwezi kumtazama Rais wala raia yeyote usoni. Tafadhali nenda zako nifikirie la kufanya."

"Fikiria bila kusahau kwamba mpango umeharibika," Joram alisema akiinuka na kutoka nje. Akamuaga katibu na kutoka hadi mbele ya lifti ambapo alibonyeza kidude cha kuteremkia. Lifti ilipofika, aliteremka hadi chini.

Mlango wa lifti ulipofunguka masikio ya Joram na abiria wote waliotoka ndani ya lifti hiyo yalidakwa na kelele za ghafla zilizotoka katika umati uliokuwa ukijaa haraka haraka chini ya jengo hilo la wizara. Joram akawa mmoja kati ya watu waliokimbilia sehemu hiyo kutazama kinachotokea. Lilikuwa jambo la kutisha kuliko alivyotarajia. 'Bwana mkubwa' ambaye alikuwa akiongea naye muda mfupi tu uliopita alikuwa kalala chali akivuja damu nzito kutoka katika majeraha ya kutisha ya kichwa kilichoonekana kufumuka, miguu iliyovunjika na kiuno ambacho kilionekana kuvunjika kabisa.

"Nimemwona akijitupa mwenyewe toka dirishani," alidai mtu mmoja.

"Mimi pia..."

Joram akaitazama saa yake na kuondoka mahala hapo kwa mwendo wa haraka. Mbele kidogo, alipungia teksi na kumweleza dereva wapi alihitaji kupelekwa. Ilimfikisha kwa muda mzuri. Joram akateremka na kuiendea ofisi aliyoihitaji ambamo aliomba kuonana na 'Afande mkubwa zaidi'.

Akaelekezwa ofisi yake.

Alimkuta afande huyo kabadilika kabisa kwa magwanda ya kijeshi yenye nyota nyingi mabegani kinyume kabisa cha yale ya kiraia aliyovaa katika mkutano wao wa siri. Afande huyo alimtazama Joram mara moja na kujikuta akishikwa na hofu kubwa.

Ghafla, akasahau furaha aliyokuwa nayo muda mfupi alipokuwa akiwaza kesho itakavyokuwa siku tofauti mno kwake. Siku ambayo itamkaribisha katika dunia ya kutumia bila hofu ya kuishiwa, dunia ya kumchukua msichana yeyote amtakaye bila kuogopa sheria wala wazazi wake, dunia ya yeye kuwa na amri juu ya kuishi na kufa kwa mtu yeyote katika nchi hii. Naam, dunia itakayomweka hadharani, kila mtu akimtetemekea. Alikuwa akisubiri saa zitimie ili atimize wajibu wake kuikaribisha dunia hiyo.

Katika muda huo wa kusubiri, hakutarajia kabisa kuonana na
kijana huyu aliyeketi mbele yake akivuta sigara na kutabasamu kisirisiri.
"Nani wewe? Na wataka nini hapa?" akajitia kuuliza.

"Tunafahamiana sana afande. Nadhani huwezi kusahau kuwa muda mfupi uliopita tulikuwa wote katika mkutano fulani. Kwa jina naitwa Joram Kiango."

"Sikufahamu wala siufahamu mkutano huo."

Labda," Joram alijibu. "Lakini naamini utaufahamu vizuri. Baada ya muda mfupi polisi watakapokutia pingu na kukuhifadhi hadi kesho ambapo picha yako na wenzako mkiwa mkutanoni zitakapotolewa gazetini na maongezi yenu kusikika katika Redio Tanzania. Ama hufahamu kilichonileta mbele yenu ilikuwa kupata picha hizo?

“U mtu hatari usiye na shukrani hata chembe,” Joram alifoka. “Wadhifa ulionao ni mzito. Mamilioni ya Watanzania wangeweza kuumudu wadhifa huo lakini taifa limekukabidhi wewe. Ili ulilinde. Ili uwe mstari wa mbele kulinda silaha na masilahi yake. Lakini wewe unageuza silaha walizokupa wao kuwaangamiza. Unashiriki katika mikataba ya kupokonya masilahi yao. Huoni aibu kuuza wananchi. Aibu ilioje! Kwa kweli hustahili kuishi.”

Afande huyo akainua uso kumtazama Joram kwa hasira, “Toka nje bwana mdogo,” akafoka. “Toka, vinginevyo nitakudhuru!”

“Lazima nikueleze kwanza nilichokusudia…”

“Toka. Toka!” akafoka.

“… Kwamba taifa hili si zizi la ng’ombe ambalo mtu yeyote anaweza kuligeuza rasilimali yake kwa faida yake binafsi na mabwana zake.”

“Toka!”

“Na…”

“Toka!” Safari hii ‘afande’ alikuwa na bastola mkononi. Bastola aliyotoa ndani ya mtoto wa meza. Ilimwelekea Joram kifuani. “Toka vinginevyo nitakuua!”

Sauti yake iliwavuta wengi. Wakaja na kuduwaa mlangoni wakiwa hawayaamini macho yao mkubwa kaielekeza bastola kwa raia ambaye alionekana hana hatia wala hofu.

“Kifo change kitaongeza uzito wa madhambi yenu juu ya damu
nyingi zisizo na hatia ambazo mmemwaga. Hakitaleta mabadiliko yoyote wala kufanikisha mipango yenu ya kishetani…”

Mara mlipuko wa bastola ukasikika. Kila mtu alifumba macho kwa miali ya mlipuko huo. Walipoyafunua, walimwona bwana mkubwa kasahau kiti chake na kukaa chini, kainamisha kichwa ambacho kilikuwa kimefumuka kwa risasi hiyo. Bado, mkono wake uliishikilia bastola hiyo iliyotimiza wajibu.

Umati ulipiga kelele za hofu na mshangao. Joram aliacha umati huo katika hali hiyo na kutoka nje ambako alipata shida kidogo kupata usafiri. Watu wote walikuwa wakikimbilia kufuata mlipuko huo. Joram akapishana nao hadi nje ya jengo hilo ambako alijipatia usafiri.

Safari ilimfikisha katika wizara nyingine. Akaifuata ofisi ya mtu mkubwa moja kwa moja na kuomba kumwona.

“Huwezi kumwona mtu,” katibu alidai. “Amepata habari mbaya. Hana hali nzuri kuweza kuonana na mtu yeyote.”

“Habari ipi?”

“Ya kifo. Bwana mkubwa serikalini kafa na alikuwa rafiki yake mkubwa.”

Joram akashangaa habari zinavyosafiri haraka haraka. Ni hicho alichohitaji. Genge hilo hatari lifahamu kuwa limefahamika na limevunjika. Mipango yao isiweze kuendelea. Joram akatabasamu huku huku akigeuka ili aondoke zake. Lakini mara hamu ya kuuona uso wa mtu mkubwa baada ya habari njema kama hiyo ikamshika.
Akamgeukia katibu wake na kumwambia: “Nataka kumwona. Ni lazima nimwone. Siwezi kuondoka bila kumfariji. Mimi ni rafiki yake pia.”

Alipoona achelewa kuruhusiwa, alijielekeza mlangoni na kuuendea. Akagonga mara moja na kuufungua. Alimkuta bwana mkubwa kasimama nyuma ya meza mkono wake ukizungusha namba za simu, mkono wa pili ukiwa umeshika shavu. Mkono uliokuwa kwenye simu ulisita ghafla mara macho yake yalipokutana na yale ya Joram ambaye alikuwa akitabasamu.

“Pole mzee.”

“Nani wewe? Joram!” mtu mkubwa alifoka. “Tafadhali toka nje ya ofisi yangu.”

“Ndiyo,” Joram alijibu. “Lakini si kabla ya kukumbusha kuwa wenzako wametangulia kwa heshima kidogo. Hawatawajibika kutazamana na umati ambao utajaa mahakamani kukutazama kwa mshangao wewe na wenzako pindi mkijibu maswali ya Jaji Mkuu. Wala hawataning’inia juu ya kitanzi na kufa polepole huku wakijutia uroho wao na utovu wa shukrani ambao wamekufanyeni kuwa fisi mbele ya kondoo badala ya wachungaji. Aibu iliyoje kuwa na kiu ya utajiri kiasi hicho, pole tena mtu mkubwa.”

Mtu huyo alimtazama Joram kwa macho yenye mchanganyiko wa hasira na aibu. Kisha aliutia mkono wake katika mfuko wa koti na kutoa pakiti ya vidonge vidogo vidogo vya usingizi ambavyo alivimimina mkononi na kuvitupia kinywani. Alivyohakikisha amevimeza alimtazama tena Joram na kusema, “Siwezi kukubali kuitazama jamii….siwezi…” macho yake yakaanza kubadilika.

Akajibwatika chini akisahau kiti na kuketi sakafuni huku akijaribu kuyafumbua macho yake kwa juhudi kubwa. Hakufaulu. Mara akayafumba na kutulia.

Joram alifahamu kuwa huo ulikuwa usingizi ambao usingeisha. “Kifo cha amani kuliko alivyostahili,” aliwaza akitoka zake polepole na kumtupia katibu ‘kwa heri’ bila kumtazama usoni.

Nje ya jengo hilo Joram alisita na kuwaza kwa furaha. Nusu ya kazi ilikuwa imekwisha. Mizizi mingi ilikwishang’olewa. Uliosalia ni ule mzizi wa shina; mzizi wa fitina; Kwame au Joe Kileo. Huyu alikuwa mtu hatari na bado alikuwa na Neema tayari kumdhuru endapo angejua mambo yanamwendea kombo.

Hivyo, alihitajiwa kupatikana haraka, katika hali ya uangalifu zaidi. Hali ambayo Joram alihitajika kuwa mkamilifu kwa kila hali. Kwa bahati baya hakuwa na silaha zozote za haja mfukoni zaidi ya visu kadhaa vilivyohifadhiwa katika mfuko wa siri. Lakini kwa ajili ya haja kubwa ya kumpota Neema akiwa hai bado, Joram alijikuta ndani ya teksi akielekea jengo la Snow Fund.

Gari liliposimama, Joram alijikuta akiruka nje na kutazamana na Inspekta Mkwaju Kombora ana kwa ana. Kombora alikuwa na bastola wazi mkononi, nyuma yake, askari sita wenye bunduki aina ya Sub-Mashine Gun wakimfuata kwa uangalifu.

“Joram,” Kombora alimwita kwa nguvu alipomwona. “Umekuwa wapi muda wote huu? Kijana, nasikitika muda hautoshi kuweza kuzungumza mengi. Lakini kwa ufupi tu safari hii ulichogundua ni kitu kizito ambacho kingeifanya nchi hii igeuke dimbwi la damu ama iwe zizi ambalo mchungaji ni fisi mwenye njaa.”

“Nami nasikitika pia Inspekta kuwa umegundua mapema kuliko nilivyotaka,” Joram akamjibu. “Ningependa kukamilisha kazi hii peke yangu kwa faida ya watu ambao wengi wao wana vyeo vikubwa serikalini. Nilikuwa nikiwaonea aibu au huruma kuwafanya wasimame mbele ya wananchi waliowaamini madaraka hayo na kukiri madhambi yao. Kwa bahati umeniwahi.
Hata hivyo, wengi wameshafuata njia inayowastahili. Wamejiua wenyewe. Utapata taarifa kamili baada ya muda mfupi.

“Kadhalika, huko Kigamboni iko nyumba moja ambamo amelala marehemu asiye na hatia, Komba ambaye ndiye hasa aliyesaidia siri hii ya hatari kutoka nje. Ameuawa na jambazi hatari ambalo bado liko hai katika nyumba hiyohiyo. Nimelifunga vizuri. Halina nafasi ya kutoroka. Mara tu upatapo nafasi, nitapenda kupata askari ambao nitawaelekeza katika nyumba hiyo. Napenda Bon afe kwa kitanzi.”

“Kwa nini Joram?” Komba alifoka. “Kwa nini hukusema mapema? Anaweza kutoroka!” Kisha akajisahihisha kwa kusema polepole, “Kweli haikuwepo nafasi. Tuombe Mungu nimkute hai. Atajuta kuzaliwa. Sasa ni kumwingilia huyu kiongozi wao, Kwame.”

“Kwame ni mtu hatari sana,” Joram alikumbusha tena. “Na bado anaye Neema mikononi mwake. Bila shaka yuko katika jengo hilihili. Nadhani utahakikisha usalama wa Neema Inspekta.”

“Usitie shaka.”

“Wakaanza kuingia ndani wakiwapita wafanyakazi wa ofisi hiyo ambao kwa muda mrefu, walikuwa wamechanganyikiwa kwa matukio ya kutisha ambayo yalikuwa yakiitokea ofisi hii kutwa nzima. Waliduwaa juu ya viti vyao au wima wakimtazama Kombora, Joram na askari wote ambao waliingia na kuiendea ofisi ya mkurugenzi mtendaji.

“Hana nafasi ya kutoroka,” Kombora alimnong’oneza Joram. “Jumba hili limezingirwa kila upande. Askari wengine wako juu ya paa. Sijui atatokea wapi.”

“Usisahau usalama wa Neema Inspekta,” Joram aliasa tena. “Kwa kweli kazi hii ningependa kuifanya mwenyewe. Sina imani sana na askari wako…”

Kombota alimkatiza Joram kwa kumwambia, “Neema atatoka salama. Askari wote wameonywa waangalie sana risasi zao zisimguse msichana wako walao unywele. Natumaini watafanya kazi nzuri. Nimechagua wale ambao ni hodari kwa shabaha tu.”

Wakaifikia ofisi ya Kwame. Waligonga mara kadhaa bila jibu. Kombora akaita kwa nguvu ingawa alijua mlango huo ulikuwa maalumu kwa kutokuruhusu sauti kutoka nje. Alipochoka alielekeza bastola yake katika kitasa na kuifyatua. Risasi ya .45 maalumu kwa polisi haikusita kutimiza wajibu.

Chumba walikikuta kitupu, Kombora akatoa macho ya mshangao. Lakini Joram alizunguka nyuma ya meza na kuchungulia hapa kisha pale, mara sakafu ikafunguka na kuacha mwanya wenye ngazi iliyoelekea chini. Kombora akawa wa kwanza kuifuata. Joram alifuatia akifuatiwa na askari.

Huko chini walijikuta katika ukumbi wenye vyumba vingi vyumba vyote vilikuwa vimefungwa. Risasi ya bastola ya Kombora ikavifungua vyote. Waligundua mengi; akiba ya silaha, nyaraka za siri na dawa aina aina. Ni katika chumba cha mwisho ndimo walipopata kitu walichokuwa wakihitaji. Walimkuta Kwame kashika bastola mkononi mbele ya msichana aliyeketishwa sakafuni, nusu uchi kwa jinsi mavazi yake yalivyotatuka katika hali ya kuadhibiwa sana.

“Neema!” Joram alipiga kelele.

“Neema, ndiyo,” Kwame aliwajibu akitabasamu kifedhuli. “Ni mpenzi wako. Lakini endapo unampenda, waambie rafiki zako wote pamoja na mkubwa wao anayejiita Inspekta warudi walipotoka haraka. Mimi na wewe pamoja na mpenzi wetu tutaondoka pamoja hadi nje ya jiji ambapo nitawapeni uhuru wenu nami nichukue uhuru wangu.”

Kwame alichukua uamuzi huo baada ya kupata taarifa ikimfahamisha kuwa Joram alikuwa ametoweka machoni mwa walinzi wake. Taarifa hiyo ilifuatwa na vifo vya washiriki wenzake pamoja na kuambiwa kuwa askari walikuwa wakiizingira ofisi yake ndipo akawa hana njia zaidi ya hiyo.

Kombora akamgeukia Joram kwa mshangao. Alitarajia madhara, lakini hakutarajia madhara hayo yawe katika hali hiyo. Hakutarajia kumkuta Kwame akiwa na bastola mkononi akimtazama msichana asiye na hatia na ambaye ametoa mchango madhubuti kuiokoa nchi katika madhara ya mtu huyo. Msichana mzuri, Neema Iddi. Wakati huohuo, hakuwa tayari kuacha mtu huyo anusurike mbele ya macho yake mwenyewe hasa baada ya kuziona picha alizofotoa Joram pamoja na kusikiliza kanda ambayo ilinasa mengi yanayotosha kuwa ushahidi kamili dhidi ya watu hawa waovu.

“Labda hunifahamu vyema Inspekta,” Kwame alimjibu baada ya tabasamu lingine la kebehi. “Mwambie, Joram. Mwambie mimi ni nani. Nadhani wewe wanifahamu zaidi yake.”

“Nakufahamu sana,” Kombora alijibu. “Wewe ni jasusi mkubwa uliyepewa jukumu la kuharibu siasa na uchumi wa nchi kwa njia yoyote. Umefanikiwa kuwalaghai watu kadhaa kwa vishawishi vya kishetani na kupanga kuangusha utawala halali wa nchi hii usiku wa leo.”

“Kumbe wafahamu…” Kwame alijibu.

“Kwa bahati mbaya bwana Kwame au Joe Kileo mipango yako yote imeharibika. Utakachofanya ni kujitoa kwetu ili uwekwe mahabusu kusubiri hukumu kwa makosa yako yasiyohesabika. Umemwaga damu zisizo na hatia umethubutu kula njama dhidi ya nchi na wananchi. Umesababisha fujo na ghasia. Kwa kweli unastahili kula kitanzi Kwame. Ni hapo mabwana zako watakapofahamu kuwa nchi hii si uwanja wa mpira ambapo wanaweza kutegemea wapendavyo,” Kombora aliendelea kufoka.

“Kumbe wanifahamu Kombora!” Kwame alijibu akitabasamu kifedhuli. “Kwa bahati mbaya siwezi kushikwa nanyi. Nitaondoka na msichana huyu hadi nje ambako nitaamua wapi nielekee. Mkinilazimisha nitakubali kufa, lakini si kabla ya kuhakikisha bastola hii inaifumua sura nzuri ya msichana huyu. Nadhani hutapenda kushuhudia hilo mtakatifu Inspekta Kombora. Na Joram? Utafurahi mpenzi wako asulubiwe mbele yako?”

Wote walikubali kuchanganyikiwa. Joram alisaga meno kwa hasira. Lakini hakuona lipi afanye lipi aseme katika hali hiyo. Ingawa bastola ya Kwame ilikuwa ikimwelekea Neema, lakini macho na mawazo yake yalikuwa kwa umati huo uliomzunguka silaha zao zikimtazama kwa uchu.

Hivyo, hakuona wala kutarajia pindi Neema alipoinuka na kuachia pigo kali ka karate ambalo lilifanya bastola hiyo ipae angani. Wakati huo bastola zote zilifyatuka na risasi saba kuuteketeza uso na kifua cha Kwame. Alikufa kabla hajatua chini. Hakuwa na haja ya kupapatika!

“Neema!” Joram aliita kwa nguvu akimkimbilia na kumwinua pindi alipoanguka kwa mshindo wa bastola. Alikuwa hai… hakuwa na jeraha….

“Neema!” Joram aliita tena akimkumbatia kwa nguvu.

MWISHO

Tutarudi na roho zetu?

1

KAMA maji ya bahari ya hindi yangekuwa na hisia, basi yangejisiskia fahari sana kwa kupata fursa nyingine ya kuiburudisha miili ya viumbe hawa wawili ambao walikuwa wakiogelea kandokando ya ufuko huku wakicheza na kucheka. Walifanya picha ya kuvutia sana, hasa sura zao nzuri zilipoibuka na kutoka majini na kumezwa na tabasamu lililosababishwa na mzaha waliokuwa wakifanyiana chini ya maji. Baada ya kuogelea kwa muda walirejea nchi kavu ambako walijibwaga juu ya mchanga ulioruhusu joto likaushe maji miilini mwao.

Ufuko pia ungekuwa na kila sababu ya kusherehekea johari ya kulaliwa na viumbe kama hawa kwani walioana kimaumbile kama pacha, ingawa hawakuwa mtu na dada yake. Walikuwa kama jozi ya kiatu cha kiume kwa cha kike. Mwanamume hakuwa mwingine zaidi ya yule kijana mwenye umbo refu, kakamavu, lililokaa kiriadhariadha na sura nzuri, yenye dalili zote za hekima, ushujaa na ucheshi. Kwa jina anaitwa Joram Kiango.

Naye msichana alibahatika kupewa umbo lenye kila kitu ambacho msichana anahitaji kuwa nacho, wakati huohuo akiwa na kile ambacho mvulana legelege asingekuwa nacho. Ni yule ambaye akutazamapo ungependa aendelee kukutazama, achekapo unafarajika, atembeapo unaburudika, yule ambaye kuna madai kwamba alikuja duniani kwa makosa baada ya kuumbwa ili awe malaika. Kama madai hayo si kweli, basi yako mbali sana na uongo. Hata jina lake halikutofautiana sana na sura yake. Wanamwita Nuru.

Baada ya kuhakikisha kuwa miili yao ilikuwa imekauka, wakajifuta vizuri; kisha wakayachukua mataulo yao na kwenda kwenye gari lao. Macho ya watu wengi, Waswahili kwa watalii ambao walikuwa katika ufuko huo, hayakukoma kuwafuata. Kutazamwatazamwa, hasa wanapokuwa pamoja, halikuwa jambo geni tena kwao. Mara kwa mara macho ya kiume yalimwandama Nuru, hali ya kike yakimfuata Joram, kila mahala walipopita. Walijifunza kuyazoea hata wakaanza kusahau kuwa wanatazamwa. Hivyo, walipolifikia gari waliingia na kulitia moto wakilielekeza mjini kwa mwendo usio wa haraka.

Hawakuwa na sababu yoyote ya kufanya haraka. Ratiba yao ya starehe ilikuwa ikielekea kwisha mapema zaidi ya walivyokusudia. Walikuwa wamekubaliana wakae katika miji yote mashuhuri hapa nchini kwa muda wa wiki nzima kila mji. Lakini hii ilikuwa wiki ya pili tu na tayari walikuwa wameishi Zanzibar, Moshi, Arusha, Dodoma, Mwanza na kujikuta wamerejea Dar es salaam. Kila mji waliuona unakinaisha baada ya siku mbili tu. Maisha ya hotelini waliyaona yanawafaa watu wavivu, nazo mbuga za wanyama ziliwasisimua watalii, ilihali miji iliwaridhisha wenyeji, na safari za hapa na pale zilikinaisha.

Hivyo, ingawa walirejea Dar es Salaam na kuendelea na starehe zao wakiishi katika hoteli ya Kilimanjaro na ingawa waliendelea kucheza na kucheka, na hakuna aliyetamka neno, lakini bado haikuwa siri tena kuwa maisha ya kula, kulala… kula tena, kulala tena yalianza kuwachosha. Maisha hayo yalianza usiku ule ambao Joram Kiango asingeweza kuusahau, usiku ambao hadi leo unamtia maumivu moyoni kila anapokumbuka alivyodhulumiwa haki na wajibu wake wa kuitia risasi katika kichwa cha Proper, yule katili ambaye, pamoja na kuwaangamiza watu wengi wasio na hatia, alimwua Neema Iddi kinyama. Ni siku hiyo ambayo Joram aliitupa bastola yake na kuamua kuishi kivivu kama wanavyoishi watu wengine. Msichana huyu Nuru alihusika sana katika mkasa huo ambao tayari mtu mmoja aliuandikia kitabu na kukiita SALAMU TOKA KUZIMU. Nuru alishindwa kuachana na Joram na hangeweza kustahimili kumwona Joram akiteseka na msiba huo peke yake.

Alimfuata na kumsihi hata palipopambazuka wakajikuta wako pamoja, juu ya kitanda kimoja.

Tangu hapo hawakuachana, Joram hakuwa mtu anayeweza kuachwa kirahisi. Naye Nuru kadhalika, alitofautiana sana na wale wanawake wazuri ambao uzuri wao ni pale wanapokuwa wamevaa nguo tu. Alikuwa na mengi ambayo aliyatenda kwa nia moja tu; kumfariji Joram naye Joram alijikuta akianza kujisamehe. Lakini asingeweza kusahau…

Walipowasili chumbani mwao walijipumzisha vitandani mwao kwa muda huku wakilainisha koo zao kwa vinywaji vitamu. Kisha wakafuatana bafuni na kuyaondoa maji ya chumvi miilini mwao kwa kuoga vizuri kwa sabuni. Baada ya hapo walikwenda katika chumba cha maakuli ambapo walikula na kujiburudisha kwa vinywaji vikali na maongezi laini.

Akiwa katika vazi lililomkaa vema, suti ya kijivu iliyooana na viatu vyeusi kama kawaida, alikuwa tishio kubwa kwa wanaume waliokuja na wasichana wao. Hata hivyo, walijifariji kwa kujua kuwa asingekuwa “mwendawazimu” wa kuvutwa na yeyote kwani aliyeketi nae hakuwa msichana wa kawaida. “Kwanini watu kama wale wanaishi hapa bongo?” mtu mmoja alimnong’oneza jirani yake. “Tazama wanavyopendeza! Wangeweza kwenda zao nje na kutajirika sana endapo wangecheza mchezo mmoja tu wa sinema”

“Kweli kabisa,” aliungwa mkono. “Hata maumbile yao yanafikiana. Yule dada anatosha kabisa kumtia mwanaume yeyote wazimu kiasi cha kumfanya auze nyumba.”

Maongezi hayo hayakumfikia Joram wala Nuru. Lakini alikwishazoea kuyasoma katika macho ya watazamaji wake. Hivyo, alitabasamu kidogo na kuagiza kinywaji kingine. Nuru alikuwa akiongea neno. Joram aliitika bila kumsikia. Waliendelea kunywa kwa muda hadi walipoamua kuwa wametosheka. Ndipo walipofuatana katika ukumbi wa muziki ambapo walisikiliza muziki na kucheza kwa saa kadhaa. Walipokinai walikiendea chumba chao ambacho kiliwalaki na kuwapa usiri. Katika usiri huo, kwa mara nyingine, miili yao iliburudika na kusherehekea afya zao.

Kesho yake, baada ya kifungua kinywa walitazamana katika hali ya kuulizana siku hiyo waitumie vipi. Nuru aliweza kuzisoma dalili za kuzikinai ratiba zao ambazo zilikuwemo katika macho ya Joram. Ingawa walikuwa wakistarehe na kujiburudisha furaha, ilikuwa dhahiri kuwa burudani hizo, kama zilikuwa zikiuburudisha mwili wa Joram, kamwe hazikuwa zikiburudisha akili yake. Ingawa uso wake ulitabasamu mara kwa mara, lakini roho yake iliwaka kwa hasira kali dhidi ya adui zake, adui wa taifa na maendeleo ya jamii, adui ambao walifanya maovu mengi yasiyokadirika na kumtia lile donda la rohoni kwa kumuua kikatili msiri wake mkuu, Neema. Kwa dhamira ya kumsahaulisha Joram uchungu huo ndipo Nuru akajitoa kwake mwili na roho. Lakini ilikuwa dhahiri kuwa jeraha hilo lilikuwa bichi katika roho ya Joram, na lisingepona kabisa isipokuwa kwa dawa moja tu:kulipiza kisasi. Hayo aliyaona wazi katika macho ya Joram ingawa alijisingizia kufurahia starehe zao.

Iko siku Nuru aliwahi kumwambia, “Sikia Joram. Huonekani kufurahia lolote tunalofanya. Kwa nini usiirudie ofisi yako na kuendeleza harakati zako? Nitakuwa kama alivyokuwa Neema. Nitakusaidia kwa hali na mali.”

Joram alicheka na kumjibu, “Mara ngapi nikwambie kuwa nimeacha shughuli hizo. Nitaendelea kustarehe hadi nitakapoishiwa na senti yangu ya mwisho.Ndipo nitakapotafuta kazi na kuifanya kwa Amani na utulivu kama vijana wenzangu.”

“Kwanini lakini? Kifo cha msichana mmoja tu kinakufanya usahau wajibu wako!”

“Sivyo Nuru. Isieleweke kuwa nimechukia kwa ajili ya kufiwa na Neema. Yeye ni mmoja tu kati ya mamia ya wasichana wanaouawa kwa dhuluma na ukatili ainaaina ulioko duniani. Ni mmoja tu kati ya maelfu ya vijana wanaoteseka kwa shida ambazo wanazipata kwa makosa ya watu wengine. Ni mmoja tu kati ya mamilioni ya binadamu wanaoumia kwa umasikini ambao hawakuuomba na dhiki ambazo hazina umuhimu wowote.”

“Sidhani kama nimekuelewa Joram, unazungumza kama mshairi.”

“Labda. Ninachotaka kusema ni kwamba bastola yangu haitoshi kukomesha maovu yote yanayotendeka hapa duniani. Kote Afrika, na duniani kwa ujumla, binadamu hawako sawa kiuchumi. Wako wanaoshinda njaa na kuna wanaomwaga chakula. Kama kweli nakusudia kuondoa dhuluma na ukatili kwa nchi dhidi ya nchi nyingine, basi sina budi kuukomesha pia ukatili dhidi ya mwingine. Maadamu hayo yako nje ya uwezo wangu, naona sina budi kusahau yaliyopita na kuanza kula na kunywa kama vijana wenzangu.”

“Hasira hizo Joram. Upende usipende ukweli ni huo huo: bastola yako haiwezi kuwaelekea viongozi wazembe na wenye choyo ambao wanasababisha hali ngumu kwa mwananchi. Lakini inawajibika kuwakomoa maadui ambao dhamira yao ni kuhakikisha hatulifikii lengo letu la kujenga taifa ambalo raia wake wanafaidi matunda ya uhuru wao. Unafahamu fika kuwa wanatunyima nafasi ya kufanya hayo”…

Maongezi hayo yalifanyika siku chache zilizopita. Nuru aliyakumbuka tena leo baada ya kuziona dalili za kukinai katika macho ya Joram. Alijua na kuamini, kama wanavyoamini watu wote wanaomfahamu Joram, kuwa starehe yake kuu ni pale anapopambana na adui na burudani yake ni hapo anapowashinda. Vinginevyo Joram alikuwa akijisingizia starehe.

“Leo wapi mpenzi”, Nuru aliona amchokoze.

“Leo najisikia kulala tu”.

“Kulala mchana! Tangu lini umeanza tabia hiyo?”

“Tangu nilipoacha kuwa Joram Kiango na kuamua kuwa kijana mtumiaji anayeitwa Joram Kiango.”

“Nilijua utachoka, Joram. Kwanini usirudi ofisini na kuanzia leo?”

“Sikia Nuru. Usianzishe tena ule ubishi ambao siupendi. Wakati wote nitakuwa hapa nikiendelea kutumia.”

“Sidhani kama unasema ukweli. Huonekani mtu wa kustarehe maishani.”

Joram hakumjibu. Alijilaza kitandani na kujisomea gazeti.

Kisha jirani yao wa chumba cha pili aliingia akiwa katokwa na macho. Hakujali kupiga hodi. Wala macho yake hayakuvutwa kuuhusudu uzuri wa Nuru kama ilivyokuwa kawaida yake. Badala yake alimwendea Joram kitandani akisema, “Hujasikia? Samora amekufa!Ndege yake imeanguka huko Afrika Kusini.”

“Amekufa!” Nuru alishangaa.

“Amekufa. Sio bure. Iko namna. Haiwezi kuwa ajali ya kawaida.”

“Afrika Kusini? Alienda fanya nini huko?” Joram aliuliza kwa utulivu. Hata hivyo macho yake yaliwaka kwa hasira, ingawa hakupenda kuidhihirisha kwa Nuru.

“Siku hizi hata taarifa za habari husikilizi Joram?” Nuru alisema.

“Samora hakwenda Afrika Kusini. Alikuwa akitoka Zambia ambako alikutana na rais Mobutu na Waziri Mkuu Mugabe kutafuta mbinu za kuiwekea Afrika Kusini vikwazo zaidi vya kiuchumi”.

“Wanasema chanzo cha ajali hakijapatikana. Bila shaka watakuwa wameisababishia ajali hiyo kwa njia moja au nyingie,” alisema kwa masikitiko.

“Nadhani wamezoea kutuangamiza wapendavyo. Kwao sisi ni sawa na vifaranga waliofugwa. Yeyote ambaye hawampendi wanamponda kwa urahisi. Jambo la kusikitisha ni kwamba sisi hatuwezi kuwafanya lolote. Baya zaidi ni kwamba hatujui tutaendelea kuuawa mpaka lini.Kwanza, walimuua Mondlane: Sasa wamemuua mrithi wake, Samora. Na siyo hao tu. Viongozi wengi wa Afrika wameondokea kuwa kama mifugo yao. Tunaorodha ndefu ya viongozi wetu wanaouawa au kupinduliwa kwa matakwa yao. Tutaendelea kuvumilia mpaka lini?” Nuru alikuwa kama mtu anayezungumza peke yake.

Lakini macho yake yalikuwa yakimtazama Joram. Alitamani aone kitu katika macho yake. Hakukiona. Jambo hilo lilimfanya ainame chini na kuruhusu matone kadhaa ya machozi yamdondoke.

Yalikuwa machozi ya hasira zaidi ya huzuni.

Kifo hiki cha kijana shujaa aliyeheshimiwa kote dunia, aliyependwa na wapenzi wake na kuogopwa na adui zake; kilifuatiwa na minong’ono mingi kote dunia. Watu walisema hili na lile, wakipingana na kuafikiana.

“Walimuua…”

“Bila shaka.”

“…Njama za Afrika Kusini.”

“Na vibaraka vyao.”

Siku chache baadae maongezi yalibadilika.

“Umesikia? Makaburu wanadai kuwa wataendelea kuwaadhibu viongozi na wananchi wote wa nchi za mstari wa mbele ambao wanajifanya vichwa ngumu.”

“Kweli? Washenzi sana wale. Wanaweza kufanya lolote”.

Na baada ya siku chache mambo yalianza kutukia. Duniani kote magazeti yalikuwa na habari ya kutisha:

Watu mia nne wamefariki, mia tisa kujeruhiwa na maelfu kuponea chupuchupu katika ajali isiyo ya kawaida iliyotokea huko Lagos Naijeria. Watu hao walikuwa katika uwanja wa mpira wakitazama shindano kati ya timu ya taifa ya nchi hiyo na Zaire. Dakika chache kabla ya mchezo huo kwisha, moto mkali ulilipuka na kuubomoa uwanja mzima na kusababisha maafa hayo. Wachunguzi wa mambo wanahisi kuwa huenda utawala wa Afrika Kusini unahusika.

Kabla watu hawajaisahau habari hiyo, ilifuata nyingine ya kutisha vilevile.

Harare.

Maghala manane ya serikali, ambayo yalikuwa yamehifadhi chakula, yameungua moto kwa pamoja. Chanzo cha moto huo hakijajulikana. Jambo la kushangaza ni jinsi maghala hayo yalivyoungua kwa pamoja ingawa yako katika wilaya mbalimbali za nchi hiyo. Kuna mashaka kuwa tukio hili kwa njia moja au nyingine linahusiana na yale maafa ya Nigeria.

Na baada ya siku chache;

Dar es Salaam.

Katika matukio ya kutisha na kushangaza yanayozidi kutokea nchi zenye msimamo wa kimapinduzi za Afrika, leo asubuhi Tanzania imepatwa na pigo zito la kusikitisha. Jengo la Benki kuu ambalo lilikuwa likikamilisha marekebisho, baada ya ule moto wa awali limeungua tena. Safari hii haielekei kuwa kuna matengenezo yoyote yanayoweza kulirekebisha zaidi ya kujengwa upya. Chanzo cha moto huu hakijafahamika.

Habari hizi ziliitisha Afrika na kuishangaza dunia. Kila mtu aliyezisikia redioni na kuzisoma magazetini alishangazwa na matukio haya ambayo mfano wake haukupata kutokea katika historia ya Afrika na dunia.

Ajali ni jambo la kawaida. Kadhalika, kuna watu wanaoamini kitu kinachoitwa 'mkosi' na 'bahati mbaya.'Lakini mikosi mingi kiasi hiki na bahati mbaya kama hizi kuziandama nchi chache za Afrika, zenye msimamo mmoja katika suala la ukombozi, ni jambo ambalo lilisababisha nyongeza katika fikra za wasomaji na wasikilizaji wa vyombo vya habari. Kitu kinachoitwa 'roho mbaya' kilipenya katika fikra hizo, ingawa hakukuwa na hakika katika mawazo hayo. Baadhi hata waliwahi kutamka hadharani kuwa kuna mkono wa mtu katika matukio hayo.

Mawazo hayo yalifuatwa na hofu katika mioyo ya wananchi na serikali zao walipojiuliza,"Kipi kingefuata?"

"Joram, tutakaa kimya kusubiri maafa zaidi?" Nuru alimwuliza Joram baada ya kusoma habari hizi za tukio la Benki Kuu katika gazeti. Alijitahidi kustahamili kutosema lolote alipoyasoma matukio ya Lagos na Harare. Lakini hili la nyumbani lilimgusa zaidi. "Aibu iliyoje!" aliendelea. "Tuendelee kustarehe kwa vinywaji na muziki huku tukisubiri siku ambayo maafa mengine yatatokea! Haiwezekani Joram. Lazima tufanye jambo."

Ndiyo. Habari hizo hazikumpendeza Joram. Hata hivyo, alizisoma kama raia wengine, bila ya kudhihirisha dalili yoyote ya nia ya kufanya lolote kama alivyokuwa awali. Jambo hilo lilimfanya Nuru atokwe na machozi. "Serikali inao polisi na wapelelezi wake, ambao inawalipa pesa nyingi," Joram alisema. "Mimi ambaye nimeacha shughuli hizo nitasaidia nini?"

"Huwezi kusema hivyo Joram! Siamini kama moyo wako wa uzalendo umedidimia kiasi hicho."

"Haujadidimia. Uko palepale, kama ilivyo mioyo ya wazalendo wengine."

"Lakini wewe si mzalendo wa kawaida, Joram. Taifa linakuthamini na kukutegemea. Huwezi kulisaliti kiasi hicho bila sababu ya kuridhisha. Lazima ufanye jambo."

"Ndiyo. Nitafanya jambo. Nitastarehe na kuendelea kustarehe kama wanavyofanya vijana wenzangu. Njoo kitandani, Nuru. Tafadhali, njoo tustarehe. Acha wenye shibe waendelee kulinda shibe yao. Wewe na mimi tuna nini katika nchi na dunia hii?"

"Joram…"

"Nuru, njoo tafadhali. Na kama umenichoka sema nimtafute Nuru mwingine ambaye hachoshwi na starehe."

Nuru angependa kukataa. Lakini asingeweza. Akamfuata Joram kitandani na kujilaza kando yake huku machozi yakimtoka kama kondoo anayesubiri kuchunwa.

SURA YA PILI

KATI ya watu ambao wameisumbukia nchi hii, wakiziweka roho zao katika minada ya maafa na kwato za mauti kuilinda nchi isimezwe na jangwa la misukosuko inayosababishwa na majasusi hatari, ni mzee huyu; Mkwaju Kombora. Tangu utoto wake baada ya kumaliza kidato cha sita, alijikuta akitoka chuo hadi chuo, akifundishwa mbinu mbalimbali za kupambana na adui. Baada ya kuhitimu vizuri alijikuta kava magwanda ambayo mabega yake hayakukoma kubadilikabadilika hadi alipojikuta Inspekta wa kikosi hiki maalumu. Kupanda kwake ngazi mara kwa mara kulitokana na moyo wake wa kishujaa na juhudi zisizo kifani katika kuwakabili adui wa nchi. Mara kwa mara aliwashinda adui zake isipokuwa safari chache ambazo alielekea kukata tamaa. Hata hivyo, asingekosa kumshukuru Mungu kwani nyakati hizo alitokea kijana yule ambaye alisaidia kuwanasa adui kwa hila zake za kutatanisha, kijana ambae jina lake lisingeweza kumtoka akilini; Joram Kiango.

Kombora asingeusahau mchango wa kijana huyu katika mikasa ile ambayo Mswahili mmoja ameamua kuandika vitabu ili apate chochote kile na kuviita Dimbwi la Damu, Mikononi mwa Nunda, Najisikia kuua tena na Salamu kutoka Kuzimu. Hata hivyo, kama polisi wengine, Kombora asingeweza kutamka hadharani kuwa Joram alifanya lolote la haja isipokuwa alibahatisha na kuhatarisha maisha yake.

Lakini leo Kombora alitamani kumbembeleza Joram, hata kwa kumuangukia miguuni, endapo ingebidi, ili amsaidie kuutatua mkasa huu uliokuwa ukimtoa jasho yeye na polisi wenzake wote wa nchi zilizo mstari wa mbele kwenye ukombozi Kusini mwa Afrika.

Mambo mengi, yalikuwa yakitokea mazito na ya kutisha zaidi ya walivyoyafahamu wananchi wa kawaida ambao wanategemea gazeti, redio na televisheni ziwape habari. Kila mmoja alisikia mikasa ya kuteketea kwa mamia ya maisha ya watu wasio na hatia ambao walipata ajali ya kutatanisha katika uwanja wa mpira huko Naijeria. Pia, ni wengi waliosikia juu ya kuungua kwa maghala ya chakula bila sababu mahususi inayoeleweka huko Harare. Zaidi, hakuna Mtanzania ambaye hakupata kuzisikia habari za kuungua tena kwa jengo la Benki kuu lililokuwa likikamilishiwa shughuli za kujengwa upya.

Hayo ni maovu yaliyosikika katika vyombo vya habari na mitaani. Hayakumtisha sana Kombora. Lakini kulikuwa na haya ambayo bado yalikuwa siri mioyoni mwa wakubwa wachache wa ngazi za juu katika idara ya usalama, ambayo hayasemeki wala kutangazika.

Viongozi wanane wa vyama kadhaa vya wapigania uhuru wa Afrika Kusini na mwakilishi wa PLO hapa nchini, ambao walikuwa wakikutana kwa faragha katika jengo moja jijini Dar es Salaam, walifariki ghafla katika moja ya ajali hizo zisizoeleweka. Hakuna anayefahamu kikamilifu chanzo cha vifo hivyo, isipokuwa kwamba walikufa kwa kuungua moto uliolipuka ghafla katika chumba chao cha mkutano. Juhudi zote za kutafuta chanzo cha moto huo hazikuwa na mafanikio.

Zaidi ya hao, kuna wale mawaziri wa nchi zisizofungamana na upande wowote ambao walinusurika katika ajali ambayo haikutofautiana na hiyo ya Dar es Salaam. Mkutano wao uliandaliwa kufanyika katika chumba fulani katikati ya jiji la Lusaka. Wakati wakijiandaa kwenda huko lilitukia suala jipya ambalo liliuchelewesha msafara wao kwa zaidi ya nusu saa. Kuchelewa huko kuliyaokoa maisha yao kwani chumba hicho kililipuka kwa moto mkubwa uliyoyapoteza maisha ya wafanyakazi wawili wa chumba hicho na kuharibu vifaa vyote. Kama awali, chanzo cha moto huo hakikupata kufahamika.

Hayo ni baadhi tu ya mambo yaliyokuwa yakitokea. Kulikuwa na hisia kuwa mkono wa utawala wamakaburu wa Afrika Kusini ulikuwamo katika vitendo hivyo. Lakini hisia hizo hazikuwa na uhakika kamili, hasa baada ya ushahidi mdogo ulikuwa ukielekea kutoweka kwa njia nyingine ya kusikitisha.

Ushahidi huo ulielekea kuchipuka baada ya ule moto uliotekeza Benki Kuu. Yuko askari mmoja aliyesema kuwa aliamini moto huo ulisababishwa na mtu mmoja aliyefika katika jengo hili usiku na kujiita kuwa ni mmoja kati ya mafundi ambao walikuwa wakishughulikia jengo hilo. Jengo lilikuwa chini ya ulinzi mkali wa askari huyo na alimwamuru kusimama mikono juu. Mtu huyo alisihi kwa maneno mengi kuwa, alisahau kitu muhimu sana kwake katika jengo hilo, jambo lililomfanya askari huyo amruhusu kuingia ndani baada ya kumkagua kwa makini. Mtu huyo aliingia harakaharaka na baada ya dakika kadhaa alirudi huku akiwa ameshika hirizi mkononi na kusema kwa furaha,"Nilikuwa nimesahau hii, ndugu yangu. Bila ya kuwa na hii mfukoni siwezi kuishi saa ishirini na nne."

Askari huyo hakumwamini sana mtu huyo, kutokana na jinsi alivyomuona mkakamavu asiyehofu hata kuelekezwa mtutu wa bunduki. Hivyo, jengo hilo lilipolipuka moto saa kadhaa baadaye, alilielezea tukio hilo kwa wakubwa zake ambao walimweka kati ya watu ambao walilazimika kuongea na Kombora ana kwa ana. Baada ya kumsaili kwa mapana na marefu Kombora alielekea kuamini kuwa mtu huyo aliyeingia katika jengo hilo usiku alihusika, kwa njia moja au nyingine, katika janga hilo. Lakini pindi walipobuni mbinu za kuanzisha msako wakumtafuta, askari huyo aliyekuwa mtu pekee aliyewahi kumwona alikutwa akielea baharini pwani ya Magogoni, akiwa maiti. Hakuna aliyeweza kueleza kilichomtoa kwake Magomeni Mikumi na kuja kuogelea kwa mara ya mwisho Magogoni.

Ilikuwa dhahiri kuwa aliuawa.

Jambo hilo lilimfanya Inspekta Kombora na wenzake wazidi kuamini kwamba kulikuwa na namna katika ajali hizo zilizotokea katika miji mbalimbali ya Afrika huru. Juhudi zao za kutafuta chanzo na watendaji wa maafa hayo hazikuelekea kuzaa matunda yoyote zaidi ya hisia tu kwamba Afrika Kusini ilihusika. Hisia hizo ziliongezewa uzito na vitisho vilivyoletwa kwa njia mbalimbali zikitishia uhai wa maisha ya watu na nchi ambazo eti zingeendelea na msimamo wao wa kuibana Afrika Kusini. Licha ya kusababisha hofu na mashaka, vitendo hivyo, vingeweza kupunguza hamasa ya moyo wa kimapinduzi katika fikra za mashujaa endapo hisia hizo zingeachiwa kuendelea.

Ni hapo ndipo Kombora alipozikumbuka silaha zote na kutamani zielekezwe Afrika Kusini. Ni hapo pia alipowakumbuka mashujaa wote na kutamani waelekee Afrika Kusini. Na kati ya mashujaa hao jina la Joram Kiango lilitangulia kumjia akilini.

Hiyo ilikuwa baada ya kuwasiliana na wakuu wote wa vikosi maalumu vya upelelezi katika nchi zote zilizokwisha husishwa na maafa hayo ya kutatanisha. Walishauriana kuwa kila nchi ifanye juu chini kuhakikisha kisa cha maafa hayo kinafahamika na, ikiwezekana, maafa hayo yakomeshwe. Ndipo Kombora alipoanza kufanya kila juhudi. Tumaini pekee ambalo lilielekea kumpatia walao fununu, yaani yule askari mlinzi wa benki kuu, sasa lilikuwa limeuawa kwa hila. Harakati za kupeleleza nani alihusika katika kumuua hazikuzaa matunda yoyote. Hivyo, Kombora alijikuta hajapiga hatua yoyote katika jukumu hilo. Badala yake alijiona kama kiwete au mtu aliyepooza, ambaye anasubiri maafa ya moto unaomjia kasi.

“Joram lazima ashirikishwe,” Kombora alifoka kimoyomoyo.

Alikuwa na habari zote za Joram, kuwa tangu baada ya mkasa wa Salamu Toka Kuzimu aliiacha ofisi yake na kuanza maisha ya kipuuzi katika mahoteli na mabaa, akijistarehesha na yule msichana mzuri wa Arusha. “Yeye si mtu wa kuupoteza muda wake katika mabaa. Kipaji chake kinahitajika sana katika vita hivi. Lazima apatikane.”

Alimtuma mtu ambaye alizunguka katika hoteli kubwakubwa na kumpata Joram. Lakini, kama Kombora alivyotegemea, majibu ya Joram yalikuwa ya kijeuri kiasi kwamba mtu huyo alijiona mjinga na kurudi akiwa amechukia, jambo ambalo jioni hii lilimfanya Inspekta Kombora ayavue magwanda yake na kuvaa mavazi ya kawaida, kisha akajitoma katika ukumbi wa hoteli ya Embassy ambamo aliambiwa kuwa Joram alikuwamo.

Akiwa mtu ambaye halewi kwa urahisi, tunaweza kusema kuwa Joram alikuwa amechangamka pale Kombora alipoikaribia meza yake na kuomba kuketi.

“Karibu sana Inspekta, karibu uketi,” alisema kwa uchangamfu huku akimwita mhudumu wa hoteli hiyo. “Leo naweza kusema kuwa ni siku tukufu sana kwangu kutembelewa na Inspekta Mkuu. Habari za siku nyingi mzee?”

“Polepole kijana,” Kombora alisema. “Wanasema siku hizi hata kuta zina masikio”.

“Kwani kuna lolote la siri tunaloongea mzee? Siku hizi mambo yote ya siri nimeachana nayo. Nimeamua kuwaraia mwema na mtulivu kama ulivyokuwa ukinitaka niwe,” Lilikuwa jibu la Joram.

Kombora hakutia neno. Akamgeukia Nuru na kumsalimu, “Bila shaka huyu ndiye yule dada ambaye alikuwa na balaa la kulazimishwa kushirikiana na yule mwuaji aliyekusudia kuwaangamiza viongozi wengi wasio na hatia?” Joram na Nuru waliitika kwa vichwa. “Ni msichana shujaa sana. Msichana wa kawaida angeweza kupoteza kichwa chake mara baada ya kukabiliwa na mkasa mkubwa kama ule,” alimaliza akipokea kinywaji chake na kuanza kunywa.

“Sivyo mzee,” Nuru alijibu. “Kila nikifikiria kile kitendo naona aibu kubwa sana. Nisingestahili kukubali kulazimishwa kushiriki katika mauaji ambayo yangekuwa ya kinyama kama yale. Ingawa yule jasusi Proper alilaghai kuwa ungekuwa mzaha wa kawaida, lakini bado sikustahili kuafikiana naye. Uzalendo wangu ulitiwa dosari na kitendo kile. Najaribu kutafuta nafasi ya kuudhihirishia moyo wangu, lakini sijafanikiwa…”

“Joram ananinyima nafasi hiyo!” Nuru aliongeza baada ya kusita kidogo.

“Ni hilo tu ulilotaka kusema Nuru,” Joram alidakia. “Na hata Inspekta nadhani amefuata kujadili hilo. Sivyo mzee?”

Inspekta aliimeza bia iliyokuwa kinywani mwake. Kisha akajibu, “Kiasi ni kweli kuwa niko hapa kujadili hilo, kiasi siyo kweli.” Alisita kidogo na kuendelea,”Unajua hatujaonana kwa muda mrefu? Tangu ulipoondoka Arusha kwa hasira baada ya kuitupa bastola yako hatujaonana. Nilifika katika chumba cha dada huyu nusu saa baadaye na kuukuta ubongo ule na bastola. Nilidhani umemwua wewe. Lakini bastola yako haikuwa imefyatuliwa hata risasi moja. Mara kikatokea kile kitabu ambacho kilinifanya nielewe yote yaliyotokea. Ndipo nikaelewa kwanini umekasirika na kuamua kuwa mnywaji”.

“Niite mlevi, Inspekta, sijali.”

“Hapana. Wewe si mlevi na wala huwezi kuwa mlevi. Ni mnywaji tu, mnywaji ambaye hanywi kwa ajili ya kupenda kunywa, isipokuwa kwa ajili ya hasira baada ya kunyang’anywa fursa ya kuitia risasi kwa mkono wako katika kichwa cha yule mshenzi. Sivyo Joram!” Kombora alitulia akimtazama Joram. Mara akakumbuka kuwa alikuwa hajavuta sigara kwa muda mrefu. Akatoa moja na kuiwasha baada ya kuwataka radhi jirani zake.

“Kuacha hadhi yako ipotee kwa ajili ya kukosa nafasi ya kumwua mtu mmoja tu duniani!” Kombora aliendelea, “Sioni kama ni haki. Ziko nafasi nyingi za kufumua vichwa vya watu wenye haki kabisa ya kufumuliwa. Hati maalumu inatayarishwa ambayo itakuruhusu kufanya lolote kama afisa yeyote wa usalama mwenye jukumu maalumu. Zaidi kimetengwa kifungu maalumu cha fedha ambacho kitaingizwa katika akaunti yako ili pesa zisiwe kipingamizi…”

“Taratibu Inspekta,” Joram alimkatiza. “Vipi? Mbona mnanitendea mema mengi hivyo? Kama sikosei unachotaka kusema ni kwamba unaniomba nishiriki katika kutafuta kiini cha maafa haya yanayotendeka katika nchi za mstari wa mbele. Na kama sikosei mtu uliyemtuma kwangu amekupa majibu yangu rasmi, msimamo wangu ni uleule. Na utaendelea kuwa uleule. Kama mlimfahamu Joram ambaye alikuwa mpenzi wa Tanzania na Afrikakwa ujumla, lazima muelewe kuwa Joram huyo amekufa. Aliye hai, mbele yako, ni Joram mpya, Joram ambaye wala hana kiu ya kushiriki kwa njia moja au nyingine katika masuala yoyote ya nchi. Aliyeko mbele yako ni Joram wa mastarehe, Joram wa kutumia. Hata dada yangu Nuru hapa nadhani anaelewa.”

Ndipo Kombora alipoona ugumu wa kazi iliyokuwa mbele yake. Kumshawishi Joram ilikuwa sawa na kulilazimisha jabali lielee juu ya maji. Akiwa mtu ambaye hakuzowea kuwabembeleza binadamu wengine, hasa wanaume, Kombora alisema kwa sauti iliyoficha hasira na unyonge, “Pengine unajua unachokifanya. Lakini nadhani hujui kiwango gani cha madhara yanayolikaribia taifa hili endapo tutashindwa kuukomesha uovu huu unaonyemelea. Niruhusu nikusimulie mambo ya kutisha ambayo hayajavifikia vyombo vya habari.”

“Haitasaidia,” Joram alimjibu. “Utaupoteza bure muda wako. Ninachohitaji kusikia ni habari za burudani tu. Kama kuna burudani mpya ambayo sijaiona, kinywaji kipya ambacho sijakinywa au muziki mpya ambao sijausikia, nitafurahia endapo utanisimulia. Juu ya vifo vya marais na raia wenye hatia na wasio na hatia, si kazi yangu tena.”

“Hata hivyo, sauti yako haifanani kabisa na madai yako Joram. Kuna watu ambao silika yao ni kukesha katika mabaa na madansi, wewe si mmoja wao. Kuna wanaostarehe kusubiri maafa ya kusikitisha, wewe si mmoja wao, Joram. Kuna wanaofurahia ladha ya pombe na utamu wa muziki zaidi ya kazi na ushujaa, wewe si mmoja wao vilevile.”

“Zamani, Inspekta. Sasa hivi mimi ni mmoja wao na nitaendelea kuwa mmoja wao. Na kama huna maongezi mengine zaidi ya haya mzee nitashindwa kuendelea kukusikiliza,” Joram alimaliza akitoa sigara yake na kuiwasha.

Kombora hakujua afanye nini ili amshawishi Joram. Alimtazama Nuru kama aliyehitaji msaada wake. Akayaona macho yake mazuri yaliyojaa huzuni katika hali ya kukata tamaa. Hilo, kiasi lilimfariji Kombora. Alifahamu kuwa anaye msaidizi ambaye angesaidia katika juhudi zake za kumrejesha Joram Kiango katika dunia ya Joram Kiango. Akiwa si mgeni katika dunia hii Kombora alielewa kuwa mwanamke mzuri ni silaha. Hivyo, akamtupia Nuru jicho la kumtaka aelewe kuwa anautegemea msaada wake. Kisha akainuka na kuaga bila ya kumaliza kinywaji chake.

“Hukufanya vizuri, Joram,” Nuru alimwambia.

“Mfuate mkafanye vizuri”.

“Sivyo, sikia…”

Nuru akavunjika moyo. Uchungu mkubwa ukamwingia rohoni. Akajilazimisha kuendelea kunywa pombe, lakini haikumuingia. Baada ya jitihada nyingi alimtaka Joram radhi, akaondoka kutangulia chumbani kwao.

"SAMAHANI, naweza kuketi hapa?" mtu mmoja alisema akimsogelea Joram mara tu Nuru alipoondoka.

Alikuwa mtu wa umri wa kati. Sura yake ilionyesha dalili zote za kutosheka, macho yake yakionyesha kila dalili ya kuelemika. Kiasi alionekana kama ambaye pombe ilianza kumshinda nguvu, japo alitembea kwa uhakika.

Joram alimtazama kwa makini kabla ya kumjibu, "Una haki ya kukaa popote. Nchi huru hii."

"Asante," mtu huyo alijibu huku akijibweteka kitini. Baada ya dakika mbili tatu za kunywa na kuvuta kwa utulivu alimgeukia Joram na kumwambia, "Samahani. Sinabudi kulitoa dukuduku langu. Siku zote nimekuwa na hamu ya kuipata fursa hii ya kuketi nawe meza moja. Kama sikosei u Joram Kiango."

Joram alimtazama mtu huyo kwa makini. Alipochelewa kumjibu mgeni wake aliendelea, "Tumekuwa tukikutana mara kwa mara katika majumba ya starehe. Kilichonifanya nikufahamu ni msichana huyo mzuri unayefuatana nae. Kwa kweli, sina budi kukupa pongezi zako. Wazuri nimewaona wengi, wa aina yake sikupata kumwona. Ulimpataje yule dada, Joram?"

Jambo moja lilimvutia Joram katika kumsikiliza mtu huyu. Jambo la pili lilijitokeza. Sauti. Ilikuwa sauti ya kawaida, ikizungumza kiswahili cha kawaida katika masikio ya watu wa kawaida. Lakini katika masikio ya Joram Kiango, Joram ambaye sasa alikuwa amekaa chonjo, sauti hiyo ilificha uhalisia fulani.

"Unadhani una haki gani ya kunifahamu, na kumfahamu msichana wangu hali mimi sikufahamu hata kidogo?" Alimwuliza.

Kama ambaye alilitegemea jibu hilo mgeni huyo alijibu mara moja, japo kwa kusitasita, "Mimi! kwa jina naitwa Ismail Chonde. Ni mfanyabiashara wa siku nyingi. Nimezaliwa na kukulia hapahapa ingawa siku hizi naishi Nairobi."

"Na unawezaje kunifahamu kwa urahisi kiasi hicho?"

"Nasoma vitabu, nasoma magazeti. Hakuna asiyekufahamu Joram." Sauti iliendelea kuwa na walakini katika hisia za Joram. "Inaelekea bado una maswali uliyotaka kuniuliza bwana Chonde. Nataka kumuwahi huyo msichana unayemwita mzuri".

"Kweli. Inaonyesha aliondoka hapa akiwa amechukia."

Joram alitabasamu. "Naona umeona mengi zaidi ya hilo."

"Ndiyo, nimeona na kusikia mengi. Kwa kweli, endapo hutaniona mlevi, nilichokusudia kuongelea ni yule mzee aliyekuacha muda uliopita. Namfahamu yule. Ana madaraka makubwa serikalini. Kama sikosei alikuwa akikushawishi utoe mchango wako katika kupeleleza matukio haya. Na niliona akiondoka bila furaha. Yaelekea umemkatalia. Hivi kweli umekataa katakata?"

Joram alimtazama kwa makini zaidi. "Sielewi maswali yako yanaelekea wapi," baadaye alisema.

"Inashangaza," Chonde aliongeza. "Joram ninayemfahamu mimi hawezi kuipoteza nafasi nzuri kama hii ya kuonyesha ushujaa wake. Afrika iko katika mashaka makubwa. Watu wanakufa hovyo. Majumba yanalipuka hovyo. Bara zima liko mashakani. Joram ninayemfahamu mimi angeitoa hata roho yake kujaribu kupambana na hali hii."

Joram aliipima sauti hiyo, akiilinganisha na uso wa msemaji. Ingawa aliongea kama mtu mwenye uchungu kwa nchi na bara lake, bado hisia fulani zilimfanya Joram aone kitu kama kebehi katika macho yake, kama kwamba alikuwa na hakika kuwa Joram na U Joram wake wote asingeweza kufanya lolote. Wazo hilo lilimuongezea Joram hamu ya kuendelea kumsikiliza.

“Bado sijaelewa unalotaka kusema,” alichochea.

“Sidhani kama wewe ni mzito wa kuelewa kiasi hicho.”

Wakatazamana, kila mmoja akimsoma mwenzake. Kisha Chonde aliangua kicheko kirefu kilichomwacha Joram akitabasamu. Baada ya kicheko hicho akaongeza, “Samahani endapo umeniona mhuni au mlevi. Sikuwa na nia mbaya zaidi ya kuzungumza nawe na kufahamiana. Kwa kheri.” Aliinuka na kuondoka akielekea maliwatoni. Mwendo wake ulikuwa wa kilevi zaidi ya sauti yake.

Joram aliendelea kunywa taratibu. Alipomwona rafiki yake huyo mpya akitoka nje ya hoteli na kusikia mlio wa gari likiondoka, akaenda mapokezi ambapo alimsalimu tena msichana aliyekuwa hapo na kumuuliza kwa upole, “Samahani dada. Hivi huyu bwana aliyetoka sasa hivi anakaa hoteli hii?”

“Yule, hakai hapa. Huwa anatokeatokea tu. Kila mara huja na msichana. Leo ndio kwanza nimemwona peke yake. Sijui wamekosana nini na msichana huyo, maana huyu bwana anaonekana pesa si moja kati ya matatizo yake,” msichana huyo alieleza.

“Pengine hawajakosana,” Joram alimchokoza.

“Wamekosana. Bila hivyo asingenikonyeza mara mbili.”

Joram alicheka. Maongezi hayo yalikatizwa kidogo kwa simu ambayo msichana huyo alikuwa akiijibu. Alipotaka kuanza tena maongezi iliingia simu nyingine. Ambayo msichana huyo alionekana kuifurahia zaidi. Alizungumza kwa furaha huku akitabasamu. Baada ya kutoa chombo cha kuongelea alimgeukia Joram na kusema, “Unaona? Nimekwambia leo hana mtu. Ananiambia nikimaliza kazi nimkute hoteliya New Africa, chumba namba 104.”

“Ndipo anapokaa?” Joram alihoji.

“Bila shaka.”

Baada ya mazungumzo hayo Joram aliirudia meza yake na kuendelea kunywa. Mawazo yake yalimfikiria Chonde. Hakuelewa dhamira ya maongezi yake yote yale ilikuwa nini hasa. Alishuku kuwa pengine alikusudia kupata undani wa Joram na uamuzi wake. Kwanini? Zaidi Joram alishuku kuwa mtu huyo hawakukutana kuzungumza kiajaliajali, bali alikuwa akimfuata yeye au Kombora kwa ajili hiyo. Juu ya yote hayo zile hisia za Joram katika sauti ya mtu huyo zilizidi kujiimarisha akilini mwake. Aliona kama ulikuwemo walakini fulani katika sauti ya kiswahili chake ambao uliutia dosari Utanzania wake. Hayo na kile alichoona katika macho ya mtu huyo vilimtia Joram hamu ya kumfahamu vizuri.

Hivyo, dakika tano baadaye alijikuta mitaani akielekea New Africa. Alipofika hapo alimwendea mfanyakazi wa mapokezi na kujitia akizungumza naye hili na lile huku macho yake yakiwa kazini kutazama endapo ufunguo wa chumba namba 104 ulikuwepo. Aliuona. Akauliza juu ya mtu wa chumba fulani ambacho aliona ufunguo wake haupo.

“Yuko ndani. Ameingia sasa hivi.”

“Ngoja nikamwone.”

Badala ya kwenda chumba hicho, Joram alipanda gorofani hadi chumba namba 104 ambacho kilikuwa kimefungwa. Kuacha kwake tabia ya kutembea na bastola hakukumfanya aache kutembea na vifaa vyake vidogovidogo, kama funguo malaya ambazo hazishindwi kuifungua kufuli yoyote ya kawaida. Hivyo, kitasa hicho cha mlango wa Chonde kilimpotezea nusu dakika tu.

Chumbani humo, Joram aliurudisha mlango na kuufunga kwa ndani. Kisha aliangaza huku na huko kwa makini. Kilikuwa chumba cha kawaida kama vilivyo vyumba vingine vya hoteli. Hivyo, Joram hakuwa na kazi ngumu zaidi ya kupekuwa magodoro na viti. Hakuona chochote. Ndipo alipoliendea Kabati na kulifungua. Ndani ya kabati hilo mlikuwa na sanduku kubwa ambalo pia Joram alilifungua. Mlikuwa na pesa za kutosha pamoja na mavazi. Vitu hivyo havikumvutia. Macho yake yalivutiwa na makaratasi mbalimbali ambayo aliyapekua kwa makini. Mengi yalikuwa makaratasi ya kawaida ambayo yalimwezesha kumfahamu mtu wake kuwa aliitwa Afith Chonde. Baada ya kupekuwa zaidi aliipata hati yake ya usafiri. Aliifunua harakaharaka huku akisoma mihuri mingi iliyopigwa katika hati hiyo kuonyesha nchi Chonde alizozitembelea. Alikuwa anatembea sana. Mihuri ya Nairobi, Lagos, Lusaka, Harare, London, New York, Hong Kong, Tripol n.k ilionekana waziwazi. Hilo lilimfanya Joram azidi kuvutiwa na mtu huyo. Hakuonekana kama mfanyabiashara mkubwa kiasi hicho. Zaidi ya vipindi alivyokuwa akitumia mji hadi mji vilikuwa vifupi mno kiasi kwamba Joram alishuku kuwa hakuwa akifanya biashara za kawaida. Hivyo, akaongeza umakini katika upekuzi wake.

Kama alivyotegemea, Joram aliigundua mifuko ya siri katika begi hilo, mifuko ambayo maafisa wa forodha wasingeweza kuipata bila ya ujuzi maalumu. Katika mifuko hiyo, Joram alipata bastola moja aina ya revolver, maandishi mbalimbali ambayo alijaribu kuyasoma hakagundua kuwa hawezi kwani yaliandikwa kimafumbomafumbo katika hali kamili ya kijasusi. Pamoja na kijaluba kidogo cha chuma ambacho kilikuwa kimefungwa kwa ufunguo. Kijaluba hicho kilimvutia Joram zaidi. Alihisi kuwa kilikuwa kimeficha mengi zaidi ya yale aliyokwishayaona. Hivyo, akaanza kuzijaribu funguo zake malaya. Zilimchukua dakika kadhaa kugundua kuwa kamwe asingeweza kukifungua kijisanduku hicho. Kilitengenezwa maalumu kupambana na hila zozote za kufunguliwa pasi ya utaalamu wa mwenyewe. Kiu ya Joram juu ya kumjua vyema mtu huyu ikazidi kuneemeka. “Vipi awe na kisanduku kama hicho? Kilificha nini? Na maandishi haya ya siri yanasema nini? Siyo bure. Liko jambo,” aliropoka.

“Ndiyo. Kuna jambo,” sauti ilizungumza nyuma ya Joram. Akageuka hima na kukutana na uso wa Chonde ambao ulikuwa ukimtazama kwa kebehi. Alikuwa kaketi juu ya kochi. Alivyoingia chumbani humo kwa ukimya kama jini na kuketi kwa utulivu kwa kipindi chote hicho ni jambo ambalo lilizidi kumwongezea Joram ushahidi kuwa alikuwa hachezi na binadamu wa kawaida. Joram akageuka na kumtazama Chonde huku akiruhusu moja ya zile tabasamu zake za kishujaa, tabasamu ambalo lilifuatwa na sauti yake tulivu akisema, “Tuseme nimefumaniwa”.

“Umefumaniwa. Na una bahati mbaya kuwa umefumaniwa na kifo. Binadamu hanichezei mimi na akaendelea kuishi,” Chonde alisema akianza kuinuka taratibu. “Ulijifanya umeacha maisha yako ya kuingilia mambo yasiyokuhusu. Kumbe ulikuwa ukijifurahisha kwa kujidanganya mwenyewe. Umekosea sana.” Akamtazama kwa dharau na kebehi. “Huwa nafurahia zaidi kuwaua watu wangu kwa mikono,” alisema akizidi kusogea.

Mzaha haukuwemo katika macho na sauti ya Chonde. Alionekana mtu anayejua anachokifanya, jambo ambalo lilimfanya Joram asogeze mkono kuiendea ile bastola ambayo ilikuwa imelala kando yake. Kama alikuwa ameuhisi wepesi wa Chonde basi alikuwa hajauona. Mara tu mkono huo ulipoifikia bastola tayari mguu wa Chonde ulitua juu ya mguu huo. Wakati huo huo Joram alipokea ngumi mbili ambazo zilizomfanya apepesuke na kuisahau bastola. Chonde hakuwa na roho mbaya kiasi hicho. Alimpa muda wa kujiandaa. Joram akavuta pumzi kwa nguvu na kuanza kumwendea Chonde. Alimshitua kwa mkono wa kulia, Chonde aliudaka na wakati huohuo kumkata Joram judo ya mgongo ambayo ilimfanya aanguke kifudifudi. Alipoinuka Chonde alikuwa akimsubiri huku akicheka, “Wanasema Tanzania kuna mtu mmoja tu wa kujihadhari nae, ambaye anaitwa Joram Kiango. Niko naye chumbani, sioni Ujoram wake.”

Maneno hayo yalimwuma Joram zaidi ya kipigo alichopokea. Akainuka ghafla na kumwendea Chonde akitumia mitindo yake yote ya kupigana. Vipigo kadhaa vilimpata Chonde. Lakini kwa jinsi vipigo hivyo vilivyopigwa kwa hasira havikuwa na madhara makubwa kwa Chonde. Dakika chache baadaye Joram alijikuta chali sakafuni, kasalimu amri. Chonde akaendelea kutabasamu.

Sasa Joram alimtazama Chonde kwa mshangao zaidi ya hasira. Ni mtu wa aina gani huyu anayeweza kumwadhibu kama mwanae? Bila shaka si mtu wa kawaida. Amejifunza mengi kama anavyoonekana kujua mengi. Pamoja na kwamba kipindi kirefu kilikuwa kimepita bila ya Joram kufanya mazoezi ya viungo wala akili, pamoja na kule kuzoea starehe za mahotelini na ulevi mwingi, bado hakuona kama binadamu yeyote angekuwa na haki au uwezo wa kumfanya apendavyo kama Chonde alivyokuwa amemfanya.

Ile hamu iliyokuwa imelala usingizini ikaibuka upya katika moyo wake, hamu ya mapambano, vitisho, maafa, damu, na mikasa, hamu ya kuwatia adabu watu wanaopenda kuwafanya vibaya binadamu wenzao. Chonde alionekana kama mmoja wao. Joram akamtazama tena na kutabasamu kwa uchungu huku akisema, “Haya, umeshinda. Kinachofuata?”

“Kifo chako,” Chonde alimjibu kijeuri. “Siwapendi vijana watundu kama wewe. Kufa, huna budi.”

“Kosa langu.”

“Unapenda kufa?”

Joram alifikiri kwa makini angefanya nini kuiahirisha hukumu hiyo ya kifo. Muda. Alihitaji muda ili ikiwezekana itokee njia moja au nyingine ya kuyaokoa maisha yake. Akaanza maongezi kwa sauti ambayo aliifanya dhaifu kuliko ilivyokuwa, akimwuliza Chonde hili na lile. Chonde alikuwa mgumu wa kutoa habari kama jabali. Kati ya maneno ya kashfa na matusi kwa Joram, nchi na bara zima hakutamka neno lolote ambalo lilimfanya Joram amjue yeye ni nani na anafanya nini katika ulimwengu wa ujasusi. Alichoambulia ni zile hisia tu kwamba Chonde hakuwa raia wa kawaida.

"Umeahirisha sana kifo chako," Chonde alisema baadaye kama aliyekuwa akizisoma fikra za Joram. "Sasa iliyobaki ni kazi ndogo ya kukutoa uhai. Nitakuua kwa mkono wangu wa kushoto. Maiti yako itaokotwa kesho ikiwa imevunjikavunjika kama mtu aliyeanguka toka ghorofani. Kwa jinsi ulivyobadilika kitabia watu hawatashangaa kusikia kuwa umejirusha dirishani."

Baada ya maneno hayo, aliinuka na kumwendea tena Joram kwa utulivu kama awali, lakini macho yake yalitangaza kitu kimoja tu, kifo.

Joram alijiandaa, akijua kuwa vita vilivyokuwa mbele yake vilikuwa vikubwa kuliko vyote alivyowahi kupambana navyo, vita vya kuitetea roho yake. Akaikusanya akili yake yote na kumsubiri Chonde kishujaa.

Mara mlango ukagongwa.

Chonde aligutuka kwa mshangao na kuutazama mlango huo. Joram hakuipoteza nafasi hiyo. Aliruka na kuufanya mguu wake utue katika shingo ya Chonde. Lilikuwa pigo ambalo Chonde hakulitegemea. Likamtia mweleka. Lakini pigo la pili alilitegemea, akalikwepa na kuachia judo ambayo Joram aliikinga. Papo hapo mlango ukagongwa tena na kufunguka ukiruhusu sura ya msichana mzuri kuingia.

Alikuwa yule msichana wa mapokezi wa hoteli ya Embassy. Alitokwa na macho ya mshangao kuona miili yenye jasho, michubuko na damu, ya wanaume hao, ikiwa tayari kuvamiana. Wote walimtazama msichana huyo, Chonde akimlaani, Joram akimshukuru. Akiwa kama hajui lipi la kufanya msichana huyo aliduwaa mlangoni, Mdomo wazi.

"Karibu ndani. Tulikuwa tukifanya mazoezi ya viungo na huyo rafiki yangu," Chonde alimhimiza akivaa tabasamu ambalo lilificha kabisa mauaji yaliyokuwa katika uso huo dakika iliyopita. "Karibu ndani. Nawe ndugu yangu nenda zako sasa. Tutakutana siku nyingine".

Joram aliyarekebisha mavazi yake na kutoka chumbani humo taratibu. Hakuwa amesahau kumwachia msichana huyo tabasamu jingine la shukrani.

"Nadhani hakuna njia nyingine zaidi ya kumlazimisha," Kombora alikuwa akifoka katika kikao cha dharura kilichofanyika usiku huo. "Hawezi kuachwa aendelee kustarehe katika mabaa huku taifa na bara zima likiwa mashakani. Mchango wake unahitajika."

Kikao hicho kilihudhuriwa na viongozi wote wa ngazi za juu katika idara zote za usalama nchini. Kiliitishwa ghafla baada ya kuokotwa barua moja ya vitisho katika ofisi ya Waziri Mkuu, barua ambayo iliandikwa kwa ufupi sana ikidai kuwa ajali za kimiujiza zingeendelea kuipata nchi ya Tanzania na zote zilizo mstari wa mbele, endapo serikali isingechukua hatua za haraka kukomesha msimamo wake wa kupinga utawala wa kibaguzi wa Afrika Kusini. Barua hiyo iliongeza kwamba safari hii moto ungeiteketeza hospitali ya Muhimbili, hoteli ya Kilimanjaro, Jengo la Kitega Uchumi na baadae Ikulu.

Aliyeiokota barua hiyo na kuisoma aliwaonyesha wakubwa wake ambao waliikabidhi kwa Waziri Mkuu. Baada ya kuisoma yeye pia, alikwenda Ikulu ambako alimpa Rais.

"Upuuzi ulioje huu. Hatutaacha kuwatetea ndugu zetu wanaoteswa bila makosa kwa ajili ya vitisho hivi. Havikuanza leo. Wala haviwezi kwisha leo. Tutapigana hadi mtu wetu wa mwisho katika kuilinda hadhi ya mtu mweusi katika bara letu hili." Pengine Rais alijibu hivyo akifoka kwa hasira. "Barua hiyo wakabidhi watu wa usalama. Nadhani hawatakubali kuendelea kuchezewa kiasi hiki. Waambie kwamba hatutaki upuuzi wowote ulioandikwa katika waraka huu haramu utokee." Huenda Rais aliongeza hayo.

Hakuna aliyeshiriki katika maongezi yao ya faragha, isipokuwa hisia hizo zinakuja kwa jinsi Waziri Mkuu alivyomwita Inspekta Kombora katika ofisi yake na kumkabidhi barua hiyo. Baada ya Kombora kuisoma kwa makini Waziri Mkuu alimwambia, "Ni barua ya khatari sana. Na imeandikwa na watu khatari, watu wenye kichaa. Kufuatana na hali ilivyo hatuwezi kukubali kuwa watumwa au mateka wa Makaburu kwa kuhofia ukatili wa vitisho vyao. Lazima tupambane nao ana kwa ana kama tunavyopambana nao katika uwanja wa mapambano. Tuliwashinda

Msumbiji, Angola na Zimbabwe. Kwa nini tusiwashinde Namibia na Afrika Kusini? Tutawashinda. Wao wanajua hivyo, ndiyo sababu inayowafanya wakimbie toka katika uwanja wa mapambano na kuja huku kupigana kiuoga."

"Kama tulivyoshuku kitambo, mikasa hii haikuwa ya kawaida. Kulikuwa na mkono wa mtu, mkono wa mtu huyu ambaye ameandika barua hii na kuthubutu kuipenyeza katika ofisi yangu. Ingawa haijafahamika mbinu gani wanatumia kuweza kuanzisha mioto hii, nadhani hutashindwa kufanya juu chini ili uugundue na kuukomesha kabisa upuuzi huu."

Akijua uzito wa jukumu hilo ndipo Kombora aliporudi ofisini na kuitisha kikao hiki kilichokuwa kikiendelea. Walijadiliana kwa mapana na marefu kulikuwa na nini hasa hata majumba yalipuke moto ilihali uchunguzi kamili ulionyesha kuwa haikuwepo kasoro yoyote ya umeme. Hawakupata jibu. Walijaribu kuzijumuisha taarifa zote za upelelezi juu ya nani anaweza kuwa alihusika katika kusababisha mioto hiyo lakini bado hazikuwepo dalili zozote zilizoleta matumaini. Wakapanga mipango mipya. Wakawaandaa wapelelezi na vyombo kadha wa kadha katika majumba yaliyotajwa. Wakawekwa watu katika mahoteli, viwanja vya ndege na vituo vyote vya usafiri kuchunguza nani anaingia, nani ametoka na ameleta nini. Zaidi ya yote hayo, ndipo lilipotolewa tena pendekezo la kumshirikisha kila mtu mwenye uwezo wa kuchangia katika upelelezi. Hapo ndipo jina la 'Joram' lilipowatoka midomoni. Ikawashangaza wajumbe kusikia kuwa hata baada ya kuombwa na Kombora alikataa katakata kushiriki katika kazi hiyo. Joram waliyemfahamu alikuwa hangoji kuombwa au kutumwa bali alijituma. Vipi Joram huyu?

Ndipo mzee Kombora alipoibuka na uamuzi wa kumshurutisha. "Lazima tumlazimishe. Kama ameacha upelelezi kwa ajili ya mwanamke, basi atarudia upelelezi kwa ajili ya mwanamke. Yote hayo niachieni mimi," Inspekta Kombora aliwaambia.

Baada ya kikao hicho, alimchukua msaidizi wake mmoja na kumpeleka chemba. "Sikia," akamweleza, "Nakutaka uwe msiri wangu, wewe peke yako. Unaweza kutunza siri?"

"Bila shaka. Isipokuwa ya wizi na mauaji tu."

"Hii si ya mauaji wala wizi. Nataka unisaidie kumteka mtu nyara."

"Kuteka mtu nyara? Hiyo mbona haiko mbali sana na wizi? Na kama sikosei ni hatari zaidi ya wizi."

"Ndiyo. Lakini mtu tunayemtaka atafurahi sana. Bado ni msichana mzuri sana," Kombora alivuta pumzi kwa nguvu kisha akaongeza, "Nataka tumteke yule msichana wa Joram. Hiyo ndiyo njia pekee ya kumlazimisha."

Baada ya kujadiliana kwa muda walielewana. Wakaandika barua ambayo ilikusudiwa iwe imetoka kwa mteka nyara akidai kuwa amemteka msichana huyo na angemwua endapo Joram angethubutu kujihusisha na upelelezi unaoendelea nchini dhidi ya maafa ya kutatanisha. Licha ya barua hiyo, pia waliandaa damu ambayo ilipatikana kwa msaada wa daktari mmoja wa hospitali yao Ocean Road ili waidondoshe chumbani humo kuonyesha kuwa kulikuwa na mapambano ambayo yalisababisha damu kumwagika.

"Tunacheza mchezo mchafu sana, mchezo wa aibu. Lakini hatuna budi," Kombora alisema baada ya matayarisho yote ya kwenda katika chumba cha Joram.

Uchunguzi uliwapa fununu kuwa Joram alikuwa akiishi katika hoteli hiyo ya Embassy. Habari za mwisho usiku huo zilieleza kuwa Joram alipoachana na Kombora usiku huo alikuwa peke yake akinywa bia wakati msichana wake alipoondoka kwenda chumbani, na kwamba baada ya muda mrefu Joram alionekana akitoka nje na hadi sasa alikuwa hajarudi. Kombora alitegemea kuwa muda huo ulitosha kumfikia msichana huyo, kumshawishi na akikataa, kumlazimisha kisha kuondoka naye kwa siri kabla Joram hajarudi.

Walifanya hivyo.

Waliifika hoteli na kukiendea chumba chake kwa siri kubwa. Mlango waliukuta ukiwa wazi. Wakaufungua na kuingia huku wakiufunga nyuma yao. Macho yao yalivutwa na dalili za vurugu katika chumba hicho. Vitu vilikuwa vimetupwa ovyoovyo, matandiko yakiwa yamepinduliwa na masanduku kufunguliwa. Juu ya meza kulikuwa na karatasi yenye damudamu. Upande wa pili wa karatasi hiyo kulikuwa na maandishi ambayo yalikuwa barua ya wazi kwa Joram Kiango, barua ambayo haikutofautiana sana na ile ambayo Kombora aliiandaa:

Ndugu Joram,

Tunayo furaha kukufahamisha kuwa tumemchukua msichana wako na tutakuwa nae hadi hapo tutakapomaliza shughuli zetu. Hii ni kwa ajili ya kukuonya usithubuti kujihusisha na mambo yoyote yanayoitokea nchi hii. Endapo utakuwa mtoto mtiifu kama ulivyo siku hizi, hatadhurika, nawe utakuwa salama. Vinginevyo, utakipokea kichwa chake kwa njia ya posta na kisha kitafuata kifo chako.

Amri

Kombora aliisoma tena barua hiyo, kisha akamgeukia msaidizi wake na kumnong'oneza, "Tumechelewa sana. Wenzetu wametuwahi." akampa barua hiyo ili aisome.

"Sasa tutafanya nini?" askari huyo aliuliza baada ya kuisoma.

"Rudisha kila kitu kama kilivyokuwa. Fanya hima tuondoke hapa haraka," alimhimiza akianza kusogea mlangoni.

"Nilidhani tungemsubiri Joram!"

"Hakuna haja. Akirudi atajua la kufanya." Wakatoka na kuifuata njia ya kawaida. Wakiwa katika mavazi ya kiraia, watu wachache sana waliwatupia macho zaidi ya mara moja. "Jambo moja la kupendeza ni kwamba," Kombora alikuwa akisema. "Wamemchokoza Joram. Hawamfahamu vizuri. Wataujutia uamuzi wao"

Joram alifika chumbani kwake dakika kadhaa baadaye. Akiwa mchovu, jicho moja likiwa limevimba kwa pambano lake na chonde, alipitiliza hadi bafuni ili ayaepuke maswali ya Nuru. Huko ndani alioga vizuri, akaisafisha damu yote na kushevu kikamilifu. Kisha akarudi chumbani ambako macho yake yalivutwa na vurugu iliyokuwa imetokea.

Alitazama vitanda vyote na kutoiona dalili ya Nuru. Akaenda mezani ambako hakushangaa kukuta ujumbe ule ukiwa juu ya karatasi yenye damudamu. Akausoma kwa makini, akiuchunguza mwandiko huo ambao ulikorogwa katika hali ya kupoteza uhalisi wake. Akatikisa kichwa na kutokwa na tabasamu jembamba.

Usiku huo alilala huku kalisahau tabasamu hilo katika uso wake.

SURA YA NNE

ASUBUHI hiyo, baada ya kuoga na kufungua kinywa, Joram alichukua simu na kupiga namba mbili tatu akitaka kuzungumza na rafiki zake wa zamani. Alipowapata aliwapa maekelezo fulanifulani kwa lugha ambayo wangeielewa wao tu. Baada ya hapo akajitokeza mitaani na kuanza matembezi. Akiwa kavaa vizuri suti yake ya kijivu aina ya three peace, kofia ikiwa imezifunika nywele zake ili kuficha mchubuko uliokuwa upande wa kushoto na miwani myeusi ikilificha jicho lake ambalo lilikuwa halijatii dawa kikamilifu, alionekana kama alivyotaka, mwungwana asiye na tatizo lolote mwilini wala akilini.

Msafara wake wa kwanza uliishia Barabara ya Sokoine katika tawi la Benki ya Taifa ya Biashara City Drive. Aliingia ndani na kuomba kuonana na meneja. Akaelekezwa hadi katika chumba ambamo alikaribishwa vizuri na afisa huyo ambaye uso wake ulimdhihirishia Joram kuwa hakuwa akiwajibika ili kuitikiwa wito bali kuwajibika kulikuwemo katika damu yake tangu alipozaliwa.

"Nikusaidie nini ndugu yangu?"

"Naitwa Joram Kiango. Ninayo akaunti hapa."

“Nakufahamu sana, ingawa ni mara yangu ya kwanza kukuona ukija huku kwetu. Mara nyingi unaishia huko huko kwenye pesa.” Baada ya kutabasamu kidogo kwa mzaha huo aliongeza harakaharaka. “Umefuata mkopo?”

“Hapana mzee,” Joram alimjibu. “Nikikopa nitashindwa kulipa. Ninachohitaji ni kutazama uwezekano wa kuweka mali yangu fulani ya thamani katika akaunti mnayoita Self-Custody. Ningependa mnifahamishe utaratibu ulivyo.”

Meneja alitikisa kichwa huku akisema, “Hilo tu? Kwanini wamekusumbua hadi huku? Utaratibu wake si mrefu sana. Ziko fomu maalumu ambazo utajaza. Baada ya hapo utakabidhiwa ufunguo mmoja, ufunguo wa pili tutakuwa nao. Utakwenda huko chini na kuhifadhi mali yako hadi siku ambayo utapenda kuikagua au kuichukua. Malipo yake ….”

Joram alimsikiliza kwa makini, akitupa swali moja moja. Kisha alimwomba meneja akatazame hali ilivyo huko chini kabla hajajaza fomu zozote. Meneja akainuka na kushuka nae hadi shimoni. Walipita vyumba vya kuhifadhi nyaraka, baadhi vinahifadhiwa pesa na kimoja alielezwa kuwa kiliazimwa na Benki Kuu baada ya jengo lao kuharibika kwa moto. Baada ya kupewa picha kamili ya ulinzi na usalama wa hifadhi hiyo Joram aliaga na kuahidi kuwa angerudi baadaye kukamilisha kazi hiyo.

Toka hapo Joram alipita hapa na pale akifanya hili na lile, sigara baada ya sigara zikiteketea mdomoni, mwendo wake ukiwa wa utulivu kama mtu asiye na tatizo lolote ulimwenguni. Ungemwona kamwe usingefikiria kama mtu ambaye usiku wa jana mpenzi wake alitekwa nyara, bila shaka baada ya kuteswa sana.

Ni hali yake hiyo ya utulivu ambayo ilimshangaza Inspekta Kombora alipokutana nae katika mtaa wa Samora. Kombora alisimamisha gari lake na kumfuata Joram kando ya duka alipokuwa kasimama. “Joram,” alisema baada ya kumsalimu. “Nasikia yule msichana wako ametekwa nyara”.

“Hata mimi nasikia hivyo,” lilikuwa jibu la Joram.

“Mbona hufanyi lolote.”

“Nifanye nini? Barua imenionya nisithubutu kufanya lolote. Vinginevyo, msichana wa watu atauawa. Unapenda afe, Inspekta?”

Kombora alitikisa kichwa kwa mshangao. “Joram niliyemfahamu mimi alikuwa hapokei amri kwa watu kama hao, hasa katika suala hili ambalo ni la uhai na kifo cha mtu na taifa zima. Mimi nilidhani wamekuchokoza. Nikategemea kuwa wangejutia uamuzi wao. Nilikosea?”

“Umekosea sana Inspekta. Joram unayezungumza naye si yule wa awali. Usishangae, Inspekta. Usiupoteze bure mshangao wako. Bado kuna mengi utayasikia juu ya Joram huyu ambayo yatakushangaza zaidi,” Joram alisema huku akitupa kipande kimoja cha sigara na kuwasha nyingine. Alipomuona Kombora kama mtu ambaye hajui la kufanya au asiyeyaamini masikio yake, akaamua kuondoka polepole. Kombora alimsindikiza kwa macho yake yaliyojaa mshangao na huzuni.

Baada ya pitapita hii ya hapa na pale, Joram alirejea chumbani kwake ambako alijipumzisha kwa muda.Wafanyakazi na baadhi ya wapangaji wenzake, ambao walikuwa wamemzoea Nuru, walimsumbua Joram kwa kutomuona.

“Anaumwa?”

“Hapana. Kapata safari ya ghafla.”

“Bila kuaga?”

“Ilikuwa ghafla.”

Aliujenga vyema uongo wake huo hadi ukafanana na ukweli. Jioni hiyo, baada ya kula, kuoga na kupiga simu nyingine alijitokeza mitaani na kuanza matembezi yake. Safari hii matembezi hayo yaliishia Ilala, nyumbani kwake. Alielekea chooni ambako alifunua mahala fulani pa siri ukutani na kutoa kijisanduku alichokuwa kakificha hapo. Alishangaa kukuta kikiwa kitupu bila ya bastola na risasi zake ambazo alikuwa ameziweka huko. Hifadhi hii ilikuwa siri yake binafsi. Mtu pekee ambaye aliifahamu siri hiyo ni Neema Idd ambaye sasa ni Marehemu. Mtu mwingine ambaye angeweza kufahamu ni Nuru. Uko usiku mmoja, kati ya zile chache ambazo waliwahi kulala katika nyumba hii, alimtoroka Nuru akidhani yuko usingizini, akaja hapa na kuisafisha bastola hii. Pengine Nuru aliwahi kumchungulia. Lakini Nuru huyo sasa yuko mikononi mwa wateka nyara. Nani mwingine aliyeijua siri hii? alijiuliza kwa hasira, hasira ambazo zilimfanya atupe kasha hilo na kutoka nje baada ya kuifunga milango yote kwa ukamilifu. Msafara huu uliishia katika hoteli ya Embassy. Akaagiza vinywaji na kuanza kunywa. Baada ya bia mbili akaenda kaunta kuzungumza na yule msichana wa mapokezi.

“Shem, za kutwa.”

“Nzuri sana, shemeji,” msichana huyo alizungumza kwa furaha huku akimtazama Joram kwa mshangao. “Pole sana shemeji,” aliongeza.

“Kwa?”

“Ule mchezo wa jana. Unajua mimi mpaka sasa siamini kama mlikuwa mnacheza tu. Nilidhani mlikuwa mnapigana. Yule bwana kashikilia kuwa ni mchezo tu”.

“Ulikuwa mchezo. Mazoezi ya viungo. Wazungu huita practice.”

“Mpaka mtoane damu?”

2

Tutarudi na Roho Zetu Sehemu ya Tatu

ILIPOISHIA TOLEO LILILOPITA

Nzuri sana, shemeji,” msichana huyo alizungumza kwa furaha huku akimtazama Joram kwa mshangao. “Pole sana shemeji,” aliongeza.

“Kwa?”

“Ule mchezo wa jana. Unajua mimi mpaka sasa siamini kama mlikuwa mnacheza tu. Nilidhani mlikuwa mnapigana. Yule bwana kashikilia kuwa ni mchezo tu”.

“Ulikuwa mchezo. Mazoezi ya viungo. Wazungu huita practice.”

“Mpaka mtoane damu?”

SASA ENDELEA

Hakujua Joram alivyoisherehekea habari hiyo. Alitupa maneno mengine mawili matatu, kisha akairudia meza yake. Akaendelea kunywa na kuvuta. Japo alionekana katika hali ya utulivu, lakini macho yake yalikuwa makini, yakimtazama kila anayeingia na kutoka. Aliwaona wengi. Na kati yao alikuwemo yule ambaye alihitaji kumwona.

Alikuwa rafiki au adui yake, Chonde. Aliingia na kuifuata meza ambayo haikuwa na mtu, akaketi. Mara tu Joram alipomwona akainuka na kwenda kupiga simu ambayo alizungumza maneno machache sana. Kisha alikirudia kiti chake na kumwita mhudumu ambaye aliombwa kuleta bia nne. Mhudumu huyo alipozifikisha chupa hizo Joram alimwelekeza azipeleke kwa Chonde. Kisha alitulia akimtazama Chonde alivyokuwa akibishana na mtumishi huyo kwa zawadi hiyo ambayo hakujua ilikotoka hadi alipoelekezwa na kumwona Joram. Akazipokea na kuanza kunywa.

Lakini baada ya dakika kumi meza ya Joram ilifurika kwa chupa kumi zilizoletwa na mtumishi yuleyule kwa niaba ya Chonde. Walitazamana kwa muda. Baada ya muda Chonde alihamia meza ya Joram.

“Za tangu jana?”

“Siyo mbaya.”

Wakaendelea kunywa kwa muda. Kila mmoja akimsoma mwenzake. Kisha Chonde alitokwa na kicheko chembamba. Joram aliungana naye kwa tabasamu dogo.

“Pole sana.”

“Kwa?”

“Yale ya jana.”

“Lilikuwa zoezi tu. Usijali.”

Kikafuata kimya kingine, kimya ambacho Joram alikivunja kwa kuanzisha maongezi ambayo Chonde alizungumza kwa uangalifu akiepuka lolote ambalo Joram alihitaji kufahamu juu yake. Pamoja na Joram kuzungumza kwa ujanja na hila za kila aina, bado Chonde alimfanya ajione mtoto sana katika dunia ya upelelezi na mzembe katika elimu ya saikolojia. Ni hapo alipozidi kuamini kuwa Chonde hakuwa mtu wa kawaida. Na kama alikuwa jasusi bado hakuwa jasusi la kawaida. Alikuwa zaidi. Jambo hilo liliongeza hasira za Joram dhidi ya mtu huyo. Amshinde vipi katika mapambano ya mwili na amshinde tena katika mapambano ya kiakili? Hata hivyo Joram hakujali sana, akijua kuwa dakika hii ambayo anaipoteza na Chonde, mahala fulani, yuko mtu ambaye anaifanya kazi ile ambayo yeye alishindwa kuifanya jana, kazi ya kufungua kile kijaluba cha Chonde na kuona kimehifadhi nini hata kilindwe kwa kiwango kama kile. Hivyo, akaamua kumruhusu Chonde aendelee kumlaghai na kumdhihaki.

“Mwanamapinduzi aliyekata tamaa,” Chonde alisema. “Aibu ilioje kukata tamaa hali nchi yako iko mashakani? Si ungejaribu kutoa mchango wako?”

Joram hakumjibu.

Kisha kama aliyekumbuka jambo Chonde alisema ghafla, “Nasikia msichana wako ametekwa nyara!”

“Umesikia wapi?”

“Kwani ulidhani siri?”

Hilo lilimshitua Joram. Alishangaa kuona mtu huyo alivyo mwepesi wa kupata habari. Baada ya kuisoma barua ile Joram hakuipeleka polisi wala kuchukua hatua zozote zaidi ya kutabasamu tu. Lililomfanya asifanye lolote hasa ni kule kuwa kwake na uhakika kuwa barua ile aliielewa zaidi ya mwandishi wake alivyotaka aielewe. Bila shaka mtu huyo alikuwa amezidokoa habari hizo kwa polisi. Jambo hilo lilimfanya azidi kumfanya Joram kuamini kuwa hakuwa mtu mwenye mkono mrefu tu bali alikuwa na masikio mapana.

Yeyote aliyeketi kando akiwatazama watu hawa wawili wakiongea angeamini kuwa ni kikao cha marafiki wa siku nyingi. Asingeamini kuwa yalikuwa kama maongezi baina ya Chatu na Mbwa, au baina ya Malaika Gabriel na Ibilisi.

Yule msichana wa mapokezi alikuwa mmoja kati ya watu walioamini hivyo. Alikuwa amewatazama kwa muda mrefu na kushuhudia wanavyocheka na kutabasamu, akayasahau mashaka yote aliyokuwa nayo juu ya urafiki wao na kuamini kuwa pambano la jana lilikuwa zoezi la viungo. Hivyo, alizama katika shughuli zake na kuwatupia jicho mara moja moja.

Chonde alikuwa akifunua mdomo kuongea kitu wakati saa yake ilipotoa mlio ambao haukuwa wa kawaida. Ulikuwa mlio wa sauti nyembamba sana, ulimfikia Joram kwa mbali sana. Chonde aliitazama saa hiyo kwa utulivu, kisha alimtazama Joram kwa makini zaidi. Dakika mbili baadae aliendelea kunywa kwa utulivu. Dakika ya tatu aliinuka na kuaga kuwa anaelekea msalani. Joram alisubiri dakika tano, kisha akamfuata. Hakumkuta. Akafahamu kuwa mlio katika saa ya chonde ulikuwa ishara ambayo ilimkumbusha kitu fulani, jambo lililomfanya Joram kuhofia mtu wake ambaye wakati huu alikuwa katika chumba cha Chonde. Hivyo, akakiendea kibanda cha simu na kuzungusha namba za simu za chumba hicho. Haikupokelewa. Toka kwenye simu, Joram alitoka nje ya hoteli na kukodi gari ambalo lilimpeleka New Afrika. Akajipenyeza kwa hila hadi ghorofani, mbele ya chumba hicho. Akatega sikio na kusikiliza kwa makini. Chumba kilikuwa kimya kabisa. Ukimya huo ulimtisha sana. Aliyaamini sana masikio yake. Na kwa vyovyote alitegemea kuwa na mtu chumbani humo. Akasikiliza kwa makini zaidi. Bado hakusikia chochote. Akaufungua mlango taratibu na kuchungulia.

Macho yake yalivutiwa na mtu aliyelala chali juu ya sakafu utumbo wake ukiwa nje, macho yake yakidhihirisha kuwa roho ya mtu huyu pia ilikuwa nje. Kabla Joram hajajua kuwa ilimpasa kuingia chumbani humo au la, sauti nzito aliyoifahamu sana ilimhimiza ikisema, “Usiogope. Karibu ndani.”

Msemaji alikuwa kajificha nyuma ya mlango, bastola kubwa ikiwa mkononi mwake ikimtazama Joram kwa uchu.

“Ingia na ufunge mlango. Nadhani hutapenda kufia hapo mlangoni kama paka. Njoo ndani ufe kistaarabu kidogo.”

Joram akaingia. Hakujishughulisha kumtazama Chonde aliyesimama nyuma ya mlango na bastola yake. Badala yake alimtazama marehemu na kushuhudia alivyouawa kinyama. Tumbo lake lilikuwa limebomoka kwa kitu ambacho hakikuwa risasi wala kisu. Bila shaka ulikuwa mlipuko wa bomu. Kifo hicho kilimsikitisha sana Joram. Huzuni ikamshika. Kwa huzuni hiyo alimgeukia Chonde na kufoka kwa hasira akisema, “Shetani mkubwa. Kwa nini umemwua mtu huyu asiye na hatia?”

“Ni wewe uliyemwua,” Chonde alimjibu Joram.

“Mimi! Nimemwua vipi?”

“Usijifanye hufahamu. Bila shaka ni wewe uliyemtuma kuifanya kazi ile ambayo mwenyewe ilikushinda. Kazi ya kujua katika kisanduku hicho mna nini. Nami nikifahamu kuwa pamoja na kukuadhibu, kama nilivyokuadhibu usiku wa jana usingekata tamaa ndipo niliamua kutega bomu dogo kando ya kisanduku hicho. Wakati huohuo mtu yeyote anayekigusa saa yangu inaniashiria. Hivyo tulivyokuwa tukinywa hapo hotelini nilishangaa kuona dalili za mtu.

“Nikafahamu kuwa mtu asiye na hatia anakufa. Nimemkuta kisha kata roho.” Akageuka kumtazama marehemu kwa muda. Kisha aliyarejesha macho katika uso wa Joram na kusema, “Ni wewe uliyestahili kuwa chali, utumbo nje, badala ya mtu huyu, Joram.”

Joram asingeweza kukanusha. Kifo cha kijana huyo kilimsikitisha sana. Alikuwa mmoja kati ya vijana wake smart ambao huwatumia kwa hili na lile, kijana ambaye alikuwa amemsaidia sana katika harakati zake zilizopita. Hakupata kushidwa hata mara moja isipokuwa leo ambapo ameyapoteza maisha yake. Joram akajilaumu kumtuma katika kadhia hiyo. Hamu yake ilikuwa ni kumshinda na kuutawanya ubongo wake sakafuni…

Kama aliyekuwa akiyasoma mawazo yake, vilevile Chonde aliongeza kwa sauti nzito, “Hata mimi sikufahamu kama wewe ni mtu hatari sana Joram. Unastahili kufa mara moja.”

Maisha yakiwa ukingoni, Joram alijua kuwa alihitaji kuikusanya akili yake yote ili ajiokoe. Hakujua afanye nini. Walikuwa na bastola moja tu, na ilikuwa katika mikono ya Chonde. Kuipata bastola hilo ilikuwa ndoto ya mchana. Chonde alikuwa macho kama kipepeo. Na bado Joram asingemudu kuitumia mikono yake. Hata hivyo, alitegemea kitu kimoja tu kimsaidie kutafuta muda wa kuokoa maisha yake. Muda. Muda waweza kufanya maajabu. Hata asipookoka, si inapendeza endapo ataufaidi uhai wa dakika chache zaidi.

"Najua ninakufa," alisema. "Nadhani unafahamu vizuri kuwa nakufa kwa ajili ya tamaa ya kutaka kujua siri uliyoificha katika kijisanduki hicho. Nifanyie basi wema wa mwisho. Nifungulie kisanduku hicho nife nikijua mna nini."

Chonde alicheka, "Tatizo lako Joram ni kule kufikiria kuwa unacheza na mtoto mdogo. Unachojaribu kufanya ni kuvuta muda. Wakati huohuo unathubutu kuendelea na upelelezi wako ili endapo lolote litatokea – kitu ambacho siamini – utoroke na kutoa siri hiyo nje. Kwa taarifa yako siri iliyoko katika kisanduku hicho ni nzito kuliko bara zima la Afrika. Kwa maneno mengine, ni siri ambayo dunia nzima inapigania kujua. Kwa bahati mbaya watu tunaoifahamu siri hiyo ni wachache sana. Na tumeshona midomo. Hata maiti siwezi kuisimulia siri hiyo. Nadhani hilo linakutosha. Sasa jiandae kufa. Ungependelea risasi ya kichwa au kifua?"

Joram alimtazama usoni na kuliona tabasamu la kifedhuli katika macho yake, tabasamu ambalo halikuwa na mzaha. Akajaribu kuicheza tena karata yake ya mwisho. "Jana ulinishinda kwa judo. Vipi ukiniua kwa mikono? Nadhani ni aibu na dalili za uoga kutumia risasi pasipo na umuhimu."

Chonde alicheka tena. "Ningependa kukuua kwa mikono mitupu. Hata hivyo, sina muda wa kutosha. Umebakiwa na nusu dakika ya kuishi. Utapenda kufa ukiwa umefumba macho au nikuue ukinitazama?"

Sasa mzaha ulikuwa mbali na sauti ya Chonde. Mauaji yalikuwa wazi katika macho yake. Joram akajua kuwa maisha yake yamefika ukingoni. Akiwa ameshuhudia vifo vingi vya risasi alitabasamu kimoyomoyo na kuamini kuwa hatimaye zamu yake imefika. Hata hivyo, bado aliyapenda maisha. Bado aliipenda dunia. Na alikuwa akiiacha moja kwa moja. Hivyo, badala ya kuyafumba macho yake aliyafumbua kwa nguvu na kuyakaza usoni. Hiyo pia aliifanya kuwa karata yake ya mwisho kwani kuua si mchezo, hasa kumwua kiumbe asiye na uwezo wa kujitetea.

Ilimsaidia. Nusu ya dakika ilipita Chonde kaielekeza bastola katika kifua cha Joram, kidole chake kikigusa kiwambo cha kufyatulia risasi, lakini alisita kuifyatua. Mara mlipuko wa bastola ukasikika. Joram alijirusha kando na kutua chini ambapo aliruka tena hadi upande wa pili wa kitanda. Risasi mbili tatu zaidi zikasikika, kama zinazopigwa bila shabaha yoyote. Kisha kimya kikafuata. Kimya hicho kilitoweka kwa mkoromo wa mtu aliyekuwa akikata roho. Ndipo Joram alipojiinua na kuchungulia. Ikamshangaza kumuoa Chonde kalala chini, kifudifudi, damu zikimvuja katika tundu kubwa la risasi katika uso wake. Joram alichupa na kuirukia bastola iliyokuwa mikononi mwa Chonde. Akajicheka kwa kuona akipokonya bastola kutoka katika mikono ya marehemu aliyekata roho kitambo. Akaikimbilia suit case ya chonde pamoja na kile kisanduku. Akavichukua na kuanza kutoka.

Mara mlango ulifunguka ukifuatwa na bastola ambayo ilichungulia kwa uangalifu. Bastola ikaingia ikifuatiwa na binadamu ambaye aliufunika uso wake kwa kofia kubwa na miwani. Alikuwa kavaa suruali na koti la kiume katika hali ambayo ingemfanya mtu yeyote amfikirie kuwa pande la mwanamume. Lakini Joram alimfahamu mara moja. Akaitelemsha bastola yake ambayo aliishika na kumkimbilia huku akisema kwa furaha, "Nuru nawezaje kukushukuru Nuru?"

Walikumbatiana na kubusiana kwa furaha.

Kisha walitengana mara moja na kutazamana. "Umewezaje kunifahamu mara moja kwa urahisi kiasi hiki? Tangu nimetoweka watu wanashindwa kunifahamu".

"Nadhani nakufahamu zaidi ya wanawake wote. Zaidi ya hayo nani mwingine ambaye anaweza kuhatarisha maisha yake kuipenyeza risasi katika tundu la ufunguo ili kumwua mtu ambaye alikuwa tayari kuniangamiza? Kwa kweli sijui namna ya kukushukuru Nuru!"

Wakakumbatiana tena.

"Nuru! Niliwahi kukwambia kuwa u mzuri? Niliwahi kukuambia kuwa hawakukosea waliposema kuwa wewe ni binadamu aliyekuja duniani kwa makosa badala ya kuwa malaika kama ulivyokusudiwa? Nadhani walikosea Nuru. Wewe ni malaika. Tazama ulivyo mzuri! Tazama ulivyotokea na kuipokonya roho yangu kutoka katika kinywa cha mauti. Nuru, nawezaje kukushukuru Nuru?"

Hayo yalipita katika kichwa cha Joram wakiwa wamekumbatiana. Joram alitamani kuyatamka kwa sauti, lakini hakufanya hivyo. Badala yake alisema, “Nakupenda.”

Ilikuwa mara ya kwanza kwa Nuru kumsikia Joram akilitamka neno hilo. Mara kwa mara alimtesa kwa kutojua kama kweli alimpenda au la. Ingawa walifanya mapenzi, mara nyingi, lakini bado Joram hakuwahi kulitamka neno hilo kwa sauti ambayo ililipa uzito kama huo. Kadhalika, macho yake hayakufichua mapenzi yake kwa hali yoyote. Hivyo, kwake ilikuwa zaidi ya habari njema. Hata hivyo, bado alikuwa na la kusema. “Sikuamini Joram,” alimnong’oneza. “Pamoja na kutoweka kwangu nikiwa nimetekwa nyara hukujishughulisha kunitafuta. Walao kutoa taarifa polisi.”

Joram akaangua kicheko. “Usinichekeshe Nuru. Waweza kuwa ulifanikiwa kuwalaghai watu wote pamoja na polisi, lakini mimi hukunidanganya. Nilijua kuwa ilikuwa hila uliyoiandaa tu ili unishawishi kuingia katika vita. Mwandiko wa barua ile pamoja na kuuvurugavuruga, kwa mtu aliyesomea miandiko kama mimi, nilifahamu kuwa ni wako. Vilevile ile damu iliyodondoka pale haikuwa na uzito wowote. Nilijua umejikata kidole makusudi. Na ile vurugu iliyofanyika chumbani haikuwa na umuhimu. Kwa vyovyote, majasusi khatari kama hawa wasingefanya mchezo usio na umuhimu kama ule. Hivyo, nilikuwa nikikusubiri nikitegemea utokee na tuendelee na starehe zetu.”

“Starehe?” Nuru aliuliza kwa mshangao. Alishangaa kuona Joram alivyoigundua hila yake kwa urahisi. Ilimshangaza zaidi alipodai starehe wakati wamesimama kando ya maiti mbili ambazo zilikuwa hata hazijapoa kwa ajili yao. “Starehe Joram? Nilidhani tumeingia kazini.”

Joram akatabasamu. “Sikia Nuru, siyo tabia nzuri kuzungumza kando ya maiti za binadamu. Pamoja na kwamba bastola zilizotumika zilikuwa na viwambo vya kupoteza sauti bado mtu yeyote anaweza kutokea na kutukuta katika hali hii. Nasi hatuna muda wa kuyajibu maswali ya polisi. Twende zetu mara moja,” alimaliza akiichukua mizigo yake na kuanza kutoka. “Nifuate. Twende kwa utulivu kama tutokao chumbani kwetu.”

“Kumbuka tu wanaume wawili,” Nuru alisema akitabasamu.

Waliteremka na kuiacha hoteli bila ya tatizo lolote. Watu wawili watatu waliokutana nao waliwatazama kikawaida.

Baada ya kuingia mitaani Nuru aliifichua bastola na kumpatia Joram akisema. “Chukua bastola yako. Samahani kwa kuichukua bila idhini yako. Nadhani uliihitaji sana. Ningeweza kukupotezea maisha.”

Tabasamu likamtoka Joram. “Hata hivyo umeniokoa. Kama ningeingia nayo pengine Chonde angeniua kwanza na kunisimanga baadaye,” Joram alijibu. “Nimepata nyingine. Hii umeipataje?”

“Nilienda kwako kuichukua”.

“Na umewezaje kunusa kuwa niko katika chumba kile nikisubiri kufa hata ukaja kuniokoa?”

“Ni rafiki yako aliyekuokoa. Hayati Edward ambaye, kwa bahati mbaya, mshenzi yule amemwua. Unajua nilipotoka hotelini kwa kisingizio cha kutekwa nyara, nilienda kujificha kwake? Tulijadiliana nae namna ya kurudisha moyo wako katika msimamo unaotakiwa. Mara ukampigia simu na kumpa maelekezo ya kwenda kufungua kisanduku hicho. Aliponieleza maelezo yako na jinsi ulivyoponea chupuchupu mara ya kwanza ndipo nilijua kuwa umerudi kazini. Nilitaka nije kwako mara moja. Lakini yeye aliniomba nisifanye pupa. Akaniomba nifuatane nae katika hoteli na kujificha kando nikimlinda. Nilifanya hivyo. Mara nikaona mtu mwenye dalili za kikafiri akiingia chumbani humo, bastola mkononi; ingawa ilifichwa sana. Kabla sijafahamu la kufanya nilikuona wewe pia ukinyatia na kuingia. Ndipo nilipojivuta mlangoni na kuchungulia katika tundu la ufunguo. Nikamwona Chonde akiwa tayari kukuua. Sikuwa na la kufanya zaidi ya kumlenga na… na …”

Mara Nuru aliangua kilio. Akamgeukia Joram na kumkumbatia kwa nguvu akisema, “Nimeua mtu… Nimeua mtu, Joram…”

“Watu huuawa,” Joram alimnong’oneza. “Hebu jitahidi kuwa msichana shujaa kama ulivyo, Nuru. Usingemwua angeniua. Watu watakusikia. Twende zetu chumbani.”

“Lakini nimeua, Joram… nimeua…”

Ulikuwa usiku mfupi sana kwa Joram. Alikuwa na mengi ya kufanya ambayo hakuweza kuyatekeleza. Ilimchukua muda mrefu kumshawishi Nuru kwa vinywaji na mahaba ili asahau hofu yake ya kuua mtu. Baada ya usiku wa manane ndipo Nuru alipoacha kuweweseka na kupitiwa na usingizi mzito. Lakini alimkumbatia Joram kwa nguvu. Ilimlazimu Joram kutumia hila fulani na kujitoa mikononi mwake na kumfanya akumbatie mto.

Akinyata kwa utulivu, Joram alikiendea kisanduku cha marehemu Chonde na kutazama uwezekano wa kukifungua. Isingekuwa kazi rahisi. Ilihitaji utaalamu wa hali ya juu au risasi ya bastola. Joram hakuwa tayari kuitumia risasi kwa hofu ya kumwamsha Nuru. Na utaalamu siyo jambo ambalo lingepatikana kwa dakika moja. Hivyo, alikiweka kando kisanduku hicho na kuuchukua mfuko wa Chonde ambao haukumchukua muda kuufunua mifuko yake ya siri ambamo alitoa nyaraka mbalimbali na kuzisoma kwa makini. Yale maandishi wa kijasusi ni jambo jingine ambalo lilihitaji muda na utulivu mkubwa ili kueleweka. Hivyo, hakupoteza muda kujaribu kuyasoma. Badala yake alichukua hati ya kusafiria ya Chonde, kile kijisanduku na nyaraka zote alizoona muhimu. Vitu vingine alivifungafunga katika mfuko na kuvificha mahala ambapo aliamini kuwa visingepatikana kwa urahisi.

Baada ya hapo alichukua begi lake na kutoa vitu vyote vilivyokuwemo. Alichukua kinyago fulani cha hoteli na kukifunga katika mfuko wa nailoni na kuutumbukiza katika begi lake. Akalinyanyua kupima uzito wake. Kisha akaliweka mezani, na kuacha balbu ambayo ilikuwa ikitoa nuru nyekundu iendelee kuwaka. Akalitupa taulo lililokuwa kiunoni mwake na kujilaza kitandani kwa utulivu akiutoa mto aliokuwa ameukumbatia Nuru na kuichukua nafasi hiyo. Akainua mikono ya Nuru na kuifanya ituwe kiunoni mwake. Akayafumba macho yake na kujifanya kulala. Lakini asingeweza kulala alikuwa akiyasubiri mapambano kwa hamu.

Joram hakujua kuwa alikuwa amepitiwa na usingizi mzito. Alipoamka alikutana na macho mazuri ya Nuru yakimtazama kwa utulivu. “Za asubuhi, mpenzi,” Nuru alimsalimu Joram.

“Nadhani siyo mbaya.”

Nuru alitulia kidogo kabla ya kuongeza, “Nilikuwa nikisubiri uamke ili tuzungumze mpenzi. Nadhani haya yatakuwa maongezi yetu ya mwisho”.

“Kwa vipi?”

“Unajua jana nimeua mtu? Wakati wowote polisi watafika hapa na kunitia pingu. Endapo nitanusurika kitanzi siwezi kunusurika kifungo cha maisha.” Akasita tena na kuongeza, “Leo nimeota mpenzi. Nimeota nikining’inia juu ya kitanzi. Wewe na watu wengine mkiwa kando mkinicheka. Nilijaribu kukuita unisaidie lakini sauti haikuweza kutoka.”

Joram akacheka. “Nani aliyekwambia kuwa utafungwa? Polisi wangemfahamu mtu aliyemwua bila shaka ungepata medali ya dhahabu badala ya kukuvika pingu. Licha ya hayo, hawawezi kabisa kufahamu nani alimwua. Unajua, uliingia hotelini mle ukiwa mwanamume? Ni mimi tu niliyeweza kukufahamu,” Joram akacheka tena. “Lakini yote hayo ya nini? Leo tunaenda zetu Nairobi.”

“Kufanya nini?”

“Kutumia.”

Nuru akashikwa na mshangao. “Nilidhani umeingia kazini Joram.”

Joram alitabasamu kabla ya kumjibu akisema. “Kuna mpelelezi mwenzangu maarufu anayeitwa Willy Gamba, aliwahi kusema kazi na dawa. Mpelelezi ni binadamu vilevile. Lazima astarehe na kuburudika. Yawezekana tutaenda Nairobi tukiwa kazini. Sasa, sikia Nuru. Nitafunga mizigo yetu yote na kukutaka ukanisubiri Uwanja wa ndege. Hapana usiende Terminal II nenda kanisubiri Terminal I uwanja wa zamani. Nataka twende kwa ndege ya kukodi.”

“Ndege ya kukodi!” Nuru hakustahamili kuficha mshangao wake. “Kwa kweli, suala zima linanitatanisha. Kwanza, nadhani hatuna pesa za kutosha kutuweka hotelini kwa siku tatu zaidi.”

“Nani aliyesema kuwa hatuna pesa?”

Saa mbili baadaye Joram alikuwa mtaa wa Sokoine akielekea benki ya City Drive. Mkononi alikuwa na mfuko wake mkubwa ambao ulionekana mzito. Alipoingia benki alimfuata meneja aliyeongea nae jana ambaye alimpokea katika hali ya kujuana. Baada ya salamu za kawaida Joram alipewa fomu alizotakiwa kujaza. Akajaza kwa makini na kuzirejesha kwa meneja ambaye alizipitia. Kisha alitakiwa kuonyesha mali yake aliyohitaji kuhifadhi kwa utaratibu wa Self-Custody. Akafungua begi lake na kutoa kinyago.

“Ni hicho tu?” meneja aliuliza. “Nilidhani una kidani cha almasi,” akamjibu kwa sauti ya mzaha.

Moyoni meneja huyu aliamini kabisa kuwa ndani ya kinyago hicho mlikuwa na kipande cha almasi au Tanzanite. Kwani hakuona sababu nyingine ambayo ingemfanya Joram ajiingize katika gharama kubwa kwa ajili ya kinyago cha Mmakonde mmoja.

“Hiki kina thamani kama roho yangu,” Joram alimjibu meneja.

“Ni kumbukumbu ambayo iliachwa na babu mzaa babu ambayo inalinda ukoo wetu. Niliwahi kudhani kwamba ni utamaduni wa kipuuzi nikakidharau, lakini yalinipata makubwa. Nusura nipoteze roho. Tangu nimekithamini na kuwa nacho, mambo yameniendea kama ninavyotaka.”

Meneja huyo alielekea kumwamini. Wakainuka na kuelekea shimoni. Waliwapita wafanyakazi wanaotunza akaunti za watu, ambao hawakujishughulisha kuwatazama zaidi ya ule mtazamo wa kawaida. Wakateremka ngazi na kuingia vyumba vya chini. Ni hapo Joram alipomgusa meneja huyo bega na kumwambia, “Sikia bwana meneja. Sihitaji kuhifadhi kinyago hiki wala kitu kingine. Nahitaji pesa. Za kigeni.”

Sauti yake ikiwa ileile, makini, iliyotulia, ikamfanya meneja huyo kudhani kuwa huo ulikuwa utani mwingine wa Joram. Hivyo, aligeuka akitabasamu. Lakini tabasamu lake liliyeyuka ghafla na nafasi yake kumezwa na hofu iliyochanganyika na mshangao mara alipokutana na bastola kubwa ikimchungulia kifuani.

“My God,” aliropoka kwa hofu.

“Usiogope,” Joram alimnongoneza. “Endapo hutakuwa mbishi hutaumia. Kwanza pesa hizo sio zako. Nifunguliea nichukue kidogo na kuondoka zangu.”

“Sina ufunguo,” meneja alijibu. “Zaidi ya hayo, vitasa hivi hufunguliwa na watu wawili kwa pamoja. Sioni unavyoweza kuzichukua.” Akavuta pumzi kwa nguvu kabla ya kuongeza, “Licha ya hayo ndugu Joram, nashindwa kuamini kama kweli unadiriki kukifanya kitendo hicho. Unajua wewe ni mtu mwenye hadhi kubwa hapa nchini na duniani kote. Kwa nini uichafue hadhi hiyo? Kama unataka pesa hata ungeiomba serikali ungepewa. Hakuna asiyejua mchango wako katika kuilinda nchi hii.”

“Yaelekea huufahamu ubahili wa serikali hii wewe,” Joram alimcheka. “Sasa tusipoteze muda. Mimi ninazo funguo ambazo zinafungua kila kufuli. Sidhani kama kufuli zenu zitashindikana. Nitakupa funguo hizo ujaribu mmoja baada ya mwingine. Nitakuwa nyuma yako nikikutazama. Ukifanya ujinga utapoteza maisha yako.”

Juhudi hizo hazikufua dafu. Ndipo alipoamua kufumua kitasa kwa risasi. Bastola ilikuwa na kiwambo cha kupoteza sauti, na, kwa hivyo, ulitokea mlio wa kawaida tu.

Dakika iliyofuata walikuwa ndani ya chumba cha fedha za kigeni, Joram akiwa kamsimamia meneja ambaye aliamriwa kutoa kinyago na kupakia mabunda ya noti za Dollars, Pounds na nyinginezo. Mfuko uliposhiba, Joram alimwamru meneja huyo kuondoka. Aliuchukua mfuko na kumtaka atangulie.

“Tutatokea mlango wa uani na kwenda nje kupitia geti. Bastola itakuwa mfukoni lakini tayari kuvunja mgongo endapo utafanya ujanja au ujinga wowote. Tembea kama kawaida bila kugeuka nyuma.”

Walitoka na kuelekea uwani badala ya ofisini. Wafanyakazi wawili watatu waliwatazama kwa mshangao lakini tabasamu la Joram liliufanya mshangao wao utoweke. Tabasamu hilohilo liliwafanya askari wa geti wasishuku lolote kumwona meneja wao katangulia akitokea mlango ambao huutumika kwa nadra sana.

Barabarani Joram alimtaka meneja huyo kuendelea na safari akiifuata barabara ya Samora bila kugeuka nyuma. Meneja huyo alitembea kwa dakika kadhaa. Aliipita Benki ya Nyumba na kuifikia barabara ya Samora. Hapo alisimama kungoja amri nyingine. Hakusikia. Akatulia kwa muda akiogopa kugeuka nyuma. Alipoona macho ya wapita njia yakianza kumtazama kwa maswali ndipo alipojitahidi kugeuka nyuma. Akajikuta akiwa peke yake. Hakujua Joram yuko wapi. Kwanza aliduwaa kwa muda. Kisha alirudiwa na fahamu, akainuka na kuondoka mbio kurudi ofisini. "Tumeibiwa," alimwambia mfanyakazi wa kwanza aliyekutana nae. Akaingia ofisini kwake na kuvuta king'ora cha ishara. Dakika chache baadaye polisi waliwasili na kuanza kuuliza maswali yao.

Wakati huo Joram alikwisha badili mavazi yake na kuvaa yale ya kizee pamoja na ndevu za bandia zilizojumuishwa na miwani kumfanya aonekane mtu mwingine kabisa. Kadhalika alikwisha badili teksi mbili ambazo zilimteremsha sehemu mbalimbali. Hii ya tatu alimwambia dereva, "Airport, tafadhali. Fanya mwendo wa kuruka."

Dereva hakumwangusha.

Wakati polisi walipoanza kuweka vizuizi vya njiani, yeye alikuwa akimaliza kumlipa bwana fedha nauli ya ndege.

SURA YA TANO*

JIJI la Nairobi lilimraki Joram Kiango na Nuru kwa hewa yake yenye ubaridi ambao ulikuwa kinyume kabisa cha joto waliloliacha Dar es Salaam. Waliuacha Uwanja wa Kimataifa wa Kenyatta kwa teksi ambayo iliwafikisha Hilton Hotel.

"Mr. and Mrs. Charles Moris," Joram alijitambulisha katika kitabu cha wageni.

Mhudumu wa mapokezi aliwatazama kwa muda akivutiwa na sura na maumbile yao. Kisha aliwapatia chumba kimoja Self-Contained, kama walivyotaka. Akawakabidhi kijana mmoja ambaye aliwaongoza hadi katika chumba chao ghorofa ya nane. Baada ya kuwafikisha aliwapa ratiba ya chakula, vinywaji na maelekezo mengine ambayo masikioni mwa wasikilizaji wake yalikuwa kama wimbo baada ya kuyasikia mara kwa mara. Walimkubalia yote na kumtupia maswali huku mara kwa mara wakimuonyesha meno kulijibu tabasamu lake ambalo halikuwa na mpaka. Kisha Joram alimfukuza kwa kumpa noti ya shilingi mia moja ambayo ilidakwa kwa heshima zote na kupotelea mfukoni.

"Wakati wowote, ukihitaji chochote usisite kuniita, mzee. Naitwa James," alieleza akitoka.

"Bila shaka, James".

Mara tu walipobaki peke yao, Nuru alimtupia Joram jicho lililojaa maswali. Alipoona Joram hatamki lolote aliamua kuzungumza. "Nadhani una mengi ya kunieleza Joram. Kila nilipojaribu kukuuliza kisa cha safari yetu tulipokuwa angani hukupenda kunijibu."

"Sidhani kama kweli. Ulikuwa hupendi kuzungumza mbele ya yule rubani."

"Kwa nini? Kwani kuna siri yoyote?"

"Bila shaka. Ulipokuwa uwanja wa ndege Dar es Salaam ulikuwa umejivika mavazi ya kizee tofauti na ulivyokuwa asubuhi. Ulipofika hapa jambo la kwanza ulilofanya ilikuwa kujibadili mavazi na kuwa kama ulivyo. Tulipofika hapa umelipa kwa fedha za kigeni bila shaka yoyote. Umezipata wapi? Na…"

"Alaa! Hivi sijakwambia? Kati ya pesa nyingi tulizopata katika mfuko wa marehemu Chonde nyingi zilikuwa za kigeni," Joram alidakia. "Nadhani nilikuonyesha Nuru."

"Ulinionyesha. Na kwa nini umeamua kupanga kwa jina la bandia?" Nuru aliendelea kusaili. "Na hapo watakapoomba kuiona hati ya usafiri utawaonyesha nini?"

“Hilo lisikusumbue. Uongo sikuanza jana. Lakini sababu kubwa iliyonishawishi kuandika jina la bandia ni hofu ya kusumbuliwa na waandishi wa habari. Unawajua walivyo, Nuru. Mara nyingi hawana kitu cha kuandika. Hivyo, wanapopata kijambo watakikuza ili kijae ukurasa. Umaarufu wangu nchini Tanzania ni jambo ambalo waandishi wa Nairobi wanaweza kuliondolea uvivu kwa haki kabisa.” Akasita na kucheka kidogo. Halafu akaendelea, “Hapana Nuru. “Tumekuja kustarehe. Tunahitaji kustarehe. Nairobi ni mwanzo tu wa starehe zetu. Toka hapa, tutakwenda zetu London, Paris, Hong Kong, New York na kokote ambako roho itatuita. Lazima tufurahi.Binadamu huishi mara moja tu. Hana budi kuitumia nafasi hiyo ili akifa awe amefaidi maisha.”

Joram aliongea kwa sauti imara, ingawa Nuru alihisi na kuamini kuwa hakuwa mkweli. Hata hivyo, kwa kadri alivyomfahamu alihisi kuwa Joram alikuwa na jambo, jambo ambalo lilikuwa halijakamilika kichwani mwake na hakuona haja la kuliongelea. La sivyo, ingewezekanaje Joram ashambuliwe na mtu, Nuru amuokoe kwa kumwua mtu huyo, waache maiti chumbani na kukodi ndege hadi huku, wapange kwenda zao bila sababu yoyote maalumu? Hiyo si itakuwa hadithi? Bila shaka kuna jambo.

Nuru alilingoja jambo hilo kwa hamu. Baada ya kuwa na Joram kwa muda mrefu, baada ya kukinaishwa na starehe, na baada ya risasi aliyoifyatua kuondoa roho ya mtu, roho ya Nuru ilikuwa juujuu ikitegemea jambo, jambo jipya. Jambo ambalo litampa haki na wadhifa halisi wa kuwa na Joram Kiango kama alivyokuwa hayati Neema Idd. Alikuwa ameamua kuichukua nafasi ya Neema, katika mwili na akili ya Joram si kuichukua kwa kunywa pombe na kucheza muziki. Ni kuichukua kikazi. Na ni kazi hiyo ambayo aliisubiri kwa hamu.

Nuru alipomtazama tena Joram alimwona kazama katika mawazo mengi. Akamwacha na kuingia bafuni ambako alioga kwa utulivu. Alipotoka bafuni hakumuona Joram. Badala yake alipata kipande cha karatasi Joram akimtaka radhi kuwa amelazimika kwenda maktaba mara moja.

Upweke ulimfanya aamue kwenda chumba cha maongezi ambako alijipatia bia mbili huku akiitazama televisheni. Aliangalia vipindi kadhaa vya burudani na taarifa za habari. Hakukuwa na mapya zaidi ya yale ambayo yameondokea kuwa ya kawaida masikioni na machoni mwa binadamu. Macho yalipokinai televisheni, aligeukia chupa ambayo ilikuwa mbele yake.

Mara akatanabahi ameketi na mtu ambaye alikuwa akizungumza. “Nasema, samahani naweza kuketi nawe?”

“Bila samahani?”

Mtu huyo aliketi na kuanza kumwaga vinywaji na maongezi. Maongezi yake yaligeuka kumtaka Nuru. Alisema mengi, akidai kwa viapo kuwa hakupata kumuona msichana aliyeumbika kama Nuru, kwamba alikuwa tayari kufa ili ampate. Mara mikono yake ikakosa utii. Ikaanza kutambaa juu ya mapaja ya Nuru. Ni hilo lililomwondoa hapo na kumrudisha chumbani kwao.

Joram alikuwa hajarudi. Saa kadhaa tayari zilikuwa zimepita. Alipotahamaki, usiku ulikuwa umeingia. Alikula peke yake chumbani humo akiogopa kwenda chumba cha maakuli ambako kulikuwa na wanaume ambao hawakuzoea kukubali kuwa mwanamke angeweza kuwa pale peke yake. Uchovu ulimfanya ajilaze kitandani. Hakujua usingizi ulivyomchukua. Alipoamka alijikuta yuko mikononi mwa Joram.

“Samahani mpenzi,” Joram alimnong’oneza.

Hakujishughulisha kumjibu kwa maneno. Badala yake alilijibu busu la Joram kwa vitendo. Kisha usingizi ulimchukua tena. Alipoamka aliupeleka mkono kumkumbatia Joram. Akajikuta akigusa godoro tupu. Joram hakuwa kitandani. Alipofumbua macho alimwona kainama mezani akisoma kwa makini. Akanyoosha mkono na kuichukua saa yake ndogo ya mkono kuitazama. Ilikuwa saa kumi na nusu za alfajiri. Hakuona sababu ya kumsumbua Joram. Akajifunika na kujaribu kulala. Usingizi haukuafikiana nae. Baada ya kuoga na kufungua kinywa asubuhi hiyo Joram alimwomba Nuru kuwa angerudi tena maktaba. “Leo nitamaliza shughuli zangu. Baada ya hapo tutakuwa pamoja katika kila la heri na shari,” alimweleza. Kisha akampatia kitita cha noti akimwambia.”Unajua tutakuwa na msafara mrefu? Nataka uende huko ukiwa katika hali halisi ya kuvutia kila macho ya mwanamume. Kwa hiyo, tafadhali leo pitapita madukani ununue kila vazi ambalo litakustahili. Usijali bei. Kumbuka pesa tunayo.”

Nuru alizipokea na kumuuliza, “Na wewe huhitaji nguo mpya?”

“Nahitaji. Hata hivyo, sina haraka. Wanaume huwa hawatazamwitazamwi kama wanawake.”

“Najua unahitaji muda wa kuwa peke yako,” Nuru alimwambia. “Endelea baba, siwezi kukuzuia.”

Mara tu Nuru alipoondokaJoram aliingia kazini. Alifungua begi lake na kutoa nyaraka za Chonde ambazo alitumia kila njia, kuzielewa. Akatoa kitabu ambacho alikipata kwa taabu sana kinachoeleza mbinu mbalimbali za kusoma maandishi ya mafumbo.

Akaketi na kuanza kutumia kitabu hicho kuyasoma tena maandishi ya Chonde. Haikuwa kazi ndogo. Ilihitaji muda mrefu na utulivu mkubwa. Alichofanikiwa ni kupata mwongozo ambao ulieleza namna ya kukifungua kile kisanduku. Akakifungua bila tabu yoyote.

Ndani mlikuwa na vijigololi kumi na viwili. Joram alikiinua kimoja na kukitazama kwa makini. Katikati ya kigololi aliona vidude vilivyokuwa vikichezacheza mfano wa saa za electronic. Alikitazama kigololi kwa makini akijaribu kutafuta umuhimu wake, hakuupata. Chini ya vigololi hivyo Joram alipata ramani ambayo alipoikunjua alikuta kuwa ni ya Jiji la Dar es Salaam. Ramani hiyo ilionyesha majengo maarufu kama Ikulu, vituo vya kijeshi, mabenki, na kadhalika. Vitu vyote hivyo vilikuwa vimewekewa namba za kirumi kuanzia moja na kuendelea. Namba ya jengo la benki kuu iliyoungua ilikuwa imewekewa alama ya x kwa wino mwekundu.

Mara baada ya kuona hayo Joram alipatwa na wasiwasi. Alihisi kuwa, kwa namna moja ama nyingine, Chonde alihusika na moto ulioteketeza Benki Kuu. Hofu yake kubwa ilikuwa zile hisia kuwa alama zilizofuata ambazo zilikuwa hazijawekwa x kwa wino mwekundu zilikuwa katika orodha zikisubiri, jambo ambalo lingeleta maafa na madhara makubwa kwa nchi na wananchi. Zaidi, ingekuwa ushindi mkubwa kwa maadui wa taifa. Hivyo, kwa mara nyingine, alifanya sherehe moyoni kushangilia kifo cha Chonde.

Kisha alifunga sanduku hilo kikamilifu na kuirudia meza ambayo aliinamia na kuanza kujifunza tena mbinu za kuyasoma maandishi hayo kwa makini zaidi.

Alikuwa hajatulia vizuri mlango ulipofunguka ghafla na Nuru kuingia huku macho yake yakiwa mekundu kwa mchanganyiko wa hasira na mshangao. Alisimama akitweta na kumtazama Joram kwa namna ya mtu ambaye hakujua la kusema.

“Usiniambie kuwa kuna mtu aliyekuvamia kwa nia ya kukunajisi mchana wote huu,” Joram alimwambia kwa dhamira ya kumfariji.

“Acha mzaha Joram. Sikutegemea kama ungekuwa mtu wa kufanya kitendo kama kile.”

Joram aliinua uso wake kumtazama.

“Kufanya nini?”

“Kuiba”.

“Kuiba?”

Nuru akamkazia jicho la hasira. “Usijifanye hufahamu. Dunia nzima sasa inafahamu. Kwa kweli, sikutegemea kabisa. Imenishangaza kukuona katika televisheni ukitangazwa kama mtu hatari ambaye ameweza kuiba fedha za kigeni ambazo nchi yake inazitegemea kama dawa.” Akasita akamtazama kwa chuki ambayo ilichanganyika na mshangao, “Kwanini ulifanya hivyo, Joram?”

“Bado siamini kama amefanya hivyo,” mtu mmoja alikuwa akifoka pia, akiwa kaketi katika kundi la watu wenye hasira na mshangao kama yeye. Mabega yao yalikuwa yakimeremeta kwa nyota ambazo zilipamba magwanda yao kudhihirisha madaraka yao.

“Amefanya, lakini siamini kama Joram ni mtu wa kutenda kitendo cha aibu kama hiki. Jambo la kusikitisha zaidi ni jinsi habari hiii ilivyovuja kiasi cha kuyafikia masikio ya adui zetu. Leo nimesikia habari hizo na Afrika Kusini,” Kombora aliendelea kulalamika.

“Ujerumani pia imetangaza afande,” mtu mmoja aliongeza.

“BBC vilevile,” mwingine aliongeza.

“Unaona, basi? Unaona habari mbaya zinavyosafiri upesiupesi? Pamoja na kwamba Joram ametuasi kimsimamo tulikuwa na haki ya kumsetiri kwasababu ya vitendo vyake vya nyuma. Sasa nadhani hatuna tunachoweza kufanya. Maji yamekwishakumwagika, hayazoleki. Lililopo ni kutafuta uwezekano wa kumpata na kurudisha pesa zote, hasa za kigeni.”

“Hilo ndio tatizo mzee,” msaidizi wake mmoja alijibu. “Taarifa za mwisho zinathibitisha kuwa hayupo kabisa hapa nchini. Kuna dalili kuwa ametorokea nchi jirani kwa ndege ya kukodi.”

“Lazima, lazima apatikane,” Kombora alisisitiza. “Pesa alizochukua ni nyingi sana na zinahitajika sana. Hana haki ya kuzifuja kwa starehe zake binafsi. Wasiliana na nchi jirani zote. Wasiliana na Interpol. Waarifu kuwa tunamhitaji Joram kwa hali na mali. Maadamu siri imekwishafichuka, hakuna haja ya siri tena.”

Baada ya majadiliano marefu jalada hilo lilifunikwa na kuletwa jingine ambalo lilikuwa “zito” Zaidi. Lilihusu mkasa au maafa yaliyotukia taifa pamoja na lile tishio la maisha na majumba muhimu. Walipima juhudi zao zote wakilinganisha habari mbalimbali. Haikuwepo dalili yoyote ya kujenga matumaini.

Kisha wakavirudia vifo vya watu wawili katika chumba kimoja cha hoteli hapa Jijini. Dalili zilionyesha kuwa marehemu walikuwa watu wasiofahamiana kabisa. Pekuapekua yao katika chumba hicho haikuwapatia kitu chochote zaidi ya mavazi ambayo yalionyesha kuwa yameshonwa nchi za nje. Nyaraka walizohitaji, ambazo zingeweza kuwasaidia, hawakuzipata. Ilielekea vifo hivi vingeingia katika yale majalada ambayo kesi zake hazikuwahi kutatuliwa. Hivyo, baada ya kuzitazama tena picha za marehemu wote, zilirudishwa katika majalada na kufungiwa.

Kikao kikaendelea.

“Kwanini umefanya hivyo, Joram?” Nuru aliendelea kufoka.

Joram, ambaye alionekana kimawazo yuko maili kadha wa kadha nje ya chumba hicho, alimtazama Nuru kwa muda. Kisha ikawa kama amemkumbuka. Tabasamu dogo likamtoka, likifuatwa na sauti nzito, “Ilikuwa lazima nifanye vile, iko siku utaelewa Nuru.”

“Nitaelewa!” Nuru alifoka, “Nitaelewa nini, mwanamume mwenye heshima zake na hadhi yake duniani anapothubutu kuingia benki na kuiba pesa ambazo nchi na watu wake wote wanazitegemea? Siwezi kuelewa kabisa, Joram. Ambacho naweza kuelewa ni wewe kuondoka sasa hivi na kwenda zako ofisi ya Ubalozi wetu ukaombe radhi na kurudisha kila senti. Tafadhali fanya hivyo, Joram.”

Hilo lilisababisha kicheko kwa Joram. “Nina haki ya kula pesa za Tanzania kama wengi wao wanavyozila, Nuru. Huoni watu wenye mishahara ya shilingi elfu mbili wanavyojenga majumba ya mamilioni? Unadhani wanazipata wapi bila ya wizi? Tofauti yangu na wao ni kwamba mimi nimeiba kimachomacho, wao wanaiba kisirisiri. Mwizi ni mwizi tu.” Akasita kidogo kabla ya kuendelea, “Acha tuzitumie Nuru. Acha tuzifaidi. Hii ni nafasi pekee katika maisha yetu ambayo hatujaisahau. Jisikie starehe…”

“Siamini kama maneno hayo yanatamkwa na Joram Kiango. Kwanini umebadilika kiasi hicho Joram?”

Kabla Nuru hajapata jibu mlango uligongwa na kufunguka taratibu. James aliingia. Uso wake ulionyesha kuwa alikuwa na habari ambayo si nzuri sana. Baada ya kubadilishana salamu za kawaida aliwataka radhi na kumchukua Joram chemba.

“Kaka, samahani. Unajua pamoja na kujiita kwako Charles Morris, ni watu wachache sana ambao waliamini? Sura yako si ngeni kabisa hapa Kenya. Umetokea mara nyingi katika magazeti na televishani. Wewe ni yule mpelelezi mashuhuri Joram Kiango. Sivyo, kaka?”

Joram alipochelewa kumjibu, James aliendelea, “Ziko habari mbaya zilizotokea katika vyombo vya habari. Inasemekana umetoroka kwenu ukiwa umechukua fedha nyingi za kigeni. Kwa jinsi ninavyokufahamu nashindwa kuamini kama ni kweli. Lakini hilo si muhimu sana kwa sasa. Nilichofuata ni kukufahamisha kwamba sasa hivi wapelelezi wa hoteli hii wamekaa kikao wakilijadili suala lako. Waweza kutiwa msukosuko

mkubwa. Kwa hiyo, nakushauri utafute mbinu yoyote ambayo itakufanya uokoe maisha yako. Nina ndugu yangu anayeishi Nyeri. Anaweza kukuficha kwa muda."

Joram alicheka na kumshukuru James. "Usijali rafiki yangu. Nitajua la kufanya. Kwa sasa niache nijipumzishe kidogo na kufikiria la kufanya." Baada ya hayo aliutia mkono wake mfukoni na kuutoa ukiwa umeshikilia noti kumi za mia mia ambazo zilidakwa na James kabla hazijamfikia. "Kajipatie bia mbili," alimwambia akigeuka na kurudi chumbani.

"Unaona Joram? Twende zetu ofisi ya Ubalozi," Nuru alimdaka juujuu kwa maneno hayo.

"Kufanya nini?" Joram alizungumza kwa upole kama kawaida yake. "Tutakwenda zetu tunakotaka. Sasa hivi uwe binti mtulivu na ufanye kama nitakavyokuambia, tafadhali. Baada ya dakika chache tutakuwa zetu angani tukielekea katika mji mwingine wenye starehe kuliko huu."

"Haiwezekani, Joram. Lazima ukaombe radhi na kurudisha pesa za watu," Nuru aliendelea kukanusha.

"Alikuwa ameishi na Joram kwa muda mrefu. Lakini alikuwa hajapata kumuona Joram anavyokasirika. Leo hii aliziona hasira zake. Aliiona nuru kali na tena baridi, ikijitokeza katika sauti yake ndogo, nzito, aliposema taratibu, "Haya. Nenda zako ofisi za Ubalozi. Chukua na pesa zetu uwapelekee."

Dakika mbili tatu baadae mzee mmoja wa kiume, mwenye mvi nyingi na ndevu za kutosha alionekana akitoka katika hoteli hiyo. Alikuwa kafatana na kijana wa kiume mwenye sura nzuri ambaye alikifunika kichwa chake kwa kofia pana na macho kwa miwani ya jua. Mikononi mwao walikuwa na mifuko yao. Wafanyakazi waliowatazama wakiondoka hawakuweza kukumbuka wageni hawa waliingia lini na iwapo walikuwa katika vyumba vipi. Waliwasindikiza kwa macho hadi walipotoka nje na kukodi teksi.

Kati ya wafanyakazi walioshuhudia wakiondoka ni James Kamau. Hata ndoto haikumjia kuwa alikuwa akiwatazama Joram Kiango na Nuru wakiondoka.

SURA YA SITA

SAA chache walikuwa angani tena, katika Ndege ya Shirika la Ndege la Uingereza, wakielekea London kupitia Cairo, Misri.

Sasa habari za "Wizi wa Joram" zikiwa zimetapakaa duniani kote, zikienezwa na kila chombo cha habari, haikuwa kazi ndogo kwao kuipata fursa hii ya kuiacha nchi ya Kenya. Polisi mitaani na katika vituo vyote vya usafiri walikuwa macho wakimtazama kila mtu ambaye alielekea kufanana na Joram. Passport na vitambulisho vyao vilitazamwa kwa makini zaidi, huku maswali mengi yakiulizwa. Hata hivyo, Joram na Nuru walifaulu kupenya vizingiti vyote huku wakicheka kimoyomoyo, kwani askari hao hawakuwatazama kabisa kwa jinsi walivyojibadili kimavazi na kitabia, kinyume kabisa cha matarajio ya askari.

Nuru aliuficha uzuri wake kwa kuiondoa ile hali ya uvulana aliotoka nayo hotelini na kujivika nywele zilionekana nusu zingemezwa na mvi. Mavazi yake pia yalikuwa yale ambayo vijana wasingependa kuyatupia macho zaidi ya mara mbili. Jambo ambalo lilifanya wawe sawa na huyu mzee mkongwe aliyekuwa akitembea kidhaifu, mfuko mgongoni na mkwaju mkononi. Hali zao pia zilikuwa za wakazi halisi wa Nairobi. Hati zao za halali pamoja na picha zao zilifichwa vilivyo katika mifuko ya siri iliyokuwemo katika mfuko waliorithi toka kwa hayati Chonde.

Ndani ya ndege Joram alitulia akinywa bia aliyoletewa kwa utulivu, huku mara chache akimtupia Nuru maongezi mafupi mafupi. Baada ya muda ambao haukuwa mrefu alipitiwa na usingizi. Aliamka ndege ilipokuwa ikitua katika Uwanja wa Ndege wa Cairo. Misukosuko ya abiria wanaoshuka na kuingia ilipopungua walizungumza na Nuru maongezi machache ambayo dhamira yake kubwa ilikuwa kuwafanya watazamike kama watu wa kawaida wasio na dosari yoyote machoni mwa wasafiri wengine.

Safari ilipoanza tena Joram alikiweka kiti chake katika hali ya kulala akimwacha Nuru akipekua kitabu chake kutafuta alipokuwa ameishia. Ikiwa safari ndefu, ya kuvuka bahari kubwa kama hii ya Atlantic, Joram alikusudia kutumia vyema kufidia usingizi ambao hakuupata kiukamilifu alipokuwa Nairobi. Na ndivyo ilivyomtukia. Hakupata nafasi ya kuyafumbua macho yake kuyatazama maji mengi yaliyotapakaa kote. Alipoamshwa na Nuru na kutazama dirishani, alishangaa kuona wakizunguka juu ya Jiji la London wakisubiri kutua.

“Imekuwa safari fupi kuliko nilivyotegemea,” alisema.

“Hata! Ilikuwa safari ndefu sana kama ilivyo,” lilikuwa jibu la Nuru.

Taratibu, ndege ikashuka na kutua bila msukosuko wowote katika uwanja mashuhuri wa Heathrow. Pilikapilika za abiria kuchukua mizigo na kutaka kutoka mapema zikaanza. Joram na Nuru, wakiwa miongoni mwa abiria walioshuka mwisho, walichukua mizigo yao na kupita katika ofisi za forodha na abiria wengine waliokuwa wakisubiri usafiri.

Dereva mmoja, msichana, wa shirika la usafiri la Avis and Hertz, aliwafuata na kuwashawishi kuingia katika gari lake. Akawapeleka mjini katika Hoteli maarufu duniani ya Wilson Place ambapo walijipatia chumba maridadi. Mapokezi yakiwa ya kistaarabu, huduma za kistaarabu, na wahudumu waliosomea ustaarabu, yote yaliwafanya waone kama wako nyumbani badala ya ugenini, jambo ambalo liliwafanya wasijali chochote juu ya malipo makubwa yanayodaiwa na hoteli hiyo.

Kuna mzungu mmoja, mshairi, au mpenzi tu wa taifa lake ambaye aliwahi kusema: “When a man is tired of London, he is tired of life for there is all that life can afford,” kwamba binaadamu anayekinaishwa na Jiji la London basi amekinaishwa na maisha kwa ujumla kwani London inacho kila kitu ambacho maisha ya binaadamu yanahitaji. Joram na Nuru wasingemwona mtu huyo kuwa mwongo sana. Pamoja na kwamba wote hawakuwa wageni sana wa jiji hili, macho yao yaliendelea kuvutwa na vitu mbalimbali siku yao ya pili walipoamua kuzunguka jijini.Walikodi gari lililowatembeza kila mahali kufuata matakwa yao. Kwanza, walipenda kuona mto ule maarufu unaougawa mji wa London, Thames. Waliyatazama maji yake yanayopita kwa utulivu pamoja na madaraja yake murua. Kisha walizunguka katika miji ya Kingstone, Bromley, Croyon na kwingineko, wakiona mambo tofautitofauti katika mitaa mashuhuri kama Oxford, Kingsway, Dean na Sheftebury. Usiku ulipoingia walikwenda katika jumba la Her Majesty kutazama michezo ya kuigiza.

“Kesho tutakwenda kutembea Epping Forest,” Joram alimnong’oneza Nuru walipokuwa wakirudi hotelini kwao.

“Ningependa kuingia Richmond Park,” Nuru alimjibu.

“Nilipokuja kozi hapa miaka minne iliyopita nilidhamiria kuingia lakini sijui ilikuwaje nikashindwa, safari hii nisingependa kushindwa tena.”

“Huwezi kushindwa. Tuna muda na pesa. Tutafanya kila kitu ambacho roho itatutuma kufanya. Nafasi kama hii hutokea mara chache sana katika miaka ya maisha yote ya binaadamu.”

Chumbani kwao walivua uzee na kuurudia ujana wao. Wakatazamana na kucheka kidogo. Kisha walikumbatiana na kuongozana kitandani. Muda mfupi baadaye Nuru alikuwa akikoroma taratibu, huku Joram akinyata kukiacha kitanda. Aliiendea mizigo yao na kuikagua kwa makini. Kila kitu kilikuwemo kama kilivyokuwa kimehifadhiwa. Akatoa kile kisanduku chenye vigololi na kuvitazama kwa makini. Kisha alivirudisha na kuchukua vitabu vyake ambavyo alikuwa akivisoma au kufanya majaribio ya maandishi na mahesabu kwa umakini na utulivu. Mara kwa mara alichana karatasi hii na kujaribu ile, mara akiacha kuandika na kuanza kusoma kwa umakini, kisha akianza tena kuandika.

“Siwezi kukusaidia mpenzi?”

Sauti ilimzindua Joram kutoka katika lindi hilo la shughuli iliyokuwa mbele yake. Aligeuka na kumtazama Nuru ambaye alitulia nyuma yake, uchi kama alivyozaliwa, macho yake yakitazama mahesabu katika karatasi za Joram.

“Samahani kwa kukuvuruga. Nimekuwa nyuma yako kwa zaidi ya saa nzima sasa. Nadhani hata hujui kuwa kumepambazuka.”

Ndipo Joram alipotupa macho nje. Hakuamini. Nuru ya jua lililochomoza kitambo ilikuwa ikipenya dirishani kwa uangalifu. “Samahani Nuru. Usingizi ulinipaa ndipo nikaja mezani kupoteza muda,” alisema akianza kufunika karatasi zake.

“Kupoteza muda?” Nuru alimwuliza. “Nimekutazama kwa muda mrefu sana. Hata kuna nyakati ambazo ulikuwa ukisema peke yako. Najua una jambo ambalo linakusumbua, jambo ambalo umeamua kuliweka siri rohoni mwako. Hutaki kunishirikisha. Huniamini hata kidogo! Sijui nifanye nini ili uniamini Joram!”

“Ndiyo. Afanye nini ili amwamini?” Joram alijiuliza. Msichana huyo ambaye ameacha kila kitu hata kazi na nchi yake ili awe pamoja naye! Msichana ambaye kuwa nae kumemsaidia sana katika kujifariji na msiba wa Neema na aibu aliyoipata kwa kushindwa kumuua Proper! Msichana ambaye majuzi tu aliyaokoa maisha yake kwa kumwua mtu ambaye angemwangamiza bila huruma! Zaidi ni msichana mzuri wa sura na tabia, msichana ambaye ni ndoto ya kila mwanaume!

“Sikia Joram, huwezi kukadiria kiasi gani nakuamini na kukutegemea. Sifai kuambiwa lolote. Kwako mimi ni mwanamke tu ninayefaa kwa mapenzi ya kimwili. Siwezi kuwa Neema ambaye alikuwa mwenzi wako kikazi ambaye kimwili hukuwahi kumgusa.”

“Sivyo Nuru.”

“Wala sifahi lolote hata kukusaidia katika hesabu za fizikia unazopiga au kusoma maandishi hayo na kuyalinganisha na hayo ya kijasusi kama unavyofanya. Sifai hata kwenda maktaba kukusaidia kupekua walao kitabu unachokihitaji.”

“Nuru!” Joram alifoka kwa sauti ambayo masikioni mwa mtu asiyemfahamu ingekuwa ya kawaida tu. “Nilidhani wewe ni mtu pekee unayeweza kunielewa. Nilidhani unaifahamu tabia na msimamo wangu. Sina tabia ya kuyachukua matatizo yangu na kuyabwaga mikononi mwa binadamu mwingine. Sijazowea kuchukua fumbo ambalo limenishinda kufumbua na kumwomba mtu mwingine anisaidie. Wala tabia hiyo siwezi kuianza leo. Hivyo, ninapokuambia sina la kukuambia maana yake sina la kukuambia. Nadhani umenielewa.”

“Nadhani nimekuelewa. Hata zile pesa ulizozipokonya City Drive, ambazo tunachezea sasa naamini ni fumbo jingine ambalo hukupenda kulifumbua. Sivyo mpenzi?”

Joram akatabasam, “Yaelekea mimi na wewe tutakuwa na safari ndefu kimaisha.”

Wakashikana mikono na kurudi kitandani.

Baada ya kuzitawala na kuzinyonya sana nchi zetu nyingi za Kiafrika, na baada ya ‘kutoa’ uhuru shingo upande, Uingereza iliendelea kujifanya baba na mama wa makoloni yake ya awali. Falsafa hii ndiyo chanzo cha vijimsaada kadha wa kadha. Eti pia Uingereza ndiyo mtaalamu wa habari zinazohusu nchi zilizokuwa chini ya himaya yake. Na habari ambazo hupata nafasi katika vyombo vya habari mara nyingi huwa ni zile ambazo si nzuri sana kwa masikio ya wasikilizaji, yaani habari za aibu, kushindwa, rushwa udikteta, uzembe na kadhalika. Uteuzi huu wa habari hizo mbovu na kuacha zile njema ni ushahidi mwingine ambao huonyesha kuwa Uingereza ingependa kuendelea kuitawala Afrika hadi siku ya mwisho ya dunia.

Habari za wizi wa fedha za kigeni katika Tanzania zilikuwa tamu mno katika magazeti, redio na televisheni zote za Uingereza. Zilipambwa kwa wino na rangi mbalimbali na uongo ainaaina hata zikawa kubwa kuliko zilivyostahili kuwa. Hiyo ilitokana hasa na mwizi wa pesa hizo alivyokuwa mtu maarufu duniani. “Ndivyo walivyo waafrika…” liliandika gazeti moja.”Kati yao hakuna mwaminifu…” Gazeti jingine lilipendekeza kuwa Tanzania isipate msaada wowote wa kimataifa bila ya pesa hizo kurudishwa. “Tunaamini kilichofanyika ni njama tu baina ya Joram na viongozi wa serikali yake,” Televishen moja ilitangaza.

Habari hizo zilianza kuwa za kawaida machoni na masikioni mwa Joram na Nuru. Hawakuzijali wala kuzishughulikia. Hata hivyo, kuna gazeti hili ambalo liliwashtua zaidi. Mwandishi wake alikuwa amesafiri hadi Dar es Salaam ambako alifanya utafiti wake binafsi, akihonga hapa na kuiba habari pale hata akawa ameunganisha taarifa ambayo ilidai kuwa Joram alikuwa ametorokea Nairobi kwa ndege ya kukodi. Mwandishi huyo alisafiri hadi Nairobi ambako utafiti wake ulimfikisha katika chumba alichokuwa Joram na Nuru kwa majina bandia. “Kwa kila hali sasa hivi Joram yuko London,” lilieleza gazeti hilo. “Dunia haiwezi kupumbazwa na hila zake za kujibadili sura na umbile. Kwa hali ilivyo, atakuwa akiishi katika hoteli kubwa kwa jina la bandia.”

“Imekuwa tabia ya kawaida,” gazeti hilo liliendelea kueleza. “Kila wanapofanya madhambi yao huko kwao hukimbilia huku. London imejaa watu weusi ambao wanaishi wanavyotaka baada ya kufanya maovu – au mema ambayo yalionekana maovu – huko makwao. Wako wachoyo, wahujumu, wazembe, wanafiki na kadhalika. Wengi wameziacha nchi zao zikiwa masikini zaidi huku roho za watu zikiteketea katika vita na mauaji yasiyo na mwisho. Uingereza tunawakaribisha na kuishi nao kama binadamu wenzetu. Miongoni mwa watu hawa sasa yumo Joram Kiango, mtu aliyejifanya na akaaminika kuwa ana roho ya kipekee yenye upendo na ushujaa kama ngao kwa jamii yake. Kumbe alikuwa fisi katika ngozi ya kondoo. Huyu, Uingereza haiwezi kumstahamili. Lazima apatikane, ahukumiwe na kupokonywa kila senti aliyobaki nayo.”

Nuru alimaliza kuisoma habari hii huku akitetemeka kidogo. Lakini ilimshangaza alipoinua uso na kukutana na ule wa Joram ambao ulikuwa ukichekelea. Hilo lilimshangaza. Akiwa mtu ambaye ameishi na Joram kwa kipindi cha kutosha, alikuwa na hakika kuwa amemfahamu Joram vya kutosha. Asingelaghaika kama watu wengine kung'amua wakati gani anacheka kwa hasira na wakati upi anajifanya kuchukia hali amefurahi. Tabasamu hili, ambalo lilikuwa likiendelea kuchanua katika uso wa Joram, halikuwa tabasamu batili, bali tabasamu halisi, tabasamu ambalo huutembelea uso huu kwa nadra sana. Hivyo, ilimshangaza sana Nuru. Alimtegemea Joram kujisingizia kucheka huku rohoni akibabaika na kukata tamaa. Si kushangilia kama aliyepata tuzo au ushindi mkubwa baada ya shindano gumu.

"Sijakuelewa Joram, sidhani kama hii ni habari njema," alimwambia.

"Wala sidhani kama una haki ya kutegemea habari njema tangu ulipokubali kuandamana na mwizi mkubwa kama huyu," Joram alimjibu taratibu. Alipoona uso wa Nuru bado una maswali na dalili za kutoridhika, aliongeza, "Kinachonichekesha ni huyu Mwingereza anavyojifanya ana uchungu na nchi yetu kuliko sisi wenyewe. Utafiti aliofanya hautokani na moyo wake wa kuwajibika bali ni nguvu alizonazo kiuchumi, uwezo ambao ameuiba toka katika makoloni miaka nenda rudi." Alikohoa kidogo kabla ya kuongeza, "Hawawezi kunitisha kabisa. Nitaishi hapa nikistarehe katika jiji hili kubwa ambalo linapendeza kwa madini yaliyoibwa toka makwetu, yaliyochimbwa kwa jasho la babu zetu. Nitaondoka hapa tu tutakapokuwa tayari kuondoka. Sivyo, dada Nuru?"

"Nilichosema ni jinsi unavyoifurahia habari hii badala ya kuionea aibu. Sikutegemea. Au nakosea. Pengine hili ni fumbo jingine?"

Joram hakumjibu.

***

Jioni hiyo maisha yaliendelea kama kawaida. Joram alijipitisha hapa na pale akifanya hili na lile. Sasa ilikuwa dhahiri kwa Nuru kuwa alikuwa katika shughuli kubwa na ngumu kinyume cha alivyoiruhusu sura na sauti yake kuonyesha. Nuru hakujisumbua kumuuliza lolote akichelea kupoteza muda wake kwani ingekuwa sawa na kumpigia mbuzi gitaa ukimtegemea kucheza rumba. Hata hivyo, Nuru alipopata wasaa alimkabili Joram na kumwambia taratibu,"Unadhani mwandishi yule anatania anaposema watafanya juu chini kututafuta? Huoni kama tunaweza kupatikana? Hila hizi za kujibadili si zimekuwa teknolojia ya kawaida siku hizi? Sidhani kama zinaweza kutusaidia."

"Najua, mpenzi. Ninachojivunia ni wingi wa watu na ukubwa wa jiji hili. Itachukua muda hadi wafike hapa na kutukamata. Wakati huo hatutakuwa hapa tena, bali tutakuwa angani tukimalizia kuitembelea nchi ya mwisho ya dunia. Usijali Nuru. Starehe bila hofu yoyote…"

Joram hakuumalizia usemi wake kabla ya kuusikia mlango ukigongwa. Wakatazamana huku wakisikiliza. Mlango uligongwa tena kwa nguvu kuliko mwanzo. Joram hakuwa mgeni na ugongaji wa polisi. Kwa mara ya kwanza akajikuta kuwa alikuwa amekosea sana kuwadharau polisi wa Uingereza kiasi hicho. Akamtupia Nuru jicho ambalo lilibeba ujumbe ambao masikioni mwa Nuru ulieleza waziwazi "Cheza nao." Papo hapo akatoka na kuingia bafuni huku akiufunga mlango nyuma yake.

Mlango ulipogongwa tena Nuru aliinuka na kuufungua. Kama alivyotegemea mlango ulipofunguka aliingia askari mmoja mwenye cheo cha Sajenti akifuatana na mmoja kati ya maofisa wa hoteli hiyo.

"Samahani sana dada," afisa huyo alieleza. "Tumelazimika kukusumbua kidogo. Nadhani utatuwia radhi. Huyu hapa ni Sajini Brown kutoka Scotland Yard, yuko katika ziara ya kuwatembelea wageni wote wa hoteli hii ili kutazama hati zao za usafiri na maswali madogo madogo ambayo nadhani utamjibu. Ni mzunguko wa kawaida tu kwa ajili ya tukio dogo ambalo wangependa kulikamilisha ili wasirudi tena katika hoteli hii."

"Bila samahani,"Nuru alijibu akimgeukia polisi huyo ambaye alikuwa akitoa kitambulisho chake.

"Kwa kawaida hapa kwetu hatusumbui wageni," askari huyo alieleza. Tunatimiza ombi la INTERPOL tu," alisita akimtazama Nuru kwa makini zaidi. Sijui dada unaitwa nani?"

"Mrs Prosy Godwin".

"Kutoka?"

“Naijeria”.

“Yuko wapi bwana Godwin?”

“Ametoka, nadhani atarudi baada ya dakika chache.”

“Naweza kuona hati zenu za usafiri pamoja na nyaraka nyingine kama zipo?”

“Bila shaka,” Nuru alimjibu akiendea mfuko ambao aliufungua na kutoa hati. Akazikabidhi kwa askari huyo ambaye alianza kuzipekuapekua.

Dakika hiyohiyo mlango wa bafu ulifunguka. Askari alipogeuka kutazama alikutana na pigo ambalo lilitua katika shingo yake kikamilifu. Pigo lililokusudiwa kummaliza, lakini halikutimiza wajibu. Lilimfanya apepesuke na kuegemea ukuta. Mkono wake ukapaa kukinga pigo la pili huku mkono wake wa pili ukisafiri kuitafuta bastola. Joram hakuruhusu mkono huo utoke na bastola. Aliachia judo ambayo ilitua ubavuni mwa askari huyo na kumlegeza. Pigo lililofuata lilimlazimisha kuanguka sakafuni. Baada ya kazi hiyo ndipo Joram alipomgeukia afisa wa hoteli ambaye alikuwa kaduwaa, mdomo wazi, kama asiyeamini macho yake.

“Mwinue ndugu yako na umpeleke bafuni,” Joram alimwamuru.

“Vipi bwana Godwin? Nadhani hukumwelewa huyu bwana. Alikuwa hana nia mbaya zaidi ya… ya…”

Joram hakuwa na muda wa kuchezea. Alijua afisa huyu alihitaji nini kumtoa mshangao. Pigo moja tu, ambalo halikutegemewa lilimfanya afisa huyo aanguke chini kama gunia. Hima, Joram alianza kuwavutia bafuni mmoja baada ya mwingine. Kisha aliufunga mlango wa bafu kwa funguo na kumfuata Nuru ambaye pia alikuwa ameshangaa.

“Kwa nini umefanya hivyo Joram? Haikuwepo kabisa haja ya kuwashambulia. Askari huyo asingegundua lolote. Sasa watajua kuwa uko hapa na wataanza kututafuta kwa udi na uvumba.”

Si kitu. Kwa nini tujikombekombe kwao? London si mji mzuri pekee yake katika dunia hii. Bado tuna haja ya kuiona miji mingine.”

“…Ni mtu wa hatari duniani. Ameidhihirishia dunia kuwa hana tofauti na yule mwuaji mwingine anayetafutwa duniani kote, Carlos. Sasa kinachotakiwa kufanyika si kumtafuta yeye bali roho yake. Vinginevyo, dunia itakuwa imestarehe ikisubiri kuimarika kwa kiumbe mwingine wa hatari zaidi ya faru mwenye wazimu.”

Hayo yalikuwa mapendekezo ya mwisho katika gazeti lile lililohisi kuwepo kwa Joram Jijini London, na hatimaye kuandika juu ya tukio la kutisha lililowapata askari wa Scotland Yard na Afisa wa hoteli. Watu hao ambao walifunguliwa kutoka katika bafu saa kadha wa kadha baada ya Joram kuondoka zake, walieleza jinsi walivyowakabili watu ambao mtu yeyote asingefahamu kuwa wangeweza kuwa Joram Kiango na Nuru. Askari huyo alieleza hayo akiwa katika chumba cha X-ray, kuangalia uwezekano wa kuungika kwa mbavu zake tatu zilizovunjwa na Joram.

Baada ya kuongea nao kwa marefu na mapana ndipo waandishi wa gazeti hilo wakatoa habari hizo zikiwa zimepambwa kwa picha nyingi za kuchora, picha ambazo ziliwachora Joram na Nuru katika sura na mavazi tofauti; wakijaribu kuonyesha jinsi gani wanavyoweza kujibadili. Chini ya michoro hiyo kulikuwa na maelezo yaliyoandikwa kwa herufi nzito yakisema; “Unashauriwa kujihadhari nao. Ukimwona ua kwanza, uliza maswali baadaye.”

3

Gazeti hilo lilisomwa kote duniani. Maelezo yake yalidakwa na TV na redio zote duniani. Watu wengi, ambao walimchukia Joram walizidi kushangilia, hali wale waliompenda walizidi kushangaa.

"Sijui amepatwa na nini mtoto huyu,"Inspekta Kombora alifoka huku akilitupa gazeti hilo mezani. "Yuko London na anafanya anavyojua. Anazidi kulipaka matope jina lake ambalo tayari amelichafua."

Ilikuwa dhahiri kwa yeyote amtazamaye Kombora machoni kwamba alikuwa hajapata usingizi wa kutosha kwa muda mrefu. Mambo mengi yalimkabili kichwani kiasi cha kumpokonya hata hamu ya kula. Angewezaje kustarehe wakati siku zilikuwa zikisogea huku halijapatikana lolote la haja katika kukomesha tishio kutoka nchi adui ambalo lilitaka serikali iache msimamo wa kimapinduzi, la sivyo ajali zingeendelea kutokea. Tanzania kuacha kuzisaidia nchi zinazopigania haki na uhuru wake ilikuwa ndoto ya kupendeza. Kamwe isingetokea. Lakini kuendelea kusaidia nchi hizo huku ukisubiri maafa ya hatari sana, kwa nchi yake na rafiki zako hali huna uwezo wa kufanya lolote ilikuwa ndoto ya kusikitisha sana, ndoto ambayo ingeweza kutokea.

Walikuwa wamefanya yote ambayo wangeweza kufanya katika juhudi za kuhakikisha usalama. Yote; mema kwa maovu. Magereza ya Keko na Ukonga yalikuwa yamejaa wageni wengi ambao ama waliingia nchini kinyume cha utaratibu, au hati zao zilitia mashaka. Wote hawa walihojiwa kwa maneno na vitendo. Waliokuwa watakatifu waliachiwa, wenye madhambi ya magendo na uzururaji wakifunguliwa mashitaka. Ni mtu mmoja tu ambaye alielekea kuwa na mengi au machache ambayo yangehusiana na usalama wa nchi.

Huyu alikamatwa katika hoteli ya New Africa baada ya kulala hapo kwa siku moja. Wapelelezi walimshuku baada ya kumsikia akiulizauliza maswali juu ya watu walikufa katika hoteli hiyo; ni wa aina gani na walikufa vipi. Alipokamatwa na kutakiwa kutoa vitambulisho, hati zake zilionyesha kuwa ni mwanachama wa ANC ambaye ametoroka kutoka Namibia. CID waliwasiliana na ofisi hizo. Jina la Kweza halikuwemo katika orodha ya wanachama wa ANC. Ndipo lilipofunguliwa bomba la maswali dhidi yake. Na ni hapo ilipodhihirika kuwa hakuwa mtu wa kawaida jinsi alivyoweza kuyajibu maswali yote kwa ukamilifu kama ambaye alijiandaa kuyajibu.

Begi lake ambalo lilikaguliwa harakaharaka bila ya kuonekana chochote, lilipekuliwa tena. Baada ya jitihada kubwa iligundulika mifuko ya siri ambayo ilificha silaha, vyombo vya mawasiliano na vitu mbalimbali vya kijasusi. Alipoulizwa alikovipata alikanusha kuwa havifahamu, wala hakupata kuviona vitu hivyo. Ni majibu hayo ambayo yalimuudhi Kombora hata akaamua apelekwe katika chumba cha mateso ili, kama hasemi, autapike ukweli. Taarifa zilizomjibu Ispekta Kombora zilisema kuwa alikuwa hajasema lolote.

Ndipo alipolitupa gazeti alilokuwa akisoma habari za Joram, na kumtoa akilini kwa muda. Akaondoka na kuingia katika lifti ambayo ilimteremsha chini ya ardhi kiliko chumba cha mateso. Kombora hufika katika chumba hiki kwa nadra sana. Harufu ya mchanganyiko wa damu, kinyesi, jasho na machozi ni jambo moja ambalo humfanya aape kuwa asingerudi tena kila anapofika humu. Jambo jingine ni sura za watesaji. Sura hizi humtisha zaidi ya mateso yenyewe, zikimfanya aamini kuwa watu hao kama kweli wana roho, basi wana roho za chuma. Nayo macho ya wanaoteswa si jambo ambalo macho ya mtu mstaarabu yatapendezwa kuangalia.

Leo hii alimkuta Kweza, au kilichosalia katika umbo la aliyekuwa Kweza; akiwa amelala sakafuni, sura yake ikiwa haitambuliki kwa kuvimba na kuchubuka. Vidole vyake vyote tayari vilikuwa vimevunjika, jicho moja limetumbuka na meno manne yamepotea. Watesaji walikuwa wamemwinamia wakimdunga sindano ambayo ilikuwa na waya, iliyotokea katika soketi ya umeme.

"Mwachieni kidogo," Kombora aliamuru akikiendea kiti na kuketi. "Mleteni hapa."

Kweza alisimamishwa mbele ya Kombora, akitetemeka kwa uchungu na maumivu makali. Nusura Kombora amhurumie, huruma hiyo ilimtoka mara moja mara alipomfikia mtu huyo; mtu mweusi; kibaraka, msaliti wa juhudi za weusi wenzake katika kujikomboa kutoka kwenye udhalimu ambao umewaandama miaka nenda rudi. Mtu kama huyu ahitaji kuhurumiwa hata chembe.

“Wewe!” Akafoka. “Kwa nini hutaki kusema ukweli? Kama ukisema ukweli tutakuacha uende zako.”

Pamoja na maumivu aliyokuwanayo mtu huyo, alicheka, “Nimekwisha sema kila kitu. Tatizo lenu ni kwamba hamtaki kuelewa ninachosema. Na juu ya kuniacha niende zangu nimewaambieni mara nyingi kuwa sihitaji kwenda popote. Naomba mkichoka kunitesa, mniue.”

“Umesema ukweli? Ukweli gani?”

“Nimesema kuwa mimi sifahamu chochote juu ya maswali mnayoniuliza. Nilichofuata ni kumtafuta rafiki yangu Chonde ambaye inasemekana amefariki. Nilitaka kufahamu amefariki vipi ili niitulize roho yangu.

“Chonde rafiki yako vipi?”

“Alikuwa rafiki wa kalamu. Sikuwahi kuonana naye ana kwa ana.”

Kombora alimtazama kwa makini. Macho yake makali yalimfanya Kweza aangue tena kicheko dhaifu huku akisema, “Mnaupoteza bure muda wangu na wenu. Mimi sifahamu chochote. Nanyi hamna lolote ambalo mnaweza kufanya zaidi ya kusubiri maafa kama nilivyoambiwa. Mwenye akili ningemshauri aikimbie nchi hii mapema badala ya kusubiri kifo cha kutisha cha moto mkali utakaokuja na ufukara wa kutisha baada ya moto huo.” Akaangua kicheko kingine dhaifu. Safari hii alicheka kwa muda hata akateleza kutoka mikononi mwa askari waliomshika na kuanguka chini. Hapo chini alitulia kwa muda kisha akapapatika na kukata roho.

Kombora na wenzake walisogea na kuimana wakimtazama. Hakuna aliyefahamu kama alikuwa na sumu kinywani au aliitapika roho yake. “Miujiza, iliyoje!”

SURA YA SABA

WALIKUWA wameitembelea miji mingi maarufu ya dunia. Walionja anasa na starehe za kila mji. Baada ya kutoroka kutoka London kwa hima walikwenda Ufaransa ambako walipitia miji mbalimbali na kuingia Paris. Toka Paris walikwenda New York ambako hawakukaa sana kabla ya kuruka tena hadi Washington, HongKong, Moscow na kwingineko.

Ingawa ziara yao ilikuwa ya starehe, lakini ilikuwa ziara ngumu kiasi cha kumtatanisha Nuru na kumsisimua Joram. Safari zao nyingi zilikuwa za kujificha ficha usiku na mchana kuwaepuka polisi na wapelelezi ambao ama walimhitaji Joram kwa makosa ama kuzishuku hati zao za usafiri, ambazo mara kwa mara zilikuwa za bandia. Hila za hali ya juu, pamoja na ruswa nzito, ni njia pekee iliyowafanya wafanikiwe kuiepuka mitego yote ya CID, KGB, INTERPOL na wapelelezi wa nchi mbalimbali.

Katika tukio moja kwenye mji mmoja, ilimlazimu Joram kujifanya mwanamke malaya ili kuwaepuka polisi ambao waliizingira hoteli aliyokuwemo. Polisi hao walipoingia katika chumba ambamo walitegemea kumnasa Joram walijikuta wakirudi nje kwa aibu baada ya kukuta wasichana wawili, waliofanana kwa uzuri, wakiwa nusu uchi juu ya kitanda chao kwa namna ya kufanya mapenzi ya wao kwa wao. Wakati askari hao wakisubiri nje ili kuwahoji vizuri, Joram na Nuru walitumia dirisha kuondoka zao na kila kilichokuwa chao.

Katika tukio jingine Joram alilazimika kuiteka nyara ndege ndogo ya abiria na kuilazimisha kutua katika uwanja ambao haukukusudiwa jijini New York. Kutoka uwanjani hapo walipata kinga kwa risasi za askari walioizingira ndege hiyo kwa kuwachukua rubani na msaidizi wake huku wakizielekeza bastola katika vichwa vyao. Polisi walikuwa wakiwafuata kwa mbali, televisheni ikiwaona na kuwaonyesha kwa kila mtu. Lakini ilifika mahali ambapo si polisi wala rubani waliojua kilichotokea. Polisi waliikuta ndege hiyo ikiwa imesimama kando ya nyumba, marubani wakiwa usingizini kwa kunusa dawa fulani bila kutaraji. Watu walioshuhudia tukio hilo, wakiwa hawajui kinachotokea, walidai kuwa waliwaona “vijana wazuri” msichana na mvulana wakishuka kutoka ndege hiyo na mizigo yao na kuingia katika jumba la jirani ambamo hawakuonekana wakitoka tena.

Harakati na machachari yao katika miji mbalimbali ziliondokea kuwa habari ambazo ziliwavutia sana waandishi wa habari. Mara kwa mara televisheni, redio na magazeti zilitoa habari zinazowahusu; Leo kaonekana hapa; hapa kafanya hivi; pale alifanya vile, na kadhalika.

Habari hizo zilipambwa kwa picha zao zinazovutia, kurudiwarudiwa kwa historia ya maisha ya Joram kiango pamoja na kutiwa chumvi nyingi ili kugusa masikio ya watu wote na kumsisimua kila mmoja. Hivyo, jina lilipanuka na athari kuneemeka. Ilikuwa kama dunia imesita kushughulikia masuala yaliyo muhimu na kuandamana na Joram katika ziara yake hii ndefu, jambo ambalo lilimfanya kila mpelelezi kuwa na hamu kubwa ya kubahatika kumtia mikononi Joram ili amfikishe kunakohusika.

Jambo ambalo lilimshangaza Neema katika mkasa huo mzima ni jinsi ambavyo alielekea kufurahishwa na jinsi habari hizo za aibu juu yake zilivyopata nafasi kubwa katika vyombo vya habari. Iliendelea kumfurahisha Joram badala ya kumchukiza. Nuru ambaye alimfahamu Joram asivyopenda sifa alijikuta akijawa na msgangao kwa mabadiliko hayo ya Joram.

Hata hivyo mshangao wake ulianza kupungua pale Joram alipoanza au alipolazimika kumshirikisha katika baadhi ya mambo aliyokuwa akiyafanya. Jambo la kwanza lilikuwa mazoezi ya viungo. walifanya kila starehe, lakini baada ya starehe, wakiwa chumbani kwao, walifanya mazoezi makali ya viungo. Mazoezi ambayo awali yalimtoa Nuru jasho, machozi na damu. Lakini baada ya muda machozi na damu vilikoma na jasho kupungua. Akawa hodari, akiwa bega kwa bega na Joram katika kila jambo. Zoezi la pili lilikuwa la matumizi ya silaha mbalimbali ambazo Joram alikuwa akizinunua kwa siri sana.

Alimwelekeza Nuru namna ya kuzificha mwilini, namna ya kuzitumia na kumfundisha jinsi ya kulenga shabaha kwa ukamilifu. Nuru alikuwa mwepesi wa kuelimika.

Hayo yaliufanya moyo wa Nuru uwe na tumaini kubwa. Sasa aliamini kuwa Joram alikuwa na jambo fulani zito la muhimu ambalo alikuwa akishughulikia. Pengine katika safari hiZo za mji hadi mji alikuwa akimhitaji mtu kwa madhambi fulani. Mtu gani huyo? Na ni madhambi gani aliyoyafanya?

Maswali ambayo yaliimarika hasa kutokana na simu nyingi ambazo Joram alikuwa akipiga kwa rafiki zake sehemu mbalimbali ulimwenguni, ambazo mara kwa mara zilikuwa katika mafumbo ya aina aina. Japo alimsikiliza kwa makini Nuru hakuambua chochote cha haja, zaidi ya kuishia kuhisi tu. Wakati wote huo Joram hakukoma kujifungia.

Halafu ikaja jioni ya leo, ambapo Joram alionekana mtulivu kuliko ilivyokuwa siku zote. Sigara ziliteketea mdomoni mwake moja baada ya nyingine, macho yake yakimtazama Nuru ambaye alikuwa ameketi juu ya meza ya kuvalia akishughulikia nywele zake. Joram alimtazama kwa makini kwa dakika kadhaa, kisha alimsogelea na kumshika bega.

“Nilichoshika hapa ni kipande murua cha kazi ya sanaa ambayo ni mfano halisi wa kazi ya Muumba. Nadhani hana budi kujivunia mafanikio yake”, alisema akitabasamu.

Nuru aliinua uso kumtazama.

“Kwa bahati mbaya kazi hii ya sanaa iki katika hatari ya kuharibika endapo itandelea kuandamana na binadamu wenye akili mbaya kama Joram Kiango”.

Hilo lilimfanya Nuru atabasamu. Alijua Joram anaelekea wapi. Siku hizi mbili alikuwa akimchunguza kwa makini na kuona mabadiliko katika fikira zake. Alikuwa akiona na kushuhudia kutoweka kwa ile starehe ya kujisingizia katika nafsi ya Joram na badala yake starehe kamili kuchukua nafasi yake. Mfano wa mtu ambaye yuko katika jahazi hafifu katikati ya bahari iliyochafuka anapobahatika kufika pwani salama. Hivyo alijua kuwa Joram ana neno. Akamhimiza kulisema kwa kumwambia, “Unachotaka kufanya Joram ni kunitisha… Lazima uelewe kuwa sitishiki ng’oo. Tumekuwa nawe katika heri na shari. Tutakuwa pamoja jehanamu na peponi. Usijisumbue kuniambia lolote lenye dhamira ya kututenga”.

Joram akacheka. “Una akili nyepesi sana Nuru”, akamwambia. “Nilichokuwa nikielekea kukuomba ni kukushauri urudi nyumbani, uniachie kazi iliyoko mbele yangu. Ni kazi chafu, ya hatari, yenye nuksi, ambayo sidhani kama itanifanya nirudi nyumbani na roho yangu”.

“Nimekwisha sema usijisumbue kunitenga. Nina hamu na kazi nzito, chafu yenye damu. Sijasahaun nilivyoshirikishwa kuwaangamiza wakuu wa nchi wasio na hatia. Nahitaji kujitakasa. Ni damu pekee itakayonitakasa. damu ya adui wa Afrika.

Joram aliduwaa huku akimtazama msichana huyo. Hakuwa na shaka kuwa msichana huyo ni shujaa. Lakini hakujua kuwa ni shujaa kiasi hicho. Ndiyo, alimtegemea sana katika msafara wake. Lakini hakukusudia kumwingiza katika mkasa ambao ilikuwa dhahiri kuwa pamoja na ugumu wa maandalizi yake ya muda mrefu hadi sasa matekeo yake yalikuwa gizani. Yeye alikuwa tayari kwenda, tayari kufanya kazi inayompeleka;

uwezekano wa kurudi haukumsumbua. Kufa kusingemtisha sana mradi atakuwa ameifanya kazi yake. Kifo chake ni jambo moja, kusababisha kifo cha mtoto wa watu, mzuri kama Nuru, ni jambo jingine.

"Sikia Nuru. Labda huelewi… Nakusudia kwenda toka hapa sio nchi ya kawaida. Ni nchi ambayo kuna watu wenye kiu kubwa ya damu ya mtu mweusi na njaa kubwa ya roho zetu. Na ninahitaji kujipeleka moja kwa moja mikononi mwao. Kwa ufupi nategemea kwenda Afrika Kusini…".

"Tutakwenda pamoja".

…Na ninachokwenda kufanya ni hujuma. Wakinigundua watanitafuna mbichi".

"Watatutafuna pamoja".

Joram akaduwaa. "Labda nikufunulie kila kitu kilivyo Nuru", Joram akamwambia. ""Nisubiri", alisema akiliendea begi lake lililokuwa limefurika kwa vitabu aina aina pamoja na encyclopedia ambazo Joram alikuwa akizitumia kwa muda mrefu kujaribu kuyasoma yake maandishi ya kijasusi ambayo aliyapata katika mfuko wa hayati Chonde. Humo alitoa karatasi ndefu, iliyoandikwa kwa mashine, ikiwa tafsiri ya maandishi hayo. Alimkabidhi Nuru na kumwabia asome haraka haraka.

MPANGO KABAMBE WA KUIFANYA AFRIKA ITUPIGIE MAGOTI

Taarifa hii ni siri kubwa miongoni mwa watu wachache sana, wa ngazi za juu katika serikali yetu. Ni taarifa ya mafanikio ya jaribio lililofanyika muda mrefu, kwa gharama kubwa, baina ya wana sayansi wetu na waliotoka katika nchi marafiki duniani; juu ya uwezekano wa kufanya nguvu za nukria zitusaidie katika kuwaweka Waafrika, na ikiwezekana dunia nzima katika kwato zetu.

Itakumbukwa kuwa kifungu kikubwa cha pesa kilitengwa ili kufanyia majaribio haya. Kwa siri kubwa sana mtambo madhubuti ulijengwa na setilaiti kutupwa angani. Mbili kati ya setilaiti hizo zilidondoka katika nbahari ya Hindi kabla ya kuonyesha matokeao. Lakini setilaiti ya tatu imetimiza majibu. Majaribio yamefanywa na kuleta matokeo ya kuridhisha kabisa. Mtu wetu alitumwa Lagos na kutega gololi maalumu ambazo baada ya kufyatuliwa zimeifanya setilaiti hiyo iliyoundwa kwa madini yanayoifanya isionekane kwa macho iweze kuingia katika anga la nchi hiyo na kuachia bomba la moto mkali ambao uliteketeza uwanja na watu kadhaa. Jaribio la pili lilifanywa huko Harare ambako maghala yaliteketea. Jaribio la tatu na la mwisho linakusudiwa kufanywa Tanzania, katika jengo la Benki Kuu inayojengwa. Hatuna shaka kuwa jaribio hilo litafanikiwa.

Baada ya jaribio hilo ndipo tutaanzisha mpango wa kuzifanya nchi zote zinazojiita za mstari wa mbele, kutupigia magoti. Mtu wetu anayekwenda Tanzania ni mtu wa kutegemewa, aliyeishi huko miaka mingi. Atapewa pesa nyingi zitakazomwezesha kwenda mahala popote duniani, na kumnunua mtu yeyote. Huyu atakuwa na jukumu la kusubiri amri yetu ili aachie vipigo vingine ambavyo vitaifanya Afrika itokwe na machozi huku dunia ikilalamika…

Nuru aliinua kichwa ghafla kumtazama Joram. Tayari uso wake ulikuwa umelowa jasho la hofu na mshangao. "Joram" Nuru alifoka, "Mungu wangu. Huoni kama hii ni habari ya kutisha kuliko zote? Tunawezaje kustarehe hivi huku nchi yetu ikiwa mashakani?".

"Imenichukua siku nyingi kuigundua. Waliyaficha maandishi hayo kwa hila ambazo zingemtoa jasho mtu yeyote mwenye akili timamu. Hata hivyo ugunduzi huu hautatusaidia chochote. Kama ulivyosoma setilaiti hiyo iko angani na haionekani kwa macho. Inaendeshwa na mtambo ambao uko katika himaya yao, bila shaka ukilindwa kwa hali na mali. Hakuna njia nyingine zaidi ya kuubomoa mtambo huo".

"Je. Tukitoa siri hii kwa dunia?", Nuru alimuuliza Joram.

"Haisaidii. Umoja wa Mataifa utalalamika na kuilaani Afrika Kusini. Pengine watawekewa vikwazo vya kiuchumi. Unadhani hayo yatawafanya watuhurumie?". Mara ngapi wamelaaniwa? Mara ngapi wamewekewa vikwazo? Hapana Nuru. Lazima nifike Afrika Kusini. Dawa ya moto ni moto".

Nuru alitulia kwa muda akiitafakari taarifa hii kwa makini. Mara aliinuka na kumwendea Joram. Akamkumbatia na kumnong'oneza masikioni. "Samahani sana mpenzi. Nilikuelewa vibaya sana ulipoiba pesa benki. Vilevile nilishangaa unavyozitumia pesa hizo vibaya kwenda huku na kule ukuwa hujali matusi ya waandishi wa habari. Sasa nimekuelewa. Nimeelewa kwanini ulifanya vile. Ulikuwa ukijiandaa kwenda Afrika Kusini.

Ulichofanya ilikuwa kuilaghai dunia ili uonekane mhalifu na mkimbizi asiyeweza kuishi popote isipokuwa Afrika Kusini. “Sivyo mpenzi?”. Joram alipochelewa kujibu Nuru aliongeza, “Mpenzi. Wewe ni shujaa kuliko mashujaa wengine niliopata kuwasikia. Tutakwenda pamoja Afrika Kusini…”.

“Tatizo siyo kwenda Nuru. Tatizo ni kurudi. Unaoneje, tutarudi na zoho zetu?”.

Wakati Joram na Nuru walipokuwa wakizungumza hayo, Kombora alikuwa Ikulu mbele ya Rais akitokwa na jasho jembamba. Alifika ofisini, akiwa hoi kwa ukosefu wa usingizi wa siku kadhaa. Mara alipopata simu ambayo ilimtaka kwenda Ikulu mara moja, alilitia gari lake moto na kufunga safari hiyo ya dharura hadi Ikulu ambako alielekezwa katika chumba cha faragha. Humo aliwakuta Rais, Waziri Mkuu, Waziri wa Ulinzi na Katibu Mkuu katika Wizara ya Ulinzi. Aliwasalimu kishujaa, ingawa tayari moyo ulikuwa ukimdunda kwa kujua kuwa hakuwa tayari kuyajibu maswali yao.

“Nini hiki? Rais alimwuliza akimsogezea kijibarua ambacho kiliandikwa kwa mkono.

Kombora alikipokea na kukitazama. Hakuwa na haja ya kukisoma kwani ilikuwa moja kati ya zile barua ambazo zilikuwa zikiwafikia wakubwa wa nchi za mstari wa mbele mara kuwatisha ili waache msimamo wao dhidi ya Afrika Kusini.

“Isome,” Rais alihimiza.

Kombora akakisoma. Mara alielewa sababu ya kusisitiziwa aisome. Ilisema: “ONYO LA MWISHO.” Ikarudia kutaja sehemu muhimu ambazo aliyeandika barua hiyo alikusudia kuzichoma, sehemu ambazo ni pamoja na Ikulu. Baada ya kuikodolea macho, Kombora aliyarudisha katika uso wa Rais. “Nimeisoma mzee.”

“Barua hiyo imekutwa katika ofisi yangu,” Rais alieleza. “Ni dhahiri kuwa aliyeileta anao uwezo na nafasi ya kufanya lolote katika nchi na ofisi hii. Kwanini mmempa haki hiyo?”

Kombora hakujibu. Hakujua ajibu nini. Yeye na vijana wake wote walikuwa taabani katika mapambano haya. Majasusi wengi ya Afrika Kusini yalishikwa, lakini halikutokea lolote ambalo lingeweza kusaidia kukomesha vitisho vya ainaaina. Mengi yalikuwa majasusi wa kawaida, ambayo ama hawakuwa na lolote la haja au yalitumwa kwa ajili ya masuala yasiyo na uzito mkubwa. Wapelelezi wake ambao walikuwa nje pia walivitesa vichwa vyao bila ya kupata matunda ya kuridhisha. Nusura Kombora apate hasira kwa lawama hizo ambazo hakuona kama zinamstahili. Alitamani ainuke, atangaze kujiuzulu. Lakini hayo hakuyafanya kwa kukumbuka kuwa hasira si dawa. Na licha ya hayo aliona wazi kuwa lawama zilimstahili. Kufanya kazi ni kupata matokeo ya kazi hiyo. Kazi isiyo na matokeo haiwezi kuitwa kazi.

“Sina haja ya kukulaumu,” Rais aliendelea. “Nauona ugumu wa jukumu mlilonalo. Nilichokuitia ili kukukumbusha kwa mara nyingine ni kuwa hata kwa bei ya roho zetu hatuwezi kukubali kufuata masharti ya utawala huu dhalimu. Lazima tupambane nao. Na huu ni wakati pekee wa kuonyesha moyo wetu. Uoga hauwezi kutufanya tukubali kuwa mateka wa utawala haramu kama huu. Lazima tushinde,” akasita kidogo akimtazama Kombora kwa makini. “Inspekta,” aliongeza kwa sauti ya amri kidogo. “Huu ni wakati wako. Kuna wakati wa njaa; wakulima hutakiwa kuiokoa nchi; wakati wa uhaba wa fedha za kigeni wafanyakazi viwandani huombwa kujitoa mhanga; wakati wa vita jeshi hulazimika kulinda nchi. Huu ni wakati wako, Inspekta. Nchi inakuhitaji na kukutegemea. Gavana wa Benki amepewa amri ya kukupa kifungu chochote cha pesa unazohitaji, Mkuu wa jeshi ameambiwa akuruhusu kutumia kikosi chochote na Bunge limependekeza uruhusiwe kufanya lolote. Kazi kwako,” Rais alimaliza akainuka na kutoka.

Kombora alipumbazuka kidogo juu ya kiti hicho. Jasho jembamba lilikuwa likimtoka. Mara akajilaani kwa kusita kuleta barua ya kujiuzulu kwake. Hakujua angefanya nini zaidi. Aliwatazama viongozi ambao walikuwa wametulia, wakimtazama. Kiongozi mmoja alitamka neno ambalo halikumfikia Kombora. Mwingine alitikisa kichwa. Kombora akainuka na kuwaaga. Alipoifikia gari yake ndipo alipokumbuka kuwa ile barua ya vitisho bado alikuwa nayo mkononi. Akaitia mfukoni na kuamuru gari limrudishe ofisini.

Kidole kimoja kamwe hakivunji chawa; Kombora aliwaza akiwa kaketi ofisini mwake akifikiria afanye lipi zaidi kufanikisha vita hivi ambavyo havikuwa na uelekeo maalumu. Akamwagiza opereta wake kumpatia viongozi wa ofisi zote za usalama katika nchi za mstari wa mbele, pamoja na Naijeria. Alipowapata alipanga nao kufanya mkutano wa dharura ambao ulikusudiwa kujadili hali inayozikabili nchi zao. Ilikuwa kama wote walikuwa wakiusubiri kwa hamu wito huu. Wakaafikiana kukutana Jijini Dar es Salaam siku mbili baadae.

Kombora, akiwa mwenyeji, alikuwa Mwenyekiti wa Mkutano huu uliofanywa kwa siri kubwa. Mkutano huu ulijumuisha watu wenye sura mbalimbali, umri tofauti, viwango tofauti vya elimu; wote wakiwa na dhamira moja. Kila mmoja alieleza tishio lililokuwa likiikabiri nchi yake na

kila mmoja alieleza hatua ambazo tayari zilikuwa zimechukuliwa. Lakini wote waliafikiana kuwa matunda ya juhudi zao hayakuwa ya kuridhisha. Wote walifahamu kuwa matunda ya maafa yaliyokuwa mbele yao siku za usoni, endapo yasingekomeshwa, yangesababisha maafa na vilio ambavyo historia haikupata kuvishuhudia.

"Jambo linalotisha zaidi ni maoni au hisia za wanasayansi wetu," mjumbe mmoja alieleza. "Wanaamini kuwa moto huu unatokea angani katika chombo ambacho hakionekani kwa macho. Hivyo, jukumu letu ni kukilipua chombo hicho. Tutawezaje wakati hatukioni?"

"Labda tuilazimishe Afrika ya Kusini ikiteremshe."

"Hilo ndilo tatizo. Tutawezaje kuilazimisha? Tumejaribu kutazama uwezekano wa kuishambulia kijeshi kwa pamoja na kuona si rahisi. Wao wamejiimarisha sana kiulinzi angani, majini na nchi kavu. Nasi Waafrika umoja wetu unalegalega kiasi kwamba hatuwezi kuafikiana mara moja. Vilevile, wakati tutakapokuwa tukijiandaa kwenda huko madhara waliyotishia yatakuwa yakiendelea kutukia."

"Lakini haiwezekani tukubali kuwa hatuwezi kufanya kitu," Kombora alieleza kwa sauti. "Lazima tufanye jambo. Jema au baya, lazima tulifanye mapema."

Aliungwa mkono.

Mara simu ikaroma katika meza ya Kombora. Akaitazama saa yake na kuona kuwa zilikuwa zimesalia dakika nane kutimia saa kumi za alfajiri. Akainua simu hiyo na kusikiliza. Ilipigwa na msaidizi wake ambaye alimwomba atoke nje mara moja. Kombora akawataka radhi wageni wake na kutoka.

Dakika chache baadaye alirudi ndani akiwa kaandamana na mgeni mmoja ambaye alikuwa katika hali ya kusikitisha. Mgeni huyo alikuwa mtu mweupe, aliyevaa mavazi yaliyochakaa. Mwili wake ulikuwa umejaa majeraha na mikwaruzo mingi kiasi cha kumfanya aonekane mahututi. Hata hivyo, macho yake yalikuwa na uhai.

"Huyu ni mgeni ambaye amekamatwa huko mpakani mwa Malawi na Tanzania leo," Kombora alieleza. "Amesema ametoroka kutoka Afrika ya Kusini kuja baada ya kuponea chupuchupu. Maelezo yake nadhani yatatufaa katika kikao hiki," alimaliza akimwashiria mtu huyo kujieleza.

"Kwanza ningependa ieleweke kuwa mimi sio mzungu, "mtu huyo alisema. "Mimi ni mtu mweusi, mzaliwa wa Soweto," alisema akifungua vifungo vya shati lake. Kila mmoja alitokwa na macho ya mshangao kwa kuona kuanzia tumboni alikuwa na ngozi nyeusi. "Ngozi hii nyeupe iliyokaa usoni na mikononi ni matokeo ya plastic surgery ambayo nilifanya miaka kumi iliyopita ili niweze kuingia miongoni mwa makaburu na kuiba siri zao ili zitusaidie katika vita vyetu vya kujikomboa," alisita kidogo. Kisha akaendelea. "Nimefanya kazi mbalimbali katika jeshi hilo, daima nikiwa macho kupeleleza hiki na kile. Majuzi ndipo nilipogundua jambo la kutisha zaidi. Niligundua kuwa umejengwa mtambo ambao unaendesha Setilaiti ambayo haionekani kwa macho inayotumiwa kuteketeza majumba na sehemu muhimu za kiuchumi katika nchi za kiafrika. Nikaanza upelelezi wa makini kutafuta uwezekano wa kuangamiza tishia hilo. Kwa bahati mbaya, walinishuku katika upelelezi wangu. Sikuwa na la kufanya zaidi ya kuikimbiza roho yangu. Hata hivyo, nimeona mengi, nadhani naweza kutoa mchango madhubuti ambao utatuwezesha kushinda."

Wakuu hao wa upelelezi walimtazama mtu huyo kwa makini kisha wakatazamana. Mmoja alicheka, mwingine akatabasamu.

"Hatimaye…." mmojawao alinong'ona.

SURA YA NANE

KATIKA jumba fulani, mtaa fulani, jijini Johannesburg, makaburu wanne waliketi katika ofisi moja wakisikiliza taarifa za kijasusi kutoka Tanzania. Jasusi moja lilikuwa likiwaarifu kwa kutumia chombo maalumu juu ya msafara wake na mafanikio ya shughuli zake.

"Nimefika salama na kuwakabili nikiwa katika hali ya kusikitisha iliyonifanya niaminike kama mmoja wao. Wameumeza kabisa uongo wangu. Sasa hivi wananiamini sana. Wameniuliza mwaswali mengi na nimewajibu kiume nikiwapa taarifa za uongo. Nadhani wamekusudia kuwatuma wapelelezi wao huko, ingawa hawakupenda kunishirikisha moja kwa moja. Hata hivyo, msijali, nitakuwa macho nikiarifu kila kitendo chao hatua kwa hatua."

Makaburu wakatazamana tena na kutabasamu kwa namna ya kupongezana. Mmoja wao hakuona kama tabasamu linamtosha. Yeye aliangua kicheko. Kisha aliona kicheko hakitoshi. Akainuka na kuliendea kabati lililokuwa nyuma yake ambamo alitoa chupa kubwa ya pombe kali, aina ya JohnWalker na glasi nne. Akazileta mezani na kuziweka mbele ya kila mmoja. Akaifungua na kumimina. “Lazima tusherehekee ushindi.” Baadae akaongeza, “Sitoi ruhusa ya kunywa ofisini isipokuwa inapobidi kufurahi. Mwanadamu hana budi… Cheers…”

Kaburu huyu kwa jina aliitwa Von Iron, kwa sura hakutofautiana sana na mtoto mchanga ingawa kiumbo alikaribiana na kiboko aliyeshiba vizuri. Yeye ndiye aliyekuwa kiongozi wa kamati hii maalumu ya BOSS ambayo iliundwa kuzishughulikia kikamilifu nchi za kiafrika ‘zinazojitia kichwa ngumu.’ Amekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hili la kijasusi tangu lilipoundwa miaka mingi iliyopita. Mara kwa mara kazi yake imekuwa nzuri kwa wakubwa zake. Haikupata kutokea mpango aliouandaa ukashindwa kutoa mafanikio, jambo ambalo lilimpa heshima na hadhi machoni mwa weupe na kumfanya jazanda ya mauti katika fikra za weusi. Ni yeye aliyebuni uwezekano wa kuitumia nguvu ya nyuklia kuwaangamiza Waafrika. Hakuwa Mwanasayansi, lakini alipewa jukumu la kushirikiana nao, akiwa na uhuru wa kutumia kiasi chochote cha pesa hadi majaribio yalipofanyika na kutoa matunda ya kupendeza. Kadhalika, ni yeye aliyebuni mpango wa kuwapa ngozi nyeusi baadhi ya wapelelezi wao, kwa kupoteza pesa nyingi katika hospitali zinazofanya Plastic Surgery. Watu hao waliingizwa kwa hila katika vikundi vya wapigania uhuru na kujifanya wenzao huku wakitoa siri zote na hata kuua inapobidi. Mmoja wa watu hao ni huyu ambaye alikuwa akiwafurahisha sana kwa taarifa zake kutoka Tanzania.

Yeye alifanyiwa mabadiliko ya ngozi yake miaka mitano iliyopita, akawa mweusi na kutibua mambo mengi katika chama cha SWAPO na ANC. Majuzi alirudishwa Ulaya ambako alirudishiwa ngozi ya mtu mweupe usoni na mikononi, kisha akatumwa Tanzania ambako waliona ni chimbuko la misukosuko yote dhidi ya utawala wao, na hasa ili wajue nini kinafanyika katika kutapatapa kwa Serikali na wananchi wa Tanzania juu ya mtambo wao wa aina yake ulioko angani baada ya kutoeleweka kilichomtukia mtu wao, Chonde, hata akafa katika hoteli moja. Zaidi, huyu alikuwa amepewa akiba ya kutosha ya zile gololi zinazouongoza mtambo huo kulipua miradi teule ili wakati utakapowadia waachie pigo hili walilokusudia kulifanya, “Pigo la mwisho.”

Umaarufu wa Von Iron dhidi ya ngozi nyeusi ulichipuka katika roho yake tangu utotoni baada ya kukua katika familia ya kitajiri ambayo iliwatenda waafrika kama wanyama. Hayati baba yake alikuwa na mgodi wa dhahabu. Watumishi wengi walifanya kazi humo huku wakilipwa ujira hafifu mno kiasi cha kuwafanya washindwe kuyamudu maisha. Jambo hilo hakuna aliyeonekana kulijali, hata katika fikra za Von ikajengeka kwamba mtu mweusi ni chombo cha mtu mweupe, ambacho hakina haki wala thamani.

Halafu ikatukia maafa katika mgodi. Baba yake alikuwa katika moja ya ziara zake adimu wakati ilipotokea hitilafu hii ambayo hadi leo chanzo chake hakifahamiki. Hitilafu hiyo ilisababisha maafa makubwa kwa wafanyakazi wengi, weusi kwa weupe. Hayati Iron mwenyewe aliponea chupuchupu. Kama asingejitokeza mtumishi wa Kiafrika, mzee mkongwe, ambaye alitumia nguvu zake zote kumtoa katika chumba kilichokuwa kimefunikwa kwa mawe, siku hiyo angeyapoteza maisha yake. Hata hivyo, jukumu hilo lilimgharimu mzee huyo maisha yake kutokana na majeraha mabaya aliyopata. Kifo hicho kilimsikitisha sana mzee Iron hata akajitolea kuishi na mtoto pekee wa mzee huyo ambaye alikuwa msichana mzuri, ingawa uzuri huo ulipotoshwa na unyonge aliokuwa nao rohoni. Uamuzi wa kuishi na Mwafrika katika nyumba moja, ukiwa jambo geni sana wakati huo, uliisababishia familia yake mgogoro mkubwa, hasa mkewe. Lakini Iron hakulikubali hilo asilani. Badala yake akazidisha mapenzi kwa msichana huyo huku akiahidi kumpeleka masomoni, nje ya nchi.

Halafu ikatokea. Mzee Iron akafumaniwa na msichana huyo. Ilikuwa habari iliyojaa aibu kubwa masikioni mwa kila mtu mweupe. Lakini Iron hakuona aibu. Alikitetea kitendo chake na kukataa matakwa ya mkewe kwamba msichana huyo yatima afukuzwe. Hata mkewe alipotishia kujiua Iron hakukubali kumtupia msichana huyo lawama ambazo hazikumstahili. Ikatokea tena. Wakafumaniwa kwa mara ya tatu. Hapo mama Iron hakustahamili zaidi. Alirudi chumbani ambako alichukua bastola na kumwua msichana yule mweusi.

Mzee Iron alizirai kwa hasira. Fahamu zilipomrudia aliipokonya bastola hiyo kutoka mikononi mwa mkewe na kumpiga risasi mbili kifuani. Kisha alijilenga kichwa na kufyatua risasi zote zilizosalia. Vifo vyao vilikuwa simulizi kubwa mitaani kwa muda mrefu. Vilimwacha Von katika msiba wa uyatima, msiba ambao ulizaa hasira dhidi ya mtu mweusi; akijua kuwa ni mtu mweusi aliyemnyima haki ya kuwa na wazazi. Jambo hilo lilimfanya siku zote awe mstari wa mbele katika kutukuza na kutekeleza taratibu zote za ubaguzi. Daima alikuwa mkatili kuliko wakatili, mnyama kuliko wanyama dhidi ya mtu mweusi. Matokeo yake yakawa kupata vyeo vilivyomwezesha kuwa na mamlaka juu ya uhai na kifo kwa kila mtu mweusi katika shirika hili la kijasusi. Wengi waliuawa kwa ajili yake, mengi yaliendelea kufanyika ili kumkomoa mtu mweusi kutokana na mapendekezo yake. Lakini hakukoma kuendelea kubuni. Mtambo uliokuwa angani ukisubiri kuiharibu Afrika huru ulikuwa moja tu kati ya ubunifu wake.

Pamoja na kutenda mengi ya kikatili, pamoja na kuhakikisha watu weusi wengi wasio na hatia wakipoteza maisha yao, bado Von hakuona kama viumbe hawa walielekea kumpigia mtu mweupe magoti. Badala yake waliendelea kusimama kiume wakitetea haki yao. Alipokufa huyu, alizaliwa huyu, wimbo uleule ukiwa mdomoni. Hata Mandela, ambaye alikuwa kifungoni, alipoteswa bado aliendelea kuwa na msimamo uleule. Hilo, kiasi lilimtisha sana kaburu Von. Hakuwaelewa kabisa watu hawa. Wana nini katika damu yao?

Swali hilo lilikuwa likimletea maswali mengine ambayo yalijenga hisia fulani, maswali yaligongana kichwani mwake. Alikuwa akijiuliza: baba yake aliona nini katika nywele kavu, ngozi nyeusi na sura ya kusikitisha ya yule msichana wa Kiafrika hata akadiriki kumwua mkewe na kujiua mwenyewe! Aliwahi kusikia hadithi ya mtu mwingine ambaye alimwacha mkewe na kukimbia na msichana mweusi hadi Marekani ambako walifunga ndoa. Wana nini watu hawa? Iko siri gani ndani ya ngozi zao zinazotisha? Labda ingebidi alifumbue fumbo hili kwa kumpata mmoja ili aonje? Lakini…mweusi… Hapana. Mara kwa mara aliyafukuzia mbali maswali hayo ambayo yalimjia bila taarifa, hasa alipoukumbuka uyatima wake.

“Cheers,” Von aliropoka tena.

Wenzake wakageuka na kumtazama kwa mshangao. Kisha wakatabasamu kimyakimya, wakiendelea kunywa taratibu. Baada ya vinywaji hivyo, Von aliamua waendelee na kikao chao.

Walivuta mafaili ya suala la Chonde na kuangalia wamefikia wapi juu ya kisa cha kifo chake na mali zake zilielekea wapi. Bado haikueleweka nani alimuua na maiti ya pili chumbani mle ilikuwa ya nani. Zaidi haikufahamika vitu alivyokuwa navyo, ambavyo ni vya hatari na siri kubwa, vilikwenda wapi. Kitu kimoja walikuwa na hakika nacho. Vitu hivyo havikufika mikononi mwa polisi, jambo ambalo liliwafanya waafikiane kuwa watu waliomwua Chonde na kumwibia pesa nyingi na vitu alivyokuwanavyo ni majambazi wa kawaida, ambayo yangevitupa vifaa vile muhimu kama takataka na nyaraka za siri kama uchafu. Kitu ambacho wangejua kukitumia ni pesa za Tanzania na za kigeni ambazo zingewachukua miezi mingi kabla ya kuzimaliza.

Pesa hazikuwa tatizo kwa akina Von. Walilitupa suala hilo kando bila kinyongo, hasa wakijua kuwa tayari mtu wao mwingine, Clay, alikuwa nchini Tanzania akiwa na kila kitu kilichohitajika na tayari kwa yote waliyohitaji kufanya. Alikuwa na nafasi nzuri zaidi ya Chonde kwani uongo aliokwenda nao ungemfanya aonekane kama almasi machoni mwa maafisa wa usalama wa nchi zote za mstari wa mbele za Kiafrika.

“Nadhani iliyobaki ni kuongeza ulinzi katika mtambo wetu,” Von aliendelea. “Ingawa Clay yuko kwao na atatuarifu kila wanachokusudia kufanya, lakini kuna mengine watakayoshindwa kumwambia. Ni wazi kuwa watatumwa wapelelezi waje, lakini sitaki warudi. Nadhani tunaelewana.”

Akaungwa mkono.

Mara simu ya dharura ikaanza kulia. Ikiwa simu ambayo hulia kwa nadra sana, Von aliinua mkono na kuidaka mara moja. “Von hapa,” akanguruma katika chombo cha kusemea.

“Bosi, hapa ni kikosi cha ulinzi wa anga. Ndege zetu za ulinzi zimeizunguka ndege moja ambayo ina watu wanne tu, rubani na msaidizi wake na abiria wawili ambao ni mwanamke na mwanamume. Rubani wa ndege hiyo anaomba kutua, akidai kuwa ametekwa nyara na abiria hao ambao wamejitambulisha kama Joram Kiango na mpenzi wake Nuru. Tunauliza kama tuwaruhusu kutua au tuwalipue”.

“Nani, Joram?” Von aliuliza.

“Ndiyo. Joram Kiango. Yule…”

Mara Von akalikumbuka jina hilo vizuri. Halikuwa jina la kupendeza hata chembe masikioni mwake, ingawa siku mbili tatu zilizopita limesikika kwa namna ya kupendeza kiasi. Joram kuja Afrika Kusini! Baada ya kuharibu mipango yao mingi ya kuikomoa Tanzania! Bila shaka ni kujaribu kujificha baada ya kuiibia nchi yake akiba yote ya pesa za kigeni. Vizuri. Tutampa hifadhi ya kudumu. Anaweza kujificha milele katika makaburi yetu. Hatuna roho mbaya.

“Umesema Joram siyo? Sikia. Huna haja ya kutumia silaha kubwa. Anaweza kufa polepole. Mwambie atue.”

Kwa Afrika Kusini ilikuwa kama nafasi ya dhahabu. Vyombo vyote vya habari vilishangilia kwa nguvu kuwasili kwa Joram na Nuru katika nchi yao. Waliipamba habari hiyo kwa kutia chumvi nyingi juu ya wizi wake. Walieleza jinsi alivyopokonya pesa hizo, alivyozitumia kwa starehe sehemu mbalimbali duniani, alivyofaulu kuwalaghai polisi wote wa dunia, na mwisho alivyoona hana hila zaidi ya kukimbilia Afrika Kusini, ili ajifiche maisha.

“Huu ni mfano hai kwa watu weusi kote ulimwenguni,” mtangazaji mmoja wa televisheni alieleza. “Hakuna asiyemfahamu huyu Joram. Alijifanya mpigania haki, usawa na usalama wa watu wake. Amesababisha vifo vya watu wengi ambao walikuwa na nia njema ya kuikomboa nchi yake. Ndivyo walivyo watu weusi wote. Wanawalaghai wenzi wao na kuwafanya waote mikia misituni eti wakidai haki na uhuru. Matokeo yake ni kuwafanya, hao wenzi wao, vijakazi, wakati wao wakituna matumbo mara tu baada ya kupata madaraka. Natumaini watu weusi wote mnaodanganywa mtaitumia nafasi hii kuuona ukweli wa mambo. Ngozi nyeusi ni dalili ya laana. Nywele fupi ni dalili ya akili ndogo. Bila hekima na uongozi wa mtu mweupe Afrika ingekuwa bado gizani, na endapo ataondoka mtu mweupe giza litarudi…”

Hayo yalisemwa baada ya watu kuwatazama Joram na Nuru wakitoka katika ndege iliyowaleta, huku wakiwa wametanguliwa na rubani ambaye walikuwa wamemshikia bastola. Nje ya ndege Joram aliitupa chini bastola yake na kuweka mikono yake juu. Ndipo Polisi wa makaburu ambao walikuwa wameuzingira uwanja wakiwasubiri, wakajitokeza na kuwakimbilia. Wakawavamia na kuwakagua harakaharaka. Walipoona kuwa hawana silaha nyingine wakawaongoza kuliendea gari lililokuwa likisubiri. Muda wote huo kamera za televisheni na zile za wapiga picha wa magazeti ziliwaelekea Joram na Nuru kwa ukamilifu. Kama kuna chochote kilichowashangaza watazamaji ni jinsi sura za vijana hawa zilivyoonekana tulivu, nzuri, zisizo na dalili zozote za ugangwe kama walivyotegemea.

Msafara wa gari uliishia katika jumba moja kubwa lenye ghorofa kadhaa. Humo, badala ya lifti waliyoingia kuwapandisha juu iliwateremsha chini ambako walijikuta katika chumba kilichoelekea kuwa maalumu kwa kuhoji mateka. Askari waliokuwa nao waliamuru kusubiri, kisha wakatoka na kuufunga mlango nyuma yao. Baada ya muda walileteawa chakula na vinywaji. Wakala na kunywa.

Baada ya muda, kama walivyotegemea, walianza kutembelewa na maafisa wa upelelezi, ambao waliuliza maswali kemkem. Maswali yote waliyajibu kwa ukamilifu kama walivyojiandaa; kwamba walikuwa wameishiwa na hila za kuwaepuka INTERPOL wakaona hawana njia nyingine zaidi ya kukimbilia huku ambako wangehitaji hifadhi.

Baada ya maswali yalifuata mawaidha na badala ya mawaidha ikawa kashfa. “Wewe kama Joram Kiango ambaye nchi yako na Afrika nzima ilikutegemea huoni aibu kufanya ulivyofanya na kuja huku?” aliulizwa

“…Utajisikiaje utakapolazimika kufuata matakwa yote ya ubaguzi na kulazimika kushuhudia Waafrika wanavyonyanyaswa?”

“…Unaweza kukiri hadharani kuwa viongozi wote wa Afrika ni wadanganyifu na hawajui watendalo?”

“…Ukipewa bastola ili umuue mpigania uhuru yeyote atakayematwa, utafanyaje?”

“…Huyu msichana na uzuri wake wote ni malaya? Mbona anakubali kuandamana na mwizi?”

Yalisemwa mengi zaidi ya hayo. Yako ambayo Joram alijibu kwa namna ambavyo alijua walimtegemea kujibu. Mengine hakuyajibu, akijua kuwa walimtegemea kutojibu. Mengine ilimlazimu kuinama kwa haya akiwa na hakika kwamba walitarajia aone aibu. Baadhi ya maswali aliyakwepa kijanja akijua ni mitego iliyokusudiwa kumnasa.

Kutoka hapo walipelekwa katika chumba kilichokuwa na mitambo mingi ambayo eti ingeonyesha kama walikuwa wakisema ukweli au la. Waliwekwa katika mitambo hiyo na kuanza kuulizwa tena maswali. Yote hayo Joram alikwishamfafanulia Nuru kabla hawajaondoka Paris kuja Kinshasa, Zaire, ambako waliiteka nyara ndege ile ya kukodi. Alimweleza kuwa ambacho mtambo kama huo unaweza kuonyesha ni dalili za moyo kudunda na damu kuchemka mara unapoulizwa swali ambalo litakushtua au unapobuni uongo. Hivyo, endapo utazungumza kwa kujiamini haitaonekana dalili yoyote.

Ndivyo ilivyotukia. Saa chache baadaye walichukukuliwa na gari kutoka katika chumba hicho na kupelekwa katikati ya mji ambako waliingizwa katika nyumba moja kubwa na kuelekezwa katika chumba kilichokuwa na vitanda viwili. Humo walikuta mizigo yao yote. Ingawa mizigo yao ilikuwa kama ilivyokuwa, lakini Joram hakusita kugundua kuwa tayari ilikuwa imekaguliwa kwa ukamilifu. Hilo alilithibitisha baada ya kufungua na kukuta kila kitu kimo isipokuwa furushi la pesa zilizokuwa zimesalia. Hilo pia alilitegemea. Hivyo, hakubabaika. Akamwendea Nuru na kumvuta mkono akimwelekeza kitandani ambako alimketisha ili ampumzike kidogo.

“Pole,” alimwambia.

“Kwa?”

“Usumbufu.”

“Mbona bado sijasumbuka. Naamini huu ni mwanzo tu, kuna mengi yanayokuja na nitakuwa tayari kuyakabili yote…”

“Shii,” Joram alimnyamazisha. “Usijisikie huru kiasi hicho,” alinong’ona. “Bado tuko chini ya ulinzi mkali. Yawezekana wanatutazama na kutusikiliza. Kiswahili si lugha ngumu kiasi hicho. Endelea kujihadhari.”

Moyoni Joram alikuwa na sherehe kubwa. Alikuwa akishangilia mafanikio ya msafara huo ambao ulienda kama alivyokusudia kuelekea kuzaa matunda. Kufika Afrika Kusini na kupata mapokezi yenye hadhi kwa kiwango hiki ilikuwa jambo pekee la pili ambalo alilihitaji sana. Jambo la awali ambalo alihakikisha limefanikiwa kabla hajabandua mguu wakekuiacha dunia huru na kujitosa jehanamu kiasi hiki ilikuwa kulisafirisha sanduku lake ambalo lilikuwa na kila kitu alichohitaji katika jukumu lililokuwa mbele yake. Kati ya vitu vilivyokuwemo ni pamoja na pesa za matumizi muhimu, silaha aina aina, madawa ya kila aina, ramani mbalimbali, ngozi na sura za bandia ambazo zingemfanya aonekane mtu mweupe, na zaidi ya yote ni vile vijigololi maalumu ambavyo alivipata kutoka kwa hayati Chonde.

Ilikuwa imemgharimu uongo mkubwa na pesa kuweza kulifikisha sanduku lile katika nchi hii. Alikuwa ametumia hila za kumwendea mfanyabiashara wa Kimarekani ambaye alikuwa akisafirisha mizigo yake moja kwa moja kutoka Ufaransa. Baada ya kujijenga kwake kwa urafiki bandia alimhadaa kuwa amepata oda ya kuuza madawa ya kulevya nchini Afrika Kusini. Mmarekani huyo alikataa kabisa kujihusisha kwa hali yoyote katika biashara ya aina hiyo. Joram alikazimika kumpigia magoti kwa maneno huku akimpa pesa nyingi na kumwahidi sehemu kubwa ya faida. Ndipo sanduku hilo liliposafiri pamoja na mizigo mingine muhimu ya Joram. Na aliarifiwa kuwa sanduku hilo limefika salama. Ilimpendeza sana Joram kuona kati ya watu wengi waliokuja kiwanjani kushuhudia wateka nyara hao wakitelemka kutoka ndani ya ndege, mmoja wao alikuwa Mmarekani huyo aliyeitwa Moore. Ilimpendeza zaidi kuwa Moore hakuweza kufahamu kuwa mteka nyara huyo ndiye yule aliyekuwa rafiki yake siku tatu zilizopita nchini Ufaransa. Joram akiwa amekariri ramani ya nyumba ya Moore kama anavyovifahamu viganja vyake vya mkono, alikuwa akiisubiri kwa kiu kibwa fursa ya kuweka mikononi mwake mizigo yake.

Kabla ya kuoga kama alivyohitaji kufanya, Joram alijitia shughuli na kufanya kama anayepanga vitu chumbani kwake vizuri. Alichokuwa akifanya hasa ni kitu au vitu fulani na haukupita muda kabla ya kukiona alichokuwa akitafuta. Kipande kidogo sana cha kioo kilichokuwa kimejitokeza sakafuni katika pembe moja ya chumba kama kilichosahauriwa na waashi kwa bahati mbaya. Joram alijua kuwa nyuma yake kipande hicho kulikuwa na nyaya ambazo zilisafiri hadi kwenye mtambo ambao ulikuwa na jukumu la kupeperusha kila wanachoongea au hata kuwaona. Baada ya kuona hayo Joram alilidhika, akijua kuwa alikuwa hana haraka ya kuwa msiri. Alihitaji faragha kwa usiku mmoja tu, na katika usiku huo alijua ambacho angefanya kuufanya mtambo huo ushindwe kuwajibika kwa dakika kadhaa.

Wakaoga.

Wakalala.

Jasho jembamba lilikuwa likiwatoka maofisa wanne wa Boss ambao walikuwa katika chumba fulani wakiwashuhudia Joram na Nuru walipokuwa wakifanya mapenzi katika chumba chao. Maofisa hao walikuwa wamekaa katika chumba hicho kwa muda mrefu, dhamira yao kuu ikiwa kupata hakika kama kweli Joram alikuwa hana hila nyingine iliyomleta Afrika Kusini zaidi ya ukimbizi. Taarifa za maofisa wote waliotumwa kuwahoji na ambao walikagua mizigo yao haikuonyesha hila wala ila yoyote. Hata hivyo upinzani uliokuwepo uliishia kuamuliwa kuwa wapewe chumba hiki na kuachiwa uhuru kiasi fulani ili waendelee kuchunguzwa. Chumba hiki kilikuwa maalumu na siri kubwa isipokuwa kwa maofisa wachache wa ngazi za juu. Ndipo jukumu la kuwatazama Joram na Nuru likawaangukia kaburu Von Iron na wenzake.

Ndipo walipolazimika kutokwa na jasho. Kwani walikuwa wakitazama kwa namna moja ilikuwa kama picha ya kupendeza sana, kwa maaana nyingine picha ya kuchukiza, inayotesa na kuadhibu.

Ilikuwa picha ya kupendeza wakati walipokuwa wakiwatazama Joram na mpenzi wake Nuru walipokuwa wakitazamana kwa mapenzi pindi wakati wakijiandaa kulala. Ikaanza kuchukiza walipoanza kuvua mavazi yao na kuketi kama walivyozaliwa huku wakibusiana. Na ilianza kutesa walipojibwaga kitandani na kufanya mapenzi kiroho mbaya bila kujali au kujua kama wanatazamwa, kana kwamba walikuwa wakiwaonyesha watazamani kwa makusudi.

Von Iron aliuzima mtambo huo na kulifuta jasho lililokuwa katika paji lake la uso. Hakujiamini kuwatazama wenzake machoni, akihofu wasije wakasoma kitu alichokuwa akikisoma akilini. “Tukutane kesho…” Von aliamuru akianza kutoka nje. Bila kuinua macho aliweza kuhisi kuwa wenzake walikuwa wakimhurumia zaidi ya walivyokuwa wakijihurumia wao. Alijua vilevile kuwa wenzake hao walijua kama alivyojua yeye kuwa baada ya kuagana nao angerudi katika chumba hicho.

Alirudi.

Akiwa peke yake aliwatazama kwa makini na uhuru zaidi, akisherehekea kila hatua iliyofuata katika mapenzi yaliyokuwa yakiendelea mtindo mmoja juu ya kitanda. Tangu alipokuwa amewaona Nuru na Joram katika televisheni hajua kuwa wangeweza kuwa wazuri kiasi hiki. Kadhalika

hakutegemea kuwa Mwafrika aliyevua nguo angeweza kuwa kiumbe mzuri kama hawa, aliwategemea kuwa viumbe wa kutisha sana kama mizimu. Kumbe sivyo.

Aliendelea kuwatazama. Alijipinda na kujinyoosha kwa maumivu na tamaa kubwa huku mkono wake mmoja akiubembeleza uume wake, mkono wake wa pili ukiwa umelea kichwa kwa wivu wa masikitiko. Starehe au mateso yake yalikoma Joram alipozima taa.

Von alijifariji kwa kuizima mitambo hiyo na kubonyeza ile ambayo ilimfanya akague ulinzi na usalama wa ule mtambo wa nyuklia unaoendesha Satilaiti maalumu iliyoko angani ikisubiri kufanya kazi ambayo haitafutika katika kurasa za historia ya dunia. Aliuona ulinzi ulivyokuwa makini. Askari wanne wenye machine guns walikuwa wakipita kwa zamu kulikagua jengo hilo. Ndani mafunzi wenye silaha walikuwa machio wakikagua mwenendo wa mtambo huo kwa umakini na uangalifu mkubwa. Von aliweza kuona katika screen kubwa iliyokuwa mbele ya wanasayansi hao jinsi setileiti hiyo ilivyokuwa ikielea huku na huko katika bahari ya Hindi kando ya pwani ya Afrika Mashariki. Alitabasamu kidogo alipojikumbusha utaalamu wa hali ya juu uliotumika katika kuunda chombo hicho hata kisiweze kuonekana kwa macho ya kawaida.

Kisha alibonyeza mahali fulani kuondoa mtambo huo machoni kwake. Badala yake alibonyeza mahali ambapo palimwezesha kuona gereza la ardhini ambamo kulikuwa na mateka au wafungwa ambao walitakiwa kuteswa hadi kufa. Humo kulikuwa na kila aina ya mateso. Haikuwepo njia yoyote ya kuweza kutoka isipokuwa kwa funguo maalumu ambazo alidhihifadhi yeye mwenyewe.Von aliwatazama wafungwa au mateka hao waliokuwa wakikaribia kufa. Baadhi yao walikuwa weupe, Mmarekani mmoja ambaye alikuwa mpumbavu kiasi cha kuamua kuwasaidia wapigania haki wa Afrika Kusini, pia walikuwepo Warusi wawili ambao pia tabia zao hazikuwa tofauti na mzungu huyo pamoja na watu weusi watatu. Ni hawa watu weusi ambao walimfanya Von aangue kicheko kwa sauti. Alijiuliza walikuwa wamepatwa na nini weusi hawa hata wakathubutu kujileta wenyewe huku kama wapumbavu. Mtu atajipeleka jehanamu na kutegemea atatoka salama?

Zimesikika habari nyingi za watu ambao waliwahi kufa na baada ya siku kadhaa kufufuka. Watu hao hudai kuwa walipokuwa wafu wamefika peponi na kuwaona malaika. Haijawa kutokea hata mtu mmoja ambaye aliwahi kwenda jehanamu na akarudi duniani. Hawa weusi aliwaona kama watu walipenda sana kufa vifo vya kikatili. Jambo la kusikitisha kwao ni kwamba BOSS iliarifiwa tangu walipoondoka Naijeria na Tanzania na kuja Botswana. Iliarifiwa pia walipoanza mbibu za kuvuka mpaka. Hivyo hila zao za mmoja kujifanya wendawazimu asiyejua analofanya na mwingine kujitia mkimbizi anayeishi kambi ya wapigania uhuru hazikuwa na mafanikio yoyote. Von hakupenda kuwaona ana kwa ana. Aliamua wafungiwe katika chumba cha mauti wasubiri kifo. Hawa walikuwa wawili tu kati ya wanane ambao walikuwa wamekamatwa siku mbili zilizopita. Wawili walikuwa wameuawa kwa mateso wakati wakihojiwa. Mmoja alikuwa amejiua mwenyewe kwa sumu baada ya kumvamia askari aliyekuwa akimhoji na kumjeruhi vibaya kwa kisu kabla hajameza vidonge ambavyo vilimuua mwenyewe.

Wapelelezi hawa walikuwa ni matokeo ya juhudi za kuthibitisha uwezekano wa kuwepo kwa mtambo maalumu unaoziadhibu nchi za Kiafrika. Von alifahamu kuwa bado wangekuja wengi zaidi, weupe kwa weusi, lakini kamwe wasingefika popote pa haja. Na kamwe wasingefika popote kwani zilikuwa zimesalia siku mbili tu kabla ya Afrika huru kuipigia magoti Afrika Kusini na kusubiri vilio na maombolezo yasiyo na mfano. Von alicheka tena, safari hii kwa kujipongeza akijua kuwa sifa ndogo kuwa na wadhifa kama aliokuwa nao sasa. Roho za watu wengi kuwa mikononi mwako zikisubiri tamko lako kabla ya kuteketezwa!

Kisha Von aliufunga mtambo huo na kurudi nyumbani kwake. Akiwa kapera ambaye hakujua lini angeoa alijikuta akikosa usingizi alijikuta akimfikiria Nuru na kumwonea Joram wivu. Bila kufahamu anachokifanya Von alijikuta akiapa kwa jina la Mungu kuwa asingekufa kabla hajamuonja. “Mara moja tu…” alijiambia. “Nione wana nini wanawake weusi…”

Kesho yake aliamuru Joram na Nuru waletwe katika ofisi yake. Akiwa amezungukwa na wasaidizi wake Von alijitahidi kuwatazama Joram na Nuru kwa namna tofauti kabisa na ile iliyokuwa ikipita katika akili yake.

“Sina haja ya kuwahoji chochote”, Von aliwaambia kwa sauti nzito. “Kwa kiasi mlichohojiwa naamini mmeonyesha kuwa mmechoshwa na upuuzi wa hawa viongozi wanaojiita wanamapinduzi katika nchi zenu. Sivyo?”

“Kwa maana hiyo mngependa kuishi huku daima. Msimamo wenu ni wa kishujaa. Nawapenda watu shujaa. Ni hilo ambalo limenisukuma kuwaacha hai pamoja na kuwapa heshima ya kuwaita hapa ili niwape habari njema”.

Joram akiwa amesimama mbele yake, akiwa kamshika Nuru mkono, hakuwa na haja ya kuambiwa huyu ni nani katika nchi hii. Alimfahamu mara moja kuwa alikuwa mkuu wa shirika la kijasusi la utawala huu. Kwa maana nyingine alikuwa adui yake namba moja. Mtu ambaye asingeondoka bila kumpa adhabu ya risasi ya kichwa kwa hatia ya kusababisha maafa kwa Waafrika wengi wasio na hatia. Hata hivyo Joram hakuonyesha dalili yoyote katika macho yake alipouliza kwa upole, “Habari njema ipi? Tumeruhusiwa kupewa uhuru zaidi ya huu tulionao? Tunajiona kama ndio tuko kifungoni”.

“Mko huru kuliko mnavyostahili”, Von alimjibu Joram. “Habari njema niliyotaka kuwapeni ni juu ya uhalibifu ambao utazitokea nchi za Kiafrika kesho saa nne mchana endapo hawatawatuma viongozi wao hapa leo kuweka saini mikataba ya kuwa watiifu kwa utawala huu na kutothubutu kuwasaidia wendawazimu wanaodai uhuru wa Namibia na haki hapa Afrika Kusini. Kama hawatafanya hivyo hadi saa tatu na nusu za mchana. Nyie mtapewa heshima ya kushuhudia moja kwa moja Ikulu zinavyoungua, majengo yanavyoteketea na watu kupoteza maisha. Mtabahatika kushuhudia jambo la kupendeza. Jambo la kihistoria”.

Macho yake yaliwatazama Joram na Nuru kwa umakini. Nao wakifahamu kuwa kuna kitu kilitakiwa kuonekana katika macho yao, Joram aliruhusu tabasamu kidogo huku Nuru akifuta machozi.

“Ni habari njema”, Joram alisema polepole baadaye akauliza. “Habari njema…, tunaweza kuruhusiwa kurudi chumbani kwetu?”.

Binadamu hajapata kuwa na adui mwingine, mkubwa na mkatili katika maisha yake zaidi ya kifo. Ni kifo pekee ambacho kimeishinda akili ya binadamu. Hakukosea yule mwanamuziki aliyeimba “kifo hakina huruma, kifo ni kiboko yao”. Hutokea binadamu akawa na shughuli zote, siku nenda rudi bila kukipa kifo wazo lolote hadi kinapotokea bila kutegemewa. Ni hiyo sababu pekee inalomfanya mwanadamu asitokwe na jasho la hofu siku zote za maisha yake kwa kuogopa kifo. Kwa vile hutokea bila ya kutegemewa.

Hivyo hakuna kifo kibaya kama kifo cha kusubiri siku na saa. Hasa kifo cha kinyama na cha kikatili kama hiki ambacho kilikuwa kikitegemewa na watu kadha wa kadha katika nchi kadha wa kadha za Kiafrika. Leo ilikuwa imewadia siku ile. Siku ambayo Afrika ya Kusini ilikuwa imetoa kuwa ingekuwa ya mwisho kabla ya kuachia pigo la mwisho ambalo lingeiteketeza miji yote ya nchi zilizoko mstari wa mbele.

Pamoja na ukweli kwamba tukio hili lilikuwa limeamriwa kuwa siri kubwa sana miongoni mwa wahusika, kama yale mengine ambayo huishia katika masikio ya wachache na hutoweka bila ya raia wa kawaida kuyapata, lakini hili kwa njia moja ama nyingine lilikuwa limevuja na kusambaa mitaani. Jambo ambalo lilisababisha mashaka na hofu kubwa mitaani. Wananchi waumini wa dini walitoroka makazini na kukimbilia kwenye makanisa na misikiti ili kutubu dhambi zao zote na kumbembeleza Muumba awanasuwe awanasuwe katika janga hili. Wale ambao hawakumwamini Mungu walitulia katika vikundi vikundi wakizungumza kwa utulivu. Wachache sana waliamua kuyamalizia maisha yao huku wakinywa pombe katika baa ambazo hazikufunguliwa milango.

Viongozi wa Chama na Serikali walikuwa katika vikao vya dharura wakijaribu kujadiliana hili na lile. Lolote la haja halikupatikana, japokuwa yalitokea mapendekezo mengi. Jambo ambalo kila mmoja alitamani kutamka ingawa ulimi ulishindwa kutamka hadharani kwa aibu, ni ambalo lingewahakikishia wananchi uhai na usalama wao. Lakini maadamu ungekuwa uhai usio na uhuru, na usalama usio na uhakika na hakuna aliyethubutu kupendekeza hivyo. Iliyonaki ilikuwa kupeana moyo tu kuwa haiweze kutokea, na endapo itatokea cha kufanya ni kujaribu kuepuka majengo ambayo yanaweza kuelekea kuyavuta macho ya muuaji. Ilielezwa pia kuwa kote nchini wananchi walikuwa wakichimba mahandaki kwa ajili ya kujificha.

Ikulu, Rais na baraza lake la mawaziri walikuwa katika kikao cha muda mrefu. Kikao ambacho kilichukua siku nzima, hata usiku ukaanza kukaribia. Inangawa kilikuwa kikao cha siri sana, lakini ilikuwa dhahiri kuwa chochote ambacho kilikuwa kikijadiliwa ndani hakikupata ufumbuzi ya tatizo. Mmoja alikuwa amependekeza kwa mara nyingine kuwa nafasi hiyo itumike kuivamia Afrika Kusini kijeshi, “Ili tukomeshe kabisa suala hili la kutishiwa na kuonewa mara kwa mara. Tutumie majeshi yetu yote ya nchi za mstari wa mbele kuingia nchini humo na kuanzisha mapambano ili kuunda utawala halali. Najua, adui ana jeshi imara na silaha kali sana. Lakini wingi witu wetu utasaidia tutashinda…”

Mapendekezo hayo yalijadiliwa lakini hayakuonekana kama yangekuwa jibu la kuziokoa nchi za Afrika na kumaliza tatizo ambalo lilikuwa mbele likisubiri saa chache ili litokee. mwingine akatoa wazo. “Si rahisi kutumia masaa manane yaliyobaki kukusanya majeshi na kuyaongoza katika nchi nyingine na kuanzisha vita. Zaidi yote, hatari au mkasa ambao uliokuwa ukisubiriwa ulikuwa ukitokea angani, hivyo uvamizi huo usingesaidia au kuzuia maafa hayo…”. Baraza la mawaziri liliendelea kujadiliana kwa utulivu katika ukumbi huo wa Ikulu. Jengo hilo likiwa miongoni katika majengo kadhaa yaliyokuwa katika orodha ya kulipuliwa ilikuwa kana kwamba Rais na mawaziri wake walikuwa wameamua kikisubiri kifo hicho kwa pamoja; kufa kiofisa…

Binadamu aliyekuwa na hali mbaya kuliko wote nyumbani nchini Tanzania aliitwa Inspekta Mkwaju Kombora. Yeye alikuwa akitaabika kimwili na kiakili. Juhudi zake zote, pamoja na wenzake wa kutoka nchi mbalimbali, zilikuwa kama upuuzi. Upelelezi ulikuwa haukuzaa matunda yoyote yale. Na hasa upelelezi huo ulikuwa kama umewafanya wazidi kujipalia mkaa wa moto; kwani ilikuwa dhahiri kuwa kila jambo linaloafikiwa hapa wakati huo huo utawala wa makaburu unakuwa na taarifa nalo. Hayo yalithibitika alipoarifiwa kuwa wapelelezi wote waliotumwa kuingia Afrika Kusini walikuwa mikononi mwa makaburu. Ilikuwa kama waliopelekwa kufa makusudi kabisa. Jambo ambalo lilimfanya ashuku mara moja kwamba miongoni mwao alikuwemo chui aliyejivika ngozi ya kondoo.

Hivyo Insipekta Kombora aliugeuza upelelezi wake kutoka mstari wa mbele na kuanza kuchunguza mstari wa nyuma. Na haukupita muda kabla dalili hazijajitokeza kuwa huyu mgeni aliyedhaniwa kuwa msamaria mwema, ambaye alileta fununu nyingi kutoka Afrika Kusini angehitaji kuchunguzwa zaidi. Uchunguzi ukaanza katika vikosi vyote vya wapigania uhuru duniani, katika vyuo na hospitali ambazo alidai amepitia na hata Afrika Kusini. Taarifa zilizidi kuongeza haja ya kutazamwa kwa makini. Na haukupita muda kabla kabla ya watu waliokabidhiwa jukumu la

kumwangalia hawajatoa taarifa kuwa alikuwa mtu wa BOSS. Habari hiyo ilimuumiza sana Kombora. Alitoa amri kuwa mtu huyo aliyejiita Clay achunguzwe kwa makini sana, kwani kwa vyovyote leo ilikuwa siku ya mwisho iliyotolewa na utawala huo haramu na lazima angekuwa na jambo la kuarifu kwa mabwana zake.

Baada ya hayo Insipekta Kombora aliendelea na shughuli katika ofisi yake. Alipokea na kujibu simu na walkie talkie nyingi ambazo hakuona kama zilikuwa zikimsaidia chochote. Aliwasiliana na maofisa wenzake katika nchi za Zambia, Zimbabwe, Angola, Msumbiji, Naijeria na kwingineko kujaribu kuona wamefikia wapi. Hakuna alichopata zaidi zaidi ya yale aliyotegemea. Kwamba wananchi walikuwa wakitaabika na kulalamika mitaani katika hali ya hofu kubwa. Kwamba hata makazini hawakuwa wamekwenda.

4

Ofisi ilikuwa haikaliki. Kila Kombora alipojaribu kutulia juu ya kiti, kiti hakikuelekea kuafikiana naye. Kila alipoinuka ili atoke, hakujua angeelekea wapi. Unawezaje kutulia na huku unahesabu saa kusubiri kifo au maafa ya kusikitisha ambayo ni aibu kwako, kwa taifa lako na bara lako zima? Aliendelea kutaabika kimwili na kimawazo, akipokea na kusikiliza habari kutoka sehemu mbalimbali. Mara zilimfikia habari za Joram na Nuru kuwa walikuwa wameingia Afrika Kusini na kuomba hifadhi ya kisiasa. Kwa kombora zilikuwa habari za kushangaza sana. Habari za kusikitisha. Habari zinazotia aibu. Joram Afrika kusini! Hata hivyo, alikwishachoka kushangazwa na habari za kijana huyu anayeitwa Joram. Mambo yote aliyokuwa akiyafanya, ambayo yaliwafikia watu wa habari, Kombora aliyasikia au kuyaona katika vyombo vya habari. Angeweza kumsifu Joram kwa mbwembwe zake ambazo ziliwafanya polisi wote wa miji mbalimbali na nchi zilizoendelea washindwe kumtia mikononi. Lakini kila alipokumbuka kuwa mbio hizo za Joram zilikuwa za kukimbiza akiba pekee za pesa ya kigeni alizoibia nchi yake alijisikia vibaya. Hayo yakifuatwa na tishio lililokuwa likizidi kusogea, vilimfanya ajilazimishe kuliondoa jina hilo akilini mwake.

"… Inspekta Kombora anaongea. Namba ngapi hiyo?…" alijibu sauti katika walkie talkie iliyokuwa mkononi mwake. Alipotajiwa namba alijikuta akisikiliza kwa makini zaidi. Ilitoka kwa kiongozi wa makachero ambao walikuwa wakifuatilia nyendo za Clay.

"… Inaelekea kama tutamkamata red handed, mzee. Sasa hivi anaunganisha mitambo yake ya mawasiliano…"

"Nisubiri. Nakuja mara moja."

Dakika mbili tatu baadaye, Kombora alikuwa miongoni mwa polisi wanne waliokuwa katika chumba fulani katika hoteli ya Kilimanjaro. Chumba hiki kilikuwa cha nne kutoka chumba cha Clay. Hata hivyo, kutokana na mitambo waliyoitega kitaalamu, japo hawakuwa wakimwona, waliweza kumsikia anavyoongea katika chombo fulani cha kijasusi.

"Sikiliza mzee… sikia…" askari mmoja alimwambia Kombora huku akitweta.

"…Ndiyo. Ndiyo… nimefanikiwa kupanda katika majumba ya kutosha. Moja Ikulu.. hapa Kilimanjaro moja… jengo la IPS moja… Kitegauchumi… Muhimbili… Benki Kuu ya muda… Tipper… kiwanda cha Urafiki na sehemu mbalimbali muhimu. Tunachosubiri ni saa moja tu. Ikifika, kwa jinsi nilivyotega inaelekea jiji zima litalipuka. Mimi nitaondoka hapa wakati wowote…"

"Unasikia mzee?… Unasikia?…"

Kombora hakusubiri kumsikiliza afisa huyo. Aliwaamuru kumfuata kukiendea chumba cha Clay. Kinyume cha mategemeo yao waliukuta mlango ukiwa wazi. Naye alikuwa kaketi kwa utulivu juu ya kochi, gazeti mkononi. Yeyote ambaye angeingia bila ya kufahamu kinachotokea angemdhania kuwa alikuwa akisoma gazeti.

Aliwalaki Kombora na wenzake kwa utulivu wa kushangaza. "Karibuni. Vipi, mbona ghafla hivyo? Kuna habari mpya?" aliuliza.

“Inuka na uweke mikono yako juu,” Kombora alifoka, tayari akiwa na bastola yake mkononi akiifanya idadi ya bastola zilizomwelekea kuwa nne.

“Vipi Inspekta! Mbona sielewi?…”

“Mikono yako juu!” Kombora alinguruma.

Clay akainuka na kuiweka mikono yake angani.

“Acha gazeti.”

Aliliachia. Ndipo kilipoonekana kikasha kidogo chenye ukubwa wa kiberiti ambacho alikuwa nacho mkononi. Kombora alimsogelea na kuiweka bastola kifuani mwake huku akimwuliza kwa ukali, “Nini hicho?”

“Kwa nini Inspekta?… Hiki sikifahamu. Nimekiokota sasa hivi tu.”

Jibu hilo lilimchukiza Kombora kupita kiasi. Alijibu kwa pigo zito la ngumi ambalo lilitua barabara katika uso wake. Clay alipepesuka lakini hakuanguka, jambo ambalo lilimshangaza na kuzidi kumchukiza Kombora. Pamoja na umri wake mkubwa hakumbuki lini alipata kumpiga mtu ngumi nzuri kama hiyo na mtu huyo akaendelea kusimama. Akarudi nyuma hatua mbili na kumwamuru askari mmoja amkague. Ni hapo lilipotukia jambo ambalo halikutegemewa. Kwa wepesi usio kadirika Clay alichomoa kisu na kumchoma askari huyo. Kisu cha pili kilimkwaruza Kombora mkononi. Papo hapo alichupa mlangoni akienda zake. Lakini hakuwa mwepesi zaidi ya risasi tatu za polisi ambazo zilimfanya aanguke mlangoni kifudifudi. Wakamvuta chumbani na kumlaza kitandani bila kujali damu zilizoendelea kumtiririka kutokana na majeraha makubwa ya risasi hizo. Wakamkagua na kumpokonya bastola nyingi na visu sita zaidi.

“Sema haraka, ulikuwa ukiwaarifu nini mabwana zako?” Kombora alimwuliza.

“Itakusaidia nini Inspekta?” alihoji kwa udhaifu na maumivu makali. “Huna unaloweza kufanya. Bado saa chache sana. Kama utapenda kufahamu nilikuwa nikiwaarifu mafanikio ya kazi yangu. Nimefaulu kutega katika majengo mbalimbali. Wakati utakapowadia mlipuko utakaotokea utakuwa wa kupendeza sana. Laiti ningekuwa hai nione na kusikia vilio vyenu!”

Kombora hakujua aseme nini. Hakujua kama ilimpasa kumtisha au kumbembeleza mtu huyu ambaye kila dalili ilionyesha kuwa angekufa haraka. “Mpelekeni hospitali,” aliamuru.

“Ya nini Inspekta? Sipendi kufa kwa moto… naweza kufa kwa njia nzuri zaid…”

Kombora hakumsikiliza. Akamgeukia askari wake aliyekuwa mahututi. Yeye pia hakuwa na dalili ya kuishi sana. Kisu kilimwingia kifuani upande wa moyo. Jambo hilo lilipandisha hasira za Kombora dhidi ya Clay. Akamgeukia na kumtazama usoni.

Alimwona akitafuna kitu. Akakumbuka majasusi mengi ya utawala huo yalivyokuwa yakiishi na sumu kali mdomoni. Matumaini ya kupata habari zozote za haja yalikuwa mbali. Akamgeukia na kumwuliza taratibu, “Sema tafadhali… tunawezaje kuzuia mkasa huu ulioko mbele yetu?”

Clay alicheka kwa maumivu huku akijikongoja kusema, “Labda uchukue furushi moja katika mfuko wangu ukaangalie unachoweza kufanya.”

Moyoni alifahamu kuwa mfuko huo ulikuwa na akiba nyingine ya vile vigololi, ambavyo alikuwa hajamaliza kuvitega. Hivyo, aliamini kuwa Kombora angevifikisha Central Police na kulifanya jengo lao liwe moja ya majengo mengi yatakayopigwa na radi hii iliyoundwa na binadamu. Hilo likamfanya ajitahidi kucheka, tena kifedhuli huku akisema kwa tabu, “Usijali Inspekta… muda si mrefu tutakutana huko kuzimu… Tutakuwa wengi sana… mimi natangulia…”

Kombora hakuona kama mtu mwenye roho ya kinyama kama huyo alistahili kufa kiungwana kiasi hicho. Hivyo, akaichomoa bastola yake na kumsindikiza akhera kwa risasi ya kichwa ambayo ilimfumua kabisa fuvu lake.

Walitazamana kwa macho yaliyojaa hisia. Mmoja akitabasamu, mwingine akiinama kwa haya. Mmoja akainua mkono wake na kuutua juu ya paja la mwenziwe. Mwingine akaufunika mkono huo kwa kiganja chake na kuanza kuutomasatomasa kimahaba. Mkono wa pili ukainuliwa na kutua juu ya kifua cha mwenziwe, ukitafuta uwezekano wa kupenya, ndani ya mavazi yake. Vijilima viwili, laini, vilivyosimama kwa namna ya kupendeza macho katika kifua hicho havikuruhusu mkono huo kupenya kwa urahisi. Mkono ukaviacha vilima hivyo na kuanza kufungua vifungo vya vazi hilo. Mara kimojawapo cha vilima hivyo kikajitokeza, kikimeremeta kwa wekundu na uhai wake. Wakatazamana tena. Kisha akakisogeza kinywa chake na kukifanya kimeze chuchu za kijilima hicho. Mdomo ulipohama kifuani ulikwenda katika kinywa cha mwingine ambako ulianza kunyonya ulimi uliokuwa ukisubiri. Mara wakaachana na kuanza kuvua mavazi yao moja baada ya jingine. Tahamaki wakawa wamesimama kama walivyozaliwa, kila mmoja akishangazwa au kuridhishwa na uzuri wa mwingine. Kisha wakakumbatiana kwa nguvu. Mmoja aliguna, mwingine akanong'ona.

"Nuru…"

"Joram…"

Kitanda kikawalaki na kuwafariji. Hawakuhitaji shuka. Walikuwa kama walivyohitaji kuwa, wakifanya mapenzi kwa namna ambayo walihitaji, kwa kiwango ambacho hakikadiriki. Vitendo vyao vilifuatiwa na maneno ya mapenzi ambayo yalisikika kwa sauti ya kike, mara chache sana yakijibiwa kwa sauti nzito ya kiume.

Kisha ghafla, vitendo na sauti zao vilitoweka machoni na masikioni mwa mtu ambaye alikuwa akishuhudia kila kitendo chao, "Shit," mtu huyo, kwa jina Von Iron, alifoka. Alikuwa akikifuatilia kila kitendo kwa tamaa kubwa, huku akiburudika. Lakini haikuwa burudani rahisi kwani kuona huko kulimfanya atetemeke mwili mzima na roho kwa uchu na tamaa, huku jasho likimtoka na damu kuchemka. Alijaribu kujifariji kwa kuubembeleza uume wake kwa mkono wake huku macho yake yakiwa yamekazwa kutazama katika mtambo wake. Mkono haukuwa na faraja yoyote. Mara mbili aliutoa na kuufuta kwa leso yake kwa jinsi ulivyochafuka kwa manii yaliyomtoka kwa wingi. Alitamani aondoke hapo na kuacha kutazama vitendo hivyo, lakini macho hayakumruhusu. Akaendelea kutazama, akiendelea kujifariji kwa mkono wake. Moyo wake ulikuwa unadunda na alishindwa kustahimili zaidi ya mkono kujifariji. Alihitaji mwananmke. Na si mwanamke yeyote isipokuwa yule mwanamke aliyekuwa akimtesa sana, mwanamke wa Kiafrika; Nuru.

Mwanamke mweusi! Von alishangaa kimoyomoyo. Ana wazimu? Hata hivyo, alijua kimoyomoyo kuwa asingestahimili hadi atakapompata. Alijifariji kwa kujiambia kuwa angemwua baaada ya kutenda naye mara moja tu, ili yasije yakampata yaliyompata hayati baba yake.

Ni tamaa hiyo ambayo ilimfanya akatae katakata madai ya wenzake waliomtaka amruhusu Joram na msichana wake wauawe mara moja.

"Ni jambo la hatari lisilo na busara kumwacha hai mtu hatari kama huyo hasa katika kipindi hiki," mwenzake mmoja alimwambia. "Japo amekimbia kwa na hawezi kurudi, lakini ni mtu ambaye hafai kuaminika. Kumwacha hai ni sawa na kuishi na nyoka chumba kimoja."

"Atafanya nini?" Von alikuwa amekanusha. "Hana awezalo kufanya. Bado saa chache sana tutamleta katika televisheni atazame nchi yake inavyoteketea. Baada ya hayo tutamchinja kwa urahisi kama kondoo. Usijali. Waache waishi usiku mmoja zaidi."

Usiku ni kitu alichokuwa akikisubiri kwa hamu, akikumbuka yale aliyoyaona usiku wa jana. Na ulipowasili hakuwaalika wenzake kwenda kutazama. Kwa kisingizio cha "Kumchunguza kwa makini."

Alikwenda peke yake. Akaburudika kwa faraja inayotesa. Hivyo, vitendo hivyo vilipotoweka machoni mwake, lilikuwa kama pigo kwake. Aliamini kuwa kulikuwa na hitilafu ya mitambo iliyowaunganisha na chumba hicho. Lakini kwa kuwa mitambo hiyo ilikuwa automatic, na ilitegeshwa kwa namna ya kuweza kujirekebisha yenyewe, alisubiri kwa utulivu.

Katika kipindi hicho cha kusubiri ndipo ilipomjia wazo la kuyafikiria mambo ambayo yangetokea mara tu baada ya usiku huu. Kesho, wakati kama huu bila shaka nchi kadhaa za Kiafrika zitakuwa katika maombolezo makubwa huku majeneza yakiwa yamejaa maiti zilizoungua na hospitali zikishindwa kuhimili idadi ya majeruhi watakaoponea chupuchupu. Mpango huo uliotokana na ubunifu wake ulipita kwa tabu sana baada ya wakubwa kulalamika kwamba ulikuwa wa kikatili mno lakini yeye Von na wenzake wachache walifaulu kuwashawishi na wakaafiki baada ya kuwakumbusha tena na tena kuwa ANC ilikuwa haifanyi mchezo bali ilikusudia kupokonya utawala, jambo ambalo lingewatia watu weupe wote

mashakani, chama hicho kinapewa onyo kali, onyo ambalo kamwe lisingeweza kusahauliwa. Dawa ya moto ni moto… na sasa wakati huo wa kutumia dawa hiyo, iliyokuwa ikichemshwa kwa muda mrefu na gharama kubwa ulikuwa unawadia. Lipi lingeweza kumpendeza Von zaidi ya hilo? Nani angeweza kufurahi zaidi yake?

Mara akajisikia kucheka kwa furaha. Alijisikia kusheherekea kila chozi litakalotoka katika uso mweusi kwani machozi hayo kwake yangekuwa faraja ambayo isingemsahaulisha ukatili wa mtu mweusi ambaye alimfanya awe yatima. Maelfu ya weusi yatateketea kwaajili ya malaya mmoja mweusi, aliwaza. Watakilipia kifo cha mama yake mpendwa, pamoja nao Joram Kiango na msichana wake… aliendelea kuwaza. Lakini kabla ya kifo chao lazima ampate huyu msichana anayeitwa Nuru. Aliyoyaona kwa macho yake yalikuwa hayastahimiliki. Alihitaji kuyaona kwa vitendo. Alihitaji kuijua siri iliyomo katika ngozi hii nyeusi, siri ambayo ilimfanya amkose mama na baba milele, baada ya hapo ndipo Nuru angemfata Joram akhera.

Mawazo hayo yalimpandisha mori hata akakumbuka kuyarejesha macho yake katika screen iliyokuwa ikimwonyesha chumba cha Nuru na Joram. Hakuona chochote. Mitambo bado ilikuwa haifanyi kazi. Akaitazama saa yake. Ilikuwa ikikaribia saa kumi za alfajiri. Saa mbili zilikuwa zimepita tangu mitambo hii ilipokorofisha. Von hakuamini. Isingewezekana kuwa mitambo hiyo iwe haifanyi kazi kwa muda wote huo ilikuwa imepangwa kuwa ingeweza kujiwasha yenyewe dakika tano tu baada ya kila hitilafu. Vipi leo ikatae? Na hasa akiwemo Joram Kiango ambaye, pamoja na matatizo yote aliyokuwa nayo, iliamriwa asiachwe huru zaidi ya dakika tano?

Hima Von aliinua simu na kuzungusha namba za mmoja wa makachero waliopewa jukumu la kulala macho katika jumba hilo alimokuwemo Joram. “Sikia,” Von alimwambia kwa sauti ya amri. “Tumia kisingizio chochote uingie katika chumba chake humo ndani fanya kila hila uone kwanini mashine hii imegoma kufanya kazi.”

Akiwa anaijua vizuri kazi yake, mtu huyo alivaa ovaroli lake jeupe na kuchukua vifaa vya umeme hadi chumbani kwa Joram. Aligonga mlango kama kawaida. Kisha akagundua kuwa ulikuwa wazi. Akaufungua polepole na kuingia. Macho yake yalidakwa na umbo la Nuru akiwa kavaa vazi la kulalia, jepesi kiasi cha kufichua umbo lake zuri la ndani kwa kiwango cha kutosha. Kando ya Nuru alisimama kijana wa Kizungu aliyevaa nguo zake zote, suti, kama ambaye alikuwa hajalala kabisa. Fundi huyo bandia alidhani kuwa kabla ya kubisha hodi mara ya kwanza aliwasikia wakicheka. Lakini hayo yalimtoka akilini mara alipomwona msichana huyo akiangua kilio huku akisema kwa kwikwi.

“Afadhali umefika fundi, nadhani utanisaidia.”

“Kuna nini?” kachero huyo aliuliza.

“Huyu hapa,” Nuru alisema akiuelekeza mkono kwa mzungu aliyesimama kando kwa utulivu. “Huyo ameingia humu chumbani kwa nguvu na kutaka kuninajisi. Mtoe nje, tafadhali.”

“Yuko wapi bwana wako?”

“Yuko bafuni.”

“Anafanya nini muda wote huo?” fundi bandia aliuliza huku akizidi kumkodolea Nuru kwa macho yenye tamaa. Mara macho yake yaliuona mfuko uliokuwa wazi kando ya kabati. Akaona vitu vilivyokuwemo. Aligutuka kidogo na kurudi nyuma huku akiupeleka mkono wake mgongoni kuchukua bastola yake. Alikuwa amechelewa sana. Wakati huohuo kisu kilipenya katika kifua chake. Pigo la pili lilimfanya ateremke sakafuni bila ya ubishi. “Mzungu” aliyekitumia kisu hicho alikitupa uvunguni na kuifuta mikono yake kwa shuka.

“Fanya haraka Nuru,” alihimiza akiirudia maiti na kuilaza vizuri kando ya kitanda.

Dakiaka chache baadaye mlinzi aliyekuwa akililinda jengo hilo kwa mlango wa nyuma aliwaona vijana wawili wazungu, mvulana na msichana wakimjia. Mikononi walikuwa na mizigo yao ambayo haikuwa chochote zaidi ya mifuko midogomidogo.

“Tunawahi uwanja wa ndege,” kijana wa kiume alieleza.

Ingawa walizungumza kiingereza kamili lakini mlinzi huyo alishuku jambo katika sauti hiyo hasa akiwa analifahamu jengo hilo lilivyo, hakuamini kuwa walikuwa wasafiri wa kawaida.

“Naweza kuona vitambulisho vyenu?”

“Bila shaka,” mwanaume alijibu akiutia mkono wake mfukoni. Ulitoka na kisu ambacho kilididimia katika kifua cha mlinzi huyo. Maumivu makali yaliyochanganyika na mshangao vilimfanya afyatue bunduki yake bila shabaha yoyote. Mara akaanguka chini na kukata roho.

Mlio wa bunduki alfajiri tulivu kama hiyo, uliwashitua watu wengi. Zaidi yao wote alikuwa Von Iron, aliyekuwa bado kaketi katika chumba kilekile, akisubiri matokeo ya mtu aliyetumwa chumbani kwa Joram. Alisubiri kwa muda ambao aliuona mrefu kupindukia. Alipojaribu kuwasiliana naye kwa walkie talkie ndogo iliyokuwa imevaliwa kama saa ya mkono hakupata majibu yoyote. Akaendelea kusubiri. Na katika subira hiyo ndipo aliposikia mlio wa bunduki ambao hakuutegemea. Akafanya hima kumtuma kachero mwingine katika chumba hicho. Mara moja akapata majibu ambayo yalimfanya atokwe na jasho jembamba.

Dakika chache baadaye alikuwa miongoni mwa maafisa sita wa ngazi za juu katika BOSS waliosimama chumbani humo mbele ya maiti ya mwenzao, ambayo yalilala sakafuni juu ya dimbwi la damu nzito. Joram hakuwemo, wala msichana wake. Vitu vyao vichache vilikuwa vipo, ingawa baada ya kupekuliwa havikuonekana na chochote cha haja zaidi ya mavazi na vitabu. Katika vitabu hivyo kilipatikana kitabu kimoja cha Physics ambacho kilionekana kuwa kilisomwa sana kwa jinsi kilivyokuwa kimepigiwa mistari chini ya maneno fulanifulani. Baada ya uchunguzi mdogo ilidhiirika kuwa msomaji alizingatia mambo ya setilaiti na nyuklia. Hilo liliwafanya waunge mbili na mbili na kupata nne.

“Ana wazimu,” Von alifoka. “Kama amekuja hapa akiwa na ndoto ya kufahamu chochote juu ya setilaiti yetu hii maalumu wazimu unamsumbua. Amekuja kuinadi roho yake.” Akawageukia wenzake na kuwatazama kwa lile jicho lake kali la kutisha, jicho ambalo lilikuwa msingi uliowafanya waendelee kumwogopa na kutomkosoa. “Mnasikia? Mtafuteni haraka, aletwe hai, atakufa taratibu kama mbwa wenzake.”

Kabla hawajatawanyika kutoka chumbani humo, ziliwafikia habari nyingine mbaya zaidi. Maiti ya mmoja wa walinzi wa jengo hilo imeokotwa ikiwa na kisu kifuani. “Aliuawa kwa aina ya kisu ambacho kimemwua huyu.” Kachero huyo alieleza.

“Mnaona?” Von alinguruma. “Sasa namtaka akiwa hai au maiti. Haraka iwezekananvyo, tafadhali…”

Kulitangazwa msako mkali katika jiji la johanesburg mitaa yote ilifurika makachero ambao walichunguza kila uchochoro. Ilikuwa siku ngumu mno kwa watumishi weusi ambao walilazimika kuwahi kazini asubuhi hiyo. Wengi wao waliambulia kuishia katika vituo vya polisi ambako waliteswa na kusumbuliwa kwa kosa ambalo hawakulifahamu. Mtu au watu waliokuwa wakitafutwa hawakupatikana. Badala yake hadi mapambazuko kulikuwa na taarifa ya vifo vya watu wanane zaidi, watano wakiwa wameuwa kwa kisu, watatu kwa risasi za bastola. Wengi kati ya marehemu hao walikuwa watu wakubwa katika ofisi zao au walinzi wa majumba fulanifulani yenye umuhimu mkubwa. Ilikuwa dhahiri kuwa hiyo ilikuwa kazi ya Joram Kiango.

Von alizidi kupandwa na hasira. Hakuelewa kabisa dhamira na manufaa ya mauaji hayo. “Wazimu unamsumbua,” aliwaza. Kisha alihisi kuwa ameelewa. Joram alikuwa akilipiza kisasi dhidi ya maafa yatakayoipata nchi za afrika saa chache baadaye bila shaka alikuwa akijifariji kwa kumwaga damu zisizo na hatia. “Anajisumbua,” Von alisema. “Atalazimishwa kutazama katika televisheni, moto utakavyoiteketeza Dar es Salaam. baada ya hapo ndipo atakapokufa kifo cha kusikitisha…

Von akaamuru ufanyike msako mkubwa zaidi. Polisi wote na jeshi la ulinzi wakaingizwa katika msako huo. Kila mmoja aliambiwa anamtafuta nani na afanye nini baada ya kumpata. “Akileta ubishi muue, vinginevyo mlete hai.”

Ingawa Von alitegemea habari hiyo iwe siri, lakini hakufahamu iliyafikia vipi masikio ya watu wa habari. Ilimshangaza televisheni ilipokatiza matangazo yake ya kawaida na kueleza kutoweka kwa Joram Kiango na mauaji aliyokuwa akiyafanya. Ikatolewa picha ya Joram na msichana wake walipokuwa wakishuka kutoka ndege iliyowaleta nchini humu ikiwa imetekwa nyara. Pia zilionyeshwa baadhi ya maiti alizoziua.

“…jihadhari nae, ukimwona muue kwanza, muulize maswali badaye…”

Mtangazaji wa kipindi hicho alieleza.

Tangazo hilo liliamsha hofu ambayo haikupata kuonekana katika jiji hilo. Watu walizidi kubababika wakiogopa hata kuifungua milango yao ilipogongwa na yeyote. Wako ambao kazini hawakutaka kwenda.

Dakika chache baadaye ilibidi Von ajitokeze katika televisheni na kuwataka wananchi wasiwe na hofu yoyote, kwamba kutoroka kwa Joram lilikuwa tatizo dogo sana ambalo lingerekebishwa kwa muda mfupi. Akawafahamisha kuwa badala ya hofu leo ingekuwa siku yao ya kufanya sherehe kwani Afrika na dunia nzima itaziona nguvu za Afrika Kusini. “Wote ambao wamekuwa wakionea kijicho na kuitesa nchi yetu leo watatupigia magoti,” aliendelea. “Tulieni, msiwe na wasiwasi wowote. Ikifika saa nne fungueni redio na taelevisheni zenu muone…”

Watu hao ambao walikuwa wakitafutwa kwa udi na uvumba, alfajiri iliwakuta wakiwa wamesimama mbele ya hoteli moja ndogo katika mtaa uliojaa watu waliokuwa wakijadiliana. Macho yao yaliwatazama raia hao wa makaburu waliojaa wasiwasi kwa dhihaka. Kadhalika, waliwakebehi askari na poli ambao walikuwa wakipita huku na huko katika mtaa na vichochoro huku wakiwapita bila ya kuwatupia macho. Isingekuwa rahisi kwa mtu yeyote kuwashuku kwa urahisi. Pamoja na kukesha, pamoja na kuchoka kwa kazi ya kwenda hapa na pale huku wakilazimika kuua na kuua tena, bado walijitahidi kuwa katika hali ya kawaida kama raia yeyote wa kawaida katia nchi hiyo. Hali ambao ilitokana na mavazi waliyovaa pamoja na rangi yao.

Yeyote aliyewaona aliamini kuwa alikuwa akiwaona vijana wengine wa kikaburu. Hayo yalikuwa matokeo ya moja ya shughuli nyingi ambazo Joram alifanya kwa gharama kubwa sana aliposafiri hapa na pale katika miji mbalimbali. Alimpata mtaalamu ambaye aliwatengenezea ngozi za bandia zilizovaliwa usoni, mikononi na kufunika vichwa vyao kwa nywele za kizungu. Vitu hivyo ni miongoni mwa mali zake ambazo alizisafirisha kwa hila kwa kumtumia yule Mmarekani Moole.

Kwa ujumla Joram aliona kuwa mambo yote yalikuwa yakienda kama yalivyopangwa, ingawa kiasi yalianza ghafla kuliko alivyotegemea. Alishtuka sana jana alipoambiwa na yule kiongozi wa BOSS kwamba leo saa nne wangeilipua Dar es Salaam na miji mbalimbali ya nchi za Kiafrika kwa ile silaha yao iliyoko angani. Hivyo, hakuwa na simile tena moyoni. Ndipo alipolazimika kufanya mapenzi ya hali ya juu na Nuru akiwa na hakika kuwa anatazamwa na ule mtambo wao ambao alikwisha uona. Alifanya hivyo ili kuwapumbaza watazamaji hao. Baada ya hapo ndipo alipofanya hila kukorofisha mtambo huo. Katika kipindi hicho cha kutoonekana aliondoka na kupenyapenya kwa hila katika viochochoro hadi nyumbani kwa Moole ambako alibisha mlango na kufunguliwa na Moole mwenyewe. Alipoomba mzigo wake Moole alikanusha kabisa kwamba hakuwa amechukua mzigo wa mtu kama huyo. Lakini ngumi mbili tatu zilimfanya amwongoze ghalani ambako Joram alimvamia na kumfunga mikono na miguu, kisha akaufungua na kuchukua vile vitu muhimu tu. Akarudi haraka hadi chumbani kwake ambako, akisaidiwa na Nuru alipekuapekua na kupata ramani walizoziandaa, pesa na vitu vingine. Ni wakati Joram alipomaliza kujivisha ngozi hizo zilizomfanya aonekane kama alivyo sasa, alipoingia yule kachero wa kwanza. Hila aliyoitumia Nuru ya kujifanya kuwa alikuwa akipambana na mzungu aliyetaka kumnajisi ilimsaidia sana. Ndipo kachero huyo alipopata kile alichostahili kupata. Nao akafanya haraka kumsaidia Nuru kuvaa “Uzungu” wake na alipokamilika walivichukua vilivyokuwa muhimu na kuingia mitaani.

Wakiwa wameikariri ramani hiyo kikamilifu, kazi waliyoifanya mitaani humo ilikuwa kufuata yale majengo waliyokusudia na kutega vile vigololi vilivyopatikana kwa Chonde na kuvitegesha katika kipindi cha saa tatu kamili. Walifanya kazi hiyo kwa ukamilifu kuliko walivyotegemea. Watu wachache ambao walilazimika kupoteza maisha ni wale walioshuku jambo au kujaribu kuwazuia kufanya kazi yao. Wakiwa hawajui kuwa wanapambana na nani watu hao walikufa kwa utulivu kabisa, isipokuwa yule ambaye kifo kilimtetemesha hata akaamua kuruka dirishani kutoka ghorofa ya nne akiwa na kisu kifuani.

Sasa kazi ya kutega vigololi ikiwa imekwisha, Joram alimtazama Nuru na kumnong’oneza, “Awamu iliyobaki ni yangu peke yangu. Ni lazima niingie katika mtambo wao na kuulipua. Nikiweza kuulipua kabla ya madhara tuliyoandaa katika jiji hili kutokea litakuwa jambo jema sana. Nikishindwa, mioto itakapoanza nenda pale ambapo nimekuonyesha katika ramani ukanisubiri.”

“Hatuwezi kwenda wote?”

“Haiwezekani. Tumelijadili hilo mara nyingi sana.”

Wakakubaliana.

5

MKOBA wake wenye silaha zake zote ukiwa umetulia mkononi, kwa utulivu na uhakika kama mzigo wowote ambao haukuchukua chochote cha haja, Joram alipiga hatua moja baada ya nyingine katika mitaa ya mji mkuu wa Afrika Kusini. Alipishana na wengi akiandamana na wengi wenye misafara yao.

Kitu fulani katika damu yake kilimnong'oneza kuwa anafuatwa. Hilo halikumshangaza. Tangu alipoachana na Nuru alifahamu fika kuwa angepinga ushauri wake wa kumsubiri pale alipomwelekeza hadi atakapoimaliza awamu hii ya mwisho ambayo ilikuwa ya hatari mno. Akiwa ameshangazwa na ushujaa wa msichana huyu, jinsi alivyokuwa tayari kuihatarisha roho yake kwa hiari, aliamini kabisa kuwa asingekubali kuikosa fursa hii ya mwisho, fursa ambayo endapo ingefanikiwa isingefutika katika kurasa za matukio muhimu ya kihistoria duniani.

Hivyo, hakujishughulisha kugeuka nyuma, kwa hofu ya kuwafanya makachero, ambao aliamini wamezagaa kote mitaani wakimtafuta, kumshuku. Badala yake aliendelea na safari yake huku akitafuta nafasi na wasaa ambao ungemwezesha kumtia Nuru chenga ya mwili. Hakuumaliza mtaa huo kabla fursa hiyo haijajitokeza. Katika kona ya mtaa huo Joram alikuta mahala palipokuwa na ajali ya magari matatu yaliyogongana.

Watu wengi walikuwa wamejazana kuitazama ajali hiyo. Kati yao, Joram aliweza kuona nyuso za watu wenye dalili ya ukachero na uaskari. Hakuwajali. Badala yake alijitia mmoja kati ya raia waliokuwa wakiitazama miili ya madereva wawili ambao hawakuwa na dalili ya uhai.

Aliitumia fursa hiyo kutoa kofia mfukoni na kuivaa kichwani, pamoja na kuyafunika macho yake kwa miwani ya jua. Kisha akajipenyeza katika kundi hilo na kutokea tayari akiwa amemchanganya Nuru. Hivyo, akaendelea na safari yake, mluzi mdomoni, tabasamu usoni na hadhari moyoni.

Baada ya mitaa kadhaa aliumaliza mji. Kwa mbali, alililona jengo lenye mtambo aliokuwa akiuhitaji. Ili kuthibitisha alitumia hila kuitazama ramani yake. Hakuwa amekosea. Akaendelea na safari yake akianza kujikumbusha kwa mara nyingine hila ambazo aliziandaa ili zimwezeshe kufanikisha jukumu lililokuwa mbele yake. Hakuwa amekosea.

Akaendelea na safari yake akianza kujikumbusha kwa mara nyingine hila ambazo aliziandaa ili zimwezeshe kufanikisha jukumu lililokuwa mbele yake. Moyoni alijua kabisa kuwa alikuwa akikaribia mbele ya domo la mauti lililo wazi. Kuingia ulikuwa wajibu wake, lakini kutoka kinywani humo akiwa hai ni jambo ambalo hakuwa na hakika nalo.

Hakuogopa. Lakini kutokuogopa hakukumfanya astahimili kujikuta akitokwa na sala ndefu kimoyomoyo, jambo ambalo hakumbuki kwa mara ya mwisho alilifanya lini.

"Bado yuko mbele yetu mzee…" Taarifa ilimfikia Von Iron ambaye alitulia katika ofisi yake, mara kwa mara akitazama saa yake ya mkononi. "… Tufanyeje mzee? Tumuue?…" sauti iliendelea.

"Nimesema mwacheni," Von alinguruma katika walkie talkie iliyokuwa mbele yake. "Mfuateni hadi mtakapopata nafasi nzuri mumkamate. Tunamtaka hai."

"Anaelekea kuwa anaweza kuleta madhara, mzee. Anaweza kuwa na silaha…" sauti iliendelea.

"Unataka kuniambia kuwa wanaume wanne mnashindwa kumkamata malaya mmoja tu wa Kiafrika?"

“Sivyo, mzee. Lakini…”

“Lakini nini? Mnachotakiwa kufanya ni kumleta hapa akiwa hai, ili atueleze wapi alikotorokea Joram Kiango. Mkishindwa kufanya hivyo nadhani hamtashangaa kwa lolote litakalowapateni.” Alimaliza na kufunga redio hiyo.

Taarifa ya kuonekana kwa Nuru ilimfikia nusu saa iliyopita. Fununu iliyosaidia kupatikana kwake ililetwa na mtu aliyefia hospitali baada ya kuruka dirishani kwa maumivu ya kisu. Kabla ya kukata roho mtu huyo alifaulu kutamka kuwa aliuawa na msichana wa kizungu mwenye lafudhi ya Kiafrika. Wakagundua kuwa mafanikio yote ya Joram yalitokana na hila ya kujifanya mzungu.

Ndipo wakuelekeza upelelezi kwa namna nyingine. Na haukupita muda kabla hajatiliwa mashaka msichana huyu ambaye alikuwa akitembea mitaani kwa namna ambayo si ya kawaida kwa wasichana, asubuhi kama hiyo. Mtu alimsogelea. Akamsalimu. Majibu aliyopata yaliutia kasoro uzungu wake kutokana na lafudhi. Mwingine alimkaribia.

Akajitia kukosea na kuugonga mkoba wake, kisha aliinama mbiombio kumsaidia kuuokota. Alishangazwa na wepesi wa msichana huyo katika kuuokota mkoba huo. Alimtazama vizuri zaidi. Akaona dalili ya Uzungu bandia katika uso na mwili wake. Ndipo akaandamwa, bila ya yeye kufahamu, dakika yoyote akiwa tayari kupigwa risasi, endapo Iron angeafiki…

Iron hakuwa tayari kuafikiana na makachero hao waliojaa hasira na uchu wa kumuua Nuru. Hakuafiki kwa kuwa yeye pia alijawa na uchu moyoni, uchu wa kumpata Nuru akiwa hai, uchu wa kuonja kile ambacho aliambulia kukishuhudia kwa macho tu. Ndiyo, kufa, Nuru alikuwa hana budi. Lakini angeweza kufa baadaye. Hakuiona sababu yoyote ya kufanya haraka.

“Bosi tumeamua kumnasa…” taarifa ziliendelea kumfikia.

“Mkamateni.”

Mara zikasikika purukushaniu katika chombo hicho. Zilifuatiwa na milio ya risasi tatu. Moyo wa Iron ulidunda kwa hofu. Asingevumilia endapo msafara wa risasi hizo ungeishia katika mwili wa Nuru kabla…

“Bosi amemjeruhi mtu wetu… turuhusu tummalize…”

“Nasema mleteni akiwa hai,” Iron alinguruma.

Mara chombo cha mawasiliano kikazimwa. Dakika chache baadaye mlango wa ofisi ya Iron ulifunguka na kumruhusu msichana ambaye alikuwa akisukumwa kwa mitutu ya bastola nne kuingia chumbani humo huku akipepesuka. Alikuwa hai. Lakini jeraha la kisu katika mkono wake wa kulia, kuchubuka shavuni, na uvimbe usoni, vilidhihirisha kuwa aliupigania uhai wake kwa gharama kubwa.

“Ameua watu wawili,” kiongozi wa msafara huo alieleza.

“Atajuta…” lilikuwa jibu pekee la Iron.

“Amegoma katakata kuelekeza alikojificha mwenzake.”

“Ataeleza.”

Makachero hao walishangazwa kiasi na tabia hiyo mpya ya kiongozi wao. Hakuwa Von Iron waliyemfahamu. Von Iron waliyemfahamu angekuwa wa kwanza kutamka kwa ukali “ua.” Na endapo kifo kisingetokea mapema Von Iron waliyemfahamu angeshuhudia ukatili wa hali ya juu

ukitendeka katika mwili wa msichana huyo jeuri aliyetisha, hasa jinsi ngozi yake ya bandia iliyobanduka hapa na pale kwa purukushani na kufanya mabaka ya ngozi yake asilia yajitokeze kwa namna ya kuchekesha na kutisha kiasi.

“Sikieni,” Von aliwaamuru. “Huyu niachieni mimi. Nitajua la kumfanya. Fanyeni hivi, endeleeni kumtafuta Joram Kiango. Mkimpata namtaka vilevile. Hai au maiti. Sawa?”

“Sawa, bosi,” waliafiki wakitoka mmojammoja, baada ya kutazamana tena kwa mshangao.

Walipobaki peke yao Von Iron alikiacha kiti chake na kumsogelea Nuru. Akamkazia macho yake makali. Mara alilazimika kuyainamisha macho hayo mara moja baada ya kuona kitu ambacho hakupata kukiona katika macho ya msichana yeyote, kitu kisichoelezeka kwa ukamilifu, kitu kama nuru ya aina yake ambacho kilifunua mapazia fulani na kuacha barabara ndefu inayoelekea kusikojulikana; kilichomfanya Joram ayaepuke macho hayo ni zile hisia za kutatanisha ambazo zilimjia ghafla zikimfanya ajihisi kama anayeifuata barabara hiyo akielekea huko ambako hakujulikana, katika dunia nyingine inayotatanisha.

“Una habari kuwa maisha yako yamo mikononi mwangu?” Von Iron aliuliza.

Hakupata jibu, jambo ambalo lilimfanya ainue tena macho na kumtazama Nuru.

Ile nuru ya kutisha aliyoiona awali katika macho hayo haikuwepo tena. Badala yake alikutana na macho yaleyale aliyoyategemea, macho aliyotamani kuyaona, macho ya msichana, yenye dalili zote za usichana. Mara akawakumbuka marehemu wazazi wake. Akakumbuka kuwa ni kitu fulani katika maumbo ya msichana mweusi kama huyu ambacho kiliwafanya waondoke duniani kwa aibu na uchungu, kitu ambacho Von alikuwa akikitamani ili akione au kukionja. Leo ilikuwa fursa ya kipekee. Atamtumia msichana huyu kumfunulia siri hiyo, kisha angemwua.

“Una habari kuwa maisha yako yamo mikononi mwangu?” alilirudia swali lake.

Bado Nuru hakumjibu. Aliendelelea kusimama paleplae alipokuwa, uchovu ukimsumbua, maumivu yakimtesa. Moyoni hasira kali ilikuwa ikichemka dhidi ya watu hawa. Hakuwa na shaka kuwa maisha yake yalikuwa ukingoni. Lakini si hilo lililomtia hasira. Hasa alisikitika kwa kule kuona kuwa amekamatwa kabla ya kazi ya mwisho kukamilika. Japo alikuwa na hakika kuwa Joram alikuwa hajakamatwa, lakini aliamini kuwa ingekuwa haki yake kushirikiana na Joram bega kwa bega katika awamu ya mwisho kama walivyofanya katika ile ya awali. Kiasi, vilevile, alikuwa akijiuliza kama hakuwa amefanya makosa kwenda kinyume cha matakwa ya Joram na kumfuata kwa siri badala ya kumsubiri kama alivyoamriwa. Alijuwa wazi kuwa ni kitendo hicho ambacho kilimtia mashakani.

Hata hivyo, hakuwa na hofu kubwa sana juu ya maisha yake. Hakuamini kuwa kifo kilikuwa karibu kiasi hicho. Mipango waliyoiandaa ilimtia hakika kuwa ingetokea fursa nzuri ambayo ingempa mwanya wa kutoroka hadi nchi jirani za mstari wa mbele. Imani hiyo ilijengeka katika moyo wake mara alipojikuta amezungukwa na askari wenye silaha, lakini wakiwa hawana dalili ya kuzitumia silaha hizo dhidi yake. Hata baada ya kutoa bastola yake na kuwaua wawili kati yao walifyatua silaha zao kwa dhamira ya kumtisha tu; akajua kuwa walimtaka hai ili wamlazimishe kutoa siri fulani. Hivyo, hata alipozidiwa nguvu, baada ya kuvamiwa na kupigwa sana, hakuwa na shaka sana.

Na hasa huyu mtu mnene anayeonekana kama kiongozi wao. Huyu ambaye tamaa ya kimwili ilikuwa wazi katika macho yake. Kosa analofanya huyu la kumtamani lingeweza kabisa kusaidia kuyaokoa maisha yake na ya Joram Kiango. Alichohitaji ni muda kidogo.

Suala hili la kupendwa au kuhitajiwa kimapenzi halikumshangaza. Kwa kweli, alilitegemea. Joram alikuwa amemfafanulia hilo pia walipokuwa wakijiandaa kuingia nchini humu. Alimweleza kwa lugha ya kishairi akisema “Katika silaha zote za mwanamke uzuri unazitangulia.” Akamweleza kinagaubaga nini la kufanya. Hata walipokuwa wakifanya mapenzi kitandani, kabla ya Joram kutumia hila ya kuharibu kile chombo chao cha kutazamia alimnong’oneza, “Tutafanya kila kitu. Najuwa wanatutazama, usione haya. Nataka tuwatie homa ili endapo watatukamata, watamani kuyashuhudia waliyoyaona kwa vitendo. Nafasi ambayo natumaini hutashindwa kuitumia.”

Haya, sasa nafasi hiyo imetokea… Nuru alijiambia kimoyomoyo. Akayainua macho yake, akayalegeza kidogo, akiruhusu tabasamu dogo. “Najua kuwa ninakufa…” alimjibu Iron kwa sauti ndogo ambayo masikioni mwa mwanaume ilitosha kuanzisha kongamano fulani baina ya mwili na damu.

Kufa huna budi! Iron alisema rohoni… utakufa kifo kibaya. Lakini itakuwa baada!… kwa mdomo alisema, “Nimesema maisha yako yamo mikononi mwangu. Vitendo vyenu vilikuwa vuya kinyama mno. Pamoja na kupokelewa vizuri katika nchi hii na kuahidiwa kuishi kwa amani na starehe,

bado mmediriki kufanya mambo yasiyoeleweka. Mnapita kuua watu wasio na hatia bila sababu yoyote. Naamini huo ni ushauri wa huyu mwendawazimu uliyefuatana naye. Unafahamu alikokimbilia?"

"Sifahamu…"

"Amekutoroka," Iron alidakia. "Amekutoroka. Bila shaka hivi sasa anajaribu kuitoroka nchi. Hafiki mbali. Dakika yoyote ataletwa hapa akiwa hai au maiti," alimaliza akimkazia macho Nuru. Macho yake yalikumbuka alichohitaji. Akazisahau hasira zake dhidi ya Joram na kumnong'oneza Nuru kwa sauti ambayo kwake ilijaa upendo. "Suala lako ni tofauti bi mdogo. Una nafasi nzuri ya kusamehewa madhambi hayo iwapo tu… iwapo…"

Mara Iron alijikuta hajui lipi zaidi amwambie Nuru. Hakuwa hodari wa kutongoza. Ingawa alisoma riwaya nyingi za mapenzi, lakini ilikuwa vigumu sana kila alipotamani kuyaweka aliyoyasoma katika vitendo. Sababu moja kati ya nyingi zilizomfanya hadi leo awe hana mke ni hiyo ya kutojua kuwakabili wanawake wote aliowahitaji walikuwa kama wanaomdhihaki kwa kusubiri aseme nini. Wale ambao hakuwataka ndio waliojileta kwake kwa urahisi. Alipolewa hakubabaika kuwalaki. Lakini leo, kichwani akiwa hana hata tone moja la pombe, hakuona vipi ampate Nuru. Akaduwaa akimtazama.

Nuru aliuhisi unyonge huo. Akaamua kusubiri.

Nusu dakika ilipotea kabla ya Iron kujua aseme nini. Kisha alikumbuka kuwa alikuwa na akiba nzuri ya vinywaji vikali. Akafungua kabati na kutoa chupa moja ya John Walker ambayo aliimimina katika glasi. Alimkaribisha Nuru ambaye alikataa. Akaimimina tumboni mwake. Glasi ya pili ilimchangamsha. Akarudisha vifaa hivyo katika kabati na kumsogelea Nuru na kumgusa bega huku akinong'ona kwa sauti ambayo kichwani mwake alihisi imejaa mahaba. "Wewe ni msichana mzuri sana wa Kiafrika. Sijapata kumwona mwingine wa aina yako." Mkono wake ukagusa pale ambapo ngozi ya bandia ya Uzungu aliyoivaa Nuru ilikuwa imebandukabanduka kwa purukushani. Akaishika na kuibandua. Gundi nyepesi iliyotumiwa kuiambatanisha ngozi hiyo ya nailoni na mwili iliacha mabaka meupe. Lakini nyuma ya mabaka hayo ulijitokeza uso mzuri, uso asilia wa Nuru. "Wewe ni mzuri kama ulivyo. Huhitaji kabisa ngozi hii," Iron alisema akizidi kuzibandua ngozi sehemu za mapajani.

Sasa aliyesimama mbele yake hakuwa tena yule msichana wa Kizungu. Alikuwa msichana wa Kiafrika, msichana mzuri, ambaye kwa muda, uzuri wake ulimpumbaza kaburu Iron. Kisha tamaa ikamzidi nguvu, mikono yake ikapoteza utulivu na kuanza ziara kutambaa katika mwili wa Nuru. Mara ulimi wake ukaanza kudai njia katika kinywa cha Nuru, huku akitweta kwa nguvu na kunong'ona maneno ambayo Nuru hakuyaelewa. Hakutofautiana na sokwe mweupe aliyeonjeshwa asali.

Kila kitendo cha Von kilizidisha hasira katika moyo wa Nuru. Mikono hiyo ilipoyafikia matiti yake na kuyachezea, akahisi kama aliyeguswa na kinyaa ulimi ulipokuwa ukibishana na meno yake ukitafuta mwanya wa kuingia mdomoni mwake, aliona kichefuchefu. Ambacho alitamani kufanya ni kutumia fursa hiyo kuachia pigo ambalo lingeondoa uhai kisha kutafuta fursa ya kutoroka. Hata hivyo, hakuthubutu kufanya hivyo kwa kuchelea kuharibu mambo. Hakukoma kuitazama saa kubwa iliyokuwa ukutani. Kila dakika iliyopita alikuwa akisheherekea kimoyomoyo. Sasa ilikuwa imebaki kama saa moja tu kabla ya mitego waliyoitega kufyatuka. Wakati huo asingekosa mwanya wa kutoroka. Kabla ya hapo alihitaji kuubembeleza muda kwa bei yoyote.. isingemgharimu chochote kuendelea kuliruhusu jitu nene liendelee kujipumbaza katika mwili wake. Mara moja mbili akaguna na kutetemeka kwa namna ya kumfanya aonekane kama aliyeshikwa na ashiki.

Kitendo hicho kilichochea wazimu wa Iron. Mara akapambua mavazi ya Nuru. Mikono yake iliyokuwa ikitetetemeka iligombana na vifungo vya mavazi huku akizidi kunong'ona hili na lile. "Sikiliza…" Nuru alimweleza akiushika mkono wake na kuutoa mapajani mwake huku akimfinyafinya. "Hapa ni ofisini. Mtu yeyote anaweza kuingia…"

"Hii ni ofisi yangu," Von alikoroma. "Hamna anayeweza kuingia bila ruhusa yangu."

"Sio vizuri."

"Tafadhali…" kisha Von alijilaumu kwa kutamka neno hilo. Vipi amtafadhalishe mtu mweusi? Zaidi, mtu ambaye roho yake iko katika mikono yake. Akaupeleka mkono wake wa pili katikati ya mapaja ya Nuru kwa nguvu kidogo. Nuru aliyabana mapaja yake. Ni hapo Von alipokumbuka kuwa isingekuwa kazi ndogo kumtenda msichana huyu bila hiari. Hakuwa amezisahau zile picha za sinema ambazo huonyesha jasho linavyowatoka watu wanaojaribu kunajisi. Wala asingesahau yaliyosemwa katika kile kitabu cha mapenzi alichowahi kusoma, "… hicho ni kitu pekee ambacho mwanamke ana mamlaka nacho… kitu pekee anachoweza kujivunia… rasilimali yake pekee…" hivyo, akajikuta akilazimika kutumia njia nyingine. "Una habari kuwa maisha yako yamo mikononi mwangu? Dakika yoyote nitakayosema ufe utakuwa marehemu. Najaribu kukuokoa kwa kuwa sioni kama unastahili kufa mapema kiasi hiki," alimweleza Nuru.

“Nitajuaje kama hunidanganyi? Nitajuaje kama baada ya kumaliza shida zako hutaniua?” Nuru alisema akimlegezea macho.

“Nakuhakikishia kuwa utakwenda zako kwa amani na furaha kokote unakotaka kwenda.” Von alipoona hajaaminika kikamilifu alimwacha Nuru kwa muda na kuliendea kabati ambalo alilifungua na kutoa bahasha kubwa. Ndani ya bahasha hiyo mlikuwa na pesa nyingi za nchi mbalimbali. “Hizi ni pesa zenu. Ni miongoni mwa vitu vyenu mlivyonyang’anywa mlipofika hapa. Sasa hivi nakukabidhi pesa hizi ukae nazo ili utakapoondoka zako ukaishi popote unapotaka.” Alimpa Nuru na kuziweka katika mfuko wake. Alikuwa akicheka kimoyomoyo akifahamu kuwa mara baada ya kuimaliza hamu yake na kumwua Nuru angezirejesha fedha hizo katika himaya yake. “Sasa tunaweza kuendelea,” alisema akianza upya kuchezea mwili wa Nuru.

Nuru hakumzuia mara moja. Alikuwa hajafahamu atumie hila ipi kumchelewesha tena. Safari hiyo kilichomwokoa Nuru ni king’ora kilichotoa mlio wa aina ya paka aliyekabwa koo katika moja ya mitambo ya Von. Sauti hiyo ilimfanya Von aruke hadi kwenye simu ambako aliichukua na kusikiliza kwa makini. Sauti nyembamba ilisema kwa wasiwasi, “Bosi, inaelekea kuna jambo la hatari katika mtambo maalumu. King’ora cha hadhari kimekuwa kikilia kwa muda mrefu. Simu za walinzi wetu huko hazipokelewi.”

“Impossible,” Von alifoka. “Unataka kuniambia kuwa maafa yanayotokea mjini yanaweza kuhamia huko nje ya mji?”

“Inaelekea, mzee. Kwa sababu huyu mtu anayeitwa Joram haelezeki. Aweza kuwa huko sasa hivi.”

“Impossible,” alifoka tena. “Na kama kweli kaenda huko, basi kajipeleka mwenyewe kaburini.” Von alisita kidogo. Kisha aliongeza, “Sikia. Andaa helikopta yangu na dereva. Nataka kufika huko mara moja. Nataka kushuhudia kwa macho yangu mwenyewe mtu huyo anayejiita Joram Kiango anavyosulubiwa.

Huko angani Nuru aliziona vizuri kabisa maiti nne za askari wa Makaburu zilizovalia magwanda na silaha zao mikononi. Zilikuwa zimelala sakafuni mbele ya lango kubwa la chuma ambalo lilizunguka ua wa seng’enge uliozunguka jumba kubwa. Helikopta ililizunguka jengo hilo mara tatu, Von akitazama kwa darubini huku na kule. Aliporidhika alimwamuru rubani kutua kando ya ua huo katika kichaka kilichoutenga mtambo huo na mji.

Kutoka mjini hadi hapa, ilikuwa safari ya dakika mbili tatu tu. Kabla ya kuanza safari hiyo Von alitupiana maneno makali na msaidizi wake ambaye alishangazwa na uamuzi wa Von kumpeleka Nuru huko. Alimwambia, “Sikubali kabisa. Nadhani ni wewe mwenyewe uliyeweka sharia ya kupigwa risasi mtu yeyote atakayekaribia mtambo ule, awe raia wa nchi au mgeni. Vipi aende huyu ambaye tunamhisi kuwa ni mwenzi wake ambaye amefika huko kufanya mashambulizi?”

“Huyu ni mateka wangu,” Von alimjibu. “Bado nina mengi ya kumsaili. Zaidi ya hayo, kama kweli Joram yuko huko tutamtumia huyu kumfanya Joram asithubutu kuendelea na chochote anachoota kichwani mwake.”

“Bado sikubali,” msaidizi huyo alieleza. “Nimeandaa kikosi cha askari wanne ambao ungefuatana nao huko. Kadhalika, nilikuwa nikisubiri amri yako ili nitumie askari wengine hamsini kwa gari. Inaelekea yote niliyofanya ni bure.”

“Ni bure kabisa,” Von alimjibu. “Unajua kabisa kuwa mtambo ule unalindwa katika hali isiyo na shaka kabisa. Hata kama atafanikiwa kuingia ndani hawezi kabisa kufanya madhara yoyote. Baada ya juhudi zake zote ataambulia kufa tu. Hivyo, nakushauri urudi na hao askari wako uliowaandaa. Nitakwenda mimi, huyu mateka na dereva tu. Sawa?”

Msaidizi huyo alimtazama Von kwa hasira ya mshangao. Alizithamini sana hekima zake katika masuala yote ya kiusalama katika nchi hii miaka yote aliyokuwa naye. Lakini vitendo vyake saa chache zilizopita vilimchanganya kabisa. Vilikuwa vitendo ambavyo havikubaliki. Yeye, kama mtu wa pili katika usalama wa utawala huu, hakuona kama alistahili kumtii Von hata kwa hilo. Hivyo, alimtupia jicho la hasira na kumwambia, “Kwa mara ya kwanza nitafanya kinyume cha matakwa yako.”

“Na kwa mara ya kwanza nakuambia kuwa… kuwa… hufai kufanya kazi chini yangu. Baada ya suala hili nitaangalia suala lako,” Von alisema akimsukumiza Nuru katika helikopta na kumwamuru rubani kuondoka.

Hata hivyo, rohoni alikuwa na mashaka kwa uamuzi wake huu. Alijua kabisa kuwa alikuwa akifanya kosa kubwa kufuatana na Nuru huko aendako. Hata hivyo, alifahamu fika kuwa hii ilikuwa nafasi yake pekee ya kufanya naye mapenzi na baadaye kumwua. Kimojawapo cha vyumba kadhaa

katika jengo la mtambo huu kilikuwa chumba maalumu cha faraja kwa ajili yake na wakubwa wachache sana. Chumba hicho kilikuwa na mitambo ya televisheni, ambayo ilitumia nguvu ya setilaiti yao hiyo iliyoko angani kuitazama miji mbalimbali ya Afrika kinaganaga. Vilevile kulikuwa na chombo maalumu ambacho kinaweza kutazama shughuli zote zinazofanyika katika chumba hicho. Mara kwa mara Von hujifungia humo na kutazama utendaji kazi wahandisi bila ya wao kuwa na habari. Mhandisi mmoja aliwahi kupoteza kazi na maisha yake baada ya kushukiwa na Von kuwa alikuwa na dhamira mbaya kwa mtambo huu. Hivyo, kifo chake machoni mwa watu wengi kilionekana kama ajali tu iliyosababishwa na dereva mlevi kugonga mtu anayetembea kando ya barabara katika mitaa ya Johanesburg. Leo Von alitegemea kukitumia chumba hicho kujistarehesha na mwili wa Nuru kabla ya kutulia na kuanza kuangalia kwa furaha watu wanavyoteketea kwa moto katika miji ya Dar es Salaam, Lagos, Lusaka, Harare na kwingineko.

Furaha iliyokuwa ikichemka katika fikra za Von iliingia nyongo mara baada ya helikopta yake kupita juu ya jengo hilo na kushuhudia walinzi wake walivyolala ovyo wakiwa maiti. Hivyo, akamtupia Nuru jicho la chuki. Tamaa aliyokuwanayo dhidi yake ilianza kuyeyuka na nafasi yake kuchukuliwa na hasira kali. Alitamani ammalize papo hapo na kuyasahau yote aliyokuwa akiyawaza juu yake. Hata hivyo, wazo jingine lilimjia akilini. Nuru alionekana katili sana ambaye haogopi kifo kama wanawake wengine anaowafahamu. Hata hivyo, anaweza kufa baada ya kutaabika sana. Hakuna mateso ambayo yatamtaabisha zaidi ya kushuhudia kifo cha mpenzi wake, Joram Kiango. Akiwa na hakika kabisa kuwa Joram alikuwa maala fulani katika jengo hilo akifa au kusubiri kifo, Von alitoa bastola yake na kuigongagonga katika kisogo cha Nuru. “Twende,” alimwamuru, baada ya kumtaka rubani asubiri katika helikopta.

Nuru alitelemka na kufuata maelekezo ya Von. Waliipita miili ya marehemu waliolala ovyo, damu ikivuja kutoka katika majeraha ya risasi miilini mwao.

Von alimshangaa Joram, peke yake, aliwezaje kuwaangamiza askari wengi kiasi hicho bila wao kufanya lolote. Lakini haikumshangaza Nuru hata kidogo. Wala Nuru hakuhitaji kusimuliwa. Akiwa mtu anayemfahamu Joram na hila zake nyingi alijua kuwa alitumia njia moja au nyingine kuwafikia askari hao waliojiamini kwa silaha zao aina ya machine gun. Baada ya hapo alitoa hati zake za bandia kuwaonyesha askari hao, hati ambazo zilifungwa kinamna kiasi cha kuhifadhi hewa ya sumu ambayo, bila shaka, iliwafanya askari kulewa ghafla na hivyo, kuwaua mmoja baada ya mwingine haikuwa kazi ngumu.

Kilichomshangaza Nuru ni kutofahamu Joram alikuwa akifanya nini muda wote huo katika eneo la hatari kama hilo. Alikadiria kuwa dakika tano zingetosha kabisa kuuteketeza mtambo huo na kutoweka. Na kwa mujibu wa ramani yao ndani ya kiwanda hicho hamkuwa na ulinzi wowote zaidi. Vipi asitokee na kummaliza mtu huyu mnene ili waondoke zao?

Von hakumpa nafasi ya kuwaza zaidi. Alikuwa akimsumbua mbele kwa mtutu wa bastola yake harakaharaka. Nuru hakuwa mzito wa kuelewa kuwa Von alikuwa akimtangulia kwa dhamira ya kumfanya ngao endapo lolote lingetukia kinyume na mategemeo yake.

Baada ya kukagua vyumba mbalimbali wakafika katika chumba cha Von. Ukiondoa makochi na kabati lililojengwa ukutani chumba hicho hakikutofautiana na maabara au studio ya aina yake machoni mwa Nuru. Mashine na mitambo mingi ilikuwa imepangwa kwa tafsiri fulani, kuta zikiwa screen zilizopangwa katika hali ya kupokea habari mbalimbali. Von aliisogelea mashine moja ambayo machoni mwa Nuru ilikuwa kama kompyuta na kubonyeza swichi ainaaina. Kioo katika ukuta mmoja kilipata uhai na kuanza kuonyesha mambo ya ajabuajabu. Baada ya hali kutulia Nuru aliona kuwa walikuwa wakitazama chumba baada ya chumba katika jengo hilo. Kilitokea chumba ambacho kilikuwa na mitambo mingi ya kutisha. Chumbani humo Nuru aliwaona wahandisi watatu waliokuwa makini wakichapa kazi ya kuongoza mitambo bila dalili yoyote kuwa mambo yanakwenda mrama. Hilo lilimfurahisha sana Von. Akaangua kicheko kwa furaha. Ni yeye aliyependekeza kuwa kwa usalama wa mitambo ishara za hatari zisiwafikie wahandisi hao, wasije wakapata hofu na kusababisha setilaiti iliyoko angani kukosa uongozi wa ardhini, jambo ambalo lingeweza kusababisha maafa na hasara isiyokadirika. Kwa jinsi jengo hilo lilivyoandaliwa Von alikuwa na hakika kabisa kuwa ingemhitaji binadamu mwenye moyo wa malaika kuwafikia wahandisi hao na kuuharibu mtambo huo. Joram hakuwa na moyo huo. Ni hilo lililomtia nguvu. Sasa ameamini kuwa hakukosea. Kwa muda, aliwatazama wahandisi hao wanavyoshughulikia. Wakijua kuwa leo ilikuwa siku ya kazi kubwa walifanya kila kitu kwa juhudi na umakini wa hali ya juu. Kisha Von alibonyeza sehemu nyingine. Chumba hicho kikahama na vyumba vingine kuanza kupita katika kioo.

“Nataka tumwone mpenzi wako anavyokufa au alipofia,” alimweleza, tabasamu la kifedhuli likiyasindikiza maneno yake. “Keti tafadhali. Keti ili uone kwa starehe.”

SURA YA KUMI NA MOJA

KIOO kilionyesha vyumba mbalimbali ambavyo vilijitokeza na kupita. Kila chumba kilikuwa na vitu mbalimbali vilivyoyavuta macho ya Nuru. Lakini ilielekea kuwa havikuwa vyumba Von alivyovihitaji. Aliuendesha mtambo huo harakaharaka kwa kubonyeza kidude hiki na kile kama karani anayepiga chapa. Mara kilitokea chumba ambacho Von alikuwa akikitafuta. Katika chumba hicho, ambacho kilionekana kidogo, walikuwemo watu wawili waliokuwa wakipigana. Mmoja hakuwa mtu bali jitu. Lilikuwa pande la mwanamume, refu, nene, jeusi lenye magumi manene na macho ya kutisha. Lilikuwa likipigana kwa maguvu yote katika hali ambayo ilionyesha kuwa lilikusudia kuua kwa mikono. Jitu hili halikuwa na dalili yoyote ya uchovu wala maumivu yoyote. Kinyume kabisa cha mtu wa pili ambaye lilikuwa likipambana naye. Huyu alikuwa kijana wa kizungu, mwenye dalili zote za ushujaa na ufundi wa kupigana ngumi na karate. Lakini ufundi wake haukuwa na dalili yoyote ya

kuonyesha kulishinda jitu hili kwani tayari kijana huyo alikuwa akivuja damu hapa na pale katika majeraha ya kutisha, huku akiwa na dalili za uchovu mkubwa.

"Unaona?" Von alisema akicheka. "Mpenzi wako yuko mashakani. Wakati wowote ataaga dunia. Hajatokea binadamu aliyewahi kumshinda Toto na kukivuka chumba kile akiwa hai."

"Kwanza Nuru hakuelewa. Kisha akaelewa. Kijana wa kizungu aliyekuwa akipambana na jitu hilo la kutisha hakuwa mwingine zaidi ya Joram Kiango, akiwa bado katika hali ya Uzungu bandia. Moyo ulimdunda Nuru kwa hasira kuona akiwa ameketi hapa, juu ya kiti cha starehe, hali Joram anateseka peke yake. Akamgeukia Von kutazama uwezekano wa kumwua na kwenda kumsaidia Joram Kiango. Alikutana na macho makali ya Von ambayo yalimtazama katika hali ya kuyasoma mawazo yake kinaganaga. Bastola yake ilikuwa imara mkononi, ikimwelekea Nuru kifuani. Nuru hakuwa na la kufanya zaidi ya kuyarejesha macho yake katika screen na kulitazama pambano hilo lilivyokuwa likiendelea. Kichwani alikuwa akijiuliza kwa mshangao ni jitu la aina gani hili, kubwa kupindukia, jeusi kupindukia lenya nguvu kupindukia ambalo, badala ya kutumia maguvu hayo kupambana na utawala dhalimu wa makaburu bado, linawatetea kiasi hiki?

Alijilazimisha kutulia na kuendelea kulitazama pambano hilo la kutisha. Joram alibadili mbinu mbalimbali, akikwepa kiufundi karibu kila konde lililotupwa na jitu hilo, pamoja na kulipachika makonde mazito. Lakini haikusaidia. Joram hakuweza kupita chumba hicho kukiendea chumba cha pili ambako angeifikia mitambo aliyokusudia kuilipua. Kwa muda, Nuru alimwona Joram kama mtu aliyekata tamaa, akifikiria kuitumia bastola yake ambayo bila shaka ingewaweka tayari wahandisi aliokuwa akiwanyatia au kurudi alikotoka. Hapana, alimwona vizuri zaidi. Joram alikuwa akiwaza kwa makini huku akilitazama jitu hilo ambalo lilitulia kimya, likimsubiri kwa utulivu kama ambalo halikuwa na uhusiano wowote na matukio yote yaliyokuwa yakitendeka. Baada ya kulitazama sana jitu hilo Joram alifuta jasho na damu iliyojaa usoni mwake na kutamka maneno fulani ambayo hayakuwafikia Nuru na Von. Alitamka neno jingine.

Jitu hilo lilitulia kama lililosikia lugha yoyote ya dunia. Joram alipolisogelea hatua moja lilikaa tayari kwa mapambano. Aliposogea hatua ya pili lilirusha ngumi nyingi mfululizo. Joram akarudi nyuma na kuangua kicheko. Kicheko chake kilipokelewa na Von Iron ambaye alikuwa akilitazama pambano hilo kwa furaha. "Naanza kumheshimu mpenzi wako. Tayari amegundua kuwa hapigani na binadamu wa kawaida."

Nuru alijikuta akijiuma mdomo kwa hasira. Kwa nini muda wote huo alikuwa hajagundua hilo? Joram alikuwa hapambani na binadamu. Alikuwa akipambana na jitu lililoundwa kwa mkono wa binadamu katika umbo la binadamu, yaani robot. Aliwahi kusikia kuwa matajiri wengi wamekwishaanza tabia ya kuyaweka madude haya kama walinzi wao badala ya binadamu wa kawaida ambaye hutokea siku akakukimbia au kukugeuka.

"Sasa tuone atafanya nini," Von alikuwa akisema.

Nuru aliyafuata macho yake kumtazama Joram ambaye alionekana akiacha kujisumbua kupambana na jitu hilo na kuchungulia kwa makini, alifunua hiki na kile. Pilikapilika zake hizo zilimwezesha kufunua mahala ambapo kulikuwa na waya ainaaina hadi alipoona jitu hilo likijiweka sawa kama askari katika gwaride. Kisha lilianguka kifudifudi.

Nuru alishangilia kimoyomoyo. Kwa mshangao alimwona Von akishangilia vilevile. "Ana akili. Amegundua kuwa dude hilo linaendeshwa kwa nguvu ya sumaku ya umeme ambayo mitambo yake iko pale alipofunua. Ana akili…" Von alisema katika hali hiyo ya kushangilia. Alizidi kucheka. Nuru alizidi kushangaa kwa kutomwelewa hadi alipoongeza, "Ana akili ndiyo. Lakini zitamsaidia nini? Kwa kweli, jitu lile lina huruma sana. Muda wote huu lilikuwa likimrudisha kwa makonde ili asiende kujiua mwenyewe. Sasa mtazame. Ona mpenzi wako anavyojiua… Ona…"

Roho ikiwa juu Nuru, hakuwa na la kufanya zaidi ya kutazama. Alimwona Joram akitazama saa yake na kuanza mwendo wa haraka kukiendea chumba alichokuwa akikihitaji. Mwendo wake ulikuwa wa hadhari na uhakika, macho yakiwa wazi, mikono tayari kwa lolote ambalo lingetukia. Mara aliufikia mlango wa mwisho, uliomtenga na lengo lake. Alinyoosha mkono na kugusa kitasa. Papo hapo ardhi miguuni mwake ilifunuka na Joram kudidimia ghafla. Juhudi zake za kushika kando hazikuzaa matunda yoyote. Ardhi ilijifunika kama ilivyokuwa na Joram kupotea kama ndoto iliyofikia ukingoni.

"Tayari…" Von alichekelea.

Nuru alijikuta yuko wima mbele ya Von akinyoosha mikono kumpiga huku akifoka, "Yuko wapi Joram? Sema yko wapi?…"

Pigo la kitako cha bastola ambalo lilitua barabara kichwani mwake lilimpoteza fahamu. Fahamu zilipomrudia alikuwa amelazwa chali juu ya kochi alilolikalia awali. Alikuwa uchi kama alivyozaliwa, mavazi yake yaliyochakaa yakiwa yametupwa kando. Von alikuwa kaketi palepale alipokuwa,

sigara mdomoni. Macho yake yalimtazama Nuru kwa namna ya mtu aliyekuwa ameikata kiu yake ya muda mrefu. Nuru alimtazama kisha akajitazama na kuona alivyochafuka. Hakustahimili. Aliinuka na kumwendea Von kwa nia ya pambano jingine. Lakini hakumfikia. Hatua mbili alizozipiga zilimfanya ashindwe kuendelea na badala yake kuanguka sakafuni. Hata hivyo, mdomo haukuwa na udhaifu kiasi hicho.

“Wewe ni mshenzi kuliko washenzi wote niliopata kuwaona,” alifoka. “Mwanaume hayawani… Haya unasubiri nini? Niue kama ulivyomwua Joram. Niue…”

Von alitabasamu kifedhuli. Kitendo cha mapenzi ambacho kilimchukua dakika moja, Nuru akiwa hana fahamu, kiliupa moyo wake faraja kubwa. Hakutegemea. Mara akawa ameelewa kisa cha baba yake kupoteza maisha kwa ajili ya msichana mweusi. Hata hivyo, baada ya kuionja ladha aliyohitaji sana alianza kuiona athari ya kumwacha kiumbe huyo aendelee kuwa hai. Mapambano aliyoyaona baina ya Joram na robot yalikuwa yanatosha kabisa kumwonyesha watu hawa walivyo wapiganaji wasiokata tamaa. Joram amekwisha, lakini huyu japo ni mwanamke yungali hai, na anaweza kufanya lolote. Kifo cha haraka alichokidai kilikuwa halali yake kabisa.

Hata hivyo, angehitaji kumwona akifa kwa mateso zaidi. Angependa kuona tena anavyotaabika kushuhudia mji wao mashuhuri wa Dar es Salaam unavyoteketea. Angependa kuuona uso wake ukijaa hofu na majonzi kama ulivyofanya wakati Joram alipokuwa akiadhibiwa na robot Toto, na hasa pale alipodidimia ardhini.

“Ungependa kufa sasa hivi au baadaye kidogo?” aliuliza bila mzaha wowote katika sauti yake. “Saa moja na dakika chache baadaye kioo, ambacho kilikuwa kikionyesha mchezo wa ngumi baina ya mpenzi wake na Toto, kitaonyesha mchezo wa kupendeza zaidi. Jiji lenu la Dar es Salaam na miji mbalimbali ya Tanzania na nchi nyinginezo, litapata sura mpya, sura ya kupendeza. Natumaini ungependa kuliona hilo pia kabla hujafa ili upate habari ambayo utamsimulia Joram huko kuzimu alikotangulia.”

Nuru, nguvu na fahamu zikizidi kumrejea, aliufurahia uamuzi wa Von. Aliyakumbuka maneno fulani ya Joram, kati ya mengi aliyokuwa akimpa, aliposema: katika mambo haya, kila dakika ambayo inaweza kukuweka hai zaidi inunue kwa bei yoyote. Aliamua kuafikiana na Von. Wazo hilo hasa lilimjia baada ya kukumbuka kuwa, kama walichofanya ni kitu chenye uhakika, dakika chache kuanzia sasa jiji la Johanesburg litakuwa mashakani na Von atakuwa akisema mengine. Nafasi kama hiyo itakapowadia asingeshindwa kuitumia.

Hivyo, alijifanya mnyonge zaidi. Akajiweka kitini hapo katika hali iliyotosha kumsumbua mwanamume yeyote. Von alikwisha timiza Fula yake ya kimwili kwa Nuru. Hata hivyo, Nuru alijua fika kwamba, kutokana na tabia ya roho ya Fula ya mwanaume; dakika chache baadaye angerudiwa na Fula ileile kwa kiwango kikubwa zaidi.

“Wewe ni mshenzi…” alimchokoza tena ili atazamwe wakati huohuo akiyalegeza macho yake na kuzidi kujiweka juu ya kochi kinamna fulani.

Kitu hiki ambacho asili kiliwekwa baina ya mwanaume na mwanamke, kitu ambacho hakielezekai kikamilifu kwa maneno, kilitimiza wajibu wake. Nuru alibaini kuwa Von na ukatili wake, pamoja na kuamini kwake kuwa ametosheka na kukinai, alianza upya kutaabika. Macho yake hayakuweza tena kutulia, mikono yake ilikuwa haikai pamoja. Alihangaika, akienda hapa na pale na kushika hiki na kile. Tahamaki akawa ameketi kochi moja na Nuru, mkono wake mmoja ukikosa kochi na kuangukia juu ya paja nono la Nuru.

“Wewe ni mtu mbaya sana,” Nuru alisema, sauti ikiwa laini, huku akijitia kusogea kando kidogo.

“Sikiliza…”

Nuru alijitia kumsikiliza. Alichofanya hasa ilikuwa kuupima uwezekano wa kumzidi Von maarifa aikwapue bastola yake ambayo ilikuwa imara kama hirizi katika mkono wake wa pili.

Von hakuwa mgeni kwa silaha hii ambayo ilikuwa ikitumiwa na Nuru. Alifahamu fika kuwa msichana huyu alikuwa akitumia mbinu ili ayaokoe maisha yake. Lakini kufahamu huko hakukukata shauku yake ya kutamani tena. Alitamani tena, kwa mara ya mwisho. Nuru angefanya nini? Kama kuna kisu basi Nuru alikuwa ameshika makali yake yeye akiwa ameshikilia mpini. Hata hivyo, alijua kuwa anacheza mchezo hatari, anacheza na nyoka. Haikuwa busara kuchezea roho kando ya shimo la mauti lililowazi kiasi hicho. Ni hilo ambalo lilimfanya aendelee kuishikilia bastola kama roho yake.

Wakati huo Von alikwishaibonyeza mitambo yake ambayo alisema ingemwezesha kuiona setilaiti hiyo ikishuka taratibu toka angani na kuiendea anga ya Tanzania ambapo ingesubiri muda uliopangwa kabla ya kuanza kuachia dhoruba za hewa ambayo ingezusha moto wa kutisha. Katika kioo hicho waliweza kuyaona mawingu mazitomazito yakipita katika kioo. Kisha dude la ajabu likajitokeza. Lilikuwa kubwa, jeusi lenye muundo wa ndege aina ya kunguru. Lilikuwa likisafiri kwa mwendo mkali sana kama linaloifuata televisheni hiyo.

Von aliinuka ghafla huku ameshikwa na mshangao. Aliiendea meza iliyokuwa na chombo chenye vidude vingi alivyokuwa akivibonyeza na kuvikagua kwa makini. Alibonyezabonyeza na kutazama tena katika kioo. Alikuwa kama ambaye hakuyaamini macho yake kuliona dude hilo likizidi kusogea. Mara jiji la johanesburg likajitokeza katika kioo hicho, majumba fulanifulani makubwa yakitoa nuru nyekundu kama gari linaloonyesha linaelekea upande upi. Nuru hiyo ilipokelewa au kujibiwa na dalili hiyo ya moto kutoka katika domo la chombo hicho ambacho sasa kilikuwa kikielea juu ya mji.

Nuru aliyaelewa majumba yote hayo ambayo yalionyesha alama za moto. Ni yale ambayo yeye na Joram walifanikisha kutega vile vigololi walivyovipata kutoka kwa hayati Chonde. Akaitazama saa yake. Ilikuwa ikikaribia muda uleule ambao Joram alikuwa ameviandaa vidude vile kufanya kazi. Alitamani apige ukulele wa furaha. Tangu walipoanza harakati hizo hakuwa na hakika kama walikuwa wakifanya kitu chenye uhakika. Wala hakumwona Joram kuwa na hakika hiyo, pamoja na kufunua majitabu mengi ambayo yalikaribiua kumtia wazimu. Kumbe alijua anachokifanya! Ndoto yake imetukia kuwa kweli.

Wakati Nuru akifanya sherehe hiyo moyoni, Von alikuwa akitaabika kichwani. Hakuelewa kinachotokea. Dalili zilizojitokeza zilikuwa za kutisha kabisa, zisizokubalika. Ilionyesha kuwa wakati wowote mji wa Johanesburg ungekuwa ukiwaka moto, Johannesburg badala ya Dar es Salaam, aliwaza kwa hasira. Haikuwepo njia nyingine ya kufanya zaidi ya kuamuru setilaiti hiyo iharibiwe na kuanguka. Si kitu ikiangukia mji na kuua watu kadhaa. Heri nusu shari kuliko shari kamili. Ni hilo alilokusudia kufanya, kuinua simu na kuwapa wahandisi amri hiyo.

Hilo pia hakuweza kulifanya. Alijikuta akitazamwa na bastola yake mwenyewe, ambayo alihisahau kando alipokuwa akihangaika na mitambo. Bastola ilikuwa imara mikononi mwa Nuru, macho yake yasiyo na mzaha yakitangaza shari. “Pokea chako, mwuaji mkubwa,” Nuru alinong’ona akifyatua bastola.

Kwanza Von hakusikia maumivu. Alihisi kitu kikipenya kifuani na kuupapasa moyo wake. Kisha alisikia moyo ukiwaka moto. Akahisi kifo. Alipiga ukelele wa nguvu akichupa kumwendea Nuru mikono yake ikiwa wazi, tayari kumkaba koo. Lakini Nuru alimwepuka kwa urahisi na kumwongezea risasi nyingine ambayo ilimfumua fuvu la kichwa chake. Akadondoka chini na kulala kwa utulivu kama nguruwe aliyechunwa kwa maji ya moto.

Nuru aliyatazama matokeo ya kazi yake harakaharaka. Akaibusu bastola hiyo. Kisha akafanya haraka kujivika mavazi yake. Baada ya hapo alikimbilia kabati la Von ambalo alilifunua na kuanza kupekuapekua harakaharaka. Alipata alichokitaka. Ilikuwa ramani ya jengo hilo, ikiwa tofauti na ile waliyoitumia awali. Aliisoma himahima, kwa makini, kisha akaiweka mfukoni na kuuendea ukuta ambao ulikuwa na funguo nyingi. Akazichukua na kuziweka katika mfuko wake. Kisha, bastola ikimtangulia, alitoka chumbani humo mbio kama miguu yake ilivyoweza kumruhusu.

Kuanguka umbali wa zaidi ya mita ishirini kutoka angani hadi juu ya sakafu ngumu sio mchezo. Bila ya uhodari wake wa karate na sarakasi, kama Joram asingefikia kichwa basi angefikia mgongo na kuvunjikavunjika. Lakini alijitahidi kusahau uchovu na maumivu makali aliyokuwanayo, akaikusanya akili yake pamoja na kubingirika. Hata hivyo, fahamu zilimtoka kwa dakika kadhaa.

Uhai ulipomrudia alifungua macho yake kwa taabu na kutazama pande zote. Aligutuka kujikuta akiwa amelala katikati ya mizoga mingi ya binadamu, baadhi ikiwa mifupamifupa, baadhi ikiwa imevimbiana, mingine ikiwa imeoza kabisa. Mara akapatwa na harufu kali ya kutisha, harufu ambayo iliambatana na mainzi mengi manene ya kutisha, ambayo yalikuwa yakirukaruka katika hali ya kushangilia mawindo haya rahisi. Licha ya mainzi hayo Joram aliwaona panya wakubwa mithili ya paka waliokuwa wakifanya karamu katika miili ya binadamu hao. Panya mmoja alikuwa akipita kumzunguka Joram huku akimtazama kwa namna ambayo ilionyesha kuwa alitamani kuanza kumla akiwa hai bado.

Moyo ulimdunda Joram. Ingawa hakujua au kupata kuhisi hofu katika moyo wake lakini kitu fulani kilimpanda moyoni na kumtia hasira na kichefuchefu. Alihisi kama aliyeruka jivu na kukanyaga moto. Kama kufa kwa nini afe kifo kibaya kama hiki? Afe huku anaona? Huku analiwa na panya? Kwa nini asingeruhusu lile dude limwue?

Kisha alijikaza kiume na kujikongoja kusimama wima. Ilikuwa baada ya kujikumbusha ule usemi wake wa mara kwa mara kuwa “Binadamu hufa kwa uzee, hufa kwa ajali, hufa kwa maradhi. Lakini kuna binadamu ambao hufa kwa uvivu vilevile, hasa katika shughuli hizi za upelelezi.” Wazo hilo lilimtuma aanze kutembeatembea humo akitafuta mwanya ambao ungeweza kumtoa nje ya kaburi hilo.

Alizitazama kuta na kugundua kuwa zilijengwa kwa chuma cha pua, zikiwa kama chumba kirefu chenye upana wa mita kumi kwa ishirini. Akatazama juu, akiangalia uwezekano wa kupanda hadi huko alikoangukia. Ilikuwa ndoto nyingine. Ukuta ulikuwa laini mithili ya kioo ambacho kingemshinda hata paka.

Afanye nini? Aketi kukisubiri kifo? Alijiuliza. Hapana, lazima ajitahidi kutafuta mwanya. Lazima kuna mahala pengine penye mlango unaotumiwa kuwaleta watu hawa kusubiri kifo. Akaendelea kutembea akiiruka mizoga na wakati mwingine kulazimika kukanyaga mifupa. Mainzi na panya vilimwongezea msukosuko kwa kukimbia hapa na pale, bila ya shaka kwa mshangao wa kuona mlo wao ukitembea ovyoovyo kwenda huko na huku.

Joram alichunguza kila ukuta kwa makini. Hatimaye, aliufikia ukuta uliokuwa na mlango wa chuma uliofungwa kwa nje. Alijaribu kuutingisha mlango huo bila ya mafanikio. Ulikuwa mlango imara kama ukuta huo. Akautia mkono wake mfukoni na kuitoa bastola yake ambayo aliilenga mlangoni na kuifyatua. Risasi iliugonga na kuanguka ardhini kama gololi. Hata bomu lisingeubomoa mlango huo, jambo lililomfanya Joram aduwae kwa mara nyingine akifikiri la kufanya.

Mara macho yake yakavutwa na maiti moja iliyokuwa ikitikisika. Akaisogelea na kuitazama kwa makini. Naam, ilikuwa na uhai mdogo mwilini mwake. Miguu yake ilikuwa imekatwa na Joram aliona vilevile kuwa jicho lake moja lilikuwa limeng'olewa. Huyu alikuwa mtu mweupe, kinyume cha wengi ambao walikuwa weusi. Bila ya shaka alikuwa Mrusi.

"Pole," Joram alimwambia.

"Wewe ni nani?" mtu huyo aliuliza kwa udhaifu.

"Itakusaidia nini kunifahamu?" Joram alimjibu. "Unakaribia kufa."

Mtu huyo alicheka kidogo kabla ya kujikongoja kusema polepole, "Kweli. Haiwezi kunisaidia chochote. Hata hivyo, naona wewe utakufa kabla yangu. Mwenzio hii siku ya kumi na nne bado naishi."

Joram hakuona kama kuna umuhimu wowote wa kuendelea kumsikiliza mtu huyo aliyekaribia kukata roho. Lakini hakukuwa na jambo muhimu la kufanya na akaendelea kumsikiliza. Haikuchukua muda kabla hajafahamu kuwa Mrusi huyo alikuwa mmoja kati ya watu wengi waliokuwa wakiuawa kinyama baada ya kushukiwa kuwa walikuwa wakifanya upelelezi dhidi ya utawala wa makaburu.

Pango hili lilichimbwa maalumu kwa ajili ya kuwaangamiza watu hao kwa siri baada ya mateso mengi. Wengi waliachwa na kufa kwa majeraha waliyoyapata, lakini adhabu kubwa iliyowaangamiza ilikuwa njaa.

"Usishanagae," aliambiwa. "Ni njia pekee ya kutuwezesha kuishi." Alipomwona Joram akizidi kushangaa aliongeza, "Au unaogopa kula maiti? Sikia, unaweza kunila nikiwa hai. Sina dalili ya kupona. Na ninavyokuona unaonyesha kuwa tuko pamoja katika kupambana na utawala huo haramu. Unaweza kunila ukaishi kwa wiki moja zaidi, pengine mwujiza utatokea nawe ukapona na kuendelea na pambano. Usiogope wala usinishukuru. Wala sitaki kujua wewe ni nani. Haitanisaidia."

Joram aliona kama angerukwa na akili endapo angeendelea kuketi hapo akimsikiliza mtu huyo ambaye ilikuwa dhahiri kuwa uhai mdogo aliobakiwa nao ulikuwa mdomoni mwake tu. Akaondoka hapo taratibu na kuurudia mlango huo ambao alitulia tena akiutazama kwa makini.

Bado hakujua angeweza kufanya nini kuufungua. Ingehitaji mwujiza. Harufu ya maiti hizo, kelele za panya na mainzi yaliyokuwa yakishangilia bahati zao, vilizidi kumsumbua. Joram alijua kuwa harufu na usumbufu huo vingemwua kabla hajasikia njaa.

Aliutazama tena mlango kwa uchungu na hasira. Akatamani apige magoti na kumwomba Mungu ili afanye mwujiza mlango ufunguke. Hilo hakufanya. Ingekuwa unafiki kwani hakuwa amemwomba Mungu walao kwa kumshukuru kwa miaka mingi sasa. Vipi amkumbuke wakati wa shida? Na vipi ategemee mwujiza mkubwa kiasi hicho wakati enzi ya miujiza ilikwishapita? Hii ilikuwa enzi nyingine, enzi ya kutumia akili na nguvu.

Bado hakuona kama alikuwa na lolote ambalo angeweza kulifanya kujitoa katika gereza hilo kwani kwa kila hali alijiona kama aliyefikia mwisho wa msafara wake kimaisha. Kwa mara ya kwanza alilaani bahati yake.

Si kwa hofu wala uchungu aliyoipata katika gereza hilo ambalo halikutofautiana na kuzikwa hai. Hasa alijilaumu kwa kuikosa fursa ya kujionea kwa macho yake mwenyewe utawala wa makaburu na raia wake watakavyotaabika pindi mitego aliyoitega itakapofyatuka na silaha ambayo waliiandaa kuwateketeza watu wasio na hatia itakapowageukia. Joram, kama alivyo, hakuna ambacho kingemsisimua zaidi ya hilo. Aone macho ya mshangao yanavyowatoka wakubwa wa utawala na machozi yaliyochanganyika na kamasi yanavyowatiririka juu ya mashavu yao meupe. Aone majumba yao makubwa waliyoyajenga kwa jasho la wanyonge yakiteketea na kubomoka kama milima ya barafu. Na hatimaye, aone setilaiti yao ikianguka katikati ya mji wao baada ya mitambo inayoiweka angani kulipuliwa. Ndiyo.

Ni hayo tu aliyoyahitaji Joram. Ni hayo ambayo yalimfanya ayahatarishe maisha yake kwa muda wote huu na hata kumwaga damu isiyo na hatia, ili, afanikishe dhamira yake. Hayo, kuyashuhudia kwa macho yake kungempendeza zaidi ya pesa na kumsisimua zaidi ya starehe. Kwa nini amekuwa hana bahati hiyo? Alijiuliza.

Kisha alimkumbuka Nuru. Kiasi hofu ikamrudia alipojiuliza kama atafanikiwa kunusurika katika mapambano haya. Alikuwa amempa maelekezo yote muhimu na kusisitiza wakati gani aanze safari ya kutoroka zake endapo asingemwona.

Bila shaka hakuna hatakayehangaika kumtafuta msichana mmoja ambaye hana tofauti na wasichana wengine wakati mamia ya watu yakiungua, maelfu yakikimbia kwa fujo na mamilioni yakiwa yamepigwa na butwaa, wakati majumba na viwanda vitakuwa vikiteketea kwa moto mkali ambao mfano wake haujapata kutokea katika historia ya nchi hii na dunia kwa ujumla, wakati chombo kisichoonekana kwa macho ya nguvu ya kawaida kitakuwa kikielea angani; na baadaye kuanguka; nguvu yake inayokifanya kielee angani na za madini inayokifanya kutoonekana zikiwa zimekwisha.

Hapana, Joram hakuona kama Nuru angeshindwa kuitumia fursa hiyo. Bila shaka baada ya kumchanganya kwa hila alipokuwa akimfuata, atayafuata maelezo yote.

Joram asingejisamehe endapo lolote lingemtukia msichana yule na kumpotezea maisha. Licha ya kwamba uzuri wa Nuru haukustahili kuharibiwa kwa mkono wa Kaburu yeyote katili, ushujaa wake ulikuwa nguzo ambayo Joram aliitegemea sana. Yote aliyoyatenda, hekima na juhudi za Nuru zilimsaidia. Mungu msaidie arudi salama, alimwombea.

Utulivu aliokuwa nao pindi akiwaza hayo ulimfanya panya mmoja amrukie kifuani na kujaribu kumwuma. Joram alimkwepa na kuliachia teke dhaifu ambalo panya alilikwepa vilevile. Hata hivyo, panya huyo alimfanya ayatoe mawazo yake nje na kuyarudisha katika pango hilo la mauti. Harufu mbaya ya binadamu waliooza ikamrudia tena akilini na moyoni. Akajisikia kutapika lakini akajikaza kisabuni.

Kisha alikumbuka kumtupia jicho jingine yule Mrusi. Akashangaa kuona kundi dogo la panya likiwa juu ya uso wake, wakimla. Kwanza alishangaa, kisha akaelewa. Mrusi huyo alikuwa amekata roho! Kichefuchefu kikamrudia tena Joram. Alitamani afumbe macho asiendelee kuona ukatili wa panya hao kumla mtu ambaye dakika chache walikuwa wakizungumza naye, mtu ambaye bila shaka ni mwema sana. Vinginevyo angewezaje kujitolea aliwe akiwa hai? Joram aliuliza.

Ghafla mwujiza ulitokea.

Joram aliuona mlango ukitikisika na hatimaye kufunguka. Yeyote ambaye angeingia Joram alitegemea kumlazimisha ama amwue kwa risasi ama amtoe chumbani humo. Hivyo, alisubiri kwa hamu akitazama kwa makini tayari kwa lolote, heri au shari.

Bastola ilichungulia ikiwa katika mkono wa kike. Ilifuatwa na uso mzuri, wenye jasho na damu. Uso wa Nuru.

“Joram?” alipiga ukelele wa furaha mara alipomwona Joram kasimama kando akimtazama.

“Naweza kuyaamini macho yangu?” Joram alimwuliza akiwa bado amesimama palepale. “Wewe ni Nuru kweli au malaika?” aliongeza.

Hakupata muda wa kujibiwa. Tayari Nuru alikuwa kifuani mwake kamkumbatia kwa nguvu huku akilia kwa sauti ndogo. Wakati ikimpambazukia Joram kikamilifu kuwa haikuwa ndoto – huyu alikuwa Nuru halisi aliyekuja kumwokoa – alianza kuinua mikono yake ili naye amkumbatie. Lakini Nuru tayari alikuwa amejitoa mikononi mwake na kumvuta nje harakaharaka huku akisema, "Twende zetu. Wakati umewadia."

Joram alimfuata kikondoo.

Wakiwa nje baada ya kupigwa na hewa safi, fahamu zilimrudia Joram kikamilifu. Saa yake ilikuwa imevunjwa katika mapambano na jitu lile, aliitazama ya Nuru na kuelewa kwa nini aliambiwa wakati umewadia. Uhai ukamrudia mara moja rohoni, ingawa kimwili alikuwa bado dhaifu. "Niambie Nuru tafadhali. Niambie, mitego tuliyoitega haijafyatuka tu? Mji haujaungua?"

Badala ya kumjibu Nuru alimwambia, "Sikiliza."

Kwa mbali mjini kulikuwa na kelele nyingi za hofu. Vilio na milipuko ya kutisha ilisikika kutoka katika kila upande. Walisikiliza kwa nusu dakika, kisha Joram alitabasamu na kusema polepole, "Nadhani inatosha. Wanakufa wenye hatia na wasio na hatia. Sasa iliyobaki ni ile kazi moja ya mwisho. Kuulipua huu mtambo."

Alimshika Nuru mkono na kuanza kukiendea tena chumba cha mitambo. Nuru, akiwa na ramani halisi ya jengo hilo, alimshauri Joram wapitie wapi. Dakika mbili baadaye tayari walikuwa wamewasili katika chumba hicho.

Wahandisi watatu walikuwa chumbani humo, jasho likiwatoka kwa mshughuliko wa kutoelewa kinachotokea, hawakuweza kuwaona Joram na Nuru walioingia ghafla. Walipotanabahi walikuwa wakitazamana na bastola mbili. Wakaduwaa. Mshangao wao ulikoma pale risasi za mfululizo zilipopenya katika miili yao na kuwafanya waangukiane, damu zikiwavuja.

Joram aliikimbilia mitambo hiyo na kuanza kuikoroga kama alivyokusudia. Alipotosheka aliyatoa mabomu yake ya mkono na kuyatega sehemu mbalimbali za mtambo huo. Mara tu alipomaliza alimshika Nuru mkono na kutoka naye mbio.

Nje ya jengo, kwa mbali, waliona moto mkali uliokuwa ukipaa angani kwa namna ya kutisha. Kisha waliona kitu kingine cha kutisha. Kundi la askari wenye silaha likija mbio kiwandani huko.

Joram aliduwaa kidogo, akijiuliza wafanye nini. Kurudi ndani isingewezekana kwani jumba hilo pia lingelipuka wakati wowote. Na kukimbia ingewachukua hatua chache kabla ya kukamatwa na risasi za askari hao. Lakini Nuru, alijua la kufanya. Alimwongoza Joram katika upenyo alioutumia na Von hadi nje ya uwa ambako walipiga mbio wakitegemea kumkuta rubani akiwemo, ili wamlazimishe kwa bastola kuendeshwa kutoka nchini humo. Hakuwemo. Bila shaka "miujiza" iliyokuwa ikitokea ilimtia kiwewe hata akaondoka zake, au alikimbilia familia yake kwa matumaini ya kuiokoa. Hivyo, kiasi Nuru alikata tamaa. Lakini Joram alimrejesha matumaini alipomwamuru kupanda mara moja. Wakaingia.

Joram alikuwa na ujuzi wa nadharia juu ya kuendesha helikopta. Alilazimika kujikumbusha ujuzi huo kwa vitendo, jambo ambalo liliwagharimu zaidi ya dakika mbili. Wakati huo askari walikwishawaona na kuanza kuwafuata kwa nguvu zaidi.

Askari mmoja aliamua kutokimbia, badala yake aliilenga bunduki yake na kuiandaa kupiga.

Wakati huohuo jambo jingine la kushangaza lilitokea. Jumba hilo, ambalo lilikuwa hifadhi ya mitambo haramu lililipuka kwa mshindo mkubwa. Moto wa kutisha ulipanda juu na kusambaa kote.

Wakati askari hao walipokuwa wakitazama hilo, pia kwa mshangao, helikopta ilikuwa angani. Walipokumbuka kupiga risasi ilikuwa ikigeuzwa kuelekea Botwasana.

SURA YA KUMI NA MBILI

"… NA kama anafanya mauaji hayo kulipiza kisasi dhidi ya maafa ambayo utawala huu utayafanya katika nchi hii saa chache zijazo, bado si kitendo cha kujivunia sana, kwani haitasaidia kitu," Kombora alinong'ona. Alikuwa akisema peke yake, akiwa kimya katika ofisi yake.

Hayo yalimtoka mara baada ya kutazama televisheni na kusikia habari za kutatanisha kutoka BBC, bila shaka zikiwa zimekuja kutoka Afrika Kusini bila hiyari ya utawala huo, kwamba Joram alikuwa ametoweka kutoka katika jumba alilowekwa nchini humo. Kwamba mauaji ya ajabuajabu dhidi ya makaburu katika nchi hiyo yalitokea usiku huo. Na kwamba kulikuwa na mashaka kuwa mwuaji au wauaji hao hawakuwa wengine zaidi ya Joram na Kiango na yule msichana anayefuatana naye, Nuru.

Habari hizo, zikiwa zimewasili pindi vyombo vyote vya habari nzito zaidi ya hiyo zilipokelewa kama habari ndogo na kupuuzwa mara moja. Kwa wananchi wa Tanzania na nchi nyingine ambazo zilikuwa mashakani zikisubiri maafa makubwa kwa hofu na mashaka makubwa, walizipokea kwa shangwe na vigelegele kwa dakika mbili tatu, dakika zilizofuata ikawa imesahauliwa. Hofu ikachukua nafasi yake. Wakaendelea kusubiri, kusubiri kifo.

Waumini wa dini walikisubiri kifo katika makanisa na misikitini. Wakristo walichubuka magoti kwa sala ndefu zilizoambatana na vilio. Waislamu walivunjika migongo kwa kwenda rakaa huku wakimlilia Mola. Wasiomjua Mola walikisubiri kwa namana mbalimbali. Wako waliotulia kwa utulivu, wako waliopiga kelele na kuna wachache ambao waliamua kufa wakiwa wamelewa; hivyo, chochote walichokuwa nacho walikitumia kununulia pombe. Watoto ambao walipata hisia fulani kutokana na tofauti katika tabia za wazazi wao walitulia kimya, kwa mara ya kwanza maishani mwao wakionja ladha ya hofu. Hata wanyama wanaofugwa, kama kuku, mbwa, mbuzi na ng'ombe hawakuwa katika hali ya kawaida kwani ilikuwa siku yao ya kwanza ambayo hawakushuhudia binadamu akila mayai, kuchinja mbuzi wala kumkamua ng'ombe.

Jeshi liliwekwa katika hali ya hadhari, tayari kwa lolote ambalo lingeweza kutukia. Lakini kwa vile madhara hayo yalikuwa hayafahamiki yangetokea upande upi, na silaha ipi ingeweza kuyazuia, ilikuwa dhahiri kuwa jeshi hilo lisingeleta upinzani wowote. Ilikuwa kama waliowekwa tayari kusubiri kifo.

Rais na mawaziri wake, pamoja na viongozi wa ngazi za juu katika Chama walijiinamia juu ya viti vyao vya Ikulu. Mengi yalikuwa yamesemwa, mengi yalifanywa, lakini halikuwepo lolote lililoelekea kuwa kipingamizi kwa maafa yaliyokuwa yakiendelea dakika baada ya dakika. Wao pia ilikuwa kana kwamba waliamua kusubiri kifo kwa pamoja. Mara kwa mara walitazama saa zao kisha wakatazamana. Kisha kiongozi mmoja aliinuka baada ya kumnong'oneza jirani yake kuwa anakwenda haja. Hakurudi. Mwingine aliondoka taratibu kwa madai hayohayo. Yeye pia hakurudi. Yuko ambaye alikwenda moja kwa moja msikitini. Kuna aliyekwenda kanisani. Mwingine alikwenda nyumbani ambako aliungana na familia yake, kusubiri kifo.

Tahamaki Rais alijikuta kabaki na Waziri wake Mkuu. Walitazamana kwa muda, kisha mmoja aliyaepuka macho ya mwenziwe, wakizitazama saa zao. Zilisalia dakika tano tu. Wakatazamana tena. Wakazitazama tena saa zao. Dakika tatu… Dakika mbili… mmoja alimsika mwenziwe akiguna. Mwingine aliinuka akiwa kaloa jasho ambalo hakufahamu lilivyoishinda air conditioner ambayo ilikuwa ikifanya kazi kikamilifu. Kisha aliketi tena na kuyafumba macho yake.

Dakika moja…

Dakika yoyote kuanzia sasa! Kombora aliwaza akitoka dirishani alikokuwa akichungulia na kukirudia kiti chake. Alikuwa ameamua lolote ambalo lingetukia limkute katika ofisi yake. Hakuiona haja ya ya kutaabika wala kwenda kushuhudia maisha yanavyowatoka wanawe endapo nyumba yake ingetukia kuwa moja kati ya nyumba zisizo na bahati.

Mara mawazo ambayo hakutaka yamjie akilini yakamtoka. Mawazo ya upweke, unyonge na msiba mkubwa, mawazo ambayo yalikuwa yakimfunulia hali ambayo angekuwa nayo endapo ingetukia yeye kuwa mmoja kati ya wale watakaosalimika na familia yake nzima kuteketea. Angeishi vipi bila ya mama watoto wake, yule mwanamke mpole ambaye hajaacha kumwonea haya kwa kiwango kilekile walipokuwa wachumba hadi leo ambapo wamekuwa pamoja zaidi ya miaka thelathini. Angeishi vipi bila ya watoto wake wanne, mmoja akiwa mwanamume ambaye amehitimu Chuo Kikuu na kuajiriwa mwaka jana na wale wa kike ambao wote wameolewa na kumpatia wajukuu watano? Maisha yangekuwa vipi endapo yote hayo yangebadilika ghafla kwa ajili ya ukatili wa utawala dhalimu wa weupe wachache huko kusini?

Kisha alikumbuka saa yake. Dakika kumi zilikuwa zimepita! Hakuyaamini macho yake. Akayainua na kupiga hatua mbili tatu kuliendea dirisha. Akachungulia chini. Mitaa yote ya Dar es Salaam ilikuwa imetulia kabisa. Kelele ndogo zilisikika kwa mbali kutoka katika viwanda kadhaa ambavyo vilikuwa vikiendelea na kazi. Kombora aliirudia meza yake na kuketi. Masikio yake yalikuwa wazi yakisubiri kwa hofu kudaka mlio wowote wa mashaka ambao ungesikika. Macho pia yalikuwa wazi yakitazama angani kupitia dirishani.

Dakika ishirini!

"Wakati wo…" alitaka kutamka. Sauti yake ilikatizwa na ukelele wa ghafla ambao ulivuma ghafla katika anga. Bila ya kutegemea aliyafumba macho yake kwa nguvu na kutamani kuweka vidole masikioni ili asisikie zaidi. Kelele ziliendelea kwa mvumo mkubwa zaidi. Hisia zilimfanya Kombora

adhani kuwa zilikuwa kelele za kushangilia badala ya vilio na maombolezo kama alivyotarajia. Akasikiliza kwa makini zaidi. Naam. Watu walikuwa wakipiga vigelegele na kucheka kwa nguvu.

Watu wote!

Kama waliopatwa na wazimu!

Dakika moja baadaye Kombora alikuwa miongoni mwa watu wengine katika chumba cha habari, ghorofa ya mwisho. Askari hao walikuwa wakitokwa na machozi ya furaha huku wakisikiliza redio BBC ambayo ilikuwa ikiendelea na taarifa.

…hadi sasa inaaminia kuwa utawala wa Afrika Kusini haujafanikiwa kuuzima moto huu mkali ambao unateketeza majumba mbalimbali ya mjini johanesburg. Kadhalika, haijafahamika watu wangapi wamefariki na wangapi ni majeruhi japo inaaminika kuwa idadi hiyo itakuwa kubwa sana.

Kadhalika, mtambo wa siri ambao ulikuwa umejengwa na utawala huo ukiendesha setilaiti ya aina yake, isiyoonekana kwa macho, umelipuliwa na wahandisi wake wote kuteketea. Inasemekana kuwa baada ya mtambo huo kulipuka chombo hicho cha ajabu kimeanguka katikati ya mji wa Johanesburg na kusababisha madhara makubwa kwa maisha na mali za wananchi. Kadhalika, inaaminika kwamba afya za wananchi katika mji huo zitakuwa mashakani kutokana na nguvu ya nyuklia zilizoshirikishwa katika kukiunda chombo hicho. Kwa kila hali inaonyesha dhahiri kuwa Joram Kiango alishirikiana na mwenzi wake, yule msichana mzuri, Nuru, wameshiriki kwa njia moja au nyingine katika kufanya haya yaliyofanyika huko Afrika Kusini. Na endapo wasingekifanya walichokifanya dakika hii Afrika nzima ingekuwa katika msiba kwani kulikuwa na mipango ya mtambo huo kuzishambulia nchi zote za mstari wa mbele kwa pamoja…

Kombora hakustahimili. Machozi mengi yalimtoka na kuteleza juu ya mashavu yake, machozi ya furaha. Joram Kiango tena! Kwa mara nyingine ameliokoa taifa lake na Afrika nzima kuepuka kipigo cha kikatili ambacho kisingesahaulika. Joram, ambaye alimfikiria vibaya kwa kutoweka kwake na pesa nyingi za umma ambazo amezichezea duniani kote.

Ghafla, ikampambazukia Kombora. Joram hakuwa ameziiba zile pesa. Alizichukua kwa mtindo ule ili ionekane kama ameziiba ili azitumie kwa shughuli hii pamoja na kuaminika kama msaliti mara aingiapo nchini Afrika Kusini. Angeweza kuchukua hata zote! Kombora aliwaza. Angeweza kuzitumia apendavyo! Kijana huyu ni nani kama sio malaika aliyeletwa kuishi kama binadamu kwa manufaa ya binadamu wengine?

Kombora alirejea ofisini kwake. Mara tu alipoketi simu zilianza kumsumbua. Nyingi zilikuwa za waandishi wa habari zikiuliza hili na lile. Swali kubwa lilikuwa kutaka kujua kama kweli ni Joram Kiango aliyeifanya kazi hiyo ambayo majeshi yote ya nchi za Kiafrika yasingeweza kufanya. Zaidi walitaka kujua Joram yuko wapi.

Simu ambayo ilimsumbua Kombora kuliko zote ni ile iliyotoka Ikulu. Alizungumza na Rais mwenyewe. “Tunamtaka haraka kijana huyu ndugu Kombora. Kuna tuzo maalumu ya ushujaa ambayo inamsubiri…”

Kwa kadri Kombora alivyomfahamu Joram, hakuamini kama angepatikana kwa urahisi kiasi hicho, na hasa kujitokeza aipokee tuzo hiyo hadharani.

Siku mbili baadaye uhai ulilirudia jiji la Dar es Salaam kama kawaida. Pilikapilika za mitaani, viwandani na maofisini ziliendelea mtindo mmoja. Kila uso ulikuwa na furaha, tabasamu likiwa karibukaribu. Jina la Joram lilikuwa katika fikra za kila mmoja. Ambao hawakupata kumfahamu waliuliza huyu Joram ni nani?

“Humfahamu?” waliulizwa huku wakitazamwa kama wapumbavu.

Tawi la Benki ya City Drive lilikuwa na uhai vilevile. Wateja wengi walifurika kama kawaida wakiweka au kuchukua pesa, kuangalia hesabu zao na shughuli nyingine mbalimbali. Pilikapilika hizo ziliwafanya wasimtazame zaidi ya kawaida mzee huyu aliyevaa kanzu nyeupe na koti jeusi, ambaye alikuwa na nywele na ndevu nyingi nyeupe kwa wingi wa mvi. Mkononi alikuwa na mfuko mnene wa ngozi. Aliwapita wateja wote, akipokea shikamoo zake hadi chumbani kwa meneja ambaye alimpokea kwa heshima zote, kwani haikuwa mara kwa mara kutembelewa na watu wenye umri kama huo.

“Marahaba,” Babu huyo aliitikia. “Wewe ndiye meneja mwenyewe?”

“Ndiye.”

“Ndiyo wewe uliyeibiwa zile pesa za kigeni?”

“Ni mimi, mzee.”

“Basi huu hapa mzigo wako,” mzee huyo alisema akifungua mfuko huo na kutoa mabunda ya noti. Pesa za kigeni na shilingi chache za Tanzania. “Nimetumwa na kijana mmoja anayesema anaitwa Joram nikuletee. Amesema nikuombe radhi sana kwa kuzichukua. Alikusudia kuzitumia kwa safari yake lakini alipata pesa nyingine kutoka kwa jasusi moja ambalo alilikamata kule New Africa Hotel. Hivyo, alizitumia pesa zile badala ya hizi. Hata hivyo, amesema zimepungua kidogo atalipa…”

Meneja alikuwa hamsikilizi kwa makini. Mshangao ulikuwa umemshika. Alimtazama mzee huyo kwa muda kisha aliinama na kuanza kuzihesabu kwa mabunda. Katika hesabu ya harakaharaka zilipungua dola mia mbili. Akazirudisha katika mfuko wake na kuinua uso ili amshukuru mzee na kumwambia la kufanya. Hakumwona. Mzee alikuwa ameondoka bila ya kuaga alipokuwa kainamia meza.

Meneja huyo aliduwaa. Kisha alikumbuka la kufanya. Akauchukua mfuko huo wa pesa na kuondoka nao hadi katika gari lake. Akalitia moto hadi katika ofisi ya Kombora ambako alimwona moja kwa moja na kumsimulia mkasa mzima.

“My God,” Kombora alifoka. “Aliyezileta pesa hizo kwako hakuwa mzee. Alikuwa kijana sana, Joram Kiango mwenyewe!”

Meneja huyo alizidi kushangaa. “Mbona alikuwa mzee, Inspekta? Hata sauti yake ilionyesha…”

“Huyo ni Joram,” Kombora alimkatiza. “Ametumia moja ya mbinu zake ili asipatikane na kupewa heshima yake. Amejifanya mkongwe kama alivyofanya katika mkasa ule ulioitwa Salamu Toka Kuzimu.” Kombora alijiinamia kwa muda. “Tulimhitaji sana,” alisema kama aliyemsahau Meneja huyo wa Benki na badala yake kujizungumzia peke yake. “Anahitajika. Kumtafuta haitasaidia kitu. Kwa jinsi ninavyomfahamu hatajitokeza hivi karibuni hadi hapo mchango wake utakaposahauliaka, au litakapotokea suala jingine linalohitaji ushujaa.”

MWISHO

richard MWAMBE
12
MSAKO
wa
MWANAHARAMU

Msako wa mwanaharamu

1

Katika Pori fulani huko BAGAMOYO

PORI LILIONEKANA TUPU, hakukuwa na kipya zaidi ya miti ileile ya kila siku, kila mmoja ukiwa mahala pake. Kutokana na miti hiyo kuwa mbalimbali kiasi, iliwezekana kiumbe chochote kutembea katika pori hilo bila kupata shida. Mvumo wa upepo wa wastani kutoka baharini vilipiga mruzi kila mara, ukipanda na kushuka. Ndege wa porini kama dudumizi na tetere na wengine wengi walikuwa wakitoa sauti zao kuashiria Magharibi imekaribia huku wengine wakionekana angani wakirudi kwenye viota vyao wakiwa makundimakundi. Ndani ya pori hili lenye miti mikubwa na midogo na mimea yenye mfano wa kamba kamba ambazo zingetoa upinzani kwa binadamu kutembea kwa kuwa si mazingira yake kulikuwamo na watu watatu wakitafuta kitu, mwanaume mmoja na wanawake wawili.

“Una uhakika Chiba kuwa ni eneo hili?” Gina akauliza.

“Ndio ni eneo hili, maana kila nikiangalia kwenye rada yangu hapa, ishara inaishia hapa,” Chiba akajibu wakati huo Jasmine akiwa ameketi juu ya mzizi wa mti mkubwa. Gina akachukua ile rada kutoka katika mkono wa Chiba na kuitazama; juu katika kioo chake kulionekana mchoro kama wa ramani iliyopigwa picha kwa satellite na kitu kama doti nyekundu ilikuwa ikiwakawaka kwa kufifia.

“Mbona hii signal kama inafifia?”

“Betri inakwisha muda si mrefu, kumbuka tangu asubuhi inafanya kazi na sijaichaji ina wiki sasa,” Chiba akajibu na kufungua chupa yake ya maji. Jasho lilikuwa likimtiririka bila mafanikio ya kile anachokitafuta. Jasmine akiwa na begi lake mgongoni lenye vifaa vyake vya kazi alikuwa akisikiliza tu hakujua nini cha kuongea.

“Lakini Chiba, uelekeo ndio huu, tuko sahihi?” Jasmine aliuliza kwa taabu kidogo kutokana na uchovu uliomkabili. Watu hawa watatu walikuwa katika pori hilo katikati ya Bagamoyo na Mbegani kwa operesheni maalum ambayo ilikwishawachukua siku mbili katika eneo hilo na isioneshe mafanikio.

“Yaani kiukweli kabisa eneo hasa ni hili, tatizo ni wapi kwa maana signal yangu inaishia hapa na haiendelei kuonesha kama kuna eneo lingine, hatuna budi kupiga kambi hapa na kulala usiku huu,” Chiba aliwaeleza wenzake.

“Ha, nani alale hapa porini?” Jasmine aling’aka huku akiwa kapata nguvu ya kusimama.

“Wote lazima tulale hapa,” Chiba akasisitiza.

“Hakuna kulala hapa ni mpaka tupate jibu ndiyo itakuwa njia ya kutoka ndani ya pori hili,” Gina naye akasisitiza kwa kuongezea sentensi nyingine.

“Enhe! Hilo ndilo nilikuwa nalisubiri kwa muda mrefu sana, nilifikiri mmechoka kumbe bado mna nguvu,” Chiba aliwaeleza. Wakapeana moyo na kuendelea kutafuta humo porini kwenye vichaka na juu ya miti huku jua likichwea na kagiza kuanza kuingia taratibu.

- * *

Dakika chache baadae giza lilikuwa juu ya uso wa nchi wakati Gina, Jasmine na Chiba wakiwa wametawanyika kila mtu upande wake, wakiendelea kuwasiliana kwa walk talk zao ambazo ziliunganishwa kwa mtambo mdogo uliobebwa katika begi la Gina. Majira kama ya saa nne usiku hivi ndipo Gina alipoona kitu kilichomshtua.

“Shiiit!” akang’aka na kuwaita wenzake kwa kutumia chombo hicho. Dakika nne baadae wote waliungana wakimulika eneo hilo na tochi zilizofungwa vichwani na kuwekwa katika paji la uso wa kila mmoja wao, zote tatu zikamulika mahala pale.

“Hii ni simu ya Scoba!” Chiba akawaambia kisha akasimama wima na kuwa kama anayeangalia kitu katika vichaka hivyo huku akihema kwa nguvu.

“Vipi?” Gina akauliza.

“Kwa vyovyote hapa ni eneo la tukio”.

Jasmine akaiokota ile simu kwa mkono wenye gloves na kuiweka ndani ya mfuko wa plastiki kisha wakaanza kupita vichakani polepole huku wakiangalia kwa makini. Saa moja baadae Gina akakutana na kitu kingine, mkufu, wakauokota na kuuweka kwenye mfuko mwingine wa plastiki. Wakati msako huo ukiendelea Gina alikuwa akijawa na machozi lakini alijaribu kujibana asilie kwa sauti, moyo wake ulipoteza matumaini.

Saa sita usiku, ukimya ukiwa mkubwa katika mapori hayo, Jasmine alijikwaa vibaya na kuangukia kitu kama binadamu.

“Oh, Shiit!” akapiga kite huku akijiinua kutoka pale alipoanguka. Kurunzi yake ikamulika mwili wa binadamu uliolala kimya ukiwa na damu iliyoganda katika nguo yake iliyofanana na ovaroli la kijani cha mgomba.

“Scoba! Aiyaaaa!!!” Chiba alijikuta akichanganyikiwa alipouona mwili wa Scoba na kuutambua kwa ile beji yake iliyobanwa katika mkanda wake wa kiunoni. Alikuwa amelala kimya akiwa katapakaa nyasi kila mahali na parachute lake likiwa kando juu ya miti midogo midogo.

Daktari Jasmine harakaharaka, akashusha begi lake na kutoa kifaa cha kupima mapigo ya moyo ‘Stethoscope’ na kuipachika masikioni mwake huku tayari Chiba amekwishafungua jaketi la juu la Scoba na kumwacha kifua wazi. Jasmine baada ya kupachika masikioni mwake kile chombo, upande wa pili akauweka juu ya kifua cha Scoba upande wa kushoto na kutulia kimya huku akikihamisha hamisha lakini eneo lile lile.

Wote walibaki kimya wakiweka matumaini yao kwa mwanadada huyo daktari. Baada ya kusikiliza kwa makini mkubwa huku akifinya sura na kuiachia akachukua kitu kingine na kumfunga katia kiungo cha sehemu ya juu ya mkono na ile ya chini, kile chombo kilikuwa kama mpira Fulani wenye kitu kama saa upande mmoja, kisha akapachika kile kidubwasha cha kwanza pale upande wa juu wa kiwiko na kufanya kama anajaza upepo kwa kuminyaminya kitufe kingine na mara ule mpira ukajaa upepo na kubana sawia mkono wa Scoba, Jasmine akawa akiangalia kile kitu kama saa huku akiusoma ule mshale wake uliokuwa ukitikisikatikisika huku ukirudi chini. Aliporidhika akauachia ule upepo na kutoa ile mashine.

“Vipi?” Chiba akawahi kuuliza.

“Mzima, ila mapigo ya moyo yako chini sana,” Jasmine akajibu huku akichukua kitu kingine ndani ya begi lake, akatoa chupa ya maji ‘drip’ na kumpa Chiba aishike kwa juu kwa mtindo wa kuinging’iniza kisha akachukua sindano na kutoboa moja ya mishipa ya Scoba katika mkono wake na kupachika ule mpira, akachezea kidubwasha fulani na kisha akasimama akiwa kajishika kiuno. Akitazama huku na huko.

“Tumsogeze hapo kwenye hako kamti,” akasema na kisha Chiba akampa Gina ile chupa aendelee kuishika wakati yeye na Jasmine wakimsogeza Scoba mpaka walipopataka na kumuweka vizuri.

“Piga kambi mwanaume, tufungue zahanati,” Jasmine akamwambia Chiba ambaye tayari alitoa katika begi lake aina ya kitambaa kigumu kisichopitisha maji, akakibana kwa vyuma Fulani alivyovito humohumo na kisha akafyatua kitu kama mwamvuli mkubwa na kufunika mahali hapo, wote wakawa ndani ya kijumba kidogo kilichoweza kuwahifadhi dhidi ya wadudu sumbufu.

“Atapona?” Chiba aliuliza.

“Bila shaka,” akajibiwa na Jasmine.

“Sasa Amata atakuwa wapi? Au inawezekana akawa jirani hapa hapa?” Gina aliuliza kwa dukuduku.

“Nafikiri ni maeneo haya haya kama alifanikiwa kuruka kama mwenzake, maana Scoba inaonekana aliruka na hapa anaonekana ameumia sehemu ya nyuma ya shingo kwa kuwa ndiyo inayoonesha uvimbe,” Jasmine alieleza.

“Tuendelee kumtafuta maana bibi yake huko aliko kila dakika anapiga simu mpaka kero,” Chiba aliwaambia wenzake.

“Na anavyompenda, yaani leo halali, na bila kumzuia angekuja huku porini,” Gina akaongeza.

“Eeh jamani huko mbali, kwani sisi hatupendi?” Jasmine akauliza kwa shaka.

“Sijasema hivyo, wote anatupenda kama watoto wake, ni jambo zuri sana”. Wakiwa katika kuongea mara wakasikia michakacho ya watu au wanyama, hawakujua ni kitu gani, Chiba akanyanyuka na kukamata shotgun yake mkononi tayari kwa lolote na wakati huohuo Gina naye alikuwa tayari upande wa pili wa kibanda kile naye shotgun ikiwa mkononi inasubiri amri tu.

Ndani ya kile kibanda Jasmine naye alikuwa tayari na bastola mkononi.

Kutoka katika kile kichaka wakaibuka vijana wanne wakiwa na mbwa watatu, mikononi mwao walikuwa wameshikilia mavisu makubwa na mikono yao ikiwa imelowa damu.

“Amani jamani!” mmoja wa wale vijana akasema.

“Amani kwa wote,” Chiba akajibu wakati huo Gina alikwishasimama pembeni na bunduki yake ilikuwa ikwaelekea vijana hao.

“Vipi porini hapa na usiku huu? Hamuogopi? Hili pori sio zuri kabisa ndugu zangu, fanyeni hima muondoke,” mmoja wa wale vijana aliyekuwa kifua wazi aliwaeleza Chiba na wenzake.

“Tupo kazini kaka,” Chiba akajibu.

“Najua lakini hili eneo lina mambo ya ajabu, watu wengi hupotea humu na hawajulikani wanakokwenda, vitu vya ajabu hunekana na kukipambazuka huwa tunashuhudia mabaki ya miili ya binadamu,” mwingine akaeleza.

“Hapa ndio Mlingotini, wakiwakamata watawatoa sadaka,” Yule wa kwanza akaeleza.

“Nimewaelewa, nisikilizeni, mnamwona huyu?” Chiba akawafunulia kile kihema na wale jamaa wakamwona Scoba aliyekuwa amelala kimya na ile drip ya maji ikiendelea kushuka na kuingia mwilini mwake.Wale jamaa wakatazamana na kisha kurudisha macho kwa Chiba.

“Huyu ni nani?” wakauliza.

“Rafiki yangu, nimekuja kumtafuta huku tangu jana asubuhi haonekani,” Chiba akaeleza.

“Hamjaona mwingine kama huyu?” Gina akadakia swali.

“Hapana ila jana kuna kitu cha ajabu kimetokea huko baharini, tuliona kama ndege sijui ikiwaka moto anagani kisha ikaanguka baharini nafikiri, kwani tulipokuja kutazama hatukuona chochote,” wakeleza. Ikawa zamu ya Gina na Chiba kuangaliana.

“Eneo gani mlipoona huo moto au mlipuko?”

“Huku, usawa wa baharini, halafu ule moto ukaangukia huko huko,” wakajibu huku wakionesha uelekeo wa tukio lile kwa vidole vyao. Chiba akamtazama Gina kisha wote wakatikisa vichwa vyao kuashiria wameelewa jambo.

“Tunafanyaje?” Gina akauliza. Chiba akabaki kimya akifikiri jambo.

“Jamani twendeni kijijini hapa mahala si pazuri hata kidogo,” mmoja wa wale watu akatoa ombi na kisha msafara ukaanza kwa kumbeba Scoba huku na huku kwa kutumia miti iliyofanywa kama machela.

“Tukiwa kijijini tutawaonesha vizuri kule ambako tuliona tukio hilo,” mwingine akaeleza huku msafara ukiendelea katika mapori na usiku wa giza nene.

- * *

Siku iliyofuata…

MADAM S aliweka sawa pazia la dirisha ofisini kwake kisha kurudi kitini kukaa kama mwanzo huku kichwa chake kikiwa hakijatulia hata kidogo. Aliitazama saa yake ya ukutani na kurudisha macho yake mezani kwa mara nyingine kabla hajagutuliwa na mlio mkali wa kengele ya simu. Akainyakua kwa shauku na kuiweka sikioni, akashusha pumzi kwa nguvu huku mkono mmoja akiwa kajishika moyoni.

“Ndiyo, Chiba…” akaitikia namna hiyo huku uso wake ukijawa na shauku ya kujua kilichojiri.

“Operesheni imefanikiwa kwa asilimia hamsini, tumempata Scoba katika hali mbaya lakini sasa anaendelea vyema…”

“…Endelea…”

“…bado hatujampata Kamanda Amata na pia hatuna fununu yoyote juu yake,” Chiba akajibu na kutulia kimya.

“kwa hiyo nini kimewakuta hasa kwa maelezo ya Scoba?”

“Scoba bado hawezi kuongea, ila tunafanya utaratibu wa kumfikisha hospitalini kwa matibabu zaidi, ila kwa haraka haraka tumegundua kuwa ndege waliyokuwa wakitumia ama imepata hitilafu na kuanguka au imetunguliwa…”

“Mungu wangu! Mmeona mabaki yoyote ya ndege au imekuwaje?”

“Hapana Madam, hakuna mabaki ya ndege tuliyoyaona ila kwa uchunguzi tulioufanya inaonekana ndege hiyo imeangukia baharini…”

“Sawa, kwa hiyo tunahitajika kugeuka samaki sivyo?” Madam akauliza kwa lugha tata.

“Ndiyo Madam, inabidi iwe hivyo,” Chiba akajibu.

“Sawa, aaaaaaa… nipe dakika kadhaa kisha nitakupigia,”

“Copy!” Chiba akakata simu.

Madam S alitulia na kutuliza akili yake huku akiizungusha huku na kule, kisha akapiga ngumi mezani na kuinua simu yake akaiweka sikioni na kubofya tarakimu kadhaa. Upande wa pili ukaitikia.

“Hello!” sauti nzito ikalipenya sikio la mwanamama huyo.

“Msaada wa haraka tafadhali…”

“Wapi?” ile sauti ikauliza.

“Nyumba ya samaki,”

“Copy!” ile simu ikakatwa. Madam S akatoka ofisini na kuvaa koti lake la suti alilokuwa amelitundika kwenye kining’inizio kilichochongwa kwa fimbo ya mpingo, akatoka na kuubana mlango nyuma yake.

- * *

KURASINI…

Ndani ya meli mbovu iliyotelekezwa kwa miaka mingi katika eneo hilo watu wawili walikutana kwa mazungumzo ya dakika zisizozidi tano. Madam S alikuwa akitazamana na Inspekta Simbeye katika mkutano huo wa dharula.

“Ndiyo Madam!” Simbeye alianza namna hiyo mara tu baada ya kuingia katika meli hiyo chakavu iliyozama nusu na kubaki nje nusu ilihali ndani yake kuna mitambo ya kuchunguza usalama wa baharini kama rada ambazo huweza kuona kitu chochote kisicho samaki kikiwa zaidi ya maili mia moja chini ya maji. Vijana wanaoijua kazi hiyo wa Jeshi la Polisi na lile la Wananchi walikuwa wakifanya kazi humo usiku na mchana; hakuna aliyewaona wakiingia wala wakitoka, na hakuna aliyewahi kujua kama meli hilo linalozidi kuoza kwa nje kwa nini lilikuwa halihamishwi mahala hapo.

“Njiwa wangu amepigwa manati, kadondoka majini, alikuwa na mayai mawili, moja nimelipata lakini lingiine mpaka sasa sijalipata wala kuliona…” Madam alimwambia Simbeye.

“Oh, pole sana, nilipata taarifa ila sikujua mayai ya nani! Sasa unatakaje?” akauliza Simbeye.

“Nahitaji samaki, japo wawili tu wakaangalie kule chini?”

“Umesomeka Madam,” Simbeye akajibu kisha akaagana na Madam S na kuondoka zake kutoka ndani ya meli hilo.

Dakika mbili baadae, boti iendayo kasi inayojulikana kwa jina la ‘KINYAMKERA’ inayoweza kupita juu na chini ya maji ilichomoka ndani ya meli hiyo ikiwa na vijana watatu waliovalia tayari kwa kuendesha maisha majini. Safari kuelekea katika bahari ya Bagamoyo ilikuwa imewiva.

- * *

Simu ya Chiba akafurukuta mfukoni akainyanyua na kiuiweka sikioni.

“Tuko njiani!”

“Copy!” kisha ile simu ikakatwa. Chiba akawatazama wenzake.

“Madam yuko njiani!” akawaambia.

Wakaitikia kwa vichwa huku wakiwa tuli wakiangalia huku na kule kwa vifaa vyao maalum, pia wakitumia kompyuta kumtafuta Kamanda Amata kwa picha za satellite wakijaribu ku-ping tarakimu za utambulisho wake lakini haikuonekana hata dalili za mtu huyo kuonekana. Chiba alimtazama Jasmine aliyekuwa na Gina muda huo.

“Dokta, vipi mgonjwa?” akamuuliza.

“Yuko poa, naona sasa anaweza kuongea japo si kwa ufanisi sana,” Jasmine akajibu na kisha wote wakarudi kwenye ile hema yao ambayo sasa walikuwa wameijenga tena kijijini pembezoni kidogo. Nukta hiyo hiyo kifaa cha mawasiliano mgongoni mwa Gina kikakoroma, akaukwanyua mkonga wa chombo hicho na kuupachika sikioni.

“Unasomeka,” akitikia.

“Nipe uelekeo tafadhali…”

“ Nyuzi 278 Kaskazini kwa kipimo wima na 120.56 Mashariki kwa kipimo ulalo,” Gina akajaribu kujibu kwa kutumia vipimo vya ardhini kuielekeza helkopta hiyo ya polisi kufika eneo lile bila tabu. Haikuchukua muda lile helkopta liliwasili eneo hilo na kutafuta uwazi ili litue. Lilipopata nafasi ya kufanya hivyo likatua katika uwanja wa shule. Chiba, Gina na Jasmine sasa wakisaidiwa na vijana wa pale kijijini walimbeba Scoba hadi kwenye dege hilo na kumpakia kisha wakaondoka zao bila kuchelewa.

“Poleni kwa kazi vijana,” madam aliwapa pole.

“Asante lakini kazi haijaisha,” Gina akawa wa kwanza kujibu.

“Najua msijali, mnaweza kutazma chini?” akawauliza. Kisha wote wakajaribu kuangalia kwa kupiti kioo kikubwa kilicho chini ya dege hilo.

“Nini kile?” Gina akauliza.

“Vijana washafika wanajaribu kutazama kama Kamanda atakuwa kabaki huko au vipi, wamekuja na boti inayopita ndani ya maji,”

“Waoh!” Gina akashangaa

“Lakini sina uhakika kama Amata atakuwa huko kwenye maji, maana kama yuko huko basi amekwishakufa,” Jasmine akaeleza dukuduku lake.

“Usiseme hivo Jasmine,” Chiba alimkata kauli.

“Kamanda hawezi kufa kijinga hivyo!” Scoba alijibu kwa tabu kidogo, wote wakageuka kumtazama kutoka pale alipolala.

“Naona ana nguvu sasa, anaweza kuongea” Dkt. Jasmine alimweleza Madam S.

“Yeah, ila ngoja tufike mahala salama,” akaeleza Madam na wote wakahafiki.

- * *

Wale vijana watatu wakiwa chini ya maji waliweza kufika eneo ambalo ndege ile iliangukia, vilikuwa vipande vichache vilivyonasa katika miamba na mapango ya baharini, haikuwa ndege kamili au vile vipande havikukamilika. Waliendelea kuchunguza hapa na pale ndipo wakagundua kuwa ndege ile ilidunguliwa kutokana na alama kubwa nyuma kabisa upande wa chini, kipande hiko hakikuathiriwa na mlipuko ule.

Walifanya juu chini na kufanikiwa kupata kisanduku cheusi (black box) ambacho kazi yake ni kurekodi mwenendo mzima wa ndege ikiwa angani. Walipokipata na kukihifadhi kazi iliyobaki ilikuwa ni kutafuta binadamu wa pili kama ataonekana. Saa nzima ilipita hawakufanikiwa, walipekuwa kila kona ya mwamba na pango lakini hakukuwamo mtu yeyote wala mabaki yake. Walipokamilisha awamu hiyo ya zoezi wakaondoka zao na kurudi kwenye boti yao. Wakiwa ndani ya boti hiyo ya kisasa walitoa taarifa kwa Simbeye na wakatakiwa kurudi mara moja.

- * *

SHAMBA (Safe HOUSE)

Scoba aliketi kimya juu ya kiti cha vono, mbele yake kulikuwa na Madam S na Jasmine.

“Nina uhakika Kamanda hajafa, ama ameangukia mbali au yuko mahala, kwa sababu yeye alikuwa wa kwanza kutoka kwa parachute,” Scoba alieleza.

“Kwani nini hasa kimewatokea?” Madam alisaili.

“Tumedunguliwa, lakini hatujui hata kombola limetokea upande gani, sasa inakuwa ngumu kueleza, mi nilmestuka kitu kimeshafika mkiani, kilichofuatia sikuwa na jinsi zaidi yaku – evacuate. Mwamvuli wa Amata ulikuwa wa kwanza kufyatuka na kumtoa nje na mimi ulifuatia,” akaeleza. Madam S akabaki kimya kabisa akiwa hajui la kusema, baadae akarudisha uso kwa Gina.

“Mwanaharamu aliyefanya hivi lazima apatikane,” Madam S akasema kisha akamgeukia Scoba.

“Lakini kuna mlichogundua?”

“Kiukweli bado, pale tulikuwa tunakiona kijiji cha Kaole na vile vya pembezoni zaidi ni mapori mpaka Mbegani”.

“Sasa nani kawatungua?”

“Inawezekana kabisa ni wanajeshi wa kambi ya Mlingotini kwani tulipita pande hizo hatukuwa na ruhusa yoyote,” Scoba akaeleza na Madam S akatikisa kichwa. Kisha akatoka na kuwaacha Jasmine na Scoba yeye akatokomea katika chumba kingine.

Dakika kama tano baadae akarudi na taarifa nyingine kwa Scoba kuwa kambi ya jeshi ya Mlingotini hawajadungua ndege yoyote eneo hilo kwani wao hawawezi kudungua ndege bila idhini ya mkuu wa kikosi.

“Basi, kutakuwa na kambi ya siri eneo hilo, hili ndio tatizo la serikali kuuza viwanja kiholela, hata mnayemuuzia hamumjui wengine magaidi hawa,” Scoba akazungumza huku akisimama.

Madam S alimtazama Scoba kwa tuo na kisha akamtupia swali.

“Hatujamuona kamanda kabisa hata kwenye mitambo yetu haonekani, kama hajafa atakuwa wapi?”

“Kamanda hawezi kufa, tuendelee kumtafuta,” Scoba akajibu.

Rudi siku tatu nyuma… ‘siku ya tukio’

SHAMBA

KAMA NI SURA YA HASIRA basi ilionekana wazi kwa Madam S alipokutana na vijana wake ndani ya nyumba yao ya siri huko Gezaulole. Kikao hiki kiliitishwa haraka sana baada ya tukio lisilotegemewa kutokea eneo la Darajani katika Barabara ya Nyerere, saa sita mchana kweupe.

Kamanda Amata alikuwa kajiinamia kama awazae jambo wakati wengine wakijaribu kuchanganya akili kwa hili na lile juu ya hilo.

“Lakini mi nilisema kuwa mtu yule asilindwe na askari wa kawaida kwani ana mbinu nyingi za kujiokoa,” Chiba akaeleza.

“Yeah ni kweli lakini kumbuka pia sisi si kazi yaetu kulinda watuhumiwa,” Madam akamjibu. Ukimya mwingine ukatawala.

“OK!” sauti ya Madam S ikawazindua vijana wale watano waliokuwa katika lindi la mawazo ya sintofahamu.

“Lazima tumsake na tumtie mkononi, mtu mmoja hawezi kutunyanyasa sisi tena wanataaluma wa kazi hii. Tutamsaka na kumleta tena hapa, Chiba jaribu kufuatilia wapi anaweza kuwa ameelekea ili tuone la kufanya,” Madam akatoa amri na Chiba akaondoka eneo hilo kuelekea kati kachumba chake maalum.

“Usione niko kimya yaani huyu bwana ananiumiza kichwa, nikikumbuka jinsi nilivyompata kwa shida, we acha tu!” Kamanda Amata alimwambia Madam S huku akitoka eneo hilo.

“Najua lakini naamini tutampata tena,”

“Ndiyo tutampata lakini kwa jinsi ile ina maana huyu jamaa bado ana nguvu sana na hatujui kajipanga namna gani,”

“Unalosema ni kweli, kwani hata mbinu iliyotumika kutekwa kwake mbele ya mikono ya polisi haijawahi kutokea na wala hatukutegemea, imekuwa kama filamu ya Hollywood, aisee!” Madam alimweleza Amata huku wote wakitembea kwenye ujia mrefu ndani ya jengo hilo.

“Yatupasa tuwe makini sana, hatujui mara hii ataibukia wapi. Na tukimpata safari hii atajuta kuzaliwa dume,” Amata akaongea kwa uchungu.

Madam S akasimama na kumtazama kijana huyo aliyekuwa amekwishasonga mbele kwa hastua kama tatu hivi, naye akasimama baada ya kumwona bosi wake kafanya hivyo, wakatazamana.

“Utamfanya nini?” Madam akauliza.

“Nitamtoa korodani!”

“Na we’ unaweza!”

Kisha wakaendelea na safari yao katika jingo hilo.

- * *

CHIBA alikuwa ametingwa kwenye mitambo yake, kompyuta kadhaa zilimzunguka na mashine nyingine mbalimbali. Ndani ya chumba hicho aliweza kuikusanya dunia yote na kuiweka ndani ya kioo kimoja cha kompyuta. Msako wake aliuanzia palepale eneo la tukio, Darajani, akijaribu kufuatilia uelekeo wa chopa iliyombeba mtuhumiwa wao mara tu baada ya kukombolewa kutoka katika mikono ya polisi, ndani ya gari ya chuma alipofungwa minyororo miguuni na mikononi na kuacha askari sita wakiwa hawana uhai.

Chombo chake kilimuonesha uelekeo wa Kaskazini Mashariki, yaani maeneo ya Mbweni mpaka Bagamoyo, lakini alishangaa kila akifika eneo fulani la Mbegeni ule mtambo ulikiuwa unashindwa kueleza uelekeo sahihi wa kile chombo, akajaribu na kujaribu lakini alishindwa. Akashusha pumzi ndefu na kujiegemeza kitini kabla ya kunyanyua simu na kumjulisha Madam S juu ya hilo. Ilichukua dakika moja tu mwanamama huyo kuwasili ndani ya chumba hicho maalum cha mawasiliano. Baada ya kuongea mawili matatu na Chiba walifikia azimio la kumsaka mtu huyo iwe angani au ardhini. Kikao kikaitishwa tena na wote wakakutana.

Meza hii ndiyo daima hufanyiwa maamuzi mazito na mepesi, ya kukata au kuua, kutesa au kutekenya, vyote huamuliwa hapa. Ukiitazama utaiona tu, kwanza inaviti sita kwa idadi yao, kila mtu hukaa kiti hicho hicho kila wakati, ni sawa na kusema ndicho ‘afisi’ yake kwa hapo, meza ya duara.

Mara tu baada ya kukutana, kikao kikaanza kwa kumsikiliza Chiba akieleza kile alichokigundua katika mtafuto wake wa kimtandao.

“Haya kama alivyotueleza Chiba, sasa hapa tunakwenda kimakundi, kundi moja na la kwanza litakuwa angani hili ni Scoba na Amata, kundi la pili Gina na Chiba mtakuwa ardhini mkifuatilia kwa chini na la tatu ni mimi (Madam S) na Jasmine tutakuwa katika uokoaji. Hivyo basi sasa tuingie kazini”. Madam S alipanga kikosi chake, hakuna aliyekuwa na mashaka katika hilo kwani walijua kuwa mwanamama huyo huwa hakosei kwenye kupanga. Kila kitu kikawekwa sawa, kila mmoja na mwenzake wakajipanga ni wapi pa kuanzia, kazi ikaanza.

JESHI LA WANAMAJI KIGAMBONI

KAMANDA AMATA NA CHIBA waliwasili katika kambi hiyo majira ya saa tisa alasiri wakiwa tayari kwa shughuli hiyo ngumu. Wakati huohuo Chiba na Gina walikuwa tayari katika gari wakielekea Tegeta mpaka Mbweni kuendeleza msako.

Baada ya Kamanda na Chiba kusaini kabrasha fulani fulani pale jeshini tayari kuchukua ndege ndogo inayoweza kutua na kuruka majini, walikabidhiwa kofia ngumu za kuvaa na kupewa maelekezo machache na rubani wa jeshi kisha wakaingia katika ndege hiyo ndogo yenye uwezo wa kubeba watu watatu tu. WAkaketi na kufunga mikanda, Scoba kama kawaida yake ndiye alikuwa rubani mkuu wa kuirusha ndege hiyo.

“Hivi wewe kuna kitu hujawahi kuendesha?” Amata akauliza kwa utani.

“Kipo,”

“Kipi?”

“Ungo”.

Wote wakaangua kicheko na wakati huo tayari injini ilikuwa ikizunguka na Scoba akiitoa ndege hiyo mahala pake kuelekea katikati ya bahari tayari kuruka na kuanza safari ya msako.

Dakika tano baadae walianza kuliona jiji la Dar es salaam kutoka juu jinsi linavyopendeza. Muda wote walikuwa wakiwasiliana na Chiba na Gina waliokuwa wakisafiri kwa gari kuelekea upande huo. Walipofika eneo ambalo walihisi ndipo hasa wanapopataka, juu kabisa ya anga la Bagamoyo, pande za Mbegani kuja Kaole walikuwa wakitumia darubini maalumu yenye nguvu kutazama chini kama wanaweza kuona chochote chenye maana kwao huku picha zile moja kwa moja zikirushwa mpaka kwenye kompyuta ya Chiba ambayo alikuwa nayo ndani ya gari hiyo iliyokuwa ikiendeshwa kwa kasi na mwanadada Gina.

“Mpaka sasa hatuoni chochote zaidi ya misitu na nyumba za wenyeji,” Kamanda alimwambia Chiba.

“Scoba Scoba, shusha ndege chini zaidi angalau futi elfu mbili tuone kama twaweza kugundua chochote,” Chiba akatoa maagizo na Scoba akateremsha ndege hiyo kama alivyoagizwa, wakaanza tena kutazama kwa kile chombo huku ndege hiyo ikizunguka huku na huko bila kutua chini. Baada ya mzunguko wa muda mrefu, wakaingia na upande wa bahari na kwenda mbali karibu na pwani ya Zanzibar, kisha wakarudi tena upande wa Pumbuji.

“Hey! Amata, hebu cheki pale!” Scoba akamshtua Amata, naye akatazama kwa ile darubini.

“Shiit, kile ni kisiwa sivyo?” Amata akauliza.

“Hiki kisiwa nakijua, kulikuwa na kitu pale cheupe kinang’aa kama paa jipya lakini kimepotea na kuchukua rangi ya uoto uliopo,” Scoba aliongeza.

Kamanda Amata akamwonesha ishara ya kidole ya kwamba aizungushe ndege hiyo na kukizunguka kile kisiwa ikiwa ni pamoja na kuteremka chini zaidi.

“Scoba unaanza kuzeeka, lile ni pori tu!” Amata akamwambia Scoba huku akigeuza ile darubini upande mwingine wa Kaole. Bado ndege ilikuwa haijamaliza kuzunguka kile kisiwa, Scoba aliendelea kutazama kwa makini sana.

“Kwa hiyo tunafanyaje?” Scoba akauliza.

“Tucheki na upande ule kuleeeee,”

“Ok!” Scoba akajibu na kuiweka sawa ile ndege kisha akainyanyua juu ili kuendelea mbele.

- * *

Scoba hakuwa amekosea kwa kile aichokiona, na Amata vilevile hakuwa amekosea kwa kile alichokisema, hivyo basi kila mmoja alikuwa sawa kwa wakati wake. Katika eneo hilo kulikuwa na kisiwa kikubwa kilichozungikwa na mikoko na uoto mwingi wa baharini.

Hiyo kama haitoshi, ndani ya kisiwa hiki kulijengwa jingo kubwa lenye vitu vingi sana, na ujenzi wa jingo hili ulikuwa ukifanyika kwa siri sana, hakuna mwananchi aliyejua wala kiongozi wa serikali. Walichokiona wao ni nyumba moja tu ya kawaida sana iliyojengwa juu ya kisiwa hicho, lakini kumbe chini yake kulikuwa na ngome kubwa iliyojengwa kwa ustadi sana. Na kati ya vyumba vingi vilivyopo, kimojawapo kilikuwa na mitambo ya rada, inayoweza kuona chombo chochote kinachopita angani usawa wa kisiwa hicho au kinachokuja majini usawa wa kisiwa hicho. Ndani ya chumba hicho kulikuwa na wataalam wanaofanya kazi kwa siri na zamu kila siku kwa saa ishirini na nne.

Siku hii, watu watatu walikuwa ndani ya chumba hicho wamejifungia, walikuwa wametingwa kusoma kitu kikubwa kama saa lakini hiki hakikuwa na tarakimu yoyote isipokuwa kilikuwa na mistari ya duara kadhaa na mstari mmoja wa rangi ulikuwa unazunguka huku na kule.

Mlio wa kitu kama bip ukaanza kusikika ndani ya chumba kile. Mlio huo ulianza kusikika kwa mbali sana lakini baadae ukawa na sauti kubwa.

“Vipi?” mmoja akauliza.

“Kuna kitu kama ndege hapa naiona inaelekea upande huu wetu,” akajibiwa. Yule bwana akasogea karibu na kile chombo na kuangalia.

“Mmmhh! Ni ndege hii hebu washa ile camera kubwa tuone,”

Nukta hiyo hiyo, kitu kama antenna kikaibuka kutoka katikati ya mapori na kusimama wima kati ya miti. Ndani ya chumba hicho waliweza kuona picha halisi ya ndege ile.

“Nani hawa?” mwingine akauliza huku akiwa katumbua macho.

“Sijui, hebu toa taarifa kwa mkuu wa kikosi,”

Yule kijana akatoka na kuelekea pembeni kisha akachukua simu na kukoroga tarakimu fulani.

“Mkuu, kuna ndege tunaiona kwenye rada inaelekea upande huu, hatua gani tuchukue?” Yule kijana akaongea huku akitweta.

“Subiri nakuja hukohuko,” akajibiwa.

Sekunde kumi hazikupita mlango ukafunguliwa na mtu mmoja mwenye tambo kubwa la kimazoezi akaingia; moja kwa moja akaiendea ile meza na kutazama ile picha iliyopigwa kwa kamera ya siri.

“Shiit! Hii ni ndege ya jeshi, fanyeni hivi, ikifika mbali jaribuni kuona nini kinaendelea ndani kisha mitumie hizo picha afisini kwangu,”akawaambia. Wale jamaa wakaendelea kuisoma kila inavyozunguka, na baada ya kukaa kwenye kona nzuri waliweza kuipiga picha na kuona nini kipo ndani ya ndege hiyo. Wakapeleka taarifa kuwa kuna watu wawili wanaoonekana kupiga picha fulani. Kutoka kwa Yule jamaa akawaamuru wajaribu kunasa mawasiliano yao ili kusikia nini kinazungumzwa.

Zoezi hilo halikuchukua hata dakika mbili, kutoka katika kile chumba, wakaweza kunasa mawasiliano kati ya Amata na Chiba. Baada ya kujua kuwa ni wao wanaowindwa amri tu ikatolewa na mkuu wa kikosi.

“Ilipue,” akawaamuru.

“Haiwezi kutuletea matatizo tukiilipua?” kijana mmoja akauliza.

“Nimesema lipua tena haraka!”

Hakukuwa na lingine, missile equipment ikafunguliwa na kujitokeza juu kidogo ya ardhi lakini ndani ya msitu huo wa mikoko kisha ikafyatuliwa na moja kwa moja ikafuata ndege ile iliyokuwa na Amata na Scoba ndani. Mlipuko haukuwa wa kutisha sana lakini ndege ile ilikatikavipande na kuangukia baharini.

- * *

Ndani ya ile ndege, Scoba alisikia kengele iliyopiga kwa nguvu, akatazama kwenye dashboard yake na kuona ishara kuwa wapo kwenye shabaha

“Amataaaaaa!” akapiga kelele baada ya kuona kwenye kuwa wamedunguliwa. Kitendo bila kuchelewa, Kamanda Amata akabonyeza kidubwasha kilicho chini ya kiti chake na vyuma vilivyoshika kiti hicho vikaachiana wakati huo tayari Scoba keshabinya kinobu kilichoandikwa neno ‘Evacuate’. Ile ndege ikafunguka juu na kiti cha Amata kikatolewa nje na kuiacha ile ndege.

Hakuna alichokishuhudia zaidi ya mlipuko mkubwa angani na ile ndege kupasuka vipandevipande.

“Scoobbbaaaaa!!!!!” Kamanda Amata alipiga kelele akiwa hewani lakini hakumwona Scoba. Vyuma vilivyoruka kimojawapo kikampiga kichwani Amata akapoteza fahamu akiwa anaelea angani huku parachute lililokuwa tayari limefunguka likimbeba na kumteremsha taratibu.

Scoba, mara tu baada ya Amata kutupwa nje alifyatua kiti chake lakini alichelewa nukta kadhaa, wakati kile kiti kikimrusha nje lile kombora likawa tayari limeshaipiga ile ndege eneo la kati kati, akajikuta ananasa kwenye vyuma vya ndege hiyo. Akajitahidi na kujifyatua lakini parachute lake liliharibika vibaya, akajitahidi kuliongoza ili adondokee nchi kavu akafanikiwa. Kutokana na kuchanika kwa parachute hilo alifika chini kama mzigo na kujipiga vibaya akatulia kimya kwa sekunde kadhaa, macho yake yakiwa bado yanatazama anga la dhahabu jioni hiyo na taratibu akaanza kuhisi giza huku sauti za ndege zikipote kwa mbali, akazirai.

Amata akiwa hana fahamu alidondokea baharini na kupigwa pigwa na mawimbi mpaka kando kidogo. Jua la jioni lilikuwa tayari linang’aza sehemu hiyo na misafara ya ndege nayo ilikuwa ikirudi viotani.

- *

Huku chini kwenye gari, kioo cha kompyuta ya Chiba kikawa cheusi ghafla, hakuna chochote kilichoonekana.

“Vipi tena?” akajiuliza.

“Vipi kwani?” Gina akauliza.

“Nahisi hatari, maana sauti ya mwisho nilioisikia ni ya Scoba akimwita Amata, hebu weka gari pembeni kwanza,” Chiba akamwambia Gina. Naye akafanya hivyo, ile gari ikasimama kando mwa barabara katika eneo la Zinga. Chiba akajaribu kucheza na kompyuta yake lakini hakuna alichoweza kuona zaidi ya ujumbe wa ‘Error 706’ uliokuwa ukijitokeza mara kwa mara, akaifunga ile kompyuta na kumgeukia Gina.

“Vipi?” Gina akauliza, lakini kutoka katika macho ya Chiba aliweza kuuona mshangao uliokosa mwelekeo.

“Huko hali si shwari, siwapati Amata na Scoba,” Chiba akajibu huku akijiweka sawa kitini na kuinua simu ndogo iliyofungwa ndani ya gari hiyo.

“Unataka kuniambia nini?” Gina akauliza huku mikono yake iliyokuwa imeshika usukani sasa ilianza kutetemeka na alionekana kubana meno yake ama akizuia kilio au akinyima uchungu nafasi ya kujiweka hadharani.

“Mawili, ama ndege ina hitilafu au wamedondoka,” Chiba akajibu na wakati huo tayari simu iko sikioni akimwitikia Madam S.

“Nakusoma Chiba!” Madam S akaitikia

“Kuna hali isiyoeleweka, Simpati ndege angani, mawasiliano yamekatika,” Chiba akamwambia.

“Unataka kusema nini?”

“Sauti ya mwisho niliyoisikia inaashiria hatari, Scoba alimwita Amata kwa nguvu kisha nikasikia kishindo na ukimya kwa asilimia 101,” akaeleza.

Kupitia simu hiyo ya upepo, Chiba aliweza kumsikia Madam S akishusha pumzi kwanguvu.

“So?” Madam S akarudi hewani mara hii sauti yake haikuwa kama kwanza, ilikuwa imejaa kitetemeshi.

“Probably, men down!!” Chiba akamaliza hhuku macho yake yakitona machozi.

Akatulia kumsikiliza bosi wake akimpa maelekezo kadhaa kisha huku akiitikia tu kwa kuguna pasi na kusema neno lolote.

“Clear and out!” akaitikia na kukata simu kisha akaipachka mahala pake na kumtazama Gina.

“Madam anasemaje?”

“Anasema tuwahi na Dkt. Jasmine anakuja na vitendea kazi vya kutosha kwa msaada wa haraka. Gina akaingiza gari barabarani na kutimua mbio kama kichaa, akageuza na kurudi nyuma kidogo kisha akaikamata Mapinga aliiacha barabara ya kwenda Dar es salaam na kupinda kushoto kuchukua nyingine kuelekea Mbegani.

“Shiiit!” Gina aliendelea kugugumia huku akikanyaga mafuta kama kichaa, mshale wa mwendo kasi ulikuwa katika namba 110 na vumbi lililoachwa nyuma halikuwa la kawaida. Baada ya mwendo wa takribani dakika arobaini na tano, Gina alisimamisha gari karibu na kijiji fulani, Chiba akajitokeza juu ya gari na darubini yake na kuangalia kwa darubini katika uwanda wa nyasi fupifupi. Darubini hii ilikuwa ni ya kisasa sana, yenye madini yanayiwezesha kuona hata katikati ya giza, na kupambanua kila inachokiona na kukupa maelekezo kuwa kitu hicho kipo kilomita ngapi. Baada ya dakika kadhaa akaingia ndani, na kuchukua kifaa kingine kama simu lakini kilikuwa kikubwa zaidi, akakiwasha na kubonya vitu fulani fulani kisha akaanza kuangalia, rangi na michoro mbalimbali inayotokea katika kile kioo, baada ya sekunde kadhaa kukawa na kijitaa kinachowaka eneo Fulani la kioo cha kile kidubwasha.

2

“Gina, twende mbele zaidi,” akamwambia Gina, na ile gari ikaondolewa mahala pale mpaka kwenye njia panda ya kuwenda kwenye magofu ya Kaole na ile ya kwenda Bagamoyo mjini.

“Subiri!” Chiba alimwambia, kisha akamwambia aelekee kulia. Gina moja kwa moja akachukua barabara hiyo na kupita magofu ya Kaole akaendelea mbele mpaka alikokuta njia inaishia na kukutana na mkondo wa maji uliokatisha eneo hilo.

“Tunafanyaje?” akauliza.

“Tuache gari hapa, twende kwa miguu tufuate hii signal inawezekana ni Amata au Scoba, ila mmoja kati yao signal yake imepotea kabisa sijui tutampataje,” Chiba alijibu huku akiwa tayari kakanyaga ardhi ya eneo hilo akichukua hiki na kile ndani ya begi lake kabla hajaliweka mgongoni. Wakiwa bado wanaendele kutafuta hapa na pale katika vichaka hivyo, saa moja baadaye ndipo Jasmine alipoungana nao na kuweka nguvu pamoja jioni hiyo kufanya mtafuto huo mgumu.

Rejea sasa…

KURASINI

MARA BAADA YA KUMALIZA SHUGHULI za Shamba, Madam S alirudi katika afisi ile ya siri iliyotengenezwa ndani ya meli mbovu katika bahari ya Kurasini, wapiga mbizi waliotumwa kuutafuta mwili wa Amata walirejea na boti yao 'KINYAMKERA'. Inspekta Simbeye na Madam S walikuwa wakisubiri kwa hamu huku wakiwa hawana mazungumzo mengi. Taarifa hiyo haikutangazwa na mtu yoyote wala hakuna chombo cha habari kilichothubutu kuvunja amri hiyo ya usalama wa taifa.

"Hatujapata mwili wa mtu yeyote kule majini!" kijana mmoja kati ya wale watatu waliokwenda kuchunguza yale mabaki ya ndege, ikiwezekana na kuupata mwili wa Amata walifikisha taarifa hiyo kwa Inspekta Simbeye na Madam S waliyekuwa ndani ya lile meli bovu.

"Isipokuwa tumepata hiki kiboksi cha kurekodi mwenendo wa ndege, taarifa ambazo tumezipata kutoka humu ni kuwa ndege hii ilipoteza mawasiliano angani kwa ghafla kwa kitu kama mlipuko. Baada ya uchunguzi kule chini ya maji, tumegundua kuwa ile ndege imedunguliwa, na kombora lililotumika ni RPG Rocket kwa kuwa tumefanikiwa kuona mabaki yake," kijana mwingine akaelelzea kwa ufasha zaidi na kuwasilisha vyuma vya kombora hilo.

"RPG Rocket?" Madam S akadakia kwa kuuliza."Unataka kunambia kuwa ndani ya nchi hii kuna watu wanamiliki silaha nzito za kivita kama jeshi, hii ni hatari, ni hatari sana," Madam S alizungumza huku akionekana wazi kukosa utulivu wa mwili na roho kwa swala hilo.

Oh! Shit, atakuwa wapi Amata? Madam akajiuliza pasi na kupata jibu sahihi ndani mwake.

"Sawa naomba hiyo taarifa yote katika nakala laini tafadhali," Madam S aliomba huku akilielekea dirisha dogo na kutazama nje kwa nukta kadhaa kabla ya kugutuliwa na sauti ya kijana yule akiwa tayari na taarifa ile mkononi mwake ikiwa ndani ya CD. Akaipokea na kuondoka katika ofisi ile ya ajabu.

Baada ya kujiridhisha na kila kitu, akaagana na Simbeye na kutolewa katika ile afisi mpaka eneo maalumu la nchi kavu upande wa Kigamboni, kutoka hapo akatembea hatua chache na kuchukua gari yake aliyoiacha kwenye afisi moja ya chama na kuelekea tena Shamba.

- * *

Madam s aliwasili katika jumba hilo kwa njia anayoijua mwenyewe, shughuli za ndani humo zilikuwa zikiendelea kama kawaida. Ni Chiba tu aliyekuwa anajua ujio huo kwani kila anayeingia ndani ya jumba hili huweza kumwona kupitia kamera ndogo za usalama ambazo si rahisi kugundulika na mtu wa kawaida. Ndani ya sebule kubwa alipomwacha Scoba alimkuta palepale akifunua funua gazeti na kusoma hapa na pale.

"Kweli, tulifanya kosa kuwakabidhi wale askari lindo la mtu hatari kama yule, lakini tungefanyaje wakati hao ndiyo wenye jukumu la kulinda wahalifu?" Madam S akauliza huku akitembea na kujitupia kochini. Sauti hiyo ilimgutua Scoba, kwa sababu hakusikia hata kelele ya wayo wa mwanamama huyo.

"Yeah, ni sahihi sana kwa hilo lakini yule mtu uhatari wake ni wa kimataifa zaidi, tazama jinsi walivyo muokoa hao majahiri wake, ile ni mbinu ya kivita Madam," Scoba aliongea.

"Kiukweli walidhamiria, maana hata kumkamata kwake yule bwana hakukuwa rahisi, tulipata tabu sana pale Bombay, lakini tulimleta. Halafu kumuona anatutoka mikononi kirahisi namna ile, lo, nina uhakika Amata huko aliko si ajabu bado anamsaka, na akimpata hawezi kumleta na roho yake," Scoba akazungumza.

Ukimya ukatawala kati ya hao watu wawili, kila mmoja akiwaza lake. Scoba akarudisha mawazo yake kwenye mtanange wa Bombay.

Miezi mitatu nyuma

SAFARI YA BOMBAY – INDIA

“Una uhakika utamleta?” Madam S akamwuliza Amata.

“Tumeanza kudharauliana siyo?” Amata akajibu swali kwa swali.

“Siyo kudharauliana, maana wewe nakujua, mi nikikwambia umlete hai we utaleta viatu vyake tu nikiwa na maana utakuwa ushanyofoa roho yake,”

“Inategemeana, daima nikiona mtu mbishi kufika mzima lazima nimgawanye mara mbili, yaani nimtenganishe mwili na roho na hapo ndipo nambeba kirahisi,” wote wakacheka kwa maneno hayo.

“Sawa, serikali iko tayari kukupa msaada wowote utakaouhitaji, maana waziri mkuu kaagiza mtu huyo aletwe hapa,” Madam akamwambia Amata kwa msisitizo.

“Tawile, zimefika na ataletwa,” kisha akapiga saluti na kugeuka kulitazama jengo la Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere.

“Kamanda Amata, Pancho Panchilio ana mtandao mkubwa sana ndani na nje ya nchi, uwe makini, timu ya utafiti ipo huko siku nne zilizopita na wameshafanya kazi kubwa sana wanakusubiri wewe ukamalizie,” Madam S aliendelea kutoa rai yake kwa kijana huyo shupavu.

“See you soon!” (Tutaonana punde tu) akamuaga Madam na kuondoka zake.

- * *

“Wapi tena? Maana mwenzetu huishiwi safari weye,” Mhudumu wa ukaguzi wa Swissport akamtania kwa kuwa alikuwa akimfahamu hasa kwa kumwona mara nyingi uwanjani hapo.

“Umeanza Lulu, naenda Uhindini mara moja,”

“Uje na zawadi tu,”

“Usijali, kacholi zenye pilipili utapata,” Kamanda akajibu na kuishia kwenye chumba cha kupumzikia wasafiri. Baada ya nusu saa kupita aliondoka na ndege ya Shirika la Air India.

UWANJA WA NDEGE WA KIMATAIFA WA

CHHATRAPATI SHIVAJI – BOMBAY

KAMANDA AMATA aliingia katika jiji hilo usiku wa manane, moja kwa moja alitoka nje ya jengo hilo. Kando tu ya maegesho ya uwanja huo, aliweka begi lake chini, akaingiza mkono mfukoni na kutoa sigara akaibana kwa midomo yake miwili huku kichungi cha sigara hiyo kikiwa ndani ya kinywa chake. Mkono mwingine ukatoa kiberiti cha gesi na kukiwasha. Mara baada ya kuiwasha akavuta kavuta pafu mbili kisha akaizima na kuisigina na kiatu chake.

Mbele yake akapita mzee mmoja na kujikoholesha, umbali wa sentimeta kama mia hivi akaonesha ishara ya mkono ya kumtaka Amata amfuate. Kamanda Amata akaona ishara ile na kumfuata mpaka kwenye gari moja ya kizamani, Ford Anglia.

“Mr. Spark!” akaita kwa sauti yake nzito.

“Mavalanka,” Kamanda naye akajibu. Yule mzee akachukua lile begi na kulitupia ndani, kisha akaingia mlango wa dereva na kumwacha Amata akiufungua ule wa abiria.

“Karibu sana Bombay. Ni mara yako ya kwanza kufika?”

“Ndiyo, sijawahi kuja Bombay wala India kwa ujumla,”

“Ha! ha! ha! ha! Hakika utafurahia maisha katika kila nukta ambayo utapata nafasi ya mapumziko, wasichana wazuri wenye maumbo ya kuvutia watakuburudisha sana kwenye maklabu ya usiku na kadhalika, ila uwe mwanagalifu wengine wanakuwa kazini,” Yule mzee alimwambia Amata.

“Mi najua hii nchi ya kidini bwana, inakuwaje kuna klabu za usiku?”

“Akh! Klabu za usiku zipo duniani kote…”

“Ila sina tabia hiyo,” kamanda akajibu kwa mkato.

“Ah weeeeeeee! Nakujua vyema kijana. Ok, tuyaache hayo, Hoteli ya Grand Hyatt inakufaa sana,” alimwambia huku akikunja kona na kuingia katika lango kuu la hoteli hiyo na kuegesha gari yake.

“Unaona?” akauliza.

“Nini?”

“Hoteli kubwa nzuri ya kisasa ina bwawa la kuogelea kule juu na casino nzuri kabisa,” Yule mzee akamwambia huku akimsaidia kushusha lile begi.

“Asante sana, tutaonana tena,” Kamanda akamuaga huku akivuta hatua kuelkea ile hoteli lakini kabla hajafika langoni kuu la kuingilia mapokezi akapokelewa na vijana waliondaliwa kwa kazi hiyo kwa kila msafiri anayekuja.

Akafanya itifaki zote za mapokezi na kuingia katika chumba chake. Mara baada ya kuufunga mlango alikitazama chumba hicho kikubwa jinsi kilivyo na kilivyopangwa samani zake kwa mtindo wa kuvutia. Akainua saa yake ya mkono na kuifyatua upande wa juu, lile eneo lenye mishale ya saa likafunuka kama kifuniko na kuacha sehemu ya chini ikiwa na kitu fulani chenye uwezo wa kutambua aina yoyote ya mlipuko na kuonesha kama kuna mitambo ya kunasa sauti lakini akakuta kuna usalama wa kutosha. Akairudisha saa yake kisha akaliendea dirisha kubwa na kusogeza pazia pembeni. Majengo marefu kwa mafupi yalimkaribisha, taa za kupendeza za barabarani na majumba ya starehe zilionekana wazi zinavyopishana angani.

“Bombay!” akasema kwa suti ndogo.

Akiwa bado dirishani hapo akagutushwa na hodi iliyobishwa mlangoni, akauendea taratibu na kuufungua kwa hadhari kubwa. Sura ya mwanadada mrembo wa Kihindi ilimpokea kwa tabasamu lenye bashasha lililojaa na kuufanya uso wa mwanadada huyo kuwa wa mviringo, vishimo vilivyojitokeza katika mashavu yake vikawa kama vidimbwi vya maji katika jangwa.

“Samahani kuna mzigo wako hapa, tulisahau kukupatia pale kaunta,” yule msichana aliyekadiriwa kuwa na miaka ishirini hivi alimwambia Amata kwa sauti tamu iliyozitikisa kwa upole ngoma za masikio yake. Akainua mkono na kuipokea bahasha iliyokuwa mkononi mwa dada huyu huku akiking’ang’ania kiganja cha mkono huo.

“Mmm asante, unaitwa nani?” Kamanda akaanza ubembe wake.

Yule binti hakujibu kwanza, akamtazama Amata juu mpaka chini, akameza mate.

“Sukaina!” akajibu.

“Oh! Sukaina, jina zuri sana, asante kwa mzigo au kuna lingiine?”

“Hapana!” akajibu na kuanza kuondoka.

“Sukaina!” Kamanda akaita na yule binti akageuka.

“Napenda kuonana nawe ukimaliza kazi leo,”

“Mmmmm! Bwana wangu anakuja kunichukua, kwaheri,” akajibu na kuondoka zake.

Kamanda Amata akabaki katumbua macho akimwangalia yule mrembo akipotelea kwenye lifti huku vazi lake zuri lenye kumetameta likimfanya kuonekana mrembo zaidi. Macho yaliposhiba akarudi ndani na kuifungua ile bahasha.

Bastola moja ndogo ililala ndani yake ‘Beretta 92FS 99mm’, Kamanda Amata akaichukua na kuigeuzageuza, bado ilionekana mpya na haijatumika kabisa. Pembeni yake kulikuwa na kasha iliyojaa risasi, akaichukua na kuichana kisha akazijaza katika ile bastola na kuipima kidogo kama inafiti mkononi mwake. Bastola kama hii aliitumia zamani kidogo hivyo alishaanza kuipoteza ufanisi wake, kifaa chake cha kuzuia sauti nacho kilikuwa pamoja nayo. Akavuta memo ndogo na kuisoma.

‘Mgahawa wa Dinasty saa 2:15 asubuhi, meza namba 5’

Alipomaliza kuisoma akainkunja na kuitia kwenye begi lake kisha akaliendea bafu. Baada ya kuoga na kujiweka vizuri aliutafuta usingizi usiku huo na kuupata kwa tabu.

MGAHAWA WA DINASTY – saa 2:10 asubuhi

Akiwa ndani ya suti safi Amata aliteremka katika taksi na kuingia ndani ya mgahawa ule, mlangoni alipokelewa na mwanadada wa Kihindi aliyevalia vazi la kitamaduni, akamkaribisha na kumwonesha ukumbi wenye ukubwa wa wastani ambao ndani yake kulikuwa na watu walioketi wakipata ama kahawa au chai kila mmoja na kile alichopenda. Harufu ya vyakula na marashi ya Kihindu viliikinaisha pua ya Amata kwa sekunde chache, moja kwa moja akaiendea meza namba tano ambayo haikuwa na mtu yeyote aliyeketi hapo.

Pembeni mwa meza hiyo dirisha kubwa la kioo liliruhusu mtu yeyote kuona mandhari safi ya jiji la Bombay, na pia ungeweza kuwaona kwa uzuri watu waliokuwa wakipita huku na kule kwa shughuli mbalimbali. Katika usawa kabisa wa meza ile lakini upande wa nje kulikuwa na barabara kubwa iliyokuja kuungana na hiyo iliyo hapo. Amata aliitazama ile barabara iliyokwenda asikokujua.

N Ave Road! Amata alisoma kibao kikubwa cha rangi ya kijani kilichoonekana kupitia dirisha hilo kikiitambulisha barabara hiyo iliyonyooka kiasi kwamba mtazamaji aliweza kuona mpaka mwisho wake kama sio mbovu wa macho. Akiwa katika kushangaa huko akahisi kama mtu anaketi katika kiti cha mbele yake, akageuka taratibu na kugongana macho na Chiba aliyekuwa kajigeuza kidogo sura yake kwa kujiweka vichunusi vya hapa na pale na uvimbe wa bandia katika paji lake la uso.

“Karibu Bombay!” aliongea kwa sauti iliyoonesha kuwa na kikohozi kikali kwani mara kwa mara alikuwa akikohoa.

“Nimeshakaribia komredi,” akajibu na kujiweka sawa huku kifungua kinywa kikiteremshwa mezani taratibu na mhudumu aliyeijua kazi yake, wakasitisha mazungumzo yao kusubiri zoezi hilo lifanyike.

“Hapa kazi iliyopo ni ndogo tu lakini ni ngumu,” akaongea huku akiangalia huku na huko.

“Mbona unaongea kama una wasiwasi na jambo?”

“Lazima kuwa na wasiwasi kwani jamaa wamenishuku tangu juzi wakati nafuatilia nyendo za mwanaharamu, lakini niliwatoka hawakunipata tena”.

“Ningeshangaa!” Amata akaongezea.

“Sasa Kamanda, mpango upo hivi, Pancho Panchilio ana makazi yake ndani ya Hekalu Hanuman. Hili ni hekalu la Kihindu. Geuka kulia, tazama hiyo barabara,”

“N Ave Road,” akasoma tena yale maandishi kwenye lila bango.

“Barabara hii moja kwa moja mbele inakutana na barabara ya SB Patil na kufanya njia panda,”

“Enhe!”

“Hapo sasa ndipo penye hilo hekalu, nimemwona kwa macho yangu japo ilikuwa kazi ngumu sana, sijui tutamchukuaje,” Chiba alimweleza Amata aliyekuwa kanyamaza kimya akisikiliza huku akili yake ikizunguka kwa kasi ya ajabu.

“Kuna ulinzi mkali au vipi?” akauliza.

“Kuna kamera sabini na nne nje, na ndani zisizopungua thelethini, pale wanaingia Wahindu tu, mtu mweusi huna nafasi, kuna walinzi pande zote ndani na nje wenye vifaa vinavyoweza kumtambua yeyote mwenye nia mbaya na eneo hilo. Isitoshe ni eneo la hekalu ambalo hata viongozi wengi hupenda kuabudia hapo,” Chiba aliuliza.

“Nakusikiliza,” Kamanda alimwambia.

“Inabidi tumchukue akiwa hai,”

“Na tukimchukua tunampeleka wapi?”

“Bahrain House, pembezoni mwa Bombay karibu na bahari, jengo hilo halitumiki, limetelekezwa, tutafanya shughuli yetu humo na kuondoka naye.”

“Safi sana Chiba, nitahitaji kutembelea hekalu hilo ili nilione kwa ukaribu,” Kamanda akasema.

“Haina haja,” akaingiza mkono mfukoni na kuchomoa kipande cha karatasi, akakikunjua na kukiweka mezani.

“Hii hapa ni ramani ya jengo hilo,” akamwonesha.

Wakatazama pamoja, Chiba akamwonesha Amata kila kona yenye kamera na ulinzi wa binadamu, walipojiridhisha, akairudisha mfukoni ramani ile.

“Sawa Chiba, nimeona, lakini bado mi na wewe hatujui hasa huyu mtu anaishi kona gani pale au anakuja na kutoka,” Kamanda akazungumza..

“Aaaa aisee halafu kweli, hapo sikutumia umakini,” akakiri.

“Usiwe na shaka, huyu mtu atakamatika tu hata awe na mizizi mingi kama mnazi, atang’oka tu,” Kamanda alisema.

“Nakuamini kamanda, Madam S atakuwa hapa muda si mrefu,” Chiba akazungumza.

“Safi, sasa fanya hivi kama inawezekana Madam aombe usafiri binafsi, aje na ndege ili tukimtia mkononi huyu jamaa tuondoke naye kiurahisi, kumbuka kwenye ndege ya abiria akileta vurugu ni hatari kwa mamia ya watu,” Kamanda alimpa maagizo Chiba.

- * *

Kama kawaida ya Jiji la Bombay, watu walikuwa wengi barabarani, pikipiki za magurudumu matatu, usiseme, zilikuwa zikisafirisha watu huku na kule. Kwa ujumla kulikuwa na magari machache sana lakini pikipiki zilitawala kila kona. Kamanda Amata alikuwa ndani ya moja ya ‘Bajaj’ hizo akielekea upande mwingine wa jiji.

“Mwenyeji wetu hapa ni Sha Kapur, yeye ni mwanausalama mstahafu, anajua mengi na Madam S alinishauri kukutana naye,” Chiba aliendelea kuongea huku akiwa katika bajaj nyingine tofauti na ile aliyopanda Amata. Lakini kwa kutumia kifaa kidogo kabisa cha mawasiliano aliweza kusikilizana vyema na swahiba wake huyo,

“Lazima tumuone, lakini kwanza ngoja nilione hilo hekalu hata kwa nje,” Amata akajibu.

“Yote heri,”

Kamanda Amata aliteremka na kumlipa yule dereva, alipoinua uso wake mbele akaona lile hekalu kubwa linalopendeza kwa macho. Hekalu la Hanuman.

Ilikuwa mchana wa saa saba watu wakipishana kuingia na kutoka ndani ya hekalu lile huku ibada zikisikika kwenye vipaza sauti, watu waliopendeza kwa mavazi mbalimbali ya tamaduni za Kihindi walikuwa eneo hilo akina mama kwa akina baba, watoto kwa vijana. Umbali kama wa mita ishirini kutoka katika lango kuu la hekalu hilo kulikuwa na kundi la watu waliokuwa wakinunua vitu fulani ambavyo hakuvijua vizuri ni vitu gani. Akavuta hatua mpaka eneo lile. Amata alikuwa tofauti kwa mavazi, hakuna aliyevaa suti eneo lile, kila jicho lilimtazama yeye.

Karimati, kachori na vyakula mbalimbali vya Kihindi vilikuwa hapo, Kamanda Amata akasogelea mahala pale na kuinama kutazama kwa ndani kumuona muuzaji.

“Svagata,” (Karibu) sauti nyororo ya kike ikapenya masikioni mwa Amata.

“Dhan’yavada,” (Asante sana) akajibu kawa lugha hiyo ya Kihindi na kumtazama mwanadada huyo, macho yao yalipogongana kila mmoja akabaki kakodoa. Amata hakuamini anayemwona na wala mwanadada huyo hakuamini aliye mbele yake.

“Amata!” akabaki kama aliyepigwa shoti ya umeme.

“Hapa si salama, njoo huku, nifuate,” Yule msichana akaondoka na kumwachia kijana wake aendelee na kazi hiyo.

- * *

Chiba alitikisa kichwa na kumtazama Amata akiondoka na Yule mwanamke.

“Hili ndilo tatizo la huyu jamaa, keshanasa,” Chiba alinung’unika. Akajitoa pale aliposimama na kusogea upande wa pili ili amwone vizuri Kamanda anaelekea wapi, akasimama mahali penye kiduka, akaagiza kinywaji na kuendelea kumtazama swahiba wake akipotelea ndani ya nyumba mojawapo katika eneo hilo, hatua kama mia mbili kutoka katika lile hekalu. Naye taratibu akaachana na kinywaji chake na kuendelea kutembea huku akipiga mruzi kuelekea eneo lile, alipofika hakuwaona kabisa isipokuwa lango lililofungwa na kubaki bila mlinzi. Akatazama huku na huku hakuna mtu; akavuka na kuliendea lile lango, alipolisukuma, likasukumika; akajipenyeza ndani taratibu na kusimama wima huku lile lango likijifunga nyuma yake.

Ukimya wa eneo lile ulimtia wasiwasi Chiba, akapepesa macho yake huku na kule hakuona mtu wala kiumbe hai chochote chenye uwezo wa kujongea. Mimea mirefu ilikuwa ikiyumbayumba kwa upepo wa taratibu. Kati ya mimea mingi iliyoshikana na kushonana kulionekana nyumba moja ndogo iliyonakshiwa kwa nakshi za kiajemi.

Hapa hakuna usalama! akawaza na kuichomoa bastola yake kutoka mafichoni na kuiweka kiganjani tayari kwa lolote. Mwendo wake wa minyato ulifanya aonekane kama mvamizi wa eneo hilo.

- * *

“Amata! Nini kimekuleta India?”

“Sikutegemea kabisa kukuona SaSha,”

“Hapa ni nyumbani vyovyote ujavyo tegemea kuniona,” SaSha alimwambia Amata huku akiwa amekumbatiwa na kuegemea ukuta, nyuso zao zikitazamana na pumzi kupishana kwa kasi. Taratibu vinywa vya wawili hawa vikaanza kukaribiana huku mihemo ikiongezeka.

Mlio wa kengele ulimshtua SaSha na kumsukuma Amata pembeni, akasogea dirishani na kuvuta pazia taratibu; kutoka ndani aliweza kumwona Chiba. Lakini Chiba hakuweza kumwona SaSha kutokana na dirisha lile kufichwa na mimea iliyotambaa kwa nje.

SaSha akachomoa bastola na kuiweka tayari akiulelekea mlango. Kamanda Amata taratibu akavuta pazia kutazama kilicho nje.

“SaSha!” akaita kwa sauti ndogo. SaSha akageuka kumtazama akampa ishara ya kurudi.

“Kijana wangu huyo, ananilinda, anaitwa Chiba”. SaSha akarudisha bastola yake na kufungua mlango huku akinyosha mikono yake juu kuonesha ishara ya amani.

“Karibu Chiba, tafadhali hapa ni mahala salama,” SaSha akamwambia Chiba na wakati huo Chiba akashusha bastola yake na kuiweka katika kikoba chake.

“Karibu ndani,” akamwambia huku akiingia ndani ya ile nyumba. SaSha akaweka vinywaji mezani na wote wakaendelea kunywa taratibu huku wakibadilishana mawazo.

“Amata, kuna nini Bombay? Maana wewe huwezi kuja sehemu kama hii kwa likizo,” SaSha akauliza tena.

“Nimemfuata mwanaharamu,”

“Nani na yuko wapi?”

“Mwanamke! Hutakiwi kumjua we endelea na kazi yako hili halikuhusu, nimeshakujibu,” Amata akajibu kwa ukali kidogo. Akamgeukia Chiba na kumtambulisha.

“Anaitwa Sasha, ni agent wa shirika la kijasusi la CBI hapa India, alikuwa Tanzania miaka kadhaa nyuma katika sakata lileee la yule gaidi, kama unakumbuka,”

“Nakumbuka, sakata la Jegan Grashan?” Chiba akauliza.

“Ndiyo,” akajibiwa na kisha ukimya ukatawala. Kamanda Amata akanyanyuka na kuliendea dirisha la upande wa nyuma akatazama na kuona shughuli mbalimbali zikiendelea, hakuweza kujua kama ni za uvuvi au ni kitu gani, akampa ishara Chiba asogee pale dirishani. Nukta chache, Chiba alikuwa pamoja na Amata huku mkono akiwa na darubini ndogo lakini yenye nguvu kubwa, inayoweza kupima na kukuandikia umbali wa hicho kitu kilipo kutoka uliposimama wewe. Amata akiweka machoni na kutazama, kwa mbali kulikuwa na boti iliyoonekana ikija upande huo.

“Tazama hiyo boti,” akamwambia Chiba huku akimpa ile darubini na yeye akaiweka machoni na kutazama.

“Amata!” akaita baada ya kutazama kwa sekunde kadhaa.

Ile boti ilifika karibu na pwani lakini ilishindwa kusogea kutokana na kupwa kwa maji, watu kama nane walisogea kule baharini na kumbeba mtu mmoja kwenye kiti maalumu kama mfalme wa kikoloni. Huku watu wengine wakirusha maua na kuonekana kama wanampa heshima mtu huyo.

“Shiit!” Chiba aling’aka na kumpa ile darubini Amata.

“Vipi?”

“Pancho Panchilio,” akajibu Chiba, “laiti ingekuwa tummalize, basi hapa ndipo tungeiushangaza Dunia,” akaongeza.

“Bibi yako anataka amnase kofi kabla hajafungwa,” Amata akasema na wote wakacheka. SaSha akafika hapo dirishani na kumnyang’anya darubini Amata kisha akaanza kuangalia yeye.

“Waoh! Chief anarudi,” SaSha akajisemea kwa sauti huku akirudisha darubini kwa Amata.

“Ni nani Yule?” Chiba akahoji baada ya kugundua kuwa mwanamke huyo anamjua Pancho kama Chfu.

“Yule ni Chief wa ukoo fulani ambao unamiliki hilo hekalu hapo, ni mtu mwema sana kiasi kwamba watu wa ukoo wake umtukuza kama mfalme,” SaSha akawaeleza Chiba na Amata wakati huo Chiba alikuwa akinasa mazungumzo yale kwa kutumia pete aliyokuwa ameivaa kidoleni mwake.

“Kwa hiyo anakuja kuwasalimu watu wake?” Kamanda akauliza lakini swali lake lilikuwani la kutaka tu uhakika wa jambo ambalo Chiba hakulichunguza sawasawa.

“No! hapo ndipo anapoishi,” SaSha akajibu huku akimtazama Amata.

“Nitakwenda kumsalimu au vipi Chiba?” Amata akapendekeza.

“Oh! No! hamuwezi kumuona, huwa haonekani kwa urahisi hivyo hususan kwa ninyi watu weusi. Watu wake humuona kwa nadra sana, kupata muda wa kuzungumza naye labda ni dakika tano tu na ni mara moja kwa mwezi,” SaSha akaendelea kueleza.

“Anaitwa nani?” Chiba akauliza.

“Premji Kanoon,” SaSha akajibu; Chiba na Amata wakatazamana na kubaniana macho. Amata akarudisha darubini machoni na kutazama ule msafara. Wale vijana waliombeba waliendele kutembea na kuiacha pwani kisha wakaingia kwenye ngome kubwa ambayo ndani yake ndiko kuna hilo hekalu. Walipopotelea ndani yake, akashusha ile darubini na kumrudishia Chiba ambaye aliificha ndani ya koti lake. Amata akamwangalia SaSha.

“Anaishi wapi?” akauliza.

“Humo humo ndani, chini ya hilo hekalu kuna kasri kubwa sana ambalo ndilo anloishi siku zote. Kesho ni sikukuu ya Diware, watu wengi kuliko hapo unapoona watakuja, nafikiri utaweza kumwona vizuri kwani baada ya ibada kuna sherehe kubwa kwenye uwanja huko nyuma zinazoambatana na michezo mbalimbali,” SaSha akaeleza.

“Ok, natamani kuhudhuria,”

“Bila shaka, jioni ni kwa kila mtu,” SaSha akamaliza kuongea na kuwapa vinywaji wawili hao.

- * *

Premji Kanoon aliteremshwa kutoka katika kile kiti akakanyaga chini kwa miguu yake na moja kwa moja akaingia kwenye kijimlango kidogo na kujifungia. Akateremshwa chini ya ardhi ambako kulikuwa na kasri lake lisilo na bugudha. Alipofika tu akapewa huduma zote zilizomstahili ikiwa pamoja na kukandwakandwa mabegani, kuoshwa miguu kupakwa mafuta ya kunukia katika nyayo zake na mambo mengine mengi. Chumba chote kilinukia udi, aliinuka na kusogea karibu na sanamu moja lenye ukubwa wa wastani, akainamisha kichwa chake huku akiwa kabana viganja vya mikono yake kifuani kwa uchaji wa hali ya juu. Sekunde kadhaa akamaliza na kutoka eneo hilo huku akimwagiwa maua mazuri ya kunukia naye akakanyaga juu yake.

Hatua chache akalifikia sanamu lingine, akasimama mbele yake na lile sanamu likasogea pembeni taratibu, akapita na likarudi mahala pake. Kilikuwa chumba kidogo chenye giza, kikamteremsha chini zaidi na huko akaingia kwenye ukumbi wa wastani uliokuwa uking’azwa kwa taa zinazobadilisha rangi. Akaketi kwenye kiti kimoja kikubwa kilichokuwa nyuma ya meza yenye nakshi za kupendeza. Mbele yake kulikuwa na watu wanne, vijana wakakamavu wenye miili ya wastani, vichwani mwao walivaa vilemba ambavyo viliwatambulisha kuwa wao ni Singasinga.

Akajikohoza kidogo na wale vijana waliendelea kusimama pale wakiwa kimya kabisa. Pancho Panchilio au wao wanamwita Premji Kanoon.

“Sina lingine, nataka auawe au wauawe,” akasema.

Wale jamaa wakaitikia kwa vichwa tu, hawakuongea lolote; pembeni yao kukatokea picha kubwa ya Amata.

“Mnamwona huyu?” akawauliza, wote wakageuka na kuitikia kwa vichwa.

“Mna uhakika ndiye mliyemwona uwanja wa ndege?”

Wakajibu tena kwa kutikisa vichwa.

“Vizuri, sasa nataka auawe mara moja yeye na yule wa mwanzo, watu wa jamii kama hii hawafai kuishi kwa sababu huaribu mipango ya watu. Sikilizeni, huyu mnayemwona kwenye picha ni mtu hatari sana, mnapokwenda kumshambulia hakikisheni mmejipanga vizuri, mnanielewa?” akawauliza.

“Ndiyo, tunakuhakikishia jua la kesho hawezi kuliona kamwe!” mmoja aliyesimama mbele ya wenzake akajibu kwa ushupavu. Zile taa zikazimika na Pancho akapotea kwenye milango yake ya siri.

MKESHA WA DIWALI

“Kamanda Amata!” SaSha akaita kwa sauti ya chini.

“Niambie mtoto mzuri,” Amata akajibu.

“Unalala hapa siyo?”

“No! natoka sasa maana usiku huu tuna kazi ya kufanya. Kesho uje pale Grand Hyatt Hoteli, utanikuta,” kamanda akamwelekeza.

“Mmmmm! Nikikufumania maana wewe huwezi kulala bila mwanamke,”

“Acha uongo,” akamjibu huku akijinasua kutoka katika mikono ya SaSha iliyokuwa imembana pale kitandani, akaingia bafuni na kujiweka sawa, alipojitumbukiza ndani ya suti yake na kutokomea nje ya jengo lile.

“Swiiiiiiiiiih!” sauti ya mruzi ilimshtua Amata akasimama na ghafla gari moja ikatokea mbele yake na kusimama.

“Twenzetu kumekucha!” Ilikuwa sauti ya Chiba, akajipakia garini na wakaondoka kwa kasi.

“Kamanda tuko matatani, jamaa wamejipanga wanajua kama upo hapa, nilichofurahia ni kuwa wanakuzungumzia wewe na hawajui kama mimi niko hapa,” Chiba akaeleza huku akiongeza kasi ya gari yake kumbe hakuwa akijua kuwa wenzake walishammaizi muda mrefu.

“Asee, watakuwa wamejuaje kama niko hapa?”

“Ah hapo ni sehemu mbili tu ama uwanja wa ndege au hotelini, watu kama hawa huwa na macho mengi na masikio kila mahali,” Chiba akaongea harakaharaka.

“Sasa Chiba na sisi tugeuze kibao, kazi yetu tuifanye leo hii hii usiku tukichelewa kitanuka, maana wanaweza kusali wale tukageuka panya kwenye nchi ya watu,” Kamanda akaongea huku akijiweka vizuri kitini,

“Twende hotelini, nikachukue begi langu niliweke humu garini maana kuanzia sasa kambi popote”.

Chiba akakunja kona kali na kujikuta kapita katika taa nyekundu, honi za magari zikasikika kila upande, lakini hakusimama akakanyaga mafuta na ile gari ikazidi kuunguruma kwa nguvu.

HOTELI YA GRAND HYATT

GIZA LILIKUWA likishindana na taa za umeme zilizopendezesha jengo hilo la hoteli. Siku hiyo ambayo ilikuwa ni usiku wa kuamkia sherehe kubwa sana kwa dini za Kihindi ulijawa na watu wengi. Wale waliopenda ibada walienda mahekaluni na wale waliopenda starehe walienda kwenye makasino.

Gari moja, dogo, jeusi likaegesha katika maegesho na vijana wawili wakateremka, vijana hao wenye mandevu na maviremba vichwani mwao hawakuwa na la kuongea wala kusalimiana na yeyote waliomuona. Mmoja wao akainua simu na kupiga, akaongea maneno machache na kuiweka mfukoni ile simu kisha akauendea mlango mkubwa wa ile hoteli. Moja kwa moja alisimama mbele ya kaunta na kubadilishana maneno kadhaa na mhudumu aliyekuwa hapo na kutoka kuelekea kunako lifti za kupanda juu.Yule mwenzake alibaki kwenye makochi ya mapokezi akivuta gazeti hili na lile, mtego.

- * *

“Chiba wewe nisubiri upande uleeee, mi naingia kutoa begi tu napitia mlango wa nyuma kisha tunaondoka bila kuaga,” Amata akamwambia Chiba wakati akiufunga mlango wa gari hiyo na kumwacha Chiba akiondoka taratibu kuelekea upande wa pili wa ofisi hiyo. Amata akavuta hatua za nusu kukimbia na nusu kutembea, akazikwea ngazi na moja kwa moja akaifuata kaunta na kukaribishwa na yule binti wa jana yake, Sukaina.

“Ndiyo mrembo! Ujumbe wangu wowote?” akauliza.

“Ujumbe wako nimekupelekea chumbani tayari,”

“Sasa mbona hukusubiri hukohuko unikabidhi?” Amata akaanza maneno yake ya ubembe.

“Mmmm na wewe, tangulia nakuja,”

“Waja kweli au ndiyo kunipaka mafuta kwa mgongo wa chupa?”

“Naja kweli we tangulia dakika kumi nitakuwa nimefika maana ndiyo nafunga ofisi natoka. Nikukute kitandani sawa bebi?” Sukaina akarusha maneno ya kumlegeza Amata huku akijuwa wazi kuwa ni kitu gani kitakachomtokea kijana huyo. Yule jamaa aliyekaa pale kwenye kochi akamwoneshea ishara ya dole gumba Sukaina na kunyanyuka taratibu kuelekea kule ndani alikoenda Amata.

Kamanda Amata alibofya kitufe cha kuiita lifti lakini alihisi vinyweleo vyake vikisimama na mwili ukisisimka, akarusdi nyuma hatua mbili na kugeuka akapanda kwa ngazi za kawaida mpaka ghorofa ya nne kulikokuwa na chumba chake. Alipoufikia mlango, akautazama juu hadi chini, kisha akatupa jicho pale kwenye kitasa kile cha kielektroniki ambacho kufungua ulipaswa ku-chanja kwa ‘smart card’ kisha mlango ungefunguka. Moyo wake ukawa mzito kufanya jambo hilo, jicho lake lilipotua kwenye ile sehemu akagundua uwa mlango ule umefunguliwa kwa maana alama yake ya kiuzi alichokitengeneza kama kifundo fulani na kukipachika katika ule mfereji wa kuchanjia kadi haukuwepo. Akachomoa bastola yake ‘Berreta’ na kupachika kile chombo cha kupoteza sauti kisha akachomoa kadi yake nyingine na kuchanja, mara mlango ukajinasua loki zake. Akaufungua ule mlango kwa kasi na kubamiza kwa nyuma, kumbe yule mjinga alijificha upande huo. Akajikuta akipigwa na mlango usoni, akatoka pale huku bastola ikimwanguka chini na mkono kajishika pua.

Amata alirudisha bastola yake kikobani na yule bwana alipogeuka, alikutana na makonde mawili ya maana yaliyopita yote usoni, akayumba na kujibamiza mezani kabla hajaenda chini ambako hata hakufika kwani teke kali la Amata lilitua usoni na kumtupia upande wa pili wa kitanda. Kamanda Amata akaweka tai yake vizuri na kufunga upya saa yake, kisha akaruka kitanda na kutua upande wa yule bwege ambaye alikuwa akijiandaa kunyanyuka ilhali hali yake tayari ilikuwa tete. Alipotua sakafuni alihisi mlango ukifunguka tena nyuma yake, bila kuuliza, alichomo bastola na kujirusha chini huku tayari keshafyatu risasi mbili zilizoishia tumboni mwa yule mjinga wa pili na kumbwaga chini huku akigombania roho yake isimwache.

Amata akageuka haraka na kumrudia yule wa kwanza ambaye tayari alikuwa amesimama na kujiandaa kwa mapambano.

“Umemuua Rajiv! Sasa zamu yako,” akaunguruma huku shati lake likiendelea kulowa kwa damu zilizokuwa zikichirizika kutoka puani mwake.

“Tulia mpumbavu wewe,” Amata alimjibu kwa lugha hiyo ya Kihindi aliyokuwa akijarobu kumwemwesa japo maneno mawili.

“Tupa bastola tupambane, hujui kama nchi hii ndiko alikozaliwa Amitah na Mithun?” lile jamaa likamwambia Amata.

“Hamna tabu,” Amata akaipachika kwenye kikoba chake. Wakati akifanya hilo Yule jamaa alitua kifuani mwa Amata kwa miguu yake miwili. Amata akapepesuka na kujibamiza ukutani huku akimwona jamaa akitua sakafuni kwa miguu yake ileile. Kabla hajatulia, Amata alijizungusha huku akiwa amebonyea na kuwa mdogo kama mbuzi, mguu wake wa kulia uliozunguka kwa kasi ulimchota ngwala yule bwana aliyekuwa akijaribu kuruka ili akwepe pigo hilo, lakini haikuwa hivo kwani alichotwa vibaya na kubamiza kisogo chini huku kiwiliwili kikimfuatia juu yake. Alijitahidi kunyanyuka lakini guu la Amata likatua kwa nguvu kifuani na kumafanya ateme damu.

“Unamjua Premji Kanoon?” akamwuliza.

“Husilitaje bure jina la mtu huyo,”

Kamanda Amata akamwinamia na kumchapa kofi moja kali lililomwacha taabani.

“Nani mshirika wenu hapa?”

“Hatuna mshirika,” akajibu kwa taabu. Kamanda Amata akachomoa kisu cha kukunja na kukifyatua hewani, ile ncha yake ikachachamaa juu, alipokishusha kilitua kwenye nyama ya paja.

“Aaaaaiiiiiggghhhh! Sukaina wa mapokezi,” akajibu huku akifumba macho na kubana meno.

“Shenzi kabisa wewe,”

Akakichomo na kukifuta damu kwa nguo za yule jamaa huku akisimama na kukipachika mahala pake. Damu ilikuwa ikimbubujika pale chini. Amata akafungua kabati na kutupia vitu vyake ndani ya begi lake.

‘Haina haja ya kupoteza muda’ akawaza na kuivuta bastola yake.

“We mjinga salamu hii umpe mungu wako Premji Kanoon, mwambie Kamanda Amata yuko hapa,” akafytaua risasi na kuvunja goti la mguu wake mmoja, kisha akasonya na kupotea akiacha maumivu, kifo na kilio ndani ya chumba hicho.

- * *

Amata akatupi begi lake katika kiti cha nyuma na kujiweka kiti cha mbele.

“Vipi?” Chiba akauliza.

“Mmoja kafa, mwingine atakuwa kiwete milele na wengine tunawafuata leo hii hii,” Kamanda akajibu huku Chiba akiondoka eneo lile na kutokomea gizani.

“Itawezekana kufunga kazi usiku huu? Maana nilikadiri saa sabini na mbili,” Chiba akauliza huku akiiacha barabara kubwa na kuingia kwenye barabara ya vumbi iliyopita katika miti mingi ambayo moja kwa moja ilikuwa ikielekea Bahrain House.

“Usijali, hapa kazi tu, ndani ya saa hizi arobaini na nane tayari huyu mtu atakuwa mikononi mwetu. Naamini Madam atafanya ulivyomwambia,” Kamanda akaeleza huku akiweka bastola yake na silaha nyingine tayari tayari.

“Usihofu juu ya Madam, ameona jua kabla yetu”.

Chiba akaegesha gari ndani ya jengo hilo na kuteremka kisha akaingia mahala fulani na kuchukua silaha mbili tatu na mavazi ya kutumia katika hali halisi itakayowakumba, mabomu ya machozi na vinyago vya kuzuia sumu hiyo, mavazi ya kuogelea na mitungi ya hewa mine. Sehemu nyingine ya jengo hilo akafungua boti ndogo iliyokuwa kwenye kitoroli na kuivuta kwa mikono yake mpaka, ndani yake akatupia vile vitu na kuisukuma mpaka majini. Bahari haikuwa mbali na jengo hilo kuukuu: Kamanda Amata na Chiba wakaingia kwenye boti na kuiwasha, safari ikaanza.

“Watatusubiri kwa njia ya barabara, sisi tutaingia kwa njia ya maji!” Chiba akasema.

3

“Ulijiandaa sana kijana!” Amata akamsifia.

“Ndiyo, maana maelekezo mengi tayari nilipewa na Madam S nimwone Yule mzee ndiye akanipa ramani ya mji huu na lile kasri la Pancho,” Chiba akaeleza.

“Amekwisha, Gabacholi yule!” Amata akasema huku akifungua chupa ndogo ya Grants na kuigugumia kinywani.

“Aaaaaaakkhhhh!” akashusha pumzi iliyoashiria ukali wa kinywaji hiko.

- * *

Chiba alizima mlio wa injini ya boti na kuiacha iseleleke taratibu mpaka ilipo karibia umbali kama wa mita mia tano hivi. Wakati huo Amata alikuwa tayari amekwishavaa nguo zake za kupigia mbizi, mitungi yake mgongoni na begi dogo lilisiloingia maji mbele ya tumbo lake.

“Chiba, hapa kazi tu, mi naingia kwa njia ya maji nafikiri ni njia rahisi kama ulivyonambia, na wewe pitia hii hii lakini upande wa pili sote tukaibukie ndani na kutafuta njia ya kumnasa mtu huyo, tukishamtia mkononi kila mtu aangalie ustaarabu wa kuitoka hiyo himaya lakini tukutane Bahrain,” Kamanda Amata alimweleza mkakati mzima Chiba kisha akajitupa majini na kupotelea humo.

Chiba akaendele kupiga kasia kuisogeza ile boti mpaka kwenye mimea ya baharini iliyojazana upande mmoja wa peninsula hiyo. Akaegesha naye akavaa vifaa vyake na kujitupa majini kwa uelekeo mwingine.

- * *

Ndani ya hekalu hilo sherehe za mwanga ‘Diwali’ zilikuwa zikiendelea, watu walikuwa wakiimba na kucheza, kwa ujumla palichangamka. Premji Kanoon au Pancho Panchilio alikuwa ameketi sehemu ya juu kabisa akifuatilia michezo na burudani zote zilizokuwa zikiendelea katika ukumbi huo. Kando yake alikaa na watu wengine kadhaa huku wanawake kama nane hivi warembo wa kuvutia walikuwa wakimpepea, wengine wakileta vinywaji na kadhalika. Nyuma yake alisimama mtu mmoja, mwanaume mwenye tambo kubwa, aliyefuga sharubu zake na kuzichanua huku na kule kama askari wa Kijerumani enzi za mkoloni. Mikono yake aliifungamanisha nyuma. Macho yake yalionekana kutopepeswa upande wowote ule. Na katika kila upande au kona ya jengo lile walionekana vijana waliovalia sare na vitambaa vyao vichwani mwao wakirandaranda huku na kule.

Kamanda Amata aliibuka majini na kujikuta kwenye chumba ambacho ndani yake kuna boti kubwa la kifahari lililoegeshwa.

‘Nimekuja wakati mzuri, ningekuja mchana kusingekuwa na maji hivi,’ akawaza huku akivua ule mtungi na kuuweka kando, akatoa na yale mavazi yake kisha akafungua begi lake na kujipachika kila silaha aliyoihitaji mwilini mwake. Sauti ya viatu vya mtu aliyekuwa akija upande huo vilimfanya atulie tuli huku kisu chake kikiwa ngangari kiganjani.

“Inabidi tuiwashe kwanza ili injini ipate moto. Mkuu anasema hana budi kwenda Punjawar usiku huu,” Sauti ya kwanza iliongea.

“Mbona ghafla hivi wakati sherehe hii yote kaandaa kwa ajili ya watu wake?” Sauti ya pili ikauliza.

“Mi mwenyewe sielewi aisee, ngoja tuwashe kabisa yeye akifika ni kuondoka tu,” ile sauti ya kwanza ikarudia.

‘Nimsubiri kwenye boti?’ Amata akajiuliza moyoni.

‘Uamuzi mbaya utakuwa’ akajijibu mwenyewe na nukta hiyohiyo yule jamaa akaibukia kwenye mlango mmoja wa chumba hicho. Amata akaruka kwa wepesi na kumvamia huku akiwa tayari kamdidimiza kisu moyoni. Akamshusha chini taratibu na kumsukumia kwenye maji. Kisha akatulia kwani bado mwingine alikuwa akija upande huo.

“Kumar! Kumar!” Yule wa pili akaita. Lakini hakukuwa na jibu kutoka kwa swahiba wake, akaendelea kwenda na alipofika kwenye kile chumba hakuamini anachokiona. Mwili wa Kumar ulikuwa ukielea kifudifudi majini. Mshtuko wake ulikuwa zahiri shahiri, akainua redio yake na kuomba msaada.

“Kumar mara cuka hai! Kumar mara cuka hai!” (Kumar amekufa! Kumar amekufa), Amata akajibana kimya nyuma ya pipa kubwa lililojaa vipuli mbalimbali. Dakika hiyohiyo watu kama saba wenye silaha wakaingia katika kile chumba.

‘Nimecheza blanda’ akajiambia, akachomoa bastola yake iliyofungwa kifaa cha kuzuia sauti na kuiweka tayari. Risasi ya kwanza akapiga mtungi wa kuzimia moto na poda iliyokuwa ndani yake ikatoka kwa kasi na kuwachanganya wale jamaa. Kamanda Amata akapita kwa kasi huku watatu waliokuwa mbele yake wakiwa chali kwa risasi kutoka kwenye bastola yake, sekunde mbili tu alikuwa keshafika mlangoni na kuufunga kwa nje akiwaachia kizaazaa. Ujia mrefu ulimkaribisha. Ving’ora vya hatari vikalia kila kona, mvurugano ukaanza kila kona, burudani zikasimama na kelele za vilio nzikaanza huku na kule.

- * *

Chiba aligundua hali ile baada ya kusikia kelele za watu, akapachika head set yake masikioni tayari kwa kazi.

“Amata vaa barakoa yako kazi inaanza,” Chiba akaongea kwenye kile kifaa na kisha akavaa kinyago chake cha kuzuia gesi ya machozi na kinachoweza kumfanya aone gizani bila tabu. Akatazama huku na kule akaona sensor ya moshi ambayo ikipata moshi basi huruhusu maji kumwagika, akatazama huku na kule akaona ua jirani, akavuta karatasi la urembo lilikuwa hapo akawasha moto na kisha akasogeza karibu na ile sensa, nukta hiyohiyo jengo zima likaanza kutiririsha maji, Chiba akaifuata swichi kubwa ya umeme na kuizima kisha akaondoa fyuzi na kuzitupa mbali. Sasa jengo lote lilikuwa giza na jenereta liligoma kuwaka, tayari kijana huyo wa TSA alishapita na kuondoa betri. Yale maji yaliyokuwa yakimwagika nayo yakakatika ghafla.

- * *

UKUMBI wote ulishikwa na kimuhemuhe, Amata alichomoa bastola yake yenye mabomu ya machozi na kutawanya huku na kule. Moshi huo mzito uliwafanya watu kukohoa bila kikomo, wakiishiwa nguvu na wengine kuanguka chini hawajiwezi.

Pancho Panchilio, aliinuliwa pale alipoketi na vijana wake kama saba hivi wakawa wamemzunguka kwa kumlinda wakiwa na silaha zisizojua huruma. Kutokana na gia lile walishindwa kumwona sawasawa Amata hivyo ilikuwa ni rahisi kwake kuwatawanya kwa risasi. Zilipomwishia akaruka sarakasi na kutua karibu kabisa na Pancho Panchilio huku miguu yake ikiwatandika mateke walinzi wawili waliobaki. Pancho alitaka kukimbia kuingia kwenye mlango mmoja lakini hakufanikiwa, ngwala moja maridadi ilimbwaga chini vibaya, wale vijana walipojaribu kunyanyuka, risasi za Chiba ziliwarudisha chini na Amata akapata nafasi ya kuinuka na kukutana uso kwa uso na Pancho.

“Twende nyumbani mwanaharamu wewe!” kamwambia huku akimtandika konde moja kali lililomfanya ayumbe na kupoteza mwelekeo. Konde la pili likamrudisha chini akiwa hoi, pamoja na ule moshi kumlegeza. Amata alijikuta akishikwa na hasira akikumbuka mtu huyo alichowafanyia yeye na wenzake kule Kerege katika mkasa uliopewa jina la Kitisho.

Kabla hajafanya lolote, akajikuta akipigwa na kitu kizito kisogoni, lakini mpigaji hakulenga sawasawa, Amata akageuka na kupeleka mashambulizi makali yaliyolifanya lile jitu lipoteane lenyewe kwa lenyewe. Lilipotulia likajikuta likitandikwa risasi mbili za kifua.

“Hatuna muda wa kupoteza, nasikia ving’ora vya wanoko huko nje,” Chiba alimwambia Amata, na wakati huo huo, Amata akamkamata mkono Pancho na kumkokota kwa nguvu. Mirindimo ya risasi bado ilikuwa ikiendelea, moshi wa machozi ulikuwa umechanganyika na ule wa baruti na kulete harufu ya tatu.

“Ondoka naye Amata, mi nalinda mkia wako,” Chiba alimwambia tena braza ‘ake na Kamanda Amata akatoka na Pancho, alipoona upinzani umekuwa mkali akambeba Pancho na kuruka naye ghorofa ya chini yake wakafika hoi. Amata akawahi kunyayuka na kutumia bastola yake nyingine kupambana na wawili watatu waliokuiwa mahali hapo na kujaribu kumletea zengwe.

Haraka akaiwahi gari iliyokuwa imeegeshwa hapo na kufungua mlango.

‘Asante sana’ akashukuru baada ya kukuta funguo ikining’inia, akafungua buti.

“Ingia!” akamwamuru Pancho huku akiwa amekiinua kile kinyago chake na kukiweka kwa juu, Pancho akapigwa butwaa kumwona kiumbe huyo matata.

“Unashangaa nini? Ingia unanipotezea muda,” kamanda akang’aka lakini Pancho hakutaka kufanya hivyo. Konde moja la tumbo likamfanya Pancho ajiinamie huku amejishika tumbo lake, teke la kusukuma lilipeleka mpaka kwenye buti na Kamanda Amata akamalizia kufunga buti hilo kwa mguu kisha akaingia kwenye usukani, akaiwasha gari hiyo na kutoka kwa kasi huku akigonga geti na kukunja kushoto. Mfukuzano na gari za polisi ulichukua nafasi katika barabara za Bombay. Amata aliwapeleka nje ya mji kwenye barabara ya hatari kabisa, yenye mteremko mkali na wenye kona za ajabu, ambapo wengine waligwaya na waliojaribu walijikuta wakiishia shimoni.

Baada ya kuhakikisha wote kawaacha mbali Amata alichukua uelekeo wa Bahrain house na kuliacha jiji hilo. Saa tisa za usiku akaegesha gari ndani ya jengo hilo kuukuu, akateremka akiwa hafai kwa vumbi lililomkaa mwilini. Akafungua buti na kumtoa Pancho aliyekuwa kajikunyata ndani yake.

“Shuka!” akamwamuru naye akashuka. Akamkokota mpaka ndani ya chumba kimoja kikubwa.

“Pancho Panchilio au Premji Kanoon, karibu katika himaya yangu, mara hii ni zamu yako,” Sauti ya Madam S ikasikisa na taa yenye nuru hafifu ikawaka. Madam S akainuka alipoketi na kumjongelea mtu huyo. Kofi moja kali lilitua shavuni mwa Pancho na kumwacha akitetemeka.

“Ulifikiri utafanikiwa kunikimbia? Twende nyumbani nikakuoneshe kama mimi ni Head of T.S.A,” Madam akaunguruma na kumpa pingu Amata naye akamfunga mikono yake na mnyororo akautia miguuni mwake. Akamkokota mpaka kwenye ile gari waliokuja nayo na Chiba mara ya kwanza.

“Nafasi yako ni kwenye buti tu, akamwingiza na kulifunga kisha akatulia nyuma ya usukani huku kushoto akimwacha Madam S.

“Chiba, Chiba, wapi?” Kamanda akauliza kwenye kile chombo chake.

“Naegesha boti nimefika,” akajibu.

“Weka kiberiti,” akampa agizo. Baada ya sekunde chache Chiba aliungana na wenzake na kuingia siti ya nyuma.

“Mzigo uko wapi?” akauliza Chiba.

“Upo mahala pake,” akajibu huku akiondoka eneo lile na kupita njia za vichochoroni.

“Kilomita ishirini na mbili kijiji cha Malve” Madam S alimwambia Amata na moja kwa moja akaelekea huko nje kabisa ya mji.

Hali ya utulivu ilitawala kijiji kile watu wote walikuwa wamelala ndani ya nyumba zao, ni miti tu iliyokuwa ikitikiswa na upepo wakati Amata akiegesha ile gari katika moja ya kichaka karibu na barabara kubwa inayoelekea baharini, barabara ya vumbi. Dakika mbili tu Scoba akatua na ndege ndogo aina ya Boeing yenye uwezo wa kubeba watu watano lakini yenye nguvu na kasi ya kutosha. Ndege hii ilinunuliwa na serikali ya Tanzania kwa kazi maalumu kama hizi na pia kwa ulinzi wa haraka wa Rais wa nchi inapobidi. Nje ya kumhudumia Rais, ni TSA pekee waliweza kuitumia ndege hii na ni kwa kibali cha Rais tu.

Scoba, akatumia barabara hiyo kutua kwa kutumia mwanga wa tochi alizowasha Madam S akiwa chini kwa ishara aliyompatia. Hakuna kusubiri, walimkokota mtu wao na kumpakia ndegeni, huku kwa mbali wakisikia ving'ora vya polisi vikielekea upande wao.

"Haraka, haraka, haraka," Madam alihimiza na mlango ukafungwa, Scoba moja kwa moja aliiongeza nguvu ile ndege na kuodoka kwa kasi huku akiwaacha wale polisi wakijaribu kufyatua risasi bila mafanikio. Dakika moja ndege ile ikawa angani ikikata bahari na kuelekea katika anga ya kimataifa ambako huna ruhusa kuifanya lolote.

- * *

"Na leo hii utatakiwa kusema siri zote ulizozificha mwanaharamu wewe!" Madam S alimwambia Pancho kwa ukali mara baada ya ndege ile kukaa sawa angani na kila mtu kuweza kufanya shughuli yoyote. Pancho Panchilio alitulia kimya akiangalia kwa jicho la kukata tamaa huku mwili wake ukionekana bado kukosa nguvu kwa kipigo cha rasha rasha alichokipata kutoka kwa Amata.

"Kamanda mwondoe hapa mpeleke kwenye chumba cha mwisho,"

Kamanda Amata akanyanyuka na kumchukua Pancho kwa kuushika ukosi wa shati lake, akamkokota mpaka katika chumba hicho na kumtupia humo. Mlango ukafungwa na ukimya ukatawala.

"Najua hauko peke yako kwenye mtandao huu, Mahmoud na mwenzake tulishawakamata wewe ukatutoroka kijanja. Na wale vibaraka wako wengine kule Kerege tumewakamata na wengine wamekufa wenyewe lakini wewe bado umetukimbia. Hukutukimbia tulikuwa tunaendelea kukuchunguza na sasa arobaini zako zimefika, haya nitajie mmoja baada ya mwingine kabla hatujatua Dar es salaam," Madam S alionekana kuwa na hasira kali juu ya mtu huyo. Pacho alibaki kimya hakuzungumza lolote.

"Jeuri!" Amata akasema, kisha ghafla akapiga teke kwenye korodani lililomfanya Pancho apige kelele za maumivu na kuikusanya mikono yake yenye pingu katika eneo hilo.

"Utasema?" Kamanda akauliza. Lakini Pancho bado alibaki kimya huku akigugumia kwa maumivu makali. Amata akachukua kiberiti cha gesi na kukiwasha kisha moto wake akauweka chini ya kidevu cha Pancho. Maumivu aliyoyapata kwa moto ule uliokuwa ukiichoma ngozi akashindwa uvumilivu.

"Aaaaaaiiigghhh! niache! niache! nasema! nasema!" akapiga kelele.

"Sema, upo na nani kwenye mtandao?" Amata akauliza.

"Kamba Sebule, Kamba Sebule," akataja jina la mtu mkubwa ambaye ni balozi wa nchi wa Tanzania katika nchi fulani.

"Na mna misheni gani hapa?"

"Mapinduzi ase aaaaiyyayayay aaaaiiiggghh! We muuaji wewe," akalia kwa uchungu.

"Mwingine nani?"

"Alibaki huyo huyo, aaaaaaghhh!"

“Hutaki kusema ee? Sasa nakutupa nje kwa huna faida wewe,” Kamanda akamwambia Pancho kisha akamtazama Madam S.

“Madam! Jishike vyema namtupa nje huyu mshenzi,”

Akabonyeza kitufe fulani na mlango ukafunguka taratibu, upepo mkali ukaingia ndani na kuleta ufumbufu mkubwa huku ndege ile ikiwa juu futi 40000.

“Utasemaaa au husemiii?” Kamanda aliuliza kwa kelele huku akimtazama Pancho. Akabaki kimya bila jibu. Amata akamsukuma na kumtanguliza kichwa nje, akamsukuma nje. Pancho akatoka mlangoni na kuning’inia vibaya.

“Aaaaaiihhhh, weweeeeeee! Niache nasema kila kituuu, ohhhhh! Nooooo!” Pancho akapiga kelele.

“Sema, mna misheni gani?”

“Mapinduzi, mapinduzi asee,” kutokana na upepo mkali Pancho aliyumba na kujigonga kwenye ubavu wa ndege. Kamanda Amata akatumia nguvu zake zote na kumvuta ndani akambwaga kando huku ule mlango ukijifunga taratibu. Pancho alipoteza fahamu na kutulia kimya.

“Kamba Sebule,” madam S akarudia jina hilo.

“Vipi?” Amata akauliza.

“Inabidi achunguliwe mara kwa mara asije kutupotea kuanzia sasa,” akajibu.

Madam S na Amata wakatoka katika chumba kile na kumwacha Pancho akiwa hajitambui damu ikitiririka usoni huku pingu na mnyororo vikiwa vimemdhibiti.

“Vipi?” Chiba akauliza.

“Poa, yupo huko kapumzika,”

“Yuko down?” (amekufa?)

“Hapana anaelea tu,” (hapana amezimia tu)

“Kinachoendelea?” Chiba akauliza.

“Kamba Sebule, yupo kwenye mtandao,” Amata akajibu huku akiketi sawia kitini. Chiba alibaki kakodoa macho kwa taarifa hiyo, hakutegemea mtu kama Kamba Sebule kuhusika kwenye mtandao wa maovu kama huo.

DAR ES SALAAM – saa 2:30 asubuhi

Saa tano ziliwaweka hewani na asubuhi ya saa mbili na nusu waliwasili uwanja wa ndege wa jeshi, Dar es salaam. Gari jeusi lenye boksi kubwa nyuma lilisogea taratibu mpaka kwenye ile ndege na kusimama jirani kabisa. Pancho Panchilio aliteremshwa na kuingizwa kwenye hiyo gari haraka na kufungiwa humo, askari wawili wenye silaha wakaingia pia sehemu ya nyuma, milango ikafungwa na safari ikaanza.

“Asanteni sana kwa kazi vijana,” Madam S aliwashukuru Amata na Chiba.

“Ndiyo wajibu wetu,” Chiba akaitikia.

“Sasa mpumzike kisha kesho jioni tuonane ili tuweke mambo sawa juu ya mtu huyu,” Madam akamaliza kusema na kuingia garini, Scoba akaondosha gari iliyombeba Madam S. Chiba na Amata waliingia kwenye gari jingine alilokuja nalo Gina wote wakaondoka uwanjani hapo.

Siku hiyohiyo …

BAGAMOYO

VIJANA KAMA SABA hivi walikuwa katika chumba kimoja cha jengo lililochini ya ardhi katika kisiwa kimojawapo kati ya visiwa vinne katika bahari ya Bagamoyo. Vijana hao wote walivalia mavazi meusi na kofia zao zilificha hadi nyuso na kuruhusu macho tu kuonekana. Mikono yao waliifutika kifuani na kufanya wote wawe katika mtindo mmoja wa kupendeza. Kati yao mmoja ndiye alikuwa na mkanda mpana mwekundu katika kiuno chake.

Vijana hawa walikuwa ni jeshi la siri sana la Pancho Panchilio, walikuwa wamefuzu mafunzo Ninjutsu huko Uchina kwa nyakati tafauti. Gabacholi huyu aliwaajiri na kuwaweka katika himaya yake, maalum kwa kazi maalum.

“Komredi ametekwa,” akawaambia wale vijana wengine.

“Usiku wa kuamkia leo pale Bombay, washenzi wamemchukua komredi na mpaka tunavyoongea sasa ameshafikisha hapa nchini,” akaendelea kusema; “hii inaonesha dharau kubwa sana kwetu, kwa kuwa wale jamaa tulifanikiwa kuwateka wote wakatutoka kwa namna ya kibabe sasa naona wametugeukia sisi. Hatuwezi kuwaacha, sasa ni vita na vita hii ninaitangaza sasa. Komredi lazima akombole ndani ya saa sabini na mbili hata kama atakuwa amefichwa Ikulu, ohi?”

“Oha!” wakajibu kwa pamoja kumaanisha kuwa wanajua na wanaelewa kile walichoambiwa, wakaiondoa mikono yao kifuani na kukutanisha viganja kisha wakainama. Baada ya mazungumzo mafupi wakatawanyika na wawili kati yao wakabaki pamoja na Yule aliyevaa vazi lenye mkanda mwekundu wakaketi katika meza hiyo ya duara pamoja wakijadiliana jambo.

“Tutatumia gharama yoyote tumpate,” mmoja wao akasema.

“Hilo ndilo hasa nalitaka tuzungumze, mambo waliyoyafanya Bombay kule si madogo, wamedhalilisha hekalu la Hanuman,” mwingine akadakia.

“Yote tuyaache, mpango wao ukoje mpaka sasa na wapi amehifadhiwa?” Yule wa kwanza akavunja mazungumzo.

“Kutoka chanzo chetu cha habari wanasema jamaa kahifadhiwa Keko, lakini kesho kutwa atafikishwa Kisutu mahakamani,” Yule kiongozi akajibu.

“Baaasi mpaka hapo kazi imekwisha, lazima atekwe ama anavyokwenda au anavyotoka,” mwingine akajibu huku akipiga ngumi mezani.

“Nani wa kulainisha mipango? Si unajua wote wapo lupango,” Kiongozi akauliza.

“Aaaaa Mkuu hilo ni dogo, Kamba Sebule na Maliapopo si wapo? Watafanya kazi,”

“Na hata hizi habari ni Maliapopo aliyenipatia na yuko sambamba na kila linaloendelea atatujulisha,” akamaliza na kuwaomba vijana wakae tayari kwa lolote watakaloambiwa.

GEREZA LA KEKO

PANCHO PANCHILIO aliketi sehemu ya peke yake, mikono yake ikiwa na pingu kama alivyoletwa siku iliyotangulia. Chumba chenye mtindo wa duara kilichojengwa kwa vyuma imara pande zote, ndimo alimohifadhiwa mtu huyo. Taa yenye mwanga mkali wa watts 750 ikawashwa na kummulika mtu huyo muda wote, joto kali likamtesa, mwili ukatota kama aliyemwagiwa maji.

“Aaaaaigh Shit!” aling’aka baada ya taa ile kummulika usoni moja kwa moja kila ajigeuzapo.

“Acha kupiga makelele ya kitoto bwege we!” Madam S alimwambia huku akisogea taratibu na vijana wake Chiba na Amata wakiwa nyuma yake.

“Kesho mahakamani,” akamwambia.

“Afadhali haki ikatendeke maana hapa mnanionea tu,” Pancho akajibu.

“Haki? Unaijua haki wewe? Ungeijua haki ungefanya yote uliyoyafanya? Pancho au nikuite Premji Kanoon, nchi iliyokulea unaweza kuifanyia haya? Kudhulumu haki, haki ya mwananchi mdogo anayevuja jasho la chumvi na kulilamba kwa kukosa maji safi ya kunywa lakini wewe na mabwanyenye wenzio wenye matumbo makubwa yasiyo na shukrani mnahamisha fedha na kuzificha ughaibuni,” akameza mate, na kuendelea, “Pancho! Kweli kabisa unadiriki kukifutilia mbali kikosi hiki unachokiona ili tu uendeleze biashara yako haramu, unaniteka mimi wewe, unateka vijana hawa uwaue halafu ufanye nini kwenye nchi hii? Kila anayekaribia kung’amua madhambi yako unataka ummalize. Siku yako imefika, nimekufuata India kwa gharama ili nikuoneshe kama mimi ndiye Madam Selina, mwanamke wa chuma tena chuma cha pua, kama kukuua ningeshakuua long time ila nilitaka kwanza nikuoneshe jeuri yangu kisha nikusweke jela maisha yako yote …”

“Kamwe, Pancho Panchilio hawezi kuingia jela, ha! Ha! Ha! hiyo sahau we mwanamke, utaiona miujiza yangu kabla ya kufika jela au hata mahakamani, mtatafutana ninyi nakwambia na hapo ndipo mtashuhudia mmoja mmoja wenu akianguka na kufa wakati mi narudi kuishi maisha yangu ya anasa. Ikitokea wewe ukabaki hai basi nitakualika kwenye tafrija kubwa pale Kilimanjaro Hoteli kisha utaona nani na nani wamealikwa, ndipo utakapojiona upumbavu wako we mwanamke ni mwanamke tu…”

Madam S alijikuta akishikwa na hasira akachomoa bastola yake.

“Rudia maneno yako nikupasue fuvu hilo,” aliongea kwa hasira.

“Ha! ha! ha! ha! Muoneni bibi yenu huyu, hana akili kabisa,” aliwaambia kina Chiba na Amata. Kama alifikiri anamuuzi mwanamama huyo pekee, basi alikosea sana, kitendo cha ghafla, Pancho alijikuta akipoke teke moja la kilo nyingi usoni, akajipiga kisogo ukutani kisha akaanguka sakafuni, kimya!

“Funga domo lako! Punguani wewe,” Amata akaunguruma. Sekunde chache Gabacholi huyo akajiweka sawa tena mara hii sura yote ilikuwa nyekundu.

“Tena wewe! Wewe! Wewe! Ipo siku yako. Nitakutoa huo utumbo niuanikie nguo,” Pancho alimwambia Amata.

“Utafanya hayo kabla bastola yangu haijafumua ubongo wako,” Amata akamaliza na kumtazama Madam S aliyekuwa amekunja sura kwa uchungu.

“Kesho Mahakamani,” Madam akamwambia Pacho na kugeuka kuanza kutoka ndani ya chumba kile maalum.

- * *

SIKU ILIYOFUATA

Asubuhi ya siku iliyofuata, Pancho Panchilio aliandaliwa tayari na kupelekwa mahakamni ili kusikiliza shitaka lake. Magari ya magereza na lile la FFU yalikuwa tayari mbele ya gereza hilo la Keko. Ulinzi mkali uliimarishwa kuzunguka ngome hiyo kwani taarifa kwa vyombo vya usalama ilikwishatolewa kuwa mtuhumiwa huyo ni mtu hatari sana. Vijana wa kazi walikuwa tayari kwa lolote.

Akiwa chini ya ulinzi mkali, Mhindi jeuri huyo alitembezwa taratibu huku miguu yake ikiwa imefungwa kwa minyororo na kisha mnyororo huo huo kuunganishwa na kuishika pingu iliyoifunga mikono yake. Msafari ulianzia Keko kuelekea Kisutu ambako shauri lake lilitakiwa kusikilizwa. Kwa kuwa barabara zote yaani ya Chang'ombe, Nyerere, Bibi Titi zilizuiwa magari kupita kwa dakika kadhaa, iliwachukua dakika kama kumi na tano tu kuwasili katika mahakama hiyo huku Pancho akiwa ndani ya gari maalumu iliyozibwa pande zote.

Mahakama ilifurika watu, kama kawaida, waandishi wa magazeti na wale wa televisheni walikuwa bize kutafuta habari lakini zaidi kuipata picha ya mtu huyo. Baada ya yote kukamilika na shauri hilo kuahirishwa, Pancho alitakiwa kurudishwa rumande mpaka baada ya mwezi mmoja ambapo ushahidi utakuwa umekamilika. Gari lile lililomchukua kutoka Gereza la Keko, ndiyo iliyokuja gerezani hapo kumbeba kwa mara nyingine na sasa ilikuwa na kazi ya kumrudisha mahabusu. Alitolewa akiwa chini ya ulinzi mkali mnyororo wake miguuni na pingu mkononi, moja kwa moja akaingizwa ndani ya gari hiyo isiyo na dirisha hata moja katika eneo la kuifadhi wahalifu. Baada ya kufungwa mlango wake askari wawili wenye silaha walikaa katika kijichumba kidogo wakiwa na bunduki zilizoshiba vyema.

Msafara ukaanza kutoka katika gereza hilo, gari la polisi likatangulia mbele likipiga ving'ora vya kuomba njia, kisha likafuatia hilo lililombeba mhalifu na mwisho kulikuwa na gari jingine la askari magereza wenye silaha, safari kuelekea Gereza la Ukonga na sio Keko tena ikaanza kwa kasi huku gari nyingine zikiacha njia na kuupisha ule msafara uende. Kasi iliyokuwa kwa gari zile haikuwa ya kawaida, kila mtu alishangaa na kujiuliza 'kuna nini?'

Wakati huohuo…

Barabara ya Shaurimoyo na Nyerere

Ndani ya gari moja lililoegeshwa muda mrefu katika Barabara ya Shaurimoyo, watu sita walikuwa kimya kwa muda mrefu, na mara ukimya ule ukakatishwa kwa biip moja ya simu ya kiongozi wao. Kutoka kiti cha mbele alichoketi akageuka nyuma na kuwatazama viajan wake.

"Mko tayari? Tunafanya kazi sasa, dakika tatu kila kitu kiwe kimekamilika, kwa kuwa wao hawajajiandaa kwa hilo basi itakuwa ushindi ni upande wetu, ohi?"

"Oha!" wakaitikia vijana wa kazi waliovalia nguo za khaki, na bunduki zenye risasi tele migongoni mwao, nyuso zao zilikuwa tayari kufunikwa na barakoa za kukinga gesi ya machozi, walikamilika.

Kiongozi wa operesheni hiyo aliinua redio yake ya upepo na kuiweka karibu na kinywa chake.

"Namba one, namba one, stand by!" akaongea.

"Umesomeka, namba one stand by," akajibiwa.

"Namba one on your marks… Get set… go!" Yule kiongozi alitumia mtindo unaotumika na wanariaadha kutimua mbio.

Kutoka upande wa Keko, karibu kabisa na eneo la daraja la leri pembezoni mwa Kiwanda cha Uchapaji cha Taifa, liliwashwa tingatinga na kuchomoka kwa kasi kuelekea barabara ya Nyerere. Hamad! Wakati ule msafara unafika na lile tingatinga linafika, ajali mbaya isiyosemeka ikatokea. Lile tingatinga likaigonga gari ya mbele ya polisi na kuharibu vibaya, haikuishia hapo, iliigonga ile gari ya kubeba mhalifu na kuikunga njia, ikaibana karibu na gema la daraja. Mtafutano wa watu ukaanza asubuhi hiyo katika eneo lile.

Kutoka kwenye lile gari la askari maalum wa magereza, waliruka na kutua nje kila mmoja akachukua sehemu yake kwa kuangalia nini kinatokea. Kabla hawajakaa sawa, gari aina ya Range Rover ikaingia kwa kasi na vijana kama sita hivi wakateremka haraka na kulizunguka eneo lile, mabomu saba ya machozi yakatua ardhini na wao wakavaa barakoa zao tayari kuzuia adha ya gesi ile ya machozi. Wawili kati yao haraka wakaenda

kuufungua ule mlango wa lile gari, risasi zikaanza kulindima kutoka kwa wale vijana wa magereza na polisi, wakashambuliana na wale majambazi. Jambazi mmoja akapigwa risasi na kudondoka lakini hakufa bali alijeruhiwa vibaya.

Mlango ukafunguka, mmoja wa askari bado alikuwa ana nguvu zake, alimpiga yule jambazi kwa kitako cha SMG kichwani, akapepesuka na kushindwa kustahimili akaaguka chini, Yule mwenzake akatumia risasi ya moto na kupiga askari wote wa ndani kisha akaingia na kumfungua bosi wake. Mabomu ya machozi yaliongezwa na mosi ukatapakaa eneo lote.

Yule jambazi aliyetoka na Pancho akapiga aina Fulani ya mluzi na wale wenzake wote wakakimbili garini, lakini jambazi mmoja aliyekuwa mwisho ambaye kiutaratibu lazima apande mwisho, akamchapa risasi yule jambazi mwenzake aliyekuwa na hali mbaya pale chini ili kuzuia asije ongea lolote, nukta hiyo hiyo ukasikika mlio wa helkopta eneo lile, nalo likazidisha vumbi, wale majambazi na mtu wao wakajitupa ndani yake na lile dege likapotelea angani.

“Upo Salama Mkuu,” Kiongozi akamwambia Pancho.

“Yeah, hongereni kwa kazi,” akawapongeza wakati huo wakimwondoa ile minyororo na pingu mikononi mwake.

“Ha! Ha! Ha! Ha! mmewapiga chenga ya mwili,” Pancho aliwasifu vijana wake kwa lugha ambayo Yule dereva hakuielewa.

“Ijapokuwa tunasikitika tumepoteza wawili,”

“Usijali, hiyo ni najali kazini,”

“Sawa Boss”.

Ilikuwa kama filamu hivi, kwa ughafla wa tukio lile ambalo halikuchukua hata dakika tatu, askari waliokuwa wakisindikiza mhalifu huyo walijikuta hoi. Wamezidiwa ujanja, ijapokuwa waliwapiga risasi wawili lakini wao walipoteza wawili pia. Utulivu ukarudi, kilichobaki kilikuwa na mtapakao wa moshi na harufu ya baruti inayoishia kwa upepo. Watu walikuwa wakisogea taratibu kuona kulikoni. Polisi nao walifika na kuweka ulinzi eneo hilo ikiwa pamoja na kufunga barabara.

Mkuu wa polisi mkoa wa Dar es salaam alikuwa hapo akiangalia hali halisi, sura yake ikikunja ndita sehemu ya juu ya macho yake, hasira isiyojificha ilionekana wazi wazi.

“Washenzi hawa,” akang’aka kwa hasira.

Wakati polisi wengine wakiendelea kupima hapa na pale yeye bado alikuwa akiendelea kuwasiliana kwa redio yake.

“Nipo eneo la tukio, mmeona helkopta yoyote ikipita maeneo hayo?” akawauliza polisi wa anga ambao daima kazi yao ni kuvichungulia vya juu.

“Vipi Mkuu?” sauti ya Inspekta Simbeye ilimfanya yule RPC kushtuka na kumwangali mtu huyo. Wakapigiana saluti za kijeshi kisha mazungumzo yakaendelea.

“Kwa hiyo wamekuja na helkopta mpaka hapa na kumchukua mtu wao?”

“Ndiyo, lilikuwa ni shambulizi la ghafla na la ufundi wa hali ya juu ijapokuwa hata vijana wetu wamefanya kazi kubwa mpaka kuwalaza hawa wawili, sema tu ndiyo hivi wameshakufa, laiti wangekuwa hai pangechimbika,” akamaliza kusema RPC na kumwacha Simbeye akikagua hapa na pale kuona kama kuna lolote la ajabu katika ajali hiyo, alitazama hiki akagusa kile, alipindua hiki na kusimamisha kile kule arimuradi tu afanye kitu.

SHAMBA

Mchana huohuo

Simu ya mkononi ya Madam S iliita kwa fujo, alipotupa jicho mezani akaona simu inayowakawaka ni ile ya taarifa nyeti.

“Shiit, nini tena?” akaongea kwa sauti ya kuonesha kuwa hajafurahia simu hiyo, akainyakuwa na kuitega sikioni kwanza.

“Hello Sellina!” mara moja akaitambua sauti hiyo.

“Ndiyo Simbeye vipi (…) what! Unasema, (…) acha masihara katika kazi asee,”

“…Madam habari ndiyo hiyo, Pancho Panchilio kaokolewa na jamaa zake kwa njia za kikomandoo”.

Madam S akakata simu na kuitupia mezani kisha yeye mwenye akajitupa kitini na kushusha pumzi ndefu. Akawaita vijana wake wote na kuwapa taarifa hiyo ambayo iliwachanganya mpaka wakachanganyikiwa. Lakini la kutokea tayari lilikuwa limetokea.

04

KIJIJI CHA MINDE – BAGAMOYO

“Babu! Babu!” kijana wa makamo alimwita babu yake huku akiwa anahema kama aliyefukuzwa na mbwa.

“We, nini?” babu yake aliyekuwa ameketi chini na wavuvi wenzake wakiwa wanasuka nyavu zao alimjibu kwa kumwuliza.

“Ame- ameam- amemka, yule mtu ameamka…”

Yule mzee akawatazama wale wavuvi wenzake na wote wakakurupuka na kukimbimbilia kwenye ile nyumba walimomlaza huyo mtu. Walipofika waliingia taratibu bila kufanya kelele na kumtazama.

“Oooh! Ameamka, asante binti kwa dawa ulizompatia,” yule babu alimshukuru binti aliyekuwa kando na chungu chake kikubwa kilichojaa maji ya kijani.

“Bila asante, ni wajibu wangu kumsaidia,” akajibu.

Wale wazee wakasogelea kitanda na kumzunguka wakimtazama, naye pia alizidi kuwatazama kwa kuwashangaa.

“Niko wapi? Niko wapi hapa?” akauliza kwa ukali na kumkunja kanzu mzee mmoja aliyekuwa jirani na yeye.

“Aaah a a a! kijana tulia kwanza, hapa upo mahali salama kabisa,” mzee mwingine alimsihi mtu huyo kwa lugha ya pwani.

“Wewe ni nani kijana?” Yule mzee akauliza.

Yule mtu akawashangaa tena, akawatazama na kuwakazia macho, kisha akajitahidi kukaa na kuegemea ukutani.

“Naitwa Amata,” akajibu kwa kifupi.

“Amata! Pole sana Amata, tumekuokota baharini ukisukwasukwa na mawimbi makali. Mungu mkubwa kwani yalikupeleka mpaka kwenye mikoko nasi tumekuona huko, nini kilikupata kijana,”

Amata akanyamaza kimya akifikiria jambo, akijaribu kuvuta kumbukumbu kwa lile lililotokea.

Saa 20 Zilizopita…

Ajali ya ndege.

Mara tu baada ya kiti cha Amata kufyatuka na kutoka nje wakiwa angani, parachute alilokuwa akitumia Amata likagoma kufyatuka, akahangaika nalo huku msukosuko ukiendelea. Kutoka kwenye ile ndege akaanza kuanguka kwa kasi huku akielekea baharini.

“Scobaaaaaa!!!!” aliita kwa nguvu lakini mwito wake haukuwa na nguvu kwani Scoba naye alikumbwa na maswahiba yake. Kutokana na lile parachute kushindwa kufunguka, Amata alitua baharini kwa kishindo na kuzama kwa sekunde kadhaa kabla ya kuibuka juu. Kwa mbali aliiona kitu kama boti ikija kwa kasi na kupunga mikono kuomba msaada lakini badala ya msaada wale jamaa wakafyatua risasi kumshambulia, Amata akapiga mbizi na risasi mbili zikampata eneo la mbavu. Maumivu yake yalimweka kwenye hali mbaya kiasi kwamba alijikuta akipoteza nguvu. Jua lilififia machoni pake, kiza kikayafumba macho, akajikuta anapoteza nguvu na ukimya mkuu ukamchukua.

“Nimekwisha!” akajitahidi kutamka kwa taabu.

“Ma-da-m S” akajitahidi kuita kwa nguvu lakini bado aliona giza likimzidi nguvu.

- * *

“Shabash, nimempata kwisha habari yake,” kijana mmoja alikuwa akishangilia kwenye ile boti. Huku akipiga risasi nyingine hewani.

“Una uhakika?” Mwenzake akauliza.

“We sogeza mashine pale uone, maiti tu ile,”

Ile boti ikasogea mpaka pale na kuukuta mwili wa Amata ukiwa kifudifudi juu ya maji baada ya kuibuka. Wakautazama na kuondoka zao.

“Buriani, hatuna historia ya kubeba maiti,” yule nahodha wa chombo akageuza na kuondoka zao mpaka katika kambi yao iliyojengwa katika moja ya visiwa vilivyozunguka eneo hilo huku bado wakipiga risasi hewani kuoneshya.

- * *

Mawimbi ya bahari yakausukasuka mwili wa Amata na kuutupia kwenye mikoko iliyofungana katika pwani ya eneo hilo, na kunasa huko. Jioni ya saa kumi na mbili hivi wavuvi kutoka kijiji cha Minde walikuwa wakipita kuelekea katika shughuli zao huko katikati ya bahari, wakiwa na karabai zao wakipita pembezoni kabisa karibu na ile mimea ndipo walipouaona mwili huo.

“We hebu mulika pale,” mzee mmoja akamwambia nahodha wa chombo hicho.

“Nini?”

“Yule siyo mtu Yule?” wakatazama kwa makini na kugundua ni mwili wa binadamu, wakashuka na kutumbukia majini mpaka eneo lile.

“Oh Shit, si ajabu akawa hai huyu, mtazame!” wakamgeuza geuza na kuamua kumbeba. Safari ya kwenda uvuvini ikaghairishwa na wazee wale wakaamua kurudi kijijini. Walifika na kumshusha Amata kisha wakamlaza chini mkekani huku wakisogeza moto jirani ili kumpa joto. Mzee mmoja alikwenda kumwita binti anayesifika kujua dawa za asili, akaja na kuanza kumfukizia Amata moshi wa mchanganyiko wa majani na magome makavu ya miti.

“Hajafa bado huyu?” mzee mmoja akauliza.

“Hapana hajafa huyu, ila amezimia na yuko mbali sana katika mzimio wake, ninamwita polepole ataamka tu,” yule binti akajibu.

Matibabu hayo ya kienyeji yaliendelea mpaka asubuhi yake na mchana wa siku hiyo Amata alirudiwa na fahamu

Siku ilofuata

Amata alitoka nje ya nyumba hiyo majira ya saa nne asubuhi, akasimama nje na kuangalia upande wa baharini, akiwa hajui ni wapi alipo mpaka dakika hiyo. Akiwa bado hajisikii vyema sana hasa sehemu fulani za mwili wake ambako kulikuwa na kitu kama jeraha aliendelea kutembea hapa na pale pale kijijini akiangalia hiki na kile. Kila hatua chache alisimama kutokana na maumivu aliyokuwa akiyasikia katika maeneo ya mbavu. Kila alkisjidhika aligundua kuwa kulikuwa na majeraha. Nyuma yake akahisi mchakacho wa nyayo za binadamu, akasimama na kusubiri.

“Naona una nguvu sasa,” sauti nyororo ya kike ikasikika nyuma yake, akageuka na kugongana macho na mwanadada mrembo aliyekuwa ndani ya mavazi ya kawaida kabisa ya kijijini.

“Ndiyo, sasa najisikia nafuu zaidi, ila maumivu tu eneo hili,” akamjibu na kumwonesha eneo lenye maumivu.

“Pole, unywe ile dawa niliyokupa, ndani ya saa sita mpaka kumi zijazo utajisikia sawa kabisa, ni dawa nzuri kwa majeraha kama hayo,” Yule mwanadada akamweleza.

“Unaitwa nani?” Amata akauliza.

“Minde!” akajibu huku wakiwa wanatazamana na Amata.

“Asante Minde, umeokoa maisha yangu, unastahili zawadi, zawadi kubwa kabisa. Niambie hapa ni wapi?”

“Hapa ni Minde,”

“Minde tena?” Amata akauliza kwa kupata uhakika.

“Ndiyo, usishangae, kijiji hiki kinaitwa Minde na mimi naitwa Minde,” yule mwanadada akamweleza Amata kisha akauchomoa mfuko wa plastiki ndani ya kanga yake kuukuu na kumpa Amata. Alipoupokea alihisi wazi uzito wa kiasi wa mfuko huo, akaufungua ndani na kuangalia, akatabasamu kisha akamwangalia binti yule kwa kumkazia macho.

“Minde!” akaita kwa sauti tulivu.

“Umevipata wapi hivi?” akauliza.

“Nimevitoa kwenye nguo zako ulizovaa,” akajibiwa. Kamanda Amata akavimwaga juu ya jiwe lililokuwa jirani. Kwanza akachukua bastola iliyokuwa hapo, akaivuta slider yake na kuirudisha, akaifyatua kitako na kuchomoa magazine iliyojaa risasi, akazipachua moja moja na baadae akazirudishia tena. Akamtazama Minde akamwona jinsi alivyojawa na woga.

“Mbona unaogopa?” akamwuliza.

“Mmm umejuaje kama naogopa?”

“Nikimwangalia mtu usoni huwa najua kila kinachofanyika ndani ya ubongo wake,” wote wakacheka.

“Basi we unafaa kuwa mtabiri!”

Amata akachukua waleti iliyokuwa pamoja na hivyo, akaifungua na kukuta kila kitu chake kipo salama, ndani yake licha ya vitambulisho kulikuwa na fuba la pesa za kitanzania kama shilingi laki tatu hivi, akachomoa noti kadhaa zilizofungwa vyema. Akazihesabu harakaharaka zilikuwa shilingi laki moja.

“Hii zawadi yako Minde,” akamkabidhi, binti yule akamtazama Amata kwa jicho la uchu na kumshukuru kwa kibantu. Amata alimkumbatia Minde mikononi mwake huku akimwangalia usoni na kuyaona macho yanayojaa machozi.

4

“Minde, nahitaji kuondoka sasa, nitakuja kukusalimia tena,” akamuaga lakini ilikuwa ngumu kwa Minde kumruhusu Amata kutoka pale, alimbembeleza akae japo siku moja zaidi lakini Amata alijua wazi kuwa kwa vyovyote wenzake watakuwa wakimtafuta. Akaichukua saa yake sasa hii ilikuwa ya mwisho kuitoa katika ule mfuko, akaizungusha mahala fulani na kutazama kwenye kioo, kisha akamtazama Minde.

“Hapa ni Bagamoyo?”

“Ndiyo”

Baada ya kama saa tatu hivi, Minde alimruhusu Amata kuondoka kwa minajiri ya kuonana tena, Amata akaagana na wale wazee na kuanza kufuata barabara taratibu kuelekea barabara kubwa ambapo angepata usafiri wowote.

MASAKI – saa 1:30 usiku

MADAM S alisimamisha gari ndani ya uwa wa nyumba yake na kuruhusu lile lango lijifunge lenyewe nyuma yake. Aliposhuka garini akavuta hatua kuelekea mlango mkubwa wa kuingilia ndani huku akitumia simu yake ya mkononi kuzima kengele za hatari ambazo huziacha zikifanya kazi kama yeye hayupo. Akaufungua mlango na kuingia ndani alipouelekeza mkono wake kuwasha taa, taa zikawaka zenyewe na sebule yote ikang’azwa na mwanga wa kupendeza.

Madam S alipigwa na mshangao, akabaki akikodoa macho huku mkono wa kuume ukiwa tayari na bastola kiganjani.

“Amani iwe nawe!” sauti ya Amata ikasikika.

“Uhhhhh! Siku nyingine utakuja kufa wewe, kwanza ulikuwa wapi?” Madam S akaanza kufoka huku akishusha pumzi ndefu.

“Nilikuwa kuzimu, na sasa nimefufuka katika wafu,” Amata akajibu.

“Shiiiit! Mzima wewe? Au mzuka!”

“Njoo unipapase maana mzuka hauna mifupa wala nyama,” Amata akajibu.

“Oh! No, hebu ujinga wako…”

Madam S akainua simu yake na kubofya tarakimu fulani fulani kisha akaweka sikioni na kusungumza na mtu wa upande wa pili.

“Hello (…) sawa, njoo haraka nyumbani kwangu,” alipomaliza hayo akakata simu.

Moja kwa moja akakiendea kiti kilicho mbele kinachotazamana na mgeni wake huyo huku bado bastola yake ikiwa mkononi.

“Ina maana bado hujaamini kama ni mimi?” Amata akauliza kwa mashaka.

“Watu ni wataalam huweza kujigeuza vyovyote watakavyo…” Madam akajibu huku sura yake bado ikionesha shaka kuu, “kweli wewe ni Amata?” akamuuliza tena.

“Ndiyo Madam!”

“Jina lako lingine…”

“Mr. Spark!”

“Lingine…”

“Inspekta Jaffary…”

“Na ulilotumia Arusha kwa Abiseilim…”

“Jaffari Makono…”

“State of Living…”

“Living of state!”

“Good!” Madam akaafiki na kuirudishia usalama bastola yake kisha akaitia katika pochi. Hatua nne nyingine zikamfikisha katika jokofu, akatoa pombe kali na bilauri tatu, akaja nazo mezani na kuketi, akajimiminia na kumpatia Kamanda kisha akajiegemeza kitini na kumtazama kijana huyo kwa makini.

“Nini kilikupata Amata, na ulikuwa wapi?” akauliza. Amata akainua fulana yake aliyoivaa na kumuonesha Madam S jeraha la risasi kwenye nyama za ubavu wake. Lilikuwa jeraha bichi kabisa lililoonesha dalili zote ya kuwa bado linahitaji tiba ya kitaalamu.

“Shiiiit! Risasi?”

“Ndiyo!” akajibu na kunyamaza kwa sekunde kadhaa, akavaa fulana yake na kuinua bilauri iliyojaa pombe, akapiga funda moja la maana kisha akaitua mezani kwa kishindo.

“Sifi tena kama hii haijaniua,” akajibu huku akifunika na kumwacha Madam S akiwa kinywa wazi kisha Amata akamsimulia kila kilichomsibu.

Hadithi ile ya kuogofya ilimfanya Selina atahayari, mara kadhaa alionekana akifinya macho, mara nyingine akishtuka na kadhalika. Hakuamini jinsi ambavyo kijana wake amepona katika hali isiyoelezeka.

“Tumshukuru huyo mwanadada aliyekupatia tiba ya mitishamba, si tungeshakukosa!” Madam akamwambia.

“Hata wale wazee pia ambao wameniokota, washukuriwe…”

“Of coz!” Madam akamwambia a kutulia huku akiitazama simu yake, kisha akamtazama tena Amata.

“Kamanda Amata, nilishatakiwa kutangaza kifo chako lakini nilikataa na kuwahakikishia kuwa upo hai kwa sababu najua wazi kuwa ni Mungu atakayeichukua roho yako lakini si binadamu mwingine awaye yote,” Madam akaeleza.

“Umenea sawa, vipi kuhusu Scoba?” Amata akauliza maana hakuwa akijua chochote kuhusu mtu huyo.

“Scoba tulimpata usiku wa siku hiyohiyo, sasa ni mzima na anaendelea vyema, hataki kabisa kusikia habari za kuwa wewe umekufa,”

“Yuko wapi?”

“Shamba. Bado yuko shamba na hatuwezi kumwacha hadharani, tuliliweka hivyo ili kuhakikisha kuwa tumekupata kama si wewe basi mwili wako,” Madam akaeleza.

“Nipo hai, na ninaishi kwa mara nyingine tena, je; mlifanya lolote kwa kumsaka Pancho?”

“Hapana kamanda, tuliliacha kama lilivyo, tuliona kwanza tuhakikishe habari ya wewe kisha ndiyo tujue kama ni kuweka matanga au kama ni kufanya sherehe…”

“Fanya sherehe…” Amata akadakiza kusema.

“Mpenzi wako Gina hana raha kabisa kwani hata yeye ana huzuni na kifo chako,” Madam S akaendelea kuzungumza na Amata juu ya tukio hilo lililowapa mshtuko mkubwa na kuwafanya kiasi fulani kutikisika.

Wakati huohuo honi za gari zikasikika getini Madam S akabonya swichi maalumu iliyowekwa ukutani na kuruhusu geti hilo kufunguka. Gari dogo aina ya RAV 4 likaingia ndani. Amata akasimama pale alipo na kulitazama gari hilo likiingia taratibu.

Jasmine! Akawaza na kurudi kitini.

Hali ya Jasmine ilikuwa ileile pindi tu alipoingia nyumbani kwa Madam S, alipatwa na mshtuko alipomuona Amata pale kitini.

“Ni wewe? Amata nooo!!!!” akapagawa na kumkumbatia kwa nguvu hapo hapo kitini, “sijui Gina atafurahi kiasi gani akikuona, maana nahisi karibu anarukwa na akili kwa kukukosa…” akalalama. Baada ya mazungumzo ya kina, Amata alimwonesha Jasmine lile jeraha ubavuni mwake. Naye kama daktari akalitazama kwa mbali na alipoona hawezi kujua vyema ukubwa wa jeraha hilo akachukua mipira ya mikono na kuivaa, kisha akalitomasa taratibu kila upande.

“Asssss!!!! Taratibu bwana!” Amata akagugumia maumivu.

“Nilitaka nijue linauma kiasi gani, risasi au kitu gani?” akahoji.

“Risasi!” Amata akajibu wakati Jasmine akitulia kwenye stuli.

“Inabidi tusafishe,” akamwambia.

“No, nina dawa nimepaka hapo, huo weusi sio uchafu,” akamjibu.

“Risasi wameitoa? Lazima nijue…”

“Mi sijui, nilipostuka nimejikuta nagangwa tu!”

“Good, lazima tufike Shamba ili niweze kutazama kwa Ultra Sound, nijwe na uhakika kama imetoka au bado ipo,” Dkt. Jasmine akamwambia Amata.

“Sawa dokta! Utahitaji kunichoma sindano?”

“Sindano muhimu, yaani ushujaa wote huo unaogopa sindano?”

“Sindano ni sindano mama!!!”

“Ok, hata hivyo inabidi sasa kwenda pamoja Shamba tukaweke mikakati yetu vizuri hakuna kulala,” Madam aliwaeleza vijana wake na wote wakajipanga kuondoka. Chiba na Gina nao wakapewa taarifa za kufika huko usiku huo

Usiku huohuo…

Madam S, Amata na Jasmine walikuwa kundi la kwanza kuwasili katika afisi hizo za siri. Moja kwa moja walimfikisha Amata katika chumba chao kidogo ambacho kwacho uganguzi wote na utabibu hufayika. Kilisheheni mitambo tiba ya kisasa ambayo ingeweza kuwekwa kwenye hospitali kubwa lakini hapa iliwekwa

kwa kazi maalumu. Amata akafikishwa ndani ya chumba hiki na kutakiwa kulala juu ya kitanda ambacho juu yake kulifungwa taa kubwa yenye mwanga mkali pamoja na vifaa vingine.

SHAMBA

Akiwa hana fulana wala suruali isipokuwa nguo maalum aliyotakiwa kuvaa, alitulia kimya kitandani. Jasmine akawasha mtambo huo na kuweza kufuatilia kila kilichoonekana katika luninga yake pale ukutani. Baada kama ya dakika tano za kumulika huku na huku akakipachika kidubwasha 'Transducer Probe' kile mahala pake. Akashusha pumzi na kumtazama Madam S.

"Vipi?" Madam akauliza.

"Hamna kitu, risasi kama ilikuwepo basi wameshaitoa kwa njia yao, na kinachonishangaza ni kuwa hili jeraha liko vizuri tu kwa ndani kasoro hapa nje tu, na panaonekana kuwa panaendelea vizuri, kweli hizi dawa za shamba zina nguvu," Jasmine akamwambia Madam S.

"Haya kaa!" Amata akaambiwa naye akakaa juu ya kile kitanda.

"Unajisikiaje sasa?" Madam S akamuuliza.

"Niko poa, unaweza kuingia kazini?"

"Kama kawaida, na ni lazima nimtie mkononi huyu Premji anayejiita Pancho!" Amata akajibu.

"Noooo! Hauna budi kupumzika kwa saa sabini na mbili kabla ya mikiki mingine haijaanza…" Jasmine akamwambia.

"Sawa dokta…"

- * *

Chiba na Gina waliingia katika jumba hilo kwa nyakati tafauti na kujikuta ndani wakiwa hawajui nani na nani wamekwishafika. Kwa jinsi jumba hilo lilivyojengwa kwa ndani, huwa ni vigumu kutambua nani kaingia na yuko wapi. Kila mmoja alikuwa na chumba chake kilichokuwa na kila kitu na angeweza kukaa humo hata mwezi pasi na kutoka nje. Zaidi ya hapo kulikuwa na chumba cha mikutano, chumba cha mazoezi 'GYM', baa ndogo, jiko, na afisi tafauti. Kama ukikaa katika afisi ya Chiba ungeweza kujua wote waliongia ndani ya nyumba hii kwani ni yeye tu anayeweza kuona kwenye kamera za usalama milango yote ya kuingili humo ndani na maeneo mengine. Iliitwa SAFE HOUSE kwa sababu inaweza kumficha mtu na asionekane katika jamii kwa muda usiojulikana. Kulikuwa na sehemu ya kuhojia wahalifu, ikiwa imesheheni kila zana ya kutesea, kulikuwa na chumba cha matibabu na maegesho ya magari ndani kwa ndani. Kwa ujumla jumba hili lilikuwa na sehemu kubwa mbili yaani 'ground floor' na 'underground floor'. Ground Floor ilikuwa ni nyumba ya kawaida sana ambayo wageni wote waliokuja kwa siri walifikia hapo. Underground floor ndiyo ilikuwa na hayo makolokolo yote, na mlango wa kuingilia ilikuwa ni siri yao. Mhalifu yeyote aliyefikishwa hapo aliondolewa sox ya usoni pindi afikapo katika chumba cha mahojiano na si zaidi ya hapo. Lakini 'Shahidi' alifikishwa katika 'ground floor' na mambo yake yalifanyikia hapo. Hakuna aliyekuja katika jumba hili macho wazi zaidi ya TSA, hata Mheshimiwa Rais akitaka kufika hapa lazima afichwe sura yake asione wapi anakwenda.

Kikazi iliitwa Safe House na kimaisha waliita Shamba.

Madam S na Kamanda Amata wakapanda ghorofa ya juu kutoka shimoni ili kukutana na wapendwa wao. Ilikuwa furaha ya aina yake walipokutana tena na Kamanda Amata, kila mmoja alikuwa na hamu ya kutaka kujua hasa ni nini kilimsibu mwenzi wao huyo hata kutoweka kwa siku hizo tatu kama sio nne. Gina ndiye

haswa aliyeonekana kuchanganyikiwa zaidi kwa kumwona Amata hakuamini kabisa kwani alishajua mtu amekufa alikuwa akisubiri tu taarifa ya kiofisi.

“Mmefurahi sana ee?” Madam S akawauliza.

“Ndiyo maana yake, hii ni furaha ya kukutana pamoja maana tulikwishachanganyikiwa,” Chiba akaeleza.

“Ok basi sherehe iishe na sasa tuangalie kazi,”

Wote wakaketi vitini katika meza yenye umbo la yai huku wakimwacha madam S upande wa peke yake kama kiongozi.

“Hatutakiwi kuchelewa kwani adui yetu anaweza kututoroka na tusimwone tena,” ilikuwa ni sentensi ya kwanza katika kufungua kikao hicho kutoka kwa Madam S. Na wote wakatikisa vichwa.

“Tunapaswa kuingia kazini, tukamsake huyu mwanaharamu, tumtie nguvuni, hastahili kuishi nje ya gereza,” akaendelea kuongea mara hii akionekana wazi kuwa ana hasira moyoni mwake.

“Sawa Madam, sasa tunajipangaje kwa maana bila shaka pale walipodunguliwa Scoba na Amata ndipo kwenye makazi ya mtu huyo ijapokuwa hapajaonekana wazi,” Chiba akaeleza wasiwasi wake.

“Ndio, msako huu utafanyika katika eneo hil…”

“Ina maana mpaka sasa Pancho atakuwepo bado? Nina wasiwasi atakuwa keshaondoka nchi hii,” Gina alimkata kauli Madam S.

“Yupo hajaondoka, tulidhibiti njia zote za kutokea nje ya nchi kuanzia viwanja vya ndege, bandari mpaka stendi za mabasi na hasa kule mipakani, kila basi linapekuliwa kwa umakini na kila abiria anafanyiwa uchunguzi wa kina kwani anaweza kujibadilisha sura na akaondoka. Kwa jinsi hiyo hatujapata jibu kama amekamatwa,” Chiba alieleza.

“Kwa hiyo yupo,” Scoba akaeleza.

“Kamanda Amata ana jeraha yampasa kupumzika kwani hawezi mikikimikiki kwa sasa,”

Jasmine aliliambia jopo, ndipo na wengine wakapata kujua kuwa Amata alikuwa amejeruhiwa.

Wote wakageuka kumtazama kwa huruma.

“Alikwambia nani, hii show tunaingia wote jukwaani na lazima mtu huyo akamatwe ndani ya saa 24 kutoka sasa. Hata kama ni kukodi vifaru, tutakodi na kuchimbua eneo lote lile,” Amata akawajibu.

“Ndio maana nakupenda mpenzi,” Gina akamalizia.

“Art of War,” Kamanda akamwambia Gina huku akimtazama usoni kisha wote wakacheka.

Simu ya mkononi ya Madam S ikaita, akaitazama kwenye kioo na kukunja sura kisha akawatuliza kwa ishara ya mkono na kuiweka sikioni ile simu wakati huo Chiba akiwa tayari keshapachika kifaa chake cha kurekodi sauti hiyo.

"…na kwa sababu mnajifanya mnajua, sasa sikilizeni redio usiku huu mtaelewa kuwa sitaki kutaniwa…"

Na ile simu ikakatika baada ya sauti hiyo ya mkoromo kukoroma sikioni mwa Madam S. Private number! Akawaza Madam S na kuishusha taratibu.

Sura ya Kamanda Amata ikabadilika na kuwa sura ya kazi, akatazamana na Madam S wasipate jibu wakatia huo, Chiba aliondoka na simu ya Madam S na kuingia katika chumba chake cha kazi kuifanyia uchunguzi simu hiyo ilipigwa kutoka uelekeo gani.

"Pancho Panchilio au kibaraka wake, hawezi kuwa mwingine, atapatikana tu," Chiba akajibu.

"Hawana maisha marefu, Sun Tzu ametufundisha kwenye Art Of War 'If the enemy leaves door open, you must rush in…'" (Kama adui ameacha mlango wazi, fanya hima kuingia) Amata akasema huku akijiweka vyema kitini, "adui yetu kaacha mlango wazi, tusichelewe!" akamalizia. Madam S akatikisa kichwa na kumtazama Gina.

"Gina, fanya kazi niliyokupa sasa," akamwambia binti huyo. Gina naye hakuchelewa akasimama na kuondoka katika chumba hicho.

Saa 7 Usiku…

Hali ya hewa ya Jiji la Dar ilikuwa tulivu kabisa, giza nene lisilo na mbalamwezi lilitawala wakati Gina akiegesha gari lake eneo la Upanga katika barabara ya Ally Hassan Mwinyi, karibu kabisa na hoteli ya Palm Beach. Kamanda Amata akiwa ameketi upande wa kushoto katika kiti cha abiria, aliiweka vizuri bastola yake tayari kwa lolote.

"Vipi?" Gina akauliza.

"Sina utani na mtu sasa hivi," Amata akamjibu Gina, kisha wakateremka garini, "vijana wako wapi?" akauliza.

"Wameshafika tayari wapo kwenye pozisheni zao," Gina akajibu. Kisha wakavuta hatua kuielekea hoteli hiyo ambayo siku hiyo ya wikiendi watu walijazana kwa starehe mbalimbali.

- * *

KAMBA SEBULE alikuwa akifurahia maisha ndani ya ukumbi mkubwa uliokuwa na michezo mbalimbali ya kujipatia pesa. Akiwa na walinzi wake binafsi, alijumuika pamoja na wengine wengi waliokuwa hapo kutafuna maisha. Si kwamba walifanya hivyo kwa sababu ya ukata ili wajipatie pesa ya kujikimu, la, walikuwa na ukwasi wa kutosha, walijumuika ili kuzichezea na si kucheza. Furaha haikuweza kujificha katika nyuso za wote waliozunguka eneo hilo huku wadada warembo wakitumbuiza kwa muziki uliokuwa ukipigwa mubashara kutoka jukwaani, wakicheza kwa minenguo ya Kikongo huku wakiwa wamevalia nusu utupu. Mijanaume yenye uchu ilikuwa imezunguka jukwaa hilo lililojengwa juu kidogo na kutazama wadada hao wakifanya mambo yao hadharani, macho yakiwatoka pima kana kwamba wakitazamacho kitaanguka ili wakigombanie.

Kamba Sebule, kigogo wa serikali, aliendelea kuburudika na rafiki zake waliofanana na yeye kiuchumi, waliokuwa wakicheza 'poker' na wakati mwingine 'Lucky Wheel' na kufurahia pesa waliyokuwa wakiivuna. Mmoja wa walinzi wake alionekana kuchezwa na machale kidogo, akatoa kitu kama picha katika mfuko wake wa shati na kuiangalia kwa sekunde kadhaa kisha akairudisha mfukoni, na kumwinamia Kamba Sebule, akamnong'oneza kitu.

- * *

Gina na Amata walijichanganya ndani ya ukumbi huo, wakipenyapenya katia ya watu wengi waliokuwa wakienda huku na kule na macho yao yakifanya kazi ya ziada ya kutazama huyu ni nani na nani ni huyu.

“Nahisi wametugundua,” Gina akamwambia Amata.

“Ndiyo nimeona, yule mtu inaonekana ana picha ya mmoja wetu, kwa nini katembea nayo?

Lazima tuipate na tujue kaipataje,” Kamanda Amata akamwambia Gina.

“Wanatutazama,” Gina akamwambia Amata.

“Ndiyo, ondoka nenda chooni, wakija nami nakuja hukohuko,” Amata akatoa maelekezo na Gina akayafuata bila kuhoji. Akavuta hatua kuelekea chooni, kama alivyofikiria Amata ndivyo ilivyokuwa.

Daima akili zetu zipo namna hii! Amata akajiambia kisha akendelea kuweka jicho lake kwa watu hao. Yule mlinzi mmoja akambonyeza mwenzake na wote wawili wakatoka kuelekea kule chooni wakamwacha Kamba Sebule na mlinzi mwingine mmoja, wakiahidi kuwa wanarudi muda tu. Kamanda Amata naye akajinyanyua taratibu na kuelekea upande uleule.

Gina aliingia katika choo cha wanawake, ndani ya kichumba kidogo, akafungua maji na kusimama kando, dakika moja ikapita, akafunga maji, akajiweka tayari huku akipiga mruzi na kufuatisha wimbo uliokuwa ukisikika kutoka ukumbini. Akafungua mlango kutoka nje na ndipo alipokutana na vijana hao. Gina akajifanya kupita katikati yao kama hajui kinachoendelea.

Mmoja wa wale walinzi akamzuia kwa kifua chake kipana asipite, Gina hakuuliza wala hakupoteza muda, alimsukuma kando akadakwa na Kamanda Amata kwa nyuma. Amata akamgeuza na kumpiga kichwa kisha akamdaka kolomeo kwa kono lake la kulia na kumfanya mtu huyo aanze kutapatapa kutafuta pumzi.

Gina aligeuka ghafla na kumchapa ngumi nzito yule wa nyuma yake, nae akajibu shambulizi lakini Gina alikanyaga mguu wake ukutani na kuepa shambulizi hilo, alipotua chini alimpa pigo moja la karate lililompata barabara na kumwacha akiwewe weseka alipotulia alijikuta mbele ya domo la bastola ya mwanamke huyo. Kamanada Amata aliendelea kumbana kolomeo yule jamaa mwingine huku akimhoji.

“Nani bosi wako?” Amata akauliza.

“Kamba, Ka-ka-mmmbbba!” akajibu kwa tabu huku akianza kulegea.

“Makazi ya Kamba yako wapi?”

“U-pa-ngggga!”

“Ofisi yake iko wapi?”

“Mtaa wa Ka-ka-lu-ttttaaaa namba 25!” akajibu na kuanza kutapatapa kwa nguvu.

Yule jamaa aliyetazamana na domo la bastola ya Gina akajaribu kutafuta mbinu ya kujiokoa wakati huo nje ya choo hicho walisikika watu wakiingia kujisaidia. Gina akashusha bastola yake na kuifutika kiunoni, kosa. Yule jamaa akarusha ngumi iliyompata Gina usoni na kumyumbisha kiasi fulani. Ngumi ya pili Gina akaudaka mkono na kuuzungusha kwa nguvu.

“Aaaaaiiiiiggggghhhh!” akatoa yowe la uchungu, huku mifupa ya mkono ikiachana, akamrudisha mbele na kumpiga futi la kwenye korodani kabla hajajibwaga chini na kujipigiza kwenye sinki la kunawia maji na kutulia sakafuni akikoroma. Kamanda Amata akafungua mlango wakatoka na Gina na kuwaacha watu wakitukana na kusonya huku wakiingia ndani kujisaidia.

“Mama majambaziiiiiiii!” ilisikika sauti ya kike ikipiga yowe kutoka chooni.

Pameharibika! Kamanda akawaza na moja kwa moja akamshika mkono Gina na kurudi ukumbini, hali ya taharuki ikaugubika ukumbi huo, walinzi wa hoteli wakaingia kuangalia kulikoni.

“Ita vijana,” Kamanda akamwambia Gina, naye akachomoa simu yake ya upepo na kuwaita waingie. Moja kwa moja walisimama kwenye ile meza ya ‘poker’.

“Upo chini ya ulinzi, Kamba Sebule,” Gina alimwambia huku Kamanda Amata akiwa kasimama pembeni, bado kulikuwa hakujatulia. Mheshimiwa huyo alitulia kimya macho yake yakiwa juu ya ile meza yakiangalia karata zilizopangwa juu yake.

“Wewe ni nani, na una mamlaka gani ya kuniambia mimi hayo?” Kamba akauliza bila kugeuka.

“Tii sheria bila shuruti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo iliyonipa malaka hayo,” Gina akaunguruma.

“We mtoto wa kike hivi ushawahi kuzaliwa? Hujui I ni sawa na baba yako mzazi?” Kamba akalalama.

“Kamba Sebule sitaki kutumia nguvu kwani nimekuja na nguvu kubwa kuliko unavyofikiri,”

Kamba Sebule akageuka taratibu na kukutana na sura ya Kamanda Amata, hakuamini kama ni mtu kweli au mzimu. Akarudisha macho kwa Gina na kukutana na sura ya mwanamke mrembo lakini isiyoonesha hata chembe ya tabasamu. Akatanabahi kwa vijana walioingia ndani ya ukumbi kwa dakika moja iliyofuata, walikuwa na nyama za kimazoezi, fulana zilizowabana zilidhihirisha hilo.

“Huna adabu msichana!” Kamba akaunguruma na kuchomoa simu yake lakini kabla hajaiweka sikioni ilinyakuliwa na Amata, na alipotaka kuleta tabu Gina alimtandika pigo moja uso na kumrudisha mezani akiwa hoi.

“Tia pingu!” akawaambia vijana wa polisi nao wakatekeleza na kuondoka naye.

05

“Kijiji chote kimeteketezwa kwa moto!” Mkuu wa nchi alisikika akiongea kwa kututumka, mbele yake alikuwa Madam S amesimama.

“Huyo ni shetani! Lazima utawala wake usambaratishwe na watenda mema,” Madam akajibu.

“Sikiliza Sellina,” akasimama kwa msisitizo, “Nahitaji uchunguzi wa siri na ikiwezekana huyu mtu akamatwe,” akasisitiza.

“Najua wajibu wangu mheshimiwa, mzuie Waziri wa Mambo ya ndani asitumie nguvuy kubwa, acha mimi nikafanye kazi, ikifika wakati wa kuhitaji vijana wake nitakwambia, ila kwa sasa waache wale wa Bagamoyo kwa kuwa ni eneo lao, naondoka sasa,” akamaliza Madam S na kutoka mle ofisini.

Akiwa ndani ya gari yake akampigia Amata na Gina wakutane ofisi ndogo, akaitazama saa yake tayari ilitimu saa 4 usiku.

Kweli kazi za serikali ni za kujitolea, watu wamelala sisi tunahangaika! Akawaza mwenyewe huku akiliacha langa la Ikulu na kuelekea afisini kwake.

KITUO CHA POLISI CHA SULENDER BRIDGE

“Bagamoyo, Ba- ba –gamo-yo koh! koh! koh!” Kamba Sebule aliongea mengi baada ya kipigo cha polisi kukolea mwilini mwake kwa amri ya Kamanda Amata.

“Bagamoyo kubwa, sehemu gani?” Kamanda akauliza.

“Si nime-wa-jib…”

Mkanda wa jeshi ukatua mgongoni mwake na kumletea maumivu makali.

“Unafikiri tunacheza hapa? Tuambie ni kijiji au ni sehemu gani?” mmoja wa polisi aliuliza.

“Kisi-wa-wa-ni, Kale-b-be” mwishowe akatamka ijapokuwa kwa tabu kidogo.

Kamanda Amata akatikisa kichwa juu chini huku akimtazama Gina. Simu yake ikaanza kufurukuta mfukoni akaitoa na kutazama ‘Madam S’ ilijiandika juu ya kioo, akaingiza tarakimu fungushi na kuiweka sikioni.

“Tukutane wodini haraka mama anaumwa Tena Sana Aisee,” ilikuwa ni ujumbe wa sauti aliyoutuma. Akageuka na kumtazama Gina, kisha akarudisha macho kwa wale vijana wa polisi.

“Sasa muhifadhini huyu mpaka nitakapowapa amri nyingine, sisi tunatoka,” akawaambia wakati wakiondoka na kuingia garini.

- * *

OFISINI NDOGO

Ndani ya ofisi hiyo Madam S alikutana na vijana wake wote watano, aliwapa ujumbe aliyoupata kutoka Ikulu ambako kama kawaida yake alikwenda kupeleka ripoti ya siku. Kwa harakaharaka alionekana hayuko sawa kwani alikuwa akifanya vitu na kuongea kwa harakaharaka.

“Kijiji cha Kitopeni kimevamiwa na kuchomwa moto huku raia wakipigwa vibaya leo jioni hii,” madam aliongea harakaharaka huku akiwa kasimama wima.

“Kitopeni Bagamoyo?” Gina alidaka kwa swali.

“Ndiyo!”

Wakatazamana kisha wakarudisha macho kwa Madam S, hakuna aliyekuwa na swali wala kuongea ila ndani ya macho yao kulibaki na mshangao wa dhahiri kabisa. Walikijua kijiji huki vema kwa sababu ndipo walipomuokota Scoba majuma kadhaa nyuma.

“Kitopeni ndo wapi?” Amata aliuliza.

“Ni usawa ule ambao ndege yenu ilidunguliwa,” akajibiwa na Madam S.

“Bila shaka ni wao, haina kupoteza muda TSA Kazini,” Chiba alisema huku akinyanyuka na kuungwa mkono na wenzake.

“Bila shaka, nimezuia polisi wa huku kufika kule kwanza nataka sisi tuingie kwanza ili tufanye uchunguzi wa awali ambao kwetu ni uchunguzi wa msingi wa kumjua mhalifu,” madam S aliwaambia kisha kila mmoja akaanza kuchukua kinachomfaa katika stoo iliyojengwa ndani humo.

“Kamanda Amata, una jeraha, halijapona, ni vyema usifanye mikiki mikiki yoyote ile,” Jasmine alimwambia Amata.

“Hapana, wacha niende, kama ni Pancho basi mara hii hatakiwi kuishi, huu ni uhalifu mkubwa sana haijawahi kutokea kwenye historia ya nchi hii,” Amata akaunguruma.

Dakika kumi zilizofuata, Land Cruiser V8 ilifuatana na Range Rover zote zikielekea Kitopeni, ndani yake kulikuwamo na hao vijana watano. Gari ya kwanza alikuwapo Amata, Chiba na Gina ambaye aliukamata usukani na ile ya nyuma alikuwamo Jasmine na Scoba pamoja na Madam S. mwendo waliokuwa wakipita nao ulikuwa si wa kawaida. Kama wananchi walizoea kuishangaa misafara ya viongozi kwa mwendo kasi basi hii ilikuwa funga kazi ila hakuweza kuona kwa sbabu tayari ilikuwa usiku.

Kila mmoja alikuwa akiwaza lake kichwani, ukimya ulikuwa ukitawala kila nukta katika gari hilo ambalo Chiba alikuwa akiliongoza.

KIJIJI CHA KITOPENI

Usiku huu ni moshi na vilio ndivyo vilivyosikika katika eneo hilo.

Haya mambo nilikuwa nayaona kwenye filamu tu kumbe yapo hata huku siku hizi! Amata akawaza huku akiendelea kula karanga zilizokuwa ndani ya chupa ndogo.

“Na we na makaranga yako!” Gina akaalalama.

“Makaranga jina la mtu!” Amata akajibu huku akiendelea na shughuli yake. Muda kidogo wakaegesha magari yao na kuteremka chini, darubini vifuani mwao, bastola viunoni. Walikuwa tayari kwa lolote.

Wananchi wa kitopeni walikuwa wamejikusanya pamoja, wengine wakiomboleza vifo wengine wakiwa hawana makazi na wengine maumivu makali ya majeraha waliyoyapata katika shambulio hilo.

TSA waliteremka kutoka katika magari yao na kuanza kufanya chunguzi zao za hapa na pale kwa kuhoji na kutazama hali halisi ya eneo hilo.

“Mnasema hao watu walikuwa wangapi?” Amata alimuuliza mmoja wa wanakijiji aliyeonekana kujishughulisha sana kuwasaidia wenzake.

“Walikuwa kama kumi au kumi na tano walikuja wakitokea mashambani huku,” yule kijana alieleza.

“Tuliwaona wanaibuka kule baharini sisi tukakimbia,” mmoja wa watoto aliyekuwa hapo alisema. Kamanda Amata akiwa na Chiba na Madam S walisikiliza maelezo ya wahanga wote walioweza kuongea, kisha wakaitana pembeni.

“Sikia Chiba na Amata hawa bila shaka wamekuja kwa kupiga mbizi,” Madam aliwaambia.

“Kwa maana hiyo hawa jamaa wanaweza kuwa na makazi eneo hilihili,” Chiba akaongeza.

“Kisiwa cha Kalebbe,” Kamanda akawaambia kisha wakamwita tena yule kijana na kumwomba awatajie majina ya visiwa vilivyo karibu na eneo hilo. Akawatajia kwa majina na kuwaonesha kisiwa hicho cha Kalebbe ambacho kilikuwa katikati ya visiwa vingine.

“Mnafikiri pale atakuwa anaishi mtu? Sio rahisi kisiwa kile kule ndio kuna mtu kajenga nyumba yake ndogo,” yule jamaa akaonesha kisiwa ambacho kina jengo la kawaida tu na lilionekana vizuri kwa darubini walizokuwa wakitumia vijana hawa.

“Ok,” Madam akaitikia na kumwacha yule kijana kuondoka.

“Madam, baada ya kumbana yule Kamba Sebule kule polisi kasema wana maskani yao kisiwa cha Kalebbe, so nafikiri sasa ni kuanza uchunguzi wa kisiwa hicho mara moja. Cha muhimu hapa tuache polisi wafanye kazi na sisi tuondoke tukajipange vyema, wasijue kama tumeingia hapa,” Kamanda akatoa maelekezo.

“Sawa, twendeni tukapige kambi Hoteli ya Ocean Breeze, na afisi yetu itahamia hapo mpaka kieleweke…” Madam akawaambia na wote wakaingia kwenye gari na kuondoka huku wakiacha polisi wakiendelea na nyajibu zao.

HOTELI YA OCEAN BREEZE – BAGAMOYO

Ni hoteli kubwa ya kifahari, iliyojengwa kandokando ya Bahari ya Hindi. Jingo hili lenye ghorofa sita lilizungukwa na miti mirefu na mizuri sana iliyotengeneza kivuli kinene wakati wa jua. Usiku huo Madam S na vijana wake waliwasili tayari kwa malazi ya siku hiyo. Katika meza ya mapokezi kila mmoja akajitambulisha kwa jina la bandia na kuchukua vyumba kwa mapumziko huku akili yao ikiwa kazini kwa muda wote.

Kijua cha asubuhi kilipochomoza pande za Mashariki kilimkuta Amata na Gina nje kwenye kibaraza cha ghorofa ya nne ya hoteli hiyo ambayo ilitazamana na Bahari ya Hindi na hapo ndipo wakagundua kuwa ipo karibu na bandari ya mji huo mkongwe, Pumbuji ya zamani, Bagamoyo ya sasa. Pembeni ya meza yao kulikuwa na darubini kubwa ‘Oberwerk’, yenye nguvu, ilikuwa na urefu wa inchi 24 iliyosimamishwa kwenye stendi madhubuti. Huku wakiburudika na kinywaji lakini akili zao zilikuwa katika kisiwa cha Kalebbe ambapo ndipo hasa walipoamini adui wao alipo. Juu ya meza hiyo hiyo kulikuwa na karatasi ambayo kwayo walikuwa wakiandika vitu fulanifulani wanavyovielewa wao.

“Tutaingiaje pale?” Gina aliuliza.

“Simple tu, ama tutasubiri giza la leo au twende kibabe mchana huu. Ila wazo zuri ni kuuchukua mchana huu na kukichunguza kisiwa kile ili tujue in and out, si ajabu tukapata njia nyepesi sana ya kufika pale kuliko tunavyofikiri”.

Gina akatazama saa yake ilikuwa tayari saa tatu za asubuhi, jua linazidi kwenda juu na joto nalo likiendelea kushika hatamu. Simu ya Amata ikaita pale mezani.

“…hello… Madam!” akaipokea.

“…vipi kamanda, kuna lolote huko?”

“…yeah, tunaangalia bado lakini hatujapata ufumbuzi ila taratibu tutapata,”

“…ok, kazi njema, niko na vijana hapa. Tunawaomba mfanye kazi tu na si vinginevyo,” kisha wote wakacheka.

Amata akainuka na kuingia chumbani akachukua simu na kupiga mapokezi akomba kuletewa vinywaji. Dakika tatu baadae, kijana aliyevalia nadhifu kabisa, nguo za kitamaduni akaleta vinywaji hivyo mpaka pale walipoketi.

“Asante sana,” Kamanda akamshukuru.

“We unaitwa nani?” akamwuliza.

“Naitwa Nassoro,”

“Nassoro unajua kisiwa cha Kalebbe?” Kamanda akauliza. Nassoro akamtazama kwanza kabla ya kujibu swali hilo.

“We cha nini?” akajibu kwa swali.

“Aaaaah! Usiwe kama Watanzania wengine kwa kujibu swali kwa swali. Napenda kwenda kukitembele kama utanipa maelezo zaidi juu yake, au kama mna vipeperushi vyake,”

“Kile ni kisiwa cha mashetani, watu huwa hawaendi kule,” Nassoro akajibu kwa kifupi.

“Nahitaji kwenda,” Kamanda akamwambia Nassoro.

“Sawa, karibu sana, si nimekwambia kisiwa cha mashetani, hivyo huwa yanaenda mashetani tu,” Nassoro akajibu na kuondoka.

Gina na Amata wakatazamana. Anajua kitu huyu! kila mmoja akawaza sawa na mwenzake. Amata akainua mkono na kubofya saa yake hapa na pale kisha akaisogeza karibu na kinywa chake.

“…muweke jichoni, amevaa shati la kitenge na suruali nyeusi na kofia ya kitenge, ni mwenyeji wa hapa tulipo…”

“…copy…” Chiba akajibu kwa njia ileile.

Mara kwa mara Gina alikuwa akisimama na kuiendea ile darubini na kuchungulia ndani yake kuona kama kuna lolote geni, na alipomaliza kuchungulia alibonyeza kidubwasha fulani na kupiga picha ya hicho anachokiona, na ile taswira ilisafiri mpaka kwa Chiba kwenye mashine ndogo mfano wa simu na wao waliweza kuitazama vizuri na kuangalia kama kuna mabadiliko yoyote.

Mara hiyo saa ya Kamanda Amata ikaanza kumfinya, akaitazama kwenye kioo na kubofya mahala fulani kisha akapachika kifaa chake sikioni na kusikiliza.

“…yuko jichoni, kaingia mapokezi, anatumia simu ya mezani…” Chiba akamwambia Amata.

“Sawa! Jaribu kudukua chochote katika hilo…”

Chiba akaondoa ukurasa wa juu katika chombo chake hicho na kupachika vizuri vifaa vya masikioni, akabofys hapa na pale juu ya kioo na kujaribu kutafuta mawimbi ya simu hiyo kama ataweza kuyapata.

“…. ko wawili, wanatumia darubini kubwa kutazama kisiwa (…) hapana sijui kabisa (…) sawa sawa, nitahakikisha hilo!”

Chiba aliweza kukamata mawasiliano ya simu hiyo kwa urahisi sana tafauti na alivyofikiria, akatikisa kichwa na kumtumia taarifa Amata kwa njia ya simu yao.

“…tegemea ugeni…” Amata akamwambia.

Wakakata mawasiliano, Amata akarudisha macho kwa Gina.

“Vipi?” Gina akauliza.

“Poa,” Amata akajibu na kusimama, akavuta hatua chache kuingia chumbani, akauelekea mkoba wake na kuchomoa bastola moja, akaijaza risasi za kutosha. Nyuma yake akahisi kama kuna mtu kasimama, akahisi mikono ikigusa mabegani, hakugeuka kwani ulaini wa mikono hiyo alishajua ni nani anayemgusa.

“Vipi ushaanza kufikiri kuua!”

“Akili yangu tayari ishaanza kuzunguka, nahisi kutokea hatari ndani ya muda mfupi ujao, jiweke tayari nawe pia,” akamwambia Gina na kumgeukia. Gina akaweka mikono yake kiunoni mwa Amata.

“Nimemiss!” akamwambia.

“Sio wakati wake, au na wewe ni mmoja wao unataka kunilaghai kwa mapenzi?” Kamanda akajibu na kujitoa katika himaya ya Gina.

“Ningekuwa mmoja wao ningeshawateketeza nyote mpaka sasa, hujui kama sdui mbaya ni yule aliye miongoni mwako?” Gina akamwambia huku akimwachia kijana huyo kama alivyotaka. Amata akaipachika bastola yake kiunoni “mwanamke unamaneno wewe ka mtoto wa Kizaramo,” akasema huku akiiendea ile darubini, akaweka macho yake pale na kutazama tena. Mara hii kitu kipya kikaonekana, kwa mbali aliona kitu cheupe katikati ya bahari.

Nini kile! akajiuliza na kukiweka vizuri katika muonekano sawa. Boti, ilikuwa ni boti iliyoonekana kuja kwa kasi na kutimua maji hayo kuyafanya kuwa meupe, akabonyeza kile kitufe na kupiga ile picha. Akaendelea kuangalia ile boti iliyokuwa ikisogea kwa kasi, sasa aliweza kuiona vizuri, ndani yake kulikuwa na watu watatu, wanaume wawili, waliovaa nguo nyeupe za kisasa, mmoja alikuwa akiongoza boti hiyo na mwingine alikuwa nyuma kabisa. Katikati yao kulikuwa na mwanadada mrembo sana aliyeketi kwenye kiti na bilauri iliyojaa kinywaji, akabonyeza tena kile kitufe na kuisafirisha ile picha.

- * *

Kifaa kile cha Chiba kikatoa ukelele hafifu, akakinyakuwa na kutazama, picha.

“Ugeni kama ulivyotabiriwa,” Chiba akamwambia Madam S huku akimpa kile kimashine ambacho kilimwezesha kuona zile picha vizuri. Muda huohuo akamwona yule kijana akitoka katika chumba fulani na kuelekea nje, Madam S akamwita kwa mruzi, kijana akageuka na kusogea pale mezani.

“Nahitaji vinywaji kijana,” akamwambia.

“Oh! Samahani kuna mgeni nampokea hapo gatini naomba nikuitie mhudumu mwingine,” Nassoro akajibu. Madam S akamshika mkono kwa nguvu na kumkazia macho.

“Kwa nini unataka kupoteza bahati kijana,” akamwangalia juu mpaka chini.

Nassoro akajikuta njia panda, akashindwa kuamua, alijuwa wazi kuwa kumkatalia huyu mama kama mteja haiwezekani na kutokwenda kumpokea huyo mgeni nako ni jambo linguine lisilowezekana.

“Ok, niitie mtu mwingine,” Madam akamwambia na kumwacha. Nassoro akaenda na kumwita mwhudumu mwingine wa kike ili amsikilize Madam. Yule mwanadada akaifikia meza waliyoketi Madam S na Chiba.

“Samahani, huyo anayekuja huko ni mgeni gani?” akamwuliza yule mhudumu badala ya kumuagiza vinywaji.

“Malkia, Malkia wa Kalebbe!”

“Malkia?” Madam akauliza na wakati huohuo yule mwanadada aliyejulikana kama malkia akaingia akiwa anafuatana na Nassoro na moja kwa moja akaenda kuketi kwenye meza iliyopambwa maua mazuri kabisa. Kulikuwa na siti mbili moja ikabakia wazi. Vazi alilovaa mwanadada huyo ndiyo kilikuwa kivutio kingine, alivaa bikini nyeupe na juu yake akavaa vazi lingiine jeupe jepesi kabisa lililokuwa wazi sehemu ya mbele na kuruhusu mwili wake kuonekana.

Nassoro akasogeza vinywaji pamoja na kibweta cha kuwekea jivu la sigara, huyo malkia mwenye mwili wa kisichana zaidi aliketi na kukunja nne huku akiwashiwa sigara na kijana huyo na kuanza kuvuta taratibu.

Madam S akamtumia ujumbe Kamanda Amata juu ya huo ugeni. Haikupita dakika moja, Kamanda Amata akajitokeza kutoka katika ngazi na kuvuta hatua fupifupi kuielekea ile meza. Akiwa ndani ya suti nadhifu nyeupe, shati jeupe na tai nyeusi.

- * *

“Bila shaka hautajiuliza mengi kwa mimi kuketi mbele ya mwanamke mrembo kama wewe, Malkia wa Kalebbe, hakika Mungu anajua kuumba kwa maana jinsi ulivyo hakuna mwanaume rijali atakayepita mbele yako bila kujikwaa hata kama sakafu ni ya marumaru,” Amata akaanza swaga na kuketi huku akichukua matunda madogo ya strawberry na kuyatia kinywani kisha kuyatafuna taratibu.

Mwanamke huyo alijikuta akiangua kicheko cha mwaka kwa maneno hayo matamu na ya kufurahisha. Hakuwahi kukaliwa mbele na kijana asiye na hadhi kama huyu, hili ndilo haswa lililomfanya acheke.

“Hakika kuna wanaume wameumbwa kufurahisha wanawake, lo, ulifikiri nini kuzungumza yote hayo?” akauliza huku bado akiendelea kucheka. Nassoro, mhudumu mahsusi wa malkia huyo akawasili pale mezani na kumtaka radhi Amata kuiacha meza ile.

“Oh, asante Nassoro, lakini mwache, mwache kanifurahisha sana huyu, mpe kinywaji tafadhali,” malkia akamwambia Nassoro naye akafanya hivyo. Ingawa juu ya meza ile kulikuwa na kinywaji ambacho bado kilijaa pomoni, lakini Amata alileteawa kinywaji kingine kabisa, kikawekwa mezani na kumiminwa kwenye bilauri safi, akaiinua na kuipunga hewani kisha yule malkia naye akafanya hivyo wakagonga cheers kwa afya.

“Nitasikia raha sana nikikunywesha japo kidogo,” Amata aliendelea na ubembe wake.

“Oh! No! kinywaji ni kwa ajili yako, enjoy little puppy!” akamwambia, Amata akaiinua na kukinywa chote kisha akaishusha ile bilauri mezani.

“Waoh, you are so strong man,” (wewe ni jasiri)

“Yes I am,” (ndiyo) Amata akajibu.

“Mmmmh you are smart!” Yule mwanamke akaendelea kumsifu Amata.

“Kawaida yangu!” akamjibu.

“Hebu nambie huko Dar, unafanya kazi gani?” akahoji.

5

“Mimi ni mwandishi wa habari, nina kampuni yangu inaitwa AGI Investment, tunashughulika na utafutaji wa habari za kitaifa na kimataifa, kuandika makala mbalimbali na habari za uchunguzi,” Amata akaeleza huku akimpatia kadikazi mwanamke huyo mwenye sura ya kuvutia.

Mazungumzo yakaendeleakwa kina kati ya wawili hao, Amata alikuwa akijaribu kucmchokonoa kwa maswali ili kujua mengi kuhusu kisiwa hicho, na mwanamke yule alikuwa akijibu pasi na wasiwasi wowote. Yule mwanadada aliyejitambulisha sasa kwa jina kamili la Zulekha alimwambia mengi sana juu ya kisiwa cha Kalebbe na Amata akamweleza mengi juu ya kampuni na kazi yake.

Nusu saa ikapita katika mazungumzo yao Amata hakuendelea kunywa kile kinywaji ila sasa alikuwa ni mzungumzaji zaidi kila Zulekha alipomhamasisha kunywa zaidi yeye aliishia kumimina tu, akimwambia ‘usijali nitakunywa’.

“Utapenda kunitembelea?” Zulekha akauliza huku akiumauma ncha ya ulimi wake.

“Kama utanitembelea mimi kwanza!” akamjibu namna hiyo.

Zulekha, akatazama chini kwa sekunde kadhaa, kisha akamtazama Amata usoni bila haya.

“Unataka nikutembelee?” Zulekha akauliza huku akirembua macho yake.

“Ndiyo, kisha nami nitakutembelea wewe!”

“Good boy! Utaniweza?” Zulekha akauliza huku mkono wake ukiishika ile ya Amata pale mezani.

“Kwa nini unauliza hivyo?”

“Kwa sababu ninyi vijana wa mjini mnakula sana chips, mkifika kwenye sita kwa sita mnahema kama mbwa anayekimbilia mfupa,”

“Hah! Hah! Hah! Mi siyo aina hiyo ya mwanaume,” Kamanda akajibu na mara hiyo, Zulekha akainuka na vazi lake likajimwaga na kuacha eneo kubwa la mbele wazi. Akamtazama kijana huyu shababi kwa jicho kimahaba.

“So?”

“Let’s feast!” Zulekha akamalizia na kumpa mkono Amata, wakatembea kwa hatua za madaha kuelekea katika ngazi ambazo ziliwafikisha ghorofa ya juu, ndani ya chumba cha Amata. Kama kuna kitu ambacho Kamanda alikuwa akijipanga kujibu ni juu ya lile darubini, maana kwa ubembe wa mwanamke huyo angeweza kutaka kuchungulia, ndipo angeona nyumba yake inavyoangazwa kwa ukaribu lakini walipoingia ndani ile darubini haikuwepo. Gina mara tu baada ya kusikia mazungumzo ya wawili hao akajua safari yao itafikia ndani ya chumba hicho, hivyo akaibeba ile darubini na kutoka nayo huku moyo ukimuuma wivu.

Wawili hao wakajitupa kitandani na mabusu motomoto yakachukua nafasi yake. Amata aliufurahia utundu wa mwanamke huyo maana alikuwa akimrambaramba kila kona ya mwili wake na yeye akaonesha utundu wote anaoujua. Dakika kama arobaini na tano hivi wakabaki kama walivyozaliwa na kila mmoja akaanza kufurahia kile afanyacho mwenzake na kujikuta wamezama katika mahaba mazito. Amata akasahau kazi, Zulekha akasahau kazi. Miguno na sarakasi za ajabu ajabu zikaendelea juu ya kitanda hicho.

“Uko vizuri kijana! Karibu nyumbani kwangu, sasa tutaweza kuzungumza mengi,” Zulekha akamwambia Amata baada ya kila mmoja kuridhika na huduma ya mwenzake.

“Namwogopa mumeo!”

“A ha! Hah! Hah! Hah! Sina mume… isitoshe ndani ya nyumba ile kuna mambo mengi, we utakuja kama mfanyabiashara kisha mengine mi najua tutafanyeje,” akamsihi kijana huyo. Kwa Amata hii ilikuwa ni nafasi ya pekee kuweza kufika kwenye jumba lile ambalo ndilo haswa lilikuwa limewaleta hapo Bagamoyo. Lakini kichwa chake tayari kilimwambia hapo kuna hatari ya kulubuniwa na kutekwa kirahisi.

“Vipi mbona hunipi jibu? Au hutaki kuijua Kalebbe? Utakosa habari!”

Amata akamgeukia na kumtazama machoni, akaona hila ya wazi kabisa kwa mwanamke huyu.

Sina budi kufanya hili, the opportunitry never come twice! Akawaza na kujiinua kitandani.

“Sawa, twende zetu!” akamwambia mwanamke huyo aliyejilaza kitandani kifua wazi, matiti yake kama ya msichana anyevunja ungo yalimfanya aonekane mrembo kama samaki-mtu. Zulekha akatabasamu na kumuuliza, “Upo peke yako?”

“Yes, peke yangu,” Amata akajibu. Kisha wote wakajiandaa kwa safari, wakatoka nje ya hoteli hiyo na kuelekea gatini ambako ile boti bado ilikuwa ikimsubiri. Wakaagana na Nassoro na kuondoka zao.

- **Katika Kisiwa cha Kalebbe vijana wa Pancho walibaki wakitazamana baada ya kutazama picha nzuri ya Zulekha na Amata pale kitandani. Picha hii iliyonaswa na mtambo uliofungwa katika jumba hili, ni wachache tu walioujua. Wale vijana walimwita mkubwa wao wa kitengo na kumwonesha anachofanya mwanamke huyo. Walijua wazi kuwa kila picha wanayoiona lazima Pancho anaiona kama ilivyo. Wote wakajikuta wakiduwaa mbele ya sikirini hiyo udenda ukiwatoka na miili yao ikikosa utulivu kila waliposhuhudia mke wa bosi wao akibanjuliwa na Kamanda Amata.

Nusu saa ilipita na kisha wakaona sasa safari inaanza ya kuja kisiwani.

“Anamleta, hakikisheni analipa yote aliyoyafanya kwa mwanamke huyu,” Yule mkubwa wao akatoa amri kisha akawapa tahadhari wengine kuwa wampokee kama mgheni wa bosi, wasimletee matata yoyote mpaka waambiwe vinginevyo.

Ndani ya kisiwa hiki, gabacholi huyu alikuwa amewekeza vitu vingi sana kwa siri, kulifungwa darubini kubwa ya kutumia umeme ambayo iliwawezesha viajana wake kuona nyendo zote za mtu wamtakaye. Mara tu baada ya kupata taarifa kutoka kwa mtu wao, Nassoro, ndipo wakaazimia kumtuma Zulekha kwa ajili ya kumnasa mtu huyo, maana walijua mwanaume hawezi kuponyoka kirahisi kwa mwanamke mrembo kama huyu. Na hii ndiyo ilikuwa kazi kubwa ya Zulekha kwa bwana wake, Pancho.

Pancho alipata taarifa ya ugeni huo akafurahi sana na mara hii alihakikisha kumtia adabu kijana huyu ambaye bado anakumbuka mambo aliyomfanyia huko India na kwenye ndege wakati wa kurudi.

- **

Gina aliinuka kitini na kuibeba ile darubini, haraka akaufungua mlango wa chumba cha Amata na kuingia ndani, akapita mpaka kwenye kibaraza kilekile akaiweka tena na kuanza kuchungulia na kuiona ile boti ikipotelea majini.

“Shit! Janaume linapenda wanawake hili, limeshatekeka kilaiiniiii,” akajikuta akiongea peke yake alipomuona Amata akiwa na Zulekha katika ile boti, akasonya na kuiacha ile darubini huku akiondoka na moyo uliyojaa wivu maana alijua wazi uwa Kamanda lazima keshamtafuna mwanadada huyo. Alipofika mlangoni, akakumnbana na Chiba na Madam S.

“Rudi ndani,” Madam akamwamuru huku Chiba tayari akiwa kwenye ile darubini akitazama ile boti.

“Jiandaeni kwa kazi ya kumkamata yule mwanaharamu, Amata atatuletea taarifa kama mtu huyo yupo au la,” Madam aliwaambia huku akibofyabofya simu yake hapa na pale, akaiweka sikioni.

“Hey!!! Scoba na Jasmine! Stand by! Tukutane Ocean Breeze ndani ya nusu saa, chambo tumeshatupa mtoni bado kuvua samaki,” akamaliza.

“…copy…” akajibiwa na ile simu ikakatika. Mipango ya kina ikapangwa na mwanamama huyu, akawaweka vijana wake katika hari ya mapambano, akawatia moyo na kuwaasa hili na lile.

- * *

“Karibu sana Kalebbe,” Zulekha akamkaribisha Amata huku akimsubiri ateremke katika boti ile.

“Asante sana, aaaaaaaaah nimefurahi kukanyaga kisiwa hiki,” Amata akajibu huku akiteremka taratibu wakati vijana wakiendelea kuifunga ile boti gatini. Kwa mwendo wa taratibu walitembea katika mchanga mweupe wa pwani ya kisiwa hicho na kufika kwenye kijumba kidogo tungekiita kibanda, lakini kilijengwa kwa unadhifu sana na kilionekana chenye thamani. Pembezoni palikuwa na nyumba nyingine nzuri tu lakini ilionekana haina watu. Yule mwanamke, akaweka kiganja chake cha mkono wa kulia katika kitu kama kioo kilichokuwa mlangoni hapo, kisha akasogeza zura yake, mwanga mwekundu ukapita kati ya macho yake, akatamka jina lake na kisha kubofya tarakimu fulani fulani, ule mlango ukafunguka, wakaingia wote wane, yaani yeye, Amata na vijana wawili na ule mlango ukajifunga nyuma yake.

Ngazi ndefu ilionekana kuteremka, wakaifuata na walipofika chini kama mita ishirini hivi, kulikuwa na njia pacha tatu. Zulekha akasimama na kumtazama Amata.

“Usiogope! Hii ni nyumba ya siri sana na ni watu wachache tu nje ya familia hii wanaopata fursa ya kuiona. Ila mtu wa kawaida akiiona na kuigundua basi huyo huwa hawezi kuishi,” akamwambia huku akimtazama. Amata akatikisa kichwa na kugeuka nyum,a akakutana machi na wale jamaa wawili walioshiba vyema.

“Ukienda kushoto, unaenda kwenye nyumba ya mzee, kulia unaenda kwenye idara ya usalama na sisi tunakwenda moja kwa moja,” akamwambia kisha akaongoza njia ile na Amata akamfuata.

Wakatokea kwenye jumba kubwa la kifahari, lenye kila samani inayostahili kuitwa ‘samani ya ndani’. Kamanda Amata aliitazama ile sebule ya kifahari, iliyozungukwa na kuta za aina yake huku upande mmoja kukiwa na ukuta wa kioo unaoruhusu kuona mandhari ya chini ya maji. Hakuweza kuamini kama katika nchi hii kuna watu wanaoishi kitajiri namna hii. Akatikisa kichwa huku akitazama tu na asijue wapi pa kuketisha makalio yake.

“Kinywaji tafadhali,” mwanadada mrembo mwenye asili ya Kihindi, wa kadiri ya miaka ishirini na tano hivi alimkaribisha kinywaji cha matunda kilichojaa kwenye bilauri.

“Asante sana mrembo … sharubati tu au kuna kingine?” akauliza huku akiwa kamshika mkono wake.

“Oh, sio hivyo, mgeni hawezi kuwa mwenyeji namna hiyo,” Zulekha alimwambia Amata huku akimwondoa yule binti katika himaya yake. Kamanda Amata bado alikuwa akishangaa mandhari safi ya jengo hilo hata akasahau kama ana kinywaji mkononi mwake.

“Huu ndiyo utukufu wa Premji Kanoon, nchi ndani ya nchi,” Zulekha akamwambia Amata huku akiichukua ile bilauri na kuitua mezani, akamkubatia kijana huyo kimahaba huku sura zao zikitazamana.

“Sasa jumba kama hili umewezaje kulijenga hapa?” Amata akauliza.

“Kawaida tu, mafundi kutoka Japan waliifanya kazi hii mchana na usiku baada ya kupata matatizo katika nyumba yetu ya Kerege,” Zulekha akaeleza.

“Mlpata matatizo Kerege?” Amata akauliza.

“Ndiyo!”

“We na nani?”

“Mi’ na mume wangu kipenzi Premji Kanoon, utamwona muda si mrefu kwani ametoka kwa kuwa kesho tunatarajia kuondoka,” Zulekha akajibu kwa ufasaha huku Amata akitikisa kichwa na saa yake ikifanya kazi ya kurekodi.

“Kwa nini mwataka kuondoka?”

“Watu wanataka kumuua mume wangu, na inaonekana ni watu wa serikali, hata swahiba wake aliyefanya mchakato wa kumuuzia kisiwa hiki amekamatwa majuzi tu, hii hali imekuwa mbaya kwake na kwangu pia kwa kuwa hana furaha, hata kitandani hanipi nitakacho…” mwanamke akafunguka na Amata akaendelea kusikiliza kwa utulivu maneno hayo.

Tungechelewa kidogo tu angetutoka kwa mara nyingine! Amata akawaza huku akimtazama mwanamke huyo usoni.

“Unaonekana ni kijana mtulivu, mdadisi, unayependa kujua mambo…”

“Na lingine umelisahau, napenda warembo kama wewe,” Amata akamalizia kusema.

“Warembo ni sumu, watakupeleka pabaya,” Zulekha akamwambia huku akiketi kitini, akawasha sigara yake na kuketi kwenye sofa kubwa la vono.

“Mr….. Spark! Pale Oceanic Breeze umefika lini?”

“Nimefika siku tano zilizopita,” akajibu.

“Spark una maswali kama mpelelezi,” Zulekha akazidi kusaili.

“Si nimekwambia kuwa mimi ni mwandishi wa habari,” akajibu jibu la uongo kabisa.

“Aaaaa! Hah! Hah! Hah! Hapo nitakubaliana na wewe, na nilishasahau kama umenambia …” akamtazama kwa kulegeza macho huku sigara aliyoibana katia ya kidole cha kati na shahada ikiendelea kufuka moshi, “… sasa Bagamoyo kuna habari gani iliyokuleta?” Zulekha aliketi sawia katika kaiti chake akimtazama kijana huyo.

“Inasemekana kuna ndege ndogo imepotea upande huu wa Bagamoyo hiyo sasa ndiyo iliyonileta kuandika hiyo juu ya hilo tukio,”

“Unashirikiana nani?”

“Mimi kama mwandishi wa kampuni ya kuitegemea, naiandika hiyo habari ya uchunguzi kwa ajili ya kuiuza kwa mashirika makubwa, niko peke yangu hapa kwani waandishi wangu wengine wana kazi nyingine za kufanya,” Amata akaeleza.

“Oh, good kazi nzuri sana,” Zulekha akamwambia Amata na wakati huohuo simu ya ukutani ikaita, akanyanyuka na kuiendea akaipokea.

“…Ndiyo, sasa hivi?… ok!” akaitazama saa kubwa ya ukutani ilikuwa ikimwambia kuwa muda huo ilikuwa ni saa kumi na moja jioni. Akarudi pale mezani na kumalizia kinywaji chake.

“Mume wangu karibu anaingia, unapenda kuungana nami kumlaki?” Zulekha akamwambia Amata.

“Yah, bila shaka,” akajibu.

**-

Wote wawili wakaongozana mpaka nje kwa upande wa pili wa kisiwa hicho, pale walikuta wanaume watatu weusi, wenye miili iliyoshiba, walionyoa ndevu zao kama Rick Ross, kutokana na ukimya wao naye hakuwasalimia, bali aliungana na Zulekha kutulia kusubiri.

Helkopta moja kubwa ya kifahari iliteremka taratibu katika pwani hiyo iliyojengwa kinamna, kisha ikazima injini yake, na utulivu ukarejea. Kamanda Amata akapachika miwani yake usoni si kwa sababu ya jua kali bali miwani hiyo ilikuwa ikipiga picha na kuzisafirisha kielektroniki kwenda kwa Chiba na timu yake. Mlango ukafunguliwa, mtu mnene kiasi, Muhindi, aliyevalia suti nyeusi ya bei mbaya, kwa mtazamo tu alionekana ni tajiri, akateremka pamoja na watu wengine wawili ambao moja kwa moja aliwatambua kwa kuwa ni watu wa juu serikalini. Pancho alipogongana macho na

Pancho akatamani kuanguka lakini akajikaza kisabuni. Alijua kuwa kijana huyo keishakufa hata alipopata taarifa ya ugeni wa dharula kutoka kwa mkewe hakudhania hata kama ni nani atakuwa amefika. Bahati mbaya sana kutokana na kikao cha siri na watu wake hakuweza hata kufungua kompyuta yake kuangali nini kinaendelea, labdal angeweza kuna yale aliyoyafanya na mkewe. Zulekha akamwendea na kumkumbatia kisha akambusu.

“Mgeni, nimekutana naye Ocean Breeze baada ya kupewa taarifa na mtu wetu, nimemkaribisha nyumbani kwa sababu najua utakuwa na aja ya kuzungumza naye kadiri ya lile alilokuja kufanya hapa Bagamoyo, anaitwa Mr. Spark,” Zulekha akatambulisha. Preji au Pancho akabaki kimya akaimwangalia mkewe na kisha Amata. Zulekha akageukia kwa Amata.

“Kutana na mume wangu mpenzi Mr. Premji Kanoon,” akamalizia. Pancho alikutana macho yake na yale ya Amata ambayo yalifichwa kwenye miwani ya rangi nyeusi, miwani iliyokuwa ikirekodi video matukio yote hayo ambayo yalikuwa yakitukia mbele yake.

“Karibu sana, jisikie nyumbani,” Pancho akamkaribisha Amata, pale alipotaka kupewa mkono alijifanya kutokuona akapita na kisha wengine wakafuatia nyuma yake. Kichwa cha Pancho kilianza kuchanganyikiwa kwa kumwona mtu huyo hatari kwa maisha yake akiwa hapo, hakuelewa kama Zulekha kamleta hapo kwa nia ya kuwa kamteka au ndiyo amelaghaiwa kwa mapenzi, lilikuwa swali lisilo na jibu. Baada ya milango miwili mitatu hivi akatokea kwenye sebule kubwa, akasimama kwa sekunde kadhaa kisha akawaambia watu wake.

“Naomba niacheni peke yangu kisha mniitie Zulekha nahitaji kupumzika kidogo,” Pancho akwaambia vijana wake na wale wageni, wakaondoka eneo lile.

- * *

Chiba akatikisa kichwa huku akiendelea kutazama kompyuta yake, iikuwa ni kama vile yeye ndiye kakutana uso kwa uso na mtu huyo.

“Vipi?” Madam akauliza.

“Amewasili kisiwani, na alikuwa na watu wengine wawili ambao nawajua fika! Njoo mwenyewe ushuhudie,” Chiba akamjibu Madam S huku akiirudisha nyuma ile picha na kumwnesha bosi wake. Madam S akatazama zie sura na kusikitika.

“Watu wanauza nchi kila kukicha!” akasema.

“Ndiyo hivyo!”

“Wamekwisha…” akamalizi huku akitoka pale mezani. Akawaita vijana wake na kuanza kuwapanga jinsi ya kuvamia kisiswa hicho, maana walijua kuchelewa kwao kungeweza kumweka pabaya Kamanda Amata. Njia iliyohafikiwa na wote ni kupiga mbizi na kisha kuangusha mziki katika kisiwa hicho.

- * *

Pancho alimtazama Zulekha kwa jicho kali, akameza mate ya hasira.

“Unamjua mgeni uliyemleta humu ndani ni nani?” akamuuliza.

“Ni mwandishi wa habari aliyevutiwa sana na hiki kisiwa hiki, ijapokuwa amekuja kwa kazi nyingine nikaona nimkaribishe kama fursa ya kujitangaza. Na ni wewe mwenye we uliniambia hayo,” Zulekha akajibu.

Kofi moja la kulia lilitua shavuni mwake akadondokea kitandani.

“Huna akili mwanamke! Huna akili kabisa, unaweza kuleta mashetani ndani ya nyumba hii, we hujiulizi kwa nini nyumba hii imejengwa chini ya ardhi?” Pancho akang’aka.

“Sasa mimi kosa langu nini?” Zulekha akaamka kitandani na kupiga kelele huku akiuliza, hasira zikamshika mishipa ikamtoka, “wewe mwenyewe ndiye uliyeniambia hayo leo hii unanigeuka? Nimepigiwa simu na Nassoro kijana wako mtiifu wa Ocean Breeze nikaenda na bahati nakutana na mtu huyu kwa nini nisimlete nyumbani ili aone kwa macho kila anachotaka, mara ngapi wewe umewaleta watu humu ndani na kunitambulisha kuwa ni watalii na wafanyabisahara? Hukuwahi kunambia kuwa hata mwili wangu niutumie kumkamata adui, sasa huyu nimekulea, awe adui au rafiki…”

“Naona unanipanda kichwani sasa, sivyo?” Pancho akachomoa bastola na kumwoneshea Zulekha.

“Nenda kwa huyo mgeni wako kamwulize yeye ni nani akwambie kisha uniletete jibu haraka!!!”

Zulekha akatoka chumbani na kumwacha mumewe akiwa kafura kwa hasira, alihisi kuchanganyikiwa kwani hakujua ni nini kinatokea, maana alilofanya ni lile ambalo mumewe ulitaka daima, lakini kwa nini amwadhibu kiasi hiki? Zulekha alihisi hasira kali sana dhidi ya mumewe, akapita kwenye korido ndefu na kuingia katika sebule kubwa ambako mwanzo aliketi na Amata, hakumkuta, isipokuwa kijana mmoja aliyekuwa akiangalia usalama wa eneo lile.

Kamanda Amata alikuwa kasimama mbele ya dirisha moja kubwa sana akitazama nje na shughuli mbalimbali zinazoendelea za wafanyakazi wa himaya hiyo.

“Mr. Spark!” akaita. Amata akageuka na kumwendea pale aliposimama, Zulekha hakusema lolote, akainua chupa ya whisky na kumimina kwenye bilauri iliyokuwa juu ya stuli na kumpa Amata kisha akainua nyingine na kujimiminia yeye, wakagonga chias na kila mmoja akapiga funda moja la nguvu. Lkitu ambacho alikigundua kwa mwanamke huyu ni kitu kama uvimbe katika shavu lake, akajua kwa vyovyote kuna jambo.

“Wewe ni nani?” Zulekha akauliza huku akionekana wazi sura yake kubadilika. Amata akapiga funda jingine na kumtazama mwanamke huyo wa Kihindi.

“Nimekwisha jitambulisha kwako ya kuwa mimi ni nani, bado unataka zaidi? Basi mwambie aliyekutuma akwambie mimi ni nani,” kisha akainyosha juu ile bilauri yake na kuinywa mfululizo, alipoitu kwenye stuli ilikuwa haina kitu. Akamtazama tena Zulekha pasi na kupapasa macho

“Naitwa, Amata, Kamanda Amata, Tanzania Secret Agency nambari moja; una lingine?” akamweleza mara tu baada ya kuiweka bilauri yake mezani. Na ni nukta hiyohiyo, alipojikuta amezungukwa na vijana wenye silaha kile upande. Aligeuka huku na huku na kukutana na sura zilizokunjamana kwa uchu wa kuua, Short Gun zilizosheheni risasi, zenye hamu ya kufyatuka.

“Mikono juu tafadhali,” akaamriwa na ye akatii.

Kijana mwingine akampekua na kutoa bastola mbili ndogo mifukoni mwake, visu vidogo vitatu na vitambulisho vingine vingine ikiwamo kadi za benki na kadhalika.

“Unaniambi wewe ni mwandishi wa habari kumbe ni mpelelezi?” Zulekha akamwuliza kisha akamnasa kofi na kusogea pembeni. Amata alivumilia maumivu huku akimtazama Zulekha kwa jicho baya sana.

Utalipa tu! Akajisemea moyoni. Pancho Panchilio akaingia sebuleni pale na kumkuta Amata akiwa chini ya ulinzi mkali.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Amataaaa, Kamanda Amata, leo umejileta mwenyewe kwenye nyumba ya shetani. Uroho wako wa mapenzi ya wanawake umekukamatisha, huna maana kabisa, nashindwa kujua kwa nini serikali ikakuamini hata kukupa hicho cheo wakati wewe ni mpumbavu kati ya wapumbavu wa nchi hii! Karibu sana Kalebbe, maana ulitaka kuja kupaona kama nilivyoelezwa na mke wangu Zulekha basi ngoja nikutembeze kidogo ili ufahamu mahali hapa,”

Pancho alimchukua Amata na kumtembeza katika jumba hilo huku vijana wake wakilinda msafara huo kwa bunduki nzito kila kona ya jengo. Kila kitengo alimwonesha bila kumficha na kumwelezea lakini hakumruhusu kuuliza swali, kil kitengo alikuta vijana wakifanya kazi kwa mori wa ajabu, wengi hawakuwa Waafrika, bali Wahindi na Waarabu, weusi walikuwa kwenye ulinzi tu. Katika chumba cha rada aliweza kuona kwa picha jinsi ndege yao ilivyolipuliwa.

“Aaaaa hah! hah! hah! Umeona, ninaweza kulipua ndege yoyote inayopita hapa, siogopi!” akajitapa kisha akaamuru watoke waende chumba cha mwisho. Baada ya kuzunguka ndani ya jengo lote hilo wakasimama mbele ya mlango mmoja wa chuma. Pancho akamtazama kijana huyu na kufungua kinywa chake kusema.

“Kamanda Amata, na sasa nataka nikuoneshe kitengo hiki ambacho kila anayeingia lazima achnganyikiwe ka teknolojia iliyofungwa ndani yake,” aliposema hayo akabofya kitufe fulani na lile lango likafunguka. Kilikuwa chumba tupu, hakukuwa na chochote ndani yake. Pancho akaingia.

“Karibu ushuhudie kilichomo, usiogope,” akamwambia. Kengele za hatari zikalia kichwani mwa Amata, akaingia ndani ya kile chumba kipweke, nyuma yake wakaingia vijana wawili walioshiba kimazoezi na wale wenye silaha wakabaki mlangoni. Kwenye maeneo kama haya huwa Amata hana subira zaidi ya kupigania uhai wake tu japo kwa sekunde ya mwisho. Alivuta hatua mbili mbele na kugeuka ghafla, akamchapa konde moja mmoja wa wale jamaa waliongia nyuma yake. Yule jamaa akayumba kidogo kwa kuwa hakutegemea dhopruba kama ile. Yule wa pili akaudaka mkono wa Amata lakini kabla hajafanya lolote, alipigwa kichwa kizito na kwenda chini. Kamanda Amata akaruka hewani na kutawanya miguu yake, akawachapa mateke makali kila mmoja akaenda chini bila kipingamizi. Wale wenye silaha wakashindwa wafanyeje, maana walijua kufyatua risasi kungeweza kujeruhi watu wao.

Alipotua chini Amata akaruka sarakasi ya chini kwa chini na guu lake likatua katika koromeo la mmoja wao, akaguna kwa uchungu. Alipojigeuza alijikuta anatazamana na mtutu wa Short Gun, akajizungusha na kumtia ngwala aliyeshika hiyo bunduki, akaenda chini huku bunduki ile ikimtoka mikononi, akaiwahi na kuikamata, bila huruma aliwatwanga wote wanne kwa kirasi na kuwaacha marehemu. Si mlangoni wala ndani ya kile chumba, hakukuwa na mtu.

Uko wapi mwanaharamu? akajiuliza na kuchungulia kupitia ule mlango, nakasikia watu wanaoongea wakija upande huo, akarudi ndani na kujificha nyuma ya mlango akisubiri huku mkononi mwake akiwa kaikamatia ile bunduki aliyoichukua kwa yule jamaa.

“Ni hapa jamani, ingieni kwa makini,” sauti moja ikasema. Wale waliokuja kama ni kuokoa jahazi walishuhudia damu na miili isiyo na uhai. Amata akaendelea kutulia palepale, wale jamaa wakamwingiza mmoja kama chambo, akaangaza angaza huku na huko akiziangalia maiti za wale jamaa watatu pale chini.

“Huyu jamaa hayupo bwana,” akawaambia wenzake.

“Basi msako uanze atakuwa humuhumu ndani, kumbuka hawezi kutoroka hapa ni kisiwani,” mwingine akahimiza huku wakitoka mle ndani na kupotelea huku na huko. Amata akatoka taratibu na kufuata korido moja kwa moja mpaka kwenye ile njia panda waliyopita na Zulekha wakati wakiingia kwenye jumba hilo. Akakunja kushoto na kuufikia mlango imara wa chuma, akajaribu kuufungua kwa kutumia zile namba alizozikariri pindi alipomwona Zulekha akifungua zikakubali lakini akadaiwa alama za vidole, akashindwa. Akatafakari cha kufanya akakosa jibu. Alipokuwa akijiandaa kubadilisha mbinu akasikia michakacho ya miguu ya mtu anayetembea haraka haraka huku akiongea.

“Kawaua wote, wote watatu, huyu jamaa hafai, inabidi auawawe,” yule mtu alionekana anaongea na kitu kama simu ya upepo. Amata akamvizia, alipotokezea tu eneo lile, akaruka na kutua shingoni mwake, akamkaba kabali namba sita.

“Tulia,” akamwambia. Ile redio pale chini ikawa inaendelea kuita,

“Jota! Jota! Umepatwa na nini?” sauti ya upande wa pii ikauliza. Kamanda Amata akaitazama ile redio na kuivuta kwa mguu wake.

“Fungua mlango!” akamwambia yule jamaa ambaye sasa alimfahamu kwa jina la Jota.

“Mi sijui, “ akajibu kwa shida kutokana na ile kabali aliyopigwa na Amata, akamwachia na kumsukumizia mlangoni.

“Fungua,” Amata alimwambia huku bunduki ikimtazama mtu huyo, akapapasa namba hii na ile na kuweka alama zake za vidole kisha macho, mlango ukafunguka. Kamanda Amata akamrukia teke la kusukuma yule jamaa akaangukia ndani, kisha yeye akafuata na kufyatua risasi zilizowaangusha watu wawili waliojitokeza na kumwacha mmoja tena wa kike akiwa kasimama.

“Kamanda Amata,” Zulekha akaita, “umeniharibia ndoa yangu,” akaongeza kusema.

“Nioneshe mumeo, serikali inamtafuta kwa udi na uvumba,” Amata akamwambia.

“Wewe ni mbaya sana sivyo nilivyofikiria,” Zulekha akaongea huku chozi likimtoka.

“Nilitaka nifike hapa, na nakushukuru kwa kunifikisha na sasa ninavyokwambia namhitaji mumeo, Pancho Panchilio na sio Premji Kanoon kama unavyomjua, gaidi anayehatarisha maisha ya nchi na wananchi, ametoroka mikono ya serikali kibabe, sasa siku zake zimekwisha. Nioneshe alipo kabla na wewe sijakumaliza,” Amata aliongea huku akiwa kakunja sura kwa hasira.

“Sasa mbona unakunja sura namna hiyo, kijana mzuri hatakiwi kujizeesha mwili wake,” Zulekha alisema hayo huku akimfuata taratibu.

“Tulia hivyohivyo kabla sijakuua kwa bastola yako mwenyewe,” sauti ikasikika kutoka nyuma yake. Kutokea katika dirisha kubwa lililokuwa mbele yake aliweza kuona taswira ya mtu yule vizuri sana. Amata hakuwa na muda wa kupoteza katika eneo hilo ambalo lingeyagharimu maisha yake muda wowote. Aligeuka na kumtandika yule jamaa kwa kitako cha bunduki, akaaangukia juu ya meza huku bastola ikimtoka mikononi, Amata akachumpa kwa ustadi na kuinyakuwa huku mkono mwingine akiwa tayari na saa yake ya mkono ambayo bwana huyo aliichukua pamoja na bastola. Yule bwana akaamka na kusimama wima huku mbele akimtazama Amata aliyekuwa akiibonya ile saa hapa na pale.

“Mnaweza kuja sasa, kazi imeanza,” akaongea huku akiitazama ile saa kisha akaivaa mkononi mwake. Yule mjinga akatumia muda huohuo, akaruka tik tak kwa minajiri kumpiga mikono na kidevu cha Amata lakini akakuta anapiga hewa kwani mwenzake alikwishaondoka eneo hilo na kutua upande mwingine mpaka kwa Zulekha aliyekuwa amebaki kaduwaa. Yule bwana alipotua na kukuta Amata hayupo, akajivuta kasi kumwendea, akaruka hewani akiitanguliza miguu yake mbele. Amata akaepa na kumpa pigo moja la karate mbavuni na kuvunja ubavu mmoja,

akajibwaga chini kama mzigo, alipojaribu kusimama alikutana na teke lingine katika ubavu wake wa pili, akaanguka chali na guu la Amata likatua kifuani mwake kwa kishindo.

“Aaaaaaiiiggghhh!!!” Yule jamaa akapiga yowe la maumivu huku akijaribu kwa nguvu zote kuuondoa mguu ule lakini alishindwa.

“Boss wako yuko wapi?” akamuuliza.

Akiwa katika kumuuliza akahisi kitu kizito kikikifikia kisogo chake, akageuka haraka na kutua upande wa pili wa yule mtu huku tayari mkononi bastola yake imetulia, alipocheza na kifyatulio, kijana mmoja aliyekuwa na chuma kizito mikononi mwake alijibwaga chini na kuwa marehemu. Amata akajishika kisogoni na kujifuta damu kutoka kwenye jeraha lililofanywa na pigo lile. Ilionekana mpigaji hakuwa mzoefu kwani angempata sawasawa basi lazima angepoteza fahamu lakini haikuwa hivyo. Amata akatazama alipkuwapo Zulekha katika ile sebule, hayupo, akatazama hapa na pale hasimwone.

Shit! Kaenda wapi huyu mwanamke? akajiuliza bila kupata jibu, akamgeukia tena yule jamaa.

“Hah !hah! hah! hah! Umecheza pata potea, leo nakumaliza kwa risasi yangu,” yule bwana akajigamba na kunyanyuka kwa taabu kutoka pale alipolala, wakati huo Amata bastola yeke ikiwa chini sakafuni, akaikanyaga kwa ncha ya mguu wake na kuibetua, ile bastola ikaruka hewani na Amata akaidaka kwa kono lake la kulia, sekunde hiyohiyo kifua cha yule jamaa kilitobolewa mara mbili na risasi za Amata, akarudi chini kwa kishindo.

“Buriani!” akamwambia.

Kamanda Amata akasikia sauti ya chopa, akatoka ndani ya chumba kile na kutafuta njia ya kutokea nje, ngumu. Alipofanikiwa kutoka ndani ya chumba kile akajikuta kwenye zile korido, huku na kule ving’ora vya hatari vilikuwa vikilia, kimenuka. Akakimbilia upande wa kushoto na kukutana na vijana waliovalia kijeshi na kujining’inizia silaha nzito, kabla hawajakaa sawa, akawafumua kwa risasi na kuwabwaga, akachukua shotgun walizokuwa nazo, akanyofoa na maguruneti mawili waliyokuwa nayo, akaendelea na safari. Moja ya milango mingi aliyoikuta hapo ni ule aliyokuwa anautaka. Akabonya kikengele na ule mlango ukafunguka, ndani yake kulikuwa na vijana wanne waliokuwa wamekaa kwenye luninga nne tofauti wakiongoza mitambo yote ya jengo hilo kuanzia rada, kamera za usalama na silaha zilizofungwa ardhini.

“Mtulie hivyo hivyo! Bosi wenu yuko wapi?” akawauliza huku akiondoa pini kwenye moja ya bomu la mkono (guruneti) alilokuwa nalo mkononi, wale jamaa wakatazamana na kukosa jibu.

“Najua ninyi mnafahamu, haya, mmoja baada ya mwingine, mniambie bosi wenu yuko wapi ama la, nateketeza chumba kizima na kwangu si hasara,” akawaambia tena huku akiwa amelishika lile bomu kwa mkono wake.

“Boss yupo na sasa anaondoka,” mmoja akajibu kwa kitetemeshi.

“Nioneshe alipo,” akamwambia na yule kijana akazungusha kitu fulani na kwenye luninga ya mbele yake kukaonekana helkopta iliyokwisha washa injini tayari kuondoka, rubani na watu wengine wawili walikuwa tayari ndani yake huku nje kukionekana watu kama watano wenye silaha wakiwa wameweka ulinzi.

“Umeshamkosa boss, anaondoka na mkewe,” kijana mwingine akaongea kwa nyodo wakati alipoona taa ya kuomba kufunguliwa mlango huo wa nje ikiwaka, akabonyeza kinobu cha kijani na kule nje ule mlango ukafunguka. Amata aliinua bunduki na kumfumua risasi ya mgongo.

“Aaaaaiiiiihhhhh umeniua mshenzi wewe,” yule bwana alilalama huku damu zikimvuja.

“Kufa tu, kwani we ulivyotaka kuniua kwenye ndege majuzi ulifikiri sikuoni,” akaiendea moja ya swichi kubwa iliyokuwa mezani hapo ambayo ambayo ilifanana na mkono wa gia ya gari, akabonyeza kitufe cha pembeni yake na runinga kubwa ikawaka mbele yake.

“Unataka kufanya nini wewe!” mmoja nakapiga kelele.

“Tulia mseng* wewe!” akamtuliza huku akimwonesha bastola. Kwenye kile kioo akaiona ile helkopta inayomsubiri Pancho na yeye na mke wake wakielekea kupanda tayari kuondoka.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Haondoki mtu hapaaaaa!” akasema kwa sauti na kuitembeza ile ‘gia’ mpaka alipohakikisha ameiweka sawa ile helikopta.

Mlipuko mkubwa ukatokea, ile helkopta ikalipuka na kuteketea kabisa ikamwacha Pancho na akiwa hana ujanja, akarudishwa ndani na walinzi wake.

Kamanda Amata akabaki anashangaa kwani yeye bado alikuwa hajafanya ulipuzi ule.

- * *

Chiba na Gina waliibuka katika kichaka cha mikoko, kila mmoja akiwa na silaha yenye akili. Chiba akamwonesha Gina ishara ya kuwa afungue mlango, Gina akaweka begani bunduki kubwa na kuufumua mlango wa chuma uliokuwa hapo, kisha wakaelea huko huku wakimwaga risasi kila upande anapoonekana adui. Wakaingia ndani na kuanza kupita kila korido na mlango wakiwapa kipigo adui zao huku wakishinikiza wapi Pancho atapatikana. Kelele za vilio na mirindimo ya risasi viligubika mle ndani vikisindikizwa na moshi wa baruti. Gina akashusha barakoa yake na kuuficha uso wake dhidi ya moshi huo uliokuwa ukimuumiza macho, na Chiba akafanya vivyo hivyo.

“Tumsake mwanaharamu,” Chiba akamwambia Gina, wakaanza kubomoa mlango mmoja baada ya mwingine wakipekua ndani kote wasimwone.

- * *

Kamanda Amata alipotaka kuondoka ndani ya kile chumba aliona taa fulani ikiwaka kama ile ya kwanza, akaiendea na kutazama iliandikwa ‘Escape Chamber’ akajua kwa vyovyote Pancho yupo upande huo.

“Control room, Control room!” moja ya redio ndani ya chumba hicho iliita, Amata akainyakua.

“Control Room is under attack,” akajibu na kuhisi kigugumizi upande wa pili.

“We ni nani unayeongea?” ile sauti ikamuuliza.

“Mimi ni Kamanda Amata, TSA namba 1, na sasa niko njiani kuja hukohuko uliko,” akajibu na kuiweka mezani ile redio kisha akaliachia lile bomu na yeye kutoka kasi. Kilichotokea nyuma yake ni mlipuko ambao uliharibu mitambo yote ya lile jengo. Amata alitupwa mbali na kuanguka vibaya kutokana na nguvu ya ule mlipuko, akajiinua lakini mara hii alianza kusikia maumivu makali katika sehemu yake ya ubavu.

Akanyanyuka kwa taabu na kutembea huku akijitegemeza ukutani kwa mkono mmoja na mwingine akijishika ubavuni kwenye jeraha lake.

“Kamanda!” akasikia akiitwa nyuma yake alipogeuka akakutana na mtu aliyevaa barakoa usoni mwake lakini kwa mwendo tu alimgundua kuwa ni Gina.

“Gina!”

“Yap! Pole sana Kamanda, nikuondoe eneo hili,”

“No! no! itafute escape chamber ndipo alipo mtu wetu,” Kamanda akamwambia Gina, naye akainua walkie talkie yake akaongea na Chiba na kumpa ujumbe huo huku akimpa taarifa Scoba na Jasmine kuingia kazini. Haikupita muda waliungana na Chiba na kuufikia mlango huo, mlango wa chuma uliofungwa ukafungika.

“Watakuwepo hadi sasa? Maana hii ni ‘escape’” Chiba akaeleza.

“Nimeharibu system nahisi watakuwa humo ndani kwani kwa sasa hakuna mlango unaoweza kufunguka kirahisi,” Amata akawaeleza.

Gina akainua tena ule mbunduki na kuuweka begani, bonyezo moja tu, ule mlango ulifumuka vibaya, na Chiba akajitosa ndani muda huohuo, Gina akafuatia na Amata akawa wa mwisho, saka nikusake. Kilikuwa chumba kikubwa ambacho ndani yake kulikuwa na boti iendayo kasi, Amata alipoitazama akajua wazi kuwa ile boti kwa muundo wake ina uwezo wa kupita chini ya maji.

“Wapo humuhumu,” akawaeleza wenzake.

“Vaeni barakoa zenu!” Kamanda akawaambia na wote wakavaa.

“Gina,” akaita na kumpa ishara. Gina akainua bunduki moja fupi na kufyatua kitu kama bomu kilichotoa moshi mkali sana kisha wakaendelea kutazama hapa na pale. Haikupita muda wakasikia mtu akikohoa. Gina akawahi na kufungua mlango mdogo uliokuwa mahala hapo.

“Toka mwenyewe!” alimwambia Zulekha aliyekuwa kajificha hapo, “na mumeo yuko wapi?” akauliza.

“Ushasema mume wangu we wa nini?” akajibu huku akikohoa sana. Gina akageuza ile bunduki na kumpiga nayo shavuni, ikampeleka chini Zulekha, akamshika mguu na kumburuza mpaka karibu na mlango, Amata akamkanyaga mgongoni.

“Tulia mrembo, tulia hivyohivyo,” Amata akamwambia Zulekha.

- * *

Helkopta kubwa lenye magurudumu lilikanyaga ardhi ya kisiwa cha kalebbe, wa kwanza kuteremka alikuwa Madam S, akafuatiwa na Jasmine kila mmoja alikuwa na bastola kiunoni mwake. Dakika hiyohiyo, helkopta nyingine ya polisi nayo ikafika eneo hilo a kuteremsha vijana kama kumi hivi waliotimia, kikosi maalumu cha kupambana na ujambazi chini ya Kamanda Tossi. Wakazunguka eneo kwa uhodari kabisa wakihakikisha kila anayepatikana anawekwa chini ya ulinzi na kufungwa pingu.

Madam S na Jasmine waliingia ndani huku vijana wachache wa polisi wakiwasindikiza nyuma na mbele. Nje ikafika boti iendayo kasi ‘KINYAMKERA’ ikAteremsha vijana wengine wenye silaha wakifuatana na Inpekta Simbeye, idara imekamilika. Wale vijana wakaingia ndani na wengine wakabaki nje kama kawaida. Kwa mawasiliano yao waliweza kujua Gina, Chiba na Amata wako upande gani, wakaenda huko.

- * *

Kamanda Amata aliliangalia moja ya kabati kubwa katika chumba walichoingia mara hii, kabati hilo lilimtia wasiwasi kwa jisi lilivyokaa na mahala liliPowekwa, akaliendea na kulipapasa huku na kule, akashika kitasa na kujaribu kukivuta, hakuna mlango uliofunguka.

“We mwanamke eleza mumeo alipo kabla sijatumia nguvu,” akamwambia Zulekha.

Zulekha hakujibu isipokuwa mikono yake ilikuwa kinywani mwake kama mtu anayeshangaa jambo. Kwa hali hiyo Amata alijua wazi kuwa amtafutaye yupo eneo hilo. Juu ya kitasa kile kulikua na kitu kama jiwe la yaspi ili kuongeza nakshi ya kabati hilo, akaliminya lile jiwe na kabati zima likasogea kando, ndani yake kulikuwa na uwazi ambao bila kificho Pancho alionekana ndani yake. Kutoka ndani mle, akatoka kwa kasi kwa minajiri ya kumvamia Amata lakini kabla hajamfikia, alikutana na konde zito lililomfanya ateme damu, la pili lilitua shavuni na kuacha meno kadhaa sakafuni la tatu lilimpeleka chini mzima mzima.

“Mwanaharamu mkubwa wewe, leo nimekutia mkononi kwa mara ya mwisho,” Amata aliunguruma huku bado akijishika ubavu wake.

“Simama,” akamwamuru lakini Pancho hakufanya hivyo. Akasahau maumivu yake na kumnyanyua kisha akamsimamisha mbele yake na kumkwida shati, akampiga kichwa kimoja kizito mpaka Pancho akaona nyota za ajabu zikimzunguka.

“Wewe unaweza kutusumbua sisi?” akamwuliza.

“Mwacheee!” Zulekha akajirusha kumvamia Amata huku mkononi akiwa na kisu, hakuna aliyejua wapi kakipata kisu hicho lakini hata hivyo hakuna aliyekumbuka kumpekuwa pindi walipomkamata. Gina kwa wepesi wa ajabu, aliinua bastola lake na kumfumua Zulekha kabla hajaufikia mwili wa Amata na kumbwaga chini akiwa hana uhai.

“Kwaheri Malkia wa Kalebbe!” akasema kwa sauti ya chini huku akishusha mikono wenye bastola chini. Pancho akapagawa kwa kitendo hicho, akajitoa kwa Amata na kumfuata Gina.

“Umemuua mke wangu!” akapiga kelele.

“Na wewe nakuua,” Gina aliongea. Amata alipoitazama sura ya Gina aliona wazi hakuna mswalie Mtume, alijirusha na kumpiga teke la mbavu Pancho akajibwaga upande wa pili na risasi ya Gina akapita peupe na kukiteremsha kioo kikubwa kikubwa ambacho kiliyaruhusu maji ya bahari kuingia ndani, mshike mshike. Wakamnyanyua Pancho na kutoka naye ndani ya chumba kile wakikimbia.

Mvumo wa maji ulisikika dhahiri shahiri yakianza kujaa upande wa chini wa jingo hilo, Amata akiwa na Gina na Pancho aliyeshikwa huku na huku walijitahidi kupanda ngazi kwa haraka kuelekea upande wa juu. Kengele za kuashiri hatari zilisikika kila kona na kila aliye ndani ya jengo hilo alijitahidi kuwahi kutoka.

Madam S na Jasmine walikuwa wa kwanza kufika nje huku wakijaribu kuwasiliana na Amata na wengine. Haikupita muda, waliwaona wakitokea katika kile kibanda kidogo. Madam S akawahi na kumkamata Pancho huku vijana wa polisi wakimtia pingu tayari kwa safari.

“Umekamatika mwanaharamu!” Madam S alimwambia mbaya wake wakati akifungwa pingu.

“Peleka kwenye helkopta!” Madam akatoa amri.

“Hapana Madam! Hilo si wazo zuri,” Amata akajibu.

“Fanya uwezavyo Kamanda, hakikisha tunakutana karakana!” Madam akamwambia huku yeye na wengine wakielekea kwenye ile helikopta.

Pancho akaingizwa kwenye ile boti, akifuatana na Amata na Chiba wakaondoka na mtu wao kuelekea Dar es salaam. Boti ile iendayo kasi ilikuwa ikipita chini ya maji na haikuchukua muda kuwasili katika ofisi yao iliyo ndani ya meli mbovu maeneo ya Kurasini. Wakamshusha na kumuingiza ndani ya meli hiyo.

Pancho aliketishwa kwenye stuli ya chuma, huku Chiba na Amata wakisimama pembeni.

“Mtawafunga wengine lakini si mimi,” pancho aliwaambia vijana hao.

“hatutaki ngonjera zako, fala wewe!” Chiba akamuwahi

“Aliyekwambi sisi tunakufunga nani? Leo hii tunakuua,” Amata akajibu huku mkono wake bado ukiwa ubavuni mwake.

“Ha! Ha! Ha! Nani aliyekwambia mtu hufa kijinga hivyo?” Pancho akaongeza swali la kuuzi.

“Kama alivyokufa mkeo Zulekha kwa mkono wa mwanamke, na wewe utakufa hivyohivyo kwa mkono wa mwanamke,” Chiba akamwambia.

Mara mlango wa chumba hicho ukafunguliwa na Madam S akaingia pamoja na Inspekta Simbeye wakifuatana na Gina, Jasmine na Scoba. Madam S akamtazama Muhindi huyo kwa hasira.

“Chagua kifo chako haraka!” akamwambia.

“We Kibibi, kukukosa kule Kerege usikiri nimekusamehe, ninyi ni waharibifu wa mipango ya watu, nitakuua ndani ya dakika hii,” Pancho aliongea na sekunde hiyohiyo alijinyanyua kwa kasi na kuchomoa bastola ya Simbeye kwa kutumia mikono yake iliyofungwa pingu, akimpiga kikumbo cha maana inspekta huyo na kumwacha akienda kujibamiza mezani. Kabla watu hawajakaa vizuri alikwishamgeukia Madam S na kumnyooshea bastola hiyo.

Kamanda Amata na Chiba walijikuta wakipigwa butwaa kwa tukio hilo, wakiwa katika kujiandaa nini wafanye wakasikia bastola ikilalama.

“Pah! Pah! Pah!” kila mtu ndani ya chumba kile aliziba masikio na kuinama chini. Pancho alijikuta akitazamana na bastola ya Gina, alisukumwa na kujibamiza ukutani kisha alijibwaga ardhini huku kichwa na kifua chake vikiwa vimetobolewa vibaya kwa risasi.

Gina alaiteremsha mkono wenye bastola taratibu na kuurudisha mahala pake huku akitoa sonyo refu.

“Hakuna madhara, TSA 5 katekeleza wajibu wake wa leo,” Gina aliongea na ndipo watu walipotazama na kumwona msichana huyo akiwa anapumua kwa nguvu.

“Asante Gina, leo umefanya kazi yako hasa,” Madam S akamkumbatia Gina kisha wakatoka kuelekea mahala pengine.

- * *

Baada ya siku nne…

AFISI NDOGO

“Kazi iliyotuumiza kichwa imekamilika, kila mmoja wenu kafanya vizuri kwa upande wake, natoa pole kwa Amata kwa majeraha aliyopata lakini ndiyo kazi yetu,” Madam S aliongea akiwa kasimama wima mbele ya meza yake ambayo nyuma yake kulikuwa na bendera ya Taifa na ile beji kubwa ya TSA ukutani. Upande wa pili kulikuwa na vijana watano, wa kike wawili na wa kiume watatu, waliosimama kwa ukakamavu huku kila mmoja akiwa na beji yake ya kazi katika mkanda wake.

“Pongezi nyingi kutoka Baraza la Usalama la Taifa, Mheshimiwa Rais anawapa pongezi kwa kzi nzito ya kuhakikisha mtandao huu unapotezwa,” akawaambia.

“Mtakwenda likizo wawili wawili kwa muda wa wiki mbili kila mmoja. Wataanza Gina na Amata kisha Jasmin na Chiba, Scoba na mimi tutakuwa wa mwisho kwa sababu maalum. Lakini kumbukeni hii ni likizo kazini, muda wowote nikiwahitaji mtafika hapa”.

Gina akamtazama Amata na kutoa tabasamu. Baada ya Madam S kumaliza kauli yake, wakaketi na kupata vinywaji huku wakibadilishana mawazo ya hapa na pale juu ya kazi yao na kila mmoja akijaza fomu za likizo

.

HOTELI YA RED STAR

“Mmmmmm Kamanda Amata, you are so sweet!” Gina alilalama huku akimpapasa Amata kifuani.

“Nashukuru kwa kuniokoa,”

“Ndiyo kazi yangu kukulinda mpenzi, nisipokulinda mimi nani atafanya hilo?” Gina akaongea kwa sauti ya kivivu, “unazeeka Amata hata mtoto huna,” akaongeza.

“We unaye?”

“Mi umri bado!”

“Unataka kunizalia mmoja?”

“Sio mmoja tu, hata ishirini…” Gina akajibu.

“Ooooh Gina,” Kamanda akajiinua na kuitazama saa yake, ilikuwa saa nne asubuhi.

“Unaenda wapi?”

“Twende tukaoge,”

“Oh, no! bado Kamanda mi nataka tena,”

“Mmmmh beibi,”

“Mmmm nini, nipe cha asubuhi bwana,”

Kamanda akarudi kitandani na kuanza kumbusu Gina kimahaba huku wote wakiwa hivyohivyo bila nguo, mchezo ukaanza upya kama si kuendelea.

Mara simu ya mkononi ya Amata ikaanza kuita kwa fujo, mlio huo haukumpa tabu kujua ni nani anayepiga. Akaitazama kwenye kioo na kuona kuwa hakukosea. ‘Madam S’ iliandika.

MWISHO

Kitisho

1

Mbowe club saa 1:23 usiku

RADI kali ilipasua anga na kufanya mchoro wa kutisha, mwanga wake ulilipoteza giza kwa sekunde kadhaa, kila kilichojificha kilionekana wazi.

Hakuna mtu hata mmoja aliyekuwa nje muda huo. Ni mvua kubwa na ngurumo za kutisha zilitawala kila kona, ilikuwa ni hali ya kuogofya sana. Mifereji na mito ya dhalura ilianzishwa na maji ya mvua hiyo.

Kama ilivyo ada katika jiji la Dar es salaam, barabara zote zilikuwa zimejaa maji, kama ukiwa dereva mgeni basi hutoweza kujua ni wapi barabara ilipo. Sehemu kubwa ya mji hasa katikati ya jiji gari nyingi ziliegeshwa kando ya barabara kusubiri mvua iishe lakini haikuwa hivyo kwani mvua ilikazana zaidi ya saa nne.

Wakati hayo yote yakiendelea, ndani ya ukumbi mkubwa wa starehe unaojulikana kama 'Mbowe Club' watu hawakuwa wakijua kama nje kuna mvua, disco liliendelea kwa nguvu zote, watu walicheza, wakanywa na kuburudika. Katika kaunta kubwa ya ukumbi huo kulikuwapo walevi kadhaa ambao tayari walikwishabadilisha lugha ya mawasiliano kutoka Kiswahili na kuwa Kiingereza.

Gina binti Komba Zingazinga alikuwa ni miongozi mwa watu wachache waliokuiwa wamesaliwa na akili zao na utashi pia, alikuwa akinywa kinywaji chake taratibu huku jamaa mmoja akijitahidi kumzengea zengea lakini asifanikiwe. Kila wakati alionekana kuitazama saa yake aliyoivaa mkononi na aliposhusha mkono aliinua ule uliokamata ile bilauri yenye kiuno iliyojaa mvinyo kutoka Dodoma. Baada ya kupiga funda moja kasha la pili aliiteremsha taratibu na kuiweka juu ya mbao mwororo iliyoifunika na kuipendezesha kaunta ya ukumbi huo. Macho yake yalikuwa yakizunguka huku na kule yakitazama au kutafuta kitu ambacho hata yenyewe hayakukijua.

Upande wa pili wa ukumbi huo, kwenye sakafu iliyojengwa juu kidogo na ili uifikie itakulazimu kuzikwea ngazi kadhaa, kulikuwako watu watatu, wawili wanaume na mmoja mwanamke. Mwanaume mmoja alikuwa na tambo kubwa lililojaa kimazoezi, enzi za utoto wetu tungeweza kumwita Pawa, lakini enzi hizi wanamwita Baunsa, yote hayo ni mabadiliko ya nyakati. Watu wale watatu walikuwa wakiongea jambo Fulani na meza yao ilikuwa imechakazwa kwa pombe kalikali na sahani za nyama zilizokuwa zikipishana, vyote hivyo vilimiminwa katika matumbo hayo matatu. Ilikuwa ni vigumu kusikia nini wanachokiongea kutokana na muziki mkubwa uliokuwa ukipigwa ndani humo. Kati ya kaunta alipokuwapo Gina na ule upande kulitenganishwa na kundi la vijana waliokuwa wacheza muziki huo kwa mitindo mbalimbali. Gina alihakikisha hapotezi macho yake upande ule kwani mwili wake ulikuwa ukisisimka mara kwa mara na hiyo kwake ilikuwa ni ishara ya hatari.

Dakika chache baadae alimuona Yule mwanamke akiinuka na kutoka katika vile viti, akitembea kwa mwendo wa ki-levi levi. Akamtazama na kujua mara moja kuwa alikuwa anaelekea chooni, Gina akajikuta akishuka kutoka kwenye kiti kirefu alichokuwa amekalia, akaigugumia pombe yake yote kinywani mwake, kasha akavuta hatua fupifupi akikumbana na walevi na wacheza muziki akaelekea kule alikokwenda Yule mwanamke.

Halafu nitamwuliza nini? Akajiuliza pa si na kupata jibu. Lakini aliendelea kuvuta hatua kuelekea kule chooni, akapinda kona ya kwanza na kuingia kwenye milango Fulani iliyokuwa ikielekea huko atakako, mbele kidogo alimuona Yule mwanamke akiingia katika moja milango ya vyoo vile. Gina; mkono wa kulia ukiwa nyuma ya suruali yake ndani kidogo ya jaketi lake, sikwambii alishika kitu gani, aliuendea ule mlango, mara ghafla akaanza kuhisi kitu kikimfinya mkononi mwake, ilikuwa ni saa kubwa ya mkononi, saa yenye uwezo wa kupokea nukushi, kupiga picha za mjongeo na mnato, yenye uwezo wa kurekodi sauti na pia unaweza kuitumia kama simu. Akainua mkono na kubofya kitufe Fulani kasha akasubiri kidogo. Wakati akisubiri kijimkanda hicho chembamba kikitoka kwenye saa yake, Yule mwanamake bado alikuwa chooni.

Mama yuko mahututi Shamba, Tena Saan Aisee! Uikuwa ni ujumbe uliosomeaka hivyo katika kile kijimkanda. Akakikata na kukitia mfukoni mwake kisha akaanza safari ya kutoka ndani ya Klabu ile, akili yake ilikwisha sahau juu ya Yule mwanamke, akapita mlangoni na kukumbana kikumbo na Yule mwanaume mwenye tambo kubwa, akielekea kule choo cha wanawake, Gina akasukumwa pembeni; na Yule bwana akapita.

Nje ya Klabu hiyo ndipo alipokutana na mvua ya kutisha, akapachua kikofia katika ukosi wa jaketi lake na kukivaa kisha akaliendea gari lake, mita kadhaa kabla hajalifikia akapiga breki na kuacha kinywa wazi, hakuamini anachokiona. Vioo vyote vya gari yake vilikuwa vimevunjwa, tairi hazina upepo na ndani kulijaa maji ya mvua. Wameiba? Akajiuliza, kisha kwa mwendo wa tahadhari akasogea kwenye lile gari, juu ya kiti cha dereva kulikuwa na bahasha ngumu ya khaki, akatazama huku na kule, alipojihakikishia usalama akaingiza mkono kwa minajiri ya kuichukua ile bahasha ijapokuwa ilionekana kulowana.

Daraja la sarenda saa 1:55 usiku.

BMW nyeusi iliyokuwa iking'azwa kwa mwanga wa radi, ilshuka katika barabar hiyo ya Kenyata kwa kasi sana ikitokea maeneo ya Masaki. Ilipofika katika makutano ya barabar hiyo na ile ya Ally Hassan Mwinyi mkabala na Ubalozi wa Ufaransa iliingia barabara kubwa bila kungalia usalama huku ikirusha maji juu kutokana na mvua kubwa iliyokuwa ikinyesha usiku huo.

Madam S alikuwa katulia kwenye usukani akiiongoza gari hiyo ya Mwingereza kwa umahiri mkubwa. Akakunja ushoto na kukanyaga mafuta kueleka mjini. Ilikuwa ni tabu kuona mbele kutokana na wingi wa mvua, barabara imejaa maji, umeme umekatika, ilikuwa ni shida juu ya shida. Madam S hakujali alilikanyaga daraja la Salenda na kuendelea mbele, lakini kabla hajalimaliza, hamad, kulikuwa a mwili wa mwanadamu uliolala barabarani huku mikono yake ikiwa imefungwa nyuma. Akaiyumbisha gari kuukwepa mwili huo, gari ikasota na kukosa muelekeo, akarudisha usukani kulia kuukwepa mwamba wa daraja, akaknyaga krachi na kuachia mafuta kasha akatoa gia ya tano na kushusha ya nne, kutahamaki gari yake ilikuwa ikihamia barabara ya pili, akakanyaga breki lakini ikashindwa kusimama, akaknyaga tena breki bado gari ilikuwa ikiendelea, ikapanda tuta lakutenga barabara, ikajipigia na kutua barabara ya pili, akili ikamrudia, akavuta breki ya mkono na ile BMW ikaserereka na kujizungusha.

Kishindo kikubwa kikasikika, BMW iligongana na Land Rover Defender, ikaangushwa pembeni. Madam S akajikuta kwenye pori la mikoko chini ya daraja la Salenda, akafyatua mkanda, akapiga kioo cha mbele kwa kukikanyaga kwa mguu, akatoka, akajipapasa na kukuta bastola zake zipo salama.

Damu zilizikuwa zikitiririka semu ya paji la uso juu kidogo ya jicho la kulia, wakati akijitahidi kusimama, radi kali ilipiga na kufanya mwanga mkubwa uliong'aza vichaka vyote, Madam S akaona mbele yake kama kivuli cha mtu aliyesimama nyuma yake. Akajua ni mawenge ya ajali tu, akageuka nyuma na mara ghafla akakutana na pigo la kitu kizito kilichotua katikati ya paji la uso, akayumba vibaya lakini mikono yake tayari ilikuwa imekwishachomoa bastola zake, kabla hajafyatua akafunikwa na gza nene lililomfanya ashindwe kuona chchote, akaanguka kama mzigo na bastola zikimtoka mikononi mwake.

Ofisi ya usalama wa taifa saa 2:00 usiku.

MAAFISA wa Idara ya Usalama wa Taifa walikuwa wakiendelea na shughuli zao kama kawaida usiku huo. Katika moja ya ofisi za jengo hilo, vijana wawili na msichana mmoja walikuwa bize kutazama luninga nyingi zilizowazunguka zinazoonesha maeneo mbalimbali muhimu ya Jiji la Dar es salaam. Kupitia luninga hizo waliweza kuona moja kwa moja kile kinachotokea kwenye maeneo hayo kama Uwanja wa ndege, Bandarini, Stesheni ya Treni, Uwanja wa Sabasaba, Makao makuu ya Rais na maeneo mengine mengi ambayo yamepewa umuhimu wa pekee kwa sababu hii au ile.

Avant, msichana mbichi wa miaka takribani thelathini hivi alikuwa katingwa kuangalia tukio la ajali iliyotokea daraja la Salenda, bado alikuwa anapata shida kujua hasa nini kinaendelea kutokana na ile picha kufichwa na mvua ilikua ikinyesha eneo hilo lakini kila ilipokuwa radi ikipiga ndipo alipoweza kuona kitu, baada ya dakika kadhaa alipuuza na kuendelea kutazama maeneo mengine.

Mubah akajikohoza kidogo na kumgutusha Avanti kutoka pale alipokuwa akitazama.

"Si ukapime, au Mama yako anajua?" Avanti akamtania Mubah.

"Unanianza we mrembo, mi nasubiri time hapa niingie viwanja!" Mubah akajibu, huku akitoka kwenye kiti chake na kukiendea kile alichoketi Avant, akasimama nyuma yake, machoye akiwa kayakaza kwenye ile luninga.

"Shiit! Avant, nini hicho?" akauliza huku akisogea jirani zaidi.

"Ajali, imetokea kama dakika kumi hivi," Avant akajibu.

"Kwa nini usipige simu polisi wawahi kama kuna chochote cha kuokoa?" Mubah akahoji.

"Sasa Mubah, Salenda pale kituo kipo jirani wataenda tu," akaeleza huku akimtazama Mubah usoni.

"Yaani wewe! Kitendo cha kuitega kamera pale hatukufanya kwa makosa, lile ni eneo nyeti sana, kama ni ajali lazima polisi wafike mapema ili kuondoa kilichopo, pale vipngozi asilimia 99 wanapita, ikiwa hujuma utalaumiwa wewe kwani ndio eneo lako la kutazama leo!" Mubah akalalamika huku akiliendea kabati dogo lililo hapo jirani.

Avant akainua simu na kubofya tarakimu Fulani Fulani kasha akatoa taarifa hiyo kituo cha polisi cha Salenda. Haikupita dakika tano tayari kupitia luninga yake aliweza kuona gari na nyendo za polisi eneo hilo bila kujali mvua iliyopo. Avant aliendelea kutazama huku akigonga gonga karamu yake.

§§§§§

Gina alivuta hatua na kuingia katika lango kuu la Ofisi Nyeti, Shamba, akabofya namba zake za siri, kasha akaweka kiganja chake juu ya kioo Fulani kilichopo mlangoni na baada ya hapo akafanya kama anachungulia, kijimwanga chekunfu kikapita kati ya macho yake na kitasa cha ule mlango kikafyatuka, akaufungua na kuingia ndani. Moja kwa moja akaingia chumba Fulani na kuvua jaketi alilovaa, akabadilisha nguo na kurudi katika hali ya ukavu, akatoka na kutembea mwendo mfupi kabla hajagonga mlango Fulani kwa mtindo wa pekee na mlango ule ukafunguliwa.

“Karibu Gina!” Dkt Jasmine akamkaribisha na nukta chache baadae akampatia kikombe cha kahawa.

“Hawajafika?” Gina akauliza.

“Hapana, we ndiye wa kwanza, leo sijui kuna nini, labda kwa sababu ya mvua,” Dkt. Jasmin akaeleza.

Gina akashusha pumzi ndefu, mazungumzo mengine yakaendelea huku wakiwasubiri wengine, kila mara walikuwa wakitazama saa zao, hakuna simu wa taarifa yoyote iliyokuwa ikifika katika nyumba hiyo, Gina na Jasmine wakaanza kupata wasiwasi. Jasmine akainua uso na kuitazama saa kubwa ya ukutani, ikamwonesha kuwa ni saa 3:15 usiku.

“Hapana Gina, hii sio kawaida, tuanze kuwatafuta mmoja baada ya mwingine,” Dkt. Jasmin akamweleza Gina, kasha wote wawili wakaenda kwenye chumba maalumu cha mawasiliano, ndani ya chumba hicho ambamo ndiyo ofisi ya kudumu ya Chiba wa Chiba kulijawa na makompyuta na luninga nyingi huku na kule, simu za upepo, za kawaida na zile za satellite zilikuwepo. Kila kitu kilikuwa kinafanya kazi kwani haikuruhusiwa kuzima chochote labda tu kama kuna matengenezo, kila mmoja akaketi katika kiti chake na kuanza kucheza na simu zao za siri zilizounganishwa moja kwa moja.

Hakuna simu ya mkononi iliyokuwa ikipatikana si ya Madam S wala ya nani, walipigwa na butwaa na kubwa simu za nyumbani zote zilikuwa zikiita bila kukoma hazikupokelewa. Gina akamgeukia Dkt. Jasmine.

“Oya Shost, hapa ni mguu kwa mguu nyumba moja baada ya nyingine tukapate kujua kilichojiri,” Gina akamwambia Jasmine kasha wote wakaingia vyumbani na walipotoka walikuwa katika mavazi ya kazi, kila moja alibeba silaha anazoamini zingemfaa usiku huo kwani hawakujua hatari itakayowakabili. Wakiwa katika harakati hizo ndipo Gina alipokumbuka ile bahasha.

“Nisubiri Jasmine!” akarudi kwenye kile chumba akaichukua ile bahasha, bado ilikuwa imelowa akaichana taratibu na kuitoa karatasi ya ndani kwa uangalifu.

“Nini Gina?” Jasmine akauliza.

“Hii bahasha niliiokota kwenye ari yangu lakini sikuwahi kuifungua ndani,” akamjibu.

Gina alibaki kakodoa macho baada ya kukutana na kichwa cha habari kikubwa kilichosomeka ‘KITISHO!’ kisha chini yake kuliandikwa sentensi moja tu

Mwisho wa zama zenu umefika, mtaongea na Mzee Ngurumo.

Maneno hayo yalizigonga kwa nguvu nyoyo za wadada hawa, wakabaki wakitazamana, wkageuza macho yao wakaitazama tena ile karatasi.

“Gina!” Jasmine akaita.

“Jasmine!” naye akaitikia na wote wakatoka na kuingia kwenye gari ya Jasmine na kuondoka eneo hilo.

§§§§§§

Kerege – bagamoyo saa 4:07 usiku

TOYOTA Hilux Double Cabins, iliingia taratibu getini na kuegeshwa karibu na bustani ya maua iliyotengenezwa ndani ya ngome kubwa iliyobeba jengo la kifahari kuliko fahari yenyewe. Walinzi kadhaa walionekana kwenye kona zake, hawakushughulika kabisa na gari hiyo bali kila mmoja alishika lindo lake.

Dereva akashuka na watu wengine kama watatu hivi wakashuka, wakazunguka nyuma na kufungua funiko kubwa la alluminium lililotengenezwa ili kufunika mzigo uliopo ndani yake.

“Washushe hao, kisha wapeleke Kuzimu,” mmoja wa wale vijana aliyekuwa ameketi mbele akawaagiza wenzake kasha yeye akazikwea ngazi kulielekea jengo hilo lililoendezeshwa kwa taa zenye marembo mbalimbali.

Sauti za viatu vyenye kisigino kigumu zilisikika zikitembea lakini aliyevaa hakuonekana, Bwana Mpaya alibaki kusimama na kutazama kule sauti ile ilikokuwa ikitokea na asione mtu zaidi ya giza lililomlaki isipokuwa aliposimama yeye mwanga ulikuwapo na kufaya nuru ya kupendeza. Kasha ukimya ukatawala na sauti nzito ikalipenya lile giza.

“Ndio Bwana Mpaya, karibu sana, natumaini umekamilisha nililokutuma, sivyo?” alikuwa ni Pancho Panchilio aliyeyafikia masikio ya Mpaya aliyekuwa amesimama katikati ya sebule pana lakini asimwone anayeongea naye, isipokuwa sauti tu.

“Ndiyo Boss, tumewaleta lakini hali zao ni mbaya sana,” akaeleza.

“Vizuri sana, nani na nani mmempata?” akauliza tena.

“Tumempata Boss wao na Mtaalamu wao wa kompyuta,” akajibu.

“Ha! ha! ha! ha! ha!” akacheka cheko la pesa.

“Ok, wape vijana posho yao kama nilivyokwambia kisha unitafutie kichwa cha Kamanda Amata, huyu hasa ndiye mwiba kwangu, nataka apotee kwenye uso wa nchi ili binadamu tule vizuri, kuna pesa ndefu sana nimeiandaa mkilikamilisha hili,” Pancho akiwa mafichoni mwake akakohoa kidogo wakati Mpaya alikuwa akitoka, “Sikia Mpaya, hakikisha ukimuua Kamanda Amata, mkate kichwa, kisha kiwiliwili mkichome moto na kichwa mniletee, mbwa wangu hawajala nyama siku nyingi sana, maana Yule ni shetani anaweza kujiunganisha tena halafu akaangusha balaa, kwa heri!”

Alipomaliza kusema hayo na taa ndani ya jengo lile zikazimika.

2

KAMANDA Amata akaitazama gari yake aia ya Subaru Forester jinsi ilivyochakazwa kwa risasi, akashusha pumzi ndefu.

Wadude hawa wangeniua! Akajisemea moyoni huku akijaribu kuiwasha nayo ikawaka, akairudisha barabarani na kushika njia ya kwenda mjini, alijipapasa mifukoni hakuiona simu yake, wala saa yake mkononi haikuwepo. Any way! Akajipa moyo. Huku akiendelea kuutafuta mji wa Dar es salaam, saa ya ndani katika gari yake ilimwonesha kuwa ni saa tano za usiku.

Gina sijui kama atanielewa, maana tulikubaliana saa moja na robo, labda nitamkuta! Akaendelea kuongea na nafsi yake, huku akiiacha Gongo la Mboto na kuitafuta Uwanja wa Ndege. Katikati ya safari yake akafungua redio ndani ya gari na kusikiliza kinachoendelea. Ilikuwa ni kituo kimoja cha redio binafsi kikirusha habari hiyo ya dharula iliyoyanasa masikio ya Amata usiku huo.

…Mwili wa Mheshimiwa huyo umekutwa sakafuni bila uhai na kitu kama matundu ya risasi yakionekana kifuani mwake. Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wake ili kuwakama waliohusika na mauaji hayo…

Amata akakanyaga breki kali na kuitoa gari barabarani kwani taarifa hiyo haikujitosheleza kwake, akaegesha gari pembeni na kutazama huku na kule hakuona mtu kupita eneo hilo, pembeni yake kulikuwa na bar iliyokuwa ikiendelea kuburudisha watu kwa vinywaji na vilaji, akashuka na kuiendea, alipofika tu akakutana na mwanadada mrembo aliyevalia nguo nyeupe juu na sketi nyeusi chini.

“Karibu kaka, karibu kiti,” Yule dada akamkaribisha Amata huku akifuta meza iliyokuwa hapo. Ijapokua haikuwa nia ya Kamanda kuketi, akajikuta amefanya hivyo, “Pole!” neon hilo likaupasua moyo wa Amata akamtazama Yule dada Mhudumu wa bar.

“Pole ya nini?” akauliza

“Una damu kichwani,” akamwambia.

“Shiit!” akang’aka na kujigusa, kweli akahisi maumivu na kitu kama jeraha.

“Asante sana!” akamjibu, “Unaweza kunisaidia simu yako?” akamwuliza.

“Haina salio lakini, halafu ni kisimu cha tochi,” akajibu kwa aibu.

“Naomba hivyo hivyo.”

Yule mwanadada akachomoa simu yake akampatia Amata. Ilikuwa ni simu iliyochakaa, iliyoonekana kupita katika mikono mingi ya watu mpaka kuifikia mikono hii ya huyu Mhudumu wa baa. Ilifungwa kwa mipira ya manati, betri lake lilishikiliwa na kipande cha mpira wa manati. Hakujali, aliitazama vyema kasha akaanza kubofya hapa na pale.

“Haina vocha hiyo!” Yule Mhudumu akaeleza tena.

“Usijali, kaniletee Bia baridi sana bila glass tafadhali,” Kamanda akamwagiza Yule dada lakini alilotaka yeye haikuwa bia ila zile dakika mbili za kubaki peke yake. Vidole vyake vikaanza kutomasa tarakimu Fulani Fulani na alipomaliza, akapumzika, wakati huo bia yake ilikuwa imefika, akaigusa, akamwonesha Yule Mhudumu alama ya dole gumba, kisha akabaki na hamsini zake.

Meseji iliyofuata katika simu hiyo ilikuwa ni kutoka katika kampuni moja ya simu nchini, Kamanda Amata alikuwa amechukua muda wa hewani kwa namna yao ya siri na sasa simu ile Kimeo ilipata uhai.

Akaanza kupiga namba za maswahiba wake wa kazi, Chiba; simu haikuita kabisa, Madam S vivyo hivyo, akaduwaa wa sekunde kadhaa, haikuwa kawaida kwa watu hao kuwakosa kwenye simu, akili ya Kamanda ikiruka chogo chemba. Mbele yake kulikuwa na luninga kubwa iliyokuwa ikionesha matukio mbalimbali ya Kitaifa na lile lililomvutia ni ajali ya Salenda, alisahau kupiga simu na kutazama tukio lile. Kamanda Amata alikaza jicho kutazama picha hizo lakini hakuzitilia maanani kwani wakati wa mvua ajali kama hizo ni za kawaida sana.

“Kaka hadi bia imepoa!” Yule Mhudumu alipita tena kwenye ile mea aliyokaa Amata.

“Oh, sorry,” akamjibu kasha akainua chupa na kujijiminia mafunda kadhaa, alipoishusha ilikuwa nusu tu.

Akaitazama tena ile simu akabofya tarakimu nyingine, akaweka sikioni, simu ikaita na kuita haikupokelewa kama ilivyokuwa kwa simu za nyumbani za Chiba na Madam S, akashusha pumzi. Nini kinaendelea? Akajiuliza. Akarudia kuipiga namba ya mwisho, akaweka simu sikioni, baada ya dakika moja ile simu ikakwapuliwa na sauti nyororo ya kike ikasikika tofauti na alivyotegemea.

“…Polisi Kituo cha Kati, nikusaidie nini?” ile sauti ikauliza.

“Mwenye Ofisi, Inspekta Simbeye yupo?” Kamanda akauliza.

“…Inspekta leo alitoka kama mida ya saa tisa alasiri, hajarudi bado…” Yule mwanadada akajibu.

“Alisema kuwa atarudi au aliacha maagizo yoyote?” Kamanda akauliza.

“…alisema tu kuwa angerudi kabla ya saa kumi na ni kawaida yake kutoka saa tisa na kurudi saa kumi kila siku, lakini leo mpaka sasa hajarudi…” sauti ile iliendelea kueleza.

“We umeingia kazini saa ngapi?” akamwuliza.

“…nimeingia saa nane nitatoka saa nne usiku… samahani lakini naogea na nani?” Yule mwanadada alipouliza hivyo simu ikakatika.

Ndipo Kamanda alipojikuta hayuko peke yake mezani, mbele yake kulikuwa na mwanamke mmoja aliyevaa vazi refu jeusi, hijab na kujificha uso wote isipokuwa macho. Kamanda Amata akamtazama mtu huyo kwa tuo, akainua chupa yake na kupiga funda la mwisho, alipoishusha ilikuwa haina kitu ndani.

“Kwa nini unapenda kudhalilisha dini ya watu? Unaingia baa na vazi kama hilo?” Kamanda akaanza uchokozi, lakini Yule mtu hakujibu kitu, alikuwa akimwangalia tu. Jinni au! Akajiwazia, kabaridi ka haja kakapita kutoka utosini mpaka unyayoni.

§§§§§§

GINA aliegesha gari mita mia mbili hivi kutoka katika lango la kuingilia nyumba ya Madam S kule Masaki, akateremka na Jasmine akafanya vivyo hivyo, kisha wote wawili wakarudi taratibu wakiachina nafasi ya mita kadhaa katikati.

Lango la mbele lilikuwa limefungwa, Gina alitazama huku na huko hakuona hata dalili ya binadamu kupita myaa ule, isipokuwa manyunyu tu ya mvua yalikuwa yakimnyurunyuta mwilini mwake. Akajipapasa katika kiuno cha suruali yake na kufatua kijipini chenye ncha mbili zilizojikunja kwa mtindo wa pekee, kishapo akachukua kipini kingne kutoka kwenye kibanio cha nywele zake, akatanguliza kile chenye ncha mbili katika tundu la funguo ya lango hilo, akachukua kile cha tatu na kukitumbukiza kati, akafanya manuva kidogo tu, kitasa kutoka Uingereza kikafyatuka na kuuruhusu lango lile kuwa wazi.

Skunde mbili zikapita, ya tatu na ya nne bila Gina kuingia ndani ya wigo ule mkubwa, akatazama tena usalama, bado barabara ilikuwa tupu, hakumuona Jasmine, moja kwa moja akajua kuwa kwa vyovyote keshajiweka katika kona maalum ya kumlinda swahiba wake. Akaingia ndani ya wigo huku bastola yake aina ya Winchester ikiwa mkononi. Akatembea kwa hadhari kubwa huku na huko akitazama hakuona mtu. Hatua tatu kuelekea mlango wa nyumba hiyo, ndipo alipoona kitu kilichomshtua sana, akasimama mapigo ya moyo yakimwendea kasi kifuai mwake.

Mbele yake kulikuwa na mwili wa Binadamu uliolala chali ukiitupa mikono yake huku na huko, hakuwa na uhai. Gina akajiweka tayari kwani aliona huo unaweza kuwa mtego kwake, akatazama jumba la Madam S, taa za ndani zilikuwa zikiwaka kwa mwanga wa kupendeza, ina akajikuta anaishiwa nguvu, akainua mkono wake na kuizungusha saa yake kwa namna ya pekee kasha akaisogeza karibu na kinywa chake.

“…Jasmine …” akaita, hakupata jibu, akazidi kuingiwa na wasiwasi. Dina akatulia pembeni ya ule mwili, akahisi kama kuna mtu anayekuja nyuma yake, akakamata bastola yake barabara, liwalo na liwe, akageuka ghafla tayari kwa shambulizi, hakuna mtu.

Shiit! Akajisemea. Akauruka ule mwili na kuufikia mlango wa nyumba ile kubwa, akatoa gloves mfukoni na kuivaa, kisha akashika kitasa kwa mkono wa kushoto uliokuwa na gloves akaingia ndani ya sebule pana, iliyomlaki bila hiana. Kila kitu kilikuwa katika utulivu wa hali ya juu sana, hakukuonekana kama kulikuwa na purukushani yoyote ndani ya nyumba hiyo, akajivuta kuelekea chumba cha Madam S, akaufikia mlango na kuujaribu, ulikuwa umefungwa. Akatumia hila ileile na kuufungua. Hata chumbani kulikuwa tulivu kabisa, hakukuwa na ishara yoyote iliyoonesha kama kulikuwa na pambano la kufa na kupona.

Akaenda pembeni mwa kitanda upande wa kichwani, akachuchumaa na kubonya vijinamba Fulani vya kificho ambavyo kwa mtu wa kawaida huwezi kuvigungua mpaka mmiliki akuoneshe. Droo moja ikafunguka na ndani yake ikajifunua kompyuta kubwa ika simama mbele yake, Gina akatikisa kichwa juu chini, kwani alijua kama hiyo kompyuta haipo mahala pake basi hali ya Taifa iko hatarini. Alikumbuka maneno ya Madam S siku alipomkaribisha nyumbani kwake kwa mara ya kwanza.

….heri mimi nife lakini hii kompyuta ibaki. Nikifa au nikipotea kabla hamjatangaza kifo change hakikisheni mnang'oa kompyuta hii na kuikimbiza Shamba kisha mtangaze matanga. Siri yote ya Taifa hili ipo hapa, mipango yote mibaya na mizuri ipo humu, watu wote wabaya na wazuri wapo humu…

Gina alijikuta analia machozi peke yake, nifanyeje, niondoke nayo? Akajiuliza, nitaifikisha Shamba salama? Akajiuliza bila majibu. Gina alijikuta kachanganyikiwa, hajui la kufanya, aichukue au aiache, kichwani mwake alielewa kuichukua kompyuta hiyo ina maana kuwa Madam S kafa au katoweka, na je kama kuna wanaotaka na wameshindwa kuipata hatoweza kuwa kawarahisishia kazi?

Ulikuwa ni mgongano mkubwa wa mawazo kati ya roho, moyo na ubongo wake, akaamua kuiacha. Akabofya tena zile tarakimu na ile kompyuta ikajirudisha ndani taratibu na kujigia mahala pake. Gina akashusha pumzi ndefu, akaitazama bastola yake na kunyayuka taratibu, akaufuata mlango na kutoka akiufunga nyuma yake.

KAWE – saa 4:02 usiku

LAND CRUISER ya polisi ilikuwa nje ya lango kubwa la nyumba ya Mheshimiwa Mbunge wa jimbo la Miroroso, wananchi wasio na dogo nao walijumuika nje ya nyumba hiyo wakikodoa kodoa macho kushangaa tukio hilo lisilo la kawaida. Hakuna aliyejali mvua ya rasharasha iliyokuwa ikiendelea kunyesha, watu walijikusanya kwa kujikunyata kutazama.

Ndani ya jumba hilo kulikuwa na Polisi waliovaa kiraia wenye bunduki kubwa kubwa wakiwa wanatembea hapa na pale, mwili wa marehemu Mbunge ulikuwa ndani ya chumba chake cha kulala. Polisi waliokuwa huko chumbani wakifanya taratibu zao za uchunguzi walikuwa wamekamilisha kazi yao, walitoka sebuleni na kuwapisha vijana wachache kutoka idara ya dharula ya kampuni binafsi ambayo husambaza gari za wagonjwa mitaani kwa minajiri ya kusaidia hali za dharula kama hizo.

Waliufunga sawia mwili wa Mheshimiwa katika mfuko maalumu na kuupakia kwenye machela yenye magurudumu, kasha wakaisukuma kuelekea kwenye gari yao iliyokuwa imeegeshwa pembeni tu mwa jumba hilo. Vilio vilisikika, wananchi wakalia na kuomboleza, walimpenda Mheshimiwa, ijapokuwa alipojenga jumba lake haikuwa jimboni mwake lakini bado alitoa misaada ya hali na mali kwa waliomzunguka.

"Alikuwa shujaa, kwa vyovyote wametumwa kumuua," mwombolezaji mmoja alisikika akisema huku akifuta machozi yake.

Baada ya zoezi hilo ndipo Wananchi waliruhusiwa kuingia ndani na kuanza msiba huo. Hakuna aliyeamini kabisa juu ya lililotokea.

Lakini ilibaki hivyo kuwa Mbunge wa jimbo la Miroroso aliuawa na watu wasiojulikana.

§§§§§§

Kamanda Amata aliwekwa kati ya watu wawili huku mmoja na huku mwingine, mbele yake kulikuwa na mwingine tena ukiacha dereva aliyekuwa akiongoza gari hiyo. Wote walivaa maguo yaliyowaficha miili na sura zao. Hakuna aliyeongea; ile gari ilipita daraja la Salenda na kufuata uelekeo wa kwenda Mwenge, baada tu ya kupita daraja hilo, ikakunja kulia na kufuata ile Kenyata Drive, ilipomaliza maofisi ya Mabalozi iliiacha ile ya kwenda Coco Beach na kukunja kushoto, nyumba ya nne mbele ikasimama.

"Usilete makeke yako ya kipumbavu, tunataka kompyuta anayotumia boss wako basi," akaambiwa na kuteremshwa chini, wakauendea mlango mkubwa na kuufungua, Kamanda Amata akatangulia mbele na wale jamaa wakamfuata nyuma, wote watatu walkuwa na Shot Gun mikononi mwao.

Wakatembea taratibu na kuipita ile maiti pale nje, moja kwa moja wakaingia ndani ya sebule, mmoja wao akasimama nje ya mlango wa sebule kuweka usalama, mwingine akabaki sebuleni na wa mwisho akaenda na Amata mpaka chumba cha Madam S.

“Usilete ujanja wako, tunajua kuwa ni wewe tu unayeweza kuitoa hiyo kompyuta hapo, haya fanya hivyo,” akamwambia huku akiwa kasimama umbali wa mita kama mbili hivi. Kamanda Amata akaiendea ile droo na kuingza mkono wake mahala Fulani, akapapasa anavyojua yeye, mara ile droo ikajivuta mbele na kufunguka, hakuna kompyuta! Yule mjinga akabaki katoa macho, akashangaa mahala pale hakuna kompyuta waliyokuwa wanaitaka ilhali wao walikuwa na uhakika kuwa ipo hapo baada ya kufanya uchunguzi wa kina.

“Haipo?” akauliza.

“Si unaona mwenyewe haipo!” Kamanda akajibu.

“Imeenda wapi?” akarusha swali la kijinga.

“Mimi na wewe tumeingia pamoja sasa nitajuaje ilipokwenda?” Kamanda akajibu kwa swali. Kama kuna kosa alilolifanya Yule mtekaji na atalijutia kuzimu ni ktendo cha kwenda kuhakikisha kwa macho kuwa Kompyuta ile haipo pale. Kamanda Amata kama umeme, kutoka pale alipokuwa amechuchumaa kuitoa ile Kompyuta, alijikunjua na kutawanya miguu yake sentimeta mbili kutoka usawa wa sakafu, Yule mjinga alipigwa ngwala kutoka upande wa nyuma na kujibwaga akitanguliza kisogo, yowe na kishindo vilimshtua Yule wa sebuleni akaja kwa kasi. Kamanda Amata alijirusha upande wa pili wa chumba na risasi zilizotoka katika bunduki ya Yule mtu wa pili zikachimba sakafu.

Kabla Yule bwana hajajiweka sawa, mwendo wa sekunde moja tu aliyoitumia kufanya shabaha ya pili dhidi ya Kamanda Amata, alijikuta akipaishwa juu na kujibwaga kama mzigo sakafuni tayari damu ilikuwa ikimtoka kama bomba. Amata alishuhudia hilo kwa haraka sana hakuelewa nini kinatokea.

Wamegeukana? Akajiuliza.

“Upo salama Kamanda Jitokeze!” sauti ya Gina ilimrudishia matuamaini. Kamanda Amata akajitokeza mzima mzima, lo! Domo la shot gun lilikuwa likimtazama umbali wa mita tatu tu kutoka pale alipo.

“Umeharibu utaratibu, nilikwambia usifanye makeke yoyote sasa wewe umekiuka kanuni, namuua huyu Malaya wako kasha naondoka na wewe,” sauti ya mtekaji ilisikika. Kamanda Amata akaona sasa mchezo usio rasmi unaanza kwani hakuwa na taarifa yoyote juu ya hii hatari.

“Umeshasema Malaya, we muue tu, hana thamani kwangu!” Kamanda akajibu.

“Leo hana thamani kwako wakati kila siku unamlala nyumbani kwako!” Yule mtekaji akaendele kuropoka, maneno ambayo yalimtia hasira Gina, akajaribu kukukuruka lakini hakuweza kutoka kwani kono la mtekaji lilimbana koo na akajihisi kukosa pumzi. Kamanda Amata alaimtazama Gina anavyoteseka, akawasiliana naye kwa macho, gina alielewa kitendo alichokifanya Kamanda.

Gina aliachia mkono wake kutoka kwenye ule wa Mtekaji lakini bado alikuwa kabanwa kwa kabala, akajizungusha na kukamata uume wa mtekaji huyo, akaubana kwa nguvu na kuuzungusha ghafla. Yule mtekaji akapiga kelele za maumivu, akamwachia Gina akabaki katoa macho ya kutisha, Gina akaendelea kuuzungusha huku amezikamata na korodani zake, Yule mtekaji akaanguka chini, Gina hakumwachia mpaka alipohakikisha kamtoa roho.

“Asante Gina!” Kamanda akamshukuru wakakumbatiana.

“Kompyuta Gina,” Kamanda akamwambia.

“Usiwe na shaka, nimekwishaitoa muda mrefu, wakati naondoka ndipo nilipoona hiyo gari inakuja, nikajibana hapo kwenye kochi kubwa upande wa nyuma hamkuniona. Niliposikia kile kishindo huko chumbani mlipo, nikajua kumekucha, nikamwona huyu wa sebuleni akija kwa kasi huko ndani, name nikajitokeza kumwahi kabla hajaleta madhara, ndipo nikamfumua bichwa lake, lakini sikujua kama kuna mwingine huku nje ndo huyu mpumbavu akanibana kabala. Pole sana Kamanda, nafurahi kukuona, Idara imetikiswa!” Gina alieleza kinachojiri.

“Gina haina haja ya kukaa hapa, twende tukajipange juu ya hili,” Kamanda akamwambia huku wakitoka. Walipofika karibu na geti, Gina akauchukua begi kubwa alilokuwa amelificha hapo wakatoka nje.

“We ulikujaje hapa?” kamanda akamwuliza.

“Shiiit!” Gina aling’aka baada ya kugeuka na kutoiona gari aliyokuja nayo. Akageuka kwa Kamanda na kumtazama usoni.

“Dr. Jasmine!” akamwambia huku chozi likimtoka. Amata akamtazama na kisha akaliendea lile gari walilokuja nalo na wale watekaji, akaingia, bahati nzuri halikuhitaji ufunguo, lilikuwa ni la kubonya tu nalo likawaka, wakaingia barabarani kuondoka.

KUZIMU – shimo la mauti

Kilikuwa chumba kikubwa chenye vijichumba vingi vidogo kwa vikubwa, kwa ujumla kilitisha kwani mafuvu ya vichwa vya binadamu yalipambwa ukutani kama mapambo ya kawaida, taa nyekundu kwa buluu ndizo zilizong’aza eneo hilo la kutisha, kulikuwa na friji kubwa mithiri ya chumba cha kuhifadhia maiti. Sehemu nyingine kulikuwa na stoo iliyohifadhi kila aina ya vikorokoro vya kutisha maalumu kwa ajili ya kutesea, kunyongea, na hata kuulia kabisa.

Chumba hiki kilijengwa chini kabisa ya jumba la kifahari la Mhindi Pancho Panchilio eneo la Kerege njia ya kwenda Bagamoyo, hakuna aiyejua kinachoendelea. Kwa nje lilikuwa ni jumba linalovutia kuliangalia, asilimia kubwa ya wananchi wa eneo hilo hawakuwahi kumjua wala kumwona mmiliki wa kasri hilo, ni watoto tu waliopenda kusemajumba lile ni la wanyonya damu kutokana na mambo kadhaa waliyokuwa wakiyaona, mara watu wameletwa huku nyuso zao zimefungwa vitambaa vyeusi na mambo kadha wa kadha kiasi kwamba ilipelekea watoto wa kitongoji hicho kukaa mbali na jumba hilo.

Lakini tofauti na watu wazima, wao waliwachapa fimbo watoto wao waliokuwa wakisema maneno hayo kutokana na kwamba kutoka ndani ya jumba hilo waliweza kupelekewa maji safi kwa mabomba maalum yaliyounganishwa na pampu kubwa na yenye nguvu, hivyo waliondokana na kero ya maji ya kunywa.

Mwili wa Madam S ulibwagwa chini kama roba la chumvi, haukuwa na uzima wowote.

Kibosho, akaangalia hali ya chumba kizima walichouhifadhi mwili huo, aliporidhika nacho akatikisa kichwa juu chini na kuwageukia watu wake.

“Ulinzi wa nguvu zaidi ya ule wa Ikulu, sawa?” akaagiza.

“Sawa Mkuu!” wakajibu. Akawaacha na kutoka, akaelekea chumba kingine, akakuta vijana wakimsulubu vikali Chiba wa Chiba huku akiwa ananing’inia kwenye minyororo, mwili wote ulitota damu, hakutamanika, hakuangalika. Kibosho alisimama mlangoni.

“Karibu sana kuzimu!” akamwambia Chiba aliyekuwa hawezi hata kuinua uso, “Wewe ndiye kinara wa kuvuruga mitandao ya watu sivyo, sasa utakuwa binadamu wa kwanza kushuhudia kifo chako mwenyewe baada ya kuwaona wenzako wote wako hapa, mbuzi nyie, nani aliwadanganya kuwa mna uwezo wa Kijasusi wa kuitisha Dunia? Sasa leo mtapambana na Shetani nah ii ndiyo himaya yake,” akaongeza kusema kisha akageuka kando akawatazama vijana wake walioonekana wana uchu wa kuua.

“Na Yule bibi, mfungeni kama huyu, lakini msimtese mpaka azinduke kama bado hajafa ili mateso yote ayashuhudie kwa akili na ufahamu wake, nimekuja hapa kwa kazi moja tu,” akamgeukia Chiba “Kuua!” akamaliza na kutoka huku akifuatiwa na vijana watatu wenye misuli ya ajabu. Chiba akiwa katika ile minyororo hakufanya lolote zaidi ya kutulia tu na kusubiri kuona nini kinaendelea.

§§§§§

Kamanda Amata waliitelekeza ile gari eneo la Hoteli ya Sheratoni na kisha wao kutembea kwa miguu mpaka ilipo ofisi ya Madam S. ilikuwa tayari imepita saa tano usiku, walinzi wakawapokea na kuwaruhusu kupita kwani walishazoea kuwa muda wowote watu hao huwa wanaingia ofisini. Moja kwa moja jicho la Kamanda Amata likaenda kwenye maegesho na hakuliona gari la Madam S, wakaingia ofisini na kuketi katika viti vyao kwa

namba zao, kwani katika ofisi hiyo kila moja alikuwa na kiti chake kadiri ya namba zao za kikazi. Ukimya ulichukua nafasi kati yao, hakuna aliyeongea kwa sababu wakiwa hapo ni Madam S huwa anasema alichowaitia.

Kamanda Amata akamgeukia Gina.

“Gina, hili eneo si salama kwa sasa!” akamwambia.

“Yaani mi sina amani na eneo lolote, hata kitanda change nakiogopa, natamani kutoroka,” akajibu.

“Kutoroka! Sio suluhisho,” Kamanda akamwambia huku akinyanyuka na kufungua jokofu lililowekwa vinywaji vya kila aina, akatoa Konyagi ndogo na kuketi kitini, akachanganya na Sprite kisha akanywa taratibu. Gina alionekana kuwa mwenye mawazo mengi sana. Wakiwa katka ukimya huo mara simu ya mezani ikaita kwa fujo. Kila mmoja aliitazama hakuna aliyeipokea, baada ya kukerwa na kelele ya chombo hicho Kamanda Amata akaiinua na kuiweka sikioni bila kuongea.

“Kamanda Amata”, kisha cheko zito na la dharau likafuata, “…leo mtaishi kama digidigi, na nitawafuata popote mlipo mpaka nihakikishe nawamaliza, kwa taarifa yako, kibibi chako ninacho hapa nusu mfu, na wengine wawili, mmoja tayari ni marehemu kama unataka kumwona nenda kwenye vichaka vya Gongo la Mboto njia panda ya kwenda kwenye makaburi ya Wachina… tuachane na hilo, naihitaji hiyo kompyuta usiku huu… nipe kompyuta nikupe marehemu wako ukazike…”

Hasira ya Kamanda Amata ikawaka juu ya huyo asiyemwona,

“…kama unaitaka hii kompyuta njoo uichukue!” akamjibu.

“…Nataka uniletee wewe mwenyewe kwa mkono wako au huyo Malaya wako ambaye pamoja nawe mmeshanipotezea watu wangu watatu, kama hamtaki basi nitaichukua mwenyewe…” ile sauti ikaendelea.

“Acha uoga wewe! Kama unajiamini jitokeze tupambane, atakayeshinda atachukua kompyuta!” Kamanda akaongea kwa jazba, tayari konyagi ilishaanza kufanya kazi ichwani.

Yule mtu wa upande wa pili akacheka sana kisha akaendelea

“…sifanyi hiyo michezo ya kitoto, lakini nakuhakikishia kuwa nitaipata hiyo kompyuta, na nitazichukua roho zenu wote sita kabla ya jua kuchomoza,” akapiga mkwara.

“Na mimi nakuhakikishia kuwa nitakuwa nimekwisha kutoa roho yako na vibaraka wako kabla ya jua kuchomoza, shetani wewe!” alipomaliza kusema hayo, akainuka kitini.

“Unaenda wapi Kamanda?” Gina akauliza.

“Huyu mshenzi keshanitia wazimu, nitahakikisha namjua usiku huu huu na namng’oa koromeo lake, hawezi kufanya dharau na kitengo nyeti kama hiki, huyu hafai kuishi,” Amata aliongea kwa hasira.

Gina naye akasimama wima na lile begi lenye kompyuta mkononi, “Na hii je? Maana inaonekana wana uchu nayo,” akamwambia Amata.

“Tia kwenye sefu salama hapo hata uje na kifaru huwezi kuitoa,” akamweleza.

“Sijui namba za kufungulia,”

“Oh, sorry!” Kamanda akaichukua ile kompyuta na kuingia kwenye kijichumba kidogo kisha akaiweka mahala salama na kutoka na lile begi, akafungua kabati linguine na kutoa kompyuta iliyofanana na ile lakini ilikuwa mbovu siku nyingi, akaipachua hard disk na kulichukua lile ganda tupu akalitia kwenye begi, kisha wakatoka na kuchukua gari mojawapo iliyo kwenye maegesho.

“Gina, upo vizuri? Akili ipo sawa?” Kamanda akamwuliza. Gina hakujibu, alionekana kujawa na hofu kuu, Kamanda akamwangalia na kumwuliza tena.

“Gina, unakumbuka The Art f War?” akamwuliza.

“Hapana Kamanda!” akajibu. Kamanda Amata akatikisa kichwa baada ya jibu hilo.

“Gina wewe ni mwana usalama na haya mambo umejifunza chuoni hutakiwi kusahau mama, sawa?”

“Sawa!”

“Sikiliza Sun Tzu aliandika ‘Jifanye mchovu unapokuwa na nguvu na jifanye una nguvu unapokuwa mchovu’, hata mimi Gina ninaogopa maana simjui adui yangu kasimama wapi, lakini lazima na mimi nimtishe hiyo ndiyo Art Of War,” Kamanda alimtoa hofu Gina.

“Nimekuelewa Kamanda, sasa tunapambana vipi na huyu hayawani?” Gina akauliza. Kamanda akabaki kimya kwa muda, kisha akamgeukia Gina.

“Gina, naomba nisikujibu, na wala usinambie unachofikiria, unajua kwa nini?” akamuuliza.

“Hapana!” akajibu.

“Art of War inasema ‘Ifanye mipango yako iwe siri, isipenyeke kama giza la usiku, na unapojitokeza jitokeze kwa nguvu kama radi’ sio maneno yangu nia Sun Tzu na daima huwa napenda kufuata maneno yake ndiyo maana unaona hapa nilipo,” alipotaka kupachika ufunguo kwenye switchi ya gari Gina akamdaka mkono.

“Kamanda! Hayo uliyosema si ajabu hata adui anayajua,” akafungua mlango na kumvuta Kamanda nje, kisha wakaelekea getini na kutoka nje mpaka barabarani.

“Naona sasa umeanza kujua unalotakiwa kufanya, vizuri sana Gina!” Kamanda akampongeza kisha wakaingia kwenye tax na kutokomea.

Breki ya kwanza ilikuwa mje ya ukumbi wa Jiji mkabala na bandari ya boti za Zanzibar, wakalipa na kisha wakapotelea gizani.

Katika kaunta ya kituo cha Polisi cha Kati, kulikuwa na PC wawili na WP mmoja, Kamanda Amata na Gina walikwea ngazi na kusimama mbele yao. Wale Polisi mara moja walimtambua Gina na kusimama imara kwa kumpa heshima yake ya kijeshi.

“Inspekta Simbeye, ameonakana tena huku?” Gina akauliza.

“Yupo afande, amekuja muda si mrefu,” Yule WP akajibu.

“Naomba tumwone!” Gina akasema hayo huku tayari ameshaanza safari ya kuifuata ofisi hiyo.

Inspekta Simbeye alionekana kuzeeka ghafla kwani mashavu yake yalikuwa yameshuka kiasi kwamba Kamanda Amata alitamani kucheka.

“Shikamoo mzee!” Amata alianza kwa kuamkia kama kawaida akikutana na Inspekta huyo.

“Sina haja ya shikamoo yako, nakupigia simu Amata hupatikani kwa nini?” akauliza kwa hasira.

“Inspekta, kama ulivyowakosa wengine wote na mimi pia usingeshangaa, hata mimi sina mji wa kupokea, hali ni mbaya, nilikutafuta ulikuwa umetoka,” kamanda akajibu.

“Kamanda Amata! Ni nani huyu anayetufanya sisi wapumbavu kiasi hiki, Mheshimiwa Mbunge wa Miroroso ameuawa usiku wa leo, ni masaa mawili tu yalopita,” kabla hajaendelea Kamanda akamkatisha.

“Na hilo hasa ndilo limenileta kwako, nilitaka kujua ni nani aliyeuawa maana nimesikia tua lakini sikujua ni nani aliyeuawa!”

“Ni Mbunge wa Miroroso,” Simbeye akajibu.

“Ok, nimeelewa Inspekta, sasa picha inaanza kujijenga taratibu na itakamilika tu,” Kamanda akajibu.

“Huu umekuwa usiku mbaya sana, siwezi kulala kwa kuwa kifo cha huyu Mbunge kimekuja wakati mambo haya ya vita vya Ufisadi mliyopambana nayo huko Uswizz bado hayajapoa, na huyu Mbunge ndiye alikuwa mstari wa mbele kabisa katika kuyafichua, je huu si mnyororo mmoja?” Inspekta akaonesha wazi hofu yake.

“Nimekupata Inspekta, naomba niondoke kisha tuwasiliane dakika arobaini na tano zijazo,” Kamanda akajibu kisha akaondoka na kufuatiwa na GINA

2

HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI- SAA 6:47 USIKU

KAMANDA Amata akifuatana na Gina waliingia moja kwa moja chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali hiyo, wakamkuta Daktari akiendelea na uchunguzi. Wakiwa wanaongozwa na muuguzi waliingia ndani ya chumba hicho. Walipofika wakaonesha vitambulisho vyao kwa Yule daktari, hivyo hakuwatilia shaka.

“Karibuni sana!” akawakaribisha.

“Asante!” Gina akawa wa kwanza kujibu.

“Sijui niwasaidie nini? Maana nimechoshwa na maswali yenu yanayofanana,” Yule daktari akauliza huku akiwa amesitisha kuendelea kufanya uchunguzi.

“Nataka kujua maraehemu amekufaje?” Kamanda akauliza.

“Amepigwa risasi,” akajibu daktari.

“Ngapi?” Gina akawahi.

“Mbili za kifuani,” akajibu.

Kamanda Amata akasogea jirani na kutazama yale majeraha yalivyojipanga, moyo wake ukapiga chogo chemba, yalikuwa mithiri ya yale ya Frederick Masawe na Petit kule Uswizz, akatazama kwenye paji la uso la marehemu akaona alama ndogo ya risasi nyembamba iliyopenye bila uharibifu.

“Daktari, nah ii je?” akauliza. Yule Daktari akasogea na kwa kutumia kurunzi yake maalumu akagundua tundu hilo, wakamgeuza marehemu na kisogozi wakakuta matone machache ya damu.

“Amepigwa risasi tatu,” Kamanda akaeleza, “Asante Daktari, tulitaka kujua hilo tu,” wakamwacha na kuondoka zao.

“Kamanda hii kazi nyingine sasa,” Gina akamwambia Amata.

“Usijali Gina, hii kazi lazima imalizike usiku huu, kimya kimya mpaka kitaeleweka, leo nataka tufanye kazi hii ngumu mi na wewe tu, jua likichomoza tujue nini tumefanya na dunia ya pili isijue nini kimefanyika, usiogope, Art Of War iliyoandikwa na Sun Tzu inasema ‘Nenda taratibu kama upepo na muwe karibu kama miti. Shambulia kama moto na uwe imara kama Mlima’” Kamanda akamwambia Gina huku wakitoka nje ya chumba hicho.

“Twende nyumbani kwanza tukachukue dhana za kutosha kisha tuingie rasmi kwenye mpambano, tufanye haraka kabla watu wetu hawajapata madhara zaidi, Gina, piga simu Polisi Mabatini waambie kuna mwili wa marehemu kule Gongo la Mboto ili waende kutazama, na kama adui alitegemea kutunasa huko atapambana na vijana wa khaki,” Kamanda alimwambia Gina na mara baada ya Gina kufanya hivyo, wakaingia kwenye Tax.

“Kinondoni makaburini tafadhali!” Kamanda akamwambia dereva tax, kisha wakaondoka eneo hilo. Baada ya kuuacha Mtaa wa Mindu na kuchukua barabara ya Umoja wa Mataifa ndipo kamanda alipogundua kuwa kuna gari ikiwafuata, akamtazama dereva ambaye alionekana hajui chochote, walipopita shule ya Sekondari Tambaza ile gari ikawapita kwa kasi na kuwazuia kwa mbele.

Watu watatu walishuka kwa kasi kwenye ile gari, mikononi wakiwa na Shot Gun, waliishambulia ile tax kwa risasi na kuichakaza vibaya.

Kamanda Amata alimvuta dereva na kumsweka chini, mtawanyiko wa vyoo uliwafanya kushindwa kufanaya lolote, Gina alishuhudia lile begi likinyakuliwa na alipotaka kulitetea alipigwa na kitako cha bunduki akarudi chini, wale jamaa wakaondoka kwa kasi na gari yao wakapotelea katika mitaa ya Upanga.

Kamanda Amata akajinyanyua na kutoka nje, akamtoa Gina kisha Yule dereva ambaye alikuwa katika hali mbaya, hakuguswa na risasi lakini hofu ya milio ya zile mashine ilimfanya kuachia mkojo bila kujijua.

Kamanda Amata akachomoa kadi moja ya kibiashara na kumpatia Yule kijana, “Kesho jioni unitafute!” kisha yeye na Gina wakapotea eneo lile kabla Polisi hawajafika.

Walipokuwa wakikimbia, Gina alikuwa akiishiwa nguvu kila muda ukienda.

“Kamanda, Kamanda! Nakufa!” alilalamika.

“Jikaze Gina!” akamhimiza lakini hali haikuwa nzuri, Gina akaanguka chini. Kamanda akamtazama vizuri akaona mchaniko mkubwa a kichwani na damu zikimvuja eneo moja la mgongo karibu na nyonga, ilikuwa ni risasi iliyompata barabara katika eneo hilo.

“Shiiitttt!”

Akatazama huku na kule, akaona gari ikija kwa mbali, akamweka Gina chini na kuizuia kwa kuingia barabarani, hakuuliza, alimbeba Gina haraka na kumwingiza kwenye gari.

“Nifikishe Mtaa wa Upanga Seaview haraka!” akaamuru.

“Aliyekwambia hii tax ni nani?” Yule deeva akajibu kijeuri huku akizima gari na kuchomoa ufunguo. Kamanda Amata hakuwa na muda wa kupoteza, alfungua mlango akazunguka upande wa dereva, akafyatu lock na kumvuta nje, akamtupia barabarani kisha akakaa kwenye usukani, akachomoa kadi yake ya benki na kuivunja katikati, akaislaidi, katikati yake pakatokea ufunguo mdogo wenye meno mawili akaupachika kwenye swichi ya gari n kuiwasha kisha akaingia barabarani na kumwacha Yule mmiliki wa gari akipiga kelele.

§§§§§

SAA saba na nusu usiku ilimkuta Kamanda Amata katika jumba kubwa lililojengwa kandokando ya bahari ya Hindi huko Upanga, akaegesha gari mahala pake kisha akamtoa Gina ambaye tayari alikuwa amekwishapoteza fahamu.

“Usife Gina, usife tafadhali, subiri kidogo Gina!” kamanda alikuwa akiongea kama aliyechanganyikiwa huku kambeba Gina katika mikono yake akielekea ndani ya jumba hilo.

Dr. Khadrai alikuwa mlangoni akimwangalia kijana huyo ambaye wamekutana mara chache sana katika harakati za maisha yao.

“Karibu Amata, pole sana!” akamkaribisha na kumwongoza moja kwa moja mpaka kwenye chumba maalum ambacho kilishehenu kila aina ya kifaa tiba unachokijua, akamwonesha kitanda pa kumlaza Gina. Dr. Khadrai akamtazama Gina harakaharaka kisha akamtazama kamanda Amata. Akavuta mashine yake kubwa na kuchukua trei iliyojaa vikorokoro kisha akaanza kazi yake ya kitabibu, kwa kumsafisha Gina majeraha na kumtoa risasi iliyokuwa imenasa ndani. Kamanda Amata hakuwa na muda wa kusubiri.

“Daktari, maadam yuko mikononi mwako, naomba niende, kama kuna shida yoyote naomba unitaarifu kwa namba hizi,” akampa namba za Gina, kisha yeye akachukua simu mbili za Gina, akachukua saa na kumwachia simu moja ndogo ambayo si rahisi kwa mtu mwingine kuitumia kwa jinsi ilivyo.

“Amata usiwe na wasiwasi, huyu hajadhurika sana, akiamka tu nitakwambia,” kisha akaendelea na kazi yake.

KEREGE – saa 7:35 usiku.

PANCHO Panchilio alishusha siga alilokuwa amelipachika kinywani mwake na kulibana kwenye kibompoli maalumu cha kuzimia dubwasha hilo. Akainua macho yake na kutega masikio akisikiliza michakacho ya miguu ya mtu aliyekuwa akitembea sebuleni. Kwa jinsi alivyoijenga nyumba yake hiyo, yeye aliweza kumwona kila mtu lakini wale watu hawakuweza kumwona yeye nah ii iliwafanya kusikia sauti daima na kutokuona sura ya bosi wao.

“Karibu sana!” sauti yake ikaijaza sebule yote.

“Mkuu tumefanikiwa kuipata kompyuta uliyotuagiza Mkuu!,” Yule mtu akasema.

“Vizuri sana, sikufanya kosa kabisa kuwachagua ninyi watu makini katka kazi hii, je wale hayawani wawili mmewapata?” akauliza.

“Hapana hatujawapata lakini bila shaka wamefia kwenye gari waliyokuwa wakiitumia kwani tumeishambulia kwa risasi za kutosha,” akajibu, mara hakusikia kitu zaidi ya ukimya uliofuwatiwa na sonyo refu.

“Fanculato!” akatukana, “Kwa nini msihakikishe kama amekufa? Yule bwana ni hatari sana, hakikisheni mnapata habari zake usiku huu, naitaka roho yake kabla hakujapambazuka, potea!” akamukuza.

Pancho Panchilio alikuwa amekodi vikosi viatatu kwa nyakati tofauti na vyote kuvipa kazi moja tu ya kukisambaratisha kikosi cha TSA kuanzia Madam S mpaka wa mwisho. Mipango ya kazi hiyo ilipangwa kitaalamu sana na ilitumia mbinu za hali ya juu, mpaka dakika hiyo alikuwa tayari amefanikisha kwa asilimia sitini ya kile alichokidhamiria, nab ado muda wake bado ulikuwa unaruhusu kumalizia asilimia zilizobaki. Alihakikisha vikosi vyake hivyo havijuani na wala havikutani lakini vyote alikuwa amevipa kazi ileile kwa saa zilezile za kutekeleza lakini muda tofauti wa kufanya kazi.

Hakuona hasara sana kwa kupoteza vijana watatu usiku ule yeye aliishupalia dhamira yake tu ndio maana alikodi watu hao.

Kikosi cha kwanza kiliongozwa na Kibosho, Kanali wa jeshi aliyehasi na kupotea pasikojulikana, sasa alirudi baada ya kuitwa na Mhinidi huyo kwa kufanya kazi kama hizo. Kikosi cha pili kiliongozwa na mtu mmoja hatari kutoka nchi jirani aiyejulikana kama Kaburu na kikosi cha tatu kiliongozwa na mpiganaji aliyebobea kwenye taaluma ya kuua bila kukusidia huyu alikuwa ni mtaalmu wa kucheza na kifo mbele ya binadamu yeyote Yule, ni jambazi la kimataifa kutoka Kigoma, alijulikana kama Naima.

Hawa wote walipewa kazi kwa nyakati tofauti na wenyewe hawakujuana kama wana kazi moja kwa maana kila mtu hiyo ilikuwa ni siri kwake. Walipewa saa kumi na mbili za usiku tu kukamilisha kazi hiyo ngumu. Nao waliwasaka wabaya wao kwa hali na mali kuhakikisha wanamfurahisha bosi wao, malipo waliyopewa ni makubwa na yaliwapa jeuri ya kufanya hivyo.

Usiku huo kwao, ulikuwa usiku wa kazi.

3

KAMANDA Amata alikuwa kachanganyikiwa akili kwa namna moja au nyingine, alikuwa akiona kama ndoto inayotokea mbele yake, hakuamini kama wamewahiwa namna hiyo na kwa kasi ya ajabu, alijiuliza kila wakati ni nani mwenye uwezo wa kuwanasa namna hiyo, hakupata jibu zaidi ya hapo aligundua kuwa kwa vyovyote ni watu hatari wanaojua nini wanafanya na kwa wakati pia alielewa watu hao wamepewa kazi kwa muda maalumu hivyo nay eye kama ilimpasa kuwa saidia wenzake alitakiwa ajipe muda maalum na muda wa kazi yake uwe mdogo kuiko muda wa adui zake pia ucheze ndani ya muda wa adui zake. Alitikisa kichwa kana kwamba kuna mdudu akimtembea kwenye ubongo wake, akaitazama saa yake, saa zinayoyoma kwelikweli.

Ilikuwa inakaribia saa nane usiku alipokuwa akifungua geti la nyumbani kwake, akaingia na kulifunga nyuma yake, kisha akasimama kidogo kuangalia nini kinaendelea huku na kule, kwa macho yake makali aliweza kuona ua moja kubwa likitikisika kidogo, akaelewa wazi kuwa mtikiso huo lazima kuna kitu na si wa upepo kwani hali yah ewe ilikuwa imetulia sana na haikuwa na upepo. Damu ikamtembe haraka mwilini, hakufanya lolote, akauendea mlango wa nyumba kubwa na alipoufikia alikuta karatasi iliyoning’inizwa mlangoni, kisu chembamba chenye makali kuwili kilitumika kuishikia hiyo karatasi pale mlango.

Mwisho wa zama zenu umekwisha, mtaongea na Ngurumo.

Ulikuwa ujumbe uliosomeka katika karatasi hiyo pale juu. Akakikamata kile kisu na kukichomoa kwa nguvu, akakibusu, akaiokota ile karatasi na kuishika mkononi kisha akaingia ndani na kuuacha mlango wa nyumba yake bila kuufunga makusudi tu. Moja kwa moja akakiendea chumba chake na kufungua kabati kubwa lililokuwa mbele yake. Akavuta fulana yake nyeusi kaba shingo ya mikono mirefu akaivaa ikitanguliwa na vesti nyeusi pia. Kizibao cheusi chenye mifuko mingi ya kuwekea zana mbalimbali kikafuata juu yake, na zana zake zikapachikwa, bastola nne zilizosheheni risasi zikakaa mahala pake, visu vidogodogo vikawekwa mahala pake, paketi za risasi zikawekwa mahala pake, Shotgun mbili zikabanwa mahala pake nazo zikiwa zimetimia. Akakusanya vikolokolo vya kutosha kwa pambano hilo ambalo hakujua ni nani haswa anakwenda kupambana naye.

Akiwa kasimama kwenye kioo, anajiweka sawa, akahisi vinyweleo vyake vikisimama, mwili ukamsisimka, akajua kuna jambo, akalisubiri huku akijifanya hajui lolote.

Palepale kwenye kioo alimuona mtu akiingia kwa minyato kumfuata, Kamanda alitamani kucheka kwa sababu hata kama alikuwa akinyata wakati yeye alikuwa akimuona kwenye kioo ni kazi bure. Akamsubiri amkaribie ili ajue nini cha kumfanya. Yule mtu akajiandaa kwa waya aliokuwa kaufunga kutoka mkono hu mpaka ule mwingine.

Anataka kunikaba, Kamanda akawaza. Kisha kwa kasi ya ajabu akageuka na guu lake lenye nguvu likatua kichwani mwa Yule mtu, akajibwaga na kujibamiza kwenye mwamba wa kitanda, yowe la maumivu likamtoka, kabla hajafanya lolote akamnyanyua na kumpa kichapo kikali, alipohakikisha kuwa hali aliyokuwa nayo hawezi fanya lolote akamkalisha chini na kumwegemeza ukutani, akamtikisa na kumtazama usoni.

“Nani bosi wako?” akamwuliza.

“Si-si-simjui!” akajibu kwa tabu.

“Unanileta utani siyo?” akamwuliza kwa ukali.

“Kweli simjui, mi natumwa tu na kulipwa ujira mkubwa wa kunitosha, kwa hali ya nchi yetu nakubali kufanya kazi yoyote kwa malipo yoyote,” akajieleza.

“Nafikiri hunijui sawa sawa sasa utanijua!” Kamanda akamwambia kisha akamkamata korodani zake na kuziminya kwa nguvu.

“Aaaaaiiiiggggghhhh…. Niache, niache nitasema,” akalia kwa uchungu.

“Sema, nani bosi wako, nani aliyekutuma kuja hapa?” kamanda akauliza sasa kwa ukali zaidi.

“Kweli kaka sim-ju-jui…” akajibu huku akijigeuza geuza.

Kabla Kamanda hajauliza linguine, akashuhudia povu jeupe likitoka kinywani mwa Yule mtu.

“Shiiit! Limejiua,” akang’aka kwa sauti, akaanza kumpekua.

Katika moja ya mfuko wa suruali yake akatoa simu ya mkononi, zaidi ya hapo hakuona chochote cha maana. Akaitazama ile simu, akaenda kwenye kitabu cha majina akakuta majina matano tu, la kwanza kabisa likamvutia, lilikuwa limeandikwa kwa jina moja tu ‘Naima’, kisha akaliangalia la pili na la tatu. Akaamua kuanza kampeni na jina hilo la kwanza.

Akaperuzi upande wa ujumbe mfupi, akakutana na ujumbe kutoka kwa Naima uliotumwa ndani ya dakika kumi zilizopita lakini ulionekana kutojibiwa.

‘…Akifika nijulishe nije nimalize kazi…’

ujumbe ulisema hivyo.

Lilifikiri litaniweza, sasa naanza na Naima, kawaza na kuamua kuujibu ule ujumbe.

Kamanda Amata akaujibu ule ujumbe, kisha akaburuza mwili wa Yule mtu na kuubwaga katika mlango wan je kisha yeye akalitoa pikipiki lake na kuliegesha nje kabisa, akisubiri kuona kinachoendelea.

Akiwa nje ya nyumba yake, juu yapikipiki lake kubwa akasubiri kimya nje kabisa ya nyumba yake.

Dakika tano hazikupita, mwanga wa taa za gari ukaonekana ukijitokeza katika kona ya barabara na kuelekea mtaa huo ilipo nyumba ya Kamanda Amata. Ilikuwa Ford Ranger nyeusi, haikuwa na namba za usajili, ikasoge polepole na kuegeshwa karibu kabisa na lango la nyumba hiyo, watu watatu wakashuka, mmoaj kati yao alikuwa mwanamke, alionekana ndiye akiongoza wengine, aliwapanga, mmoja alimwamuru abaki langoni, yeye na mwingine aliyeonekana pande la jitu waliingia ndani.

§§§§§

Naima na lile jitu moja kwa moja waliingia getini na kutembea kwa mainyato huku silaha zikiwa mikononi mwao. Wakiwa wanajigawa kiufundi zaidi kuuelekea mlango, walishangazwa na ukimya uliotawala, lakini hawakujali. Lilikuwa ni lile pande la mtu lililotangulia kuuendea mlango, kabla halijafika likajikwaa kwenye kitu kama gogo.

“Aah!” likajivuta na kujibwaga mbele. Lilipogeuka nyuma likaona mwili wa binadamu, “Shiit! Amemuua,” akasema kwa sauti.

“Nani amemuua?” Naima akauliza, kisha akashusha silaha yake na kusogea pale ulipo ule mwili, akaugeuza, na kuchomoa kijikaratasi kilichopachikwa kinywani mwa marehemu.

…Naanza na wewe…

Naima akageuka huku na kule asione mtu, anaanza na mimi! Hata kama Naima alikuwa ni muuaji mzuri kitaaluma lakini alijikuta akishikwa na ubaridi wa ghafla. Wakaingia ndani wakatafuta huku na kule hawakuona mtu zaidi ya redio kubwa iliyokuwa ikipiga muziki laini wa ‘Killing me softly’ akasonya na kutoka nje. Wakabeba mwili wa mwenzao na kutoka nao. Wakaubwaga katika nyuma ya pikap yao na kufungia. Kisha nao wakaingia garini na kuondoka.

§§§§§§

Kamanda Amata akawasha pikipiki lake, bila kuwasha taa, akaingia barabarani na kuwafuata taratibu, wakaikamata barabara ya Kinondoni na kuvuka daraja la Salenda kisha wakaelekea mjini, moja kwa moja mpaka Mbowe Club, wakaegesha gari na kuteremka kisha wakapotelea ndani.

Kamanda Amata akaingia baada yao na kuhakikisha hawapotezi katika himaya ya macho yake, akaketi katika moja ya viti vya kaunta na kuagiza glass moja ya Whisky akachanganya na sprite baridi kisha akawa anakunywa taratibu.

Wale jamaa wakaketi mahala Fulani wakijadiliana jambo lakini wakionekana kuwa na wasiwasi, kila mara Naima alionekana kuisoma ile karatasi na kuiweka tena mfukoni. Mara lile jitu la miraba mine likanyanyuka na kutoka mahala pale likamwacha Naima na mwingine mmoja. Kamanda Amata alipogeuka hakuliona lile jitu limeingilia kona gani, akili yake ikazunguka mara mbili, akateremka katika kile kiti na kujichanganya katikati ya watu waliokuwa wakiburudika na uziki katika ukumbi huo. Dakika kadhaa baadae akaliona lile jitu pale kaunta likinga’aang’aa macho, likabeba vinywaji na kuelekea kule lilikokaa tangu mwanzo, yote hayo Kamanda Amata alikuwa akiyatazama kutoka katika kundi la watu wale. Alipoona kuwa hakuna aliye na yeye alirudi tena kaunta na kuagiza kinywaji, lakini hakuweza kukimaliza baada ya kumwona Naima akinyanyuka kitini na kuelekea nje, Kamanda Amata naye akatoka na kumfuatilia mwanadada huyo.

Naima alisimama kati ya magari na kuweka simu yake sikioni kisha akaendelea kuongea na aliyekuwa upande wa pili.

Naima akiwa anaendelea kuongea na simu alihisi ubaridi ukimgusa maeneo ya shingoni, akashtuka akataka kugeuka.

“Tulia!” sauti nzito ya Kamanda Amata ikapenya sikioni mwake. Naima akatulia kama alivyoamuriwa, “Nilikwambia nitaanza na wewe, na ndiyo sasa naanza,” akaongeza.

“Weweni nani?” Naima akauliza kwa sauti yake nyororo inayoweza kumnyong’onyesha mwanaume yeyote Yule rijali.

“Mimi ni Yule mnayenitafuta, Kamanda Amata, na nataka unambie watu wangu wako wapi?” Kamanda akaongeza swali kisha akatulia. Naima naye alitulia bila kujibu, akitafakari la kufanya. Baada ya sekunde kadhaa, uamuzi aliofuanya haukuwa mzuri hata kidogo. Aligeuka na pigo kali kwa Kamanda Amata, lakini Kamanda aliliepa kiufundi huku bastola yake ikimtoka mikononi. Naima aliruka sarakasi kwa minajiri ya kuiwahi le bastola lakini kabla hajafika alijikuta akipokea teka la nguvu mbavuni na kutupwa upande wa pili, akajiinua haraka na kusimama wima kumkabili Amata. Amata alijiweka sawa mwili wake na kumwendea kama mbogo, Naima alijiweka sawa na kuvamiana na Amata, kama Kamanda alifikiri mwanamke huyo anapigika kirahisi alikosea, mapigo matatu ya haraka yalimwingia Kamanda akajikuta anapoteza netweki, akajaribu kujitutumua lakini akajikuta amedhibitiwa ka mikono imara ya mwanamama huyo.

Naima alijirusha hewani kama jani la mkorosho na kuachia dabo kiki za maana zilizotua sawia kifuani mwake na kumpeleka chini.

Kisha Naima akatua chini kwa miguu miwilia akimtazama Kamanda Amata akigalagala chini.

“Ha ha ha ha niliambiwa kuwa Amata ni mwanamume wa chuma kaa mbali naye! Chuma kiko wapi hapa? Na sasa nakuua kwa mkono wangu kwani nimeahidiwa pesa nyingi sana kama roho yako nikiipeleka kwa bosi wangu,” Naima aliongea kwa kujiamini huku akiiweka sawa mikono yake tayari kumshushia pigo la mwisho kijana huyo. Alipomjia kumvamia alimshuhudia Kamanda Amata akijirusha kutoka chini kwa mtindo wa ajabu na guu lake la kulia likatua chini ya kidevu cha Naima, akanyanyuliwa na kubwagwa upande wa pili meno kadhaa yakimtoka.

“Mpo chini ya ulinzi!” sauti kali ikasikika upande mwingine. Kamanda alipotupa jicho akaona polisi eneo hilo, akaruka sarakasi na kutua upande wa pili wa gari, akajibana sehemu ambayo kutokana na nguo zake hakuweza kuonekana, akitazama linaloendelea.

Amata alishuhudia wale polisi wawili wakichezea kichapo cha maana kutoka kwa Naima, wakishindwa kujitetea hata kwa ngumi moja kwani kipigo kilikuwa cha sekunde kadhaa lakini kikali.

Huyu mwanamke ni balaa! Akajisemea, upo muda wake nitamtia mkononi tu, akajisemeana kusonya.

KEREGE – saa 8 usiku.

KIKAO cha dharula kiliitishwa ndani ya kasri la Pancho Panchilio, watu watatu walingia ndani ya jumba hilo kupitia milango tofauti kiasi kwamba hata walinzi tu hawakuweza kuwaona wageni hao. Walijikuta ndani wakiwa waneketi katika mtindo wa duara na Yule kinara wao akiwa mbele pa si na kuonekana. Wote waliketi kimya kabisa wakisubiri mkuu wao aongee.

Akajikohoza kidogo kutengeneza koo lake, kisha akafungua kikao hicho kisicho rasmi.

“Wajumbe mtashangaa nimewaita ghafla usiku huu, lakini lengo ni kuwapa taarifa ya kile kinachoendelea mpaka sasa,” Pancho alianza.

“Ndio tunakusikiliza,” mjumbe mmoja akaitikia.

“Vikundi vyetu vimefanya kazi kubwa sana na vimefanikiwa kuwakamata watu watatu, yaani namba moja, namba tatu na namba nne, na hali zao ni kifo muda wowote,” akaendelea.

“Ndiyo hata mimi nilikwishasema kuwa, hawa wakikamatwa ni kuwaua tu na maiti zao tunateketeza kwa moto ili kupoteza ushahidi,” Mjumbe mwingine akaongeza.

“Lakini sasa kuna kikwazo kimoja,” Pancho akatulia hapo.

“Kikwazo gani tena?” akauliza mjumbe.

“Namba moja wao ndiyo anyelete shida na kati ya watu wetu tuliowapa kazi kumbukeni ni vikosi vitatu mashuhuri, watu wane wameshapoteza maisha kwa mkono wake,” akawapa ujumbe uliowashtua kidogo.

“Unasema!” Mjumbe mmoja akaonekana kuanza kuchanganyikiwa.

“Habari ndiyo hiyo! Hivi sasa vijana wapo mtaani wanamsaka mshenzi huyo, mmoja kati ya hao tumemuua yupo katika machaka ya Gongo la Mboto ambako huko pia tumemkosakosa Amata ijapokuwa vijana wetu walilishambulia vikali gari lake lakini alitoweka.”

“Huyo siyo binadamu ni shetani, kwanza mi siku zote sijawahi kumwona japo nimefanya juu chini nimwone japo kwa sekunde moja, namsoma tu vitabuni,” mjumbe ambaye ni mzee kuliko wote aliongeza na wote wakacheka.

“Sasa tunafanyaje?”

“Vikosi vyetu vipo kazini, bado vinasakana na huyo Amata, hwa tulio nao nafikiri ni kuwamaliza kuwaweka hapa ni hatari kwani wakipata nguvu madhara yake ni makubwa,” Pancho akashusha pumzi, “Ila hapa kuna habari njema,” aliposema hayo wote wakakaa sawa.

“Tumeipata kompyuta mama, ile ambayo anatumia boss wao Yule bibi,” akawaambia.

“Eewaaaa hilo nalo neon asee!”

“Sasa ina neno fungushi ndiyo tatizo (password), maana humu ndimo kuna siri zote za hawa jamaa, nilikuwa nawasubiri kwa pamoja tuamue la kufanya,” akaeleza.

“Ni kutumia nguvu tu kupata hiyo password, wenyewe wanaijua, sasa wape kazi vijana watumie nguvu ili kupata hiyo password tujue kilichomo, hawawezi kutupanda kichwani,” Mjumbe mzee akatoa wazo.

§§§§§

Taarifa za kupatikana kwa mwili wa Scoba zilimfikia Kamanda Amata, nguvu zilimwishia kabisa hakuwa hata na la kufanya. Aliitazama saa yake mkononi ilikuwa saa nane na uchafu wake, muda unayoyoma, hakujali aliliwasha pikipiki lake na kuelekea hospitali ya jeshi Ukonga ambako aiambiwa mwili huo umehfadhiwa kwenye chumba maalum.

Hakuamini alipomkuta Scoba kalala kimya huku madaktari wakijaribu kupigania uhai wake wa mwisho. Kamanda Amata alisimama mlangoni na kisha akarudi nje, akajinaamia kwenye ukuta machozi yakimtoka.

Akachomoa mfukoni simu yake na kuiweka sikioni, akamsubiri mtu wa upande wa pili ajibu.

“Ndiyo konokono vipi?” sauti ile ikauliza.

“Konokono anahitaji miguu ya kutembea!” kamanda akaeleza kwa lugha waliyoelewa wenyewe.

“Mwambie aje kuchukua!” akajibiwa na simu ikakatika.

Kamanda Amata akapiga namba nyingine na kuisikiliza.

“Hello!” sauti ikaita.

“TSA namba moja anaongea!” akajibu lile itikio.

“Unasema nani a-a-naonge-a” kigugumizi kilimshika mtu wa upande wa pili.

“TSA namba moja ninaongea, Mkuu naomba tuonane ofisini kwako usiku huu, haraka sana,” Kamanda akatoa amri.

“Kuna nini Namba moja?” akauliza Mkuu wa Usalama wa Taifa Bwana Hosea.

“We naomba tuonane tutajua hapohapo kuna nini…”

“Ok! Copy and paste,” Hosea akajibu huku akikiacha kitanda na kumbusu mkewe Techla aliyekuwa kazama usingizini, kalala fofofo.

USALAMA WA TAIFA – saa 8:40 usiku.

MKUU wa kitengo cha Usalama wa Taifa, Bwana Hosea aliwasili katika jengo hilo na kupokelewa na walinzi, kila mmoja alishangaa kumwona mtu huyo usiku mnene kama huo, kuja kwake halikuwa tatizo, tatizo ni kuja ghafa na bila taarifa. Hakuongea na mtu, alipita moja kwamoja katia sebule kubwa ya kupokelea wageni.

“Mkuu mbona hivyo vipi?” Avanti alimtupia swali walipokutana koridoni.

“Salama tu, upo nani ofisini?” akamuuliza.

“Nipo na Muba,” akajibu.

“Ok, kuna lolote la ajabu mliloliona? Au taarifa mliyoipata?” akamwuliza.

“Ni ajlia iliyotokea Salenda, lakini tumeishaianyia kazi, na mauaji ya Mheshimiwa Mbunge wa Miroroso,” Avant akamweleza.

“Ok, nitawaona baadae kama nitawahitaji,” akamwambia huku akiiendea ofisi yake.

Dakika moja tu baada ya yeye kuingia katika jingo hilo, pikipiki kubwa la Kamanda Amata lilifika getini.

“Jitambulishe!” ilikuwa sauti ya mlinzi.

Kamanda Amata, akataja namba yake ya siri inayomtambulisha kikazi badala ya kitambulisho. Ukimya ukachukua nafasi kisha geti likafunguliwa naye akaingia. Akaegesha pikipiki lake na kuuendea mlango mkubwa, moja kwa moja ofisini kwa Hosea. Akamkuta Mkuu huyo akiwa ametulia kitini na bastola yake kaiweka uchi mezani.

“Karibu Namba moja!” akamkaribisha kwa hofu sana.

“Asante Mkuu! Samahani kwa kukusumbua maana imebidi umwache shemeji,” akamtania.

“Usijali, ndiyo kazi zetu hata yeye anajua, niambie Namba moja, vipi usiku huu, maana hujawahi fika ofini kwangu zaidi ya mwaka mmoja sasa,” akaanza kumhoji.

“Mkuu hali ni mbaya! Ni Kitisho!” kamanda akaanza namna hiyo.

“Unasema?” akauliza.

“Nasema idara ina hali mbaya!” akakazia.

“Kamanda Amata, TSA 1, nini tatizo?” Hosea akauliza.

“Mkuu, Madam S hajulikani alipo, Chiba, Dr. Jasmine wote hawajulikani walipo, Gina yuko mahututi kwa Dr. Khadrai, Scoba naye habari yoyote inaweza kutokea,” Kamanda akaeleza na kuangusha chozi.

“Kamanda Amata…!” Hosea akanyanyuka kitini na kuliendea dirisha kubwa la ofisi yake, alionekana wazi kuchanganyikiwa na taarifa hiyo, akajishika kiuno, akatikisa kichwa, akajipigapiga kichwani mara kadhaa kana kwamba analazimisha kukumbuka kitu, akasonya na kugeuka alipo Kamanda Amata.

“Eti unasemeje? Ina maana wametekwa au wameuawa?” akauliza tena kama hakusikia aliloambiwa.

“Siwezi kujua kama wametekwa au wameuawa! Ila wametoweka, na hapa unaponiona ninatafutwa kwa ubani na uvumba,” Kamanda akaeleza.

Mara hodi katika mlango wa ofisi hiyo ikabishwa.

“Ingia!” Hosea akaitikia, “Vipi, usiku huu sasa!”

“Samahani Mkuu, kuna taarifa hapa ambayo ungeikuta asubuhi lakini maadam upo ni muhimu kuiona tena haraka iwekanavyo,” Mubah akakabidhi karatasi ndogo kwa Hosea kisha yeye akaondoka. Hosea akaitazama kwa makini, akairudiarudia kuisoma kama haielewi.

“Japokuwa si kazi yako lakini tazama hii taarifa,” akampa Kamanda Amata, akaipokea na kuisoma, moyo ukamlipuka, akaanza kuhema kwa nguvu.

…Moja ya gari zenu imepata ajali leo wakato wa mvua kubwa katika daraja la Salenda, ndani ya gari hajapatikana majeruhi wala maiti, tunaomba ushirikiano wenu…

Ilikuwa ni sehemu ya taarifa hiyo, Kamanda Amata akashusha ile karatasi na kuiweka mezani.

“Naomba niwe na haraka!” akamwambia Hosea.

“Bila shaka kamanda!” akamjibu. Amata akachukua simu ya ofisini kwa Hosea na kuzungusha tarakimu kadhaa kisha akaweka sikioni.

Akaongea na mtu aliyemtaka kisha akaishusha simu na kuiweka mahala pake.

“Kamanda, njoo huku!” Hosea akamwambia kisha wakatoka na kuelekea chumba cha mawasiliano.

Wakaingia katika chumba kipana ambacho kilikuwa na kila aina ya mawasiliano ikiwe zile kamera za mabarabarani na sehemu nyeti Dar es salaam.

“Nyie, hii ajali imetokea saa ngapi?” Hosea akauliza.

“Saa moja kama na nusu hivi Mkuu!” Mubah akajibu.

“Sasa, saa moja mpaka sasa nane, na mnajua gari iliyopata ajali ni ya kwetu, eh! Mubah, Avant mlikuwa mnafanya nini humu ndani…?” Hosea aliongea kwa hasira, Mubah na Avant wakabaki kimya huku Mubah akimtazama Avant kwa chini.

“Hebu rudisha nyuma nione hiyo picha kwanza!” Kamanada akaomba. Avant akafanya hivyo na ile picha ikafika mahala pake, Kamanda Amata akashuhudia ile gari ikiacha njia na kupanda tuta la katikati kisha ikajipiga mwambani na kupinduka vibaya kabla ya kutumbukia kwenye mikoko chini ya daraja. Akairudiarudia kama mara tano hivi, kisha akamgeukia Hosea.

“Vipi?”

“Hii ni gari pekee ya Madam S japo siioni vizuri kutokana na mvua lakini bila shaka, tazama hapa, hapa, hii ni BMW umeona ee?” akamwonesha vizuri Hosea.

“Nyie vijana muwe makini nyie! Siku nyingine nitawafaya, sasa unajua kwa kuchelewa kupata hii taarifa meshaliweka pabaya Taifa na ninyi kazi yenu ni kuangalia usalama wa Taifa, nipigieni simu wakati wowote ule nitakuja kazini,” Hosea alilalama.

“Samahani boss, siku niliyopiga simu mkeo Techla alinitukana eti mi ni hawara wako,” Avant alilalamika.

“Avant haya ni mambo ya kazi achana na mke wangu! Sawa?” akafoka na kutoka ofisini. Wakasimama kwenye korido yeye na Kamanda Amata wakijadilia jambo.

“Sasa Mkuu, yaani hapa muda hautoshi, lazima kwanza niione hiyo gari kisha nijue la kufanya, na mimi nahusisha matukio haya na lile la mauaji ya Mbunge,” Kamanda akaeleza.

“Hapo umenichanganya kidogo!” Hosea akamwambia Kamanda.

“Nilikwenda kukagua maiti ya Mheshimiwa, mauaji yake yamefanana kabisa nay a wale waliouawa Uswizz, mlenga shabaha alifanya vile vile, kumbuka huyu Mbunge ni Yule mwenye kelele za kuibua mambo bungeni hasa sakata hili la kutorosha mapesa nje ya nchi,” kamanda akaeleza kwa undani mambo mbalimbai anayoyatilia mashaka.

Hosea, Mkuu wa idara ya Usalama wa Taifa wa nchi akabaki kinywa wazi, akajishika kidevuni hasijue la kufanya.

“Ok Kamanda, sasa ulikuwa unasemaje?” Hosea akarudisha mazungumzo nyuma.

“Mkuu kwanza nilikuwa nakupa hiyo taarifa na unajua taarifa zetu huwa ni salama kwa kuziongea ana kwa ana,” akamweleza.

“Ok Kamanda, sasa ulikuwa unasemaje?” Hosea akarudisha mazungumzo nyuma.

“Mkuu kwanza nilikuwa nakupa hiyo taarifa na unajua taarifa zetu huwa ni salama kwa kuziongea ana kwa ana,” akamweleza.

“Idara, imepata taarifa kama ulivyoileta, sasa wewe endelea na harakati zako, na mi hapa nawaita vijana wangu usiku huu, ili kuanza uchunguzi wa kina nitakutaarifu muda wowote nikipata lolote, nawe unitaarifu muda wowote ukipata lolote, kama kuna mahala utahitaji nguvu nafikiri una kibali cha kuomba jeshi la polisi muda wowote sivyo?” Hosea akunguruma.

“Ndivyo!” Kamanda akajibu.

“All the best!”

KITUO CHA POLISI SALENDA – saa 9:11 usiku

GARI ya Madam S haikutazamika mara mbili, kwa ujumla ukiitazama ni kama imegeuzwa nje ndani; ndani nje, vyoo vyote hakuna, injini iko nje na mengine mengi. Kamanda Amata akaitazama kwa kina, akaikagua hapa na pale kwa utaratibu maalum sio kama ule wa polisi wa haraka haraka, yeye aliangalia kimoja kwa kingine. Akakagua magurudumu na kisha akatulia kimya.

Akiwa katika kuangalia ndani ya gari hiyo ndipo alipoona kitu cha pekee kabisa, heleni, heleni ambayo yeye anaifahamu sana, akaiokota akaitia mfukoni mwake. Kisha akamgeukia polisi aliyekuwa naye mahala hapo.

“Twende eneo la tukio!” akamwamuru.

Yule WP aliyekuwa zamu akajiweka tayari kwa safari fupi ya usiku huo, wakapiga hatu mbili.kamanda akamsimamaisha.

“We WP! Tunakoenda huko unafikiri kupo salama? Hata kama hamruhusiwi kubeba silaha, mimi nakwambia kachukue silaha,” akamwambia kwa ukali.

Dakika mbili baadae Yule WP alikuwa na SMJ iliyoshiba vyema, wote wakakaa juu ya pikipiki kubwa aina ya BMW wakaelekea darajani.

Mikoko mingi ilikuwa imekatika huku na kule, kwa ujumla palisambaratika.

“Mlikuja wangapi?” Kamanda akamwuliza.

“Tulikuja watatu,” Yule WP akajibu.

“Hamkukuta mtu hapa, majeruhi wala maiti?” akauliza.

“Hatukukuta,” akajibu.

“Njoo hapa!” Kamanda akamwita, kisha akamwonesha alama za miburuzo.

“Unaona hii, huyu ni mtu kaburuzwa kutoka hapa ilipoangukia gari mpaka kule juu labda, na hizi ni alama za viatu vya huyo aliyemburuza,” akamweleza. “Tazama hiki kioo cha mbele, hii ni risasi, kioo cha ajali hakiwezi kupasuka namna hii, kwa hiyo ajalia hii kabla haijatokea dereva alipigwa risasi,” akaendelea kumjuza.

Baada ya kuridhika na hapo wakarudi kituoni.

“Wote mlilikuwepo ajalini?” akauliza tena.

“Hapana walikuwapo watatu tu,” akajibiwa.

“Naomba wote waliokuwepo wafike hapa haraka!” akaamuru. Sekunde tu. Askari watatu wakasimama mbele ya Kamanda Amata akiwemo Yule WP.

“Vueni viatu!” akawaamuru. Nao wakavua na kuviweka pembeni.

Akavichukua kimoja kimoja na kuvigeuza chini kuangali soli za viatu hivyo, akawarudishia. Kisha akawashukuru na kuondoka kituoni hapo, alipovuka tu daraja la Salenda, mbele ya ubalozi wa Ufaransa akasimamisha pikipiki lake, akaichukua ile heleni na kuipachua katikati kisha akaipachika sikioni kama earphone.

Kwanza akasikia miruzi mikali, kisha utulivu ukafuata na sauti ya Madam S ikasikika kwa mabli kidogo.

…Nataka wote tukutane ofisini, Shamba, Chiba na mimi tumepata ujumbe wa kitisho, hili sio la kupuuzia, (ukimya ukatawala) nimetoka nyumbani, naelekea shamba, ofisi za Ubalozi, Daraja la Salenda…

Kisha ikasikika sauti ya maumivu, na kelele ya kishindo kikubwa kilichojirudia mara kadhaa.

…Angalieni kwa chini, ndani ya gari, fanyeni haraka. Atakuwa amekufa huyu! Sawa tu, mchukueni hivyo hivyo…

Akasikia sauti ya kitu kama kijiwe kikianguka kisha ukimya ukatawala. Kamanda Amata akashusha pumzi ndefu, akaitoa ile earphone na kuiweka tena kama heleni kisha akaiweka mfukoni, pepo wa hasira akampanda, akapiga kiki moja na pikipiki lile likakubali sheria, akaingiza barabarani na kuchukua barabara ya Kinodoni, kisha akakunja ile ya Kawawa akaambaa nayo mpaka Kigogo akatobolea Tabata akasonga mbele.

GEREZA LA UKONGA- saa 10:01 alfajiri.

MBELE ya Kamanda Amata kulikuwa askari Magereza mmoja aliyekuwa zamu usiku huo, baada ya kuwasiliana na Mkuu wa gereza na kuwasili pale, wote kwa pamoja wakakaa ndani ya chumba kidogo kwa mazungumzo ya kikazi.

“Ndio bwana!” Yule Mkuu wa gereza akaanzisha mazungumzo.

“Asee Mkuu, nahitaji kuona rekodi ya wageni wanaomtembelea Kanayo O. Kanayo na Mahmoud Zebaki, hilo tu!” Kamanda akatoa ombi lake.

Punde si punde ikaletwa rekodi karibu ya mwezi mzima, kila mtu alitembelewa mara nyingi na mkewe isipokuwa tu kwa Mahmoud Zebaki, huyu zaidi ya mkewe alikuwa akitembelewa na mtu mwingine aliyejiandikisha kwa jina la Ravi Kumar, Amata akatikisa kichwa. Akatazama juu huku na kule.

“Mna kamera za usalama hapa gerezani?” akauliza.

“Ndiyo zipo,” Mkuu wa gereza akajibu.

“Naomba nione rekodi yake ya tarehe 21 May mwaka huu,” wakanyanyuka wote na kupita kwenye ujia mrefu mpaka ofisi nyingine ndogo ambako walimkuta kijana mmoja mwenye cheo cha koplo, akafanya hivyo walivyoomba.

Tarehe ile mwezi ule saa ile, akaonekana mtu mwenye asili ya Kihindi akiingia katika chumba cha kuongelea, kisha Mahmoud Zebaki akaja pale wakafanya mazungumzo mafupi kama dakika tano tu. Kamanda Amata alikuwa akiangalia midomo yao na matendo yao, walipokuwa wakiagana. Mahmoud aliiweka mikono yake juu ya mbao iliyokaa kama meza katikati yao ijapokuwa walitenganisha na nondo, na Yule Mhindi akaweka juu

yake na kuiondoa. Kamanda Amata akatazama sana kitu hicho na kukirudisha nyuma mara kadhaa akagundua kuwa kabla ya Ravi kuweka mikono juu ya mikono ya Mahmoud kuna kitu alikuwa akikisoma au kukiangalia kwa makini. Kisha akaondoka na kumwacha Mahmoud akiwa na tabasamu pana.

Walipoangalia tukio la siku nyingine walimuona Ravi akifuatana na mke wa Mahmoud na mazungumzo yao yalikuwa yalionekana wazi hayakuwa ya Kiswahili bali lugha Fulani kama si Kihindi basi ni Kibangla.

“Asante Mkuu!” Kamanda akashukuru.

“Umeridhika? Ni wajibu wetu kulinda Taifa, mimi na wewe,” Yule Mkuu wa gereza akamweleza Kamanda Amata.

“Ni kweli, nikiwa na shida yoyote juu ya haya nitakutaarifu,” akamjibu.

“Bila shaka, muda wowote karibu sana,” wakaagana na Kamanda Amata akaondoka. Kamanda Amata akashika njia na pikipiki lake kuelekea mitaa ya Msasani ambako nyumba ya Mahmoud Zebaki ndiko iliko na familia yake yote iko huko, akiwa njiani akapiga simu kwa kutumia simu ileile ya Gina kwa Inspekta Simbeye, akaomba askari watatu wenye kibali cha upekuzi na gari haraka sana, akapatiwa.

Saa kumi na moja alfajiri alikuwa tayari amewasili Msasani Peninsula na ile gari ilikuwa tayari iko pale.

“Mko kamili?” akawauliza.

“Ndio afande!” wakajibu.

Wakagonga na kuingia ndani ya jumba hilo, walinzi hawakuwa na tatizo baada ya kuona serikali imefika hapo. Wakagonga mlango mkubwa na mfanyakazi wa ndani akatoka.

Walipouliza kuhusu mama mwenye nyumba wakajibiwa hayupo lakini kwa kuwa walikuwa na kibali cha upekuzi na walipita kwa Mjumbe wa shina ambaye alifuatana nao upekuzi ukaanza, nusu saa iliwachukua polisi wale kupekuwa nyumba huku wote waliobaki wakiwa wameanyang’anywa simu zao za mikononi, hakuna kibaya walichokipata isipokuwa kitabu cha kumbukumbu kilichoonesha kuwa Yule mama amekwenda Zanzibar likizo yeye na watoto wake. Ndani ya kijitabu hicho pia baada ya kupekuwa sana wakakuta namba za simu za watu mbalimbali ikiwemo Ravi Kumar, na namba hiyo iliandikwa tarehe 21 May. Kamanda Amata aaliendea likitabu likubwa la TTCL linaloitwa Yellow Page na kutafuta jina hilo mpaka akalipata, na kugundua mtu huyo anakoishi, Mtaa wa India kitalu namba 453RF, wakaagana na Mjumbe wa shina na kuondoka zao mpaka mtaa huo, haikuwa tabu kufika ghorofa ya tatu na kumkuta bwana huyo akiwa hoi kwa usingizi.

“Nyie taka nni kwagu, usiku hii bana!” Ravi alalamika. Kamanda Amata hakuwa na shaka naye kwani picha aliyoiona ni ilele iliyosimama mbele yake.

“Mchukueni huyo, tuondoke naye,” Kamanda akaamuru.

“Jamani mmi nafanya nini nyinyi? Manonea sana raia nyie bana, acheni mimi tawapa pesa jingi sana mfungue maduka!” akalalama.

“Kelele!” Kamanda akamkoromea kisha wakampakia kwenye gari ya polisi mpaka kituo cha kati. Wakamwifadhi chumba maalum.

3

“Ulijiandaa sana kijana!” Amata akamsifia.

“Ndiyo, maana maelekezo mengi tayari nilipewa na Madam S nimwone Yule mzee ndiye akanipa ramani ya mji huu na lile kasri la Pancho,” Chiba akaeleza.

“Amekwisha, Gabacholi yule!” Amata akasema huku akifungua chupa ndogo ya Grants na kuigugumia kinywani.

“Aaaaaaakkhhhh!” akashusha pumzi iliyoashiria ukali wa kinywaji hiko.

- * *

Chiba alizima mlio wa injini ya boti na kuiacha iseleleke taratibu mpaka ilipo karibia umbali kama wa mita mia tano hivi. Wakati huo Amata alikuwa tayari amekwishavaa nguo zake za kupigia mbizi, mitungi yake mgongoni na begi dogo lilisiloingia maji mbele ya tumbo lake.

“Chiba, hapa kazi tu, mi naingia kwa njia ya maji nafikiri ni njia rahisi kama ulivyonambia, na wewe pitia hii hii lakini upande wa pili sote tukaibukie ndani na kutafuta njia ya kumnasa mtu huyo, tukishamtia mkononi kila mtu aangalie ustaarabu wa kuitoka hiyo himaya lakini tukutane Bahrain,” Kamanda Amata alimweleza mkakati mzima Chiba kisha akajitupa majini na kupotelea humo.

Chiba akaendele kupiga kasia kuisogeza ile boti mpaka kwenye mimea ya baharini iliyojazana upande mmoja wa peninsula hiyo. Akaegesha naye akavaa vifaa vyake na kujitupa majini kwa uelekeo mwingine.

- * *

Ndani ya hekalu hilo sherehe za mwanga ‘Diwali’ zilikuwa zikiendelea, watu walikuwa wakiimba na kucheza, kwa ujumla palichangamka. Premji Kanoon au Pancho Panchilio alikuwa ameketi sehemu ya juu kabisa akifuatilia michezo na burudani zote zilizokuwa zikiendelea katika ukumbi huo. Kando yake alikaa na watu wengine kadhaa huku wanawake kama nane hivi warembo wa kuvutia walikuwa wakimpepea, wengine wakileta vinywaji na kadhalika. Nyuma yake alisimama mtu mmoja, mwanaume mwenye tambo kubwa, aliyefuga sharubu zake na kuzichanua huku na kule kama askari wa Kijerumani enzi za mkoloni. Mikono yake aliifungamanisha nyuma. Macho yake yalionekana kutopepeswa upande wowote ule. Na katika kila upande au kona ya jengo lile walionekana vijana waliovalia sare na vitambaa vyao vichwani mwao wakirandaranda huku na kule.

Kamanda Amata aliibuka majini na kujikuta kwenye chumba ambacho ndani yake kuna boti kubwa la kifahari lililoegeshwa.

‘Nimekuja wakati mzuri, ningekuja mchana kusingekuwa na maji hivi,’ akawaza huku akivua ule mtungi na kuuweka kando, akatoa na yale mavazi yake kisha akafungua begi lake na kujipachika kila silaha aliyoihitaji mwilini mwake. Sauti ya viatu vya mtu aliyekuwa akija upande huo vilimfanya atulie tuli huku kisu chake kikiwa ngangari kiganjani.

“Inabidi tuiwashe kwanza ili injini ipate moto. Mkuu anasema hana budi kwenda Punjawar usiku huu,” Sauti ya kwanza iliongea.

“Mbona ghafla hivi wakati sherehe hii yote kaandaa kwa ajili ya watu wake?” Sauti ya pili ikauliza.

“Mi mwenyewe sielewi aisee, ngoja tuwashe kabisa yeye akifika ni kuondoka tu,” ile sauti ya kwanza ikarudia.

‘Nimsubiri kwenye boti?’ Amata akajiuliza moyoni.

‘Uamuzi mbaya utakuwa’ akajijibu mwenyewe na nukta hiyohiyo yule jamaa akaibukia kwenye mlango mmoja wa chumba hicho. Amata akaruka kwa wepesi na kumvamia huku akiwa tayari kamdidimiza kisu moyoni. Akamshusha chini taratibu na kumsukumia kwenye maji. Kisha akatulia kwani bado mwingine alikuwa akija upande huo.

“Kumar! Kumar!” Yule wa pili akaita. Lakini hakukuwa na jibu kutoka kwa swahiba wake, akaendelea kwenda na alipofika kwenye kile chumba hakuamini anachokiona. Mwili wa Kumar ulikuwa ukielea kifudifudi majini. Mshtuko wake ulikuwa zahiri shahiri, akainua redio yake na kuomba msaada.

“Kumar mara cuka hai! Kumar mara cuka hai!” (Kumar amekufa! Kumar amekufa), Amata akajibana kimya nyuma ya pipa kubwa lililojaa vipuli mbalimbali. Dakika hiyohiyo watu kama saba wenye silaha wakaingia katika kile chumba.

‘Nimecheza blanda’ akajiambia, akachomoa bastola yake iliyofungwa kifaa cha kuzuia sauti na kuiweka tayari. Risasi ya kwanza akapiga mtungi wa kuzimia moto na poda iliyokuwa ndani yake ikatoka kwa kasi na kuwachanganya wale jamaa. Kamanda Amata akapita kwa kasi huku watatu waliokuwa mbele yake wakiwa chali kwa risasi kutoka kwenye bastola yake, sekunde mbili tu alikuwa keshafika mlangoni na kuufunga kwa nje akiwaachia kizaazaa. Ujia mrefu ulimkaribisha. Ving’ora vya hatari vikalia kila kona, mvurugano ukaanza kila kona, burudani zikasimama na kelele za vilio nzikaanza huku na kule.

- * *

Chiba aligundua hali ile baada ya kusikia kelele za watu, akapachika head set yake masikioni tayari kwa kazi.

“Amata vaa barakoa yako kazi inaanza,” Chiba akaongea kwenye kile kifaa na kisha akavaa kinyago chake cha kuzuia gesi ya machozi na kinachoweza kumfanya aone gizani bila tabu. Akatazama huku na kule akaona sensor ya moshi ambayo ikipata moshi basi huruhusu maji kumwagika, akatazama huku na kule akaona ua jirani, akavuta karatasi la urembo lilikuwa hapo akawasha moto na kisha akasogeza karibu na ile sensa, nukta hiyohiyo jengo zima likaanza kutiririsha maji, Chiba akaifuata swichi kubwa ya umeme na kuizima kisha akaondoa fyuzi na kuzitupa mbali. Sasa jengo lote lilikuwa giza na jenereta liligoma kuwaka, tayari kijana huyo wa TSA alishapita na kuondoa betri. Yale maji yaliyokuwa yakimwagika nayo yakakatika ghafla.

- * *

UKUMBI wote ulishikwa na kimuhemuhe, Amata alichomoa bastola yake yenye mabomu ya machozi na kutawanya huku na kule. Moshi huo mzito uliwafanya watu kukohoa bila kikomo, wakiishiwa nguvu na wengine kuanguka chini hawajiwezi.

Pancho Panchilio, aliinuliwa pale alipoketi na vijana wake kama saba hivi wakawa wamemzunguka kwa kumlinda wakiwa na silaha zisizojua huruma. Kutokana na gia lile walishindwa kumwona sawasawa Amata hivyo ilikuwa ni rahisi kwake kuwatawanya kwa risasi. Zilipomwishia akaruka sarakasi na kutua karibu kabisa na Pancho Panchilio huku miguu yake ikiwatandika mateke walinzi wawili waliobaki. Pancho alitaka kukimbia kuingia kwenye mlango mmoja lakini hakufanikiwa, ngwala moja maridadi ilimbwaga chini vibaya, wale vijana walipojaribu kunyanyuka, risasi za Chiba ziliwarudisha chini na Amata akapata nafasi ya kuinuka na kukutana uso kwa uso na Pancho.

“Twende nyumbani mwanaharamu wewe!” kamwambia huku akimtandika konde moja kali lililomfanya ayumbe na kupoteza mwelekeo. Konde la pili likamrudisha chini akiwa hoi, pamoja na ule moshi kumlegeza. Amata alijikuta akishikwa na hasira akikumbuka mtu huyo alichowafanyia yeye na wenzake kule Kerege katika mkasa uliopewa jina la Kitisho.

Kabla hajafanya lolote, akajikuta akipigwa na kitu kizito kisogoni, lakini mpigaji hakulenga sawasawa, Amata akageuka na kupeleka mashambulizi makali yaliyolifanya lile jitu lipoteane lenyewe kwa lenyewe. Lilipotulia likajikuta likitandikwa risasi mbili za kifua.

“Hatuna muda wa kupoteza, nasikia ving’ora vya wanoko huko nje,” Chiba alimwambia Amata, na wakati huo huo, Amata akamkamata mkono Pancho na kumkokota kwa nguvu. Mirindimo ya risasi bado ilikuwa ikiendelea, moshi wa machozi ulikuwa umechanganyika na ule wa baruti na kulete harufu ya tatu.

“Ondoka naye Amata, mi nalinda mkia wako,” Chiba alimwambia tena braza ‘ake na Kamanda Amata akatoka na Pancho, alipoona upinzani umekuwa mkali akambeba Pancho na kuruka naye ghorofa ya chini yake wakafika hoi. Amata akawahi kunyayuka na kutumia bastola yake nyingine kupambana na wawili watatu waliokuiwa mahali hapo na kujaribu kumletea zengwe.

Haraka akaiwahi gari iliyokuwa imeegeshwa hapo na kufungua mlango.

‘Asante sana’ akashukuru baada ya kukuta funguo ikining’inia, akafungua buti.

“Ingia!” akamwamuru Pancho huku akiwa amekiinua kile kinyago chake na kukiweka kwa juu, Pancho akapigwa butwaa kumwona kiumbe huyo matata.

“Unashangaa nini? Ingia unanipotezea muda,” kamanda akang’aka lakini Pancho hakutaka kufanya hivyo. Konde moja la tumbo likamfanya Pancho ajiinamie huku amejishika tumbo lake, teke la kusukuma lilipeleka mpaka kwenye buti na Kamanda Amata akamalizia kufunga buti hilo kwa mguu kisha akaingia kwenye usukani, akaiwasha gari hiyo na kutoka kwa kasi huku akigonga geti na kukunja kushoto. Mfukuzano na gari za polisi ulichukua nafasi katika barabara za Bombay. Amata aliwapeleka nje ya mji kwenye barabara ya hatari kabisa, yenye mteremko mkali na wenye kona za ajabu, ambapo wengine waligwaya na waliojaribu walijikuta wakiishia shimoni.

Baada ya kuhakikisha wote kawaacha mbali Amata alichukua uelekeo wa Bahrain house na kuliacha jiji hilo. Saa tisa za usiku akaegesha gari ndani ya jengo hilo kuukuu, akateremka akiwa hafai kwa vumbi lililomkaa mwilini. Akafungua buti na kumtoa Pancho aliyekuwa kajikunyata ndani yake.

“Shuka!” akamwamuru naye akashuka. Akamkokota mpaka ndani ya chumba kimoja kikubwa.

“Pancho Panchilio au Premji Kanoon, karibu katika himaya yangu, mara hii ni zamu yako,” Sauti ya Madam S ikasikisa na taa yenye nuru hafifu ikawaka. Madam S akainuka alipoketi na kumjongelea mtu huyo. Kofi moja kali lilitua shavuni mwa Pancho na kumwacha akitetemeka.

“Ulifikiri utafanikiwa kunikimbia? Twende nyumbani nikakuoneshe kama mimi ni Head of T.S.A,” Madam akaunguruma na kumpa pingu Amata naye akamfunga mikono yake na mnyororo akautia miguuni mwake. Akamkokota mpaka kwenye ile gari waliokuja nayo na Chiba mara ya kwanza.

“Nafasi yako ni kwenye buti tu, akamwingiza na kulifunga kisha akatulia nyuma ya usukani huku kushoto akimwacha Madam S.

“Chiba, Chiba, wapi?” Kamanda akauliza kwenye kile chombo chake.

“Naegesha boti nimefika,” akajibu.

“Weka kiberiti,” akampa agizo. Baada ya sekunde chache Chiba aliungana na wenzake na kuingia siti ya nyuma.

“Mzigo uko wapi?” akauliza Chiba.

“Upo mahala pake,” akajibu huku akiondoka eneo lile na kupita njia za vichochoroni.

“Kilomita ishirini na mbili kijiji cha Malve” Madam S alimwambia Amata na moja kwa moja akaelekea huko nje kabisa ya mji.

Hali ya utulivu ilitawala kijiji kile watu wote walikuwa wamelala ndani ya nyumba zao, ni miti tu iliyokuwa ikitikiswa na upepo wakati Amata akiegesha ile gari katika moja ya kichaka karibu na barabara kubwa inayoelekea baharini, barabara ya vumbi. Dakika mbili tu Scoba akatua na ndege ndogo aina ya Boeing yenye uwezo wa kubeba watu watano lakini yenye nguvu na kasi ya kutosha. Ndege hii ilinunuliwa na serikali ya Tanzania kwa kazi maalumu kama hizi na pia kwa ulinzi wa haraka wa Rais wa nchi inapobidi. Nje ya kumhudumia Rais, ni TSA pekee waliweza kuitumia ndege hii na ni kwa kibali cha Rais tu.

Scoba, akatumia barabara hiyo kutua kwa kutumia mwanga wa tochi alizowasha Madam S akiwa chini kwa ishara aliyompatia. Hakuna kusubiri, walimkokota mtu wao na kumpakia ndegeni, huku kwa mbali wakisikia ving'ora vya polisi vikielekea upande wao.

"Haraka, haraka, haraka," Madam alihimiza na mlango ukafungwa, Scoba moja kwa moja aliiongeza nguvu ile ndege na kuodoka kwa kasi huku akiwaacha wale polisi wakijaribu kufyatua risasi bila mafanikio. Dakika moja ndege ile ikawa angani ikikata bahari na kuelekea katika anga ya kimataifa ambako huna ruhusa kuifanya lolote.

- * *

"Na leo hii utatakiwa kusema siri zote ulizozificha mwanaharamu wewe!" Madam S alimwambia Pancho kwa ukali mara baada ya ndege ile kukaa sawa angani na kila mtu kuweza kufanya shughuli yoyote. Pancho Panchilio alitulia kimya akiangalia kwa jicho la kukata tamaa huku mwili wake ukionekana bado kukosa nguvu kwa kipigo cha rasha rasha alichokipata kutoka kwa Amata.

"Kamanda mwondoe hapa mpeleke kwenye chumba cha mwisho,"

Kamanda Amata akanyanyuka na kumchukua Pancho kwa kuushika ukosi wa shati lake, akamkokota mpaka katika chumba hicho na kumtupia humo. Mlango ukafungwa na ukimya ukatawala.

"Najua hauko peke yako kwenye mtandao huu, Mahmoud na mwenzake tulishawakamata wewe ukatutoroka kijanja. Na wale vibaraka wako wengine kule Kerege tumewakamata na wengine wamekufa wenyewe lakini wewe bado umetukimbia. Hukutukimbia tulikuwa tunaendelea kukuchunguza na sasa arobaini zako zimefika, haya nitajie mmoja baada ya mwingine kabla hatujatua Dar es salaam," Madam S alionekana kuwa na hasira kali juu ya mtu huyo. Pacho alibaki kimya hakuzungumza lolote.

"Jeuri!" Amata akasema, kisha ghafla akapiga teke kwenye korodani lililomfanya Pancho apige kelele za maumivu na kuikusanya mikono yake yenye pingu katika eneo hilo.

"Utasema?" Kamanda akauliza. Lakini Pancho bado alibaki kimya huku akigugumia kwa maumivu makali. Amata akachukua kiberiti cha gesi na kukiwasha kisha moto wake akauweka chini ya kidevu cha Pancho. Maumivu aliyoyapata kwa moto ule uliokuwa ukiichoma ngozi akashindwa uvumilivu.

"Aaaaaaiiigghhh! niache! niache! nasema! nasema!" akapiga kelele.

"Sema, upo na nani kwenye mtandao?" Amata akauliza.

"Kamba Sebule, Kamba Sebule," akataja jina la mtu mkubwa ambaye ni balozi wa nchi wa Tanzania katika nchi fulani.

"Na mna misheni gani hapa?"

"Mapinduzi ase aaaaiyyayayay aaaaiiiggghh! We muuaji wewe," akalia kwa uchungu.

"Mwingine nani?"

"Alibaki huyo huyo, aaaaaaghhh!"

"Hutaki kusema ee? Sasa nakutupa nje kwa huna faida wewe," Kamanda akamwambia Pancho kisha akamtazama Madam S.

"Madam! Jishike vyema namtupa nje huyu mshenzi,"

Akabonyeza kitufe fulani na mlango ukafunguka taratibu, upepo mkali ukaingia ndani na kuleta ufumbufu mkubwa huku ndege ile ikiwa juu futi 40000.

“Utasemaaa au husemiii?” Kamanda aliuliza kwa kelele huku akimtazama Pancho. Akabaki kimya bila jibu. Amata akamsukuma na kumtanguliza kichwa nje, akamsukuma nje. Pancho akatoka mlangoni na kuning’inia vibaya.

“Aaaaaiihhhh, weweeeeeee! Niache nasema kila kituuu, ohhhhh! Nooooo!” Pancho akapiga kelele.

“Sema, mna misheni gani?”

“Mapinduzi, mapinduzi asee,” kutokana na upepo mkali Pancho aliyumba na kujigonga kwenye ubavu wa ndege. Kamanda Amata akatumia nguvu zake zote na kumvuta ndani akambwaga kando huku ule mlango ukijifunga taratibu. Pancho alipoteza fahamu na kutulia kimya.

“Kamba Sebule,” madam S akarudia jina hilo.

“Vipi?” Amata akauliza.

“Inabidi achunguliwe mara kwa mara asije kutupotea kuanzia sasa,” akajibu.

Madam S na Amata wakatoka katika chumba kile na kumwacha Pancho akiwa hajitambui damu ikitiririka usoni huku pingu na mnyororo vikiwa vimemdhibiti.

“Vipi?” Chiba akauliza.

“Poa, yupo huko kapumzika,”

“Yuko down?” (amekufa?)

“Hapana anaelea tu,” (hapana amezimia tu)

“Kinachoendelea?” Chiba akauliza.

“Kamba Sebule, yupo kwenye mtandao,” Amata akajibu huku akiketi sawia kitini. Chiba alibaki kakodoa macho kwa taarifa hiyo, hakutegemea mtu kama Kamba Sebule kuhusika kwenye mtandao wa maovu kama huo.

DAR ES SALAAM – saa 2:30 asubuhi

Saa tano ziliwaweka hewani na asubuhi ya saa mbili na nusu waliwasili uwanja wa ndege wa jeshi, Dar es salaam. Gari jeusi lenye boksi kubwa nyuma lilisogea taratibu mpaka kwenye ile ndege na kusimama jirani kabisa. Pancho Panchilio aliteremshwa na kuingizwa kwenye hiyo gari haraka na kufungiwa humo, askari wawili wenye silaha wakaingia pia sehemu ya nyuma, milango ikafungwa na safari ikaanza.

“Asanteni sana kwa kazi vijana,” Madam S aliwashukuru Amata na Chiba.

“Ndiyo wajibu wetu,” Chiba akaitikia.

“Sasa mpumzike kisha kesho jioni tuonane ili tuweke mambo sawa juu ya mtu huyu,” Madam akamaliza kusema na kuingia garini, Scoba akaondosha gari iliyombeba Madam S. Chiba na Amata waliingia kwenye gari jingine alilokuja nalo Gina wote wakaondoka uwanjani hapo.

Siku hiyohiyo …

BAGAMOYO

VIJANA KAMA SABA hivi walikuwa katika chumba kimoja cha jengo lililochini ya ardhi katika kisiwa kimojawapo kati ya visiwa vinne katika bahari ya Bagamoyo. Vijana hao wote walivalia mavazi meusi na kofia zao zilificha hadi nyuso na kuruhusu macho tu kuonekana. Mikono yao waliifutika kifuani na kufanya wote wawe katika mtindo mmoja wa kupendeza. Kati yao mmoja ndiye alikuwa na mkanda mpana mwekundu katika kiuno chake.

Vijana hawa walikuwa ni jeshi la siri sana la Pancho Panchilio, walikuwa wamefuzu mafunzo Ninjutsu huko Uchina kwa nyakati tafauti. Gabacholi huyu aliwaajiri na kuwaweka katika himaya yake, maalum kwa kazi maalum.

“Komredi ametekwa,” akawaambia wale vijana wengine.

“Usiku wa kuamkia leo pale Bombay, washenzi wamemchukua komredi na mpaka tunavyoongea sasa ameshafikisha hapa nchini,” akaendelea kusema; “hii inaonesha dharau kubwa sana kwetu, kwa kuwa wale jamaa tulifanikiwa kuwateka wote wakatutoka kwa namna ya kibabe sasa naona wametugeukia sisi. Hatuwezi kuwaacha, sasa ni vita na vita hii ninaitangaza sasa. Komredi lazima akombole ndani ya saa sabini na mbili hata kama atakuwa amefichwa Ikulu, ohi?”

“Oha!” wakajibu kwa pamoja kumaanisha kuwa wanajua na wanaelewa kile walichoambiwa, wakaiondoa mikono yao kifuani na kukutanisha viganja kisha wakainama. Baada ya mazungumzo mafupi wakatawanyika na wawili kati yao wakabaki pamoja na Yule aliyevaa vazi lenye mkanda mwekundu wakaketi katika meza hiyo ya duara pamoja wakijadiliana jambo.

“Tutatumia gharama yoyote tumpate,” mmoja wao akasema.

“Hilo ndilo hasa nalitaka tuzungumze, mambo waliyoyafanya Bombay kule si madogo, wamedhalilisha hekalu la Hanuman,” mwingine akadakia.

“Yote tuyaache, mpango wao ukoje mpaka sasa na wapi amehifadhiwa?” Yule wa kwanza akavunja mazungumzo.

“Kutoka chanzo chetu cha habari wanasema jamaa kahifadhiwa Keko, lakini kesho kutwa atafikishwa Kisutu mahakamani,” Yule kiongozi akajibu.

“Baaasi mpaka hapo kazi imekwisha, lazima atekwe ama anavyokwenda au anavyotoka,” mwingine akajibu huku akipiga ngumi mezani.

“Nani wa kulainisha mipango? Si unajua wote wapo lupango,” Kiongozi akauliza.

“Aaaaa Mkuu hilo ni dogo, Kamba Sebule na Maliapopo si wapo? Watafanya kazi,”

“Na hata hizi habari ni Maliapopo aliyenipatia na yuko sambamba na kila linaloendelea atatujulisha,” akamaliza na kuwaomba vijana wakae tayari kwa lolote watakaloambiwa.

GEREZA LA KEKO

PANCHO PANCHILIO aliketi sehemu ya peke yake, mikono yake ikiwa na pingu kama alivyoletwa siku iliyotangulia. Chumba chenye mtindo wa duara kilichojengwa kwa vyuma imara pande zote, ndimo alimohifadhiwa mtu huyo. Taa yenye mwanga mkali wa watts 750 ikawashwa na kummulika mtu huyo muda wote, joto kali likamtesa, mwili ukatota kama aliyemwagiwa maji.

“Aaaaaigh Shit!” aling’aka baada ya taa ile kummulika usoni moja kwa moja kila ajigeuzapo.

“Acha kupiga makelele ya kitoto bwege we!” Madam S alimwambia huku akisogea taratibu na vijana wake Chiba na Amata wakiwa nyuma yake.

“Kesho mahakamani,” akamwambia.

“Afadhali haki ikatendeke maana hapa mnanionea tu,” Pancho akajibu.

“Haki? Unaijua haki wewe? Ungeijua haki ungefanya yote uliyoyafanya? Pancho au nikuite Premji Kanoon, nchi iliyokulea unaweza kuifanyia haya? Kudhulumu haki, haki ya mwananchi mdogo anayevuja jasho la chumvi na kulilamba kwa kukosa maji safi ya kunywa lakini wewe na mabwanyenye wenzio wenye matumbo makubwa yasiyo na shukrani mnahamisha fedha na kuzificha ughaibuni,” akameza mate, na kuendelea, “Pancho! Kweli kabisa unadiriki kukifutilia mbali kikosi hiki unachokiona ili tu uendeleze biashara yako haramu, unaniteka mimi wewe, unateka vijana hawa uwaue halafu ufanye nini kwenye nchi hii? Kila anayekaribia kung’amua madhambi yako unataka ummalize. Siku yako imefika, nimekufuata India kwa gharama ili nikuoneshe kama mimi ndiye Madam Selina, mwanamke wa chuma tena chuma cha pua, kama kukuua ningeshakuua long time ila nilitaka kwanza nikuoneshe jeuri yangu kisha nikusweke jela maisha yako yote …”

“Kamwe, Pancho Panchilio hawezi kuingia jela, ha! Ha! Ha! hiyo sahau we mwanamke, utaiona miujiza yangu kabla ya kufika jela au hata mahakamani, mtatafutana ninyi nakwambia na hapo ndipo mtashuhudia mmoja mmoja wenu akianguka na kufa wakati mi narudi kuishi maisha yangu ya anasa. Ikitokea wewe ukabaki hai basi nitakualika kwenye tafrija kubwa pale Kilimanjaro Hoteli kisha utaona nani na nani wamealikwa, ndipo utakapojiona upumbavu wako we mwanamke ni mwanamke tu…”

Madam S alijikuta akishikwa na hasira akachomoa bastola yake.

“Rudia maneno yako nikupasue fuvu hilo,” aliongea kwa hasira.

“Ha! ha! ha! ha! Muoneni bibi yenu huyu, hana akili kabisa,” aliwaambia kina Chiba na Amata. Kama alifikiri anamuuzi mwanamama huyo pekee, basi alikosea sana, kitendo cha ghafla, Pancho alijikuta akipoke teke moja la kilo nyingi usoni, akajipiga kisogo ukutani kisha akaanguka sakafuni, kimya!

“Funga domo lako! Punguani wewe,” Amata akaunguruma. Sekunde chache Gabacholi huyo akajiweka sawa tena mara hii sura yote ilikuwa nyekundu.

“Tena wewe! Wewe! Wewe! Ipo siku yako. Nitakutoa huo utumbo niuanikie nguo,” Pancho alimwambia Amata.

“Utafanya hayo kabla bastola yangu haijafumua ubongo wako,” Amata akamaliza na kumtazama Madam S aliyekuwa amekunja sura kwa uchungu.

“Kesho Mahakamani,” Madam akamwambia Pacho na kugeuka kuanza kutoka ndani ya chumba kile maalum.

- * *

SIKU ILIYOFUATA

Asubuhi ya siku iliyofuata, Pancho Panchilio aliandaliwa tayari na kupelekwa mahakamni ili kusikiliza shitaka lake. Magari ya magereza na lile la FFU yalikuwa tayari mbele ya gereza hilo la Keko. Ulinzi mkali uliimarishwa kuzunguka ngome hiyo kwani taarifa kwa vyombo vya usalama ilikwishatolewa kuwa mtuhumiwa huyo ni mtu hatari sana. Vijana wa kazi walikuwa tayari kwa lolote.

Akiwa chini ya ulinzi mkali, Mhindi jeuri huyo alitembezwa taratibu huku miguu yake ikiwa imefungwa kwa minyororo na kisha mnyororo huo huo kuunganishwa na kuishika pingu iliyoifunga mikono yake. Msafari ulianzia Keko kuelekea Kisutu ambako shauri lake lilitakiwa kusikilizwa. Kwa kuwa barabara zote yaani ya Chang'ombe, Nyerere, Bibi Titi zilizuiwa magari kupita kwa dakika kadhaa, iliwachukua dakika kama kumi na tano tu kuwasili katika mahakama hiyo huku Pancho akiwa ndani ya gari maalumu iliyozibwa pande zote.

Mahakama ilifurika watu, kama kawaida, waandishi wa magazeti na wale wa televisheni walikuwa bize kutafuta habari lakini zaidi kuipata picha ya mtu huyo. Baada ya yote kukamilika na shauri hilo kuahirishwa, Pancho alitakiwa kurudishwa rumande mpaka baada ya mwezi mmoja ambapo ushahidi utakuwa umekamilika. Gari lile lililomchukua kutoka Gereza la Keko, ndiyo iliyokuja gerezani hapo kumbeba kwa mara nyingine na sasa ilikuwa na kazi ya kumrudisha mahabusu. Alitolewa akiwa chini ya ulinzi mkali mnyororo wake miguuni na pingu mkononi, moja kwa moja akaingizwa ndani ya gari hiyo isiyo na dirisha hata moja katika eneo la kuifadhi wahalifu. Baada ya kufungwa mlango wake askari wawili wenye silaha walikaa katika kijichumba kidogo wakiwa na bunduki zilizoshiba vyema.

Msafara ukaanza kutoka katika gereza hilo, gari la polisi likatangulia mbele likipiga ving'ora vya kuomba njia, kisha likafuatia hilo lililombeba mhalifu na mwisho kulikuwa na gari jingine la askari magereza wenye silaha, safari kuelekea Gereza la Ukonga na sio Keko tena ikaanza kwa kasi huku gari nyingine zikiacha njia na kuupisha ule msafara uende. Kasi iliyokuwa kwa gari zile haikuwa ya kawaida, kila mtu alishangaa na kujiuliza 'kuna nini?'

Wakati huohuo…

Barabara ya Shaurimoyo na Nyerere

Ndani ya gari moja lililoegeshwa muda mrefu katika Barabara ya Shaurimoyo, watu sita walikuwa kimya kwa muda mrefu, na mara ukimya ule ukakatishwa kwa biip moja ya simu ya kiongozi wao. Kutoka kiti cha mbele alichoketi akageuka nyuma na kuwatazama viajan wake.

"Mko tayari? Tunafanya kazi sasa, dakika tatu kila kitu kiwe kimekamilika, kwa kuwa wao hawajajiandaa kwa hilo basi itakuwa ushindi ni upande wetu, ohi?"

"Oha!" wakaitikia vijana wa kazi waliovalia nguo za khaki, na bunduki zenye risasi tele migongoni mwao, nyuso zao zilikuwa tayari kufunikwa na barakoa za kukinga gesi ya machozi, walikamilika.

Kiongozi wa operesheni hiyo aliinua redio yake ya upepo na kuiweka karibu na kinywa chake.

"Namba one, namba one, stand by!" akaongea.

"Umesomeka, namba one stand by," akajibiwa.

"Namba one on your marks… Get set… go!" Yule kiongozi alitumia mtindo unaotumika na wanariaadha kutimua mbio.

Kutoka upande wa Keko, karibu kabisa na eneo la daraja la leri pembezoni mwa Kiwanda cha Uchapaji cha Taifa, liliwashwa tingatinga na kuchomoka kwa kasi kuelekea barabara ya Nyerere. Hamad! Wakati ule msafara unafika na lile tingatinga linafika, ajali mbaya isiyosemeka ikatokea. Lile tingatinga likaigonga gari ya mbele ya polisi na kuharibu vibaya, haikuishia hapo, iliigonga ile gari ya kubeba mhalifu na kuikunga njia, ikaibana karibu na gema la daraja. Mtafutano wa watu ukaanza asubuhi hiyo katika eneo lile.

Kutoka kwenye lile gari la askari maalum wa magereza, waliruka na kutua nje kila mmoja akachukua sehemu yake kwa kuangalia nini kinatokea. Kabla hawajakaa sawa, gari aina ya Range Rover ikaingia kwa kasi na vijana kama sita hivi wakateremka haraka na kulizunguka eneo lile, mabomu saba ya machozi yakatua ardhini na wao wakavaa barakoa zao tayari kuzuia adha ya gesi ile ya machozi. Wawili kati yao haraka wakaenda kuufungua ule mlango wa lile gari, risasi zikaanza kulindima kutoka kwa wale vijana wa magereza na polisi, wakashambuliana na wale majambazi. Jambazi mmoja akapigwa risasi na kudondoka lakini hakufa bali alijeruhiwa vibaya.

Mlango ukafunguka, mmoja wa askari bado alikuwa ana nguvu zake, alimpiga yule jambazi kwa kitako cha SMG kichwani, akapepesuka na kushindwa kustahimili akaaguka chini, Yule mwenzake akatumia risasi ya moto na kupiga askari wote wa ndani kisha akaingia na kumfungua bosi wake. Mabomu ya machozi yaliongezwa na mosi ukatapakaa eneo lote.

Yule jambazi aliyetoka na Pancho akapiga aina Fulani ya mluzi na wale wenzake wote wakakimbili garini, lakini jambazi mmoja aliyekuwa mwisho ambaye kiutaratibu lazima apande mwisho, akamchapa risasi yule jambazi mwenzake aliyekuwa na hali mbaya pale chini ili kuzuia asije ongea lolote, nukta hiyo hiyo ukasikika mlio wa helkopta eneo lile, nalo likazidisha vumbi, wale majambazi na mtu wao wakajitupa ndani yake na lile dege likapotelea angani.

“Upo Salama Mkuu,” Kiongozi akamwambia Pancho.

“Yeah, hongereni kwa kazi,” akawapongeza wakati huo wakimwondoa ile minyororo na pingu mikononi mwake.

“Ha! Ha! Ha! Ha! mmewapiga chenga ya mwili,” Pancho aliwasifu vijana wake kwa lugha ambayo Yule dereva hakuielewa.

“Ijapokuwa tunasikitika tumepoteza wawili,”

“Usijali, hiyo ni najali kazini,”

“Sawa Boss”.

Ilikuwa kama filamu hivi, kwa ughafla wa tukio lile ambalo halikuchukua hata dakika tatu, askari waliokuwa wakisindikiza mhalifu huyo walijikuta hoi. Wamezidiwa ujanja, ijapokuwa waliwapiga risasi wawili lakini wao walipoteza wawili pia. Utulivu ukarudi, kilichobaki kilikuwa na mtapakao wa moshi na harufu ya baruti inayoishia kwa upepo. Watu walikuwa wakisogea taratibu kuona kulikoni. Polisi nao walifika na kuweka ulinzi eneo hilo ikiwa pamoja na kufunga barabara.

Mkuu wa polisi mkoa wa Dar es salaam alikuwa hapo akiangalia hali halisi, sura yake ikikunja ndita sehemu ya juu ya macho yake, hasira isiyojificha ilionekana wazi wazi.

“Washenzi hawa,” akang’aka kwa hasira.

Wakati polisi wengine wakiendelea kupima hapa na pale yeye bado alikuwa akiendelea kuwasiliana kwa redio yake.

“Nipo eneo la tukio, mmeona helkopta yoyote ikipita maeneo hayo?” akawauliza polisi wa anga ambao daima kazi yao ni kuvichungulia vya juu.

“Vipi Mkuu?” sauti ya Inspekta Simbeye ilimfanya yule RPC kushtuka na kumwangali mtu huyo. Wakapigiana saluti za kijeshi kisha mazungumzo yakaendelea.

“Kwa hiyo wamekuja na helkopta mpaka hapa na kumchukua mtu wao?”

“Ndiyo, lilikuwa ni shambulizi la ghafla na la ufundi wa hali ya juu ijapokuwa hata vijana wetu wamefanya kazi kubwa mpaka kuwalaza hawa wawili, sema tu ndiyo hivi wameshakufa, laiti wangekuwa hai pangechimbika,” akamaliza kusema RPC na kumwacha Simbeye akikagua hapa na pale kuona kama kuna lolote la ajabu katika ajali hiyo, alitazama hiki akagusa kile, alipindua hiki na kusimamisha kile kule arimuradi tu afanye kitu.

Mchana huohuo

Simu ya mkononi ya Madam S iliita kwa fujo, alipotupa jicho mezani akaona simu inayowakawaka ni ile ya taarifa nyeti.

“Shiit, nini tena?” akaongea kwa sauti ya kuonesha kuwa hajafurahia simu hiyo, akainyakuwa na kuitega sikioni kwanza.

“Hello Sellina!” mara moja akaitambua sauti hiyo.

“Ndiyo Simbeye vipi (…) what! Unasema, (…) acha masihara katika kazi asee,”

“…Madam habari ndiyo hiyo, Pancho Panchilio kaokolewa na jamaa zake kwa njia za kikomandoo”.

Madam S akakata simu na kuitupia mezani kisha yeye mwenye akajitupa kitini na kushusha pumzi ndefu. Akawaita vijana wake wote na kuwapa taarifa hiyo ambayo iliwachanganya mpaka wakachanganyikiwa. Lakini la kutokea tayari lilikuwa limetokea.

04

KIJIJI CHA MINDE – BAGAMOYO

“Babu! Babu!” kijana wa makamo alimwita babu yake huku akiwa anahema kama aliyefukuzwa na mbwa.

“We, nini?” babu yake aliyekuwa ameketi chini na wavuvi wenzake wakiwa wanasuka nyavu zao alimjibu kwa kumwuliza.

“Ame- ameam- amemka, yule mtu ameamka…”

Yule mzee akawatazama wale wavuvi wenzake na wote wakakurupuka na kukimbimbilia kwenye ile nyumba walimomlaza huyo mtu. Walipofika waliingia taratibu bila kufanya kelele na kumtazama.

“Oooh! Ameamka, asante binti kwa dawa ulizompatia,” yule babu alimshukuru binti aliyekuwa kando na chungu chake kikubwa kilichojaa maji ya kijani.

“Bila asante, ni wajibu wangu kumsaidia,” akajibu.

Wale wazee wakasogelea kitanda na kumzunguka wakimtazama, naye pia alizidi kuwatazama kwa kuwashangaa.

“Niko wapi? Niko wapi hapa?” akauliza kwa ukali na kumkunja kanzu mzee mmoja aliyekuwa jirani na yeye.

“Aaah a a a! kijana tulia kwanza, hapa upo mahali salama kabisa,” mzee mwingine alimsihi mtu huyo kwa lugha ya pwani.

“Wewe ni nani kijana?” Yule mzee akauliza.

Yule mtu akawashangaa tena, akawatazama na kuwakazia macho, kisha akajitahidi kukaa na kuegemea ukutani.

“Naitwa Amata,” akajibu kwa kifupi.

“Amata! Pole sana Amata, tumekuokota baharini ukisukwasukwa na mawimbi makali. Mungu mkubwa kwani yalikupeleka mpaka kwenye mikoko nasi tumekuona huko, nini kilikupata kijana,”

Amata akanyamaza kimya akifikiria jambo, akijaribu kuvuta kumbukumbu kwa lile lililotokea.

Saa 20 Zilizopita…

Ajali ya ndege.

Mara tu baada ya kiti cha Amata kufyatuka na kutoka nje wakiwa angani, parachute alilokuwa akitumia Amata likagoma kufyatuka, akahangaika nalo huku msukosuko ukiendelea. Kutoka kwenye ile ndege akaanza kuanguka kwa kasi huku akielekea baharini.

“Scobaaaaaa!!!!” aliita kwa nguvu lakini mwito wake haukuwa na nguvu kwani Scoba naye alikumbwa na maswahiba yake. Kutokana na lile parachute kushindwa kufunguka, Amata alitua baharini kwa kishindo na kuzama kwa sekunde kadhaa kabla ya kuibuka juu. Kwa mbali aliiona kitu kama boti ikija kwa kasi na kupunga mikono kuomba msaada lakini badala ya msaada wale jamaa wakafyatua risasi kumshambulia, Amata akapiga mbizi na risasi mbili zikampata eneo la mbavu. Maumivu yake yalimweka kwenye hali mbaya kiasi kwamba alijikuta akipoteza nguvu. Jua lilififia machoni pake, kiza kikayafumba macho, akajikuta anapoteza nguvu na ukimya mkuu ukamchukua.

“Nimekwisha!” akajitahidi kutamka kwa taabu.

“Ma-da-m S” akajitahidi kuita kwa nguvu lakini bado aliona giza likimzidi nguvu.

- * *

“Shabash, nimempata kwisha habari yake,” kijana mmoja alikuwa akishangilia kwenye ile boti. Huku akipiga risasi nyingine hewani.

“Una uhakika?” Mwenzake akauliza.

“We sogeza mashine pale uone, maiti tu ile,”

Ile boti ikasogea mpaka pale na kuukuta mwili wa Amata ukiwa kifudifudi juu ya maji baada ya kuibuka. Wakautazama na kuondoka zao.

“Buriani, hatuna historia ya kubeba maiti,” yule nahodha wa chombo akageuza na kuondoka zao mpaka katika kambi yao iliyojengwa katika moja ya visiwa vilivyozunguka eneo hilo huku bado wakipiga risasi hewani kuoneshya.

- * *

Mawimbi ya bahari yakausukasuka mwili wa Amata na kuutupia kwenye mikoko iliyofungana katika pwani ya eneo hilo, na kunasa huko. Jioni ya saa kumi na mbili hivi wavuvi kutoka kijiji cha Minde walikuwa wakipita kuelekea katika shughuli zao huko katikati ya bahari, wakiwa na karabai zao wakipita pembezoni kabisa karibu na ile mimea ndipo walipouaona mwili huo.

“We hebu mulika pale,” mzee mmoja akamwambia nahodha wa chombo hicho.

“Nini?”

“Yule siyo mtu Yule?” wakatazama kwa makini na kugundua ni mwili wa binadamu, wakashuka na kutumbukia majini mpaka eneo lile.

“Oh Shit, si ajabu akawa hai huyu, mtazame!” wakamgeuza geuza na kuamua kumbeba. Safari ya kwenda uvuvini ikaghairishwa na wazee wale wakaamua kurudi kijijini. Walifika na kumshusha Amata kisha wakamlaza chini mkekani huku wakisogeza moto jirani ili kumpa joto. Mzee mmoja alikwenda kumwita binti anayesifika kujua dawa za asili, akaja na kuanza kumfukizia Amata moshi wa mchanganyiko wa majani na magome makavu ya miti.

“Hajafa bado huyu?” mzee mmoja akauliza.

“Hapana hajafa huyu, ila amezimia na yuko mbali sana katika mzimio wake, ninamwita polepole ataamka tu,” yule binti akajibu.

Matibabu hayo ya kienyeji yaliendelea mpaka asubuhi yake na mchana wa siku hiyo Amata alirudiwa na fahamu

Siku ilofuata

Amata alitoka nje ya nyumba hiyo majira ya saa nne asubuhi, akasimama nje na kuangalia upande wa baharini, akiwa hajui ni wapi alipo mpaka dakika hiyo. Akiwa bado hajisikii vyema sana hasa sehemu fulani za mwili wake ambako kulikuwa na kitu kama jeraha aliendelea kutembea hapa na pale pale kijijini akiangalia hiki na kile. Kila hatua chache alisimama kutokana na maumivu aliyokuwa akiyasikia katika maeneo ya mbavu. Kila alkisjidhika aligundua kuwa kulikuwa na majeraha. Nyuma yake akahisi mchakacho wa nyayo za binadamu, akasimama na kusubiri.

“Naona una nguvu sasa,” sauti nyororo ya kike ikasikika nyuma yake, akageuka na kugongana macho na mwanadada mrembo aliyekuwa ndani ya mavazi ya kawaida kabisa ya kijijini.

“Ndiyo, sasa najisikia nafuu zaidi, ila maumivu tu eneo hili,” akamjibu na kumwonesha eneo lenye maumivu.

“Pole, unywe ile dawa niliyokupa, ndani ya saa sita mpaka kumi zijazo utajisikia sawa kabisa, ni dawa nzuri kwa majeraha kama hayo,” Yule mwanadada akamweleza.

“Unaitwa nani?” Amata akauliza.

“Minde!” akajibu huku wakiwa wanatazamana na Amata.

“Asante Minde, umeokoa maisha yangu, unastahili zawadi, zawadi kubwa kabisa. Niambie hapa ni wapi?”

“Hapa ni Minde,”

“Minde tena?” Amata akauliza kwa kupata uhakika.

“Ndiyo, usishangae, kijiji hiki kinaitwa Minde na mimi naitwa Minde,” yule mwanadada akamweleza Amata kisha akauchomoa mfuko wa plastiki ndani ya kanga yake kuukuu na kumpa Amata. Alipoupokea alihisi wazi uzito wa kiasi wa mfuko huo, akaufungua ndani na kuangalia, akatabasamu kisha akamwangalia binti yule kwa kumkazia macho.

“Minde!” akaita kwa sauti tulivu.

“Umevipata wapi hivi?” akauliza.

“Nimevitoa kwenye nguo zako ulizovaa,” akajibiwa. Kamanda Amata akavimwaga juu ya jiwe lililokuwa jirani. Kwanza akachukua bastola iliyokuwa hapo, akaivuta slider yake na kuirudisha, akaifyatua kitako na kuchomoa magazine iliyojaa risasi, akazipachua moja moja na baadae akazirudishia tena. Akamtazama Minde akamwona jinsi alivyojawa na woga.

“Mbona unaogopa?” akamwuliza.

“Mmm umejuaje kama naogopa?”

“Nikimwangalia mtu usoni huwa najua kila kinachofanyika ndani ya ubongo wake,” wote wakacheka.

“Basi we unafaa kuwa mtabiri!”

Amata akachukua waleti iliyokuwa pamoja na hivyo, akaifungua na kukuta kila kitu chake kipo salama, ndani yake licha ya vitambulisho kulikuwa na fuba la pesa za kitanzania kama shilingi laki tatu hivi, akachomoa noti kadhaa zilizofungwa vyema. Akazihesabu harakaharaka zilikuwa shilingi laki moja.

“Hii zawadi yako Minde,” akamkabidhi, binti yule akamtazama Amata kwa jicho la uchu na kumshukuru kwa kibantu. Amata alimkumbatia Minde mikononi mwake huku akimwangalia usoni na kuyaona macho yanayojaa machozi.

4

“Minde, nahitaji kuondoka sasa, nitakuja kukusalimia tena,” akamuaga lakini ilikuwa ngumu kwa Minde kumruhusu Amata kutoka pale, alimbembeleza akae japo siku moja zaidi lakini Amata alijua wazi kuwa kwa vyovyote wenzake watakuwa wakimtafuta. Akaichukua saa yake sasa hii ilikuwa ya mwisho kuitoa katika ule mfuko, akaizungusha mahala fulani na kutazama kwenye kioo, kisha akamtazama Minde.

“Hapa ni Bagamoyo?”

“Ndiyo”

Baada ya kama saa tatu hivi, Minde alimruhusu Amata kuondoka kwa minajiri ya kuonana tena, Amata akaagana na wale wazee na kuanza kufuata barabara taratibu kuelekea barabara kubwa ambapo angepata usafiri wowote.

MASAKI – saa 1:30 usiku

MADAM S alisimamisha gari ndani ya uwa wa nyumba yake na kuruhusu lile lango lijifunge lenyewe nyuma yake. Aliposhuka garini akavuta hatua kuelekea mlango mkubwa wa kuingilia ndani huku akitumia simu yake ya mkononi kuzima kengele za hatari ambazo huziacha zikifanya kazi kama yeye hayupo. Akaufungua mlango na kuingia ndani alipouelekeza mkono wake kuwasha taa, taa zikawaka zenyewe na sebule yote ikang’azwa na mwanga wa kupendeza.

Madam S alipigwa na mshangao, akabaki akikodoa macho huku mkono wa kuume ukiwa tayari na bastola kiganjani.

“Amani iwe nawe!” sauti ya Amata ikasikika.

“Uhhhhh! Siku nyingine utakuja kufa wewe, kwanza ulikuwa wapi?” Madam S akaanza kufoka huku akishusha pumzi ndefu.

“Nilikuwa kuzimu, na sasa nimefufuka katika wafu,” Amata akajibu.

“Shiiiit! Mzima wewe? Au mzuka!”

“Njoo unipapase maana mzuka hauna mifupa wala nyama,” Amata akajibu.

“Oh! No, hebu ujinga wako…”

Madam S akainua simu yake na kubofya tarakimu fulani fulani kisha akaweka sikioni na kusungumza na mtu wa upande wa pili.

“Hello (…) sawa, njoo haraka nyumbani kwangu,” alipomaliza hayo akakata simu.

Moja kwa moja akakiendea kiti kilicho mbele kinachotazamana na mgeni wake huyo huku bado bastola yake ikiwa mkononi.

“Ina maana bado hujaamini kama ni mimi?” Amata akauliza kwa mashaka.

“Watu ni wataalam huweza kujigeuza vyovyote watakavyo…” Madam akajibu huku sura yake bado ikionesha shaka kuu, “kweli wewe ni Amata?” akamuuliza tena.

“Ndiyo Madam!”

“Jina lako lingine…”

“Mr. Spark!”

“Lingine…”

“Inspekta Jaffary…”

“Na ulilotumia Arusha kwa Abiseilim…”

“Jaffari Makono…”

“State of Living…”

“Living of state!”

“Good!” Madam akaafiki na kuirudishia usalama bastola yake kisha akaitia katika pochi. Hatua nne nyingine zikamfikisha katika jokofu, akatoa pombe kali na bilauri tatu, akaja nazo mezani na kuketi, akajimiminia na kumpatia Kamanda kisha akajiegemeza kitini na kumtazama kijana huyo kwa makini.

“Nini kilikupata Amata, na ulikuwa wapi?” akauliza. Amata akainua fulana yake aliyoivaa na kumuonesha Madam S jeraha la risasi kwenye nyama za ubavu wake. Lilikuwa jeraha bichi kabisa lililoonesha dalili zote ya kuwa bado linahitaji tiba ya kitaalamu.

“Shiiiit! Risasi?”

“Ndiyo!” akajibu na kunyamaza kwa sekunde kadhaa, akavaa fulana yake na kuinua bilauri iliyojaa pombe, akapiga funda moja la maana kisha akaitua mezani kwa kishindo.

“Sifi tena kama hii haijaniua,” akajibu huku akifunika na kumwacha Madam S akiwa kinywa wazi kisha Amata akamsimulia kila kilichomsibu.

Hadithi ile ya kuogofya ilimfanya Selina atahayari, mara kadhaa alionekana akifinya macho, mara nyingine akishtuka na kadhalika. Hakuamini jinsi ambavyo kijana wake amepona katika hali isiyoelezeka.

“Tumshukuru huyo mwanadada aliyekupatia tiba ya mitishamba, si tungeshakukosa!” Madam akamwambia.

“Hata wale wazee pia ambao wameniokota, washukuriwe…”

“Of coz!” Madam akamwambia a kutulia huku akiitazama simu yake, kisha akamtazama tena Amata.

“Kamanda Amata, nilishatakiwa kutangaza kifo chako lakini nilikataa na kuwahakikishia kuwa upo hai kwa sababu najua wazi kuwa ni Mungu atakayeichukua roho yako lakini si binadamu mwingine awaye yote,” Madam akaeleza.

“Umenea sawa, vipi kuhusu Scoba?” Amata akauliza maana hakuwa akijua chochote kuhusu mtu huyo.

“Scoba tulimpata usiku wa siku hiyohiyo, sasa ni mzima na anaendelea vyema, hataki kabisa kusikia habari za kuwa wewe umekufa,”

“Yuko wapi?”

“Shamba. Bado yuko shamba na hatuwezi kumwacha hadharani, tuliliweka hivyo ili kuhakikisha kuwa tumekupata kama si wewe basi mwili wako,” Madam akaeleza.

“Nipo hai, na ninaishi kwa mara nyingine tena, je; mlifanya lolote kwa kumsaka Pancho?”

“Hapana kamanda, tuliliacha kama lilivyo, tuliona kwanza tuhakikishe habari ya wewe kisha ndiyo tujue kama ni kuweka matanga au kama ni kufanya sherehe…”

“Fanya sherehe…” Amata akadakiza kusema.

“Mpenzi wako Gina hana raha kabisa kwani hata yeye ana huzuni na kifo chako,” Madam S akaendelea kuzungumza na Amata juu ya tukio hilo lililowapa mshtuko mkubwa na kuwafanya kiasi fulani kutikisika.

Wakati huohuo honi za gari zikasikika getini Madam S akabonya swichi maalumu iliyowekwa ukutani na kuruhusu geti hilo kufunguka. Gari dogo aina ya RAV 4 likaingia ndani. Amata akasimama pale alipo na kulitazama gari hilo likiingia taratibu.

Jasmine! Akawaza na kurudi kitini.

Hali ya Jasmine ilikuwa ileile pindi tu alipoingia nyumbani kwa Madam S, alipatwa na mshtuko alipomuona Amata pale kitini.

“Ni wewe? Amata nooo!!!!” akapagawa na kumkumbatia kwa nguvu hapo hapo kitini, “sijui Gina atafurahi kiasi gani akikuona, maana nahisi karibu anarukwa na akili kwa kukukosa…” akalalama. Baada ya mazungumzo ya kina, Amata alimwonesha Jasmine lile jeraha ubavuni mwake. Naye kama daktari akalitazama kwa mbali na alipoona hawezi kujua vyema ukubwa wa jeraha hilo akachukua mipira ya mikono na kuivaa, kisha akalitomasa taratibu kila upande.

“Asssss!!!! Taratibu bwana!” Amata akagugumia maumivu.

“Nilitaka nijue linauma kiasi gani, risasi au kitu gani?” akahoji.

“Risasi!” Amata akajibu wakati Jasmine akitulia kwenye stuli.

“Inabidi tusafishe,” akamwambia.

“No, nina dawa nimepaka hapo, huo weusi sio uchafu,” akamjibu.

“Risasi wameitoa? Lazima nijue…”

“Mi sijui, nilipostuka nimejikuta nagangwa tu!”

“Good, lazima tufike Shamba ili niweze kutazama kwa Ultra Sound, nijwe na uhakika kama imetoka au bado ipo,” Dkt. Jasmine akamwambia Amata.

“Sawa dokta! Utahitaji kunichoma sindano?”

“Sindano muhimu, yaani ushujaa wote huo unaogopa sindano?”

“Sindano ni sindano mama!!!”

“Ok, hata hivyo inabidi sasa kwenda pamoja Shamba tukaweke mikakati yetu vizuri hakuna kulala,” Madam aliwaeleza vijana wake na wote wakajipanga kuondoka. Chiba na Gina nao wakapewa taarifa za kufika huko usiku huo

Usiku huohuo…

Madam S, Amata na Jasmine walikuwa kundi la kwanza kuwasili katika afisi hizo za siri. Moja kwa moja walimfikisha Amata katika chumba chao kidogo ambacho kwacho uganguzi wote na utabibu hufayika. Kilisheheni mitambo tiba ya kisasa ambayo ingeweza kuwekwa kwenye hospitali kubwa lakini hapa iliwekwa

kwa kazi maalumu. Amata akafikishwa ndani ya chumba hiki na kutakiwa kulala juu ya kitanda ambacho juu yake kulifungwa taa kubwa yenye mwanga mkali pamoja na vifaa vingine.

SHAMBA

Akiwa hana fulana wala suruali isipokuwa nguo maalum aliyotakiwa kuvaa, alitulia kimya kitandani. Jasmine akawasha mtambo huo na kuweza kufuatilia kila kilichoonekana katika luninga yake pale ukutani. Baada kama ya dakika tano za kumulika huku na huku akakipachika kidubwasha 'Transducer Probe' kile mahala pake. Akashusha pumzi na kumtazama Madam S.

"Vipi?" Madam akauliza.

"Hamna kitu, risasi kama ilikuwepo basi wameshaitoa kwa njia yao, na kinachonishangaza ni kuwa hili jeraha liko vizuri tu kwa ndani kasoro hapa nje tu, na panaonekana kuwa panaendelea vizuri, kweli hizi dawa za shamba zina nguvu," Jasmine akamwambia Madam S.

"Haya kaa!" Amata akaambiwa naye akakaa juu ya kile kitanda.

"Unajisikiaje sasa?" Madam S akamuuliza.

"Niko poa, unaweza kuingia kazini?"

"Kama kawaida, na ni lazima nimtie mkononi huyu Premji anayejiita Pancho!" Amata akajibu.

"Noooo! Hauna budi kupumzika kwa saa sabini na mbili kabla ya mikiki mingine haijaanza…" Jasmine akamwambia.

"Sawa dokta…"

- * *

Chiba na Gina waliingia katika jumba hilo kwa nyakati tafauti na kujikuta ndani wakiwa hawajui nani na nani wamekwishafika. Kwa jinsi jumba hilo lilivyojengwa kwa ndani, huwa ni vigumu kutambua nani kaingia na yuko wapi. Kila mmoja alikuwa na chumba chake kilichokuwa na kila kitu na angeweza kukaa humo hata mwezi pasi na kutoka nje. Zaidi ya hapo kulikuwa na chumba cha mikutano, chumba cha mazoezi 'GYM', baa ndogo, jiko, na afisi tafauti. Kama ukikaa katika afisi ya Chiba ungeweza kujua wote waliongia ndani ya nyumba hii kwani ni yeye tu anayeweza kuona kwenye kamera za usalama milango yote ya kuingili humo ndani na maeneo mengine. Iliitwa SAFE HOUSE kwa sababu inaweza kumficha mtu na asionekane katika jamii kwa muda usiojulikana. Kulikuwa na sehemu ya kuhojia wahalifu, ikiwa imesheheni kila zana ya kutesea, kulikuwa na chumba cha matibabu na maegesho ya magari ndani kwa ndani. Kwa ujumla jumba hili lilikuwa na sehemu kubwa mbili yaani 'ground floor' na 'underground floor'. Ground Floor ilikuwa ni nyumba ya kawaida sana ambayo wageni wote waliokuja kwa siri walifikia hapo. Underground floor ndiyo ilikuwa na hayo makolokolo yote, na mlango wa kuingilia ilikuwa ni siri yao. Mhalifu yeyote aliyefikishwa hapo aliondolewa sox ya usoni pindi afikapo katika chumba cha mahojiano na si zaidi ya hapo. Lakini 'Shahidi' alifikishwa katika 'ground floor' na mambo yake yalifanyikia hapo. Hakuna aliyekuja katika jumba hili macho wazi zaidi ya TSA, hata Mheshimiwa Rais akitaka kufika hapa lazima afichwe sura yake asione wapi anakwenda.

Kikazi iliitwa Safe House na kimaisha waliita Shamba.

Madam S na Kamanda Amata wakapanda ghorofa ya juu kutoka shimoni ili kukutana na wapendwa wao. Ilikuwa furaha ya aina yake walipokutana tena na Kamanda Amata, kila mmoja alikuwa na hamu ya kutaka kujua hasa ni nini kilimsibu mwenzi wao huyo hata kutoweka kwa siku hizo tatu kama sio nne. Gina ndiye

haswa aliyeonekana kuchanganyikiwa zaidi kwa kumwona Amata hakuamini kabisa kwani alishajua mtu amekufa alikuwa akisubiri tu taarifa ya kiofisi.

“Mmefurahi sana ee?” Madam S akawauliza.

“Ndiyo maana yake, hii ni furaha ya kukutana pamoja maana tulikwishachanganyikiwa,” Chiba akaeleza.

“Ok basi sherehe iishe na sasa tuangalie kazi,”

Wote wakaketi vitini katika meza yenye umbo la yai huku wakimwacha madam S upande wa peke yake kama kiongozi.

“Hatutakiwi kuchelewa kwani adui yetu anaweza kututoroka na tusimwone tena,” ilikuwa ni sentensi ya kwanza katika kufungua kikao hicho kutoka kwa Madam S. Na wote wakatikisa vichwa.

“Tunapaswa kuingia kazini, tukamsake huyu mwanaharamu, tumtie nguvuni, hastahili kuishi nje ya gereza,” akaendelea kuongea mara hii akionekana wazi kuwa ana hasira moyoni mwake.

“Sawa Madam, sasa tunajipangaje kwa maana bila shaka pale walipodunguliwa Scoba na Amata ndipo kwenye makazi ya mtu huyo ijapokuwa hapajaonekana wazi,” Chiba akaeleza wasiwasi wake.

“Ndio, msako huu utafanyika katika eneo hil…”

“Ina maana mpaka sasa Pancho atakuwepo bado? Nina wasiwasi atakuwa keshaondoka nchi hii,” Gina alimkata kauli Madam S.

“Yupo hajaondoka, tulidhibiti njia zote za kutokea nje ya nchi kuanzia viwanja vya ndege, bandari mpaka stendi za mabasi na hasa kule mipakani, kila basi linapekuliwa kwa umakini na kila abiria anafanyiwa uchunguzi wa kina kwani anaweza kujibadilisha sura na akaondoka. Kwa jinsi hiyo hatujapata jibu kama amekamatwa,” Chiba alieleza.

“Kwa hiyo yupo,” Scoba akaeleza.

“Kamanda Amata ana jeraha yampasa kupumzika kwani hawezi mikikimikiki kwa sasa,”

Jasmine aliliambia jopo, ndipo na wengine wakapata kujua kuwa Amata alikuwa amejeruhiwa.

Wote wakageuka kumtazama kwa huruma.

“Alikwambia nani, hii show tunaingia wote jukwaani na lazima mtu huyo akamatwe ndani ya saa 24 kutoka sasa. Hata kama ni kukodi vifaru, tutakodi na kuchimbua eneo lote lile,” Amata akawajibu.

“Ndio maana nakupenda mpenzi,” Gina akamalizia.

“Art of War,” Kamanda akamwambia Gina huku akimtazama usoni kisha wote wakacheka.

Simu ya mkononi ya Madam S ikaita, akaitazama kwenye kioo na kukunja sura kisha akawatuliza kwa ishara ya mkono na kuiweka sikioni ile simu wakati huo Chiba akiwa tayari keshapachika kifaa chake cha kurekodi sauti hiyo.

"…na kwa sababu mnajifanya mnajua, sasa sikilizeni redio usiku huu mtaelewa kuwa sitaki kutaniwa…"

Na ile simu ikakatika baada ya sauti hiyo ya mkoromo kukoroma sikioni mwa Madam S. Private number! Akawaza Madam S na kuishusha taratibu.

Sura ya Kamanda Amata ikabadilika na kuwa sura ya kazi, akatazamana na Madam S wasipate jibu wakatia huo, Chiba aliondoka na simu ya Madam S na kuingia katika chumba chake cha kazi kuifanyia uchunguzi simu hiyo ilipigwa kutoka uelekeo gani.

"Pancho Panchilio au kibaraka wake, hawezi kuwa mwingine, atapatikana tu," Chiba akajibu.

"Hawana maisha marefu, Sun Tzu ametufundisha kwenye Art Of War 'If the enemy leaves door open, you must rush in…'" (Kama adui ameacha mlango wazi, fanya hima kuingia) Amata akasema huku akijiweka vyema kitini, "adui yetu kaacha mlango wazi, tusichelewe!" akamalizia. Madam S akatikisa kichwa na kumtazama Gina.

"Gina, fanya kazi niliyokupa sasa," akamwambia binti huyo. Gina naye hakuchelewa akasimama na kuondoka katika chumba hicho.

Saa 7 Usiku…

Hali ya hewa ya Jiji la Dar ilikuwa tulivu kabisa, giza nene lisilo na mbalamwezi lilitawala wakati Gina akiegesha gari lake eneo la Upanga katika barabara ya Ally Hassan Mwinyi, karibu kabisa na hoteli ya Palm Beach. Kamanda Amata akiwa ameketi upande wa kushoto katika kiti cha abiria, aliiweka vizuri bastola yake tayari kwa lolote.

"Vipi?" Gina akauliza.

"Sina utani na mtu sasa hivi," Amata akamjibu Gina, kisha wakateremka garini, "vijana wako wapi?" akauliza.

"Wameshafika tayari wapo kwenye pozisheni zao," Gina akajibu. Kisha wakavuta hatua kuielekea hoteli hiyo ambayo siku hiyo ya wikiendi watu walijazana kwa starehe mbalimbali.

- * *

KAMBA SEBULE alikuwa akifurahia maisha ndani ya ukumbi mkubwa uliokuwa na michezo mbalimbali ya kujipatia pesa. Akiwa na walinzi wake binafsi, alijumuika pamoja na wengine wengi waliokuwa hapo kutafuna maisha. Si kwamba walifanya hivyo kwa sababu ya ukata ili wajipatie pesa ya kujikimu, la, walikuwa na ukwasi wa kutosha, walijumuika ili kuzichezea na si kucheza. Furaha haikuweza kujificha katika nyuso za wote waliozunguka eneo hilo huku wadada warembo wakitumbuiza kwa muziki uliokuwa ukipigwa mubashara kutoka jukwaani, wakicheza kwa minenguo ya Kikongo huku wakiwa wamevalia nusu utupu. Mijanaume yenye uchu ilikuwa imezunguka jukwaa hilo lililojengwa juu kidogo na kutazama wadada hao wakifanya mambo yao hadharani, macho yakiwatoka pima kana kwamba wakitazamacho kitaanguka ili wakigombanie.

Kamba Sebule, kigogo wa serikali, aliendelea kuburudika na rafiki zake waliofanana na yeye kiuchumi, waliokuwa wakicheza 'poker' na wakati mwingine 'Lucky Wheel' na kufurahia pesa waliyokuwa wakiivuna. Mmoja wa walinzi wake alionekana kuchezwa na machale kidogo, akatoa kitu kama picha katika mfuko wake wa shati na kuiangalia kwa sekunde kadhaa kisha akairudisha mfukoni, na kumwinamia Kamba Sebule, akamnong'oneza kitu.

- * *

Gina na Amata walijichanganya ndani ya ukumbi huo, wakipenyapenya katia ya watu wengi waliokuwa wakienda huku na kule na macho yao yakifanya kazi ya ziada ya kutazama huyu ni nani na nani ni huyu.

“Nahisi wametugundua,” Gina akamwambia Amata.

“Ndiyo nimeona, yule mtu inaonekana ana picha ya mmoja wetu, kwa nini katembea nayo?

Lazima tuipate na tujue kaipataje,” Kamanda Amata akamwambia Gina.

“Wanatutazama,” Gina akamwambia Amata.

“Ndiyo, ondoka nenda chooni, wakija nami nakuja hukohuko,” Amata akatoa maelekezo na Gina akayafuata bila kuhoji. Akavuta hatua kuelekea chooni, kama alivyofikiria Amata ndivyo ilivyokuwa.

Daima akili zetu zipo namna hii! Amata akajiambia kisha akendelea kuweka jicho lake kwa watu hao. Yule mlinzi mmoja akambonyeza mwenzake na wote wawili wakatoka kuelekea kule chooni wakamwacha Kamba Sebule na mlinzi mwingine mmoja, wakiahidi kuwa wanarudi muda tu. Kamanda Amata naye akajinyanyua taratibu na kuelekea upande uleule.

Gina aliingia katika choo cha wanawake, ndani ya kichumba kidogo, akafungua maji na kusimama kando, dakika moja ikapita, akafunga maji, akajiweka tayari huku akipiga mruzi na kufuatisha wimbo uliokuwa ukisikika kutoka ukumbini. Akafungua mlango kutoka nje na ndipo alipokutana na vijana hao. Gina akajifanya kupita katikati yao kama hajui kinachoendelea.

Mmoja wa wale walinzi akamzuia kwa kifua chake kipana asipite, Gina hakuuliza wala hakupoteza muda, alimsukuma kando akadakwa na Kamanda Amata kwa nyuma. Amata akamgeuza na kumpiga kichwa kisha akamdaka kolomeo kwa kono lake la kulia na kumfanya mtu huyo aanze kutapatapa kutafuta pumzi.

Gina aligeuka ghafla na kumchapa ngumi nzito yule wa nyuma yake, nae akajibu shambulizi lakini Gina alikanyaga mguu wake ukutani na kuepa shambulizi hilo, alipotua chini alimpa pigo moja la karate lililompata barabara na kumwacha akiwewe weseka alipotulia alijikuta mbele ya domo la bastola ya mwanamke huyo. Kamanada Amata aliendelea kumbana kolomeo yule jamaa mwingine huku akimhoji.

“Nani bosi wako?” Amata akauliza.

“Kamba, Ka-ka-mmmbbba!” akajibu kwa tabu huku akianza kulegea.

“Makazi ya Kamba yako wapi?”

“U-pa-ngggga!”

“Ofisi yake iko wapi?”

“Mtaa wa Ka-ka-lu-ttttaaaa namba 25!” akajibu na kuanza kutapatapa kwa nguvu.

Yule jamaa aliyetazamana na domo la bastola ya Gina akajaribu kutafuta mbinu ya kujiokoa wakati huo nje ya choo hicho walisikika watu wakiingia kujisaidia. Gina akashusha bastola yake na kuifutika kiunoni, kosa. Yule jamaa akarusha ngumi iliyompata Gina usoni na kumyumbisha kiasi fulani. Ngumi ya pili Gina akaudaka mkono na kuuzungusha kwa nguvu.

“Aaaaaiiiiiggggghhhh!” akatoa yowe la uchungu, huku mifupa ya mkono ikiachana, akamrudisha mbele na kumpiga futi la kwenye korodani kabla hajajibwaga chini na kujipigiza kwenye sinki la kunawia maji na kutulia sakafuni akikoroma. Kamanda Amata akafungua mlango wakatoka na Gina na kuwaacha watu wakitukana na kusonya huku wakiingia ndani kujisaidia.

“Mama majambaziiiiiiii!” ilisikika sauti ya kike ikipiga yowe kutoka chooni.

Pameharibika! Kamanda akawaza na moja kwa moja akamshika mkono Gina na kurudi ukumbini, hali ya taharuki ikaugubika ukumbi huo, walinzi wa hoteli wakaingia kuangalia kulikoni.

“Ita vijana,” Kamanda akamwambia Gina, naye akachomoa simu yake ya upepo na kuwaita waingie. Moja kwa moja walisimama kwenye ile meza ya ‘poker’.

“Upo chini ya ulinzi, Kamba Sebule,” Gina alimwambia huku Kamanda Amata akiwa kasimama pembeni, bado kulikuwa hakujatulia. Mheshimiwa huyo alitulia kimya macho yake yakiwa juu ya ile meza yakiangalia karata zilizopangwa juu yake.

“Wewe ni nani, na una mamlaka gani ya kuniambia mimi hayo?” Kamba akauliza bila kugeuka.

“Tii sheria bila shuruti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo iliyonipa malaka hayo,” Gina akaunguruma.

“We mtoto wa kike hivi ushawahi kuzaliwa? Hujui I ni sawa na baba yako mzazi?” Kamba akalalama.

“Kamba Sebule sitaki kutumia nguvu kwani nimekuja na nguvu kubwa kuliko unavyofikiri,”

Kamba Sebule akageuka taratibu na kukutana na sura ya Kamanda Amata, hakuamini kama ni mtu kweli au mzimu. Akarudisha macho kwa Gina na kukutana na sura ya mwanamke mrembo lakini isiyoonesha hata chembe ya tabasamu. Akatanabahi kwa vijana walioingia ndani ya ukumbi kwa dakika moja iliyofuata, walikuwa na nyama za kimazoezi, fulana zilizowabana zilidhihirisha hilo.

“Huna adabu msichana!” Kamba akaunguruma na kuchomoa simu yake lakini kabla hajaiweka sikioni ilinyakuliwa na Amata, na alipotaka kuleta tabu Gina alimtandika pigo moja uso na kumrudisha mezani akiwa hoi.

“Tia pingu!” akawaambia vijana wa polisi nao wakatekeleza na kuondoka naye.

05

“Kijiji chote kimeteketezwa kwa moto!” Mkuu wa nchi alisikika akiongea kwa kututumka, mbele yake alikuwa Madam S amesimama.

“Huyo ni shetani! Lazima utawala wake usambaratishwe na watenda mema,” Madam akajibu.

“Sikiliza Sellina,” akasimama kwa msisitizo, “Nahitaji uchunguzi wa siri na ikiwezekana huyu mtu akamatwe,” akasisitiza.

“Najua wajibu wangu mheshimiwa, mzuie Waziri wa Mambo ya ndani asitumie nguvuy kubwa, acha mimi nikafanye kazi, ikifika wakati wa kuhitaji vijana wake nitakwambia, ila kwa sasa waache wale wa Bagamoyo kwa kuwa ni eneo lao, naondoka sasa,” akamaliza Madam S na kutoka mle ofisini.

Akiwa ndani ya gari yake akampigia Amata na Gina wakutane ofisi ndogo, akaitazama saa yake tayari ilitimu saa 4 usiku.

Kweli kazi za serikali ni za kujitolea, watu wamelala sisi tunahangaika! Akawaza mwenyewe huku akiliacha langa la Ikulu na kuelekea afisini kwake.

KITUO CHA POLISI CHA SULENDER BRIDGE

“Bagamoyo, Ba- ba –gamo-yo koh! koh! koh!” Kamba Sebule aliongea mengi baada ya kipigo cha polisi kukolea mwilini mwake kwa amri ya Kamanda Amata.

“Bagamoyo kubwa, sehemu gani?” Kamanda akauliza.

“Si nime-wa-jib…”

Mkanda wa jeshi ukatua mgongoni mwake na kumletea maumivu makali.

“Unafikiri tunacheza hapa? Tuambie ni kijiji au ni sehemu gani?” mmoja wa polisi aliuliza.

“Kisi-wa-wa-ni, Kale-b-be” mwishowe akatamka ijapokuwa kwa tabu kidogo.

Kamanda Amata akatikisa kichwa juu chini huku akimtazama Gina. Simu yake ikaanza kufurukuta mfukoni akaitoa na kutazama ‘Madam S’ ilijiandika juu ya kioo, akaingiza tarakimu fungushi na kuiweka sikioni.

“Tukutane wodini haraka mama anaumwa Tena Sana Aisee,” ilikuwa ni ujumbe wa sauti aliyoutuma. Akageuka na kumtazama Gina, kisha akarudisha macho kwa wale vijana wa polisi.

“Sasa muhifadhini huyu mpaka nitakapowapa amri nyingine, sisi tunatoka,” akawaambia wakati wakiondoka na kuingia garini.

- * *

OFISINI NDOGO

Ndani ya ofisi hiyo Madam S alikutana na vijana wake wote watano, aliwapa ujumbe aliyoupata kutoka Ikulu ambako kama kawaida yake alikwenda kupeleka ripoti ya siku. Kwa harakaharaka alionekana hayuko sawa kwani alikuwa akifanya vitu na kuongea kwa harakaharaka.

“Kijiji cha Kitopeni kimevamiwa na kuchomwa moto huku raia wakipigwa vibaya leo jioni hii,” madam aliongea harakaharaka huku akiwa kasimama wima.

“Kitopeni Bagamoyo?” Gina alidaka kwa swali.

“Ndiyo!”

Wakatazamana kisha wakarudisha macho kwa Madam S, hakuna aliyekuwa na swali wala kuongea ila ndani ya macho yao kulibaki na mshangao wa dhahiri kabisa. Walikijua kijiji huki vema kwa sababu ndipo walipomuokota Scoba majuma kadhaa nyuma.

“Kitopeni ndo wapi?” Amata aliuliza.

“Ni usawa ule ambao ndege yenu ilidunguliwa,” akajibiwa na Madam S.

“Bila shaka ni wao, haina kupoteza muda TSA Kazini,” Chiba alisema huku akinyanyuka na kuungwa mkono na wenzake.

“Bila shaka, nimezuia polisi wa huku kufika kule kwanza nataka sisi tuingie kwanza ili tufanye uchunguzi wa awali ambao kwetu ni uchunguzi wa msingi wa kumjua mhalifu,” madam S aliwaambia kisha kila mmoja akaanza kuchukua kinachomfaa katika stoo iliyojengwa ndani humo.

“Kamanda Amata, una jeraha, halijapona, ni vyema usifanye mikiki mikiki yoyote ile,” Jasmine alimwambia Amata.

“Hapana, wacha niende, kama ni Pancho basi mara hii hatakiwi kuishi, huu ni uhalifu mkubwa sana haijawahi kutokea kwenye historia ya nchi hii,” Amata akaunguruma.

Dakika kumi zilizofuata, Land Cruiser V8 ilifuatana na Range Rover zote zikielekea Kitopeni, ndani yake kulikuwamo na hao vijana watano. Gari ya kwanza alikuwapo Amata, Chiba na Gina ambaye aliukamata usukani na ile ya nyuma alikuwamo Jasmine na Scoba pamoja na Madam S. mwendo waliokuwa wakipita nao ulikuwa si wa kawaida. Kama wananchi walizoea kuishangaa misafara ya viongozi kwa mwendo kasi basi hii ilikuwa funga kazi ila hakuweza kuona kwa sbabu tayari ilikuwa usiku.

Kila mmoja alikuwa akiwaza lake kichwani, ukimya ulikuwa ukitawala kila nukta katika gari hilo ambalo Chiba alikuwa akiliongoza.

KIJIJI CHA KITOPENI

Usiku huu ni moshi na vilio ndivyo vilivyosikika katika eneo hilo.

Haya mambo nilikuwa nayaona kwenye filamu tu kumbe yapo hata huku siku hizi! Amata akawaza huku akiendelea kula karanga zilizokuwa ndani ya chupa ndogo.

“Na we na makaranga yako!” Gina akaalalama.

“Makaranga jina la mtu!” Amata akajibu huku akiendelea na shughuli yake. Muda kidogo wakaegesha magari yao na kuteremka chini, darubini vifuani mwao, bastola viunoni. Walikuwa tayari kwa lolote.

Wananchi wa kitopeni walikuwa wamejikusanya pamoja, wengine wakiomboleza vifo wengine wakiwa hawana makazi na wengine maumivu makali ya majeraha waliyoyapata katika shambulio hilo.

TSA waliteremka kutoka katika magari yao na kuanza kufanya chunguzi zao za hapa na pale kwa kuhoji na kutazama hali halisi ya eneo hilo.

“Mnasema hao watu walikuwa wangapi?” Amata alimuuliza mmoja wa wanakijiji aliyeonekana kujishughulisha sana kuwasaidia wenzake.

“Walikuwa kama kumi au kumi na tano walikuja wakitokea mashambani huku,” yule kijana alieleza.

“Tuliwaona wanaibuka kule baharini sisi tukakimbia,” mmoja wa watoto aliyekuwa hapo alisema. Kamanda Amata akiwa na Chiba na Madam S walisikiliza maelezo ya wahanga wote walioweza kuongea, kisha wakaitana pembeni.

“Sikia Chiba na Amata hawa bila shaka wamekuja kwa kupiga mbizi,” Madam aliwaambia.

“Kwa maana hiyo hawa jamaa wanaweza kuwa na makazi eneo hilihili,” Chiba akaongeza.

“Kisiwa cha Kalebbe,” Kamanda akawaambia kisha wakamwita tena yule kijana na kumwomba awatajie majina ya visiwa vilivyo karibu na eneo hilo. Akawatajia kwa majina na kuwaonesha kisiwa hicho cha Kalebbe ambacho kilikuwa katikati ya visiwa vingine.

“Mnafikiri pale atakuwa anaishi mtu? Sio rahisi kisiwa kile kule ndio kuna mtu kajenga nyumba yake ndogo,” yule jamaa akaonesha kisiwa ambacho kina jengo la kawaida tu na lilionekana vizuri kwa darubini walizokuwa wakitumia vijana hawa.

“Ok,” Madam akaitikia na kumwacha yule kijana kuondoka.

“Madam, baada ya kumbana yule Kamba Sebule kule polisi kasema wana maskani yao kisiwa cha Kalebbe, so nafikiri sasa ni kuanza uchunguzi wa kisiwa hicho mara moja. Cha muhimu hapa tuache polisi wafanye kazi na sisi tuondoke tukajipange vyema, wasijue kama tumeingia hapa,” Kamanda akatoa maelekezo.

“Sawa, twendeni tukapige kambi Hoteli ya Ocean Breeze, na afisi yetu itahamia hapo mpaka kieleweke…” Madam akawaambia na wote wakaingia kwenye gari na kuondoka huku wakiacha polisi wakiendelea na nyajibu zao.

HOTELI YA OCEAN BREEZE – BAGAMOYO

Ni hoteli kubwa ya kifahari, iliyojengwa kandokando ya Bahari ya Hindi. Jingo hili lenye ghorofa sita lilizungukwa na miti mirefu na mizuri sana iliyotengeneza kivuli kinene wakati wa jua. Usiku huo Madam S na vijana wake waliwasili tayari kwa malazi ya siku hiyo. Katika meza ya mapokezi kila mmoja akajitambulisha kwa jina la bandia na kuchukua vyumba kwa mapumziko huku akili yao ikiwa kazini kwa muda wote.

Kijua cha asubuhi kilipochomoza pande za Mashariki kilimkuta Amata na Gina nje kwenye kibaraza cha ghorofa ya nne ya hoteli hiyo ambayo ilitazamana na Bahari ya Hindi na hapo ndipo wakagundua kuwa ipo karibu na bandari ya mji huo mkongwe, Pumbuji ya zamani, Bagamoyo ya sasa. Pembeni ya meza yao kulikuwa na darubini kubwa ‘Oberwerk’, yenye nguvu, ilikuwa na urefu wa inchi 24 iliyosimamishwa kwenye stendi madhubuti. Huku wakiburudika na kinywaji lakini akili zao zilikuwa katika kisiwa cha Kalebbe ambapo ndipo hasa walipoamini adui wao alipo. Juu ya meza hiyo hiyo kulikuwa na karatasi ambayo kwayo walikuwa wakiandika vitu fulanifulani wanavyovielewa wao.

“Tutaingiaje pale?” Gina aliuliza.

“Simple tu, ama tutasubiri giza la leo au twende kibabe mchana huu. Ila wazo zuri ni kuuchukua mchana huu na kukichunguza kisiwa kile ili tujue in and out, si ajabu tukapata njia nyepesi sana ya kufika pale kuliko tunavyofikiri”.

Gina akatazama saa yake ilikuwa tayari saa tatu za asubuhi, jua linazidi kwenda juu na joto nalo likiendelea kushika hatamu. Simu ya Amata ikaita pale mezani.

“…hello… Madam!” akaipokea.

“…vipi kamanda, kuna lolote huko?”

“…yeah, tunaangalia bado lakini hatujapata ufumbuzi ila taratibu tutapata,”

“…ok, kazi njema, niko na vijana hapa. Tunawaomba mfanye kazi tu na si vinginevyo,” kisha wote wakacheka.

Amata akainuka na kuingia chumbani akachukua simu na kupiga mapokezi akomba kuletewa vinywaji. Dakika tatu baadae, kijana aliyevalia nadhifu kabisa, nguo za kitamaduni akaleta vinywaji hivyo mpaka pale walipoketi.

“Asante sana,” Kamanda akamshukuru.

“We unaitwa nani?” akamwuliza.

“Naitwa Nassoro,”

“Nassoro unajua kisiwa cha Kalebbe?” Kamanda akauliza. Nassoro akamtazama kwanza kabla ya kujibu swali hilo.

“We cha nini?” akajibu kwa swali.

“Aaaaah! Usiwe kama Watanzania wengine kwa kujibu swali kwa swali. Napenda kwenda kukitembele kama utanipa maelezo zaidi juu yake, au kama mna vipeperushi vyake,”

“Kile ni kisiwa cha mashetani, watu huwa hawaendi kule,” Nassoro akajibu kwa kifupi.

“Nahitaji kwenda,” Kamanda akamwambia Nassoro.

“Sawa, karibu sana, si nimekwambia kisiwa cha mashetani, hivyo huwa yanaenda mashetani tu,” Nassoro akajibu na kuondoka.

Gina na Amata wakatazamana. Anajua kitu huyu! kila mmoja akawaza sawa na mwenzake. Amata akainua mkono na kubofya saa yake hapa na pale kisha akaisogeza karibu na kinywa chake.

“…muweke jichoni, amevaa shati la kitenge na suruali nyeusi na kofia ya kitenge, ni mwenyeji wa hapa tulipo…”

“…copy…” Chiba akajibu kwa njia ileile.

Mara kwa mara Gina alikuwa akisimama na kuiendea ile darubini na kuchungulia ndani yake kuona kama kuna lolote geni, na alipomaliza kuchungulia alibonyeza kidubwasha fulani na kupiga picha ya hicho anachokiona, na ile taswira ilisafiri mpaka kwa Chiba kwenye mashine ndogo mfano wa simu na wao waliweza kuitazama vizuri na kuangalia kama kuna mabadiliko yoyote.

Mara hiyo saa ya Kamanda Amata ikaanza kumfinya, akaitazama kwenye kioo na kubofya mahala fulani kisha akapachika kifaa chake sikioni na kusikiliza.

“…yuko jichoni, kaingia mapokezi, anatumia simu ya mezani…” Chiba akamwambia Amata.

“Sawa! Jaribu kudukua chochote katika hilo…”

Chiba akaondoa ukurasa wa juu katika chombo chake hicho na kupachika vizuri vifaa vya masikioni, akabofys hapa na pale juu ya kioo na kujaribu kutafuta mawimbi ya simu hiyo kama ataweza kuyapata.

“…. ko wawili, wanatumia darubini kubwa kutazama kisiwa (…) hapana sijui kabisa (…) sawa sawa, nitahakikisha hilo!”

Chiba aliweza kukamata mawasiliano ya simu hiyo kwa urahisi sana tafauti na alivyofikiria, akatikisa kichwa na kumtumia taarifa Amata kwa njia ya simu yao.

“…tegemea ugeni…” Amata akamwambia.

Wakakata mawasiliano, Amata akarudisha macho kwa Gina.

“Vipi?” Gina akauliza.

“Poa,” Amata akajibu na kusimama, akavuta hatua chache kuingia chumbani, akauelekea mkoba wake na kuchomoa bastola moja, akaijaza risasi za kutosha. Nyuma yake akahisi kama kuna mtu kasimama, akahisi mikono ikigusa mabegani, hakugeuka kwani ulaini wa mikono hiyo alishajua ni nani anayemgusa.

“Vipi ushaanza kufikiri kuua!”

“Akili yangu tayari ishaanza kuzunguka, nahisi kutokea hatari ndani ya muda mfupi ujao, jiweke tayari nawe pia,” akamwambia Gina na kumgeukia. Gina akaweka mikono yake kiunoni mwa Amata.

“Nimemiss!” akamwambia.

“Sio wakati wake, au na wewe ni mmoja wao unataka kunilaghai kwa mapenzi?” Kamanda akajibu na kujitoa katika himaya ya Gina.

“Ningekuwa mmoja wao ningeshawateketeza nyote mpaka sasa, hujui kama sdui mbaya ni yule aliye miongoni mwako?” Gina akamwambia huku akimwachia kijana huyo kama alivyotaka. Amata akaipachika bastola yake kiunoni “mwanamke unamaneno wewe ka mtoto wa Kizaramo,” akasema huku akiiendea ile darubini, akaweka macho yake pale na kutazama tena. Mara hii kitu kipya kikaonekana, kwa mbali aliona kitu cheupe katikati ya bahari.

Nini kile! akajiuliza na kukiweka vizuri katika muonekano sawa. Boti, ilikuwa ni boti iliyoonekana kuja kwa kasi na kutimua maji hayo kuyafanya kuwa meupe, akabonyeza kile kitufe na kupiga ile picha. Akaendelea kuangalia ile boti iliyokuwa ikisogea kwa kasi, sasa aliweza kuiona vizuri, ndani yake kulikuwa na watu watatu, wanaume wawili, waliovaa nguo nyeupe za kisasa, mmoja alikuwa akiongoza boti hiyo na mwingine alikuwa nyuma kabisa. Katikati yao kulikuwa na mwanadada mrembo sana aliyeketi kwenye kiti na bilauri iliyojaa kinywaji, akabonyeza tena kile kitufe na kuisafirisha ile picha.

- * *

Kifaa kile cha Chiba kikatoa ukelele hafifu, akakinyakuwa na kutazama, picha.

“Ugeni kama ulivyotabiriwa,” Chiba akamwambia Madam S huku akimpa kile kimashine ambacho kilimwezesha kuona zile picha vizuri. Muda huohuo akamwona yule kijana akitoka katika chumba fulani na kuelekea nje, Madam S akamwita kwa mruzi, kijana akageuka na kusogea pale mezani.

“Nahitaji vinywaji kijana,” akamwambia.

“Oh! Samahani kuna mgeni nampokea hapo gatini naomba nikuitie mhudumu mwingine,” Nassoro akajibu. Madam S akamshika mkono kwa nguvu na kumkazia macho.

“Kwa nini unataka kupoteza bahati kijana,” akamwangalia juu mpaka chini.

Nassoro akajikuta njia panda, akashindwa kuamua, alijuwa wazi kuwa kumkatalia huyu mama kama mteja haiwezekani na kutokwenda kumpokea huyo mgeni nako ni jambo linguine lisilowezekana.

“Ok, niitie mtu mwingine,” Madam akamwambia na kumwacha. Nassoro akaenda na kumwita mwhudumu mwingine wa kike ili amsikilize Madam. Yule mwanadada akaifikia meza waliyoketi Madam S na Chiba.

“Samahani, huyo anayekuja huko ni mgeni gani?” akamwuliza yule mhudumu badala ya kumuagiza vinywaji.

“Malkia, Malkia wa Kalebbe!”

“Malkia?” Madam akauliza na wakati huohuo yule mwanadada aliyejulikana kama malkia akaingia akiwa anafuatana na Nassoro na moja kwa moja akaenda kuketi kwenye meza iliyopambwa maua mazuri kabisa. Kulikuwa na siti mbili moja ikabakia wazi. Vazi alilovaa mwanadada huyo ndiyo kilikuwa kivutio kingine, alivaa bikini nyeupe na juu yake akavaa vazi lingiine jeupe jepesi kabisa lililokuwa wazi sehemu ya mbele na kuruhusu mwili wake kuonekana.

Nassoro akasogeza vinywaji pamoja na kibweta cha kuwekea jivu la sigara, huyo malkia mwenye mwili wa kisichana zaidi aliketi na kukunja nne huku akiwashiwa sigara na kijana huyo na kuanza kuvuta taratibu.

Madam S akamtumia ujumbe Kamanda Amata juu ya huo ugeni. Haikupita dakika moja, Kamanda Amata akajitokeza kutoka katika ngazi na kuvuta hatua fupifupi kuielekea ile meza. Akiwa ndani ya suti nadhifu nyeupe, shati jeupe na tai nyeusi.

- * *

“Bila shaka hautajiuliza mengi kwa mimi kuketi mbele ya mwanamke mrembo kama wewe, Malkia wa Kalebbe, hakika Mungu anajua kuumba kwa maana jinsi ulivyo hakuna mwanaume rijali atakayepita mbele yako bila kujikwaa hata kama sakafu ni ya marumaru,” Amata akaanza swaga na kuketi huku akichukua matunda madogo ya strawberry na kuyatia kinywani kisha kuyatafuna taratibu.

Mwanamke huyo alijikuta akiangua kicheko cha mwaka kwa maneno hayo matamu na ya kufurahisha. Hakuwahi kukaliwa mbele na kijana asiye na hadhi kama huyu, hili ndilo haswa lililomfanya acheke.

“Hakika kuna wanaume wameumbwa kufurahisha wanawake, lo, ulifikiri nini kuzungumza yote hayo?” akauliza huku bado akiendelea kucheka. Nassoro, mhudumu mahsusi wa malkia huyo akawasili pale mezani na kumtaka radhi Amata kuiacha meza ile.

“Oh, asante Nassoro, lakini mwache, mwache kanifurahisha sana huyu, mpe kinywaji tafadhali,” malkia akamwambia Nassoro naye akafanya hivyo. Ingawa juu ya meza ile kulikuwa na kinywaji ambacho bado kilijaa pomoni, lakini Amata alileteawa kinywaji kingine kabisa, kikawekwa mezani na kumiminwa kwenye bilauri safi, akaiinua na kuipunga hewani kisha yule malkia naye akafanya hivyo wakagonga cheers kwa afya.

“Nitasikia raha sana nikikunywesha japo kidogo,” Amata aliendelea na ubembe wake.

“Oh! No! kinywaji ni kwa ajili yako, enjoy little puppy!” akamwambia, Amata akaiinua na kukinywa chote kisha akaishusha ile bilauri mezani.

“Waoh, you are so strong man,” (wewe ni jasiri)

“Yes I am,” (ndiyo) Amata akajibu.

“Mmmmh you are smart!” Yule mwanamke akaendelea kumsifu Amata.

“Kawaida yangu!” akamjibu.

“Hebu nambie huko Dar, unafanya kazi gani?” akahoji.

5

“Mimi ni mwandishi wa habari, nina kampuni yangu inaitwa AGI Investment, tunashughulika na utafutaji wa habari za kitaifa na kimataifa, kuandika makala mbalimbali na habari za uchunguzi,” Amata akaeleza huku akimpatia kadikazi mwanamke huyo mwenye sura ya kuvutia.

Mazungumzo yakaendeleakwa kina kati ya wawili hao, Amata alikuwa akijaribu kucmchokonoa kwa maswali ili kujua mengi kuhusu kisiwa hicho, na mwanamke yule alikuwa akijibu pasi na wasiwasi wowote. Yule mwanadada aliyejitambulisha sasa kwa jina kamili la Zulekha alimwambia mengi sana juu ya kisiwa cha Kalebbe na Amata akamweleza mengi juu ya kampuni na kazi yake.

Nusu saa ikapita katika mazungumzo yao Amata hakuendelea kunywa kile kinywaji ila sasa alikuwa ni mzungumzaji zaidi kila Zulekha alipomhamasisha kunywa zaidi yeye aliishia kumimina tu, akimwambia ‘usijali nitakunywa’.

“Utapenda kunitembelea?” Zulekha akauliza huku akiumauma ncha ya ulimi wake.

“Kama utanitembelea mimi kwanza!” akamjibu namna hiyo.

Zulekha, akatazama chini kwa sekunde kadhaa, kisha akamtazama Amata usoni bila haya.

“Unataka nikutembelee?” Zulekha akauliza huku akirembua macho yake.

“Ndiyo, kisha nami nitakutembelea wewe!”

“Good boy! Utaniweza?” Zulekha akauliza huku mkono wake ukiishika ile ya Amata pale mezani.

“Kwa nini unauliza hivyo?”

“Kwa sababu ninyi vijana wa mjini mnakula sana chips, mkifika kwenye sita kwa sita mnahema kama mbwa anayekimbilia mfupa,”

“Hah! Hah! Hah! Mi siyo aina hiyo ya mwanaume,” Kamanda akajibu na mara hiyo, Zulekha akainuka na vazi lake likajimwaga na kuacha eneo kubwa la mbele wazi. Akamtazama kijana huyu shababi kwa jicho kimahaba.

“So?”

“Let’s feast!” Zulekha akamalizia na kumpa mkono Amata, wakatembea kwa hatua za madaha kuelekea katika ngazi ambazo ziliwafikisha ghorofa ya juu, ndani ya chumba cha Amata. Kama kuna kitu ambacho Kamanda alikuwa akijipanga kujibu ni juu ya lile darubini, maana kwa ubembe wa mwanamke huyo angeweza kutaka kuchungulia, ndipo angeona nyumba yake inavyoangazwa kwa ukaribu lakini walipoingia ndani ile darubini haikuwepo. Gina mara tu baada ya kusikia mazungumzo ya wawili hao akajua safari yao itafikia ndani ya chumba hicho, hivyo akaibeba ile darubini na kutoka nayo huku moyo ukimuuma wivu.

Wawili hao wakajitupa kitandani na mabusu motomoto yakachukua nafasi yake. Amata aliufurahia utundu wa mwanamke huyo maana alikuwa akimrambaramba kila kona ya mwili wake na yeye akaonesha utundu wote anaoujua. Dakika kama arobaini na tano hivi wakabaki kama walivyozaliwa na kila mmoja akaanza kufurahia kile afanyacho mwenzake na kujikuta wamezama katika mahaba mazito. Amata akasahau kazi, Zulekha akasahau kazi. Miguno na sarakasi za ajabu ajabu zikaendelea juu ya kitanda hicho.

“Uko vizuri kijana! Karibu nyumbani kwangu, sasa tutaweza kuzungumza mengi,” Zulekha akamwambia Amata baada ya kila mmoja kuridhika na huduma ya mwenzake.

“Namwogopa mumeo!”

“A ha! Hah! Hah! Hah! Sina mume… isitoshe ndani ya nyumba ile kuna mambo mengi, we utakuja kama mfanyabiashara kisha mengine mi najua tutafanyeje,” akamsihi kijana huyo. Kwa Amata hii ilikuwa ni nafasi ya pekee kuweza kufika kwenye jumba lile ambalo ndilo haswa lilikuwa limewaleta hapo Bagamoyo. Lakini kichwa chake tayari kilimwambia hapo kuna hatari ya kulubuniwa na kutekwa kirahisi.

“Vipi mbona hunipi jibu? Au hutaki kuijua Kalebbe? Utakosa habari!”

Amata akamgeukia na kumtazama machoni, akaona hila ya wazi kabisa kwa mwanamke huyu.

Sina budi kufanya hili, the opportunitry never come twice! Akawaza na kujiinua kitandani.

“Sawa, twende zetu!” akamwambia mwanamke huyo aliyejilaza kitandani kifua wazi, matiti yake kama ya msichana anyevunja ungo yalimfanya aonekane mrembo kama samaki-mtu. Zulekha akatabasamu na kumuuliza, “Upo peke yako?”

“Yes, peke yangu,” Amata akajibu. Kisha wote wakajiandaa kwa safari, wakatoka nje ya hoteli hiyo na kuelekea gatini ambako ile boti bado ilikuwa ikimsubiri. Wakaagana na Nassoro na kuondoka zao.

- **Katika Kisiwa cha Kalebbe vijana wa Pancho walibaki wakitazamana baada ya kutazama picha nzuri ya Zulekha na Amata pale kitandani. Picha hii iliyonaswa na mtambo uliofungwa katika jumba hili, ni wachache tu walioujua. Wale vijana walimwita mkubwa wao wa kitengo na kumwonesha anachofanya mwanamke huyo. Walijua wazi kuwa kila picha wanayoiona lazima Pancho anaiona kama ilivyo. Wote wakajikuta wakiduwaa mbele ya sikirini hiyo udenda ukiwatoka na miili yao ikikosa utulivu kila waliposhuhudia mke wa bosi wao akibanjuliwa na Kamanda Amata.

Nusu saa ilipita na kisha wakaona sasa safari inaanza ya kuja kisiwani.

“Anamleta, hakikisheni analipa yote aliyoyafanya kwa mwanamke huyu,” Yule mkubwa wao akatoa amri kisha akawapa tahadhari wengine kuwa wampokee kama mgheni wa bosi, wasimletee matata yoyote mpaka waambiwe vinginevyo.

Ndani ya kisiwa hiki, gabacholi huyu alikuwa amewekeza vitu vingi sana kwa siri, kulifungwa darubini kubwa ya kutumia umeme ambayo iliwawezesha viajana wake kuona nyendo zote za mtu wamtakaye. Mara tu baada ya kupata taarifa kutoka kwa mtu wao, Nassoro, ndipo wakaazimia kumtuma Zulekha kwa ajili ya kumnasa mtu huyo, maana walijua mwanaume hawezi kuponyoka kirahisi kwa mwanamke mrembo kama huyu. Na hii ndiyo ilikuwa kazi kubwa ya Zulekha kwa bwana wake, Pancho.

Pancho alipata taarifa ya ugeni huo akafurahi sana na mara hii alihakikisha kumtia adabu kijana huyu ambaye bado anakumbuka mambo aliyomfanyia huko India na kwenye ndege wakati wa kurudi.

- **

Gina aliinuka kitini na kuibeba ile darubini, haraka akaufungua mlango wa chumba cha Amata na kuingia ndani, akapita mpaka kwenye kibaraza kilekile akaiweka tena na kuanza kuchungulia na kuiona ile boti ikipotelea majini.

“Shit! Janaume linapenda wanawake hili, limeshatekeka kilaiiniiii,” akajikuta akiongea peke yake alipomuona Amata akiwa na Zulekha katika ile boti, akasonya na kuiacha ile darubini huku akiondoka na moyo uliyojaa wivu maana alijua wazi uwa Kamanda lazima keshamtafuna mwanadada huyo. Alipofika mlangoni, akakumnbana na Chiba na Madam S.

“Rudi ndani,” Madam akamwamuru huku Chiba tayari akiwa kwenye ile darubini akitazama ile boti.

“Jiandaeni kwa kazi ya kumkamata yule mwanaharamu, Amata atatuletea taarifa kama mtu huyo yupo au la,” Madam aliwaambia huku akibofyabofya simu yake hapa na pale, akaiweka sikioni.

“Hey!!! Scoba na Jasmine! Stand by! Tukutane Ocean Breeze ndani ya nusu saa, chambo tumeshatupa mtoni bado kuvua samaki,” akamaliza.

“…copy…” akajibiwa na ile simu ikakatika. Mipango ya kina ikapangwa na mwanamama huyu, akawaweka vijana wake katika hari ya mapambano, akawatia moyo na kuwaasa hili na lile.

- * *

“Karibu sana Kalebbe,” Zulekha akamkaribisha Amata huku akimsubiri ateremke katika boti ile.

“Asante sana, aaaaaaaaah nimefurahi kukanyaga kisiwa hiki,” Amata akajibu huku akiteremka taratibu wakati vijana wakiendelea kuifunga ile boti gatini. Kwa mwendo wa taratibu walitembea katika mchanga mweupe wa pwani ya kisiwa hicho na kufika kwenye kijumba kidogo tungekiita kibanda, lakini kilijengwa kwa unadhifu sana na kilionekana chenye thamani. Pembezoni palikuwa na nyumba nyingine nzuri tu lakini ilionekana haina watu. Yule mwanamke, akaweka kiganja chake cha mkono wa kulia katika kitu kama kioo kilichokuwa mlangoni hapo, kisha akasogeza zura yake, mwanga mwekundu ukapita kati ya macho yake, akatamka jina lake na kisha kubofya tarakimu fulani fulani, ule mlango ukafunguka, wakaingia wote wane, yaani yeye, Amata na vijana wawili na ule mlango ukajifunga nyuma yake.

Ngazi ndefu ilionekana kuteremka, wakaifuata na walipofika chini kama mita ishirini hivi, kulikuwa na njia pacha tatu. Zulekha akasimama na kumtazama Amata.

“Usiogope! Hii ni nyumba ya siri sana na ni watu wachache tu nje ya familia hii wanaopata fursa ya kuiona. Ila mtu wa kawaida akiiona na kuigundua basi huyo huwa hawezi kuishi,” akamwambia huku akimtazama. Amata akatikisa kichwa na kugeuka nyum,a akakutana machi na wale jamaa wawili walioshiba vyema.

“Ukienda kushoto, unaenda kwenye nyumba ya mzee, kulia unaenda kwenye idara ya usalama na sisi tunakwenda moja kwa moja,” akamwambia kisha akaongoza njia ile na Amata akamfuata.

Wakatokea kwenye jumba kubwa la kifahari, lenye kila samani inayostahili kuitwa ‘samani ya ndani’. Kamanda Amata aliitazama ile sebule ya kifahari, iliyozungukwa na kuta za aina yake huku upande mmoja kukiwa na ukuta wa kioo unaoruhusu kuona mandhari ya chini ya maji. Hakuweza kuamini kama katika nchi hii kuna watu wanaoishi kitajiri namna hii. Akatikisa kichwa huku akitazama tu na asijue wapi pa kuketisha makalio yake.

“Kinywaji tafadhali,” mwanadada mrembo mwenye asili ya Kihindi, wa kadiri ya miaka ishirini na tano hivi alimkaribisha kinywaji cha matunda kilichojaa kwenye bilauri.

“Asante sana mrembo … sharubati tu au kuna kingine?” akauliza huku akiwa kamshika mkono wake.

“Oh, sio hivyo, mgeni hawezi kuwa mwenyeji namna hiyo,” Zulekha alimwambia Amata huku akimwondoa yule binti katika himaya yake. Kamanda Amata bado alikuwa akishangaa mandhari safi ya jengo hilo hata akasahau kama ana kinywaji mkononi mwake.

“Huu ndiyo utukufu wa Premji Kanoon, nchi ndani ya nchi,” Zulekha akamwambia Amata huku akiichukua ile bilauri na kuitua mezani, akamkubatia kijana huyo kimahaba huku sura zao zikitazamana.

“Sasa jumba kama hili umewezaje kulijenga hapa?” Amata akauliza.

“Kawaida tu, mafundi kutoka Japan waliifanya kazi hii mchana na usiku baada ya kupata matatizo katika nyumba yetu ya Kerege,” Zulekha akaeleza.

“Mlpata matatizo Kerege?” Amata akauliza.

“Ndiyo!”

“We na nani?”

“Mi’ na mume wangu kipenzi Premji Kanoon, utamwona muda si mrefu kwani ametoka kwa kuwa kesho tunatarajia kuondoka,” Zulekha akajibu kwa ufasaha huku Amata akitikisa kichwa na saa yake ikifanya kazi ya kurekodi.

“Kwa nini mwataka kuondoka?”

“Watu wanataka kumuua mume wangu, na inaonekana ni watu wa serikali, hata swahiba wake aliyefanya mchakato wa kumuuzia kisiwa hiki amekamatwa majuzi tu, hii hali imekuwa mbaya kwake na kwangu pia kwa kuwa hana furaha, hata kitandani hanipi nitakacho…” mwanamke akafunguka na Amata akaendelea kusikiliza kwa utulivu maneno hayo.

Tungechelewa kidogo tu angetutoka kwa mara nyingine! Amata akawaza huku akimtazama mwanamke huyo usoni.

“Unaonekana ni kijana mtulivu, mdadisi, unayependa kujua mambo…”

“Na lingine umelisahau, napenda warembo kama wewe,” Amata akamalizia kusema.

“Warembo ni sumu, watakupeleka pabaya,” Zulekha akamwambia huku akiketi kitini, akawasha sigara yake na kuketi kwenye sofa kubwa la vono.

“Mr….. Spark! Pale Oceanic Breeze umefika lini?”

“Nimefika siku tano zilizopita,” akajibu.

“Spark una maswali kama mpelelezi,” Zulekha akazidi kusaili.

“Si nimekwambia kuwa mimi ni mwandishi wa habari,” akajibu jibu la uongo kabisa.

“Aaaaa! Hah! Hah! Hah! Hapo nitakubaliana na wewe, na nilishasahau kama umenambia …” akamtazama kwa kulegeza macho huku sigara aliyoibana katia ya kidole cha kati na shahada ikiendelea kufuka moshi, “… sasa Bagamoyo kuna habari gani iliyokuleta?” Zulekha aliketi sawia katika kaiti chake akimtazama kijana huyo.

“Inasemekana kuna ndege ndogo imepotea upande huu wa Bagamoyo hiyo sasa ndiyo iliyonileta kuandika hiyo juu ya hilo tukio,”

“Unashirikiana nani?”

“Mimi kama mwandishi wa kampuni ya kuitegemea, naiandika hiyo habari ya uchunguzi kwa ajili ya kuiuza kwa mashirika makubwa, niko peke yangu hapa kwani waandishi wangu wengine wana kazi nyingine za kufanya,” Amata akaeleza.

“Oh, good kazi nzuri sana,” Zulekha akamwambia Amata na wakati huohuo simu ya ukutani ikaita, akanyanyuka na kuiendea akaipokea.

“…Ndiyo, sasa hivi?… ok!” akaitazama saa kubwa ya ukutani ilikuwa ikimwambia kuwa muda huo ilikuwa ni saa kumi na moja jioni. Akarudi pale mezani na kumalizia kinywaji chake.

“Mume wangu karibu anaingia, unapenda kuungana nami kumlaki?” Zulekha akamwambia Amata.

“Yah, bila shaka,” akajibu.

**-

Wote wawili wakaongozana mpaka nje kwa upande wa pili wa kisiwa hicho, pale walikuta wanaume watatu weusi, wenye miili iliyoshiba, walionyoa ndevu zao kama Rick Ross, kutokana na ukimya wao naye hakuwasalimia, bali aliungana na Zulekha kutulia kusubiri.

Helkopta moja kubwa ya kifahari iliteremka taratibu katika pwani hiyo iliyojengwa kinamna, kisha ikazima injini yake, na utulivu ukarejea. Kamanda Amata akapachika miwani yake usoni si kwa sababu ya jua kali bali miwani hiyo ilikuwa ikipiga picha na kuzisafirisha kielektroniki kwenda kwa Chiba na timu yake. Mlango ukafunguliwa, mtu mnene kiasi, Muhindi, aliyevalia suti nyeusi ya bei mbaya, kwa mtazamo tu alionekana ni tajiri, akateremka pamoja na watu wengine wawili ambao moja kwa moja aliwatambua kwa kuwa ni watu wa juu serikalini. Pancho alipogongana macho na

Pancho akatamani kuanguka lakini akajikaza kisabuni. Alijua kuwa kijana huyo keishakufa hata alipopata taarifa ya ugeni wa dharula kutoka kwa mkewe hakudhania hata kama ni nani atakuwa amefika. Bahati mbaya sana kutokana na kikao cha siri na watu wake hakuweza hata kufungua kompyuta yake kuangali nini kinaendelea, labdal angeweza kuna yale aliyoyafanya na mkewe. Zulekha akamwendea na kumkumbatia kisha akambusu.

“Mgeni, nimekutana naye Ocean Breeze baada ya kupewa taarifa na mtu wetu, nimemkaribisha nyumbani kwa sababu najua utakuwa na aja ya kuzungumza naye kadiri ya lile alilokuja kufanya hapa Bagamoyo, anaitwa Mr. Spark,” Zulekha akatambulisha. Preji au Pancho akabaki kimya akaimwangalia mkewe na kisha Amata. Zulekha akageukia kwa Amata.

“Kutana na mume wangu mpenzi Mr. Premji Kanoon,” akamalizia. Pancho alikutana macho yake na yale ya Amata ambayo yalifichwa kwenye miwani ya rangi nyeusi, miwani iliyokuwa ikirekodi video matukio yote hayo ambayo yalikuwa yakitukia mbele yake.

“Karibu sana, jisikie nyumbani,” Pancho akamkaribisha Amata, pale alipotaka kupewa mkono alijifanya kutokuona akapita na kisha wengine wakafuatia nyuma yake. Kichwa cha Pancho kilianza kuchanganyikiwa kwa kumwona mtu huyo hatari kwa maisha yake akiwa hapo, hakuelewa kama Zulekha kamleta hapo kwa nia ya kuwa kamteka au ndiyo amelaghaiwa kwa mapenzi, lilikuwa swali lisilo na jibu. Baada ya milango miwili mitatu hivi akatokea kwenye sebule kubwa, akasimama kwa sekunde kadhaa kisha akawaambia watu wake.

“Naomba niacheni peke yangu kisha mniitie Zulekha nahitaji kupumzika kidogo,” Pancho akwaambia vijana wake na wale wageni, wakaondoka eneo lile.

- * *

Chiba akatikisa kichwa huku akiendelea kutazama kompyuta yake, iikuwa ni kama vile yeye ndiye kakutana uso kwa uso na mtu huyo.

“Vipi?” Madam akauliza.

“Amewasili kisiwani, na alikuwa na watu wengine wawili ambao nawajua fika! Njoo mwenyewe ushuhudie,” Chiba akamjibu Madam S huku akiirudisha nyuma ile picha na kumwnesha bosi wake. Madam S akatazama zie sura na kusikitika.

“Watu wanauza nchi kila kukicha!” akasema.

“Ndiyo hivyo!”

“Wamekwisha…” akamalizi huku akitoka pale mezani. Akawaita vijana wake na kuanza kuwapanga jinsi ya kuvamia kisiswa hicho, maana walijua kuchelewa kwao kungeweza kumweka pabaya Kamanda Amata. Njia iliyohafikiwa na wote ni kupiga mbizi na kisha kuangusha mziki katika kisiwa hicho.

- * *

Pancho alimtazama Zulekha kwa jicho kali, akameza mate ya hasira.

“Unamjua mgeni uliyemleta humu ndani ni nani?” akamuuliza.

“Ni mwandishi wa habari aliyevutiwa sana na hiki kisiwa hiki, ijapokuwa amekuja kwa kazi nyingine nikaona nimkaribishe kama fursa ya kujitangaza. Na ni wewe mwenye we uliniambia hayo,” Zulekha akajibu.

Kofi moja la kulia lilitua shavuni mwake akadondokea kitandani.

“Huna akili mwanamke! Huna akili kabisa, unaweza kuleta mashetani ndani ya nyumba hii, we hujiulizi kwa nini nyumba hii imejengwa chini ya ardhi?” Pancho akang’aka.

“Sasa mimi kosa langu nini?” Zulekha akaamka kitandani na kupiga kelele huku akiuliza, hasira zikamshika mishipa ikamtoka, “wewe mwenyewe ndiye uliyeniambia hayo leo hii unanigeuka? Nimepigiwa simu na Nassoro kijana wako mtiifu wa Ocean Breeze nikaenda na bahati nakutana na mtu huyu kwa nini nisimlete nyumbani ili aone kwa macho kila anachotaka, mara ngapi wewe umewaleta watu humu ndani na kunitambulisha kuwa ni watalii na wafanyabisahara? Hukuwahi kunambia kuwa hata mwili wangu niutumie kumkamata adui, sasa huyu nimekulea, awe adui au rafiki…”

“Naona unanipanda kichwani sasa, sivyo?” Pancho akachomoa bastola na kumwoneshea Zulekha.

“Nenda kwa huyo mgeni wako kamwulize yeye ni nani akwambie kisha uniletete jibu haraka!!!”

Zulekha akatoka chumbani na kumwacha mumewe akiwa kafura kwa hasira, alihisi kuchanganyikiwa kwani hakujua ni nini kinatokea, maana alilofanya ni lile ambalo mumewe ulitaka daima, lakini kwa nini amwadhibu kiasi hiki? Zulekha alihisi hasira kali sana dhidi ya mumewe, akapita kwenye korido ndefu na kuingia katika sebule kubwa ambako mwanzo aliketi na Amata, hakumkuta, isipokuwa kijana mmoja aliyekuwa akiangalia usalama wa eneo lile.

Kamanda Amata alikuwa kasimama mbele ya dirisha moja kubwa sana akitazama nje na shughuli mbalimbali zinazoendelea za wafanyakazi wa himaya hiyo.

“Mr. Spark!” akaita. Amata akageuka na kumwendea pale aliposimama, Zulekha hakusema lolote, akainua chupa ya whisky na kumimina kwenye bilauri iliyokuwa juu ya stuli na kumpa Amata kisha akainua nyingine na kujimiminia yeye, wakagonga chias na kila mmoja akapiga funda moja la nguvu. Lkitu ambacho alikigundua kwa mwanamke huyu ni kitu kama uvimbe katika shavu lake, akajua kwa vyovyote kuna jambo.

“Wewe ni nani?” Zulekha akauliza huku akionekana wazi sura yake kubadilika. Amata akapiga funda jingine na kumtazama mwanamke huyo wa Kihindi.

“Nimekwisha jitambulisha kwako ya kuwa mimi ni nani, bado unataka zaidi? Basi mwambie aliyekutuma akwambie mimi ni nani,” kisha akainyosha juu ile bilauri yake na kuinywa mfululizo, alipoitu kwenye stuli ilikuwa haina kitu. Akamtazama tena Zulekha pasi na kupapasa macho

“Naitwa, Amata, Kamanda Amata, Tanzania Secret Agency nambari moja; una lingine?” akamweleza mara tu baada ya kuiweka bilauri yake mezani. Na ni nukta hiyohiyo, alipojikuta amezungukwa na vijana wenye silaha kile upande. Aligeuka huku na huku na kukutana na sura zilizokunjamana kwa uchu wa kuua, Short Gun zilizosheheni risasi, zenye hamu ya kufyatuka.

“Mikono juu tafadhali,” akaamriwa na ye akatii.

Kijana mwingine akampekua na kutoa bastola mbili ndogo mifukoni mwake, visu vidogo vitatu na vitambulisho vingine vingine ikiwamo kadi za benki na kadhalika.

“Unaniambi wewe ni mwandishi wa habari kumbe ni mpelelezi?” Zulekha akamwuliza kisha akamnasa kofi na kusogea pembeni. Amata alivumilia maumivu huku akimtazama Zulekha kwa jicho baya sana.

Utalipa tu! Akajisemea moyoni. Pancho Panchilio akaingia sebuleni pale na kumkuta Amata akiwa chini ya ulinzi mkali.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Amataaaa, Kamanda Amata, leo umejileta mwenyewe kwenye nyumba ya shetani. Uroho wako wa mapenzi ya wanawake umekukamatisha, huna maana kabisa, nashindwa kujua kwa nini serikali ikakuamini hata kukupa hicho cheo wakati wewe ni mpumbavu kati ya wapumbavu wa nchi hii! Karibu sana Kalebbe, maana ulitaka kuja kupaona kama nilivyoelezwa na mke wangu Zulekha basi ngoja nikutembeze kidogo ili ufahamu mahali hapa,”

Pancho alimchukua Amata na kumtembeza katika jumba hilo huku vijana wake wakilinda msafara huo kwa bunduki nzito kila kona ya jengo. Kila kitengo alimwonesha bila kumficha na kumwelezea lakini hakumruhusu kuuliza swali, kil kitengo alikuta vijana wakifanya kazi kwa mori wa ajabu, wengi hawakuwa Waafrika, bali Wahindi na Waarabu, weusi walikuwa kwenye ulinzi tu. Katika chumba cha rada aliweza kuona kwa picha jinsi ndege yao ilivyolipuliwa.

“Aaaaa hah! hah! hah! Umeona, ninaweza kulipua ndege yoyote inayopita hapa, siogopi!” akajitapa kisha akaamuru watoke waende chumba cha mwisho. Baada ya kuzunguka ndani ya jengo lote hilo wakasimama mbele ya mlango mmoja wa chuma. Pancho akamtazama kijana huyu na kufungua kinywa chake kusema.

“Kamanda Amata, na sasa nataka nikuoneshe kitengo hiki ambacho kila anayeingia lazima achnganyikiwe ka teknolojia iliyofungwa ndani yake,” aliposema hayo akabofya kitufe fulani na lile lango likafunguka. Kilikuwa chumba tupu, hakukuwa na chochote ndani yake. Pancho akaingia.

“Karibu ushuhudie kilichomo, usiogope,” akamwambia. Kengele za hatari zikalia kichwani mwa Amata, akaingia ndani ya kile chumba kipweke, nyuma yake wakaingia vijana wawili walioshiba kimazoezi na wale wenye silaha wakabaki mlangoni. Kwenye maeneo kama haya huwa Amata hana subira zaidi ya kupigania uhai wake tu japo kwa sekunde ya mwisho. Alivuta hatua mbili mbele na kugeuka ghafla, akamchapa konde moja mmoja wa wale jamaa waliongia nyuma yake. Yule jamaa akayumba kidogo kwa kuwa hakutegemea dhopruba kama ile. Yule wa pili akaudaka mkono wa Amata lakini kabla hajafanya lolote, alipigwa kichwa kizito na kwenda chini. Kamanda Amata akaruka hewani na kutawanya miguu yake, akawachapa mateke makali kila mmoja akaenda chini bila kipingamizi. Wale wenye silaha wakashindwa wafanyeje, maana walijua kufyatua risasi kungeweza kujeruhi watu wao.

Alipotua chini Amata akaruka sarakasi ya chini kwa chini na guu lake likatua katika koromeo la mmoja wao, akaguna kwa uchungu. Alipojigeuza alijikuta anatazamana na mtutu wa Short Gun, akajizungusha na kumtia ngwala aliyeshika hiyo bunduki, akaenda chini huku bunduki ile ikimtoka mikononi, akaiwahi na kuikamata, bila huruma aliwatwanga wote wanne kwa kirasi na kuwaacha marehemu. Si mlangoni wala ndani ya kile chumba, hakukuwa na mtu.

Uko wapi mwanaharamu? akajiuliza na kuchungulia kupitia ule mlango, nakasikia watu wanaoongea wakija upande huo, akarudi ndani na kujificha nyuma ya mlango akisubiri huku mkononi mwake akiwa kaikamatia ile bunduki aliyoichukua kwa yule jamaa.

“Ni hapa jamani, ingieni kwa makini,” sauti moja ikasema. Wale waliokuja kama ni kuokoa jahazi walishuhudia damu na miili isiyo na uhai. Amata akaendelea kutulia palepale, wale jamaa wakamwingiza mmoja kama chambo, akaangaza angaza huku na huko akiziangalia maiti za wale jamaa watatu pale chini.

“Huyu jamaa hayupo bwana,” akawaambia wenzake.

“Basi msako uanze atakuwa humuhumu ndani, kumbuka hawezi kutoroka hapa ni kisiwani,” mwingine akahimiza huku wakitoka mle ndani na kupotelea huku na huko. Amata akatoka taratibu na kufuata korido moja kwa moja mpaka kwenye ile njia panda waliyopita na Zulekha wakati wakiingia kwenye jumba hilo. Akakunja kushoto na kuufikia mlango imara wa chuma, akajaribu kuufungua kwa kutumia zile namba alizozikariri pindi alipomwona Zulekha akifungua zikakubali lakini akadaiwa alama za vidole, akashindwa. Akatafakari cha kufanya akakosa jibu. Alipokuwa akijiandaa kubadilisha mbinu akasikia michakacho ya miguu ya mtu anayetembea haraka haraka huku akiongea.

“Kawaua wote, wote watatu, huyu jamaa hafai, inabidi auawawe,” yule mtu alionekana anaongea na kitu kama simu ya upepo. Amata akamvizia, alipotokezea tu eneo lile, akaruka na kutua shingoni mwake, akamkaba kabali namba sita.

“Tulia,” akamwambia. Ile redio pale chini ikawa inaendelea kuita,

“Jota! Jota! Umepatwa na nini?” sauti ya upande wa pii ikauliza. Kamanda Amata akaitazama ile redio na kuivuta kwa mguu wake.

“Fungua mlango!” akamwambia yule jamaa ambaye sasa alimfahamu kwa jina la Jota.

“Mi sijui, “ akajibu kwa shida kutokana na ile kabali aliyopigwa na Amata, akamwachia na kumsukumizia mlangoni.

“Fungua,” Amata alimwambia huku bunduki ikimtazama mtu huyo, akapapasa namba hii na ile na kuweka alama zake za vidole kisha macho, mlango ukafunguka. Kamanda Amata akamrukia teke la kusukuma yule jamaa akaangukia ndani, kisha yeye akafuata na kufyatua risasi zilizowaangusha watu wawili waliojitokeza na kumwacha mmoja tena wa kike akiwa kasimama.

“Kamanda Amata,” Zulekha akaita, “umeniharibia ndoa yangu,” akaongeza kusema.

“Nioneshe mumeo, serikali inamtafuta kwa udi na uvumba,” Amata akamwambia.

“Wewe ni mbaya sana sivyo nilivyofikiria,” Zulekha akaongea huku chozi likimtoka.

“Nilitaka nifike hapa, na nakushukuru kwa kunifikisha na sasa ninavyokwambia namhitaji mumeo, Pancho Panchilio na sio Premji Kanoon kama unavyomjua, gaidi anayehatarisha maisha ya nchi na wananchi, ametoroka mikono ya serikali kibabe, sasa siku zake zimekwisha. Nioneshe alipo kabla na wewe sijakumaliza,” Amata aliongea huku akiwa kakunja sura kwa hasira.

“Sasa mbona unakunja sura namna hiyo, kijana mzuri hatakiwi kujizeesha mwili wake,” Zulekha alisema hayo huku akimfuata taratibu.

“Tulia hivyohivyo kabla sijakuua kwa bastola yako mwenyewe,” sauti ikasikika kutoka nyuma yake. Kutokea katika dirisha kubwa lililokuwa mbele yake aliweza kuona taswira ya mtu yule vizuri sana. Amata hakuwa na muda wa kupoteza katika eneo hilo ambalo lingeyagharimu maisha yake muda wowote. Aligeuka na kumtandika yule jamaa kwa kitako cha bunduki, akaaangukia juu ya meza huku bastola ikimtoka mikononi, Amata akachumpa kwa ustadi na kuinyakuwa huku mkono mwingine akiwa tayari na saa yake ya mkono ambayo bwana huyo aliichukua pamoja na bastola. Yule bwana akaamka na kusimama wima huku mbele akimtazama Amata aliyekuwa akiibonya ile saa hapa na pale.

“Mnaweza kuja sasa, kazi imeanza,” akaongea huku akiitazama ile saa kisha akaivaa mkononi mwake. Yule mjinga akatumia muda huohuo, akaruka tik tak kwa minajiri kumpiga mikono na kidevu cha Amata lakini akakuta anapiga hewa kwani mwenzake alikwishaondoka eneo hilo na kutua upande mwingine mpaka kwa Zulekha aliyekuwa amebaki kaduwaa. Yule bwana alipotua na kukuta Amata hayupo, akajivuta kasi kumwendea, akaruka hewani akiitanguliza miguu yake mbele. Amata akaepa na kumpa pigo moja la karate mbavuni na kuvunja ubavu mmoja,

akajibwaga chini kama mzigo, alipojaribu kusimama alikutana na teke lingine katika ubavu wake wa pili, akaanguka chali na guu la Amata likatua kifuani mwake kwa kishindo.

“Aaaaaaiiiggghhh!!!” Yule jamaa akapiga yowe la maumivu huku akijaribu kwa nguvu zote kuuondoa mguu ule lakini alishindwa.

“Boss wako yuko wapi?” akamuuliza.

Akiwa katika kumuuliza akahisi kitu kizito kikikifikia kisogo chake, akageuka haraka na kutua upande wa pili wa yule mtu huku tayari mkononi bastola yake imetulia, alipocheza na kifyatulio, kijana mmoja aliyekuwa na chuma kizito mikononi mwake alijibwaga chini na kuwa marehemu. Amata akajishika kisogoni na kujifuta damu kutoka kwenye jeraha lililofanywa na pigo lile. Ilionekana mpigaji hakuwa mzoefu kwani angempata sawasawa basi lazima angepoteza fahamu lakini haikuwa hivyo. Amata akatazama alipkuwapo Zulekha katika ile sebule, hayupo, akatazama hapa na pale hasimwone.

Shit! Kaenda wapi huyu mwanamke? akajiuliza bila kupata jibu, akamgeukia tena yule jamaa.

“Hah !hah! hah! hah! Umecheza pata potea, leo nakumaliza kwa risasi yangu,” yule bwana akajigamba na kunyanyuka kwa taabu kutoka pale alipolala, wakati huo Amata bastola yeke ikiwa chini sakafuni, akaikanyaga kwa ncha ya mguu wake na kuibetua, ile bastola ikaruka hewani na Amata akaidaka kwa kono lake la kulia, sekunde hiyohiyo kifua cha yule jamaa kilitobolewa mara mbili na risasi za Amata, akarudi chini kwa kishindo.

“Buriani!” akamwambia.

Kamanda Amata akasikia sauti ya chopa, akatoka ndani ya chumba kile na kutafuta njia ya kutokea nje, ngumu. Alipofanikiwa kutoka ndani ya chumba kile akajikuta kwenye zile korido, huku na kule ving’ora vya hatari vilikuwa vikilia, kimenuka. Akakimbilia upande wa kushoto na kukutana na vijana waliovalia kijeshi na kujining’inizia silaha nzito, kabla hawajakaa sawa, akawafumua kwa risasi na kuwabwaga, akachukua shotgun walizokuwa nazo, akanyofoa na maguruneti mawili waliyokuwa nayo, akaendelea na safari. Moja ya milango mingi aliyoikuta hapo ni ule aliyokuwa anautaka. Akabonya kikengele na ule mlango ukafunguka, ndani yake kulikuwa na vijana wanne waliokuwa wamekaa kwenye luninga nne tofauti wakiongoza mitambo yote ya jengo hilo kuanzia rada, kamera za usalama na silaha zilizofungwa ardhini.

“Mtulie hivyo hivyo! Bosi wenu yuko wapi?” akawauliza huku akiondoa pini kwenye moja ya bomu la mkono (guruneti) alilokuwa nalo mkononi, wale jamaa wakatazamana na kukosa jibu.

“Najua ninyi mnafahamu, haya, mmoja baada ya mwingine, mniambie bosi wenu yuko wapi ama la, nateketeza chumba kizima na kwangu si hasara,” akawaambia tena huku akiwa amelishika lile bomu kwa mkono wake.

“Boss yupo na sasa anaondoka,” mmoja akajibu kwa kitetemeshi.

“Nioneshe alipo,” akamwambia na yule kijana akazungusha kitu fulani na kwenye luninga ya mbele yake kukaonekana helkopta iliyokwisha washa injini tayari kuondoka, rubani na watu wengine wawili walikuwa tayari ndani yake huku nje kukionekana watu kama watano wenye silaha wakiwa wameweka ulinzi.

“Umeshamkosa boss, anaondoka na mkewe,” kijana mwingine akaongea kwa nyodo wakati alipoona taa ya kuomba kufunguliwa mlango huo wa nje ikiwaka, akabonyeza kinobu cha kijani na kule nje ule mlango ukafunguka. Amata aliinua bunduki na kumfumua risasi ya mgongo.

“Aaaaaiiiiihhhhh umeniua mshenzi wewe,” yule bwana alilalama huku damu zikimvuja.

“Kufa tu, kwani we ulivyotaka kuniua kwenye ndege majuzi ulifikiri sikuoni,” akaiendea moja ya swichi kubwa iliyokuwa mezani hapo ambayo ambayo ilifanana na mkono wa gia ya gari, akabonyeza kitufe cha pembeni yake na runinga kubwa ikawaka mbele yake.

“Unataka kufanya nini wewe!” mmoja nakapiga kelele.

“Tulia mseng* wewe!” akamtuliza huku akimwonesha bastola. Kwenye kile kioo akaiona ile helkopta inayomsubiri Pancho na yeye na mke wake wakielekea kupanda tayari kuondoka.

“Hah! Hah! Hah! Hah! Haondoki mtu hapaaaaa!” akasema kwa sauti na kuitembeza ile ‘gia’ mpaka alipohakikisha ameiweka sawa ile helikopta.

Mlipuko mkubwa ukatokea, ile helkopta ikalipuka na kuteketea kabisa ikamwacha Pancho na akiwa hana ujanja, akarudishwa ndani na walinzi wake.

Kamanda Amata akabaki anashangaa kwani yeye bado alikuwa hajafanya ulipuzi ule.

- * *

Chiba na Gina waliibuka katika kichaka cha mikoko, kila mmoja akiwa na silaha yenye akili. Chiba akamwonesha Gina ishara ya kuwa afungue mlango, Gina akaweka begani bunduki kubwa na kuufumua mlango wa chuma uliokuwa hapo, kisha wakaelea huko huku wakimwaga risasi kila upande anapoonekana adui. Wakaingia ndani na kuanza kupita kila korido na mlango wakiwapa kipigo adui zao huku wakishinikiza wapi Pancho atapatikana. Kelele za vilio na mirindimo ya risasi viligubika mle ndani vikisindikizwa na moshi wa baruti. Gina akashusha barakoa yake na kuuficha uso wake dhidi ya moshi huo uliokuwa ukimuumiza macho, na Chiba akafanya vivyo hivyo.

“Tumsake mwanaharamu,” Chiba akamwambia Gina, wakaanza kubomoa mlango mmoja baada ya mwingine wakipekua ndani kote wasimwone.

- * *

Kamanda Amata alipotaka kuondoka ndani ya kile chumba aliona taa fulani ikiwaka kama ile ya kwanza, akaiendea na kutazama iliandikwa ‘Escape Chamber’ akajua kwa vyovyote Pancho yupo upande huo.

“Control room, Control room!” moja ya redio ndani ya chumba hicho iliita, Amata akainyakua.

“Control Room is under attack,” akajibu na kuhisi kigugumizi upande wa pili.

“We ni nani unayeongea?” ile sauti ikamuuliza.

“Mimi ni Kamanda Amata, TSA namba 1, na sasa niko njiani kuja hukohuko uliko,” akajibu na kuiweka mezani ile redio kisha akaliachia lile bomu na yeye kutoka kasi. Kilichotokea nyuma yake ni mlipuko ambao uliharibu mitambo yote ya lile jengo. Amata alitupwa mbali na kuanguka vibaya kutokana na nguvu ya ule mlipuko, akajiinua lakini mara hii alianza kusikia maumivu makali katika sehemu yake ya ubavu.

Akanyanyuka kwa taabu na kutembea huku akijitegemeza ukutani kwa mkono mmoja na mwingine akijishika ubavuni kwenye jeraha lake.

“Kamanda!” akasikia akiitwa nyuma yake alipogeuka akakutana na mtu aliyevaa barakoa usoni mwake lakini kwa mwendo tu alimgundua kuwa ni Gina.

“Gina!”

“Yap! Pole sana Kamanda, nikuondoe eneo hili,”

“No! no! itafute escape chamber ndipo alipo mtu wetu,” Kamanda akamwambia Gina, naye akainua walkie talkie yake akaongea na Chiba na kumpa ujumbe huo huku akimpa taarifa Scoba na Jasmine kuingia kazini. Haikupita muda waliungana na Chiba na kuufikia mlango huo, mlango wa chuma uliofungwa ukafungika.

“Watakuwepo hadi sasa? Maana hii ni ‘escape’” Chiba akaeleza.

“Nimeharibu system nahisi watakuwa humo ndani kwani kwa sasa hakuna mlango unaoweza kufunguka kirahisi,” Amata akawaeleza.

Gina akainua tena ule mbunduki na kuuweka begani, bonyezo moja tu, ule mlango ulifumuka vibaya, na Chiba akajitosa ndani muda huohuo, Gina akafuatia na Amata akawa wa mwisho, saka nikusake. Kilikuwa chumba kikubwa ambacho ndani yake kulikuwa na boti iendayo kasi, Amata alipoitazama akajua wazi kuwa ile boti kwa muundo wake ina uwezo wa kupita chini ya maji.

“Wapo humuhumu,” akawaeleza wenzake.

“Vaeni barakoa zenu!” Kamanda akawaambia na wote wakavaa.

“Gina,” akaita na kumpa ishara. Gina akainua bunduki moja fupi na kufyatua kitu kama bomu kilichotoa moshi mkali sana kisha wakaendelea kutazama hapa na pale. Haikupita muda wakasikia mtu akikohoa. Gina akawahi na kufungua mlango mdogo uliokuwa mahala hapo.

“Toka mwenyewe!” alimwambia Zulekha aliyekuwa kajificha hapo, “na mumeo yuko wapi?” akauliza.

“Ushasema mume wangu we wa nini?” akajibu huku akikohoa sana. Gina akageuza ile bunduki na kumpiga nayo shavuni, ikampeleka chini Zulekha, akamshika mguu na kumburuza mpaka karibu na mlango, Amata akamkanyaga mgongoni.

“Tulia mrembo, tulia hivyohivyo,” Amata akamwambia Zulekha.

- * *

Helkopta kubwa lenye magurudumu lilikanyaga ardhi ya kisiwa cha kalebbe, wa kwanza kuteremka alikuwa Madam S, akafuatiwa na Jasmine kila mmoja alikuwa na bastola kiunoni mwake. Dakika hiyohiyo, helkopta nyingine ya polisi nayo ikafika eneo hilo a kuteremsha vijana kama kumi hivi waliotimia, kikosi maalumu cha kupambana na ujambazi chini ya Kamanda Tossi. Wakazunguka eneo kwa uhodari kabisa wakihakikisha kila anayepatikana anawekwa chini ya ulinzi na kufungwa pingu.

Madam S na Jasmine waliingia ndani huku vijana wachache wa polisi wakiwasindikiza nyuma na mbele. Nje ikafika boti iendayo kasi ‘KINYAMKERA’ ikAteremsha vijana wengine wenye silaha wakifuatana na Inpekta Simbeye, idara imekamilika. Wale vijana wakaingia ndani na wengine wakabaki nje kama kawaida. Kwa mawasiliano yao waliweza kujua Gina, Chiba na Amata wako upande gani, wakaenda huko.

- * *

Kamanda Amata aliliangalia moja ya kabati kubwa katika chumba walichoingia mara hii, kabati hilo lilimtia wasiwasi kwa jisi lilivyokaa na mahala liliPowekwa, akaliendea na kulipapasa huku na kule, akashika kitasa na kujaribu kukivuta, hakuna mlango uliofunguka.

“We mwanamke eleza mumeo alipo kabla sijatumia nguvu,” akamwambia Zulekha.

Zulekha hakujibu isipokuwa mikono yake ilikuwa kinywani mwake kama mtu anayeshangaa jambo. Kwa hali hiyo Amata alijua wazi kuwa amtafutaye yupo eneo hilo. Juu ya kitasa kile kulikua na kitu kama jiwe la yaspi ili kuongeza nakshi ya kabati hilo, akaliminya lile jiwe na kabati zima likasogea kando, ndani yake kulikuwa na uwazi ambao bila kificho Pancho alionekana ndani yake. Kutoka ndani mle, akatoka kwa kasi kwa minajiri ya kumvamia Amata lakini kabla hajamfikia, alikutana na konde zito lililomfanya ateme damu, la pili lilitua shavuni na kuacha meno kadhaa sakafuni la tatu lilimpeleka chini mzima mzima.

“Mwanaharamu mkubwa wewe, leo nimekutia mkononi kwa mara ya mwisho,” Amata aliunguruma huku bado akijishika ubavu wake.

“Simama,” akamwamuru lakini Pancho hakufanya hivyo. Akasahau maumivu yake na kumnyanyua kisha akamsimamisha mbele yake na kumkwida shati, akampiga kichwa kimoja kizito mpaka Pancho akaona nyota za ajabu zikimzunguka.

“Wewe unaweza kutusumbua sisi?” akamwuliza.

“Mwacheee!” Zulekha akajirusha kumvamia Amata huku mkononi akiwa na kisu, hakuna aliyejua wapi kakipata kisu hicho lakini hata hivyo hakuna aliyekumbuka kumpekuwa pindi walipomkamata. Gina kwa wepesi wa ajabu, aliinua bastola lake na kumfumua Zulekha kabla hajaufikia mwili wa Amata na kumbwaga chini akiwa hana uhai.

“Kwaheri Malkia wa Kalebbe!” akasema kwa sauti ya chini huku akishusha mikono wenye bastola chini. Pancho akapagawa kwa kitendo hicho, akajitoa kwa Amata na kumfuata Gina.

“Umemuua mke wangu!” akapiga kelele.

“Na wewe nakuua,” Gina aliongea. Amata alipoitazama sura ya Gina aliona wazi hakuna mswalie Mtume, alijirusha na kumpiga teke la mbavu Pancho akajibwaga upande wa pili na risasi ya Gina akapita peupe na kukiteremsha kioo kikubwa kikubwa ambacho kiliyaruhusu maji ya bahari kuingia ndani, mshike mshike. Wakamnyanyua Pancho na kutoka naye ndani ya chumba kile wakikimbia.

Mvumo wa maji ulisikika dhahiri shahiri yakianza kujaa upande wa chini wa jingo hilo, Amata akiwa na Gina na Pancho aliyeshikwa huku na huku walijitahidi kupanda ngazi kwa haraka kuelekea upande wa juu. Kengele za kuashiri hatari zilisikika kila kona na kila aliye ndani ya jengo hilo alijitahidi kuwahi kutoka.

Madam S na Jasmine walikuwa wa kwanza kufika nje huku wakijaribu kuwasiliana na Amata na wengine. Haikupita muda, waliwaona wakitokea katika kile kibanda kidogo. Madam S akawahi na kumkamata Pancho huku vijana wa polisi wakimtia pingu tayari kwa safari.

“Umekamatika mwanaharamu!” Madam S alimwambia mbaya wake wakati akifungwa pingu.

“Peleka kwenye helkopta!” Madam akatoa amri.

“Hapana Madam! Hilo si wazo zuri,” Amata akajibu.

“Fanya uwezavyo Kamanda, hakikisha tunakutana karakana!” Madam akamwambia huku yeye na wengine wakielekea kwenye ile helikopta.

Pancho akaingizwa kwenye ile boti, akifuatana na Amata na Chiba wakaondoka na mtu wao kuelekea Dar es salaam. Boti ile iendayo kasi ilikuwa ikipita chini ya maji na haikuchukua muda kuwasili katika ofisi yao iliyo ndani ya meli mbovu maeneo ya Kurasini. Wakamshusha na kumuingiza ndani ya meli hiyo.

Pancho aliketishwa kwenye stuli ya chuma, huku Chiba na Amata wakisimama pembeni.

“Mtawafunga wengine lakini si mimi,” pancho aliwaambia vijana hao.

“hatutaki ngonjera zako, fala wewe!” Chiba akamuwahi

“Aliyekwambi sisi tunakufunga nani? Leo hii tunakuua,” Amata akajibu huku mkono wake bado ukiwa ubavuni mwake.

“Ha! Ha! Ha! Nani aliyekwambia mtu hufa kijinga hivyo?” Pancho akaongeza swali la kuuzi.

“Kama alivyokufa mkeo Zulekha kwa mkono wa mwanamke, na wewe utakufa hivyohivyo kwa mkono wa mwanamke,” Chiba akamwambia.

Mara mlango wa chumba hicho ukafunguliwa na Madam S akaingia pamoja na Inspekta Simbeye wakifuatana na Gina, Jasmine na Scoba. Madam S akamtazama Muhindi huyo kwa hasira.

“Chagua kifo chako haraka!” akamwambia.

“We Kibibi, kukukosa kule Kerege usikiri nimekusamehe, ninyi ni waharibifu wa mipango ya watu, nitakuua ndani ya dakika hii,” Pancho aliongea na sekunde hiyohiyo alijinyanyua kwa kasi na kuchomoa bastola ya Simbeye kwa kutumia mikono yake iliyofungwa pingu, akimpiga kikumbo cha maana inspekta huyo na kumwacha akienda kujibamiza mezani. Kabla watu hawajakaa vizuri alikwishamgeukia Madam S na kumnyooshea bastola hiyo.

Kamanda Amata na Chiba walijikuta wakipigwa butwaa kwa tukio hilo, wakiwa katika kujiandaa nini wafanye wakasikia bastola ikilalama.

“Pah! Pah! Pah!” kila mtu ndani ya chumba kile aliziba masikio na kuinama chini. Pancho alijikuta akitazamana na bastola ya Gina, alisukumwa na kujibamiza ukutani kisha alijibwaga ardhini huku kichwa na kifua chake vikiwa vimetobolewa vibaya kwa risasi.

Gina alaiteremsha mkono wenye bastola taratibu na kuurudisha mahala pake huku akitoa sonyo refu.

“Hakuna madhara, TSA 5 katekeleza wajibu wake wa leo,” Gina aliongea na ndipo watu walipotazama na kumwona msichana huyo akiwa anapumua kwa nguvu.

“Asante Gina, leo umefanya kazi yako hasa,” Madam S akamkumbatia Gina kisha wakatoka kuelekea mahala pengine.

- * *

Baada ya siku nne…

AFISI NDOGO

“Kazi iliyotuumiza kichwa imekamilika, kila mmoja wenu kafanya vizuri kwa upande wake, natoa pole kwa Amata kwa majeraha aliyopata lakini ndiyo kazi yetu,” Madam S aliongea akiwa kasimama wima mbele ya meza yake ambayo nyuma yake kulikuwa na bendera ya Taifa na ile beji kubwa ya TSA ukutani. Upande wa pili kulikuwa na vijana watano, wa kike wawili na wa kiume watatu, waliosimama kwa ukakamavu huku kila mmoja akiwa na beji yake ya kazi katika mkanda wake.

“Pongezi nyingi kutoka Baraza la Usalama la Taifa, Mheshimiwa Rais anawapa pongezi kwa kzi nzito ya kuhakikisha mtandao huu unapotezwa,” akawaambia.

“Mtakwenda likizo wawili wawili kwa muda wa wiki mbili kila mmoja. Wataanza Gina na Amata kisha Jasmin na Chiba, Scoba na mimi tutakuwa wa mwisho kwa sababu maalum. Lakini kumbukeni hii ni likizo kazini, muda wowote nikiwahitaji mtafika hapa”.

Gina akamtazama Amata na kutoa tabasamu. Baada ya Madam S kumaliza kauli yake, wakaketi na kupata vinywaji huku wakibadilishana mawazo ya hapa na pale juu ya kazi yao na kila mmoja akijaza fomu za likizo

.

HOTELI YA RED STAR

“Mmmmmm Kamanda Amata, you are so sweet!” Gina alilalama huku akimpapasa Amata kifuani.

“Nashukuru kwa kuniokoa,”

“Ndiyo kazi yangu kukulinda mpenzi, nisipokulinda mimi nani atafanya hilo?” Gina akaongea kwa sauti ya kivivu, “unazeeka Amata hata mtoto huna,” akaongeza.

“We unaye?”

“Mi umri bado!”

“Unataka kunizalia mmoja?”

“Sio mmoja tu, hata ishirini…” Gina akajibu.

“Ooooh Gina,” Kamanda akajiinua na kuitazama saa yake, ilikuwa saa nne asubuhi.

“Unaenda wapi?”

“Twende tukaoge,”

“Oh, no! bado Kamanda mi nataka tena,”

“Mmmmh beibi,”

“Mmmm nini, nipe cha asubuhi bwana,”

Kamanda akarudi kitandani na kuanza kumbusu Gina kimahaba huku wote wakiwa hivyohivyo bila nguo, mchezo ukaanza upya kama si kuendelea.

Mara simu ya mkononi ya Amata ikaanza kuita kwa fujo, mlio huo haukumpa tabu kujua ni nani anayepiga. Akaitazama kwenye kioo na kuona kuwa hakukosea. ‘Madam S’ iliandika.

MWISHO

Kitisho

1

Mbowe club saa 1:23 usiku

RADI kali ilipasua anga na kufanya mchoro wa kutisha, mwanga wake ulilipoteza giza kwa sekunde kadhaa, kila kilichojificha kilionekana wazi.

Hakuna mtu hata mmoja aliyekuwa nje muda huo. Ni mvua kubwa na ngurumo za kutisha zilitawala kila kona, ilikuwa ni hali ya kuogofya sana. Mifereji na mito ya dhalura ilianzishwa na maji ya mvua hiyo.

Kama ilivyo ada katika jiji la Dar es salaam, barabara zote zilikuwa zimejaa maji, kama ukiwa dereva mgeni basi hutoweza kujua ni wapi barabara ilipo. Sehemu kubwa ya mji hasa katikati ya jiji gari nyingi ziliegeshwa kando ya barabara kusubiri mvua iishe lakini haikuwa hivyo kwani mvua ilikazana zaidi ya saa nne.

Wakati hayo yote yakiendelea, ndani ya ukumbi mkubwa wa starehe unaojulikana kama 'Mbowe Club' watu hawakuwa wakijua kama nje kuna mvua, disco liliendelea kwa nguvu zote, watu walicheza, wakanywa na kuburudika. Katika kaunta kubwa ya ukumbi huo kulikuwapo walevi kadhaa ambao tayari walikwishabadilisha lugha ya mawasiliano kutoka Kiswahili na kuwa Kiingereza.

Gina binti Komba Zingazinga alikuwa ni miongozi mwa watu wachache waliokuiwa wamesaliwa na akili zao na utashi pia, alikuwa akinywa kinywaji chake taratibu huku jamaa mmoja akijitahidi kumzengea zengea lakini asifanikiwe. Kila wakati alionekana kuitazama saa yake aliyoivaa mkononi na aliposhusha mkono aliinua ule uliokamata ile bilauri yenye kiuno iliyojaa mvinyo kutoka Dodoma. Baada ya kupiga funda moja kasha la pili aliiteremsha taratibu na kuiweka juu ya mbao mwororo iliyoifunika na kuipendezesha kaunta ya ukumbi huo. Macho yake yalikuwa yakizunguka huku na kule yakitazama au kutafuta kitu ambacho hata yenyewe hayakukijua.

Upande wa pili wa ukumbi huo, kwenye sakafu iliyojengwa juu kidogo na ili uifikie itakulazimu kuzikwea ngazi kadhaa, kulikuwako watu watatu, wawili wanaume na mmoja mwanamke. Mwanaume mmoja alikuwa na tambo kubwa lililojaa kimazoezi, enzi za utoto wetu tungeweza kumwita Pawa, lakini enzi hizi wanamwita Baunsa, yote hayo ni mabadiliko ya nyakati. Watu wale watatu walikuwa wakiongea jambo Fulani na meza yao ilikuwa imechakazwa kwa pombe kalikali na sahani za nyama zilizokuwa zikipishana, vyote hivyo vilimiminwa katika matumbo hayo matatu. Ilikuwa ni vigumu kusikia nini wanachokiongea kutokana na muziki mkubwa uliokuwa ukipigwa ndani humo. Kati ya kaunta alipokuwapo Gina na ule upande kulitenganishwa na kundi la vijana waliokuwa wacheza muziki huo kwa mitindo mbalimbali. Gina alihakikisha hapotezi macho yake upande ule kwani mwili wake ulikuwa ukisisimka mara kwa mara na hiyo kwake ilikuwa ni ishara ya hatari.

Dakika chache baadae alimuona Yule mwanamke akiinuka na kutoka katika vile viti, akitembea kwa mwendo wa ki-levi levi. Akamtazama na kujua mara moja kuwa alikuwa anaelekea chooni, Gina akajikuta akishuka kutoka kwenye kiti kirefu alichokuwa amekalia, akaigugumia pombe yake yote kinywani mwake, kasha akavuta hatua fupifupi akikumbana na walevi na wacheza muziki akaelekea kule alikokwenda Yule mwanamke.

Halafu nitamwuliza nini? Akajiuliza pa si na kupata jibu. Lakini aliendelea kuvuta hatua kuelekea kule chooni, akapinda kona ya kwanza na kuingia kwenye milango Fulani iliyokuwa ikielekea huko atakako, mbele kidogo alimuona Yule mwanamke akiingia katika moja milango ya vyoo vile. Gina; mkono wa kulia ukiwa nyuma ya suruali yake ndani kidogo ya jaketi lake, sikwambii alishika kitu gani, aliuendea ule mlango, mara ghafla akaanza kuhisi kitu kikimfinya mkononi mwake, ilikuwa ni saa kubwa ya mkononi, saa yenye uwezo wa kupokea nukushi, kupiga picha za mjongeo na mnato, yenye uwezo wa kurekodi sauti na pia unaweza kuitumia kama simu. Akainua mkono na kubofya kitufe Fulani kasha akasubiri kidogo. Wakati akisubiri kijimkanda hicho chembamba kikitoka kwenye saa yake, Yule mwanamake bado alikuwa chooni.

Mama yuko mahututi Shamba, Tena Saan Aisee! Uikuwa ni ujumbe uliosomeaka hivyo katika kile kijimkanda. Akakikata na kukitia mfukoni mwake kisha akaanza safari ya kutoka ndani ya Klabu ile, akili yake ilikwisha sahau juu ya Yule mwanamke, akapita mlangoni na kukumbana kikumbo na Yule mwanaume mwenye tambo kubwa, akielekea kule choo cha wanawake, Gina akasukumwa pembeni; na Yule bwana akapita.

Nje ya Klabu hiyo ndipo alipokutana na mvua ya kutisha, akapachua kikofia katika ukosi wa jaketi lake na kukivaa kisha akaliendea gari lake, mita kadhaa kabla hajalifikia akapiga breki na kuacha kinywa wazi, hakuamini anachokiona. Vioo vyote vya gari yake vilikuwa vimevunjwa, tairi hazina upepo na ndani kulijaa maji ya mvua. Wameiba? Akajiuliza, kisha kwa mwendo wa tahadhari akasogea kwenye lile gari, juu ya kiti cha dereva kulikuwa na bahasha ngumu ya khaki, akatazama huku na kule, alipojihakikishia usalama akaingiza mkono kwa minajiri ya kuichukua ile bahasha ijapokuwa ilionekana kulowana.

Daraja la sarenda saa 1:55 usiku.

BMW nyeusi iliyokuwa iking'azwa kwa mwanga wa radi, ilshuka katika barabar hiyo ya Kenyata kwa kasi sana ikitokea maeneo ya Masaki. Ilipofika katika makutano ya barabar hiyo na ile ya Ally Hassan Mwinyi mkabala na Ubalozi wa Ufaransa iliingia barabara kubwa bila kungalia usalama huku ikirusha maji juu kutokana na mvua kubwa iliyokuwa ikinyesha usiku huo.

Madam S alikuwa katulia kwenye usukani akiiongoza gari hiyo ya Mwingereza kwa umahiri mkubwa. Akakunja ushoto na kukanyaga mafuta kueleka mjini. Ilikuwa ni tabu kuona mbele kutokana na wingi wa mvua, barabara imejaa maji, umeme umekatika, ilikuwa ni shida juu ya shida. Madam S hakujali alilikanyaga daraja la Salenda na kuendelea mbele, lakini kabla hajalimaliza, hamad, kulikuwa a mwili wa mwanadamu uliolala barabarani huku mikono yake ikiwa imefungwa nyuma. Akaiyumbisha gari kuukwepa mwili huo, gari ikasota na kukosa muelekeo, akarudisha

usukani kulia kuukwepa mwamba wa daraja, akaknyaga krachi na kuachia mafuta kasha akatoa gia ya tano na kushusha ya nne, kutahamaki gari yake ilikuwa ikihamia barabara ya pili, akakanyaga breki lakini ikashindwa kusimama, akaknyaga tena breki bado gari ilikuwa ikiendelea, ikapanda tuta lakutenga barabara, ikajipigia na kutua barabara ya pili, akili ikamrudia, akavuta breki ya mkono na ile BMW ikaserereka na kujizungusha.

Kishindo kikubwa kikasikika, BMW iligongana na Land Rover Defender, ikaangushwa pembeni. Madam S akajikuta kwenye pori la mikoko chini ya daraja la Salenda, akafyatua mkanda, akapiga kioo cha mbele kwa kukikanyaga kwa mguu, akatoka, akajipapasa na kukuta bastola zake zipo salama.

Damu zilizikuwa zikitiririka semu ya paji la uso juu kidogo ya jicho la kulia, wakati akijitahidi kusimama, radi kali ilipiga na kufanya mwanga mkubwa uliong'aza vichaka vyote, Madam S akaona mbele yake kama kivuli cha mtu aliyesimama nyuma yake. Akajua ni mawenge ya ajali tu, akageuka nyuma na mara ghafla akakutana na pigo la kitu kizito kilichotua katikati ya paji la uso, akayumba vibaya lakini mikono yake tayari ilikuwa imekwishachomoa bastola zake, kabla hajafyatua akafunikwa na gza nene lililomfanya ashindwe kuona chchote, akaanguka kama mzigo na bastola zikimtoka mikononi mwake.

Ofisi ya usalama wa taifa saa 2:00 usiku.

MAAFISA wa Idara ya Usalama wa Taifa walikuwa wakiendelea na shughuli zao kama kawaida usiku huo. Katika moja ya ofisi za jengo hilo, vijana wawili na msichana mmoja walikuwa bize kutazama luninga nyingi zilizowazunguka zinazoonesha maeneo mbalimbali muhimu ya Jiji la Dar es salaam. Kupitia luninga hizo waliweza kuona moja kwa moja kile kinachotokea kwenye maeneo hayo kama Uwanja wa ndege, Bandarini, Stesheni ya Treni, Uwanja wa Sabasaba, Makao makuu ya Rais na maeneo mengine mengi ambayo yamepewa umuhimu wa pekee kwa sababu hii au ile.

Avant, msichana mbichi wa miaka takribani thelathini hivi alikuwa katingwa kuangalia tukio la ajali iliyotokea daraja la Salenda, bado alikuwa anapata shida kujua hasa nini kinaendelea kutokana na ile picha kufichwa na mvua ilikua ikinyesha eneo hilo lakini kila ilipokuwa radi ikipiga ndipo alipoweza kuona kitu, baada ya dakika kadhaa alipuuza na kuendelea kutazama maeneo mengine.

Mubah akajikohoza kidogo na kumgutusha Avanti kutoka pale alipokuwa akitazama.

"Si ukapime, au Mama yako anajua?" Avanti akamtania Mubah.

"Unanianza we mrembo, mi nasubiri time hapa niingie viwanja!" Mubah akajibu, huku akitoka kwenye kiti chake na kukiendea kile alichoketi Avant, akasimama nyuma yake, machoye akiwa kayakaza kwenye ile luninga.

"Shiit! Avant, nini hicho?" akauliza huku akisogea jirani zaidi.

"Ajali, imetokea kama dakika kumi hivi," Avant akajibu.

"Kwa nini usipige simu polisi wawahi kama kuna chochote cha kuokoa?" Mubah akahoji.

"Sasa Mubah, Salenda pale kituo kipo jirani wataenda tu," akaeleza huku akimtazama Mubah usoni.

"Yaani wewe! Kitendo cha kuitega kamera pale hatukufanya kwa makosa, lile ni eneo nyeti sana, kama ni ajali lazima polisi wafike mapema ili kuondoa kilichopo, pale vipngozi asilimia 99 wanapita, ikiwa hujuma utalaumiwa wewe kwani ndio eneo lako la kutazama leo!" Mubah akalalamika huku akiliendea kabati dogo lililo hapo jirani.

Avant akainua simu na kubofya tarakimu Fulani Fulani kasha akatoa taarifa hiyo kituo cha polisi cha Salenda. Haikupita dakika tano tayari kupitia luninga yake aliweza kuona gari na nyendo za polisi eneo hilo bila kujali mvua iliyopo. Avant aliendelea kutazama huku akigonga gonga karamu yake.

§§§§§

Gina alivuta hatua na kuingia katika lango kuu la Ofisi Nyeti, Shamba, akabofya namba zake za siri, kasha akaweka kiganja chake juu ya kioo Fulani kilichopo mlangoni na baada ya hapo akafanya kama anachungulia, kijimwanga chekunfu kikapita kati ya macho yake na kitasa cha ule mlango kikafyatuka, akaufungua na kuingia ndani. Moja kwa moja akaingia chumba Fulani na kuvua jaketi alilovaa, akabadilisha nguo na kurudi katika hali ya ukavu, akatoka na kutembea mwendo mfupi kabla hajagonga mlango Fulani kwa mtindo wa pekee na mlango ule ukafunguliwa.

“Karibu Gina!” Dkt Jasmine akamkaribisha na nukta chache baadae akampatia kikombe cha kahawa.

“Hawajafika?” Gina akauliza.

“Hapana, we ndiye wa kwanza, leo sijui kuna nini, labda kwa sababu ya mvua,” Dkt. Jasmin akaeleza.

Gina akashusha pumzi ndefu, mazungumzo mengine yakaendelea huku wakiwasubiri wengine, kila mara walikuwa wakitazama saa zao, hakuna simu wa taarifa yoyote iliyokuwa ikifika katika nyumba hiyo, Gina na Jasmine wakaanza kupata wasiwasi. Jasmine akainua uso na kuitazama saa kubwa ya ukutani, ikamwonesha kuwa ni saa 3:15 usiku.

“Hapana Gina, hii sio kawaida, tuanze kuwatafuta mmoja baada ya mwingine,” Dkt. Jasmin akamweleza Gina, kasha wote wawili wakaenda kwenye chumba maalumu cha mawasiliano, ndani ya chumba hicho ambamo ndiyo ofisi ya kudumu ya Chiba wa Chiba kulijawa na makompyuta na luninga nyingi huku na kule, simu za upepo, za kawaida na zile za satellite zilikuwepo. Kila kitu kilikuwa kinafanya kazi kwani haikuruhusiwa kuzima chochote labda tu kama kuna matengenezo, kila mmoja akaketi katika kiti chake na kuanza kucheza na simu zao za siri zilizounganishwa moja kwa moja.

Hakuna simu ya mkononi iliyokuwa ikipatikana si ya Madam S wala ya nani, walipigwa na butwaa na kubwa simu za nyumbani zote zilikuwa zikiita bila kukoma hazikupokelewa. Gina akamgeukia Dkt. Jasmine.

“Oya Shost, hapa ni mguu kwa mguu nyumba moja baada ya nyingine tukapate kujua kilichojiri,” Gina akamwambia Jasmine kasha wote wakaingia vyumbani na walipotoka walikuwa katika mavazi ya kazi, kila moja alibeba silaha anazoamini zingemfaa usiku huo kwani hawakujua hatari itakayowakabili. Wakiwa katika harakati hizo ndipo Gina alipokumbuka ile bahasha.

“Nisubiri Jasmine!” akarudi kwenye kile chumba akaichukua ile bahasha, bado ilikuwa imelowa akaichana taratibu na kuitoa karatasi ya ndani kwa uangalifu.

“Nini Gina?” Jasmine akauliza.

“Hii bahasha niliiokota kwenye ari yangu lakini sikuwahi kuifungua ndani,” akamjibu.

Gina alibaki kakodoa macho baada ya kukutana na kichwa cha habari kikubwa kilichosomeka ‘KITISHO!’ kisha chini yake kuliandikwa sentensi moja tu

Mwisho wa zama zenu umefika, mtaongea na Mzee Ngurumo.

Maneno hayo yalizigonga kwa nguvu nyoyo za wadada hawa, wakabaki wakitazamana, wkageuza macho yao wakaitazama tena ile karatasi.

“Gina!” Jasmine akaita.

“Jasmine!” naye akaitikia na wote wakatoka na kuingia kwenye gari ya Jasmine na kuondoka eneo hilo.

§§§§§§

Kerege – bagamoyo saa 4:07 usiku

TOYOTA Hilux Double Cabins, iliingia taratibu getini na kuegeshwa karibu na bustani ya maua iliyotengenezwa ndani ya ngome kubwa iliyobeba jengo la kifahari kuliko fahari yenyewe. Walinzi kadhaa walionekana kwenye kona zake, hawakushughulika kabisa na gari hiyo bali kila mmoja alishika lindo lake.

Dereva akashuka na watu wengine kama watatu hivi wakashuka, wakazunguka nyuma na kufungua funiko kubwa la alluminium lililotengenezwa ili kufunika mzigo uliopo ndani yake.

“Washushe hao, kisha wapeleke Kuzimu,” mmoja wa wale vijana aliyekuwa ameketi mbele akawaagiza wenzake kasha yeye akazikwea ngazi kulielekea jengo hilo lililoendezeshwa kwa taa zenye marembo mbalimbali.

Sauti za viatu vyenye kisigino kigumu zilisikika zikitembea lakini aliyevaa hakuonekana, Bwana Mpaya alibaki kusimama na kutazama kule sauti ile ilikokuwa ikitokea na asione mtu zaidi ya giza lililomlaki isipokuwa aliposimama yeye mwanga ulikuwapo na kufaya nuru ya kupendeza. Kasha ukimya ukatawala na sauti nzito ikalipenya lile giza.

“Ndio Bwana Mpaya, karibu sana, natumaini umekamilisha nililokutuma, sivyo?” alikuwa ni Pancho Panchilio aliyeyafikia masikio ya Mpaya aliyekuwa amesimama katikati ya sebule pana lakini asimwone anayeongea naye, isipokuwa sauti tu.

“Ndiyo Boss, tumewaleta lakini hali zao ni mbaya sana,” akaeleza.

“Vizuri sana, nani na nani mmempata?” akauliza tena.

“Tumempata Boss wao na Mtaalamu wao wa kompyuta,” akajibu.

“Ha! ha! ha! ha! ha!” akacheka cheko la pesa.

“Ok, wape vijana posho yao kama nilivyokwambia kisha unitafutie kichwa cha Kamanda Amata, huyu hasa ndiye mwiba kwangu, nataka apotee kwenye uso wa nchi ili binadamu tule vizuri, kuna pesa ndefu sana nimeiandaa mkilikamilisha hili,” Pancho akiwa mafichoni mwake akakohoa kidogo wakati Mpaya alikuwa akitoka, “Sikia Mpaya, hakikisha ukimuua Kamanda Amata, mkate kichwa, kisha kiwiliwili mkichome moto na kichwa mniletee, mbwa wangu hawajala nyama siku nyingi sana, maana Yule ni shetani anaweza kujiunganisha tena halafu akaangusha balaa, kwa heri!”

Alipomaliza kusema hayo na taa ndani ya jengo lile zikazimika.

2

KAMANDA Amata akaitazama gari yake aia ya Subaru Forester jinsi ilivyochakazwa kwa risasi, akashusha pumzi ndefu.

Wadude hawa wangeniua! Akajisemea moyoni huku akijaribu kuiwasha nayo ikawaka, akairudisha barabarani na kushika njia ya kwenda mjini, alijipapasa mifukoni hakuiona simu yake, wala saa yake mkononi haikuwepo. Any way! Akajipa moyo. Huku akiendelea kuutafuta mji wa Dar es salaam, saa ya ndani katika gari yake ilimwonesha kuwa ni saa tano za usiku.

Gina sijui kama atanielewa, maana tulikubaliana saa moja na robo, labda nitamkuta! Akaendelea kuongea na nafsi yake, huku akiiacha Gongo la Mboto na kuitafuta Uwanja wa Ndege. Katikati ya safari yake akafungua redio ndani ya gari na kusikiliza kinachoendelea. Ilikuwa ni kituo kimoja cha redio binafsi kikirusha habari hiyo ya dharula iliyoyanasa masikio ya Amata usiku huo.

…Mwili wa Mheshimiwa huyo umekutwa sakafuni bila uhai na kitu kama matundu ya risasi yakionekana kifuani mwake. Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wake ili kuwakama waliohusika na mauaji hayo…

Amata akakanyaga breki kali na kuitoa gari barabarani kwani taarifa hiyo haikujitosheleza kwake, akaegesha gari pembeni na kutazama huku na kule hakuona mtu kupita eneo hilo, pembeni yake kulikuwa na bar iliyokuwa ikiendelea kuburudisha watu kwa vinywaji na vilaji, akashuka na kuiendea, alipofika tu akakutana na mwanadada mrembo aliyevalia nguo nyeupe juu na sketi nyeusi chini.

“Karibu kaka, karibu kiti,” Yule dada akamkaribisha Amata huku akifuta meza iliyokuwa hapo. Ijapokua haikuwa nia ya Kamanda kuketi, akajikuta amefanya hivyo, “Pole!” neon hilo likaupasua moyo wa Amata akamtazama Yule dada Mhudumu wa bar.

“Pole ya nini?” akauliza

“Una damu kichwani,” akamwambia.

“Shiit!” akang’aka na kujigusa, kweli akahisi maumivu na kitu kama jeraha.

“Asante sana!” akamjibu, “Unaweza kunisaidia simu yako?” akamwuliza.

“Haina salio lakini, halafu ni kisimu cha tochi,” akajibu kwa aibu.

“Naomba hivyo hivyo.”

Yule mwanadada akachomoa simu yake akampatia Amata. Ilikuwa ni simu iliyochakaa, iliyoonekana kupita katika mikono mingi ya watu mpaka kuifikia mikono hii ya huyu Mhudumu wa baa. Ilifungwa kwa mipira ya manati, betri lake lilishikiliwa na kipande cha mpira wa manati. Hakujali, aliitazama vyema kasha akaanza kubofya hapa na pale.

“Haina vocha hiyo!” Yule Mhudumu akaeleza tena.

“Usijali, kaniletee Bia baridi sana bila glass tafadhali,” Kamanda akamwagiza Yule dada lakini alilotaka yeye haikuwa bia ila zile dakika mbili za kubaki peke yake. Vidole vyake vikaanza kutomasa tarakimu Fulani Fulani na alipomaliza, akapumzika, wakati huo bia yake ilikuwa imefika, akaigusa, akamwonesha Yule Mhudumu alama ya dole gumba, kisha akabaki na hamsini zake.

Meseji iliyofuata katika simu hiyo ilikuwa ni kutoka katika kampuni moja ya simu nchini, Kamanda Amata alikuwa amechukua muda wa hewani kwa namna yao ya siri na sasa simu ile Kimeo ilipata uhai.

Akaanza kupiga namba za maswahiba wake wa kazi, Chiba; simu haikuita kabisa, Madam S vivyo hivyo, akaduwaa wa sekunde kadhaa, haikuwa kawaida kwa watu hao kuwakosa kwenye simu, akili ya Kamanda ikiruka chogo chemba. Mbele yake kulikuwa na luninga kubwa iliyokuwa ikionesha matukio mbalimbali ya Kitaifa na lile lililomvutia ni ajali ya Salenda, alisahau kupiga simu na kutazama tukio lile. Kamanda Amata alikaza jicho kutazama picha hizo lakini hakuzitilia maanani kwani wakati wa mvua ajali kama hizo ni za kawaida sana.

“Kaka hadi bia imepoa!” Yule Mhudumu alipita tena kwenye ile mea aliyokaa Amata.

“Oh, sorry,” akamjibu kasha akainua chupa na kujijiminia mafunda kadhaa, alipoishusha ilikuwa nusu tu.

Akaitazama tena ile simu akabofya tarakimu nyingine, akaweka sikioni, simu ikaita na kuita haikupokelewa kama ilivyokuwa kwa simu za nyumbani za Chiba na Madam S, akashusha pumzi. Nini kinaendelea? Akajiuliza. Akarudia kuipiga namba ya mwisho, akaweka simu sikioni, baada ya dakika moja ile simu ikakwapuliwa na sauti nyororo ya kike ikasikika tofauti na alivyotegemea.

"…Polisi Kituo cha Kati, nikusaidie nini?" ile sauti ikauliza.

"Mwenye Ofisi, Inspekta Simbeye yupo?" Kamanda akauliza.

"…Inspekta leo alitoka kama mida ya saa tisa alasiri, hajarudi bado…" Yule mwanadada akajibu.

"Alisema kuwa atarudi au aliacha maagizo yoyote?" Kamanda akauliza.

"…alisema tu kuwa angerudi kabla ya saa kumi na ni kawaida yake kutoka saa tisa na kurudi saa kumi kila siku, lakini leo mpaka sasa hajarudi…" sauti ile iliendelea kueleza.

"We umeingia kazini saa ngapi?" akamwuliza.

"…nimeingia saa nane nitatoka saa nne usiku… samahani lakini naogea na nani?" Yule mwanadada alipouliza hivyo simu ikakatika.

Ndipo Kamanda alipojikuta hayuko peke yake mezani, mbele yake kulikuwa na mwanamke mmoja aliyevaa vazi refu jeusi, hijab na kujificha uso wote isipokuwa macho. Kamanda Amata akamtazama mtu huyo kwa tuo, akainua chupa yake na kupiga funda la mwisho, alipoishusha ilikuwa haina kitu ndani.

"Kwa nini unapenda kudhalilisha dini ya watu? Unaingia baa na vazi kama hilo?" Kamanda akaanza uchokozi, lakini Yule mtu hakujibu kitu, alikuwa akimwangalia tu. Jinni au! Akajiwazia, kabaridi ka haja kakapita kutoka utosini mpaka unyayoni.

§§§§§§

GINA aliegesha gari mita mia mbili hivi kutoka katika lango la kuingilia nyumba ya Madam S kule Masaki, akateremka na Jasmine akafanya vivyo hivyo, kisha wote wawili wakarudi taratibu wakiachina nafasi ya mita kadhaa katikati.

Lango la mbele lilikuwa limefungwa, Gina alitazama huku na huko hakuona hata dalili ya binadamu kupita myaa ule, isipokuwa manyunyu tu ya mvua yalikuwa yakimnyurunyuta mwilini mwake. Akajipapasa katika kiuno cha suruali yake na kufatua kijipini chenye ncha mbili zilizojikunja kwa mtindo wa pekee, kishapo akachukua kipini kingne kutoka kwenye kibanio cha nywele zake, akatanguliza kile chenye ncha mbili katika tundu la funguo ya lango hilo, akachukua kile cha tatu na kukitumbukiza kati, akafanya manuva kidogo tu, kitasa kutoka Uingereza kikafyatuka na kuuruhusu lango lile kuwa wazi.

Skunde mbili zikapita, ya tatu na ya nne bila Gina kuingia ndani ya wigo ule mkubwa, akatazama tena usalama, bado barabara ilikuwa tupu, hakumuona Jasmine, moja kwa moja akajua kuwa kwa vyovyote keshajiweka katika kona maalum ya kumlinda swahiba wake. Akaingia ndani ya wigo huku bastola yake aina ya Winchester ikiwa mkononi. Akatembea kwa hadhari kubwa huku na huko akitazama hakuona mtu. Hatua tatu kuelekea mlango wa nyumba hiyo, ndipo alipoona kitu kilichomshtua sana, akasimama mapigo ya moyo yakimwendea kasi kifuai mwake.

Mbele yake kulikuwa na mwili wa Binadamu uliolala chali ukiitupa mikono yake huku na huko, hakuwa na uhai. Gina akajiweka tayari kwani aliona huo unaweza kuwa mtego kwake, akatazama jumba la Madam S, taa za ndani zilikuwa zikiwaka kwa mwanga wa kupendeza, ina akajikuta anaishiwa nguvu, akainua mkono wake na kuizungusha saa yake kwa namna ya pekee kasha akaisogeza karibu na kinywa chake.

"…Jasmine …" akaita, hakupata jibu, akazidi kuingiwa na wasiwasi. Dina akatulia pembeni ya ule mwili, akahisi kama kuna mtu anayekuja nyuma yake, akakamata bastola yake barabara, liwalo na liwe, akageuka ghafla tayari kwa shambulizi, hakuna mtu.

Shiit! Akajisemea. Akauruka ule mwili na kuufikia mlango wa nyumba ile kubwa, akatoa gloves mfukoni na kuivaa, kisha akashika kitasa kwa mkono wa kushoto uliokuwa na gloves akaingia ndani ya sebule pana, iliyomlaki bila hiana. Kila kitu kilikuwa katika utulivu wa hali ya juu sana, hakukuonekana kama kulikuwa na purukushani yoyote ndani ya nyumba hiyo, akajivuta kuelekea chumba cha Madam S, akaufikia mlango na kuujaribu, ulikuwa umefungwa. Akatumia hila ileile na kuufungua. Hata chumbani kulikuwa tulivu kabisa, hakukuwa na ishara yoyote iliyoonesha kama kulikuwa na pambano la kufa na kupona.

Akaenda pembeni mwa kitanda upande wa kichwani, akachuchumaa na kubonya vijinamba Fulani vya kificho ambavyo kwa mtu wa kawaida huwezi kuvigungua mpaka mmiliki akuoneshe. Droo moja ikafunguka na ndani yake ikajifunua kompyuta kubwa ika simama mbele yake, Gina akatikisa kichwa juu chini, kwani alijua kama hiyo kompyuta haipo mahala pake basi hali ya Taifa iko hatarini. Alikumbuka maneno ya Madam S siku alipomkaribisha nyumbani kwake kwa mara ya kwanza.

….heri mimi nife lakini hii kompyuta ibaki. Nikifa au nikipotea kabla hamjatangaza kifo change hakikisheni mnang'oa kompyuta hii na kuikimbiza Shamba kisha mtangaze matanga. Siri yote ya Taifa hili ipo hapa, mipango yote mibaya na mizuri ipo humu, watu wote wabaya na wazuri wapo humu…

Gina alijikuta analia machozi peke yake, nifanyeje, niondoke nayo? Akajiuliza, nitaifikisha Shamba salama? Akajiuliza bila majibu. Gina alijikuta kachanganyikiwa, hajui la kufanya, aichukue au aiache, kichwani mwake alielewa kuichukua kompyuta hiyo ina maana kuwa Madam S kafa au katoweka, na je kama kuna wanaotaka na wameshindwa kuipata hatoweza kuwa kawarahisishia kazi?

Ulikuwa ni mgongano mkubwa wa mawazo kati ya roho, moyo na ubongo wake, akaamua kuiacha. Akabofya tena zile tarakimu na ile kompyuta ikajirudisha ndani taratibu na kujigia mahala pake. Gina akashusha pumzi ndefu, akaitazama bastola yake na kunyayuka taratibu, akaufuata mlango na kutoka akiufunga nyuma yake.

KAWE – saa 4:02 usiku

LAND CRUISER ya polisi ilikuwa nje ya lango kubwa la nyumba ya Mheshimiwa Mbunge wa jimbo la Miroroso, wananchi wasio na dogo nao walijumuika nje ya nyumba hiyo wakikodoa kodoa macho kushangaa tukio hilo lisilo la kawaida. Hakuna aliyejali mvua ya rasharasha iliyokuwa ikiendelea kunyesha, watu walijikusanya kwa kujikunyata kutazama.

Ndani ya jumba hilo kulikuwa na Polisi waliovaa kiraia wenye bunduki kubwa kubwa wakiwa wanatembea hapa na pale, mwili wa marehemu Mbunge ulikuwa ndani ya chumba chake cha kulala. Polisi waliokuwa huko chumbani wakifanya taratibu zao za uchunguzi walikuwa wamekamilisha kazi yao, walitoka sebuleni na kuwapisha vijana wachache kutoka idara ya dharula ya kampuni binafsi ambayo husambaza gari za wagonjwa mitaani kwa minajiri ya kusaidia hali za dharula kama hizo.

Waliufunga sawia mwili wa Mheshimiwa katika mfuko maalumu na kuupakia kwenye machela yenye magurudumu, kasha wakaisukuma kuelekea kwenye gari yao iliyokuwa imeegeshwa pembeni tu mwa jumba hilo. Vilio vilisikika, wananchi wakalia na kuomboleza, walimpenda Mheshimiwa, ijapokuwa alipojenga jumba lake haikuwa jimboni mwake lakini bado alitoa misaada ya hali na mali kwa waliomzunguka.

"Alikuwa shujaa, kwa vyovyote wametumwa kumuua," mwombolezaji mmoja alisikika akisema huku akifuta machozi yake.

Baada ya zoezi hilo ndipo Wananchi waliruhusiwa kuingia ndani na kuanza msiba huo. Hakuna aliyeamini kabisa juu ya lililotokea.

Lakini ilibaki hivyo kuwa Mbunge wa jimbo la Miroroso aliuawa na watu wasiojulikana.

§§§§§§

Kamanda Amata aliwekwa kati ya watu wawili huku mmoja na huku mwingine, mbele yake kulikuwa na mwingine tena ukiacha dereva aliyekuwa akiongoza gari hiyo. Wote walivaa maguo yaliyowaficha miili na sura zao. Hakuna aliyeongea; ile gari ilipita daraja la Salenda na kufuata uelekeo wa kwenda Mwenge, baada tu ya kupita daraja hilo, ikakunja kulia na kufuata ile Kenyata Drive, ilipomaliza maofisi ya Mabalozi iliiacha ile ya kwenda Coco Beach na kukunja kushoto, nyumba ya nne mbele ikasimama.

"Usilete makeke yako ya kipumbavu, tunataka kompyuta anayotumia boss wako basi," akaambiwa na kuteremshwa chini, wakauendea mlango mkubwa na kuufungua, Kamanda Amata akatangulia mbele na wale jamaa wakamfuata nyuma, wote watatu walkuwa na Shot Gun mikononi mwao.

Wakatembea taratibu na kuipita ile maiti pale nje, moja kwa moja wakaingia ndani ya sebule, mmoja wao akasimama nje ya mlango wa sebule kuweka usalama, mwingine akabaki sebuleni na wa mwisho akaenda na Amata mpaka chumba cha Madam S.

“Usilete ujanja wako, tunajua kuwa ni wewe tu unayeweza kuitoa hiyo kompyuta hapo, haya fanya hivyo,” akamwambia huku akiwa kasimama umbali wa mita kama mbili hivi. Kamanda Amata akaiendea ile droo na kuingza mkono wake mahala Fulani, akapapasa anavyojua yeye, mara ile droo ikajivuta mbele na kufunguka, hakuna kompyuta! Yule mjinga akabaki katoa macho, akashangaa mahala pale hakuna kompyuta waliyokuwa wanaitaka ilhali wao walikuwa na uhakika kuwa ipo hapo baada ya kufanya uchunguzi wa kina.

“Haipo?” akauliza.

“Si unaona mwenyewe haipo!” Kamanda akajibu.

“Imeenda wapi?” akarusha swali la kijinga.

“Mimi na wewe tumeingia pamoja sasa nitajuaje ilipokwenda?” Kamanda akajibu kwa swali. Kama kuna kosa alilolifanya Yule mtekaji na atalijutia kuzimu ni ktendo cha kwenda kuhakikisha kwa macho kuwa Kompyuta ile haipo pale. Kamanda Amata kama umeme, kutoka pale alipokuwa amechuchumaa kuitoa ile Kompyuta, alijikunjua na kutawanya miguu yake sentimeta mbili kutoka usawa wa sakafu, Yule mjinga alipigwa ngwala kutoka upande wa nyuma na kujibwaga akitanguliza kisogo, yowe na kishindo vilimshtua Yule wa sebuleni akaja kwa kasi. Kamanda Amata alijirusha upande wa pili wa chumba na risasi zilizotoka katika bunduki ya Yule mtu wa pili zikachimba sakafu.

Kabla Yule bwana hajajiweka sawa, mwendo wa sekunde moja tu aliyoitumia kufanya shabaha ya pili dhidi ya Kamanda Amata, alijikuta akipaishwa juu na kujibwaga kama mzigo sakafuni tayari damu ilikuwa ikimtoka kama bomba. Amata alishuhudia hilo kwa haraka sana hakuelewa nini kinatokea.

Wamegeukana? Akajiuliza.

“Upo salama Kamanda Jitokeze!” sauti ya Gina ilimrudishia matuamaini. Kamanda Amata akajitokeza mzima mzima, lo! Domo la shot gun lilikuwa likimtazama umbali wa mita tatu tu kutoka pale alipo.

“Umeharibu utaratibu, nilikwambia usifanye makeke yoyote sasa wewe umekiuka kanuni, namuua huyu Malaya wako kasha naondoka na wewe,” sauti ya mtekaji ilisikika. Kamanda Amata akaona sasa mchezo usio rasmi unaanza kwani hakuwa na taarifa yoyote juu ya hii hatari.

“Umeshasema Malaya, we muue tu, hana thamani kwangu!” Kamanda akajibu.

“Leo hana thamani kwako wakati kila siku unamlala nyumbani kwako!” Yule mtekaji akaendele kuropoka, maneno ambayo yalimtia hasira Gina, akajaribu kukukuruka lakini hakuweza kutoka kwani kono la mtekaji lilimbana koo na akajihisi kukosa pumzi. Kamanda Amata alaimtazama Gina anavyoteseka, akawasiliana naye kwa macho, gina alielewa kitendo alichokifanya Kamanda.

Gina aliachia mkono wake kutoka kwenye ule wa Mtekaji lakini bado alikuwa kabanwa kwa kabala, akajizungusha na kukamata uume wa mtekaji huyo, akaubana kwa nguvu na kuuzungusha ghafla. Yule mtekaji akapiga kelele za maumivu, akamwachia Gina akabaki katoa macho ya kutisha, Gina akaendelea kuuzungusha huku amezikamata na korodani zake, Yule mtekaji akaanguka chini, Gina hakumwachia mpaka alipohakikisha kamtoa roho.

“Asante Gina!” Kamanda akamshukuru wakakumbatiana.

“Kompyuta Gina,” Kamanda akamwambia.

“Usiwe na shaka, nimekwishaitoa muda mrefu, wakati naondoka ndipo nilipoona hiyo gari inakuja, nikajibana hapo kwenye kochi kubwa upande wa nyuma hamkuniona. Niliposikia kile kishindo huko chumbani mlipo, nikajua kumekucha, nikamwona huyu wa sebuleni akija kwa kasi huko ndani, name nikajitokeza kumwahi kabla hajaleta madhara, ndipo nikamfumua bichwa lake, lakini sikujua kama kuna mwingine huku nje ndo huyu mpumbavu akanibana kabala. Pole sana Kamanda, nafurahi kukuona, Idara imetikiswa!” Gina alieleza kinachojiri.

“Gina haina haja ya kukaa hapa, twende tukajipange juu ya hili,” Kamanda akamwambia huku wakitoka. Walipofika karibu na geti, Gina akauchukua begi kubwa alilokuwa amelificha hapo wakatoka nje.

“We ulikujaje hapa?” kamanda akamwuliza.

“Shiiit!” Gina aling’aka baada ya kugeuka na kutoiona gari aliyokuja nayo. Akageuka kwa Kamanda na kumtazama usoni.

“Dr. Jasmine!” akamwambia huku chozi likimtoka. Amata akamtazama na kisha akaliendea lile gari walilokuja nalo na wale watekaji, akaingia, bahati nzuri halikuhitaji ufunguo, lilikuwa ni la kubonya tu nalo likawaka, wakaingia barabarani kuondoka.

KUZIMU – shimo la mauti

Kilikuwa chumba kikubwa chenye vijichumba vingi vidogo kwa vikubwa, kwa ujumla kilitisha kwani mafuvu ya vichwa vya binadamu yalipambwa ukutani kama mapambo ya kawaida, taa nyekundu kwa buluu ndizo zilizong’aza eneo hilo la kutisha, kulikuwa na friji kubwa mithiri ya chumba cha kuhifadhia maiti. Sehemu nyingine kulikuwa na stoo iliyohifadhi kila aina ya vikorokoro vya kutisha maalumu kwa ajili ya kutesea, kunyongea, na hata kuulia kabisa.

Chumba hiki kilijengwa chini kabisa ya jumba la kifahari la Mhindi Pancho Panchilio eneo la Kerege njia ya kwenda Bagamoyo, hakuna aiyejua kinachoendelea. Kwa nje lilikuwa ni jumba linalovutia kuliangalia, asilimia kubwa ya wananchi wa eneo hilo hawakuwahi kumjua wala kumwona mmiliki wa kasri hilo, ni watoto tu waliopenda kusemajumba lile ni la wanyonya damu kutokana na mambo kadhaa waliyokuwa wakiyaona, mara watu wameletwa huku nyuso zao zimefungwa vitambaa vyeusi na mambo kadha wa kadha kiasi kwamba ilipelekea watoto wa kitongoji hicho kukaa mbali na jumba hilo.

Lakini tofauti na watu wazima, wao waliwachapa fimbo watoto wao waliokuwa wakisema maneno hayo kutokana na kwamba kutoka ndani ya jumba hilo waliweza kupelekewa maji safi kwa mabomba maalum yaliyounganishwa na pampu kubwa na yenye nguvu, hivyo waliondokana na kero ya maji ya kunywa.

Mwili wa Madam S ulibwagwa chini kama roba la chumvi, haukuwa na uzima wowote.

Kibosho, akaangalia hali ya chumba kizima walichouhifadhi mwili huo, aliporidhika nacho akatikisa kichwa juu chini na kuwageukia watu wake.

“Ulinzi wa nguvu zaidi ya ule wa Ikulu, sawa?” akaagiza.

“Sawa Mkuu!” wakajibu. Akawaacha na kutoka, akaelekea chumba kingine, akakuta vijana wakimsulubu vikali Chiba wa Chiba huku akiwa ananing’inia kwenye minyororo, mwili wote ulitota damu, hakutamanika, hakuangalika. Kibosho alisimama mlangoni.

“Karibu sana kuzimu!” akamwambia Chiba aliyekuwa hawezi hata kuinua uso, “Wewe ndiye kinara wa kuvuruga mitandao ya watu sivyo, sasa utakuwa binadamu wa kwanza kushuhudia kifo chako mwenyewe baada ya kuwaona wenzako wote wako hapa, mbuzi nyie, nani aliwadanganya kuwa mna uwezo wa Kijasusi wa kuitisha Dunia? Sasa leo mtapambana na Shetani nah ii ndiyo himaya yake,” akaongeza kusema kisha akageuka kando akawatazama vijana wake walioonekana wana uchu wa kuua.

“Na Yule bibi, mfungeni kama huyu, lakini msimtese mpaka azinduke kama bado hajafa ili mateso yote ayashuhudie kwa akili na ufahamu wake, nimekuja hapa kwa kazi moja tu,” akamgeukia Chiba “Kuua!” akamaliza na kutoka huku akifuatiwa na vijana watatu wenye misuli ya ajabu. Chiba akiwa katika ile minyororo hakufanya lolote zaidi ya kutulia tu na kusubiri kuona nini kinaendelea.

§§§§§

Kamanda Amata waliitelekeza ile gari eneo la Hoteli ya Sheratoni na kisha wao kutembea kwa miguu mpaka ilipo ofisi ya Madam S. ilikuwa tayari imepita saa tano usiku, walinzi wakawapokea na kuwaruhusu kupita kwani walishazoea kuwa muda wowote watu hao huwa wanaingia ofisini. Moja kwa moja jicho la Kamanda Amata likaenda kwenye maegesho na hakuliona gari la Madam S, wakaingia ofisini na kuketi katika viti vyao kwa

namba zao, kwani katika ofisi hiyo kila moja alikuwa na kiti chake kadiri ya namba zao za kikazi. Ukimya ulichukua nafasi kati yao, hakuna aliyeongea kwa sababu wakiwa hapo ni Madam S huwa anasema alichowaitia.

Kamanda Amata akamgeukia Gina.

“Gina, hili eneo si salama kwa sasa!” akamwambia.

“Yaani mi sina amani na eneo lolote, hata kitanda change nakiogopa, natamani kutoroka,” akajibu.

“Kutoroka! Sio suluhisho,” Kamanda akamwambia huku akinyanyuka na kufungua jokofu lililowekwa vinywaji vya kila aina, akatoa Konyagi ndogo na kuketi kitini, akachanganya na Sprite kisha akanywa taratibu. Gina alionekana kuwa mwenye mawazo mengi sana. Wakiwa katka ukimya huo mara simu ya mezani ikaita kwa fujo. Kila mmoja aliitazama hakuna aliyeipokea, baada ya kukerwa na kelele ya chombo hicho Kamanda Amata akaiinua na kuiweka sikioni bila kuongea.

“Kamanda Amata”, kisha cheko zito na la dharau likafuata, “…leo mtaishi kama digidigi, na nitawafuata popote mlipo mpaka nihakikishe nawamaliza, kwa taarifa yako, kibibi chako ninacho hapa nusu mfu, na wengine wawili, mmoja tayari ni marehemu kama unataka kumwona nenda kwenye vichaka vya Gongo la Mboto njia panda ya kwenda kwenye makaburi ya Wachina… tuachane na hilo, naihitaji hiyo kompyuta usiku huu… nipe kompyuta nikupe marehemu wako ukazike…”

Hasira ya Kamanda Amata ikawaka juu ya huyo asiyemwona,

“…kama unaitaka hii kompyuta njoo uichukue!” akamjibu.

“…Nataka uniletee wewe mwenyewe kwa mkono wako au huyo Malaya wako ambaye pamoja nawe mmeshanipotezea watu wangu watatu, kama hamtaki basi nitaichukua mwenyewe…” ile sauti ikaendelea.

“Acha uoga wewe! Kama unajiamini jitokeze tupambane, atakayeshinda atachukua kompyuta!” Kamanda akaongea kwa jazba, tayari konyagi ilishaanza kufanya kazi ichwani.

Yule mtu wa upande wa pili akacheka sana kisha akaendelea

“…sifanyi hiyo michezo ya kitoto, lakini nakuhakikishia kuwa nitaipata hiyo kompyuta, na nitazichukua roho zenu wote sita kabla ya jua kuchomoza,” akapiga mkwara.

“Na mimi nakuhakikishia kuwa nitakuwa nimekwisha kutoa roho yako na vibaraka wako kabla ya jua kuchomoza, shetani wewe!” alipomaliza kusema hayo, akainuka kitini.

“Unaenda wapi Kamanda?” Gina akauliza.

“Huyu mshenzi keshanitia wazimu, nitahakikisha namjua usiku huu huu na namng’oa koromeo lake, hawezi kufanya dharau na kitengo nyeti kama hiki, huyu hafai kuishi,” Amata aliongea kwa hasira.

Gina naye akasimama wima na lile begi lenye kompyuta mkononi, “Na hii je? Maana inaonekana wana uchu nayo,” akamwambia Amata.

“Tia kwenye sefu salama hapo hata uje na kifaru huwezi kuitoa,” akamweleza.

“Sijui namba za kufungulia,”

“Oh, sorry!” Kamanda akaichukua ile kompyuta na kuingia kwenye kijichumba kidogo kisha akaiweka mahala salama na kutoka na lile begi, akafungua kabati linguine na kutoa kompyuta iliyofanana na ile lakini ilikuwa mbovu siku nyingi, akaipachua hard disk na kulichukua lile ganda tupu akalitia kwenye begi, kisha wakatoka na kuchukua gari mojawapo iliyo kwenye maegesho.

“Gina, upo vizuri? Akili ipo sawa?” Kamanda akamwuliza. Gina hakujibu, alionekana kujawa na hofu kuu, Kamanda akamwangalia na kumwuliza tena.

“Gina, unakumbuka The Art f War?” akamwuliza.

“Hapana Kamanda!” akajibu. Kamanda Amata akatikisa kichwa baada ya jibu hilo.

“Gina wewe ni mwana usalama na haya mambo umejifunza chuoni hutakiwi kusahau mama, sawa?”

“Sawa!”

“Sikiliza Sun Tzu aliandika ‘Jifanye mchovu unapokuwa na nguvu na jifanye una nguvu unapokuwa mchovu’, hata mimi Gina ninaogopa maana simjui adui yangu kasimama wapi, lakini lazima na mimi nimtishe hiyo ndiyo Art Of War,” Kamanda alimtoa hofu Gina.

“Nimekuelewa Kamanda, sasa tunapambana vipi na huyu hayawani?” Gina akauliza. Kamanda akabaki kimya kwa muda, kisha akamgeukia Gina.

“Gina, naomba nisikujibu, na wala usinambie unachofikiria, unajua kwa nini?” akamuuliza.

“Hapana!” akajibu.

“Art of War inasema ‘Ifanye mipango yako iwe siri, isipenyeke kama giza la usiku, na unapojitokeza jitokeze kwa nguvu kama radi’ sio maneno yangu nia Sun Tzu na daima huwa napenda kufuata maneno yake ndiyo maana unaona hapa nilipo,” alipotaka kupachika ufunguo kwenye switchi ya gari Gina akamdaka mkono.

“Kamanda! Hayo uliyosema si ajabu hata adui anayajua,” akafungua mlango na kumvuta Kamanda nje, kisha wakaelekea getini na kutoka nje mpaka barabarani.

“Naona sasa umeanza kujua unalotakiwa kufanya, vizuri sana Gina!” Kamanda akampongeza kisha wakaingia kwenye tax na kutokomea.

Breki ya kwanza ilikuwa mje ya ukumbi wa Jiji mkabala na bandari ya boti za Zanzibar, wakalipa na kisha wakapotelea gizani.

Katika kaunta ya kituo cha Polisi cha Kati, kulikuwa na PC wawili na WP mmoja, Kamanda Amata na Gina walikwea ngazi na kusimama mbele yao. Wale Polisi mara moja walimtambua Gina na kusimama imara kwa kumpa heshima yake ya kijeshi.

“Inspekta Simbeye, ameonakana tena huku?” Gina akauliza.

“Yupo afande, amekuja muda si mrefu,” Yule WP akajibu.

“Naomba tumwone!” Gina akasema hayo huku tayari ameshaanza safari ya kuifuata ofisi hiyo.

Inspekta Simbeye alionekana kuzeeka ghafla kwani mashavu yake yalikuwa yameshuka kiasi kwamba Kamanda Amata alitamani kucheka.

“Shikamoo mzee!” Amata alianza kwa kuamkia kama kawaida akikutana na Inspekta huyo.

“Sina haja ya shikamoo yako, nakupigia simu Amata hupatikani kwa nini?” akauliza kwa hasira.

“Inspekta, kama ulivyowakosa wengine wote na mimi pia usingeshangaa, hata mimi sina mji wa kupokea, hali ni mbaya, nilikutafuta ulikuwa umetoka,” kamanda akajibu.

“Kamanda Amata! Ni nani huyu anayetufanya sisi wapumbavu kiasi hiki, Mheshimiwa Mbunge wa Miroroso ameuawa usiku wa leo, ni masaa mawili tu yalopita,” kabla hajaendelea Kamanda akamkatisha.

“Na hilo hasa ndilo limenileta kwako, nilitaka kujua ni nani aliyeuawa maana nimesikia tua lakini sikujua ni nani aliyeuawa!”

“Ni Mbunge wa Miroroso,” Simbeye akajibu.

“Ok, nimeelewa Inspekta, sasa picha inaanza kujijenga taratibu na itakamilika tu,” Kamanda akajibu.

“Huu umekuwa usiku mbaya sana, siwezi kulala kwa kuwa kifo cha huyu Mbunge kimekuja wakati mambo haya ya vita vya Ufisadi mliyopambana nayo huko Uswizz bado hayajapoa, na huyu Mbunge ndiye alikuwa mstari wa mbele kabisa katika kuyafichua, je huu si mnyororo mmoja?” Inspekta akaonesha wazi hofu yake.

“Nimekupata Inspekta, naomba niondoke kisha tuwasiliane dakika arobaini na tano zijazo,” Kamanda akajibu kisha akaondoka na kufuatiwa na

Ginaa

2

HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI- SAA 6:47 USIKU

KAMANDA Amata akifuatana na Gina waliingia moja kwa moja chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali hiyo, wakamkuta Daktari akiendelea na uchunguzi. Wakiwa wanaongozwa na muuguzi waliingia ndani ya chumba hicho. Walipofika wakaonesha vitambulisho vyao kwa Yule daktari, hivyo hakuwatilia shaka.

“Karibuni sana!” akawakaribisha.

“Asante!” Gina akawa wa kwanza kujibu.

“Sijui niwasaidie nini? Maana nimechoshwa na maswali yenu yanayofanana,” Yule daktari akauliza huku akiwa amesitisha kuendelea kufanya uchunguzi.

“Nataka kujua maraehemu amekufaje?” Kamanda akauliza.

“Amepigwa risasi,” akajibu daktari.

“Ngapi?” Gina akawahi.

“Mbili za kifuani,” akajibu.

Kamanda Amata akasogea jirani na kutazama yale majeraha yalivyojipanga, moyo wake ukapiga chogo chemba, yalikuwa mithiri ya yale ya Frederick Masawe na Petit kule Uswizz, akatazama kwenye paji la uso la marehemu akaona alama ndogo ya risasi nyembamba iliyopenye bila uharibifu.

“Daktari, nah ii je?” akauliza. Yule Daktari akasogea na kwa kutumia kurunzi yake maalumu akagundua tundu hilo, wakamgeuza marehemu na kisogozi wakakuta matone machache ya damu.

“Amepigwa risasi tatu,” Kamanda akaeleza, “Asante Daktari, tulitaka kujua hilo tu,” wakamwacha na kuondoka zao.

“Kamanda hii kazi nyingine sasa,” Gina akamwambia Amata.

“Usijali Gina, hii kazi lazima imalizike usiku huu, kimya kimya mpaka kitaeleweka, leo nataka tufanye kazi hii ngumu mi na wewe tu, jua likichomoza tujue nini tumefanya na dunia ya pili isijue nini kimefanyika, usiogope, Art Of War iliyoandikwa na Sun Tzu inasema ‘Nenda taratibu kama upepo na muwe karibu kama miti. Shambulia kama moto na uwe imara kama Mlima’” Kamanda akamwambia Gina huku wakitoka nje ya chumba hicho.

“Twende nyumbani kwanza tukachukue dhana za kutosha kisha tuingie rasmi kwenye mpambano, tufanye haraka kabla watu wetu hawajapata madhara zaidi, Gina, piga simu Polisi Mabatini waambie kuna mwili wa marehemu kule Gongo la Mboto ili waende kutazama, na kama adui alitegemea kutunasa huko atapambana na vijana wa khaki,” Kamanda alimwambia Gina na mara baada ya Gina kufanya hivyo, wakaingia kwenye Tax.

“Kinondoni makaburini tafadhali!” Kamanda akamwambia dereva tax, kisha wakaondoka eneo hilo. Baada ya kuuacha Mtaa wa Mindu na kuchukua barabara ya Umoja wa Mataifa ndipo kamanda alipogundua kuwa kuna gari ikiwafuata, akamtazama dereva ambaye alionekana hajui chochote, walipopita shule ya Sekondari Tambaza ile gari ikawapita kwa kasi na kuwazuia kwa mbele.

Watu watatu walishuka kwa kasi kwenye ile gari, mikononi wakiwa na Shot Gun, waliishambulia ile tax kwa risasi na kuichakaza vibaya.

Kamanda Amata alimvuta dereva na kumsweka chini, mtawanyiko wa vyoo uliwafanya kushindwa kufanaya lolote, Gina alishuhudia lile begi likinyakuliwa na alipotaka kulitetea alipigwa na kitako cha bunduki akarudi chini, wale jamaa wakaondoka kwa kasi na gari yao wakapotelea katika mitaa ya Upanga.

Kamanda Amata akajinyanyua na kutoka nje, akamtoa Gina kisha Yule dereva ambaye alikuwa katika hali mbaya, hakuguswa na risasi lakini hofu ya milio ya zile mashine ilimfanya kuachia mkojo bila kujijua.

Kamanda Amata akachomoa kadi moja ya kibiashara na kumpatia Yule kijana, “Kesho jioni unitafute!” kisha yeye na Gina wakapotea eneo lile kabla Polisi hawajafika.

Walipokuwa wakikimbia, Gina alikuwa akiishiwa nguvu kila muda ukienda.

“Kamanda, Kamanda! Nakufa!” alilalamika.

“Jikaze Gina!” akamhimiza lakini hali haikuwa nzuri, Gina akaanguka chini. Kamanda akamtazama vizuri akaona mchaniko mkubwa a kichwani na damu zikimvuja eneo moja la mgongo karibu na nyonga, ilikuwa ni risasi iliyompata barabara katika eneo hilo.

“Shiiitttt!”

Akatazama huku na kule, akaona gari ikija kwa mbali, akamweka Gina chini na kuizuia kwa kuingia barabarani, hakuuliza, alimbeba Gina haraka na kumwingiza kwenye gari.

“Nifikishe Mtaa wa Upanga Seaview haraka!” akaamuru.

“Aliyekwambia hii tax ni nani?” Yule deeva akajibu kijeuri huku akizima gari na kuchomoa ufunguo. Kamanda Amata hakuwa na muda wa kupoteza, alfungua mlango akazunguka upande wa dereva, akafyatu lock na kumvuta nje, akamtupia barabarani kisha akakaa kwenye usukani, akachomoa kadi yake ya benki na kuivunja katikati, akaislaidi, katikati yake pakatokea ufunguo mdogo wenye meno mawili akaupachika kwenye swichi ya gari n kuiwasha kisha akaingia barabarani na kumwacha Yule mmiliki wa gari akipiga kelele.

§§§§§

SAA saba na nusu usiku ilimkuta Kamanda Amata katika jumba kubwa lililojengwa kandokando ya bahari ya Hindi huko Upanga, akaegesha gari mahala pake kisha akamtoa Gina ambaye tayari alikuwa amekwishapoteza fahamu.

“Usife Gina, usife tafadhali, subiri kidogo Gina!” kamanda alikuwa akiongea kama aliyechanganyikiwa huku kambeba Gina katika mikono yake akielekea ndani ya jumba hilo.

Dr. Khadrai alikuwa mlangoni akimwangalia kijana huyo ambaye wamekutana mara chache sana katika harakati za maisha yao.

“Karibu Amata, pole sana!” akamkaribisha na kumwongoza moja kwa moja mpaka kwenye chumba maalum ambacho kilishehenu kila aina ya kifaa tiba unachokijua, akamwonesha kitanda pa kumlaza Gina. Dr. Khadrai akamtazama Gina harakaharaka kisha akamtazama kamanda Amata. Akavuta mashine yake kubwa na kuchukua trei iliyojaa vikorokoro kisha akaanza kazi yake ya kitabibu, kwa kumsafisha Gina majeraha na kumtoa risasi iliyokuwa imenasa ndani. Kamanda Amata hakuwa na muda wa kusubiri.

“Daktari, maadam yuko mikononi mwako, naomba niende, kama kuna shida yoyote naomba unitaarifu kwa namba hizi,” akampa namba za Gina, kisha yeye akachukua simu mbili za Gina, akachukua saa na kumwachia simu moja ndogo ambayo si rahisi kwa mtu mwingine kuitumia kwa jinsi ilivyo.

“Amata usiwe na wasiwasi, huyu hajadhurika sana, akiamka tu nitakwambia,” kisha akaendelea na kazi yake.

KEREGE – saa 7:35 usiku.

PANCHO Panchilio alishusha siga alilokuwa amelipachika kinywani mwake na kulibana kwenye kibompoli maalumu cha kuzimia dubwasha hilo. Akainua macho yake na kutega masikio akisikiliza michakacho ya miguu ya mtu aliyekuwa akitembea sebuleni. Kwa jinsi alivyoijenga nyumba yake hiyo, yeye aliweza kumwona kila mtu lakini wale watu hawakuweza kumwona yeye nah ii iliwafanya kusikia sauti daima na kutokuona sura ya bosi wao.

“Karibu sana!” sauti yake ikaijaza sebule yote.

“Mkuu tumefanikiwa kuipata kompyuta uliyotuagiza Mkuu!,” Yule mtu akasema.

“Vizuri sana, sikufanya kosa kabisa kuwachagua ninyi watu makini katka kazi hii, je wale hayawani wawili mmewapata?” akauliza.

“Hapana hatujawapata lakini bila shaka wamefia kwenye gari waliyokuwa wakiitumia kwani tumeishambulia kwa risasi za kutosha,” akajibu, mara hakusikia kitu zaidi ya ukimya uliofuwatiwa na sonyo refu.

“Fanculato!” akatukana, “Kwa nini msihakikishe kama amekufa? Yule bwana ni hatari sana, hakikisheni mnapata habari zake usiku huu, naitaka roho yake kabla hakujapambazuka, potea!” akamukuza.

Pancho Panchilio alikuwa amekodi vikosi viatatu kwa nyakati tofauti na vyote kuvipa kazi moja tu ya kukisambaratisha kikosi cha TSA kuanzia Madam S mpaka wa mwisho. Mipango ya kazi hiyo ilipangwa kitaalamu sana na ilitumia mbinu za hali ya juu, mpaka dakika hiyo alikuwa tayari amefanikisha kwa asilimia sitini ya kile alichokidhamiria, nab ado muda wake bado ulikuwa unaruhusu kumalizia asilimia zilizobaki. Alihakikisha vikosi vyake hivyo havijuani na wala havikutani lakini vyote alikuwa amevipa kazi ileile kwa saa zilezile za kutekeleza lakini muda tofauti wa kufanya kazi.

Hakuona hasara sana kwa kupoteza vijana watatu usiku ule yeye aliishupalia dhamira yake tu ndio maana alikodi watu hao.

Kikosi cha kwanza kiliongozwa na Kibosho, Kanali wa jeshi aliyehasi na kupotea pasikojulikana, sasa alirudi baada ya kuitwa na Mhinidi huyo kwa kufanya kazi kama hizo. Kikosi cha pili kiliongozwa na mtu mmoja hatari kutoka nchi jirani aiyejulikana kama Kaburu na kikosi cha tatu kiliongozwa na mpiganaji aliyebobea kwenye taaluma ya kuua bila kukusidia huyu alikuwa ni mtaalmu wa kucheza na kifo mbele ya binadamu yeyote Yule, ni jambazi la kimataifa kutoka Kigoma, alijulikana kama Naima.

Hawa wote walipewa kazi kwa nyakati tofauti na wenyewe hawakujuana kama wana kazi moja kwa maana kila mtu hiyo ilikuwa ni siri kwake. Walipewa saa kumi na mbili za usiku tu kukamilisha kazi hiyo ngumu. Nao waliwasaka wabaya wao kwa hali na mali kuhakikisha wanamfurahisha bosi wao, malipo waliyopewa ni makubwa na yaliwapa jeuri ya kufanya hivyo.

Usiku huo kwao, ulikuwa usiku wa kazi.

3

KAMANDA Amata alikuwa kachanganyikiwa akili kwa namna moja au nyingine, alikuwa akiona kama ndoto inayotokea mbele yake, hakuamini kama wamewahiwa namna hiyo na kwa kasi ya ajabu, alijiuliza kila wakati ni nani mwenye uwezo wa kuwanasa namna hiyo, hakupata jibu zaidi ya hapo aligundua kuwa kwa vyovyote ni watu hatari wanaojua nini wanafanya na kwa wakati pia alielewa watu hao wamepewa kazi kwa muda maalumu hivyo nay eye kama ilimpasa kuwa saidia wenzake alitakiwa ajipe muda maalum na muda wa kazi yake uwe mdogo kuiko muda wa adui zake pia ucheze ndani ya muda wa adui zake. Alitikisa kichwa kana kwamba kuna mdudu akimtembea kwenye ubongo wake, akaitazama saa yake, saa zinayoyoma kwelikweli.

Ilikuwa inakaribia saa nane usiku alipokuwa akifungua geti la nyumbani kwake, akaingia na kulifunga nyuma yake, kisha akasimama kidogo kuangalia nini kinaendelea huku na kule, kwa macho yake makali aliweza kuona ua moja kubwa likitikisika kidogo, akaelewa wazi kuwa mtikiso huo lazima kuna kitu na si wa upepo kwani hali yah ewe ilikuwa imetulia sana na haikuwa na upepo. Damu ikamtembe haraka mwilini, hakufanya lolote, akauendea mlango wa nyumba kubwa na alipoufikia alikuta karatasi iliyoning’inizwa mlangoni, kisu chembamba chenye makali kuwili kilitumika kuishikia hiyo karatasi pale mlango.

Mwisho wa zama zenu umekwisha, mtaongea na Ngurumo.

Ulikuwa ujumbe uliosomeka katika karatasi hiyo pale juu. Akakikamata kile kisu na kukichomoa kwa nguvu, akakibusu, akaiokota ile karatasi na kuishika mkononi kisha akaingia ndani na kuuacha mlango wa nyumba yake bila kuufunga makusudi tu. Moja kwa moja akakiendea chumba chake na kufungua kabati kubwa lililokuwa mbele yake. Akavuta fulana yake nyeusi kaba shingo ya mikono mirefu akaivaa ikitanguliwa na vesti nyeusi pia. Kizibao cheusi chenye mifuko mingi ya kuwekea zana mbalimbali kikafuata juu yake, na zana zake zikapachikwa, bastola nne zilizosheheni risasi zikakaa mahala pake, visu vidogodogo vikawekwa mahala pake, paketi za risasi zikawekwa mahala pake, Shotgun mbili zikabanwa mahala pake nazo zikiwa zimetimia. Akakusanya vikolokolo vya kutosha kwa pambano hilo ambalo hakujua ni nani haswa anakwenda kupambana naye.

Akiwa kasimama kwenye kioo, anajiweka sawa, akahisi vinyweleo vyake vikisimama, mwili ukamsisimka, akajua kuna jambo, akalisubiri huku akijifanya hajui lolote.

Palepale kwenye kioo alimuona mtu akiingia kwa minyato kumfuata, Kamanda alitamani kucheka kwa sababu hata kama alikuwa akinyata wakati yeye alikuwa akimuona kwenye kioo ni kazi bure. Akamsubiri amkaribie ili ajue nini cha kumfanya. Yule mtu akajiandaa kwa waya aliokuwa kaufunga kutoka mkono hu mpaka ule mwingine.

Anataka kunikaba, Kamanda akawaza. Kisha kwa kasi ya ajabu akageuka na guu lake lenye nguvu likatua kichwani mwa Yule mtu, akajibwaga na kujibamiza kwenye mwamba wa kitanda, yowe la maumivu likamtoka, kabla hajafanya lolote akamnyanyua na kumpa kichapo kikali, alipohakikisha kuwa hali aliyokuwa nayo hawezi fanya lolote akamkalisha chini na kumwegemeza ukutani, akamtikisa na kumtazama usoni.

“Nani bosi wako?” akamwuliza.

“Si-si-simjui!” akajibu kwa tabu.

“Unaniletea utani siyo?” akamwuliza kwa ukali.

“Kweli simjui, mi natumwa tu na kulipwa ujira mkubwa wa kunitosha, kwa hali ya nchi yetu nakubali kufanya kazi yoyote kwa malipo yoyote,” akajieleza.

“Nafikiri hunijui sawa sawa sasa utanijua!” Kamanda akamwambia kisha akamkamata korodani zake na kuziminya kwa nguvu.

“Aaaaaiiiiggggghhhh…. Niache, niache nitasema,” akalia kwa uchungu.

“Sema, nani bosi wako, nani aliyekutuma kuja hapa?” kamanda akauliza sasa kwa ukali zaidi.

“Kweli kaka sim-ju-jui…” akajibu huku akijigeuza geuza.

Kabla Kamanda hajauliza linguine, akashuhudia povu jeupe likitoka kinywani mwa Yule mtu.

“Shiiit! Limejiua,” akang’aka kwa sauti, akaanza kumpekua.

Katika moja ya mfuko wa suruali yake akatoa simu ya mkononi, zaidi ya hapo hakuona chochote cha maana. Akaitazama ile simu, akaenda kwenye kitabu cha majina akakuta majina matano tu, la kwanza kabisa likamvutia, lilikuwa limeandikwa kwa jina moja tu ‘Naima’, kisha akaliangalia la pili na la tatu. Akaamua kuanza kampeni na jina hilo la kwanza.

Akaperuzi upande wa ujumbe mfupi, akakutana na ujumbe kutoka kwa Naima uliotumwa ndani ya dakika kumi zilizopita lakini ulionekana kutojibiwa.

‘…Akifika nijulishe nije nimalize kazi…’

ujumbe ulisema hivyo.

Lilifikiri litaniweza, sasa naanza na Naima, kawaza na kuamua kuujibu ule ujumbe.

Kamanda Amata akaujibu ule ujumbe, kisha akaburuza mwili wa Yule mtu na kuubwaga katika mlango wan je kisha yeye akalitoa pikipiki lake na kuliegesha nje kabisa, akisubiri kuona kinachoendelea.

Akiwa nje ya nyumba yake, juu yapikipiki lake kubwa akasubiri kimya nje kabisa ya nyumba yake.

Dakika tano hazikupita, mwanga wa taa za gari ukaonekana ukijitokeza katika kona ya barabara na kuelekea mtaa huo ilipo nyumba ya Kamanda Amata. Ilikuwa Ford Ranger nyeusi, haikuwa na namba za usajili, ikasoge polepole na kuegeshwa karibu kabisa na lango la nyumba hiyo, watu watatu wakashuka, mmoaj kati yao alikuwa mwanamke, alionekana ndiye akiongoza wengine, aliwapanga, mmoja alimwamuru abaki langoni, yeye na mwingine aliyeonekana pande la jitu waliingia ndani.

§§§§§

Naima na lile jitu moja kwa moja waliingia getini na kutembea kwa mainyato huku silaha zikiwa mikononi mwao. Wakiwa wanajigawa kiufundi zaidi kuuelekea mlango, walishangazwa na ukimya uliotawala, lakini hawakujali. Lilikuwa ni lile pande la mtu lililotangulia kuuendea mlango, kabla halijafika likajikwaa kwenye kitu kama gogo.

“Aah!” likajivuta na kujibwaga mbele. Lilipogeuka nyuma likaona mwili wa binadamu, “Shiit! Amemuua,” akasema kwa sauti.

“Nani amemuua?” Naima akauliza, kisha akashusha silaha yake na kusogea pale ulipo ule mwili, akaugeuza, na kuchomoa kijikaratasi kilichopachikwa kinywani mwa marehemu.

…Naanza na wewe…

Naima akageuka huku na kule asione mtu, anaanza na mimi! Hata kama Naima alikuwa ni muuaji mzuri kitaaluma lakini alijikuta akishikwa na ubaridi wa ghafla. Wakaingia ndani wakatafuta huku na kule hawakuona mtu zaidi ya redio kubwa iliyokuwa ikipiga muziki laini wa ‘Killing me softly’ akasonya na kutoka nje. Wakabeba mwili wa mwenzao na kutoka nao. Wakaubwaga katika nyuma ya pikap yao na kufungia. Kisha nao wakaingia garini na kuondoka.

§§§§§§

Kamanda Amata akawasha pikipiki lake, bila kuwasha taa, akaingia barabarani na kuwafuata taratibu, wakaikamata barabara ya Kinondoni na kuvuka daraja la Salenda kisha wakaelekea mjini, moja kwa moja mpaka Mbowe Club, wakaegesha gari na kuteremka kisha wakapotelea ndani.

Kamanda Amata akaingia baada yao na kuhakikisha hawapotezi katika himaya ya macho yake, akaketi katika moja ya viti vya kaunta na kuagiza glass moja ya Whisky akachanganya na sprite baridi kisha akawa anakunywa taratibu.

Wale jamaa wakaketi mahala Fulani wakijadiliana jambo lakini wakionekana kuwa na wasiwasi, kila mara Naima alionekana kuisoma ile karatasi na kuiweka tena mfukoni. Mara lile jitu la miraba mine likanyanyuka na kutoka mahala pale likamwacha Naima na mwingine mmoja. Kamanda Amata alipogeuka hakuliona lile jitu limeingilia kona gani, akili yake ikazunguka mara mbili, akateremka katika kile kiti na kujichanganya katikati ya watu waliokuwa wakiburudika na uziki katika ukumbi huo. Dakika kadhaa baadae akaliona lile jitu pale kaunta likinga’aang’aa macho, likabeba vinywaji na kuelekea kule lilikokaa tangu mwanzo, yote hayo Kamanda Amata alikuwa akiyatazama kutoka katika kundi la watu wale. Alipoona kuwa hakuna aliye na yeye alirudi tena kaunta na kuagiza kinywaji, lakini hakuweza kukimaliza baada ya kumwona Naima akinyanyuka kitini na kuelekea nje, Kamanda Amata naye akatoka na kumfuatilia mwanadada huyo.

Naima alisimama kati ya magari na kuweka simu yake sikioni kisha akaendelea kuongea na aliyekuwa upande wa pili.

Naima akiwa anaendelea kuongea na simu alihisi ubaridi ukimgusa maeneo ya shingoni, akashtuka akataka kugeuka.

“Tulia!” sauti nzito ya Kamanda Amata ikapenya sikioni mwake. Naima akatulia kama alivyoamuriwa, “Nilikwambia nitaanza na wewe, na ndiyo sasa naanza,” akaongeza.

“Weweni nani?” Naima akauliza kwa sauti yake nyororo inayoweza kumnyong’onyesha mwanaume yeyote Yule rijali.

“Mimi ni Yule mnayenitafuta, Kamanda Amata, na nataka unambie watu wangu wako wapi?” Kamanda akaongeza swali kisha akatulia. Naima naye alitulia bila kujibu, akitafakari la kufanya. Baada ya sekunde kadhaa, uamuzi aliofuanya haukuwa mzuri hata kidogo. Aligeuka na pigo kali kwa Kamanda Amata, lakini Kamanda aliliepa kiufundi huku bastola yake ikimtoka mikononi. Naima aliruka sarakasi kwa minajiri ya kuiwahi le bastola lakini kabla hajafika alijikuta akipokea teka la nguvu mbavuni na kutupwa upande wa pili, akajiinua haraka na kusimama wima kumkabili Amata. Amata alijiweka sawa mwili wake na kumwendea kama mbogo, Naima alijiweka sawa na kuvamiana na Amata, kama Kamanda alifikiri mwanamke huyo anapigika kirahisi alikosea, mapigo matatu ya haraka yalimwingia Kamanda akajikuta anapoteza netweki, akajaribu kujitutumua lakini akajikuta amedhibitiwa ka mikono imara ya mwanamama huyo.

Naima alijirusha hewani kama jani la mkorosho na kuachia dabo kiki za maana zilizotua sawia kifuani mwake na kumpeleka chini.

Kisha Naima akatua chini kwa miguu miwilia akimtazama Kamanda Amata akigalagala chini.

“Ha ha ha ha niliambiwa kuwa Amata ni mwanamume wa chuma kaa mbali naye! Chuma kiko wapi hapa? Na sasa nakuua kwa mkono wangu kwani nimeahidiwa pesa nyingi sana kama roho yako nikiipeleka kwa bosi wangu,” Naima aliongea kwa kujiamini huku akiiweka sawa mikono yake tayari kumshushia pigo la mwisho kijana huyo. Alipomjia kumvamia alimshuhudia Kamanda Amata akijirusha kutoka chini kwa mtindo wa ajabu na guu lake la kulia likatua chini ya kidevu cha Naima, akanyanyuliwa na kubwagwa upande wa pili meno kadhaa yakimtoka.

“Mpo chini ya ulinzi!” sauti kali ikasikika upande mwingine. Kamanda alipotupa jicho akaona polisi eneo hilo, akaruka sarakasi na kutua upande wa pili wa gari, akajibana sehemu ambayo kutokana na nguo zake hakuweza kuonekana, akitazama linaloendelea.

Amata alishuhudia wale polisi wawili wakichezea kichapo cha maana kutoka kwa Naima, wakishindwa kujitetea hata kwa ngumi moja kwani kipigo kilikuwa cha sekunde kadhaa lakini kikali.

Huyu mwanamke ni balaa! Akajisemea, upo muda wake nitamtia mkononi tu, akajisemeana kusonya.

KEREGE – saa 8 usiku.

KIKAO cha dharula kiliitishwa ndani ya kasri la Pancho Panchilio, watu watatu walingia ndani ya jumba hilo kupitia milango tofauti kiasi kwamba hata walinzi tu hawakuweza kuwaona wageni hao. Walijikuta ndani wakiwa waneketi katika mtindo wa duara na Yule kinara wao akiwa mbele pa si na kuonekana. Wote waliketi kimya kabisa wakisubiri mkuu wao aongee.

Akajikohoza kidogo kutengeneza koo lake, kisha akafungua kikao hicho kisicho rasmi.

“Wajumbe mtashangaa nimewaita ghafla usiku huu, lakini lengo ni kuwapa taarifa ya kile kinachoendelea mpaka sasa,” Pancho alianza.

“Ndio tunakusikiliza,” mjumbe mmoja akaitikia.

“Vikundi vyetu vimefanya kazi kubwa sana na vimefanikiwa kuwakamata watu watatu, yaani namba moja, namba tatu na namba nne, na hali zao ni kifo muda wowote,” akaendelea.

“Ndiyo hata mimi nilikwishasema kuwa, hawa wakikamatwa ni kuwaua tu na maiti zao tunateketeza kwa moto ili kupoteza ushahidi,” Mjumbe mwingine akaongeza.

“Lakini sasa kuna kikwazo kimoja,” Pancho akatulia hapo.

“Kikwazo gani tena?” akauliza mjumbe.

“Namba moja wao ndiyo anyelete shida na kati ya watu wetu tuliowapa kazi kumbukeni ni vikosi vitatu mashuhuri, watu wane wameshapoteza maisha kwa mkono wake,” akawapa ujumbe uliowashtua kidogo.

“Unasema!” Mjumbe mmoja akaonekana kuanza kuchanganyikiwa.

“Habari ndiyo hiyo! Hivi sasa vijana wapo mtaani wanamsaka mshenzi huyo, mmoja kati ya hao tumemuua yupo katika machaka ya Gongo la Mboto ambako huko pia tumemkosakosa Amata ijapokuwa vijana wetu walilishambulia vikali gari lake lakini alitoweka.”

“Huyo siyo binadamu ni shetani, kwanza mi siku zote sijawahi kumwona japo nimefanya juu chini nimwone japo kwa sekunde moja, namsoma tu vitabuni,” mjumbe ambaye ni mzee kuliko wote aliongeza na wote wakacheka.

“Sasa tunafanyaje?”

“Vikosi vyetu vipo kazini, bado vinasakana na huyo Amata, hwa tulio nao nafikiri ni kuwamaliza kuwaweka hapa ni hatari kwani wakipata nguvu madhara yake ni makubwa,” Pancho akashusha pumzi, “Ila hapa kuna habari njema,” aliposema hayo wote wakakaa sawa.

“Tumeipata kompyuta mama, ile ambayo anatumia boss wao Yule bibi,” akawaambia.

“Eewaaaa hilo nalo neon asee!”

“Sasa ina neno fungushi ndiyo tatizo (password), maana humu ndimo kuna siri zote za hawa jamaa, nilikuwa nawasubiri kwa pamoja tuamue la kufanya,” akaeleza.

“Ni kutumia nguvu tu kupata hiyo password, wenyewe wanaijua, sasa wape kazi vijana watumie nguvu ili kupata hiyo password tujue kilichomo, hawawezi kutupanda kichwani,” Mjumbe mzee akatoa wazo.

§§§§§

Taarifa za kupatikana kwa mwili wa Scoba zilimfikia Kamanda Amata, nguvu zilimwishia kabisa hakuwa hata na la kufanya. Aliitazama saa yake mkononi ilikuwa saa nane na uchafu wake, muda unayoyoma, hakujali aliliwasha pikipiki lake na kuelekea hospitali ya jeshi Ukonga ambako aiambiwa mwili huo umehfadhiwa kwenye chumba maalum.

Hakuamini alipomkuta Scoba kalala kimya huku madaktari wakijaribu kupigania uhai wake wa mwisho. Kamanda Amata alisimama mlangoni na kisha akarudi nje, akajinaamia kwenye ukuta machozi yakimtoka.

Akachomoa mfukoni simu yake na kuiweka sikioni, akamsubiri mtu wa upande wa pili ajibu.

“Ndiyo konokono vipi?” sauti ile ikauliza.

“Konokono anahitaji miguu ya kutembea!” kamanda akaeleza kwa lugha waliyoelewa wenyewe.

“Mwambie aje kuchukua!” akajibiwa na simu ikakatika.

Kamanda Amata akapiga namba nyingine na kuisikiliza.

“Hello!” sauti ikaita.

“TSA namba moja anaongea!” akajibu lile itikio.

“Unasema nani a-a-naonge-a” kigugumizi kilimshika mtu wa upande wa pili.

“TSA namba moja ninaongea, Mkuu naomba tuonane ofisini kwako usiku huu, haraka sana,” Kamanda akatoa amri.

“Kuna nini Namba moja?” akauliza Mkuu wa Usalama wa Taifa Bwana Hosea.

“We naomba tuonane tutajua hapohapo kuna nini…”

“Ok! Copy and paste,” Hosea akajibu huku akikiacha kitanda na kumbusu mkewe Techla aliyekuwa kazama usingizini, kalala fofofo.

USALAMA WA TAIFA – saa 8:40 usiku.

MKUU wa kitengo cha Usalama wa Taifa, Bwana Hosea aliwasili katika jengo hilo na kupokelewa na walinzi, kila mmoja alishangaa kumwona mtu huyo usiku mnene kama huo, kuja kwake halikuwa tatizo, tatizo ni kuja ghafa na bila taarifa. Hakuongea na mtu, alipita moja kwamoja katia sebule kubwa ya kupokelea wageni.

“Mkuu mbona hivyo vipi?” Avanti alimtupia swali walipokutana koridoni.

“Salama tu, upo nani ofisini?” akamuuliza.

“Nipo na Muba,” akajibu.

“Ok, kuna lolote la ajabu mliloliona? Au taarifa mliyoipata?” akamwuliza.

“Ni ajlia iliyotokea Salenda, lakini tumeishaianyia kazi, na mauaji ya Mheshimiwa Mbunge wa Miroroso,” Avant akamweleza.

“Ok, nitawaona baadae kama nitawahitaji,” akamwambia huku akiiendea ofisi yake.

Dakika moja tu baada ya yeye kuingia katika jingo hilo, pikipiki kubwa la Kamanda Amata lilifika getini.

“Jitambulishe!” ilikuwa sauti ya mlinzi.

Kamanda Amata, akataja namba yake ya siri inayomtambulisha kikazi badala ya kitambulisho. Ukimya ukachukua nafasi kisha geti likafunguliwa naye akaingia. Akaegesha pikipiki lake na kuuendea mlango mkubwa, moja kwa moja ofisini kwa Hosea. Akamkuta Mkuu huyo akiwa ametulia kitini na bastola yake kaiweka uchi mezani.

“Karibu Namba moja!” akamkaribisha kwa hofu sana.

“Asante Mkuu! Samahani kwa kukusumbua maana imebidi umwache shemeji,” akamtania.

“Usijali, ndiyo kazi zetu hata yeye anajua, niambie Namba moja, vipi usiku huu, maana hujawahi fika ofini kwangu zaidi ya mwaka mmoja sasa,” akaanza kumhoji.

“Mkuu hali ni mbaya! Ni Kitisho!” kamanda akaanza namna hiyo.

“Unasema?” akauliza.

“Nasema idara ina hali mbaya!” akakazia.

“Kamanda Amata, TSA 1, nini tatizo?” Hosea akauliza.

“Mkuu, Madam S hajulikani alipo, Chiba, Dr. Jasmine wote hawajulikani walipo, Gina yuko mahututi kwa Dr. Khadrai, Scoba naye habari yoyote inaweza kutokea,” Kamanda akaeleza na kuangusha chozi.

“Kamanda Amata…!” Hosea akanyanyuka kitini na kuliendea dirisha kubwa la ofisi yake, alionekana wazi kuchanganyikiwa na taarifa hiyo, akajishika kiuno, akatikisa kichwa, akajipigapiga kichwani mara kadhaa kana kwamba analazimisha kukumbuka kitu, akasonya na kugeuka alipo Kamanda Amata.

“Eti unasemeje? Ina maana wametekwa au wameuawa?” akauliza tena kama hakusikia aliloambiwa.

“Siwezi kujua kama wametekwa au wameuawa! Ila wametoweka, na hapa unaponiona ninatafutwa kwa ubani na uvumba,” Kamanda akaeleza.

Mara hodi katika mlango wa ofisi hiyo ikabishwa.

“Ingia!” Hosea akaitikia, “Vipi, usiku huu sasa!”

“Samahani Mkuu, kuna taarifa hapa ambayo ungeikuta asubuhi lakini maadam upo ni muhimu kuiona tena haraka iwekanavyo,” Mubah akakabidhi karatasi ndogo kwa Hosea kisha yeye akaondoka. Hosea akaitazama kwa makini, akairudiarudia kuisoma kama haielewi.

“Japokuwa si kazi yako lakini tazama hii taarifa,” akampa Kamanda Amata, akaipokea na kuisoma, moyo ukamlipuka, akaanza kuhema kwa nguvu.

…Moja ya gari zenu imepata ajali leo wakato wa mvua kubwa katika daraja la Salenda, ndani ya gari hajapatikana majeruhi wala maiti, tunaomba ushirikiano wenu…

Ilikuwa ni sehemu ya taarifa hiyo, Kamanda Amata akashusha ile karatasi na kuiweka mezani.

“Naomba niwe na haraka!” akamwambia Hosea.

“Bila shaka kamanda!” akamjibu. Amata akachukua simu ya ofisini kwa Hosea na kuzungusha tarakimu kadhaa kisha akaweka sikioni.

Akaongea na mtu aliyemtaka kisha akaishusha simu na kuiweka mahala pake.

“Kamanda, njoo huku!” Hosea akamwambia kisha wakatoka na kuelekea chumba cha mawasiliano.

Wakaingia katika chumba kipana ambacho kilikuwa na kila aina ya mawasiliano ikiwe zile kamera za mabarabarani na sehemu nyeti Dar es salaam.

“Nyie, hii ajali imetokea saa ngapi?” Hosea akauliza.

“Saa moja kama na nusu hivi Mkuu!” Mubah akajibu.

“Sasa, saa moja mpaka sasa nane, na mnajua gari iliyopata ajali ni ya kwetu, eh! Mubah, Avant mlikuwa mnafanya nini humu ndani…?” Hosea aliongea kwa hasira, Mubah na Avant wakabaki kimya huku Mubah akimtazama Avant kwa chini.

“Hebu rudisha nyuma nione hiyo picha kwanza!” Kamanada akaomba. Avant akafanya hivyo na ile picha ikafika mahala pake, Kamanda Amata akashuhudia ile gari ikiacha njia na kupanda tuta la katikati kisha ikajipiga mwambani na kupinduka vibaya kabla ya kutumbukia kwenye mikoko chini ya daraja. Akairudiarudia kama mara tano hivi, kisha akamgeukia Hosea.

“Vipi?”

“Hii ni gari pekee ya Madam S japo siioni vizuri kutokana na mvua lakini bila shaka, tazama hapa, hapa, hii ni BMW umeona ee?” akamwonesha vizuri Hosea.

“Nyie vijana muwe makini nyie! Siku nyingine nitawafaya, sasa unajua kwa kuchelewa kupata hii taarifa meshaliweka pabaya Taifa na ninyi kazi yenu ni kuangalia usalama wa Taifa, nipigieni simu wakati wowote ule nitakuja kazini,” Hosea alilalama.

“Samahani boss, siku niliyopiga simu mkeo Techla alinitukana eti mi ni hawara wako,” Avant alilalamika.

“Avant haya ni mambo ya kazi achana na mke wangu! Sawa?” akafoka na kutoka ofisini. Wakasimama kwenye korido yeye na Kamanda Amata wakijadilia jambo.

“Sasa Mkuu, yaani hapa muda hautoshi, lazima kwanza niione hiyo gari kisha nijue la kufanya, na mimi nahusisha matukio haya na lile la mauaji ya Mbunge,” Kamanda akaeleza.

“Hapo umenichanganya kidogo!” Hosea akamwambia Kamanda.

“Nilikwenda kukagua maiti ya Mheshimiwa, mauaji yake yamefanana kabisa nay a wale waliouawa Uswizz, mlenga shabaha alifanya vile vile, kumbuka huyu Mbunge ni Yule mwenye kelele za kuibua mambo bungeni hasa sakata hili la kutorosha mapesa nje ya nchi,” kamanda akaeleza kwa undani mambo mbalimbai anayoyatilia mashaka.

Hosea, Mkuu wa idara ya Usalama wa Taifa wa nchi akabaki kinywa wazi, akajishika kidevuni hasijue la kufanya.

“Ok Kamanda, sasa ulikuwa unasemaje?” Hosea akarudisha mazungumzo nyuma.

“Mkuu kwanza nilikuwa nakupa hiyo taarifa na unajua taarifa zetu huwa ni salama kwa kuziongea ana kwa ana,” akamweleza.

“Ok Kamanda, sasa ulikuwa unasemaje?” Hosea akarudisha mazungumzo nyuma.

“Mkuu kwanza nilikuwa nakupa hiyo taarifa na unajua taarifa zetu huwa ni salama kwa kuziongea ana kwa ana,” akamweleza.

“Idara, imepata taarifa kama ulivyoileta, sasa wewe endelea na harakati zako, na mi hapa nawaita vijana wangu usiku huu, ili kuanza uchunguzi wa kina nitakutaarifu muda wowote nikipata lolote, nawe unitaarifu muda wowote ukipata lolote, kama kuna mahala utahitaji nguvu nafikiri una kibali cha kuomba jeshi la polisi muda wowote sivyo?” Hosea akunguruma.

“Ndivyo!” Kamanda akajibu.

“All the best!”

KITUO CHA POLISI SALENDA – saa 9:11 usiku

GARI ya Madam S haikutazamika mara mbili, kwa ujumla ukiitazama ni kama imegeuzwa nje ndani; ndani nje, vyoo vyote hakuna, injini iko nje na mengine mengi. Kamanda Amata akaitazama kwa kina, akaikagua hapa na pale kwa utaratibu maalum sio kama ule wa polisi wa haraka haraka, yeye aliangalia kimoja kwa kingine. Akakagua magurudumu na kisha akatulia kimya.

Akiwa katika kuangalia ndani ya gari hiyo ndipo alipoona kitu cha pekee kabisa, heleni, heleni ambayo yeye anaifahamu sana, akaiokota akaitia mfukoni mwake. Kisha akamgeukia polisi aliyekuwa naye mahala hapo.

“Twende eneo la tukio!” akamwamuru.

Yule WP aliyekuwa zamu akajiweka tayari kwa safari fupi ya usiku huo, wakapiga hatu mbili.kamanda akamsimamaisha.

“We WP! Tunakoenda huko unafikiri kupo salama? Hata kama hamruhusiwi kubeba silaha, mimi nakwambia kachukue silaha,” akamwambia kwa ukali.

Dakika mbili baadae Yule WP alikuwa na SMJ iliyoshiba vyema, wote wakakaa juu ya pikipiki kubwa aina ya BMW wakaelekea darajani.

Mikoko mingi ilikuwa imekatika huku na kule, kwa ujumla palisambaratika.

“Mlikuja wangapi?” Kamanda akamwuliza.

“Tulikuja watatu,” Yule WP akajibu.

“Hamkukuta mtu hapa, majeruhi wala maiti?” akauliza.

“Hatukukuta,” akajibu.

“Njoo hapa!” Kamanda akamwita, kisha akamwonesha alama za miburuzo.

“Unaona hii, huyu ni mtu kaburuzwa kutoka hapa ilipoangukia gari mpaka kule juu labda, na hizi ni alama za viatu vya huyo aliyemburuza,” akamweleza. “Tazama hiki kioo cha mbele, hii ni risasi, kioo cha ajali hakiwezi kupasuka namna hii, kwa hiyo ajalia hii kabla haijatokea dereva alipigwa risasi,” akaendelea kumjuza.

Baada ya kuridhika na hapo wakarudi kituoni.

“Wote mlilikuwepo ajalini?” akauliza tena.

“Hapana walikuwapo watatu tu,” akajibiwa.

“Naomba wote waliokuwepo wafike hapa haraka!” akaamuru. Sekunde tu. Askari watatu wakasimama mbele ya Kamanda Amata akiwemo Yule WP.

“Vueni viatu!” akawaamuru. Nao wakavua na kuviweka pembeni.

Akavichukua kimoja kimoja na kuvigeuza chini kuangali soli za viatu hivyo, akawarudishia. Kisha akawashukuru na kuondoka kituoni hapo, alipovuka tu daraja la Salenda, mbele ya ubalozi wa Ufaransa akasimamisha pikipiki lake, akaichukua ile heleni na kuipachua katikati kisha akaipachika sikioni kama earphone.

Kwanza akasikia miruzi mikali, kisha utulivu ukafuata na sauti ya Madam S ikasikika kwa mabli kidogo.

…Nataka wote tukutane ofisini, Shamba, Chiba na mimi tumepata ujumbe wa kitisho, hili sio la kupuuzia, (ukimya ukatawala) nimetoka nyumbani, naelekea shamba, ofisi za Ubalozi, Daraja la Salenda…

Kisha ikasikika sauti ya maumivu, na kelele ya kishindo kikubwa kilichojirudia mara kadhaa.

…Angalieni kwa chini, ndani ya gari, fanyeni haraka. Atakuwa amekufa huyu! Sawa tu, mchukueni hivyo hivyo…

Akasikia sauti ya kitu kama kijiwe kikianguka kisha ukimya ukatawala. Kamanda Amata akashusha pumzi ndefu, akaitoa ile earphone na kuiweka tena kama heleni kisha akaiweka mfukoni, pepo wa hasira akampanda, akapiga kiki moja na pikipiki lile likakubali sheria, akaingiza barabarani na kuchukua barabara ya Kinodoni, kisha akakunja ile ya Kawawa akaambaa nayo mpaka Kigogo akatobolea Tabata akasonga mbele.

GEREZA LA UKONGA- saa 10:01 alfajiri.

MBELE ya Kamanda Amata kulikuwa askari Magereza mmoja aliyekuwa zamu usiku huo, baada ya kuwasiliana na Mkuu wa gereza na kuwasili pale, wote kwa pamoja wakakaa ndani ya chumba kidogo kwa mazungumzo ya kikazi.

“Ndio bwana!” Yule Mkuu wa gereza akaanzisha mazungumzo.

“Asee Mkuu, nahitaji kuona rekodi ya wageni wanaomtembelea Kanayo O. Kanayo na Mahmoud Zebaki, hilo tu!” Kamanda akatoa ombi lake.

Punde si punde ikaletwa rekodi karibu ya mwezi mzima, kila mtu alitembelewa mara nyingi na mkewe isipokuwa tu kwa Mahmoud Zebaki, huyu zaidi ya mkewe alikuwa akitembelewa na mtu mwingine aliyejiandikisha kwa jina la Ravi Kumar, Amata akatikisa kichwa. Akatazama juu huku na kule.

“Mna kamera za usalama hapa gerezani?” akauliza.

“Ndiyo zipo,” Mkuu wa gereza akajibu.

“Naomba nione rekodi yake ya tarehe 21 May mwaka huu,” wakanyanyuka wote na kupita kwenye ujia mrefu mpaka ofisi nyingine ndogo ambako walimkuta kijana mmoja mwenye cheo cha koplo, akafanya hivyo walivyoomba.

Tarehe ile mwezi ule saa ile, akaonekana mtu mwenye asili ya Kihindi akiingia katika chumba cha kuongelea, kisha Mahmoud Zebaki akaja pale wakafanya mazungumzo mafupi kama dakika tano tu. Kamanda Amata alikuwa akiangalia midomo yao na matendo yao, walipokuwa wakiagana. Mahmoud aliiweka mikono yake juu ya mbao iliyokaa kama meza katikati yao ijapokuwa walitenganisha na nondo, na Yule Mhindi akaweka juu

yake na kuiondoa. Kamanda Amata akatazama sana kitu hicho na kukirudisha nyuma mara kadhaa akagundua kuwa kabla ya Ravi kuweka mikono juu ya mikono ya Mahmoud kuna kitu alikuwa akikisoma au kukiangalia kwa makini. Kisha akaondoka na kumwacha Mahmoud akiwa na tabasamu pana.

Walipoangalia tukio la siku nyingine walimuona Ravi akifuatana na mke wa Mahmoud na mazungumzo yao yalikuwa yalionekana wazi hayakuwa ya Kiswahili bali lugha Fulani kama si Kihindi basi ni Kibangla.

“Asante Mkuu!” Kamanda akashukuru.

“Umeridhika? Ni wajibu wetu kulinda Taifa, mimi na wewe,” Yule Mkuu wa gereza akamweleza Kamanda Amata.

“Ni kweli, nikiwa na shida yoyote juu ya haya nitakutaarifu,” akamjibu.

“Bila shaka, muda wowote karibu sana,” wakaagana na Kamanda Amata akaondoka. Kamanda Amata akashika njia na pikipiki lake kuelekea mitaa ya Msasani ambako nyumba ya Mahmoud Zebaki ndiko iliko na familia yake yote iko huko, akiwa njiani akapiga simu kwa kutumia simu ileile ya Gina kwa Inspekta Simbeye, akaomba askari watatu wenye kibali cha upekuzi na gari haraka sana, akapatiwa.

Saa kumi na moja alfajiri alikuwa tayari amewasili Msasani Peninsula na ile gari ilikuwa tayari iko pale.

“Mko kamili?” akawauliza.

“Ndio afande!” wakajibu.

Wakagonga na kuingia ndani ya jumba hilo, walinzi hawakuwa na tatizo baada ya kuona serikali imefika hapo. Wakagonga mlango mkubwa na mfanyakazi wa ndani akatoka.

Walipouliza kuhusu mama mwenye nyumba wakajibiwa hayupo lakini kwa kuwa walikuwa na kibali cha upekuzi na walipita kwa Mjumbe wa shina ambaye alifuatana nao upekuzi ukaanza, nusu saa iliwachukua polisi wale kupekuwa nyumba huku wote waliobaki wakiwa wameanyang’anywa simu zao za mikononi, hakuna kibaya walichokipata isipokuwa kitabu cha kumbukumbu kilichoonesha kuwa Yule mama amekwenda Zanzibar likizo yeye na watoto wake. Ndani ya kijitabu hicho pia baada ya kupekuwa sana wakakuta namba za simu za watu mbalimbali ikiwemo Ravi Kumar, na namba hiyo iliandikwa tarehe 21 May. Kamanda Amata aaliendea likitabu likubwa la TTCL linaloitwa Yellow Page na kutafuta jina hilo mpaka akalipata, na kugundua mtu huyo anakoishi, Mtaa wa India kitalu namba 453RF, wakaagana na Mjumbe wa shina na kuondoka zao mpaka mtaa huo, haikuwa tabu kufika ghorofa ya tatu na kumkuta bwana huyo akiwa hoi kwa usingizi.

“Nyie taka nni kwagu, usiku hii bana!” Ravi alalamika. Kamanda Amata hakuwa na shaka naye kwani picha aliyoiona ni ilele iliyosimama mbele yake.

“Mchukueni huyo, tuondoke naye,” Kamanda akaamuru.

“Jamani mmi nafanya nini nyinyi? Manonea sana raia nyie bana, acheni mimi tawapa pesa jingi sana mfungue maduka!” akalalama.

“Kelele!” Kamanda akamkoromea kisha wakampakia kwenye gari ya polisi mpaka kituo cha kati. Wakamwifadhi chumba maalum.

3

KEREGE

“SASA mtataja password au hamtaji? Tunajua kama ninyi mnaijua ofisi nzima na sisi tunataka kuwasha hii kompyuta,” John the Killer ‘JoKi’ akiwa na mjeledi mkononi mwake alikuwa akimuhoji Chiba aliyekuwa hoi kwa kipigo huku mikono na miguu yake ikiwa imefungwa kwa minyororo imara. Kila alipoiangalia ile kompyuta Chiba alshikwa na woga wa kutaja password, kwa maana alijua wazi kuwa akitaja tu basi siri za za idara zimemwagika.

Upande wa pili Madam S alikuwa amerudiwa na fahamu lakini bado akajifanya amepoteza fahamu akiskiliza kila kinachoendelea, damu iliyoganda usoni kwa majeraha ya vioo, maumivu makali ya mkono na mguu yalimfanya ajikute anashindwa kustahimili hali ile, aliwaza sana alipogundua kuwa wale jamaa wameikamata ile kompyuta na vijana wake wote alishawaambia ni heri kufa kuliko kutaja hiyo password.

“Anhaaa! Bibi ameamka, verygood!” JoKi akavuta hatua mpaka kwa Madam S, akatikisa kichwa chake, kisha akamkanyaga kwa nguvu kwenye mguu wake uliioonesha kila dalili ya kuwa umevunjika kwa jinsi ulivyovimba.

“Aaaaaiiiiggghhhh! Ms**ge wewe!” Madam akapiga yowe la uchungu na kutoa tusi, JoKi akamtandika teke la usoni, Madam S akajigonga ukutani kwa kisogo na kutulia bado kwenye ile minyororo, kwa kuwa alikuwa hajafungwa miguu yake na alijiinua kwa kutumia nguvu ya mikono kwa kujiegemeza na ile minyororo, alijisungusha hewani na kumtandika teke JoKi, lililomsukuma na ye akajibamiza ukutani na kupasuka kwenye paji la uso.

Mtesi mwingine akampiga na shoti ya umeme Madam S akapiga kelele na kutulia.

JoKi akajipapasa usoni na kukuta damu zikimwagika, akamtazama Madam S kwa hasira sana, “Umefanya jambo baya sana mwanamke! Utajuta leo nakwambia!” JoKi akauzungusha mjeledi wake na kumcharaza vibaya Madam. Chiba alishindwa la kufanya.

“Mwachee!” akapiga kelele kutoka pale chini. Wale jamaa wakaanza kucheka kwa kejeli, “Ipo saa yenu, na haiku mbali, mtajuta kuiona siku ya leo,” akaongea huku akiuma meno.

“Tutajuta saa ngapi ilhali alfajiri hii nyote mnauawa?” mmoja wao akasema.

“Hata kama mkituua, nawaapia mtajuta kuiona siku ya leo!” Chiba aliendelea kusisitiza.

“Kelele wewe, nguruwe jike we!” JoKi akafoka. Na wakati huo huo watu wane wakaingia ndani ya chumba kile wote wakiwa wamevaa maguo meusi na soksi usoni; ni macho tu yaliyokuwa yakionekana.

“Karibuni wazee!” JoKi akakaribisha.

“Madam S, na kikosi chako, serikali ilkutuma kufuatilia nyendo za watu au kulinda usalama wa Taifa dhidi ya hila za Mabeberu?” mmoja wao akauliza.

“Beberu lenyewe ndio wewe!” Madam S akajibu kwa taabu kidogo lakini waliayaelewa maneno yake.

“Unajibu utumbo! Madam ! unakitaka kifo kabla ya wakati wake sio, subiri subiri bado nusu saa ya kukuua kwanza utimize haja yetu moja tu kisha tunakuua ili upumzike na mateso haya,” mwingine akadakia.

“Inaonekana mnanifahamu vema sio? Mimi siogopi kifo, nishakutana na kifo zaidi ya mara mia tano sasa hicho unachosema wewe wala sikiogopi, lakini naomba mniue kabla sijawaua ninyi,” akaongea kijeuri.

Kosi kali likatua shavuni, la pili, la tatu, la nne, kisha sonyo kali likafuata, “Acha ujeuri, usibishane na Mkuu!” Yule mtu wa pili akamaliza alilolifanya.

“Yote yatarudi kama usiponiua sasa!” madam akamwambia Yule bwana.

Jasmine akaletwa ndani akiwa na kamba mikononi na tambala chafu lililoshindiliwa kinywani, akasukumiziwa mle chumbani.

“Wawili wameshakufa,” Yule bwana aliyezungumza mwanzo akamwonesha picha ya mwili wa Scoba. Madam S akaangusha chozi, “Hakika mtalipa roho ya huyo mtu kwa gharama kubwa!” akalalama.

“Never!” Yule bwana akajibu.

Madam S akamtemea mate usoni, “Never say never again!”.

“Huyu mwanamke jeuri mpeni disprini kwanza!” amri ikatolewa, umeme ukawashwa na shoti zikamchapa Madam S takriban sekunde thelethini.

“Stop!” ikatolewa amri ya pili, umeme ukazimwa,

“Nilishawaambia, ukifuata nyayo zap aka utapotea, sasa ninyi ni manunda na sasa mtapotea hakika,” sauti yenye lafudhi ya kihindi kwa mbali ikasikika kutoka kwenye soksi jeusi lililomfunika mtu huyo.

“Haya nataka password ya hii kompyuta!” ile sauti ya kihindi ikaendelea. Alipoichukua ile kompyuta kutoka kwa kijana mmoja ndipo Chiba alipoiona kwa uvunguni na kugundua kuwa kompyuta ile si yenyewe, akamtazama Madam S, akajikohoza mara tatu kwa mtindo wa pekee, Madam akaelewa kuwa ule ni wito akamtazama Chiba, Chiba akayazungusha macho yake kwa namna ya ajabu huku akibana na kuachia kope zake, Madam S akaelewa anachoambiwa kuwa kompyuta ile ni feki.

Akawatajia password ya hiyo kompyuta, wale jamaa wakaanza kuifungua, ilipoanza kufunguka wakafurahi sana na kuondoka zao.

“Tunarudi muda si mrefu kuwaua!” mmoja wao akasema.

Wakaondoka zao.

KITUO CHA POLISI KATI –saa 11 alfajiri.

KIPIGO alichokipata Ravi Kumar kutoka katika mikono ya vijana wataalam wa kazi hiyo alitapika kila alichokijua juu ya sakata hilo, ingawaje alionekana vingi hafahamu lakini alimtaja mshirika wake mkubwa aliyekuwa akimpa maagizo ya kupeleka Gerezani au kuchukua na kuleta kwake, huyu hakuwa mwingine ni Pancho Panchilio.

“Kwa hiyo Pancho ndiye alikuwa anakutuma?” kamanda akauliza.

“Ndiyo kabisa yaani, ni jeje huyo, lakini mimi sijui nini alikuwa anaadika,” akajieleza.

“Pancho anaishi wapi?” akauliza Kamanda.

“Mimi mtaniua, sijui naishi wapi najua ofisi yake tu,” Ravi akajibu huku akilia na damu zikimtoka kinywani na puani.

“Na huyu Mke wa Mahmoud umemjuaje?” kamanda akauliza.

“Huyu manamuke bana, nilikutanishwa na jeje tu,” akaeleza.

“Sasa yuko wapi?” swali linguine.

“Aliniaga anaenda Zanzibar na atarudi jumamosi hii,” akajibu.

“Zanziba sehemu gani?”

“Mimi hapana jua jamani, mambo ya familia hayo!” akaanza kulia.

Kamanda Amata akaanza kupekuwa simu moja baada ya nyingine za wale wafanyakazi, ndipo katika simu ya msichana wa kazi alipokuta ujumbe mfupi wenye maagizo Fulani kuwa mtu yeyote akiuliza aseme mama huyo kaenda Zanzibar lakini alipochunguza haraka kwa makampuni ya simu aliambiwa namba hiyo mara ya mwisho ilikuwa ikisoma eneo la Laskazoni Tanga.

Kamanda Amata akaagiza kwa Inspekta Simbeye kuwa huyo mama akamatwe mara moja, simu ikapigwa Tanga, kituo kikuucha polisi, masako wa panya wa kimya kimya ukaanza.

“Kamanda Amata,” Simbeye akaita, kisha akampa ishara ya mkono kumwita pembeni.

“Vijana wangu wawili wameuawa eneo la Klabu ya Mbowe! Masaa matatu yaliyopita,” akamnong’oneza.

“Pole sana Inspekta, walikuwa kazini, wamekufa kishujaa, na muuaji atapatikana tu!” kamanda Amata akajibu na kutoka kituoni hapo.

4

JOKI alitulia mezani kupokea taarifa zote za vikosi kazi walivyovituma kuwasaka watu hao, vikosi vinavyoongozwa na wapiganaji hodari kuanzia makabiliano ya ana kwa ana na hata yale ya silaha za kila aina. Alishangaa tu kuwa muda unakwenda lakini hapati jibu lolote juu ya kupatikana au kuonekana kwa Kamanda Amata ambaye nguvu zote walikuwa wameelekeza kwake, isitoshe ilikwisha amuriwa kuwa akipatikana wala haina haja kumleta na uhai wake bali ni kumuua kwa vyovyote vile.

Aliitazama saa yake, pambazuko lilikuwa kwenye miimo ya mlango ulio mbele yake. Wamepatwa nini hawa? Mbona muda umetutupa mkono! Alijisemea kwa sauti ndogo iliyotosha kujisikia yeye mwenyewe. Kichwa kilikuwa kikimzunguka kila mara alitamanai kuinua simu awapigie kuliza lakini alikumbuka kuwa makubaliano yao hayakuwa hivyo bai wao wakikamilisha kazi watampigia simu kama walivyofanya kwa wengine wote.

Akiwa katika kuwaza, simu yake iliita, akaiinua na kuiweka sikioni akiwa na shauku ya kujua nini kimetokea katika msakao huo.

“JoKi !” sauti iliita kisha ikakata.

“Sema, mmekamlisha kazi?” akauliza.

“Hapana JoKi, muda tulioupanga kukamilisha kazi umepita, lakini hatujafanikiwa kumpata Yule hayawani, tufanyeje?” Mkuu wa kikosi cha kwanza akajieleza.

JoKi akatulia kimya kwa fungu la sekunde, akashusha pumzi na kuitoa simu sikioni; tayari alikuwa amesahau anaongea na nani, akakumbuka, akajicheka na kurudisha simu sikioni.

“Subiri kidogo, nitakupa jibu,” JoKi akajibu. Akaitua simu chini na kuhisi kuchanganyikiwa, akabofya namba Fulani na kusikiliza. Naima alikuwa upande wa pili.

“Yes JoKi!” akaitikia.

“Niambie mmefikia wapi na harakati?” JoKi akauliza.

“Bad! Very bad! Huyu jamaa kwanza keshaua mtu mmoja, nimepambana naye lakini Polisi wameharibu muvi, kanitoroka,” akaeleza.

JoKi akapiga ngumi mezani baada ya kujua uwa keshapoteza watu wane katika harakati zake.

“Shiit!” akang’aka, “Unamwonaje?” akauliza.

“Mtepetevu, simshindwi hata kidogo, nab ado namsaka kwani amenijeruhi,” Naima akajigamba. Baada ya kuongea na Naima akapigia kikosi cha tatu nacho majibu ni yaleyale kuwa mtu huyo hajaonekana. Ni Naima peke yake aliweza kumwona na kupambana naye japo kwa sekunde chache. JoKi akatoa maagizo kuwa vikosi viwili vibaki kazini na kikosi kimoja kirudi kambini kwa ajili ya kutekeleza majukumu mengine. Kati ya vikosi viwili vilivyobaki kumsaka Amata kikosi cha Naima nacho kilikuwamo.

Tayari giza lilianza kuuachia mwanga nafasi ya utawala, kwa pande zote mbili huo haukuwa muda rafiki kufanya makeke yoyote lakini haikuwa na jinsi. Pande zote mbili zilikuwa kazini kwa umakini zaidi.

JoKi aliwapanga watu wake vyema katika jiji la Dar es salaam kuwa popote watakapomuona Kamanda Amata wasifanye lolote bali waitaarifu ofisi nayo itajua nini cha kufanya ili kumaliza kijana huyo shababi.

§§§§§

KATIKATI YA JIJI LA DAR ES SALAAM-saa 1:02 asubuhi.

MITEGO MIWILI ilitegwa mahsusi kwa ajili ya Kamanda Amata, wakati huu wa jua hawakutakiwa kumuua ila walipewa amri moja tu ya kutoa taarifa kwamba kaonekana sehemu Fulani kisha kazi ya kummaliza ifanyike bila tabu.

Kikosi cha kwanza chenye watu wane kilikuwa jirani kabisa na jingo la JM Mall ambapo ndani yake, juu; ghorofa ya sita kuna ofisi ya AGI Investiment inayomilikiwa na Kamanda Amata kama Mkurugenza huku Gina akiwa kama Katibu wake, hapo ndipo hupangia mipango yote migumu na kuigeuza kuwa myepesi, nani afe na nani hasife, nani aokolewe na nani atoswe yote yalijadiliwa hapo kwa usiri mkubwa wakati leseni ya kampuni hiyo ni ya ufaulishaji mizigo bandarini.

Watu waliaanza kulijaza jiji, mishemishe za hapa na pale zilianza kuzikumba kona za jiji la Dar es salaam, jua nalo lilipanda angani taratibu likitokea pande zile za Kigamboni. Naima alikuwa ametulia katika moja ya mbao za magazeti akitazama habari nzito iliyobeba magazeti mengi ya siku hiyo.

…Mbunge wa Miroroso auawa kikatili nyumbani kwake Msasani…

Moja ya gazeti liliandika hivyo kwa wino mzito, watu walijazana kusoma habari hiyo, kila kona ya jiji liliongelewa hilo.

“Washamuua huyo! Nchi hii utaiweza!” mmoja wa madereva Tax aliropoka

“Ndiyo hivyo, hii nchi ya wenyewe hii, alikuwa anaongea sana huyu, washamtengeneza!” mwingine alidakia.

“Badala msikitike wapigania haki wanapotezwa nyie mnashabikia kwa maneno ya ajabu,” mara hii mshona viatu alimalizia.

Mazungumzo juu ya hilo yakatawala kila kona ya eneo lile, kufumba na kufumbua gazeti la Mbiu ya Mnyonge likapotea mbaoni, likaisha kabisa kwa kuwa liliandika vizuri habari hiyo.

Naima alisikiliza yote hayo, akakitazama kidole chake cha shahada cha mkono wa kuume akatabasamu na kusogea pembeni ya eneo hilo, aliwatazama vijana wake wawili aliobaki nao katika kikosi chake akawapa ishara kuwa mambo yako sawa.

Kamanda Amata alikuwa akisubiriwa katika maeneo yake muhimu ya kujidai, yeye hakuwa na habari ya lolote katika kuwindwa huko. Asubuhi hiyo alirudi nyumbani kwake japo kujiweka sawa na kuanza awamu mpya ya mapambano ya mchana, muda ulimpiga kikumbo, alipenda kuibuka kidedea kabla ya jogoo kuwika lakini akajikuta akikabiliwa na mambo mengi ya kiupelelzi ili kuwajua adui zake walivyo, lakini hakujuwa bado wamejipanga vipi, kitu kilichompa ujasiri siku hiyo, ni kule kuwa peke yake katika uwanja wa mapambano, kumbe hakuhitaji kutumia akili ya pili kumlinda mwingine; lakini pia alijua wazi kuwa nalo ni hatari ubwa kwani macho ya adui yake yatakuwa na kazi moja tu ya kumtazama yeye kila anaponyanyua wayo wa mguu wake. Aliegesha pikipiki lake mahala pake na kulizima, akatulia kusikiliza lolote kama lipo, ukimya ulitawala, hakuna jipya, akavua kofia lake na kulipachika juu ya kioo cha pikipiki hilo kisha yeye kujitoma ndani huku mkono mmoja ukiwa ndani ya jaketi lake.

Alipohakikisha kila kitu ni salama, akaingia chumbani mwake na kujiweka sawa kivingine.

Alipotoka ndani; alikuwa ndani ya suti ya kijivu iliyotanguliwa na shati la buluu bahari, akalielekea jokofu na kuchukua dumu la maziwa, akamimina kwenye kikombe kikubwa, soseji tatu nene pamoja na slesi kadhaa za mkate, vikapashwa kwa microwave na toaster.

Nje ya nyumba ya Amata kulikuwa na pub ya kisasa ambayo iliendesha shughuli zake saa saa ishirini na nne, asubuhi hiyo iliyokuwa na hali ya mawingu, bado watu wachache walionekana kuwapo eneo hilo ama wakiongea hiki na kile au wakipata supu ya kongolo. Hilo halikuwa tatizo kwa Amata, aliitoa gari yake nje na kuiweka sawa tayari kwa safari, akafunga geti lake kwa kutumia rimoti maalum kwa kazi hiyo.

Huku macho yake yakifanya kazi ya ziada ya kuatzama huku na kule akili yake ilipisha uamuzi wa kuhamisha tiba za Gina na Scoba kwenda shamba ili kuepusha lolote ambalo adui yake anaweza kulifanya, kwa maana kama ni watu aliyoawategemea basi ni hao tu. Aliingia kwenye gari yake aina ya Volks Wagen, au wengi mngependa kuiita Golf, akashusha kioo taratibu na kumtazama binti aliyekuwa akipita mbele ya gari yake. “Duniani kuna viumbe mwe!” akajisemea na kisha akaingiza gia namba moja na kuondoka taratibu, alipoumaliza wigo wa ile Pub, akatupa jicho kutazama kijia kile alichoingilia Yule mwanadada, akalisanifu umbo la msichana huyo kwa nyuma, lo; akashindwa afanye nini, akaodoa gari yake na kuikamata barabara ya KInondoni kuelekea daraja la Salenda, alipoikanyaga tu barabara ile na kwenda mwendo wa mita kama 200 hivi, akatazama kioo chake cha ndani na kuona gari nyingine nyeupe ikiingia barabarani kutokea njia ileile. Hakuitilia shaka lakini alitaka kupata uhakika kama gari hiyo ana nasaba nayo au la.

Kabla hajafika kwenye makutano, akakunja kulia na kuingia ofisi za ubalozi wa Uswizz, akaweka gari katika maegesho yake, hakushuka. Akaiona ile gari ikipitiliza, hapo nay eye akatoa gari yake na kurudi barabarani, alipokunja kulia hakuiona ile gari, akajua hisia zake hazikuwa sawasawa, akaingia barabarani na kuifuata barabara ya Bagamoyo mpaka Salenda na kukunja kushoto kuingia barabara ya Ocean kisha akaegesha gari yake kwa mbele kidogo akitazama kama kunayeyote anayefuatilia nyendo hizo. Alipohakikisha hakuna jipya, akakodi Tax na kuelekea Sea View.

“Nishushe hapa!” akamwamuru dereva Tax kisha akamtupia not ya 5000 na kutokomea zake.

§§§§§

DR. KHADRAI ALIKUWA BIZE NA MGONJWA WAKE, kama Mzuka Kamanda Amata akasimama katika mlango wa chumba hicho.

“Karibu Amata,” akamkaribisha kitini.

“Asante nimekaribia, anaendeleaje huyo?” akauliza mara baada ya kuketi kitini.

“Anaendelea vyema, ameamka ila bado fahamu hazijamrudia, lakini si muda mrefu atakuwa sawa, lakini, Amata, huyu atatakiwa kupumzika kama miezi mitatu hivi asifanye shughuli za mikiki mikiki,” akaeleza.

“Ok, umeeleweka kabisa. Sasa Khadrai ipo hivi, hali ya kiusalama sio nzuri sana, na nimekuja hapa kwa jambo moja tu,” Kamanda akainuka kitini, na kuliendea dirisha kubwa la aluminium na kuchungulia nje, akaiona ile gari ikiegeshwa mahala Fulani jirani kabisa na lile jumba la Khadrai, akarudi na kusimama karibu kabisa na daktari huyo, “Sikiliza, wewe na huyu Gina nitawapeleka Safe House, leo hii, kila kitu kipo kule utatumia ofisi ya Dr. Jasmine”.

“Ni wapi huko?” Khadrai akauliza.

“We jua ni Safe House, iko wapi hilo sio swali kwa sasa, haya mwandae mgonjwa wako kwa safari, ukiwa tayari unambie, nitatumia gari yako pia,” akamwambia huku akitokea sebuleni, ukimya wa jumba hilo ulibaki hivyo hivyo, akatzama huku na huko, akachomoa bastola yake ndogo kabisa na kuiweka sawa, akavuta hatua kuuelekea mlango wa kutokea nje, akabana dirishani kutazama.

Mlinzi wa geti aliliendea kufungua baada ya kusikia mbisho, Kamanda akatulia palepale akitazama huku bastola yake ikiwa tayari kutekeleza itakaloamuriwa. Yule mlinzi akafungua geti, mtu mmoja akaingia ndani akifuatiwa na wengine wawili, alikuwa amevalia suti nyeupe kabisa na wale wenzake vivyo hivyo, hakuwa Mtanzania, wala hakuwa Mwafrika, kutoka pale dirishani Kamanda Amata akajihisi kupata ubaridi wa ghafla.

“Smart Killer!” akajisemea, kisha akarudi ndani kwa Daktari Khadrai.

“Kaeni humu, msitoke nje wala kuchungulia,” akarudi sebuleni, na kukuta wageni wake wakiujia mlango mkubwa wa nyumba ilhali mlinzi anagalagala chini pale getini.

“Haina haja ya kutukaribisha,” Yule mtu aliongea kwa Kifaransa safi huku wale wenzake wakiwa kimya na mikono yao wameifumbata ndani ya makoti yao, Yule bwana mkubwa alijishika kiuno na kuyaachia mabastola yake waziwazi yakining’inia.

“Karibuni, karibuni viti,” akawakaribisha huku yeye akikiendea kimoja ya viti hivyo.

“Hatuna haja ya kukaa! Tumeshakaa sana kwenye ndege tuliyokuja nayo!” tunataka kitu kimoja tu hapa na tunaondoka na ndege ya saa tano,” Yule bwana akajibu kijeuri huku akichomoa bastola moja na kuifunga kiwambo cha sauti.

“Kitu gani?” Amata akauliza.

“Roho, roho yako inayokutia ujeuri ndiyo tunayoitaka sisi!” Yule bwana akaeleza, huku akiwa tayari kainua bastola yake na kuielekezea katika paji la uso la Amata. Uongo wa Amata ulikuwa ukifanya kazi kwa kasi ya ajabu kuliko kawaida yake akitazama huku na kule kwa kuzungusha macho, akiwatazama wote watatu na kuuona kwa haraka haraka uhatari wa viumbe hao waliovalia sare mpaka mtindo wa viatu vyao ulikuwa wa kipiganaji kabisa. “Kazi ipo, hapa ni kufa nakupona,” Kamanda akawaza.

§§§§§

KANAYO O. KANAYO ALIKETI KATIKA NUSU UKUTA akiangali mechi ya mpira wa miguu kati ya afungwa mashabiki wa Yanga na Simba. Nywele zilianza kupoteza mng’ao wake, ndevu zilizokosa mnyoaji mzuri anayeijua kazi yake nazo zilikuwa hoi, uzee ulinyemelea mwili huo ambao

ulikuwa wa kupendeza kwa mafuta na unyunyu wa gharama. Akiwa ametingwa katika kutazama mechi hiyo ambayo upande wa Yanga ulishinda 3-0 kama kawaida, alihisi kitu kikipenyeshwa kwenye kiganja cha mkono wake.

Ilikuwa kijikaratasi kidogo, akamtazama huyo aliyeifanya kazi hiyo, akamwona na kumbania jicho kisha akaifungua ile karatasi na kuisoma, alipomaliza, akaikunja na kuondoka zake.

Ndani ya chumba chao cha kulala chake cha kulala kilichokuwa na kitanda kimoja kidogo chenye tandiko tu bila godoro, aliketi kwa utulivu na kuingiza mkono uvunguni akachomoa bahasha ndogo na kuifungua ndani.

"…Kazi imeanza mtaani, tumekamata watatu, tumewaweka kwenye hali mbaya wawili, bado mmoja, Kamanda Amata.

Tumeleta Smart Killer kama mlivyoagiza, tukimmaliza yeye ndipo tutafanya plan B, kaa tayari kwa taarifa ya mapinduzi.

Mafisadi; kama wanavyotuita, tutaendelea kuwapo tu na tutaiburuza nchi kwa noti zetu.

Cheers!…"

Akaikunja ile karatasi na kuitia kinywani huku akitabasamu.

§§§§§

MAHMOUD ZEBAKI alitema karatasi iliyokuwa kinywani mwake na kuipachika uvunguni mwa kitanda chake, akatabasamu kwa tabasamu pana. Ijapokua ngozi yake ilikuwa kavu kwa kukosa japo Vaseline lakini bado ilionesha afya kwa mbali, jela ni jela tu. "Hawatuwezi hawa, tutaendelea kutafuna pesa tu, fisadi sio peke yangu kuna Magurubembe huko nje hawayajui, na kesi yetu tutashinda," akajipa moyo huku akisimama na kutembea hapa na pale.

Kesi ya matumizi mabaya ya madaraka na pesa za umma waliyoshitakiwa Mahmoud Zebaki, aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Uswizz na Kanayo O. Kanayo aliyekuwa Waziri katia Wizara nyeti ya Serikali ilikuwa ikiunguruma katika Mahakama ya Kisutu, kila mara iliposomwa iliahirishwa na watu hao kurudisha lumande. Wananchi wengi walilalamika kwani hawakuelewa kwanini kesi hiyo inapigwa danadana kiasi hicho, wakati Wananchi wakilalama kuwa watu hao 'wasulibiwe', walioshika mpini wanasema 'uchunguzi unaendelea'.

§§§§§§

Kama kuna kitu kilimuuzi Pancho Panchilio alipokuwa ofisini kwake ni kitendo cha kudanganywa juu ya ile kompyuta, alipoifungua akiwa ofisini mwake ilifunguka na kumuonesha picha moja tu ya fuvu lenye ujumbe chini yake 'Ni zamu yako kufa'. "Kama wao ni wajanja basi mimi ni zaidi, na ile kompyuta lazima niipate leo hii," akajiwazia huku mwili wake ukitetemeka kwa hasira. Aliinuka na kuliendea dirisha kubwa la kioo na kuitazama mandhari ya jiji la Dar es salaam, akasonya na kuichomoa bastola yake, alipogeuka alifyatua na kuisambaratisha ile kompyuta pale mezani, akairudisha bastola yake na kurudi kitini. "Fanya nililokuagiza, kumbuka sisi ndiyo tunaokulinda hapa nchini na hata nchi yako haijui kama upo hapa kutokana na makosa uliyoyafanya huko," aliyakumbuka maneno ya Kanayo O. kanayo siku alipokwenda kumtembelea gerezani.

"Lazima ufe leo Kamanda," akajisemea na kujibwaga kitini. Aliinamisha kichwa chake mezani huku mikono yake ikizitimua nywele zake za Kihindi kama anayetafuta kitu Fulani humo, kisha akakiinua ghafla na kutazama mlangoni. Akapiga ngumi mezani, akanyanyuka na kuibeba briefcase yake, akatoka mpaka kwenye ofisi ndogo ya katibu wake.

"Boss, mbona mapema?" Yule binti akauliza.

"Usijali, natoka, kuna kazi naenda kuifanya, nitarudi hapa kesho, aaah no hapana, naweza kuchukua hata siku mbili nje ya ofisi, nitakupigia baadaye," alikuwa akiongea huku akibabaika hapa na pale. Akatoka ofisini na kuiendea gari yake kabla hajapotelea mjini.

KITUO CHA POLISI CHA KATI- muda huohuo

INSPEKTA SIMBEYE hakujua nini la kufanya asubuhi hiyo, wingu jeusi lilikuwa limekigubika kichwa chake, alijua la kufanya lakini alishindwa kulifanya. Hapo ndipo moyo wake uliporudisha uamuzi wa kustahafu kazi hiyo, uamuzi ambao ulikataliwa pindi ulipowafikia wakubwa, ulikataliwa kwa sababu ya utendaji kazi wa kiumbe huyo alijulikana kwa cheo kama jina, Inspekta. Aliipenda kazi yake sana, hata baadaye akafanya kazi nyingi kwa kushirikiana na Idara nyeti za Usalama wa Taifa, alikuwa mpole, mnyeyekevu, msiri, mwenye huruma, lakini makini katika kazi na hakufanya makosa. Hakupenda kukumbatia ujinga wala upumbavu. Alikuwa mkufunzi wa mafunzo ya polisi wapya pale CCP na ndipo alipokuatana na Kijana Amata alipoingia mafunzoni.

Mara kwa mara alikuwa akimtazama kijana huyo mchangamfu kwa jicho la pekee, “Anafaa,” alijisemea huku akitikisa kichwa alipokuwa akishuhudia shabaha ya aina yake iliyokuwa ikilengwa mazoezini, wepesi wa kufanya michezo ya karate na kungfu, alivutiwa. Alimjua vema, vema sana na alimwamini kuliko unavyofikiria.

Alijiinua kichwa chake na kuitazama picha kubwa ya Mwl. Nyerere iliyokuwa imening’inia ukutani, “Tutakumbatia waovu mpaka lini ilhali wanajulikana walipo?” alijikuta akiiuliza ile picha bila kujua kuwa haiwezi kumjibu, akatikisa kichwa. “Usifanye lolote juu ya mtu huyo! Mwache kama alivyo mpaka oda ya juu itakapotoka,” aliikumbuka sauti hiyo iliyomfikia kupitia simu yake ya ofisini pale alipoomba kumkamata bwanyenye huyo aliyezaliwa India na kutarajia kufia Tanganyika.

Akasonya, akaisogeza kofia yake pembeni na kuinyanyua simu yake, akabofya zile namba unazozifahamu, akaiweka sikioni, tayari moyo wake ulipitisha maamuzi, kifua chake kilikuwa kikipanda na kushuka, “Nitajua la kumfanya!” alijiambia.

§§§§§

§§§§§

NYUMBANI KWA DR. KHADRAI

SIMU ya Kamanda Amata ikaita kutoka mfukoni mwake, Yule bwana aliyekuwa amemlenga sawia Kamanda Amata akijiongelesha kwa Kifaransa chake safi, akayumbisha jicho kidogo. Kama kuna kosa ambalo Kamanda Amata alikuwa akilisubiri lifanyike basi hilo lilikuwa haswa, ndilo lenyewe.

Aliipiga ile bastola kwa pigo la nguvu, ikachomoka mikononi mwa Yule bwana, kisha akamsukuma kwa nguvu na kuwapamia wale wawili wa nyuma, wakati huo Kamanda tayari hakuwepo eneo lile, alijirusha na kuviringika na kochi kubwa. Risasi takribani tano zilifumua kochi lile kisha utulivu ukafuata. Wale mabwana wakiwa na bastola zao mikononi mwao walitulia kama masanamu, hawakutikisika, Yule kiongozi wao alikuwa akihema, hakuamini anachokiona. Ni sekunde mbili hadi tatu tukio hilo lilikuwa limekamilika, akawapa ishara vijana wake waende kuangali upande wa pili wa kochi kama mtu huyo yuko hai au la.

Walitawanyika mmoja upande huu na mwingine upande wa kule, wakaenda mbali na kochi lile huku wakitembea bila kufanya ukelele wowote kwa miguu yao kutokana na viatu walivyovivaa.

Kamanda Amata alikuwa ametulia kimya huku lile kochi likiwa limemfunika nusu na miguu yake ikiwa nje ya kochi lile, lakini kiwiliwili kilifunikwa ndani yake, hakujitikisa alitulia tuli kabisa. Wale mabwana walipoona hali ile wakasimama kila mmoja upande wake, mmoja akashusha bastola yake na kuipachika mahala pake, kisha akachomoa kisu kidogo na kukirusha sawia kwenye mguu wa Amata, kikachoma kwenye ‘kigimbi’ kikatulia palepale. Kamanda hakutikisika japo maumivu makali yalimwingia moyoni. Akatulia tuli akiwacheza shere akisubiri wasogee kabisa eneo lile.

“Amekufa huyo!” Yule aliyerusha kisu aliwaambia wenzake kisha kila mmoja aliteremsha bastola yake na kukaribia eneo hilo. Ni nukta hiyo hiyo Kamanda alitumia nguvu zake zote akanyanyuka kwa kasi na aliuzungusha mguu na kumchapa ngwala mmoja wao, naye akajibwaga kama gunia la chumvi ya Uvinza, chali sakafuni, alipotaka kujiinua kiufundi alichelewa, kwani kwa jinsi alivyojizungusha Amata aliipiga tena mikono yake Yule bwana akarudi chini.

Yule kiongozi wao aliruka sarakasi ‘back’ baada ya kuona lile kochi likija kwake, kabla hajajipanga alisuhudia kijana wake aliyebaki akijishika koromeo, tayari kisu kikali kilichomolewa na Amata katika mguu wake na kurushwa kwa ustadi. Yule Kiongozi alipandwa na hasira, akaichomoa

tena bastola yake na kuiweka sawa kuua. Kama umeme Amata alijirusha na kuinuka kumuwahi Yule aliyeanguka, alipoona ile bastola inafyatuliwa alijikusanya chini na Yule jamaa kisha akamweka ngao na risasi tatu zilimfumua mgongo wake akabaki hana uhai.

Kitendo hicho kilimchukiza Yule Kiongozi wao, kwani alijiona bwege kwa kuuawa mbele ya macho yake watu wake anaowategemea kwenye kazi kama hizi. Aliilegeza tai yake na kuruka hewani kumwendea Kamanda Amata. Amata akajiweka sawa na kuandaa pigo la maana ambalo kusudio lake lilikuwa ni kupasua korodani lakini Yule bwana alikuwa mjuvi wa mambo, alijigeuza hewani na kutanguliza mikono, pigo alilolitoa hapo, lilimpeleka Kamanda Amata kwenye kabati la vioo na kujibamizapo. Vioo vilitawanyika eneo lote na vingine vilimwachia michuno ya hapa na pale. Hakupotea muda alijichomoa na kujiweka sawa. Yule mjinga alikuwa hafai, alitembeza kichapo kwa Amata na kuhakikisha kamnyongonyesha katika kila kona ya mwili.

“Shenzi sana, umeniulia watu wangu!” aliongea kwa ukali kwa lugha ya Kifaransa.

“Hata wewe utakufa!” Kamanda Amata aliongea kwa shida huku akijivuta kujiinua kutoka pale alipojibwaga.

“Nani wa kuniua? Nimetumwa kukuua wewe tu!” akaendelea kuongea kwa sauti lake baya la kukwaruza.

§§§§§

Dr. Khadrai aliposikia kishindo cha kabati kuvunjika na vyombo vyake kumwagika, alijikunyata kwenye moja ya kona ya chumba hicho, kisha vishindo vya kipigo kizito vilifuatia. Kishindo kile cha kabati ndicho kilichomshtua Gina na fahamu zake zikamrudia upya, akatzama huku na kule kwa mshangao.

Alipomtupia jicho Yule daktari hakuwa anamfahamu.

“Kuna nini? Hapa ni wapi?” akauliza haraka haraka, akajaribu kujinyanyua lakini maumivu yake makali yakamrudisha kitandani.

Dr. Khadrai akasimama huku machozi yakimtoka.

“Amata anauawa!” akajibu.

“What?” Gina akauliza kwa mshangao. Akatazama huku na kule kwenye trey ya daktari huyo akaona vikorokoro kadhaa vimejaa. Akateremka kitandani huku mkono wake mmoja ukiwa umejishika eneo lile alilopigwa risasi.

“Ah aaaaa! Tulia kitandani, wewe hali yako hii haitaki mikiki mikiki, utajiumiza Gina!” Dr. Khadrai alimsihi Gina huku akijaribu kumrudisha kitandani. Gina hakukubali.

“Wacha nife, lakini bosi wangu hawezi kufa ndani ya mita tano toka kwangu,” akajivuta mpaka kwenye kabati kubwa.

“Gina unataka kufanya nini?” Dr. Khadrai akauliza alipomwona Gina akipekua boksi na kutoa bomba la sindano, kisha akasogeza sogeza vitu vingine na kulifumania boksi lililokuwa na dawa za ganzi.

“Gina acha!” Khadrai alimwambia kwa sauti ya chini lakini ya ukali. Gina akamchana lile bomba la sindano, akaipachika sindano bombani na kuchoma kile kizibo cha ile dawa akafyonza yote na bomba likajaa, kisha akamkabidhi Khadrai.

“Nichome haraka sana!” aliamuru.

Dr. Khadrai hakujua la kufanya.

“Nyingi hii tuipunguze!” akasihi.

“We! Nataka yote hiyo, choma, muda unakwenda!” Gina aliamuru, Dr. Khadrai huku akijua kuwa afanyacho si sahihi kwani ile dawa ilikuwa nyingi sana, lakini afanye nini, akamdunga Gina katika eneo la jirani kabisa na lile jeraha lililokuwa limefunikwa kwa bandeji. Gina alitulia kama dakika moja tu na kuhisi eneo la jereha lake ni pazito na hapaeleweki, hakusikia maumivu tena.

Kishindo kikubwa cha mtu kujibamiza ukutani kilimshtua Gina, akachukua forceps na kuufungua mlango kwa nguvu, akajitokeza msambweni, kwa mbali alimuona Kamanda Amata akigalagala chini huku lile jamaa likiwa linajinadi kummaliza. Kishindo cha mlango kufunguliwa kilimgutusha mtu huyo, lakini alipogeuka tu forceps ilizama kwenye shavu lake. Kwa hasira, alimpiga ngumi mbili Gina na kumtupa upande wa pili, alimwendea alimnyayua na kumtupa chini, Gina hakuweza kujitetea, aliruka kiutaalamu na kusimama, pigo la kwanza alilipangua vizuri, la pili na la tatu, lakini la nne lilimchanganya na kupata kipigo cha mbwa mwizi.

Kamanda Amata akanyanyuka kwa hasira na kumwendea mtu huyo.

“Geuka huku mjinga wewe unaonea wanawake sio!” Kamanda akampa maneno ya kejeli. Yule bwana akageuka na kukumbana na makonde mazito ya Amata yasiyo na idadi, Yule bwana alijitahidi kuyapangua mapigo hayo lakini alijikuta anaelemewa. akaanguka sakafuni na mara akajiinua na kwa wepesi w ajabu akajirusha hewani akatawanya miguu yake kwa kufanya shambulio a ghafla lakini Kamanda Amata alikwisha iona hiyo, naye akajirusha juu kisha wote wawili wakakutana hewani. Guu la Amata likatua tumboni kwa Yule jamaa alipoanguka akafikia juu ya meza ya kioo na kuitawanya vipande vipande, Kamanda Amata akasimama kwa miguu yake miwili huku tayari akijipanga kimapigano, akavua koti lake na kulitupa pembeni, Yule bwana naye akafanya vivyo hivyo. Kamanda akafyatua vifungo vya mikono ya shati, na Yule bwana akafanya vivyo hivyo, Amata akajiweka sawa kwa Karate na yyule bwana naye akajiweka tayari, wakabaki wakitazamana.

Mchezo ukaanza, mapigo takribani kumi na tano kutoka kwa Kamanda Amata yalipanguliwa kitaalamu na hakuna hata pigo moja lililomfikia Yule muuaji. “Napambana na mjuvi,” akajisemea. Akajiweka tena sawa na kupeleka mashambulizi ya kasi na haraka, Yule bwana alikuwa mwepesi ajabu, aliyakinga kwa kasi ileile na kumnyima Kamanda hata nafasi ya pigo moja, wakatulia tena kimya.

“Come baby, sasa namaliza kazi yangu!” Yule muuaji alijigamba kwa KIfaransa chake, kisha akajitutumua na kumfuata Kamanda Amata kwa namna ya ajabu, pigo moja lilitua lilitua kifuani mwa Kamanda Amata, akayumba nyuma na kujibamiza ukutani, nukta hiyohiyo Yule bwana alikuwa akileta wayo wa guu lake kukanyaga ama kifua au koromeo, Amata akasubiri kucheza na sekunde ya mwisho, akabonyea chini na kujizungusha, akamchota ngwala moja maridadi, Yule muuaji badala ya kuanguka akaruka sarakasi na kusimama tena lakini kabla hajatulia alikutana na mapigo matatu ya karate kutoka kwa Gina yaliyotua sawia tumboni, Gina akaruka ‘shufan’ na kutua nyuma yake, pigo lingine maridadi likatua kweny uti wa mgongo. Yule bwana akasukumwa kwenda mbele na akajikuta akikumbana na Kamanda Amata kwa kichapo cha maana, shughuli nzito.

Alipoona anazidiwa kwa mapigo na mbinu aliamua uamuzi wa ajabu kidogo, “Llive today fight tomorrow!” alijisemea na kujirusha kwenye dirisha la kioo, akatua nje na kuruka sarakasi akauruka ukuta mrefu na kutua nje yake, akapotea.

Amata akatoka kasi ndani ya ile nyumba, akasikia gari ikiwashwa na kupigwa norinda, akatazama huku na kule, akaona Toyota Duet iliyokuwa pembeni, akaingia haraka kisha akampigia kelele Gina aliyekuwa nje hapo afungue geti, akatoka kasi na kukunja kulia kuifuata ile gari.

§§§§§

JoKi alichanganyikiwa kwa maana kila alipopiga simu kwa wageni wake simu yake haikujibiwa kabisa, alikuwa akizunguka huku na kule na simu yake mkononi. Baadae akapiga kwa Naima na kumpa taarifa ya watu hao, akamwomba Naima akae tayari kwa lolote litakaloamuriwa. “Kazi hii iishe mapema kabla serikali haijaamka,” aliyakumbuka maneno ya bosi wake, akajikuta akiuma meno kwa hasira na uchungu.

Akiwa kasimama nje, akitazama walinzi waliokuwa wakiendelea kuweka ulinzi wa ngome hiyo, alijikuta hana uamuzi, “Ina mana huyu mshenzi katuzidi kete? Maana muda wa kuwasiliana umefika lakini kimya,” aliwasiwasika moyoni mwake, moyo wake ukapiga kite kwa ukimya huo.

Kutoka katka mitego yake hakukuwa na taarifa ya Kamanda kuonekana mjini, taarifa alokuwa nayo ilikuwa ni kamanda kuonekana nyumbani kwake na kisha maeneo ya Sea View, akaelekeza nguvu huko kwa kukituma kikosi namba mbili kikiambatana na Smart Killer aliyekodiwa kutoka nchi za mbali akakamilishe kazi hiyo pa si na fujo.

Mara simu yake ikaita, akainyanyua na moja kwa moja alijua ni huyo jamaa yake akaiteguwa na kuitia sikioni huku akiingia ndani.

“Hello!” akaita.

“Hey JoKi, ile kazi imekuwa ngumu, vijana wangu wawili wameuawa na Yule mjinga ndani ya sekunde tatu tu, nimebaki peke yangu,” Yule muuaji akaongea harakaharaka akihema.

“Sasa uko wapi?” JoKi akauliza.

“Nimetoroka na gari nipo barabara ya Ocean, Yule jamaa hafai ni shetani,” akaeleza.

“Jitahidi umpotee urudi kisha tujipange kummaliza kwa shambulio moja hata kama itabidi kukodi B-52 itabidi,” JoKi aliongea kwa hasira na kuiendea simu ya mezani.

§§§§§

CHIBA aliendelea kulala palepale chini, fahamu zake zilikuwa zimerudi sawasawa lakini alijikuta nguvu za kufanya lolote hana, alimtazama Madam S, bado mnyororo uliotumika kumfunga ulimshika sawasawa, alionekana kachoka sana na mwili wake ulikuwa umetona damu hapa na pale. Chumba kilifungwa, lakini kwa nje kulikuwa na ulinzi mkali bila shaka. Alijaribu kujigeuza; bado alikuwa na hali mbaya alishindwa, akaendelea kulala pale chini huku akili yake ikianza kufanya mapambano na kufikiri jinsi ya kujiokoa kwani mpaka muda huo hakujua Kamanda ana hali gani na yuko wapi, kitendawili.

Ndani ya chumba hicho kulikuwa na kamera moja ya usalama iliyokuwa inaonesha matukio yote ya ndani ya chumba hicho na kusafirisha picha hizo moja kwa moja kwenye chumba cha usalama chenye luninga zinazoonesha jumba lote ndani na nje, hata sisimizi akipita wanajua na moja kwa moja mlinzi wa eneo husika hupigiwa simu ya upepo kuulizwa juu ya hilo. Kiujumla kulikuwa na ulinzi wa uhakika si wa kubabaisha.

Chiba aliitazama ile kamera kwa jicho upande, ilikuwa imetazama upande mmoja kwa muda mrefu, upande ambao Madam S alikuwa amefungwa. Mara nyingi kamera hiyo ilikuwa ikizunguka huku na kule kutazama chumba kizima. “Au opereta amelala?” akajiuliza moyoni na kutokuwa na jibu.

Aliitazama minyororo aliyofungwa nayo Madam S, akabaki kusonya kwa maana ilikuwa imefungwa kwa kufuli madhubuti kabisa, linalofungwa kwa tarakimu maalum; ujanja hakuna. Aliuma meno kwa hasira na uchungu, aliona wazi watu hao jinsi walivyowadhalilisha kwa kuwanyanyasa namna hiyo.

Mara akasikia mlango ukifunguliwa na vijana wawili wenye silaha wakaingia huku nyuso zao zikiwa zimefichwa kwa soksi nyeusi, kisha akafuatia mtu mwingine, yeye hakuwa na silaha yoyote lakini mwili wake uliositiriwa na fulana iliyombana ulionekana wazi jinsi gani mtu huyo alivyokuwa mwanamazoezi. Hakuongea, alionesha ishara ya kidole kwa Chiba, wale vijana wawili wakaweka silaha zao migongoni na kumfunika kwa mfuko mweusi kisha kumnyanyua Chiba kumtowa nje ya chumba kile huku wakimwacha Madam S akiwatazama bila kusema neno.

§§§§§

Kilikuwa ni chumba kingine chini ya ardhi, chumba ambacho kilikuwa kikitisha zaidi ya kile cha kuhifadhia maiti, damu zilikuwa zimefanya maua ya ajabu kwenye kuta zake nyeupe na hakuna aliyezisafisha, vitu kama vining’inizio na vitanzi vilikuwepo upande mmoja wa chumba kile. Chiba akatolewa ule mfuko usoni mwake na macho yake yakapambana na hali hiyo ya kuogofya ya chumba hicho.

Hewa nzito ilikijaza chumba hicho kilichokuwa na kila dalili za umauti.

“Karibu sana Kuzimu,” JoKi alimwambia Chiba mara tu walipomfunua lile limfuko, “Unaweza kukitalii chumba hiki ambacho kamwe huwezi kukiona mahala pengine zaidi ya hapa ulipo,” akamwonesha kwa mkono chumba hicho, “Na sasa utaona demo ya kazi ya chumba hichi kama ifuatavyo,” kisha akapiga kidole chake hewani.

Watu wengine wawili wakaingia na mtu aliyefungwa mithili ileile ya Chiba, akafungwa katika moja ya zile kamba karibu na ukuta, nyuma tu ya kichwa chake, ukutani, kulikuwa na damu iliyoganda, Yule mtu akavuliwa lile limfuko kama ilivyokuwa kwa Chiba, Chiba akamwona, akashtuka na kukodoa macho, hakuamini anachokiona.

“Usishangae! Na demo yetu itaanzia hapa!” JoKi akamwambia Chiba aliyekuwa kabaki kimya akitetemeka kwa hasira lakini bado kamba zilimdhibiti na hakujua la kufanya.

§§§§§

SCOBA alifumbua macho, akili ikamrudia na kujikuta kwenye kitanda cha hospitalini, linga ikiwa pembeni na chupa ya maji ikiyatiririsha kwa matone madogo madogo yaliyokuwa yakitembea ndani ya mrija mrefu wa plastiki na kuingia mwilini mwake kupitia sindano iliyochomwa kwa ufundi kabisa katika mshipa wa mkono wake. Macho yake yakanyanyuka na kutamtazama huyo aliyesimama jirani yake ambaye alimwona miguu tu pindi alipokuwa akiangalia ule mrija wa maji ulioingia mwilini mwake.

Mubah alikuwa amesimama akiwa ndani ya suti yake nyeusi ya mikono mifupi au mimi hupenda kuziita ‘suti za mbao’.

“Scoba!” Mubah akaita. Muba akamtazama usoni hakuwa anamjua mtu huyo, “Usihofu, akampoza na kumwonesha kitambulisho chake, “Niko upande wako, nimekuja kukuchukua, vipi una nguvu za kutosha?”

“Yeah! Niko fiti, hawa washenzi hawajaniumiza ila tu walinipiga na kitu gani sijui kichwani wakanipotezea network,” Scoba akajibu. Mara muuguzi mmoja waliyevalia mavazi rasmi ya kiuguzi akiongozana na daktari aliyevalia kijeshi na juu yake kujitupia koti kubwa jeupe, walikifikia kitanda cha Scoba.

“Hauna majeraha, wala hakuna mfupa wako uliovunjika, hatuna budi kukuruhusu ila unatakiwa utumie dawa kali za maumivu,” Yule daktari akamwambia Scoba huku akiwa anaandika andika vitu Fulani, kisha akararua ile karatasi kutoka kwenye faili lake na kumpa Mubah. Muuguzi akaondoa ile sindano mkononi mwa Scoba.

“Simama!” akamwambia.

Scoba akasimama kwa tabu kidogo alipokuwa wima, akashika kichwa, akayumba kidogo kisha akasimama imara, akajinyoosha mwili; uko fiti. Akapiga push up kama kumi na tano hivi kisha akasimama imara, akachukua vidonge viwili kutoka kwa Yule Muuguzi na kuvimeza.

“Baada ya dakika thelethini waweza kufanya lolote, utakuwa poa!” Yule Muuguzi akamwambia huku akiondoka.

“Asante kwa ukarimu wako mrembo,” akamshukuru huku akimwangalia na jicho lake kutua kwenye nyama za nyuma za binti huyo aliyejaliwa shepu, “Mwe!” akajikuna kichwa, kisha wakaondoka.

4

OFISI ZA USALAMA WA TAIFA- Saa 3:20 asubuhi

KIKAO KIZITO CHA IDARA ya Usalama wa Taifa kilikuwa kikiendelea ndani ya ofisi hizo, kila mtu alipigwa na butwaa kwa taarifa alizokuwa akizipata kutoka kwa Hosea. Ilikuwa ni asubuhi na mapema tu walipoitwa kutoka kwenye kona zao tofauti za kazi zao na kukutana hapo. Mara hii Scoba aliungana nao katika kikao hicho.

“Mpaka sasa ni huyu ambaye anaweza kutujuza juu ya watu hao! Kamanda Amata alikuwa hapa lakini na yeye haelewi watu hawa ni akina nani, anajaribu kupambana kiume kutegua kitendawili hiki, labda Scoba mwenyewe atueleze kilichompata kwa kifupi, kisha tuchukue hatua ya haraka,” Hosea akalieleza jopo.

Scoba akajikohoza kusafisha koo kisha akafungua kinywa kueleza mkasa uliomkuta.

SAA 16 ZILIZOPITA – Mtaa wa SHABAN ROBERT

Scoba aliegesha gari yake kandokando ya barabara hiyo mahala ambapo Tax nyingi huegeshwa, akateremka na kuliendea benchi ambalo madereva wa kijiwe hicho hukaa kusubiria wateja huku wakinywa kahawa na kupiga soga kama kawaida yao.

Akiwa ametingwa na mchezo wa draft aliyokuwa akiucheza na mwenzake huku wengine wakishangilia. Mara karibu kabisa ya mguu wake aliona mguu mwingine uliovikwa kiatu cha kike ukisimama na kumkanyaga kidogo, linguine lililomshtua ni ukimya uliofika ghafla.

“Aaa mrembo huyo! Karibu bibie,” sauti ya mmoja wa madereva ilisikika. Scoba akainua uso wake na kukutana na uso wa mwanadada, uso laini husio na chunusi, akashusha jicho mpaka kifuani, lo; kifua kilijaa sawia, matiti madogo yaliyobanwa na sidiria ya kisasa yaliongeza utamu na kusisimua mwanaume yeyote rijali.

“Twende!” Yule mrembo akamwambia Scoba.

“Na mimi?” Scoba akauliza.

“Ndiyo na wewe, nataka gari yako mie, maana we wajua kuendesha vile nitakavyo,” Yule mrembo akamwambia.

Scuba akanyanyuka na kujipukuta vumbi katika makalio yake,

“Haya mama twende kama wanitaka mimi,” wakaondoka na kuingia kwenye gari.

“Waitwa nani mrembo?” Scoba akaanza uchokozi.

“Naima,”

“Waoh, una jina zuri sana,”

“Kwa nini?” Naima akauliza.

“We huoni? Hata maana yake tu, mtu mwenye nguvu na uwezo mkubwa wa fikra ndiyo maana ya jina Naima, so sweet!” Scoba aliendelea kuonge huku akiingiza gari barabarani.

“Asante; twende Magomeni kuna watu wangu pale kisha utupeleke Kijiwe Samli tuna shughuli kule, leo nitakukodi siku nzima, shing’ ngapi?” Naima akauliza huku akiuvuta mkoba wake na kufungua zipu, maburungutu ya noti yalikuwa yamelala kimya.

“Kwa wewe mrembo sikuumizi, nipe Laki moja tu,” akamwambia.

“Haina tabu, nitakuongezea na hamsini,”

Wakakamata barabara ya Samora mpaka kwenye mzunguko wa Picha ya Askari, moja kwa moja wakapita Maktaba na kuikamata ile ya Morogoro mpaka Magomeni.

“Ingia Mapipa, mtaa wa tatu!” Naima akamwelekeza, Scoba akafanya hivyo, mbele ya nyumba moja iliyokwisha kwisha hivi akaegesha gari, Naima akateremka na kumwacha Scoba, akaingia kwenye ile nyumba. Baada ya dakika kama tano hivi akatoka yeye na vijana watatu, wakaingia garini, wale vijana wakaketi nyuma na Naima akaketi mbele.

“Kijiwe Samli,” akamwambia Scoba. Scoba aliwatazama kwenye kioo cha ndani wale vijana ambao hata kusalimia hawakusalimia, nywele zikamsisimka, akaihisi hatari mbele yake, akawasha gari na kuondoka zake. Wakiwa barabara ya Nyerere kuelekea maeneo ya Vingunguti mmoja wa wale vijana akawaambia wenzake kuwa kabla ya kwenda kwenye shughuli yao basi wapiti japo wapate mbili mbili, wakafanya hivyo, wakakunja kulia na kuchukua barabara ya Kiembe Mbuzi.

Kizota Pub.

“Egesha gari hapo,” mmoja wao akaamuru na Scoba akafanya hivyo. wakateremka na kuingia kwenye Pub hiyo, wakachagua viti na kuketi.

“Mwambie Angel kama kawaida,” kijana mwingine akamwagiza Mhudumu wa Bar na baada ya hapo vinywaji vikaletwa wakaanza kuburudika.

Iiwachukua dakika kama kumi natano hivi na kilamtu alikuwa kapata mbili, wakanyanyuka kuondoka.

Scuba alipokuwa katika usukani aliana kuahisi macho mazito, alijaribu kuyafungua lakini yalimuwia mazito, akaanza kupoteza umakini barabarani, aliendelea kupambana na hali ile lakini ikawa ngumu, akaegesha gari pembeni.

“Vipi?” Naima akamwuliza.

“Mmenipa nini nyie? Nyie majambazi ee?” akaongea kwa shida sana kwani kinywa chote kilimuwia kizito. Mlango wa nyuma ukafunguliwa, kijana mmoja akashuka na kumtoa Scoba kwenye usukani akaketi yeye, Scoba akawekwa nyuma mtu kati.

“Tueleze Madam S anaishi wapi?” swali hilo lilimrudishia akili Scoba ghafla, akawatazama wale vijana huyu kisha Yule.

“Ninyi mnamjua Madam S?” akawauliza.

“Hatuna muda wa kujibu swali lako, jibu swali letu,” Sauti ya mwingine ikasisitiza.

“Siwezi kuwajibu swali lenu,” Scoba alijibu kwa dharau.

“Unajifanya nunda siyo, kumbuka tuko wane hapa, tutakumaliza,”

“Hata mkiwa kumi au ishirini, siwezi kuwaambia,” akaendelea kuwadindia zaidi. Tayari ile gari ilikuwa ikiuwacha mji na kuelekea Gongo la Mboto. Domo la bastola likatua kwenye ubavu wa Scoba.

“Tulia, ukileta ujeuri wako tu nakumaliza,” akaambiwa. Scoba hakusubiri, alimshindilia kichwa Yule mwenye bastola, akamtindika ngumi huyu wa pili, vurugu ikaamka kwenye gari. Yule jamaa aliinua bastola lakini kabla hajafanya lolote mkono wake ukadakwa na bastola ilipofyatuka ikapita sentimeta chache kutoka kwa Naima ambaye ilibidi alalie upande wa dirisha, na ile risasi ikapasua kioo cha mbele. Dereva akayumba barabarani na kuitoa gari nje akasimama.

Naima aliachia pigo moja kali la ‘pigo la kifo’ lililotua sawia katika uso wa Scoba, akageuka huku akipiga yowe la uchungu, pigo la pili likatua shingoni na kumfanya Scoba kutepeta. Yule mwenye bastola alamshindilia pigo la kisogoni kwa bastola yake Scoba akazimika.

Kila mmoja alikuwa anathema kwa shughuli hiyo ya sekunde chache.

“Amekufa?” mmoja aliuliza.

“Akaongee na babu zake, mtupeni vichakani huko,” Naima akaamuru na Scoba akashushwa na kutupwa katika chaka.

§§§§§

SCOBA alimaliza kusimulia mkasa uliyompata, kila mmoja alisikitika sana na hali hiyo, minong’ono ikachukua nafasi kati yao.

Hosea akajikohoza na kurudisha ukimya kwa namna hiyo, “Ok, sasa nataka tuingie kazini ili kuwapata hao watu laeo kabla jua halijazama,” akatoa amri. Wakiwa bado katika kikao icho mara simu ya mezani katika chumba cha mikutano ikachukua uhai. Hosea akaipokea na kuiweka sikioni.

“Mkuu, katika barabara ya Ocean kuelekea Ikulu – Magogoni kuna gari zinafanya fujo,” ilikuwa sauti ya Avanti aliyekuwa katika chumba cha mawasiliano cha Teknohama. Baada tu ya taarifa hiyo jopo zaima likanyanyuka likimfuata Bwana Hosea na kuelekea kwenye chumba hicho kutazma hicho walichoambiwa.

Katika luninga kubwa kulikuwa kukionesha ramani ya jiji la Dar es salaam na kuonesha maeneo yote muhimu kwa ajili ya usalama wa Taifa. Zilionekana gari mbili zikielekea Upande wa Ikulu kutokea Hospitali ya Ocean Road.

“Zuia haraka, point namba mbili ifanye kazi tafadhali!” Hosea aling’aka na muda huo huo Avant aliinua kitu kama simu na kukiweka sikioni kisha akaboinyeza tufe Fulani na kuongea maneno machache, akatulia.

Bado macho hayo yote yalikodoa bila kufumba yakiangalia tukio hilo, hakuna aliyejua ni nini kinaendelea. Scoba alitulia akitazama kwa makini, akapenya katikati ya watu na kusogea karibu na Avant.

“Naomba nione picha inayowezekana tafadhari,” akamwambia Avant, naye akafanya manuva Fulani kwenye mashine yake wakaweza kuona vipande vya picha za magari hayo, Scoba alitazama kwa makini.

“Unaitambua hiyo gari?” Hosea akamwuliza.

“Yeah, kama sikosei hii Toyota Duet ni ya dada mmoja hivi ana uhusiano na Kamanda Amata, huyu dada ni daktari pale Agha Khan na huwa wakati mwingine tunamtumia kwa hili na lile, anaishi Upanga Sea View,” Scoba alieleza.

“Kamanda Amata,” Hosea akanong’ona, kisha akawaangalia watu wake, “Namtaka huyo anayefukuzana na Amata sasa hivi!!” akatoa amri na kuondoka mle ndani huku akiweka sawa miwani yake. Maafisa wale wakatazamana kisha mmoja akawapa ishara ya kutoka katika chumba kile.

“Ili tufike haraka eneo lile kwa foleni za Dar lazima tutumie njia ya anga, Chopa tafadhali, Scoba twende zetu,” afisa mmoja aliyeonekana kuwa na cheo cha juu kati yao alitoa amri hiyo, Scoba akakabidhiwa nafasi ya kuliongoza dude hilo, pamoja naye watu wengine wawili walikwea ndani yake wakiwa wamekamilika, bunduki ndogo na kubwa zilihusika, mashine ikanyanyuka.

§§§§§

Barabara ya Ocean ilikuwa imekumbwa na taharuki, Kamanda Amata, mwili wake ukiwa unavuja damu hapa na pale alikuwa akiendesha Toyota Duet kwa mwendo wa hatari akiifukuza gari ya mbele yake ambayo ilionekana wazi kuendeshwa na mtu anayeijua kazi yake. Ovateki zilizokuwa zikifanywa na huyo jamaa ni za hatari mpaka kila mtu alikuwa akishika kichwa kuhofia maisha ya hao walio ndani ya vyombo hivyo.

Walipokaribia njia panda ya Gymkhana na Ocean Road; Kamanda Amata akazipita gari mbili na kuingia upande wa kulia, baada ya kuisoma akili ya adui yake kuwa atapinda upande huo, hakuwa mbali na mawazo ya mtu huyo, gari zile zikakutana katikati ya njia panda na kusababisha ajali mbaya iliyohusisha gari kama nne hivi. Gari ya Kamanda Amata kutokana na udogo wake ilijifinya chini ya Land Cruiser Hard Top.

Gari aliyokuwa akiitumia Yule jamaa baada ya kukutana na ile ya Amata, alijaribu kuikwepa akajikuta akiingia katika ukuta wa Hospitali na ukuta ule kuvunjika vibaya. Mguu wake ulikuwa umenasa chini kwenye pedo, alijitahidi kuutoa na kufanikiwa. Akajivuta na kutoka nje kwa kupitia dirishani.

Kamanda Amata naye akajitoa taratibu huku mwili wake ukivuja damu. Kama kawaida ya Watanzania kama kawaida yao wakaanza kujazana, vibaka nao wakitafuta bahati yao, Kamanda Amata alijitupa nje na kudondokea barabarani.

Yule bwana alitazama huku na kule na kuona kundi la watu likija kwenye eneo la tukio, sura yote ilijaa damu, nguo alizovaa hazikutamanika. Mngurumo wa helkopta ndiyo uliomfanya aamue aliloamua, alitazama juu na kuona helkopta hiyo ikisogea eneo hilo, katika mlango wake mtu mmoja aliyevalia suti nyeusi akiwa kakamata bunduki yenye nguvu,

“Nimekwisha!” akajiwazia. Kitendo bila kuchelewa alichomoa bastola yake na kupiga tanko ya mafuta ile gari yake.

Mlipuko mkubwa ukatokea na gari kadhaa zilizokuwa eneo hilo zilishika moto, moshi ulitanda eneo lote, kelele za watu zikasikika huku na kule. Kamanda Amata akaenda pembeni kabisa na kuanza kutazama wapi adui yake alipo. Haikumchukua muda kumwona mtu huyo akiwa anatoroka kwa kujichanganya na watu.

“Shabash! Huwezi kunitoroka,” akasema kwa sauti ndogo, akavuta hatua na kuyapita magari matatu yaliyokuwa yamejibana hapo, akatokea upande wa pili na kumwona adui yake akipotelea katika kundi la watu. Kutokana na wingi wa watu ilikuwa ngumu kupenya eneo lile, akafikiri kwa haraka kuwa hapo ni kutumia plan B ili kumpata, lakini kabla hajatekeleza hilo. Gari ya polisi ilifika eneo hilo kwa mbwembwe na walipofika tu waliteremka haraka wakiwa na bunduki zao mikononi, mara moja walimwona Yule mtu aliyekuwa akijichanganya na watu.

Inspekta Simbeye akiwa na bastola yake mkononi, akatoa amri mtu huyo akamatwe mara moja, lakini mtu Yule naye hakuwa tayari kukamatwa namna hiyo, alichomoa bastola yake na kupiga risasi mbili hewani na kufanya hali ya taharuki mahala pale, baada ya kupiga hewani ile risasi, akashusha mkono na kufyatua tena, risasi ile ilimkosa mlengwa ikampata mmoja wa raia aliyekuwa eneo lile na kumjeruhi, hapo ndipo hasira za wananchi zilipopanda, walimvamia Yule bwana bila hata kujali polisi waliopo, walipiga na kupiga mpaka mtu Yule akapoteza uhai.

Ile Chopa ikateremka taratibu na kujiegesha pembezoni mwa ufukwe wa bahari, vijana watatu Smart Guys wakateremka na kuifikia ile maiti iliyopigwa vibaya na wananchi, Scoba aliteremka pia huku akiacha dude lile likiunguruma kwa hasira, Inspekta Simbeye na vijana wake wakawasili.

“Shiit!” akafoka Simbeye, “Siyo Mtanzania huyu!” akamalizia.

Akainua uso na kuangaza huku na kule wakatia huo tayari utepe wa polisi ulikuwa umezunguka eneo hilo na kuzuia Wananchi kufika hapo. Gari za zima moto tayari zilikuwa zikizima moto uliounguza gari takribani tano eneo hilo.

Kamanda Amata akatazama hali iliyokuwa hapo, akafikiria kama ajitokeze au la, lakini hiyo huwa si kawaida yake, alipigwa na bumbuwazi alipomuona Scoba, “Ni yeye au nimechanganyikiwa?” akajiuliza, kisha taratibu akaondoka eneo hilo huku akijiweka sawa uso wake. Akapotea eneo hilo.

CHIBA alimtambua mara moja Yule mtu pale mbele, ni mtu a;iyekuwa akitafutwa kwa muda mrefu, kutoweka kwake kulisababisha maandamano makubwa ya waandishi wa habari, alikuwa mwandishi nguli wa habari nchini. Wananchi waliongea, katuni zikachorwa ikasemekana watu wa Usalama wa Taifa wamemteka na siku yoyote angeonekana akiwa hana macho, au meno. Au kucha.

“Kwa nini? Kwa nini walimteka na kumleta huku?” akajiuliza bila majibu.

“Unamjua huyu?” JoKi akamuuliza.

“Ndiyo namjua, na kwa nini mmemfanya hivi?” akamuuliza.

“Aaaaa ha ha ha ha, hii ni serikali kaka, ina Rais, Mawaziri, Wabunge, Wanausalam kama sisi na kadhalika, na ina maadui kama wewe. Nusu saa ijayo nawe nitakufanya hivi,” alipomaliza kusema hayo, risasi moja ilikipasua kichwa cha Yule mwandishi na kutawanya damu iliyonganyika na ubongo. Chiba alitetemeka kwa hasira.

“Jiandae, nitawapanga wote hapa na kuwa fumua mmoja mmoja huku nikitengeneza filamu ya kumbukumbu kama za wadi ya kusherehekea miaka mingapi sijui ya uhuru wa nchi yako,” akaongea kwa kebehi.

“Hicho ni kitisho!” Chiba akaunguruma kwa hasira.

“Kitisho! Kitisho ee,” JoKi alipomaliza hiyo sentensi, aliinua mkono kwa minajiri ya kumchapa kofi Chiba. Chiba aliigundua hiyo dhamira yake akasubiri kitendo hicho, kiganja cha mkono wa JoKi kilipolifikia shavu Chiba aligeuka ghafla na kukidaka kidole kimoja kwa kinywa chake, akakibana barabara kwa meno yake imara.

“Aaaaaaiiiiggggghhh!” JoKi alipiga kelele za maumivu, alijitahidi kuuchomoa mkono wake kinywani mwa Chiba lakini ilikuwa kazi bure, alitumia mkono mwingine kumpiga ngumi za tumboni na kwingine lakini Chiba hakukiacha. Wenzake walijaribu kumnasua lakini wapi.

“Mwache au la nakupiga risasi,” mmoja wao alimwambia Chiba. Lakini Chiba hakujali alizidi kung’ata na kung’ata, mishipa ya hasira ikiwa imedinda usoni na shingoni. Yule mlinzi alitumia kitako cha bunduki kumpiga Chiba mbavuni lakini Chiba hakuachia. Wakati JoKi akijitutumua kujinasua alimpiga kichwa kizito Chiba, Chiba akayumba na kuanguka chini kama mzigo kutokana na kamba alizofungwa.

JoKi akamtazama Chiba kinywani akona damu zikitiririka, mara chiba akatema kidole kutoka kinywani mwake, JoKi akajitazama mkono wake, hakuna kidole kimoja, hasira ikawaka huku akipiga kelele kama mtoto.

“Na bado ukiniua mimi wapo watakaokata miguu yako kwa meno!” Chiba akazungumza kwa gadhabu.

“Jeuri sana wewe, si ndiyo?” mlinzi mwingine akauliza huku akimpa bunduki mwenzake ili amwadhibu.

“Mtieni adabu Mwanaharamu huyo nakuja sasa hivi,” JoKi aliagiza kisha yeye akatoka huku damu zikimmwagika. Yule mlinzi alivuta teke kali kumpiga Chiba pale chini, Chiba akajizungusha na kumchota ngwala ya maana, Yule mlinzi alipiga mweleka na kudondoka chini akitanguliza kisogo, akatoa yowe la uchungu, Chiba akainua miguu yake iliyofungwa na kuitua kwa nguvu katika koromeo la mtu huyo.

“We mwache mwenzio! Mi nakuua!” mlinzi wa pili alimpiga Chiba kwa kitako cha bunduki aina ya Rifle na Chiba akatulia kimya, huku akimwacha Yule mlinzi akiwa hana uhai.

§§§§§§

Hali ya Gina ilibadilika baada ya jeraha lake kumwaga damu nyingi, Dkt. Khadrai alijitahidi kuona namna ya kumsaidia, hakuna na damu ya akiba nyumbani kwake kwani ni ni kinyume cha sheria. Akiwa bado hajui la kufanya, mlango ukafunguliwa, Kamanda Amata akaingia ndani, moja kwa moja akafikia katika chumba hicho cha matibabu na kumkuta Gina akiwa tena kitandani.

“Vipi dokta?” akauliza.

“Hali imebadilika, damu nyingi imetoka katika jeraha lake,” akajibu.

“Oh Come on Gina. Sasa tunafanyaje?”

“Hapa nikupata damu nyingine kumwongezea, haraka,” Khadrai akajibu huku bado akiwa hai hai kumsaidia Gina.

“Ita gari yenu ya wagonjwa!”

“Oh, nilisahau kabisa, asant kunikumbusha,” akachukua simu yake ya upepo ambayo madaktari wote wanazo kwa ajaili ya mawasiliano ya karibu kama inahitajika. Akaita gari na na kuagiza ije na damu kabisa.

Dakika kumi hazikupita gari ya wagonjwa ilifika eneo hilo, Gina na Dr. Khadrai waliingia na safari ya kuelekea Agha Khan ilianza kwa mbwembwe kama kawaida ya madereva wa gari hizo.

Gina alilazwa katika hospitali hiyo chumba maalum ambacho hakuruhusiwa mtu yeyote kuingia zaidi ya Dr. Khadrai tu na baadae alimjuza Amata kuwa Gina yuko mahala hapo.

§§§§§§

Kamanda Amata aliiacha hospitali ya Agha Khan na kuingia mtaani, akatembea mpaka barabara ya Ally Hassan Mwinyi, alipoona hali ya hewa ni ya utulivu, akachukua simu yake na kupiga namba ya Mkuu wa Usalama wa Taifa, Bwana Hosea na kumwuliza juu ya Scoba, akajibiwa kuwa Scoba yupo salama na anaendelea vyema.

“Ok, ninamwitaji sasa tuingie kazini kwa nguvu zote,” akamwambia Hosea.

“Haina tabu kwani huyu ni wa kwenu, mkutano wapi?” Hosea akauliza.

“Kanisa kuu la Mtakatifu Joseph dakika kumi baadae,” kisha simu ikakatika. Amata aliingia kwenye tax iliyoegeshwa jirani kabisa, na kuitaka impeleke mpaka JM Mall ilipo ofisi yake ya siri au tuiite ofisi binafsi.

Aliwasili katika jengo hilo mida ya kama saa sita hivi, moja kwa moja akaiendea mbao ya magazeti na kutazama nini kilichoandikwa. Habari zilikuwa zile zile za jana yake ila zilikolezwa wino tu. Akapita taratibu na kuuendea mlango mkubwa wa jengo hilo. Akasimama kidogo karibu na mashine za kutolea pesa, akatzama huku na kule, kila mtu alikuwa akiendelea na hamsini zake, akasogea pembeni na kubonya kidubwasha cha lifti, ilipofika akaingia na kuiamuru imfikishe ghorofa ya nne.

Alipofika ghorofa ya nne aliteremka na kwa kutumia ngazi alipanda kwenda ghorofa ya sita ambako ofisi yake ndipo ilipo. Akaufikia mlango na kusita kidogo, jicho lake likatua chini ya mlango, kulikuwa na ncha ya bahasha ikichungulia nje, akaivuta kwa vidole vyake na kuitazama. Ilikuwa bahasha nyeupe, ndani ilikuwa na kitu kama kadi ya kibiashara, akaitazama kwa makini sana, akataka kuichana, akasita, akafungua mlango wake na kuucha wazi, akatulia kidogo, kisha akaingia ndani na kutembea taratibu. Kila kitu kilikuwa kama alivyokiacha mara ya mwisho, hakuna kilichoguswa wala kusogezwa. Moja kwa moja akaiendea jokofu ndogo iliyokuwa hapo akafungua, akatazama chupa zake za kinywaji, akacheka kidogo kisha akafunga, ijapokuwa alikuwa na kiu lakini hakuchukua chochote baada ya kuona mpangilio wa zile chupa umegeuzwa kwani yeye na Gina walikuwa na mpangilio wao maalum.

“Kama mmeweka sumu mtakunywa wenyewe,” akawaza kisha akavuta droo yake na kupekua hapa na pale, akachukua saa yake ya mkononi na kuivaa, akachukua miwani yake yenye uwezo wa kurekodi picha mjongeo, kuona nyuma bila kugeuka, bastola yake ndogo kuliko zote inayotosha kwenye kiganja cha mkono akaipachika mahala pake.

Akalivua koti lake na kulitupia huko, akavua shati na kuvaa fulana nyeupe inayobana mwili kisha akarudishia kila kinachohitajika, akafungua kijikabati kidogo na kutoa kikoti cha Kodroy akakivaa juu yake, pesa kama shilingi za Kitanzania laki tano akazitia kibindoni. Akaiinua bastola yake na kuisukuma slide mbele nyuma, “Iko fiti,” akawaza na kuikubali, kisha akafyatua magazine na kuiweka mezani, akapanga risasi zake nane na kuirudishia mahala pake, akaislide tena na risasi moja ikatumbukia chemba, akailoki na kuitia mkandani.

Akatulia kwa sekunde kadhaa kisha akaamua kutoka kwa nguvu zote kwenda kumsaka mbaya wake ambaye mpaka nukta hiyo hakujua yuko wapi. Alitoka na kuufunga mlango nyuma yake, akaingia kwenye lifti kwa minajiri ya kuteremka chini, kabla mlango haujajifunga, kijana mwingine akawahi kuingia na kusimama jirani na Amata lakini kwa nyuma. Kamanda Amata aliichomo miwani yake na kuivaa kisha kumtasama kupita vioo vidogo vilivyo kwenye miimo ya miwani hiyo.

Yule kijana alikuwa ametulia tuli hasemi lolote lakini kwa jinsi macho yake yalivyokuwa yakipepesa, Amata akajua kuwa huyo si mtu mwema, akajiweka tayari kwa lolote kwani mwili wake kw muda huo ulikuwa ukichemka damu ukizingatia bado ndugu zake hakujua wako wapi, kitendawili.

Aiendelea kumtizama huku akiangalia tarakimu zinazobadilika kutoka kumi na tano na kuteremka chini kwenda G, akamwona mtu huyo akiingiza mikono ndani ya kijaketi chake, akajua nini kinataka kutokea, akajiweka sawa.

Lakini alikuwa anatamani kucheka kila akimtazama kijana huyo aliyeonekana kujawa na wasiwasi. Ilionekana katika kazi hizo huyu atakuwa ni mwanafunzi tu kwa jinsi asivyojiamini, Amata akanyoosha mkono na kubofya tarakimu zile kwa kuingiza namba kama sita hivi na lifti ikasimama ghafla. Yule kijana alitoa waya kwenye koti lake na kutaka kumkaba Amata.

Kamanda Amata hakupoteza muda, alimjifanya anaudaka ule waya kumbe ilikuwa ni danganya toto, alipiga kiwiko cha mbavu dogo akalegea, alimnyanyua kwa kumshika mikono yake na kupigiza upande wa pili, akambwaga chini hoi. Kisha akapiga goti moja na kuondo amiwani yake usoni.

“We ni nani?” akamuuliza.

“Mi-mi-mi ni-metu-mwa,” akajibu huku akijikinga mikono yake usoni.

“Najua umetumwa, wewe ni nani?”

“Jose,” akajibu.

“Nani aliyekutuma?” akamchapa swali linguine.

“Mdada mmoja, yuko hapo nje,”

“Kavaaje na anaitwa nani?” Yule kijana hakujibu hilo swali, akabaki akimwemwesa mwemwesa midomo, Amata akamwinua kichwa na kumpigiza chini kwa nguvu.

“Nasemaaaa!” akalia kwa uchungu.

“Haya sema!” akamlazimisha kusema, mara hii bastola ikiwa mkononi.

“Simjui jina, alinipa hiki, akaniahidi pesa,” akatoa kadi ya kibiashara na kumpatia.

Kamanda Amata akaitazama na kusoma jina na namba za simu zilizopo, lakini alishangaa kuona jina la mwenye kadi ni la kiume. “Haijalishi, ndiyo njia zao hizi,” akawaza, akamtazama Yule kijana, yuko hoi pale chini, akamwacha na kufyatua zile namba kisha akaiamuru ile lifti iende juu kabisa. Huko akatoka na kuiacha akatumia ngazi kuteremka mpaka ghorofa ya sita ilipo ofisi yake, akaichukua ile kadi, na kuandika zile tarakimu katika mashine maalumu ambayo ina uwezo wa kukupigia simu ukajua unaongea na binadamu kumbe kompyuta, unachokifanya ni kulisha maneno kisha kuyaoanisha na yale ya upande wa pili, kwamba huyu akisema hivi yenyewe iseme vile, kisha akaunganisha ile mashine na simu yake ndogo aliyoipachika kwa mkono huku kisikilizio chake kikiwa masikioni, akatoka na kuondoka zake.

§§§§§

NAIMA akiwa ndani ya gari yake pamoja na wenzake wawili, aliipachika darubini yake machoni na kutazama kwa makini kwenye lango kuu la JM Mall, alichokiona sicho alichokitegemea, alimwona Kamanda Amata akitokea pale mlangoni na kuivaa miwani yake, kisha akatembea kuielekea gari moja aina ya Toyota Carina Ti, Kafungua buti na kujifanya anatazama vitu Fulani Fulani.

Naima na kijana wake mmoja wakatoka na kuwahi pale kwenye ile gari, Yule jamaa akamwona bado Amata ameinama akifanya shughuli zake kwenye ile gari iliyokuwa katika maegesho pweke upande wa pili wa lile jingo.

Kamanda Amata akahisi tayari kuna hatari, akatazama kwenye kioo chake cha siri kwenye ile miwani na kuona watu wawili wakimsogelea kwa mwendo wa Mamba awindapo, akataka kufanya makeke lakini akilini akawaza kutumia Art of War, jifanye mnyonge unapokuwa una nguvu, akaendele na shughuli yake.

“Usilete makeke yako ya kitoto, bunduko mbili zenye nguvu ziko nyuma yako na nkyingine kubwa ipo ghorofa ya pili, tulia hivyohivyo,” sauti ya Naima ikaunguruma.

Kamanda Amata alishalitegemea hilo na alijua kuwa ahadi yake na Scoba ilikuwa imetimia kwani wanapoahidiana kukutana Kanisa kuu la St Joseph, basi ujue hapo JM Mall ndiyo Kanisa Kuu.

“Simama!” akamwamuru.

Kamanda akafanya hivyo, kisha lile jitu la miraba minne likaja na kumpekuwa likachukua bastola tu bila kuona silaha nyingine zilizotapakaa mwilini mwa Amata. Naima akiwa mkononi na Shot Gun akamwongoza Kamanda Amata ndani ya gari hiyohiyo, Yule jitu akaketi kwenye usukani, Amata akawekwa nyuma huku Naima akiwa kampachika domo la Shot Gun katika ubavu wake.

Kamanda Amata alipotoka pale nyuma ya gari aliacha buti bila kufunga ila alilipachika kwa namna anayoijua yeye. Scoba alikuwa akiona mambo yote hayo, alipoingia tu garini na kuiwasha, alinyata taratibu na kufungua buti kisha akaingia ndani yake na kujiweka humo, akarudisha lile funiko na kuliegesha kwa namna ya ajabu, ile gari ikaondoshwa mahala pale na kuelekea kusikojulikana.

§§§§§

Simu ya kukamatwa kwa Kamanda Amata ilipokelewa kwa furaha sana na JoKi, naye muda huo huo akaingia katika chumba cha mawasiliano na Boss wake asiyeonekana sura na kumpa habari hiyo njema.

Pancho Panchilio alitamani aruke angani lakini hakuweza, aliinua simu yakena kuwapa ujumbe huo wenzi wake na kuwa wakutane huko kwenye kasri lao ili wamalize kazi waliyoidhamiria.

Ilimchukua dakika kadhaa tu Pancho Panchilio kuingia katika kasri lake huko Kerege kwa njia ya siri ambayo ni yeye tu aiyekuwa akiijua na kuitumia, na kila Mjumbe wake naye alikuwa na njia tofauti ya kuingilia, wao walikutana tu ndani ya jengo hilo.

Haikupita muda Mjumbe mmoja mmoja aliingia katika kasri hilo na kukutana kwenye chumba chao ambacho kwacho siku zote hufanyia mazungumzo na mipango yao.

7

ZANZIBAR

NURU MUSABAHA alitulia tuli kwenye kochi kubwa huku jicho lake likiwa kwenye luninga kupata habari mbalimbali kutoka Bara, mara kwa mara moyo wake ulikuwa ukilipuka na kujawa hofu lakini baadae alitulia tena, hata aliposikia unyayo wa paka yeye alihisi kama sijui kitu gani, alijua kila kinachoendelea huko Bara na kusudi kitekelezeke, alitakiwa kutoroka namna hiyo na kusubiri hali itulie na mumewe Mahmoud Zebaki awe na matumaini ya kurudi uraiani.

Asubuhi hiyo majira kama ya saa nne hivi, kila alipojaribu kuwasiliana na Ravi, simu hakupatikana, nah ii ndiyo ilimfanya achanganyikiwe zaidi, “Kwa nini hapatikani?” alijiuliza pa si na majibu. Kabla ya kuja Zanzibar alimshauri Ravi waondoke pamoja baada ya kuusuka mpango huo na mtu wasiyemjua, lakini Ravi yeye alikataa katakata kuondoka, akiamini kuwa maadam watu hao watakamatwa kwa siri yeye watamjuaje ilhali ni raia wa kawaida tu.

Alikuwa akisoma gazeti juu ya habari ya marehemu Mbunge lakini alihisi haelewi akalitupa huko, akazima TV na kujinyanyua kitini akasimama wima. Akavuta hatua fupi kukielekea chumba cha kulala lakini akiwa humo bado akili yake haikumkaa sawa, akaamua kubadilisha nguo alizokuwa amevaa, akavalia suruali ya jeans nyeusi, fulana moja yenye picha ya Madonna na kubebwa na neno Holyday , akajiangalia kwenye kioo na kujiona yuko fiti ukizingatia na shepu aliyonayo ya mchanganyiko wa Kimanyema na Kipemba basi utamu mtupu.

Alipojiweka vizuri akachukua pesa kidogo na kujaza mfukoni,

“Nikalale hotelini,” akawaza kisha akavuta juba lake na kujifunika mwilini akaacha macho tu kisha akanyanyua kijimkoba chake na kuanza safari ya kuondoka eneo hilo.

Alipoukaribia mlango tu, akasikia hodi ikibishwa, akasita kuuendea mlango, “Nani atanifuata huku?” akajipa moyo na kuuendea mlango, akaufungua.

“Karibu sana, nikusaidie nini?” Nuru akamwuliza huyo aliyegonga mlango.

§§§§§

Alikuwa kijana mtanashati, aliyeva suti yake nyeusi, miwani nyeusi akitazamana na Nuru pale mlangoni, Yule kijana alimwangalia Nuru chini mpaka juu na kulistaajabu umbo la mwanamke huyo, “Tangu lini Mpemba akawa na shepu ya maana kama hii?” akajiuliza.

“Mimi ni polisi Detective,” akajitambulisha na kumwonesha kitambulisho.

“Kwa hiyo mi nifanyeje, nikupandishe cheo au?” Nuru akauliza kijeuri lakini moyoni mwake alikuwa hoi, alihisi kijimkojo kwa mbali lakini akajikaza kikike.

“Hii ni barua ya wito wa kufika kituo cha polisi cha kati mara moja,” Yule kijana akamweleza. Nuru akaisoma pasi na kuishika kwai hakutakiwa kufanya hivyo. macho yake yakaonekana wazi kuwa na machozi.

“Nimefanya nini mimi mpaka michukue?” kauliza.

“Swali gumu mama, mi natekeleza wajibu, ukifika kituoni ndipo watakueleza yote,” akajibu Yule kijana.

“Ok, ngoja nijiandae,” Nuru akaomba.

“Hapana, hivyo hvyo ulivyo, mbona utarudi sasa hivi tu!” Yule kijana akamwambia na mara hiyo akaja mwenzake mwanamke WP aliyevaa kiraia na kumchukua Nuru mpaka kwenye gari. Safari ikaanza mpaka kituoni. Alipofika pale danadana ilikuwa ile.

“Na sisi pia tumepewa oda hiyo kutoka juu, hivyo madai yako yote utapewa majibu kutoka Dar es salaam,” akajibiwa hivyo na mkuu wa kituo.

Nuru aliishiwa nguvu, mapigo ya moyo yakashuka, akawa wa kupepewa tu, wakamvua viatu, wakamlegeza mkanda, wakambeba kwenye gari ya polisi mpaka hospitali ya Mnazi Mmoja.

Nuru alijua linalomkabiri, akashindwa kuvumilia.

§§§§§

Baada ya kujiganga na kupata unafuu wa maumivu alisonya huku akijiangalia kidole chake na kushikwa na hasira kali juu ya Chiba, “Atanikoma huyu mshenzi!” aliongea mwenyewe: Akainuka na kwenda huko kunakoitwa kuzimu alipofika katika chumba kile, alishamgaa kukuta mwili wa mlinzi umelala bila uhai, alipopepesa macho pembeni hakuona mtu mwingine.

“Shiit!” akang’aka kwa hasira na kuugeuza ule mwili, “Shetani huyu, kamuuaje huyu jamaa ilhali alikuwa na silaha mkononi?” akajiuliza kisha akaondoka kuelekea chumba kile alichomfungia kwanza. Akiwa njiani akakutana na Yule mlinzi wa pili.

“JoKi, huyu mateka ni hatari, kamuua Ngwabi kwa miguu yake,” Yule mlinzi akaeleza.

“Sasa yuko wapi?” JoKi akauliza.

“Nimemtupa huko kwenye chumba, sijui kafa au mzima maana nimempa kipigo cha maana,” akaendelea kueleza. Kisha wote wawili wakafuatana kwenda kumwangalia Chiba. Kweli hali yake ilikuwa mbaya, alilala mithili ya mfu, damu zikimvuja kichwani baada ya kupigwa sana kwa kitako cha bunduki.

“Safi sana! Sasa njoo nikupe maagizo mengine,” wakafuatana mpaka chumba walichomwacha Madam S.

“Unamwona huyu Kibibi, huyu atauawa kwa kukatwa na msumeno wa umeme nusu saa ijayo, yule mrembo ambaye hatujamfanya chochote kibaya, tutafanya naye ngono mbele ya wenzake kabla ya kumuua, yeye lazima afe kwa kuingiliwa, huyo mpumbavu huko uliyemwka vibaya kwa kipigo, tutamchinja na huyo anayekuja anayejifanya ndiye mjuaji yeye atakufa kwa kulowekwa kwenye tindikali, ni hivyo tu. Kwa hiyo waambie wenzako muandae hivyo yote, nusu saa jopo lote litakuwa hapa kwa kazi hiyo,” akamaliza JoKi huku akicheka na ubaya wa sura yake kuonekana wazi mbele ya kila anayemtazama.

Sonyo kali likamtoka Madam S, “Mnajisumbua tu!” akaongea kwa shida sana huku akiwa bado kafungwa na ile minyororo.

“Unasemaje we Kibibi?” JoKi akamuuliza Madam S. kisa akatoka na kuufunga ule mlango nyuma yake huku akiwaacha wale walinzi wawili pale langoni wakiwa wamesimama kwa ukakamavu.

§§§§§

Scoba bado alitulia kimya ndani ya buti la gari, akichungulia mara kwa mara kujua ni wapi wanaelekea, mpaka wakati huo alishaanza kujua maana tayari waliiacha Bunju A na kuelekea mbele.

“Kumbe ishu zote Bagamoyo!” alijisemea na kuendelea kutulia ndani ya lile buti kuona mwisho wa safari ni wapi na vipi ataweza kuanzisha msinambe.

“Lazima wajue kama sisi ni T.S.A,” akajisemea huku bado akifungua kidogo lile buti ili kuona wapi wapo.

Scoba alifikiria kwanza kuanzisha msinambe huo kabla hawajafika katika ngome yao, lakini baadae akaona wazi kuwa siyo vyema kwani kuna wenzao ambao hawajui walipo, hivyo ni bora kufika katika ngome ya watu hao kisha kwa pamoja waweze kufanya kazi hiyo. Akiwa amezama katika mawazo hayo akahisi ile gari inakata kona, akafungua buti kidogo na kutazama nje.

“Tumekata kushoto,” akajisemea, kisha akatulia tena.

Ndani ya gari hiyo hakuna aliyeonge wote walitulia kimya kana kwamba hakukuwa na mtu ndani yake. Ile gari ikasimama mahala Fulani, Scoba akajiweka tayari, akatega sikio kusikia nini kinaongelewa huko nje.

“Mpo wenyewe tu?” akasikia sauti kutoka nje ikiuliza.

“Kama unavyotuona,” Naima akajibu.

“Ok, ingizeni gari mpaka egesho namba sita mtakuta maagizo yenu,” ile sauti ikasema na kisha ile gari ikaingia taratibu na mara ikasimama tena.

“Vipi?” sauti ya Naima ikamfikia Scoba ndani ya buti.

“Hamjafunga buti, na mna bahati polisi hawakuwaona,” ile sauti ya mwanzo ikasema. Scoba akaona mtu kasimama nyuma ya buti, akatoa bastola yake na kuiweka tayari kwa lolote. Yule mtu akashika lile funiko la buti akalifunga kwa kulisukuma.

“Aiyaaa!” Scoba alinung’unika kimoyomoyo akajaribu kulitikisa lile funiko lo, limefungwa, akatulia na kusukuti kuona nini cha kufanya na atatoka vipi. Ijapokuwa hilo kwake alikuwa tatizo lakini tatizo lilikuwa ni muda. Ile gari ikatoka pale na kuingia ndani kwa ni alihisi baada ya kusikia mlio wa geti lililokuwa likijitembeza kuruhusu gari hilo liingine ndani, kisha likasimama mahali.

Scoba alijua kutika getini mpaka hapo walipo ni kama mita ishirini na kwa jinsi mlio wa gari ulivyobadilika akajua wameingia ndani ya kitu au jingo. Akatulia kusikia kinachoendelea nje.

“Ha ha ha ha, Umekamatika paka wewe!” sauti ya JoKi ilisikika,

“Naomba mumshushe kwa umakini sana, na silaha zenu ziwe tayari akileta ujanja muueni tu, hawezi kutusumbua akili sisi, kwanza mfikisheni Golgotha mkamtie adabu ila hakikisheni mmemfunga vizuri,” JoKi aliasa. Scoba alitulia kimya akisubiri kujua nini kitajiri, mpaka hapo alijua wazi kuwa ni yeye tu mwenye uwezo wa kuwakomboa wengine wote.

§§§§§

Naima aliwaomba wale jamaa kumtoa Kamanda ndani ya gari,

“Hana fahamu huyo amenusa Mandrax kwa wingi sana,” akawaambia. Vijana wane wakasogea na kuweka bunduki zao migongoni kisha wakamteremsha Amata na kumsimamisha chini.

“Hana ujanja huyo!” JoKi akawaambia.

“Mpelekeni ndani nakuja mwenyewe kumpa adabu,” Naima akawaambia, na wale vijana wakamburuza mpaka mpaka ndani ya kile chumba walichoagizwa na kuanza utaratibu wa kumfunga.

Muda wote huo Kamanda Amata alijifanya kalala fo fo fo kutokana nay ale madawa kumbe la, alikuwa akiwavunga na kusubiri muda kuafaka wa kuwaonesha kama yeye ni T.S.A 1.

§§§§§

Scoba alipoona tayari utulivu umerejea na kuna langa limefungwa akaona sasa ni wakati wa kufanya makeke yake. Akafyatua mkanda wake wa kiuno na kuchomoa kitu kama pini hivi, akaipachika sehemu Fulani katika kile kitasa kwa upande wa ndani, kisha kwenye kiatu chake akachomoa kitu kama chipio na kukipachika upande wa pili wa ile loki, akajaribu kufanya anayojua na sekunde tatu zilikuwa nyingi, kikaachia.

“Waohhh!!” akapumua kwa nguvu kisha aakachungulia nje na kuona giza tupu.

Akaichukua miwani yake na kuivaa akaibana vyema kabisa ili isije kuanguka akiwa kwenye harakati, miwani hii ilimpa uwezo wa kuona gizani. Alipoivaa tu akaanza kuona vyema ndani ya giza lililomo katika jengo lile. Akaangaza na kuona kuna kamera moja ya usalama upande ule ambao yeye anapaswa kutokea, kutokana na giza hilo hakujali, akafungua buti taratibu na kutoka akitanguliza mguu mmoja bila kufanya kelele yoyote. Akarudishia buti na kulibana tena. Alipokwisha kulibana akashtuka na kujishika kinywa,

“Shit! Mi mpumbavu sana!” alijisemea maneno hayo alipogundua kuwa amesahau bastola kwenye buti. Sasa hakuwa na silaha yoyote, hakuna jinsi. Akajibana ukutani, kisha akajivuta taratibu mpaka karibu na mlango ambao bila shaka ndipo walipoingilia na Kamanda Amata, akashika kitasa na kukivuta chini taratibu, kisha akausukuma, ulikuwa wazi,

“Missing in action!” akajisemea kisha akaingia ndani ya korido ndefu, akaivua miwani na kuruhusu ining’inie shingoni mwake.

Ndani ya korido hii kulikuwa na mwanga wa kutosha, hakukuwa na mlango wowote isipokuwa mbele yake umbali wa kama mita mia moja aliona kuna kingo za chuma akajua kwa vyovyote kuna ngazi za kuteremka chini. Kikwazo kimoja kikawa mbele yake, katikati ya korido kulikuwa na kamera nyingine ya usalama, na ujia ule ulikuwa mwembamba kiasi kwamba huwezi kupita mbali na kamera hiyo,

5

HALI YA GINA ILIRUDI NA KUWA NZURI, ijapokuwa bado alikuwa wodini lakini huduma aliyoipata kutoka kwa Dr. Khadrai na jopo lake ilimfanya aweze hata kuongea. Kichwa kilimzunguka alipojaribu kufikiri ni wapi wenzake wote watakuwepo.

“Khadrai, hivi hauna dawa ya kuniondolea maumivu kabisa niingie kazini?” akauliza. Khadrai akabaki kucheka tu.

“Gina, naona akili yako haiku sawa, endelea kulala, hali yako ni mbaya sana usifanye lolote la mikikimikiki,” akajibiwa.

“Moyo unaniuma sana kuona siwezi kufanya lolote,” akamwambia Khadrai.

“We Gina tulia hapa, hakuna baya litalotokea kama unavyowaza,” Khadrai akampa matumaini. Alipotaka kuondoka, Gina akamzuia, “Khadrai, naomba mkoba wangu,” akamwambia na Khadrai akampa, Gina akapekua ndani na kutoa bastola moja aina ya Beretta, akaikagua ipo sawa akaitia ndani ya shuka mkono wa ke wa kulia.

“Ya nini Gina?” Khadrai akuliza.

“We nenda! Nenda!” akamwambia huku akimpa ishara ya mkono.

Kgadrai akatoka ndani ya kile chumba na mara akakutana na watu wawili waliosimama mbela yake, wakamwonesha vitambulisho, maafisa wa polisi.

“Tunahitaji kumwona WP Gina kikazi,” wakamwambia huku wakipita kuelekea ndani ya kile chumba. Wakafungua mlango na kukuta Gina amelala kimya, drip mkono ni mwake na mipira ya oksijeni puani mwake. Khadrai akapigwa na butwaa maana hakumwacha Gina na oksijeni isipokuwa drip tu.

“Gina, Gina!” akaita mmoja wao. Gina akabaki kimya kabisa kama hasikii ilhali alikuwa akisikia kila jambo, mkono wake wa kulia tayari ulikamata bastola iliyokuwa haina usalama na risasi moja ilikuwa tayari ndani ya chumba cha shughuli.

Baada ya kuona kimya cha Gina wakatazamana na kupeana ishara kwa kubaniana macho, mmoja wao akaurudisha mlango na Yule mwingine akaenda na kuondoa ule mpira wa oksijeni. Gina kama umeme, alichomoa bastola yake kwenye shuka na kuanza na Yule aliyekuwa akifunga mlango, alimlenga shabaha na kufumua bega lake kisha akajibiringisha na kudondokea upande wa pili wa kitanda akiicha sindano ya drip ikichomoka yenyewe. Kutoka uvunguni alimchapa risasi Yule mwingine na kuvunja mifupa ya ugoko, alipodondoka akammalizi risasi ya moyoni. Kisha akasimama na kumtazama Yule aliyekuwa akifunga mlango wakati huo akimwagika damu begani hana la kufanya.

Gina alizunguka kitanda na kusimama kando ya marehemu Yule na kumtazama huyo aliyemjeruhi.

“Nimekujeruhi makusudi fala we!” akamwambia kwa hasira, akafyatua risasi nyingine na kupiga bega la pili, “Niambie, watu wangu wako wapi?” akamwuliza.

Yule jamaa alibaki analia tu, “Umentia kilema cha maisha weweee!”

“Nini kilema nakuua kama usiposema,” akamwambia.

“Utanionea tu huyu uliyemuua ndiye anajua kila kitu,” akajibu huku akibuujikwa damu.

“Jeuri siyo?” Gina akamuliza na kumkanyaga kwa nguvu bega lake.

“Aaaaaaiiigghhh! Nasema, nasema, nasema!”

“Sema!”

“Wapo Kerege, Bagamoyo,” akajibu.

“Na wewe bosi wako nani?”

“Mtu mkubwa, mkubwa serikalini,” akajibu.

“Nani mtaje kwa jina!” Gina akang’aka.

“Kigogo, Ki-go-go,” akaongea kwa taabu. Gina akaelewa anachokifanya akamwahi na kumtandika ngumi ya shavu, Yule jamaa akatema kidonge cha manjano, kidoge cha sumu kali ambacho huficha kinywani wanapozidiwa kwa maswali huwa ni bora kujiuwa kuliko kutoa siri.

“Shenzi sana wewe, ulifikiri utaniwahi? Sasa utaenda kueleza yote kwa wanaojua cha kukufanya,” Gina alilalama, kisha akachukua simu ya Khadrai nakubofya namba Fulani Fulani.

“Ndiyo Inspekta Simbeye (…), Agha Khan hapa hospitali haraka,” akatoa ujumbe upate wa pili na kumwacha Yule jamaa akipewa huduma ya kwanza ili kuzuia damu zisiendelee kumtoka. Gina aliiweka vizuri bastola yake na kuirudisha kwenye pochi yake. Khadrai alikuwa hana amani kabisa, akamtazama Gina bila kumuuliza chochote, Gina akaweka vizuri kilichochake.

“Vipi Gina?” Khadrai akatupa swali.

“Hapa hakuna usalama, najua wapi nitakwenda, asante kwa msaada wako.”

“Lakini Gina hali yako bado mama,” Khadrai akamwambia.

“Najua, lakini kwa hali ilivyo ni hatari,” Gina akajibu huku akitembea kwa kuchechemea kidogo kutokana na lile jeraha lake.

Dakika kumi na tano baadae, Inspekta Simbeye akaingia katika ile hospitali akifuatana na vijana wake mahiri kabisa waliobeba silaha za kutosha, wakateremka na kupanda mpaka ghorofa ya tatu.

Baada ya kukamilisha mambo yao ya kiusalama waliondoka na ule mwili pamoja na Yule majeruhi kwa mahojiano zaidi.

“Gina, pole sana, unajisikiaje lakini?” Simbeye alimuuliza Gina.

“Maumivu makali sana, lakini hapa siwezi kulala, pia sina amani kwa kuwa sijui watu wangu wako wapi,” Gina akajibu huku amejilaza katika kitanda cha kitabibu.

“Pole, sasa itabidi upelekwe Lugalo mahali ambapo pana usalama zaidi,”

Wakakubaliana hilo na utaratibu wa kila kitu ukafanyika. Ijapokuwa Gina alikubali kwa shingo upande kwa kuwa yeye alipenda kuingia msambweni kuwasaka wenzi wake.

Inspekta Simbeye, aliyekuwa akilitumikia jeshi la Polisi kwa kofia mbili, moja kama Inspekta wa Polisi lakini ya pili ni ile ya Ukachero wa serikali, Usalama wa Taifa, aliwekwa pale kwa mpango maalumu wa kuchunguza maafisa wa Jeshi hilo kama kuna lolote baya wanalolifanya juu ya nchi hii.

Kerege – bagamoyo

WAJUMBE WA KIKAO KILE CHA DHARULA walipiga makofi baada ya kupewa taarifa kuwa watu wao wote wamepatikana isipokuwa mmoja ambaye wao kama wao hawakuona kama anaweza kuwa na dhara lolote.

“Kazi imekwisha!” Pancho aliwaambia wenzi wake.

“Vijana wamefanya kazi ngumu na nzuri wanastahili pongezi,” mwingine aliongezea.

Baada ya furaha yao hiyo kukamilika na kugongeana bilauri kama ishara ya kupongezana,; Pancho Panchilio aliwataka watu wake kuteremka kuzimu ili kushuhudia kile kilichoitwa ‘Hukumu ya Mwisho’.

“Na tutawafuatilia mbali katika uso wa dunia,” Pancho aliwaambia wenzi wake. Kisha kila mmoja akavaa uso wake wa bandia akiwa sehemu yake ambayo mpaka hapo hawakuweza kuonana sawasawa. Wakavaa kisha Pancho akiwa katika guo jeusi akifuatiwa na wajumbe wake watatu wakatoka na kuteremka ngazi kuelekea bondeni walikopenda kukuita Kuzimu.

§§§§§

Scoba aliendlea kusukuti huku bado akiwa kasimama hakujua lipi lakufanya mbele ya kamera ile. Baada ya kuumiza sana kichwa akakumbuka kipande kimoja cha kisa ambacho aliwahi kusimuliwa na Kamanda Amata jinsi anavyozipita kamera kama hizo, akatabasamu kisha akajirusha kwa kutanua miguu na kunata ukutani, akiwa katanua miguu yake na kukanyaga huku na kule na mikono hivyo hivyo, akanata juu kabisa na kuanza kujivuta kwa namna ambayo wewe huwezi hata kidogo, ukimtazama unaweza kusema na mjusi au kenge.

Aliifikia ile kamera na kuushika waya wake kutoka nyuma akauchomoa, kisha akajiachia na kutua chini taratibu. Kisha akaenda kwa mwendo wa kasi mpaka katika zile ngazi, alipofika tu alikutana uso kwa uso na mtu mmoja aliyekuwa akipanda juu, Scoba akaruka na kutua juu ya ukingo wa ngazi uliotengenezwa kwa mabomba ya aluminiam akaseleleka na mguu mmoja akamtandika teke Yule mtu kisha akajiachia na kumshukia pale chini; kabla hajasema lolote akambana koo kwa goti lake.

“Wako wapi?” akamwuliza.

“Akina nani?” Yule bwana aliongea kwa taabu.

“Wako wapi watu wangu? Mmewaweka wapi?” akauliza kwa ukali lakini kwa sauti ambayo haiwezi kwenda popote.

“Hakuna watu wako huku aliyekwambia wapo ni nani?” Yule bwana akajibu kiujeuri. Scoba akamnyonga mkono na kuuvunja, Yule bwana akapiga yowe la uchungu, Scoba akaona itakuwa noma, akamkamata na kumvunja shingo kisha akaichukua bunduki yake aina ya S.M.G na kuteremka ngazi mpaka kwenye maboksi Fulani akajificha. Watu wawili wakapita eneo lile wakitangulizana, akatulia na kusubiri Yule wa pili ili amputeze lakini alighairi baada ya kusikia mazungumzo yao matamu.

“Wanauawa wote, tena sasa hivi,” mmoja akamweleza mwenzie.

“Yaani ni historia,” mwingine akamuunga mkono. Alipopita wa kwanza akamwacha wa pili akamkata na kabala moja matata sana kisha akamvuia kwenye maboksi taratibu na kumtuliza. Yule wa kwanza akajkuta kila akiongea hakuna kuungwa mkono akageuka kutazama kulikoni akakutana macho na Scoba. Bila kuchelewa Scoba alirusha kisu maridadi kabisa na kumchoma koromeo, akajibwaga chini.

§§§§§

Madam S alifunguliwa minyororo na kukokotwa kuelekea katika chumba cha mauaji, Chiba naye akachukuliwa kikondoo namna hiyo, Dr. Jasmin kwa kuwa yeye hakuteswa kama wengine alitembea mwenyewe mpaka ndani ya chumba kile cha kutisha.

“Wafunge pale huyo bibi na huyo kijana mtukutu, kisha mlete huyo rembo mbichi hapa,” JoKi alitoa amri nayo ikatekelezwa. Walipomaliza wakaambiwa wakamlete Kamanda Amata li kazi ya mauaji ianze kama ilivyopangwa. Amata akaletwa, na ye kama kawaida akatuliaa na kukokotwa mpaka ndani ya chumba kile kinachonuka damu mbichi na iliyoganda, macho yake yalikuwa yakiwatazama wote waliojipanga mle ndani wakiwa na silaha nzito nzito. Mara hiyo hiyo Pancho na watu wake waliingia ndani ya chumba kile na kusimama mahala Fulani.

“Sasa tunataka tuanze shughuli yetu, karamu ya damu, JoKi! Nataka ufanye kazi hii kama nilivyokuagiza, lakini kwanz ahuyo mrembo lazima aingiliwe nah ii ni motisha kwenu vijana wangu haya na muanze kazi sasa ya kumuingilia,” Pancho akatoa amri, vijana wawili walioshiba kimazoezi wakamvamia Jasmin, mmoja akaanza kumvua nguo kwa nguvu huku mwingine akishusha zipu yake kuuchomoa mshededе.

Yule jamaa aliyekuwa akimvua nguo Jasmine alijikuta kwenye wakati mgumu baada ya kuchapwa makonde mawili matamu kabisa, akapepesuka pambeni na kujipanga upya, alipomwendea Jasmin ili ampe kibano alikutana na mapigo matano ya karate ya haraka haraka yaliyompeleka chini. Yule mwingine alitoa macho baada ya kujikuta dudu lake likikatika vipande viwili.

“Aaaaaaiiiggghhhh!!!” alipiga kelele huku akijiangalia, kila tu akashtuka waliposikia sauti ya kisu kikitua ardhini huku kikiwa kimekata dhakari ya Yule bwana.

“Shit! Muue huyo mwanamke haraka!” JoKi alitoa amri huku akiwakinga Pancho na wenzake.

“Nini JoKi?” Pancho akauliza.

“Tumevamiwa!” akatamka neno hilo na hapo hapo alishuhudia minyororo aliyofungwa Kamanda Amata ikikatika kwa shabaha maridhawa kutoka kwa Scoba. Amata aliruka sarakasi maridadi na risasi nne zilichimba chini, alipotua chini tayari alikuwa na shingo ya mtu, alimkamata na kumzungusha kichwa, Yule bwana akatoa macho na kuachama kinywa chake,kisha akambwaga chini. Alipogeuka huku na kule, JoKi hayupo, Pancho na watu wake hawapo.

“Scoba fungua hao, fanya juu chini wafike kwenye gari, hii kazi niachie mimi niimaize, pumbavu zao,” Kamanda Amata akampa maagizo Scoba kisha yeye akajibana mahali na S.M.G mkononi, akanyata kwa tahadari akiwa hajui wapi wale watu wamepotea ghafla namna hiyo. Mara taa zote zikazimika, giza likachukua nafasi ndani ya jingo hilo.

Scoba akaivaa miwani yake na kuendelea kuona vizuri kabisa, akawafungua Chiba na Madam S.

“Asante T.S.A 4, hakikisheni humu ndani hatoki mtu akiwa hai,” Madam S alitoa amri mara moja kama cheo chake kilivyo.

Mara sauti ikasikika kutoka katika vipaaza sauti vizivyoonekana.

“Ak! Ak!Ak! Ak! Hii ndiyo himaya ya Shetani, Taifa ndani ya nchi, hamjafanya lolote na hakika hamtatoka humu mkiwa hai, lazima muongee na bwana ngurumo,” ile sauti ikacheka tena kwa dhihaka.

“Usimsikilize huyo hanithi, Scoba ongoza mbele Jasmine linda nyuma ninyi ndio mna nguvu kwa sasa mi namaliza kazi,” Kamanda Amata akatoa maelekezo kisha kwa mwendo wa taratibu alipita kwenye ujia mrefu ulioonekana ukienda mahala Fulani.

“Nitakukamata tu, na leo itajulikana mbivu na mbichi,” akajisemea. Mara nyuma yake akasikia kama mtu aiyetua ghafla kwa miguu laini, akageuka ghafla na kujikuta akipata pigo moja kali la kung fu, akayumba na kusimama tena, akajikuta akipigwa ngwala tamu, akapaa hewani na kujibwaga chini, akajikunja na kujiinua kwa ustadi. Alikuwa ni Naima aliyemtembezea mchezo huo.

“Malaya mkubwa wewe! Sasa umeingia mikononi mwangu!” Kamanda akaunguruma.

Mara ile sauti ikasikika tena ikicheka na cheko lake likifanya mwangwi,

“Mtoto wa kike kutoka Kigoma lazima akuoneshe kazi”.

Mara taa zikawaka, Naima akajizungusha huku akipiga vijikelele kama nyau, akampelekea pigo la kwanza Kamanda akaliona, la pilia akaliona la tatu akaliona, la nne Kaliepa kwa chini na kujizungusha kwa kasi, aliupiga mguu wa Naima lakinia Naima aliruka sarakasi hiyo ile ngwala

ikamkosa, Naima alitua sakafuni na kupiga teke kali huku akiruka tik tak; hilo lilimpata Amata na kumuinua juu juu na kumbwaga chini mzima mzima.

Naima alitua sakafuni na kusimama kwa madoido huku akimwonesha ishara ya mkono Amata akimwambia, " Come to me boy, come to me boy".

Dharau hizo Amata alizichoka, akajirusha kujiinua, Naima akataka kumwahi, akaruka teke ambalo lilikusudiwa kutua kidevuni mwa Amata lakini akaikinga mikono yake na kuudaka mguu wa Naima, akauzungusha kwa minajiri ya kuuvunja lakini Naima naye akaruka hewani na kujizungusha sambasamba na akili ya Amata na mguu wa pili akirusha teke lingine lakini Amata akaliepa na kumwachia, wote wakaanguka chini. Amata akawahi kuinuka na kujiweka sawa, Naima alipoinuka alikutana na mapigo kumi na mbili ya karate, kwa kasi aliyoitumia Kamanda Amata , Naima aliweza kuyakinga mapigo manne tu na nane yaliyofuata yalimwacha hoi.

"Come to me bitch!" Kamanda Amata akamwita kwa dharau, Naima damu zilimtoka kinywani na puani, alijifuta bila mafanikio.

"Hesabu ushakufa Naima!" Amata alimwambia.

Naima akasonya na kujitutumua kumvamia Amata, akakutana na kono lenye nguvu lilimtandika ngumi moja ya maana katika ziwa lake la kushoto. Naima alisimama ghafla akiwa katoa macho, akijitahidi kuongea lolote lakini alijikuta hawezi. Alipotaka kuanguka Amata akamwahi, akamtazama husoni, akambusu kwenye paji la uso. Mara taa zikazimika akasikia sauti ya bastola inayoondolewa usalama, akawahi kuruka na kumwacha Naima akifumuliwa vibaya na risasi hizo.

"Tulia, fuata maelekezo yangu, sasa hivi sina masihara na kiumbe yoyote Yule, nipeleke walipo mabosi wako," akaamuru.

JoKi akiwa mikono juu, akatulia kama alivyoamuriwa, akataka kugeuka, Kamanda akamzuia.

"Sijakwambia ugeuke, nimekwambia unipeleke walipo vinyamkera wako," akamwambia tena. JoKi akatafakari jambo,

"Sasa bila kugeuka nitakupelekaje walipo? Hivi ninyi mnachokifanya mnakijua? Mtajuta kuzaliwa ndani ya nchi hii," JoKi akaongea.

"Funga domo lako kibaraka tu wewe, na sasa utatujua sisi ni nani, mlifikiri jaribio lenu litafika wapi? Haya nioneshe hao vinyamkera wako," Amata akaamuru.

"Siwezi kukuonesha na huna la kunifanya," alijibu JoKi huku akigeuka mzima mzima na kukutana na Amata aliyekuwa amefura kwa hasira.

"Ha ha ha ha, Kamanda Amata, nasikia tu unavyovuma katika visa vyako vya kubahatisha, safari hii maji yapo shingoni ee?" akaongea kwa ngebe zilizompandisha hasira Amata, akaiweka vizuri bunduki aliyoishika mkononi mwake.

"Amata, wanaume wakutanapo huweka silaha chini na kupambana kwa mikono," akaongea kwa dharau huku mikono yake kaiweka kiunoni kana kwamba anaongea na mtu wa kawaida mbele yake.

"Najua hila zako, ichukue wewe utumie kunishambulia," Amata akamwambia huku akimrushia ile bunduki. JoKi akainua mikono yake ili kuidaka na ndilo kosa alilolifanya. Konde moja la kilo nyingi lilitua sawia mbavuni, la pili na la tatu, JoKi akawa hoi, akajaribu kujipanga lakini Amata hakumpa nafasi kwani alimvurumishia makonde yasiyo na idadi mpaka akaenda chini na kuanza kubingirika kwenye ngazi, akafka chini akiwa hoi.

"Kelele zote mi nilijua unaweza mchezo kumbe hamna kitu, boya tu, haya simama sasa," Amata akamwambia JoKi. Bado JoKi alikuwa pale chini, Kamanda Amata akamsogelea. Joki alifyatuka kasi na kumtia ngwala Amata, lakini hakukubali, aliruka beki na kusimama kwa miguu yake miwili, wakati huo tayari JoKi nae alikuwa wima. Kamanda Amata alirusha teke lililopanguliwa vyema na JoKi. JoKi alipeleka mashambulizi ya karate kwa Kamanda lakini mapigo yote yalikingwa kwa ufundi wa hali ya juu. Wakasimama pande ofauti wakitazamana kama majogoo hasimu, yenye uhasama wa kudhulumiana tetea.

JoKi alifyatuka na kucheza karate kadhaa kwa kumwelekezea mapigo ya hatari Amata, lakini alijikuta hapati kitu baada ya Kamanda Amata kuyacheza vizuri na kubaki imara akimtazama JoKi aliyeishiwa cha kufanya. JoKi akajikunja na kuanza upya mashambulizi, safari hii alikuja na ujanja mwingine ambao umakini kwa kamanda Amata ulihitajika. JoKi alipeleka mashambulizi makali ya mikono na wakati huo huo akibadilika na kutumia miguu yake. Kasi ya mashambulizi hayo ilimfanya kamanda Amata apate tabu kucheza na akili mtu huyo, lakini yote ya yote Kamanda Amata aliyakinga kwa ufundi. JoKi alimpiga ngwala ya nguvu na Amata .lirushwa juu, lakini akiwa hewani alijigeuza na kutumia mguu mwingine na kumzabua teke kali la shavu na kumvunja taya. JoKi akayumba na kujibamiza ukutani huku akijishika taya lake la chini lililohama mahala pake. Hakumjali, alimpa mapigo makali na kumwacha akiwa hoi sakafuni hajielewi, akamfuata na kumkamata kichwa chake akambamiza ukutani kwa nguvu kisha akamwinua mzima mzima.

“Nioneshe walipo,” akamwambia huku akiwa kamkunja vyema shati lake, damu zikimvuja.

“Wapo safe house,” akajibu huku mabonge ya damu yakimtoka kinywani.

“Safe house ndo wapi?” akamwuliza.

“Ipo chini kabisa ya jingo hili, lakini huwezi kufika kabla hujauawa,” akamjibu huku akitoa cheko la ajabu kisha akatokwa na uhai.

§§§§§

Kazi nzito ilikuwa upande wan je ambako Scoba na Jasmin walikuwa wakiwadhibiti walinzi wa jengo hilo. Watu wa kijiji hicho walikimbia mbali wakisema majambazi yamevamia jumba hilo.

Chiba alipita huu na kule na kutokea kwenye mlango mmoja ulioandikwa ‘Control Room’ akauchezea huo mlango kidogo tu na kujikuta ndani. Chumba kikubwa kilichojawa na mitambo ya mawasiliano, kompyuta na vitu vingine, kutoka pale ndipo alipoona kamera zote za usalama za eneo lile jinsi zilivyokuwa zikifanya kazi na kuangaza kila eneo, alitikisa kichwa baada ya kuona ugumu wa kazi yao ulikuwa wapi kwani walionekana kila walipokwenda, jambo la kwanza alizima tambo uliokuwa ukiwaunganisha watu wote wa jengo hilo kwa simu maalum za ndani ‘Voip’. Baada ya hapo akaelekea mahala palipokuwa na kitu kama kabati lenye switch mbalimbali, akaelewa ni switch za milango, akaibofya na kufungua milango yote ya jumba hilo kisha akaharibu mfumo mzima.

Akiwa katika shughuli hiyo akasikia mlio hafifu wa bastola inayoondolewa usalama.

“Nani alikwambia?” sauti ikatoka nyuma yake, “Haya mikono kichwani kisha geuka taratibu,” aliamuriwa. Chiba aliweka mikono kichwani na kugeuka kwa kasi na kuipiga teke ile bastola kisha akajirusha sarakasi na kuichukua mikononi mwake, Yule bwana alijikuta hana ujanja, macho yakamtoka. Kisha akamuongoza kwenye mitambo yake.

“Nioneshe mabosi wako walipo,” akamwamuru. Yule bwana hakuwa na aujanja aliwasha luninga mojawapo iliyowaonesha wale mabwanyenye kila mmoja akiwa katika harakati za kuiacha himaya hiyo, Chiba alibaki kinywa wazi, hakuamini kile anachokiona, aliwatambua watu wale kwa uwazi kabisa bila kificho akajikuta akiishiwa nguvu. Alipogeuka nyuma kumtazama Yule kijana hakumuona, katoweka. “Shiit!” akang’aka na kuiweka bastola yake vyema mkononi mwake kisha akaanza kuzunguka humo ndani kumtafuta.

Yule kijana alijificha kimya upande wa pili wa mashine zile, mkononi alikuwa na kisu akimvizia Chiba kufika upande huo ili amfanyie kweli, masikini, hakujua anacheza na kiumbe cha aina gani katika tasnia hiyo ya mchezo wa visu. Katika kupita akitafuta, Chiba alimwona Yule kijana akichungulia, akajifanya hamwoni kabisa na kuendelea kutafuta huku kampa mgongo. Yule kijana akaona hapo ndipo pa kumpata adui yake, akatoka mzima mzima na kisu mkononi kumpamia Chiba kwa nyuma. Chiba alimkwepa na kumdaka mkono, akauzungusha na kumnyanyua kisha kumbwaga chini na kumbana vyema.

“Nipe namba za milango!” akamwamuru.

“Sizijui,” akajibu huku akikunja sura kwa maumivu.

Chiba akaunyonga mkono kwa nguvu, “Taja, kabla sijakumaliza,” akamlazimisha huku akiunyonga ule mkono.

“Nataja, na-ta …” kabla hajamaliza, Chiba alishuhudia Yule kijana akitoa macho na kisu kimedinda shingoni mwake,

“Wamemuua!” akajisemea; kwa kasi ya ajabu alikichomoa kile kisu na kukirusha upande kilipotokea huku yeye mwenyewe akibiringika kuliacha eneo lile, akashuhudia risasi zikiufumua mwili wa Yule kijana ilhali mtu aliyemlenga akidondoka jirani na mlango bila uhai. Chiba akasimama chapchap na kuangaza macho huku na huko, chumba kilikuwa kimya, hakuna mtu zaidi yake na zile maiti mbili tu. Akahakikisha usalama kisha akazipekua zile maiti na kupata funguo moja ambayo hakujua hata ni ya kitu gani, akaitia mfukoni. Hakuzijali maiti akapanda juu ya kiti cha magurudumu kilichokuwa hapo na kuanza kucheza na zile kompyuta. Alishangaa kuona kuwa wale jamaa walikuwa wamejiunganisha na vitengo vyote muhimu vya serikali wakipata siri mbalimbali za vitengo hivyo.

Akaendelea kupekuwa na kukuta habari nyingi za Usalama wa Taifa zikiwa katika moja ya kompyuta hizo.

“Ni nani hawa?” akajiuliza bila kupata jibu. Akasogeza kiti chake na kuelekea kwenye luninga kubwa iliyoonesha jingo lote ndani na nje na kuanza kukagua sehemu moja baada ya nyingine, akatazama vyumba mbalimbali vya jingo hilo na kugundua kuwa bado walikuwa hawajafika hata nusu ya hifadhi ya jingo hilo.

“Shiit!” alijikuta aking’aka na kujisukuma kwa nguvu mpaka kwenye meza ndogo yenye simu na kuiyakua kisha akabofya namba fuklani na kuweka sikioni.

“…Inspekta Simbeye, Chiba anaongea hapa!” akaijibu sauti ya pili iliyoitikia simu hiyo.

“…Oh, Chiba, nafarijika kusikia sauti yako Kamanda wangu, nipe dondoo,” akamwambia.

“…Inspekta naomba haraka iweekanavyo uje na vijana wa kazi wasiopungua kumi na tano wenye silaha nzito zilizoshiba, eneo ni Kerege, Bagamoyo, plot namba KG/BY 1230p…” kisha akakata simu. Alipogeuka kwenye luninga hakuwaona wale Mabwanyenye kwenye vyumba vyao, wametoroka! Akazima swichi kubwa na umeme ukakatika kila kona ya jengo lile, akilenga kuwanasa kama walikuwa wakijaribu kutoroka na chombo chochote kitumiacho umeme, kisha akachukua silaha kutoka kwa mmoja wa maiti wale na kutaka kutoka kwenye kile chumba, akakumbuka kitu; akarudi.

Akaenda kwenye moja ya kisanduku na kutaka kufungua akashindwa, akagundua kuna funguo hutumika, akafikiri kidogo na kuchukua kale kafunguo alikochomoa ka Yule jamaa, akatumbukiza na kuzungusha kidogo tu, mlango ukafunguka. Ilikuwa na sisytem unity iliyounganisha kompyuta zote ikiwa na maana kuwa ilihifadhi data zote za wale jamaa. Kwa kutumia ile bunduki akavunja kufuli lililokuwako nyuma ya dubwasha hilo, akaondoa funiko lake na kutazama anachokitaka, akafyatua waya nene nene zilizojaa huko, akavuta dubwasha Fulani kubwa kubwa na kulichomoa kutoka kwenye system ile, akatikisa kichwa kwa ushindi, kisha akatokomea nalo.

§§§§§

“Hapana, lazima niende!” Gina alimsisitizia Inspekta Simbeye.

“Gina nimekuleta huku ili upumzike, sasa acha tupeleke kikosi katika eneo la tukio,” Inspekta Simbeye akambembeleza Gina lakini Gina hakukubaliani na bembelezo hilo. Mwisho alikubali kwa shingo upande kubaki Hospitali ya Lugalo chini ya uangalizi wa madaktari wa kijeshi.

Inspekta Simbeye alichukua vijana wachache wanaojua kazi, kikosi maalumu cha kukomesha ujambazi kilichoundwa na Kamanda Toss kikaingia kwenye Land Cruiser za Polisi. Kutoka kituo kikuu gari hizo zilichukua uelekeo wa Makongo mpaka Mwenge waipomchukua Inspekta huyo na kuongoza kwenda Kerege. Kwenye gari hizo hakuna aliyeongea, kila mmoja alikuwa kimya kabisa akiitafakari shughuli inayomkabili, bunduki zilikuwa tayari zimejazwa risasi na magazine za akiba zikipachikwa kwenye vikoba maalum tayari kupokea zile zilizopo chemba pale itakapobidi.

KEREGE

KAMANDA AMATA BAADA YA KUHAKIKISHA JOKI AMEKATA ROHO; akaondoka upesi eneo lile, kila alipokuwa akipita kutazama tazama alikuwa safari hii milango iko wazi kabisa, hakuna tena milango ya siri, kazi ya Chiba ilisaidia. Akaiendea lifti ili aweze kushuka chini kabisa ya jengo hilo. Kwa mbali akiwa anasikia milio ya risasi za piga nikupige alijua wazi kuwa huko kazi inaendelea.

Ghafla akasimama kwenye moja ya kona za ndani ya jingo hilo baada ya kusikia michakacho ya viatu vya mtu anayekuja upande wake, akajiandaa kwa shambulizi la dharula, alipohisi mtu huyo amekaribia, alijitoa mzima mzima lakini pigo lake likakingwa kwa ustadi wa hali ya juu.

“Oh, sorry asee! Chiba vipi?” kumbe alikuwa Chiba.

“Yeah, hapa ni kujilinda muda wote, tuelekee chini, hawa jamaa wako huko,” Chiba akatoa maelekezo na kisha wote wakateremka kwa kutumia ngazi kwa maana Chiba alikuwa amezima umeme na kufanya lift zote zisifanye kazi. Haikuwachukua muda kuwasili chini kabisa ya jingo hilo kubwa na la kisasa, “Lilijengwa kwa miaka mingapi hili?” Kamanda akajiuliza, huku wakiufuata mlango mmoja baada ya mwingine, lakini vyumba vyote vilionekana tupu.

“Hawapo Chiba, laiti ningewapata!” Kamanda alimwambia Chiba huku akiiteremsha silaha yake kutoka mikononi na kuiweka mahala pake.

“Nimempa taarifa Inspekta, yuko njiani,” Chiba akatoa taarifa kwa Kamanda.

“Safi sana Chiba, kumbuka hapa sote hatuna mawasiliano na dunia ya nje,” kamanda akaitikia kisha wakaendelea kupekua chumba kimoja na kingine. Katika moja ya vyumba hivyo kulionekana kuna mlango wa siri lakini ulikuwa wazi ndani yake, akausogelea na kuchungulia ndani yake, ulikuwa ujia mrefu sana uliopotelea gizani.

“Hii ni njia ambayo kwa vyovyote wametorokea,” Kamanda akamwambia Chiba.

“Kila mmoja alikuwa na njia yake Kamanda, hapa alitumia mmoja wao,” Chiba akajibu. Kamanda Amata akageuka kumtazama kama akihoji kitu, lakini mwisho aliuliza.

“Umejuaje?” akamwuliza.

“Nimewaona katika dakika zao za mwisho kutoroka lakini mshenzi mmoja akanivamia; katika kupambana naye ndipo nilipowapoteza sikuona wametorokaje lakini walikuwa vyumba tofauti,” akaeleza.

“Umenikiwa kuona sura zao?” akauliza tena.

Chiba akatulia kwa nukta chache kwa maana aliwaona mara hii wakiwa hawana vinyago na aliwatambua kuwa ni vigogo wakubwa serikalini, “Je kama walitumia sura za bandia kutughilibu?” akawaza, kisha akamtazama Amata.

“Hapana, walificha sura zao kama kawaida,” akajibu.

“Ok, tutawajua tu, usiguse kitu watu wa Foresinc Bureau waje kufanya kazi yao ya kunasa alama za vidole na nyinginezo,” kamanda akamwambia Chiba huku wakitoka na kuelekea chumba kingine, nako wakakuta mambo hayo hayo, wakatoka na kupita vyumba vingine kama vitatu vilivyoonekana viko katika mtindo huohuo. Wakaviacha na kuendelea na uchunguzi wao zaidi na zaidi. Katika ghorofa ya chini wakagundua jambo ambalo liliwatia hofu, mioyo yao ikashtuka, kama wangekuwa na mioyo myepesi wangeziamia au hata kufa kabisa.

“Hawa ni mashetani!” Chiba akasema.

“Nin hiki?” Kamanda akauliza huku akivuta hatua ndani ya chumba hicho kikubwa, “Hawa jamaa hawastahili kuishi kabisa, ningewatia mkononi wangejuta kuzaliwa,” akaongeza.

“Kamanda, hapa msaada wa haraka unahitajika, nafikiri vijana watakuwa tayari nje,” akasema Chiba.

§§§§§

LAND CRUISER ZA POLISI ziliingia kwa fujo eneo lile na vijana wa kazi wakaruka tayari kuanza kudhibiti eneo hilo. Ilikuwa kama sinema ya kizungu vile. Inspekta Simbeye akawapanga vijana kuzunguka jingo hilo na wengine kuingia ndani kupitia langoni kuu, haikuchukua dakika kumi tayari walizingira na risasi kadhaa zilirindima ndani ya wigo huo, kisha kundi la watu waliokuwa katikanulinzi wa jingo ilo waliwekwa chini ya ulinzi.

“Hivi hili jumba lina milikiwa na nani?” Simbeye akajiuliza bila kupata jibu. Vijana wake bado wakiwa katika sakasaka hiyo upande wa pili wa jingo walipomweka chini ya ulinzi Madam S na Jasmine. Kutii sheria bila shuruti, Madam S akiwa kachafuka damu zilizoganda, alisalimisha silaha yake na Jasmine akafanya hivyo kisha wakatiwa pingu. Inspekta Simbeye aliwaona wakiletwa kwake wakiwa na pingu mikononi, wakaamuriwa kukaa chini pembeni kidogo kwa wenzao.

Scoba alitokea pale ambapo gari ya Gina iliegeshwa baada ya kutekwa na kuletwa huku, moja kwa moja akaliendea langoni na kulifungua na kuchungulia nje kwa minajiri ya kuwashambulia waliopo huko na apate jinsi ya kutoa gari hi;lo na kuwaokoa wengine kama walivyopanga, alishangaa alipoona vijana wenye silaha wakiwa wamewalaza chini vijana wengine kama kumi hivi tena kifudifudi, kwa jinsi alivyowaona tu akajua ni Polisi, akajitokeza mzima mzima na bunduki yake mkononi.

“Jisalimishe kama ulivyo, weka silaha chini,” amri ikatoka upande wa nyuma yake, Scoba akafanya hivyo na kuamuriwa asogee mbele, akafungwa pingu na kulazwa chini kama wenzake.

§§§§§

“Inspekta!” Kamanda Amata aliita wakati alipokutana na Simbeye katika uwanja wa himaya hiyo, huku akishangaa huku na kule kuwaona wenzake wote wamepigwa pingu isipokuwa yeye na Chiba ambaye bado alimwacha ndani.

“Kamanda Amata! Pole kwa kazi na janga hili,” akampa pole huku akimpa mkono.

“Asante Inspekta, tunafuga mashetani nchi hii Inspekta, naomba vijana kama watano hivi na wewe mwenyewe, pamoja na mama yangu muache huru hakuna baya hapa tupo kazini, tuingie ndani ya jengo hili, tupite na muone wenyewe mchezo wa kuwapa watu viwanja bila kujua nia na malengo yao,” Kamanda alilalama. Madam S na Jasmine wakafunguliwa pingu zao, Scoba naye alkadhalika.

“Usishangae hawa ni watu kama wewe!” Inspekta alimwambia mmoja wa polisi ambaye alishangaa amri anayopewa ya kuwaweka huru watu hao.

Muda si mrefu, vijana watatu wakaingia ndani ya himaya hiyo wakiwa na suti nadhifu, mach yao yakiwa yamezibwa na miwani nyeusi, hakika walikuwa watanashati na nyuma yao aliwafuata mzee wa makamo mwenye mvi kadhaa kichwani mwake.

“Karibu sana Bwana Hosea, nafurahi umefika,” Inspekta alimkaribisha wakapeana mikono kisha wote wakaongozana kuingia katika jingo hilo.

Hakuna aliyekuwa akiongea, kila mmoja alikuwa makini kutazama kila kilichopo ndani humo, hakuruhusiwa mtu yeyote kugusa chochote kwa mikono uchi.

Chiba aliliongoza jopo hilo baada ya kukutana nao humo ndani, akawaingiza chumba cha mawasiliano, jopo hilo likabaki hoi.

“Tazama huu mtambo, unanasa habari kutoka ofisi zote za serikali, simu zote za kiofisi kuanzia za Rais na watu wake zote zinanaswa hapa, ona hii kompyuta ni kubwa sana inafanya mambo mengi sana, inanasa picha kule Uwanja wa Ndege, nah ii kama unavyoona inaonehsa mazingira yote ya Ikulu,” Chiba alikuwa akieleza.

Hosea akabaki kajishika kiuno, taratibu jasho lilikuwa likimtiririka.

“Nani mmiliki wa jumba hili, na alikuwa na lengo gani na Taifa hili?” akauliza, lakini wote walikuwa hawana jibu.

“Hatujamaliza, twendeni huku chini, naomba muwe na roho kavu kwa unyama uliopo huku,” Chiba akawaambia kisha akawafikisha ‘Kuzimu’, “Hapa ndipo wanapotumia kuua wabaya wao, mnauona ule mwili, mnaweza kuutambua, Mkuu?” akauliza. Hosea na vijana wake wakauendea na kuuangalia vyema, wakaugeuza huku na huko.

“Hapana simfahamu huyu,” Hosea akajibu.

“Ni mwandishi anayetafutwa na jeshi la Polisi kwa miezi mingi sasa, ameuawa mbele ya macho yangu,” Chiba akawaeleza.

“Chilese Zuberi,” Inspekta Simbeye akataja jina la Mwamndishi huyo, akachuchumaa kumwangalia vizuri na jeraha baya la risasi likiwa limeharibu kabisa sehemu ya nyuma ya kichwa chake.

Walipotoka hapo wakaelekea kwenye chumba kingine, na kukuta miili ya watu watano iliyofungwa kwa kuning’inizwa.

“Unyama gani huu?” akajiuliza Hosea. Wakatazama mwili mmoja baada ya mwingine na kuitambua miili ile kuwa ni ya watu ambao walipotea katika mazingira ya kutatanisha na hawakuonekana tena, mmoja wao akiwa Mwanasiasa machachari kabisa.

“Nimegundua kitu,” Simbeye akasema huku akiwageukia wenzake.

“Nini Inspekta,” Hosea akauliza.

“Kutokana na watu tuliowakuta humu wakiwa marehemu, na mikasa yao ambayo jeshi la polisi lilichukua kama vyanzo vya upotevu wao, kuna mtandao unaofanya kazi hii,” Simbeye akasema.

“Yeah, upo sahihi, siku zote wanalaumiwa Usalama wa Taifa pindi miili hii ikiokotwa haina kuchwa au meno, lakini hii nyumba ya nani? Lazima ukweli ujulikane,” Hosea akaongeza. Walipomaliza kukagua kila kona mle ndani wakatoka nje na kukuta tayari jeshi la Polisi limefika zaidi na waandishi wa habari kama kawaida yao walikuwa wametanda nje wakijaribu kupata habari hii na ile.

Madam S, Chiba, na Jasmine wakaingia kwenye gari maalum iliyokuja hapo, iliyofunikwa kwa vioo vyeusi, bila kupoteza muda ikaondoka eneo lile. Kamanda Amata na Scoba walibaki pamoja na vijana wa Polisi kuhakikisha kila kitu kinaenda sawa. Akiwa kafuatana na vijana wawili wenye silaha waliingia vyumba vya chini na kupita ile milango iliyoonekana kama njia waliyotorokea wale mabwana, walitembea katika njia tofauti, moja ya njia hizo alipia Kamanda Amata na kijana mmoja wa Polisi mwenye silaha, njia nyingine aliingia Scoba na kijana mwingine nay a tatu aliingia Inspekta Simbeye na kijana wake. Cha kushangaza njia hizo tatu hazikukutana, kila moja ilikwenda kutokea mahala pake, na zilitokea kwenye nyumba tatu tofauti, utata. Mara tu baada ya hilo, uchunguzi mkali juu ya nyumba hizo, umiliki wake na uhalali wa kuwa hapo uliendelea; Mjumbe wa shina na Mwenyekiti wake walikuwa katika hali ngumu ya kuhojiwa hili na lile. Walipopata majibu ambayo kwayo yaliridhisha wakawaacha na kuondoka zao.

SHAMBA – baada ya siku 3

MADAM S, CHIBA, JASMINE, SCOBA, GINA NA KAMANDA AMATA wote walikuwa wameketi katika meza kubwa ya duara, kila mmoja mbele yake alikuwa na kabrasha lililojaa makaratasi. Walikuwa na majeraha ya hapa na pale, Gina bado alikuwa akiendelea kuuguza jeraha lake lakini sasa akiwa chini ya uangalizi wa Dkt. Jasmine.

Ukimya ulichukua nafasi kwa kila mmoja, walikutana tena katika meza hiyo ambayo daima wakikaa hapo basi ujue kuna maamuzi magumu ya kufanya. Gina alijigeuza na kujiweka vizuri kitini kwake huku mikono yake ikiwa juu ya meza na sura akiwa ameikunja kidogo.

“Pole sana Gina,” Madam S alimpa pole mwanadada huyo, akajikohoza, “Niliwaita siku tano zilizopita tuonane kwa kikao cha dharula lakini baadae nikagundua kosa nililolifanya, anyway, haina haja ya kuljadili bali tuangalie lile ambalo sasa ndio nimewaitia kabla ya kutazama lile nililotaka niwaeleze siku tano zilizopita ambalo litamhusu Kamanda zaidi,” akaongeza, alionekana wazi hata uongeaji wake haukuwa ule wa kawaida kwani

bado alihisi maumivu ya hapa na pale na alihitaji mapumziko. Kipindi hicho cha siku tatu, T.S.A wote walikuwa pamoja Shamba, huko Gezaulole, wakipumzika na kuweka mikakati mipya, hakuna aliyejua walipo isipokuwa wao wenyewe.

“Kurasa ya kwanza kabisa kuna majibu kutoka kitengo cha utambuzi wa alama za mikono na vidole,” madam Sakawaambia na kila mtu akapekua jalada lake na macho kuyatumbulia hapo.

“Is it?” Gina alikuwa wa kwanza kupayuka.

“Yes It is,” Chiba akadakia. Wote wakamtazama kwa jicho kali.

“Una maana gani?” Madam akamuuliza.

“Nilikuwa nasubiri tu haya majibu kama yataoana na yangu, nilipozifanyia crossmatch hizi alama za vidole ambazo nilizipata kwenye vitasa vya milango ya mwisho ya vile vyumba vya chini, licha ya hivyo tu niliwahi kupata baadhi ya picha zao sekunde chache kabla hawajatoroka lakini sikuwa nauhakika nao kwani siku hizi teknolojia imekuwa; mtu anaweza kutengeneza sura ya Rais na kuivaa, hivyo sikuliweka wazi hili, lakini niliwaona na kila mmoja alikuwa mahala pake, bila kinyago cha usoni,” akawaeleza kisha akanyanyuka na kuiendea droo ndogo akatoa flash na kuipachika kwenye kompyuta mpakato, kisha akawasha chombo cha kutolea picha ukutani na dakika moja baadae picha zilianza kuonekana.

Pancho Panchilio, mfanyabiashara mkubwa nchini, mshawishi wa mambo mengi ya kisiasa, mwenye asili ya Kihindi, watu wengi walimjua kama si kwa jina basi kwa sura. Mhindi huyu alilindwa kwa jinsi zote, hagusiki. Alikuwa tajiri sana mwenye malori makubwa ya kusafirisha, aliwekeza kwenye sekta ya usafiri hasa sekta ya anga. Kwa ujumla alikuwa mwema mbele ya Watanzania, alitoa misaada mingi hapa na pale, alijenga mahospitali, mashule na kusaidia watoto yatima sehemu mbalimbali za nchi.

Picha ya pili nayo ilitia shaka kwa wote angu waliposoma katika lile jalada na sasa wakiona ushahdi ule wa Chiba kwa njia ya picha. Kigogo mkubwa serikalini, aliyepewa dhamana na Wasakatonge kisha anawazunguka na kuwafanyia mambo yasiyoelezeka kwa maandishi. Maisha yanakuwa magumu kila uchwao ilhali wengine wakitunisha matumbo yao kwa njia mbadala za unyonyaji na ukandamizaji.

Picha ya tatu nayo ilikuwa yaleyale, Kigogo mwingine kwenye wizara Fulani naye alikuwamo ndani ya jopo hilo la udhalimu.

Haikuishi hapo, Chiba kutoka katika Hard Disk aliyoichomoa katika ile kompyuta yao, alifumua majina mengine ya watu mbalimbali ambao kila mwezi huchukua mgawo wa pesa lukuki kwa mambo yao binafsi, wapo viongozi wa juu, wa kati na wa chini; si wanasiasa tu hata wafanyabiashara nao walikuwapo tena wengi.

“Inatosha!” Madam akamwambia Chiba, naye akazima ule mtambo wake.

“Sasa nataka operesheni ianze mara moja, taarifa tayari zipo panapohusika, lakini Pancho Panchilio akamatwe mara moja, pamoja na hawa vigogo wawili. Leo hii wanatakiwa kuwa pale kituo cha kati kwa mahojiano zaidi.

KATIKA JENGO NYETI LA SERIKALI

“Boss kuna mgeni anataka kukuona,” sauti nyororo ya Katibu Muhtas ilipenye kwenye sikio la Mheshimiwa Sikotu Sambwene, mmoja wa watu wazito na ‘vingunge’ katika Serikali.

“NIlikwambia sitaki kuonana na wageni au hukunielewa?” Sikotu akauliza kwa ukali, “Mwambie sina muda wa kuonana na watu sasa; aje mwezi ujao,” akaongeza kuongea kwa ukali uleule. Akiwa bado katika kumfokea huyo Katibu wake; mlango ulifunguliwa na Madam S akajitoma ndani mzima mzima na kusimama kando.

“Mgeni wako ni mimi,” akamwambia Mh. Sikotu. Mheshimiwa Yule alijkuta katika wakati mgumu, alijitupa kitini na kumtazama mwana mama huyo aliyeingia kibabe katika ofisi hiyo.

“We; nenda,” akamwambia Yule Katibu wa Mheshimiwa.

“Unafuata nini hapa?” Skotu akauliza.

“Sina jibu la kukwambia ninachokifuata, maana bila shaka unajua ninachokifuata kwako, nina swali moja tu ambalo ukinijibu shida yangu itakuwa imeisha,” Madam S aimwambia Sikotu huku akiwa kasimama mbali kwa tahadhari.

Mhesimiwa Sikotu akajifuta jasho ilhali mashine ya kupoza hewa iikuwa bize ikifanya kazi hiyo, akaweka kitambaa chake ndani ya koti lake na kumtazama mwanamama huyo aliyesimama mbele yake.

“Unasemaje?” akauliza.

“Unafahamu nini au kipi juu ya jumba kubwa la kifahari lililoko Kerege kitalu namba KG/BY 1230p?” akauliza Madam S. Sikotu akabaki kaduwaa, hakuwa na jibu. Madam S hata kabla hajapewa jibu hilo akatupa swali lingine.

“Unajua nini juu ya mwandishi wa habari mashuhuri aliyepotea miezi miwili nyuma?”

“Hivi we mwanamke una kichaa!” Sikotu akang’aka huku akiwa wima macho yamemtoka.

“Na ukichaa wangu ndio umenifikisha hapa leo, ulifikiri ukijiziba sura mbele yangu sintokujua? Kwa taarifa yako kutokana na kazi yangu, sauti zenu wote nyie nimezikariri, hukuweza kujificha mbele yangu ulipokuwa ukiongea, Sikotu, kiongozi mwenye dhamana, unajishusha hadhi kwa tamaa yako ya pesa mzee, utastahafu kwa fedheha baba, hebu jiangalie hapa,” Madam S akamtupia picha kumi na tano zinazomwonesha ndani ya jengo lile ambazo zilinaswa kwa kamera za usalama. Sikotu alizitupia jicho na machozi yakaanza kumtoka.

“Mwisho wa ubaya ni aibu, na mshahara wa dhambi mauti,” Madam S akainua akakusanya picha zake na kuzirudisha mkobani.

“Tutaonana mahakamani,” akageuka na kuondoka, akaufunga mlango nyuma yake na nukta hiyo hiyo vijana wawili waliovalia sare za jeshi la polisi waliingia ndani ya ofisi ile, pingu ikawekwa mezani.

“Siwezi kwenda popote, kwanza ni ninyi ni nani? Nani kawatuma? Ninyi mna kibali cha kunikamata mimi? Mnaitaka kazi yenu au?” Sikotu alikuwa kama akiweweseka, akavua koti na kulitupaa kando, mwili wote ulikuwa umelowa kwa jasho kana kwamba kamwagiwa maji.

Mmoja wa wale askari akatoa waraka ulioidhinishwa kukamatwa kwake, akamwonesha kwa mbali huku akimkatalia kuushika kwa mikono yake. Sikotu hakuwa na la kufanya aliahangaika, Yule askari kijana akamsogezea pigu ikiwa wazi ajipachike mikono yeye mwenyewe. Sikotu akavuta saraka katika meza yake akaitoa bastola iliyokuwamo ndani yake, wale askari wakaweka silaha zao tayari wakimwamuru kuweka chini bastola yake. Akaitumbukiza kinywani kwa minajiri ya kujilipua.

“Weweeee aaacchhhaaaaa!!!” mmoja wa askari akapiga kelele na wakati huo huo mlio wa risasi ulisikika na Mheshimiwa Sikotu akabwaga chini huku damu zikicafua vibaya shati lake, bastola yake ikitupwa mbali.

“Ha ha ha ha haujafa kiongozi lazima ufike mahakamani,” Sauti ya Chiba ilisikika nyuma ya wale askari, wakageuka na kumwona kijana huyo aliyekuwa ndani ya suti nadhifu akiiteremsha bastola yake. Chiba alipiga mkono wa Sikotu kwa risasi yake na kuumiza vibaya kiganja chake kabla hajajilipua.

WAKATI HUO HUO – ofisi nyingine ya serikali

“Una la kujitetea hapo?” Scoba na Gina walisimama mbele ya meza kubwa wakimtupia swali hilo mtu mkubwa mwenye tumbo la maana akilikuna kwa mbali. Alionekana wazi kuchanganyikiwa kwa hilo, hakuwa na la kujitetea.

“Gina, mtie pingu!” Scoba alitoa amri na Gina akaitekeleza. Gavana wa benki kuu ya Tanzania, Dkt. Shekibindu akavikwa pingu na kutolewa ofisini mpaka nje kwenye gari ya polisi, na moja kwa moja akapelekwa kituo cha kati kwa mahojiano zaidi.

WAKATI HAYO YOTE YAKITUKIA…

Kamanda Amata alisimama mikono yake akiwa kaikutanisha nyuma ikining’iniza bastola yake ndogo ya Kiitaliano ijulikanayo kama Beretta, huku usoni kajivika miwani safi nyeusi, suti yake ilimkaa vyema mwilini, kiatu chake kilichong’azwa kwa kiwi hakikuongopa kuonesha taswira ya kila kilichokaribu.

“Hajaonekana kabisa ofisini,” Msichana aliyeonekana kama Katibu wa Pancho Panchilio alimjibu Amata kwa swali aliloulizwa sekunde chache zilizopita.

“Tangu lini?” akauliza tena.

“Ana siku nne sasa, mara ya mwisho aliondoka hapa majuzi akiwa kama aliyechanganyikiwa, sikujua anakwenda wapi na wala hakusema, tangu hapo hakurudi tena,” Yule msichana akaendelea kueleza.

“Unapajua nyumbani kwake?”

“Hapana, mimi ni mfanyakazi tu huwa tunaonana hapa ofisini bas,” akajibu.

“Ok, naomba niingie ofisini kwake,” Kamanda akaomba.

“Pamefungwa, na funguo ni moja tu anayo mwenyewe,”

“We niruhusu au nikataze,” Kamanda akasisitiza.

“Sawa ingia, mi nakwambia hayupo,” Yule mwanadada

akaendelea kujibu.

“Usihofu, mimi ni afisa wa polisi,” akamwonesha kitambulisho bandia cha upolisi. Akauendea mlango na kuufungua kwa jinsi zake zilezile. Ilikuwa ofisi pana yenye kila kitu ndani yake, hakukuwa na mtu, akaiendea simu na kuitazma kisha akabonyeza kitufe cha kuiruhusu itoe ujumbe wowote uliopo.

“…Mheshimiwa booking yako imekamilika na tiketi yako tutakutumia soon katika email yako… enjoy your flight…”

Akili ya Kamanda ilisimama ghafla, “Katoroka!” akajikuta anajiuliza bila kupata jibu, akaiendea kompyuta ya mezani na kuipekua hapa na pale mpka alipopata email ya Panchilio ambayo ilikuwa wazi bila kufungwa akapekua e mail zilizoingia saa sabini na mbili zilizopita. Ilikuwa ni hiyo email ya tiketi ya ndege iliyoondoka saa arobaini zilizopita na ndege moja ya shirika la huko Uarabuni, safari yake ilionekana kuishia Bangalore, India.

“Hayawani huyu kaniwahi,” akawaza huku akitoka na nakala ya ile ytiketi aliyoitoa kwenye mashine kule ndani.

“Unaitwa nani?” akmwuliza Yule binti alipokuwa akitoka.

“Naitwa Ruth,”

“Mwenyeji wa wapi?” akamwuliza.

“Wa Arusha,” akajibu.

Kamanda Amata akamtupia jicho la wizi huku akiiondoa miwani yake usoni na kutuza muono wake juu ya kifua cha binti huyo kilichojaa vyema, matiti yaliyowekwa ndani ya sidiria yakitamanisha kila lijari. Kamanda akameza mate, akajikohoza, akaingiza mkono mfukoni na kutoa kadi ndogo ya kibiashara akampatia.

“Tuonane jioni ya leo, Hotel ya Land Mark, saa mbili kamili usiku,”

Ruth akamtupia jicho kijana huyo aliyekuwa akiipachika tena miwani usoni mwake, akaibetua midomo yake na kuuma chanda chake kwa meno ya mbele.

“Ok!” akaitikia. Kamanda Amata akauona mshtuko wa wazi mbele yake kutoka usoni mwa Yule dada, akageuka nyuma na ndipo alipogundua kuwa hawako peke yao, watu wawili walisimama nyuma yake, waliojazia kimazoezi. Akageuka na kupita katikati yao akaondoka na kuwaacha. Alipolifikia gari lake akasimama na kugeuka nyuma, akawaona wale vijana wamesimama mlangoni wakimwangalia. Akasimamisha tax na kuondoka huku akiliacha gari lake palepale.

HATIMA

“Pancho Panchilio ametoroka,” kamanda alimwambia Madam S walipokutana katika mgahawa wa Steers.

“Atapatikana tu, na lazima tumpate iwe kwa mvua iwe kwa jua,” Madam akajibu.

GEREZA LA UKONGA saa tatu baadae

“Mmefurahi sasa sio? Maana rafiki zenu wamekuja kuungana nanyi, msijali tunamleta na Yule Gabacholi, tunamfuata hukohuko India,” Madam S akamwambia Kanayo na Mahmoud Zebaki waliokuwa wakitumikia kifungo chao.

“Tunakata rufaa!” Kanayo akajibu.

“Kateni tu kwani nimewafunga kamba, hiyo ni haki yenu kimsingi na kikatiba,” Madam S aliwajibu huku akinyanyuka na kuondoka.

Kanayo akasonya kwa gadhabu, “Our day will come!”(Siku yetu inakuja) akamwambia Madam S. akageuka kumtazama Kanayo O Kanayo, “Yes, will come soon, we shall face each other in the battle field,” (ndiyo inakuja punde tu, tutaonana kwenye uwanja wa mapambano)

§§§§§

Aiwa chumbani kwake, alimtazama Gina aliyekuwa mbele yake na vazi jepesi la usiku, Amata alijikuta akipata shida maeneo ya kati kwajinsi mwili wa mrembo huyo ulivyokuwa ukiita. Gina akageuka na kumtazama.

“Vipi? Arts of War ni ipi kwa mi na wewe sasa?” alimuuliza huku akijilaza ktandani na kuruhusu sehemu kubwa ya mwili wake kujiachia wazi.

"…mwili huo uliookotwa kando kando ya pwani ya Coco ni wa msichana wa kati ya miaka 25 na 30. Kamanda wa Polisi mkoa wa Dar es salaam Ndugu Sekuru, amethibitisha kutokea tukio hilo na uchunguzi unaendelea kuwabaini waliofanya mauaji hayo…"

Sauti ya Mtangazaji wa TV ilimtoa Kamanda Amata katika kifua cha Gina na kutupia macho katika kioo hicho.

"Shittt!" akang'aka, "Wamemuua Ruth!" akaongeza huku akisimama.

"Ndio tatizo lako, ukisikia mwanamke kauawa unahuzunika lakini mwanume unapotezea, mwanaume Malaya wewe!" Gina akalalamika huku akikaa kitandani.

"Gina, huyu ni sekretari wa Pancho Panchilio," akamweleza.

"What? Usinambie," Gina naye akahamanika.

"Kwa nini wamemuua msichana mzuri kama Yule, masikini Ruth!"

MWISHO

simulizi yenye ucheshi


FRANK MASAI
THE LOST BOYS
Three men in love with one chick
RK
A RAJKAJ ENT

SIMULIZI The Lost Boys

1

ALFRED MUSITA.

ANAPENDA kujiita Fred. Jina ambalo kazoeleka kuitwa na rafiki zake pamoja na ndugu zake pia. Ni kijana mwenye asili ya Kiarabu na Kiafrika, yaani Chotara kwa lugha yetu pendwa ya Kiswahili.

Ni kijana mwenye kila sifa ya kuitwa mtanashati na mtu yeyote duniani. Akiwa kavaa kofia au mzula, waweza sema huyu ni muafrika wa kawaida tu!, ila akivua ndiyo utamtambua kuwa ni mchanganyiko hasa kutokana na nywele zake nyingi na zilizojiviringa vizuri kabisa. Kwa kifupi jamaa ni mzuri na mtanashati.

Baba yake ambaye ni maarufu kwa jina la Mzee Musita, ni Mtanzania halisi kabisa kutoka Mbeya. Na mama yake ni mtu wa Iran.

Alfred au Fred, yeye aliamua kuchukua dini ya baba yake ya kikristo kwa sababu muda mwingi aliishi na baba kuliko mama.

Baada ya kumaliza kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya wavulana, Bwiru, Fred alichaguliwa kuendelea na masomo yake ya kidato cha tano na sita Morogoro Sekondari, na alichukua masomo ya biashara kwa sababu ya hamasa aliyokuwa akipewa na baba yake Mzee Musita, ambaye alikuwa ni maarufu sana hapa Tanzania kutokana na biashara mbalimbali alizokuwa anazimiliki.

Alipomaliza kidato cha sita, matokeo yake yalikuja vizuri, hivyo alichaguliwa kuendelea na masomo hayo katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam au UDSM kama wengi hapa Tanzania walivyokiita. Na kama alivyokuwa anaota kila siku, aliweza kutimiza ndoto yake kwa kwenda kuchukua masomo ya Uhasibu.

Kwenye maisha yake tofauti na ya shule, Fred alikuwa ni mpole na mtulivu sana. Hakupenda kufuatilia wanawake japo wanawake wengi walimtaka kimapenzi na wengine kuomba japo wawe naye tu!. Naweza kusema ni dini ambayo alikuwa ameiweka kichwani mwake, ndiyo hasa ilimfanya ajiweke mbali na jinsia ya kike.

Aliishi kwa njia ya maneno ya MUNGU. Hata kwa wale wanawake waliokuwa wanamtakia wazi kuwa wanampenda na kumuhitaji, alikuwa anawakatisha tamaa kwa kutumia maneno hayo kutoka kwenye vitabu vitakatifu.

Kuhusu wazazi wake hasa baba yake, alikuwa si tajiri sana wala masikini kupindukia. Biashara alizokuwa anazifanya, zilikuwa zinampa chakula pamoja na makazi mazuri kabisa ya kulala yeye na mwanae yule wa pekee. Kila alichokitaka Fred, alikipata kwa wakati muafaka kama alivyoahidiwa.

Mama yake Fred alisha-talikiana na Mzee Musita hivyo hakuwa mtu wa mara kwa mara kuonana na Fred, na hata wakionana basi ni kwa muda mchache. Hiyo ni kutokana na mme wake mpya kuwa anambana sana pamoja na wivu.

Na sababu kubwa ya Mzee Musita kutalikiana na Mama Fred, ilikuwa ni rangi ya watu hawa wawili, mmoja Mwarabu na mwingine Mnyakyusa halisi, yule mweusi kabisa. Hapo wazazi wa Mama Alfred, waliingilia na kumtaka mtoto wao aolewe na Mwarabu mwenzake, na hicho ndicho kilichotokea.

Ukitoa Mama Fred kuonana na mwanae uso kwa uso ambapo ilikuwa nadra sana. Walikuwa pia wanawasiliana katika mitandao ya kijamii na MMS.

Neno la dini, ndilo lililokuwa kipaji chake huyu bwana mkubwa.

Hiyo ni kwa kifupi kuhusu Alfred Musita.

HASSAN JENGE.

Huyu alipenda kujiita Hans J, lakini wenzake walishambadilisha jina hilo toka akiwa kidato cha pili kwa kumuita Crazy Hans au kwa Kiswahili Kichaa Hans. Hiyo ni kutokana na mambo pamoja na tabia aliyokuwa nayo.

Hans J, yeye alikuwa ni mrefu kiasi, huku mwili wake ukijengwa kwa rangi ya maji ya kunde.

Baba yake, Mzee Jenge, alikuwa ni Mngoni na mama yake alikuwa ni Mchaga. Mchanganyiko huo, ulimfanya Hassan aonekane ni mtanashati kupindukia.Ndiyo maana yake, jamaa alikuwa ni Handsome haswaa.

Kuhusu tabia huyu jamaa, unaweza kusema ni mhuni sana kama ukimuangalia kwa nje tu!. Kila muda nywele zake zilikuwa tim-tim. Na alipenda sana kuvaa suruali za jinzi na kuzipiga mlege mkubwa tu.

Fulana zake mara nyingi zilikuwa ni mitumba tu. Hakuwahi kuingia dukani na kununua shati au nguo yoyote humo.

Licha ya hayo yote, yaani kuvaa kihuni, kutimua nywele, na kuvaa vitu vya mtumba, huyu Hans alikuwa anajipenda sana. Muda wote alionekana msafi wa kila kitu.Hizo nywele japo zilikuwa tim-tim, lakini zilikuwa ni safi na za kung'aa kutokana na mafuta aliyokuwa anayapaka.

Mwili wake uliyojaa kiasi, na mavazi aliyokuwa anayavaa, ndicho hasa kilimfanya huyu jamaa azidi kuteka wanawake wengi pale alipokuwa anasoma na kuishi.

Kidato cha nne, yeye alimalizia Makongo na baadae aliamua kuendelea na kidato cha tano na sita katika shule ya Sekondari Merriwa iliyopo Dodoma. Alipomaliza masomo hayo, alipata alama za juu pia, na kuchaguliwa kwenda kuendelea na masomo yake katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Alikuwa ni mtu wa Sayansi, na aliweza sana kuyamudu masomo yake hayo. Mara nyingi alikuwa anafanya mambo ya hatari sana na ya kushtua kwa kutumia hiyo Sayansi yake, na ndio sababu kubwa ya wanafunzi wenzake kumuita Crazy Hans.

Akiwa kidato cha pili katika shule ya Muheza Muslim iliyopo Tanga. Huyu Hans aliwahi kuchukua kemikali na kuzichanganya kwenye chombo kimoja, na baadae alichukua mchanganyiko huo na kuufungia kwenye chupa ya soda. Aliporidhika, akatoka nje na kuitupa chupa ile kwenye eneo lililokuwa halina watu.

Chupa ilipodondoka, eneo lile la shule lilikuwa kama limevamiwa na magaidi kutokana na mlipuko uliotokea pale. Ilikuwa ni mshike-mshike wa kufa mtu pale shuleni, kuanzia waalimu hadi wanafunzi. Na hata Hans alipoitwa kujibu mashitaka, wala hakuwa na wasiwasi.

Pale alipofukuzwa shule kwa kitendo kile, yeye aliona hamna shida. Uwezo waliokuwa nao familia yake, ulimfanya apelekwe Makongo, ambapo kama ukichaa, ndiyo ulimpanda vya kutosha.

Nje ya maisha hayo, Hans J alikuwa ana wadogo zake wawili wa kike ambao wakati yeye anaingia UDSM, wao walikuwa kidato cha nne. Wakati huo, baba yake alikuwa ni daktari bingwa hapa Tanzania na mama yake alikuwa ni Mbunge wa viti maalumu.

Hivyo suala la umasikini kwao, wala halikuwepo kabisa. Walikuwa wanajiweza sana, na hawakupata kichwa, eti kwa kuwa mama na baba matajiri, basi tusisome. Hiyo ilikuwa hamna kwa watoto wa familia ile, walikuwa wanasoma kupita maelezo.

Uso wake mpana na wenye usiriazi kila mara, pamoja na kutokuwa na chunusi wala vidoa, huku ukipendezeshwa na rangi ya maji ya kunde, ndiyo nyenzo kubwa iliyofanya wasichana wengi washindwe kulala bali kumuwaza Hans J.

Jamaa alikuwa anatakwa na wanawake wengi sana, kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Lakini hakuwahi kuwa na yeyote kati yao.Alikuwa ni mgumu kupitiliza, yaani alikuwa haelewi ni nini maana ya mapenzi na wala alikuwa hana mpango wa kujua maana yake.

Ukiwatoa mama na wadogo zake, Hans hakuwahi kuwafikiria wanawake wengine wa nje hata mara moja katika kalia yake ya maisha.

Jina lake la Crazy Hans, halikuja hivi-hivi. Licha ya vituko vingi vya kisayansi alivyokuwa anavifanya, lakini pia alikuwa ni bingwa wa kuwaumbua wanawake hadharani hasa wale waliokuwa wanamtaka. Hilo pia,lilichangia jina la ukichaa kuendelea kukua siku hadi siku.

Mabinti wengi walikuwa wanawatumia wadogo wa Hans kumletea ujumbe za mapenzi. Lakini mara nyingi kwa Hans, mjumbe alikuwa anauawa tu!. Hao madogo walikuwa wanachezea sana makwenzi na mateke kama wakithubutu kuleta ujumbe hizo.

Sasa kafaulu kuingia UDSM. Huko msimamo wake utakuwaje? Endelea kusoma tu!

JUNIOR KING NICKSON.

Au King Jr kama alivyojiita kisanii. Huyu yeye alimaliza kidato cha nne katika shule iitwayo Bunazi iliyopo Mwanza. Na baada ya kumaliza na yeye akafanikiwa kuendelea na masomo yake ya kidato cha tano na cha sita katika shule ya Sekondari ya Mwanza, iliyopo huko-huko Mwanza. Yeye alikuwa ni mpenzi wa masomo ya sanaa au arts kwa kiingereza, na aliyafaulu vizuri sana, hivyo naye akachaguliwa kuendelea katika chuo hicho-hicho cha Dar Es Salaam au UDSM.

King alikuwa ni msanii halisi kabisa. Uwezo wake wa kuongea na ucheshi uliopindukia kutoka mdomoni mwake,ndiyo unanifanya niseme haya yote na ndiyo chanzo cha King kuwa maarufu sana katika kila shule aliyokuwa anasoma na kwa kila mtaa aliokuwa anaukanyaga.

Ukitoa hayo ya ucheshi na wingi wa maneno,King alikuwa anaweza kupiga gitaa na kuimba vizuri sana kama R.Kelly au Ne-Yo. Sauti yake maridadi na ya kuvutia,ndiyo ilifanya watu wengi kuja karibu yake na kupata radha maridhawa ya muziki wa Junior.

Nje ya hayo,King yeye alikuwa ana pacha wake wa kike ambaye walikuwa hawaendani hata kidogo,kuanzia tabia hadi sura. Wakati King Jr akiwa bingwa wa sanaa,dada yake alikuwa ni mkali wa mambo ya Sayansi,hivyo ukiwakuta pamoja,basi ujue kuna kitu kinaendelea,labda wameagizwa au wanakula. Kwa kifupi walikuwa hawaendani.

Familia yao ilikuwa ni ya kawaida sana. Baba alikuwa ni Mkufunzi wa chuo cha Mtakatifu Aguastino na mama yeye alikuwa ni Afisa kilimo na mifugo pale Mwanza mjini.

Junior alikuwa si mrefu wala mfupi.Pia alikuwa ni mweusi kiasi huku uso wake mwembamba na wa kuvutia ukimfanya azidi kuwa mtanashati. Macho yake ambayo kiasi fulani yalikuwa ni ya kurembua,ndiyo yalikuwa kivutio cha wanawake wengi pale alipokuwa anasoma na kulipokuwa na makazi yao.

Ukiachilia mbali umbo lake la kisukuma lililobeba kifua kipana kama cha wacheza mpira wa kikapu,Junior pia alikuwa ni bingwa wa kuyapangilia mavazi yake. Kila mara alikuwa ni msafi kama macho ya samaki aliye-baharini.

Kama kawaida ya wasanii. Junior alikuwa ni mjanja na mwepesi sana katika kuongea kama nilivyosema hapo mwanzo,lakini tatizo lake yeye alikuwa ni muoga sana wa wanawake pamoja na mapenzi kwa ujumla.

Kila muda alijiweka mbali sana na mapenzi,hiyo ni kutokana na kusikia habari kutoka kwa watu wa karibu yake,ya kuwa mapenzi yanawaumiza. Mapenzi hayo-hayo,ndiyo yalimfanya dada yake aamue kwenda Sayansi. Sasa Junior,akawa hataki hata kuyasikia bali alipenda kuyaandika na kuyaimba.

Kama ilivyokuwa kwa Hans na Fred,naye Junior au King,wanawake walikuwa wanajigonga kwake kama kawaida,ila ujanja wake sijui niseme wa kijinga,aliweza kuwakimbia.

Mara kwa mara pacha wake alikuwa anakuja na rafiki zake mbalimbali nyumbani kwao,na kwa makusudi kabisa,Junior anaachiwa uwanja wa kuongea na rafiki mmoja-wapo. Basi yeye huongea hadithi nyingine tofauti,na wala alikuwa amuangalii huyo msichana ishara zake,bali akiona msichana huyo anaweka mikao ya ajabu-ajabu,yeye huchukua gitaa lake na kutoka nje na kuanza kulipiga.

Sasa kabahatika kufaulu vizuri kidato cha sita na kafanikiwa kujiunga na chuo kikuu cha Dar es Salaam katika mchepuo wa Sanaa au Arts. Na moja kwa moja baada ya kufika chuo,anapangwa chumba kimoja na Alfred,Hassan na Suarez Emmanuel ambaye historia yake sikuipata,kwani katika mkasa huu hakucheza sana kama walivyocheza hawa watatu wengine. Ila Suarez yeye alikuwa ni mtu wa mpira wa miguu sana na pale chuoni alikuwa anachukua masomo ya uandishi wa habari.Utamuona naye mambo yake.

CHUONI DAR ES SALAAM.

Kila mmoja alikuwa katika harakati zake za kuchukua funguo za Hostel za chuo kile kikuu,ili aende kukiandaa na kumpumzika kwa ajili ya kuianza siku mpya pale chuoni.

Wa kwanza kuingia katika chumba namba sita G (6G),alikuwa ni Hassan Jenge,ambaye baada ya kuingia,alitoa makorokoro fulani yakiwa mengi sana. Akayaweka kwenye kitanda cha pembeni. Kisha akatoa nguo zake kwenye begi na kuziweka kwenye kabati moja la upande wa kushoto. Nguo hizo ni kama alizirundika tu! Kwani alikuwa hajazikunja wala kuzinyoosha.

Baada ya kuridhika na uvundikaji huo wa nguo zake,Hans J alitoa shuka zake mbili na kutandika kwenye kitanda kimoja cha chini kabisa kati ya viwili vilivyofuatana upande ule wa kulia.

Baada ya kuweka mazingira ya kitanda chake katika hali nzuri,akaenda kwenye kile kitanda kingine kilichokuwa upande wa kushoto ambapo ndipo alipoweka makorokoro yake. Akachukua baadhi ya makorokoro yale na kuyaunga vizuri na kupata umbo moja la pembe nne.

Baada ya kupata umbo lile,alichukua kichupa kimoja chenye maji,na kuweka kidogo kwenye lile umbo. Akafunga vizuri kile kichupa,kisha akatoa mfuko mmoja mdogo na kuingiza mkono wake kwenye mfuko ule. Alipoutoa mkono,alitoka na unga-unga fulani wa rangi nyekundu. Akauweka mle kwenye lile umbo,na hapo-hapo yale maji yalibadilika na kuwa kama masizi.

Hapo Hans J alitabasamu na kwa uangalifu mkubwa,alifunika umbo lile kwa kifuniko kimoja kilichokuwa pale pembeni.

Alitikisa kwa nguvu lile umbo na kwa haraka akafungua kabati lake na kutupia yale makorokoro mengine,halafu kwa taratibu sana,akaanza kama kutega lile umbo kwenye kabati lake hasa ile sehemu yenye kitasa. Baada ya kuridhika na kutega kwake,taratibu akaanza kulifunga kabati lake,na alipofanikiwa alirudi kitandani kwake na kujilaza.

Baada ya dakika kama saba,akaingia Alfred Musita au Fred. Yeye alikuwa kabeba begi lake vizuri kabisa huku masikioni akiwa kaweka earphone. Alipofika,akamsalimia Hans J na baadae akaweka begi lake kwenye kitanda cha chini cha upande wa kushoto,kitanda kile-kile ambacho Hans J aliweka makorokoro yake.

Fred alifungua begi lake,akatoa shuka mbili na kutandika kitanda cha juu kwenye ule upande wa kushoto. Baada ya kutandika akatoa biblia na rozali,akaviweka pembeni ya mto wake na kisha akaanza kutoa nguo zake.

“Dogo yaonekana unapenda sana kusali”.Hans alianza kumuongelesha Fred wakati akimuona anapanga nguo zake pale kitandani.

“Sana kaka,si wajua MUNGU ndiye kila kitu?Hata yeye alisema,mimi ndimi nuru ya ……”.Hakumaliza kauli yake Fred akakatishwa na Hans.

“Aaagh,embu nitolee mambo ya upako hapa. Sitaki uanze kunihubiria”.Alimwambia Hans.

“Ha ha haaa. Usijali kaka,ipo siku utaniamini”.Fred akamjibu huku akiendelea kutoa nguo zake kwenye begi,na kuziweka pale kitandani kwa kuzipanga vizuri kabisa.

“Unaonekana upo smart sana dogo,kama shori bwana. Unapanga-panga minguo mwenyewe kama unasafiri kwenda mbinguni”.Hans akaendelea kumchokoza Fred huku akiwa amelala pale kitandani kwake.

“Hamna kaka. Si wajua tena,mende wengi chuoni”.Alijibu Fred kwa upole kabisa.

“Haya bwana. Unapenda sana vitanda vya juu eeh. Shida yako uwe unatuchora vizuri wa chini. Sasa ukizingua tu! Sijui unajidai unapumua pumua,tunakuchoma na bikari”.Hans aliendelea kumzingua Fred.

“Hamna noma kaka,siwezi kufanya hivyo”.Fred alionesha upole wake na heshima kwa Hans.

“Safi sana dogo. Hiyo ndiyo heshima nayoitaka. Kama mkiwa wote hivi humu gheto. Nitafurahi sana”.Hans akamsifu Fred na wakati huo Fred alikuwa kamaliza kutoa na kupanga nguo zake pale kitandani,kisha akaanza kuelekea kule kwenye makabati.

“Dogo angalia hilo kabati la kushoto,usithubutu kuligusa kwani utakuwa na sura mbaya kwa masaa kumi mbili”.Hans akatoa onyo ambalo Fred alilielewa na kutoligusa lile kabati ambalo Hans aliweka vitu vyake.

Yeye Fred akaweka nguo na baadhi ya vitu vyake kwenye kabati mojawapo la katikati.

Pale chumbani kulikuwa na makabati manne.Moja upande wa kushoto ambalo Hans aliweka mazaga yake.Mawili yalikuwa katikati ambapo mojawapo,Fred aliweka vitu vyake. Na lingine lilikuwa upande wa kulia.

FRED akapanga nguo zake kwenye lile kabati na baadae akalifunga vizuri. Pale nje ya kabati alibandika stika yenye ujumbe wa MUNGU,uliosema MIMI NI MZABIBU WA KWELI,NANYI NI MATAWI YANGU.

“Ha ha haa,kwa hiyo dogo wewe ni zabibu au matawi?”.Hans akaanza tena uchokozi kwa Fred.

“Mimi ni matawi kaka. Na Yesu Kristo ndiye mzabibu wa kweli ambaye anajua shida ya matawi aliyoyabeba,na ajuaye jinsi gani ya kuyaokoa”.Fred nae alijibu vilevile kwa heshima na kujiamini.

“Safi sana dogo,nimetokea kukupenda kwa sababu una heshima. Vipi una demu?”Hans akaanza kumchimba tena Fred.

“Demu ndiyo nini kaka”.Akauliza Fred huku akionekana dhahiri kuwa hajui maana ya demu.

“Kha! Haya majanga sasa. Yaani jitu zima kama wewe hujui maana ya demu. Kudadeki,kuna kazi ya kukufundisha ili uwe born-town”.

“Bado sijakuelewa kaka”.

“Demu ni mwanamke. Nimekuuliza una girlfriend?”.

“Ahaaa,ujue na nyie lugha zenu ngumu sana. Demu kwa kikwetu ni kitambaa cha kichwani. Ila jibu lako,mimi sina mwanamke. Nipo mimi kama mimi”.Fred akajibu.

“Hiyo good sana,tena sana. Mademu hawana mpango. Sijui hayo mengine yatakayokuja yana mademu au nayo ni kaaaa…..”.Hans hakumaliza kauli yake akawa ameingia King Junior huku mkono wa kulia kabeba begi na kushoto kabeba chupa ya maji, mgongoni akamaliza kwa kubeba gitaa lake.

“Dogo umeamishia nyumba yote huku?”.Hans alianza kumchokoza King baada ya kumuona.

“Kwanza mimi si dogo,halafu jibu lako ni hayakuhusu,jali biashara yako. Minywele kama mchicha”.Hapo Hans akawa kakutana kisiki cha maneno kutoka kwa msanii Junior au King Junior.

Fred alipoona hivyo,akatoka pale kabatini alipoenda kuweka vitu vyake, na moja kwa moja akapanda juu ya kitanda chake.

“Dogo inaonekana unajidai mtata sana. Hata sijakaa sawa umeshanitupia dongo si ndio eeh”.Hans aliendeleza tabia ya ubabe wake,lakini kwa Junior,ni kama alikuwa anamchampa kwa chelewa aliyevaa jinzi.

“Ndiyo maana yake,na tena kula ngumu kabla sijakushushia hili gitaa kwenye utosi wako”.Mapigo yakajibiwa na Junior.

“Mabisholoo kama nyie dawa yenu ni kuwapiga mabomu tu! Sasa ngoja. Mimi naitwa Crazy Hans,na kama nilivyo,ndivyo nilivyo hata kitabia”.Hans aliongea huku bado akiwa pale kitandani.

“Hainihusu mimi. Uwe Crazy au mtambo,mimi nakula kwa hela yangu na wewe yako. Kama vipi funga loud spika hilo”.Junior aliongea huku akitua vitu vyake kwa kuviweka kitanda kilicho chini ya kile cha Fred aliyekuwa kimya akiendelea kujiangalizia filamu ya wababe wale.

Junior baada ya kuweka vitu vyake pale kitandani,akafungua gitaa lake na kisha akalijaribu kulipiga na baadae akakaza nyuzi na kuzidi kuendelea kulipiga.

“Oyaa,makelele bwana. Unadhani tupo THT hapa. Tunataka kupumzika,wengine tumetoka mbali”.Hans alikuja juu na kwa kuwa Junior alitambua kweli kafanya kosa,aliacha na kisha akaanza kupangua nguo zake kwa ajili ya kuzipanga kama walivyofanya wengine.

“Oya Mzee wa Upako jina lako halisi wewe ni nani?”.Hans alimuuliza Fred ambaye wakati huo alikuwa anasoma biblia huku Junior akiwa anaweka nguo zake kwenye kabati la mwisho kabisa ambalo lilikuwa bado halijawekwa kitu.

“Mimi naitwa Alfred Musita kaka. Wewe jina lako pia ni nani?.Fred alijibu na kuuliza.

“Mimi naitwa Hassan Jenge au Hans J The Crazy Hans. Unachukua nini hapa?”.Hassan akaendelea kudadisi.

“Hapa nataka kusomea masomo ya Uhasibu kaka”.

“Okey. Naona una mchongo heavy sana ndio maana unataka kusomea mambo ya njururu”.

“Sijakuelewa kaka”. Fred alimwambia Hans.

“Nasema inawezekana una sehemu umewekeza kazi nzuri ndio maana umekuja kusomea mambo ya fedha”.Hans alimjibu.

“Ha ha haaa. Ina maana jamaa hakuelewa ulichokizungumza mwanzo?”.Junior aliuliza huku akicheka.

“Jamaa wa upako sana huyu,si unacheki hata kwenye kabati lake? Mtu wa GOD huyu,mtaa kapita nao mbali,ila kwa kuwa yupo karibu na waridi ni lazima atanukia”.Hans akawa kama anamjibu Junior.

“Kwani wewe mwanangu unachukua nini?”Junior akamtupia Hans swali.

“Mimi nachukua masayansi bwana. Nataka siku moja nitengeneze bunduki na mabomu yangu.

Ha ha haa. Ndoto yaweza kuwa kweli,wewe kaza tu!”.Junior alimpa moyo Hans huku akitabasam.

“Na wewe unachukua nini na jina lako ni nani?”.Hans akageuza swali na kumuelekezea Junior.

“Aaa,mimi nachukua mambo ya Arts na jina langu naitwa Junior King Nickson,au King JR kisanii zaidi”. Junior akajibu.

“Basi fresh,naona kuna wa biashara,sanaa na mwanasayansi. Sijui huyo anayekuja atakuwa mpishi au?”.Hans akaendeleza maneno yake.

“Ha ha haaa,yawezekana atakuwa msafisha vyoo,maana UDSM inatoa hadi hiyo course sasa hivi”.Junior naye akamuunga mkono Hans.

“Ha ha haaa. Inaonekana kijana wewe ni wa komedi sana. Vipi una demu?”.

“Aaagh. Hayo tuwaachie bongo muvi. Mademu sitaki hata kusikia habari zao”.

“Huo ndio mpango mzima,siyo unakuwa na kidemu kinachuna hela kichizi. Halafu baadae kinakutosa. Sifanyi ujinga huo”.Hans aliongea lakini alikuwa kamuachambali sana Fred kwa lugha aliyokuwa anaitumia.

“Kwa hiyo na wewe huna ye bebee?”.Junior akadondosha swali kwa Hans.

“Si mimi tu! Hata Mzee wa Upako hapo juu”. Hans alijibu huku akimuoneshea kidole Fred.

“Basi good. Hili gheto litakuwa la mabachela,atakae kuja kama anakindimu chake,tunamkurupua”.Junior aliongea huku akifunga kabati lake baada ya kuweka nguo zake vema.

“Eee,kama kawa kama dawa. Nduki kali anatolewa mpaka anachachawa”.Hans alimjibu Junior wakati huo Junior alikuwa anatandika kitanda chake.

Kimya kikatanda kidogo. Na mara mlango ukafunguliwa akaingia jamaa mmoja mrefu na mweupe. Alikuwa kabeba mabegi mawili makubwa na mgongoni alikuwa ana-begi lingine dogo.

“Niaje wazee”.Jamaa yule aliwasalimia wakina Junior kwa kuwapa tano.Lakini kwa Fred ikawa tofauti kidogo,yeye alitaka kushikwa mkono kama wa-baba.

“Mwanangu vipi?Mbona unataka kujidai Kawawa hapa. Embu kunja ngumi na kugonga hapa”.Yule jamaa alimwambia Fred,naye Fred akatii.

Jamaa yule alionekana ni mhuni kupita hata wakina Junior na Hans. Hata mambo yake,alionekana kama anavuta bangi hivi au ni mtu wa mtaani sana.

“Naitwa Ban Diho. Nachukua Education. Wewe mwenzangu unaitwa nani?”.Ban alianza kujitambulisha na kisha akataka kuanza kuwajua wakina Junior huku akianza na Fred.

Hapo kila mmoja akajitambulisha kwa mwenzake,na baada ya Ban kuridhika na utambulisho ule,alianza kupanga vitu vyake.

“Oya toka sehemu hiyo ya chini,ni yangu toka nyumbani mimi nilishaiwahi”.Ban alimwambia Hans baada ya kutoridhika na ile nafasi ya juu ya kitanda.

“We boya nini. Unaanza kuleta tabia toka nyumbani unadhani kwenu huku?Nenda zako huko,kama umelewa mibangi hapa watu tumelewa vinyesi. Hatoki mtu hapa”.Hans J alijibu mapigo ya Ban na kumfanya Ban apandishe hasira.

“We kuku unasemaje?”.Ban alikuwa moto kiukweli. Alimfata Hans pale alipo na kurusha kofi ambalo Junior aliliwahi na kulidaka ili lisimkute Hans na kusababisha ngumi.

“Oya,wewe si umekuta watu wameshawahi?Mbona unataka kuleta za Wajerumani na wakati zilishapitwa hizo?”.Junior alikuwa anaongea huku anamsukumia Ban kwa pembeni.

“Kwa hiyo mnanichangia au?”.Ban aliendelea kuja juu na kitendo cha Junior kuamlia kilionekana kama anachangiwa.

“Hamna,mimi naamulia ili msipigane hapa”.Junior aliongea huku akiendelea kumsukumia pembeni Ban ambaye tayari alikuwa mwekundu kwa hasira.

Muda wote Hans alikuwa tayari kwa ugomvi kwani alishasimama na hasira zilikuwa zimemkaba hadi anashindwa kuongea. Fred yeye alikuwa anacheki filamu ya kipekee kabisa pale chini.

“Nakuuliza mnanichangia?”.Ban aliendeleza lile swali lake.

“Hamna bwana mimi nakusihi uache mamb……”.Junior hakumaliza kauli yake,akasukumwa pembeni na Ban,kisha jamaa kwa mahasira yake,akaanza kuvuruga hali ya mle ndani.

Akaanza na kitanda cha Junuior,akatupa tupa mashuka chini na godoro huko. Hakuchoka Ban,akaenda kwenye kitanda cha Hans na kuanza kufanya kama alivyofanya kwa Junior.

“Si mnajidai wajanja,ngoja leo niwaoneshe”.Ban aliendelea kuwa mtawala mle ndani,safari hii alielekea kwenye makabati ya nguo.

“Shika yote,ila hilo la mwisho usijaribu hata kidogo”.Hans alitoa onyo wakati Ban anaenda kwenye yale makabati.

BAN akaanza na kule alipoweka Junior mazaga yake. Akafungua na kuanza kutupa-tupa nguo za Junior hovyohovyo. Hakuridhika,akaenda la katikati alipoweka Fred,napo akavuruga vuruga kama kwa Junior.

“Sasa ni zamu ya huku sasa”.Ban aliongea kwa sauti huku maneno yale alikuwa akimwelekezea Hans.

Muda wote wakina Junior na Alfred walikuwa hawajui Hans kaweka nini mle kabatini,naye Hans wala hakuwa na muda wa kwenda kumzuia Ban aifungue lile kabati.

Ban kwa papara,akalivamia lile kabati la Hans na kulifungua kwa papara ileile. Eee bwana eee,kuna mlipuko mmoja ulitoka pale wa ajabu balaa. Haukuwa wa sauti kubwa bali ni kama wa kukung’uta nguo hivi. Na baada ya mlipuko ule,harufu ya chumba ikabadilika,ikawa kama chooni tena kile choo cha watu waliokula dengu,mbaazi au maharage.

Ban alibaki kasimama pale kabatini kama kapigwa na shoti au kagandishwa na rimoti. Aliporejewa na fahamu aligeuka na kuwaangalia wakina Junior.

Duuh! Jamaa na weupe wake usoni,lakini alikuwa ni mweusi kama jembe jipya au buti la mwanajeshi yule mpya.

Chumba kizima kiliangua kicheko baada ya kuona sura ile. Hata Fred naye hakusita kucheka hadi ilifika kipindi akataka kudondoka pale alipokuwa kalala. Hans ndiyo kabisaa,jamaa alikuwa anacheka hadi analala.

“Hii ni nini?”Ban aliuliza baada ya kujaribu kufuta sana ule weusi. Weusi ule ulikuwa hautoki hata Ban alipojaribu kujifuta na nguo. Yaani ulikuwa umenatia haswa,hata akifuta kwa nguo,nguo inatoka bila hata alama ya yale masizi.

“Utajua mwenyewe,wewe si unajidai mjanja,endelea sasa. Na hayatoki hayo,na hiyo harufu kama umekunya,mzee utajiju. Dawa ninayo mimi tu!”.Hans alimjibu Ban huku bado akiendelea kucheka.

“Nakwambia nipe dawa”. Ban alimjia juu Hans,na kwa kuwa Hans tayari alikuwa kishachokozwa,akamtuliza kwa ngumi kama mbili za haraka,na hata Ban alipojaribu kuzirudisha,aliambulia makofi na kipigo zaidi.

Alipoona kazidiwa,alitoka nje ya chumba kile na sijui alienda wapi. Lakini akili ya Hans ilicheza haraka sana kuliko wote,si mnajua watu wa Sayansi walivyo na akili za hivyo?. Mara moja alikimbilia kwenye kabati lake na kuficha yale makorokoro mengine,kisha akaanza kutupa-tupa hovyo na nguo zake huku wakina Junior wakiwa wanamshangaa wasijue jamaa anafanya nini.

Baada ya kuridhika na ile chaghala baghala aliyoifanya,alimwambia Junior na Fred wajifanye wanaokota vitu vyao,ila kwa taratibu huku wakisubiri ujio wa Ban.

Basi wakina Junior wakaanza kufanya hivyo kama walivyopata maelekezo kutoka kwa Hans. Hazikupita hata dakika mbili.Mlango wa chumba chao ulifunguliwa na Ban aliingia na mzee mmoja wa makamo aliyejitambulisha kama ni Dean wa wanafunzi wa chuo kile. Hans na wakina Junior,wakampa heshima yake,kisha wakaendelea kukusanya vitu vyao.

“Nini kimetokea humu?”.Dean yule aliwauliza wakina Junior.

“Huyu hapa Sir,kaja humu na kuanza kutupiga makofi,tulipojitetea akaanza kuvuruga vitu vyetu”.Junior kwa usanii wake akawa anaongea huku kama analia.

“Wewe ni kweli?”.Yule Dean alimuuliza Ban ambaye alikuwa kafura kwa hasira na ule weusi aliomwagiwa,utaweza kusema jamaa katoka kuchimbwa kwenye mkaa.

“Ticha sijapiga mtu”.Ban akajibu kwa hasira huku akikana lile kosa.

“Na hizo nguo wewe ndiyo umevuruga”.Dean akamuuliza tena.

“Wamenihudhi hawa ticha,wanaleta zao hapa chuoni sio nyumbani”.Ban akawa anaendelea kujibu vilevile kwa hasira.

“Sasa kumbe wewe ndiyo una makosa,ona ulivyovuruga vitu vya wenzako. Haya na huo weusi umetoa wapi”.Dean akaendelea kumuuliza maswali Ban lakini lile swali likawa kama kicheko kwa Hans.

“Si huyo jamaa kwenye kabati lake sijui katega nini,nimefungua kikaniripukia”.Ban akajibu huku kama anajifuta yale madude yaliyomrukia usoni.

“Eti wewe,hiyo ni nini?”.Dean akamuuliza Hans.

“Ticha mimi sifahamu kabisa hiyo ni nini. Alikuja humu ndani hivyohivyo. Sisi tukadhani kachanganyikiwa.Mara kaanza kutupiga,akaona hajatosheka,akaanza kuvuruga chumba chetu. Tulipomgusa kwa kumkanya aache,tukashangaa anatoka na aliporudi,kaja na wewe”.Hans hakuwa nyuma kudanganya.

“Tena katupiga kwelikweli Ticha,sisi huyu hatumtaki hiki chumba,atatuua. Yaani kampiga kofi huyu kaka hapa eti kisa anasoma biblia pale juu”.Junior akazidi kuchombeza maneno huku akimnyooshea kidole Fred kuwa naye ni muathirika wavurugu za Ban.

“Eti wewe. Unaonekana mtu wa MUNGU sana. Huyu kakupiga?”.Dean akamuuliza Fred ambaye alikuwa kapoa sana kuliko wote.

Hans na Junior wakawa wanasubiri jibu la Fred kwani ndilo lingewatoa kwenye ule msala. Na kwa kuwa walijua Fred ni mtu wa dini sana,basi hatoweza kudanganya.

Lakini Fred alijua akitetea kwa kusema hajapigwa,basi yule jamaa angeendelea kuwa kwenye kile chumba.

“Sir. Huyu kaka mimi hadi sasa hivi sijamuelewa ni kwa nini kanivuta toka kule juu hadi chini kisha akaanza kunipiga na kunitukana. Imeniuma sana”.Fred alijibu kisha akaacha kuokota zile nguo na kupanda juu ya kitanda chake,na kilichofata hapo ni kwikwi za kilio kutoka kwake.

Huo ndio ukawa msumali wa mwisho kwa Ban kwani hata kujitetea alishindwa kabisa.

“Wewe ni mjinga,sasa utalipa ujinga wako. Okota hizo nguo moja baada ya nyingine,na kisha zikunje vizuri kabisa na hawa watakuwa wanasema hiyo ni yangu,wewe utakuwa unaweka kwenye kabati husika,sawa?”.Dean alimpa adhabu Ban,adhabu ambayo Hans hakuwahi kuifikiria kama yaweza kutokea.Kwa mara ya kwanza nguo zake zingepangwa vizuri kabatini.

“Lakini Ticha mimi sija….”.

“Muda unaenda,na sibadili mawazo. Wewe bora umalize adhabu yako ili tupange jambo lingine”.Dean alimkatisha Ban na kumwambia aanze ile kazi mara moja,huku yeye dean akienda kwenye kitanda cha Junior na kukaa ili aangalie utekelezwaji wa ile adhabu.

Ban akaanza kupanga zile nguo huku akiuliza ya nani,na baada ya kupewa jibu,aliweka kabati husika.

Ni jambo la nusu saa,tayari likawa limekamilika huku chumba kikirudi katika hali yake ya mwanzo.

“Sasa wewe beba begi lako na nifuate napoenda”.Dean alimwambia Ban na Ban akafanya alivyoambiwa. Wakatoka kwenye kile chumba na kuwaacha Junior,Fred na Hans wakicheka na kufurahi sana.

“Mzee Wa Upako,wewe ni noma. Nilidhani utatusaliti. Dah! Big up sana mzee,nimekubali hii dunia kwa sasa haina mtakatifu”.Hans aliongea akimsifu Fred kwa kitendo alichofanya.

“Aaah,kaka. Dini inakaa pembeni kama unataka kujiokoa hasa katika majanga. Ilinipasa nidanganye ili kujiokoa maana nisingefanya hivyo,tusingesoma humu. Kwa hiyo nilidanganya kwa faida, na sio kwa kumkandamiza mtu japo ni kweli nilimkandamiza”.Fred akajibu huku ametabasamu.

“Basi Fresh Mzee Wa Upako. Nadhani sasa amani itatawala. Ngoja tumsubiri huyo mpya”.Hans aliongea na kumaliza ile hadithi.

Kule kwingine. Ban akapelekwa chumba kumi na mbili A (12A)kikiwa ghorofa ya chini kabisa za Hostel ile.

Alipoingia alifarijika sana,kwani karibu wanachuo wote waliokuwapo mle alikuwa anawafahamu kasoro mmoja tu!,ambaye ndiye aliyechukuliwa na Dean na kupelekwa chumba cha akina Hans.

“Kamanda Ban.Vipi mkubwa?Mbona mweusi usoni tu?”.Jamaa mmoja alimuuliza Ban baada ya Dean kuondoka na yule mwanachuo mwingine.

“Acha tu! Mkubwa Mose. Yaani huko nilipotoka,nimefanyiwa kitu mbaya kichizi”.Ban alimjibu yule jamaa ambaye alikuwa anaitwa Moses Frank.

“Haaa,wajinga gani hao wamefanya hivyo tuwafate sasa hivi”.Jamaa mwingine ambaye pia anafahamiana na Ban aliuliza.

“Achana nao kwanza kaka mkubwa Sunday. Hawa watalipa tu! Wamejiingiza kwa makamanda,watakiona”.Ban alimjibu yule jamaa mwingine ambaye anaitwa Sunday Magembe.

“Ndio maana yake kaka. Waache kwanza,halafu wakishasahau,sisi ndiyo tunaamka. Na watakoma. Wapo chumba namba ngapi?”.Jamaa mwingine aliuliza.

“Wapo kule 6G halafu maboya tu!mwanangu Moi.Sijui hata ilikuwaje”.Ban alijibu pia swali la yule jamaa aliyeitwa Moi Shabala.

“Kwani ilikuwaje man?”.Moses alimuuliza swali Ban,naye Ban alianza kuwasimulia mkasa mzima hadi alipofika pale.

“Pumbavu zao,na watalipa. Hawajui sisi ndiyo wazee wa kazi eeh. Yale ya Bunda,tunaleta huku,watasanda tu!”.Hapo Sunday Magembe aliongea kwa kujiamini

Chumba kile kilijaa marafiki ambao walisoma pamoja katika chuo cha ualimu kilichopo Bunda,na sasa waliamua kwenda kujiendeleza kwa kuchukua shahada ya katika mchepuo uleule wa ualimu. Baada ya kusikia mwenzao kafanyia sivyo na wakina Hans,basi tayari wakawa wameweka bifu.

“Tulia tulia kamanda. Yatatoka tu hayo,mbona unaanza kurudi hali yako?”.Moi alimpa moyo Ban na kweli jamaa akatulia huku kisununu cha kulipa kisasi kikiwa moyoni mwake.

NB:Dean ni yule mtu au mkufunzi anayehusika na tabia za wanafunzi chuoni.

Baada ya Dean kuondoka na kumuacha Ban kule kwenye makao yake mapya,alienda moja kwa moja hadi katika chumba walichopangwa wakina Junior. Akaingia na kuwapa mgeni wao mpya ambaye angekuwa nao mle ndani. Naye Dean akaacha maagizo katika chumba kile hasa akisisitiza nidhamu kutawala. Akapotea eneo lile.

“Oyo. Niaje kaka”.Hans kama kawaida yake. Mzee wa kupokea wageni.

“Fresh Jombaa,ni vipi”.Alijibu jamaa yule huku akiweka begi lake mahala pa kuweza kupekulia vitu vyake vizuri.

“Humu gado tu!We wapi hiyo”.Hans akamuuliza tena.

“Aah,mimi wa Singida kaka. Nimekuja kucheki degree hapa”.Jamaa akajibu huku akifungua begi lake na kuanza kutoa baadhi ya vitu vyake kama mashuka na kuweka katika kile kitanda cha juu ya Hans.

“Jina lako kaka mkubwa”.Junior alienda moja kwa moja kwenye kuuliza jina.

“Mimi naitwa Suarez Emmanuel, man”.Suarez alijibu.

“Ahaa,okey. Mimi naitwa Junior,nachukua mambo ya sanaa. Na hawa wengine watajitambulisha wenyewe”.Junior alijitambulisha na kuwapa nafasi nao wengine wajitambulishe.

Baada ya utambulisho huo,Suarez alimaliza naye kwa kusema yeye anachukua masomo ya uandishi wa habari.

“Okey. Sasa kama wewe mwandishi wa habari,basi fanya kama unanihoji mimi kilichotokea humu”.Hans alianza mbwembwe zake. Akampa Suarez mswaki ndio afanye ni kipaza sauti,halafu akakimbilia kwenye kabati lake na kuchukua koti la suti na kulivaa.

Suarez alikuwa ni mtu wa utani sana,na kwa kuwa alikutana na watu wa aina hiyo,ikambidi naye kuendana nao ili waishi kwa furaha.

“Eheee. Ndugu mheshimiwa. Nimekutana na mtu mwenye uso mweusi sana na wakati sehemu nyingine ni chungwa,alikuwa hapo mlangoni akitokea humu. Waweza kuniambia ni nini kilimtokea?”Suarez alikuwa amemwekea ule mswaki mdomoni Hans ili asikie atakachojibu. Wakati huo yeye Junior alikuwa kaweka gitaa lake begeni na kulifanya kama kamera. Fred yeye alikuwa mtu wa kucheka tu!,maana vile vituko,hakuendana navyo hata kidogo.

“Aaah,jamaa kalipukiwa na bomu la mavi. Ha ha haaa”.Hans alijibu huku anacheka.

“Bomu la mavi ndio bomu gani hilo aisee”.Suarez nae akiwa yupo siriaz na kazi yake,akauliza.

“Ni bomu ambalo nimetengeneza mimi mwenyewe kwa kutumia kemikali zinazotumika kukaushia kidonda hospitali na kemikali ya kutengeneza harufu mbalimbali. Nilifanikiwa kutengeneza harufu ya kinyesi baada ya kuweka mchanganyiko ule pamoja. Na kwa kuwa ile sehemu niliyoiweka ilikuwa ina joto na ni plastiki,basi mchanganyiko ule ukawa masizi”.Hans alimjibu huku akiwa anatengeneza koti lake la suti hasa ile sehemu ya tai.

“Kwa hiyo mheshimiwa umejipanga vipi na mapambano na huyu mtu uliyempiga bomu?”.Suarez aliuliza swali ambalo lilimfanya Hans acheke kabla hajajibu.

“Ndugu mtangazaji acha kunichekesha bwana. Yule nimempiga kama mtoto mdogo humu. Muulize Mzee wa upako”.Hans alijibu.

“Kumbe uliongeza tena kwa kumpiga?”.Suarez aliuliza na kama akaishiwa nguvu,huku ile hali ya utani ikawa inaondoka.

Suarez alikuwa anawajua wale jamaa waliokuwa katika kile chumba. Wote walikuwa wana urafiki na Ban,na wote wanatabia kama za Ban.

“Ndiyo maana yake,nimepiga kama toto dogo hapa”.Hans yeye alijibu kiutani kama kawaida.

“Hivi wajua kuwa kile chumba nilichotoka wale waliopo ni rafiki zake yule jamaa?Yaani namaanisha kwa ulichokifanya ni lazima waje kulipa kisasi”.Hapo Hans alikaa kimya kidogo na kuyachanganua yale maneno kwa kina. Wakati huo hata Junior naye alishusha kamera yake aina ya gitaa na kukaa kitandani. Fred naye macho yakawa kodo kwani naye alihusika sana kumkandamiza Ban.

“Isitoshe wale jamaa wote wana tabia zinazofanana. Yaani ni kama wasela fulani hivi. Na wana tabia za kibabe”.Suarez aliendelea kukandamiza uoga mioyoni mwa Hans na wakina Junior.

“Aaagh!Isiwe kesi bwana. Kwa kuwa ishajulikana,basi tutakuwa makini nao. Cha msingi ni kuwa na ushirikiano. Tunasaidiana kwa kila kitu. Si mkiona napigwa,nyie mnakaa pembeni. Hapa kazikazi,ngumi kwa ngumi,wali kwa wali,wakimwaga ugali sisi tunakomba mboga”.Hans aliongea kwa kujiamini na kuwapa moyo wengine.

“Hapo umenena Crazy. Hapa mkono mkonoe tu!Hamna kuleta maujinga. Wakitupa mabangi yao gheto kwetu,sisi tunaenda kutupa mabomu,uongo wa Baba Paroko”.Junior naye alitoa wazo la kusisitiza kauli ya Hans.

“Mmh! Mimi nitafanyaje jamani?Mbona matatizo haya”.Fred alionesha wazi alikuwa anaogopa.

“Mzee waUpako usijali man. Tutakupa maujanja. Hapa aogopwi mtu. Cha msingi tuwe pamoja kila mara,labda tukiwa tumeenda darasani ndio tuachane,ila kama tupo nje ya darasa,tukae pamoja”.Hans alimtoa shaka Fred.

“Dah! Ila mimi siwezi kupigana wala kupambana nao kimaneno”.Fred alizidi kuonesha udhaifu wake.

“Usijali mzee. Mimi mwenyewe nipo upande wenu. Hawataweza kufanya chochote”.Suarez naye aliamua kuwa upande wa akina Hans.

“Sasa kuna nini tena. Hapa watakaa tu!Labda sio sisi. Hadi waombe msamaha kama wakituchokoza”.Hans alifurahi sana ujio wa Suarez katika kundi lao.

“Basi tuwe na amani na tujipange kwa mashambulizi tu!. Wakitaka vita baridi,mimi nipo hapa,naweza kuongea asubuhi hadi asubuhi tena kwa makelele. Wakitaka vita ya silaha,yupo mzee wa mabomu hapa. Wakitaka kidini dini,tunakuachia Baba Paroko. Wakitaka kutangazwa ujinga wao,tuna kamanda hapa”.Junior aliongea huku akikabidhi majukumu mbalimbali kwa met wake.

“Ndio maana yake. Hamna kudevela”.Hans alimaliza.

Kimya kikatanda na kila mtu alikuwa katika pilika zake binafsi,huyu akipiga gitaa,yule anasoma biblia,mwingine anapanga nguo zake na mwingine yeye kulala tu!.

Maisha ya chuo kwa watu hawa,yakaanza kihivyo. Yameanza kwa kuweka bifu na kundi lingine palepale chuoni.

“Mzee Ban. Naona madude yameisha sasa. Umerudi katika hali yako”.Moses aliongea baada ya Ban kutoka bafuni alikwenda kuoga.

“Kama kawa kaka mkubwa Mose. Sasa najipanga kwa kujibu mapigo ya wale wajinga”.Ban alimjibu huku akifuta maji yaliyokuwa usoni pake.

“Hapa tuwaache kama wiki ili wasahau. Wakiingia,tunawateka wote,halafu ndiyo watatutambua”.Moses aliongea kwa kujiamini.

“Kama kawa. Wewe si ndo mzee wa mipango. Mimi nakusikiliza wewe. Watajuta kuingia anga hizi”.Ban alimjibu Mose ambaye alikuwa analala kitanda cha juu ya Ban.

“Halafu na yule boya aliyesepa humu na yeye kajiunga nao. Leo nimemuona wanaenda wote kupata msosi”Hapo Sunday aliongea.

“Wote watakuwa mulemule. Si anajidai kamanda,tutamwonesha kuwa sisi ndo wenyewe”.Ban aliongea huku akiwa anasura ya kumaanisha anachokiongea.

“Na atakoma kuingia kwenye kile kikundi,mbwa yule. Tutamfanya kitu mbaya mpaka aseme nisameheni”.Moses naye aliongea kwa kujiamini huku akiwa anahasira ambayo imesababishwa na tabia ya ubabe aliyokuwa nayo.

“Ndiyo maana yake. Samaki mmoja akioza wote wameoza hao. Habari ya Bunda tunaidrop pande za UDSM”.Moi alimaliza maongezi yale na mkwara wake bila kutambua hata hao anaowaongelea tayari wamejipanga kwa lolote.

Wiki ikafika tangu chuo kile kifunguliwe huku wale majamaa waliokuwa na bifu wakiwa wamejipanga sana kwaajili ya kulipa kisasi na wengine kwaajili ya kupambana nao.

Hakuna siku ambayo utawakuta kundi la wakina Hans wakiwa peke yao,na hakuna siku ambayo utakuta kundi la akina Ban limetengana. Kwa kifupi walikuwa wanatembea katika makundi makundi kama wahuni au majambazi,hasa ukiwaangalia mavazi yao.

Wale wakina Ban walipenda sana kuvaa mavazi makubwa na kusababisha chuo wawaite WAGUMU. Wale wakina Hans wao walikuwa wazee wa vimodo kasoro Fred ambaye nae ilibidi aendane na mazingira ya chuo. Mambo ya nguo za kushonesha kila siku,yalikuwa yana kazi sana. Heri kununua majinzi ambayo hata bila kunyoosha,wewe unavaa tu!.

Hawa bado walikuwa hawana jina. Ila baadae huko mbele,waliitwa THE LOST BOYS. Hadi leo jina hilo wanalo na wamelikubali japo mwanzoni walipinga sana. Lakini mwisho wa siku walikubaliana nali na kusema kweli sisi ni THE LOST BOYS,yaani wale walioshindwa katika jambo fulani au wale washindwaji. Utawaona huko mbele.

Lile kundi la akina Ban au WAGUMU walishindwa wafanyaje ili walipe kisasi kwa wakina Hans,hiyo ni kutokana na uwepo wa sura zao kila mahali uwaonapo. Yaani ukimuona Fred,basi utamuona Junior,Hans na Suarez.

“Sasa Ban tunafanyaje mkubwa”.Moi alimuuliza Ban siku moja baada ya kuona siku zinaenda bila ya kutimiza lengo lao.

“Hapa cha msingi ni kuvamia gheto lao na kuwavurugia haswa. Kuna jambo moja tu!, ni kutafuta funguo ya chumba chao ambayo ipo nyingine kule tunapochukuliaga risiti. Mimi nitaenda kuinyofoa,wakati huo wewe Sunday utakuwa unamzingua yule Madam wakati mimi nafanya maepe”.Ban aliongea wazo ambalo lilikubalika na wote.

Walikubali hilo kwa sababu walimuamini sana Ban kwa tabia hizo. Alikuwa ni mzoefu wa hayo mambo ya kuchukua kitu bila kugundulika.

Bila kuchelewa,mpango ukafanyiwa kazi kwa Ban na Sunday kwenda ofisi za utawala,na mmoja akabaki mapokezi akiongea na dada wa pale na mwingine ambaye ni Ban akasingizia kuna makabrasha anatakiwa ayawasilishe ofisi ya mkuu wa chuo,hivyo akapewa nafasi ya kuingia mle ofisini na kupekua makabrasha hayo.

Funguo za vyumba za Hostel zile za chuo,zilikuwa zimetundikwa kwenye ubao mmojawapo mle ofisini na kila funguo ziliandikwa namba ya chumba zinapofungua.Hivyo haikuwa ngumu kwa Ban kuangaika kutafuta funguo zilipo.

Dakika tatu,walikuwa wametoka ofisini na makaratasi machache huku kwa chini yake walikuwa wameweka funguo ya kufungulia chumba cha akina Fred. Safari ya kuelekea huko,ikashika nafasi yake.

Baada ya kufika eneo la tukio. Ban Diho alitoa ule ufunguo kisha akafungua mlango ule wa chumba cha wakina Hans. Baada ya kuufungua,wakaingia ndani bila wasiwasi wowote.Wote wanne walikuwepo.

Walichofanya ni kufungua makabati ya chumba kile na kuanza kutoa nguo za waenyeji. Walizizagaza chumba kizima,wakati huo wanachuo wengi walikuwa darasani.

Baada ya kuzizagaza,Mose na Sunday wakatoka nje,kisha wakarudi na ndoo moja iliyokuwa na maji na nyingine ilikuwa na michanga au udongo ili unielewe.

“Sasa hawa si walijidai wajanja na masharobaro,ngoja leo tuwaoneshe”.Ban aliongea kwa jazba na kuchukua ndoo moja yenye udongo na kuanza kumwagia zile nguo za walizozagaza pale chini.

“Kalete mwingine”.Ban alimpa ndoo Sunday akalete udongo mwingine.

Alipoondoa Sunday,Ban akachukua ndoo ya maji na kuanza kumwaga maji juu ya udongo ule uliokuwa juu ya nguo za kina Hans. Hakuridhika na hali ile,akaanza kuukanyaga kanyaga kama anaushindilia chini.

“Kaongeze maji”.Alimpa ndoo Mose na Mose naye akatoka haraka kwenda kuleta maji. Dakika mbili,tayari wote walikuwa chumba kile kwa ajili ya kufanya akili yao inachowatuma.

“Hapa watajuta,wameingia choo cha kike halafu wamemkuta mama mkwe kachutama anajisaidia. Pumbavu zao,hapa ndio Bunda Boys”.Ban kwa hasira alikuwa anaongea huku akichukua tena ndoo ya udongo na kumwagia kwenye vitanda vya wakina Junior.Nao wale watatu wengine hawakuwa nyuma kumsaidia kwa kuendelea kukanyaga zile nguo ambazo tayari zilikuwa kwenye majanga.

Baada ya kumwaga udongo,maji yakafata juu ya vitanda ambavyo ndivyo vinawapa usingizi Junior,Hans,Fred na Suarez.

“Sasa hapo nimeridhika. Twen’zetuni”.Ban aliongea na kuwaoneshea ishara washirika wake waondoke pale.

Haikujulikana wanafanya vile ili iweje,na pia ni upotofu tu uliochanganyika na akili za kijinga ambazo zimetengenezwa na hali isiyokuwa na huruma ndani ya mioyo yao.

Waliondoka mle ndani huku wakiwa vifua mbele kana kwamba kile walichofanya ni sahihi. Lakini kwa kuwa ilipangwa katika maisha yao ije itokee vile,basi ni sahihi kwa walichokifanya,hiyo ni kiimani zaidi.

Nukta ya safari yao iliishia bafuni ambapo walijiweka safi na baadae kwenda vyumbani mwao na kuvaa mavazi nadhifu katika miili yao.

Baada ya unadhifu huo,safari nyingine iliwadia,nayo ilikuwa ni kuurudisha ule ufunguo wa chumba cha wakina Junior.

“Oya sasa hivi zamu yenu Mose na Moi. Njia ni zilezile tulizochukulia huo ufunguo. Ni zilezile za Bunda,hamna kilichoongezeka”.Sauti ya kibabe kutoka kwa Ban iliamrisha kwenda kwa Mose na Moi. Nao kwa kuwa walimwogopa Ban,wakafanya walichoambiwa.

Walitoka mle chumbani huku wakiwa na zile karatasi zao,kwa chini walifunika ile funguo.

Baada ya dakika tatu.Mose na Moi walikuwa ofisi ya utawala huku Mose akiwa mchangamfu sana kwa yule dada wa mapokezi ya ofisi ile. Wakati huo Moi alikuwa kaomba kutafuta karatasi zake ambazo alidai zinahitajika kwenye usajiri.

Kulikuwa hakuna kipingamizi kwa wanachuo kuomba kutafuta karatasi zao hasa pale wahusika wa ofisi ile wanapokuwa katika harakati zao nyingine.

Huku akiwa makini asionekane kwa watu,Moi aliuweka ule ufunguo katika sehemu iliyoandikwa namba ya funguo ile. Na alipofanikiwa,alimwambia yule dada hajaona karatasi zake,hivyo anaenda kuangalia ofisi nyingine. Bila hiyana na kutojua kilichonyuma ya pazia,dada wa watu alikubali na kumruhusu Moi kuondoka.

“Oya umefanikiwa kurudisha funguo ile bila kuonekana?”.Sauti nzito ya Ban iliuliza baada ya Moi na Mose kurudi chumbani.

2

“Usiwe na shaka Kamanda. Huwa sikosei mimi”.Moi alijigamba.

“Basi fresh. Sasa sikilizieni matokeo yakitoka,ha ha haaaa. Wameingia choo cha kike wajinga wale”.Aliongea Ban na wote walitabasamu kwa kujipongeza kwa shughuli waliyoifanya.

VIPINDI vya chuoni viliisha mida ya saa saba mchana, na sasa wanachuo wengi walikuwa wametoka madarasani kwao na kuelekea vyumbani mwao. Wengi kati ya hao,walikuwamo pia wakina Junior ambao walikuwa madarasa tofauti lakini walisubiriana ndio warudi wote chumbani kwao.

Walikuwa wakitembea huku wakicheka kutokana na kushibana kwao kwa muda mfupi. Ucheshi wa Junior na ukichaa wa Hans ulichonganyika na uchangamfu wa Suarez,ulimbadilisha sana Fred. Naye taratibu akaanza kuzoea baadhi ya misemo ya kihuni na aliitumia kuna muda. Alianza kuendana na mazingira yaliyokuwa yanamzunguka.

Baada ya mwendo wa dakika ishirini,hatimaye walifika mlangoni mwa chumba chao na kuingiza ufunguo ambao hakuwa na hiyana. Ulipita,na ulipotekenywa kwenda kulia,nao ulitii na kuufungua mlango wa chumba kile.

“Mama yangu”.Ni Junior alitoa ukelele mkubwa ambao uliwafanya wenzake nao kuingia haraka.

“Haaaa!!!”. Hans alitoa mshangao huku macho yamemtoka pima kama kaona mtu anachinjwa hadharani au kaona mtu anatembea uchi.

“Haiwezekani jamani”.Maneno yalimtoka Suarez huku akiikana ile hali aliyoiona chumbani kwao.

“Mimi naenda kusema kwa Mwalimu”.Fred aliongea hayo huku akianza kutoka nje ya chumba kile kwa lengo la kwenda kutoa taarifa kwenye uongozi wa juu.

“Njoo hapa. Unaenda wapi sasa dogo. Tulia hapa tujadiliane,muafaka ukipatikana ndo waweza kufanya utakacho”.Hans alimvuta mkono Fred na kumrudisha ndani kabla hajatokomea.

“Hapa kuna kujadiliana kaka?Embu ona walichofanya”.Fred aliongea kwa hasira huku akijitoa mikononi mwa Hans.

“Nakwambia tujadiliane ili kwanza tujue nani kafanya hivi na tuna uhakika kuwa kafanya? Sio tunamuita Mwalim halafu tunaanza kumbwela hapa”.Hans aliongea,na ushauri huo wote waliona wa maana.

Wakaingia ndani zaidi ya chumba kile na kutafuta sehemu iliyosafi na kukaa.

“Hapa ni nani mnadhani anahusika?”.Hans alianza kuongoza mjadala ule huku kila mmoja akiwa kimya na uso kumshuka kwa hali waliyokuwa wamezungukwa nayo.

“Ni lazima watakuwa WAGUMU tu!.Si unakumbuka niliwaambia kuhusu wao kufanya kisasi?Yawezekana ndio wameanza hivi”.Aliongea Suarez kwa upole huku akiwa anajitahidi kuficha mahamaniko yake ambayo yangeweza kuzaa machozi.

“Ndio haohao. Hakuna wengine. Kwa kuwa wameanza ku****** zao lazima watalipa”.Aliongea Junior kwa hasira huku akiweka tusi ndani ya maneno yake.

“Hapa twendeni kwa mwalim ili tutoe taarifa. Lazima watakuwa wale tu!”.Aliongea Fred huku msimamo wa kutoa taarifa ukiwa mbele zaidi.

“Hapa hamna kutoa taarifa wala nini.Wakijua kuwa tumechukia,ndiyo itakuwa raha yao. Cha msingi na kusafisha geto na kutoa haya manguo na kuyafua vizuri,au tukanunue nyingine ili tuwakomoe tu!. Haya magodoro nayo twaweza kuyatupa. Kuanza na mwanzo si kitu,ila lazima walipe,haki ya MUNGU watalipa”.Aliongea Junior kwa jazba zaidi.

“Eheee,huo ndio mpango. Hakuna kufaidisha wengine.Hapa ni kimyakimya,tunatoa nguo zetu,halafu hamna kuongea na mtu. Tunafua zinazoweza kutakata,hizi nyingine zilizoharibika,tunazitupa tu!. Haya magodoro,ni ya kutupa. Hayana kazi”.Hans aliungana na Junior.

“Sasa hela tutapata wapi sasa hivi katikati ya mwezi. Boom lenyewe limeisha”.Fred aliongea kwa masikitiko huku akimuangalia Hans.

“Usijali mzee nani. Tutasaidiana katika hilo”.Aliongea Suarez kumpa Fred moyo.

“Ngoja kwanza”.Hans alitoa simu yake ya mkononi na kubofya namba fulani na kisha akaiweka sikioni.

“Haloo Baba shikamoo”.Hans alianza kwa salamu baada ya simu kupokelewa.

“Huku wazima,vipi huko”.Aliendelea kuongea na mzazi wake.

“Na shida na fedha kidogo,kuna vifaa yapasa niwe navyo”.

“Haya nitashukuru sana Baba. Mwambie na mama”.

“Haya Asante”.Alimaliza maongozi yake na kuwageukia wenzake.

“Muda si mrefu kiasi cha kutosha kitaingia M-Pesa”.Hans aliongea kwa tabasamu mwanana.

“Hivi mwanangu,baba yako ndo yule Daktari mkuu wa Muhimbili?”.Junior ilibidi aulize.

“Siyo huko tu!Baba ni daktari bingwa wa magonjwa yote sugu na ni mtaalam wa kufanya opareshen zilizoshindikana”.Alijibu Hans kwa majigambo.

“Na mama yako yupo?”.Fred aliuliza.

“Mama ni mbunge wa viti maalum”.Alijibiwa.

“Mhh! Haya kaka. Ngoja tuone”.Aliongea Junior na kuacha maongezi. Hapo kilichofuata ni kusafisha chumba chao na kutoa nguo zao zote. Uzuri hawakuvunja vitu vya mle ndani,wao waliharibu nguo na sehemu ya kulala.

****

Ni muda wa saa kumi na mbili jioni.Tayari walisharudi chuoni kutoka kufanya manunuzi ya vitu vyao muhimu. Kiasi cha laki saba alichotumiwa Hans,kilitosha kununua magodoro mawili mazuri,na baadhi ya nguo zake na za Fred.

Junior yeye alikuwa hana shida sana ya mambo ya kifedha japo Hans pia alimsaidia pale alipokwama. Kwa upande wa Suarez,alikuwa kama Hans tu!. Kazi yake aliyoiacha kwa muda,ilikuwa inamuingizia pesa kila mwisho wa mwezi,kwa hiyo akawa hana shida.

“Sasa tumerudi. Tupange jinsi ya kulipa kisasi”.Aliongea Hans na wote wakawa kimya kumsikiliza.

“Cha msingi tujifanye kama hatujapatwa na majanga. Ila kwao lazima ijulikane kuwa wamepatwa na majanga. Sawa jamani”.Hans alizidi kuendesha kikao kile.

“Hapo kwenyewe. Na ngoja sasa,watajuta kutufahamu”.Aliongea Junior.

“Hapo hata mimi nimo,lazima walipe”.Fred akakomelea neno.

“Kama kawa,si wanajidai maninja. Wataona”.Suarez naye alionesha uwepo wake katika kundi.

Wakaanza kupanga cha kufanya ili kulipa kisasi,na baada ya kama nusu saa,muafaka ukapatikana wa kulipa kisasi. Kila mtu akakubali kisasi icho.Baada ya hapo shughuli nyingine zikaendelea.

Zikapita siku kama tatu bila wakina Hans kufanya chochote.Lakini muda wote huo walikuwa wanafuatilia mienendo ya akina Ban na watu wake.

Waligundua mengi sana katika fatilia yao,lakini kubwa zaidi ilikuwa ni muda wao wa kutoka na kuingia vyumbani mwao.Hiyo walifanya kimyakimya sana hadi Ban na washirika wake wakagundua kuwa wanapangiwa kitu.

Alichofanya Ban na rafiki zake ni kuwa makini na chumba chao zaidi ya kitu chochote pale chuo. Hawakujua ni nini walichopangiwa na wakina Hans na ndIo maana walihaha.

Mara wiki ya kwanza ikakata bila usumbufu wowote. Wakina Ban walitabasamu na kuona wao ni washindi katika mapambano,lakini kumbe kitu kinachoitwa subira,ni bora kuliko kukukuruka.Na hicho ndicho kilifanyika kwa Junior,Hans,Fred na Suarez.Walikuwa wanasubiri wakati muafaka wa kufanya yao.

Hatimaye wiki ya pili ikaingia huku amani ikiwatawala vilivyo Ban,Sunday,Moi na Mose au Wagumu kama walivyozoeleka kuitwa pale chuoni.

Amani iliwatawala kwa kuwa kundi pinzani lilikuwa kama halina mpango na wao bali kuheshimiana kila walipokutana. Amani ikawa amani kwa wagumu wale.

Lakini kuna siku moja ambayo sidhani kama Ban na wenzake wanaweza kuisahau siku ile kwa kilichowakuta.

Ikiwa ni usiku mmoja wenye kila hali ya kuitwa usiku tulivu,Ban alipigiwa simu na msichana ambaye aliomba akutane naye usiku uluule ambao ulikuwa ni usiku wa kama saa nne kuelekea saa tano hivi. Jamaa kwa furaha na kihelehele cha kujifanya anajua sana huku ikichagizwa na misifa aliyokuwa nayo,akaona kama ana zali kwenda kukutana na Waziri Mkuu wa Chuo kile.

Waziri Mkuu wa Chuo kile alikuwa anafahamiana sana na Suarez kwa sababu walisoma wote shule ya Sekondari na pia walikuwa wanachukua masomo yanayofanana pale chuoni.

Dada huyo,Suarez ndiye alimpanga kwa sababu wale wakina Junior walikuwa hawana kabisa marafiki wa kike,hiyo ni itikadi waliyotoka nayo huko chini. Walikuwa hawajui kabisa kama kuna kitu kinaitwa wanawake,na zaidi walikuwa hawana hata mpango wa kuongea nao.

Huyu Suarez kila siku alikuwa anawashauri sana kuongea nao,japo na yeye alikuwa hana mpenzi kutokana na hapo mwanzo kuumizwa.

Hawa wakina Junior wenyewe walipanga mpango wa kuwakomoa wakina Ban huku wakihitaji wanawake wa kuwachanganya.Hivyo kwa ujuzi kabisa wa kukakaa wiki zile mbili,waliweza kupata wasichana watatu,huku wadada hao wakipatikana kwa msaada mkubwa wa Suarez.

Wale wadada wawili,walipangwa kuwazingua Moi na Sunday na huyu Waziri mkuu,yeye alipangwa kumzingua kubwa la maadui lenyewe,Ban Diho.

Uzuri sasa upo hapa. Japo wadada hawa walipangwa kwa wiki karibu moja na nusu,lakini waliwahi kukutana na Junior,Fred na Hans mara mbili tu!.Huku yule Waziri Mkuu akiwa hajawahi kabisa kukutana na hawa watu zaidi ya Suarez.

Wasichana wale waliunda urafiki na Wagumu kwa siku kama tano. Walikuwa wana uwezo wa kuwashawishi wagumu mpaka wakafanya wanachohitaji. Muda mwingi walikuwa wanawasema sana vibaya wakina Junior kitu kilichofanya wale wagumu kupenda sana kukaa na wale mabinti wawili.

HUYU dada mwingine ambaye alikuwa na jukumu kubwa kwa Ban,yeye alikuwa haonekani na wale wadada wengine bali yeye alikuwa kaanzisha urafiki wa karibu na Ban. Huyo ndiye yule Waziri Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hakuna aliyejua nia ya wakina Junior zaidi ya yule Waziri Mkuu ambaye alipewa mkanda mzima uliotokea.Hadithi yote alipewa na Suarez.Hivyo kwa kuwa yeye alikuwa kiongozi,aliona ni heri jambo lile liishe kiuanachuo ila na yeye akiwa shahidi kama kiongozi,na ndio maana alikubali kisasi kilipwe,na kisha wote atawaita na kuwaonya kwa kuwekeana mabifu yasiyo na mpango.

Wale wadada wengine,wao walipewa hela kiasi na wala hawakuhitaji kuuliza kwa nini wamepewa majukumu yale.

****

Baada ya Ban kupigiwa simu,alitoa tabasamu kubwa kwa kitendo cha dada yule Waziri Mkuu kumuita usiku ule.

Licha ya kuwa Waziri Mkuu,pia dada yule hata angeshiriki u-miss vyuo,angepata tu!. Alikuwa ni mzuri hasa,yaani kwa pale chuo,msichana yeyote alipenda kujifananisha na yule Waziri Mkuu asiye na majigambo wala mapozi kwa mwanachuo au hata mtu baki.

Saa nne za usiku,mrembo yule anampigia simu Ban ili wakaonane. Na yeye Ban bila kufikiria, aliwaaga kwa kuwadanganya rafiki zake kuwa anaenda kukutana na mzazi wake.

Chumba chao kikabaki na Sunday,Moi na Mose. Ambao wawili kati yao,nao pia walipigiwa simu na kila mmoja kwa wakati wake akaondoka kwenda kwa hao wasichana wanachuo ambao kwa muda mfupi walishakaa vichwani mwa Wagumu.

Chumba kikabakiwa na Mose peke yake. Huyu yeye hakupangiwa mwanamke ila kuachwa kwake, ilikuwa ni makusudi.

****

Baada ya Ban kwenda huko alipoitwa,akaanza kubabaishwa na Waziri yule Mkuu kwa lengo la kupoteza muda.

Kwa kuwa mwanaume ni dhaifu sana kwa mwanamke,yaani ni sawa na mfupa kwa fisi,basi Ban naye alilegea akawa bwege kabisa.

Hakujua hayo yote ilikuwa ni fitina za wakina Junior,ndio maana hata pale aliposhikwa mkono na kuvutiwa gizani zaidi,yeye alivutika kama bwege vile. Na hatimaye kazi ya yule dada ikawa inaelekea ukingoni.

Isikupite Hii: Geza Anasakwa Auwawe Ep 01

Sasa Ban alikuwa uso kwa uso na vijana watatu waliovalia kininja.Kwanza kabisa wale maninja walizuga kama ni vibaka na wanataka kuwapora.Mmoja wapo alimvuta dada mkuu pembeni na Ban alivoona hivyo,alianza kuomba msamaha ili dada yule asifanywe chochote.

Lakini kumbe ilikuwa ni ujanja tu!Mpango ulipangwa, ukapangika. Hatimaye kwa kuwa alijidai nunda basi dada wa watu aliachwa na mzigo wake akabebeshwa yeye.

****

Baada ya kama robo saa ya tukio lile kwa Ban,likatokea tukio kama lilelile kwa Sunday na Moi. Hali iliyofanyika kwa Ban,ndiyo iliyofanyika kwa Moi na Sunday. Nao walitekwa kama kawaida.

Baada ya kutekwa na maninja wale,walivuliwa nguo zote na kubaki kama walivyozaliwa. Wakati huo Ban alikuwa kaachwa mbali kidogo huku naye kavuliwa nguo na kufungwa kamba.

Sunday na Moi,walipovuliwa nguo,wakapelekwa hadi kwa Ban ambaye alikuwa anapigwa na baridi pale alipokuwepo.

Wakawarundika na kuwafunga kamba,kisha wao wakapotea eneo lile na kuelekea vilipo vyumba vya mateka wale.

Huko walikuta mlango umefungwa na kwa kuwa walishajua kuna mtu mmoja kabaki, basi ni lazima wangegonga na kufunguliwa kwa sababu yule wa ndani angejua kuwa wale ni wakina Ban.

Mawazo yalikuwa sawa kabisa. Wakiwa vilevile kininja,waligonga mlango kistaarabu na bila hata kuulizwa ni nani,mlango ukafunguliwa. Hapo wakaingia kama kawaida maninja watatu na kumsukumia Mose ndani kwa nguvu. Naye akayumba yumba hadi akadondokea kitandani.

“Ni nani nyie”.Mose aliuliza kwa sauti ya uoga yenye utetemeshi huku macho yake makubwa na mekundu yakimtoka kama jusi lililobanwa na lango la kanisa.

“Shiiiiiiiiii. Ukipiga kelele tu! Tunaondoa shingo yako na maini yako tunaenda kulia wali kantini huku mdudu wako tunaupeleka Super Market ya Mlimani City ukauzwe kama sonseji”.Ninja mmoja alimtisha Mose. Huyo alikuwa ni Junior,lakini Mose hakutambua ni nani.

“Poa,lakini nimefanyaje?”Mose aliendelea kuuliza kwa uoga.

“Ngoja utaelewa sasa hivi”.Alijibu ninja mwingine huku akimsogezea uso kwa karibu zaidi. Huyo alikuwa Suarez,wakati huo ninja Hans yeye alishaanza kupekua makabati ya mle ndani.

Kwa msaada mkubwa walioufanya wale maninja watatu,waliweza kuvuruga nguo zao zote za mle kabatini na kuziweka sehemu moja.

“Zetu zilichafuka kichizi. Sasa zenu hazichafuki,zitafanyiwa sayansi hadi zikome”.Ninja mwingine aliyekuwa hajaongea hata mara moja,sasa alifungua mdomo wake, na baada ya hapo akatoa chupa moja kubwa ya maji.

Chupa ile ilikuwa imejaa kimiminika chenye rangi ya njano.Na alipofanikiwa kutoa chupa ile mfukoni,alitoa kichupa kingine kidogo chenye unga mwekundu.

Akachovya kidogo ule unga kwa kutumia kitu kama eye droper. Eye Droper ni kile kichupa kinachotumika kuweka dawa ya macho au ya sikio,ambacho ukitaka kuweka dawa ile,unakiminya,nacho kinatoa tone la dawa.

Baada kuuvuta ule unga kwenye eye droper,akatoa eye droper nyingine yenye maji meupe na kutonesha kwenye ile chupa kubwa ya maji. Hapo maji ya njano yakawa ya blue.

Akachukua ule unga,nao akauweka kwenye maji yale ya blue. Ghafla ulifuka moshi mkubwa sana kutoka kwenye chupa ile.

Ninja yule mwanasayansi,akatabasamu tabasamu la ushindi. Na hapo hapo alichukucha kwa nguvu hadi maji yale yakawa meusi kabisa.

Kitendo bila kuchelewa akaanza kumwagia nguo zilizokuwa mbele yake na zile walizokuwa wamevaa wakina Ban.

Baada ya hapo,alimsukuma pembeni Mose na kuanza kumwaga maji yale kidogo kidogo kwenye magodoro ya mule ndani. Aliporidhika,akamgeukia Mose na kuongea naye.

“Sisi tulikaa kimyaaa,sasa zamu yenu. Sikiliza kwa makini huko nje kitakachokuja kutokea kwa wenzako”.Huyo ni Hans alikuwa anamwambia Mose ambaye tayari alikuwa ameelewa ni wakina nani.

Alikaa kimya huku akiangalia chini kwa hasira zilizojaa uoga.

“Hiyo dawa niliyomwaga hapo,subiri kwa dakika kumi,utaona matokeo yake”.Hans alimaliza,akawakusanya washirika wake na kupotea mle ndani.

****

Kule kwa wakina Ban,walikuwa wanajitahidi kufungua zile kamba hadi wakafanikiwa.

Kwa kuwa ilikuwa ni usiku sana,waliona ni afadhari hasa pale walipoona kulikuwa hamna watu waliokuwa wanakatiza katiza.

Walijifariji na kushika njia ya kurudi chumbani kwao huku wakiwa vilevile uchi,na pale mbele walikuwa wamepaficha kwa mikono tu!.Umbali wa kutoka pale walipo hadi chumbani kwao,ilikuwa ni kama dakika tano kwa miguu.

Walipofika walikuta kumetulia sana,kitu kilichowapa moyo kuwa hakuna watu muda ule.

Wakachungulia getini kuhakikisha kama ni kweli mawazo yao yalikuwa sawa. Baada ya kuona ni kweli,wakaingia getini wakiwa wanakimbia huku wameinama eti wasionekane.

Lakini wakati wanafanya hivyo,mara mbele yao wakatokea wanachuo wenzao kama mia hivi au mia mbili,tena wanawake wakiwa kwa asilimia kubwa sana.

“Sapraiziiiiii”.Zilisikika sauti za wanawake zikisema na kuwaacha wakina Ban wakiwa wameganda na kutopata cha kufanya kwa wakati ule.

Walibaki wamekodoa macho bila kujua wafanye nini pale walipokuwa wamesimama. Kukimbia hawawezi,kutembea hawawezi wala kunyata kwao ni shida.

Baadhi ya wanachuo walitoa hadi simu zao na kuanza kuwafyatua picha kuonesha kuwa wamefurahia sana ile hali.

****

Pale wale wadada walipomaliza kazi yao ya kuwapelekea Moi na Sunday kwa wakina Junior,moja kwa moja walirudi vyumbani mwao na kuanza kuwapa taarifa wenzao wa karibu na kuwaomba wajikusanye ili wawakaribishe watu hao kwa kuwafanyia sapraizi.Na kweli walifanikiwa sana kuwakusanya wanawake wenzao.

Kwa upande wa wanaume,ilikuwa ni kazi ya Fred kuwakusanya na kuwapa taarifa za ugeni wa usiku ule,na kila aliyepata habari zile,alimtaarifu mwenzake. Hivyo kundi sasa la kuwasubiri wageni wale waliokuwa uchi,likawa kubwa na lote lilijificha nyuma ya majengo yale wanayokaa wanachuo wengine.

Pale walipowaona wakina Ban wanakuja,ndipo waliamua kuibuka huku mstari wa mbele kabisa wakiwamo wale wasichana wawili. Yule Waziri Mkuu hakuthubutu kuonesha uso wake eneo lile wala kuwapa taarifa wasichana wengine kwa sababu yeye ni kiongozi na hawezi kufanya utoto kama ule. Na isitoshe Suarez na washirika wake,walipanga mpango huo wa kuwakusanya watu bila kumwambia waziri yule,kwani wangempa taarifa hiyo,basi wangepingwa vikali.

Sasa wakina Ban uso kwa uso na umati wa watu uliokuwa unaongezeka kila dakika ili kushuhudia wagumu walivyokuwa wanaaibika. Hakuna aliyewajali kwani hawa jamaa walikuwa hawapendwi hata na wakufunzi wa chuo kile kutokana na tabia zao za kibabe,hivyo ile ikawa kama komesha kwao.

Wakati wapo katika mshangao huo,mbele yao wakatokea wakina Junior na kuanza kucheka huku wakioneshea vidole kwenye miili ile iliyokuwa tupu.

“Daaah!Mwanangu una manywele kifuani,kama chipanzee. Ha haaaaa”.Junior alitoa kejeri huku wengine wakifuata kwa cheko.

“Mwanangu na wewe uwe unanyoa bwana,khaaa!.Yaani japo umeziba kwa mkono lakini hayo manywele yametokeza hadi juu ya vidole. Nyoaga bwana”.Hapo Hans naye aliongeza udambwi wake huku akioneshea sehemu za hatari za mmoja wa wale wahanga.

“Daaah!Mwanangu huyu jamaa ana dude,hadi mkono unakataa kuziba. Ha ha haaaa,si utoe tu kaka tuone”.Junior alizidi kupaka na kusababisha vicheko vitawale eneo lile.

Wote walikuwepo mahali pale,namaanisha Junior,Fred,Suarez na Hassan. Na hapo hapo wakina Ban walishawaelewa wabaya wao. Kwa ujasiri mkubwa,waliwapangua watu na kupita katikati yao na kuwaacha wakishangilia.

Hadi wanafika vyumbani mwao,walikuwa hawaamini kama ni wao ndio wamefanyiwa yale tena na watu wadogo kama wakina Junior. Waliumia sana mioyoni mwao,lakini ndio hivyo ilikuwa imetokea.

“Na haya manguo nani kayarundika hapa?”.Ban aliuliza baada ya kuona nguo zao zimerundikwa sehemu moja.

“Walikuja hao jamaa,maninja na kufanya hivyo”.Mose alijibu kiunyonge na kusababisha Ban atake hata kumpiga ngumi,lakini alizuiliwa na wakina Sunday.

“Sasa mwanangu kafanyaje hadi umpige badala ya kuzichukua na kujistiri?”.Moi alimuijia juu Ban.

“Huyu boya,kwa nini aliwaacha wafanye hivi?”.Ban alisahau yeye alichofanyiwa na kumwona Mose ni boya.

“Kwani waliokuvua nguo wewe ni wakina nani?.Mbona hatusemi kuwa wewe ni boya. Hao hao waliokuvua ndio walimvamia na huyu. Na hii yote tunakulaumu wewe. Wewe ndiye chanzo cha sisi kuaibika pale nje sababu ya babe wako na kuanzisha mabifu na watu bila sababu. Kumbuka wewe ndiye uliwachokozaga wale,ukatuingiza na sisi na sasa leo tunaaibika. Nakwambia leo ukimgusa mtu humu,tunakuchana chana na viwembe,boya wewe”.Sunday alimwijia juu Ban hadi kila mtu aliogopa mle ndani.

Ilishazoeleka kuwa Ban ndiyo kiongozi wao na ni mbabe kuliko wale wote,hivyo walipomuona Sunday anamkoromea boss wake,wote wakaanza kuogopa kwa kitakachokuja kumtokea Sunday.

“Unasemaje wewe mbwa,rudia tena kauli yako.Sijakusikia vizuri”.Ban alimuijia juu Sunday huku anamfuata na alipomkaribia,alimdaka shingo kwa vidole vyake na kuanza kumsukumia ukutani. Hapo Sunday naye hakukubali,akamvaa Ban kwa kumkumbatia na kisha akamgeuza na kumbwagia kwenye kitanda kimoja wapo kilichokuwa karibu yake.

Kinyume na matarajio yao,wakidhani labda kitanda kitawapokea kikakamavu,haikuwa hivyo. Kitanda kile kilitoboka ghafla na kubaki chaga tu. Ni godoro zima lilikuwa kama limeoza kwani lilipukutika na kuwa kama vumbi.

Wote walikumbwa na mshangao kwa kile walichokuwa wanakiona,na kitendo bila kuchelewa.Mose aliwapa habari kuwa magodoro yao yalimwagiwa maji ambayo yanasemekana ni ya kisayansi.

Hapo kila mmoja akawa anashika godoro lake,lakini kitendo cha kuweka mkono tu!Godoro likapukutika na kubaki chaga peke yake.

Wote wakabaki midomo wazi huku kulia wakishindwa,kuongea ni kazi na kucheka ndo kabisa mtihani.

“Hata hizi nguo wamezifanya hivyo hivyo”.Mose alikomelea komeo la mwisho kwa alichokitambua.

Hapo Ban akawa kama kachanganyikiwa kabisa,na vile alikuwa uchi basi unaweza kumkimbiza Mirembe au Muhimbili wodi ya waliowehuka.

Alienda kwenye lile rundo la nguo zao na kisha akajaribu kugusa. Kweli kitu kikaitika. Nguo zote zika wa majivu.

“Daah!Hawa wasen**@@ leo wametuweza haswaa. Sina cha kusema wala kuongea hadi hapa. Sijui tutalala kwenye chaga na kujifunika ngumi au vipi. Kuaibika tumeaibika,kisa ujinga tu!”.Ban alijikuta utu uzima ukimuingia ghafla na kujilaumu kwa wichokifanya kwa wakina Junior.

“Sasa tutafanyaje hapa?”.Ilibidi Moi aulize na wakati wote wapo sawa kasoro Mose aliyekuwa kavaa bukta na singland ya kulalia.

“Sijui tutafanye aisee”.Ban ajibu huku kama machozi yanataka kumtoka.

“Hatuna hata cha kuvaa. Huku hostel vyumba vyote tumegombana nao,ni vipi tutaanza kuomba msaada wa japo mataulo ili tujifunge hadi kesho”.Ban alizidi kutia huruma.

“Naona sasa umekubali nachokisema.Huu ni ujinga wetu na uchokozi usio na maana ndio umesababisha haya yote.Ilikuwa haina haja ya kwenda kuwachafulia chumba chao wala nguo zao”.Sunday aliongea kwa jazba hadi akawa anatema tema vimate vilivyomrukia sawa kabisa Moi usoni.

“Oya mvua bwana. We badala ya kufikiria cha kufanya sasa hivi,unaanza kulaumu tu!Hayo yamepita,sasa tugange yanayokuja”.Moi aliongea huku akijifuta tule tumvua usoni.

“Muache aendelee tu!.Anajidai ndio anaona sasa hivi. Kwa nini angesipokataa siku ileile?Eti sasa hivi anajidai ndio anaona”.Ban aliongea huku bado akiwa na mawazo ya juu kilichotokea.

Wakati wapo katika mawazo hayo,ghafla mlango wao ukafunguliwa na Junior pamoja na Hans waliingia na kuwarushia baadhi ya nguo.

“Vaeni hizo. Sisi tumewafanya na kuwalinda,lakini nyie mlituacha mayatima”.Aliongea Hans na kuondoka mle ndani kwao,yeye na Junior.

Waliwapa nguo zilezile ambazo walizichafuaga wao wenyewe wakina Ban.

“Daah! Kweli nimeamini,kile unachokidharau, ndicho kitakachokuja kukustiri baadae.Tulidharau nguo hizi siku ile na kuzikinda kinda,lakini leo ndo zimekuwa za kujistiri miili yetu”.Aliongea Ban kwa hisia kali huku akimalizia kuvaa shati moja ambalo lilikuwa na baka moja kubwa mgongoni la tope waliloliweka siku za nyuma.

“Yaap.Inauma sana.Zile nguo tulipozifanya vile nadhani hata MUNGU kaona upumbavu wetu. Watu wanalia kuwa hawana nguo,lakini sisi tunaenda na kuzichakaza nguo hizo hizo bila huruma.Hii ni laana na MUNGU kalipa.Wala siwalaumu hawa jamaa,wana haki.Bila kufanya hivi,yawezekana MUNGU angelipa kivingine tu!”.Sunday naye aliongea kuungana na mwenzake.

“Ooups.MUNGU atusamehe tu!Huu ubabe usio na maana,leo umetutokea puani.Ni saa saba sasa,nani awezaye kutusikiliza na wakati hakuna hata mmoja anayetupenda hapa hostel?”.Ban alizidi kuonesha masikitiko yake.

“Daah!Sasa kama tunafikiria kulipa na kisasi,ni hapahapa tuambiane mimi nijitoe maana siwezi kufanyiwa hivi tena. Hizi ni Sayansi,ipo siku tutamwagiwa yale maji na sisi kuwa kama haya magodoro”.Mose naye alitoa mchango wake.

“Hapana. Sasa hivi ni muda wa kujirudi na kuelewana na kila mtu hapa chuo. Kaa ukiamini kuwa hawa jamaa wamejipanga sana,na wapo radhi kutumia fedha ili walipe tutachowafanyia. Sisi na vijisent vyetu vya ualimu,unadhani tunaweza kukodi wanawake na kuwavuta hawa

jamaa?.Kwanza sijawahi kuwaona na wanawake.Tuache haya mabifu yasiyo na msingi wowote.Ni muda kufuta haya yaliyotokea usiku huu".Ban aliongea kwa mara ya kwanza kauli ya kukubali kushindwa na iliungwa na mokono na washirika wake wote.

Na hapo tena mlango ulifunguliwa na kundi lote la Hans liliingia huku likipiga makofi.

"Tunashukuru sana kwa kuwa sasa mmejielewa,na imewauma pia kama ilivotuuma sisi.Ila samahani sana kwa tulichokifanya. Na nimesikia mkimtaja MUNGU kuwa kawalipa.Nasi imetuuma sana kwani tumezifanyia nguo zenu kitu mbaya na wakati kuna wengine tangu wamezaliwa hawajawahi kuvaa nguo mpya,lakini sisi tumezifanyia maafa nguo ambazo tungezipeleka kwenye kituo cha watoto yatima,wangeshukuru sana.Lakini si kitu,nadhani yote haya ni kumwachia MUNGU afanye yake. Ila namuomba sana msamaha kwa tulichokifanya".Hans ndiye aliyeongea huku wakina Ban wakiwa vichwa chini wakisikiliza ujumbe ule.

"Sasa tumemjua MUNGU,nimependa sana haya maongezi. Tusali sana jamani,haya yote ni malipo ya dhambi zetu,iliniuma sana kwa mlichotufanyia,na ndio maana nilikuwa mstari wa mbele kulipa kisasi. Lakini sasa hivi najuta kwa kushindwa kukontroo hasira zangu na kulipa kisasi wakati MUNGU hapendi hiyo hali".Aliongea Fred na kuungwa mkono na wengi mle ndani.

"SASA tumemjua MUNGU,nimependa sana haya maongezi. Tusali sana jamani,haya yote ni malipo ya dhambi zetu,iliniuma sana kwa mlichotufanyia,na ndio maana nilikuwa mstari wa mbele kulipa kisasi. Lakini sasa hivi najuta kwa kushindwa kukontroo hasira zangu na kulipa kisasi wakati MUNGU hapendi hiyo hali".Aliongea Fred na kuungwa mkono na wengi mle ndani.

Kila mmoja aliongea yake na uzuri yale maneno ya waliyokuwa wanaongea wakina Ban yalikuwa yanasikilizwa kwa uzuri kabisa na wakina Hans.

Baada ya maongezi hayo,walikubaliana kumaliza tofauti zao,na bila kinyongo waliwachukua wakina Ban na kwenda kulala nao chumbani kwao.

HUO NDIO UKAWA MWISHO WA VURUGU ZILE,HUKU THE LOST BOYS WAKIWA WAKINA BAN KWA SASA.

*****

SEASONI II

Kesho yake asubuhi taarifa zikazagaa sana kwa kilichotokea na wale waliopiga picha wakaamua kuzisambaza pale chuoni kama njugu. Kila mtu akawa na picha zile kwenye simu yake.

Hakuna aliyejua ni nani anahusika na matendo yale zaidi ya wale wasichana wawili pamoja na wagumu na kundi la akina Hans.

Yule Waziri Mkuu alizipata zile picha na alisikitika sana lakini alikuwa hana cha kufanya zaidi ya kumuita Suarez na kumuuliza kwa nini waliamua kufanya vile. Suarez alieleza kila kitu na kuwa wamekubaliana na wagumu kumaliza lile bifu.

Dada yule Waziri aliposikia wamemalizana,alifurahi sana kwani alijua kwa picha zile,lile bifu ndo ligechachamaa.Lakini baada ya kusikia bifu limeisha,alifurahi sana.

"Nimefurahi sana kusikia maneno hayo Emma. Ila kuweni makini wasije kuwageuka tena".Alionya dada aziri.

"Aaah hamna hiyo kitu".Suarez Emmanuel alimtoa shaka dada yule.

"Okey,nashukuru kusikia hivyo.Sasa nataka kuona washirika wako na kuwahasa kuhusu hili jambo na pia kuwasalimia kwa sababu sijawahi onana nao.Jana niliwaona lakini sikuwaona vizuri sababu ilikuwa giza sana".Aliongea dada yule mrembo,ombi ambalo lilipita na Suarez alimpeleka moja kwa moja kwa rafiki zake.

“Oya,yule dada aliyemzingua Ban anataka kuonana na nyie”.Suarez aliwaambia wakina Hans waliokuwa chumbani kwao wakifanya kila mtu kazi yake.

“Aaag,huyo tushamalizana naye.Hatuitaji mwanamke huku sisi”.Aliongea Hans na kuungwa mkono na Junior.

“Oya yupo hapo nje.Ngoja nimuite ili mumwambie wenyewe”.Suarez aliwaambia hivyo na kutoka na aliporudi,alikuwa na yule dada.

Wakina Hans walipomuona yule dada,wote walishikwa na butwaa,si Junior,Hans mwenyewe na Baba Paroko Fred.

“Habari zenu jamani”.Dada yule aliwasalimia lakini hakuna aliyejibu,wote walikuwa wamegandisha macho yao wakiwa hawaamini wanachokiona.

“Oya mnasalimiwa”.Ilibidi Suarez awatoe kwenye ule mkanganyiko.

“Eeeeh,unasemaje Sure”.Hans aliuliza kama anatoka usingizini.

“Dada anawasalimia huyu”.Suarez alijibu huku anataka kucheka.

“Aaah.Poa dada mambo”.Wote walijikuta wanashuka vitandani mwao na kumpa mkono dada yule kwa pamoja.

“Safi”.Dada yule alijibu huku anawashika mikono yao mmoja mmoja.

Bado kila mmoja alikuwa haamini anachokiona kwa wakati ule.Hata pale walipoachiwa mokono yao,walibaki wamegandisha bila kuishusha.

“Okey.Naona kama mna kitu.Mimi naitwa Eve Johaness,sijui wenzangu mnaitwa wakina nani”.Ilibidi yule dada ajitambulishe jina lake,lakini bado wakina Hans walikuwa wameganda tu!

“Oya mazee dada yetu anawasalimu,hamsikii au ndio mwajidai wagumu hapa”.Ilibididi Suarez afanye kazi ya ziada kuwaamsha wale majamaa walioganda kama mazombi.

Alikuwa anawaamsha huku anawapiga visogoni.

“Hamna mzee nani.Dah! Akili sijui ilienda wapi.Unasemaje dada!!??”.Hans alikuwa kama jinga fulani lilitoka kujanjarushwa na wajanja,kwa jinsi alivyoshtuka na kuuliza lile swali.

“Ee kweli.Dada umesemaje”.Naye Junior alikurupuka toka kwenye ule mshangao,wakati huo Fred alikuwa naye anajiweka sawa ili kusikia Eve atasema nini.

“Nimesema naitwa Eve Johaness.Wenzangu sijui mnaitwa wakina nani”.Eve alijitambulisha tena kwa vijana wale na kubaki akiwaangalia usoni akisubiri jibu la maombi yake.

“Okey Eve.Nataka kukuita Eve The Beautiful One,upo tayari?”.Junior alianza hivyo huku akinyoosha tena mkono wake kumpa Eve kama salaam.

“Whetever you like”.Eve naye alijibu kizungu zaidi.

“My name is Junior.Au ukipenda niite Nickson King Junior.Mi nipo Arts hapa chuoni.Masomo yangu ni muziki zaidi na lugha”.Alimaliza Junior na kumpa heshima Eve ya kuinamisha kidogo kichwa chini kama wale watumishi wa malkia wakimuona malkia anapita.

“Okey.Napenda kukuita Junior.Mimi nipo nasomea uandishi wa habari na huyu rafiki yenu”.Eve aliendelea kujitambulisha na wakati huo Hans alishasogea mbele kwa ajili ya kutoa utambulisho wake.

“Mimi napenda kukuita Sweet Eve.Your so sweet Eve.Just like an candy or honey.Nimekuwa kama mtambo baada ya kukuona”.Hans ni kama alishaanza kutupa kete zake kitu ambacho sidhani kama wenzake walikifurahia hasa Junior na Fred.

“Babu si ujitambulishe tu! Maneno mengi kama umejiunga na baba lao”.Junior alishindwa kuvumilia kwa jinsi Hans alivyokuwa anaendelea kuongea.

Uzuri wa Hans japo alikuwa hana mpango na mapenzi,lakini alikuwa anazijua kete za kuwazidi wenzake.Hadi pale walipofikia,Junior alishapoteza kete kwa kuropoka bila mpango.Na Hans alishalijua hilo,hivyo akazidisha mbwembwe za kujiongezea pointi.

“Wajua nini Eve.Napenda kujitambulisha kwako kama kijana mtulivu kabisa ila ukinichokoza ndio nakuwa kama kichaa.Sishangai huyu jamaa anavyonipigia kelele mbele ya Sweet Baby kama wewe.

But anyway.Naitwa Hassan Jenge,au Hans J.Nipo hapa UDSM katika masomo ya Sayansi.Ukisikia Hans The Scientist,ndio mimi.Karibu sana katika Ikulu yetu Sweet Eve”.Hans alijitambulisha huku akimpisha na kumwoneshea kitanda chake akakae pale”.Eve alitabasamu jambo lililofanya Hans ajione mshindi.

“Sikai sana Hans.Nitakuja siku nyingine.Usijali”.Eve alijibu huku bado kachanua tabasamu lilelile la mwanzo.

“I respect that Sweet Eve.Ila sijajua kama umelipenda jina la Sweet Eve”.Hans aliongea tena wakati huo naye Fred alishasogea mbele kwa ajili ya kujitambulisha.

“Jina lolote kwangu sawa tu!Wala usijali.Hata ukiniita tusi,hamna tatizo”.Eve alijibu huku bado katoa tabasamu lake ambalo linaweza kuhamisha ghorofa kutoka Posta na kulipeleka Banana au Kivule.

“Okey Sweet Eve”.Hans alikubali na kurudi nyuma kumwachia Fred ajitambulishe.

Kinyume na walivyotarajia labda Fred atabugiza au ataanza kuleta za Kiparoko,Fred akawa nyoka mwenye sumu kali hatari.Sumu iliyowaua wao wote.

“Habari yako mrembo.Napenda sana kutumia Kiswahili kuliko Kiingereza na ndo maana nakupa jina la Malaika badala ya Angel.

Wewe ni Malaika Eve,kwani nilipokuona nilijua kuwa umenileta taarifa nzuri kwangu kama yule Malaika alivyomtokea Bikira la Maria na kumwambia atazaa mtoto, naye atamuita Yesu.

Nawe umenitokea kama vile,na kuuacha moyo wangu ujawe na furaha kwa taarifa nzuri ya uzuri wako uliyoniletea mimi hapa leo. Wewe ni Malaika,niamini nachokwambia Eve.Wewe ni Malaika”.Fred alikuwa anaongea hayo na baada ya kumaliza alishika mkono wa Eve na kuubusu kwa huku nyuma.

“Mmmh!.Mi sina usemi hapa Suarez”.Eve alishindwa kuvumilia na kujikuta akitabasamu na kumwangalia Suarez ambaye muda wote alijiona mshindi sana kwa kuwafanya hawa watu ambao kwao wasichana walikuwa sumu.Alifurahi kuwaona wakianza kuamini kuwa msichana ni sumu isiyoua bali sumu inayonenepesha na kutoa furaha.

Ujue bado siamini".Suarez naye aliongea baada ya kushuhudia busu la kwanza kutoka kwa Fred.

"Achana na hawa Malaika wangu. Mimi naitwa Alfred Musita,au Fred……".Wakati anaendelea kujiambulisha yanayoendelea,Junior alidakia bila kujua anazidi kupoteza pointi.

"Fred au Baba Paroko,au ukishindwa kabisa muite Mzee wa Upako".Watu walikaa kimya wakimshangaa Junior kwa yale maneno.Eve naye hata tabasamu lilimuisha na kubaki katika alama za mshangao.

Fred alikuwa ni mtalaam,nahisi alimzidi sana Hans.Kwani kitendo kile cha Junior kuropoka,kilikuwa kama kumtupia kobe kwenye maji ili umuue au kumwagia petrol moto ili uzime.

"Yap.Malaika wangu.Nampenda sana Junior kwa kuwa anamalizia maneno niliyoyaanza,hivyo usishangae wala kupoteza tabasamu lako mwanana mithili ya Miss anayegombania U-miss mbinguni".Fred alimsafisha Junior wakati huo akichukua pointi nyingine kwa kurudisha tabasamu la Eve kwa maneno yake matamu.

"Kama alivyosema mkubwa wangu Junior.Humu wamezoea kuniita Mzee wa Upako kwa sababu ya kupenda kusoma Biblia.Lakini mimi nipo Biashara,nasomea Uhasibu katika chuo hichi".Fred aliendelea kujitambulisha kwa kujiamini mbele ya mrembo yule wa chuo.

"Nimefurahi kukujua Fred.Napenda kukuita Fred.Na nimependa sana uchangamfu wako".Aliongea Eve kumwelekezea maneno hayo Fred.

"Karibu sana Malaika wangu.Naomba kitu kimoja kama hutojali".Fred alizidi kuonesha mbwembwe zake za kitakatifu lakini zenye bashasha za kutosha.

"SEMA tu! Fred".Eve alimpa ruhusa Fred.

"Naweza kubusu shavu lako?".Fred alifunguka huku kamkazia macho yaliyo makavu na yasiyo na utani Eve.

"A a a a.Hiyo hamna aisee.Mimi huyu kama mgeni wangu nakataa hiyo kitu".Suarez aliingilia kati jambo lile huku akiwa hana mbavu kwa kinachotokea mbele ake.

Hans na Junior walitoka macho huku wakiwa hawaamini kinachotaka kujiri mbele ya mtu ambaye wao walimchukulia kama bonge la mtakatifu.

"Mhh!Sure umeombwa wewe au mimi?Embu mwache bwana apate anachohitaji".Eve alimpiga stop Suarez ambaye alikuwa anamsukuma Fred kwa pembeni huku akiendelea kucheka.

"Dah! Haya bwana,kwa kuwa umetoa ruhusa.Sina jinsi".Suarez ilibidi akubaliane na maneno ya Eve na kumwachia Fred ambaye alimfata Eve pale alipokuwa kasimama na kumshika kiuno,wakati huo Eve aligeuza shavu la kulia na Fred alidondosha midomo yake juu ya shavu lile linalong'aa mithili ya almasi.

"Nimefurahi kupata kiss lako Fred.Your so sweet".Eve alimwambia Fred baada ya busu lile.

"Hapana Malaika wangu.Sweet ni jina lako kwa Hans.Na mimi nimefuahi sana kupata shavu lako.Umeumbwa ukaumbika, Eve".Fred alimaliza na kurudi nyuma kwa ajili ya kusikiliza kitu kinachofuata.

"Haya jamani.Naona wa mwisho siku zote ndio kapata kinachostahili.Siku zote jiwekeni nyuma bwana,si mmeona mwenzenu".Suarez alianzisha mazungumzo baada ya kimya kidogo,wengi wao wakifikiria kilichojiri muda mfupi uliopita hasa kitendo cha Fred kuvua ngozi ya utakatifu na kujivika ngozi ya ukidunia.

Eve alikuwa mtu watabasamu muda wote kana kwamba hana tatizo kwa chochote kilichotokea muda ule.

Siku zote ili utengeneze urafiki na watu wengi ni lazima uwape wanachohitaji lakini usivuke mipaka.Busu kavu ni kitu cha kawaida sana hasa ukiwa umeelimika na kutoa ule udigitali kwa kuweka uanalojia.Namaanisha yapasa kuingia dunia wanayoishi wenzetu walioendelea lakini usisahau mila na desturi za unapotokea.

“Mimi sina neno.Nadhani wote tumeona.Sasa tumpe muda dada yetu aseme kilichomleta”.Suarez aliongea huku akimpisha Eve aweke maneno machache yaliyomleta pale.

Alichosisitiza Eve ni kumaliza bifu lililokuwa kati yao na wakina Ban ambao kwa muda huo walirudi majumbani kwao kwa sababu ya aibu iliyowakumba na kwenda kujipanga tena hasa kimavazi.

Baada ya maneno hayo,wote walikubaliana na ushauri huo na wote kwa pamoja walitoka na kumsindikiza kimwana yule ambaye kwa mara ya kwanza aliwafanya wahisi dunia ilikuwa imewapita sana katika wanawake.

****

Baada ya kumsindikiza msichana yule,wao walirudi na kuendelea na kazi zao chumbani kwao lakini maongezi makubwa yalikuwa ujio wa Eve katika maisha yao.Kila mmoja aliapa kivyake baada ya kugunduana kuwa wote wanamtaka msichana yule.

“Mimi nitamwimbia na kumpigia gitaa hadi anilalie kifuani.Huku akitamani nisiache kufanya hivyo”.Junior alijigamba mbele ya wenzake.

“Tatizo lako Junior wewe ni ropo-ropo sana.Unatakiwa kucheza na pointi kaka.Kulikuwa hakuna haja ya kuropoka saa zile,mara Mzee wa Upako,sijui unamkataza Hans asiendelee. Hizo achana nazo kijana.Fanya yako halafu uone”.Suarez alitoa ushauri wake juu ya alichokiona kwa Junior.

“Huyo tushamtoa kwenye ligi.Mimi nitampa sayansi za mapenzi hadi kila akikaa anataka kupewa sayansi hizo”.Hans naye alichombeza mikakati yake.

“Wewe Hans tatizo lako ni kujisifia kaka.Hans J mara Hans the Scientist,ooh sijui mimi ni kijana mtulivu.Hivi unadhani hakujui tabia yako?.Ulitakiwa kujitambulisha matendo yako kama yalivyo na si kuzuga zuga”.Suarez aliendelea kutoa mapungufu ya kila mmoja.

“Mimi nitampa vipande vya Biblia na kuvigeuza kuwa mistari ya mapenzi juu ya mtoto yule aliyeacha poda kwenye lips zangu.Duuuh! Wananionea tamaa”.Fred hakuwa nyuma kujisifia mbele ya wenzake.

“Wewe ulianza vizuri sana.Lakini ulipoharibu ni pale ulipotaka kiss.Kwanza manzi fikra zake zitajengeka kuwa ulitaka kuwaonesha wenzako kuwa wewe ni bora, na zaidi atakuona kama limbukeni kwa ulichokifanya.Hivyo usidhani kama umewashinda wenzako.Bado mna kazi sana ya kurekebisha hayo mambo.

Na uzuri manzi mwenyewe tangu nianze juana naye,sijawahi kumsikia ana skendo au hata boy.Kwa hiyo wazee,kazi ni kwenu”.Suarez alimaliza na kwa kuwa alikuwa anauzoefu kiasi chake,wote walitulia na kuyachanganua yale maneno yenye ushauri.

EVE JOHANESS.

Kama alivyojitambulisha kwa akina Junior.Yeye alikuwa anasomea uandishi wa habari katika chuo kile kikuu cha Dar es Salaam.Alikuwa sanjari na Suarez katika kusoma huko.

Inavyosemekana alimaliza Mbeya Day kidato cha nne na kidato cha sita alisoma na Emmanuel Suarez shule ambayo haijafahamika hadi leo.

Matokeo yake yalikuja mazuri sana na kumfanya aje pale UDSM kwa ajili ya kusomea uandishi wa habari.

Katika mapenzi alikuwa haijulikani kama alikuwa anaye au hana.Ila watu wake wa karibu wanasema kwa pale chuoni hana,na kuongeza kuwa hawajui kuhusu huko nje kwa sababu hakuwahi kuongelea masuala hayo na wenzake.

Alikuwa ni mzuri wa sura, na umbo lake jembamba kiasi lililobebwa na kiuno kilichozama ndani na kuibuka na kitambi kidogo kwa nyuma.Kitambi ambacho wahuni wanaweza kukiita ushuzi ila sisi wastaarabu tunayaita makalio.

Alikuwa ana makalio ambayo yalikuwa hayafanyi watu kusema ni ya kichina bali kusema kabarikiwa kuwa na makalio yanayowatoa wanaume wakware mimate ya uchu.

Upande wa sura,ni kweli alifaa kuitwa majina yote kasoro tusi tu!Na majina mengine mabaya-mabaya.Ila yale majina ya Malaika,Sweet na Beautiful yalifaa kabisa kuitwa binti yule mwenye kila sifa ya kuyapokea majina kwa mikono miwili.

Alikuwa si mweupe sana wala mweusi kiviile.Bali alikuwa ana-rangi ya asili ambayo kwa sisi wataalamu wa watoto hawa wa kike tungeita rangi ile ni ya chotara.

Na ndivyo ilivyo.Eve Johaness alikuwa ana asili ya baba Mtanzania tena wa Mbeya na mama alikuwa ni raia wa Uswis. Sasa Eve alichukua rangi mbili za wazazi wake,yaani ya kizungu na ile ya Kinyakyusa.

Uso wake ule ulibeba macho fulani madogo lakini si kama ya watu wa Asia,yaani Wachina au Wajapani.Yeye alikuwa ana-macho madogo lakini yenye mwangaza kutokana na kuwa ya uviringo na huku shavuni kukichagizwa na mashavu mazuri ambayo kwa mwanaume anayejua maana ya uzuri anaweza kusema yale mashavu yametengenezwa kwa unga wa ngano na si udongo.

Hiyo ni kutokana na ulaini wa mashavu yale na utamu ule wa mashavu uliongezewa bashasha za kutosha na dimpoz ambazo zilikuwa pande zote mbili,yaani shavu la kushoto na kulia.

Nikiwa bado hapo hapo kichwani,naenda hadi kwenye nywele zake ambazo kama ulizoea kumuona Rihanna mara kwa mara,basi akitokea Eve machoni kwako,hutosita kumuita Rihanna sababu ya nywele zake ambazo yeye alikuwa akizibadilisha rangi kila wiki.

Tuache haya ya kichwani.Nakupeleka kifuani.

Haya yote nakuelezea ili upate picha halisi na kujijibu mwenyewe kwa nini hawa jamaa watatu ambao wasichana kwao ni sumu,wagande na kudata huku kila mmoja akiapa kwa wakati wake kuwa watafanya kila njia ili wampate.

Alikuwa na kifua saa sita.Kama hujui kifua saa sita ni nini.Basi kaa ukijua kuanzia leo kuwa alikuwa anachuchu kiduchu ambazo zinawaacha watu wenye hela zao wakibakiwa na uchu wa kutaka hata kuziona zikiwa wazi.

Zilikuwa hazina kero wala kupigwa jeki kama zile za Nicki Minaj.Hizi hata zisipovishwa sidiria zilionekana wazi zimesimama dede.Lakini alipenda kuzipa sidiria ili asiwaumize maboya boya wa chuo kile.

Nashindwa kumwelezea uzuri wa miguu yake.Ila naweza kusema ni miguu ambayo ilifamfanya aonekane mrefu kiasi na asiyekuwa na tatizo au kusababisha watu wamcheke mtu aliyesimama naye kwa kuonekana mfupi kuliko yeye. Eve alikuwa hana maurefu hayo ya Hashim Thabit wala maurefu ya Twiga.Na zaidi hakuwa mfupi kama kifaru wala ufupi wa kuigizia vichekesho.

Mimi namjua Eve,kwani hata akitembea alikuwa si wa kujiaibisha kwa kutembea kama kundi la nyumbu au pundamilia linapita.Alikuwa hana vishindo vya wanyama hao wala kutimua mavumbi hata kama anatembea kwenye vumbi hilo.

Nje ya hayo maumbile yake.Eve alikuwa anaweza kujipanga kimavazi aisee.Hakuwa wa kuvaa makachumbali,yaani hakuwa wakuvaa nguo zenye rangi nyingi.

Si mwajua kachumbali navyokuwa na rangi nyingi? Utakuta kitunguu kina rangi yake,nyanya rangi yake,pilipili rangi yake,karoti kama zipo zitakuwa na rangi zake,pilipili hoho ukiamua kuweka inakuwa na ukijani wa kukolea kuliko pilipili ile ya kuwasha.Wengine wanaweka kageji kwenye kachumbali hiyo ambayo nayo ina-rangi yake.

Sasa kuna watu wanavaa kachumbali bwana.Lakini kwa Eve,ilikuwa tofauti sana.Kama akiamua kuvaa rangi tofauti,basi alizipangilia.Kama nyeusi alijua inaendana na rangi za kung'aa kama njano,pinki na nyeupe ambayo hiyo nyeupe inaendana na rangi yoyote.

3

Hakuwa mtu wa kuvaa rangi ya kijani kwa nyeusi kama baadhi ya wanawake wengine wa pale chuo.Ukivaa hivyo utakuwa kama jalala,yaani utaonekana mchafu.Rangi zilizofifia zinaenda na rangi za kung'aa bwana.Na ndivyo Eve alivyokuwa akijipanga katika mavazi yake.Acheni wakina Junior wadate aisee.Mtoto alikuwa anaweza haswaa.

Uzuri huo wa Eve ndio ulimfanya hata Ban adate na kuingia mwenyewe laini.Na uzuri huohuo ndio unawaingiza mtegoni wale jamaa walikuwa wanajiita Ant-Girls.Ni hatari na balaa juu yake hasa pale ilipogundulika wale wote walikuwa wanamtaka msichana mmoja,ambaye ndiye waziri mkuu wa chuo kile kwa wakati ule

HUYO NDIYE EVE JOHANESS.

****

Ilipita wiki tangu wakina Hans wakutane na Eve.Kila mmoja alikuwa anakutana na Eve kwa muda wake na kuna muda walikuwa wanakutana naye kwa pamoja na kuongea naye mambo mbalimbali yanayotokea pale chuoni na duniani.

Eve alitokea kuwaelewa sana wale jamaa kutokana na ucheshi na mambo yao.Kila mmoja alikuwa akitumia kipaji chake kufikisha hisia zake kwa mwanadada yule mlimbwende.

Aliyejua kutunga tenzi,alifanya hivyo na aliyejua kuitumia biblia kwa kugeuza mistari ya kitabu kile na kuwa mistari ya kufikisha hisia zake,naye alifanya hivyo.

Huku mwanasayansi naye akichanganya maneno na falsafa za wanasayansi na kuwa mistari ya mapenzi inayovuta hisia za kila mwanamke atakayesikia yale maneno.

Hiyo ndiyo sababu kubwa ya Eve kupenda kukaa na wale jamaa kwani kila muda alikuwa anapata maneno matamu kupitiliza.

Licha ya hayo yote kutokea,hakuna aliyewahi kumtamkia moja kwa moja kuwa wanampenda mwanamke yule.Wote walikuwa wazee wa mistari tu!.Lakini hakuna aliyewahi sema au kumwambia Eve kuwa anahitaji kuwa mpenzi wake.

Hilo ndilo lilikuwa tatizo la hawa jamaa japo wenyewe wakikutana peke yao,wanaambizana kuwa wameshampiga saundi mtoto yule na wanasubiri majibu tu!.

Mambo yalizidi kunoga pale wale wagumu waliporudi chuoni.Walikuwa wamebadilika sana kitabia,na kila mtu aliwapenda kwa nidhamu waliyoionesha baada ya kurudi.Sasa wakawa mstari wa mbele kushirikiana na wenzao huku rafiki zao wakubwa wakiwa ni walewale wakina Hans.

Hali ile ya wakina Junior kutambiana kila wanapokutana,ikazua kiriba cha roho.Kwa nini huyu hivi na mimi hivi?.

Kiriba hicho cha roho kikaanza kutengeneza wivu taratibu na matokeo ya wivu huwa ni chuki baina ya watu.Na ndicho kilichofuata baada ya wivu ule.

Kila mmoja akatafuta njia maalumu ya kumpindua mwenzake.Huyo Mtakatifu Fred naye aliamua kwenda na wale wahuni nyama kwa nyama.Kama wao waliamua kumfanyia uhuni,basi na yeye aliamua kuwa kama wao.Si mwajua kuwa ukitaka kumuua Shetani ni lazima na wewe ujivike ushetani.Basi ndivyo ilivyotokea kwa Fred.

Msaada mkubwa walioona utawasaidia ulikuwa ni kwenda kwa wagumu na kusema matatizo yao huku wakitoa kiasi cha fedha kwa ajili ya kazi hiyo kufanyika.

Hakuna aliyejua kuwa mwenzake anawatumia wagumu kumwaribia na nafasi kama hiyo ndiyo wagumu waliona kama nafasi ya kulipa kisasi chao japo kisasi hicho walikuwa hawataki kilete majanga kama kile cha mara ya kwanza.Hichi kilikuwa kisasi cha akili ambacho kilikuwa kina lengo la kuwakusanyia hela zao tu.

Naam,wagumu walipewa shavu la kufa mtu kwa ajili ya kuharibu mikakati ya mmoja wa kundi la akina Hans. Ban na wenzake walikuwa ni watu wa kuagiza tu! Tuletee ichi ili kazi ikamilike haraka,au fanya hivi na toa ichi halafu usubiri matokeo.Hiyo ndiyo ikawa kazi ya wagumu.

Kwa upande wa Suarez yeye aliamua kukaa pembeni na kuwashangaa jamaa zake kwa nini wamechanganyikiwa kiasi kile kwa muda mfupi tu!.Alikaa pembeni kwani hata alipowashauri walikuwa wagumu kuelewa na wagumu kufikiri kwa mtendo yao

Wote kwa muda tofauti ,walimpa Suarez mikakati yao. Pale alipojaribu kuwarekebisha,walimwijia juu na kumuona kama anawazingua tu!Hivyo wakaacha kabisa kumpa taarifa jamaa huyu na taarifa zikawa zinapelekwa kwa wagumu.

Suarez akawa mtu wa kutabasamu na kuwaona hawa jamaa kama marimbukeni tu!.Ipo siku watadamka na watajijua kuwa walikuwa wanabugi sana.Hivyo aliwaacha na kubaki muangalia filamu ile ya bure kabisa,yenye wingi wa vituko na vichekesho visivyokwama.

Eve yeye alikuwa hana taarifa zozote kutokana na ule mkanganyiko baina ya wale rafiki zake wapya.Yeye alichojua ni kwamba ana marafiki wenye maneno matamu yanayoweza kusababisha chakula kikajila.Hakujua kama wenzake tayari wanacheza ligi kuu na kombe likiwa ni yeye.

Na kizuri zaidi kundi lile lilikuwa pamoja kama zamani.Yaani ni kama walikuwa hawajawekeana bifu,wote walionekana wana furaha sana pale wanapokutana. Hakuna aliyejua roho ya mwenzake zaidi roho yake na MUNGU pekee.

Hawa watu watatu,namaanisha Hans,Junior na Fred.Walijipanga sana kimaneno kwa ajili ya Eve.Na mengi waliyaongea yalikuwa ni maneno matamu ambayo kiukweli hata wasichana wengine wangeyasikia au wao ndio wangekuwa wanaambiwa,sidhani kama wangekataa kuwa japo na mmoja wa wavulana hao watatu.

Ngoja nikupe maongezi ya kila mmoja wao akikutana na Eve.

JUNIOR NA EVE.

Mara nyingi Junii au alipenda sana kumpeleka Eve chuo cha kule mlimani.Na walipenda sana kukalia mawe yale ya mlimani.

Huku wakipata upepo na vinywaji mbalimbali walivyotoa supa-maketi ya Mlimani City.Junior alikuwa anam-mbeleza kwa gitaa Eve huku akitoa maneno yake ya kisanii kumwelekea mrembo yule ambaye siku zote alimuona Junii kama mtu mchangamfu na mwenye wingi wa maneno.

“Wajua nini My Beautiful”.Junior alianza kumuongelesha Eve baada kumpigia gitaa kwa muda.

“Nambie tu My Junior”.Eve naye alimwambia huku akisogea karibu kabisa kwa Junior kwani tayari alishajua maneno matamu yanaanza kumwagika kutoka kinywani kwa kachaa yule mjanja mjanja lakini bonge la boya kwa kimwana Eve.

“Nataka ufahamu kuwa fahari ya moyo wa binadamu ni kuona furaha kwa mwenzake ikikamilika bila bugudha.Kama mimi hapa sasa hivi,najisikia sana fahari kuwa na wewe na ninadhani nawe wajisikia the same way”.Junior alimuanza taratibu Eve kama hataki vile.

Eve aliyekuwa kapambwa na tabasamu huku asielewe siku ile ni nini Junii ataongea,alizidi kujipenyeza kwa Junii na kumgusa kwa makusudi na kifua chake kwenye eneo la ubavu wa kijana yule msanii.

“Endelea sasa msanii wangu.Mi najisikia fahari sana niwapo na wewe Junii.Unanifanya nisahau mengi.Embu endelea kunipa fahari hiyo My Junior”.Junior kusikia hivyo na kile kifua kilivyokuwa karibu yake,wacha kabisa.Jamaa likawa bwege kama si fala kabisa.

“Daah!Beautiful unanifanya nione dunia kama imeegemea upande wangu na vitu vyote vizuri katika maisha haya vimeterezea upande huohuo ambao mimi nipo mimi.Muda wote wanifanya nijisikie raha na amani niwapo na wewe.

Sauti yako nyembamba kama nota namba moja katika gitaa,ndiyo hasa inayonifanya nijisikie nipo hewani pale napoisikia sauti yako mwanana ya kumtoa samaki magamba bila kisu.

Nashindwa kukwambia huu kiasi gani mwenye mvuto.Ila kama MUNGU akiniuliza huu mzuri kiasi gani,naweza nikamjibu kwa kumwambia kuwa kakuumba kwa udongo wa kipekee ambao hakuna binadamu mwingine aliyewahi kuumbiwa udongo huo”.Junior alikuwa anafunguka maneno ambayo hadi leo hatujui aliyatoa wapi.

“Mmmh!My Junior,ya kweli hayo jamani?”.Eve ilibidi aulize.Lakini uliza yake ilikuwa ina jambo ndani yake.Kauliza ili Junii aendelee au kauliza ili kujua kama maneno ya Junii ni ya kweli,au kauliza ili aonekane kama kachangia kitu.Mimi na wewe hatujui,ila moja ni jibu lake.

“Sasa nikudanganye nini My Beautiful One.Embu angalia machoni pangu”.Junior alimuomba Eve atazame macho yake.Na Eve naye akatazama huku katoa lile tabasamu lake la kumtoa samaki magamba.

“Najua bado hujajua ni kwa nini umeangalia macho haya.Ila naomba kukuuliza.

Ndani ya macho haya umeona nini?”.Junii alimuuliza Eve swali ambalo laweza kukufanya ujue kama mwanamke huyo anaelewa maana ya mapenzi uliyonayo kwake au haelewi.

Inawezekana Eve alijua ni nini ajibu,lakini kwa kuwa alikuwa hataki kuonekana kama anaelewa,akajibu kinyume na mimi nayeandika nilivyodhani.

“Naona mboni My Junior”.Eve alimjibu huku bado tabasamu likitamba kwa mbwembwe usoni pake.

“My Beautiful One.Sidhani kama ndani ya macho yangu waweza kuona kitu kama hicho.Sawa kuna mboni,ila pia ukiangalia vizuri utajiona na wewe.

Nataka uelewe kuwa macho ni zaidi ya kioo.Macho ni zaidi ya kujieleza uonacho.Macho yangu ukiyaangalia,nadhani wajua wazi kuwa yanaeleza ni kiasi gani Junior mimi nashindwa kufumba macho pale napoona sura yako au napoikumbuka.Niamini My Beauty,wewe ni zaidi ya mboni uionayo wakati unaangalia macho yangu.

Siwezi kusema ya moyoni yaliyojificha lakini kama unataka kujua ya moyoni,ni lazima ujue haya ya machoni uyaonayo.

Moyo ni zaidi ya jinsi uujuavyo katika sanaa hii ya Maulana".Hapo Junior aliposema sanaa ya Maulana,alionesha tendo kwa mikono yake kwa kutengeneza duara angani.Akimaanisha sanaa ya Maulana ni Dunia.Akaendelea.

"Moyo waweza kubeba kila kitu ambacho binadamu hawezi kukibeba kwa mikono yake.Na hata mikono hiyo ikibeba,itaambulia kudondosha au kukipoteza.Lakini moyo ukiamua kubeba,umebeba tu! Ni wewe mwenyewe kuamua kupoteza au kukitupa kitu ulichokibeba.

Isikupite Hii: Geza Anasakwa Auwawe Ep 01

Kwa mfano siri za watu.Ni moyo pekee waweza kubeba hiyo kitu.Hakuna awezaye kuifanya siri hiyo ipate kopi yake kana kwamba umeihifadhi labda kwenye karatasi au CD.

Ndivyo ilivyo katika mapenzi.Kwanza ni moyo ndo una-disaidi kuwa huyu ndiye na huyu siye.Huyu aingie na huyu aisiingie.

Baada ya hapo ndio unapeleka kwenye ubongo na kumwambia ubongo aweke kumbukumbu juu ya moyo ulichoamua.Vinginevyo bila moyo kungekuwa hakuna mapenzi au upendo wowote kwa mwanadamu".Junior alikuwa anabwabwaja maneno ambayo kiasi fulani yalikuwa kama yanamfungua Eve.Na kwa mwonekano yalikuwa yanamuingia vilivyo Eve.

"Mmmh!My Junior.Lakini upendo si wajengwa kwa hisia kwanza ndio unapelekwa moyoni?".Eve ilibidi afanye kama swali lakini kiukweli alikuwa anataka kujua zaidi kupitia kwa Junior.

"Hapana My Beautiful. Hisia ni hali ya nje tu! Lakini moyo ndio kila kitu katika kuthibitisha upendo au mapenzi.

Hisia zaweza kuwa ndio au siyo.Yaani,waweza sema kuwa nampenda pale ulipomwona tu! Hizo ni hisia ndizo zimekutuma useme hivyo.Lakini siku zote moyo ndio unasema kweli kuwa umempenda.

Umewahi kusikia kuwa watu wameachana kwa sababu hawaendani au mke anakuwa nakiburi kwa mme wake na yupo tayari hata kupewa taraka ili aondoke.Umewahi sikia hiyo kitu?".Junior alimuuliza Eve.

"Hiyo nimesikia sana.Na hata rafiki zangu wamewahi kunihadithia mambo kama hayo kuwatokea".Eve alijibu huku bado yupo karibu kabisa na Junii ambaye alikuwa anamsikiliza huku anashusha juisi ya embe kwenye koo lake.

"Sasa hao walifuata hisia.Hao hisia ziliwatuma kuwa tunapendana ,na hisia hizo hizo ndizo ziliwaambia kuwa tufunge ndoa.Lakini walipotulia,waligundua kuwa mioyoni mwao hakukuwa na kitu kinachoitwa upendo bali ni hisia ndizo ziliwafanya wadhani wanapendana.

Huwa siamini kuhusu hisia hata mara moja.Hisia zaweza kusema kimbia na moyo waweza kukukataza usikimbie hasa katika hatari.Mara nyingi hisia hana ujasiri,ila moyo bwana,naupa hongera mno.Unaweza kuvumilia.".Junii alizidi kutema madini na kumwacha Eve hana neno bali tabasamu lisiloisha hamu.

Licha ya tabasamu hilo,Eve hakuthubutu kumuuliza Junii maneno yake yana maana gani.Na si Junii pekee ni hadi Hans na Fred,wote walikuwa wana maneno kama yanaendana,lakini Eve hakuweza kuuliza nia na madhumuni ya maneno hayo.

Alifanya hivyo akijua kwamba wale wavulana wamempenda na wanamuhitaji,lakini walishindwa kumwambia moja kwa moja bali kubaki wakiongea mafumbo kama wamemeza kamusi ya Wahenga.

Pia Eve alishindwa kuuliza kwa sababu alifahamu endapo atauliza tu!.Basi maneno yale yatageuka na kuwa sumu ya kumtongoza,yaani endapo atauliza basi atakuwa kawapa upenyo watu wale wanene wanachoki-feel mioyoni mwao.

Udhaifu wa kutongoza kwa vijana wale watanashati,ukawaponza na kubaki wakiumia na maumivu yao huku kila siku wakibuni misemo mipya ya kuongea.

“My Beautiful.Angalia jua”.Junior aliongea baada ya kumwacha Eve kwa muda akitafakari maneno aliyoyatoa.

“Yaah,My Junior.I see and I think it is gone”.Eve alimjibu Kiingereza Junii.Wakati huo jua ndilo lilikuwa likiwahi machweo yake,yaani ilikuwa ni muda wa saa kumi na mbili na nusu au na dakika zaidi ya thelathini.

“Noo.My Beautiful.Sijamaanisha uangalie ili unipe jibu ya kuwa linaenda kuzama.Nataka nikwambie siri moja ya jua hili ulionalo sasa hivi”.Junii alimrekebisha mawazo Eve.

“Tell me My Junior”.Eve kwa wahka naye akaitika.

“Jua ni kitu cha ajabu sana katika maisha yetu. Kwanza si choyo na halina ubinafsi kwa vitu vinavyofanana nae.Hapa na maana mwezi na nyota.

Jua katika muda wake wa kuwaka,unaweza kuuona mwezi na hata nyota.Lakini mwezi na nyota,zina ubinafsi sana.

Vitu hivi katika kuwaka kwake,huwezi kuliona jua hata kidogo.Namaanisha,jua linapozama linaachia kazi ya kuleta nuru mwezi na nyota.Na saa nyingine kukiwa kuna dalili ya mvua hasa mida ya usiku,mwezi na nyota,hujificha ndani ya mawingu na kutuacha sisi binadamu gizani.

Lakini jua,kamwe halifanyi hivyo.Litapambana na dalili ile ya mvua na saa nyingine linajificha ndani ya mawingu lakini baada ya kutufikiria sisi kuwa tupo gizani,hujitokeza na kuendelea kupambana ili tupate mwanga wake.Hiyo ni siri ya jua ambayo mimi nimeigundua”.Junii alimaliza na kumwacha Eve makusudi ili amuulize.

Kama alivyotegemea Eve akaingia line na kuuliza maana ya maneno yale.

“Haha ha haaa.My Beautiful.Kwanza tuanze kushuka huku ili turudi kwetu”.Junii alimwambia Eve,naye Eve hakuwa na kipingamizi zaidi ya kushuka katika mlima ule waliokaa karibu saa moja na nusu wakiongea na kunywa.

Huku wanatembea kurudi mjengoni wanapoishi,Junior aliendelea kutema madini yake.

“Napenda sana binadamu mwenye tabia ya jua kuliko hivi vitu vingine kama mwezi au nyota.Natamani kukwambia kuwa wewe ni kama jua kwa watu”.Eve aliposikia hivyo,alitabasamu na kumsogelea Junii tena na kupitisha mkono wake kwenye mkono wa Junii kisha akamlalia Junii kidogo kwenye bega.

“Kwa nini unasema hivyo my Junior”.Eve alimuuliza Junior huku akijiweka sawa kuzipokea sifa kedekede kutoka kwa msanii yule.

“Popote waliporafiki zako na wewe upo. Kamwe huwaachi wakiwa peke yao. Umekuwa ukiwahakisi mwanga wako kama jua lifanyavyo kwa nyota. Hutaki wakae gizani kama kuna hali hiyo. Nathibitisha haya baada ya kukuona mara nyingi sana upo karibu yetu. Hata iwe saa ngapi,tukikuita waja. Hakuna mwanadamu kama wewe,naweza kusema hivyo.

Umebarikiwa moyo wa jua,moyo ambao hutaki kumwona mwenzako akipata shida wala kuteketea. Kama nikisema wewe ni zaidi yao,sidhani kama nitakuwa nakosea. Hu mzuri kuanzia nje mpaka ndani. Hu mwema kiakili hata matendo. Upo tayari kutoa faraja kwenye mwenye simanzi na upo tayari kufariji kwa kila neno zuri kwa mwenye kuhitaji maneno ya faraja".Junior alikuwa akibwabwaja maneno mazuri na masafi kwenda kwa kimwana yule,lakini kila alipotaka kutamka hisia zake kutoka moyoni kuwa anampenda Eve,alishindwa na kubaki akiangalia mbele.

Udhaifu huo Eve aliujua hivyo ilikuwa ahueni kwake kwani kama Junior angetamka kuwa anahiotaji kuanzisha mahusiano ya kimapenzi naye,basi mambo aliyoyapaga yasingetimia.

"Mmmh!My Juu,ya kweli hayo".Eve aliuliza huku bado katoa tabasamu lake mwanana lililopamba hata njia wanayoikanyaga.

"Kwa nini nikudanganye My Beautiful. Umeumbwa kwa ajili ya watu kama sisi wenye kuhitaji faraja. Wewe ungekuwa kiungo katika mwili wa mnyama basi ungekuwa moyo au kichwa. Na kama nikiulizwa una umuhimu gani katika maisha yangu,ningesema wewe ni damu mwilini mwangu. Ukiondoka nakuwa sina uhai,ukisimama nakuwa katika koma na ukimwagika,unaniachia maumivu".Maneno yalizidi kukandamizwa na Junior.

"Mmmh!Haya bwana.Naona karibu tunafika madarasani. Natamani niendelee kukusikiliza,lakini daah!Yanibidi niende My Junii. Nitakuja kukuona tena kesho,palepale mnapopataga chakula nawenzako".Eve alikuwa anamwambia Junior baada ya kufika maeneo yalipo madarasa yao.

"Okey, My Beautiful. Uende salama na ukawaangazie wote wenye giza huko uendapo. Wewe ni jua kama nilivyokwambia,usiubane mwanga wako kwa wanaouhitaji".Junior alimwambia Eve naye Eve kuonesha kama shukrani au ili asimuumize Junior atakapoondoka,au labda kumpa moyo ili Junior ajione mwenye bahati,akambusu shavuni Junior halafu kwa sauti nyembamba na ya kubembeleza,akamnong'eneza sikioni kwa kumwambia kwa heri my Junii.

Safari yao ikaishia hapo huku Junior akibaki kaduwaa asiamini kama ni yeye aliyepewa busu zuri kama lile na mtoto mzuri kama yule.

Alimwangalia Eve jinsi anavyoenda anapoenda naye Eve kama alijua anaangaliwa na Junior,aligeuka na kisha akabusu mkono wake wa kulia na kumfanyia ishara ya kulipuliza busu lile kwenda kwa Junior.

****

Junior alifika kwa wakina Fred na aliwakuta wote watatu wapo. Wote hawa walikuwa hawana siri juu ya mambo yanayotokea wakikutana na Eve. Japo walikuwa hawafichani,lakini walikuwa wanadanganyana sana. Na ndicho kilitochotokea kwa Junior baada ya kufika mle ndani.

"Tehe! Tehe! Teheeeee. Mtabakia kushika mapembe tu!Maziwa anakamua mtu mwinginee.Tehe! Tehe! Teheee".Junior alianza mbwembwe zake kwa kucheka kama katuni.

"Naona umeshaanza kujungua mwenyewe. Haya bwana,ila hayo maneno tu! Hata vyombo vya habari siku hizi vinatemeana".Hans aliongea baada ya Junior kusema maneno yake.

"Sasa kama nyie ni washika mapembe,nisiseme?. Mnakukuruka kushikilia mapembe ng'ombe,na ling'ombe linawarusha-rusha na kuwadoboa tumboni na mapembe yake lakini hata hamkomi. Jingine limeshikilia miguu yake huku chini,linapigwa na kwato za kidevu lakini bado bishi. Utakufa Baba Paroko,hii ligi ya watu wazima.

Wewe Hans kamata mapembe na saidiwa na huyu Suarez.Wewe Baba Paroko,kamata kwato mzee. Mimi nakamua taratibuuu,kama nanawa vile. Najinywea vyangu. Nyie endeleeni kudobolewa na mapembe".Junior alikuwa anaongea hayo huku anavua viatu vyake na kwenda anapolala.

"Dah!Kwa hiyo na mimi nipo Junior".Aliuliza Suarez baada ya maneno ya Junior.

"Sasa utakosa wewe. We upo kila usehemu. Ukichoka kupigwa pembe,njoo kwa Baba Paroko umsaidie kupigwa kwato za chembe.Ha ha haaaa".Junior aliongea kwasharau na kupandisha miguu yake kitandani,kisha akalala kifudifudi.

“Daah! Haya bwana. Ila kama kweli sisi washika mapembe na kwato,sidhani kama kesho kutwa nitaenda kushindwa kukamua maziwa”.Aliongea Hans na kuficha uso wake kwa kitabu.

Maneno hayo yalimshtua Junior na kumfanya akae na kumuuliza Hans.

“Unaenda kukutana naye?”.Junior aliuliza.

“Unauliza jibu tena”.Hans akajibu kwa kifupi wakati huo Fred yeye alikuwa kimya akiwatazama wale jamaa wanachoongea. Siku zote Fred alikuwa mtulivu sana,hakuwa na papala kaika maongezi yake,ila akiongea huwa yanawachoma sana na ndio maana hata Junior aliwachoma kwa maneno yake kwani ndio tabia zao.

“Ha ha haaa,linaenda kula makombo yangu”.Junior alimwambia Hans.

“Yawezekana leo ndo mara yako ya kwanza kukutana Eve wewe. Mwenzako kesho mara ya …….. Eti mara ya ngapi Jogoo wa Jiji”.Hans alijidai kasahau idadi alizokutana nazo na Eve,hivyo akamuuliza Suarez ambaye alikuwa shabiki wa timu ya Liverpool ambao wanajiita majogoo wa jiji.

“Sijui mara ya arobaini hiyo. Daah!Ujue sina uhakika kwa sababu siku nyingine huniambiagi.Ila nahisi itakuwa mara ya arobaini au arobaini na tano hivi”.Alijibu Suarez ili kumuumiza Junior.

“Yaah! Wewe sikukwambiaga mara kumi tu! Kwani sikutaka ujue nimempeleka gesti gani. Kwa hiyo nimekutana na Eve kitu kama mara hamsini hivi mdogo wangu. Unavyosema naenda kula makombo yako,nakushangaa sana. Mi najua hata mate hujawahi kuambulia zaidi ya kuumiza miodole yako kwa kupiga gitaa.

Mgitaa wenyewe unalia kama mgobole wa kuulia tembo au ukipiga sauti nyembamba linalia kama unanoa kisu,hadi unamuumiza meno mtoto mzuri kama yule”.Hans alikuwa anamiga madongo Junior hadi chumba kizima kikawa kimetawala vicheko.

“Eti sijala mate, Thubutuu,wewe unacheza na mimi nini?Leo mtoto nimempa maneno matamu hadi kalegea na kunipa ulimi wake mwenyewe. Mi napiga saundi hata mti wa mbuyu ukizisikia uweza kukatika au kulala hapo hapo. Napiga saundi hadi simba dume linabadilika sauti na kuwa kama ya mtoto wake”.Junior alizidi kujiifia kwa uongo na kuwaacha watu wakitafakari maneno yake kwa kuwa walikuwa hawana uhakika kama ni uongo au kweli.

Uzuri wao walikuwa hawajali kuchangiwa kwa maneno. Leo unaweza kukuta Hans anasemwa na chumba kizima,halafu kesho Junior na siku nyingine ni Fred. Sasa siku ile ilikuwa ni zamu ya Junior na aliyataka mwenyewe

“Kwenda zako huko.Nilikuwa nakusikiliza kitambo.Tangu umeingia hapa”.Alikuja Fred na kumrukia kwa maneno Junior.

“Tena wewe Baba Paroko kula ngumu,kwa sababu huna sumu.Siku ile kum-kiss manzi ukajiona ndo kidumee. Mwenzako leo nimepewa lile orijino kabisa”.Junior naye akajibu mapigo kwa Fred.

“Acha kutudanganya. Domo lenyewe linanuka hadi huku halafu unasema umekula mate mtoto yule. Sijui umekunywa manini. Usituzuge hapa,huwezi kula mate na maarufu yako ya karanga mdomoni. Eti nilionea maneno matamu,unamaneno gani matamu wewe kama si kulia lia tu!. We si bongo fleva,kazi yako kulia tu!.Nenda huko kaimbe kulia lia magerezani kama ule wimbo wa Tunda. Lakini huna maneno matamu zaidi ya kujisumbua”.Aliongea Fred maneno kumwendea Junior.

“Ha ha haaa.Mzee wa Upako mpe huyo. Kazi kulia kama PNC,wagumu kama Chid Benz tunazidi kunguruma kwa mtoto hadi anasalula viwalo vyake mwenyewe”.Aliongeza Hans lakini Fred naye alimkata.

“Na wewe sepa zako hapa.Huna lolote,yule demu hujala wala nini. Kama umekula niambie umekula lini ili nikuulize swali”.Fred alimwambia Hans.

“Yule wiki iliyopita nilikuwa naye kwenye lodge moja kule Sinza. Hadi nikaoga naye”.Hans alijibu kwa kujiamini wakati huo Junior alishapewa vyake na kutulia,na Suarez yeye alikuwa mtu wa kusikiliza na kucheka kutokana na yale maongezi.

“Eheee,hapo hapo. Sasa mimi nilipiga pale wiki mbili zilizopita na kuna alama nilimwachia kiunoni.Niliandika kwa wino ambao hata ukae mwezi haufutiki. Na nilimwandika wakati kalala,hivyo hajui kama kaandikwa. Niambie,umeona alama hiyo wakati unaoga naye?Na kama umeiona,imeandikwaje. Sema ukweli usidanganye”.Fred alimuuliza Hans ambaye kidogo aligwaya baada ya maneno yale.

Hamna hata mmoja aliyekuwa anamwambia mwenzake ukweli,ilikuwa basi tu! Kutambishiana.

“Jibu.Lione kwanza kichwa lake kama kibuyu cha kuchotea maji kijijini”.Junior alimpa kavu la uso Hans baada ya kumwona kagwaya kujibu.

“Mzee waUpako umetisha. Jamaa kanywea kama mchicha japo mara ya kwanza alikuwa kajaa sufuria”.Suarez alimpa sifa Fred.

“Msijifanye mnajua hapa,kumbe tunaojua tumetulia tuli. Keshokutwa ukienda kukutana naye,mwangalie kiunoni,utakuta nimeandika kwa herufi kubwa jina langu. Hapo ndo utajua kuwa washika mapembe na kwato ni nyie,sisi wazee wa nyonyo tunakamua taratibu maziwa yetu. Mtaniambia nini nyie,mimi fundi. Udambwidambwi mwingi kama Mbwiga Wa Mbwiguke,si fundii.

Mafundi hatuchafuki,sisi wazee wa biliji tu! Sasa wewe kibarua endelea kupigwa kwato na domo lako linalonuka kama kwapa la mwehu”.Akamaliza Fred na hapo kimya kikafuata huku kila mmoja akiwa haamini alichoongea Fred.

Wote walijua ni kweli Fred anaweza kuwa ametembea na Eve hasa kwa sababu alikuwa anajiamini sana katika matendo yake. Lakini haikuwa hivyo,Fred alikuwa ni mtu wa maneno tu kama wao.

“Daah! Mzee wa Upako au Mzee wa Biliji,naona umewanyamazisha wananchi wote. Sasa nadhani watasoma,maana tambo zilikuwa nyingi sana hapa”.Suarez aliongea huku akitabasam baada ya kimya kidogo kupita.

“Hawa wote ni makuku tu! Mchana majanja,usiku yapo hoi kwa kuchoka kwa sababu ya mchana kuchakua chakua majalalani. Kila mbuzi ale kutokana na urefu wa kamba yake.

Kama leo wewe Junior uemtoka naye,hatujakufatilia. Keshokutwa Hans,hamna kumfatilia. Mimi kaniambia Jumapili. Natoka naye usiku kwenda kupata naye msosi hotelini,sitaki usumbufu. Mimi zangu hotelini,wewe Jun wajua wapi unapokutana naye na wewe Hans wajua yako. Hamna kuharibiana,sawa?”. Wote wakajibu sawa na mjadala ukafungwa hapo.

****

HANS NA EVE.

Kama walivyoahidiana siku tatu zilizopita,ndivyo ilivyokuwa mida fulani ya mchana katika siku ile ya Ijumaa.Eve akiwa na Hans katika fukwe za Coco,walikuwa wametulia kwenye kivuli kimoja cha mwamvuli wa ufukweni na kila mmoja alikuwa katikamavazi ya ufukweni.

Hans akiwa kavaa kaptula moja nyepesi ambayo ilikuwa maalumu kwa maeneo yale,alionekana mwenye tabasamu pana mbele ya mrembo Eve ambaye naye alikuwa kavaa kiblazia kidogo kilichoficha kifua chake lakini kikiacha kitovu nje,na kwa huku chini kajifunga kama mtandio wa ulioanzia maeneo ya tumboni hadi miguuni.

Muda wote Hans alikuwa anatamani ule mtandio wa Eve japo udondoke ili aone kama kweli kuna mwandiko wa Fred kwenye kiuno cha Eve.

Hans akiwa amelala pale kwenye kivuli,alimuona Eve anakuja na vikombe vya plastiki viwili ambavyo ndani yake kulikuwa na koni aina ya Vanilla. Ule mtandio aliokuwa ameuvaa ulikuwa unaangaza na kuonesha nguo yake aliyovaa ndani ambayo ilikuwa ni ya ufukweni zaidi.

Mwangaza ule wa mtandio ambao ulichagizwa zaidi na jua kali ambalo lilikuwa linawaka muda ule,ulimfanya Hans amkodelee Eve macho tangu alipokuwa anatoka kule aliponunulia koni hadi pale alipokuwa Hans.

Eve aliyaona macho yale ya Hans na alijua kachizika kwa yale mapigo.Japo aliona aibu kiasi fulani lakini ilibidi avumilie ili apate anachokitaka kwa Hans,ambacho ni maneno matamu.

Alipofika pale mbele ya Hans,alitabasamu na kumuuliza mbona anamwangalia vile.

“Bado najiuliza MUNGU alichanganya kemikali gani hadi akakutoa kiumbe kama wewe. Sidhani kama MUNGU kakuumba kwa udongo bali kemikali maalumu ambazo ukizichanganya huwezi kupata madhara bali faida ya zao kama wewe,zao lililonifanya nikuite sweet. We ni mtamu Eve”.Hans aliongea huku bado Eve akiwa amesimama mbele yake kwa tabasamu la haja toka usoni pake.

“Mmh! Hans,yanaukweli hayo usemayo?Mbona mi wa kawaida tu! Embu niangalie”.Eve aliongea hayo kama kutaka uhakika kwa Hans na hapo akageuka na kumpa mgongo kidogo Hans na kisha akamgeukia tena.

“Daah! Unajua Eve unaweza kuitoa dunia kwenye mhimili wake na kuifanya ijizungushe kwenye mhimili wako?”.Hans alifanya kama kumtupia swali Eve na kumfanya Eve atabasamu zaidi ya pale na kisha akaenda hadi pale karibu na Hans ambapo palikuwa na kiti kingine cha kulala maalumu kwa ajili ya ufukweni.

“Bwana mimi sielewi hayo Hans,hayo mambo ya dunia kujizungusha si mambo ya Jegrafia?Mimi nilisoma HKL bwana,hata sijui”.Eve aliongea kwa kudeka baada ya kukaa kwenye kile kiti mlalo cha ufukweni.

Hans kusikia hivyo ndio akajiona kama mtu mwenye bahati kuliko hata bahati yenyewe. Akainuka pale alipokuwa kalala na kisha akakaa kumwelekea Eve ambaye naye alikuwa amekaa na vikombe vyake akiwa kavishikilia.

“Leta kwanza nikusaidie hivyo vitu maana naona kama mkono yako itachoka”.Alichukua zile koni na kuziweka pembeni kisha akarudi usoni kwa Eve.

“Sweet Eve,si wajua kuwa dunia inajizunguka kwenye mhimili wake,huku inafuata njia zinazoitwa Obiti na wakati huo huo inakuwa inazunguka jua?Kwani hata hilo la form two hukijui?”.Hans alimuuliza Eve.

“Aaah!Zamani sana hiyo Hans.Ila nakumbuka kidogo”.Alimjibu Eve.

“Basi nisikutese Sweet wangu. Naposema dunia itaacha kujizungusha kwenye muhimili wake na kukuzunguka wewe,namaanisha hata dunia itakufuata wewe unachotaka. Hata ukiiambia zunguka kutoka kati kwenda kulia,itatii au ukiiambia izunguke pembeni kwenda kati napo itatii,hii ni kwa jinsi ulivyokuwa mzuri.

Kama tupo vitani,sina haja ya kubeba mabomu kama Rambo au Shoziniga,wewe ni silaha tosha ya kuwaua maadui. Una madhara matamu na si machungu kama bomu la nyukilia. Naapa mbele ya MUNGU,wewe hujaumbwa na udongo bali kemikali zenye harufu nzuri na utamu uliopitiliza. Hujawekewa asidi kwenye kemikali hizo ulizoumbiwa bali umewekewa asali ambayo siku zote nahisi MUNGU alikuwa ameihifadhi ili aje akuumbie wewe”.Hans akazidi kutema maneno matamu mbele ya mtoto mzuri Eve.

“Wewe HANS wewe. Hivi hujui MUNGU anakuona na kukusikia maneno yote unayoongea?”.Eve alimuuliza Hans huku akimwangalia kwa macho ya yaliyojaa furaha.

“Sidhani kama MUNGU anakataza mimi kukusifa wewe kwa jinsi navyokuhisi moyoni mwangu. MUNGU hakatai hilo,ila cha msingi nisivuke mipaka na kumkufuru”.Hans alimjibu Eve na kumwacha mtoto yule mwenye uzuri wa kuita bila swali.

“Mh!Haya bwana.Basi naomba koni,isije ikayayuka bure maana ikiyayuka inakuwa mbaya”.Eve alikata shauri na Hans akampatia koni na kisha wakaanza kuburudika kwa kiburudisho kile.

Wakati wanaendelea kuburudika,mara kwa mbali ikasikika sauti ya meli ikipiga honi.Hapo Eve akapata swali la kumuuliza Hans.

“Eti Hans,ni kwa nini meli na ukubwa wake haizami kwenye maji lakini shilingi mia na udogo wake inazama?”.Eve alimuuliza swali la Fizikia Hans.

Hans akatabasamu kidogo na kujiweka sawa kwa ajili ya kujibu swali hilo. Japo lilikuwa ni swali la kifizikia,lakini pia Hans alilipeleka mbali zaidi na kuwa la kimapenzi.

“Hilo swali wengi sana wanapenda kuliuliza hasa wale wasiopitia Physics. Ila kwa kuwa umeniuliza,nitakujibu na kukupa mfano hai.

Hapo tunarudi kwenye Law of Floatation,yaani hapo utalezea kuhusu vitu kuelea hasa meli.Law ina state hivi……(Akaelezea hiyo sheria ya vitu kuelea).

Sasa najibu swali lako kama ifuatavyo”.Eve alikuwa kimya na makini wakati hayo yote Hans anayaelezea.Alionekana wazi mwenye uhitaji wa kufahamu alichouliza.Hans akaendelea.

“Meli kwa huku chini kabisa,ina nafasi kubwa sana ambayo nafasi ile haina tundu hata moja litakalopitisha maji. Yaani ni kama pulizo ile sehemu au dumu ambalo halina kitu na lililofungwa na kifuniko chake. Basi na kule chini ndipo papo hivyo.

Dumu likiwa halina kitu ndani yake,waweza kuelea nalo hata kilomita mia bila kuzama,lakini endapo litaingiza maji basi ujue utazama tu.

Na meli kwa pale chini,imeundwa kwa mtindo huo. Kule chini kuna hewa na ahairuhusiwi maji kuingia. Na nafasi ile ya hewa imepimwa ili kubeba uzito fulani wa mizigo. Kama ukizidisha,ndio unakuta meli inazama.

Shilingi mia au shilingi kumi,hazijatengenezwa na nafasi chini yake bali zenyewe ni mzigo ndo maana zinazama.Umenipata?”Hans alimaliza na kumtupia Eve swali.

“Sina swali aisee,upo juu Hans nimekubali”.Eve alimjibu Hans.

“Nashukuru Sweet. Sasa ngoja nikwambie kitu kuhusu wewe”.Hans aliendeleza tena maongezi.

“Ehee”.Eve akakaa mkao wa kula kwa ajili ya kusikiliza maneno toka kwa Hans.

“MUNGU kakuumba kwa mtindo wa meli,Sweet. Hata ubebe mangapi sidhani kama waweza kuyazamisha. Sweet,najua umebeba mengi sana moyoni mwako,naomba usiyazamishe hata kama yamekuzidi. Elea nayo hadi mwisho wake,naamini MUNGU atakupa zawadi ya kipekee katika maisha yako. Kamwe usijaribu kuyazamisha haya uyaonayo na kuyasikia.

Acha nikusifie Sweet Eve. Uwezo wako wa kubeba haya niongeayo waweza shinda meli zote za jinsia yako. Sikufananishi na ile meli kubwa kama Titanic ila naweza kukufananisha na lile Safina alilotengeneza Nuhu kabla ya MUNGU kuleta Gharika”.Alipofika hapo Eve akarudi nyuma kidogo na akawa kama anamshangaa Hans kwa yale maneno.

“Wewe Hans. Hayo maneno ya Biblia umeyatoa wapi. Na Sayansi na dini ni wapi na wapi?”.Eve akauliza huku bado akimshangaa Hans.

“Ha ha haaa. Sweetie,hujui kuwa nakaa na Mzee Wa Upako? Anatupaka maujuzi mara moja moja. Japo tunajidai hatusikilizi,lakini ndio hivyo,huwa tunachukua maujanja.

Halafu asikudanganye mtu,hakuna mtu ambaye anamuamini MUNGU kama mwana Sayansi.

Ngoja nikupe kidogo kuhusu hawa Wanasayansi hasa wale wa hali ya hewa na wanaopaa na vyombo kwenda nje ya sayari hii ya dunia".Eve kusikia hivyo alisogea tena karibu na Hans na kumsikiliza.

Eve alikuwa anapenda sana kujifunza mambo mengi kupitia watu tofauti tofauti,hivyo uwepo wa Hans,Fred na Junior,ulimfanya ajifunze mengi sana asiyoyajua. Hans akaendelea.

"Kuna mwanasayansi mmoja,jina nimemsahau,ila yeye alikuwa kajiweka sana kwenye mambo ya Meteolojia,haya mambo yanayohusu hali ya hewa.

Yeye alisema kuwa, kama jua litapungua au kuongezeka uwezo wake wa kuwaka basi dunia inaweza kudondoka. Yaani zile nguvu za ukinzani ambazo ni kama sumaku,na ndizo hizo zinaiweka dunia iendelee kuzunguka katika muhimili wake bila kudondoka,eidha zinaweza kuongezeka nguvu na kuifanya dunia ipoteze mwelekeo au zinaweza kupungua nguvu na kuifanya dunia idondoke. Hiyo yote itatokana na jua kuongezeka na kupungua uwezo wake wa kuwaka.

Kwa maana hiyo,yeye alimaanisha kuwa dunia inategemea sana nguvu za jua katika kujiendesha kwake.Na huyu Mwanasayansi ana Law yake. Ngoja nitakuletea siku moja umjue.

Baada ya kusema hayo,akakaa muda mrefu na hiyo Law yake ikawa inatumika sana.Lakini baadaye lile bara la barafu linaitwa Antakatika,barafu ikaanza kuyeyuka. Vina vya vyanzo vya maji kama bahari na maziwa,vikaanza kupungua. Wachunguzi wakachunguza,wakagundua kuwa miale ya jua imekuwa mikali sana,yaani jua limeongezeka ukali wake.

Walipoenda kuitazama dunia waone kama itakuwa inapoteza mwelekeo,waliikuta ipo vilevile. Mwendo na sehemu ilipo,vilikuwa palepale. Yule mwanasayansi alitikisa kichwa na kusema mwacheni MUNGU awe vilevile MUNGU,hakuna ajuaye uwezo wa MUNGU".Hans akawa anampa soga Eve ambayo kweli ilimvuta na kumfanya awe kimya.

"Mh! Hans wewe ni kiboko".Alisifu Eve.

"Na si huyo tu! Wanasayansi wote wanamwamini MUNGU kuliko mtu yeyote. Kuna wale waliotengeneza maroboti. Wameweza vyote,lakini kumpa pumzi wameshindwa,wakasema hiyo ni kazi ya MUNGU. Hivyo japo wanajidai wajanja,lakini bado wanaenda nyumba za ibada na kumuomba MUNGU ili awasaidie".Hans alizidi kutema madini kwa mtoto mzuri.

Kimya kikapita na kila mmoja akawa anaburudika na kiburudisho chake.Ni Hans ndiye alianzisha tena maongezi mengine.

"Sweetie,wajua kuogelea?".Hans alimuuliza Eve.

"Mmmh! Mwenzako hata sijui".Alimjibu Eve.

"Twende nikakufundishe".Hans aliongea na bila kusubiri jibu alikuwa tayari kanyanyuka na kumnyooshea mkono Eve ili aushike naye anyanyuke.

Eve akabaki bila tendo.Kukataa anashindwa na kukubali anashindwa.Ila kwa kuwa alikuwa katoka na mtu,ilimbidi akubali.

Ni kama Hans alikuwa anasubiri sana kipengele kile ili aone alama ambayo Fred alisema kamchora Eve. Muda huo ukafika aisee.

Eve akatoa ule mtandio baada ya kunyanyuka na akabaki na nguo fulani kwa ajili ya ufukweni ambayo iliacha kiuno chake wazi.

Hapo Hans alicheka sana hadi Eve akauliza una nini.

“Daah!Nimemkumbuka sana Mzee Wa Upako. Jana nilimwambia natoka na wewe tunaenda beach akasema niangalie sana mavazi yangu. Sasa ndio nimekuangalia wewe mavazi yako na mimi,daah! Nimeamua nicheke tu! Hata hatuendani aisee”.Alidanganya Hans ila ukweli alicheka kwa sababu hakuona huo mwandiko ambao Fred alisema kamuandika Eve kiunoni.

“Ha ha haaa,utajiju. Wewe unakuja beach kama unaenda kucheza mpira”.Eve naye alishadadia na hapo akaanza kuelekea palipo na sehemu maalum ya kuogelea huku Hans akiwa pembeni yake.

Eve akatoa ule mtandio baada ya kunyanyuka na akabaki na nguo fulani kwa ajili ya ufukweni ambayo iliacha kiuno chake wazi.

Hapo Hans alicheka sana hadi Eve akauliza una nini.

“Daah!Nimemkumbuka sana Mzee Wa Upako. Jana nilimwambia natoka na wewe tunaenda beach akasema niangalie sana mavazi yangu. Sasa ndio nimekuangalia wewe mavazi yako na mimi,daah! Nimeamua nicheke tu! Hata hatuendani aisee”.Alidanganya Hans ila ukweli alicheka kwa sababu hakuona huo mwandiko ambao Fred alisema kamuandika Eve kiunoni.

“Ha ha haaa,utajiju. Wewe unakuja beach kama unaenda kucheza mpira”.Eve naye alishadadia na hapo akaanza kuelekea palipo na sehemu maalum ya kuogelea huku Hans akiwa pembeni yake.

Walipofika Hans ndiye alikuwa wa kwanza kujitupa majini na kuanza kuogelea huku Eve akiwa nje anaogopa kujitupa majini. Ilibidi Hans atoke na kumfata pale nje maji ya kumuuliza kwa nini ajumuiki naye.

“Mi naogopa bwana Hans”.Eve akamjibu Hans kwa sauti ya puani.

Hans akacheka kidogo na kisha akaanza tena maneno yake aliyobarikiwa na muumba.

“Ujue Eve usiwe kama mtoto mdogo bwana. Haya ni maji tulivu ambayo hayana kakala kama yale ya baharini. Haya ni maalumu hayawezi kupwa wala kujaa. Yale ya baharini kuna muda yanaenda mbali zaidi,na hapo watu ndipo wanapopata nafasi ya kuchezea fukwe za bahari. Lakini baadaye maji yale hurudi na kujaa fukwe yote hii.

Hii kama hujui inatokana na mzunguko wa dunia. Ngoja nikupe mfano hai”.Hans alitoka pale alipo Eve na aliporudi alirudi na chupa ambayo aliweka maji kiasi bila ile chupa kujaa,kisha akaanza kumwonesha anachomaanisha.

“KWA mfano,fanya hapa ndipo sisi tupo”.Akaonesha kule chini ya chupa ambapo chupa ilikuwa imesimamia.

“Si waona kuna maji eeh. Basi dunia inazunguka namna hii”.Akazungusha ile chupa hadi kule chini ambapo alisema ndipo wapo wao kukawa juu.

“Si waona maji yamehama eeh,na ukirudisha tena,maji yanajaa. Basi mfano huu ndio dunia ikifanyacho na ndio maana tunapata kupwa na kujaa kwa bahari.

Na ndivyo binadamu wengi walivyo,wapo wa kupwa na wapo wa kujaa. Kamwe usiyaogope maji bali ogopa walimwengu ambao ndio hawa watu.

Kuna muda huwa hawana madhara na mambo mengi,yaani wanakuwa wana roho nzuri na ya upole wenye wingi wa mambo. Hali hiyo hufanya watu wanajiita wanafunzi au wenye uhitaji wa kujua, waende kujiokotea chochote kupitia watu hawa.

Lakini kuna hawa wasiopenda kuchezewa sharubu,hawa ndio wazee wa kurudi na kujaa mahasira.Hawa si rahisi kuokota chochote kwao,kwani hawakupi nafasi hiyo hata kidogo. Muda wote wanakuwa wanamiliki eneo lao.

Sidhani kama wewe Swetie upo hivyo. Najua wewe ni kama mimi,siku zote ni watu wa kupwa tu! Tunaruhusu watu waokote chochote pale tunapokupwa. Kamwe usiruhusu kujaa bali jifunze kupitia wao pale wanapokuja kuokota chochote kwako".

"Mmmh! Wewe Hans hayo yote unayoongea umeyatoa wapi? Mbona kama mwanafalsafa vile. Yaani haya makubwa,na madogo yana nafuu. Haya bwana,ngoja mi niendelee kuokota".Eve alimwambia Hans baada ya Hans kuweka kikomo katika maongezi yake.

"Mi nilitaka ufahamu kuhusu kupwa na kujaa kwa bahari na ni vipi hali hii inaendana na maisha yetu. Kaa ukifahamu kuwa kila kitu hapa duniani kimeumbwa ili tukitawale sisi. Na kaa ukijua kuwa kila kitu kimeumbwa ili kitufundishe sisi jinsi ya kuishi na jinsi ya kufanya mambo yetu.

Kwa mfano,mchwa. Wale wameumbwa ili watufundishe jinsi ya kufanya kazi. Mti umeumbwa ili sisi tujue kutoa kama ujuavyo wenyewe kutoa kivuli na hewa safi". Hans aliendelea kumpa maneno mazuri Eve.

"Mmmh! Hans unanidanganya bwana. Na je bata,kuku na mbwa. Hao nao wameumbwa kwa ajili ya sisi kujifunza kupitia wao?.Embu angalia tabia zao. Wanalelewa vizuri na mama yao lakini baadaye wanakuja kuzaa naye tena. Au kama ni mbwa dume,basi kila mbwajike linamtaka,huyo tena wasema kaumbwa ili tujifunze kupitia yeye?".Eve alimuuliza swali ambalo lilimfanya Hans atabasamu kidogo na kusahau kuwa wameenda pale kuogelea na si kupiga stori.

"Kwani Sweetie,haya maisha umeumbwa kujifunza mazuri pekee?au mazuri na mabaya. Na hivi wajua kuwa mbwa anawakilisha dhambi katika vitabu vya dini? Mbwa alishalaaniwa kwa kupewa dhambi ya urafi. Huyo kuku na bata ndipo watu wanajifunzia tabia za ubakaji na mambo machafu ya kutembea hata na watu saizi ya wazazi wao.

Kila kitu duniani kimeumbwa kitufunze,niamini mimi Swetie. Lakini ndio hivyo,wapo wanaojifunza maovu na wapo tunaojifunza mazuri".Hans alimwelezea Eve na Eve alibaki bila swali bali kumwangalia Hans bila kummaliza,na mwisho alitikisa kichwa kama kusikitika lakini alikuwa haamini yale aliyoyasikia.

"Vipi Swetie,mbona wasikitika?".Hans alimuuliza.

"Wewe ni jiniazi Hans".Alisema ya moyoni.

"Ha ha haaa,twende basi kuogelea kidogo halafu tuondoke si wajua jua linaenda hilo na usafiri wa huku ni majanga tupu".Hans alitupa kete yake nyingine kumvuta Eve waende kuogelea.

"Lakini nikizama hii kesi ni yako".Eve alitoa onyo mapema huku akisogea na kukaa kisha akaweka miguu yake kwenye maji yaliyo kwenye "swimming pool" ya pale.

Hans yeye alirudi nyuma kama hatua kumi kisha akaanza kukimbia kwa kasi sana kuelekea ilipo swimming pool ile. Alipofika karibu aliruka juu huku katanguliza mguu mmoja mbele kama anampiga mtu teke la uso. Hakuruka hivyo peke yake bali aliambatanisha na sauti ya kama ya kujikakamua.

"Iyaaaaa". Baada ya sauti hiyo ilisikika sauti ya kutumbukia kwenye maji na eneo lile lilitapakaa maji kutokana na mtupo wake ule. Ni kama bomu lilitupwa kwenye swimming pool ile.

Eve kama walivyo wanawake wengine walikuwa hoi kwa kucheka na wanaume wengine waliokuwa eneo lile walikuwa wanashndwa kumtafsiri jamaa. Mbele ya mrembo kama Eve,anafanya kituko kama kile.

Hayo yote Hans hakuyafikiria bali alipoibuka toka kule alipokuwa amezama alimfata Eve pale alipo na kuanza kuongea naye huku ameweka mikono yake kwenye mapaja mazuri ya mwanadada yule.

"Njoo basi ndani na wewe".Hans aliongea kistaarabu kama si yule aliyetoka kufanya kituko muda wa dakika moja uliopita.

“Yaani wewe bwana. Unavyoongea na mambo yako kama si wewe.Embu mwone kwanza”.Eve aliongea huku katabasamu na kumshika kidevu Hans.

“Kwani nimefanya nini Swetie. Embu acha hizo bwana,njoo tuogelee”.Hans aliongea huku akishika kiuno laini cha Eve na kuanza kumvutia ndani ya maji Eve.

Eve naye alikuwa hana kipingamizi bali kuingia ndani maji ila akiwa na uwoga kiasi fulani.

“Ukiogopa ndo unazama”.Hans alitania na kumfanya Eve atake kukimbia lakini Hans alishamkamata vizuri hivyo hakuweza kuondoka.

“Usijali Sweet.Unapokuwa na mimi,usalama unakuwa mkubwa kuliko hata ukiwa na usalama wenyewe. Mimi ndiye Hans The Man,usiogope”.Hans aliongea maneno hayo kwa sauti ya kunong’ona huku kamnyanyua Eve ndani ya maji. Mikono yake mmoja ukipita chini ya mapaja na mwingine nyuma ya mgongo na wakati huo Eve alikuwa kabana mikono yake kwenye shingo ya Hans.

“Ukinizamisha Hans”.Eve aliongea huku akiwa na uoga pale Hans alipokuwa anamshusha majini taratibu.

Alifanikiwa kumshusha na alikuwa kaweka mikono yake nyuma ya mgongo wa Eve na kumwambia aiachie miguu yake isiwe inagusa chini. Eve alifanya hivyo na alionekana kama anaelea. Tabasamu likaupamba uso wa Eve hasa alipojua ladha ya maji yale kwa kuyaoga bila kuzama. Uoga ukamtoka ghafla.

Na Hans naye ni kama alikuwa anamfundisha mtoto baiskeli,taratibu akaanza kumwachia Eve. Naye Eve alikuwa makini akiichezesha miguu yake. Hadi Hans anamaliza kuiachia mikono yake kutoka katika mwili wa Eve,Eve tayari alikuwa kishaweza kuogelea kifudifudi bila kuzama.

Watu walioona tendo lile hawakusita kupiga makofi kwa furaha. Makofi yale yalikuwa kama yanaenda kwa Hans kwa sababu wengi walioyapiga walikuwa wanawake.

Sasa wale matozi waliokuja na wasichana wao,mioyo yao sijui ilikuwaje. Lakini kwa Hans ilkuwa kama hatua moja kwenda mbele. Tatizo likabaki palepale,hawezi kumwambia kama anampenda Eve.

Hilo ni tatizo ambalo limesababishwa na wao wenyewe huko walipotoka. Hawakutaka kuwa na wanawake katika maisha yao,hivyo walikuwa ni waoga na wasiojua ni wapi pa kuanzia kusema nakuhitaji uwe nami katika dunia hii ya mapenzi.

Hans kama ilivyo kwa Junior na Fred,akabaki anaumia kwa maumivu hasa pale sifa za kuwa yeye ni mume mzuri wa Eve zilipokuwa zinatoka kwa watu waliokuwepo pale kwenye swimming pool.

“Hans umeniona?”.Eve alimtoa mawazoni Hans kwa swali hilo na kumfanya Hans apambe uso wake kwa tabasamu la kuchonga.

“Yeah.You did it Swetie”.Hans aliitikia huku akimfata Eve pale alipo na kumshika vizuri kiunoni na kumwomba waondoke kwa kisingizio muda umeenda.

Walitoka ndani ya maji na kuelekea zilipo nguo zao za mtaani. Walizivaa na kuchukua usafiri wa binafsi kuelekea yalipo makazi yao.

“Yuhuuuuu”.Hans alifungua mlango wa chumba anachokaa na kuingia huku akitereza kwa mguu mmoja na kutoa sauti hiyo.

Hakuta salamu bali aliingia kwa maneno ya kujigamba kama kawaida yao,.

“Basi mtoto nikamkamata namna hii kwenye kiuno chake laini kama manyoya ya kifaranga cha kuku. Nikamvutia kwangu taratibu,mtoto akavutika na hapo mdomo wangu ukawa unaelekea kwenye kinywa chake na kisha ndimi zetu zikatoka na kuingia kinywani kwa mwenzake. Wajua nini kilitokea?”. Hans aliongea huku akibakiza swali ambalo kila mtu alijua ni wapi alikuwa anaelekea kusema.

“Kwenda zako huko,unamdanganya nani kihivyo?”.Junior ndiye alianza kuongea huku Fred yeye akiwa bize na Biblia yake.

“Hujajibu swali mdogo wangu na tuachie kelele na domo lako linalonuka kama mavunja genge. Hata Swetie aliniambia kuwa unanuka mdomo,kwa hiyo chuna tu!”.Hans alimjibu na kumnyong’onyeza Junior.

“Sasa kama uongo asiseme bwana!! Acha uongo wako”.Fred naye aliingilia. Ni kama Hans alikuwa anamsubiri Fred aongee.

“Kwenda na acha kutuzingua wewe na Biblia yako. Kwanza unamtukana MUNGU kwa kujidai mtu wake wakati liongo balaa”..Hans alimwambia Fred.

“Mimi sijui kusema uongo,sema naendana na mazingira yenyewe. Kama mnajisifu na mimi nisijisifu?”.Fred alijitetea kabla ya Hans hajaendelea na lawama.

“Kwani nini aisee,mbona mnatuweka kwenye mafumbo?”.Suarez aliwauliza Hans na Fred.

“Si huyu anayejidai Baba Paroko sijui Mzee wa Upako. Alisema kamwandika mtoto kiunoni”.Hans aliongea na kukaa kimya na kusikiliza kama Suarez atakuwa anakumbuka maneno yale.

“Eee ndiyo.Jamaa alisema”.Suarez alionesha kumbukumbu zake.

“Basi mtoto hana alama yoyote kiunoni na huyu boya alisema ile alama yaweza kukaa mwezi bila kufutika. Jiongo kichizi,hiloooo”.Hans aliongea huku akimzomea Fred.

“Ha ha haaa. Embu usinikumbushe mwenzako. Hili jamaa mnadhani ni litoto humu? Hata kwa demu linaleta huu utoto.

Leo lilijidai li-Van Damme likajitupa ndani ya mimaji kama linguruwe. Ha ha haaaa”.Fred alijibu mapigo na kumwacha Hans akiwa kama amepata hasira.

“Kwa hiyo mwanangu tunafatana eeh. Si tuliagana hakuna kuingiliana katika ishu hizi? Mmeamua kunifatilia si ndio Wa Upako”.Hans alionesha wazi kaumia kwa kitendo kile.

“Hapa tumezidi kudanganyana ndio maana tumeamua kushuhudia kama hayo msemayo ni kweli. Ha ha haaaa,jamaa likajidai li-Chuck Norris. Eti iyaaaaaa,halafu pwaaaaah. Mimaji eneo lote kama gunia la mahindi limedondoshwa toka juu ya ndege na kutua kwenye bwawa,kumbe li-mtu,halafu jitu zima tu! Ha ha haaaa”.Junior naye aliongezea maneno na kumfanya Hans limshuke kama kapigwa na maji ya baridi.

“Sisi hatujakuingilia Hans. Ila na sisi tuliamua tuje kufurahi coco ndio tukakukuta na wewe. Tungekuingilia tungekuja hadi pale,lakini hatukuja bali kukuangalia jinsi ulivyojitupa ndani ya maji kama dubuwasha.Ha ha haaaa”.Fred aliongea na kuzidi kucheka.

4

“Halafu kuna videmu pembeni vikapiga,jamani huyu kaka vipi? Mbona kama kubwa jinga,ha ha haaaa?”.Junior alizidi kuongeza kumnyong’onyeza Hans na kuendelea kuleta vicheko vya haja mule ndani hata kwa Suarez ambaye alikuwa wala hayupo katika mkumbo huo.

“Halafu pale Eve alifyonza,ulimwona Junii.Hili jamaa si lilijitupa ndani maji halafu likazama,basi demu alijifuta maji na kufyonza. Ha ha haaaa”.Fred alizidisha utani.

“Halafu likaona limemfundisha mtoto kuogelea,kumbe mtoto anajua kuogelea toka zamani kinoma”.Junior alizidi kulembesha yale maongezi huku Hans akiwa haamini yale anayoyasikia.

“Umeona eeh. Mimi si wajua mzee wa mahotelini,siku moja wakati tupo pale Ken, akaniomba twende kuogolea. Mimi nikamwambia siwezi,akasema basi twende nikamuone yeye.

Acha bwana,mtoto anazamia yule,halafu kuna muda anaibuka na kujitupa kama yule Dolphin. Sasa jamaa leo likajidai limemfundisha,ha ha haaaa. Umebumba jamaa yangu”.Fred naye walishamfundisha maneno na ujanja wa mdomoni. Yale mambo ya upole hakuwa nayo kama mwanzo.

Wakati wote Suarez alikuwa anacheka bila kuchangia chochote,ni kama hakuwepo katika yale maongezi,lakini alishindwa asimame upande gani kwa sababu wale wote ni rafiki zake,na wale wote walimkaribisha mara ya kwanza,na yeye ndiye aliyewaleta kwa Eve. Akashindwa hata kutetea bali kubaki kucheka tu!.

“Embu ona hapa mwanangu.Lione hili jamaa”.Junior aliigeuza “laptop” ikaelekea kwa Suarez ambapo ndipo na Hans alikuwepo.

Akacheza ile picha ambayo alihitaji Suarez aione. Hapo alionekana Hans akikimbia kwa kasi ya hatari na kujitupa ndani ya maji.

Suarez alicheka sana kwa sababu ilikuwa ni tendo moja la kuchekesha mno kama ungepata kulishuhudia.

“Kwa hiyo wanangu mkanirekodi pia? Si ndio eeh. Poa bwana. Mmeshinda kwa leo,ila bado hamjashinda hata kidogo”.Hans aliongea kwa kusikitika huku akikaa kitandani kwake.

“Na ukileta uboya tu!.Tunaisambaza hii muvi chuo chote. Tunaandika LITAIRA likiwa na MREMBO,na facebook tunaiweka,na wale marafiki zetu wote wa watsapp,wataipata. Si wajua kilichotokea kwa WAGUMU? Basi kaa ukijua ile ni kazi yangu mimi”.Aliongea Junior kumchimba mkwara Hans ambaye alishapoa kitambo.

Maneno mengi yaliyowatoka wakina Junior yalikuwa hayana ukweli. Eve alikuwa hajui kuogelea kweli,na siku ile Hans ndiye alimfanya aweze kufanya zoezi lile japo si sana.

Ila waliongea yale kama kumtoa Hans mchezoni kwa makusudi kwani maneno yale yangemfanya Hans kuona kama alikuwa anakejeriwa na Eve.

Kimya kikatawala huku kila mmoja akiwa anafanya yake chumbani mule. Ni Fred ndiye aliyeanzisha maongezi tena na safari hii ni baada ya meseji kuingia kwenye simu yake.

“Daah! Kabadilisha siku,eti twende Jumatatu usiku. Hili jamaa litakuwa limemchosha sana. Ila poa,mi zangu za kijentromeni,si kama litaira kujitupa kwenye maji kama litembo”.Maneno hayo yalimfanya Hans amwangalie Fred kwa jicho la ubaya lakini alishindwa cha kufanya zaidi ya kumeza mate na kuongea maneno yaliyodhihirisha kuna kisasi mbele.

“We boya sasa hivi umekuwa mjanja eeh. Sasa ngoja,tutakutana pale katikati. Nitakuonesha mimi ndiye Hans The Crazy”.Aliongea Hans na kuweka earphone zake za simu na kuanza kusikiliza kilichomo mule.

Hakusikia majibu yaliyojibiwa na Fred bali aliona njia sahihi ni kutangaza vita rasmi kati yake na wale rafiki zake.

Uzuri wa Fred alikuwa ni mtu wa kumpeleka Eve maeneo tulivu hasa mida ya usiku. Mahotelini, migahawani,sehemu za maonesho,ndipo Fred alipendelea. Hali hiyo ilimfanya asijulikane wapi ataenda siku hiyo.

****

EVE NA ALFRED.

Ilikuwa ni Jumatatu ya saa mbili za usiku kama saa ya Fred ilivyoonesha pale alipoiangalia wakati yupo katika Hotel moja maarufu jijini Dar es Salaam. Alikuwa kakaa mahali fulani ambapo angeweza kumwona yeyote atakayeingia.

Hakukaa sehemu hiyo labda amwone Eve jinsi atakavyoingia bali alikaa hivyo ili aweze kuwaona na wabaya wake ambao ni Junior na Hans.

Alitangulia kufika kwa sababu alijua umuhimu wa mwanaume kutoka na mwanamke ambaye anamuhitaji. Siku zote aliamini mwanaume rijali ni lazima afike wa kwanza eneo pangwa kati yake na mwanamke anayetoka naye.

Elimu hiyo aliipata kutoka vitabu mbalimbali vinavyotoa sifa za mwanaume rijali au gentleman kama wenzetu wa ng’ambo wanavyolitamka kwa Kiingereza.

Baada ya kutulia kwa saa moja tangu afike pale,alimuona Eve akiingia na mpokezi wa wageni wa Hoteli ile kubwa,alionekana akiongea na Eve na hapo yule mpokezi akamuonesha mahala alipo Fred. Fred naye alipoona alikuwa anaangaliwa yeye,akanyoosha mkono kuonesha kuwa yeye yupo pale.

Kwa mwendo wa madaha uliopambwa na tabasamu la haja usoni pake,mwanadada yule mrembo ambaye alifanya hata wale waliokuwamo katika hoteli ile kugeuka na kumwangalia yeye,alimfata Fred pale alipokuwepo. Naye Fred kabla ya mtoto hajafika,tayari alikuwa kasimama na kwa ajili ya kumpokea.

“Oooh,Malaika wangu. Unaonekana mrembo usiku huu”.Fred aliongea huku akimshika mkono wa Eve na kuubusu.

Fred alicheza kama alivyoelezwa na katika vitabu vingi kuhusu mwanaume rijali. Jambo alilojifunza kutoka katika kusoma kwake huko,ni kutomkumbatia mwanamke ambaye si mwanamke wako bado,bali afanye zoezi dogo tu! La kumshika mkono na kuubusu. Na Fred alifanya hivyo.

“Inaonekana nimekuweka eeh”.Eve aliuliza huku bado katabasamu.

“Si sana na pia ni haki yangu kukaa nikikusubiri wewe Malaika uliyeletwa duniani kwa ajili ya kutangaza injili njema juu ya mioyo yetu”.Fred aliongea huku akijionya kuwa hata kama mwanamke kakuweka muda mrefu,kamwe usiseme umeniweka sana na wala usiseme ndio nafika sasa hivi,bali taja muda wa kati. Yaani ule kati ya umeniweka sana na nimekuja sasa hivi.

Eve akazidi kutabasamu baada ya maneno yale na kama kawaida Fred akazidi kuonesha urijali wake kwa kumvutia kiti kwa nyuma Eve,naye Eve akakaa huku tabasamu likizidi kutanuka kuliko lile la mwanzo alilokuja nalo.

Bila kuchoshana na kama mwanaume yeyote alivyotakiwa kufanya,mhudumu alikuja pale na kuweka vinywaji huku akigawa karatasi maalumu kwa ajili ya kujichagulia chakula. Si kama muhudumu alikosea kuleta vinywaji,bali taarifa hiyo Fred alikuwa tayari kampa mapema tu!.

Eve alishindwa kuvumilia hisia zake za furaha na kujikuta akiuliza swali na tabasamu kuu likiupamba uso wake.

“Ina maana unafanya haya yote kwa ajili yangu Fred?”.Aliuliza Eve baada ya kuona kile kinywaji ndicho anakipendelea na kilikuwa na gharama kubwa sana kwenye ile hoteli.

“Malaika wangu. Siku ya kwanza kukuona nilijiuliza sana kichwani kwangu”.Fred aliongea huku akishika kile kinywaji na kuanza kukifungua kwa vidole vyake.

Ni kimywaji ambacho kipo kwenye chupa ya shampeni,chenyewe kilikuwa hakina kilevi bali hupendwa sana na wanawake japo kilikuwa na gharama kubwa. Fred akawa anakifungua huku anaweka maneno yake.

“Nilijiuliza juu yako. Ni nani huyu atazamaye kama alfajiri,mzuri kama mwezi,safi kama jua wa kutisha kama wenye bendera. Huo ni uzuri wako Malaika wangu,unatisha kwa uzuri wako kama kile kikosi cha bendera viatani. Kile kikirudi nyuma,basi wanajeshi wote hurudi nyuma,kikienda mbele basi jeshi zima huenda mbele’”.Fred aliongea maneno ya kwenye biblia katika kitabu cha wimbo ulio bora.

Sidhani kama Eve alifahamu kwani alikuwa ni mwenye tabasamu juu ya sifa zile. Wakati yote hayo yanaendelea,tayari alikuwa akamaliza kufungua kinywaji kile na kukimimina katika gilasi ambayo ililetwa kwaajili ya Eve.Baada ya kumimina,akaendelea kutema neno.

“Embu jiangalie Malaika wangu. Hatua zako malidadi kama za twiga,mapaja yako a mviringo ni kama johari. Sifa ziende kwa kazi ya mikono ya MUNGU.

Nani atashindwa kuingia gharama juu yako Malaika wangu. Kama nilivyokwambia mwanzo,umeleta taarifa nzuri kuja kwangu,nami nilipozisikia moyo uliruka juu kwa furaha kama yule mama aliyemwona Bikira Maria wakati anamimba ya YESU.

Huu mzuri Malaika wangu,na hustahili kufanyiwa chini ya haya. Kunywa kinywaji ukipendacho na chagua chakula ukionacho wewe waweza kukila na kufurahia huu mtoko wetu”.Fred alimaliza kuongea na kumkaribisha Eve ambaye alishindwa hata kusema neno juu ya maneno yale matamu kwenda kwake.

Akachukua gilasi ile yenye kinywaji na kuitia midomoni mwake na kumimina kiasi kidogo ambacho aliona kitapita vizuri kooni mwake bila kuleta kashi. Wakati huo Fred alikuwa bize akichagua chakula atakachokula.

Hakupenda kumwangalia Eve wakati anakunywa kwa sababu ya imani yake ya kuwa mwanaume rijali,huwa amchunguzi mwanamke anayemtoa out bali humpa uhuru wa kufanya chochote.

“Fred. Wewe unasoma sana vitabu vya dini,si ndio eeh”.Aliuliza Eve swali lililofanya Fred na kisha akajibu kwa kukubali kwa kichwa.

“Sasa kama ni hivyo basi na mimi nataka kukuuliza huko huko”.Aliongea Eve.

“Uliza tu Malaika wangu”.Fred alimpa nafasi Eve.

“Unaamini kuwa kuna mwisho wa dunia? Au unaamini kuwa kuna siku wote tutakufa na kufufuka tena na baadaye kukawa hakuna kifo,kama vitabu vya dini vinavyosema?”.Eve aliuliza swali ambalo kama mfuatiliaji dini huwezi kusema haamini hilo,lakini lilikuwa ni swali la kupima ulijari wa Fred.

Wanaume wengi wangejibu labda kwa kuuliza,hilo nalo swali. Lakini Fred alikuwa mtulivu na kusoma mawazo ya mwadada yule na alipopata akili yake inawaza nini,alifungua kinywa chake na kujibu.

“Naamini hilo Malaika wangu. Naamini ipo siku tutafufuka na kuonana tena. Na nitamshukuru sana MUNGU kama ataniweka na wewe pale tutakapopata ufufuko.

U mwenye bashasha na busara ambazo ni MUNGU pekee ndiye anayejua kwa nini kakupatia. Zawadi yoyote utaipata kama ukimuomba mwanaume. Hata ukisema uletewe kichwa cha Yohane Mbatizaji,utaletewa kutokana na umuhimu wako katika macho ya kila akuonaye.

Sidhani kama una moyo mgumu wa kutoelewa haya uyasikiayo. Ila najua una moyo laini kama sufi ya kondoo wa bwana. Hakuna atakayekataa kufungwa na nila yako,kwani nila yako ni laini na kila mmoja hawezi kukataa kufungwa nayo.

U Malaika uwezaye kuwa mzabibu nasi tukawa matawi yako.Kwa jinsi navyokuangalia machoni kwako,sidhani kama nitakosea kusema kama nikisema unaweza kuingia ndani ya moyo ya mtu na kuvuta kiti cha moyo huo,nawe ukakaa daima ndani yake.

Namaanisha mwanaume yeyote anaweza kukukabidhi moyo wake,akakupenda, akakuthamini na akakupa kila kitu kinachoitwa mapenzi. Niamini Malaika wangu”.Fred aliongea kiasi kwamba hata yule aliyekuja kuchukua menu ya chakula walichoagiza alikuwa katanua mdomo huku aamini yale aliyokuwa anayasikia.

“Vipi kaka,mbona umeganda?”.Fred alimuuliza yule jamaa mhudumu.

“Nimekuja kuchukua menu ya chakula kaka”.Alijibu.

“Poa.Hizi hapa”.Fred alizikusanya menu zote mbili na kumpatia.

Wakati anaondoka baada ya kupewa orodha ile ya chakula ambacho Fred na Eve waliweka tiki kwenye chakula wanachotaka,yule mhudumu aligeuka nyuma na kwa bahati nzuri alikutana na macho ya Fred.

Mhudumu alimwonesha dole gumba ambalo lilipokelewa kwa tabasamu dogo kutoka kwa Fred,na kisha mhudumu alititia ndani kwa ajili ya kuandaa huduma aliyoombwa.

“Yaani wewe unaongea kuliko hata unavyoonekana. Una maneno ambayo yanaweza kumfanya mtu ajiulize mara mia ni wapi umeyapata. Mh! Eti naweza kuwa mzabibu nanyi mkawa matawi,kwani mimi Yesu?Ha ha haaa”.Eve aliongea na kucheka kitu ambacho Fred alikipenda sana hasa baada ya kumuona mwanamke aliyembele yake anacheka kwa sababu yake.

“Wanasema ukicheka unaongeza siku za kuishi. Lakini naamini yule anayekufanya ucheke,anaongeza siku za kuishi mara mia zaidi yako.

Malaika wangu,usiku huu umeniongezea siku za kuishi katika maisha haya. Huu wa muhimu kwangu kuliko unavyodhani. Nimekufanya uongeze siku,nawe umeniongezea siku zaidi kuliko zile nilizokupa wewe. Nani kama wewe Malaika wangu,endelea kucheka nione meno yako meupe na ya kung’aa kama vazi la Malaika aliyemtokea Bikira Maria.

Endelea kucheka Malaika wangu”.Fred aliongea na kumfanya Eve atikise kicha kushoto na kulia kama anasikitika lakini alikuwa amejawa na tabasamu lililoonesha dhahiri alikuwa haamini anachosikia,au kafurahishwa na yale maneno.

“Yaani wewe. Dah! Basi bwana”.Aliongea Eve na kushindwa kumalizia kauli yake. Wakati huo mhudumu alionekana akija na sinia kubwa lililosheheni chakula walichoagiza.

Mhudumu alifika mahala pale na kisha akaweka chakula mezani.Zoezi lililofata baada ya hapo ni kuwanawisha wageni wale wenye maneno mengi ya kuvutia. Alipomaliza,aliwakaribisha naye akapotea eneo lile akiwaacha wale wawili wakijihudumia vyakula walivyoagiza.

“Unapenda kuku eee”.Fred alimuuliza Eve baada ya kuona Eve anajiwekea kuku kwenye sahani yake.

“Sana. Ni nyama moja baridi isiyo na madhara makubwa kama zilivyonyama za wanyama wengine”Alijibu Eve huku akifunua sahani fulani ambayo ndani yake ilisheheni tambi.

“Na wewe unapenda ugali kwa samaki ee”.Naye Eve alimtupia swali kwa Fred.

“Hiyo ndio sababu ya mimi kuwa imara zaidi ya chuma. Ila wewe yakupasa kula vitu kama hivyo ili ujengeke mwili na kuwa laini. Huu ugali tuachie sisi wafanya kazi ngumu”.Alijibu Fred huku anamega tonge la kwanza la ugali.

“Kwani sisi hatutakiwi kuwa imara?”.Eve alitupa swali lingine lililofanya Fred asile kwanza bali kujibu swali lile.

“Kwa mwanamke kama wewe,hupaswi kuwa imara sana kimwili bali kiakili.Nasema hayo kwa kuwa yule utakayekuwa naye,tayari atakuwa imara kwa ajili yako. Atafanya chochote kwa ajili yako,na hatokuwa tayari kukupoteza. Ni lazima awe imara na ni lazima ale ugali kwa wingi,kama mimi”.Fred aliongea na kunyanyua mkono wake wenye tonge na kuanza kula.

Eve naye alifanya vivyo hivyo lakini yeye alitumia uma na kisu ambacho hakina makali kwa ajili ya kukatia nyama ile ya kuku.

****

Walipomaliza kula,walikaa kidogo na Fred alilipia gharama za vyote vilivyotumika pale. Kilichofuata ni wao kuanza kurudi yalipo makazi yao.

“F mi nataka tutembee kwa miguu hadi chuo”.Aliongea Eve huku akisogea pembeni ya Eve na kuingiza mkono wake katikati ya ubavu na mkono wa Fred,yaani chini ya kwapa la Fred na kisha akabana mkono wake katika mkono wa Fred huku akiongeza deko la maneno yake kwa kulalia bega la kijana yule aliyekuwa kavalia suti ya kijivu iliyomkaa vizuri kama mwanamichezo wa nchi za nje anaenda kuchukua tunzo.

“Usiku huu Malaika wangu.Huogopi?”.Fred alimuuliza Eve wakati huo walishatoka nje ya hoteli ile nzuri ya nyota kuanzia tatu.

“Hivyo hivyo. Nikichoka kutembea ndio nitapanda gari”.Aliongea Eve kwa deko zaidi lililomwacha Fred bila neno bali kumsisimua na kumjaza kichwa.

“Sawa Malaika wangu. Mimi sitaki kukuhudhi. Twende sasa”.Fred alijibu na safari ya kwenda kwao ilianza.

Baada ya mwendo mfupi kidogo huku wakiwa wanapiga soga taratibu. Fred alianzisha tena maongezi yake matamu.

“Malaika wangu. Hivi unaamini kuwa mtu akifa roho yake inabaki kukulinda wewe?Namaanisha kama unandugu au yeyote anayekujali,akifa anakuachia ulinzi hapa duniani,unaamini?”.Fred alimuuliza Eve.

“Mh! Hiyo hapana kwa kweli F”.Eve alijibu na kuendelea kujikunyata kwa Fred ambapo kulimfanya Fred atoe koti lake la suti na kumfunika Eve aliyeonekana anahitaji joto japo mavazi aliyoyavaa yalikuwa hayapitishi baridi sana. Ila kwa kuwa Fred alikuwa anaigiza urijali,ilibidi kuwa hivyo.

“Asante F.Lakini kwani wewe unaamini?”.Alishukuru kwa lile koti,kisha akarudi katika mada.

“Ndio naamini. Embu angalia angani”.Eve akatazama angani wakati huo bado wanatembea njia ambayo ilikuwa na watu kiasi.

“Unaona nini?”.Fred aliuliza.

“Naona nyota na mwezi”.Eve akajibu.

“Wazungu wanasema nyota ni macho ya wale wakupendao,waliokujali wakiwa duniani na wanaopenda kukuona unafanikiwa. Macho haya yanakuangalia vizuri sana. Yaweza kuwa ya mabibi na mababu wa zamani sana. Bado wanataka kukuona ukifanikiwa. Na ndio maana kukiwa hakuna nyota,ni rahisi sana mambo mabaya kukupata”.Fred alijibu lakini hakuishia hapo.

“Hata mimi nikifa,nitakuwa nyota. Nitakulinda kwa kila ovu,nitamsimamisha kila ambaye atataka kukudhuru. Hiyo ni kwa sababu nakujali sana Malaika wangu. Kama ukiniambia nife kwa ajili hiyo,nitakufa ili nikulinde”. Fred alizidi kutiririka maneno ambayo kwa mtu wa kawaida mwanzoni anaweza asiyaamini,ila kwa jinsi yanavyoenda,anakuwa hana budi kuyaamini kwani ni maneno matamu ya kuweza kumfanya yeyote ayasikiaye,kujiona yupo juu kuliko mwanamke mwingine dunia hii.

“Sina usemi hadi hapo”.Eve alikubaliana na maneno yale.

“Tupande basi gari,mi mwenzako nasikia baridi”.Fred alitoa ombi ambalo lilipita bila pingamizi.

Wakaita usafiri binafsi ambao ni tax. Safari ya kwenda yalipo makazi yao,ikachukua nafasi.

*****

Baada ya nusu saa,tayari Eve alifika yalipo makazi yake. Fred alimuomba dereva amsubiri kidogo ili amsindikize mwanadada yule hadi getini.

Kama kawaida ya Eve,ili asipoteze urafiki na wale watu,alimpatia Fred busu moja dogo katika midomo yake na kumfanya Fred atabasamu kwa furaha huku akijiona kama anaelekea kushinda ligi ile.

“Kesho kutwa nitataka nitoke na wewe tena. Naomba hilo F”.Eve aliongea huku akimwangalia Fred machoni.

Unadhani Fred angekataa?Alijibu haraka kwa kukubali,na hapo Eve alimpatia koti lake na kufungua geti la makazi yake,kisha akaingia humo na kufunga geti lile na kumuacha Fred akiwa anatabasamu mwanana. Alishangilia kidogo na kugeuka na kuanza kulielekea gari lililowaleta hadi pale.

******

Dakika nyingine kumi na tano,Fred alikuwa kishafika anapoishi na kama kawaida aliingia kwa fujo huku akitabasamu,lakini yeye hakuwa muongeaji sana kama wakina Junior.

“Vipi kaka?Mbona hautupi matokea huko?”.Suarez Emmanuel alimuuliza Fred baada ya kuona haongei chochote kama wale wenzake.

“Gentleman huwa haadithii mambo yake”.Fred alijibu kwa kifupi huku anavua viatu vyake karibu na kabati lenye nguo zake.

“Utakuja kuongea tu,boya wewe.Ngoja uone”.Hans aliongea kwa sauti ya chini na iliyojaa kithirani. Halafu akageuka upande mwingine wa kitanda na kuendelea kusoma kitabu alichokuwa anakisoma.

Ni kama Fred hakuisikia sauti ya Hans,lakini aliisikia sema akaipuuzia kwa kuwa alijua ni utani tu.

“Subiri muone boya litakachokifanya keshokutwa,ha haa”.Fred alijibu mnong’ono wa Hans huku akipanda juu ya kitanda chake wakati huo Junior yeye alikuwa kapitiwa na usingizi muda mrefu.

Asubuhi,marafiki wale walienda darasani lakini Hans alibaki chumbani huku akisingizia anaumwa kidogo,hivyo hawezi kwenda kuhudhuria masomo ya siku ile.

Walipoondoka,Hans alitoa makorokoro yake baadhi na kuanza kuyachanganya. Alitumia saa moja kuchanganya na kujaribu kazi yake aone kama inafanya kazi.

Baada ya kuona mafanikio,alitabasamu kwa mbwembwe na kuitengenisha michanganyo ile ambayo ilikuwa ni unga mweusi na maji fulani ya njano.

Unga aliuweka kwenye kifuko kidogo cha nailoni na yale maji kiasi alifanya hivyo hivyo. Maji na unga ule vikiwa vimetenganishwa,havina madhara ila vikichanganywa pamoja,ndipo vinaweza kusababisha madhara. Hans alivitenganisha na kuvificha katika kabati lake akisubiri siku ya kuvitumia.

****

Baada ya masomo ya siku nzima. Hatimaye marafiki wale watatu walirudi chumbani kwao na walimkuta Hans akiwa amelala fo fo fo jambo lililofanya aonekane kweli jamaa ni mgonjwa.

Hakuna aliyemsumbua bali kila mmoja alianza kufanya yake huku kichwa cha Fred kikiwa kinawaza zaidi siku ya kesho yake ambapo alitakiwa kwenda kukutana na Eve.

Masaa yakaenda na kupotea,hatimaye ikafika usiku ambapo wote kwa pamoja walitoka kuelekea sehemu wanapouza chakula. Wote walionekana wana furaha,hata Hans aliyekuwa mgonjwa,alikuwa karudi katika hali yake kiasi.

Baada ya kula na kufurahi kwa pamoja,walirudi chumbani kwao huku bado furaha ikiwatawala. Hakuna aliyejua mipango ya mwenzie,ila kila mmoja alikuwa anacheka huku akipanga yake moyoni.

Usiku ukahitimishwa kwa marafiki wale kulala huku kila mmoja akiwa anaota mambo yatakayokwenda kutokea kesho yake,hasa Hans na Fred.

****

Asubuhi ya kesho yake kila mmoja aliamka mwenye tabasamu katika uso wake,matabasamu ambayo yalikuwa yanaonesha walikuwa hawana matata katika siku ile na walikuwa wazima wa afya.

Kila mmoja alianza shughuli zake ndogondogo kabla hawajaenda kujisomea na baadaye kwenda kujipatia kifungua kinywa kabla hawajaingia vipindi vya mchana ambavyo vingewapeleka hadi mida fulani ya chakula cha mchana. Hiyo ndio ilikuwa ni ratiba yao ya kila siku na waliifata vyema.

Baada ya masomo ya siku nzima,ndipo walirudi wanapoishi huku Fred akiwa anamzuka wa kufa mtu na kuona muda kama hauendi,alikuwa anabwabwaja maneno mengi kama simu la mtoto mdogo lile ambalo ukibofya namba moja linaanza kulia hivi,ukibofya namba mbili linalia vile na ukiofya namba tatu na nyingine nyingi,hulia linavyojua lenyewe.

Isikupite Hii: Pumbazo – Ep 4

Basi Fred alikuwa hivyo ,kila hadithi alitaka kuwemo hadi wenzake wakawa wanakereka.

“Baba Paroko niaje?Mbona umechangamka kama kachumbari iliyomwagiwa pilipili na ndimu halafu inaliwa na mlevi?.”Aliuliza Suarez.

“Aaah!Sitaki kujichafua kwa kununa kwani leo washika mapembe wanaisoma namba.”Fred aliongea kwa nyodo na kumaliza na cheko moja ya kejeri na majigambo kiasi chake.

“Hapo ndipo ulipokosea. Leo lazima cheko igeuke kilio.”Aliongea Hans kwa sauti ya chini lakini iliyomfikia vema Fred.

“Ha ha haaaa,anadhani na mimi nitakuwa likifaru kujitupa kwenye mimaji hadi iruke ruke pembeni. I am Gentleman”.Aliongea Fred na kuzunguka kidogo kama anacheza muziki.

Wakati hayo yote yanaendelea,walikuwa katika barabara wakorudi maskani waishipo.

“Ha ha haaa,eti likifaru. Jitu likajirusha pwaa. Duuh! Ile sehemu ikawa kama imetupwa bomu la nyukilia.Majitu mingine bwana.”Hapo Junior naye aliongea kumchokoza Hans.

“Leo mtaona historia nyingne tu!. Si watu wanajidai wamejanjaruka wakati tumewajanjarua sisi hadi leo wanavalia suruali chini ya mkanda na wakati walikuja hapa,suruali wanafungia mkanda shingoni. Kudadeki zao.”Aliongea Hans kumpiga dongo Fred.

“Ha ha haaa.Acheni kunichekesha bwana. Suruali inafungiwa shingoni,imekuwa tai hiyo?.”Suarez alisaili kinafki.

“It doesn’t matter. Nachojua nimewapiga gepu wewe na zee la kunuka domo.”Fred alijibu mapigo ya Hans na kuendelea kucheza barabarani kwa furaha.

Walindelea kurumbana hadi wakafika wanapoishi ambapo kila mmoja alijitupa kitandani kwanza ili atoe mchoko kabla ya kuikaribisha jioni.

****

Saa kumi na mbili jioni,Fred alikuwa anajiweka tayari kwa ajili ya kwenda kukutana na kimwana Eve. Mtoto ambaye kabarikiwa kila sifa ya urembo wa sura hadi tabia bila kusahau uzuri wa umbo na miondoko ya madaha. Nani ambaye angesipodata mbele ya kimwana yule matata.

Akiwa tayari kishajiwekea mavazi yake mahala pasafi na salama baada ya kuyanyoosha,Fred alitoka nje kwa ajili ya kwenda kuoga,na wakati huo aliwaacha Junior,Suarez na Hans wakiwa bize na vitabu vyao pale kitandani.

Baada ya dakika tatu za Fred kutoka nje,Hans alinyanyuka toka kitandani kwake na kwenda katika kabati lake. Hakuna aliyejua nini kinaendelea na hakuna aliyemfatilia kwa sababu walijua kaenda kwa nia binafsi.

Alifungua kabati lake na kuchukua vile vifuko viwili vya plastiki,halafu akageuka nyuma kuangalia kama Sua na Junior wanaenda na kipindi.Alipoona wapo bize na mambo yao,akaenda kwenye suruali ya Fred aliyopanga kuvaa siku ile.

Alichofanya ni kuweka vile vinailoni viwili kwenye mfuko wa nyuma wa suruali ile ya Fred.Vinailoni vile ambavyo kimoja kilikuwa na unga na kingine majimaji,ndivyo viliaribu kabisa mtoko wa Fred.

Baada ya kuhakikisha kafanikiwa kufanya zoezi lake bila kushtukiwa,Hans alirudi kitandani kwake na kuendelea kujisomea kitabu alichokuwa kakianza.

Nusu saa baadae,aliingia Fred kwa furaha huku tauro likiwa kiunoni, na shati alilotoka nalo likiwa begani na wakati huo huo mdomo wake ulikuwa unatoa mluzi wa wimbo wa Happy ulioimbwa na Pharrell Williums. Na uzuri alikuwa anaweza kucheza,hilo nalo likawa kivutio kwa rafiki zake.

Lakini ilikuwa kivutio zaidi pale alipokuwa anaendelea kucheza na mara akalitoa tauro kiunoni na kubaki na boxer moja ndogondogo iliyombana vizuri sana.

Basi kwa mbwembwe nyingi akaanza kucheza huku anaimba kiwimbo chake ambacho kilimkaa sana kichwani,tangu asubuhi.

Hata yule aliyekuwa anakisasi naye ilimbidi acheke tu! Maana jamaa alivyokuwa anayarudi na kile kiboxer,waweza sema LMFAO.

Huku anaendelea kutoa burudani ya kucheza,Fred alianza kujipaka manukato mbalimbali katika mwili wake kwa ajili ya siku ile ya faraja kwake.

Baada ya kumaliza hayo,alichukua singlend nyeupe na shati la kijani ya apple alilokuwa kalitundika kwenye kabati lake,akavaa. Alipomaliza,akatinduwa suruali yake ya kijivu,na bila kuichunguza akatinga mwilini mwake na kuichomekea vizuri mwilini.

Akachukua kioo kidogo na kuanza kutana nywele zake kabla hajachukua koti lake la kijivu ambalo alilivaa na kukamilisha suti iliyokuwa imemtoa chicha balaa. Kwa jinsi ilivyokuwa imemkaa,waweza sema huyu kocha tena Morinho au Gadiola.Au msanii mkubwa wa Marekani kama Justin Timberlake au labda Christian Ronaldo akienda kuchukua tunzo ya mchezaji bora wa dunia.Hakika jamaa alipendeza,uongo dhambi.

“Kaka leo umevunja kabati halafu ufunguo umeumeza.”Aliongea Suarez kumsifia Fred.

“Kawaida yangu,unadhani mimi wa makaptula kama tembo mtoto?.”Alijibu Fred huku akitupa dongo dogo kwenda kwa Hans.

“Na leo lazima mtu aje analia hapa.”Aliongea Hans na kugeukia upande mwingine wa kitanda chake.

“Halii mtu. Subirini kuletewa wifi yenu humu.”Fred aliendelea kuleta nyodo zake.

“Basi kaka we nenda kwa maana umeshaanza shombo zako hapa.”Aliongea Junior baada ya maneno kuntu kutoka kwa Fred.

“Naweza nisiondoke na usinifanye kitu.Ila kwa kuwa natakiwa kuondoka ngoja kwa sasa niwaache. But,siwaachi hivihivi.”Fred akatoa simu yake kwenye kipochi kilichokuwa kitandani kwake na kubofya namba kadhaa.

“Nambie Malaika wangu.Furaha ya macho yangu,utamu wa akili yangu na neno takatifu la ulimi wangu.”Fred alibwabwaja baada ya simu kupokelewa.

“Mi mzima Malaika wangu.Upo wapi sasa hivi.”Alisaili Fred baada ya salamu yake kuitikiwa.

“Okey,basi nakuja sasa hivi na teksi kuja kukuchukua,si tayari ushajiandaa ee.”Fred akaendelea.

“Aaah,Malaika wangu,wewe ndiye uwezaye kumfukuza hata shetani mbaya wa kichwa changu. Kwa nini hujali thamani nayokupa ya kutembelea taksi bali kutaka kutembea kwa miguu?.”Aliposema maneno hayo ni kama alimwamsha Hans usingizini kwani alijikuta akitabasamu kwa shangwe.

“Sawa Malaika wangu,najua unataka ufurahie uwepo wangu. Basi tutatembea.”Fred alijibu simu upande wa pili na kukaa kimya kidogo kabla hajamaliza maongezi yake.

“Sawa Malaika wangu.Nitakuja hapo baada ya nusu saa.”Fred akakata simu.

“Sasa nyie wazee wa mapembe,baadae tutaonana. Mi naanza kwenda taratibu,sitaki papara. Natembea kwa miguu hadi kwake na kisha nampeleka mtoto hotel za maana kama kawaida yangu.”Alijisifu Fred na kutoka nje huku Suarez na Junior wakimtakia safari yenye mafanikio.

“Hata usiponi-wish me lucky,lazima nitafanikiwa tu. Tembo mtoto wee.”Alirudisha kichwa chake kwa kuchungulia,ndipo aliongea maneno hayo akayaelekeza kwa Hans.

“Mi sina tatizo na wewe,utarudi tu hapa. Tutaona nani mshindi.”Alijibu Hans kwa sauti ya ujasiri na tulivu.

“Tcio bebee.Subiri wifi yako anakuja.”Aliongea Fred na kufunga mlango wa chumba kile,ikiwa tayari ni saa moja na dakika kadhaa.

*****

Fred mida ya saa moja na dakika zake arobaini na tano,alikuwa nje ya geti la makazi anayoishi Eve Johaness,mwanamke aliyekonga nyoyo za wanachuo karibu wote pale Dar es Salaam.

Ni kweli alitembea kwa miguu ili tu,asiwahi kufika na kumkuta Eve bado hajajiandaa kwani waliahidiana wakutane saa mbili za usiku ule.

Baada ya kufika,alimpa taarifa mrembo wake wa muda kwa kutumia simu yake kuwa tayari yupo nje anamsubiri. Nasema ni mrembo wa muda kwa kuwa Eve alikuwa kama kiti cha basi,leo kakaliwa na huyu,kesho kakaliwa na mwingine.Kwa hiyo huwezi kumuita huyo ni mpenzi wako wa kudumu na mbaya zaidi watu wenyewe walikuwa hata saundi hawajazitema.

“Nimekuweka sana wangu wa ukweli”.Aliongea Eve baada ya kutoka nje na kumkuta Fred akiwa kaegamia mti mmojawapo pale nje.

“Hata YESU alisema atarudi,lakini hadi sasa bado tunamsubiri.Sembuse wewe binadamu mwenzangu uliyeniahidi baada ya dakika kadhaa utakuwa nami? Siwezi kukata tamaa kusubiri kwani kufanya hivyo itabidi kwanza nikate tamaa kumsubiri YESU ndipo nikate tamaa kwako.

Swali lako nalijibu kuwa,hujaniweka hata kidogo. Ni halali yangu kukusubiri hata hadi asubuhi kwani wewe ndiye Malaika wangu. Ulindae moyo wangu na hata kichwa changu chenye wingi wa hamu ya kukuona na kukujulia hali.”Aliongea Fred kiufasaha na kumuacha Eve akiwa katika tabasamu mwanana lililokuwa linazidi kumbanjua Fred mabandu ya magome yaliyo-moyoni mwake na kuuacha moyo huo kuwa mweupe na wenye upendo ulikothiri furaha na amani.

Wakati huo alishamsubiri Eve kwa dakika kama kumi na tano. Na kweli aliwekwa sana tu! Ila kwa kuwa ni mrembo,atafanya nini sasa. Ila angekuwa dume mwenzake,sijui kama angekubali kuwekwa vile.

“Mmmh! Mimi nilidhani nimekuweka bwana maana umekuja mapema na halafu nilikuwa bado hata sijaoga wala kuchagua cha kuvaa,si waona mavazi yangu ya leo?.”Eve alijitetea huku anajiangalia.

“Hayo mavazi ni zaidi ya wewe unavyodhani. Umetoka sana Malaika wangu. Ungekuwa nchi za wenzetu,ungepita kwenye RED KAPETI,ila huku kibongo bongo,utamezewa mate na marijali kuonesha kuwa umependeza.”Fred alimpa sifa dada yule na kumuacha hana neno bali meno yaliyopangana kiustadi mdomoni mwake kutokeza na kumfanya Fred amsifu MAULANA kimoyomoyo kwa kumuumba kiumbe yule ghafi katika peo za macho yake.

Eve japo alikuwa kajikataa kuwa mavazi aliyovaa hayakuwa rasmi,ila kiukweli alikuwa katoka vibaya mun

Gauni lake la refu la silva na lenye ming’aro kadhaa kwenye mikanda iliyopita mabegani pamoja na mmoja mpana kiunoni pake,ulimfanya Eve ang’ae sana usiku ule wa haja kwa watu wale wawili.

Huku chini ali-match na viatu vya rangi ileile ya silva na juu nywele zake alizibana na banio la damu ya mzee,rangi ambayo ilikuwa inaendana na kikoti kidogo alichokiegesha mwilini mwake kabla hajakivaa kabisa pale alipofika kwa Fred.

"Mmmh!Haya bwana,sina cha kusema juu ya hilo."Eve alikata kinywa cha Fred kwa kukubaliana na maneno yake.

"Sasa nadhani twaweza kwenda Malaika wangu."Fred aliongea huku akiingiza mkono wa kulia kwenye mkono wa kushoto wa Eve kama wafanyavyo maharusi au waalikwa wawili wa jinsia tofauti wanapoingia kwenye tafrija mojawapo kubwa waliyoitwa.

Ilikuwa ni tayari saa mbili na dakika kadhaa za usiku na ilionesha wazi Eve alikuwa si wa kupanda gari hata pale Fred alipomba wafanye hivyo. Haikujulikana kwa nini,ila Eve alisema anajiona yupo vizuri kifuraha kama watatembea kwa miguu hadi huko wanapoenda.

Dakika thelathini za mwendo wao wa taratibu na wa madaha,tayari walikuwa wameshafika eneo moja la wazi lakini lenye mgahawa mkubwa ambao siku kama ile,kulikuwa kuna watu wengi sana hadi wengine wanakosa sehemu za kukaa.

Kwa kuwa wakina Eve walichelewa kiasi chake,walikuta nafasi nyingine zipo wazi kwa wale wa mwanzo kuondoka.

Walichagua nafasi moja nzuri na yenye mwanga ili waonekane hasa kwa mavazi waliyovaa usiku ule. Yalihitaji sana mwanga ili yavutie zaidi. Lakini kama Fred angelijua kitachomtokea,sidhani kama angechagua kwenda kwenye mgahawa mkubwa kama ule,na kuchagua sehemu yenye mwanga kama pale.

Lakini yote yalibaki kuwa kama ningeli……,basi ningeli….. Yalibaki kuwa majuto tu!

****

"Unapaonaje hapa Malaika wangu."Fred alianzisha maongezi baada ya kukaa mahala panapostahili na kumsubiri mhudumu kwa ajili ya kuagiza wanachohitaji.

"Oooh Fred,it is fantastic."Alijibu Eve huku akiutazama mgahawa ule juu na pembeni kama unauthaminisha.

"Mmh Malaika wangu.Mi mwenyewe najua Kiingereza lakini sipendi sana kukitumia nikiwa na wewe. Napenda tutumie Kiswahili zaidi,kwani tunakuwa huru kuelewana kuliko kutumia vingereza ambavyo havina maana sana katika maongezi yetu."Alisahihisha Fred baada ya Eve kutumia lugha ya Kiingereza katika maongezi yao.

Ni kweli Fred hakuwahi kutumia lugha nyingine akiwa na Eve,hiyo pia inakuweka vizuri katika mahusiano yako. Si njema sana kuchanganya lugha pale unapokuwa na msichana ambaye unahitaji uwe naye katika mahusiano.

Hali ya kuchanganya lugha uwapo na msichana au mwanamke,inatengeneza maono tofauti katika kichwa cha mtu uliyenaye kwa wakati huo. Na zaidi utaonekana kama unadharau sana hasa pale mtu uliyenaye kumbe shule ilimpiga ngumi katika maisha yake na hajawahi kusomea lugha unayoitumia.

Kingine utatengeneza ile kauli ya kujifanya unajua sana lugha fulani kuliko lugha ya ulimi wa mama yako. Hisia kama hizo si nzuri kama zikitengenezwa kwenye kichwa cha mwanamke uanayemtaka.

"Mh!Hapo kweli,umeniambia jambo la maana.Mimi kama mwanafunzi wa uandishi wa habari wa nchi hii,sipaswi kutumia lugha kwa kuchanganya changanya hasa pale napoulizwa swali kwa lugha fulani na mimi najibu kwa lugha tofauti niliyoulizwa nayo. Hapo sibishi Fred wangu."Aliongea Eve huku akiwa anatabasamu lisiloishiwa unyevunyevu unaosababisha kutokauka kwa tabasamu lile.

“Nashukuru Malaika wangu kwa kuelewa hilo.”Alishukuru Fred na wakati huo muhudumu nadhifu wa mgahawa ule alikuwa kaja na kuwapa menu ya chakula wafanye yao.

Baada ya dakika kadhaa,tayari chakula walichokuwa wameagiza kilishakuja mezani kwao.Kitendo bila kupoteza muda,Fred alijivuta kwa mbele ya kiti alichokalia huku kitendo kile kikiwa kama ndio kinamalizia ule mpasuko wa vile vinailoni viwili alivyokuwa kawaviweka Hans mfukoni mwa suruali ya Fred.

Kile kinailoni cha kwanza chenye maji,tayari kilishapasuka muda mchache baada ya Fred kujivuta vuta kwenye kiti chake.Na ule ubaridi wa kimiminika kile Fred aliuhisi sema aliona aibu kuinuka kwa kuwa angeonekana kama kajisaidia haja ndogo.

Sasa wakati anajivuta kwa ajili ya chakula,ndipo kile kinailoni chenye unga nacho kilipopasuka na kusababisha sasa ule unga kuchaganyika na kile kimiminika ambacho kilikuwa bado hakijakauka kabisa kwenye suruali ya Fred. Hapo ndipo balaa lilianzia.

Wakati Fred anaendelea kujilia chakula alichoagiza,mara alianza kuhisi umoto moto kwenye makalio yake. Mara ya kwanza alidhani labda ni kiti au kuna moto karibu yake,lakini alipoangalia kulikuwa hamna hali hiyo na wala kiti alichokalia kilikuwa hakina uwezo wa kupitisha joto alilolihisi.

Alitaka kusimama ili ajikague lakini aliona aibu kutokana na ule umajimaji uliokuwa katika suruali yake.Ikabidi avumilie lakini uvumilivu ule ulikuwa kama unazidi kuchochea hali ya joto kuongezeka pale alipokalia.

Taratibu Fred alianza kuona chakula kichungu na kiti kikawa kama kina upupu kwa jinsi alivyokuwa anasota kwa kwenda mbele huku makalio yake yakiwa msaada mkubwa wa kufanya hayo yote. Lakini kama angejua,angesipoendelea kufanya vile,kwani joto lilizidi maradufu ya pale mwanzo.

Masikini Baba Paroko au Mzee wa Upako,uso ukambadilika ukawa kama kasikia habari mbaya eidha ya msiba au mlipuko wa mabomu kama yale ya Mbagala.

“Vipi Fred wangu,mbona amani hamna?.”Aliuliza Eve baada ya kuona uso wa Fred umekosa amani.

“Hamna Malaika wangu,sema najihisi vibaya kidogo.”Fred aliongea huku akilazimisha tabasamu lakini hali ya makalio yake,alikuwa anaijua yeye.

“Tumbo linauma?.”Eve aliendelea kuuliza maswali kutokana na muonekano aliokuwa nao Fred. Hakika alipaswa kuuliza swali la namna ile kwa maana uso ulikuwa unakunjwa na kukunjuka kama anajisaidia kweli uwani.

“Daah! Eve nakufa.”Fred aliongea kwa sauti ya chini lakini iliyojaa uchungu mkubwa wakati anaitoa.

Mwanamke wa shoka,Eve alijua mambo yameharibika kweli,hadi kaitwa jina lake halisi na mtu ambaye hajawahi kumuita hivyo.Kweli jamaa alizidiwa nusura ya kufa.

Lakini aibu yake ndio ilimponza kwani aliona aibu kunyanyuka licha ya maumivu yaliyikuwa yamamsurubu.

Eve alinyanyuka na kwenda hadi kwa Fred alipokuwa amekaa na kumshika bega huku akijaribu kumnyanyua kichwa alichokuwa kakilaza juu ya meza.

“Fred vipi?.”Eve aliuliza.

“Naungua.”Fred naye alijibu huku akionesha wazi anaemia kwa kuungua.

“Wapi sasa.”Eve naye akawa anasaili kwa makini akifata vitendo vya Fred.

Fred hakuwa na jinsi tena kwani hali ilikuwa mbaya sana kwake. Akamuonesha pale alipokuwa amekalia kuwa ndipo panamuunguza.

Eve kwa haraka alimuomba anyanyuke bila kujua hali ambayo ingetokea baada ya Fred kunyanyuka.

Fred kwa shida na uvumilivu uliomshinda,alianza kunyanyuka taratibu na wakati huo umati mkubwa ulikuwa unaangalia ile filamu japo walikuwa hawaelewi ni nini kinaendelea.

Fred akanyanyuka na kusimama wima. Dah! Kilichoonekana ni zaidi ya wengi walivyodhani.

Ile suruali aliyokuwa kaivaa ilikuwa kama karatasi lililoungua,na hatari zaidi ni pale Eve alipojaribu kuikung’uta kwa nyuma ile suruali.

Ni majivu pekee ndiyo yaliweza kumwagika pale suruali ilivyokung’utwa.Na kibaya zaidi ule mchanganyiko wa Hans uliweza kula nguo ya nje hadi boxer la Fred kwa sehemu kubwa sana na kufanya hata makalio ya Fred kuonekana.

Ilikuwa ni ahueni kwa Fred kwani maumivu ya kuungua yalipungua lakini shughuli ilibaki kwa wale waliokuwa wanashuhudia lile tukio. Wengi wao walicheka sana tena sana.

Fred aliona jambo la msingi ni kufunga koti lake kiunoni ili kuficha ile hali yake. Na baada ya hapo alitoka mahala pale haraka na kwenda mahala kumsubiria Eve ambaye naye chakula kilikuwa kichungu japo alikilipia kwa haraka.

Baada ya kukilipia chakula kile,Eve alitoka kwa kasi kumuwahi Fred ambaye alikuwa hajielewi elewi ni nini kimemtokea kwa muda mfupi ule aliokutana na Eve.

Huku nyuma baada Eve kuondoka,wahudumu wa pale walienda kwenye meza waliyokuwa wamekaa wakina Fred na kutaka kutoa vyombo lakini bila kutegemea Hans na Junior walifika kwenye meza ile na kukataza ule msosi kutolewa.

Hans na Junior walikuwa ni watu ambao hawana aibu kabisa.Hivyo wale wahudumu walipotaka kubisha,wakina Hans walianza maneno ya kejeri yaliyowafanya wale wahudumu wawili kuondoka kwa aibu.

“Yaone kwanza.Kumbe kazi yao kula vyakula wanavyoacha wateja,leo mmenoa.Tunakichukua na kusepa nacho.Hayooo,shutuuu!.”Maneno yalimtoka Hans baada ya wale wahudumu kukubali yaishe na kuanza kuondoka eneo lile.

Hans na Junior walifanya kazi ya haraka sana kwa kuchukua kile chakula na kukimwagia kwenye mifuko misafi na baada ya hapo,walikimbilia bodaboda walizokuja nazo na kupotea eneo lile wakiwaacha baadhi ya wateja hoi kwa vicheko na wengine kukarahika na vile vitendo visivyo na aibu kutoka kwa watu wazima kama wale wakina Hans.

*****

Kwa upande wa Eve na Fred,wenyewe walichukua usafiri binafsi wa taksi na kuwapeleka katika makazi yao.

Ndani ya taksi ile,Fred alikuwa kachanganyikiwa kwa hali iliyomtokea na aliona aibu sana kumuangalia Eve. Hata pale Eve alipofika makazi yake,Fred hakuthubutu kumwangalia usoni bali alimuaga kwa ishara ya mkono tu,bila kusema.

Safari ya kupelekwa makazi yake yalipo,ikaanza na hapo ndipo amani ya moyo ilipomrudia na kuanza kufikiria filamu nzima ya kilichomtokea.

“Hans.”Aliongea Fred baada ya kufikiria kidogo.

“Huyu ni Hans mjinga yule. Yaani Hans kanifanyia hivi kweli?.”Fred aliongea kwa sauti na kumfanya dereva wa taksi aliyopanda kumtazama kwa makini kwa kupitia kioo cha dereva kile cha juu.Maana alidhani mteja wake anaweza kuwa mwehu na kusababisha mambo mengine ndani ya gari.

“Kwa hiyo kanifanyia hivi kunikomoa au kisasi? Yaani huyu Hans kweli ananiabisha mimi? Mimi!!? Kabisa mbele ya umati wa watu, watu zaidi ya mia wameona makalio yangu. Kweli kabisa Hans unaniabisha mbele ya Eve? You will pay for this.”Fred aliongea kwa uchungu lakini yule dereva wala hakuingilia bali kuwa makini tu!Mtu wake asimkabe kama atapandisha ukichaa wake.

Baada ya dakika kadhaa,hatimaye taksi ilifika yalipomakazi yake. Fred akashuka na kumlipa yule dereva ujira wake kisha huku akiwa na koti lake kiunoni kama mtoto wa shule ya msingi,alianza kuelekea kilipochumba anachoishi na wenzake.

Alipofika,alifungua mlango na kuwasha taa. Aliwaona rafiki zake wote wakiwa wamelala na wengine kama Hans kukoroma kabisa

Alichofanya Fred ni kuanza kuwaamsha wenzake kwa kuwatingisha na kuwaita kwa kuwapigia kelele.

“Oya nini bwana?Tunakatishana stimu.”Hans aliongea huku akifikicha macho yake baada ya kuamshwa.

“Pumbavu wewe. Wewe wa kunifanyia vile Hans?.”Fred aliongea kwa hasira huku akimuangalia Hans kwa jicho la kummeza mtu.

“Nimefanyaje Baba Paroko?.”Hans aliongea kama kweli hajui kitu.

“Linajifanya halijui boya hili,umeliona linajifanya eti halijui lilichofanya.”Fred alizidi kuongea na safari hii alikuwa anaongea huku anawageukia kwa zamu wakina Junior na Suarez.

“Kwani kafanyaje Mzee wa Upako?Mbona hatukuelewi? Halafu mbona koti umelifunga kiunoni? Au ndio umemvalia kibwebwe mwanaume mwenzako toka huko ulipotoka.”Aliongea Suarez na kumfanya Hans uvumilivu wa kucheka kumshinda.

“Si unaona hili boya linacheka?Linajua lilichofanya.”Fred aliongea kwa jazba na kwa sauti ya juu.

“Kafanyaje kaka?Mbona hufunguki?.”King Junior Nickson naye aliuliza.

Mara Fred akafungua lile koti lake na kulitoa kisha akawageukiwa kwa kuwapa mgongo Hans na Suarez waliokuwa wamelala upande mmoja.

“Hapa umeridhika nini boya wewe?Nakuuliza umeridhika nini.”Ee bwana suruali yake ilikuwa imeungua tokea pale karibu na mkanda hadi huku chini karibu na magoti. Hakika ilikuwa ni kituko cha mwaka au cha siku ile maana hata makalio yake yalikuwa yanaonekana wazi bila kificho. Fred alikuwa kaaibika sana kwa kweli.

“Nakuuliza umefaidika nini hapa?.”Fred alizidi kuuliza huku bado kawapa mgongo Hans na Suarez.

Wakati anafanya hayo yote,Emmanuel Suarez,yeye alikuwa katika taharuki kubwa kutokana na kile alichokuwa anakitazama.

Kinyume na hapo,kwa upande Hassan Jenge,yeye alikuwa kaishiwa nguvu kwa sababu ya kucheka kicheko ambacho kilikuwa kimevutwa kwa muda mrefu na kikakauka kabisa. Ni kama mtoto mdogo pale anapoumia sana,kuna kilio fulani anakivuta hadi kinakauka,pale akiamua kukitoa nje sasa,ni kama filimbi.

Sasa na kwa Hans ilikuwa hivyo,alikivuta kile kicheko kwa ndani na pale alipokitoa nje,ama kweli kilikuwa kicheko cha nguvu.

“Umeona boya hili linacheka.”Fred aligeuka na kuanza kumfata Hans pale alipo kwa hasira. Wakati anafanya hivyo,ndipo pia alipompa fursa Junior na yeye kujionea majanga yaliyokea katika suruali ya rafiki yake.

Naye bila kusita akaangua kicheko cha nguvu.

Fred alimfata Hans pale kitandani na kuanza kumsukuma sukuma wakati huo Hans alikuwa anagalagala kitandani hana mbavu.

“Nakwambia wewe boya leo utaniambia nimekukosea nini.”Fred aliongea kwa hasira huku anamvuta Hans aliyekuwa hajiwezi kwa kicheko.

Wakati anafanya hayo ya kuhangaika kumvuta Hans pale kitandani,huku nyuma Junior alikuwa anazidi kuwa hoi kila alipoangalia kile kilichokuwa kinatokea nyuma ya suruali ya Hans. Hakuwa mvumilivu kwa kubana kicheko bali kukiachia kwa nguvu zake zote.

“We boya nakwambia hapa utashuka mwenyewe, boya wewe.”Fred aliendelea kumvuta Hans aliyekuwa kalegea kwa kicheko.

Hali hiyo ya Fred kumvuta Hans iliendelea kwa muda wa dakika zisizopungua mbili na zilikwama pale Fred alipochana fulana iliyokatwa mikono,mali ya Hans.

“Baba Paroko umenichania Tisheti langu kwa sababu ya ujinga wako,si ndio eeh.”Hans aliongea huku kakunja uso kuonesha kachukizwa na kile kitendo.

“Nakwambia we boya leo nakuchania hadi boxer lako. Utanieleza nimekufanya nini.”Fred aliendelea kumvuta Hans pale kitandani bila kujali kama kishaifanyia unyambirisi fulana ya Hans.

“Kwani Fred ilikuwaje kaka hadi ikatokea hayo yote? Mbona unamvuta tu jamaa kama alikuwa kwenye mambo yenu?.”Suarez alimuuliza Fred baada ya kuona zogo linazidi kuwa kubwa.

“Labda unisaidie kuuliza wewe kaka maana hadi nachaniwa shati hapa bila kosa.”Hans alijibu huku akijeweka mbali na Fred kwa kujisukumia ukutani kabisa mwa kitanda chake.

“Unajua nini Sua (Shua),huyu jamaa kaniwekea makemiko kwenye mifuko ya suruali yangu. Sasa nimefika pale tulipopanga kufika,tukakaa kwenye viti,mara nikaanza kuungua……”Fred hakumalizia Suarez anayehadithiwa akamkata ulimi.

“Ulifika mlipopanga,ilikuwa wapi? Mbona unaongea mafumbo? Kama ni kwenye moto ndipo mlipofikia,sasa kwa nini usiungue?.”Suarez aliongea na kumfanya Hans aanze kucheka tena.

“Wewe Sua vipi? Gentleman ahadithii mambo yake.Au umesahau?.”Junior aliongea huku akiwa naye anacheka balaa.

“Umeona ee Junior. Gentleman ahadithii ishu zake hata kidogo,ha ha haaaa. Unaleta mambo ya kwenye video hapa.”Hans aliongea huku akiwa anazidi kujisogeza mbali na Fred aliyekuwa kajaa gesi ya hasira nusura ya kupasuka.

“Ha ha haaaaa, Think Like A lady…..”Junior aliongea na kumuoneshea kidole Hans amalizie ile sentensi.

“Act Like A Man…. Ha ha ha haaa,jamaa alikuwa anajidai Dremer.”Hans naye alimalizia sentensi ile huku akimfananisha Fred na Dremer,jamaa mmojawapo aliyeigiza filamu ya Think like a lady,Act like a man. Filamu ambayo Fred alikuwa anaingalia sana na kuigiza vitendo vya mule kwa Eve.

“Embu acheni washikaji. Mwanangu Fred endelea ili tujue kama ni kweli au si kweli,ikibidi Eve aitwe na aambiwe hii ishu.”Suarez aliongea akimwambia Fred aliyekuwa kasimama katikati ya chumba kama anawanga.

“Mwanangu nilienda na mtoto hotelini……”Kabla hajamaliza Junior akadakia tena.

“Hotelini wapi? Pale mgahawani bwana.”Junior akaropoka.

“Kumbe na wewe boya unahusika,Junii na wewe unahusika kweli kwenye hili? Aisee kweli mlikamia”.Fred aliongea kwa uchungu hadi Suarez ilim-bidi ainuke na kushuka kule juu anapolala na kumkalisha kwenye kiti kimojawapo wanachosomea mule ndani.

“Sisi tulienda kununua msosi ndio tukaona picha zima,wala mimi sijui kilichokuwa kinaendelea. Eti Sua hatujakuaga kuwa tunaenda ule mgahawa kuchukua chakula?.”Junior alijitetea.

“Waliniaga mwanangu,na wala mi mwenyewe sijui kama ulikuwa umeenda kule.”Suarez alimpunguza munkari Fred ulioanza kujaa juu ya Junior.

“Aaag,kwanza mmeongea kuhusu chakula,mimi nimeshikwa na njaa ghafla.”Hans alinyanyuka na kufuata kabati lake ambapo alilifungua na kuibuka na sinia moja kubwa kiasi.Akaliweka juu ya meza ya kusomea iliyokaribu kabisa na alipokaa Fred.

Baada ya zoezi hilo dogo la kuweka sinia juu ya meza,akapekua tena kwenye kabati lake na kuchomoa mfuko mweusi uliokuwa umenona kwa nje kutokana na chakula cha ndani kuwa na mafuta sana.

Akafungua mfuko ule na kumwagia kilichomo kwenye sinia lilipomezani.

Ghafla hali ya chumba kile ilibadilika na kupambwa na harufu nzuri ya chakula kile kilichowekwa kwenye sinia.

Lakini hali pia ilim-badilika Fred na kuwa ya taharuki zaidi. Midomo ilim-baki wazi na macho yakiwa yamekodelea kile chakula hali ambayo baadaye ilizidi kubadilika kwa midomo kutaka kuongea lakini ilishindwa na kubaki vidole kuoneshea kile chakura kilicho-mezani,ungemuona ungesema huyu jamaa ni bubu.

Hali hiyo haikumfanya Hans kujichukulia paja na kuanza kulitafuna kwa uchu. Hapo hapo na Junior aliinuka toka kwenye kitanda chake cha chini na kwenda kujichukulia kilichopo kwenye sinia lile la Hans.

“Nimekitolea jasho hiki.Kupambana na wale wahudumu hadi kukipata wadhani jambo dogo lile.”Junior aliongea huku akishika mgongo wa kuku na kuanza ku-ususomola.

“Fred vipi kaka,mboa hivyo?.”Suarez alimuuliza Fred baada ya kumuona hana la kuongea bali kushikwa na kigugumizi.

“Chakula chetu,mimi na Eve.”Fred aliongea huku machozi kama yanataka kumtoka.

“Sasa nyie mliacha chakula chote hiki,nyie vipi?Na bahati yenu vinywaji hamkununua.”Hans hakuwa nyuma kuongea japo alikuwa anabugia tambi kwenye kinywa chake.

Fred hakuvumilia hali ile. Yaani kuaibika, ka-aibika, chakula kimelipiwa bila kuliwa. Halafu mbaya zaidi wanao-kila ndio hao waliomuaibisha. Haikuwezekana kukubalika kwenye kichwa cha Fred.

Hali hiyo ya kutovumilia,ilimfanya Fred akwapue lile sinia kwenye vidole vilivyokuwa vinaendela kufakamia ule msosi wa ghari,aliougharamia mpenzi wake kwaajili yake.

“Pumbavu zenu,sasa ole wake boya asogee.”Fred aliongea huku anaelekea pembeni na sinia lile la chakula kwa lengo la kukila peke yake.

“Mwanangu na sisi tumeweka chakula chetu humo,kwani chenu kilikuwa kingi hivyo.”Junior aliongea huku akimfata Fred kule ukutani alipoenda.

“Nitakumwagia hizi tambi,kuku na haya makachumbali usoni na hutonifanya kitu,nisogelee sasa.”Baba Paroko aligeuka gaidi kwelikweli.

Junior ilibidi harudi nyuma hasa alipofikiria muwasho wa ile kachumbali mdomoni,sasa anaambiwa atamwagiwa usoni.

Fred akawa m-babe mule ndani. Akachukua paja moja la kuku na kumrushia Suarez,naye Suarez akalidaka na kulitia mdomoni kwake.

Fred akageukia ukutani na wakati huohuo akawapa wakina Hans mgongo na kuwafanya waone ile suruali ilivyokuwa imeharibika.Kicheko kikaanza kwa kasi ya ajabu lakini Fred hakujali zaidi ya kuendelea kula huku akicheza taratibu na kukata kiuno kwa mbali. Hasira zikamuisha kihivyo maana angeendelea kuwa na hasira hizo,ingekuwa hasara kwake. Cha msingi aliona bora asahau,lakini si kwamba alisahau kabisa.

*****

Kesho yake waliamka wenye furaha kama jana yake usiku kulikuwa hakujatokea kitu. Walikuwa ni watu wenye amani kupitiliza huku ikionekana wazi hakuna kisasi baina yao.

Lakini ajuaye moyo wa mwanadamu una nini,ni yeye mwenyewe binadamu pamoja na MUNGU wake.

Moyo wa Fred ulikuwa haujafurahia kabisa kile kitendo alichofanyiwa na Hans. Pia alikuwa kampatia sana hasira Junior kwa kuwa mshirika wa Hans. Hayo yote aliyaweka moyoni na kuyapangia mkakati kabambe wa kuyalipa.

Bila wale jamaa zake kujua yaliyo-moyoni mwake.Fred alionesha mwenye amani na furaha kila wakati huku akiwa mstari wa mbele kukumbushia kilichomtokea jana.

****

Siku nne mbele toka siku ya tukio la Fred,ilikuwa ni zamu ya Junior kukutana na Eve. Fred alifahamu hilo,hivyo akaanza kutafuta njia za kulipa kisasi kwa alichofanyiwa na wale rafiki zake.

Aliangaika sana na mwisho wake aliona ni bora aende kwa wagumu kuomba msaada kwani Junior alionekana ni mtu makini sana kwenye mambo yake.

Haikuwa rahisi kwa Junior kuacha nguo zake hovyo,wala kabati lake. Kifupi alizidisha umakini hasa kila alipofikiria tukio lililomtokea Fred. Sasa Alfred aliamua kuomba msaada kwa Wagumu,walewale aliowahi kuwaabisha walipofika chuoni kwa mara ya kwanza. Ndio walewale wakina Moi Shabala,Kamanda wao Ban Diho na Sunday Magembe.

“Kwa hiyo mkuu unatakaje sasa.”Kamanda wa Wagumu,Ban Diho alimuuliza Fred baada ya Fred kutoa mkasa mzima ulimkuta.

“Nataka boya naye aibike mbele ya mtoto kama mimi nilivyoaibika.”Fred aliongea kwa hamasa juu ya nia yake

“Basi usijali. Cha msingi taarifa umetupa,sisi tutapiga kazi kama kawaida ila yapasa uache kitu hapa,hatupigi kazi bila mshiko,si wajua sisi makamanda.”Ban aliongea kwa makini huku akimwangalia usoni Fred aliyewafuata chumbani kwao.

“Hilo usijali,nyie niambieni kiasi mnachotaka.”Fred alizidi kujiingiza kwenye dhamira yake ya kisasi.

Kwa kuwa wale jamaa walikuwa na kisasi na lile kundi la akina Hans,waliamua kuutumia mwanya huo kulipa walichowahi kufanyiwa.

“Hapo utaacha elfu hamsini mwanangu.”Ban alimjibu Fred na kumuacha kinywa wazi.

“Kaka mbona kitu kidogo sana lakini umekaza hivyo. Au unaenda kuua? Sitaki mauaji,nataka aibike tu!.”Fred alishindwa kuzuia hisia zake juu ya ile bei aliyotajiwa na Ban.

“Hafi mtu hapa jembe langu. Tunataka kukufanyia kazi ya uhakika. We mwenyewe si wacheki makamanda tupo wangapi? Huyo dogo ataaibika mpaka mwenyewe utakuja na kutuongeza elfu hamsini nyingine. Ila kwa sasa,sisi tunataka hiyo fifte halafu kazi nzima tutaifanya wenyewe hadi iishe.”Ban alizidi kumvuta Fred ili amuingize kitanzini kwa ile hela aliyomtajia kama gharama.

“Fanyeni elfu thelathini basi,hiyo hamsini mimi sina.”Fred alibembeleza jambo kana kwamba anachotaka kufanya ni sheria iliyoruhusiwa na tume yakutunga sheria hapa nchini.

“Kama utataka kwa bei hiyo,itabidi na wewe uwemo kwenye mchakato huo. Sisi tutakutafutia kila kitendea kazi,halafu utakamilisha kazi hiyo we mwenyewe.Unasemaje.”Ban alikuwa mkavu na mwenye msisitizo wakati anaongea hayo.

“Mazee,mimi yamenishinda na ndio maana nimekuj kwenu. Nisaidieni bwana.”Fred alizidi kubembeleza huku shingo yake kaiweka upande kuwasilisha bembelezo lile.

“Sikiliza kamanda Fred,sisi tutakupigia kazi ya maana ambayo hutatambulika kama ni wewe bali yule Hans. Na kama Junior atamshuku yule,ni lazima atataka kulipa kisasi. Sasa wewe ndiye utatuletea mteja huyo. Na yeye tutampa bei kama yako,na kama yawezekana tutaipandisha juu iwe kama elfu sabini au laki moja. Wewe ndio utakuwa unamsukuma ili alipe kiasi hicho,tena ikibidi mkopeshe kiasi kilichozidi.

Akitulipa,sisi tunakata elfu hamsini yetu,kile kilichozidi tunakupa wewe kama shukrani ya kutuletea mteja. Hapo vipi kamanda.”Safari hii aliongea Moi Shabala kibiashara zaidi.

“Hapo haina noma. Basi nipeni nusu saa kwanza nikafanye mambo benki.”Fred aliomba ruhusa na kutoka chumbani kwa akina Ban akiwa ameridhika na maamuzi yake juu ya kulipa kisasi kwa Junior.

*****

Alienda benki na kufanya muhamala wa fedha kwa kiasi cha shilingi elfu sabini. Elfu ishirini aliweka pembeni na elfu hamsini akaiweka mahala kwingine. Hapo tayari akawa amekamilisha kazi iliyompeleka benki na akawa tayari kwa ajili ya kuingia vitani,vita ya kijinga kabisa kuwahi kutokea katika maisha ya mwanadamu wa leo.

Baada ya dakika zisizopungua arobaini,Fred alikuwa chumbai kwa akina Ban akifanya makabidhiano ya fedha zile alizoenda kuzichomoa benki.

“Mzigo ndio huo hapa wazee. Nataka kazi ifanyike bila mimi kujulikana, na pia nataka siku ya tukio na mimi mnitaarifu ili niwepo eneo hilo nione kitakachotokea.”Fred alikuwa anatoa kiasi cha fedha huku anaongea hayo.

“Hamna shaka hata kidogo. Deal done.”Ban alikamilisha maongezi huku akikabidhi noti tano nyekundu,fedha halali kwa malipo nchini Tanzania kwa Sunday Magembe aliyekuwa katoa tabasamu la pongezi kwa kamanda wao,Ban.

“Basi fresh. Mambo yote ni kesho. Dogo ndio anaenda kukutana manzi. Fanyeni yenu kama kawa.”Fred aliweka hitimisho juu ya maongezi yale na kutoka nje chumba kile akiwa na uhakika wa kazi yake kufanyika bila zengwe wala kokoro.

Ama hakika alipania kufanya kisasi,kitendo cha kutoa kiasi kile cha fedha kwa ajili ya kumuaibisha mwenzako,ni kitendo cha kijasiri sana kupata kutokea kwenye dunia ya sasa,dunia iliyojaa vituko kila kona ya pembe zake. Yote yanabaki kuwa siri yake,hakuna aliyepaswa kujua kama analipa kisasi zaidi ya wale aliyowapa kazi ile.

*****

Huku nyuma baada ya Fred kuondoka,Ban alipanga jeshi lake kwa ajili yakutimiza kazi waliyokuwa wamekabidhiwa na Fred,kazi ya kuhakikisha Junior anaaibika mbele ya umati wa watu.

“Umeona maboya hayo? Sasa ni muda wa wao kuaibika,walidhani tumesahau ya siku zile? Sasa hapa ni kuwafanya waaibike bila sisi kugundulika. Yaani tunacheza chezo huku tunawapakazia wao. Tunakula hela,na bado tunawaabisha. Huo ndio mpango.”Aliongea kamanda mkuu wa chumba kile,Ban Diho.

“Hapo kamanda umecheza kama Pele. Naikumbuka sana ile siku tuliyotembea uchi. Mi kidogo nihame na chuo,ila nikajikaza kiume tu.”Moi Shabala naye aliongezea chachandu juu ya maongezi yale.

“Na hapo lazima ziwamwagike haswaa,si walijidai manunda. Sasa wamekutana na manunda square.”Ban aliongea kwa chuki iliyokuwa wazi kabisa.

“Ndio maana yake. Watajua wenyewe wakipigana,wakikatana mapanga,wakitishiana bastola na hata wakichinjana. Cha msingi sisi tupange jinsi ya kumwaibisha huyo dogo ili akome.”Mdomo wa Sunday nao haukuwa nyuma kudhibitisha kuwa yupo ndani ya wenzake na hawezi kuwatosa.

“Hapa watasanda tu!.Sisi ndio maji,ukishindwa kwa kutunawa,utatugida tu.”Ban alimaliza tambo zilizokuwa zinaendelea chumbani mule na sasa alikuwa kajiweka wima kwa jili ya kuanza kazi ya kuupanga mkakati uliokuwa umewatinga mbele yao.

BAADA ya dakika kadhaa za kukaa mule chumbani kwao.Ban na kundi lake walikuwa wameshamaliza makakati watakaoutumia kwa ajilli ya Junior,na hakika ulikuwa ni mpango wa uhakika kwa ajili ya kijana machachari pale chuo kikuu kwa kupiga gitaa la solo,kijana aliyekwenda kwa jina la Junior King Nickson.

“Kwa hiyo kila mtu acheze nafasi yake maze. Wewe Moi na Mose,anzeni leo kufatilia maeneo ambayo dogo atakuwepo,mzee nani hapo Sunday, nenda katafute dawa hiyo na mimi naanza kualika watu na ishu nyingine.”Ban alitoa majukumu ambayo tayari walikuwa wameyajadiri.

“Haina kwere Kamanda mwenyewe. Hapo wenyewe watasema yuwiii.”Sunday aliyatoa hayo huku ananyanyuka pale alipokuwa kakaa na kwenda kwenye kabati lake. Nadhani alienda kuvaa mavazi mapywa kwa ajili ya kazi hiyo ambayo waliamua kujitolea kuifanya kwa moyo mmoja.

5

Tofauti na Sunday,Mose.Moi na Ban,wao kila mmoja kwa wakati wake walitoka kwenye chumba chao na kuanza kuyafanya amabayo walikuwa wamepania kuyafanya.

******

Muda nao haugandi,mida ya jioni kundi la wagumu lilikuwa chumbani likijadiri mafanikio yao ambayo waliyapata kwa siku nzima tangu walipoachana mida fulani ya mchana.

“Dawa nimeipata na nadhani ni dawa bora kabisa kupata kutokea katika tafuta yangu dawa.”Alianza Sunday kufunguka kuhusu alichokuwa amepangiwa na Ban.

“Sina tatizo na wewe dokta. Nakuaminia sana Sajent Sunday.Sinaga tatizo na wewe.”Ban alimpongeza Sunday na wakati huo macho yake yalikuwa yanaangalia nyuso za Moi na Mose.

“Katika fatilia yetu,tumegundua yule Sharo anapenda sana kwenda na mtoto kule kwenye mlima. Sasa kwa kuwa anajua kuwa kuna jambo linaweza kumkuta,anaweza kubadili maamuzi. Badala ya kwenda mlimani,anaweza kwenda mahali popote, ili mradi paw tofauti na kule mlimani.”Mose aliongea kile anachokijua.

“Yap.Kweli kabisa,mmefanya jambo kubwa kujua hilo.Lakini sasa cha msingi yawapasa hiyo kesho kuwa karibu kabisa na geto lao,ili akitoka tu!Mnaanza kumfuatilia mwanzo mwisho anapoelekea.”Ban alizidi kuonesha uongozi bora kwa wale vijana aliokuwa nao mle ndani.

“Mimi nilikuwa nategemea majibu yenu ili niwapange watu wangu kwa ajili ya sapraizi kwa yule tozi kinyesi.”Ban akaweka bayana kile alichokuwa kakichukulia jukumu.

“Kwa hiyo watu wamepatikana?.”Moi aliuliza.

“Watu wapo wa kutosha tu!.”Ban akampa moyo Moi kwa jibu hilo fupi.

“Basi hamna shida ya kumfatilia sijui mpaka mlimani au wapi.

Akitoka pale ghetto,mimi nitakuwa naye nyuma bila yeye kujua. Na wakati huo nitakuwa nawapa taarifa kwa simu ni njia gani anapita. Nyie mtetega kwenye njia hizo. Akifika mnamkamata na kuanza kumremba remba ili apige gitaa,mnampa hadi kiti cha kukaa. Wewe mzee wa dawa,lazima uwe karibu naye. Akikupa kinywaji chake,unaweka kidawa hicho. Au kama hana,tunampongeza wenyewe kwa kumpa hata maji. Akinywa tu! Kaisha.”Moi alitoa pendekezo ambalo lilifikiriwa kwa muda kabla ya kupitishwa na bunge lile la watu wane.

“Yaweza kuwa njia rahisi zaidi kwani tunaweza kumkamatia penye watu wengi zaidi na tukafanya tukio kubwa kuliko hili ambalo tunataka kulifanya. Hivyo wazo la jamaa ni zuri sana tena sana. Limepita hilo Kapteni Moi.”Ban alikubaliana na wazo la Moi Shabala.

“Kwa hiyo ndio mpango upo hivyo,sitegemei kwa mpango huu kuingiliwa na nzi yeyote. Na mzee wa vi-medical,hakikisha kidawa unakiweka bila mtu yeyote kushtukia mchezo huo.”Ban alimaliza maongezi yale na kuanzisha habari nyingine ambazo alikuwa amezikusanya wakati anatafuta watu wa kushuhudia Junior akiabika.

*****

Hatimaye ikafika siku ambayo Junior alipanga kukutana na Eve.

Kama kawaida yake nay a wote mule chumbani.Junior alianza kujisafisha na kujiweka nadhifu kwa ajili ya mtoko ule wa maana na mtoto Eve.

Alinyoosha nguo zake na kuzichunguza sana ili asijefanyiwa kitu kama alichofanyiwa Fred na Hans. Wakati hayo yote yanaendelea.ni Suarez pekee ndiye alikuwa akiongea naye. Hassan na Alfred walikuwa kimya wakizuga wanajisomea na wakati walikuwa wanamwangalia kwa jicho la chini-chini.

“Ee bwana msalimie sana mrembo huyo.”Suarez alimuaga Junior aliyekuwa kapendeza vilivyo kwa kuvaa jinzi moja iliyomkaa vizuri,wanaziita modo.

Kwa juu alivaa fulana nzito yenye rangi ya kahawia na ina-alama ya fuvu na maandishi fulani ya vitisho. Ni kweli alipendeza,hasa pale alipoweka gitaa lake kwa nyuma kama vile msanii wan je aliyekuja kutalii Tanzania.

“Zimefika mkuu,na hao The Lost Boys hata kuniaga hawataki? Ni wishini lucky jamani.”Junior alitoa tabasamu la kejeli wakati ulimi na kinywa chake ukitamka maneno hayo.

“Maneno hayo. Ndio hayohayo yaliyomponza mwenzako.”Maneno toka kwa Hans yakamfikia vilivyo Junior na kumfanya aondoke zake.

*****

Hali ya hewa ya siku hiyo haikuwa mbaya sana. Na kama alivyofanya kwa Fred,Eve alimuomba Junior watembee kwa miguu.

Barabara nzima macho yalikuwa yanawaangalia vijana wale waliopendeza wakati wanatembea. Kila mmoja hakusita kuwasifia kuwa wamependeza.

Eve akiwa na ndani ya suruali fulani ya jinzi iliyokuwa mmekaa vizuri kabisa,na wakati huo kwa juu alivalia kitopu kilichoacha wazi kitovu chake mwanana,nani ambaye angesipomwonea wivu Junior?Ni kweli walipendeza sana kwa mwonekano wao muda ule wa saa tisa alasiri.

Safari yao licha ya pongezi nyingi,wao wenyewe walikuwa wanaifurahia kwa vicheko vya kuliwazana pamoja na kufurahishana.

Kila muda walicheka na kugonga viganja vyao bila wasiwasi wowote mioyoni mwao.

Safari ilienda lakini mwisho wake ulikuwa ni sehemu moja ya jiji la Dar es Salaam ambapo sehemu hiyo kulikuwa kuna watu wengi sana.

Ni kawaida ya eneo hilo kuwa na watu wengi hasa mida ile ya saa tisa,lakini kilichowashangaza wakina Eve,ni kuzungukwa ghafla na watu hao na wote walitaka Junior apige gitaa ndio aondoke pale.

Watu walikuwa ni wengi na wengine walikuwa ni wanachuo wanaomjua Junior vizuri sana. Sasa walikuwa wamewazingira.

“Junior tupigie gitaa kwanza ndio uondoke na mrembo wetu,vinginevyo,hatoki mtu hapa.”Jamaa mmoja aliyekuwa na mizuka ya muziki,aliongea hayo.

Junior alitabasamu na kumwangalia Eve aone ataitikia nini kwa maombi yale ya wananchi. Hatimaye Eve naye alitabasamu,kisha akaonesha ishara ya kumwambia awape burudani wale wananchi.

“Kitendo bila kuchelewa,kiti kililetwa pale walipokuwepo. Na Junior akapewa uwanja kwa ajili ya kufanya yake.

Alipokaa kabla hajalitoa gitaa lake,mara akaletewa maji ya kunywa. Naye bila kusita aliyapokea bila hata kumuangalia ni nani aliyempa yale maji. Kisa yaliyakuwa hayajafunguliwa, basi naye akaona yanafaa.

Akafungua maji yale na kuyafakamia kwa kiasi kikubwa tu!. Alipoweka chini chupa ya maji yale ya baridi,tayari alikuwa kapata mzuka wa ajabu.

Akaanza kulifungua begi la gitaa lake ili kulitoa dude lile kwa ajili ya kuburudisha wapiti njia.

Baada ya kulitoa,alianza kukaza nyuzi za gitaa lile ambapo alichukua kama dakika moja na nusu au mbili kabisa ili kufanya yote yale.

Pale aliponyanyuka kwa lengo la kuanza kulichakaza gitaa,mara tumbo lake alijisikia kama limekatwa na kisu. Hakika alishtuka lakini alishindwa kuonesha mshtuko wake kwa kuwa alikuwa mbele ya umati mkubwa wa watu.

Alidhani labda ni utani,lakini hali ilianza kumuwia vibaya pale aliponyanyua gitaa lake kwaajili ya kuanza kulikung'uta.

Ile kulinyanyua tu! Gitaa,mara akatoa gesi au hewa chafu kwa njia ile ya chooni. Ndio hivyo,Junior alipumua na kila mmoja aliyekuwa pale alisikia sauti ya pumzi ile.

"Vipi kaka? Gitaa zito?."Yule jamaa mpapulishaji alimuuliza Junior baada ya lile tukio la ajabu kutoka kwa Junior.

Naliita la ajabu kwa kuwa lilitoka katika wakati usiotegemeeka kabisa. Kweli Junior alikuwa anaaibika,na ni kweli Fred na kundi lile la wagumu walikuwa wamepania kumuaibisha kijana yule.

Hali ilizidi kuwa mbaya na kupoteza muelekeo wa Junior wote wa kupiga gitaa. Jasho lilimtoka hasa pale tumbo lilipozidi kumvuruga na kumuaribia kabisa mapozi ya kukaa.

Kila alipomwangalia Eve,macho yake yalikutana na sura ya mshangao kutoka kwa kimwana yule mrembo. Ni mikono ya Eve ndio ilikuwa inamuuliza Junior ni nin kinachoendelea.

Kila Junior alipojaribu kuvumilia hali aliyokuwa nayo tumboni mwake,alijikuta akitumbukiza watu kwenye kicheko kikubwa kupita maelezo. Junior alikuwa akipumua kila baada ya sekunde kadhaa.

Mambo yakazidi kuaribika pale alipotaka kuondoka,alijikuta tumbo likimzidi nguvu na bila kupenda alirudi kwenye kiti alichokuwa kakaa mwanzo.

Tumbo la hewa likawa tumbo la haja kubwa.Akawa ni mtu wa kuumia sana na wakati huo ule umati ulikuwa upo hoi kwa vicheko,walikuwa hawajali hali ya Junior iliyokuwa inamtesa,bali wao waliona kama ile ni fahari ya macho.

Ni Eve pekee ndiye aliyekuwa na uso wa usiriazi,kati ya wale wananchi zaidi ya mia waliokuwa hawana mbavu kwa vicheko vilivyokuwa vimewashika.

Eve alienda kwa Junior na kumuuliza kwa sauti ya chini ni nini kinachoendelea.

"Tumbo Eve."Junior alijibu kwa uchungu huku akijipinda panda pale alipokuwa kakaa.Na kile kitendo cha kuongea,ni kama nalikuwa anaruhusu haja itoke.

"Umekula nii ulipotoka?."Eve alipouliza swali hilo,Junior mawazo yake yakaenda hadi mida fulani ya mchana,alikunywa chai huku akiwa na wakina Hans. Hapo hapo akatengeneza maelezo kuwa wakina Hans walimwekea kitu kwenye ile chai.

"Hansiiiiiiii,aaagh. Umenifanyia nini wewe? Nimekufanya nini?."Junior alitoa maneno hayo huku machozi yakiwa karibu.

"Hans kafanyaje tena?."Eve ilimbidi aulize baada ya kusikia lawama zile

“Hans ndiye mwenye tabia hizi. Alimuunguzia hata Fred suruali yake ulipotoka naye siku ile.Aagh.’Junior alitamka maneno hayo na kugugumia maumivu ambayo yalikuwa hayaelezeki kabisa katika wakati ule.

Eve alisimama wima na kuchanganua maneno yale huku akiwa wazi kaamini kuwa Hans ni muhusika way ale yote hasa kwa tabia yake.

Akili ya Eve ilicheza haraka na kwenda kuchukua taksi ambayo ingemsidi kiasi fulani kuficha ile aibu.Huku nyuma alimuacha Junior akizidi kuwa hoi na sasa aliona kuwa liwalo na liwe,ni heri ajisaidie kuliko kuendelea kuumia pale kwenye kiti.

Wakati Junior amejitolea kujiachia palepale,ndipo Fred alitokea haraka na mtu ambaye baadaye alijulikana kama ni dereva wa tax. Na kitendo bila kuchelewa,walimnyanyua Junior pale kitini alipokuwa kajiinamia kwa maumivu,hapo safari ya kumpeleka kwenye taksi ilianza huku Eve akiwa nyuma na gitaa la Junior.

Ilikuwa ni pona ya swala kwenye mdomo wa mamba kwa upande wa Junior. Dereva taksi aliendesha gari kwa kasi kiasi chake hadi akafika ,ahala fulani ambapo pana choo.

Hapo Junior alifunguliwa mlango wa gari ile ndogo na moja kwa moja alichomoka kama mshale na kukimbilia uwani. Kilichoendelea huko,ni yeye na lile jengo mahususi kwa ajili ya haja kama zake.

Alikuja kutoka baada ya dakika ishirini za kufanya mambo yake. Alirudi akiwa na ahueni kubwa ambayo ingemfanya aendelee kupiga gitaa,lakini kwa aibu iliyomkuta mbele ya Eve,aliona ni bora atulie kimya hadi pale Eve alipoanzisha maongezi.

“Sasa kwa nini Hans anafanya haya yote?.”Ni swali lililoanzisha maongezi kati ya wale watu wanne waliokuwamo ndani ya taksi lakini maongezi hayo mtu wa nne ambaye ni dereva,hakupaswa kuyaingilia.

“Haijulikani aisee. Hata mimi alinitegea moto kwenye suruali yangu.”Fred alikuawa anajisafisha kama si yeye aliyeyafanya yale yote.

“Itabidi keshokutwa nimtafute ili nikae naye aniambie ni sababu gani iliyompelekea afanye huu ujinga. Ujue ni utoto sana huu. Kwanza ni tabia ya kishenzi kabisa.”Eve alionesha wazi kukasirishwa na yale matendo. Wakati huo gari ilikuwa inaelekea yalipo makazi ya Eve kabla ya kwenda kwa akina Junior.

“Na nikifika namuua.”Junior aliongea kwa hasira huku uso wake ukiwa umekunjamana kama kala kipisi cha ganda la chungwa au kala mchunga.

“Amna Junii,tutayamaliza haya mimi nay eye,msije mkapoteza urafiki wenu kwa jambo la kijinga namna hii.”Eve alitoa pendekezo ambalo Junior hakuwa wazi kulisikiliza wala kulishika.

“Nakwambia Eve yule namuua. Namuua kabisa. Nampoteza kwenye dunia hii.”Maneno makali yalimyoka Junior. Wakati huo Fred alikuwa kimya akisubiri wakati wake. Wakati ambao angemshauri Junior kilichobora zaidi.

“We muache bwana. Nitaongea naye na yataisha.Mbona mambo madogo tu!Yawezekana mmefanya kitu na ndio maana nay eye anawalipizia. Hans si mkorofi kihivyo.Ngoja niongee naye tujue ukweli upo wapi.”Eve alizidi kushauri na wakati huo gari walilokuwa wamekodisha,lilikuwa karibu kufika sehemu husika.

“Mimi nitamalizana naye tu! Leo leo”.Junior akamaliza na kuangalia pembeni ambapo kulikuwa na kioo. Muda huo ilikuwa imetimia saa kumi na nusu za jioni.

“Okey. Ni shaui yako.Ila mii naomba uache hizo fikra zako. Fred mshauri mwenzako. Mbona wewe umetulia japo alikufanyia yale?Huyu Junii yeye anajidai anahasira,shauri yenu bwana. Mimi simo. Ila ukinisikiliza,keshokutwa tutayamaliza na urafiki utaendelea kama kawaida.”Eve alimaliza na kufungua mlango wa taksi ile na kuanza kuelekea yalipo maskani yake huku akiwaacha Fred na Junior wakimaliza ngwe ya safari yao.

“Wewe Junii tulia kwanza.Unakuwa na hasira,mimi mwenyewe nimempania kinoma kumlipia kwa alichonifanyia. Cha msingi tulia kama si wewe.”Fred alimshauri Junior.

“Nitulie kwa huu ujinga aliyonifanyia?Hamna hilo,leo naua mtu.”Junior alisimamia nia yake.

“We humjui Hans,nia yake ni sisi kuaibika mbele ya demu,sasa badala ya kumuua kwa nini nay eye keshokutwa anapoenda kukutana na demu asiaibike?.”Frd alitoa wazo ambalo lilimfanya Junior kukaa kitako na kuona kama ni wazo lililojitosheleza.

“Eti eeh. Na yeye tumfanyizie nini?.”Junior akili ilirudi.

“Mimi aisee siwezi Si wajua dini yangu haniruhusu kulipa kisasi japo nilimpania?Siwezi kufanya hivyo,ila ukitaka msaada,mimi nitakupatia.”Fred alionesha wazi anakaa mbali juu ya mpango ule.

“Nitafanya mwenyewe.Lazima atalipa bwege yule. Uongo kaka? Yeye kaniaibisha vyote vile,kwa nini na mimi nimwonee huruma?Lazima alipe.”Junior alipitisha mawazo yake huku akihitaji msaada wa mawazo hayo hata kwa dereva wa taksi.

“Kwa lichofanya,hata kama ni mimi,ningelipa tu!Dini ingekaa kando.”Dereva naye alionesha umafia wake.

“Sasa ngoja aon zamu yake.”Junior aliweka kituo cha maongezi yale ambayo kwa Fred yalikuwa yanafaida kubwa.

******

SAA MOJA NA NUSU LILILOPITA.

Wakati Junior anatoka mule ndani anamoishi na wakina Hans,alianza kufuatiliwa kwa ukaribu kabisa Moses Frank,kijana machachari wa Ban Diho.

Mose alikuwa anamfatilia Junior kwa makini sana. Na kila hatua ya msingi ambayo Junior alikuwa anaipiga,Mose alikuwa anawapa taarifa rafiki zake.

Pale Junior alipofika kwa Eve.Mose alitoa taarifa,na hata alipoona wanatembea kwa miguu,alitoa taarifa hizo na kutaja mahali ambapo Junior na mshirika wake wanapita.

Taarifa hizo zikaenda na kwenda hadi pale Junior na Eve walipofika eneo moja lenye watu wengi sana. Na watu hao ndio wakataka Junior awakung’utie gitaa.

Ndani ya watu hao,kulikuwa na wengine wametumwa kwa ajili ya kumpapulisha Junior afanye hivyo.

Junior alipoona ni bora awape burudani,ndipo kijana mmoja alipewa chupa ya maji na Sunday Magembe.

Chupa ile ya maji,Sunday alikuwa kaipiga sindano kwa kuminyia dawa moja ya asili,au ya miti. Dawa ile ilikuwa inauwezo wa kumfanya mtu aharishe ndani ya dakika zisizopungua ishirini baada ya kuigida.

Haijulikani anatoa wapi dawa hizo,lakini Sunday alikuwa ni fundi wa mambo yale na ndio maana Ban alimuamini na kumkabidhi jukumu lile.

Junior naye hakuchunguza sana juu ya ile chupa aliyopewa na mtu asiyemjua.Yeye aligida maji yale na baada ya dakika mbili,mambo yakageuka na kubadili hewa ya pale.

Wakina Ban walipoona wamekamilisha kazi yao,walimpigia simu Fred aje aone mtu waliyemtuma wamuaibishe. Na Fred alipofika,alilidhika na kazi iliyofanyika ila huruma ilimuingia baada ya kumuona Junior akitambaa kwa sababu ya tumbo kumshika.

Hapo mwanzo alitaka kuona Junior anajisaidia mbele ya watu,lakini alijifikiria ni kwa nini afanye yale kwa mtu ambaye kazi yake ilikuwa ni kumcheka na kumtania?Kamwe hakushiriki kwenye kumuaibisha . Mawazo hayo ndio yalimfanya Fred kumuwahi Junior na kumuingiza kwenye taksi.

Sasa walishafika yalipo makazi yao na walimkuta Hans akiwa hana habari zozote zaidi ya jamaa yule kuchat na watu wake kwa kupitia simu.

“Vipi tena? Mbona leo mapema? Au na wewe umeungua makalio”.Hans alitania baada ya Junior kuingia.

“Wewe subiri tu!.”Junior alijibu kifupi na kukaa kitandani kwake huku zoezi la kuvua viatu vyake likifuata.

Hans hakufatilia maneno yale na wala hakuyatilia maanani zaidi ya kuendelea kufanya yake hadi pale alioona kalidhika

Kesho yake Junior akiwa na wakina Hans huko wanaposoma,alianza kutaniwa na watu ambao walishuhudia tukio zima lilivyokwenda.

“Jamaa gitaa zito hadi unajiachia mwenyewe.Ha haa.”Maneno kama hayo,Junior alikutaa nayo sana. Lakini maswali yakabaki kwenye kichwa cha Suarez pamoja na Hans.Kwa nini Junior ataniwe vile?

“Vipi kijana,mbona watu wanakuzonga hivyo?.”Suarez alitupa swali na Hans aliweka sikio vizuri kusikia kitakachomtoka Junior.

“We acha tu ndugu yangu.”Junior alijibu swali lile kiuchovu na kwa upole uliochanganyika na hali ya kujihurumia.Yote hiyo ni kwa sababu ya mzomeo uliokuwa unaendelea kumkuta pale alipokuwa anatembea na wale rafiki zake.

“Nini tena? Mbona umeishia kusikitika?.”Sua alizidi kuchimba.

“Daah!Jana yalinikuta yaliyomkuta Fred bwana.”Baada ya majibu hayo,Hans alishindwa kuvumilia kibana kicheko balikukiachia kitoke kwa uwezo wake wote.

“Kwa hiyo na wewe uliungua?.”Swali hilo toka kwa Suarez ndilo lililozidisha kicheko kwa Hans na kufanya akili ya Junior ijengeke kuwa ni Hans ndiye aliyefanya yote yale.

“Dah!Heri ingekuwa kuungua aisee.Mwenzako kidogo nijisaidie mbele ya watu. Mashuzi yalikuwa yanatoka kama stendi ya mabasi.”Jibu lile baada ya kupoteza kicheko kwa Hans na lilete huruma, likaongeza vicheko hata kwa Fred aliyekuwa kimya muda mrefu akisikiliza maongezi yale.

“Kwa hiyo ikawaje?.”Swali linguine toka kwa Suarez.

“Ndiyo hivyo.Mbele ya mtoto Eve na watu kama mia hivi.Kamanda napiga honi kama shabiby au Scandinavia linataka kusepa.”Junior aliongea kama utani ,lakini alikuwa kapania kulipa kisasi kwa Hans na hasira zilimzidi kila alipokuwa anasikia sauti ya Hans ikicheka.

“Kwa hiyo ulijisaidia mwanangu mwenyewe.”Hans huku akiwa na hali ya kucheka,alimuuliza Junior aliyekuwa anamachungu juu yake.

“Tena bora unyamaze boya wewe.”Junior alijibu kwa hasira.

“Sasa ninyamaze nini? Hapo ukute linanihisi mimi ndiye nimefanya.Acha ujinga wewe,tafuta mwizi kwa mwizi kwa vithibitisho na si kunusa kama mwizi.”Hans alitoa hali ya utani na kuweka usiriaz katika suala lile.

“Hujahisiwa,ni kweli umefanya na ni tabia yako.Hata Fred ulimfanyia hivyo majuzi.”Junior alithibitisha hisia zake juu ya Hans.

“Oya eeh,masela. Tuacheni hizo bwana.Sisi marafiki,hali hii itafanya tugombane bure.”Sua alionesha wasiwasi wake hivyo akaamua kutuliza zogo lile.

“Huyo boya,kazi kusingizia watu tu! Huyu nilimunguza kwa sababu ya kauli zak chafu.Sasa wewe umenifanya nini?. Msilete uboya wenu,mkitaka bifu semeni na sio kujidai mnatoa kesi zisizo zangu hapa. Na hamnipati ng’oo.Leo silali na nyie,maana mnaweza kunibandika hata gundi ili kesho nisionane na mtoto.”Maneno yalimwagika Hans na hapohapo akafata njia yake ambayo ilimpeleka hadi anaposihi.

Huko chumbani,Hans alichukua begi dogo na kuweka nguo zake baadhi.Kisha kama kawaida akatega mambo kwenye kabati lake na kuacha ujumbe wa kutolifungua kabati lile kwani chochote chaweza kutokea.

Hans akahama kile chumba kwa muda kwa kuhofia anachoweza kuja kufanyiwa na wakina Junior usiku au siku hiyo.

****

Baada ya kuondoka na wakina Junior kuthibitisha hilo. Junior akashindwa kutafuta njia mbadala ya kulipa kisasi chake kwa Hans.

Njia zikamwishia kabisa,na ndipo alipoenda kwa Fred na kujaribu kupata ushauri.

“Sasa hapa nafanyaje Mzee wa Upako?.”Junior alitupa swali kwa Fred baada ya kueleza nia yake iliyomshinda.

“Ndio kama nilivyokwambia. Twende kujaribu kuwaona wakina Ban.Wale wanaweza kusaidia kwa sana.” Fred alitoa pendekezo ambalo Junior aliona bora afanye hivyo.

****

Baada ya dakika kadhaa,Junior na Fred walikuwa kwenye chumba cha Wagumu wakieleza shida iliyowapeleka.

“Dah!Wazee kitambo sana sijawaona.Ishu zinaendaje.”Kamanda mkuu wa kikosi cha Wagumu,bwana Ban Diho alikuwa anaongea na wale vijana wawili.

“Tupo aisee. Ila tumekuja tuna shida moja tu!.”Junior alienda moja kwa moja katika kazi iliyompeleka pale.

“Tunakuzikiliza mwanangu”.Ban akatoa ukumbi kwa Junior.Naye Junior bila kukwepesha akaeleza kile kilichompeleka pale.

“Kwa hiyo hamjui Hans kaenda wapi,si ndio eeh.”Ban aliuliza baada ya kupata maelezo ya kina kutoka kwa Junior.

“Ndio hivyo,halafu kaaribu mambo ndio kakimbia.Na demu ankutana naye tumoro,hivyo mimi nataka na yeye kesho yamkute.”Junior akakomelea nia yake.

“Okey. Kwa kuwa umechelewa kuja halafu kazi yenyewe inamuda mchache,basi tuachie elfu sabini ili tupige kazi.”Ban alitoa pendekezo ambalo Junior alilipinga vikali huku akionesha wazi kuwa hicho kiasi ni kikubwa sana kwa kazi ile.

“Oya ongea na mwenzako bwana. Kama mnaweza,kapigeni hiyo ishu wenyewe.Sisi hatuna cha kuwasaidia.”Ban alimuelekezea maneno hayo Fred.

“Kwani we Junii unataka kulipa kiasi gani?.”Fred alimuuliza Junior mbele ya wakina Ban.

“Mi labda niwpe thelethini tu! Tena naitoa kwa sababu basi tu!.”Junior alimjibu Fred.

“Kama ni thelathini,basi sisi tutakutafutia tu huyu jamaa yupo wapi,na tutakupa cha kufanya.”Ban alitoa msimamo wa kundi lao.

“Aaag! Sasa ndio mtakuwa mmefanya nini? Mi sitaki hiyo,nataka kazi yote mpige halafu mnipe na taarifa jinsi ilivyokuwa.”Junior alipingana na ile kauli ya Ban.

“Hapo Junii hutuelewi.Hiyo elfu sabini kwako utaona ndogo kwa kitu tutakachofanya. Huyo Hans wako atalia kama mtoto mdogo. Halafu hatutokuhadithia,ni wewe wenyewe utashuhudia jinsi jamaa anavyotaabika.”Sunday aliingilia yale maongezi ili kumvuta mteja wao.

“Okey.Poa basi.Mimi na elfu hamsini,nifanyieni kwa hiyo wazee.”Junior aliingia mwenyewe mtegoni bila kujua hata Fred yupo katika biashara hiyo.

“Aaag,kaka fanya sabini bwana.Wewe mwenyewe si unacheki tupo wangapi?.”Ban alimvuta Junior ali afanye vile anavyotaka.

“Oya tunapoteza muda. Mi nakuongezea elfu ishirini,halafu tukifika home,utanirudishia.”Fred alimaliza utata ambao ulikuwa unaendelea kwa muda ule.

“Poa.Nitakupa baada ya wiki moja kwa kuwa kwa sasa nipo majalala kiaina.”Junior alikubaliana na wazo la Fred na kisha wakafanya kama inavyotakiwa kufanywa.

“Hayo ndio mambo sasa. Kesho tutakupigia simu ni wapi uje ili umuone ndugu yako anavyoumia.Ikibidi njoo na kamera kabisa.”Ban alimaliza maongezi yale ya kijinga,na kumuacha Junior hana swali tena.

Fred na Junior wakajikusanya nguvu zao na kuanza kutoka mule chumbani kwaajili ya kuelekea kwao.

Baada ya mwendo kidogo kule nje ya chumba,Fred alizuga kama kasahau kitu kule chumbani kwa akina Ban walipotoka,hivyo alimuomba Junior amsubiri mara moja kwa ajili ya kuchukua kitu hicho.

Haikuwa kweli kuwa kasahau kitu,yeye alirudi kule kwa ajili ya kuchukua hela yake. Na kweli wakina Ban wakampatia bila hiyana.Fred akarudi alipomuacha Junior.

****

Huku kwa akina Ban,timu ikapangwa kama kawaida.Waliona jinsi kumpata Hans kwa muda ule,itakuwa ni shida.Hivyo walichukua jukumu la kwenda kummendea Eve. Eidha Eve angemfata Hans au Hans angemfata Eve,hiyo ingekuwa rahisi kwao kuwafatilia wale jamaa.Kazi ya upepelezi huo,ikaenda kama kawaida kwa Moi Shabala na Moses Frank.

Sunday Magembe,alipewa jukumu lake tena la kutafuta dawa na Ban yeye alikuwa ni mzee wa kutafuta maeneo tu!.

Kazi hiyo ilianza mara mja hasa kwa Ban na Sunday. Moi na Mose,wao kazi yao ilikuwa ianze kesho.

*****

Hakuna aliyejua Hans yupo wapi hadi kesho yake ilipofika ambapo Hans alionekana maeneo anayoishi Eve akiwa kakodi taksi kwa ajili ya kumchukua mrembo yule.

Moi na Mose walipoona kuwa kuna haja ya kuchukua usafiri,waliagiza haraka bodaboda ije ili iwe rahisi kwao kuwafatilia waendako.

“Baada ya dakika kama kumi na tano,Eve alitoka ndani anapoishi na kuifata taksi iliyokuwa inamsubiri. Akapanda ndani yake na safari ilianza huku Mose na Moi wakiwa makini kuifatilia ile taksi na kuwapa taarifa kila mara wenzao.

Walijua kuwa Hans anapenda sana kumpeleka Eve sehemu zenye maji,hivyo kuna barabara ambayo walipita,walijua wazi kuwa hawa wanaelekea sehemu fulani. Hisia hizo,zikasafirishwa na kuwafikia Sunday na Ban.

Nao wakina Sunday,wakajipanga kwa ajili ya mashambulizi hayo kwa kukusanya vitu muhimu na kwenda sehemu hiyo.

Hisia zao zilikuwa ni kweli.Baada ya dakika kadhaa za bodaboda na taksi kuwa barabarani,hatimaye waliingia mahala ambapo palikuwa ni kusudio lao.

Watu walikuwa wengi sana katika sehemu ile ambao ulikuwa ni ufukwe wa Mikadi.Ufukwe ambao hauna kawaida ya kujaza sana watu kama ule wa Coco.

Hans alkuwa ni mwenye tabasamu kila mara pale alipokuwa akimuangalia Eve jinsi alivyokuwa kapendeza.

WALIJUA kuwa Hans anapenda sana kumpeleka Eve sehemu zenye maji,hivyo kuna barabara ambayo walipita,walijua wazi kuwa hawa wanaelekea sehemu fulani. Hisia hizo,zikasafirishwa na kuwafikia Sunday na Ban.

Nao wakina Sunday,wakajipanga kwa ajili ya mashambulizi hayo kwa kukusanya vitu muhimu na kwenda sehemu hiyo.

Hisia zao zilikuwa ni kweli.Baada ya dakika kadhaa za bodaboda na taksi kuwa barabarani,hatimaye waliingia mahala ambapo palikuwa ni kusudio lao.

Watu walikuwa wengi sana katika sehemu ile ambao ulikuwa ni ufukwe wa Mikadi.Ufukwe ambao hauna kawaida ya kujaza sana watu kama ule wa Coco.

Hans alkuwa ni mwenye tabasamu kila mara pale alipokuwa akimuangalia Eve jinsi alivyokuwa kapendeza.

“Leo umependeza sana.”Hans alimwaga sifa kwa kimwana yule ambaye alichanua tabasamu pana usoni pake.Hiyo ni baada ya kupata sehemu moja yenye kivuli na kukaa.

“Nawe umependeza sana. Hans ila na maongezi na wewe,tofauti na yale ya siku zote.”Eve alitoa sifa na kufunguka kilichomkutanisha na Hans kwa wakati ule.

“Niambie tu!.”Hans alijibu bila kusitasita.

“Embu nisubiri kwanza nikachukue pale koni.”Eve alinyanyuka na akiwa na mavazi yake ya ufukweni na kwenda sehemu moja ambayo kunauzwa koni.

Huku nyuma Hans akabaki peke yake akipunga upepo na ndio muda huo huo Sunday aliutumia kufanya yake.

Sunday alienda pale alipo Hans na kisha kwa utaalamu mkubwa alijidai kajikwaa na kumdondokea Hans kwenye mapaja.

Kitendo kile kilimshitua Hans lakini hali ilimrudi na kuwa nzuri pale alipogundua ni Sunday. Alimsalimia kwa furaha na Sunday naye akaitikia salamu ile huku akimuomba msamaha kwa kilichotokea.

Baada ya salamu hiyo na msamaha,Sunday alititia eneo lile kwa furaha kubwa kwa kuamini mchezo alioucheza umetimia bila shaka.

Ukweli ni kwamba,wakati Sunday anamdondokea Hans,alikuwa kashika sindano ndogo zile za kubania karatasi. Sindano ile ndio alikuwa kaipaka dawa aliyokusudi.

Kitendo cha kumdondokea,kilimpa upenyo Sunday kumchoma kidogo Hans bila ya yeye kuhisi maumivu makali kama yale ya kumdondokea.

Baada ya kufanikiwa kumchoma na kisindano kile,aimuomba msamaha na kuondoka mahala pale akimuacha Hans hana hili wala lile.

Dakika tatu mbele,Eve alirudi na makopo mawili ya koni.Moja akampatia Hans na linguine akabaki nalo yeye,kisha taratibu wakaanza kujiburudisha.

“Mimi nachotaka kujua ni kama unahusika na mambo yaliyowatokea Fred na Junior.Maana wote wanalalamika kuwa ni wewe ndiye umefanya,sasa niambie ukweli wote ikibidi niwaite wote ili mpatane maana mtu kama Junior aliapa atakuua.”Eve alianzisha maongezi hayo baada ya kubugia vijiko kadhaa vya koni aliyonunua.

“Kwa hiyo na wewe unaamini.”Hans aliuliza.

“Naweza kuamini.Lakini najua huwezi kufanya vile kama hujachokozwa.”Eve aliweka wazi hisia zake.

“Okey.Kiukweli kabisa,Fred ni mimi ndiye nimefanya lakini Junior sifahamu aliyefanya.”Hans alijibu na kusikiliza Eve atatoa maamuzi gani.

“Sasa kwa nini ulimfanyia vile Fred?.”Eve alitupa kete nyingine ya swali.

“Wanazingua wale. Ujue siku ile kule Coco eti walinirekodi kwenye kamera wakati najirusha kwenye maji,bsi ikawa utani ni utani.Huyu Fred akawa hadi ananitukana,ndio nikaona bora nilipe.”Hans akatoa sababu ambayo ilimfanya Eve acheke kidogo na kuendelea.

“Ujue ni watoto sana. Sasa hiyo inawasaidia nini?.”Swali lilitupwa lakini lilikuwa halina kitu zaidi ya Hans kunyamaza huku kainamisha kichwa chake.

“We Hans,si nakuuliza?.”Eve alimshtua Hans lakini Hans kichwa kilikuwa vilevile.

“Wewe.”Eve aliita huku anamsukuma.

“Mmmh.”Masikini Hans aliitika huku udenda unamtoka kama vile teja.

“Khaaa! Hivi nyie watu mna matatizo gani? Ona huyu naye leo.”Eve alilalamika peke yake bila mtu yeyote kumfatilia.

“Kichefuchefu.”Hans alisema maneno hayo kwa sauti ya chini kabisa.Sauti ambayo ilimfanya Eve kuuliza tena alichokisema huku anapeleka uso wake karibu namdomo wa Hans ili asikie vizuri.

Kabla hata Hans hajarudia lele neno la kichefuchefu. Eve alitapikiwa usoni na matapishi yaliyotoka mdomoni kwa Hans.

Matapishi yale yalitoka kwa wingi kwani yalijumuisha vyakula vyote alivyokula Hans tangu asubuhi ya siku ile. Yote hayo yaliishia mwilini kwa Eve ambaye alikuwa kaganda kama barafu pale kitendo kile kilipokuwa kinatokea.

Watu ambao walikuwa maeneo yale,walishindwa kuvumilia kucheka na kushangilia kwa kile walichokuwa wanakiona,amahakika Hans alipatikana na aliaibika.

Baada ya kutapika,Hans aliyekuwa kama teja,alidondokea Eve miguuni na kumfanya Eve asiweze kusimama haraka kwa muda ule.

Macho ya Hans yakiwa yaona kwa mbali,ndipo alipomuona na Junior akiwa mmoja wa watu ambao wanamcheka,tena yeye alikuwa anapiga na picha,sijui za ukumbusho au nini.

Baada ya Hans kumuona Junior,aliongea kwa sauti ya chini huku anamuoneshea kidole Junior. Hapo hapo,usingizi mzito ukambeba.

Kazi ikabaki kwa Eve kujipapatua ili ajitoe mwilini mwa Hans ambaye alikuwa kalala usingizi wa hatari.

****

Ni baada ya dakika zisizopungua mbili,ndipo aibu ile ilipomtoka Eve. Matapishi ambayo ametapikiwa na Hans alienda kwenye maji ya ufukwe ule na kujisafisha na Eve alirudi katika hali kiasi fulani. Sasa ikabaki kazi ya kumnyanyua Hans aliyekuwa kajilaza pale kichangani hajitambuni.

Ilikuwa si shuhuri ya kitoto kumnyanyua mtu kama Hans,kwani kila aliyeombwa msaada wa kufanya hivyo,alihofiwa kutapikiwa. Akili kumkichwa zikatakiwa kuchuwa nafasi katika kichwa Eve.

Alichoona cha maana mwanamke yule wa shoka ni kukimbilia nje na kumtafuta dereva taksi mmojawapo na kuja naye hadi pale alipomuacha Hans amelala.

“Haikuwa rahisi wa kitoto kumbeba jamaa yule aliyekuwa kalala fo fo fo,hajitambui wala hajielewi yupo wapi kwa muda ule.

Baada ya kufanikiwa kumpandisha katika taksi,safari iliyofuata ilikuwa ni ya kwenda hospitali.Na moja kwa moja walimpeleka katika hospitali fulani iliyopo pale Msasani na mara moja Hans akaanza kupewa huduma ya kwanza ambayo ilichukua dakika kama kumi na tano.

Dakika kadhaa nyingine,Hans alizinduka mna kuanza kushangaa ilikuwaje mpaka akawa pale. Baada ya kuvuta kumbukumbu,ndipo alipokumbuka yale yote yaliyotokea kwenye ufukwe Mikadi,na hasira zilimpanda zaidi alipokumbuka sura ya Junior ikimchukua picha.

Kitanda cha hospitali alikiona si mahala pake tena. Na kwa kuwa alikuwa hajatundikiwa dripu,aliona ni bora anyanyuke haraka ili aende walipo wakina Junior na kutaka maelezo ya kina ya kwa nini kafanya yale yote.

Alinyanyuka na kuvaa viatu vyake.Kisha alitoka nje na kukutana na Eve akiwa kwenye benchi la kusubiria huduma za pale hospitali.

Alimpita bila hata kuongea naye,kitendo kilichomfanya Eve ashangae na kumuita kwa nguvu. Lakini Hans ni kama hakusikia sauti ile na wala hakuwa na mpango nayo zaidi ya kwenda anapojua yeye.

Eve akaona hayo mengine tena. Alichofanya ni kumkimbilia kisha akamshika began a kumuuliza kulikoni.

“Wewe na wale wajinga kule,mmepanga kuniaibisha. Mmmeniwekea madawa yenu kwenye koni ili nitapike na kulala,si ndio ee.”Hans alimjibu Eve kwa hasira.

“Hee jamani,yamekuwa hayo tena.Mimi naweza kufanya hivyo jamani?.”Eve alikumbwa na taharuki ya ajabu baada ya kusikia laumu zile zilizouvunja moyo wake.

“Ushindwe kufanya hivyo kwani wewe nani?Wewe Malaika?Wewe si binadamu kama mimi tu! Mwenye kinyongo na watu na wenye chuki zilizojikita moyoni mwake. Utashindwa nini kuniwekea madawa? Kuna kitu kinamshinda mwanamke? Kuna kitu kitakushinda wewe kama hunipendi mimi?.”Hans alilopoka maneno mengi na bila hata kusubiri Eve ajitetee,aliuputa mokono wa mrembo yule na kuanza kuondoka.

“Na mwenzako Junior uliyepanga naye mchezo wote,nilimuona akinichukua picha.Sasa atakuhadithia kitakachomkuta.Wajinga nyie.”Msumali wa maneno ulikomelewa na kinywa cha Hans,kisha jamaa yule mguu na njia ukashika nafasi huku akimuacha Eve kakamata kiuno kama anaangalia ngoma ya Kisambaa au Wadigo.Hakika alipatikana,uso ulimshuka kama ngozi ya chini ya shingo ya ng’ombe.

****

Walijua kuwa Hans anapenda sana kumpeleka Eve sehemu zenye maji,hivyo kuna barabara ambayo walipita,walijua wazi kuwa hawa wanaelekea sehemu fulani. Hisia hizo,zikasafirishwa na kuwafikia Sunday na Ban.

Nao wakina Sunday,wakajipanga kwa ajili ya mashambulizi hayo kwa kukusanya vitu muhimu na kwenda sehemu hiyo.

Hisia zao zilikuwa ni kweli.Baada ya dakika kadhaa za bodaboda na taksi kuwa barabarani,hatimaye waliingia mahala ambapo palikuwa ni kusudio lao.

Watu walikuwa wengi sana katika sehemu ile ambao ulikuwa ni ufukwe wa Mikadi.Ufukwe ambao hauna kawaida ya kujaza sana watu kama ule wa Coco.

Hans alkuwa ni mwenye tabasamu kila mara pale alipokuwa akimuangalia Eve jinsi alivyokuwa kapendeza.

“Leo umependeza sana.”Hans alimwaga sifa kwa kimwana yule ambaye alichanua tabasamu pana usoni pake.Hiyo ni baada ya kupata sehemu moja yenye kivuli na kukaa.

“Nawe umependeza sana. Hans ila na maongezi na wewe,tofauti na yale ya siku zote.”Eve alitoa sifa na kufunguka kilichomkutanisha na Hans kwa wakati ule.

“Niambie tu!.”Hans alijibu bila kusitasita.

“Embu nisubiri kwanza nikachukue pale koni.”Eve alinyanyuka na akiwa na mavazi yake ya ufukweni na kwenda sehemu moja ambayo kunauzwa koni.

Huku nyuma Hans akabaki peke yake akipunga upepo na ndio muda huo huo Sunday aliutumia kufanya yake.

Sunday alienda pale alipo Hans na kisha kwa utaalamu mkubwa alijidai kajikwaa na kumdondokea Hans kwenye mapaja.

Kitendo kile kilimshitua Hans lakini hali ilimrudi na kuwa nzuri pale alipogundua ni Sunday. Alimsalimia kwa furaha na Sunday naye akaitikia salamu ile huku akimuomba msamaha kwa kilichotokea.

Baada ya salamu hiyo na msamaha,Sunday alititia eneo lile kwa furaha kubwa kwa kuamini mchezo alioucheza umetimia bila shaka.

Ukweli ni kwamba,wakati Sunday anamdondokea Hans,alikuwa kashika sindano ndogo zile za kubania karatasi. Sindano ile ndio alikuwa kaipaka dawa aliyokusudi.

Kitendo cha kumdondokea,kilimpa upenyo Sunday kumchoma kidogo Hans bila ya yeye kuhisi maumivu makali kama yale ya kumdondokea.

Baada ya kufanikiwa kumchoma na kisindano kile,aimuomba msamaha na kuondoka mahala pale akimuacha Hans hana hili wala lile.

Dakika tatu mbele,Eve alirudi na makopo mawili ya koni.Moja akampatia Hans na linguine akabaki nalo yeye,kisha taratibu wakaanza kujiburudisha.

“Mimi nachotaka kujua ni kama unahusika na mambo yaliyowatokea Fred na Junior.Maana wote wanalalamika kuwa ni wewe ndiye umefanya,sasa niambie ukweli wote ikibidi niwaite wote ili mpatane maana mtu kama Junior aliapa atakuua.”Eve alianzisha maongezi hayo baada ya kubugia vijiko kadhaa vya koni aliyonunua.

“Kwa hiyo na wewe unaamini.”Hans aliuliza.

“Naweza kuamini.Lakini najua huwezi kufanya vile kama hujachokozwa.”Eve aliweka wazi hisia zake.

“Okey.Kiukweli kabisa,Fred ni mimi ndiye nimefanya lakini Junior sifahamu aliyefanya.”Hans alijibu na kusikiliza Eve atatoa maamuzi gani.

“Sasa kwa nini ulimfanyia vile Fred?.”Eve alitupa kete nyingine ya swali.

“Wanazingua wale. Ujue siku ile kule Coco eti walinirekodi kwenye kamera wakati najirusha kwenye maji,bsi ikawa utani ni utani.Huyu Fred akawa hadi ananitukana,ndio nikaona bora nilipe.”Hans akatoa sababu ambayo ilimfanya Eve acheke kidogo na kuendelea.

“Ujue ni watoto sana. Sasa hiyo inawasaidia nini?.”Swali lilitupwa lakini lilikuwa halina kitu zaidi ya Hans kunyamaza huku kainamisha kichwa chake.

“We Hans,si nakuuliza?.”Eve alimshtua Hans lakini Hans kichwa kilikuwa vilevile.

“Wewe.”Eve aliita huku anamsukuma.

“Mmmh.”Masikini Hans aliitika huku udenda unamtoka kama vile teja.

“Khaaa! Hivi nyie watu mna matatizo gani? Ona huyu naye leo.”Eve alilalamika peke yake bila mtu yeyote kumfatilia.

“Kichefuchefu.”Hans alisema maneno hayo kwa sauti ya chini kabisa.Sauti ambayo ilimfanya Eve kuuliza tena alichokisema huku anapeleka uso wake karibu namdomo wa Hans ili asikie vizuri.

Kabla hata Hans hajarudia lele neno la kichefuchefu. Eve alitapikiwa usoni na matapishi yaliyotoka mdomoni kwa Hans.

Matapishi yale yalitoka kwa wingi kwani yalijumuisha vyakula vyote alivyokula Hans tangu asubuhi ya siku ile. Yote hayo yaliishia mwilini kwa Eve ambaye alikuwa kaganda kama barafu pale kitendo kile kilipokuwa kinatokea.

Watu ambao walikuwa maeneo yale,walishindwa kuvumilia kucheka na kushangilia kwa kile walichokuwa wanakiona,amahakika Hans alipatikana na aliaibika.

Baada ya kutapika,Hans aliyekuwa kama teja,alidondokea Eve miguuni na kumfanya Eve asiweze kusimama haraka kwa muda ule.

Macho ya Hans yakiwa yaona kwa mbali,ndipo alipomuona na Junior akiwa mmoja wa watu ambao wanamcheka,tena yeye alikuwa anapiga na picha,sijui za ukumbusho au nini.

Baada ya Hans kumuona Junior,aliongea kwa sauti ya chini huku anamuoneshea kidole Junior. Hapo hapo,usingizi mzito ukambeba.

Kazi ikabaki kwa Eve kujipapatua ili ajitoe mwilini mwa Hans ambaye alikuwa kalala usingizi wa hatari.

****

Ni baada ya dakika zisizopungua mbili,ndipo aibu ile ilipomtoka Eve. Matapishi ambayo ametapikiwa na Hans alienda kwenye maji ya ufukwe ule na kujisafisha na Eve alirudi katika hali kiasi fulani. Sasa ikabaki kazi ya kumnyanyua Hans aliyekuwa kajilaza pale kichangani hajitambuni.

Ilikuwa si shuhuri ya kitoto kumnyanyua mtu kama Hans,kwani kila aliyeombwa msaada wa kufanya hivyo,alihofiwa kutapikiwa. Akili kumkichwa zikatakiwa kuchuwa nafasi katika kichwa Eve.

Alichoona cha maana mwanamke yule wa shoka ni kukimbilia nje na kumtafuta dereva taksi mmojawapo na kuja naye hadi pale alipomuacha Hans amelala.

“Haikuwa rahisi wa kitoto kumbeba jamaa yule aliyekuwa kalala fo fo fo,hajitambui wala hajielewi yupo wapi kwa muda ule.

Baada ya kufanikiwa kumpandisha katika taksi,safari iliyofuata ilikuwa ni ya kwenda hospitali.Na moja kwa moja walimpeleka katika hospitali fulani iliyopo pale Msasani na mara moja Hans akaanza kupewa huduma ya kwanza ambayo ilichukua dakika kama kumi na tano.

Dakika kadhaa nyingine,Hans alizinduka mna kuanza kushangaa ilikuwaje mpaka akawa pale. Baada ya kuvuta kumbukumbu,ndipo alipokumbuka yale yote yaliyotokea kwenye ufukwe Mikadi,na hasira zilimpanda zaidi alipokumbuka sura ya Junior ikimchukua picha.

Kitanda cha hospitali alikiona si mahala pake tena. Na kwa kuwa alikuwa hajatundikiwa dripu,aliona ni bora anyanyuke haraka ili aende walipo wakina Junior na kutaka maelezo ya kina ya kwa nini kafanya yale yote.

Alinyanyuka na kuvaa viatu vyake.Kisha alitoka nje na kukutana na Eve akiwa kwenye benchi la kusubiria huduma za pale hospitali.

Alimpita bila hata kuongea naye,kitendo kilichomfanya Eve ashangae na kumuita kwa nguvu. Lakini Hans ni kama hakusikia sauti ile na wala hakuwa na mpango nayo zaidi ya kwenda anapojua yeye.

Eve akaona hayo mengine tena. Alichofanya ni kumkimbilia kisha akamshika began a kumuuliza kulikoni.

“Wewe na wale wajinga kule,mmepanga kuniaibisha. Mmmeniwekea madawa yenu kwenye koni ili nitapike na kulala,si ndio ee.”Hans alimjibu Eve kwa hasira.

“Hee jamani,yamekuwa hayo tena.Mimi naweza kufanya hivyo jamani?.”Eve alikumbwa na taharuki ya ajabu baada ya kusikia laumu zile zilizouvunja moyo wake.

“Ushindwe kufanya hivyo kwani wewe nani?Wewe Malaika?Wewe si binadamu kama mimi tu! Mwenye kinyongo na watu na wenye chuki zilizojikita moyoni mwake. Utashindwa nini kuniwekea madawa? Kuna kitu kinamshinda mwanamke? Kuna kitu kitakushinda wewe kama hunipendi mimi?.”Hans alilopoka maneno mengi na bila hata kusubiri Eve ajitetee,aliuputa mokono wa mrembo yule na kuanza kuondoka.

“Na mwenzako Junior uliyepanga naye mchezo wote,nilimuona akinichukua picha.Sasa atakuhadithia kitakachomkuta.Wajinga nyie.”Msumali wa maneno ulikomelewa na kinywa cha Hans,kisha jamaa yule mguu na njia ukashika nafasi huku akimuacha Eve kakamata kiuno kama anaangalia ngoma ya Kisambaa au Wadigo.Hakika alipatikana,uso ulimshuka kama ngozi ya chini ya shingo ya ng’ombe.

HANS alikamata usafiri wa bajaji na moja kwa moja akaomba umpeleke yalipomakazi yake ya zamani.Kule ambapo alihama kwa kuhofia wakina Junior wangemtenda.

Baada ya nusu saa,alikuwa tayari chumbani na kwa bahati nzuri aliwakuta rafiki zake wote wametulia wanafanya yao.

“Ehee,we boya.Kwa hiyo mkamuua kupanga na yule mchawi wa kike ili mniwekee dawa kwenye koni,nikila nitapike,si ndio ee.”Hans alilianzisha baada ya kufika mule chumbani.

“Acha kumtukana mke wangu,nitakuharibia balaa.Wewe ulichonifanyia kizuri ee.”Junior alijibu mapigo bila kuogopa hasira alizokuwa nazo Hans.

“Anamuita Malaika wangu Mchawi?.”Fred naye akanunua ugomvi.

“Mbwa nyie mmepanga na yule fala kuniaibisha mimi?Leo mtanitambua.”Hans hakuwa na subira juu ya maamuzi yake zaidi ua kwenda pale kitanda cha chini na kuanza kumshushia ngumi za haraka Junior ambaye hakutegeea kama Hans angeweza kumvamia kwa muda ule mfupi.

Fred alipoona mwenza ke Junior anapokea kichapo cha kushtukiza halafu mpango walipanga wote na isitoshe yeye ndiye anahusika sana,aliruka toka kwenye kitanda chake cha juu na kisha akamkumba Hans na kumrushia kwa pembeni na bila kusita alijiweka sawa kwa kunja ngumi tayari kwa mpambano baina yake na Hans. Mtakatifu Fred alikuwa kabadilika na kuwa mtaka tifu na yeyote.

Junior alinyanyuka haraka kitandani huku akiwa na maumivu ya ngumi nyingi za mbavu na tumbo alizopigwa na Hans,na moja kwa moja akataka kumkumba Hans pale alipo,lakini alikutana na upinzani mkubwa kutoka kwenye mikono ya Suarez,ikimuamulia asifanye lile alilokusudia.

“Mnataka kufanya nini sasa?Mnataka kufanya nini? Mnataka kupigana au kuongea yaishe kistaarabu?Nijibuni sasa hivi ili niwaachie ukumbi.”Suarez aliongea kwa sauti ya juu iliyochanganyikana na hasira ndani yake.

“Nakwambia leo naua mtu humu.Tuachie ukumbi.”Hans alijibu swali la Suarez naye akiwa na hasira.

“Tuachie ukumbi tumuoneshe huyu choko kuwa na sisi tuliumia kama yeye.”Fred alijibu kwa ujasiri bila kujali yatakayomkumba mbele.

“Okey.”Suarez alijibu nakutoka pale katikati aliposimama na kwenda mlango wa kutokea. Hapo aliuchomoa ufunguo wa mlango ule na kutoka nao nje,ambapo aliufunga mlango ule kwa nje na kuondoka zake akiwaacha wakina Hans wanatunishiana misuli mule ndani.

Sasa Hans alikuwa uso kwa uso na Fred pamoja Junior. Licha ya kutapika chakula karibu chote,lakini alikuwa anajiamini kuwa anaweza kupambana na sura zile ambazo zilikuwa zimejishindilia chakula muda si mrefu.

Hatimaye mpambano ukaanza kwa Hans kutaka kumfuata Junior maana ndiye alikuwa anahasira naye zaidi na wakati huo alisahau kuwa Fred naye anahasira na yeye kwa kumuunguza siku chache zilizopita.

Kitendo cha kumfata Junior pale alipo,kilikutana na upinzani mkubwa wa Fred kwani alirusha ngumi moja ambayo ilienda vizuri na kumkuta Hans kwenye paji la uso,au komwe au forehead kwa kiingereza,na ngumi hiyo ilimfanya Hans kutoamini kama kapigwa yeye na tena kapigwa na Fred mtu ambaye ujanja kamfundisha yeye.

“Boya umenipiga ngumi?.”Hans aliuliza huku haamini kilichotokea.

“Ulidhani nimesahau ulivyounguza suruali yangu?.”Fred alimuuliza huku anamfuata kimabavu Hans.

Hans akaona sasa kapatikana. Alichofanya ni kujitutumua ili apambane kiume sasa kwani alidhani Fred hawezi kupigana kutokana na ulokole wake,lakini ndiyo hivyo,Fred aliweka nia ya kumuumiza Hans.

Mara Hans alimrukia Fred kwa fujo kwa kumkumba na bega lake, ambapo alipiga maeneo ya tumboni kama wafanyavyo wanamieleka.Pigo lile lilimfanya Fred alie kama mbwa aliyepigwa na jiwe tumboni au kichwani.

Ni pigo moja linaloweza kukufanya utapike au utoe hewa chafu.Hans alimpa hilo Fred na kudondoka naye karibu kabisa na kwa Junior.

Junior alipoona mwenzake anasurubika,naye akaanza kumsaidia Fred kwa kumkanyaga Hans. Kwa kuwa Hans alikuwa juu na Fred chini,basi ilikuwa rahisi kwa Junior kumsurubisha Hans kwa kumkanyaga.

Hali ilikuja kumbadilikia Junior baada ya Hans kuudaka mguu wake na kuanza kunyanyuka huku bado kaushikilia. Wakati huo Fred alikuwa hoi pale chini kwa kipigo alichokipokea kwa Hans.

Sasa mguu wa Junior ulikuwa umekamatwa na Hans.Junior akawa hana mawazo ya haraka juu ya nini cha kufanya .Na wakati huo Hans alikuwa amenyanyuka wima, na kuanza kumsukumia ukutani ambapo Junior alikuwa anarudi nyuma huku anarukaruka kama kangaroo.

Walipofika ukutani,Hans alizidi kuutanua mguu wa Junior hadi akaonekana kama anapiga msamba. Junior uso ulikuwa katika kuchanganyikiwa na jinsi Hans alivyokuwa anamchanisha msamba,ndivyo Junior naye alikuwa anazidi kuumia.

“Nyie si makamanda,si mnaweza kupigana.Haya sasa,nipigeni.”Hans aliongea huku kamchanisha msamba Junior pale ukutani. Wakati huo Fred alikuwa akigaa gaa kwa maumivu pale chini.

Mara Hans aliuachia mguu wa Junior na kuanza kumwandamisha kwa makonde ya nguvu.Makonde ambayo Junior aliona ni bora achutame na kuziba kichwa chake kama vile ameona au anavamiwa na nyuki. Hans akawa ametawala kile chumba.

Zogo lile lilikuja kuisha baada ya mlango kufunguliwa na kuingia mkufunzi anayesimamia nidhamu kwa wanachuo, pamoja na waziri mkuu wa chuo kile ambaye ni Eve na huku nyuma alifatiwa na Suarez.

“Wewe embu muache ,mwenzako.”Mkufunzi alimfokea Hans huku anamfuata na kumuondoa pale alipokuwa anamwandamisha Junior kwa makonde.

“Nitawaua mimi. Mimi siyo wakunichezea kama huyu mnayemtuma aweke madawa kwenye chakula changu,nitawaua nawaambieni.”Hans Liongea huku akipumua kwa kasi kutokana na ngumi nyingi alizozirusha kumchosha.

“Nyie nyanyukeni hapo,nifateni ofisini.”Yule kiongozi alitoa amri na yeye akaanza kutoka mule chumbani.

Junior na Fred walinyanyukla taratibu na kuanza kumfata mkufunzi yule wakati huo Hans alishatoka. Eve na Saarez walikuwa wa mwisho.

*****

Huko ofisini,kesi ilisomwa na kila mtu aliongea sababu zake za kufanya yale yote lakini kamwe hawakuthubutu kuwataja wagumu au kumtaja Eve kuwa ndiye mwanamke wanayemgombania.

“Kwa hiyo wewe Junior nani aliyekuumiza tumbo?.”Yule muu wa nidhamu kwa wanafunzi alimuuliza Junior.

“Ni huyu hapa Hans.”Junior alijibu kwa uhakika.

“Sijafanya hivyo kwa huyu boya.Ila kwa huyu kweli mimi nimefanya.”Hans alijitetea huku anakubali kosa linguine.

“Kwa nini ulifanya hivyo?.”Mkufunzi alimuuliza Hans.

“Anamatusi na kejeli,nilikereka na tabia hiyo aliyonifanyia.”Hans alijibu.

“Na ni nani aliyekupa madawa hadi ukamtapikia Waziri?.”Mkufunzi alitupa swali kwa Hans.

“Ni huyu boya.Nilimuona kabisa ananipiga na icha wakati nasinzia.”Hans alijibu kwa kumtaja Junior.

“Ni kweli?.”Swali kwa mkufunzi kwenda kwa Junior.

“Ndiyo,mimi nilihusika kufanya hivyo lakini sikuweka kwenye koni bali najua mwenyewe nilichofanya atapike.”Junior alikubali kosa.

“Kwa nini ulifanya hivyo?.”Swali linguine kwenda kwa Junior.

“Ni kwa sababu yeye aliniwekea madawa ya kuharisha kwenye chakula changu.”Junior alijibu.

“Sasa mbona anakataa kuwa hajakuwekea? Au umemuhisi tu! Maana yeye hadi kakuona kwenye tukio.Wewe kwenye tukio lako alikuwepo nani ukimtoa Waziri?.”Mkufunzi alizidi kupekua ili apate jibu kamili.

Wakati huo Eve na Suarez nao walikuwepo wakifatilia ile kesi kwa makini.

“Sikuona mtu,ila baada ya kuumia sana,Eve alikuja na Fred na kuninyanyua pale nilipokuwepo.”Junior alijibu kwa usahihi swali lile.

“Waziri,ulimuita huyu Fred?.”Swali sasa likamgeukia Eve.

“Hapana.Mimi nilishangaa anajiunga na mimi kumuokoa Junior.”Eve nae alijibu kiusahihi swali lililomkabiri.

“Wewe Fred,ulijuaje kama Junior yupo pale?.”Fred naye aliulizwa lakini alikaa kimya.

“Okey.Labda swali gumu.Ngoja nijaribu hili. Unahusika na kumwekea Junior dawa ya kuhara?”.Fred aliulizwa swali na bila kusita alilijibu na kutoa sababu.

“Ndiyo nilihusika na nilifanya vile kwa kuwa alishiriki kwenye kushangilia pale nilipoaaibika. Na pia nilifanya vile ili nipate kampani ya kumkomoa huyu mjinga.”Fred alijibu swali la mkufunzi na kuwafanya Junior,Eve na Suarez kushikwa na butwaa.

“Nilijua tu!Mnazungukana wenyewe. Na uzuri mmeongea ukweli wenu,mmeokoka.”Mkufunzi aliyasema hayo huku akifunga kitabu kimoja kilichokuwa na makaratasi ambazo mara nyingi alikuwa anatolea barua za kusamisha wanachuo humo.

“Ina maana we boya ndiye uliyeniwekea dawa kwenye msosi?.”Junior allimgeukia Fred na kumuuliza swali hilo.

“Sio msosi,yale maji uliyopewa pale kabla hujaanza kupiga gitaa.Walewale niliokupeleka kwao,ndio waliiga mzigo mzima.”Fred aliongea na kumfanya Junior ashikwe na kigugumizi na wakati huo Eve na Suarez walikuwa hawaamini kama Fred naye kawa Mafia vile.

“Humu sitaki ugomvi kabisa. Nataka amani. Mmenusurika kusimamishwa chuo,msifanye nifanye hivyo,sawa?.”Mkufunzi alitoa rai yake na wote wakakubali lile suala kwa wakati ule,lakini walipanga kulianzisha baada ya kutoka mule.

“Na vilevile,huko mwendako,nikisikia mmepigana tu! Nakuja kuwasimamisha wote. Na hakuna kuhama chumba,wote mtakaa mulemule ili tuone mtafanya nini. Atakayemfanya kibaya mwenzake,wote mtaubeba msalaba,sawa?.”Mkufunzi aliongeza sheria iliyowanyong’onyeza wenye visasi.

Baada ya kesi ile,waliruhusiwa kutoka mule ofisini na kurudi chumbani kwao ambapo walikaa wamechuniana kama bi mkubwa na bi mdogo wamegombana

BAADA YA SIKU TATU.

Wakiwa hawana muda wa kuongea na kila mtu akiwa kivyake,mara kila mmoja kwa muda wake alipokea ujumbe kwa njia ya simu uklimtaka kufika eneo moja ambapo kulikuwa na ghorofa linajengwa. Ghorofa hilo siku hiyo lilisimamishwa kujengwa,hivyo meseji ile iliwaomba wale jamaa watatu waende pale.

Ulikuwa ni ujumbe kutoka kwa Eve na uliwataka kila mmoja afike pale muda wa saa nane mchana.

Japo ni ujumbe unaofanana lakini hakuna aliyejua kuwa Eve kawaita wote waende mahala pale. Kila mmoja alidhani ataenda pale peke yake. Kwa upande wa Hans yeye aliona ndio muda muafaka wa kwenda na kumwomba msamaha Eve kwa maneno aliyomtamkia siku mbili nyuma.

Huku Junor na Fred,wao waliwaza kwenda kutoa yao yaliyo moyoni.

Hatimaye saa saba na nusu ilipotimia,kile chumba cha hawa wanachuo kilikuwa hakina mtu bali wote walienda walipoitwa,kasoro Suarez ambaye yeye hakupata ujumbe wa Eve,ila naye hauwepo chumbani.

Muda huo wa saa saba ndipo kwenye lile ghorofa palitokea tafrani nyingine.Sura tatu zisizopendana zilikuwa zinaangaliana.

“Mmefata nini hapa.”Swali lilimtoka Hans.

“Niwashangae nyie,kazi kumfatilia mtu mgongoni kama mikia.Mnataka nini hapa.”Fred naye akaleta ubabe wake.

“Halafu mimi na hasira na wewe boya. Yaani wewe wa kuniwekea madawa mimi.Halafu bado na huku umenifuata.”Junior hakuwa nyuma kuonesha hasira zake juu ya Fred.

“Hapa wote tunahasira.Ila mkitaka hasira zangu ziondoke,sepeni hapa fasta.”Hans alitoa pendekezo ambalo lilipingwa vikali na matokeo yake likaanzisha vurugu nyingine.

Wale jamaa walianza kupigana tena na safari hii ulikuwa ni ugomvi wa ajabu kupita maelez. Wote watatu walikuwa wanapigana kwa kujitegemea.Kulikuwa hakuna kuchangiana.

Kipigo kiliendelea kwa dakika kama tano. Waligalagazana kwenye vumbi la ghorofa hadi wakawa kama wameoga simenti. Hakika walikuwa wamepania kuumizana.

Ugonvi ule ulisimama baada ya Eve kuingia akiwa na Suarez pamoja na jamaa mmoja mrefu na mweusi kiasi lakini akiwa ni mtanashati wa kutupwa.

Jamaa yule alivalia suti nyeusi aina ya tuxedo iliyokaa vyema mwilini mwake.Mguuni alivaa viatu vya gharama aina ya Gucci,na usoni alifunika macho yake kwa miwani ya D&G,hakika alipendeza hasa na marashi aliyojipulizia,basi ndio kabisa aliwaacha hata wale aliokutana nao njiani hoi.

“Nyie nini tena. Yaani kama matoto,sasa mnapigania nini?.”Eve aliwauliza baada ya vijana wale kutulia.

“Haya maboya kila mahala yananifata.”Junior alijibu huku uso wake uliwa katika mpauko uleule.

“Hawajakufuata.Mimi niliwaita mwenyewe ili wote mje hapa.Niliona nikiita na kuwataarifu kuwa wote mtakuwepo,mngetaa kuja.”Jibu hilo liliwafanya wale jamaa watulie huku wakiwa wanamwangalia yule mgeni aliyekuja naye Eve.

“Okey.Tuyaache hayo.Mimi niliwaita hapa ili umalize ugomvi wenu hasa ukizingatia mimi ndiye sababu kubwa.

Nia kubwa ya mimi kuwataka muwe mnakutana na mimi,ni kukusanya data ambazo zitanisaidia katika uendeshaji wa kipindi changu.

Kumbukeni mimi ni muandishi wa habari,na nilipata ofa ya kwenda kutangaza radio mojawapo kubwa hapa Tanzania.Nilitakiwa kuendesha kipindi cha mapenzi,hivyo wale wanaotaka kuniajiri walinitaka nisomee uandishi wa habari na wakati huo nakusanya data ambazo zitanifanya nikubalike kirahisi kwenye lile shirika habari.

Ndipo wazo lilikuja la kuwatumia nyie. Yale maongezi yenu,nilikuwa nayarekodi japo si yote hasa pale nilipokuwa naingia ndani ya maji.Ila nje ya hapo,nimerekodi yote na uongozi wangu umepitia na kukubali kazi yangu.Hivyo mwenzenu nimeajiriwa sababu yenu.”Eve aliyasema hayo huku akiwa ametabasamu.

“Pia sitaki kuwaacha hivi hivi,nitawalipa kiasi cha fedha kwa usumbufu niliowapa.”Eve aliweka nyongeza ya maneno yake na kisha alimuita yule mtanashati na kumwambia afanye kile alichokusudia.

Yule jamaa akatoa simu yake ndogo lakini yenye muonekano wa kuwa na gharama kubwa mno.

Akaomba namba za simu za wale jamaa na kisha kila mmoja akamtumia milioni moja moja kwakupitia mitandao wanayoitumia. Wakina Hans walifurahia sana ile kitu.

“La mwisho jamani.Najua mnanipenda sana ila nataka mumjue shemeji yenu. Ni huyu hapa,anaitwa Frank Masai. Yeye ni mwandishi mkubwa hapa Afrika lakini kwa sasa anafanya kazi BBC,shirika la habari la Uingereza.”Eve alimtambulisha yule jamaa mtanashati kwa wakina Hans jambo lililowafanya lile tabasamu kuwatoka.

“Ina maana swaga zote zile tulizokuwa tunakuletea,kumbe mwenzetu unatusanifu?Hadi tunagombana,kumbe tayari unamtu. Dah! Kweli umetuweza.”Junior aliongea kiupole.

“Mimi niliwaambia lakini.”Suarez aliongea kwa mara ya kwanza tangu afike pale.

“Kwa hiyo na wewe unajua hili?.”Hans alimuuliza Sua.

“Mi ndio nimejua leo. Lakini niliwahi kuwaambia mumuulize kwanza. Nyie mkajidai wazee wa swaga,haya mmekosa. Na nyie mmekuwa THE LOST BOYS. Kama tulivyowaita WAGUMU”.Suarez alizidi kuchonga domo.

“Okey.Nadhani mkataba wetu umeishia hapa.Ni kama mlivyonitumaga kwa Ban,nikatimiza. Na leo nimetimiza kingine. Kwaherini,na endeleeni kupigana,mimi nimemaliza.”Eve aliongea hayo na kumshika mpenzi mkono na kutoka kwenye ghorofa lile kwa madaha.

Huku nyuma wakabaki wale vijana wane wamesimama wasijue wanafanya nini.

“Dah!Kweli the lost boys ndio sisi.”Fred aliongea huku anakaa chini.

“The lost boy mwenyewe bwana,mimi sijashindwa.”Hans alijitetea kwa sauti ya juu.

“Kwani mwanangu uliwahi kumla mate kweli?.”Fred alimuuliza Junior.

“Aaah,zilikuwa zuga tu! Nimle mate demu gani hili,baya tu. Kwani na wewe uliwahi kumchora?.”Junipr alijibu na kumuliza swali Fred.

“Aaag.Kuchora kitu gani,labda hapa mzee wa masayansi.Oya nasikia ulimgonga huyu manzi.”Fred alimuuliza Hans.

“Aah. Demu mwenyewe hana mvuto,nitamgongaje mimi.Hana sifa za kugongwa na mimi.”Hans alijibu na yeye huku anakaa chini kama Fred.

“Kwa hiyo sisi ni The Lost Boys”.Fred alisema maneno hayo.

“Hilo jina silitaki.jiiteni wenyewe”.Hans akatoa onyo.

“Nyie ni The Lost Boys,hamna kubisha.”Suarez aliingilia yale maongezi na kufanya wale THE LOST BOYS kumwangalia kwa kumtamani,na mwisho wa siku walimkamata na kuanza kumwagia vumbi la mule kwenye ghorofa.

Suarez akapauka balaa.Hakukubali kufanyia vile. Akainuka haraka na kuanza kuwafukuza wale jamaa watatu.

Wale jamaa walipoona hivyo,wakaanza kukimbia kwenda nje huku Suarez akiwafuata kwa nyuma kwa kasi ya ajabu.

Mbele kidogo,walimuona Eve na mpenzi wake Frank wakiwa wanakaribia kufika kwenye gari lao aina ya Benz. Waliwapita kwa kasi yam shale hadi wale wapenzi wawili wakabaki wamesimama huku wanawaangalia wale The lost boys.

Haijapita hata sekunde, akapita Suarez kapauka balaa. Kilichofuata hapo ni tabasamu tu kwa wale wapenzi wawili.

Kwa mbele,Hans alimchenga Suarez na kuzunguka ambapo alitokea nyuma ya gari la akina Eve. Hakuna aliyemuona Hans kati ya Eve na Frank,hivyo upenyo huo Hans aliutumia kwa kunyata na kuziunga kamba mbili za viatu ambavyo alivaa mpenzi wa Eve.

Baada ya kufanikiwa,alirudi nyuma kwa kunyata na kwenda kule ambapo wenzake wapo. Aliwakuta wanagalagazana wenye dimbwi ambalo llina maji ya mvua,na yeye bila kufikiria,akachukua ndoo na kuanza kuyachota maji yale na kuwamwagia. Mara kibao kikamgeukia,Fred na washirika wake,wakampora ndoo na kutaka kumuogesha maji yale.

Hans kuona hivyo,akaanza kukimbia lakini anaelekea kule walipo Eve na Frank. Kufika pale,Hans akakaa mbele hatua kama tano ya mpenzi wa Eve.Fred akiwa na ndoo ya maji ya kwenye dimbwi,alifika na kuyamwaga kumwelekea Hans,lakini Hans aliinama na maji yale yakamkuta Frank.

Kimya kikachukua nafasi yake huku kila mmoja akiwa anaogopa kwa kile kilichotokea.

Fred na ndoo yake huku matone ya maji yakimmwagika,Junior naye akiwa anatweta kwa kukimbia sana hali ambayo hata Suarez anayo,walibaki wa mesimama wakiangalia ni nini hatma yao baada ya mpenzi wa Eve kukaa vizuri.

Hatimaye Frank aliamua kutaka kuwakimbiza lakini zile kamba ambazo amefungwa miguuni na Hans,zikamzuia na kumdondosha lakini uzuri hakudondokea kifua wala kidevu,aliweza kujibalansi na kujikuta akiwa kama anapiga pushapu.

Wale The Lost Boys walianza kucheka kitendo kile. Na kwa aibu kubwa,mpenzi wa Eve alinyanyuka haraka na kuingia garini.

Huku nje Fred,Hans,Junior na Suarez walihisi labda jamaa atatoka na bastola,wakaamua kukimbia huku wakirukaruka kwa furaha wakitamka kwa nguvu na sauti ya juu.

“WE ARE THE LOST BOYS.” Yaani wao ni walioshindwa.

MWISHO.

Roman Abramovich – Utajiri wa Damu, Risasi na Umafia

IMEANDIKWA NA : THE BOLD

****

Simulizi : Roman Abramovich: Utajiri Wa Damu, Risasi Na Umafia

1

HOW TO BECOME A BILLIONARE.?

i)Invent – kama una uwezo mzuri wa kiakili buni kitu kipya ambacho kitakuwa na uhitaji mkubwa kwenye jamii.

ii)Innovate – tafuta kitu fulani, bidhaa au huduma na kisha boresha ufanisi wake au ufanyikaji wake na kisha ifanye kibiashara huduma hiyo au bidhaa.

iii)invest – tafuta biashara au kampuni ambayo……

Wrong..!!

Haya ndiyo majibu ambayo bila shaka yanatujia vichwani endapo tukipatwa na ndoto za labda siku moja kutengeneza utajiri wa kuzidi dola bilioni moja za kimarekani. Tunafikiria kufanya bunifu, kuboresha huduma, kuwekeza au kuwa wajasiriamali. Mbaya zaidi tunaamini kwamba yeyote yule ambaye amefanikiwa kuupata utajiri wa kiwango hicho cha 'kufuru' basi twamuhusudu kwamba ni mfanyabiashara au mjasiriamali nguli na hodari au labda ni mbunifu au mgunduzi mwenye akili iliyopitiliza. Nimekuwa nikiamini hivi pia kwa miaka mingi sana huko nyuma, nakumbuka nikiwa mwanafunzi wa sekondari niliwahi kutawaliwa sana na 'wehu' wa kutamani sana siku moja kuwa billionaire. Kuna jamaa mmoja muhindi alikuwa na duka maeneo ya upanga UN road la kuuza vitu kwa rejareja. Nilikuwa na rafiki yangu anaitwa Castro, basi tulikuwa tukitoka shuleni tunapita mara nyingi sana dukani kwake kwa ajili ya kuchukua jarida la Forbes. Dukani kwa huyu jamaa ndio mahalapekee ambapo kipindi hicho nilikuwa nafahamu naweza kulipata jarida la Forbes. Nakumbuka namna ambavyo ungeniona kipindi kile macho yakijawa na tabasamu pindi nikishika tolea jipya la Forbes… namna ambavyo nilikuwa makini kufuatilia orodha ya matajiri wakubwa zaidi duniani… kipindi kile ningeweza kukutajia mabilionea wakubwa wa dunia kutoka kichwani kuanzianamba moja mpaka namba thelathini, majina yao, kiwango chao cha utajiri na majina ya kampuni zao… unguli wa Carlos Slim, Buffet na Gates… historia za kusisimua za kina Lakshmi Mital… kuibuka kwa kina Aliko Dangote na Mike Adenuga ambao walikuwa ni 'newbies' kipindi kile kwenye orodha ya Forbes. I loved it… breathed it, nilisoma Forbes kama msahafu na ikanipa ndoto za ajabu… kutamani kwamba niumize kichwa na kufanya gunduzi moja matata sana ya kunifinya siku moja kuwa na ukwasi huo kufikia dola bilioni moja za kimarekani.

Lakini kadiri ambavyo miaka iliongezeka na kuanza kufunguka macho kuelewa mfumo na mwenendo wa dunia nikaelewa kwamba kuwa bilionea ni kitu ambacho kinahitaji zaidi ya talata ya biashara, zaidi ya ujasiriamali na zaidi ya kufanya gunduzi au bunifu murua. Unaweza kuwa tajiri, unaweza kuwa milionea kwa kufanya gunduzi au bunifu makini au kuwa mfanyabiashara au mjasiriamali makini. Lakini kufikia ukwasi wa ubilionea… sio ubilionea kama ule wa Arusha wa kununua Nissan Patrol na kuwa na nyumba Njiro kesho kila mtu mtaani anakuita bilionea… hapana, naongea kuhusu ubilionea halisi wa ukwasi wa kuzidi dola bilioni moja… zaidi ya shilingi trilioni mbili za kitanzania… utajiri ambao Watanzania wawili tu wamefanikiwa kuufikia, 'mtoto wa mjini' Rostam Aziz na mhafidhina wa kibiashara Mo Dewji. Ukwasi wa ngazi hiyo unahitaji zaidi ya talanta ya ujasiriamali na biashara na zaidi ya upekee wa gunduzi na bunifu.

Niliwahi kuandika kwenye mada moja, "katika kila kila utajiri kuna ukafiri nyuma yake.!" Kuna ngazi ya utajiri ili kuifikia inahitaji purukushani, 'kash kash' na kufanya mambo ambayo yawezekana wengine hatuna kifua kuyafanya.

Nitatoa mfano… mfano wa moja wa billionare ambaye anahusudiwa sana ulimwnguni na moja ya mabilionea wa kupigiwa mfano sana ni Billionare Roman Arkadyevich Abramovich au kama ambavyo anajulikana kwenye inner circle pale Kremlin, 'Oligarch Abramivich' au 'Mr A'.

Huyu muheshimiwa akiwa na umri wa miaka 34 tu Roman tayari alikuwa na tittle ya 'Oligarch', title ambayo jamii ya Urusi imewapachika watu wenye ushawishi mkubwa nchini humo na ambao wako kwenye 'inner circle' ya utawala wa nchi ya Russia. Katika miaka hiyo 34 tayari alikuwa anamiliki kampuni kubwa ya uzalishaji mafuta ya Sibneft na pia alikuwa moja ya wanahisa wakuu wa kampuni ya RUSAL (Russia Aluminum) ambayo kwa kipindi kile ndio ilikuwa kampuni inayoongoza kwa uzalishaji mkubwa zaidi wa Aluminum wakichangia zaidi ya 9% ya Aluminium inayotumika duniani kote. Katika umri huu wa miaka 34 ni ngumu kusema kwa hakika hasa utajiri wa Oligarch Abramovich ulikuwa unafikia kiasi gani kutokana na usiri kuhusu mapato yake, lakini hakuna shaka kabisa kwamba utajiri wake ulikuwa unazidi dola bilioni 6 za kimarekani.

Unaweza kujiuliza ni kwa namna gani katika umri mdogo kiasi hicho mtu anaweza kuwa na utajiri wa kupindukia kiasi hicho na hata kuwa moja ya wamiliki wakuu wa kampuni ya kuzalisha zaidi ya 9% ya aluminium inayotumika duniani.

Nataka tutazame mfano wa Abramovich kupata picha ni kwa namna gani unapaswa kuwa na 'ngozi ngumu' kupitiliza ili kuukwaa ubilionea.

Tuanze mwanzo kabisa….

Roman Arkadyevich Abramovich ni yatima aliyelelewa katikika umasikini wa kupitiliza na baadae kufanikiwa kuwa moja ya matajiri wakubwa zaidi kuwahi kutokea duniani. Historia yake ni mwanana kabisa kumtia mtu moyo namna ambavyo unaweza 'kuinuka kutoka mavumbini na siku

moja kuketi na wafalme.' Wazazi wake walifariki angali bado akiwa mdogo kabisa kabisa na hivyo kupelekea yeye kulelewa na nduguze waliokuwa wanaishi kaskazini mwa Urusi kwenye eneo la Komi.

Japokuwa wazazi wake na yeye mwenyewe wameishi maisha yao karibia yote nchini Russia lakini asili yao hasa ni Israel. Babu yake mzaa baba, mzee Nahim Abramovich alikuwa ni mfanyabiashara ambaye aliishi pamoja na mkewe (bibi mzaa baba) Tauba Berkover waliishi wote huko jamuhuri ya Lithuania kwenye jimbo la Taurage. Baba yake Abramovich, Arkady Abramovich alikuwa ni afisa wa serikali katika jamuhuri ya Lithuania. Mama yake Abramovich aliyeitwa Irina Michaleno wazazi wake (babu mzaa mama) Vassili Michalenko na mama yake (bibi mzaa mama) Faina Grutman nao wote waliishi jamuhuri ya Lithuania. Wazazi wake (Arkady na Irina) walifariki akiwa mdogo kabisa… mama yake Abramovich, Irina alifariki Roman akiwa bado mchanga kabisa na baba yake Arkady alifariki kwa ajali ya gari miaka michache baadae. Na ndio hii ilisababisha Abramovich kwa mara ya kwanza kabisa kwenda kuishi Komi kwa nduguze, kaskazini mwa Urusi na baadae Uktah eneo lenye baridi kweli kweli na umasikini uliokithiri.

Katika ujana wake Abramovich aliwahi kujiunga na jeshi kwa muda mfupi sana kabla ya kuacha na kuanza kufukuzia ndoto zake. Kama ilivyo ndoto ya vijana wengi Tanzania miaka ya nyuma "kwenda Dar es salaam kutafuta maisha" ndicho hicho pia kinawakumba vijana wengi duniani kote kutaka kwenda kwenye miji mikubwa ya nchi zao husika, ndicho hiki pia alikifanya Roman… aliondoka Uktah na kwenda Moscow 'kutafuta maisha'. Akiwa Moscow alifanya akili ya kujiunga na kozi ya masuala ya mafuta na gesi katika taasisi ya Gubkin Institute of Oil and Gas ambako alikuwa anasoma huku akiuza matairi chakavu ya gari ili kuweza kujikimu kimaisha. Akiwa bado anapambana kutafuta nafuu ya maisha hapa Moscow ndipo pia alikutana na mkewe wa kwanza, Olga na kumuoa.

Maisha hayakuwa mepesi sana kwa Abramovich… kipindi hiki ni kipindi ambacho Urusi ilikuwa inapitia kipindi cha mpito mgumu sana wa kiuchumi na kifalsafa. Ni kipindi ambacho ujamaa ulikuwa unadondoka na ubepari kushamiri nchini Urusi. Ni kipindi ambacho Urusi ilikuwa moja ya sehemu hatari zaidi kuishi kutokana na uhuni na ubabe ambao ulikuwa unatokea Urusi na nchi nyingi za Ulaya ya Mashariki. Ni kipindi hiki ambacho nchi za ulaya mashariki zilibatizwa jina la "Wild East". Abramovich alifanya kila aina ya kazi ya hali ya chini, kuanzia kuuza bidhaa ndogo ndogo mitaani mpaka kuwa makenika kwenye viwanda na hata kuwa 'bodyguard'.

Waswahili tunasema kwamba "anayejua, anajua tu", kwamba kuna watu unaweza kuwapa ndimu ukidhani unawakomoa lakini atakushangaza kwa kuikamua na kutengeneza 'juisi ya lemonade' na kuinywa kwa raha mustarehe. Ndicho ambacho Roman alikifanya, kuanguka kwa ujamaa na kuibuka kwa ubepari, tena ubepari wa kihuni na ubabe aliona yaweza kuwa fursa adhimu kabisa kwake… akaanza kufanya biashara ya kila namna. Roman akaanzisha biashara ya kuuza midoli… ile biashara ya kuuza tairi chakavu akaikuza zaidi na kuifanya kwa upana na mpaka kuwa wakala rasmi wa tairi mpya kutoka viwandani.

Lakini moja ya biashara ambayo ilimsaidia kumpa 'connections' ilikuwa ni pale alipofungua biashara ya kutoa ulinzi binafsi (bodyguards). Pale juu nilieleza kwamba kipindi anaanza maisha Moscow Roman aliwahi kufanya kazi ya u-bodyguard, lakini safari hii sio yeye alikuwa bodyguard bali alikusanya vijana wake kadhaa na kufungua kama kampuni ya kutoa ulinzi kwa wadosi.

Nimesema kwamba hiki ni kipindi ambahi Urusi ilikuwa ni 'Wild West', kipindi ambacho uhuni na ubabe ulikuwa ndio namna ya maisha. Kipindi ambacho ujamaa unandoka, serikali ikibinafsisha nyenzo zake za kiuchumi kwa watu wachache. Hapa kwetu Tanzania tumepita pia kwenye kipindi kama hiki hiki na wazee wetu wanajua shurba waliyopitia… anguko la ujamaa na kuibuka kwa ubepari. Kipindi ambacho tulibinafsisha kila kitu na kuacha wake zetu tu. Tofauti ni kwamba hapa kwetu wajanja ambao walibinafsishiwa mali za nchi walikuwa wanashindana ni yupi ambaye atatoa rushwa kubwa zaidi… lakini kule 'Wild East' haikuwa rushwa tu pekee… naam, ilikuwa lazima utoe rushwa kubwa kumzidi mwenzako lakini aliyekuwa mtemi na muhuni zaidi ndiye ambaye angeweza kujihakikishia umiliki wa kiwanda au rasilimali husika. ilikuwa ni kula au uliwe. Jifunze kula 'nyma ya mtu' au subiri ufanywe kitoweo.

Katika biashara za makampuni makubwa kuna kitu kinaitwa 'hostile take-over'. Yaani kwa mfano bwana Mo Dewji na kampuni zake za MeTL waanze kuuza hisa za kampuni zake za MeTL Group kwa umma… anakuja mtu ambaye kwa muda mrefu alikuwa anatamani aiweke MeTL mikononi mwake… tumuite mtu huyu Paul (mfano tu). Ananunua hisa nyingi zaidi kumuwezesha kupata ujumbe wa bodi ya wakurugenzi wa MeTL. Kisha anaanza kukaa kwa siri na wanabodi mmoja mmoja na kuwashawishi kumuondoa Dewji kama MD na Mwenyekiti wa bodi … kikao kinaitwa, kura zinapigwa… bodi inamuondoa Dewji kuwa MD na mwenyekiti wa bodi na kumfanya Paul kuwa MD na mwenyekiti mpya wa bodi. Dewji anabakia kuwa mwanahisa tu wa kawaida kama wengine bila uwezo wowote wa kimaamuzi juu ya kampuni yake ambayo aliinzisha. Hii inaitwa 'hostile take-over'. Lakini kipindi hicho huko 'Wild East', Urusi ya miaka hiyo walikuwa na namna ya tofauti ya 'Hostile Take-over'. Tajiri mwenzako anakuvizia, anakuteka… anakutesa mpaka unasaini makaratasi. Kisha anakutandika risasi na kesho yake inatangzwa kuwa kampuni/kiwanda chako ni chake na mliuziana kwa maandishi na nyaraka anazo. Wiki moja baadae mwili wako unaokotwa jalalani and nobody cares, maisha yanaendelea… Wild wild East.!!

Katika mazingira kama haya ambapo miili ya matajiri, waandishi wa habari na hata viongozi wa kisiasa ilikuwa inaokotwa kila siku imetupwa mitaani unaweza kupata picha ni kwa namna gani ambavyo biashara ya u-bodyguard iliweza kushamiri. Matajiri walikuwa na hofa na maisha yao muda wote, kwa hiyo walihitaji ulinzi muda wote. Biashara ya Roman ikashamiri.

'Dili' hizi za kulinda matajiri na bishara zake za hapa na pale zilimpa 'connection' na kusaidia kujuana na watu muhimu ndani ya Moscow. Moja ya watu hawa muhimu ambaye baadae alikuja kuwa kama 'mentor' wake alikuwa ni Boris Berezovsky Mwanamahesabu nguli na mhadhiri wa chuo kikuu ambaye alikacha kufundisha chuo na kugeukia biashara ili asipitwe na upepo wa utajiri uliokuwa unavuma Urusi kipindi hicho.

Berezovsky alikuwa ni moja ya ma-Olygarch wa kwanza kabisa ndani ya Urusi. Nimeeleza pale mwanzoni Oligarchy ni watu wa namna gani. Borozevsky alikuwa ni moja ya matajiri wakubwa zaidi Urusi kipindi hicho ambaye alinufaika sana na ubinafsishaji wa mali za umma. Oligarch Boris Berezovsky hakuwa tu Oligarch bali alikuwa ni sehemu ya ma-Oligarch wachache ndani ya Urusi ambao waliojulikana kama 'The Family'.

The Family ilikuwa ni 'inner circle' ya watu wachache sana ambao walikuwa karibu na Rais wa Urusi kipindi hicho Boris Yeltsin. Watu hawa walikuwa ni wanafamilia wa Yeltsin pamoja na matajiri wachache sana akiwemo Berezovsky. Kikundi hiki cha matajiri wachache pamoja na familia ya Rais ndio kiuhalisia ndio walikuwa wanaendesha nchi.

Kwa hiyo kitendo cha Abramovich kujiweka karibu na Berezovsky ilimaanisha kwamba alikuwa amefanikiwa kujenga urafiki na moja ya watu muhimu zaidi ndani ya Urusi na mwenye ushawishi ndani ya inner cirle ya Rais.

Watu wenye asili ya uyahudi twaweza kuwachukia na kuwasema tutakavyo kwa uonevu ambao labda wanaufanya… lakini jambo moja ambalo hatuwezi kubisha ni uwezo wao wa asili kiakili na kimkakati. Japokuwa Abramovich kwa kipindi hicho alikuwa ni mrusi tu lakini kuna damu ya kiyahudi ilikuwa ndani yake na ni wakati huu ambao alidhihirisha umahiri wake kimkakati.

Baada ya urafiki wao Abramovich na Berezovsky kukomaa na kushibana, Abaramovich alimuomba Berezovsky amsaidie kumtambulisha kwa watu muhimu Kremlin. Moja kwa moja Berezovsky akahisi labda Abramovich anataka kutambulishwa kwa Rais au mawaziri na akamjibu bado hajafikia ngazi ya kutambulishwa kwa watu hao… lakini Abramovich akamwambia hapana haitaji kutambulishwa kwa Rais au mawaziri… anahitaji kutambulishwa kwa mtu anaitwa Valetin Yumachev ambaye kipindi hicho alikuwa ni afisa wa kawaida tu wa Ikulu kitengo cha habari na maelezo na hukuwa na ushawishi kwa Rais Yeltsin. Berezovsky alishangaa maana Yumachev hakuwa na ushawishi wowote ule pale Kremlin.

Ndio hapa ambapo nasema kuna watu ni 'born tacticians'… akili yao inawaza kimkakati kwa kila hatua na moja wapo ni huyu Abramovich. Abramovich alielewa wazi kabisa hawezi kutambulishwa kwa Rais na japo alikuwa na tuhela tudogo twa kubadili gari na nyumba lakini ukilinganisha na ma-Oligarch kipindi hicho yeye alikuwa ni kidagaa tu, 'hohe hahe' ambaye hawezi hata kukaa meza moja na rais. Lakini anaitaka hiyo connecvtion kuliko kitu chochote kile ili afike pale anapopataka kimafanikio. Ndipo hapa ambako aliona kitu ambacho wengine hawakukiona… Valentin Yumachev, afisa habari mdogo wa Ikulu. Abramovich aligundua kwamba Yumachev alikuwa na mahusiano ya siri ya kimapenzi na binti wa Yeltsin aliyeitwa Tatyana. Binti huyu wa Rais pia alikuwa anapendwa mno na baba yake na alikuwa moja ya watu anaowasikiliza sana na kuwaamini.

Abaramovich akapiga hesabu zake… kama akiweza kujenga urafiki wa kushibana na Yumachev, na kisha kufanya uhusisano wa Yumachev na Tatyana ukue na hatimaye labda kuoana. Maana yake ni kwamba atakuwa ni rafiki wa mkwe wa Rais wa Urusi. Na kutokea hapo kujiweka karibu na Rais kupitia mgongo wa 'best friend' wake itakuwa ni rahisi kama kusaga maini.

Berezovsky akamtambulisha Abramovich kwa Yumachev. Hata Yumachev mwenyewe akashangaa… 'mtoto wa mjini' Abramovich ambaye ni rafiki wa ma-Oligarch kutambulishwa kwake. Kwa hiyo hata urafiki ukakua kwa haraka sana Yumachev kuona ni heshima kubwa kwake kwa mtoto wa mjini kama Abramovich kumthamini na kumuona ana umuhimu.

Lakini Abramovich alikuwa anaiona 'potential' ndani ya Yumachev ambayo hata mwenyewe alikuwa haioni… Abramovich alikuwa anaona miaka mitano mbele ambayo wengine walikuwa hawaioni…

Nimeona niwekee sehemu hii ya pili usiku usiku ili tukalale na tafakuri nzito kuhusu ulimwengu wetu na nama ambavyo unakwenda

Sasa,

Kipindi hiki ambacho nimeeleza kwamba Abramovich aliomba kutambulishwa kwa Yumachev, Abramovich alikuwa ni kijana mdogo tu wa umri wa miaka 28. Kutokana na urafiki wao wa kushibana na Berezovsky, Berezovsky alimtambulisha Abramovich kwa Yumachev bila kusita. Nimeeleza kwamba kipindi hicho Yumachev alikuwa ni afisa habari tu wa Ikulu lakini hakuwa na ushawishi wowote kwa Rais Boris Yeltsin.

Lakini baada ya urafiki wa Yumachev na Abramovich kukolea… Abramovich akaanza 'kumuazima akili' Yumachev. Kumuonyesha ni kwa namna gani uhusiano wake wa kimapenzi na mtoto wa Rais wa nchi kama akichanga karata zake vyema uhusiano huo unaweza kumuinua kutoka mavumbini kwenye uafisa habari wa ikulu na pengine kumfanya kuwa moja ya watu muhimu zaidi kwenye 'inner circle' ya Rais Yeltsin.

Yule binti wa Rais ambaye Yumachev ana uhusiano naye wa kimapenzi hakuwa binti tu legelege wa kula mkate kwa siagi mezani… binti huyu alikuwa ni moja ya washauri wakuu wa Rais Yeltsin. Alikuwa ni moja ya watu wenye kuaminiwa zaidi na Rais. Sasa ambacho Abramovich alikuwa anakifanya ni kumpa mikakati ya Yumachev na kisha Yumachev anakwenda kushauriana na Tatyana na kisha wanaenda kumshauri Rais. Kadiri muda ulivyokuwa unakwenda Yumachev akaanza kuonekana kwamba naye ni mtu mwenye bongo makini na mwenye kujua mikakati. Si miezi mingi, Yeltsin akamapandisha cheo Yumachev akamfanya kuwa 'Head of Adminstration' wa Ikulu, cheo ambacho kwa kipindi hicho nchini Urusi kilikuwa adhimu mno. Si hapo tu kwa ushauri wa Abramovich Yumachev akamuoa kabisa Tatyana. Hapo ndipo hasa pale ambapo Abramovich alikuwa anapataka.

Kwa pamoja Abramovich, Yumachev na safari hii pamoja na Tatyana urafiki wao ukaota mizizi haswa. Kutokana na ukaribu huu wa Abramovich na Afisa mkuu wa masuala ya utumishi Ikulu na nchi pamoja na ukaribu na binti wa rais ambaye pia ni mshauri mkuu wa Rais moja kwa moja Abramovich akatambulishwa na 'marafiki' zake hao wawili kwa Rais Yeltsin na kutokana na uwezo wake wa hali ya juu wa kimikakati na kufikiri, Abramovich hakuchukua muda sana akawa sehemu ya 'The Family'.

Nilieleza pale mwanzoni kuhusu 'The Family', ile inner circle ya Rais Yeltsin ambayo ilikuwa inaundwa na wanafamilia ya Rais pamoja na ma-Oligarch wa Urusi. Hii 'The Family' ndio hasa ilikuwa inaendesha nchi ya Urusi kipindi kile. Sasa baada ya Abramovich kuwa sehemu ya 'The Family' kukaibuka inner circle ndani ya Inner circle. Yaani kwamba kwenye wale watu wachache ambao walikuwa wanaaminiwa mno na Rais Yeltsin (The Family) kukaibuka kikundi cha watu wachache zaidi kati yao The Family ambao walikuwa wanaaminiwa zaidi na Rais uzidi wengine wote, ndio hapa nasema inner circle ndani ya inner circle. Watu hawa walibatizwa jina la "Utatu Mtakatifu" na utatu huu mtakatifu walikuwa Abramovich, Yumachev na Tatyana.

Kijana yule yatima, aliyekimbia umasikini kutoka kwenye maisha ya kulelewa na ndugu zake jimboni Komi, ati leo hii akiwa na miaka ishirini na nane tu anaketi meza moja na moja ya binadamu mwenye ushawishi na nguvu zaidi duniani, Rais wa Urusi na tena anaketi akiwa moja ya watu ambao Rais anawaamini sana na kuwasikiliza sana.

Ndani ya hii 'The Family' Abramovich alipachikwa jina la 'Family Wallet'. Hii ni kutokana na kutumiwa sana na Rais Yeltsin na familia yake kwenye usimamizi wa masuala yao ya fedha na utajiri wao.

Nimeeleza, wakati huu ndipo ambapo Ujamaa ulikuwa umedondoka na Ubepari kuanza kushamiri… kwa hiyo kwa wanasiasa na wazee ambao wamekuwa kwenye maisha ya kijamaa hawakuwa na uelewa mpana sana wa namna ambavyo mizania ya kibepari inavyofanyakazi. Lakini Abramovich alikuwa ni mfanyabiashara japo hata kama alikuwa akiuza midoli na matairi, amekulia mtaani akijua ni namna gani kanuni za 'natural selection' zinafanyakazi… vyenye nguvu vinakula dhaifu… na zaidi ya yote Roman alikuwa na uwezo wa kuzaliwa wa kiakili, mikakati na 'kujiongeza'. Kwa hiyo akatumia ujuzi wake huu kushauri familia ya Rais namna bora zaidi ambavyo wanaweza kutunza utajiri wao… akaanza kuwafundisha na kuwezesha familia ya Rais Yeltsin kufungua offshore accounts, uwekezaji kwenye masoko ya hisa, kufungua offshore companies ambazo wamiliki wanafichwa kwenye mifumo 'complex' kujua nani hasa ni mmiliki na mambo mengine mengi ya kibepari. Kwa maneno mengine Abramovich alikuwa anawafungua macho namna ya 'kuiba' na kuficha fedha za umma kisasa katika namna ambayo ni ngumu kujulikana na namna za uhakika zaidi kwa fedha hizo kuwa salama.

Urusi ilikuwa inabadilika haraka mno… kutoka kuwa mpigia chapuo mkuu wa Ujamaa duniani na kuwa nchi ya kibepari tena ubepari wa kihuni kabisa. Japo suala la ubinafsishaji wa makampuni ya umma kwenda kwenye umiliki wa watu binafsi lilipongezwa sana na nchi za magharibi wakiona kama hatua nzuri ya nchi hiyo kuhama kutoka kwenye uchumi unaoshikiliwa na dola na kuanza kwa 'soko huru' la kiuchumi ndani ya Urusi lakini wananchi wa Urusi hawakuona kile ambacho wadosi hawa wa magharibi walikuwa wanakiona. Wananchi walikuwa na hasira wakihisi kwamba nchi yao na uchumi unaganywa kwa kikundi cha watu wachache huku wao wakiendelea kuteseka na hali duni za kimaisha.

Kipindi cha ubinafsishaji wa makampuni ya umma kuna jambo mojaambalo mwanzoni lilikuwa jema lilikuwa limefanyika kabla ya kugeuka shubiri mbeleni.

Kila mwananchi alipewa 'voucher' yenye thamani ya fedha ya Urusi rouble 10,000. Lengo la vocha hii ilikuwa ni kuwapa nafasi kila mwananchi wa urusi kumiliki hisa kwenye kampuni za serikali ambazo zilikuwa zinabinafsishwa. Kivipi? Yaani kwamba kampuni ya serikali ikiwa inauzwa na ikatangazwa kwamba kampuni hiyo ina thamani ya kiasi fulani cha fedha… ni kweli watajitokeza matajiri ambao watanunua hisa nyingi zaidi lakini bado mwananchi wa kawaida alikuwa anaweza kupeleka vocha ile ya rouble elfu kumi na akanunua hisa zenye thamani ya vocha hiyo.

Lakini kwenye miti hapana wajenzi na mtu aishiye mwituni ambaye hajui thamani ya almasi siku akiishika hawezi kuona tofauti yake na kokoto, aweza kuipiga kwenye manati kama jiwe ili aue ndege chiriku akafanye kitoweo. Ndicho ambacho kilitokea Urusi. Nchi ilikuwa ndio kwanza ilikuwa imetoka kwenye ujamaa… wananchi hawakuwa wanajua namna gani hasa ubepari unafanyakazi. Nini kilichotokea? Wajanja wachache

wakawa wanatuma mawakala wao vijijini na mijini kwa wananchi… wanawashawishi wananchi wawape vocha na wao wanawapa fedha tasilimu. Karibia kila mwananchi alikuwa anakubali. Anatoa vocha yenye thamani ya rouble 10,000 alafu yule ajenti anampa labda rouble 200 cash. Unaweza kujiuliza wananchi hawa walikuwa vichaa au?? Hapana… maarifa… maarifa… fikiri mwananchi huyu amezaliwa na kukulia kwenye ujamaa. Leo hii ati unampa kipande cha karatasi unamwambia kina thamani ya pesa (wakati yeye anaona ni karatasi tu) alafu unamwambia atumie karatasi hiyo kwenda kununua hisa za kampuni (hajui hata hisa ina maana gani zaidi ya kusikia tu kwenye rediio inatajwa)… alafu unamueleza akiwa na hisa kwenye kampuni fulani siku moja inawezekana labda (hakuna uhakika) kama kampuni hiyo husika ikianza kutengeneza faida atalipwa 'dividends' (dividends ndio 'mdudu' gani). Unaweza kuona mnyumbuliko wa mawazo ya mtu huyu aliyekulia kwenye ujamaa? Yawezekana hata sisi tungekuwa kwenye nafasi zao tungeuza vocha ya thamani ya rouble elfu kumi kwa rouble 200 cash tukale wali na nyama tushibe, tulale, tuamke tuanze kuhangaika tena kesho.

Na hii imetokea hata hapa kwetu nchini tena juzi juzi tu hapa… unakumbuka kipindi cha ruzuku ya pembejeo za kilimo za serikali katika utawala wa Mzee Kikwete? Watu walikuwa wanauza vocha kwa shilingi elfu kumi tu alafu wale mawakala wanapeleka NMB wanalipwa laki na sitini kwa kila vocha au zaidi.!! Yale yae, almasi kuiona kokote…

Sasa pale Urusi wajanja wachache sana walinunua hizi vocha na na kuzitumia kununua hisa za makampuni yaliyokuwa yanabinafsishwa… makampuni ya mafuta, gesi asilia na kadhalika. Ndipo hapa kukaibuka matajiri wale ambao nilisema wakabatizwa jina ma-Oligarch. Mbaya zaidi Yeltsin akawaweka karibu mno ma-Oligarch akishirikiana nao kuendesha nchi.

Wananchi walikuwa na hasira kweli kweli na Yeltsin.

Umaarufu wa kisiasa wa Rais Yeltsin ulikuwa umeshuka mno kupitiliza. Ukichangiwa pia kwa sehemu nyingine kutokana na matatizo ya moyo mara kwa mara akipatwa na mshituko na kufanyiwa upasuaji na kumfanya asionekane sana kwa umma.

Ukafika mwaka 1996… mwaka wa uchaguzi mkuu wa Urais. Kila mtu alikuwa anasubiri kusikia Yeltsin atamtangaza nani kama mgombea kwenye chama chake maana hakuna ambaye alikuwa anadhani kwamba Yeltsin atagombea tena maana umaarufu ulikuwa umeporomoka mno, wananchi wanamchukia na afya yake ilikuwa mgogoro.

Ajabu ni kwamba mwezi February mwaka huo 1996 Yeltsin akatangaza kwamba atawania muhula mwingine wa uonngozi. Vyama vya upinzani vilishangilia maana walijua kwamba ushindi wa kishindo uko barazani kwao.

Kabla ya kupiga kura mwezi Desemba, katikati ya mwezi July yalitolewa matokea ya kura za maoni na mgombea wa chama cha Upinzania cha Kikomunisti Bw. Gennady Zyuganov alikuwa anaongoza kwa asilimia nyingi akimuacha mbali kabisa Rais Boris Yeltsin.

Kambi ya Rais presha ikawapanda… paniki ikiwatawala. Kila mti unateleza. Hakuna mwenye kujua wafanyeje… waliona kabisa wanaelekea kuupoteza 'mnofu' wao. Nani awaokoe?

Pale mwanzoni niliandika kwamba… a born tactician, haijalishi ni mazingira gani utamuwekea lazima apate namna ya 'ku-survive', lazima aone upenyo mwembamba wa shaba kwenye giza totoro. Mpe limao ukidhani unamkomoa, ukirudi baadae utakuta amelikamua na kutengeneza juisi ya 'lemonade' akinywa kwa starehe kabisa. Hivi ndivyo ambavyo Roman Abramovich akili yake inanyumbulika… wakati ambapo timu nzima ya Rais Yeltsin imepaniki hawajui nini cha kufanya yeye aliona hiyo ndio fursa kwake kumdhihirishia Boris Yeltsin kwamba kichwa chake kimebeba mbongo ambayo sio ya mchezo mchezo…

Uchaguzi ulikuwa unakaribia, wananchi walionekana dhahiri wanaegemea upande wa mkomunisti Zyuganov. Taarifa hii si kwamba ilikuwa mbaya kwa Rais Boris Yeltsin pekee bali pia na genge lake lote la "The Family" kwa sababu ilikuwa dhahiri kwamba kama ikitokea mkomunisti Zyaganov akichukua nchi kitu cha kwanza ambacho angekifanya ni kurejesha serikalini viwanda na makampuni yote ambayo yalikuwa yamebinafsishwa na Rais Yeltsin kwa watu binafsi.Hakuna ambaye alikuwa na jawabu kichwani wa nini hasa wakifanye kunusuru kile ambacho kilikuwa kinaelekea kutokea… baadhi ya watu kwenye inner circle wakamshauri Rais Yeltsin afute uchaguzi na atawale nchi kidikteta. Lakini hili lilikuwa ni wazo la kipuuzi kabisa labda kutokana na maji kuwafika shingoni maana mfumo huu ulikuwepo Russia huko mwanzoni miongo kadhaa nyuma na ukafeli na kudondoka.

Wakati ambapo kila mtu akiwa amechanganyikiwa na kutoa mawazo yasiyo na mbele wala nyuma kuleta auheni yoyote ndipo ambapo Abramovich akaingilia kati. Akakaa mstari wa mbele na kushika usukani wa mikakati ya uchaguzi kambi ya Rais Yeltsin. Russia ilikuwa imetoka kwenye ujamaa na ubaya ni kwamba ile akili ya kijamaa bado ilikuwa haijawaisha. Kama wasemavyo, unaweza kumtoa kijana kutoka 'nanjilinji' kuja mjini lakini kamwe huwezi kuitoa 'nanjilinji' akilini mwa huyo kijana. Nchi ilikuwa imeingia kwenye ubepari lakini wazee bado walikuwa wanawaza na kufanya mambo yao kama wajamaa. Abramovich akataka kuwaonyesha namna ambavyo chaguzi zinafanyika kwenye nchi za kibepari.

Kwanza akamshawishi Rais Yeltsin amfute kazi meneja kampeni wake. Kisha nafasi hiyo akashauri apewe mtoto wa Rais Tatyana. Kwa nini? Kwanza kwasababu Tatyana atakuwa na uchungu zaidi na kampeni hiyo kwa kuwa 'ana kitu cha kupoteza' kama wasiposhinda. Lakini pia kama ambavyo nilieleza kuwa Tatyana hakuwa binti legelege wa kula mkate kwa siagi tu, bali alikuwa ni mpambanaji haswa. Lakini tatu Abramovich alitaka Tatyana ashike wadhifa wa meneja kampeni kwa kuwa alikuwa rafiki yake na walau alikuwa kwa mbali Tatyana alikuwa ameanza kuwaza nama ambavyo yeye Abramovich anawaza. Wanasema ukikaa karibu na waridi lazima unukie.

Kisha Abramivich akafanya kitu ambacho kwa kipindi kile nchini Rusia hakikuwa kimezoeleka sana japo kwa nyakati zetu hizi twaweza kuona ni cha kawaida. Abramovich akatengeneza mkakati wa namna ya 'kucheza' na media.

Jambo moja ambalo tunapaswa kulifahamu ni kwamba katika kipindi hiki kutokana na udhaifu mkubwa wa mbinu za uongozi za Yeltsin, uchumi wa Russia ulikuwa umeyumba sana kiasi kwamba mpaka serikali ilikuwa imechacha kweli kweli. Serikali kwa kipindi hicho ilikuwa inajiendesha kwa kutumia fedha za mkopo dola bilioni kumi ambazo serikali ilikuwa imekopeshwa kutoka IMF.

Sasa basi, vituo vya televisheni vyote ambavyo awali vilimilikiwa na serikali vilikuwa navyo vimebinafsishwa. Kwa hiyo hata serikali ikitaka kurusha matangazo walikuwa wanapaswa kulipia. Lakini serikali ilikuwa imechacha.

Abramovich akaitisha kikao maalumu na watu ambao walikuwa wamebinafsishiwa vituo vya habari nchini Russia na hata wale ambao wamejitutumua kuanzisha vya kwao wenyewe. Abramovich alikuwa na ombi moja tu kwao… waache kurusha habari yoyote kumuhusu Zyuganov, mpinzani mkuu wa Yeltsin ambaye alikuwa anaongoza kwenye kura za maoni na badala yake vyombo vyote vya habari virushe habari kuhusu kampeni za Rais Yeltsn.

Abramovich akawaeleza kwamba atafanya kila namna mpaka Rais Yeltsin ashinde kiti cha Urais na akishashinda 'atawakumbuka' wamiliki hao wa vyombo vya habari kwa hicho walichokifanya.

Hakuna mmliki yeyote wa chombo cha habari ambaye alikataa 'ofa' hiyo. Hakuna ambaye hakutaka 'kukumbukwa' pindi ambapo Yeltsin akishika muhula mwingine.

Katika kundi hili la wamiliki wa vyombo vya habari ambao Abramovich alikuwa anamlenga hasa alikuwa ni swahiba wake wa zamani Berezovsky. Yule Oligarch ambaye alimtambulishaga kwa Yumachev. Berezovsky alikuwa anamiliki 'media house' ambayo ndiyo ilikuwa ina ushawishi kuliko vyombo vingine vyote. Sio tu kwamba alikuwa amemlenga kwa kuwa alikuwa na media house yenye nguvu zaidi, Abramovich alikuwa na wazo lingine la siri zaidi, wazo mwanana kabisa ambalo kama likitimia basi laweza kumfanya ghafla kuwa moja ya watu matajiri zaidi nchini Russia na duniani. Nitaeleza baadae…

Kampeni ikaendelea… kufumba na kufumbua, kila televisheni, kila redio, kila gazeti kila siku kukicha kulikuwa na habari moja tu, Boris Yeltsin, Boris Yeltsin, Boris Yeltsin. Tofauti na ambavyo Yeltsin alikuwa amezoeleka kwamba sio 'mtu wa watu' lakini ghafla Yeltsin alionekana akiwa na haiba nyingine mpya kabisa. Kila siku yuko mahala fulani… leo ametembelea shule fulani ya upili Moscow, kesho yuko sokoni akisikiliza shida za wachuuzi, kesho kutwa yuko kiwanda fulani akila chakula cha mchana na wafanyakazi. Warusi walishuhudia Yeltsin mpya ambaye hawakuwahi kumuona. Yeltsin akaongeza ruzuku kwa wanafunzi, akatoa fedha nyingi kutoka serikalini mabilioni kwa ajili ya kuwalipa pensheni wazee. Na kila hatua, kila kitu haijalishi ni kikubwa au kidogo ndogo kiasi gani kiliripotiwa na kila chombo cha habari nchini Russia.

Vyombo vya habari vilimpamba kwa kila namna ambayo waliweza huku wakiwaeleza wananchi kwamba wakimchagua Zyuganov kutokana na sera zake zinaweza kuifanya Urusi kuingia kwenye vita.

Mara moja mikutano ya kampeni ya Yeltsin ikaanza kujaa watu kwa mafuriko. Yeltsin akageuka kuwa 'sweetheart' wa Warusi wote. Katika mikutano Yeltsin aliongea kama mtu muungwana tofauti na kawaida yake ya kufokafoka kama jendaheka. Aliongea kwa ustaarabu na kumwaga ahadi kedekede.

Siku ya uchaguzi ikawadia, December 5, 1996. Kura zikapigwa. Siku moja mbele matokeo yakatangazwa… Boris Yeltsin alikuwa ameshinda kti cha Urais kwa kupata 52% ya kura zote zilizopigwa. Yaani kama mtu alikuwa amelala usingizi miezi mine nyuma na kuamka siku hiyo umwambie Yeltsin alikuwa amemshinda Zyuganov angeweza kukuona ni mwendawazimu.

Yaani ndani ya miezi mine tu, 'adacadabra' za mikakati ya Abramovich zilikuwa zimebadili mioyo ya warusi kumchukia Yeltsin na sasa kuwa 'sweetheart'. Ilikuwa nikitu ambacho hata Yeltsin mwenyewe hakutegemea.

Baada ya Yeltsin kuapishwa kushika muhula mwingine wa uongozi watu wa kwanza kuhakikisha wanapata 'mnofu' mnono zaidi walikuwa ni ule Utatu Mtakatifu. Tatyana, Yumachev na Abramovich. Tatyana akateuliwa na baba yake kuwa rasmi mshauri wake mkuu. Yumachev akateuliwa kuwa katibu Mku Kiongozi… na Abramovich… naam Abramovich akateuliwa kuwa nani? Waziri Mkuu? Hapana… Waziri wa Mambo ya Nje? Hapana… Waziri wa Ulinzi? Hapana… aliteuliwa kuwa nani?

Abramovich alikataa kupewa nafasi yoyote ile ndani ya serikali. Uwendawazimu? No… Abramovich, a born tactician… anaona kile ambacho wengine hawakioni.

Alimweleza tu Yeltsin kwamba ameshiriki namna ile katika uchaguzi na kuhakikisha anashinda kwa kuwa anampenda Yeltsin kama baba yake kabisa na anadhani ndiye mtu sahihi zaidi kuingoza Russia.

Moyo wa Yeltsin ukamomonyoka na kububujikwa kabisa… hakika huu ni upendo wa kuzidi kipimo, mtu anakupigania kwa jasho na damu ushinde kiti cha Urais alafu hataki umlipe kwa kumpa cheo chochote? Yeltisn akajihisi kama amepata mtoto wa kiume ukubwani… tena mtoto mtiifu na mwenye kumpenda baba yake.

Japokuwa kipindi hiki Abramovich hakuwa tajiri kabisa hata kidogo kama tumjuavyo sasa, lakini Abramovich alikuwa anajua ni nini anakitaka… hakutaka papara ya kurukia vyeo vya serikali… alijua lengo lake hasa liko wapi. Kila kitu sasa kilikuwa kiko sawa, mkakati wake umeenda vile ambavyo alikuwa amepanga. Kitu pekee alichohitaji sasa ilikuwa ni subira… naam, subira… subira ni 'necessary ingredient of genius'.

Akasubiri serikali iundwe. Wagawane vyeo. Walioukwaa uwaziri na ukuu wa maidara washerehekee na kupongezana, kisha aingie 'kazini'.

Miezi kadhaa ikapita… serikali mpya ikiwa imeshaundwa na imetengemaa na inafanyakazi zake kama kawaida. Huu sasa ulikuwa ni wakati muafaka aliokuwa anausubiri.

Siku hiyo miezi ya mwanzoni kabisa mwa mwaka 1997 akampigia simu yule swahiba wake wa zamani, Bw. Berezovsky. Yule jamaa mwenye media house yenye nguvu zaidi kipindi kile nchini Urusi, ambaye pamoja na wamiliki wengine wa vyombo vya habari kipindi kile cha kampeni Abramovich aliwaomba wamsaidie Yeltsin kushinda kiti cha Urais na kuwaahidi Yeltsin atawakumbuka kwenye utawala wake.

Alipompigia simu na Berezovsky kumuuliza wanakutana kwa lengo gani…. Akamjibu jibu moja tu kwamba, "muda wa Rais kuwakumbuka umewadia.!"

Boris hakujua na hakuna ambaye angeweza kujua zaidi ya Abramovich mwenyewe kwamba, ndani ya wiki chache baada ya simu hiyo Abramovich alikuwa anaelekea kuwa moja ya binadamu mwenye utajiri mkubwa zaidi juu ya uso wa dunia.

Baada ya kikao hicho muhimu kati ya Berezovsky na Abramovich kufanyika na mambo ya siri kukubaliana… hatimaye ukasubiriwa utekelezaji.

2

Hapa nieleze kidogo,

Sehemu kubwa ya Urusi (kwa maana ya ardhi) ni jimbo kubwa linaloitwa Siberia. Siberia inajulikana kutokana na hali yake ya hewa ya baridi kali kupitiliza pamoja na barafu kwa muda mwingi wa mwaka. Lakini pia Siberia ina kitu kingine adhimu zaidi duniani… "dhahabu nyeusi"… mafuta. Jimbo la Siberia lina utajiri mkubwa mno wa mafuta na sehemu kubwa ya utajiri huu wa mafuta unamilikiwa na kampuni yenye kuitwa Sibneft

ambayo wanamiliki eneo la visima vya mafuta lenye eneo kubwa zaidi ambalo linaweza kulingana kabisa na ardhi yote ya nchi ya Wales kama tukilinganisha kwa ukubwa wa ardhi.

Hapa ndiko hasa ambako Abramovich alikuwa amepalenga.

Baada ya uchaguzi kuisha na serikali kuanza kufanyakazi, Abramovich akamfuata Rais Boris Yeltsin na kumkumbusha kwamba wakati wa 'kuwakumbuka' ma-oligarch waliowasaidia kwenye uchaguzi umewadia. Kama ambavyo yeye Abramovich hakutaka kupewa cheo chochote kile serikalini ndivyo vivyo hivyo pia alipendekeza kwamba ma-oligarch wengine 'wakumbukwe' kwa namna nyingine badala ya kufikiria tu kuwapa vyeo vya kiserikali.

Ukawekwa utaratibu wa kubinafsisha makampuni mengine ya umma ambayo bado yalikuwa chini ya serikali. Makampuni yakabinafsishwa kwa ma-oligarch. Abaramovich hakuzuzuka na kutaka kudandia hisa kwenye kampuni nyingine hizi, kichwani alikuwa na lengo moja tu… target moja tu ambayo alitaka kuifikia.

Visima vya mafuta ni rasilimali adhimu kwa nchi yeyote ile. Kwa hiyo japokuwa Russia ilikuwa kwenye uwendawazimu wa ubinafsishaji kiholela lakini ilipofika kwenye visima vya mafuta ilikuwa ni suala lilifanyika kwa tahadhari kubwa zaidi. Naam, viko visima vya mafuta ambavyo vilibinafsishwa lakini visima vya mafuta vya kumilikiwa na kumpuni ya Sibneft viliwekewa utaratibu maalumu na ikulu.

Uzuri au ubaya ni kwamba katika kipindi hiki ulikuwa ukiongelea ikulu ya Russia unaongelea 'Utatu Mtakatifu', Abramovich, Tatyana na Yumachev.

Watatu hawa wakaandaa utaratibu maalumu wa namna ya kuibinafsisha kampuni ya Sibneft. Nisisitize tena, Sibneft wanamiliki 'oil fields' kubwa kuzidi ardhi yote ya nchi kama Wales. Na katika miaka hii kampuni ya Sibneft ilikuwa na thamani ya zaidi ya dola Bilioni 50 za kimarekani (zaidi ya trilioni 120 za Kitanzania).

Utaratibu ukaandaliwa. Roman Abramovich akahakikisha anaweka vigezo na masharti kadhaa ya mtego mtego ili kukwamisha wengine. Hatimaye mnada wa kuiza Sibneft ukafanyika lakini ajabu ni kwamba katika mnada alijitokeza 'bidder' mmoja tu. Ni nani huyu? Nitaeleza…

Bidder huyu alitoa ofa ya kuinunua Sibneft kwa kiasi cha dola milioni 150.!! N

Nisisitize na kukumbusha tena, Sibneft walikuwa na 'oil fields' ukubwa zaidi ya nchi ya wales na 'valuation' yake ilikuwa ni zaidi ya dola bilioni 50. Auction ikafanyika… Sibneft ikauzwa kwa mwekezaji huyu.

Naamini tayari tunaweza kubashiri kwamba 'bidder' alikuwa ni Roman Abramovich. Lakini swali ni kwa namna gani Abramovich anaweza kuwa na dola milioni 150 kwa kipindi kile kuinunua Sibneft??

Nilieleza awali kuhusu kikao cha Abramovich na Berezovsky wiki kadhaa baada ya uchaguzi mkuu. Katika kikao kile Abramovich alimpa 'ofa' mentor wake huyo kwamba kwa ushawishi alionao sasa kwa Rais Yeltsin anaweza kutengeneza mazingira wao wawili wauziwe visima vyote vya mafuta na mali za kampuni ya Sibneft lakini akamweleza kuwa anahitaji kitu kimoja tu kutoka kwake… fedha. Makubaliano yao ni kwamba Berezovsky atatoa rasilimali fedha na Abramovich atahakikisha anatengeneza mazingira Ikulu na kuhakikisha kwamba kampuni hiyo inatua kwenye mikono yao.

Ndio kusema kwamba Sibneft kampuni yenye kumiliki visima vya mafuta kwenye eneo kubwa sawa na chi ya Wales, kampuni ambayo 'valuation' yake inanesa kwenye dola bilioni 50 ikauzwa kwa Abramovich na Berezovsky kwa dola milioni 150 tu… hela ya ugoro kama asemavyo mzee Rugelamarila. Yaani kitendo cha wao kukabidhiwa tu kampuni siku hiyo hiyo uwekezaji wao uliwalipa faida karibia 400%. Miaka miwili baadae uwekazaji wao huu ulikuja kuwalipa karibia mara 1000 ya fedha waliyonunulia kampuni?

Lakini kama ambavyo nilieleza awali kwamba Abramovich alikuwa mahiri wa mifumo ya kibepari inavyofanya kazi kuwazidi watu wengi nchini Russia kipindi kile na hata serikali yenyewe ambayo bado ilikuwa na tongotongo za ujamaa machoni. Kwa hiyo hata kwenye ununuzi wao wa Sibneft hawakununua tu kichwa kichwa kwa kuweka majina yao kwenye makaratasi ya umiliki bali aliweka mfumo complex wa umiliki kuhakikisha kwamba ni ngumu kufahamu hasa nani anamiliki hisa kiasi gani kwenye kampuni,na nani anapokea dividends kiasi gani na bila kusahahu kuhakikisha wanalipa kodi ndogo iwezekanavyo kwenye mapato.

Nitoe mfano kidogo kabla ya kwenda mbali zaidi… sijui ni wangapi wanakumbuka mwaka 2013 mwishoni ndugu Rostam Aziz alipouza nusu ya hisa zake za kampuni ya Vodacom kwa karibia bilioni 400 za Kitanzania. Jambo la kufurahisha ni kwamba tulipata kodi kiduchu mno, yani kiduchu haswa kutoka kwenye uuzaji huo wa hisa tofauti na ambavyo tulitegemea. Tukabaki tumeduwaa tu wengine wakimnyooshea kidole Rostam kuwa pengine 'amecheza rafu' na watu wa system. Yes, hatukupata kodi lakini Rostam hakuvunja sheria na wala hakucheza rafu kwenye ile deal. Alitumia umahiri tu wa kibiashara… hisa zake alikuwa anazihold kupitia 'private Trust' ambayo imesajiliwa nchini Mauritus kama nakumbuka vyema. Tunafahamu namna ambavyo sheria za kodi za nchi ya Mauritus zilivyo 'loose'. Kutoka hapo mtoto wa mjini Rostam akacheza na loopholes za sheria za kimatafa na hata za nchi yetu wenyewe na deal ikafanyika huku vibunda vikibaki mfukoni mwake na vingine kwenda serikali ya Mauritus na kiduchu tukapata sie akina yakhe. Maarifa… maarifa… maarifa.

Hii ndio sababu huwa naamini kwamba Idara ya Usalama wa Taifa wanapaswa kufanya mageuzi ya kusudi kabisa kuhakikisha wanaenda na kasi ya ulimwengu. Kwa mfano maafisa kwenye 'directorate' ya Collection wengi ni watu wazima. Mindset zao bado zimejiseti kana kwamba tunakabiliana na adui aliyebeba AK47. Zama zimebadilika mno, adui sasa habebi guruneti… adui sasa hivi anaweza kuwa amejificha tu mahala fulani chumbani na laptop mkononi kama silaha yake na akaitikisa nchi. Adui sasa hivi hawazi tena kupindua nchi bali anafanya hila kuhujumu mfumo wa uchumi… adui sasa hivi hataki madaraka bali anataka kumiliki njia na nyenzo za uchumi wa nchi. Tuko kwenye zama ambazo maafisa wetu wa Idara ya usalama wa Taifa wanapaswa kujua namna ya kunyumbulika na kizazi hiki cha sasa na changamoto zake.

Idara yetu kwa sehemu kubwa inafanya kazi kwa kutegemea 'Humint' kama waitavyo wenyewe na 'open source intelligence' kitu ambacho sio kibaya sana kutokana na uhalisia wa nchi yetu na uwezo wetu kama nchi na rasilimali tulizonazo. Kwa hiyo ni muhimu sana sana, kuwa na maafisa ambao wanaweza kunyumbuka na uhalisia wa nyakati tulizonazo pamoja na kuwa na mindset sahihi. Unapokuwa na maafisa wenye mindset ya enzi zile za kupambana na adui amebeba AK47 akitaka kushika dola ni ngumu kwake kung'amua vipaumbele anavyotakiwa kujishughulisha navyo na mwisho wake tutahoji juu ya ubora wa intelligence tunayoipata na mwisho wa siku itaathiri hata ufanyaji kazi wa watu wa 'directorate' inayosimamia processing. Kinachokuja kutokea ni kwamba pale kitengoni, idara inayohusika na Tasking inajikuta ina-allocate resources nyingi (kwa maana ya maafisa, muda, wataalamu mahususi) kwenye masuala ambayo pengine hayakupaswa kuwa vipaumbele. Lakini mzizi unaanzia wapi? Idara inayohusika na Collection… tupunguze maafisa watu wazima au kwa usahihi zaidi niseme tuhakikishe tuna maafisa ambao wanaendana na kizazi cha sasa na mnyumbuliko wake… sioni faida au ufanisi unaopatikana kwa kuweka watu wazima wengi kwenye idara hii. Sio kwamba wasiwepo, la hasha… mtu mzima dawa bhana… lakini tupunguze. Lazima watu walioko kwenye kitengo mahususi kwa ajili ya idara hiyo waweze kunyumbulika na zama tulizonazo… nature ya adui imebadilika mno… na sisi tunapaswa kujiboresha.

Kuna mtu atasema "…wewe The Bold unajifanya unajua kuliko Usalama wenyewe…?" tabia na swali kama hili ndio kwa umombo tunasema kuwa ni "Obnoxious".

Hivi EPA, Richmond, Escrow n.k. hizi 'abracadabra' zilivyotokea tulikuwa wapi? Hatukujua kabla ya kutokea? Tulijua. Tulikuwa na nia ya kuzuia. Yes tulikuwa na nia… kwa nini hatukufanikiwa?? Ndio maana tunashauri, kwenye hili suala la Collection ya intelijensia hebu tufanye mageuzi makini pale… nature ya adui imebadilika lazima tujue namna ya kunyumbulika na zama hizi.

Tuache hayo, nahisi naanzisha mada ndani ya mada…

Lakini nimetoa mfano huu ili kuelewa namna ambavyo Abramovich aliweza kucheza na nyakati… wananchi, serikali na hata Idara zake bado walikuwa na 'hangover' ya ujamaa wakati ambao Abramovich alikuwa tayari ana umahiri wa namna ubepari unafanyakazi.

Nimeeleza kwamba ili kuhakikisha yeye Abramovich na mentor wake Berezovsky wanaficha kiwango chao cha umiliki wa Sibneft, lakini pia kuhakikisha wanalipa kodi kiduchu iwezekanavyo na 'kucheza' za mfumo wa mgawanyo wa dividends (kiasi kidogo kilikuwa kinapaswa kwenda serikalini) Abramovich na mwenzake hawakuweka majina yao moja kwa moja kwenye nyaraka za umiliki. Je, nyaraka zilionyesha nani wamiliki wa Sinbeft.

Kipindi hicho ilikuwa ukichimba kwenye nyaraka za ulipaji wa dividends wa Sibneft unakutana na majina matano tu… CarbonRow ltd, Craven Investments, Gemini Co., MarteChelo Plc na White Pearl ltd. Makampuni manne kati ya haya matano yalikuwa yamesajiliwa nje ya Russia nchini Cyprus, moja ya nchi inayojulikana ulimwenguni kwa kuwa na sheria loose mno za masuala ya kodi na benki. Swali ni akina nani hasa wanamiliki makampuni haya? Tuchukue kwa mfano CarbonRow ukiitazama kwenye nyaraka za kumbukumbu inaonyesha kwamba CarbonRow inamilikiwa na 'private trust' inayoitwa MERITSERVUS (TRUSTEES) LIMITED. Nani anamiliki Meritservus Ltd? Dimitris Yunidis…ni nani huyu? Ukichimba ndani zaidi ni kwamba Dimitris ni Accountant ammbaye anamiliki kampuni inaofanya 'flagging' ya 'shell companies'. Kwa kifupi tu ni kwamba kadiri unavyochimba ndio unazidi kuchanganyikiwa na huwezi kuliona jina la Abramovich au Berezovsky na hata ukifanikiwa kuliona huwezi kuona kiwango cha dividends anacholipwa yeye binafsi au kiwango cha umiliki wake wa Sibneft.

Lakini inakadiriwa kwamba Abramovich alikuwa anamiliki 51% ya Sibneft na asilimia zilizobaki walimiliki Berezovsky na serikali ya Russia. Kisheria kwa sababu yeye ndiye alikuwa anamiliki hisa nyingi zaidi, kwa maneno mengine yeye ndiye alikuwa mwenye kauli ya mwisho ndani ya Sibneft , na kwa maneno mengine Sibneft ilikuwa ni kampuni yake.

Ndani ya mwaka mmoja tu baada ya yeye na Berezovsky kununua Sibneft, Roman Abramovich, kijana yatima aliyekulia kwenye umasikini wa kutupwa ambaye miaka mitatu tu nyuma alikuwa anauza wanasesele na matairi chakavu, mara moja alipanda chati na kufikia status ya ubilionea ambapo kwa kipindi kile utajiri wake ulikuwa unafikia dola 3.4 bilioni za kimarekani (kama trilioni 7 za kitanzania) na hii ikamfanya kuwa oligarch kijana zaidi kipindi hicho nchini Russia akiwa na miaka 31 tu.

Lakini wanasema penye riziki hapakosi fitina… Naam, kitendo hiki cha Abramovich kutumia ushawishi alionao Ikulu kujilimbikizia utajiri wa kutupwa kiliwaudhi baadhi ya watu wa 'system'. Kuna watu waliumia pia mtoto mdogo wa miaka 31 hata harufu ya maziwa haijamuisha ati leo anakuwa oligarch. Ikaanza minong'ono na vuguvugu la chini kwa chini kuwapiga vita Abramovich na Berezovsky.

Vuguvugu hili likaenda mbali zaidi ambapo mwendesha mashtaka mkuu wa serikali kipindi hicho Bw. Yuri Skuratov alifanya mkutano na wanahabari na kusema kwamba anakusanya ushahidi ili afungue mashtaka dhidi ya baadhi ya ma-oligarch. Japo hakuwataja majina lakini kila mtu alijua anamlenga nani.

Lakini Abramovich alikuwa mboni ya Rais Yeltsin. Rais akamuita Mwendesha Mashtaka mkuu wa serikali na kumtaka aachane na jambo hilo… Yuri Skuratov akakataa.

Yeltsin akajaribu kumfukuza kazi, lakini bunge likapinga uamuzi huo wa Rais na kumrejesha kazini Bw. Yuri Skuratov. Wabunge walikuwa na vihoro… roho ziliwauma kijana mdogo kama Abramovich kuwa na ushawishi mkubwa hivyo kwenye nchi ambayo miaka si mingi ilikuwa ndiyo 'superpower' ya ulimwengu.

Yuri Skuratov aliporejeshwa kazini na bunge kiburi kikamjaa zaidi… akaitisha mkutano mwingine na wanahabari na kuwaeleza kuwa ana ushahidi wa kutosha dhidi ya Roman Abramovich na Berezovsky na anakusudia kuwafungulia mashtaka ya kuhujumu uchumi. Watu wa system walifurahi kweli kweli wakijua huo ndio mwisho wa Abramovich… kama wangelijua kipindi kile Abramovich ni mtu wa namna gani wasingelithubutu kumtikisa. Walikuwa wanapima kina cha bahari kwa goti la mguu…

Mara ya mwisho nilieleza kuhusu mwendesha mashtaka mkuu wa serikali Bw. Yuri Skuratov akijitapa kuwa ana ushahidi wa kutosha kumfungulia mashtaka oligarch Roman Abramovich na ameweka nia kumburuza mahakamani siku si nyingi.

Kuna suala moja la msingi sana… katika nchi za Ulaya mashariki pamoja na nchi za ulimwengu wa tatu, ukiona mtu amechuma utajiri mkubwa wa kutisha basi ufahamu kuwa si mtu wa 'mchezo mchezo'. Kwa namna ambavyo serikali zetu na biashara zetu zinaendeshwa katika nchi za ulimwengu wa tatu namna pekee unaweza kuushinda 'uhuni' ni kwa kuwa 'muhuni' wewe mwenyewe pia. Mambo kwenye nchi hizi hayaendeshwi kwa kanuni za ustaarabu kama kwenye ulimwengu wa kwanza… kwa hiyo ni eidha ujifunze kula nyama za watu au usubiri wewe ufanywe kitoweo.

Ndio maana utaona kuna mjasiriamali maarufu na mwenye mafanikio makubwa sana hapa nchini, tumuhifadhi jina maana ni marehemu kwa sasa amefariki kama miezi mitatu iliyopita… alikuwa yuko vizuri haswa na kitengo chake binafsi cha ulinzi na 'intelijensia'. Kuna watu watashangaa, ati yule mzee mwenye media house kubwa nchini ana kitengo binafsi cha intelijensia? Naam, na kiko vizuri haswa… well, si kitengo kikubwa haswa kufananisha na jamaa zetu wa Oysterbay au makumbusho, bali ni kitengo cha ulinzi haswa lakini kiko very well equipped kufanya ushushushu wa kibiashara na hata mwenendo wa nchi na viongozi wake.

Na ndio maana pia Askofu maarufu sana hapa nchini ambaye hakauki kutoa matamko yenye utata unaweza kujiuliza anawezaje 'ku-survive' na hata muda mwingine vyombo vya usalama kupigwa chenga… jawabu ni hilo hilo, ana kitengo maridhawa mno cha ulinzi na usalama ambao pia wako vyema mno kwenye kufanya ushushushu. Tena huyu askofu nimeshuhudia kwa macho yangu na naweza kusema kabisa kwamba ni kitengo chake cha usalama kiko mbali zaidi kushinda hata wafanyabiashara wengi hapa nchi… kiko very sophisticated.

Kwa nini nasema haya? Ni kwa sababu sisi wafanyabiashara wetu wanayafanya haya leo hii, Roman Abramovich alikuwa ameshaanza kukifanya kitu hiki tangu miaka ya mwanzoni mwa tisini na alikuwa anakifanya kwa ufanisi mkubwa haswa.

Ndani ya kampuni ya Sibneft alikuwa ameunda kitengo maalumu cha ulinzi na usalama. Kazi ya kitengo hiki, Mosi, kilihusika na ulinzi wa kawaida wa mali za kampuni. Lakini pia ndani yake kulikuwa na idara maalumu ya siri ambayo Abramovich mwenyewe aliita SUR ambayo ilikuwa inahusika na ukusanyaji wa intelijensia juu ya washindani wao wa kibiashara pamoja na viongozi wa serikali na hapa hasa ndiko ninapotaka kupaongelea.

Kitengo hiki cha SUR kama ambavyo Abramovich mwenyewe alipendelea kukiita walikuwa na intelijensia ya kutosha juu ya viongozi wengi wa serikali na mmojawapo akiwa ni mwendesha mashtaka mkuu wa serikali Bw. Yuri Skuratov.

Wanasema kila binadamu chini ya jua kuna 'mafuvu' ameyaficha kabatini. Kila mtu ana siri ambayo anatamani afe nayo. Siku ambayo adui zako wakigugundua siri hiyo ndio inakuwa kiama chako kama ambavyo ilimtokea mwendesha mashtaka Skuratov.

Baada ya joto la mwendesha mashtaka wa serikali kutaka kumshtaki Abramovich kupanda, Oligarch Berezovsky alikaa na Abramovich kumuuliza ana mpango gani na hicho ambacho kinaelekea kutokea. Abramovich akamuondoa wasiwasi, akamwambia tu anahitaji msaada mmoja kutoka kwake.

"Anything you want.!" Berezovsky akamjibu .

Abramovich akamuomba Berezovsky ampatie nusu saa tu katika televisheni yake muda wa usiku, kiandaliwe kipindi maalumu kwa ajili yake. Nilieleza kwamba kwa kipindi hicho Berezovsky alikuwa anamiliki kituo cha televisheni ambacho ndicho kilikuwa kinatazamwa zaidi nchini Russia. Berezovsky bila kusita akawasiliana na meneja wa kituo chake cha televisheni na kumueleza kwamba atenge muda huo wa nusu saa majira ya usiku ndani ya siku mbili zijazo kwa ajili ya Oligarch Abramovich kuongea.

Muda ukapangwa na siku ya Abramovich kuongea ikawekwa kwenye ratiba.

Ikapigwa 'promo' ya kutosha kutangaza siku hiyo husika na muda husika ambao Oligarch Roman Abramovich ataongea kupitia televisheni kujibu shutuma ambazo zimekuwa zikielekezwa kwake kuhujumu uchumi wa nchi. Ajabu ni kwamba muda huu ambao ulitangazwa Abramovich ataongea ilikuwa ni saa tano usiku na kuna angalizo lilitolewa kwamba wazazi wahakikishe asiangalie mtoto mwenye umri chini ya miaka 18.

Watu walikumbwa na butwaa… Abramovich anataka kuongea nini hicho ambacho watoto hawapaswi kukisikia.?

Yuri Skuratov mwenyewe alifahamu ni 'tsunami' gani ilikuwa inakuja japo hakutaka kuamini.

Siku ikawadia, muda ukawadia… saa tano kamili usiku, Abramovich alikuwa mubashara kwenye runinga kujitetea tuhuma zake. Nadhani wengi tunafahamu namna ambavyo Abramovich anaongea, anaongea taratibu mno na kwa sura ya upole haswa. Upole wake anapoongea unaweza kumfananisha na kijana Jared Kushner, mastermind aliyemuingiza Trump whitehouse. Hapa kwetu waweza kumfananisha na marehemu mzee wetu Mengi labda au Ruge Mutahaba… wote hawa mastermind wa masuala mengi ya nchi japo kwa namna wanavyoongea taratibu na kwa upole unaweza kudhani ni magoigoi tu. Lakini waguse uone cha mtema kuni…

Kipindi kilipoanza Abramovich akajieleza kwamba anaonewa wivu na wanasiasa kutokana na mafanikio yake ya kibiashara. Abramovich akajitetea kwamba mafanikio yake hayo si kwa ajili yake tu bali pia ni kwa ajili ya familia nyingi masikini ambao nao watanufaika (miaka michache baadae Abramovich alitumia fedha zake binafsi zaidi ya dola bilioni tatu (zaidi ya trilioni 6.7 za Tanzania) kwa ajili miradi ya maendeleo kwenye moja ya majimbo masikini zaidi nchini Russia, nitaeleza).

Akajitetea zaidi kwamba wanasiasa hao wanamtumia mwendesha mashitaka Yuri Skuratov ili amchafue na kumuondolea imani kwa wananchi wenzake. Kisha Abramovich akamalizia kwa kusema kwamba anao ushahidi kuthibitisha kwamba Skuratov ni mtu wa hovyo kabisa ambaye hapaswi kuaminiwa na jamii.

Alipomaliza kusema hayo mkanda wa video ukaanza kuchezwa kwenye runinga. Video hiyo ilikuwa inamuonyesha Yuri Skuratov akiwa uchi wa mnyama kwenye chumba cha hoteli akifanya ngono mabinti wadogo wawili waliokadiriwa mmoja kuwa na miaka kumi na mitano na mwingine miaka kumi na sita. Video inamuonyesha binti mmoja akimfanyia kitendo cha ngono kwa kutumia midomo yake na huku mwingine akimpapasa mwilini na kubusiana.

(natamani kuiweka hapa video lakini sidhani kama itakuwa sawa kwa sababu za maadili na sidhani kama ni lazima sana kuitazama… nimepiga 'screenshots' tu ili walau upate picha wa kilichotokea)

Ilkuwa ni tsunami na ambayo haikutegemewa… Abramovich akaongeza kuwa anao 'ushahidi' wa wanasiasa wengi wanaompinga kuwa ni watu wa hovyo na mafisadi waliojawa wivu. Kwa maneno mengine alikuwa anatoa 'warning' kwa wapinzania wake kwamba anao ushahidi wa mauzauza wanayoyafanya gizani.

Nchi ya Urusi ilitetema usiku mzima. Kesho yake asubuhi Skuratov akajaribu kujitetea kwamba mkanda huo wa video ni feki lakini hakuna ambaye alimuamini. Yeye ambaye alikuwa kwenye harakati za kumfungulia kesi Abramovich kibao kiligeuka kwake, akafunguliwa mashataka ya unyanyasaji wa kingono kwa watoto ambao hawajafikia umri halali kisheria kujihusisha na vitendo vya ngono. Kutokana na kushtakiwa kwa kesi hiyo akashinikizwa pia kujiuzulu wadhifa wa mwendesha mashtaka mkuu wa serikali.

Skuratov akapotea kwa namna hiyo na hata tuhuma zake dhidi ya Abramovich zikafa kibudu kwa mtindo huo pamoja naye.

Abramovich sasa akawa anaogopwa pale Moscow. Wapinzani wake wakikutana naye walitamani hata wamuamkie japo ni kijana mdogo kwao. Walifahamu kuwa ana ushahidi wa mauzauza yao na anaweza kuyaachia kwa umma muda wowote ule. Hiyo ilikuwa ni kinga tosha kwake Abramovich.. sasa alikuwa ni 'untouchable'. Hakuna ambaye alikuwa anathubutu kumnyooshea kidole…

Hii ilikuwa ni fursa adhimu kwake kutimiza lengo lake la pili kwenye kujilimbikizia mabilioni ya dola. Lengo hili la pili lilikuwa ni kushikilia sekta ya uzalishaji Aluminum. Rusia ni mzalishaji mkuu wa Aluminium duniani na kipindi kile miaka ya tisini asilimia kubwa ya aluminium ambayo ilikuwa inatumika duniani ilikuwa inatoka nchini Rusia. Abramovich alikuwa anataka kuweka mguu wake kwenye sekta hii… mguu mmoja tayari alikuwa ameuweka kwa uthabiti kabisa kwenye sekta ya mafuta na gesi.

Lakini kulikuwa na tatizo kubwa zaidi linawakabili ma-oligarch. Na lilikuwa tatizo kubwa zaidi ambalo lilikuwa linatishia utajiri wao kupotea na hata uhai wao… kulikuwa na kila dalili kwamba Rais Boris Yeltsin alikuwa amekumbwa na tatizo la ugonjwa fulani wa akili.

Mwanzoni watu walidhani ni ucheshi tu lakini kadiri siku zilivyoenda kulikuwa hakuna ubishi kwamba Yeltsin alikuwa amekumbwa ghafla na tatizo la akili. Kwanza alikuwa amekuwa mlevi kupindukia… alikuwa analewa mpaka muda wa kazi. Kuna siku alikuwa anahutubia taifa akiwa amelewa chakali. Alikuwa anasoma sentesi moja dakika tano nzima. Siku nyingine alihudhuria mazishi ya jenerali wa jeshi akiwa amelewa chakali tena. Hata ulipofika muda wake wa kutoa heshima za mwisho kwa marehemu ambapo unasogelea jeneza na kupiga saluti, Yeltsin aliposogelea jeneza ili apige saluti nusura adondoke kwa kupepesuka. Ilibidi mpaka walinzi wake wamshike kama mtoto ndio asimame sawasawa na kupiga saluti.

3

Siku nyingine wako kweye halaiki ya kitaifa… wakati wimbo wa taifa unaimbwa Yeltsin akainuka na kwenda kumpokonya kipaza sauti mwendesha shughuli na kuanza yeye kuongoza kuimba wimbo wa taifa huku akiimba hovyo hovyo na kwa sauti ya ulevi.

Yeltsin alikuwa na tatizo na alikuwa anatakiwa kuondolewa madarakani haraka iwezekanavyo. Kama wakifanya uzembe na bunge likamuondoa madarakani Yeltsin na kumuweka mtu wao kuna kila dalili kwamba mali zao zote zitataifishwa na hata wao wenyewe kuishia jela maana wanasiasa wengi ndani ya Moscow walikuwa na hasira na namna ambavyo ma-oligarch wanaitafuna nchi kwa kukingiwa kifua na Yeltsin.

Lilikuwa linahitajika suluhisho la haraka kabla mambo hayajaaribika. Ma-oligarch wote walimtazama Abramovich, tumaini lao lilikuwa kwake atoe wazo wapate suluhu wa nini kifanyike.

Kwenye sehemu iliyopita nilieleza kwamba afya ya mwili na akili ya Rais Boris Yeltsin haikuwa imara mwishoni mwa miaka ya 1995 mpaka mwanzoni mwa 1996. Yeltsin alikuwa kiroja kila ambapo alikuwa mbele ya umma. Ma-oligarch wakaanza kukuna vichwa kutafuta mrithi wake kabla ya bunge la Urusi kumuondoa Yeltsin kwa lazima na kumweka mtu wao. Lakini katika juhudi hizi ma-oligarch macho yao yote yalikuwa kwa Roman Abramovich.

Sasa, nianze kwa kusema hiv…

Kuna suala moja la kushangaza sana kuhusu Putin. Kama ni mfuatiliaji wa mambo utakuwa umeshuhudia kwa mara kadhaa na kwa miaka kadhaa amekuwa na migogoro karibia na kila Oligarch nchini Urusi isipokuwa Roman Abramovich pekee. Tena ajabu ni kwamba Abramovich ikitokea anashambuliwa labda na vyombo vya habari vya magharibi, Putin huwa ni moja ya watu wa kwanza kumtetea.

Kwa nini? Kwa sababu mwaka 1996 tofauti na mategemeo ya watu wote juu ya mrithi wa Boris Yeltsin, katika kikao cha ile inner circle ya Rais, Roman Abramovich alipendekeza jina la Vladmir Putin kuwa mrithi wa kiti cha Urais wa Urusi. Katika ulimwengu wa siasa za Urusi kipindi hicho Putin hakuwa lolote wala chochote na hata wananchi wengi hawakuwa wanamjua. Putin hakuwahi hata kuwa 'balozi wa nyumba kumi'. Lakini Abramovich alimtaka Putin amrithi Yeltsin.

Kwa nini? Kuna sababu kadhaa… sababu za wazi ambazo 'alishea' na wenzake lakini pia kulikuwa na sababu binafsi ambazo wengine hawakuzijua. Ma-oligarch kama ambavyo ilikuwa kwa warusi wengine walikuwa wanataka kuijenga upya 'image' ya kiti cha rais wa Russia. Kwa kiasi fulani 'image' ya kiti cha urais wa Russia ilikuwa imechafuka kutokana na vimbwanga ambavyo Yeltsin alikuwa anavifanya. Ma-oligarch na warusi walikuwa wanataka Rais ambaye ataakisi ukakamavu, weledi na msimamo thabiti kuitetea Russia dhidi ya mabeberu ya magharibi. Vladmir Vladmirovich Putin alikuwa na sifa hizi zote.

Lakini kulikuwa na sifa nyingine ambayo wengine hawakuijua… sifa ambayo ni Vladmir na Abramovich pekee waliifahamu.

Nitakuwa sijatenda haki nikizungumzia historia kamili ya Vladmir katika makala hii kwa maana binadamu huyu haswa anastahili nitulie nimuandikie makala yake kabisa kumuhusu yeye mahususi na wala sio kuchomekea tu historia yake ndani ya makala yenye kuhusu jambo lingine. Na kwa hakika hata makala tu tutakuwa hatujatenda haki… twapaswa kumwandikia kitabu kabisa binadamu huyu ambaye kwa mwaka wa tano huu sasa Jarida la Forbes linamuorodhesha kama mtu mwenye ushawishi zaidi ulimwenguni akimpiku Obama kwenye miaka ya mwisho ya uongozi wake na akiendelea kumburuza hata Rais wa sasa Donald Trump na pia kuwapiku miamba mingine kama Rais Xi jiping na baba mtakatifu Papa Francis. Yako mengi sana ya kuyaandika kuhusu kiongozi huyu mahiri, viko visa vingi vya kusisimua ambavyo bado wengi hawavifahamu. Yako mengi ya kujifunza na iko mikasa mingi ya kuburudisha kuhusu maisha yake.

Lakini ili niweke msingi mzuri wa hoja ya kile ambacho nakusudia kukisema kuhusu yeye na Abramovich, nitachomekea kijipande kiduchu tu walau cha historia yake.

Mwaka 1975 miezi michache baada ya kumaliza elimu ya chuo kikuu Putin alijiunga na shirika la kijasusi la KGB. Mwanzoni alipojiunga na KGB alifanyakazi ndani ya Second Chief Directorate lakini baadae kidogo akahamishiwa First Chief Directorate ambayo hasa ilihusika ushushushu pamoja na ujasusi nje ya Urusi. Jukumu lake la kwanza baada ya kuhamishiwa kwenye idara hii ilikuwa ni kufatilia nyendo za raia wa kigeni na maafisa balozi mbalimbali ambazo zilikuwa katika mji wa Leningrad ambako ndiko alizaliwa, kukulia na kusoma. Baadae kidogo alihamishwa na kupelekwa Ujerumani ya Mashariki enzi zile kabla ya taifa la ujeremani kuungana. Akiwa huko alifanya kazi yake ya ushushushu kwa kutumia 'cover' ya mtafasiri mbobezi wa lugha ya kirusi kutoka kingereza na kijerumani ambapo huduma hii alikuwa anaitoa kwa wafanyabiashara na watumishi wa serikali. Hapa ufahamu kwamba Putin anaongea lugha ya kijerumani kwa ufahasa wa hali ya juu. Kazi yake kule ujerumani ilikuwa nzito kidogo… kwanza alikuwa akikusanya taarifa juu ya serikalli lakini pia alikuwa anafanya kukusanya intelijensia za 'open source'. Intelijensia ya open source ni ile inayopatikana kutoka kwenye vyanzo vya habari ambavyo umma una 'access' navyo kwa mfano magazeti, internet, televisheni, redio na kadhalika. Ukusanyaji wa intelijensia ya namna hii inaweza kuonekana kama rahisi kulinganisha na intelijensia inayokusanywa 'covertly'. Lakini kwa maoni yangu binafsi hii ni moja kazi nzito zaidi katika ukusanyaji wa intelijensia. Hebu vuta picha kwa mfano wewe ni afisa usalama hapa nchini na kazi yako ni kukusanya intelijensia ya open source. Maana yake ni kwamba muda wote usiku na mchana unatakiwa ku-monitor habari ambazo kwenye televisheni zote nchini, radio zote muhimu, usome magazeti yote ya kila siku, ufuatilie kila habari inayo-trend jamii forums, facebook, instagram na twitter. Sasa hapa ugumu sio kufuatilia tu habari bali unapaswa kuchambu 'pumba na mchele'. Ni lazima u-prioritize habari gani inaweza kuwa na value kwa idara na habari gani ya kuipuuza na kuachana nayo. Habari hizi ambazo zinaonekana kuwa na value kuna mfumo maalumu ambao Analysts wanaziingiza kwenye database ya idara ambapo siku yoyote inaweza kuhitajika kama ikionekana inakuwa complemented na intelijensia fulani ambayo imekusanywa covertly.

Hii ndio ilikuwa kazi ya Putin kule Ujerumani Mshariki.

Baada ya ukuta wa Berlin kudondoka Putin pamoja na maafisa wengine iliwabidi kukimbia Ujerumani na kuchoma moto nyumba ambayo walikuwa wanakaa ili kupoteza ushahidi wa mafaili ya ujasusi na intelijensia waliyokuwa wanakusanya. Kuna visa vya kusisimua sana vilitokea wakati huu ambao siku nikipata fursa ya kuandika kuhusu Putin nitavieleza.

Baada ya kuondoka Ujerumani, Putin alirejea Russia kwenye mji aliozaliwa wa Leningrad ambapo KGB walimpangia jukumu jipya katika chuo kikuu cha Leningrad kitengo cha masuala ya nchi za nje. Jukumu lake hasa hapo chuo kikuu lilikuwa ni kutathimini wanafunzi ambao wana 'potential' ya kujiunga na KGB. Ni katika kipindi hiki ambacho Vladmiri Putin alipanda cheo ndani ya KGB kufikia kuwa Kanali.

Nilieleza pale juu kwamba Putin alisoma pia kwenye chuo hiki. Kipindi hicho alichosomaga alijenga urafiki mkubwa na mwalimu wake aliyeitwa Profesa Anatoly Sobchak. Kwa hiyo Putin aliporejea tena chuoni hapa japo safari hii kwa kazi maalumu alifufua upya urafiki wake na Profesa Sobchak. Kwa maoni yangu pasipo urafiki huu kamwe Putin asingekuja kuwa rais wa Russia. Nikirejea baadae kidogo nitaeleza ni kwa namna gani urafiki wake na Profesa Sobchak ulimfungulia njia za siasa ndani ya Moscow na hatimaye kuwa noticed na Abramovich na kwa sababu gani hasa zilimvutia Abramovich…

Yule mwalimu wake wa chuo kikuu Profesa Anatoly Sobchak ambaye Putin aliporejea kutoka Ujerumani na kupangiwa jukumu la kishushushu chuo kikuu cha Leningrad alifufua upya urafiki naye, mwaka 1990 Profesa Sobchak aligombea kiti cha Umeya wa mji wa Leningrad na kushinda. Baada ya kushinda kiti cha Umeya alimteua Putin kuwa mshauri wake wa masuala ya Kimataifa.

Mwaka uliofuata Putin alijiuzulu nyadhifa zake zote ndani ya KGB kutokana na kutoridhishwa na msimamo mpya wa idara hiyo na utendaji wake. Nikiwa mahususi zaidi, kujiuzulu huku kwa Putin kulikuwa ni siku ya tarehe 20 August mwaka 1991. Kama unafahamu vyema historia ya Urusi unaweza kuona kwamba hiyo ilikuwa ni siku mbili tu baada ya jaribio la kumpindua rais Michail Gorbachev. Hii ilikuwa ni namna yake Putin kuonyesha kwamba hakukubaliana na kile ambacho kilikuwa kimetokea. Uamuzi huu wa kujiuzulu kutoka shirika la kijasusi la KGB ulikuwa ni mgumu sana kwa Putin kwani maisha yake yote ya ukubwa aliyaishi kama jasusi ndani ya shirika hili.

Nchini Urusi katika ofisi ya Meya shughuli zinaendeshwa kupitia kamati mbalimbali ambazo zinakuwa chini ya ofisi ya Meya. Mwaka huo huo 1991, Putin 'akaula' tena… akateuliwa kuongoza kamati ambayo inashughulika na Mahusiano ya kimtaifa, uwekezaji kutoka nje na usajili wa makampuni (tusichanganye na kile cheo chake cha awali, "Mshauri wa Meya juu ya Masuala ya Kimatifa"). Hapa ndipo ambapo nataka hasa kupawekea mkazo zaidi.

Eneo la Leningrad lina utajiri mkubwa sana wa migodi ya chuma na uzalishaji aluminium. Kwa hiyo cheo hiki kipya cha kuongoza kamati ya kushughulikia uwekezaji, usajili wa makampuni na mahusiano ya nchi za nje kilikuwa ulaji mkubwa. Siku nikiandika kuhusu Putin nitaeleza kisanga ambacho kilitokea mwaka wake wa kwanza tu baada ya kuteuliwa kuongoza kitengo hiki mpaka kupelekea kuchunguzwa na Baraza la Bunge la Mji wa Leningrad.

Niwape kwa muhtasari tu… ni kwamba katika kipindi hiki Urusi ndio ilikuwa ina-recover kutoka kwenye mdororo wa kiuchumi. Jamii nyingi zilikuwa zinaishi kwenye umasikini wa kupitiliza. Kwenye baadhi ya miji walikuwa wanaweza masharti nafuu ya uwekezaji kama vile misamaha au unafuu wa kodi.

Sasa kuna makampuni kutoka nje ya Russia ambayo kwa maelekezo ya Putin kama mwenyekiti wa kamati ya uwekezaji ya Leningrad yaliuziwa kiasi cha 'metals' zenye thamani ya dola milioni 93 kwa makubaliano kwamba walete chakula cha msaada. Chakula hiki cha msaada hakikuonekana Leningrad. Ikazuka minong'ono kwamba kuna watu Putin alikula nao dili kwenye mchezo huu. Ndipo hapa ikaundwa tume ikiongozwa na mwanamama machachali Marina Salye……. Kuchunguza kisanga hiki. Kuna vimbwanga vingi sana ndani ya skandali hii ambavyo sitaviongelea leo hii, lakini mwisho wa uchunguzi wa kamati wakatoa pendekezo kwamba Putin afutwe kazi na pia afunguliwe mashtaka.

Lakini hakuna lolote kati ya hayo mapendekezo ambayo kilitekelezwa ambalo lilitekelezwa. Kwa nini?

Ukiwa porini, ukila nyama hakikisha unakula na simba… hakuna ambaye atathubutu kukusogolea kupoka mnofu wako.

Habari za ndani zinasema kwamba kuna uwezekano mkubwa Putin alifanya dili hii kwa kushirikiana na Oligarch Berezovsky ambaye kwa kipindi kile alikuwa na ushawishi mkubwa sana ndani ya Moscow. Tunakumbuka kwamba Borozovksy pia ndiye kwa kipindi hicho alikuwa 'mentor' wa Roman Abramovich.

Skandali hii ndio kwa mara ya kwanza ilimfanya Abramovich kumfahamu Putin na kuvutiwa naye kutokana na historia yake ya kutumikia kwenye shirika la ujasusi,uimara wa misimamo yake na pia haiba yake ya kutaka mabadiliko ya kimfumo ndani ya Russia. Putin alikuwa anajulikana mjini Leningrad kutokuung mkono sera za kijamaa ambazo zilikuwa zinatumika huko nyuma kuendesha nchi.

Wanasema ukiona vyaelea ujue vimeundwa. Ni nandra mno mno kwa mtu yeyote yule kwenye ulimwengu wa sasa kupanda mpaka nafasi ya juu kabisa ya utumishi wa nchi kama vile Urais kwa bahati mbaya. Kuna watu watasema "vipi kuhusu Trump." No, it wasn't an accident. Kuna wengine wanahisi hata rais fulani hapa Afrika Mashariki mwaka 2015 aliukwaa Urais kwa bahati mbaya bila kujua historia yake ndani ya Idara ya Ujasusi wa nchi hiyo na bila kujua kikao cha kimkakati cha April 23, 2015 kilichofanyika nje kidogo ya mji wa Morogoro kati ya maafisa waandamizi wa idara ya ujasusi wa nchi hiyo na viongozi watatu wakubwa wastaafu. Too bad siwezi kuandikia hayo mambo…

Ninachotaka kusema ni kwamba ukiona vyaelea ujue vimeundwa… ni nadra mno katika ulimwengu wa leo mtu kuinuka mpaka kufikia uongozi wa juu wa nchi kwa bahati mbaya. Kila kiongozi anaundwa na kufinyangwa na mtu fulani.

Nimeeleza kwamba skandali ya uuzaji wa 'metals' zenye thamani ya dola milioni 93 ndizo ambazo zilimfanya Abramovich kumfahamu Putin na hatimaye kuvutiwa naye… sasa taratibu Abramovich akaanza kumfinyanga Putin. Huko nyuma nilishaeleza ni namna gani ambavyo Abramovich aliweza kujijenga kiushawishi na mpaka hatimaye kuwa kati ya wale wajulikanao kama "The Family" ndani ya Moscow na hata baadae ushawishi wake kupitiliza kuwa pengine mtu mwenye kusikilizwa zaidi na Rais Boris Yeltsin.

Ni katika kipindi hiki ambacho Roman Abramovich akaanza kumjenga Putin. Nitaeleza namna ambavyo Putin alikuwa anapanda ngazi kwa kasi ya ajabu mara baada ya kwenda Moscow.

Sasa,

Katika uchaguzi ambao ulifuata yaani uchaguzi wa mwaka 1995 yule Profesa rafiki wa Putin alipoteza kiti chake cha Umeya. Hii ilimlazimu Putin kuhamia Moscow kuangalia fursa nyingine. Baada ya kuwasili tu Moscow kwa ushawishi wa Abramovich Putin aliteuliwa kuwa deputy Chief wa Idara ya Presidential Property Management. Idara hii ilikuwa inahusika na menejiment ya mali za Urusi nje ya mipaka yao (kama vile uwekezaji) lakini pia Idara hii ilihusika na kuhamisha mali za nchi ambazo awali zilikuwa chini ya Shirikisho la Urusi kabla ya kuvunjika na kuzihamishia kwenye umiliki wa Urusi ya sasa. Unaweza kuona ni kwa kiasi gani jukumu huli lilikuwa ni nyeti.

Mwaka mmoja baaadae, kwa mara nyingine tena kwa ushawishi wa Abramovich Putin aliteuliwa kuwa Naibu katibu mkuu Kiongozi. Wakati anateuliwa katika nfasi hii, ile ya ile nafasi ya kwanza pia bado alikuwa anaendelea nayo (nafasi ya Deputy Chief of Presidential Property Management Department). Miezi michache baadae ile nafasi ya kwanza ambayo aliteuiwa kama Deputy chief, akapandishwa cheo kuwa Chief. Kwa hiyo kwa wakati mmoja Putin alikuwa ni Naibu katibu Mkuu kiongozi na pia alikuwa Chief of Presidential Property Management Department.

Kila baada ya miezi kadhaa Putin alikuwa anapanda cheo kwa kasi ya ajabu na kuna mahala maalumu ambako Abramovich alikuwa anataka Putin afike.

Siku ya tarehe 25, July mwaka 1998 kwa nguvu na ushawishi wa muda mrefu wa Oligarch Roman Abramovich… Putin aliteuliwa kuwa Mkurugenzi mkuu wa Federal Security Services (FSB). Hii FSB ndio idara ambayo iliundwa kurithi kazi za kijasusi za KGB ambayo ilivunjwa. Kwa hiyo kwa muda wa miaka miwili tu tangu aingie Moscow Putin alikiwa amepanda vyeo kwa kasi na sasa alikiwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa wa Russia.

Usione vyaelea, vimeundwa.

Tunarejea pale ambapo ma-oligarch walimfuata Abramovich kumuomba mawazo… ni nani anafaa kumrithi rais Boris Yeltsin??

Wao walikiwa wanauliza leo… lakini mwenzao alijiandaa kuwajibu swali hili miaka minne nyuma. Tayari alikuwa na mtu kichwani kabla hata hawajauliza au kwa usahihi zaidi, alikuwa na jibu la swalo lao kabla hata hawajaanza kuwaza kuhusu swali hilo.

Maana halisi kabisa ya mtu anayeishi kimkakati na Kuwaza kimkakati. A natural born tactician.

Hakuna kitu kizuri kama kiongozi ambaye anaweza kujitathimini na kukubali mapungufu yake na kukubali kukaa pembeni kupisha wengine. Mtu wa namna hii hata kama kuna madudu aliyafanya unajikuta unapata nafasi ya kumsamehe moyoni.

Licha ya mapungufu yake yote na vituko juu ya vimbwnga alivyovifanya kuidharaulisha Russia, lakini ulipofika wakati na kuelezwa ukweli kwamba ni muda muafaka akae pembeni kupisha mtu mwingine, Boris Yeltsin hakuifanya shingo yake kuwa ngumu.

Roman Abramovich akakutana na ma-oligarch wenzake. Akawapa pendekezo lake la nani anadhani anafaa kuwa rais mpya wa Russia. Akaweka sababu zake mezani… ma-oligarch wakakubaliana naye.

Nilieleza kwamba wale wanaojiita 'The Family' ambao ni ma-oligarch na wanafamilia ya Yeltsin kimsingi ndio ambao walikuwa wanaendsha nchi. Na ndani ya The Family kulikuwa na ule 'Utatu Mtakatifu'… Abramovich, Tatyana na Yumachev. Na katika kipindi hiki Abramovich alikuwa na nguvu ya ushawishi kwa Yeltsin kuwazidi wote hata ndani ya The Family na Utatu Mtakatifu.

Kwa hiyo ulipofika wakati wa kuzungumza suala hili zito na Yeltsin… ni Abramovich pekee yake… yeye na Yeltsin pekee walijifungia ofisini na 'kuyajenga'.

Kwanza Abramovich alimueleza Yeltsin kwa nini huu ni muda muafaka yeye kukaa pembeni na kumpisha kiongozi mpya. Baada ya Yeltsin kuukubaliana na hili, Abramovich akamueleza kuhusu pendekezo la mrithi wake. Abramovich akamueleza kwamba anapendekeza Vladimir Vladimirovich Putin, Mkurugenzi Mkuu wa FSB aanze kuandaliwa kurithi kiti hicho cha Urais. Kama ambavyo aliwafafanulia ma-oligarch ndivyo pia ambavyo alimfafanulia Rais Boris Yeltsin.

Tarehe 9 August mwaka 1999 Rais Boris Yeltsin alimteua Vladimir Putin kuwa Naibu wa Kwanza wa Waziri Mkuu. Yaani kipindi hicho ilikuwa kunakuwa na Waziri Mkuu alafu anakuwa na Manaibu watatu au wawili. Yaani mfano mzuri kama Zanzibar walivyo na 'Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais'. Kwa hiyo Putin aliteuliwa kuwa Naibu wa Kwanza wa Waziri Mkuu wa Russia. Nimeeleza kwamba kipindi hiki Russia ilikuwa kwenye mparaganyiko fulani hivi wa kimfumo. Wakati Putin alikuwa anateuliwa kuwa Naibu wa Kwanza wa Waziri Mkuu lakini nafasi ya Waziri Mkuu ilikuwa wazi. Ndani ya muda wa chini ya miezi kumi na tatu, walikuwa wameteuliwa Mawaziri Wakuu wane tofauti na kufukuzwa. Uteuzi huu wa Putin kuwa Naibu wa Kwanza wa Waziri mkuu ulitangazwa asubuhi ya tarehe hiyo 9… lakini ajabu sana ilipofika majira ya jioni siku hiyo hiyo Putin aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Russia.

Mkakati… Abramovich… Abracadabra…

Uteuzi wa Putin kuwa Waziri Mkuu mwanzoni haukushitua sana watu japokuwa hakuwa na umaarufu kwa wanasiasa wala wananchi kwa sababu kama ambavyo nimeeleza kuwa kwa muda wa kama miezi kumi na tatu tu tayari kulikuwa na Mawaziri Wakuu wane walioteuliwa na kufutwa kazi. Kwa hiyo watu walikuwa wanamuhesabia siku tu Putin kabla yay eye pia 'kutumbuliwa'… ni kama vile hapa kwetu nchini, ukiteuliwa kuongoza Wizara ya Maliasili na Utalii au Wizara ya Nishati na Madini… watu wanakuhesabia miezi tu.

Lakini siku tatu tu baada ya uteuzi wa Putin, Rais Boris Yeltsin alifanya kitu cha tofauti kulinganisha na Mawaziri Wakuu waliopita ambao aliwahi kuwateua. Katika hotuba yake kwa wananchi alitamka kwamba anatamani Putin awe mrithi wake wa kiti cha Urais siku akiondoka kwenye cheo hicho… wenye kusoma alama za nyakati wakaelewa nini kilikuwa kinaendelea. Hii haikuwa ile 'teau kisha fukuza'. Putin alikuwa anaandaliwa

4

Kwa hiyo wapinzania wa Yeltsin au tuseme wapinzani wa 'The Family' wakaanza kujipanga kuzuia hicho ambacho kilikuwa kinataka kutokea. Iikuwa wazi kwamba Yeltsin amebakiza muda mchache madarakani, kwa wapinzani wa ma-oligarch hii ilikuwa habari njema kwao kwamba walau sasa na wao watapata zamu yao kufaidi mema ya nchi. Lakini baada ya kauli ya Yeltsin kwamba anatamani kurithiwa kiti cha Urais na Putin walielewa kwamba huu ulikuwa ni mkakati wa kuanza kumnadi Putin kwa wananchi. Kwahiyo nao wakaanza mipango ya kukwamisha suala hilo lisifanikiwe.

Sasa,

nimeeelza kwenye sehemu zilizopita kwamba Yeltsin alikuwa na upinzani mkubwa sana kwa wanasiasa wengine. Upinzani huu ulikuwa na historia ndefu hata kabla hajaanza kuwalimbikizia mali ma-oligarch.

Tutazame kidogo kwa ufupi sana… Shirikisho la Russia lilivunjika December, 1991. Kama mwezi mmoja hivi baadae, yaani January, 1992 Rais Yeltsin alianzisha program mpya kukabiliana na hali ya mbaya ya kiuchumi ambayo ilisababishwa na kuvunjika kwa Shirikisho la Russia. Badala

ya program ile kusaidia badala yake ilifanya hali ya kiuchumi kuwa mbaya zaidi. Yeltsin alipingwa vikali mno kwa sera hizo mpya ambazo alizianzisha kiasi kwamba mpaka makamu wake wa Rais alikuwa anazikosoa hadharani kabisa. Likatokea wimbi la wanasiasa wengi hata wa chama chake kujiweka mbali na Yeltsin na kujipambanua kupinga sera hizo mpya za kiuchumi za Yeltsin. Matokeo yake ni kwamba Yeltsin alikuwa akipeleka miswada au mapendekezo Bungeni ili yapitishwe yalikuwa yanakwamishwa makusudi ili kumkata makali ya kutekeleza sera zake za kiuchumi. Kipindi hicho Bunge la Russia lilikuwa linaitwa "Supreme Soviet". Baada ya mvutano wa muda mrefu kati ya Yeltsin na Bunge hatimaye Yeltsin akatangaza kulivunja Bunge. Sasa katiba ya Russia kipindi hicho ilikuwa haimpi mamlaka Rais kulivunja Bunge, kwa hiyo wabunge wakagoma na wakawa wanaendelea na shughuli za kibunge. Yeltsin akaingiza vifaru vya kijeshi kwenye viwanja vya bungeni kutaka kuwatoa wabunge kwa lazima. Wabunge wakagoma… wafuasi wao wakaandamana mitaani pale Moscow… kukatokea mapigano makali kati ya wananchi waliokuwa wanaunga mkono bunge dhidi ya wafuasi wa Yeltsin na jeshi. Inakadiriwa karibia watu 1,500 walipoteza maisha kwenye yale mapigano na kuyafanya kuwa moja ya tukio baya zaidi kwenye historia ya Russia.

Loh.! Nanogewa nichambue zaidi historia hii ya Russia… but let's cut a long story short. Mapigano yale yalidumu kwa muda wa kama wiki mbili hivi kabla ya Rais Yeltsin na Bunge kufikia muafaka. Bunge walimpa masharti kadhaa ili waendelee kufanya naye kazi 'smoothly' na yeye Rais Yeltsin akatoa matakwa yake.

Moja ya makubaliano makuu ilikuwa ni kuunda upya mfumo wa Bunge la 'Supreme Soviet'. Yeltsin alihisi kwamba Bunge lilikuwa limepewa mamlaka makubwa mno kutokana na mfumo wa kijamaa ambao ulikuwa unatumika kuendesha nchi huko nyuma. Chini ya mfumo huu mpya, kwanza 'supreme soviet' litavunjwa na kuundwa 'Federal assembly' ambayo itakuwa na 'chamber' mbili. Kutakuwa na 'Lower House' kwa jina State Duma (au GosDumas kama warusi wenyewe wanavyooita), na pia kutakuwa na 'Upper House' kwa jina la Council of the Federation. (Mfumo huu bado ungali unatumika mpaka sasa).

Kwanini nimegusia historia hii? Kuna vitu viwili ambavyo nataka uvione… kwanza ni uhasama wa Bunge na rais Yeltsin kwani hata baada ya mfumo mpya kuwekwa Bunge bado lilikuwa na kinyongo naye kutokana na kile ambacho kilitokea.

Na jambo la pili nataka tufahamu kwamba ile lower house ya Bunge (State Duma) ndiyo ambayo ilikuwa na malamlaka ya kumthibitisha Waziri Mkuu mara baada ya kuteuliwa na Rais.

Sasa,

Bada ya kauli ya Yeltsin kwamba anatamani Putin awe mrithi wake wa kiti cha Urais, wapinzani wa 'The Family' wakaanza kampeni ya chini kwa chini kushawishi wabunge wa GosDumas kumpiga chini Putin.

Putin alikuwa anahitaji kura 226 ili kuthibitishwa kuwa Waziri Mkuu.

Kambi ya Yeltsin ikagundua njama hii na mara moja wakaanza kuifanyia kazi. Wanasema pesa sabuni ya roho… haijalishi ni kabila gani au nchi gani… pesa inaweza kubadili moyo wa binadamu. Ma-oligarch wakaingia kazini kumwaga fedha kwa wabunge wa GosDuma.

Siku ya August 16 kura zilipopigwa Putin aliponea chupu chupu kwa kupata kura 233. Kura saba tu zaidi.

Kwa hiyo rasmi sasa Putin alikuwa ni waziri Mkuu wa Russia.

Hatua ambayo ilikuwa inafuata ilikuwa ni kumjenga Putin kwenye mioyo ya wananchi. Kama ambavyo nimeeleza… vyombo vya habari vyote vilikuwa vinamilikiwa na ma-oligarch. Kwa hiyo kila siku vilikuwa vinaandaliwa vipindi malumu vya redio na televisheni… makala kwenye magazeti na makongamano na mikutano ya hadhara… vyote kumuhusu Vladimir Putin.

Lakini moja ya matukio ambayo yalisaidia kumuweka Putin kwenye mioyo ya warusi ilikuwa ni namna ambavyo alishughulikia tafrani ambayo ilitokana na kulipuka kwa mabomu kwenye nyumba za kupanga kwenye miji mitatu nchini urusi… tukio ambalo linajulikana kwa jina maarufu la 'Russia Appartment Bombings'. Tukio ambalo lilizua hofu kubwa ndani ya Urusi. Putin alionyesha ukakamavu wa hali ya juu na umahiri kulishughulikia suala hilo mpaka mwisho. Lakini pia Putin aliwakosha warusi kwa msimamo wake thabiti juu ya vita waliyokuwa wanaipigana Chechenya.

Miezi mitatu baadae, yaani mwezi December 1999 Rais Boris Yeltsin alijiuzulu ghafla na kwa mujibu wa katiba ya Rusia Waziri Mkuu ndiye anachukua nafasi yake na kuikaimu mpaka uchaguzi mkuu uitishwe.

Yeltisn alijiuzulu tarehe 31 December 1999… siku hiyo hiyo Putin akatangazwa kuwa Kaimu Rais wa Russia. Na siku hiyo hiyo akasaini 'decree' ya kwanza na muhimu sana kwenye historia ya Urusi. Decree hii ilikuwa na kichwa kinachosema, "On Guarantees of former President of the Russian federation and members of his family". Decree hii iikuwa inatoa kinga kwa Rais Yeltsin na wanafamilia wake wote kwamba hawatashtakiwa kwa makosa yoyote yale kama ikionekana labda kulikuwa na makosa yoyote ambayo yalitendeka kipindi cha Urais wa Yeltsin.

Na hii ilikuwa ni moja ya makubaliano kati ya Yeltsin na Abramovich kwa niaba ya ma-oligarch wenzake walipomtaka aachie ngazi… alitaka ahakikishiwe kwamba mali zake hatopokonywa na kamwe asishtakiwe.

Miezi mitatu baadae, Putin aliitisha uchaguzi mkuu ambao alishinda kiulaini kabisa. Tarehe 7 May 2000, Vladimir Vladimirovich Putin alikula kiapo kuwa Rais wa Russia.

Kazi ilikuwa imekamilika…. Abramovich… abracadabra.!!

Swahiba wake ambaye 'amemfinyanga' kwa mikono yake na kumtengenezea njia sasa alikuwa amekalia kiti cha urais wa nchi.

Kuna kitabu kitakatifu kinasema "tunakua kutoka utukufu mpaka utukufu". Na haswaaa, hii ndio hulka yetu binadamu… haijalishi tuko kileleni kiasi gani… siku zote tunataka kuipanda ngazi inayofuata. Hata uwe na kikubwa kiasi gani, nafsini tunaona tulichanacho bado hakitoshi… haijalishi tunacho kingi kiasi gani. Tunatamani, tunatafuta, tunakipata alafu tunataka zaidi… wanadamu tumeumbwa na kiu ya "kukua kutoka utukufu mpaka utukufu".

Huu sasa ulikuwa ni wakati wa Abramovich kuhamia katika hatua ya pili ya ndoto zake… ndoto kubwa zaidi. Unaweza kudhani kumiliki Sibneft kampuni kubwa zaidi ya kuzalisha mafuta nchini Russia ilikuwa inatosha.. la hasha… Roman Abramovich alikuwa anataka zaidi, na alichikuwa anakitaka safari hii kilikuwa kimono zaidi pale Russia.. Abrfamovich alikuwa anataka kujimilikisha sekta ya Aluminum ndani ya nchi ya Russia. Sekta yenye utajiri mkubwa zaidi nchini Russia lakini pia ikiwa ni sekta hatari zaidi.

Kuingia kwa Abramovich kwenye sekta hii kutakuja kuibua moja ya nyakati za hatari zaidi kuwahi kushuhudiwa nchini Russia na Ulaya mashsriki yote kiasi kwamba mpaka leo hii kipindi hicho kinajulikana kama nyakati za 'Vita za Aluminum'.

MUHIMU: Kabla sijaenda kwenye mada nijibu swali ambalo naulizwa kila mara kwenye comments na PM ili iwe clear. Utaratibu wa kujiunga na 'familia' yangu kule whatsapp ni malipo ya shilingi elfu tano kwa mwezi. That's it.

And nimeweka namba yangu, kwa hiyo ni vyema unitumie meseji direct badala ya PM. Nafungua PM mara chache sana kwa hiyo unaweza kuona sijajibu meseji yako ukajiuliza huyu somo vipi tena. PM nyingi mno, zinanielemea kwa hiyo najikuta sifungui zote.

And hili ni suala la hiyari, kwa wenye kupenda wamekuja wale ambao wanahisi hawawezi basi tutakuwa tunaonana hapa jukwaani. Nadhali hii imekaa sawa, hakuna haja ya kufanya kuhusu hili. Limeisha…

Twende kwa Oligarch Abramovich….

Nimewahi kuonana na wasomaji wangu wachache sana wa makala na vitabu vyangu. Sababu kubwa ya kutoonana sana na watu ni kwa vile katika maisha ya kawaida huwa siongei kabisa japo ni msikilizaji mzuri sana. Tunaweza kukaa nikakusikiliza kwa masaa manne straight bila kuchoka wala wala 'kuboreka'. Ubaya ni kwamba watu wengi wanategemea uwaeleze mengi na ubaya ni kwamba kwa asili huwa siongei ndio maana nachagua kuandika sana labda 'ku-compasate' energy ninayo-reserve kwa kutokuongea. Hii ni moja ya sababu kwa nini mara nyingi huwa sionani na watu… I'm not a good company kama unahitaji mtu wa 'kupiga story'. Lakini sababu ya pili ni umri… wengi wana picha fulani kichwani ya muonekano au umri wa huyu muandishi 'The Bold'. Wachache ambao nimekutana nao wote kitu kimoja huwa wanakisema ni kwamba kwa umri huu nilionao nawezaje kuandika vitu ambavyo naandika? Inawezekana wanasema hivyo as a compliment but it makes me feel very uncomfortable. Kwa hiyo napendelea kuendelea kujificha kwenye kichaka cha 'The Bold.'

Kwa nini nasema haya… unapomsoma mtu kwa muda mrefu sana na mambo makubwa ambayo ameyafanya kuna wakati fulani unaanza kujenga picha ya nje ya uhalisia.

Kwa mfano, kwa vitu vyote hivi ambavyo Roman Abramovich amevifanya… kufikia hatua ya hadhi ya Oligarch, kulichachafya Bunge la Russia, kumuondoa Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, kujimilikisha kampuni kubwa zaidi ya mafuta ya serikali, kumshawishi Rais Boris Yeltsin kuondoka madarakani na kumtengeneza Rais mpya Vladimir Putin… unaweza kudhani kwamba Abramovich ni lizee fulani hivi lililo zaliwa na kukulia kwenye 'system'… lakini nikukummbushe kwamba mpaka siku ile mwaka 2000 mwezi May kipindi Putin anaapishwa kuwa rais mpya wa Russia… Roman Abramovich alikuwa ni kijana wa miaka thelathini na tatu tu. Niweke mkazo kwa namba… miaka 33.

Kwenye sehemu iliyopita nilieleza kwamba baada ya Abramovich kujihakikishia umilki wa Sibneft na kisha kumshawishi Rais Yeltsin kuachia ngazi na baadae kumfinyanga Putin na kumweka madarakani sasa uliwadia wakati wa kuingia katika 'utukufu mpya'.

Nchi ya Urusi kwa miongo mingi sana imekuwa ndio nchi inayoongoza duniani kwa uzalishaji wa aluminium na hata matajiri wa kubwa wa Russia utajiri wao unatokana na aluminium, mafuta na gesi. Kwa hiyo sekta hii ya aluminium ni moja ya uti wa mgongo wa uchumi wa Russia.

Kwenye miaka ya tisini na mwanzoni mwa 2000 baada ya serikali kuanza ubinafsishaji holela wa mali za umma ushindani ulikuwa mkubwa haswa na Russia haijawahi kushuhudia vifo vingi vya watu mashuhuri kama kipindi hiki. Katika kipindi hiki zaidi ya matajiri mashuhuri 100 waliuwawa kinyama na miili yao kuokotwa barabarani.

Kipindi hiki kichungu kinakumbukwa kama wimbi la 'Aluminium wars'. Nitaomba kuchambua kwa kuingia miguu miwili yote nukta kwa nukta ili kukielewa nini kilitokea kwa sababu tukiweza kuelewa vyema nini kilitokea ni rahisi zaidi kuielewa hata hii Russia ya sasa na mwelekeo wake wa kisiasa.

Ilikuwaje… tuanze kwenye mzizi.

Ukuaji wa sekta ya aluminium nchini Russia ni matokeo ya miaka mingi sana ya serikali ya nchi hiyo kuwekeza nguvu kubwa sana kwenye kuendeleza sekta hii. Kama haujafahamu, aluminium inachimbwa kutoka kwenye migodi ya boksiti (bauxite) na kisha kuchakatwa kuwa alumina (aluminium oxide). Alumina iko kama unga unga fulani hivi mwepe au mfano mzuri kama 'snow' hivi. Hii ndio hutumika kuzalisha aluminium. Sasa Russia ni moja kati ya nchi za kwanza kabisa kufanya bunifu za kuchakata boksiti mpaka kupata alumina. Gunduzi za mwanasayansi kama Beyer ambaye alikuwa raia wa Austria miaka ya 1889 akiwa anafanyakazi St. Petersburg's katika kiwanda cha kemikali cha Tenteleev ambapo aligundua mbinu ya kuchakata alumina kutoka kwenye boksiti kwa kutumia alkali za kaustiki. Baadae gunduzi za watu kama Muller na Packard ambao waligundua uvunaji wa alumina kwa kuifanyia decomposition ya aluminium hydroxide na kisha kufanyia electrolysis. Katika lugha nyingine twaweza kusema kwamba warusi ndio 'pioneers' wa namna za uvunaji alumina kutoka kwenye migodi ya boksiti. Hata mapinduzi makubwa ya upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini Russia ambayo yalitokea kwenye karne ya 20 kwa kiasi kikubwa kulitokana na uhitaji mkubwa wa viwanda vya kuzalisha aluminium na malengo ya nchi hiyo kutaka kuongeza uzalishaji kila mwaka.

Kwa hiyo sekta hii ya aluminium kwa miongo mingi nchini Russia imekuwa haraka na kuwa sehemu ya uti wa mgongo wa nchi.

Sasa kwenye miaka ya tisini kipindi ambapo serikali ilikuwa inahama kutoka kwenye ujamaa na kuingia kwenye ubepari na kubinafsisha mali za umma kuna jambo la kiuhini likafanyika. Wafanyabiashara ambao walikuwa wananunua viwanda vya aluminium wakatengeneza mgogoro wa kubuni kwamba kuna upungufu mkubwa wa malighafi ya alumina ndani ya Russia ambayo ndiyo inatumika kuzalisha aluminium. Kwa kuwa serikali ilikuwa mkononi mwa ma-oligarch wakashawishi kwamba serikali iondoe kodi kwenye uingizaji alumina kutoka nje ya Russia ili 'kuboost' tena uzalishaji wa aluminium. Serikali ikaondoa kodi kwenye malighafi za utengenezaji wa aluminium na pia kubadilisha mfumo wa kodi kwenye bidhaa za aluminum. Kwa hiyo biashara ya aluminium ambayo tayari ilikuwa na fursa ya kujenga utajiri, utamu wake ukaongezeka zaidi.

Ikafika kipindi kila oligarch alikuwa anataka kumiliki kiasi fulani cha sekta hii ya aluminium.

Ubaya ni kwamba mifumo ya umilikiwa viwanda hii ambayo ilikuwa inatumika ni kama ule ambao Abramovich aliuanzisha Russia namna ambavyo alikuwa anaimiliki Sibneft kupitia msululu wa 'private trusts' na makampuni yaliyosajiliwa kwenye sehemu zinazojulika kwa ukwepaji kodi kama vile Cyprus, Jersey, Canyon Islands na kadhalika. Yaani makampuni yalikuwa yanamilikiwa kwa mifumo complex kiasi kwamba huwezi kujua ni nani hasa ni mmiliki wa kampuni. Hii ikatoa mwanya wa watu kufanya 'hostile takeovers' za kihuni. Nilieleza hii uko mwanzoni. Tajiri anawalipa hela genge fulani la mafia. Wanakuja wanakuteka… unasainishwa nyaraka kwa nguvu, unauwawa kesho mwili wako unaokotwa vichakani uking'ong'wa na nzi.

Au mshindani wako unamtumia genge linampiga risasi mchana kweupe katikati ya mji.

Kilikuwa ni kipindi cha hatari kiasi hicho. Matajiri wakubwa zaidi ya mia moja waliuwawa kinyama na miili kutupwa mitaani.

Kipindi Putin anaingia madarakani May mwaka 2000 alikuta hizi 'aluminium wars' ziko kwenye kilele chake kabisa. Watu wanauwana kugombea rasilimali za nchi.

Kuna mambo mengi unaweza usikubaliane na Putin lakini suala moja lazima umpe heshima yake ni jinsi ambavyo anaipenda nchi yake. Putin alipoingia madarakani alikuwa na falsafa kwamba ndani ya Urusi ni ruksa kutumia fursa ya ubepari kutengeneza utajiri lakini malengo yako hayo ya kujitajirisha hakikisha hayaathiri nchi. Kwa hiyo hizi vita za kugombea viwanda vya aluminium na namna ambavyo kwa miaka mingi matajiri hawa walikuwa wameachwa kukwepa kodi ilikuwa inamkera haswa. Alikuwa anahitaji suluhisho....

Uzuri alikuwa na Roman Abramovich upande wake.

Nakumbuka siku ambayo Rais Donald Trump alipomteua mkwewe Jared Kushner kuwa mjumbe maalumu wa kusuluhisha mgogoro wa Palestine na Israel alisema kwamba, kama Kushner akishindwa kusuluhisha mgogoro huo hakuna ambaye atakuja kuweza. Unaweza kuhisi kwamba kauli hii ni ya kumkweza sana Kushner... lakini kwa watu ambao wanamfahamu Kushner watakueleza kwamba kauli ile ya Rais Trump ilikuwa na ukweli kwa silimia zote. Kushner ni moja ya wanamkakati bora zaidi dunia kuwahi kushuhudia.

Ndicho hiki ambacho pia Putin alikuwa anakiona kwa Abramovich... hakuna mzigo mzito unaoweza kumshinda 'myamwezi' huyu.

Baada ya Abramovich kupewa baraka na Putin kuingia kwenye sekta ya Aluminium kwanza kabisa akaanza kutengeneza mazingira mazuri kwa yeye kufanya kile ambacho alikuwaa anakikusudia. Masuala kadhaa...

Kwanza kabisa akafungua kampuni ya ku-trade commodities. Kampuni hii iliitwa Millhouse Capital na aliisajili London Uingereza. Kupitia kampuni hii alikuwa ana-trade commodities kama vile mafuta, Gold, Silver n.k. Lakini kampuni hii ilikuwa na malengo makubwa zaidi.

Abramovich alipoanza kujiingiza kwenye sekta ya aluminium kwanza kabisa alimuomba mentor wake bwana Berezovsky kumsaidia kwa 'connection' alizonazo kwenye ulimwengu huo wa hatari wa biashara ya aluminium. Kipindi hiki Berezovsky alikuwa amejiingiza kwenye siasa na alikuwa ni mwakilishi kwenye Bunge la GosDumas. Na kwa kipindi hicho ili ushinde kiti cha kisiasa nchini Russia lazima uwe na connections na makundi ya mafia kwa ajili ya protection na kuwafanyizia wapizani wako. Kwa hiyo Abramovich alikuwa anataka kutumia connection hizi za mentor wake.

Berezovsky alimsaidia kwa kumtambulisha kwa watu wawili ambao walikuja kugeuka kuwa muhimu sana kwenye maisha ya Abramovich mpaka leo hii...

Kwanza, tunakumbuka kwamba nilieleza kuwa wakati serikali ya Yeltsin inabinafsisha mali za umma hata televisheni ya taifa iliyoitwa Perviy Kanal (First Channel) nayo ilibinafsishwa na ambaye aliichukua alikuwa ni huyu Oligarch Boris Berezovsky. Sasa, baadae Berezovky allimuingiza Russia mtu anaitwa Badri Patarkatsishvili. Huyu alikuwa ni mfanyabiashra kutoka Georgia lakini ni myahudi wa Israel. Badri aliingizwa Russia na Berezovsky na kumpa jukumu la kuendesha kituo cha televisheni ambacho alikuwa amebinafsishiwa na serikali. Lakini uhalisia kamili ni kwamba Badri alikuwa anajua haswa namna ya 'kudili' na mafia na masuala ya 'underworld'. Kwa hiyo Badri alikuwa anahakikisha usalama wa Berezosky na pia kuhakikisha wapinzani wa Berezovky wanashughulikiwa ipasavyo.

Huyu ni mtu wa kwanza ambaye Abramovich alitambulishwa na mentor wake Berezovky. Kupitia mtu Abramovich alilipa zaidi ya Dola milioni 500 kwenda kwa mafia kupitia kwenye mikono ya Badri Patarkatsishvili. Kwa ajili ya nini? Nitaeleza...

Sasa ili kuelewa ni kwa namna gani Abramovich aliingia kwa kishindo kwenye sekta ya aluminium na ku-takeover tunapaswa kumchambua mtu wa pili ambaye Abramovich alitambulishwa na Berezovky.

Pale Russia kuna bwana mmoja anaitwa Oleg Deripaska. Katika enzi za utoto wake bwana huyu alikuwa ni wale aina za watoto ambao wazungu wanawaita 'prodigy'. Watoto wenye vipaji vya kupindukia kwenye suala fulani. Deripaska alikuwa ni prodigy wa hesabu na sayansi. Kabla sijaenda mbali kuna 'pettern' hapa nataka uione nitakuja kueleza huko mbele... Pattern ya kwanza ni Berezovsky mentor wa Abramovich nilieleza pale mwanzoni alikuwa ni Profesa wa Hisabati kabla ya kujiingiza kwenye biashara, lakini pia huyu Oleg Deripaska ambaye Abramovich alitambukishwa kwake naye alikuwa ni nguli wa Hisabati tangu utoto. Pattern ya pili ambayo nataka uione ni hawa watu watatu... Abramovich, Berezovsky na Badri Patarkatsishvili wote hawa wana asili ya Israel. Utanilewa hapo mbele kwa nini nime-highlight hayo mambo mawili.

Sasa ni namna gani huyu deripaska alimsaidia Abramovich kuingia kwenye biashara ya hatari ya Aluminium kwa kishindo... nitarudi kueleza.

(Wale wote waliojipa mission ya kunitukana na kunikashifu kwenye comments nina neno moja kwenu… nyinyi ni wana wa Mungu na kwa sababu hiyo nawapenda sana)

Nilisema nitaeleza kidogo kuhusu Deripaska ambaye Abramovich alitambulishwa kwake na Berezovsky. Deripaska ni aina ya wasomi ambao wametumia taaluma yao vyema kujichumia utajiri. Tangu akiwa bado kijana mdogo tu Deripaska alikuwa na shauku kubwa mno ya kujisomea na kitu angalinacho hata sasa. Huyu bwana hata sasa ukifika ofisni kwake makau makuu ya Basic Elements jijini Moscow kwenye jengo hilo kuna kuta nyingi ambazo zina shelves za vitabu kuanzia chini mpaka juu. Deripaska alikuwa na kipawa kikubwa cha hisabati tangia utoto. Mwaka 1993 alihitimu chuo kikuu 'with honors' shahada ya fizikia kutoka Moscow State University. Miaka miwili baadae alihitimu shahada ya uzamili katika uchumi kutoka Plekhanov University of Economics.

Ndoto ya awali Deripaska ilikuwa ni kuwa msomi mbobezi kama 'Theoretical physicist'. Lakini utakumbuka kwamba kipindi hiki ndicho ambacho Soviet Union ilidondoka. Hapo awali wanafunzi wote walikuwa wanasoma kwa udhamini wa serikali lakini baada ya Soviet Union kudondoka elimu ikawa ghali na serikali kuacha kugharamia masomo ya wanafunzi. Kwa hiyo kwa kijana kama Deripaska ambaye mwenyewe anasema kwamba hata hela ya kula ilikuwa ni tatizo kwake kipindi hicho hakukuwa na uhalisia wa yeye kuweza kugharamia masomo yake mwenyewe.

Lakini pia kipindi hiki kama tulivyoona awali kilikuwa ni kipindi chenye fursa nzuri kwa mtu kujilimbikizia utajiri. Kwa hiyo Deripaska akiwa na miaka 25 tu alishawishi wanasayasi wengine kadhaa manguli wa hesabu, fizikia na hata rocket science kuungana naye kuanzisha kampuni ya 'ku-trade' metals. Kampuni hii waliita VTK, na Deripaska ndiye alikuwa mwanahisa mkubwa kuzidi wenzake. Deripaska alikuwa ni moja ya watu wa mwanzo kabisa nchini Russia kutumia mifumo ya kisayansi na 'systematics' katika kutrade commodities. Unaweza kujiuliza namna gani anatumia sayansi kutrade commodities… binafsi huwa natrade currencies na huwa nawaambia watu 'trading' ni science and mathematics na ndio maana watu wengi hawako successful wakitaka kuwa traders… kwa nini? Kwa sababu sayanasi na hisabati sio kitu chepesi.

Uzuri ni kwamba Deripaska alikuwa ni nguli wa hisabati kwa hiyo VTK ilikuwa kwa haraka sana. Deripaska alikuwa ananunua commodities kwa bei ya chini ndani ya Urusi na kwenda kuziuza kwa bei ya juu kwenye soko la dunia.

Kwenye sehemu za mwanzo kabisa za makala hii nilieleza kwamba kipindi serikali ya Russia inabinafsisha viwanda na makampuni ya umma waligawa voucher kwa wananchi ili watumie voucher hizo kununua hisa kwenye makampuni ambayo yalikuwa yanabinafsishwa. Nilieleza kwamba kila mwananchi alipewa voucher ya Rubble 10,000 za Urusi. Kama ambavyo ilitokea hapa kwetu Tanzania wakulima walivyouza vocha za pembejeo za kilimo ndivyo ambavyo pia Warusi walivyouza voucher zao kwa matajiri. Deripaska ni moja ya matajiri hawa ambao waliwekeza hela ya kutosha kununua voucher kwa wananchi.

Kama mwaka mmoja tu baadae Deripaska alitumia voucher zote na faida yote aliyoipata kwenye kutrade commodities kununua hisa kwenye kiwanda cha Sayanogorsk Aluminium Smelter. Hiki ndicho kilikuwa kiwanda kikubwa zaidi cha uzalishanji aluminium nchini Rusia. Uwekezaji wake huu mkubwa ulimpatia hisa 20% za kiwanda hiki. Kwa wingi huu wa hisa ulimfanya Deripaska kuwa mwanahisa mkubwa zaidi nyuma ya serikali kwenye kiwanda hiki. Yaani mwenye hisa nyingi zaidi alikuwa serikali na yeye alikuwa namba mbili.

Kutokana na ushawishi huo mkubwa aliokuwa nao kwenye kiwanda cha Sayanogorsk Aluminium Smelter kwa sababu ya kuwa na hisa nyingi kuzidi mtu yeyote binafsi, mwaka 1994 Deripaska alifanya ushawishi kwa wanahisa wengine na kupewa Ukurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo. Nikukumbushe tu kwamba mwaka huo 1994 wakati anapewa ukurugenzi mkuu wa smelter kubwa zaidi nchini Russia alikuwa ana miaka 26 tu.

Miaka mitatu baadae yani mwaka 1997 Deripaska alianzisha Sibirsky Aluminium Group ambayo aliitumia kama kampuni mama 'kuhold' kampuni zake zote nyingine na shares zake zote kwenye makampuni mengine.

Kwa hiyo huyu ndiye mtu wa pili ambaye Berozovsky alimtambulisha Abramovich kwake.

Naweza kusema kwamba huyu pengine ndio alikuwa mtu muhimu zaidi kwa Abramovich kumfahamu labda nyuma ya Berozosky tu pekee. Licha ya umuhimu wake mkubwa ambao tutauona hivi punde lakini pia bwana huyu walikuwa na mengi ya kufanana. Ukipiga hesabu yako sawasawa utaona kwamba Abramovich alikuwa anamzidi mwaka mmoja tu Deripaska. Yaani kipindi kile Abrampvich anapewa Baraka na Putin kuingia kwenye biashara ya Aluminium akiwa na miaka 33, Deripaska alikuwa na miaka 32.

Wote wawili walikuwa ni vijana wadogo sana. Wote wawili wametokea kwenye maisha ya hali ya chini sana. Wote wawili wanajua namna ya kuishi kimkakati. Wote wawili walikuwa na ushawishi mkubwa sana. Abramovich kwenye system ya serikali na Deripaska kwenye ulimwengu hatari wa biashara ya Aluminium.

Wenye unyoya wa kufanana… huruka pamoja.

5

Nilieleza kwamba mwaka huo alipopewa Baraka na Putin kuingia kwenye biashara ya Aluminium, Abramovich alifungua kampuni iliyoitwa Millhouse Capital ambayo ilisajiliwa nchini Uingereza. Kampuni hii ilikuwa inatrade commodities. Tufahamu kwamba mpaka muda huu kampuni hii haikuwa lolote wala chochote. Haikuwa na 'volumes' kubwa kwenye kutrade hizo commodities wala assets za maana. Thamani pekee ya kampuni hii iliyokuwa nayo ni ile u kwamba inamilikiwa na Roman Abramovich.

Abramovich alipotambulishwa kwa Deripeska alikuwa na ombi moja tu kwake… waunganishe kampuni zao Millhouse Capital ya Abramovich na Sibirsky Aluminium Group ya Deripaska na iwe kampuni moja. Kwa umombo dili kama hii wanaita 'merger'.

Unaweza kuona kwamba ombi hili lilikuwa ni la kijinga… Sibirsky Aluminium Group ilikuwa kwa muda huo ni kampuni kubwa sana ndani ya Russia inayomiliki smelters kadhaa kubwa kubwa ndani ya Russia na pia ilikuwa kampuni mama ya trading companies kama vile ile VTK ambayo deripaska aliinzisha na wanasayansi wenzake. Wakati ambapo Millhouse Capital ya Abramovich ilikuwa kama ni kampuni jina tu yenye ofisini bila mali kubwa kubwa kulinganisha na Sibirsky Aluminium Group.

Ajabu ni kwamba Deripaska hakusita hata kwa sekunde kukubali ombi hilo. Alikubali mara moja waunganishe kampuni hizo mbili kuwa moja ambayo watakuwa wanaimiliki wote.

Kwa nini akubali kirahisi hivi? Wendawazimu?… hapana, kama ilivyo kwa Abramovich ndivyo hivyo hivyo pia ilivyo kwa Deripaska… ni mtu wa mikakati. Anaiona miaka ishirini ijayo leo.

Kuna mambo mawili…

Thamani halisi ya kitu haitokani na hali yake ya sasa bali thamani yake ni ile 'potential' iliyonayo kuleta mafanikio huko mbeleni. Yaani kwamba tukiwaza kibiashara… kwa mfano utajiri au umasikini wa mtu haupimwi kwa kile alichonacho sasa bali 'potential' aliyonayo kupoteza zaidi au kuingiza zaidi kwa siku na miaka ijayo. Unaweza kuwa na milioni mia moja leo hii lakini kuna mtu akikuangalia anakuona masikini. Labda kwa namna fulani amegundua ndani ya miezi michache tu utazipoteza zote. Na unaweza kuwa na elufu kumi tu mfukoni na mtu mwingine akakuona tajiri kwa sababu anahisi potential uliyonayo mwakani tu unaweza kuwa na bilioni umelaza benki.

Napenda mifano hai, nitoe mfano mfupi halisi…

Mwaka 2008 nilikuwa na rafiki yangu tulikuwa darasa moja Tambaza High school. Huyu kwao walikuwa na haueni sana. Mzee wake alikuwa afisa mwandamizi wa serikali kwenye kitengo fulani. Alikuwa na safari za mara kwa mara nje ya nchi. Kuna safari moja aliporejea alimletea zawadi ya simu ya iPhone. Hiyo ni mwaka 2008 ambapo unaweza kutembea mjini kutwa nzima bila kuona mtu hata mmoja mwenye simu aina ya iPhone. Unaweza kupata picha ni kiasi gani yeye mwenyewe na sisi 'washkaji' zake tulikuwa 'tunavimba' shuleni… ndio hata sisi wapambe wake tulikuwa tunajiona kama simu yetu. Loooh.!!

Basi tukaanza 'uzungu uzungu' hivi… kutaka kujua mambo ambayo yanatrend huko duniani. Mara tukafahamu kuhusu facebook… hu ni mwaka 2008… sikumbuki kuwahi kumsikia mtu yeyote kabla akitaja facebook. Kilikuwa ni kitu kipya ambacho hapa nchini kilikuwa hakijulikani kabisa kabisa. Kipindi kile 'chat rooms' ndio zilikuwa maarufu sana hapa nchini. Pale shuleni kwetu ni 'genge' letu tu nadhani ndio ambao tulikuwa na akaunti za facebook na hata sisi ni baada ya kusikia ni kitu 'hot' huko duniani.

Kutokana na udadisi sikuishia tu kuitumia facebook bali nikaanza kuichimba. Ndio nikafahamu kuhusu mmiliki wake bwana Mark Zuckerberg na kipindi kile akisemwa kuwa ndio Bilionea kijana zaidi duniani akiwa na utajiri wa dola bilioni 2.4 akiwa na umri wa miaka 26 tu. Nikawa najiuliza sana… huyu mtu anawezaje kuwa tajiri mkubwa kiasi hicho wakati huduma hiyo tunaitumia bure? Kipindi kile facebook haikuwa na matangazo kama sasa na ilikuwq sehemu ya sera yao kutokuweka matangazo kwenye mtandao wao… hakukuwa na tangazo hata moja na wala walikuwa hawapokei matangazo. Na pia wala walikuwa hawajafanya ile IPO… ile kuirodhesha kwenye soko la hisa na kuanza kuuza shares kwa umma. Kipindi kile hata financial documents za kampuni zilikuwa zinaonyesha kwamba kwa mwaka wanapata zero revenue? Inakuwaje huyu mtu awe tajiri hivi? Hizi hela zinatoka wapi? Hawa wazungu wanatuzuga na uongo au nini?

Wewe unadhani hela za Mark zilikuwa zinatoka wapi kipindi kile? Kwa nini kipindi kile waseme ana utajiri wa dola bilioni 2.4?

Jawabu ni 'Speculation'… 'potential' ambayo watu wanaiona kwa kitu hicho kutengeneza faida kubwa kwa wakati ujao. Sikumbuki sawasawa lakini nadhani kipindi kile Facebook ilikuwa na watumiaji kama milioni 300 hivi duniani. Kwa hiyo kulikuwa na speculation kubwa kwamba hii kampuni siku yoyote ile 'ita-boom' na kuleta fedha nyingi. Na hii ndio ilikuwa inafanya thamani ya kampuni ya facebook kuwa kubwa na kumfanya Mark kuwa na utajiri wote ule. Lakini kiuhalisia kwa kipindi kile hawakuwa wanaingiza revenue hata kipande ukiachaa hela za investors.

Sasa hiki ndicho ambacho Deripaska alikuwa anakiona kwa Abramovich… potential. Potential gani? Abramovich alikuwa ni 'mtoto' pendwa wa Putin. Putin alikuwa anamuamini Abramovich kuzidi mtu yeyote yule. Kwa hiyo kama akiwa mmiliki mwenza wa kampuni moja na Abramovich, basi hakuna anga ambalo litawashinda kulivuka na wanaweza kutengeneza moja ya kampuni tajiri zaidi duniani.

Nilisema kuna mambo mawili… hiyo ilikuwa sababu ya kwanza. Sababu ya pili ilikuwa ya busara zaidi. Isingelikuwa busara kwake kumkatalia Abramovich kwasababu, 'If Roman wants something… Roman gets something.!" Kama angemkatalia ofa hiyo Abramovich, basi Abramovich angetafuta namna nyingine ya kukipata kiwanda hicho na njia hiyo nyingine ingekuwa hasara kwa Deripaska. Abramovich ni aina ya watu ambao lazima wapate wanachokitaka… hakuna kiunzi ambacho atashindwa kukiruka.

Kwa hiyo wakaunganisha kampuni zao, Millhouse Capital na Sibirsky Aluminium Group na kuunda kampuni mpya inayoitwa RUSAL (siku hizi inaitwa United Company RUSAL).

RUSAL ilikuwa kwa haraka sana. Walichokuwa wanakifanya… walikuwa wananunua viwanda vingine na migodi ya boksiti ndani ya Russia na nchi jirani. Maoligarch ambao walikuwa wanamiliki viwanda hivyo na migodi ilikuwa ni eidha uwauzie RUSAL kiwanda chako kwa hiari au wakichukue kwa lazima. Ukikubali kuwauzia wanakulipa hela… ukikataa kuwauzia kesho kutwa tunaokota mwili wako jalalani.

Kuna 'transcript' za mahakamani kutoka Uingereza za mwaka 2010 ambapo Abramovich aliitwa kutoa ushahidi kwenye kesi fulani, anakiri kwamba hizi aluminium wars zilikuwa moto kweli kweli kiasi kwamba yeye binafsi anakumbuka kwa miaka ya 2000 na 2001 kwa wastani wa kila baada ya siku tatu ulikuwa unasikia mwii wa oligarch fulani umeokotwa.

Na hapa ndipo ambapo ulikuja umuhimu wa Badri Patarkatsishvili yule jamaa wa kwanza aliyetambulishhwa na Berezovsky. Unapojihusisha na sekta ambayo kila kukicha unasikia wenzako wanakufa lazima uwe na tahadhali makini haswa. Huyu Badri nilieleza kwamba alikuwa anajua kudili na Mafia.

Unapomwaga damu za wenzako lazima kuna marafiki zao na ndugu zao na hata wale wengine wanajihisi nao siku utawamaliza, wote hawa watajihami kwa kutaka kukumaliza wewe. Ilifika kipindi ndani ya Russia Abramovich alikuwa hawezi hata kuonekana hadharani… kila oligarch aliyekuwa bado hai alikuwa ameweka vijana kumuwinda na kutaka kumuua. Ndio hapa ambapo Abramovich ilimbidi kulipa zaidi ya dola milioni 500 kupitia kwa Badri kwenda kuhonga kila kikundi cha mafia ndani ya Russia ambacho kilitumwa kumuua yeye na kisha kuwapa agizo jipya wakawamalize wale ambao waliwatuma awali.

Nchi ilichafuka haswa kwa vifo vya maoligarch… lakini RUSAL ilizidi kupaa. Ndani ya miaka miwili tu walikuwa wana-control karibia migodi yote muhimu ya boksiti na viwanda vyote vikubwa vya Aluminium ndani ya Russia na nchi jirani. Kuanzia viwanda vya Armenal foil mill nchini Armenia mpaka Belaya Kalitva Metallurgical plant na Novokuznetsk aluminium smelter nchini Russia. Uje migodi ya boksiti ya Friguia bauxite na Alumina complex mpaka Kindia Company. RUSAL ilipaa juu kuwa moja ya kampuni kubwa zaidi ya uzalishaji wa aluminium duniani. Lakini hapana… Abramovich hakutaka kuwa 'moja ya' kampuni kubwa duniani. Alitaka kuwa kampuni kubwa zaidi duniani ya uzalishaji aluminium.

Afanyeje? Kulikuwa na 'terget' ya mwisho… Krasnoyarsk.

Kipindi hicho jimbo la Krasnoyarsk ndilo lilikuwa na hifadhi kubwa zaidi ya migodi ya boksiti. Sasa pale Krasnoyarsk kulikuwa na kiwanda cha aluminium kinachoitwa Krasnoyarsk Aluminium Smelter. Kiwanda hiki kilikuwa kinamilikiwa na oligarch anaitwa Anatoly Bykov. Huyu oligarch alikuwa ni kijana kama wao akina Abramovich japo alimzidi Abramovich miaka miwili kwa kuzaliwa. Kampuni yake ambayo ndiyo ilikuwa inamiliki Krasnoyarsk Aluminium Smelter kwa kipindi hicho iikuwa inashika nafasi ya pili nyuma ya RUSAL kwa uzalishaji Aluminium. Abramovich tayari alikuwa amemfuata na kumpa ofa mara kadhaa kuwauzia kampuni lakini Bykov alikataa. Mpaka muda huo alikuwa amefanikiwa kukwepa majaribio 26 ya kumuua.

Kwa hiyo huyu oligarch biashara alikuwa anaijua kama wao na uhuni wa kimafia pia alikuwa anaujua.

Kama Abramovich akifanikiwa kuchukua kiwanda hiki cha Krasnoyarsk Aluminium Smelter maana yake ni kwamba atafanikiwa kuifanya RUSAL kuwa kampuni kubwa zaidi ya uzalishaji aluminium duniani.

Lakini Bykov alikuwa amejiapiza kutowauzia kiwanda chake na majaribio ya kumtoa roho yalishindikana mara 26.

Abramovich si mtu wa kukubali kushindwa vita… “Roman wants something… Roman gets something.”

Alikuwa anahitaji mbinu mpya… Abramovich alijiapiza kuwa hataki tu kuwa na ‘moja ya’ kampuni kubwa zaidi duniani ya kuzalisha aluminium…alitaka kuwa na kampuni kubwa zaidi duniani ya kuzalisha aluminium.

Alikuwa anahitaji ‘kuchemsha muarobaini’ mpya wa kumnywesha Bykov.

Kiunzi pekee ambacho kilikuwa kimebaki mbele ya Abaramovich kuifanya RUSAL kuwa kampuni kubwa zaidi ya uzalishaji wa Aluminium ilikuwa ni deal ya kiwanda cha Krasnoyarsk kinachomilikiwa na Anatoly Bykov.

Baada ya kila mbinu kutofanikiwa Abramovich akapata wazo lingine. Mbinu hii ambayo aliitumia mara ya pili inatoa picha ni kwa namna gani Abramovich alikuwa na nguvu ndani ya Russia kipindi kile.

Kama ambavyo nimeeleza kwa msisitizo kwenye sehemu zote zilizopita… biashara aluminium ilikuwa ni sekta ya hatari mno kipindi kile nchini Russia. Maana yake ni kwamba mtu yeyote yule ambaye ameweza ‘ku-survive’ na kushamiri ndani ya biashara hiyo maana yake ni kwamba alikuwa ni mtu hatari zaidi. Hii ilikuwa inamaanisha kwamba Anatoly Bykov kama wenzake wengine wote, pia hata yeye alikuwa na madudu mengi sana ameyafanya ili kuweza kushamiri kwenye biashara hiyo. Na hii ndio ilikuwa silaha ya mwisho ya Abramovich.

Sasa,

Katika jimbo la Krasnoyarsk ambako Anatoly Bykov alikuwa anaishi, kutokana na utajiri mkubwa aliofanikiwa kuuchuma huku akiwa ni kijana wa umri mdogo tu, ilimfanya kuwa kama ‘celebrity’ kwenye mji wao. Vyombo vya habari vilikuwa havikauki ofisini kwake.

Siku hiyo alikuwa anafanya mkutano na wanahabari ofisini kwake… kama kawaida pia kulikuwa na kundi la wananachi wakishangaa shangaa.

Kufumba na kufumbua gari tano zikiwa na wanajeshi karibia thelathini wa ‘special forces’ ziliingia kwa ghafla kwenye eneo la ofisi. Kundi la wananchi waliokusanyika walitawanywa kwa risasi kupigwa juu hewani huku walinzi wa Bykov wakiwekwa chini ya ulinzi. Bykov akanyakuliwa mzobe mzobe kama kuku na kupakiwa kwenye gari na kuondoka naye.

Jioni ya siku hiyo serikali ikatangaza kupitia vyombo vya habari kwamba wamemkamata Anatoly Bykov kwa shutuma ya makosa ya utekaji na mauaji.

Nchi nzima ilizizima… sintofahamu ilitanda kila mtu akijiuliza kwa nini iwe Bykov pekee wakati ni suala linalofahamika wazi kabisa kwamba maoligarch wote wanaojihusha na sekta ya aluminium mikono yao imejaa damu za roho za watu.

Wiki moja baadae Bykov alipandishwa kizimbani. Hati ya mashtaka ilisema kwamba anakabiliwa na kosa la “Kupanga njama ya kuua na utekaji”. Kesi iliunguruma na kuteka vyombo vya habari.

Ndani ya miezi miwili kesi ilikuwa imemalizwa kusikilizwa na mahakama ilimkuta Bykov na hatia na kumuhukumu kwenda jela miaka sita.

Miaka sita… ilikuwa inatosha kabisa kwa Abramovich kufanya kile alichokusidia.

Baada ya miezi mitatu tu kwa kutumia mwanya wa Bykov kuwa jela, Abramovich na Deripaska waliishawishi bodi ya wakurugenzi ya Krasnayorsk Aluminium Smelter kuwauzia kiasi kikubwa cha hisa ambacho kiliwafanya kuwa “majority share holders”. Na mwanya huo wa wao kuwa wanahisa wakuu wa kampuni wakautumia kushinikiza uamuzi wa kampuni hiyo ya Krasnoyarsk kuuzwa kwa RUSAL.

Lengo likatimia…

Kwa akili ya haraka haraka tu suala kama hili haliwezekani likafanyika kwenye nchi za magharibi au hata hapa Afrika leo hii. Lakini hivyo ndivyo mambo yalivyoendeshwa kihuni nchini Rusia miaka ya tisini na mwanzo mwa 2000. Hiyo ndio maana hasa ya ‘Wild Wild East.!”

Hii ilikuwa ni mwezi July mwaka 2002. Ndio siku ambayo RUSAL ilipanda ngazi Rasmi kuwa kampuni inayoongoza duniani kwa uzalishaji wa Aluminium. Utajiri wa Abramovich ukapaa kwa kasi ya ajabu. Na ndio hapa kwa mara ya kwanza jina lake likaanza kutajwa tajwa sana hata nje ya Russia.

Ni wazi sasa kwamba Abramovich alikuwa ni Oligarch namba moja ndani ya Rusia. Mtu pekee ambaye alikuwa na nguvu ndani ya Russia kumzidi Abramovich alikuwa ni Putin pekee. Lakini hakukuwa na mwingine yeyote yule ambaye alikuwa ana hata nusu tu ya ushawishi ambao Abramovich alikuwa nao.

Waswahili tuna msemo tunasema kwamba “mti wa riziki, ficho kivuli cha husda.” Kwamba ukipata uwe makini maana kuna watu watahisi kupata kwako kunaziba riziki zao.

Kitendo cha kijana aliyetoka familia masikini wa kutupwa. Kijana ambaye alikuwa anauza wanasesere. Kijana aliyeuza matairi chakavu leo hii kuwa mfanyabiashara mwenye ushawishi zaidi na si hivyo tu bali kuwa ‘right hand man’ wa Rais wa taifa la urusi kiliwaudhi baadhi ya maoligarch.

Abramovich alikuwa anaogopwa pale Moscow na maoligarch waliudhika sana na kitendo hiki. Yaani kinyago walichokichonga wenyewe leo hii kinawatisha?

Ajabu ni kwamba mpaka Berezovsky alichukia.

Yes, Berezovsky mentor wa Abramovich naye alichukia… sijui kama ilikuwa ni wivu au vipi. Maana Abramovich sasa alikuwa na utajiri mkubwa maradufu zaidi ya Berezovsky. Yawezekana ni wivu, au labda ni woga… Berezovsky alikuwa amechukia haswa kitendo cha Abramovich kuwa Oligarch namba moja ndani ya Urusi na ushawishi wa kupitiliza alionao mtaani na ndani ya serikali.

Vikakaliwa vikao vya siri vya maoligarch… wakafikia azimio. Azimio ambalo naamini maoligarch walioko hai mpaka sasa ambao walikuwepo kwenye kikao kile wanatamani hata kurejesha muda nyuma na kufanya azimio tofauti na lile.

Walifikia uamuzi kwamba, kama ukomunisti uliweza kudondoka ndani ya Urusi, na kama juzi juzi tu hapo waliweza kushawishi kuondoka madarakani kwa Rais Boris Yeltsin… Je, huyu anayemkingia kifua Abramovich, anayemlea na kumpa meno ya kutafuna maoligarch wengine… huyu Putin.. Putin ni nani hata wasiweze kumng’oa ili wawe wamekimaliza kabisa kinyago chao walichokichonga, Abramovich, ambacho sasa chawatisha hata usingizi hawalali kwa raha??

Kipindi hiki vita ya Chechenya ilikuwa ndio imepamba moto na Putin alikuwa anafanya ile tunaita “full scale war”.

Jamii ya kimataifa ilikuwa inapiga kelele kwamba Putin anavunja haki za binadamu na kufanya uhalifu wa kivita kutokana na ile vita ambayo alikuwa anaiendesha Chechenya.

Tunakumbuka nilieleza kuwa ile televisheni ya taifa Perviy Kanal ambayo ndio yenye kutazamwa zaidi ndani ya Rusaia ni Berezovsky alibinafsishiwa kipindi kile na utawala wa Rais Yeltsin.

Maoligarch waliompinga Abramovich mpango wao ukaanzia hapa.

Televisheni ya Perviy Kanal ikaanza kuandaa makala na chambuzi kumkosoa Rais Vladmir Putin na mbinu na nguvu anazotumia kwenye vita ya Chechenya.

Tukumbuke kwamba vyombo hivi hivi vya habari ndivyo ambavyo vilitumika kufanya propaganda ya kuijenga 'image' ya Putin kwa wananchi kipindi kile alipochaguliwa na Rais Yeltsin kuwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo walidhani kwamba kama waliweza 'kumchonga' kwa vyombo vyao vya habari wanavyovimiliki basi wanaweza kumbomoa 'image' yake taratibu kwa umma na hatimaye kumuondoa madarakani.

Was a big mistake…. Ni kweli wao walikuwa na vyombo vya habari, lakini mwenzao Putin alikuwa na kitu muhimu zaidi pembeni yake… Roman Abramovich.

Mara ya mwisho nilieleza kuhusu vyombo vya habari vinavyomilikiwa na maoligarch wakiongozwa na Berezovsky walinyoanza kumkosoa Putin kwa lengo la kumuharibia kwa wananchi na hatimaye iwe rahisi kwao kumuondoa madarakani. Baada ya ukosoaji huu Putin kwenye moja ya hotuba zake aliwaambia wananchi kwamba kuna 'genge' la maoligarch wanaomiliki vyombo vya habari wanaendesha kampeni ya kumchafua kwa malengo yao ya kisiasa.

Unakumbuka nilieleza kwamba katika kipindi hiki Berezovsky alikuwa amejiingiza kwenye siasa. Alikuwa ni mwakilishi kwenye Bunge la Duma (GosDuma). Kwa hiyo madai haya ya Putin kwamba Berezovsky na wenzake wanamchafua kwa malengo ya kisiasa yalipata mashiko kwa sababu Berezovsky alikuwa ni mwanasiasa. Kwa hiyo wananchi waliona hii ilikuwa kama ni 'move' ya Berezovsky kuutaka urais wa Urusi. Wengi hawakupendezwa na hili maana walihisi huu haukuwa wakati sahihi kubadili Rais wa nchi kwa kuzingatia kwamba nchi ilikuwa kwenye mzozo mkubwa huko Chechenya na pia ulikuwa umepita muda mchache tu tangu kumbadilisha rais wa awali, Boris Yeltsin.

Ajabu ni kwamba baada ya hotuba hii ya Putin, safari hii sio tu kwamba Berezovsky alitumia vyombo vyake vya habari kumpinga Putin bali aliitisha mkutano na wanahabari na kumkosoa Putin na sera zake wazi wazi.

Putin na Abramovich hawakutaka kukurupuka kumshughulikia Berezovsky. Walikuwa na uwezo wa kutumia vyombo vya ulinzi kumkamata na kumtia gerezani Berezovsky lakini hii isingekuwa na ufanisi sana kwa sababu tatizo halikuwa Berezovsky peke yake bali ni yeye na genge lake. Na isingekuwa busara kuwakamata maoligarch wote na kuwatia gerezani kwani kutokana na ushawishi wao ingeweza kuzua taharuki kubwa kwenye nchi. Sasa wanafanyaje? Wamuache Berezovsky aendelee kutamba kwenye vyombo vya habari na kumchafua Rais?

Hapana… nyoka akiingia ndani ya shimo usizame na wewe kumfuata… msubiri juu. Hawezi kukaa shimoni milele… msubiri atokeze kichwa juu… mfyeke na upanga.

Usiwe na pupa,

Subiri…

Nilieleza kuhusu Badri Patarkatsishvili rafiki mkubwa wa Berezovsky ambaye alimletea Russia kusimamia Televisheni yake. Berezovsky na Badri walikuwa marafiki haswa lakini kulikuwa na mtu ambaye alikuwa rafiki mkubwa zaidi wa Berezovsky, rafiki wa kushibana haswa, rafiki wa damu haswa, mboni ya jicho kweli kweli ya Berezovsky. Huyu alikuwa anaitwa Nikolai Glushkov. Licha ya urafiki wao lakini pia walikuwa washirika wakubwa kwenye biashara.

Sasa turudi nyuma kidogo,

Pale Russia kuna shirika la ndege la umma linaitwa Aeroflot. Shirika hili ni moja ya mashirika kongwe zaidi ya ndege duniani. Mwaka 1995 Glushkov aliteuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa shirika la Aeroflot. Baada ya mwaka mmoaja tangu kuteuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu kuna skandali kubwa aliibua japo haikufika kwa umma wakati ule lakini ilikuwa tafrani kubwa ndani ya 'system' ya serikali ya Russia.

Kipindi hicho ndani ya shirika kulitokea mkanganyiko mkubwa sana juu ya mapato ya shirika na matumizi yake. Glushkov akajipa jukumu la kuchimba ni nini hasa kilikuwa kinaendelea. Baada ya uchunguzi wake wa miezi kadhaa akang'amua kwamba fedha zote za shirika ambazo zilikuwa zinapatikana kutokana na mauzo ya tiketi ya ndege zilikuwa zinapelekwa kwenye zaidi ya akaunti 352 zilizotawanyika sehemu mbalimbali duniani. Akaja kugundua kuwa akaunti hizi zilikuwa zinatumiwana mashirika ya Usalama ya FSB, SVR na GRU kw ajili ya kugharamia shughuli za ujasusi nje ya Russia. Nilieleza kuhusu FSB, hawa wanahusika hasa na Couter-Intelligence na usalama wa ndani ya Russia na mipakani. SVR hawa wanahusika hasa na ujasusi nje ya Russia. GRU wao kwa kifupi twaweza kusema ni kama chombo cha intelijensia ya jeshi.

Glushkov akagundua kuwa pia waajiriwa 3,000 katiya waajiriwa wote 14,000 wa shirika la Aeroflot walikuwa ni mashushushu wa FSB, SVR na GRU.

Glushkov akakasirika na kuwaandikia barua vyombo hivyo vyote vya ujasusi. Katika barua hiyo kwanza aliwalalamikia vyombo hivyo kutumia rasilimali vya Aeroflot kwa shughuli zao za ujasusi bila ruhusa ya bodi ya Aeroflot wenyewe. Pili, aliwapa 'bili', Kiasi chote cha hela ambao mashirika ya ujasusi yalipokea kutoka Aeroflot na kuwataka warejeshe kwenye shirika.

Glushkov hakuishia hapo tu bali pia alihakikisha fedha zote ambazo zililipwa kwenye akaunti zile 352 ambazo zilikuwa bado hazijatolewa, utaratibu unafanyika akauti wakazi-freeze na kuhakikisha zinatolewa kwenye akaunti hizo. Makosa makubwa yalifanyika hapo…

Unaweza kujiuliza Glushkov aliwezaje kufanya haya dhidi ya shirika la ujasusi kama FSB, SVR na GRU? Lakini tukumbuke kwamba hii ilikuwa ni mwaka 1996 kwenye utawala wa Yeltsin ambapo maoligarch ndio walikuwa 'wenye nchi'. Glushkov alikuwa anaweza kujitutumua na kufanya yote haya kwa mgongo wa oligarch Boris Berezovsky rafiki yake wa damu wa kufa na kuzikana.

Turudi tulipoishia…. Nyoka akiingia shimoni hatumfuati… tunasubiri atokeze kichwa nje tumfyeke.

Baada ya Berezovsky kuendelea kumkosoa kwa kutumia vyombo vyake vya habari… Abramovich akaja na mkakati wa kumdhibiti.

Abramovich akafukua kaburi skandali ile ya Nikolai Glushkov rafiki kipenzi wa Berezovsky. Jambo moja ambalo kipindi kile mwaka 1996 halikufuatiliwa kwa kina ilikuwa ni namna gani fedha zile zilizobakia kwenye akaunti 352 zilitolewa. Kwa sababu kipindi kile Abramovich alikuwa ni kipenzi pia cha Berezovsky kwa hiyo kuna siri nyingi alikuwa anazijua. Mojawapo ya siri hizi zilikuwa ni nini ambacho kilitokea kwenye fedha ambazo zilihamishwa kutoka kwenye akaunti zile 352.

Fedha zili kwa maelekezo ya Glushkanov zilihamishwa kutoka kwenye akaunti zile 352 za idara za ujasusi na zote kuwekwa akaunti ya kampuni iliyosajiliwa nchini uswisi inayoitwa Andava. Kampuni hii ya Andava ilikuwa inamilikiwa na watu wawili, Nikolai Glushkov na Berezovsky. Kwa maana nyingine ni kwamba Nikolai Glushkov na Berezovsky walikuwa wamejichukulia fedha za kampuni ya umma ya Aeroflot ambazo zilikuwa zimelengwa zitumiwe na FSB, SVR na GRU.

Hii ilikuwa silaha ya kwanza ya Abramvich kumshughulikia Berezovsky.

Polisi walimkamata Glushkov na kumfungulia mashtaka ya ubadhirifu wa mali za umma. Siku chache baada ya Glushkov kukamatwa Berezovsky alikimbia Russia na kuomba ukimbizi wa kisiasa nchini Uingereza kwa maana alijua kuwa yeye pia alihusika kwenye kosa hilo ambalo Glushkov alishtakiwa nalo.

Hii haikuwa muarobaini kamili wa kumshughulikia Berezovsky kwani japo alikimbilia Uingereza lakini bado alikuwa anamiliki kituo kile cha televisheni na kampuni nyingine kadhaa ambazo zilikuwa na ushawishi kiuchumi na kisiasa ndani ya Russia.

Abramovich akapiga hatua ya pili ya mkakati wake na kusafiri moja kwa moja hadi Uingereza ambako Berezovsky alikuwa amekimbilia…

Safari ya Abramovich kwenda London ilikuwa mahususi kwa ajili ya kwenda kuonana na mentor wake huyo wa zamani akiwa na maagizo kutoka juu kwa bwana mkubwa… Putin. Maagizo haya yalikuwa 'straight' bila kupiga piga chenga. Kwamba Berezovsky anafahamu kuwa hakuna mahala ambako anaweza kujificha na mkono wa Putin ukashindwa kumfikia. Kwa hiyo Putin alikuwa anampa sharti moja tu… kwamba Berezosky amuuzie Roman Abramovich kituo cha televsheni na akikubali kufanya hivyo Putin atamuacha aishi.

Kituo hiki cha televisheni kilikuwa na thamani ya mabilioni ya dola lakini Abramovich alimuambia Berezosvky kwamba atakinunua kwa dola milioni 150 tu. Berezovsky akakataa.

Abramovich akarudi Russia kupeleka mrejesho kwa Putn kwamba Berezovsky amekataa. Putin akamtuma tena Abramovich kwenda London na ofa nyingine mpya.

Safari hii alipokutana na Berezovsky alimueleza kwamba yeye mwenyewe yuko tayari kupandisha kidogo dau lake la kununua kituo cha televisheni na atampa dola milioni 175. Na si hivyo tu bali pia kama atakubali kumuuzia kituo hicho cha televisheni basi Putin atamuachia huru rafiki yake kipenzi Glushkov ambaye tayari alikuwa anatumikia kifungo jela.

Kitendo cha kusikia kuwa rafiki yake kipenzi Glushkov ataachiwa huru, Berezovsky hakuwa na nguvu tena ya kukataa ofa ya Abramovich, akakubali kumuuzia kituo chake cha televisheni. Na huo ndio ukawa mwisho wa uhuru wa habari nchini Rusia mpaka leo hii maana kituo cha Berezovsky ndio kilikuwa na ushawishi zaidi nchini Russia. Na Abramovich baada tu ya kukinunua kutoka kwa Berezovsky alikikabidhi mikononi mwa Putin akitumie anavyotaka.

Jambo baya zaidi ile ahadi yao ya kumuachia Glushkov hawakuitimiza. Glushkov akaendelea kusota jela. Kuna kipindi akawekewa mtego akiwa amepelekwa hospitali kutibiwa maaskari magereza wakamuacha chumbani peke yake na akataka kutoroka. Akakamatwa tena na kuongezewa kifungo. Maoligarch kadhaa nao wakakamatwa kwa tuhuma za kupanga njama ya kumtorosha Glushkov. Ule mtandao wa maoligarch uliokuwa unaongozwa na Berezosvky ambao ulikuwa unampiga vita Putin na Abramovich ukasambaratishwa wote. Maoligarch wengine waliosalia wakaelewa somo… ukitaka kusurvive kibiashara ndani ya Russia kuna mtu mmoja haupaswi kumgusa… Roman Abramovich.

Nilikuwa natamani niishie hapa lakini kuna kionjo kidogo wacha nikisimulie pia ili uone uwezo wa Abramovich kucheza na 'system' ya dunia. Hata 'wazungu' wa magharibi amewahi kuwafanyia uhuni ambao hata sasa hawaamini macho yao.

Pale ulaya wana benki yao, European Bank. Mwishoni mwa mwaka 1998 kuna benki ya kirusi inaitwa SBS Agro ilichukua mkobo wa hela nyingi sana, mabilioni ya Euro. Ikapita kama miaka miwili hivi pasipo SBS Agro kulipa deni lake. Baada ya kuona deni hilo halilipwi European Bank wakahitaji dhamana ya mkopo huo kutoka kwa SBS Agro. Kama dhamana, SBS Agro wali-plegde deni la dola milioni 14 ambalo wanadai kwa kampuni inaitwa RUNICOM S.A. ambayo imesajiliwa nchini Uswisi. Na hapa ndipo ambapo jina la Abramovich linatokea… kampuni hii ya RUBICOM S.A faida yake kubwa walikuwa wanaipata kwa kuuza mafuta ya kampuni ya Sibneft kwenye nchi za ulaya. Katika kipindi hiki pia benki ile ya SBS Agro ilitangaza kufilisika. Lakini European Bank hawakuwa na wasiwasi kwa sababu deni lao lilikuwa 'guaranteed' na RUNICOM S.A… sijui kama naeleweka sawasawa…

Sasa basi,

European Bank wakaanza kuwadai RUNICOM S.A. Wakadai sana bila mafanikio… ikabidi uitishwe uchunguzi kuangalia mali za kampuni ili wajue namna gani wanaweza kurudisha fedha zao. Katika uchunguzi wao huu mkazo mkubwa uliwekwa kwenye kuingalia biashara ya mafuta ambayo RUNICOM walikuwa wanaifanya kwa sababu nyaraka zilionyesha kwamba faida yao kubwa ilitoka huko. Hawakuamini macho yao walipogundua kuwa biashara ile ya mafuta ya Sibneft kama miezi sita iliyopita ilikuwa imehamishiwa kwenye kampuni nyingine iliyosajiliwa nchini Cyprus ikiitwa RUNICOM LIMITED.

European Bank wakafura kweli kweli… hii ndio ile kwa umombo wanaita 'sleight of hand'. Ushawahi kuona mchezo wa karata tatu… anazivuruga vuruga unahisi umeona sawia kuwa shupaza iko pale mkono wa kulia lakini akifunua unakuta kuna dume la kopa. Hii iliyokuwa inafanyika twaweza kusema ilikuwa 'financial sleight of hand'… abracadabra.

Kuna kitu gani ambacho kinafanana kwenye huu msululu wote? SBS Agro waliokopa awali ni kampuni ya kirusi (Roman Abramovich ni mrusi). Walio gurantee huo mkopo RUNICOM S.A faida yao kubwa walikuwa wanaipata kwa kuuza mafuta ya sibneft kwenye nchi za ulaya (Roman Abramovich ndiye mmiliki wa Sibneft). RUNICOM LIMITED walirithishwa biashara ya mafuta ya sibneft kutoka RUNICOM S.A (Sibneft… Abramovich).

European Bank wakafura zaidi… ilikuwa wazi kwamba ujanja huu walikuwa wanafanyiwa na Roman Abramovich lakini ubaya ni kwamba huwezi kumshtaki kwa kuwa siye uliyemkopesha… walimkopesha nani? SBS Agro… European Bank wakaenda mhakamani. Kesi ikaunguruma kwa miaka miwili. Hukumu ikatolewa kwamba European Bank walipwe kiasi cha dola milioni 24. Lakini nani akulipe?? SBS Agro walishatangaza kufilisika miaka miwili iliyopita na kampuni haipo tena… nani atakulipa hela hizo? Mpaka leo hii ninapoandika makala hii deni hilli halijalipwa na kamwe halitolipwa na ubaya ni kwamba muhusika mkuu na aliyenufaika na mkopo unamjua lakini huwezi kumshitaki kwa sababu hakuna jina lake halijatokea popote kwenye nyaraka na wala hukumkopesha. Tangu kipindi hicho wazungu wanalijua vyema jina la Abramovich na ni mtu wa namna gani.

Kuna watu ukiwasimulia upande huu wa pili wa Abramovich ambao hawajawahi kuusikia watakwambia kuhusu miradi mikubwa ya kijamii ambayo aliifanya akiwa kama gavana wa Chukokta. Jibu langu siku zote ni kweli kwamba Abramovich alitumia fedha zake binafsi karibia dola blioni 3 kwa muda wote aliokuwa gavana wa Chukokta… lakini je unafahamu alinufaikaje?

Baada ya Putin kuwa Rais akampa Baraka Abramovich kuingia kwenye siaisa. Ukitoka pale Kremlin, mwendo wa ndege kama masaa tisa hivi kuna jimbo masikini mno mno linaitwa Chukokta. Hili ndilo ambalo Abramovich aligombea ugavana na kushinda. Alitumia mabilioni ya hela zake kwa ajili ya maendeleo lakini wengi wasichojua ni kwamba alinufaika zaidi. Akiwa kama gavana alikuwa anashawishi sheria ndogo za kodi na misamaha ya kodi kwa kampuni wanazoziona zinafaa. Sasa ile kampuni yake ya Sibneft visima vyake vya mafuta viko Siberia. Walichokuwa wanafanya walikuwa wanauza mafuta yao ya Sibneft kwa bei ya kutupa kwa kampuni ambazo walizisajili kwenye jimbo la Chukokta. Kisha kampuni hizi za Chukokta wanauza mafuta hayo nje ya Russia kwa kampuni dada ya Sibneft kama vile RUNICOM S.A. na walifanya hivi kwa kuwa mafuta haya yakitokea Chukokta yalikuwa na msamaha wa kodi.

Kwa hiyo ni kweli Abramovich alikuwa anasadia lakini papo papo alikuwa ananufaika zaidi.

Wale ‘maswahiba’ wake wa zamani wako wapi?

Mentor wake Boris Berezovsky ambaye alikuja kuwa adui mkubwa siku ya March 23 mwaka 2013 alikutwa amefariki bafuni nyumbani kwake Barkshire, Uingereza. Kifo chake bado kina ubishani mkubwa baadhi ya wachunguzi wa masuala ya post mortem wakisema amejiua wengine wakisema ameuwawa. Wengine wanadai alijiua baada ya kuandamwa na madeni kutokana na kushindwa kesi ambayo alimfungulia Abramovich kugombea umiliki wa Sibneft akitaka kulipwa fidia ya dola bilioni 6 kesi ambayo ilisikilizwa nchini Uingereza na Abramovich kushinda. Hili suala la kugombea Sibneft sijalieleza humu… ila kwa kifupi tu Abramovich alimpiga mchanga wa macho mentor wake… unakumbuka nilieleza kwamba enzi zile za utawala wa Yeltsin Abramovich na Berezovsky walinunua kwa pamoja Sibneft kwenye mnada wa ulaghai ambao wao pekee ndio walikuwa ‘bidders’. Nadhani tunakumbuka vyema… sasa baada ya Berezovsky kukimbia Urusi, Abramovich akafanya janja janja na kumuondoa Berezovsky kwenye umiliki. Berezosvky akafungua kesi.

Abramovich alishinda kesi.

Wanadai kwamba kesi ile ilimfilisi Berezovsky kwa kulipa gharama kubwa za mawakili.

Lakini tukitazama nyuma kidogo tuna pata picha ya tofauti na pengine kutupa dalili kuwa Berezovsky aliuwawa. Novemba mwaka 2006 mshirika wake wa karibu sana Alexander Litvinenko aliuwawa kwa Polonium hapo hapo Uingereza.

Miaka miwili baadae yule rafiki yake Badri ambaye kipindi wako Russia alikuwa anasimamia televisheni yake alikutwa amefariki chumbani kwake hapo hapo Uingereza.

Kama hiyo haitoshi yule rafiki yake kipenzi Nikolai Glushkov alimaliza vifungo vyake na kutoka jela na kukimbilia nchini Uingereza. Huyu naye mwaka jana tu hapa 2018 mwezi March amekutwa amefariki nyumbani kwake hapo hapo Uingereza.

Kwa hiyo maoligarch wote ambao walianzisha vita dhidi ya Putin na Abramovich wote wamefariki vifo vya utata wakiwa na afya njema kabisa… lakini wale wote ambao walikuwa wapole na kumuunga mkono Abramovich kama vile akina Deripaska wako hai hata sasa na utajiri wao ukizidi kupaa kila uchwao.

Mwanzoni mwa makala hii nilijenga hoja kwamba si jambo jepesi sana kuwa bilionea. Unaweza kuwa tajiri… milionea, hakuna shida wala shaka. Lakini kutengeneza utajiri wa kufikia dola bilioni moja na zaidi ni lazima ukubali mikono yako kuchafuka ‘vumbi’ kidogo. Muulize Mo Dewji, msome Gates na alichowafanyia IBM na Steve, chunguza vifo vilivyotokea mwanzoni kwa kuanzishwa kwa Facebook na alichokifanya Mark, muulize Aliko Dangote, teta na akina Motsepe na familia ya Gupta pale Afrika Kusini.

Wote hawa hawawezi kukataa kwamba “behind every great fortune lies a great crime.” Kila utajiri una ukafiri nyuma yake.

MWISHO